

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

Juzuu ya Tatu

Al-Maidah mpaka Al-A'raaf

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

IBN HAZM MEDIA CENTER
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم
للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.


Chapa ya Kwanza 2021.

Msimamizi Mkuu wa Mradi:
Yassir Salim Awadh Masoud

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

Kimehaririwa na:
Wanazuoni wa Kiislamu

Usanifu Kurasa:
Ally Said Abdallah
Ibn Hazm Media Center
P.O. Box 22197,
Dar es Salaam
Tanzania.

Kimechapwa:
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

Haki Zote Zimehifadhiwa.

Yaliyomo:

Tafsiri ya Surat Al-Maidah.....	1
Utukufu wa <i>Surat Al-Maidah</i> Wakati Ilipoteremshwa.....	1
Kueleza Wanyama Halali na Wasio Halali Kuliwa.....	5
Umuhimu wa Kuheshimu Maeneo Matakatifu.....	7
Kuchukua <i>Haddy</i> Kwenye Nyumba Takatifu ya Allah, <i>Al-Kaabah</i>	9
Ulazima wa Kuhifadhi Sehemu Takatifu na Usalama	10
Ruksa Kuwinda baada ya Kumalizika Hija	11
Uadilifu ni Lazima Wakati Wote	11
Wanyama Walioharamishwa Kuliwa.....	14
Kuharamishwa Matumizi ya <i>Al-Azlam</i> kwa kufanya Maamuzi	20
Shetani na Makafiri Wamekata Tamaa na Dini ya Waislamu.....	23
Ukamilishaji wa Dini ya Uislamu.....	24
Ruksa ya Kula Mnyama Mfu katika Hali ya Dharura.....	26
Ufafanuzi wa Vilivyohalalishwa.....	28
Ruksa ya Kutumia Wanyama Waliopewa Mafunzo Kuwinda	29
Kusoma <i>Bismillah</i> Wakati wa Kumtuma Mnyama Aliyepewa Mafunzo.....	32
Uhalali wa Kula Nyama Iliyochinjwa na Watu Waliopewa Kitabu.....	34
Ruhusa ya Kuwaoa Wanawake Safi na Watu Waliopewa Kitabu.....	36
Amri ya Kuchukua Udhu kwa Ajili ya Swala	39
Kutia Nia na Kutaja Jina la Allah تعالى kwa Ajili ya Udhu.....	41
Kuchana Ndevu kwa Vidole Wakati wa Kutia Udhu.....	42
Namna ya Kuchukua Udhu.....	42
Ulazima wa Kuosha Miguu na Sio Kupaka.....	45
Utajo wa Hadithi Zinazoonisha Ulazima wa Kuosha Miguu.....	45
Ulazima wa Kuosha Katikati ya Vidole.....	47
Kupaka Juu ya <i>Khuff</i> ni Sunnah Iliyothibitika	47
Kutayammamu kwa Mchanga Safi Wakati wa Kukosa Maji.....	48
Dua baada ya Udhu.....	49
Fadhila za Udhu.....	50
Waumini Wanakumbushwa Neema ya Fadhila na Uislamu.....	53
Ulazima wa Kusimamisha Haki.....	54
Miongoni mwa Fadhila za Allah تعالى ni Kuwazuia Makafiri.....	57
Watu wa Kitabu Wamelaaniwa kwa Kuvunja Ahadi.....	60
Viongozi wa Ansar katika Usiku wa Aqabah.....	61
Kuvunja Ahadi.....	62
Wakristo Nao Walivunja Agano Lao kwa Allah تعالى	64
Kuelezea Ukweli Kupitia Mtume na Qur'aan.....	66
Imani ya Kuamini Miungu Wengine Ukafiri wa Wakristo.....	68
Kukanusha Madai ya watu wa Kitabu kuwa wao ni Wana wa Mungu.....	68

Musa عليه السلام Anawakumbusha watu wake Fadhila za Allah تعالى	75
Hotuba za Yuwsha (Joshua) na Kalib (Caleb).....	79
Mwitikio mzuri wa Maswahaba Wakati wa Vita vya Badri.....	80
Musa عليه السلام Anaomba Dua kwa Allah تعالى dhidi ya Mayahudi	81
Kuzuiwa Mayahudi Kuingia Ardhi Takatifu kwa Miaka Arobaini.....	82
Ufunguzi wa Baitil Makdisi.....	83
Allah تعالى Anamfariji Musa عليه السلام.....	84
Kisa cha Habil (Abel) na Qabil (Cain).....	86
Adhabu Kali kwa Wanaochupa Mipaka na Kukata udugu wa Kuzaliwa.....	92
Binadamu ni Wajibu Kuheshimu Utukufu wa Binadamu Wenzie.....	94
Maonyo kwa Wafanyao Uharibifu.....	96
Adhabu ya Wasababishao Uharibifu Juu ya Ardhi.....	97
Adhabu ya Wale Wanaompiga vita Allah تعالى na Mjumbe Wake	102
Amri ya kumcha Allah تعالى kutafuta njia ya kufika kwake.....	106
Hapana Fidia Itakayokubaliwa Kutoka kwa Makafiri Siku ya Kiyama.....	108
Amri ya Kukata Mkono wa Mwizi.....	110
Ni Wakati Gani Mkono wa Mwizi Ukatwe?.....	110
Toba ya Mwizi Inakubaliwa.....	112
Usiwe na Majonzi kwa Sababu ya Tabia ya Mayahudi na Wanafiki.....	117
Mayahudi Wanabadilisha Sheria, kama vile Kurujumu Waziwazi	117
Ukaripiaji wa Malengo Mabaya ya Mayahudi, na Kusifia Kitabu Chao.....	122
Sababu Nyingine ya Kuteremshwa Aya Hizi Tukufu	124
Mwanaume Huuawa kwa Kuua Mwanamke.....	128
Kulipiza Kisasi kwa Majeraha.....	129
Hukumu Muhimu.....	129
Kusamehe Kunafuta Dhambi	130
Allah تعالى Amemtaja Isa عليه السلام na habari ya Mtume na Kuisifia Injili.....	132
Kuisifu Qur'an, na Amri ya Kutumia Sharia Yake.....	135
Kuharamishwa Kuwafanya Mayahudi, Wakristo na Maadui.....	144
Sababu ya Kuteremka Aya.....	146
Miongoni mwa Sifa za Wapenzi wa Allah تعالى na Anayewapinga.....	148
Sababu ya Kushuka Aya Hizi.....	150
Kuharamishwa Kuwafanya Marafiki Makafiri	152
Makafiri Wanakebehi Sala na Adhana.....	153
Watu wa Kitabu Wanawachukia Waumini.....	156
Watu wa Kitabu Wanastahili Adhabu Kali Siku ya Kufufuliwa.....	157
Wanafiki Wanajifanya Waumini lakini Wanaficha Ukafiri Wao.....	159
Kukaripiwa kwa Wanazuoni na Wasomi.....	160
Mayahudi Wanasema kuwa Mikono ya Allah تعالى Imefungwa!.....	163
Mikono ya Allah تعالى ni Mikunjufu.....	165
Ufunuo kwa Waislamu Huzidisha Uasi na Ukafiri kwa Mayahudi.....	166

Watu wa Kitabu Wangepuata Kitabu Chao Wangepata Mazuri.....	167
Ahadi ya Kufikisha Ujumbe wa Allah تعالى , na Ahadi ya Kupewa Ulinzi.....	169
Hapana Uokozi Isipokuwa Kuamini Qur'an.....	173
Ukafiri wa Wakristo.....	177
Isa عليه السلام ni Mtumwa wa Allah تعالى na Mama Yake ni Muumini wa.....	180
Kukatazwa (Ushirikina) na Kupetuka Mpaka katika Dini.....	182
Laana ya Mwenyezi Mungu kwa Wana wa Israil.....	184
Hadithi Zinazoelezea Kuamrisha Mema na Kukataza Machafu.....	185
Kuwakosoa Wanafiki.....	187
Kubainisha Sababu za Kushuka Aya Hizi.....	190
Hapana Utawa Katika Uislamu.....	195
Viapo Visivyodhamiriwa.....	197
Adhabu ya Kuvunja Kiapo	197
Kuharamishwa Ulevi na Kamari	202
Maana ya Kuabudu Sanamu na Kupiga Ramli.	202
Kutaja Hadithi Zinazoharamisha <i>Khamr</i> - Vilevi.....	203
Kuharamishwa Kuwinda Wanyama Pori Katika Maeneo Matakatiifu.....	212
Adhabu ya Kuuu Mnyama Pori katika Maeneo Matakatiifu	214
Wanyama wa Majini ni Halali ikiwa Aliye katika Ibada ya Hijja	220
Kuwinda Wanyama wa Bara ni haramu kwa Mwenye Kuhiji.....	222
Kuuliza Kusiko kwa Lazima Kumekatazwa	226
Tafsiri ya Wanyama Waliotajwa.....	232
Amri ya Kutaka Mtu Ajirekebishe Nafsi Yake Kwanza.....	237
Ushahidi wa Mashahidi Wawili Waadiilifu kwa Wosia.	238
Mitume Wataulizwa Kuhusu Mataifa Yao.....	242
Isa عليه السلام Anakumbushwa Neema alizopewa na Allah تعالى	245
Kushushwa kwa Meza ya Chakula Kutoka Mbinguni.....	250
Tukio la Kihistoria la Kushangaza.....	253
Isa عليه السلام Akataa Ushirikina na Athibitisha Ibada ya Mungu Mmoja	254
Ni Ukweli Pekee Utakuwa na Faida Siku ya Kiyama.....	258
Tafsiri ya Surat Al-An'am.....	261
Fadhila za <i>Suratul - An'am</i> na Kipindi cha Kuteremshwa Kwake.....	261
Sifa Njema ni za Allah تعالى Juu ya Kudura Zake na Ukubwa Wake	263
Ukaidi wa Washirikina na Onyo Kwao.....	266
Karipio kwa Wakaidi na Kukataa Kwao Mwanadamu Kuwa Mtume.....	270
Allah تعالى Ndiye Muumbaji Mtoaji Riziki, ni Wajibu Kumtii.....	273
Allah تعالى Ndiye Mnufaishaji, Mwenye Kuleta Madhara.....	279
Watu wa Kitabu Wanamjua Mtume.....	281
Washirikina Wanahojiwa Kuhusu Ushirikina Wao.....	283
Muovu Hanufaiki na Qur'an.....	284
Matumaini na Utashi Havitamnufaisha Yeyote.....	288

Kumfariji Mtume ﷺ.....	293
Washirikina Wanataka Muujiza.....	300
Maana ya <i>Umam</i>	301
Makafiri ni Kama Viziwi na Mabubu Walio Kizani.....	302
Kusimamisha Hoja kwa Washirikina.....	304
Mtume Hamiliki Hazina za Allah تعالی Wala Hajui Ghaibu.....	313
Mtume ﷺ Akatazwa Kuwarudisha Masahaba Dhaifu.....	315
Mtume ﷺ na Uhakika na Anachokilingania.....	321
Allah تعالی Ndiye Pekee Ajuaye Ghaibu.....	324
Waja Wote Wako Chini ya Uangalizi wa Allah تعالی.....	326
Kubainisha Fadhila za Allah تعالی.....	333
Mahubiri (Daawa) ni Mwongozo Usio na Kulazimishana.....	339
Marufuku ya Kukaa pamoja na Watu Wanaozikejeli Aya za Allah تعالی.....	340
Mfano wa Mwenye Kurejea Kwenye Ukafiri.....	345
Maelezo Kuhusu Kupulizwa Baragumu.....	348
Waadhi wa Ibrahim عليه السلام kwa Baba Yake.....	350
Ishara za Upekee wa Allah تعالی (<i>Tawhid</i>).....	352
Huu Ulikuwa Mdahalo kati ya Ibrahimu عليه السلام na Watu wake.....	354
Ushirikina Ndiyo Dhuluma Kubwa.....	361
Ibrahim عليه السلام Anapokea Khabari za Kutunukiwa Is-haq na Yaqub Uzeeni.....	364
Sifa Makhsusi za Nuh عليه السلام na Ibrahim عليه السلام.....	366
Ushirikina Hufuta Amali.....	368
Ubinadamu wa Mtume na Kuteremshiwa Kitabu Juu Yake.....	373
Dhalimu Mkubwa Kushinda wote ni Anayemzushia Allah تعالی.....	378
Hali za Madhalimu Hawa Wakati wa Kifo na Siku ya Kiyama.....	379
Kumjua Allah تعالی kwa Baadhi ya Ishara Zake.....	386
Karipio kwa Washirikina.....	395
Maana ya Uumbaji <i>Badi'</i>	397
Allah تعالی Ndiye Mola Wenu.....	399
Kumuona Allah تعالی Huko Akhera.....	400
Maana ya <i>Al-Baswair</i>	403
Amri ya Kufuata Wahyi.....	406
Kukatazwa Kuitukana Miungu Batili ya Makafiri.....	407
Kudai Miujiza na Kuapa Kuiamini Iwapo Itatokea.....	409
Kila Mtume Ana Maadui.....	415
Watu Wengi ni Wapotevu.....	420
Kuruhusiwa Kilichochinjwa kwa Jina la Allah تعالی.....	422
Kuharamishwa kwa Kilichochinjwa kwa Ghairi ya Jina la Allah تعالی.....	424
Wahyi wa Shetani.....	426
Kufadhilisha Kauli ya Yeyote Juu ya Hukumu ya Allah تعالی.....	428
Mfano wa Kafiri na Muumini.....	428

Wakuu wa Waovu Hila Zao na Mwisho Wao.....	431
Makafiri Wanakiri Juu ya Utukufu wa Nasaba ya Mtume ﷺ.....	435
Madhalimu Husaidiana Wao kwa Wao.....	444
Majini na Wanadamu Kusailiwa Vikali.....	445
Karipio la Kuwaangamiza Kama Hawatatii.....	452
Ubainifu wa Baadhi ya Amali za Kishirikina.....	456
Shetani Huwapambia Washirikina Wawaue Watoto Wao.....	458
Baadhi ya Mifugo Waliyojihadimishia Washirikina.....	460
Allah ﷻ Ndiye Aliyeumba Matunda, Nafaka na Mifugo.....	466
Ubainifu wa Kukatazwa Ufujaji	468
Manufaa ya Mifugo.....	469
Kuleni Nyama za Wanyama Hawa.....	470
Kubainisha Vitu Vilivyoharamishwa.....	475
Vyakula vya Halali Walivyoharamishiwa Wayahudi.....	478
Hila za Wayahudi na Laana ya Allah ﷻ Juu Yao.....	480
Fikra Potovu na Kukanushwa Kwake.....	484
Wasia Kumi.....	488
Kuisifia Qur'an na Taurati.....	504
Qur'an ni Hoja ya Allah ﷻ Juu ya Viumbe Wake.....	507
Onyo kwa Kila Acheleweshae Imani Yake na Toba Yake.....	509
Shutuma Dhidi ya Mifarakano Katika Dini.....	513
Tendo Jema Hulipwa Mara Kumi Mfano Wake.....	515
Uislamu Ndiyo Njia Iliyonyooka.....	518
Amri ya Kufanya Ikhlasu Katika Ibada.....	519
Uislamu Ndiyo Dini ya Mitume Wote.....	520
Amri ya Kufanya Utegemezi Wenye Ikhlasu ndani yake.....	524
Kila Mtu Atabeba Mzigo Wake.....	525
Allah ﷻ Amewajaalia Watu Kuwa Makhhalifa.....	527
Tafsiri ya <i>Suratu Al-A'raaf</i>.....	532
Hali za Miji Iliyoangamizwa.....	534
Ubainifu wa Kupimwa Amali.....	539
Kipambanuzi.....	540
Neema Zake Mbinguni na Duniani ni kwa Ajili ya Wanadamu.....	542
Habari ya Malaika Kumsujudia Adam عليه السلام, na Kiburi cha Ibilisi.....	542
Kuutukuzwa Ukuu wa Allah ﷻ.....	543
Iblisi Alikuwa wa Kwanza Kutumia Qiyas.....	545
Ulaghai kwa Adam عليه السلام na Hawwa na Kula Matunda ya Mti.....	552
Kuteremshwa Duniani Wote Watatu.....	556
Kuteremshwa Libasi na Pambo kwa Wanadamu.....	558
Tahadhari Dhidi ya Fitina za Shetani.....	558
Makafiri Hufanya Madhambi na Kuyategemeza kwa Allah ﷻ.....	559

Allah تعالى Haamrishi Mambo Machafu, bali Uadilifu na Ikhlasu.....	560
Maana ya Ushirikina, Kuumbwa kwa Mara ya kwanza.....	561
Amri ya Kujipamba Wakati wa Kwenda <i>Masjid</i>	566
Makatazo ya Kufanya Israfu Katika Vyakula na Mavazi.....	568
Haramu ni Mambo Machafu, Dhambi, Dhuluma.....	570
Washirikina Wazushi Watapata Fungu Lao Humu Duniani.....	573
Kuhasimiana kwa Watu wa Motoni na Kulaaniana baina Yao.....	576
Wakadhibishaji Hawatafunguliwa Milango ya Mbinguni.....	579
Maelezo Kuhusu Makazi ya Watu Wema na Hali Zao.....	582
Watu wa Jahannam Wana Majuto Juu ya Majuto.....	584
<i>Al-Araaf</i> na Watu Wake.....	587
Fadhila za Jannah Zimezuiliwa kwa Watu wa Motoni.....	590
Washirikina Hawatapata Nafasi ya Kutoa Udhuru Wao	594
Ulimwengu Uliumbwa Katika Siku Sita.....	596
Tafsiri ya <i>Istawaa</i>	597
Usiku na Mchana ni Miongoni Mwa Alama za Allah تعالى	598
Kuhamasishwa Kuomba Dua kwa Allah تعالى	600
Kukatazwa Kuchupa Mipaka katika Dua.....	601
Kukatazwa Kufanya Uharibifu Ardhini.....	601
Miongoni mwa Alama za Allah تعالى ni Kuteremsha Mvua.....	604
Kisa cha Nuhu عليه السلام na Watu Wake.....	607
Kisa cha Hud عليه السلام na Ukoo wa Kaumu ya 'Aad.....	613
Makazi ya Watu wa 'Aad.....	614
Yaliyojiri Baina ya Hud عليه السلام na Watu Wake.....	614
Mwisho wa Watu wa 'Aad Ulivyokuwa.....	618
Kisa cha Mjumbe wa 'Aad.....	620
Maskani ya Kaumu ya Thamud na Nasaba Yao.....	623
Kisa cha Nabii Swalih عليه السلام na <i>Thamud</i>	625
Thamud Walitaka Ngamia Aibuke kutoka katika Jiwe.....	625
Thamud Walimuua Ngamia.....	627
Njama za Mafisadi Kutaka Kumuuua Nabii Swalih عليه السلام	629
Kisa cha Lu't عليه السلام na Kaumu Yake.....	632
Kisa cha Shu'ayb عليه السلام na Ardhi ya Madyan.....	637
Huu ni ulingano wa Mitume wote.....	638
Maangamizo Yaliyowakumba Kaumu Zilizotangulia.....	646
Neema Huja na Imani, Wakati Ukafiri Husababisha Adhabu.....	650
Kisa cha Nabii Musa عليه السلام	657
Fimbo ya Musa عليه السلام na Kiganja Chake Cheupe.....	660
Kauli ya Watu wa Firauni ni kuwa Musa عليه السلام ni Mchawi.....	661
Wachawi Wanabadili Kamba Zao na Kuwa Nyoka Mbele ya Musa عليه السلام	663
Musa عليه السلام Anawashinda Wachawi Kisha Wanamuamini.....	665

Firauni anawatisha Wachawi baada ya Kumuamini Musa عليه السلام.....	668
Firauni anawahamasisha jamaa zake.....	672
Firauni na Watu Wake Wakabiliwa na Ukame.....	674
Allah تعالى Anawaadhibu Watu wa Firauni kwa Sababu ya Uasi Wao.....	677
Watu wa Firauni Wanagharikishwa Baharini.....	681
Wana wa Israel Wanavuka Bahari.....	683
Kuwakumbusha Wana wa Israel Juu ya Baraka za Allah تعالى Kwao.....	685
Musa عليه السلام Alifunga Swamu kwa Ajili ya Allah تعالى Siku Arubaini.....	686
Musa عليه السلام Alimuomba Allah تعالى Amuone.....	687
Allah تعالى Anamteua Musa عليه السلام na Kumpatia Mbao.....	691
Watu Jeuri Hawatapewa Ishara za Allah تعالى.....	693
Kisa cha Kuabudu Ndama.....	696
Musa عليه السلام Alizichukua Mbao baada ya Hasira Kutulia.....	703
Watu Sabini Kutoka Kwa Wana wa Israel Wanakwenda Mahali.....	706
Rehema ya Allah تعالى ni kwa Wenye Taqwa.....	709
Wasifu wa Mtume ﷺ.....	712
Utume wa Muhammad ﷺ ni wa Ulimwengu Mzima.....	717
Uchupaji Mipaka wa Wayahudi Katika Sabato.....	723
Waliovunja Sabato Waligeuzwa Manyani.....	727
Udhalili wa Milele kwa Mayahudi.....	729
Wana wa Israeli Wasambaa Ardhini.....	730
Kunyanyuliwa Mlima Turi Juu ya Vichwa vya Mayahudi.....	735
Ubainifu wa Agano Lililochukuliwa Kutoka kwa Dhuria wa Adam عليه السلام.....	737
Kisa cha Bal'am bin Ba'uraa.....	741
Ukafiri na Qadar ya Allah تعالى.....	749
Ubainifu wa Majina Mazuri ya Allah تعالى.....	752
Ubunifu wa Saa ya Mwisho na Ishara Zake.....	759
Mtume ﷺ hajui Ghaibu Wala Hawezi Kunufaisha wala Kudhuru.....	768
Watu Wote ni Wana wa Adam عليه السلام.....	770
Miungu ya Washirikina Hayasaidii Wala Hayana Uwezo.....	775
Amri ya kuwa Msamehevu.....	781
Njia za Wachamungu Wakati wa Wasiwasi wa Shetani.....	785
Ndugu wa Shetani Miongoni mwa Wanadamu.....	786
Washirikina Waomba Washuhudie Miujiza.....	788
Amri ya Kuisikiliza Qur'an.....	789
Amri ya Kumdhukuru Allah تعالى Asubuhi na Jioni.....	790

Tafsiri ya Suratul Maidah Sura ya 5

Utukufu wa *Suratul Maidah*, Wakati Ilipoteremshwa

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Asmaa Binti Yazid رضي الله عنها kuwa amesema: Hakika mimi nilikuwa nimeshika hatamu za Ngamia wa Mtume ﷺ aitwaye “*Adh'baa*” hapo ikamshukia yeye sura ya *Al-Maida* yote. Uzito wa sura hiyo ulikaribia kutikisa miguu ya mbele ya Ngamia wa Mtume ﷺ.

Na Imamu Ahmad vilevile amenukuu kutoka kwa Abdullah bin Amir رضي الله عنه, amesema: Sura ya Al-Maidah ilimshukia Mtume ﷺ hali ya kuwa akiwa juu ya mnyama wake, hivyo mnyama hakuweza kumbeba Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akateremka. Hadithi hii kaipokea Imamu Ahmad peke yake. Al-Tirmidh alinukuu kuwa Abdullah bin Amr رضي الله عنه alisema, “Sura za mwisho kuteremshwa zilikuwa *Suratu Al-Maidah* na *Suratu Al-Fat-h* (Sura ya 48)”. Al-Tirmidh alitoa maelezo, Hadithi hii ni *Hasan Gharib*,¹ na pia ilielezwa kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Surah ya mwisho kuteremshwa ilikuwa,

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١٠٠﴾

“Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi.”²

Al-Hakim aliikusanya Hadithi sawa na ile ya Al-Tirmidhi katika *Mustadrak* yake, na akasema, “Ni sahihi kwa mujibu wa vigezo vya Bukhari na Muslim ijapokuwa hawakuiandika.”³ Vilevile, Al-Hakim alisimulia kuwa Jubayr bin Nufair amesema: Nilihiji kisha nikaingia kwa mama Aisha رضي الله عنها, akasema: “Ewe Jubayr unasoma (au umeihifadhi) *Al - Maidah*.” Nikajibu, ‘ndio.’ Akasema, “Ilikuwa Surah ya mwisho kuteremshwa. Kwa hiyo, chochote kilichohalalishwa humo, basi ni halali na chochote kilichoharamishwa humo, basi ni haramu,” Al - Hakim alisema, “ni sahihi kwa mujibu wa vigezo vya Bukhari na Muslim ijapokuwa hawakuiandika.”⁴ Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa Abdur-Rahmani bin Mahdi alisimulia kuwa Muawiyah bin Saleh aliongeza kauli hii katika Hadithi ya mwisho, ‘Mimi (Jubayr) pia nilimuuliza Aisha رضي الله عنها kuhusu mwenendo wa Mtume ﷺ, na alinijibu kwa kusema: “Ni Qur’an.” An-Nasai pia aliinukuu.⁵

¹ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:436.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:437.

³ Al-Hakim 2:311.

⁴ Al-Hakim 2:311.

⁵ Ahmad 6:188 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 11138.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمَائِدَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَوْفُوا بِالْعُقُودِ ؕ أَحَلَّتْ لَكُمْ هَيْمَةَ
 ٱلْأَنْعَامِ ۖ إِنَّمَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ غَيْرِ مُحِلِّي الصَّيْدِ وَأَنْتُمْ حُرْمٌ
 ۗ إِنَّمَا اللَّهُ يَحْكُمُ مَا يُرِيدُ ۗ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَحْلُوا
 شَعِيرَ اللَّهِ وَلَا الشَّهْرَ الْحَرَامَ وَلَا الْهَدْيَ وَلَا الْقَلَائِدَ وَلَا
 ءَامِينَ الْبَيْتِ الْحَرَامِ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّن رَّبِّهِمْ وَرِضْوَانًا ۗ
 وَإِذَا حَلَلْتُمْ فَاصْطَادُوا ۗ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شِقَاقَ قَوْمٍ أَن صَدُّوكُمْ
 عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ أَن تَعْتَدُوا ۗ وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ
 وَالتَّقْوَىٰ ۗ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۗ
 إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ۗ حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالدَّمُ
 وَلَحْمُ الْخِنزِيرِ وَمَا أُهْلَ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ ۖ وَالْمُنْخَبِئَةُ وَالْمُتَوَفَّئَةُ
 وَالْمُتَرَدِّئَةُ وَالنَّطِيحَةُ وَمَا أَكَلَ السَّبُعُ إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ وَمَا
 ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ وَأَن تَسْتَقْسِمُوا بِالْأَزْلَمِ ۗ ذَٰلِكُمْ فِسْقٌ
 ٱلْيَوْمَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا مِن دِينِكُمْ فَلَا تَحْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنَ
 ٱلْيَوْمَ ٱلَّذِينَ كَمَلتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ
 لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا ۗ فَمَنِ اضْطُرَّ فِي مَخْمَصَةٍ غَيْرِ مُتَجَانِفٍ
 ۗ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ۗ

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَوْفُوا بِالْعُقُودِ ؕ أَحَلَّتْ لَكُمْ هَيْمَةَ
 ٱلْأَنْعَامِ ۖ إِنَّمَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ غَيْرِ مُحِلِّي الصَّيْدِ وَأَنْتُمْ
 حُرْمٌ ۗ إِنَّمَا اللَّهُ يَحْكُمُ مَا يُرِيدُ ۗ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا
 تَحْلُوا شَعِيرَ اللَّهِ وَلَا الشَّهْرَ الْحَرَامَ وَلَا الْهَدْيَ وَلَا الْقَلَائِدَ وَلَا
 ءَامِينَ الْبَيْتِ الْحَرَامِ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّن رَّبِّهِمْ وَرِضْوَانًا ۗ
 وَإِذَا حَلَلْتُمْ فَاصْطَادُوا ۗ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ
 شِقَاقَ قَوْمٍ أَن صَدُّوكُمْ عَنِ
 الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ أَن تَعْتَدُوا ۗ
 وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ ۗ وَلَا
 تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ ۗ وَاتَّقُوا
 اللَّهَ ۗ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ۗ

1. Enyi mlioamini! Timizeni ahadi. Mmehalalishiwa wanyama wa mifugo, ila wale mnaotajiwa. Lakini msihalalisha kuwinda nanyi mmo katika Hija. Hakika Mwenyezi Mungu Anahukumu Apendavyo.

2. Enyi mlioamini! Msivunje hishima ya alama ya Dini ya Mwenyezi Mungu wala mwezi mtakatifu, wala wanyama wanaopelekwa Makka kuchinjwa, wala vigwe vyao, wala wanaoelekea kwendea Nyumba Takatifu, wakitafuta fadhila na radhi za Mola wao Mlezi. Na mkishatoka Hija yenu basi wendeni. Wala kuwachukia watu kwa kuwa walikuzuilieni kufika Msikiti Mtakatifu kusikupelekeeni kuwafanyia uadui. Na saidianeni katika wema na uchamungu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa mtu alikuja kwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه na akamuambia, "Nishauri" Akamjibu, "Utakaposikia Kauli ya Allah تعالى,

يٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا

"Enyi mlioamini!"

Sikiliza kwa makini, kwani Atakuwa Anaamrisha jema au Anakataza ovu.' Khaythama alisema, kila kinachosomeka ndani ya Qur'an,

يٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا

"Enyi mlioamini!"

Katika Taurati kilikuwa kikisomeka: 'Enyi wenye kuhitaji.'

أَوْفُوا بِالْعُقُودِ

"Timizeni ahadi."

Ibn Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na wengineo walisema 'Ahadi', hapa maana yake mikataba.¹ Ibn Jariri رحمه الله تعالى amesema kuwa kuna muafaka juu ya rai hii.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa ina maana ya mikataba, kama vile mashirikiano waliyokuwa wakiyafanya.²

¹ At-Tabari 9:450.

² At-Tabari 9:449.

Ali bin Abi Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo ya:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَوْفُوا بِالْعُقُودِ ۗ

“Enyi mlioamini! Timizeni ahadi.”

Inarejea katika maagano, yaani, katika kile alichokiruhusu Allah تعالى, Alichokiharamisha, Alichokifaradhisha na Akakiwekea mipaka ndani ya Qur'an. hivyo msifanye khadaa au kuvunja maagano.

Allah تعالى Anafafanua Amri hii pale Aliposema:

وَالَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ أَنْ يُوصَلَ

“Na wale wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuzifunga, na wanakata Aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe,...”mpaka,

سُوءِ الدَّارِ

“Nyumba mbaya.”¹

Adh-Dhahhak alisema,

أَوْفُوا بِالْعُقُودِ ۗ

“Timizeni ahadi.” (13:25)

Inamaanisha kile Alichokihalalisha Allah تعالى na Alichokiharamisha. Allah تعالى Amechukua agano kutoka kwa wale wanaotangaza imani yao kwa Mtume ﷺ na Kitabu, kutimiza majukumu ambayo Allah تعالى Amewafaradhishia katika yenye kuruhusiwa na yasiyoruhusiwa.

¹ At-Tabari 9:452.

Kueleza Wanyama Halali na Wasio Halali Kuliwa

Allah تعالى Amesema,

أُحِلَّتْ لَكُمْ بَهِيمَةُ الْأَنْعَامِ

“Mmehalalishiwa wanyama wa mifugo.”

Ngamia, Ngombe na kondoo, kama ilivyoelezwa na Al-Hasan, Qatadah na wengineo.¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa Tafsir hii ni sawa na maana ya Wanyama wa mifugo ambao Waarabu waliwafuga. Inapasa kutaja hapa kuwa Ibn Umar, Ibn Abbas na wengine رضي الله عنهم waliitolea hoja Ayah hii na kuifanya kuwa ni ushahidi wa kuhalalishwa kula nyama ya kichanga kilichofia tumboni mwa mamaye aliyechinywa.²

Kuna Hadithi juu ya suala hili iliyokusanywa katika sunan Abu Dawud, At-Tirmidh na Ibn Majah, kutoka kwa Abu Saidi رضي الله عنه amesema, “Tulimuuliza Mjumbe wa Allah! Tunapochinja ngamia, ngo’mbe au kondoo, baadhi ya wakati hukuta mtoto ndani ya tumbo, tule au tusile nyama yake?” Akasema,

«كُلُّهُ إِنْ شِئْتُمْ فَإِنَّ ذَكَاتَهُ ذَكَاتُ أُمِّهِ»

“Kuleni kama mnataka, kwa sababu kuchinjwa kwake kulikamilika alipochinjwa mama yake.”

At-Tirmidh alisema, “Hadithi hii ni *Hasan*”³ Abu Dawud alinukuu kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema

«ذَكَاتُ الْجَنِينِ ذَكَاتُ أُمِّهِ»

“Uchinjaji wa mtoto unatimia kwa kuchinjwa mama yake.”

Hadithi hii ilikusanywa na Abu Dawud peke yake.⁴

¹ At-Tabari 9:455.

² At-Tabari 9:456.

³ Abu Dawud 3:252, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 5:48 na Ibn Majah 2:1066.

⁴ Abu Dawud 3:253.

Kauli ya Allah تعالى،

إِلَّا مَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ

“ila wale mnao tajiwa”. Ali bin Abi Talha alieleza kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa ilikusudiwa “Mnyama mfu, damu na nyama ya nguruwe.”¹ ‘Qatadah alisema, “Mnyama mfu, na waliochinjwa bila ya kutamkwa Jina la Allah تعالى wakati wa kuchinja.”²

Inaelekea, na Allah تعالى Anajua zaidi, Ayah ile inahusu na inaturejesha kwenye Kauli nyingine ya Allah تعالى،

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالْدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنزِيرِ وَمَا أُهِلَّ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ وَالْمُنْخَنِقَةُ وَالْمَوْقُوذَةُ
وَالْمُتَرَدِّيَةُ وَالنَّطِيحَةُ وَمَا أَكَلَ السَّبُعُ

“Mmeharimishiwa nyamafu, na damu, na nyama ya nguruwe, na mnyama aliyechinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na aliyekufa kwa kunyongeka koo, na aliyekufa kwa kupigwa, na aliyekufa kwa kuanguka, na aliyekufa kwa kupigwa pembe, na aliyeliwa na mnyama...”

Japokuwa wanyama waliotajwa katika Aya hii ni wale waliohalalishwa kuliwa (isipokuwa Nguruwe), wanakuwa haramu kutokana na mazingira yaliyoelezwa katika Aya (5:3) Kwa ajili hiyo Allah تعالى Amesema،

إِلَّا مَا ذَكَيْتُمْ وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصَبِ

“...ila mkimdiriki kumchinja. Na pia ni haramu kula nyama aliyechinjiwa masanamu.”

Maana: katika hao wanyama mliohalalishiwa, ni haramu nyama yake haifai kuila. Allah تعالى Amesema،

أُحِلَّتْ لَكُمْ بَهِيمَةُ الْأَنْعَامِ إِلَّا مَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ

“Mmehalalishiwa wanyama wa mifugo, ila wale mnaotajiwa.”

Maana: ila wale mtakaotajiwa kuhusu uharamu wake.

¹ At-Tabari 9:458.

² At-Tabari 9:458.

عَمِيرٌ مَّحَلِّيٌّ وَالصَّيْدِ وَأَنْتُمْ حُرْمٌ

“...lakini msihalalishe kuwinda hali nyinyi mmo katika Ihramu.”

Baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa maana ya ujumla ya ‘mifugo’ ifugwayo, inajumuisha wanyama wafugwao na binadamu, kama vile Ngamia, Ng’ombe, Mbuzi na Kondoo. Na wanyama wa mwitu ni kama vile Swala, Ng’ombe mwitu na Punda mwitu. Allah تعالی Amewatoa katika uhalali wanyama wafugwao na watu hao tuliowataja huko nyuma mfano wa Nguruwe, Mbwa n.k., pia Amekataza kuwinda wanyama mwitu wakati mtu akiwa katika *ihraam*. Pia imesimuliwa kuwa maana inayokusudiwa hapa ni, “Tumekuruhusuni aina zote za wanyama katika hali zote, isipokuwa Tuliowaharamisha katika hao, hapa kwa mtu anayewinda wanyama ilhali akiwa katika hali ya *ihraam*.” Allah تعالی Anasema,

فَمَنْ أَضْطُرَّ فِي مَخْمَصَةٍ غَيْرِ مُتَجَانِفٍ لِإِثْمِهِ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Basi yule atakayeshikika katika hali ya njaa, bila ya kukusudia kuchuma dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe na Huruma.”

Aya hii inamaanisha, “Tumeruhusu ulaji nyama ya wanyama waliokufa, kwa aliyeshikika kwa sharti ya kutokusudia uovu wala kupetuka mpaka.” Hapa Allah تعالی Anaeleza, “kama Tulivyowaruhusu kula wanyama wafugwao katika kila hali ya mazingira, basi msiwinda wanyama mkiwa katika *Ihram* kwani huu ni Uamuzi wa Allah تعالی, na Yeye ni Mwenye Hekima katika kila Analoliamrisha na Kulikataza.” Hivyo Allah تعالی Amesema,

إِنَّ اللَّهَ سَخِيمٌ مَّا يُرِيدُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anahukumu Apendavyo.”

Umuhimu wa Kuheshimu Maeneo Matakatifu na Miezi Mitakatifu

Allah تعالی Anaendelea,

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَحْلُوا شَعْتِيرَ اللَّهِ

“Enyi mlioamini! Msivunje hishima ya alama za Dini ya Mwenyezi Mungu.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “*Sha’a-ira Allah*” ina maana ya ibada za Hijja.¹ Mujahidi alisema, “*As-safa* na *Al-Marwah*, na dhabihu ni katika matukufu ya Dini ya Allah تعالى.² Aidha ilielezwa kuwa “*Sha’a-ira Allah*” ni yale Aliyoharamisha. Kwa hiyo, ina maana, msivunje Aliyoyaharamisha Allah تعالى. Na kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema,

وَلَا الشُّهُرَ الْحَرَامَ

“***Wala mwezi mtakatifu...***”, Kwani mnatakiwa kuheshimu na kutukuza Mwezi mtakatifu na kujiweka mbali na yale Aliyoyazuia Allah تعالى kwa kuanzisha mapigano. Na msisitizo ni kujiepusha na yaliyoharamishwa. Kama Allah تعالى Alivyosema,

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشُّهُرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ

“***Wanakuuliza juu ya kupigana vita katika mwezi mtakatifu. Sema: Kupigana vita wakati huo ni dhambi kubwa.***” Na

إِنَّ عِدَّةَ الشُّهُورِ عِنْدَ اللَّهِ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا

“***Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na mbili.***”

Bukhari aliandika katika sahihi kutoka kwa Abubakr رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema wakati wa Hijja ya kuaga.

«إِنَّ الزَّمَانَ قَدِ اسْتَدَارَ كَهَيْئَتِهِ يَوْمَ خَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ السَّنَةُ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا، مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرْمٌ، ثَلَاثٌ مُتَوَالِيَاتٌ: ذُو الْقَعْدَةِ وَذُو الْحِجَّةِ وَالْمَحْرَمِ، وَرَجَبُ مُضَرَ الَّذِي بَيْنَ جُمَادَى وَشَعْبَانَ»

“*Mgawanyo wa muda umerejea kama ilivyokuwa Allah تعالى Alipoumba Mbingu na ardhi. Mwaka ni miezi kumi na miwili, mine kati yake ni mitakatifu, mitatu imefuatana, (nayo ni) Dhuli-Qa’dah, Dhuli-Hijjah na Muharram, na (wa nne ni) Rajabu ya (kabila la) Mudhar ambao upo kati ya Jumada (ath-Thaniyah) na Shaaban.*”¹

Hadithi hii inathibitisha kuendelea kwa utukufu wa miezi mpaka mwisho wa dunia.

¹ At-Tabari 9:463.

² At-Tabari 9:463.

Kuchukua Haddy¹ Kwenye Nyumba Takatifu ya Allah تعالى, Al-Kabah

Kauli Ya Allah تعالى,

وَلَا أِهْدَى وَلَا أَلْفَلِئِدَ

“Wala wanyama wanaopeleka Makka kuchinjwa, wala vigwe vyao...”

Maana: Musiache ada ya kupeleka Hady (dhabihu) Makka, kwani ibada hii ni katika kuheshimu matukufu ya Dini ya Allah تعالى. Msiache kuwavisha vijiwe shingoni mwao, ili watofautishwe na wanyama wengine. Kwa kufanya hivyo, itafahamika kuwa wanyama hao wamekusudiwa kuwa Hady katika Ka'baah, atajiepusha nao yule anayekusudia ubaya. Na hilo litamshajiisha mwengine kuiga kama hivyo. Na kwa hakika, yeyote atakayelingania uongofu huo, atalipwa sawa na yule atakayeiga mfano wake, bila hata kupungua thawabu zake. Mtume ﷺ alipotaka kuhiji, alilala Dhul-Hullayfah, pia hujulikana kwa jina la Al-Aqiq. Asubuhi, Mtume ﷺ aliwazungukia wake zake, ambao walikuwa tisa wakati huo, kisha akaoga, akajipaka uturi, na akasali Rakaa mbili, kisha akafunga wanyama wake Hady na akatangaza nia ya Hajj na Umra. Hady ya Mtume ﷺ wakati huo ilikuwa Ngamia wengi, zaidi ya sitini, na walikuwa miongoni mwa wanyama wazuri, wenye afya na miili ya kupendeza, kama Allah تعالى Alivyosema,

ذَلِكَ وَمَنْ يُعْظِمَ شَعْبِيرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ ﴿٥٠﴾

“Ndio hivyo! Na anayetukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo”.

Maqatil bin Hayyan aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا أَلْفَلِئِدَ

“...wala vigwe vyao...”, Maana: “Msikiuke utakatifu wake.” Wakati wa Jahiliyyah, watu walikuwa wakijifunga vigwe na manyoya ya wanyama walipogura majumbani mwao. Washirikina wa Eneo Takatifu walitumia vigwe pamoja na matawi ya miti ya Eneo Takatifu ili waruhusiwe kupita kwa amani. Kauli hii aliikusanya Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى, ambaye pia aliinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliyesema: “Kuna Aya mbili katika surah hii (Al-Maidah) ambazo zilifutwa. Aya juu ya vigwe (5:2) na

¹ Mnyama wa Sadaka anayechinjwa na mahujaji.

فَإِنْ جَاءُوكَ فَاحْكُم بَيْنَهُمْ أَوْ أَعْرِضْ عَنْهُمْ^ط

“Basi wakikujia, wahukumu baina yao au jipuuze nao”.¹

Ulazima wa Kuhifadhi Sehemu Takatifu na Usalama wa Wale Wanaoazimia Kwenda katika Nyumba Tukufu.

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا آيِينَ الْبَيْتِ الْحَرَامِ يَتَتَفَعُونَ فَضْلًا مِّن رَّبِّهِمْ وَرِضْوَانًا^ع

“Wala wanaoelekea kwendea Nyumba Takatifu, wakitafuta fadhila na radhi za Mola wao Mlezi”.

Ayah inaamrisha: Msiwapige watu wanaokwenda katika Nyumba Tukufu ya Allah تعالى، ambao mtu akishaingia apewe hifadhi, vilevile, wale wanaoelekea katika Nyumba Takatifu wakitafuta fadhila na radhi za mola wao, wasizuiwe au kuwekewa vikwazo au kuhofishwa katika kuingia Nyumba Tukufu. Mujahid Ata, Abu Al-‘Aliyah, Mutarrif bin Abdullah, ‘Abdullah bin ‘Ubayd bin ‘Umayr, Ar-Rabi’ bin Anas, Muqatil bin Hayyan, Qatadah na wengine kadha, walisema,

يَتَتَفَعُونَ فَضْلًا مِّن رَّبِّهِمْ

“Wakitafuta fadhila na radhi za Mola wao Mlezi.” Inakusudiwa biashara.² Majadiliano haya yalitangulia kuhusu Ayah hii. Allah تعالى Amesema,

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ^ع

“Si vibaya kwenu kuitafuta fadhila ya Mola wenu Mlezi”.

Allah تعالى Amesema,

وَرِضْوَانًا^ع

“...na radhi...” Ibn Abbas رضي الله عنهما yaani, “kutafuta radhi za Mola kwa kuhiji kwao.” Ikrimah, As-Suddi na Ibn Jarir wamesema kuwa Ayah hii iliteremshwa hususani kwa Al-Hutam bin Hind Al-Bakri, ambaye alipora ng’ombe wa watu wa Madinah. Mwaka uliofuata, alitaka kufanya umrah katika Nyumba ya Allah تعالى na baadhi ya Masahaba walitaka kumshambulia akiwa njiani kwenda Makkah. Allah تعالى Aliteremsha,

¹ At-Tabari 10:332.

² At-Tabari 9: 480-481.

وَلَا ءَامِينَ الْبَيْتِ الْحَرَامِ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّن رَّبِّهِمْ وَرِضْوَانًا

“Wala wanaoelekea kwendea Nyumba Takatifu, wakitafuta fadhila na radhi za Mola wao Mlezi.”

Ruksa Kuwinda Baada ya Kumalizika Hija:

Kauli ya Allah تعالى،

وَإِذَا حَلَلْتُمْ فَاصْطَادُوا

“Na mkishatoka Hija yenu basi windeni.”

Mnapomaliza Hijjah, mnaruhusiwa kuwinda, ambapo mliharamishiwa mlipokuwa katika *Ihram*. Japokuwa Ayah hii ina amri ambayo ina nguvu baada ya muda wa kukatazwa (wakati wa *Ihram* katika kadhia hii), kwa hakika Ayah, inairejesha hukumu ya jambo hili kabla ya kukatazwa.

Kama hukumu ya mwisho ya jambo hili kabla ya kuja makatazo, ilikuwa ni wajibu basi jambo hilo nalo litakuwa wajibu, na kama ilikuwa Sunna, hukumu yake nayo itakuwa Sunna, na kama ilikuwa *Mubaha*, basi hukumu yake itakuwa *Mubaha*.

Na mwenye kusema amri hii ni ya “wajibu” kuna aya nyingi zitapingana na wajibu huu. Na anayesema; Amri hii “*Mubaha*” kuna nyingine zinakataa hukumu hiyo. Na hukumu inayoendana sambamba na maandiko yote ya kisharia ni hiyo tuliyoitaja hapo nyuma. Allah تعالى Anajua Zaidi.

Uadilifu ni Lazima Wakati Wote:

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا تَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍۭٓ أَن صَدُّوكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ أَن تَعْتَدُوا

“Wala kuwachukia watu kwa kuwa walikuzuilieni kufika Msikiti mtakatifu kusikupelekeeni kuwafanyia uadui.”

Maana ya Aya hii iko wazi, kama inavyoamrisha: Tusiwachukie baadhi ya watu, waliokuzuilieni kufika Nyumba Takatifu katika mwaka wa Hudaybiyyah, na kuwasababisha kuchupa mipaka ya Sharia ya Allah تعالى na kuwafanyia dhuluma

¹ At-Tabari 9:472, 475. Masimulizi kuhusu sababu za kushuka Aya hii si sahihi.

kwa kulipiza kisasi. Bali, muongoze kama Allah تعالى Alivyowaamuru, mumtendee haki kila mtu. Tutaielezea Aya sawa na hii baadaye.

وَلَا تَجْرِمَنكُمْ شَتَٰنَ قَوْمٍ أَن صَدُّوكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ أَن تَعْتَدُوا وَتَعَاوَنُوا عَلَى
الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ

“Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu.”

Maana: Msiendeshwe na chuki zenu kwa baadhi ya watu na kuacha haki, kwani haki imefaradhihwa kwa kila mmoja, katika hali zote.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Zayd bin Aslam alisema, “Mtume ﷺ na Masahaba wake walikuwa Al-Hudaybiyyah, washirikina walipowazulia kuzuru Nyumba Tukufu, na hilo lilikuwa gumu kwao. Baadaye, baadhi ya washirikina waliwapita kutokea mashariki wakiwa na nia ya kufanya Umrah. Masahaba wa Mtume ﷺ wakasema, “‘Tuwazuieni kufanya Umrah kama washirikina wenzao walivyotuzulia.’ Baada ya hapo Allah تعالى Alishusha Ayah hii.”¹ Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine walisema, “*Shana’an*” ni uadui na chuki, Allah تعالى Akasema tena,

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ

“Na saidianeni katika wema na uchamungu. Wala msaidiane katika dhambi na uadui.”

Allah تعالى Anawaamrisha waumini kusaidiana katika kufanya uadilifu, amali njema, ambayo ndio maana ya ‘*Al-Birr*’; na kutofanya madhambi, ambapo ndiyo maana ya “*At-Taqwa*.” Allah تعالى Amewakataza waja Wake katika kusaidiana kufanya madhambi ‘*lthm*’ na kufanya yaliyoharamishwa.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa, “‘*lthm*’ maana yake kuacha yale Aliyoamrisha Allah تعالى; ambapo uadui maana yake ni kuchupa mipaka Aliyoiweka Allah تعالى katika dini yenu, pamoja na kuvuka mipaka kwa yale Allah تعالى Aliyoyaamrisha kwake binafsi na wengine.”²

¹ At-Tabari 9:478.

² At-Tabari 9:490.

Imam Ahmad alimnukuu kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«انصُرْ أَخَاكَ ظَالِمًا أَوْ مَظْلُومًا»

“Mnusuuru nduguyo ima ni dhalimu au amedhulumiwa.”

Aliulizwa, “Ewe Mjumbe wa Allah! Tunajua kumsaidia mtu anapodhulumiwa, ni vipi kumsaidia anapodhulumu?” Akajibibu

«تَخَجُّرُهُ وَتَمَنُّعُهُ مِنَ الظُّلْمِ فَذَاكَ نَصْرُهُ»

“Kataza na mzuie asidhulumu, kufanya hivyo ndio kumsaidia.”¹

Bukhari alinukuu Hadithi hii kupitia Hushaym.² Ahmad alimnukuu mtu mmoja katika Masahaba kuwa Mtume ﷺ alisema:

«الْمُؤْمِنُ الَّذِي يُخَالِطُ النَّاسَ وَيَصْبِرُ عَلَىٰ أَدَاهُمْ أَغْظَمُ أَجْرًا مِنَ الَّذِي لَا يُخَالِطُ
النَّاسَ وَلَا يَصْبِرُ عَلَىٰ أَدَاهُمْ»

“Muumini anayechanganyika na watu na ni mwenye kusubiri katika maudhi yao ni mwenye ujira mkubwa zaidi kuliko yule asiyechanganyika na watu na si mwenye kusubiri katika maudhi yao.”³

Muslim⁴ alinukuu Hadithi inayosema,

«مَنْ دَعَا إِلَىٰ هُدًى كَانَ لَهُ مِنَ الْأَجْرِ مِثْلُ أُجُورٍ مَنِ اتَّبَعَهُ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا يُنْقِصُ
ذَلِكَ مِنْ أُجُورِهِمْ شَيْئًا، وَمَنْ دَعَا إِلَىٰ ضَلَالَةٍ كَانَ عَلَيْهِ مِنَ الْإِثْمِ مِثْلُ آثَامٍ مَنِ اتَّبَعَهُ
إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ، لَا يُنْقِصُ ذَلِكَ مِنْ آثَامِهِمْ شَيْئًا»

“Anayelingania kwenye uongofu, atapata ujira sawa na wale wanaokubali wito wake, mpaka Siku ya Kiama, bila kupunguza ujira wao chochote. Mwenye kulingania kwenye upotofu, atabeba mzungo wa madhambi sawa na aliyekubali wito wake, mpaka siku ya kiama, bila kupunguza dhambi zao chochote.”

¹ Ahmad 3:99.

² Fat'hul Al-Bari 5:117.

³ Ahmad 5:365.

⁴ Muslim 4:2060.

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالْدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنزِيرِ وَمَا أُهْلِيَ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ وَالْمُنْخَنِقَةُ وَالْمَوْقُوذَةُ
وَالْمُتَرَدِّيَةُ وَالنَّطِيحَةُ وَمَا أَكَلَ السَّبُعُ إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ وَأَنْ تَسْتَقْسِمُوا
بِالْأَزْلَمِ ذَٰلِكُمْ فَسُقُ الْيَوْمَ يَيْسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنَ الْيَوْمَ
أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيْتُ لَكُمْ الْإِسْلَامَ دِينًا فَمَنِ اضْطُرَّ فِي
مَخْصَصَةٍ غَيْرِ مُتَجَانِفٍ لِإِيمَانِهِ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣﴾

3. "Mmeharimishiwa nyamafu, na damu, na nyama ya nguruwe, na mnyama aliyechinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na aliyekufa kwa kunyongeka koo, na aliyekufa kwa kupigwa, na aliyekufa kwa kuanguka, na aliyekufa kwa kupigwa pembe, aliyeliwa na mnyama, ila mkimdiriki kumchinja. Na pia ni haramu kula nyama aliyechinjiwa masanamu. Na ni haramu kupiga ramli. Hayo yote ni upotovu. Leo waliokufuru wamekata tamaa na Dini yenu; basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi. Leo Nimeku-kamilishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni neema Yangu, na Nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo Dini. Na mwenye kushurutishwa na njaa, bila ya kupendelea dhambi, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye Kurehemu."

Wanyama Walioharamishwa Kuliwa:

Allah تعالی Anawaambia waja Wake kuwa Ameharamisha kula aina ya vyakula, kama vile *Maytah*, ambaye ni mnyama anayekufa bila kuchinjwa au kuwindwa. Allah تعالی Ameharamisha aina hii ya chakula kwa kuwa ina madhara kutokana na kuziba veni za mnyama aliyekufa. Kwa hiyo, *Maytah* inadhuru, kidini na kimaumbile, na kwa sababu hii Allah تعالی Ameiharamisha. Anayeruhusiwa katika sheria hii ni samaki, kwani samaki ni halali, hata kama amekufa kwa kuchinjwa au vinginevyo. Imam Malik رحمه الله تعالی katika kitabu chake cha Muwatta, pia Abu Dawud, At-Tirmidhi, An-Nasai na Ibn Majah katika *Sunan* zao, Ibn Khuzaymah na Ibn Hibban katika sahihi zao, zote imenukuliwa kuwa Abu hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa, "Mtume ﷺ aliulizwa juu ya maji ya bahari." Alisema,

«هُوَ الطَّهْرُ مَاؤُهُ الْجِلُّ مَيْتُهُ»

*"Maji yake ni twahara na maiti yake ni halali"*¹

Hukumu hii pia inahusu nzige, kama ilivyothibitishwa katika Hadithi ambayo tutaitaja baadaye. Kauli ya Allah تعالى،

وَالدَّمُ

"...na damu..."

Hii inahusu damu inayochuruzika, kwa mujibu wa Ibn Abbas رضي الله عنهما na Said bin Jubayr رضي الله عنه، na ni sawa na Kauli nyengine ya Ayah ya Allah تعالى،

دَمًا مَّسْفُوحًا

"...damu inayomwagika..."

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kwamba Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu 'wengu.' Akasema, 'kuleni.' Wakasema "Ni damu." Akasema, "Mlizuiwa damu inayochiririka." Abu Abdullah Muhammad bin Idris Ash-Shafi رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema،

«أَجِلُّ لَنَا مَيْتَانِ وَدَمَانِ، فَأَمَّا الْمَيْتَانِ فَالْسَّمَكُ وَالْجِرَادُ، وَأَمَّا الدَّمَانِ فَالْكَبِدُ وَالطَّحَالُ»

*"Tumehalalishiwa nyamafu mbili na aina mbili ya damu. Ama kuhusu nyamafu mbili, ni samaki na nzige. Ama damu mbili ni ini na wengu."*²

Imam Ahmad bin Hambali, Ibn Majah, Ad-Daraqutni na Al-Bayhaqi pia waliinukuu Hadithi hii kupitia Abdur-Rahman bin Zuyd bin Aslam ambaye ni msimulizi dhaifu.³

¹ Abu Dawud 1:64, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 1:224, an-Nasai 1:50, Ibn Majah 1:136. Ibnu Khuzaymah 1:59, Ibn Hibban 2:272.

² *Musnad* Ash-Shafi 2:173.

³ Ahmad 2:97, Ad-Daraqutni 4:272, Al-Bayhaqi 1:254, na wengine. Inachukulika kuwa ni sahihi kutokana na njia zake nyingi.

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَحْمُ الْخِنْزِيرِ

“Na nyama ya nguruwe...”,

Ni pamoja na nguruwe mwitu na wafugwao, na inahusu mnyama mzima pamoja na mafuta yake, kwani mafuta ni sehemu ya *Lahm* au “nyama” kwa Waarabu. Muslim alimnukuu Buraydah bin Al-Husayb Al-Aslam رضى الله عنه kuwa alisema Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ لَعِبَ بِالْتَّرْدِشِيرِ، فَكَأَنَّهَا صَبَغَ يَدَهُ فِي لَحْمِ الْخِنْزِيرِ وَدَمِهِ»

“Yeyote anayecheza Narshir (mchezo unaotumia dadu na una kamari) ni sawa na mtu anayeingiza mkono wake kwenye nyama na damu ya nguruwe.”¹

Iwapo hii ndio hali anayegusa nyama na damu ya nguruwe itakuwaje kuila? Hadithi hii ni ushahidi kuwa nyama *Lahm* ina maana mwili mzima wa Mnyama, pamoja na mafuta yake. Imenukuliwa katika Sahih Mbili kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَ بَيْعَ الْخَمْرِ وَالْمَيْتَةِ وَالْخِنْزِيرِ وَالْأَصْنَامِ»

“Allah تعالى Ameharamisha biashara ya pombe, nyamafu, nguruwe na masanamu.”

Watu waliuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Nini hukumu ya mafuta ya nyamafu, kwani yalikuwa yakitumika kwa kupakwa katika majahazi na kulainishia ngozi; na watu wanatumia kuwashia taa?” Alijibu,

«لَا، هُوَ حَرَامٌ»

“Hapana, hiyo ni haramu.”²

Katika Sahih ya Bukhari, Abu Sufyan alisimulia kuwa alimuambia ‘Heraclius, mfalme wa Roma, “Yeye (Muhammad ﷺ) alitukataza kula nyamafu na damu.”

¹ Muslim 4:1770.

² *Fat’hul Al-Bari* 4:495, Muslim 3:1207.

Allah تعالی Amesema,

وَمَا أَهْلٌ لِّغَيْرِ اللَّهِ بِهِ

“Na mnyama aliyechinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu...”

Kwa hiyo mnyama aliyechinjwa kwa kutajwa Jina lisilo la Allah تعالی, ni haramu kwa sababu Allah تعالی Alilazimisha kutajwa Jina Lake Takatifu wakati wa kuchinja wanyama, Aliowaumba, Yeyote asiyefanya hivyo, akitaja jina la asiyekuwa Allah تعالی, kama vile jina la sanamu, mizimu au sanamu ya ukumbusho, anapochinja, anaifanya nyama hii haramu, kwa mujibu wa kongamano la wanazuoni. Kauli ya Allah تعالی,

وَالْمُنْحَنِقَةُ

“Na aliyekufa kwa kunyongeka koo...”

Ima kwa kudhamiria au bahati mbaya, kama vile mnyama anapozunguka wakati amefungwa na anakufa kwa kunyongwa kwa sababu ya kuhangaika, nyama hii pia ni haramu kuliwa.

وَالْمَوْقُودَةُ

“Na aliyekufa kwa kupigwa...”

Hii inahusu mnyama aliyepigwa kwa kitu kizito mpaka kufa. Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengineo walisema ni, ‘mnyama ambaye amepigwa kwa kitu mpaka akafa.’¹ Qatadah alisema, “Watu wa Jahilliyah walikuwa wakiwapiga wanyama kwa fimbo na walipokufa waliwala.”² Ilinukuliwa ndani ya Sahih kutoka kwa Adi bin Hatim alisema, nilisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Natumia *Mirad*³ kwa kuwindia na kukamatia wanyama pori.’ Alijibu,

إِذَا رَمَيْتَ بِالْمِغْرَاضِ فَخَرَقَ فَكُلَّهُ، وَإِنْ أَصَابَ بَعْرُضِهِ فَإِنَّمَا هُوَ وَوَيْدٌ فَلَا تَأْكُلْهُ،

“Mnyama akichomwa na ncha kali, mleni. Lakini, akipigwa kwa ubapa, msimle, kwani kapigwa mpaka kufa.”⁴

¹ At-Tabari 9:496.

² At-Tabari 9:496.

³ Kipande cha mti chenye ncha kali au kilichowekewa ncha kali ya chuma kinachotumika katika kuwindia.

⁴ *Fat’hul Al-Bari* 9:518.

Kwa hiyo, Mtume ﷺ alitofautisha kati ya kumuua mnyama kwa ncha ya mshale au mti wa kuwindia, na akamhalalisha. Na aliyeuawa kwa ubapa wa kitu, akahukumu kuwa ni haramu, kwa sababu alipigwa mpaka kufa. Huu ni mtazamo ambao wamewafikiana Wanazuoni *"Fuqahaau."*

Ama kwa mnyama aliyeanguka kutoka juu huku ametanguliza kichwa na akafa, pia nyama yake imeharamishwa. Ali bin Abi Talhah alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa mnyama anayekufa kwa kuangukia kichwa, "Ni yule anayeanguka kutoka mlimani."¹ Qatadah alisema, 'ni mnyama anayeangukia kisimani.'² As-suddi alisema kuwa, 'ni mnyama anayeanguka toka mlimani au anayeangukia kisimani.'³

Ama mnyama anayekufa kwa kuchomwa pembe na mnyama mwingine, pia ameharamishwa, hata kama pembe itasababisha kidonda kibichi na kutoa damu kwenye shingo mpaka akafa. Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا أَكَلِ السَّبُعُ

"Aliyeliwa na mnyama..."

Inahusu mnyama aliyeshambuliwa na simba, chui, mbweha au mbwa, kisha mnyama pori akala sehemu yake na akafa kwa sababu hiyo. Aina hii pia imeharamishwa, si halali kumla mnyama huyo kwa makubaliano ya pamoja ya wanawazuoni wa sharia *"Ijmai"*; hata kama mnyama alivuja damu kwenye shingo yake. Wakati wa zama za Jahiliyyah, watu walikuwa wakila kondoo, ngamia, au ngombe ambao waliliwa na wanyama pori, Allah تعالى Aliharamisha tabia hii kwa waumini. Kauli ya Allah تعالى,

إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ

"Ila mkimdiriki kumchinja."

kabla ya kufa, kutokana na sababu tulizoeleza hapo juu. Sehemu hii ya Ayah imeunganishwa na,

¹ At-Tabari 9:498.

² At-Tabari 9:498.

³ At-Tabari 9:498.

وَالْمُنْخَبِقَةَ وَالْمَوْقُودَةَ وَالْمُرْدِيَّةَ وَالنَّطِيحَةَ وَمَا أَكَلَ السَّبْعُ

“Na aliyekufa kwa kusongeka koo, na aliyekufa kwa kupigwa na aliyekufa kwa kuanguka na aliyekufa kwa kupigwa pembe na aliyeliwa na mnyama (akapoteza uhai),...”

Ali bin Abi Talhah alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alieleza kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ

“...ila mkimdiriki kumchinja.”

Anasema: ‘Kama utaweza kumchinja mnyama kama ilivyoelezwa katika Ayah wakati yu hai, basi mleni, huyo atakuwa amechinjwa.’¹ Sawa na hayo yalinukuliwa kutoka kwa Said bin Jubayr, Al-Hasan Al-Basri na As-Suddi.² Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ali رضي الله عنه alisema, “Endapo utaweza kumchinja mnyama aliyepigwa na kitu au kuangukia kichwa, au kwa kuchomwa na pembe na akawa ametikisa mguu wa mbele au wa nyuma, basi mle.”³ Kauli sawa na hiyo ilipokelewa kutoka kwa Tawus, Al-Hassan, Qatadah, Ubayd bin Umayr, Adh-Dhahhak na wengine, kuwa iwapo mnyama anayechinjwa atakapotikisika ambako kunafahamisha baada ya kumchinja kuwa alikuwa yu hai, basi mnyama huyo ni halali kuliwa.⁴ Sahihi Mbili zilinukuu kuwa Rafi bin Khadi رضي الله عنه alisema, “Nilimuuliza, Ewe Mtume ﷺ! Tunachelea kuwa tunaweza kukutana na adui yetu kesho na hatuna visu, tunaweza kuwachinja wanyama kwa vipande vya mti?’ Mtume ﷺ alisema,

«مَا أَنْهَرَ الدَّمَ، وَذَكَرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ، فَكُلُّوهُ، لَيْسَ السِّنُّ وَالظَّفْرُ، وَسَأَخَذْنَاكُمْ عَنْ ذَلِكَ: أَمَا السِّنُّ فَعَظْمٌ، وَأَمَا الظَّفْرُ فَمُدَى الْحَبَشَةِ»

“Mnaweza kutumia kinachosababisha damu kuchuruzika na mnaweza kula kilichochinjwa kwa Jina la Allah تعالى. Lakini msitumie meno au kucha (Kuchinjia). Nitakuelezeni sababu, ama meno ni mifupa, na makucha yalikuwa yakitumiwa na watu wa Ethiopia kuchinjia.”⁵

¹ At-Tabari 9: 502.

² At-Tabari 9: 504, 507.

³ At-Tabari 9: 503.

⁴ At-Tabari 9: 504.

⁵ Fat’hul Al-Bari 9:554, Muslim 3:1558.

Baadaye Allah تعالى Amesema,

وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ

“Na pia ni haramu kula nyama aliyechinjiwa masanamu.”

Nusub ni masanamu ya mawe yaliyojengwa kuzunguka Ka’bah kama walivyoeleza Mujahid na Ibn Jurayj.¹ Ibn Jurayj alisema, yalikuwepo masanamu mia tatu na sitini (kuzunguka Ka’bah), walikuwa Waarabu wakiyachinjia masanamu hayo, zama za Jahiliyyah. Walikuwa wakiyarushia damu ya wanyama walioletwa Ka’bah, na nyama yake ilikatakatwa vipande na kuiweka juu masanamu.² Allah تعالى Aliharamisha mwenendo huo kwa waumini. Pia Aliwaharamishia kula nyama ya wanyama hao, ambao walichinjwa kwa ajili ya masanamu, hata kama Jina la Allah تعالى lilitajwa wakati wa kuchinjwa wanyama hao, kwa sababu ni aina ya ushirikina ambayo Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷻ waliiharamisha.

Kuharamishwa Matumizi ya *Al-Azlam* kwa Kufanya Maamuzi.

Allah تعالى Amesema,

وَأَنْ تَسْتَقْسِمُوا بِالْأَزْلَمِ

“Na ni haramu kupiga ramli.”

Aya inaharamisha, “Enyi waumini! Mmekatazwa kutumia *Al-Azlam* (mishale) kwa kufanya maamuzi,” ambayo ilikuwa ni ada ya Waarabu wakati wa Jahiliyyah. Walitumia mishale mitatu, mmoja uliandikwa “Fanya” na mwingine ‘Usifanye’ ambapo wa tatu haukuandikwa chochote. Baadhi yao waliandika kwenye mshale wa kwanza. ‘Mola wangu aliniamrisha’, na, ‘Mola wangu amenikataza’ kwenye mshale wa pili; na hawakuandika chochote kwenye mshale wa tatu. Endapo aliokota mshale usio na maandishi, mtu aliendelea kujaribu mpaka apate mshale ulioandikwa ‘fanya’ au ‘usifanye’, na mtu huyo angelitekeleza amri aliyoiokota. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa *Azlam* ilikuwa mishale iliyotumika kupata maamuzi.³ Muhammad bin Is’haq رحمه الله تعالى na wengineo walisema kuwa *Azlam* ilikuwa mishale. Sanamu kuu la kabila la Quraysh liliitwa Hubal na lilisimikwa katika mdomo wa kisima ndani ya Ka’bah,

¹ At-Tabari 9:508.

² At-Tabari 9:508.

³ At-Tabari 9:515.

pahala zawadi zikiwasilishwa na mali ya Ka'bah ikihifadhiwa. Na pale kulikuwa na mishale saba ambayo waliitumia kupata ufumbuzi wa masuala yenye mgogoro. Ufumbuzi wowote utakaopatikana kupitia njia hiyo wanauendea, na wala hawaupingi.¹ Bukhari² alinukuu kuwa Mtume ﷺ alipoingia Ka'bah (baada ya kutoka Makkah) alikuta picha za Ibrahim عليه السلام na Ismail عليه السلام ndani yake huku wakiwa wakishuka, mikononi mwao wameshika mishale. Mtume ﷺ alisema,

«فَاتْلَهُمْ اللهُ لَقَدْ عَلِمُوا أَنَّهُمَا لَمْ يَسْتَقْسِمَا بِهَا أَبَدًا»

“Allah تعالى Awapige vita (Mushirikina)! Wanajua kuwa hawakutumia mishale katika kufanya maamuzi.”

Mujahid alitolea melezo Kauli ya Allah تعالى,

وَأَنْ تَسْتَقْسِمُوا بِالْأَزْلَمِ^٣

“Na ni haramu kupiga ramli.”

Hii ni mishale ambayo Waarabu wakiitumia, na ladu zilizotumiwa na Wafursi na Warumi kuchezea kamari.³ Kauli hii ya Mujahid, kuwa mishale hii ilitumika kwa kamari, si sahihi isipokuwa tukisema kuwa walitumia mishale wakati fulani kwa kuchezea kamari na wakati mwingine kufanya maamuzi. Allah تعالى ni Mjuzi Zaidi. Tunalazimika kutaja kuwa Allah تعالى Alitofautisha baina ya kupiga ramli *“Azlam”* na kucheza kamari katika mwisho wa Surah (5:90,91).

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْحَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ
الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقَعَ بَيْنَكُمْ الْعَدَاوَةَ
وَالْبَغْضَاءَ فِي الْحَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ ۗ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَبِهُونَ ﴿٩١﴾

“Enyi mlioamini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa. Hakika Shetani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mmeacha?”

¹ At-Tabari 9: 513.

² Fat'hul Al-Bari 6:446.

³ At-Tabari 9: 512.

Allah تعالى Anasema,

وَأَنْ تَسْتَقْسِمُوا بِالْأَزْلَمِ ذَلِكُمْ فِسْقٌ

“Na ni haramu kupiga ramli. Hayo yote ni upotovu.”

Maana: Vitendo vyote hivyo ni uasi, dhambi, upotofu, ujinga na juu ya yote hayo ni ushirikina. Allah تعالى Amewaamuru waumini kuchukua maamuzi kutoka Kwake, pindi wanapotaka kufanya jambo, kwanza kwa kumuabudu Yeye na kumuomba Awaongoze kufikia maamuzi juu ya jambo husika. Imam Ahmad, Bukhari na wakusanyaji wa Sunan waliandika kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alikuwa akitufundisha namna ya kufanya katika kutaka ushauri kwa Allah تعالى juu ya jambo fulani kama alivyotufundisha sura katika Qur'an na amesema;

«إِذَا هَمَّ أَحَدُكُمْ بِالْأَمْرِ فَلْيُرْكَعْ رَكَعَتَيْنِ مِنْ غَيْرِ الْفَرِيضَةِ، ثُمَّ لِيَقُلْ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْتَخِيرُكَ بِعِلْمِكَ، وَأَسْتَقْدِرُكَ بِقُدْرَتِكَ، وَأَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ الْعَظِيمِ، فَإِنَّكَ تَقْدِرُ وَلَا أَقْدِرُ وَتَعْلَمُ وَلَا أَعْلَمُ، وَأَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ، اللَّهُمَّ إِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا الْأَمْرَ - وَيَسْمِيهِ بِاسْمِهِ - خَيْرٌ لِي فِي دِينِي وَدُنْيَايَ وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي - أَوْ قَالَ: عَاجِلِ أَمْرِي وَآجِلِهِ - فَافْضُرْهُ لِي، وَيَسِّرْهُ لِي، ثُمَّ بَارِكْ لِي فِيهِ، اللَّهُمَّ وَإِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّهُ شَرٌّ لِي فِي دِينِي وَدُنْيَايَ وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي، فَاصْرِفْني عَنْهُ، وَاصْرِفْهُ عَنِّي، وَاقْدِرْ لِي الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ، ثُمَّ رَضِّنِي بِهِ»

“Mmoja wenu anapokusudia kufanya jambo lolote, asali Rakaa mbili, ambazo siyo za faradhi, na aseme (baada ya Sala), “Ewe Allah! Nakuomba muongozo kwa Ilmu Yako, kutokana na Uweza Wako na Nakuomba kwa Fadhila Zako kubwa, kwani Wewe ni Muweza nami sina uwezo, Unajua nisichokijua, Nawe Unajua Ghaib. Ewe Allah! Endapo Unajua kuwa jambo hili (ataje jambo hilo hapa) ni jema kwa Dini yangu, maisha yangu na akhera yangu (au alisema, kwa amali zangu za sasa na baadaye), hivyo nikadirie, na lifanye sahala kwangu nilipate na nibarikie. Ewe Allah! Na kama Unajua kuwa halina kheri nami katika Dini yangu na maisha yangu na Akhera yangu, basi liweke mbali nami na niwezeshe niwe mbali nalo. Nikadirie lolote lilo bora kwangu, na Uniwezeshe niliridhie.”¹

¹ Ahmad 3:344, Fat-h Al-Bari 3:58, Abu Dawud 2:187, Tuhfat Al-Ahwadhi 2:591, An-Nasai 6:80 na Ibn Majah 1:440.

Maneno ya Hadithi hii ni kama yalivyokusanywa na Ahmad na At-Tirmidhi aliitaja kuwa ni Hasan *Sahih* na *Gharib*."

Shetani na Makafiri Wamekata Tamaa na Dini ya Waislam.

Allah تعالی Amesema,

الْيَوْمَ يَمِيسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنَ دِينِكُمْ

"Leo waliokufuru wamekata tamaa na Dini yenu."

Ali bin Abi Talhah alimnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema; Kuwa Ayah hii maana yake, "Walipoteza matumaini kuwa Waislamu wataacha Dini yao."¹

Haya ni sawa na maneno ya Ata bin Abi Rabah, As-Suddi na Muqatil bin Hayyan.²

Maana hii inaungwa mkono na Hadithi iliyonukuliwa ndani ya *Sahih* ambayo inasema,

«إِنَّ الشَّيْطَانَ قَدْ يَمِيسَ أَنْ يَعْبُدَهُ الْمُصَلُّونَ فِي جَزِيرَةِ الْعَرَبِ، وَلَكِنْ بِالتَّحْرِيشِ بَيْنَهُمْ»

"Kwa hakika Shetani amepoteza matumaini kuwa wale wanaosali katika Rasi ya Arabia watamuabudu. Lakini ataendelea kuwafitini."³

Aidha kuna uwezekano kuwa Ayah inakanusha uwezekano wa makafiri na Shetani kuwa watakuwa kama Waislam, kwani Waislamu wana, sifa zinazopigana na ushirikina na watu wake. Kwa sababu hii, Allah تعالی Amewaamuru waja Wake waumini kuwa na subira, na kuwa thabiti kuwapinga makafiri, na wala wasimuogope yeyote isipokuwa Allah تعالی Pekee. Allah تعالی Amesema,

فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِ

"Basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi." Maana: Msiwaogope wao mnaposigana nao. Bali Niogopeni Mimi na Nitakupeni ushinde juu yao, Nitawatokomeza, na kuwafanya muwe juu yao. Nitaziliwaza nyoyo zenu na Kuwanyanyua daraja zenu juu yao hapa duniani na kesho Ahera.

¹ At-Tabari 9: 516.

² At-Tabari 9: 516.

³ Muslim 4:2166.

Ukamilishaji wa Dini ya Uislamu:

Allah تعالیٰ Amesema,

أَلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

“Leo Nimekukamiliishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni Neema Yangu, na Nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo Dini.”

Hii kwa hakika ni Fadhila kubwa kutoka kwa Allah تعالیٰ kwa ummah huu, kwani Amewakamilishia Dini yao, kwa hiyo, hawahitajii Dini nyingine au Mtume mwingine isipokuwa Muhammad ﷺ.

Kwa sababu hii Allah تعالیٰ Alimfanya Muhammad ﷺ awe Mtume wa mwisho na Alimpeleka kwa binadamu na majini.

Kwa hiyo, Halali ni Aliyoiruhusu na haramu ni aliyoharamisha, Sharia ni ile aliyoiweka na kila alichokiwasilisha ni hakika na kweli, na hakina upungufu au mgongano. Allah تعالیٰ Amesema,

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

“Na yametimia Maneno ya Mola Mlezi wako kwa kweli na uadilifu.”

Maana: Ni kweli kila alichokieleza na uadilifu katika yale anayoamuru na kukataza. Allah تعالیٰ Alipowakamilishia Waislamu Dini, Fadhila Zake zilikamilika pia. Allah تعالیٰ Amesema,

أَلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

“Leo Nimekukamiliishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni Neema Yangu, na Nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo Dini.”

Maana yake: Ukubalini Uislamu kwani ni Dini ambayo Allah تعالیٰ Anaipenda na Aliyokuchagulieni, na ni ambayo Alimtuma nayo Mjumbe bora na mtukufu na Akampa moja ya vitabu Vyake vitakatifu. Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ alimnukuu Harun bin Antarah baba yake alisema, ‘Wakati Aya,

أَلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ

“Leo Nimekukamiliishieni Dini yenu.”

Ilipoteremshwa, siku ya Arafah 'Umar رضي الله عنه alilia. Mtume ﷺ alimuuliza, 'Kitu gani kinakufanya ulie?' Akajibu, 'Kinachonifanya nilie ni kuwa Dini yetu imekamilishwa kwetu. Sasa imekamilishwa, hapana kilicho kamili, bali kinapungua thamani." Mtume ﷺ alisema,

«صَدَقْتُ»

"Umesema ukweli."¹

Kinachokabiliana na maana ya Hadithi hii ni Hadithi sahihi.

«إِنَّ الْإِسْلَامَ بَدَأَ غَرِيبًا، وَسَيَعُودُ غَرِيبًا، فَطُوبَىٰ لِلْغُرَبَاءِ»

"Uislamu ulikuwa mgeni mwanzoni, na utarejea kwenye ugeni tena.
Kwa hiyo, Tuba² kwa wageni."³

Imam Ahmad alinukuu kuwa Tariq bin Shihab alisema, "Myahudi alikuja kwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه, akasema, "Ewe kiongozi wa Waumini! Kuna ayah ndani ya Kitabu chenu inayosomwa na Waislamu wote, na kama ingeliteremshwa kwetu, tungefanya hiyo siku (iliyoteremshiwa) sikukuu. Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه akamuuliza, 'Ni ayah gani hiyo?' Myahudi akasema ni Kauli Yake Allah تعالى,

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَمَّمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي

"Leo Nimekukamiliishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni Neema Yangu..."

Umar رضي الله عنه alijibu, "Wallah! Najua lini na wapi aya hii ilipoteremshwa kwa Mtume ﷺ. Ilikuwa jioni, ya siku ya Arafah, siku ya Ijumaa."⁴

Bukhari aliinukuu Hadithi hii kupitia Al-Hasan bin As-Sabbah kutoka kwa Jafar bin Awn.⁵ Aidha Muslim, At-Tirmidhi na An-Nasai⁶ waliinukuu Hadithi hii.

¹ At-Tabari 9: 519.

² Tuba maana yake "habari njema", na pia ni mti wa Peponi. Angalia Tafsiri ya Surat Ar-Ra'd 13:29 (Juzuu ya tano).

³ Muslim 1:130.

⁴ Ahmad 1:38.

⁵ Fat'hul Al-Bari 1:129.

⁶ Muslim 4:2313, At-Tirmidhi Tuhfat Al-Ahwadhi 8:407 na An-Nasai 5:251.

Katika masimulizi yaliyokusanywa na Bukhari katika kitabu cha Tafsir, kupitia Tariq, alisema, “Mayahudi walimuambia Umar رضي الله عنه, ‘Wallah! Kuna aya inayosomwa na Waislamu wote na kama ingeliteremshwa kwetu, tungeifanya siku hiyo (iliyoteremshwa) siku ya sherehe.”

Umar رضي الله عنه alisema “Wallah! Najua lini na wapi aya hii ilipoteremshwa na pahala alipokuwa Mtume ﷺ ilipoteremshwa. Ilikuwa siku ya Arafah, na nilikuwa Arafah,¹ Wallahi.” Sufyan (mmoja wa wapokezi) ana wasiwasi kama Ijumaa ilitajwa katika mapokezi hayo.

Kuchanganyikiwa kwa Sufyan ni kwamba hakuwa na uhakika kuwa Shekhe wake aliingiza kauli hii katika Hadithi au hapana. Vinginevyo, iwapo walitia shaka yeye na Shekhe wake kuwa Arafah ya Hijja ya mwisho ya Mtume ﷺ ilikuwa siku ya Ijumaa; litakuwa ni kosa ambalo halikutoka kwa mtu kama Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى. Ukweli ni kuwa ilikuwa Ijumaa, ukweli huu unakubaliwa na wanazuoni wa Sirah na Fiqh. Kuna Hadithi kadha zinazokubaliana na ukweli huu ambazo ni Sahih na *Mutawatir*. Hadithi hii ilinukuliwa pia na Umar رضي الله عنه kupitia isnad mbalimbali.

Ruksa ya Kula Mnyama Mfu Katika Hali ya Dharura:

Allah تعالى Amesema,

فَمَنْ أَضْطُرَّ فِي مَخْمَصَةٍ غَيْرِ مُتَجَانِفٍ لِإِثْمِهِ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Na mwenye kushurutishwa na njaa, bila ya kupendelea dhambi, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye Kurehemu.”

Kwa hiyo, mmoja wenu anapolazimishwa na hali, kula katika vile vilivyoharamishwa, anaruhusiwa; na Allah تعالى ni Mwingi wa Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

Allah تعالى Anaelewa wazi mahitaji ya waja wake wakati wa dhiki, na Atawasamehe, na Kuwaghufiria waja Wake. Katika Musnad na Sahih ya Ibn Hibban, ilinukuliwa kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Jina linalotumika kwa riwaya ambayo kila isnadi ya usimulizi ina idadi kubwa ya wasimulizi wenye kuaminika katika kila hatua ya isnadi.

«إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ أَنْ تُؤْتَى رُحْمَتُهُ كَمَا بُكْرَهُ أَنْ تُؤْتَى مَعْصِيَتُهُ»

“Allah تعالى Anapenda Rukhsah yake itumiwe, kama Asivyopenda kuasiwa.”¹

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Waqid Al-Laythi alisema kuwa Masahaba waliuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Tunaishi katika ardhi inayokabiliwa na njaa kila mara. Kwa hiyo, wakati gani tunaruhusiwa kula nyamafu?” Mtume ﷺ alijibu,

«إِذَا لَمْ تَضْطَبِحُوا، وَلَمْ تَغْتَبُوا، وَلَمْ تَخْتَبِرُوا بَقَلًا فَسَأْنُكُمْ بِهَا»

“Kama hamkupata chakula cha asubuhi, au kinywaji cha mchana, wala kupata mboga mboga za kula, basi kuleni nyamafu.”

Imam Ahmad² pekee aliikusanya Hadithi hii na isnadi yake inakidhi vigezo vya Sahih Mbili. Allah تعالى Amesema,

غَيْرِ مُتَجَانِفٍ لِآثِمٍ³

“Bila ya kupendelea dhambi.”

Maana: Bila ya kumuasi Allah تعالى, Hakika Allah تعالى Ameruhusu hilo, na Amelinyamazia jingine kama Alivyosema,

فَمَنْ أَضْطُرُّ فِي مَحْمَصَةٍ غَيْرِ مُتَجَانِفٍ لِآثِمٍ³ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٠﴾

“Na mwenye kushurutishwa na njaa, bila ya kupendelea dhambi, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye Kurehemu.”

Baadhi ya wanazuoni walitumia Aya hii kama ushahidi kuwa wale wanaosafiri kwa lengo la kumuasi Allah تعالى hawaruhusiwi kutumia ruhusa za wasafiri kwa sababu hizi ruhusa hazipatikani kwa kuasi, na Allah Anajua zaidi.

* * *

¹ Ibn Hibban 4:182.

² Ahmad 5:218.

يَسْأَلُونَكَ مَاذَا أُحِلَّ لَهُمْ قُلْ أُحِلَّ لَكُمْ الطَّيِّبَاتُ وَمَا
 عَلَّمْتُم مِّنَ الْجَوَارِحِ مُكَلِّبِينَ تُعَلِّمُونَهُنَّ مِمَّا عَلَّمَكُمُ اللَّهُ
 فَكُلُوا مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَاذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ وَاتَّقُوا اللَّهَ
 ۚ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٤﴾ الْيَوْمَ أُحِلَّ لَكُمْ الطَّيِّبَاتُ
 وَطَعَامُ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حِلٌّ لَّكُمْ وَطَعَامُكُمْ حِلٌّ لَهُمْ
 وَالْمَخْضَبَاتُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْمَخْضَبَاتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا
 الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ إِذَا ءَاتَيْتُمُوهُنَّ أَجُوزَهُنَّ مَحْضَبِينَ غَيْرِ
 مُسْفِحِينَ وَلَا مُتَّخِذِي أَحْدَانٍ ۚ وَمَن يَكْفُرْ بِالْإِيمَانِ فَقَدْ
 حَبِطَ عَمَلُهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٥﴾ يَأْتِيهَا
 الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ
 وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى
 الْكَعْبَيْنِ ۚ وَإِن كُنْتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا ۚ وَإِن كُنْتُمْ مَّرْضَىٰ أَوْ
 عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُم مِّنَ الْغَائِطِ أَوْ لَمَسْتُمُ
 النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا
 بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِنْهُ ۚ مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ
 مِنْ حَرَجٍ وَلَٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ
 لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٦﴾

يَسْأَلُونَكَ مَاذَا أُحِلَّ لَهُمْ قُلْ أُحِلَّ لَكُمْ الطَّيِّبَاتُ وَمَا
 عَلَّمْتُم مِّنَ الْجَوَارِحِ مُكَلِّبِينَ تُعَلِّمُونَهُنَّ مِمَّا عَلَّمَكُمُ اللَّهُ
 فَكُلُوا مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَاذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ وَاتَّقُوا اللَّهَ
 ۚ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٤﴾

4. Wanakuuliza wamehalalishiwa nini? Sema: Mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri na mlichowafundisha wanyama kukiwinda. Mnawafundisha Alivyokufunzeni Mwenyezi Mungu. Basi kuleni wali-chokukamatieni, na mkisomee Jina la Mwenyezi Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu."

Ufafanuzi wa Vilivyo-halalishwa

Katika Aya iliyopita Allah ametaja aina ya

vyakula vilivyoharamishwa, vitu vichafu, vyenye madhara kwa mlaji, ima katika mwili wake, Dini yake au mawili yote kwa pamoja, isipokuwa wakati wa dharura.

وَقَدْ فَصَّلَ لَكُمْ مَا حَرَّمَ عَلَيْكُمْ إِلَّا مَا اضْطُرَّرْتُمْ إِلَيْهِ ۚ

"Naye Amekwisha kubainishieni Alivyokuharimishieni, isipokuwa vile mnavyolazimishwa?"

Baada ya hapo Allah تعالى Amesema,

يَسْأَلُونَكَ مَاذَا أُحِلَّ لَهُمْ قُلْ أُحِلَّ لَكُمْ الطَّيِّبَاتُ

“Wanakuuliza wamehalalishiwa nini? Sema: Mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri...”

Katika Surat Al-Araf Allah تعالى Amemuelezea Muhammad ﷺ akiruhusu vitu vizuri na akiharamisha vitu vichafu. Muqatil alisema *At-Tayyibat* ni pamoja na kila kitu Waislamu walichoruhusiwa na aina tofauti ya vyakula vilivyoruhusiwa, “Kuna wakati mmoja Az-Zuhari aliulizwa juu ya kunywa mkojo kama aina ya dawa na alisema kuwa si aina ya vitu vizuri.” Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى naye alisimulia maneno haya.

Rukxa ya Kutumia Wanyama¹ Waliopewa Mafunzo ya Kuwinda

Allah تعالى Amesema:

وَمَا عَلَّمْتُم مِّنَ الْجَوَارِحِ مُكَلِّبِينَ

“...na mlichowafundisha wanyama kukiwinda.”

Ni halali kwenu wanyama waliochinjwa kwa Jina la Allah تعالى na vitu vizuri kwa mlo. Kadhalika ni halali kwenu viwindwa mlivyoviwinda kwa njia ya wanyama waliotunzwa, mfano mbwa, simba, vipanga, n.k.

Huu ni mtazamo wa jopo la wanazuoni wa sharia ya Kiislamu (Jamhuri) wakiwemo Masahaba, Tabii na Maimamu. Na katika waliosema hivyo ni Ali bin Abi Talhah, aliyeeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَمَا عَلَّمْتُم مِّنَ الْجَوَارِحِ مُكَلِّبِينَ

“...na mlichowafundisha wanyama kukiwinda.”

Inakusudiwa Mbwa waliofunzwa, vipanga na aina zote za ndege na wanyama waliofunzwa kuwinda. Hii ni pamoja na mbwa, paka shume, vipanga na

¹ Mnyama wa kuwindia.

kadhalika.¹ Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alikusanya Hadithi hii na alisema, "Sawa na hiyo ilinukuliwa kutoka kwa Khaythamah, Tawus, Mujahid, Makhul na Yahya bin Abi Kathir."² Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Ibn Umar رضي الله عنه kuwa, "Ibn Umar رضي الله عنه alisema, Mmehalalishiwa wanyama waliowindwa na ndege waliofunzwa, kama vile vipanga iwapo mtawashika kabla hawajala. Vinginevyo msile nyama yao."³ Nasema, wanazuoni wengi wanasema kuwa kuwinda na Ndege aliyefunzwa ni sawa na kuwinda na Mbwa aliyefunzwa, kwa sababu ndege hukamata wanyama kwa makucha yao, kama mbwa, kwa hiyo hapana tofauti kati yao wawili. Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliruhusu kuwa Adi bin Hatim alisema kuwa alimuuliza Mtume ﷺ, naye alisema,

«مَا أَمْسَكَ عَنْكَ كُلُّ»

"Chochote unachokimata kula."⁴

Wanyama hawa wafunzwao kuwinda huitwa *Jawarir*, kwa Kiarabu limenyumbuliwa kutoka neno '*Jarh*', maana yake achumacho mtu. Waarabu wanasena "Fulani bin Fulani hana *Jarih*." Maana: Mlezi. Aidha Allah تعالى Alisema,

وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُم بِالنَّهَارِ

"...na Anakijua mlichofanya mchana."

Maana: Jema au uovu ulilochuma au kufanya.

Kauli ya Allah تعالى,

مُكَلِّبِينَ

"...kukiwinda."

Waliofunzwa kuwinda kama mbwa aliyefunzwa kwa maana washike viwindwa hivyo kwa kucha zao. Kama mnyama akiwa ameuawa kwa kupigwa kumbo na si kwa makucha yake, basi si ruhusa kumla mnyama huyo.

¹ At-Tabari 9: 548.

² At-Tabari 9: 547-548.

³ At-Tabari 9: 549.

⁴ At-Tabari 9: 550.

Allah تعالى Amesema,

تُعَلِّمُونَهُنَّ مِمَّا عَلَّمَكُمُ اللَّهُ

"Mnawafundisha Alivyokufunzeni Mwenyezi Mungu."

Wakati mnyama atapotumwa, humkimbiza, na anapomkamata hicho kiwindwa huwa nacho mpaka bwana wake afike; na wala hakamati kwa nafsi yake mwenyewe.

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema hapa,

فَكُلُوا مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَاذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ

"Basi kuleni walichokukamatieni, na mkisomee Jina la Mwenyezi Mungu."

Mnyama anapopewa mafunzo, na akashika kiwindwa baada ya aliyemtuma kusema "Bismillah", basi ni halali kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni, hata kama kiwinda hicho kilikufa. Kuna Hadithi katika sunnah zinazoafikiana na kauli hii. Kama ilivyothibiti katika sahihi mbili kuwa Adi bin Hatim alisema, "Nilisema Ewe Mtume! Niliwatuma mbwa kuwinda na nilitamka Jina la Allah!" Alijibu:

«إِذَا أُرْسِلَتْ كَلْبِكَ الْمُعَلَّمِ وَذَكَرْتَ اسْمَ اللَّهِ فَكُلْ مَا أَمْسَكَ عَلَيْكَ»

"Iwapo, Utataja Jina la Allah تعالى, na ukamtuma mbwa wako aliyepewa mafunzo maalumu na akamkamata mnyama, ni halali kukila alichokishika."

Nikauliza, 'Hata kama atamuua mnyama?' Alijibu,

«وَإِنْ قَتَلَنَ، مَا لَمْ يَشْرَحْهَا كَلْبٌ لَيْسَ مِنْهَا، فَإِنَّكَ إِنَّمَا سَمَّيْتَ عَلَى كَلْبِكَ وَلَمْ تَسْمِ عَلَى غَيْرِهِ»

"Hata kama atamuua mnyama, isipokuwa mbwa mwingine akimsaidia, kwani ulitamka Jina la Allah تعالى ulipomtuma mbwa wako, lakini sio mbwa mwingine."

Nikauliza, 'Hakika mimi ninarusha mkuki kisha ukapata kiwindwa?' Akajibu, 'Kama mnyama atachomwa na ncha yake, mle lakini ikipigwa bapa lake, usimle, kwani atakuwa amepigwa mpaka kufa.' Katika masimulizi mengine, Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا رَمَيْتَ بِالْمِعْرَاضِ فَخَرِّقْ نُكْلَهُ، وَإِنْ أَصَابَهُ بِعَرَضٍ فَإِنَّهُ وَبِيذٌ فَلَا تَأْكُلْهُ»

*"Ikiwa mnyama wa kuwindwa atapigwa na kitu chenye ncha kali, kula, lakini akipigwa upande usio na makali, usile, kwa sababu amepigwa ndipo akafa."*¹

Katika masimulizi mengine, Mtume ﷺ amesema,

«وَإِذَا أُرْسِلَتْ كَلْبِكَ فَادْكُرِ اسْمَ اللَّهِ، فَإِنْ أَمْسَكَ عَلَيْكَ، فَأَذْرِكْتَهُ حَيًّا فَادْبَحْهُ، وَإِنْ أَدْرِكْتَهُ فَذَقْتَلْ وَلَمْ يَأْكُلْ مِنْهُ فَكُلْهُ، فَإِنْ أَخَذَ الْكَلْبُ ذِكَاثَهُ»

*"Endapo utamtuma mbwa wako kwenda kuwinda na ukataja Jina la Allah تعالى; chochote atakachowinda na ukakikuta hai, kichinje. Ukimkuta mnyama amekufa na mbwa wako hakula sehemu yake, weye kula, kwani kushika kwa mbwa ndio kuchinja."*²

Aidha katika masimulizi ya sahihi mbili, Mtume ﷺ alisema,

«فَإِنْ أَكَلَ فَلَا تَأْكُلْ، فَإِنِّي أَخَافُ أَنْ يَكُونَ أَمْسَكَ عَلَى نَفْسِهِ»

*"Pindipo mbwa atamla mnyama, msimle kwa kuchelea kuwa amewinda kwa ajili yake mwenyewe."*³

Kusema *Bismillahi* wakati wa Kumtuma Mnyama Aliyepewa Mafunzo Maalumu ya Kuwinda

Allah تعالى Amesema:

فَكُلُوا مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَادْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ ط

"Basi kuleni walichokukamatieni, na mkisomee Jina la Mwenyezi Mungu."

² Fat'hul Al-Bari 9:527, Muslim 3:1529.

³ Fat'hul Al-Bari 9:513, Muslim 3:1530.

³ Fat'hul Al-Bari 9:527, Muslim 3:1529.

Maana: Mnapomtuma. Mtume ﷺ alimuambia Adi bin Hatim,

«إِذَا أُرْسِلْتَ كَلِّبَكَ الْمُعَلِّمَ، وَذَكَرْتَ اسْمَ اللَّهِ، فَكُلْ مَا أَمْسَكَ عَلَيْكَ»

“Mnapomtuma mbwa wako uliyemfunza na ukataja Jina la Allah, kula kutokana na alichokikamata.”¹

Ilinukuliwa katika Sahih Mbili kuwa Abu Thalabah رضي الله عنه alipokea kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا أُرْسِلْتَ كَلِّبَكَ فَادْكُرْ اسْمَ اللَّهِ، وَإِذَا رَمَيْتَ بِسَهْمِكَ فَادْكُرْ اسْمَ اللَّهِ»

“Iwapo utamtuma mbwa wako mwindaji, taja Jina la Allah تعالى. Unapolenga mshale, taja Jina la Allah.”²

Ali bin Abi Talhah amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa aliitolea maelezo Aya hii

وَأَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ

“Sema ‘Kwa Jina la Allah!’”

Ukisahau hapana madhara.³ Aidha imesemwa kusudio la kuwa Ayah hii inaamrisha kutaja Jina la Allah تعالى kabla ya kula. Iliandikwa katika Sahih Mbili kuwa Mtume ﷺ alimfundisha mtoto wake wa kambo, Umar bin Abu Salamah رضي الله عنه, akisema,

«اسْمُ اللَّهِ وَكُلْ بِيَمِينِكَ وَكُلْ مِمَّا بِيَمِينِكَ»

“Taja Jina la Allah تعالى, kula kwa mkono wako wa kulia, na kula upande wa sahani ulio mbele yako.”⁴

Bukhari alinukuu kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Watu waliuliza, Ewe Mjumbe wa Allah! Baadhi ya watu – walisilimu karibuni – walituletea nyama ambayo hatujui kama Jina la Allah تعالى lilitajwa au halikutajwa wakati wa kuchinjwa! Alijibu,

«سَمُّوا اللَّهَ أَنْتُمْ وَكُلُوا»

“Tajeni Jina la Allah تعالى na muile.”⁵

¹ Fat’hul Al-Bari 9:524.

² Fat’hul Al-Bari 9:527, Muslim 3:1532.

³ At-Tabari 9: 571.

⁴ Fat’hul Al-Bari 9:431, Muslim 3:1599.

⁵ Fat’hul Al-Bari 9:550.

الْيَوْمَ أُحِلَّ لَكُمْ الطَّيِّبَاتُ وَطَعَامُ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حِلٌّ لَكُمْ وَطَعَامُكُمْ حِلٌّ لَهُمْ
وَالْحَصْنَةُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْحَصْنَةُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ إِذَا
ءَاتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسْفِحِينَ وَلَا مُتَّخِذِي أَخْدَانٍ ۗ وَمَنْ يَكْفُرْ بِالْإِيمَانِ
فَقَدْ حَبِطَ عَمَلُهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَسِيرِينَ ﴿٥﴾

5. Leo mmehalalishiwa kula vilivyo vizuri. Na chakula cha waliopewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali kwao. Na pia wanawake wema miongoni mwa Waumini, na wanawake wema miongoni mwa waliopewa Kitabu kabla yenu, mtakapo wapa mahari yao, mkafunga nao ndoa, bila ya kufanya uasharati wala kuwaweka kinyumba. Na anayekataa kuamini bila shaka amali yake imepotea, naye katika Akhera atakuwa miongoni mwa wenye khasara.

Uhalali wa Kula Nyama Iliyochinjwa na Watu Waliopewa Kitabu:

Baada ya Allah تعالی Kutaja vitu vichafu Alivyowaharamishia waja Wake waumini na vizuri Alivyowahalalishia Alisema,

الْيَوْمَ أُحِلَّ لَكُمْ الطَّيِّبَاتُ

“Leo mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri.”

Kisha, Allah تعالی Akataja hukumu juu ya wanyama wanaochinjwa na Watu wa Kitabu, Mayahudi na Wakristo,

وَطَعَامُ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حِلٌّ لَكُمْ

“Na chakula cha waliopewa Kitabu ni halali kwenu,…”

Maana: Wanyama waliochinja, kama walivyosema: Ibn Abbas, Abu Umamah, Mujahid, Said bin Jubayr, Ikrimah, Ata, Al-Hasan, Mak’hul, Ibrahim An-Nakhai, As-Suudi na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم¹. Hukumu hii ya kuhalalishiwa Waislamu kula wanyama waliochinjwa na watu wa kitabu inakubaliwa na wanazuoni, kwa sababu Watu wa Kitabu wanaharamishwa kuchinjwa kwa

¹ At-Tabari 9:573-577.

Jina lisilokuwa la Allah تعالى. Na wala hawataji wakati wa kuchinja isipokuwa Jina la Allah تعالى. Japokuwa wana imani potofu, juu ya Allah تعالى ambazo hazimstahiki Mola Mtukufu.

Imenukuliwa katika Sahih kuwa Abdullah bin Mughaffal رضي الله عنه alisema, "Tulipokuwa tunashambulia ngome ya Khaibar, mtu mmoja alitupa mkoba wa ngozi uliokuwa na mafuta, na nikaukimbilia kuuchukua na nilisema, "Sitompa mtu chochote kilichomo ndani ya mfuko huu leo." Lakini nilipogeuka nilimuona Mtume ﷺ (amesimama nyuma yangu) huku akitabasamu,¹ "Wanazuoni wanategemea Hadithi hii kama ushahidi kuwa tunaruhusiwa kula kutokana na ngawira kabla haijagaiwa. Wanazuoni wa madhehebu ya Hanafi, Shafii na Hambali wanategemea Hadithi hii kuhalalisha kula wanyama waliochinjwa na Mayahudi waliojiharamishia wenyewe, kama vile mafuta. Waliitumia Hadithi hii kama ushahidi dhidi ya wanazuoni wa Madhhab ya Maliki waliopinga hukumu hii." Ushahidi mzuri ni Hadithi iliyoandikwa katika Sahih kuwa watu wa Khaybar walimpa Mtume ﷺ zawadi ya paja la kondoo lililochomwa, lenye sumu. Mtume ﷺ alipenda kula paja la kondoo na alikula kipande, lakini kilimuambia Mtume ﷺ kuwa kiliathiri paa la kinywa chake, ambapo Bishr bin Al-Bara bin Marur رضي الله عنه alikufa baada ya kula nyama ya kondoo huyo. Mtume ﷺ aliamuru mwanamke wa Kiyahudi, Zaynab, aliyemtia sumu kondoo auawe, kwa hiyo, Mtume ﷺ na Masahaba zake walitaka kula kondoo yule na hawakuwauliza Mayahudi endapo waliondoa kile Mayahudi walichoamini kilichoharamishwa kwao, kama vile mafuta.² Kauli ya Allah تعالى,

وَطَعَامُكُمْ حَلَالٌ هُمْ

"...na **chakula chenu ni halali kwao.**" Maana: Mmeruhusiwa kuwalisha kutokana na wanyama mliowachinja. Kwa hiyo, sehemu hii ya Ayah si ya kuwaarifu Watu wa Kitabu kuwa wanaruhusiwa kula vyakula vyetu. Isipokuwa tuliichukulia kama taarifa kuwa ni kweli kuhusu hukumu waliyo kuwa nayo. Yaani, kuwa waliruhusiwa aina zote za vyakula vilivyo tajiwa Jina la Allah تعالى, ima vilichinjwa kwa mujibu wa dini yao au vinginevyo. Maelezo ya mwanzo yanakubalika zaidi. Kwa hiyo ina maana: mnaruhusiwa kuwalisha kutokana na wanyama mliowachinja kama ambavyo inaruhusiwa kula vyao, katika kuamiliana kwenye usawa. Mtume ﷺ alimpa nguo yake Abdullah bin Ubbay

¹ Fat'h Al-Bari 9:552.

² Fat'h Al-Bari 7:569.

bin Salul, ambayo alikafiniwa nayo alipokufa. Wanasema kuwa yeye Mtume ﷺ alifanya hivyo kwa sababu Abdullah alimpa kilemba chake Abbas رضي الله عنه, wakati Al-Abbas رضي الله عنه alipokuja Madinah. Ama kuhusu Hadithi

«لَا تَصْحَبْ إِلَّا مُؤْمِنًا ، وَلَا يَأْكُلْ طَعَامَكَ إِلَّا تَقِيًّا»

“Usifanye ushuba na asiye kuwa Muislamu, wala asile chakula chako ila Taqi.”¹

Hii ni kushajiisha mwenendo huo, na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

Ruhusa ya Kuwaoa Wanawake Safi wa Watu Waliopewa Kitabu:

Allah تعالى Amesema,

وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ

“Na wanawake wema miongoni mwa waumini.”

Aya inaeleza: Mnaruhusiwa kuwaoa wanawake huru, safi na waumini. Ayah inawazungumzia wanawake wasio wazinifu, ‘safi’.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyengine.

مُحْصَنَاتٍ غَيْرِ مُسَفِّحَاتٍ وَلَا مُتَّخِذَاتِ أَخْدَانٍ

“Wanawake wema, si makahaba wala si mahawara.” (4:25)

Abdullah Ibn Umar رضي الله عنهما alikuwa haoni haja ya kuwaoa wanawake wa kikristo, akisema, “Sijaona ushirikina mbaya zaidi kama mwanamke kusema Isa عليه السلام ni Mola wake, ambapo Allah تعالى Amesema:

وَلَا تَنكِحُوا الْمُشْرِكَةَ حَتَّىٰ يُؤْمِنَ

“Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini.”

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Abu Malik Al-Ghifari alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa wakati Aya ilipoteremshwa,

وَلَا تَنكِحُوا الْمُشْرِكَةَ حَتَّىٰ يُؤْمِنَ

“Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini.”

Watu hawakuoa wanawake wa kipagani. Wakati Aya ifuatayo ilipoteremshwa,

¹ Abu Dawud 5:167. ‘Abdullah bin Ubayy alikuwa akijulikana kuwa ni mnafiki.

وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ

“...na wanawake wema miongoni mwa waliopewa Kitabu kabla yenu...”

Walioa wanawake wa watu waliopewa Kitabu, “Baadhi ya Masahaba walioa wanawake wa Kikristo na hawakuona tatizo kwa hilo, wakitegemea Aya tukufu.

وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ

“...na wanawake wema miongoni mwa waliopewa Kitabu kabla yenu...”

Hivyo waliifanya Aya hii kuwa badala ya Aya iliyo katika Surat Al-Baqarah,

وَلَا تُنْكِحُوا الْمُشْرِكِينَ حَتَّى يُؤْمِنُوا

“Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini.”

Wakizingatia kuwa Aya ya mwisho inawajumuisha watu wa Kitabu katika maana yake ya jumla. Hapana mgongano hapa, ambapo Watu wa Kitabu walitajwa peke yao na wakatenganishwa na washirikina. Kama Kauli Yake Allah تعالى,

لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ مُنْفَكِينَ حَتَّى تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ﴿٦﴾

“Hawakuwa waliokufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu na washirikina waache walionayo mpaka iwajie bayana...”

Na kama Kauli Yake Allah تعالى,

﴿وَقُلْ لِلَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْأَيْمَانَ أَسْلَمْتُمْ إِنْ أَسْلَمُوا فَقَدِ اهْتَدَوْا﴾

“Na waambie waliopewa Kitabu na wasio na kisomo: Je! Mmesilimu? Wakasilimu basi wameongoka.”

Baadaye Allah تعالى Amesema,

إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ

“Mtakapowapa mahari yao...”

Hii inahusu mahari, ili muradi wanawake hao ni safi na watukufu, basi wapeni Mahari kwa moyo mkunjufu. Inafaa kutaja hapa kuwa Jabir bin Abdullah, Amir

Ash-Shabi, Ibrahim An-Nakhai na Al-Hassan Al-Basri walieleza kuwa mwanaume anapomuo mwanamke, na akazini mwanamke huyo kabla ya kumjamii, ndoa itabatilika. Katika hali hii, atarejesha Mahari aliyopewa na mume.¹

Allah تعالى Amesema,

مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسْفِحِينَ وَلَا مُتَّخِذِي أَخْدَانٍ^١

“Mkafunga nao ndoa, bila ya kufanya uasharati wala kuwaweka kinyumba.”

Kama ambavyo wanawake lazima wawe safi na kujiepusha na zina, hali hiyo inatakiwa iwepo kwa wanaume. Kwa hiyo Allah تعالى Amesema,

غَيْرَ مُسْفِحِينَ

“Bila ya kufanya uasharati.”

Kama wazinifu wafanyavyo, wala wasijiepushe na makosa, wala kukataa kuzini na yule anayewataka kufanya hivyo.

وَلَا مُتَّخِذِي أَخْدَانٍ^١

“Wala kuwaweka kinyumba.”

Maana: Wale wenye mahawara na marafiki wa kike ambao wanazini nao, kama tulivyotaja katika maelezo ya Surat An-Nisai.

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ
وَأَمْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ^٢ وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا^٣ وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَى
أَوْ عَلَى سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ أَوْ لَمَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا
صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِنْهُ^٤ مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ
حَرَجٍ وَلَٰكِنْ يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٥﴾

¹ At-Tabari 9: 585-586.

6. Enyi mlioamini! Mnaposimama kwa ajili ya Sala basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba basi ogeni. Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni vumbi lilio safi, na mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu; bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru."

Amri ya Kuchukua Udhu kwa Ajili ya Sala.

Allah تعالیٰ Amesema,

إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ

"Mnaposimama kwa ajili ya Sala."

Aya inaamrisha kuchukua udhu wakati wa kusali. Lakini udhu kwa yule ambaye hana kabisa ni wajibu juu yake. Na yule ambaye anao ni Sunna juu yake. Inasemekana mwanzoni mwa Uislamu. Waislamu walikuwa wanatawadha kwa kila Sala, lakini baadaye, amri hii ilifutwa. Imam Ahmad bin Hanbal رحمه الله تعالیٰ alinukuu kutoka kwa Sulaiman bin Buraydah, alisema kuwa baba yake alisema, Mtume ﷺ alikuwa akichukua Udhu kabla ya kila Sala. Siku ya ufunguzi wa Makka, alichukua udhu na akapaka Khofu zake na akasali Sala tano na Udhu mmoja. Umar رضي الله عنه akamuambia, 'Ewe mjumbe wa Allah! Umefanya jambo jipya ambalo hukuwahi kulifanya kabla." Mtume ﷺ akasema,

«إني عمدا فعلته يا عمر»

"Nilifanya kwa kukusudia Ewe Umar!"¹

Aidha Muslim² na wakusanyaji wa Sunan waliinukuu Hadithi hii. At-Tirmidhi alisema kuwa ni "Hasan sahih"³

¹ Ahmad 5:358.

² Muslm 1:232.

³ Abu Dawud 1:120, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 1:194, An-Nasai 1:86, Ibn Majah 1:170.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Al-Fadhli bin Al-Mubashir alisema, "Nilimuona Jabir bin Abdullah akisali Sala kadhaa kwa Udhu mmoja tu. Alipokwenda msalani, alitawadha na kupaka juu ya Khufu zake kwa mikono yake yenye maji maji, Nikasema, 'Ewe Abu Abdullah! Unafanya hivyo kwa utashi wako mwenyewe au?' Akasema, 'Kwa uhakika, Nilimuona Mtume ﷺ akifanya vivyo hivyo.¹ Hivyo, Nafanya nilichokiona akifanya Mtume ﷺ." Ibn Majah pia aliiandika Hadith hii.² Ahmad alinukuu kuwa Ubaydullah bin Abdullah bin Umar aliulizwa; "Je, ulimuona Abdullah bin Umar akichukua udhu kwa kila Sala, ima alikuwa safi au la?" Hivyo akajibu, "Asma bint Zayd bin Al-Khattab alimuambia kuwa Abdullah bin Hanzalah bin Abi Amir *Al-Ghasil* alimuambia kuwa Mtume ﷺ mwanzo aliamrisha kuchukua udhu kwa kila Sala, ima alikuwa tohara au la. Hilo lilipokuwa gumu kwake, aliamrisha kupiga mswaki kwa kila Sala na kuchukua udhu anapopata *Hadathi*. Abdullah (Ibn Umar) رضي الله عنه alidhani kuwa aliweza kufanya hivyo (kutawadha kwa kila Sala) na aliendelea kufanya hivyo mpaka alipofariki." Kama hivyo amepokea Dawud. Hadithi hii na katika mwenendo huu wa Ibn Umar رضي الله عنه unaonesha kuwa inapendekezwa na si lazima kuchukua Udhu kwa kila Sala. Na hii pia ni rai ya wanazuoni wengi.³ Abu Dawud⁴ alinukuu kuwa Abdullah bin Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alitoka msalani, hivyo wakamletea chakula. Wakamuuliza, "Tukuletee maji yako ya kutawadha?" Akasema,

«إِنَّمَا أَمْرْتُ بِالْوُضُوءِ إِذَا قُمْتُ إِلَى الصَّلَاةِ»

*"Hakika si vingine nimeamrisha kuchukua udhu ninaposimama kwa ajili ya Sala."*⁵

At-Tirmidh na An-Nasai⁶ waliandika Hadithi hii; na At-Tirmidhi alisema "Hadithi hii ni *Hasan*."

¹ At-Tabari 10:11.

² Ibn Majah 1:170.

³ Ahmad 5:225.

⁴ Abu Dawud 1:41.

⁵ Abu Dawud 4:36.

⁶ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 5:579 na An-Nasai 1:85.

Muslim alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Tulikuwa na Mtume ﷺ. Alipokwenda kujisaidia na aliporejea, aliletewa chakula, aliulizwa, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Unataka kuchukua udhu?' Akajibu,

«لِمَ؟ أَأَصْلِي فَأَتَوَضَّأُ»

"Kwa nini? Kwani nataka kusali hata nichukue udhu?"¹

Kutia Nia na Kutaja Jina la Allah تعالى kwa Ajili ya Udhu

Allah تعالى Amesema,

فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ

"Basi osheni nyuso zenu,..."

Wajibu wa kutia nia kabla ya udhu umethibitishwa na Aya hii,

إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ

"Mnaposimama kwa ajili ya Sala basi osheni nyuso zenu,..."

Hii ni sawa na msembo wa waarabu, "umuonapo kiongozi, usimame." Maana yake msimamieni.

Na sahihi mbili zimenukuu Hadithi ifuatayo,

«الْأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ وَإِنَّمَا لِكُلِّ امْرِئٍ مَّا نَوَىٰ»

"Hakika si vingine matendo yote yanategemea nia, na kila mtu atalipwa kwa nia yake."²

Pia imefaradhishwa kutaja Jina la Allah تعالى kwa ajili ya udhu. Hadithi iliyosimuliwa na Masahaba wengi inaeleza kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا وُضُوءَ لِمَنْ لَمْ يَذْكُرِ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ»

"Hana udhu yule asiyetaja Jina la Allah تعالى wakati wa kutawadha."³

¹ Muslim 1:283.

² Fat'hul Al-Bari 1:15, Muslm 3:1515.

³ Abu Dawud 1:75.

Aidha, imependekezwa kuosha mkono kabla ya kuutumbukiza ndani ya chombo chenye maji, hasa mara baada ya kuamka usingizini. Kwani sahihi mbili zilinukuu kuwa Abu Hurayra رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا اسْتَيْقَظَ أَحَدُكُمْ مِنْ نَوْمِهِ فَلَا يُدْخِلْ يَدَهُ فِي الْإِنَاءِ قَبْلَ أَنْ يَغْسِلَهَا ثَلَاثًا، فَإِنَّ أَحَدَكُمْ لَا يَدْرِي أَيْنَ بَاتَتْ يَدُهُ»

"Mmoja wenu anapoamka kutoka usingizini, asitumbukize mkono wake ndani ya chungu mpaka auoshe mara tatu, kwani mmoja wenu hajui mkono wake ulishika kitu gani usiku."³

Kwa mujibu wa wanazuoni wa Fiqh, uso unaanzia pale mstari wa nywele za kichwa kinapoanzia, bila kujali kuwepo kwa nywele au wingi wake, mpaka mwisho wa taya mbili na kidevu, na kutoka sikio hadi sikio.

Kuchana Ndevu kwa Vidole Wakati wa Kutia udhu

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Wail alisema, "Nilimuona Uthman رضي الله عنه alipokuwa anatekeleza udhu. Alipokuwa akiosha uso wake alichana ndevu zake kwa vidole vyake mara tatu, na alisema 'Nilimuona Mtume ﷺ akifanya hivyo mlivyoona nikifanya."¹ At-Tirmidh na Ibn Majah² pia waliinukuu Hadithi hii –Tirmidh aliipa daraja ya "Hasan sahihi" Ambayo Bukhari aliipa daraja ya Hasan.

Namna ya Kuchukua Udhu.

Imam Ahmad alinukuu kuwa, 'Ibn Abbas رضي الله عنهما wakati mmoja alitekeleza udhu na alichukua maji kwenye kiganja cha mkono na akasukutua kinywa na akapandisha maji puani. Akachukua tena maji kwenye kiganja na akakutanisha viganja vyake na kuosha uso wake. Akachukua tena maji kiganjani na akaosha mkono wake wa kulia, na kiganja kingine akaosha mkono wa kushoto. Kisha akapaka kichwa chake. Baadaye, akachukua maji yaliyojaa kiganja chake na

¹ Fat'hul Al-Bari 1:316, Muslim 1:233.

² Jamiu' Al-Masanid was-Sunan 17:197.

³ Tuhfat Al-Ahwaadhi 1:133 na Ibn Majah 1:148.

akayamiminia mguu wa kulia na kuosha. Kisha kama hivyo kwa mguu wa kushoto. Alipomaliza alisema, "Hivi ndivyo nilivyomuona Mtume ﷺ akitekeleza Udhu."¹ Bukhari pia aliinukuu Hadithi hii.² Allah تعالى Amesema,

وَأَيِّدِيكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ

"Na mikono yenu mpaka vifundoni..."

Maana: pamoja na viwiko. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine [Akitumia "Ila-" kwa maana ya pamoja].

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ إِلَىٰ أَمْوَالِكُمْ إِنَّهُ كَانَ حُوبًا كَبِيرًا

"Wala msile mali zao (ila-) pamoja na mali zenu. Hakika yote hayo ni jukumu kubwa."

Imependekezwa kwa wale wanaochukuaa Udhu waoshe sehemu ya juu ya mkono na kiwiko. Bukhari na Muslim walinukuu kuwa Abu Hurayra رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ أُمَّتِي يُدْعَوْنَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ غُرًّا مُحَجَّلِينَ مِنْ آثَارِ الْوُضُوءِ، فَمَنْ اسْتَطَاعَ يَنْكُمُ أَنْ يُطِيلَ غُرَّتَهُ فَلْيَفْعَلْ»

*"Siku ya kiyama, Ummah wangu utaitwa kwa ule weupe wenye kung'aa kwa sababu ya athari za Udhu, kwa hiyo yeyote awezaye kuongeza eneo la nuru yake afanye hivyo."*³

Muslim alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema: "Nilimsikia rafiki yangu wa ndani akisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema:

«تَبْلُغُ الْحِلْيَةَ مِنَ الْمُؤْمِنِ حَيْثُ يَبْلُغُ الْوُضُوءَ»

*"Miale ya nuru ya muumini inafika maeneo yanayofikiwa na maji ya udhu wake."*⁴

¹ Ahmad 1:268.

² Fat'hul Al-Bari 1:290.

³ Fat'hul Al-Bari 1:283, Muslim 1:216.

⁴ Muslim 1:219.

Baadaye Allah تعالى Amesema,

وَأَمْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ

“Na mpake nyuso zenu...”

Imeandikwa katika sahihi mbili kutoka kwa Malik bin Amir bin Yahya Al-Mazini kutoka kwa baba yake, alisema kuwa mtu mmoja alimuambia Abdullah bin Zaud bin Asim, babu yake Amr bin Yahya, na mmoja wa Masahaba wa Mtume ﷺ, “Je, unaweza kunionesha namna Mtume ﷺ alivyokuwa akitekeleza Udhu?” Abdullah bin Zayd alijibu, “Ndiyo.” Kisha aliomba birika la maji. Alijiminia kwenye mikono yake, kisha akaiosha mara mbili, kisha akasukutua kinywa chake, akaosha pua yake (kwa maji) mara tatu (kwa kuingiza maji na kuyapenga). Aliosha uso wake mara tatu, na baada ya hapo aliosha mikono yake mpaka kwenye viwiko mara mbili. Kisha akapaka kichwa chake kwa mikono yake yenye umajimaji kutoka mbele, mpaka nyuma kwenye ukosi wa shingo, na kisha akaipeleka tena mbele pale alipoanzia. Kisha akaosha miguu.¹ Udhu sawa na ule wa Mtume ﷺ ulifanywa na Ali رضي الله عنه . Katika Hadithi ya Abdul Khayr.²

Abu Dawud alinukuu kuwa Muawiyah na Al-Miqdam bin Madiyah walisimulia maelezo ya udhu wa Mtume ﷺ sawa na haya.³ Hadithi hizi zinadhihirisha kuwa ni lazima kupaka kichwa chote.

Abdul-Razzaq alimnukuu Humran bin Aban kuwa alisema, “Nilimuona Uthman bin Affan رضي الله عنه akichukua Udhu, na alimimina maji juu ya mikono yake na akaieneza mara tatu, kisha alisukutua kinywa chake, akasafisha pua zake (kwa kutia maji na kuyapenga). Kisha akaosha uso wake mara tatu, kisha mkono wake wa kulia mpaka kwenye kiwiko mara tatu, na akaosha wa kushoto mara tatu. Kisha akaipitisha mikono yake yenye umajimaji juu ya kichwa chake kisha akaosha mguu wake wa kulia mara tatu, kisha wa kushoto mara tatu. Baada ya hapo Uthman رضي الله عنه alisema, ‘Nilimuona Mtume ﷺ akichukua Udhu kama hivi, na akasema,

¹ Fath Al-Bari 1:347, Muslim 1:210.

² Abu Dawud 1:82.

³ Abu Dawud 1:88-89.

«مَنْ تَوَضَّأَ نَحْوَ رُضُونِي هَذَا، ثُمَّ صَلَّى رَكَعَتَيْنِ لَا يُحَدِّثُ فِيهِمَا نَفْسَهُ، غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ»

“Iwapo kila mmoja atatawadha kama mimi na akasali Rakaa mbili na asifikiri chochote wakati huo, basi dhambi zake zilizopita zitasamehewa.”¹

Bukhari² na Muslim³ pia waliandika Hadithi hii katika Sahihi Mbili. Katika Sunan yake, Abu Dawud pia alinukuu kutoka kwa Uthman رضي الله عنه, chini ya melezo ya Udhu, na ndani yake, ni kuwa alipaka kichwa mara moja.⁴

Ulazima wa Kuosha Miguu na sio Kupaka:

Allah تعالى Amesema,

وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ^٥

“...na osheni miguu yenu mpaka vifundoni.”

Ibn Abi Hatim alimnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما alieleza kuwa Ayah hii inahusu kuosha (miguu).⁵ Abdullah bin Mas'ud, Urwah, Ata, Ikrimah, Al-Hasan, Mujahid, Ibrahim, Adh-Dhahhak, As-Suddi, Muqatil bin Hayyan, Az-Zuhri na Ibrahim At-Taymi رضي الله عنهم walisema vivo hivyo.⁶ Hii inadhihirisha wazi ulazima wa kuosha miguu, kama walivyosema *Salaf*, na sio kupaka juu ya miguu ilivyo wazi.

Hadithi Zinazoonesha Ulazima wa Kuosha Miguu:

Tulitaja Hadithi ya Viongozi Wawili wa Waumini, Uthman na Ali رضي الله عنهما, na pia na Ibn Abbas رضي الله عنهما, Muawiyah, Abdullah bin Zayd bin Asim na Al-Miqdad bin Madiyah رضي الله عنهم, kuwa Mtume ﷺ aliosha miguu mara moja, mbili au tatu katika Udhu.

¹ 'Abdur-Razzaq 1:44.

² *Fat'hul Bari* 1:311.

³ Muslim 1:205.

⁴ Abu Dawud 1:80, 82.

⁵ At-Tabari 10:55.

⁶ At-Tabari 10:54-57.

Ilinukuliwa katika Sahih Mbili kuwa Abdullah bin Amr رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ mara moja alichelewa katika safari na alitukuta na wakati wa Sala ya Alasiri ulikaribia sana. Tulikuwa bado tunachukua Udhu (kwa haraka) na tulikuwa tunapaka miguu yetu. Akasema kwa Sauti ya Juu Sana:

«أَسْبِغُوا الرُّضُوءَ وَنَيْلٌ لِلْأَعْقَابِ مِنَ النَّارِ»

“Tawadheni sawa sawa ikoeni miguu yenu na Moto.”¹

Hadithi hii ilikusanywa kwenye Sahihi Mbili kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه. Muslim alinukuu kutoka kwa Aishah رضي الله عنها kuwa alisema Mtume ﷺ alisema,

«أَسْبِغُوا الرُّضُوءَ وَنَيْلٌ لِلْأَعْقَابِ مِنَ النَّارِ»

“Kamilisheni Udhu sawasawa. Ikoeni miguu yenu na moto.”²

Abdullah bin Al-Harith bin Jaz رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«وَنَيْلٌ لِلْأَعْقَابِ وَبُطُونِ الْأَقْدَامِ مِنَ النَّارِ»

“Okoa miguu na nyayo zako na Moto.”

Ilinukuliwa na Al-Bayhaqi na Al-Hakim, na isnadi yake ni sahihi.⁴

Muslim alinukuu katika sahihi yake kutoka kwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه kuwa alisema, kuwa mtu moja alitekeleza Udhu na akaona doa kavu sawa na ukucha katika mguu. Mtume ﷺ aliona hilo na akamuambia.

«ارْجِعْ فَأَحْسِنِ رُضُوءَكَ»

“Rejea na ukatekeleze Udhu sawasawa.”⁵

Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bayhaqi pia alinukuu kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa kuna mtu alikuja kwa Mtume ﷺ baada ya kuchukua udhu, na akaacha doa la ukubwa wa kucha mguuni mwake. Mtume ﷺ alimuambia:

¹ Fat'hul Al-Bari 1:319, Muslim 1:214.

² Fat'hul Al-Bari 1:321, Muslim 1:215.

³ Muslim 1:213.

⁴ Al-Bayhaqi 1:70 na Al-Hakim katika Al-Mustadrak 1:162.

⁵ Muslim 1:215.

«ارْجِعْ فَأَخِينِ رُضُوءَكَ»

“Rejea na ukatekeleza Udhu sawasawa.”¹

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa baadhi ya wake wa Mtume ﷺ kuwa yeye alimuona mtu mmoja akisali, akiwa na doa kavu katika mguu wake, mithili ya Dirham. Mtume ﷺ alimuamuru mtu yule kuchukua Udhu tena.² Hadithi hii ilikusanywa pia na Abu Dawud kutoka kwa Baqiyyah, ambaye aliongeza katika masimulizi yake. “Na (Mtume ﷺ alimuamuru) kurudia Sala.”³ Hadithi hii ina Isnadi yenye nguvu. Allah تعالى Anajua zaidi.

Ulazima wa Kuosha Katikati ya Vidole

Katika Hadithi iliyosimuliwa na Humran, kutoka kwa Uthman رضي الله عنه kuhusu wasifu wa udhu wa Mtume ﷺ kwamba yeye aliosha kwa kupenyeza vidole vyake katikati ya vingine.⁴ Wakusanyaji wa sunah walinukuu kuwa Lakiti bin Sabrah رضي الله عنه alisema, “Nilisema, Ewe Mtume! Nieleze kuhusu udhu. Mtume ﷺ alijibu,

«أَسْبِغِ الرُّضُوءَ، وَخَلَّلْ بَيْنَ الْأَصَابِعِ، وَبَالَغْ فِي الْإِسْتِشْقَاءِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ صَائِمًا»

“Tekeleza Udhu kwa makini, kisha osha mianya kati ya vidole na uzidishe kusuuza pua yako, isipokuwa wakati wa saumu.”⁵

Kupaka Juu ya *Khuff* ni Sunnah

Imam Ahmad bin Hambal رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Aws bin Abi Aws رضي الله عنه kuwa alisema, “Nilimuona Mtume ﷺ alitekeleza Udhu na alipaka juu ya *Khuff* zake. Kisha alisimama akasali.”⁷ Abu Dawud alinukuu Hadithi hii kutoka kwa Aws bin Abi Aws رضي الله عنه alisema katika masimulizi yake, “Nilimuona Mtume ﷺ baada ya kujisaidia, akatawadha, na akapaka juu ya *Khuff* na miguu.”

¹ Al-Bayhaqi 1:70.

² Ahmad 3:424.

³ Abu Dawud 1:121.

⁴ *Majma' Az-Zawaid* 1:235.

⁵ Abu Dawud 1:99, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 1:149, An-Nasai 1:79, Ibn Majah 1:142.

⁶ Viatu vya Ngozi.

⁷ Ahmad 4:8.

Imamu Ahmad aliandika kutoka kwa Jarir bin 'Abdullah Al-Bajali رضى الله عنه kuwa alisema, "Nilisilimu baada ya *Surat Al-Maidah* kuteremshwa na nilimuona Mtume ﷺ akipaka baada ya kusilimu kwangu."² Hadithi hii ameipokea Ahmad peke yake. Na imepokewa katika sahihi mbili toka kwa Hummam kuwa amesema: 'Jarir alikwenda haja ndogo kisha akachukua udhu na akapaka juu ya *Khuffu* zake.' Akaulizwa: 'Mbona unafanya hivi?' Akajibu; 'Ndio. Nimemuona Mtume ﷺ alijisaidia haja ndogo, kisha akapaka juu ya *Khuffu* zake mbili. Al-Amash alitoa maoni kuwa Ibrahim alisema, "Waliipenda Hadithi hii kwa sababu Jarir alisilimu baada ya kuteremshwa kwa *Surat Al-Maidah*."³ Sharia ya kupaka juu ya *Khuffu* mbili imethibiti kwa Mtume ﷺ kwa njia ya kauli na vitendo.

Kutayammam kwa Mchanga Safi Wakati wa Kukosa Maji na Ugonjwa

Allah تعالى Amesema,

وَأِنْ كُنْتُمْ مَرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ أَوْ لَمَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ يَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِنْهُ

"Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake,⁴ na hamkupata maji, basi tayamamuni vumbi liliosafi, na mpake nyuso zenu na mikono yenu."

Tulijadili hii yote katika *Surat an-Nisa* na hatuhitaji kurejea hapa. Pia tulitaja sababu za kuteremshwa Aya ya kutayamamu. Alinukuu kuwa Aisha رضى الله عنها alisema, "Nilipokuwa narejea Madinah, mkufu wangu ulikatika (na kupotea) sehemu inayoitwa Al-Bayda. Mtume ﷺ alipumzika pale na akalala usingizi huku kichwa chake kiko juu ya paja langu. Abubakar رضى الله عنه (babake Aisha رضى الله عنها) alikuja na kupiga katika ubavu wangu kwa mkono wake huku akisema, "Umewazuia watu hapo kwa sababu ya mkufu?" Hivyo natamani kama ningelikuwa nimekufa, kwa sababu (sikuweza kuondoka) Mjumbe alikuwa amelala juu ya paja langu na niliumia kutoka na maumivu yaliyosababishwa na Abubakar رضى الله عنه. Mtume ﷺ aliamka alfajiri na hapakuwa na maji. Hivyo Allah تعالى Akateremsha,

¹ Abu Dawud 1:113.

² Ahmad 4:363.

³ *Fat'hul Al-Bari* 1:589, Muslim 1:228.

⁴ Angalia *Surat An-Nisa*, na. 43; kuhusu maelezo ya 'wanawake walioguswa.'

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ

“Enyi mlionini! Mnaposimama kwa ajili ya Sala basi osheni nyuso zenu,...” hadi mwisho wa aya.

Usaid bin Al-Hudhair alisema, “Ee, familia, ya Abubakar! Allah تعالى Amewabariki watu kwa sababu yenu. Kwa hiyo nyinyi ni rehema kwa watu.”¹ Allah تعالى Amesema:

مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِّنْ حَرَجٍ

“Hapendi Mwenyezi Mungu Kukutieni katika taabu...”

Ndio maana Amewafanyia mambo mepesi kwenu. Hii ndio sababu Aliwaruhusu mtayammam mnapokuwa wagonjwa au mnapokosa maji, ili mambo yawe sawa na iwe huruma kwenu. *Tayammam* ni badala ya Udhu, na Allah تعالى Ameifanya sawa na Udhu wa kutumia maji kwa yule anayestahili, isipokuwa kwa baadhi ya mambo kama tulivyotaja hapo kabla. Kwa mfano, *Tayammam*, inahusisha tu kupiga viganja juu ya mchanga na kupaka uso na mikono. Allah تعالى Amesema,

وَلَٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“Bali Anataka Kukutakaseni na Kutimiza Neema Yake juu yenu ili mpate kushukuru.”

Kwa maana: Huenda nyinyi mtashukuru Neema Yake juu yenu kwa kile Alichokiwekea sharia juu yenu, miongoni mwa kutanuliwa wigo mpana wa matumizi, upole, huruma, wepesi na usamehevu

Dua Baada ya Udhu

Sunnah inakokoteza kumuomba Allah تعالى baada ya Udhu na inaeleza kuwa wale wanaofanya hivyo ni miongoni mwa wale wanaotaka kuzitakasa nafsi zao, kama Aya hapo juu inavyosema. Imam Ahmad, Muslim na wakusanyaji wengine wa sunnah walisimulia kuwa Uqbah bin Amir رضي الله عنه alisema, “Tulikuwa kwenye doria, tukiwalinda ngamia, na zamu yangu ilipofika nilirejesha ngamia usiku. Nilimkuta Mtume ﷺ akiwahutubia watu. Niliyasikia maneno yafuatayo:

¹ Fat'hul Al-Bari 8:121.

«مَا مِنْ مُسْلِمٍ يَتَوَضَّأُ فَيُحْسِنُ وُضُوئَهُ، ثُمَّ يَقُومُ فَيُصَلِّي رَكَعَتَيْنِ مُقْبِلًا عَلَيْهِمَا بِقَلْبِهِ وَوَجْهِهِ، إِلَّا وَجَبَتْ لَهُ الْجَنَّةُ»

“Muislamu ambaye atatekeleza Udhu wake barabara, kisha akasimama na kusali - Rakaa mbili kwa nia kamili kwenye moyo wake na mwili wake.¹ Ataingizwa peponi.

Nikasema, “Kauli njema iliyoje hii!” Mtu aliyekuwa karibu yangu alisema, “Kauli aliyosema kabla ilikuwa bora zaidi!” Nilipomuangalia, Nilimuona Umar رضي الله عنه, ambaye alisema, ‘Nilikuona umeshafika, Mtume ﷺ alisema

«مَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ يَتَوَضَّأُ فَيُبَلِّغُ أَرْقَانِيعَ الْوُضُوءِ، يَقُولُ: أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، إِلَّا فَتِحَتْ لَهُ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ الثَّمَانِيَةِ، يَدْخُلُ مِنْ أَيِّهَا شَاءَ»

“Mmoja wenu anapotekeleza Udhu vizuri na kisha akasema, ‘Nashuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na kuwa Muhammad ni mja wake na mjumbe wake, atafunguliwa milango minane ya peponi na atakuwa huru kuingia mlango autakao.”

Haya ni kwa mujibu wa kauli ya Muslim.²

Fadhila za Udhu

Malik alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا تَوَضَّأَ الْعَبْدُ الْمُسْلِمُ أَوْ الْمُؤْمِنُ فَغَسَلَ وَجْهَهُ، خَرَجَ مِنْ وَجْهِهِ، كُلُّ خَطِيئَةٍ نَظَرَ إِلَيْهَا بِعَيْنَيْهِ مَعَ الْمَاءِ أَوْ مَعَ آخِرِ قَطْرِ الْمَاءِ، فَإِذَا غَسَلَ يَدَيْهِ خَرَجَ مِنْ يَدَيْهِ كُلُّ خَطِيئَةٍ بَطَّشَتْهَا يَدَاهُ مَعَ الْمَاءِ أَوْ مَعَ آخِرِ قَطْرِ الْمَاءِ، فَإِذَا غَسَلَ رِجْلَيْهِ خَرَجَتْ كُلُّ خَطِيئَةٍ مَسَّتْهَا رِجْلَاهُ مَعَ الْمَاءِ أَوْ مَعَ آخِرِ قَطْرِ الْمَاءِ، حَتَّى يَخْرُجَ نَقِيًّا مِنَ الذُّنُوبِ»

“Muislamu au muumini anapochukua Udhu na akaosha uso wake, kila dhambi alilolitazama kwa macho yake litadondoka usoni mwake na maji au na tone moja la maji ya mwisho. Atakapoosha mikono yake, kila dhambi alilofanya kwa kutumia mikono yake litaondolewa

¹ Kwa mujibu wa An-Nawawi; “Kujisalimisha mikono na miguu na moyo kutezwa nguvu.”

² Ahmad 4:153, Muslim 1:209, Abu Dawud 1:118, An-Nasai 1:92, Ibn Majah 1:159.

*na maji, kutoka kwenye mikono yake hadi tone la mwisho la maji. Atakapoosha miguu yake, kila dhambi lililochukuliwa na miguu yake litaondoshwa na maji au tone la mwisho la maji. Mpaka atakuwa hana dhambi tena.*¹

Aidha Muslim alinukuu² kuwa Abu Malik Al-Ash'ari رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الطُّهُورُ شَطْرُ الْإِيمَانِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ تَمْلَأُ الْمِيزَانَ، وَسُبْحَانَ اللَّهِ وَاللَّهُ أَكْبَرُ تَمْلَأُ مَا بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، وَالصَّوْمُ جُنَّةٌ، وَالصَّبْرُ ضِيَاءٌ، وَالصَّدَقَةُ بُرْهَانٌ، وَالْقُرْآنُ حُجَّةٌ لَكَ أَوْ عَلَيْكَ، كُلُّ النَّاسِ يَغْدُو، فَبَايَعُ نَفْسَهُ فَمُعْتَقُهَا أَوْ مُوقِفُهَا»

*"Tawahara ni nusu ya imani, na Al-Hamdu lillah (shukrani zote Anastahili Allah تعالى) inajaza mizani na Subhana Allah na Allahu Akbar, (Sifa zote zina mstahiki Allah تعالى, na Allah تعالى ni Mkubwa) inajaza kilicho kati ya mbingu na ardhi. Saumu ni Junna (ngao), sabr (subira) ni nuru na sadaqa ni ushahidi wa (imani) na Qur'ani ushahidi kwako au dhidi yako. Kila mtu hutoka asubuhi; kuna anayeiacha huru nafsi yake na kuna anayeiangamiza."*³

Imekuja katika sahihi Muslim kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا يَقْبَلُ اللَّهُ صَدَقَةً مِنْ غُلُولٍ، وَلَا صَلَاةَ بِغَيْرِ طَهْوَرٍ»

*"Allah تعالى Hairidhii sadaqah iliyopatikana kwa njia ya Ghulul (hiana)⁴, au Sala bila tohara."*⁵

* * *

¹ Al-Muwatta' 1:32.

² Muslim 1:215.

³ Muslim 1:203.

وَأَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَمِيثَقَهُ الَّذِي وَاتَّفَقْتُمْ بِهِ إِذْ قُلْتُمْ سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ۗ وَأَتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٧﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ ۗ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَا نُ قَوْمٍ عَلَىٰ آلَا تَعْدِلُوا ۗ أَعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٨﴾ وَعَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ۖ هُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٩﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۖ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿١٠﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ هُمْ قَوْمٌ ۖ أَنْ يَسْطُوا إِلَيْكُمْ أَيْدِيَهُمْ فَكَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ وَعَلَىٰ اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾

وَأَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَمِيثَقَهُ الَّذِي وَاتَّفَقْتُمْ بِهِ إِذْ قُلْتُمْ سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٧﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ ۗ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَا نُ قَوْمٍ عَلَىٰ آلَا تَعْدِلُوا ۗ أَعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٨﴾ وَعَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ۖ هُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٩﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۖ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿١٠﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ هُمْ قَوْمٌ ۖ أَنْ يَسْطُوا إِلَيْكُمْ أَيْدِيَهُمْ فَكَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ وَعَلَىٰ اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾

7. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, na ahadi Yake iliyofungamana nanyi mliposema: Tumesikia na tumetii. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi sana wa yaliyomo vifuanii.

8. Enyi mlipoamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnyoyatenda.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۖ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿١٠﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ هُمْ قَوْمٌ ۖ أَنْ يَسْطُوا إِلَيْكُمْ أَيْدِيَهُمْ فَكَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ وَعَلَىٰ اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾

9. Mwenyezi Mungu Amewaahidi waliomuamini na wakatenda mema kwamba watapata maghufira na malipo makubwa.

10. Na wale waliokufuru na wakakanusha Ishara Zetu, hao ndio watu wa Motoni.

11. Enyi mliuamini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, walipotaka watu kukunyooshieni mikono, Naye Akaizuilia mikono yao kukufikieni. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.

Waumini Wanakumbushwa Fadhila za Ujumbe na Uislamu.

Allah تعالى Anawakumbusha waja wake waumini juu ya Radhi zake kwa kuwafaradhisia hii Dini Takatifu na Kuwapelekea Mjumbe huyu Mtukufu. Pia Anawakumbusha ahadi na mkataba waliofanya naye juu ya kumfuata Mtume ﷺ, kumuunga mkono na kumsaidia, kutekeleza sheria zake, na kufikisha ujumbe kwa niaba yake nao waliukubali,

Allah تعالى Amesema,

وَأَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَمِيثَاقَهُ الَّذِي وَاثَقَكُمْ بِهِ إِذْ قُلْتُمْ سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا

“Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, na ahadi Yake aliyofungamana nanyi mlipo sema: Tumesikia na tumetii.”

Hii ni ahadi waliyokuwa wakimpa Mtume ﷺ walipokuwa wakisilimu. Walikuwa wakisema, “Tulimpa agano la utiifu Mtume ﷺ kusikia na kutii, katika nyakati tukiwa na nguvu au kinyume chake, hata kama tulishauriwa kwa haki, na tusipinge uongozi wa watu stahili.” Pia Allah تعالى Amesema,

وَمَا لَكُمْ لَا تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالرَّسُولِ يَدْعُوكُمْ لِيُؤْمِنُوا بِرَبِّكُمْ وَقَدْ أَخَذَ مِيثَاقَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ

مُؤْمِنِينَ

“Na mna nini hata hamumuamini Mwenyezi Mungu na hali Mtume anakuiteni mumuamini Mola wenu Mlezi? Naye Amekwishachukua ahadi yenu, ikiwa nyinyi ni Waumini. (57:8)

Aidha ilisemwa kuwa Aya (5:7) inawakumbusha Mayahudi juu ya agano na ahadi Aliyoichukua Allah تعالى kutoka kwao kumfuata Muhammad ﷺ na kushirikiana na sharia yake, kama Ali bin Abi Talhah alivyonukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliyenena,

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu.”

Katika nyakati za hali zote. Allah تعالى Anasema kuwa Anajua siri na fikra ambazo zimefichwa na mioyo,

إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi sana wa yaliyomo vifuani.”

Ulazima wa Kusimamisha Haki:

Allah تعالى Amesema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ

“Enyi mliaoamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Ukweli ni kwa ajili ya Allah تعالى, na sio kwa ajili ya watu au umaarufu,

شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ

“...mkitoa ushahidi kwa haki...”

Kufuata haki na sio uhalifu. Imeandikwa katika Sahih Mbili kuwa An-Numan bin Bashir alisema, “Baba yangu alinipa zawadi, lakini ‘Amrah binti Rawahah, mamangu, alisema kuwa hatokubaliana nalo mpaka amfanye Mtume ﷺ kuwa shahidi kwalo. Hivyo, babangu alikwenda kwa Mtume ﷺ kumuomba awe shahidi wakati akipewa zawadi. Mtume ﷺ aliuliza,

«أكل ولدك نحلث مثله؟»

“Je umewapa kama hiki kwa kila mtoto wako?”

Akajibu, ‘hapana.’ Mtume ﷺ alisema,

«اتَّقُوا اللَّهَ وَاعْدِلُوا فِي أَوْلَادِكُمْ»

“Mche Allah watendee sawa sawa wanao.”

Na akasema,

«إِنِّي لَا أَشْهَدُ عَلَىٰ جَوْرٍ»

“Hakika mimi, sishuhudii dhuluma.”

Babangu alirejea na akachukua zawadi yake.”¹

Allah تعالى Amesema,

وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ عَلَىٰ ۤأَلَّا تَعْدِلُوۡا

“Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu.”

Ayah inaamuru, ‘Msiemewe na chuki dhidi ya baadhi ya watu ili kuepuka kutowatendea haki. Bali muwatendee haki wote, ima ni rafiki au adui.”

Ndio maana Allah تعالى Akasema,

أَعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ

“Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamungu.”

Hii ni bora kuliko kama mngetekeleza haki katika hali hii. Japokuwa Allah تعالى Amesema kuwa kuzingatia haki, “... **Ni karibu na Taqwa.**” Hapana hatua nyingine ya kuchukua, kwa hiyo “**Karibu.**”

Maana yake ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine,

أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقْرَرًا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا ﴿٢٤﴾

“Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makaazi bora na mahali penye starehe nzuri”. (25:24)

Baadhi ya Masahaba wa kike walimuambia Umar رضي الله عنه, “Wewe ni mkali kuliko Mtume ﷺ.” Ikiwa na maana, wewe ni mkali, na sio kwamba Mtume ﷺ ni mkali. Baadaye Allah تعالى Amesema,

¹ Fat’hul Al-Bari 5:250, Muslim 3:1242.

وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayo yatenda.”

Na hivyo hivyo, Atawalipa au Kuwaadhibu kulingana na amali zenu, ima ni nzuri au mbaya

Hivyo Kauli ya Allah تعالى baadaye,

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ مَغْفِرَةٌ

“Mwenyezi Mungu Amewaahidi walio muamini na wakatenda mema kwamba watapata maghfira.”

Ya madhambi yao,

وَأَجْرٌ عَظِيمٌ

“Na malipo makubwa.”

Ambayo ni Pepo, hii ni sehemu ya Rehema ya Allah تعالى kwa waja Wake. Hawataipata Pepo kwa hesabu ya amali zao njema, bali kwa hesabu ya Rehema Zake na Fadhila Zake, japokuwa watastahili kupata huruma Zake kwa hesabu ya amali zao njema.

Allah تعالى Amezifanya amali hizo kuwa njia inayoelekea kwenye rehema, fadhila, msamaha na kukubaliwa Kwake. Kwa hiyo, yote hayo yanatoka kwa Allah تعالى Pekee na shukrani zote zinamstahiki Yeye.

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿٥١﴾

“Na wale waliokufuru na wakakanusha Ishara Zetu, hao ndio watu wa Motoni.”

Hii inadhihirisha ukamilifu wa Allah تعالى katika haki, busara na kuhukumu, Yeye Hakosei, Yeye ni Mjuzi zaidi, Muadilifu zaidi na Muweza zaidi.

Miongoni mwa Fadhila za Allah ﷻ ni Kuwazuia Makafiri Kuwapiga Waislamu:

Allah ﷻ Amesema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ هُمْ قَوْمٌ أَن يَبْسُطُوا إِلَيْكُمْ أَيْدِيَهُمْ
فَكَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ^ط

“Enyi mlioamini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, walipotaka watu kukunyooshieni mikono, Naye Akaizuilia mikono yao kukufikieni.”

Abdul-Razzaq alimnukuu Jabir رضي الله عنه akisema, “Kuna wakati mmoja Mtume ﷻ alikaa pahala na watu walitawanyika ili kupata vivuli vya miti. Mtume ﷻ alitundika silaha yake juu ya mti na bedui alikuja akaitwaa silaha ya Mtume ﷻ na akaishikilia. Alimfuata Mtume ﷻ na akamuambia, ‘Nani awezaye kukulinda na shari yangu?’ Mtume ﷻ akajibu, ‘Allah ﷻ, Aliye juu na Aliyetukuka.’ Yule bedui alirejea swali lake mara mbili au tatu, kila wakati Mtume ﷻ alijibu ‘Allah ﷻ’. Kisha bedui yule alirejesha panga katika ala. Na Mtume ﷻ aliwaita Maswahaba wake na akawaambia yaliyojiri, wakati bedui alikaa pembezoni mwake, kwani Mtume ﷻ hakumuadhibu. Maamar alisema kuwa Qatadah alikuwa akisema kuwa baadhi ya waarabu walitaka Mtume ﷻ auawe, hivyo walimtuma yule bedui.

Kisha Qatadah alitaja Aya hii,

أَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ هُمْ قَوْمٌ أَن يَبْسُطُوا إِلَيْكُمْ أَيْدِيَهُمْ

“Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, walipotaka watu kukunyooshieni mikono.”¹

Masimulizi ya bedui huyu, ambaye jina lake ni Ghaurrath bin Al-Harith, yametajwa ndani ya Sahih.²

Muhammad bin Is-haq bin Yasar, Mujahid na Ikrimah walisema Aya hii ilishuka juu ya Bani An-Nadhir, ambao walifanya njama za kumuangushia jiwe kubwa

¹ 'Abdur-Razzaq 1:185.

² Al-Bukhari na. 4135, 4136, 3139.

Mtume ﷺ juu ya kichwa chake alipowajia kwa shauri la kuwalipia diya watu wawili waliouawa na Waislamu.¹ Mayahudi walimtaka Amr bin Jahash bin Ka'b kutekeleza udhalimu huo kwa kumuamuru amtupie Mtume ﷺ jiwe kutoka juu, atakapo kuja kwao na kukaa chini ya ukuta. Allah تعالی Alimueleza Mtume Wake juu ya mpango wao, hivyo akarejea Madinah, na Masahaba wake walifuata baadaye. Allah تعالی Aliteremsha Aya hii kuhusu kadhia hii.

وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ

“Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.”

Na wale wafanyao hivyo, basi Allah تعالی Atawatosheleza na Atawalinda dhidi ya njama za watu. Baada ya hapo, Allah تعالی Alimuamuru Mjumbe wake kuwatimua Bani An-Nadhir na alizingira eneo lao na akawalazimisha kuhama Madinah.

* * *

¹ Mtume ﷺ aliwekeana mkataba na Wayahudi kumsaidia kulipa dia ilipotakiwa.

* وَلَقَدْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَبَعَثْنَا مِنْهُمُ اثْنَيْ عَشَرَ نَقِيبًا وَقَالَ اللَّهُ إِنِّي مَعَكُمْ ۗ لَئِنْ أَقَمْتُمُ الصَّلَاةَ وَآتَيْتُمُ الزَّكَاةَ وَآمَنْتُمْ بِرُسُلِي وَعَزَّرْتُمُوهُمْ وَأَقْرَضْتُمُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا لَأُكَفِّرَنَّ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَلَأُدْخِلَنَّكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۗ فَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿١٢﴾

فِيمَا نَقَضِهِمْ مِيثَاقَهُمْ لَعَنَّاهُمْ وَجَعَلْنَا قُلُوبَهُمْ قَسِيَةً ۗ يُخَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَنْ مَوَاضِعِهِ ۗ وَنَسُوا حَظًّا مِمَّا ذُكِّرُوا بِهِ ۗ وَلَا تَزَالُ تَطَّلِعُ عَلَى خَائِبِينَ مِنْهُمْ إِلَّا قَلِيلًا مِنْهُمْ ۗ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَأَصْفَحْ ۗ إِنَّ اللَّهَ سُحُبُ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣﴾

وَمِنَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصْرِيُّ أَخَذْنَا مِيثَاقَهُمْ فَنَسُوا حَظًّا مِمَّا ذُكِّرُوا بِهِ فَأَغْرَيْنَا بَيْنَهُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۗ وَسَوْفَ يُنَبِّئُهُمُ اللَّهُ بِمَا كَانُوا يَصْنَعُونَ ﴿١٤﴾

* وَلَقَدْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَبَعَثْنَا مِنْهُمُ اثْنَيْ عَشَرَ نَقِيبًا ۗ وَقَالَ اللَّهُ إِنِّي مَعَكُمْ ۗ لَئِنْ أَقَمْتُمُ الصَّلَاةَ وَآتَيْتُمُ الزَّكَاةَ وَآمَنْتُمْ بِرُسُلِي وَعَزَّرْتُمُوهُمْ وَأَقْرَضْتُمُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا لَأُكَفِّرَنَّ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَلَأُدْخِلَنَّكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۗ فَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿١٢﴾

فِيمَا نَقَضِهِمْ مِيثَاقَهُمْ لَعَنَّاهُمْ وَجَعَلْنَا قُلُوبَهُمْ قَسِيَةً ۗ يُخَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَنْ مَوَاضِعِهِ ۗ وَنَسُوا حَظًّا مِمَّا ذُكِّرُوا بِهِ ۗ وَلَا تَزَالُ تَطَّلِعُ عَلَى خَائِبِينَ مِنْهُمْ إِلَّا قَلِيلًا مِنْهُمْ ۗ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَأَصْفَحْ ۗ إِنَّ اللَّهَ سُحُبُ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣﴾

وَمِنَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصْرِيُّ أَخَذْنَا مِيثَاقَهُمْ فَنَسُوا حَظًّا مِمَّا ذُكِّرُوا بِهِ فَأَغْرَيْنَا بَيْنَهُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۗ وَسَوْفَ يُنَبِّئُهُمُ اللَّهُ بِمَا كَانُوا يَصْنَعُونَ ﴿١٤﴾

12. Na Mwenyezi Mungu Alifanya agano na Wana wa Israili. Na Tukawateulia kutokana nao wakuu kumi na mbili. Na Mwenyezi Mungu Akasema: Kwa yakini Mimi ni pamoja nanyi. Mkisali, na mkatoa Zaka, na mkawamini Mitume Wangu, na mkawasaidia, na mkamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, hapana shaka Nitakufutieni maovu yenu na Nitakuizingeni katika bustani zipitazo

mito kati yake. Lakini atakayekufuru miongoni mwenu baada ya hayo bila ya shaka atakuwa amepotea njia iliyo sawa.

13. Basi kwa sababu ya kuvunja agano lao Tuliwalaani, na Tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu. Wanayabadilisha maneno kutoka pahala pake, na wamesahau sehemu ya yale waliyo kumbushwa. Na huachi kuvumbua khiana kutokana nao, isipokuwa wachache miongoni mwao. Basi wasamehe na waache. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao wema.

14. Na kutoka kwa wale waliosema: Sisi ni Manasara, Tulichukua ahadi yao, lakini wakashau sehemu ya waliyokumbushwa. Kwa hivyo Tukaweka kati yao uadui na chuki mpaka Siku ya Kiyama. Na hapo Mwenyezi Mungu Atawaambia waliyokuwa wakiyafanya.

Watu wa Kitabu Wamelaaniwa kwa Kuvunja Ahadi:

Allah تعالی Aliwaamuru waja Wake waumini kutekeleza ahadi na agano Alilochukua kutoka kwao kupitia mja Wake, Muhammad ﷺ. Aidha Allah تعالی Aliwakumbusha fadhila zilizo wazi na zisizo na ukomo za ukweli na uongozi Aliyompa. Baadaye Allah تعالی Aliwafahamisha ahadi Alizochukua kutoka kwa Watu wa Kitabu, waliowatangulia, Mayahudi na Wakristo. Walipovunja ahadi na maagano hayo, Allah تعالی Aliwalaani kama matokeo ya mwenendo wao na Akawafukuza katika Rehema na Fadhila Zake. Pia Alizipiga mihuri nyoyo zao kupokea muongozo na dini ya ukweli, elimu inayonufaisha na vitendo adilifu. Allah تعالی Amesema,

وَلَقَدْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَبَعَثْنَا مِنْهُمُ اثْنَيْ عَشَرَ نَقِيبًا

“Na Mwenyezi Mungu Alifanya agano na Wana wa Israili. Na Tukawateulia kutokana nao wakuu kumi na mbili.”

Viongozi hao kumi na wawili walimpa ahadi Allah تعالی ya kumsikiliza na kumtii Allah تعالی, Mjumbe Wake na Kitabu Chake kwa niaba ya makabila yao. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالی na Ibn Abbas walisema, kuwa haya yalijiri wakati Musa عليه السلام alipokwenda kupigana na adui mwenye nguvu (nchini Palestina) na ndipo Allah تعالی Akamuamuru kuchagua kiongozi kwa kila kabila.¹

¹ At-Tabari 10:113.

Viongozi wa Ansar katika Usiku wa Aqabah:

Kadhalika, Mtume ﷺ alichukua ahadi kwa Ansar katika eneo la Aqabah, walikuwepo viongozi kumi na wawili wa Ansar. Walikuwepo watu watatu kutoka kabila la Aws: Usayd bin Al-Hudayr, Said bin Khaythamah na Rifaah bin Abdul-Mundhir, au Abu Al-Haytham bin At-Tayhan. Walikuwepo watu tisa wa kabila la Khazraj: Abuu Umama As'ad bin Zurara, Sa'ad bin Rabii, Abdallah bin Ruwaha, Rafii bin Malik bin Ajlan, Barrau bin Maarur, Ubada bin Swamit, Saad bin Ubada, Abdillah bin Amri bin Haraam na Mundhir bin Umar bin (Khunayisi). Kaab bin Malik amewataja viongozi hao katika shairi lake, kama ilivyonyukuliwa na Ibn Is-haq رحمه الله تعالى.¹ Usiku ule, watu hawa walikuwa viongozi au wawakilishi wa makabila yao kwa amri ya Mtume ﷺ. Walitoa agano na ahadi ya kiapo cha utii kwa Mtume ﷺ kwa niaba ya watu wao.

Allah تعالى Amesema,

وَقَالَ اللَّهُ إِنِّي مَعَكُمْ

“Na Mwenyezi Mungu Akasema: Kwa yakini Mimi ni pamoja nanyi.”

Pamoja na ulinzi na msaada Wangu,

لَئِن أَقَمْتُمُ الصَّلَاةَ وَآتَيْتُمُ الزَّكَاةَ وَآمَنْتُمْ بِرُسُلِي

“Mkisali, na mkatoa Zaka, na mkawaamini Mitume Wangu.”

Kuhusu wanachokuleteeni katika ufunuo

وَعَزَّزْتُمُوهُمْ

“...na mkawasaidia,...”

Muwaunge katika lililo la kweli,

وَأَقْرَضْتُمُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا

“...na mkamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema,...”

Kwa kutumia katika njia Yake kwa ajili ya kutafuta radhi Zake

¹ Ibn Hisham 2:86-87.

لَأُكْفِرَنَّ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ

“...Hapana shaka Nitakufutieni maovu yenu,...”

Maana: Dhambi zenu Nitazifuta na wala sitowaadhibu, Allah تعالى Amesema

وَلَأُدْخِلَنَّكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“...na Nitakuingizeni katika bustani yapitayo mito kati yake.”

Nitawakingeni na vitu vya hatari, na Nitawapeni yaliyokusudiwa.

Kuvunja Ahadi

Allah تعالى Amesema:

فَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ

“Lakini atakayekufuru miongoni mwenu baada ya hayo bila ya shaka atakuwa amepotea njia iliyo sawa.”

kwa hiyo, wale waliovunja agano, japokuwa waliahidi kutoa kiapo kuwa hawatovunja, walivunja na kukanusha kuwa ilikuwepo, wameacha njia iliyo wazi na wakakengeuka njia ya uongofu na kufuata upotofu.

Kisha Allah تعالى Ametaja adhabu watakayopata wale waliovunja agano na ahadi waliyompa yeye.

Allah تعالى Amesema:

فَبِمَا نَقَضْتُمْ مِيثَاقَهُمْ لَعْنَتُهُمْ

“Basi kwa sababu ya kuvunja agano lao Tuliwalaani,...”

Allah تعالى Anaeleza kuwa, kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi Tuliyochukua kutoka kwao, Tuliwalaani, Tukawatoa kwenye haki, na Tukawatoa kwenye uongozi.

وَجَعَلْنَا قُلُوبَهُمْ قَنَسَةً

“...na Tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu.”

Na hawasilizi neno lolote la ushauri walisikialo, kwa sababu ya ugumu wa nyoyo zao.

تُحَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَنْ مَوَاضِعِهِ^١

“Wanayabadilisha maneno kutoka pahala pake...”

Kwa kutotekeleza na kupuuzia. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَدُسُّوا حَظًّا مِمَّا ذُكِّرُوا بِهِ^٢

“...na wamesahau sehemu ya yale waliyokumbushwa.”

Kama vile njama zao na hujumu dhidi yako, Ewe Muhammad ﷺ na masahaba wake. Mujahid alisema kuwa Aya hii inahusu njama zao za kumuua Mtume

ﷺ.¹

وَلَا تَزَالُ تَطَّلِعُ عَلَى خَائِنَةٍ مِنْهُمْ

“Na huachi kuvumbua khiana kutokana nao...”

فَاعْفُ عَنْهُمْ وَأَصْفَحْ^٢

“Basi wasamehe na waache.”

Kwa hakika, huu ni ushindi. Baadhi ya *Salaf* walisema, “Hutaweza kuwafanyia vyema zaidi wenye kumuasi Allah تعالى pamoja nawe kuliko wewe pamoja nao kumuabudu Allah تعالى.” Nyoyo zao zitajumuika katika ukweli na huenda Allah تعالى Akawaongoza waufuate uongofu sahihi. Kwa minajili hiyo, Allah تعالى Amesema:

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao wema.”

Hivyo, wasamehe wanaokukosea. Qatadah alisema kuwa aya hii ilifutwa na Kauli ya Allah تعالى,

فَقَاتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ

“Piganeni na wasiomuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho...”²

¹ At-Tabari 10:131.

² At-Tabari 10:134.

Wakristo Nao walivunja Agano Lao kwa Allah تعالى, na Matokeo Yake

Allah تعالى Amesema:

وَمِنَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصْرِي أَخَذْنَا مِيثَقَهُمْ

“Na kutoka kwa wale walio sema: Sisi ni Manasara, Tulichukua ahadi yao,...”

Maana: Wanaojiita Wakristo na wafuasi wa Isa عليه السلام mwana wa Maryam, ambapo sivyo walivyo. Tulichagua agano na ahadi kutoka kwao kuwa wanalimfuata Mtume ﷺ, kumsaidia, kumheshimu na kufuata nyayo zake. Na kuwa wanalimuamini kila Mtume aliyetumwa na Allah تعالى kwa watu duniani. Waliwaiga Mayahudi na kuvunja ahadi na maagano. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

فَنَسُوا حَظًّا مِمَّا ذُكِّرُوا بِهِ فَأَغْرَيْنَا بَيْنَهُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ

“...lakini wakasahau sehemu ya waliyokumbushwa. Kwa hivyo Tukaweka kati yao uadui na chuki mpaka Siku ya Kiyama.”

Maana yake: “Tulipanda uadui na chuki baina yao, na watabaki katika hali hii mpaka siku ya kufufuliwa.”

Kwa hakika madhehebu mbalimbali ya kikiristo yamekuwa yakihasimiana na kufanyiana uadui wao kwa wao, zikilaumiana kwa uasi na wakilaaniana. Kila madhehebu hawataki kuwasiliana na wengine, na hairuhusiwi kuingia sehemu ya wenzao ya ibada, Monarchist wanawalaumu Jacobite kwa uadui, na vivyo hivyo Nestoreans na Arians. Kila madhehebu wataendelea kuwashutumu wengine kwa ukafiri na uadui hapa duniani hadi siku ya Kiama. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَسَوْفَ يُنَبِّئُهُمُ اللَّهُ بِمَا كَانُوا يَصْنَعُونَ

“Na hapo Mwenyezi Mungu Atawaambia waliyokuwa wakiyafanya.”

Wakiwaonya na kuwatishia Wakristo kwa sababu ya uongo wao dhidi ya Allah تعالى na Mjumbe wake na madai yao ya uongo juu ya Allah تعالى, Ametukuka na Yuko juu ya yale wayasemayo kuhusu Yeye. Wakristo wanampa sifa ya Mungu mwenzu na mwana, ambapo Yeye ni Mmoja tu na Anajitosheleza, Ambaye Hakuzaa wala Hakuzaliwa, hapana mfano Wake,

¹ At-Tabari 10:134.

يَتَأْهَلُ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ
 كَثِيرًا مِمَّا كُنْتُمْ تُخْفُونَ مِنَ الْكِتَابِ وَيَعْفُوا
 عَنْ كَثِيرٍ قَدْ جَاءَكُمْ مِنَ اللَّهِ نُورٌ وَكِتَابٌ
 مُبِينٌ ﴿١٥﴾ يَهْدِي بِهِ اللَّهُ مَنِ اتَّبَعَ رِضْوَانَهُ سُبُلَ
 السَّلَامِ وَيُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِهِ
 وَيَهْدِيهِمْ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٦﴾ لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ
 قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ قُلْ فَمَنْ يَمْلِكُ مِنَ
 اللَّهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ أَنْ يُهْلِكَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ
 وَأُمُّهُ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ
 قَدِيرٌ ﴿١٧﴾ وَقَالَتِ الْيَهُودُ وَالنَّصَارَى نَحْنُ أَبْنَاءُ اللَّهِ
 وَأَحِبُّهُمْ قُلْ فَلِمَ يُعَذِّبُكُمْ بِذُنُوبِكُمْ بَلْ أَنْتُمْ بَشَرٌ مِّمَّنْ
 خَلَقَ يَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ وَلِلَّهِ مُلْكُ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ ﴿١٨﴾
 يَتَأْهَلُ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ عَلَى فَتْرَةٍ مِّنَ
 الرُّسُلِ أَنْ تَقُولُوا مَا جَاءَنَا مِن بَشِيرٍ وَلَا نَذِيرٍ قَدْ
 جَاءَكُمْ بَشِيرٌ وَنَذِيرٌ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٩﴾

يَتَأْهَلُ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ
 رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ كَثِيرًا مِّمَّا
 كُنْتُمْ تُخْفُونَ مِنَ الْكِتَابِ
 وَيَعْفُوا عَنْ كَثِيرٍ قَدْ جَاءَكُمْ
 مِنَ اللَّهِ نُورٌ وَكِتَابٌ مُبِينٌ
 ﴿١٥﴾ يَهْدِي بِهِ اللَّهُ مَنِ اتَّبَعَ
 رِضْوَانَهُ سُبُلَ السَّلَامِ وَيُخْرِجُهُم
 مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِهِ
 وَيَهْدِيهِمْ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٦﴾

**15. Enyi Watu wa Kitabu!
 Amekwishakujieni Mtume
 Wetu Anayekufichulieni
 mengi mliyokuwa mkiya-
 ficha katika Kitabu, na
 Anayesamehe mengi. Bila
 shaka imekujieni kutoka
 kwa Mwenyezi Mungu nuru
 na Kitabu kinachobainisha.**

**16. Mwenyezi Mungu
 Huwaongoa wenye kufuata
 Radhi Yake katika njia za
 salama, na Huwatoa katika
 giza Kuwapeleka kwenye**

nuru kwa Amri Yake, na Huwaongoa kwenye njia iliyo nyooka.

Kuelezea Ukweli Kupitia Mtume ﷺ na Qur'aan

Allah تعالى Anaeleza kuwa alimtuma Mtume ﷺ pamoja na muongozo na Dini ya kweli kwa watu wote duniani, Waarabu na wasio waarabu, wenye kujua kusoma na wasiojua. Allah تعالى pia Ameeleza kuwa Alimtuma Muhammad ﷺ na ushahidi ulio dhahiri na upambanuzi baina ya ukweli na uongo. Allah تعالى Amesema,

يٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَآبِ قَدْ جَآءَكُمْ رَسُوْلُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ كَثِيْرًا مِّمَّا كُنْتُمْ تُخْفُوْنَ مِنَ
ٱلْكِتَآبِ وَيَعْفُوْا عَنْ كَثِيْرٍ

“Enyi Watu wa Kitabu! Amekwisha kujieni Mtume wetu anayekufichulieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anaye samehe mengi.”

Hivyo Mtume ﷺ alielezea pale walipobadilisha, walipopotosha na kumuongopea Allah تعالى. Aidha alipuuza mengi waliyobadilisha, kwa kuwa hayakuwa na faida yoyote. Katika Mustadrak wake, Al-Hakim alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Asiye amini kurujumiwa (mzinifu mpaka kufa) atakuwa amekanusha Qur'an bila kukusudia.” Kwa ajili hiyo Allah تعالى Amesema.

يٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَآبِ قَدْ جَآءَكُمْ رَسُوْلُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ كَثِيْرًا مِّمَّا كُنْتُمْ تُخْفُوْنَ مِنَ
ٱلْكِتَآبِ

“Enyi Watu wa Kitabu! Amekwisha kujieni Mtume wetu anayekufichulieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu.”

Na kurujumiwa lilikuwa moja ya mambo waliyokuwa wakiyaficha.¹ Al-Hakim alisema, “Isnadi yake ni sahihi, na hawakuitoa.” Baada ya hapo Allah تعالى Anataja Qur'an Takatifu Aliyomteremshia Mtume wake Mtukufu ﷺ,

وَيُخْرِجُهُمْ مِّنَ ٱلظُّلُمَٰتِ إِلَى ٱلنُّوْرِ بِإِذْنِهِ وَيَهْدِيهِمْ إِلَى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ

“Na Huwatoa katika giza Kuwapeleka kwenye nuru kwa Amri Yake, na Huwaongoa kwenye njia iliyo nyooka.”

¹ Al-Hakim 4:359.

Maana yake: Njia za usalama na uadilifu,

قَدْ جَاءَكُمْ مِنَ اللَّهِ نُورٌ وَكِتَابٌ مُبِينٌ ﴿١٥﴾ يَهْدِي بِهِ اللَّهُ مَنِ اتَّبَعَ رِضْوَانَهُ
سُبُلَ السَّلَامِ

“Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru na Kitabu kinachobainisha. Mwenyezi Mungu Huwaongoa wenye kufuata Radhi Yake katika njia za salama.

Hivyo, Huwaoko kutokana na Uangamivu na Anawaeleza yaliyo bora, njia iliyo wazi zaidi. Kwa hiyo Huwahifadhi kutokana na woga, na Huwaletea mambo mazuri wayatarajiayo, wakati huo huo Akiwatoa kwenye upotofu na Akiwaelekeza kwenye uongofu.

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ ۗ قُلْ فَمَنْ يَمْلِكُ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ أَنْ يُهْلِكَ الْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَأُمَّهُ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ۗ وَاللَّهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۗ مَا يَشَاءُ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٦﴾ وَقَالَتِ الْيَهُودُ وَالنَّصَارَىٰ نَحْنُ أَبْنَاءُ اللَّهِ وَأَحِبُّهُ ۗ قُلْ فَلِمَ يُعَذِّبُكُمْ بِذُنُوبِكُمْ ۗ بَلْ أَنْتُمْ بَشَرٌ مِمَّنْ خَلَقَ يَغْفِرُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۗ وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ ﴿١٧﴾

17. Hakika wamekufuru waliosema: Mwenyezi Mungu ni Masihi mwana wa Maryamu. Sema: Ni nani mwenye kumiliki chochote mbele ya Mwenyezi Mungu ikiwa Yeye Angetaka kumuangamiza Masihi mwana wa Maryamu, na mama yake, na wote waliomo katika ardhi? Na mamlaka ya mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ni vya Mwenyezi Mungu. Huumba Apendavyo. Na Mwenyezi Mungu Anao uweza juu ya kila kitu.

18. Na Mayahudi na Wakristo wanasema: Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake. Sema: Basi kwa nini Anakuadhibuni kwa ajili ya dhambi zenu? Bali nyinyi ni watu tu kama wale wengine Aliowaumba. Humsamehe amtakaye na Humuadhibu amtakaye. Na ni wa Mwenyezi Mungu tu Ufalme wa mbingu na ardhi. Na marejeo ni Kwake Yeye.

Imani ya Kuamini Miungu Wengi na Ukafiri wa Wakristo

Allah تعالى Anaeleza kuwa Wakristo hawana imani kwa sababu wanadai kuwa Isa عليه السلام, mwana wa Maryam, mmoja wa waja na kiumbe cha Allah تعالى ni Allah تعالى. Allah تعالى ni Mtukufu kuliko wanavyomshirikisha Naye. Kisha Allah تعالى Anawakumbusha Uwezo Wake uliotimia juu ya kila kitu, na kuwa kila kitu kiko Katika Uwezo Wake na na kina Udhhibiti Wake,

فَمَنْ يَمْلِكُ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ أَنْ يُهْلِكَ الْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَأُمَّهُ وَمَنْ فِي
الْأَرْضِ جَمِيعًا^٥

“Sema: Ni nani mwenye kumiliki chochote mbele ya Mwenyezi Mungu ikiwa Yeye Angetaka kumuangamiza Masihi mwana wa Maryamu, na mama yake, na wote waliomo katika ardhi?”

Kwa hiyo endapo Allah تعالى Ametaka kufanya hivyo, basi ni nani ataweza kumzuia Yeye kufanya Atakalo? Kisha Allah تعالى Amesema,

وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا سَخَلِقُ مَا يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Na mamlaka ya mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ni vya Mwenyezi Mungu. Huumba Apendavyo. Na Mwenyezi Mungu Anao Uweza juu ya kila kitu.”

Vitu vyote vinavyoishi (vilivyopo) ni mali ya Allah تعالى na viumbe Vyake, Yeye Ana Uwezo wa Kufanya kila kitu. Haulizwi kuhusu Afanyavyo kwa Uwezo Wake, Milki Yake, Uadilifu Wake pamoja na Ukubwa Wake. Hivyo haya ndio majibu kwa imani ya kinasara. Allah تعالى Aendelee Kuwateremshia laana mpaka siku ya Ufufuo.

Kukanusha Madai ya watu wa Kitabu kuwa wao ni Wana wa Mungu

Kisha, Allah تعالى Anakanusha madai ya uongo ya Wakristo na Wayahudi ati wao ni wana wa mungu.

وَقَالَتِ الْيَهُودُ وَالنَّصَارَىٰ نَحْنُ أَبْنَاءُ اللَّهِ وَأَحِبُّهُ^٦

“Na Mayahudi na Wakristo wanasema: Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake.”

Wanadai: “Sisi ni wafuasi wa Mitume wa Allah, ambao ni watoto wake, Ambao Anawatunza. Pia Anatupenda.” Watu wa kitabu wanadai kuwa ndani ya kitabu chao kuwa kuna maneno kuwa Allah تعالی Alimuambia mja wake Israil, ‘Wewe ni kifungua mimba’. Lakini walielezea kauli visivyo na wakapotosha maana yake, baadhi ya watu wa kitabu ambao baadaye walisilimu walikanusha maana hiyo potofu. Kauli hiyo inaonesha utukufu na heshima, kama ilivyo Ada katika hutuba zao za wakati ule.

Wakristo walidai kuwa Isa عليه السلام aliwaambia, ‘Nitarejea kwa baba yangu na baba yenu.’ Maana yake, Mola wangu na Mola wenu. Ni ukweli kwamba wakristo hawakudai kuwa nao pia ni watoto wa Allah تعالی kama walivyokuwa wakidai kwa Isa عليه السلام. Bali kauli hii ya Isa عليه السلام ilitaka kuonesha ukaribu na Allah تعالی. Kwa sababu hii, waliosema wao ni watoto wa Allah تعالی na wapendwa, Allah تعالی Alikanusha madai yao.

قُلْ فَلِمَ يُعَذِّبُكُمْ بِذُنُوبِكُمْ ۗ

“Sema: Basi kwa nini Anakuadhibuni kwa ajili ya dhambi zenu?”

Mradi wake ni kuwa, kama madai yenu ni ya kweli kuwa ni watoto na wapenzi wa Allah تعالی, basi iweje Akuandalieni moto kwa sababu ya kukanusha kwenu, uongo na madai ya uzushi?

بَلْ أَنْتُمْ بَشَرٌ مِّمَّنْ خَلَقَ

“Bali nyinyi ni watu tu kama wale wengine Aliowaumba.”

Allah تعالی Amesema, nyie ni sawa na watoto wengine wa Adam عليه السلام, na Allah تعالی ni Bwana wa viumbe Wake wote.

يَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ

“Humsamehe Amtakaye na Humuadhibu Amtakaye.”

Allah تعالی Hufanya Atakalo, hapana awezaye kukwepa hukumu Yake, na ni Mwepesi wa Kuhesabu.

وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Na ni wa Mwenyezi Mungu tu Ufalme wa mbingu na ardhi.”

Kwa hiyo kila kitu ni cha Allah تعالی na kipo chini ya Nguvu na Udhhibiti Wake,

وَالَيْهِ الْمَصِيرُ ﴿١٩﴾

“Na marejeo ni Kwake Yeye.” Mwisho, marejeo yatakuwa kwa Allah تعالى na Atawahukumu waja Wake kama Apendavyo, na ni Muadilifu sana na Hakosei katika Hukumu Yake.

يَتَأَهَّلَ الْكَتَّابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ عَلَىٰ فِتْرَةٍ مِّنَ الرَّسُلِ أَنْ تَقُولُوا مَا جَاءَنَا مِن بَشِيرٍ وَلَا نَذِيرٍ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَشِيرٌ وَنَذِيرٌ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٩﴾

19. Enyi Watu wa Kitabu! Bila ya shaka amekujilieni Mtume wetu akikubainishieni katika wakati usio kuwa na Mitume, msije mkasema: Hakufika kwetu mbashiri wala mwonyaji. Basi amekujieni mbashiri na mwonyaji. Na Mwenyezi Mungu Anao Uweza wa kila kitu.

Allah تعالى Anawaambia watu wa kitabu Mayahudi na Wakristo, Anasema kuwa Amemtuma Mjumbe Wake Muhammad ﷺ kwao, Mtume wa mwisho, baada yake hapatakuwa na Mtume wala Nabii, bali, Yeye ni Nabii wa mwisho ambaye alikuja baada ya kupita muda mrefu. Kati yake ni Isa عليه السلام, mwana wa Maryam, amani iwe juu yake.

Kuna tofauti za rai kuhusu muda uliokuwepo kati ya Mtume Isa عليه السلام na Mtume Muhammad ﷺ. Abu Uthman An-Nahdi na Qatadah walisema kuwa kilikuwa kipindi cha miaka mia sita.¹ Bukhari pia alinukuu rai hii kutoka kwa Salman Al-Farsi رضي الله عنه.² Qatadah alisema katika rai yake nyingine muda huo ulikuwa miaka mia tano na sitini,³ ambapo Maamar alisema ilikuwa miaka mia tano na arobaini.⁴

Baadhi yao walisema ilikuwa miaka mia sita na ishirini. Hapana mgongano hapa hasa tunapozingatia ukweli kuwa wale waliosema kuwa kipindi hicho kilikuwa miaka mia sita walikuwa wakizungumzia mwaka wa jua, ambapo kundi la pili wakirejea miaka ya mwezi. Kuwa kuna tofauti ya takriban miaka mitatu kati ya miaka ya mwezi na miaka ya jua kila baada ya miaka mia moja. Kama ilivyo katika Kauli ya Allah تعالى,

¹ Al-Baghawi 2:23.

² Fat'hul Al-Bari 7:324.

³ Al-Baghawi 2:23.

⁴ Abdur-Razzaq 1:186.

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ سِنِينَ وَازْدَادُوا تِسْعًا ﴿١٦﴾

“Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu, na wakazidisha tisa.”

Maana yake: Miaka tisa zaidi ya miaka ya mwezi kuwa badala ya tofauti kati ya miaka ya mwezi na jua. Hivyo kukubaliana na miaka mia tatu ya watu wa kitabu waliyojua. Tutasisitiza tena kuwa muda tulioutaja hapa kati ya Isa عليه السلام, Mtume wa mwisho kwa wana wa Israil na Muhammad ﷺ, Mtume wa mwisho kwa wanadamu wote.

Katika sahihi iliyokusanywa na Bukhari, Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِإِبْنِ مَرْيَمَ لَأَنَا، لَيْسَ بَيْنِي وَبَيْنَهُ نَبِيٌّ»

“Mimi miongoni mwa watu wote, nina haki zaidi kwa mwana wa Maryamu, kwa sababu hapakuwa na Mtume kati yake nami.”¹

Hadithi hii inakanusha rai ya Al-Qudhaiy na wenzake, kuwa alikuwapo Mtume baada ya Mtume Isa عليه السلام aliyeitwa Khalid bin Sinan, Allah تعالى Alimtuma Muhammad ﷺ baada ya kipindi ambacho hakikuwa na Mtume, na muongozo wa Allah تعالى pamoja na Dini yake kufutika na watu kuanza kuabudu misalaba kulitokana wakati huo. Kwa hiyo Ihsani ya kumtuma Muhammad ﷺ ilikuwa ni fadhila iliyotimia wakati ambapo alihitajika sana.

Uovu ulijaza dunia wakati ule, na ukandamizaji na ujinga uliwagusa waja wote, isipokuwa wachache waliobaki kuwa waaminifu kwa mafundisho ya Mitume waliopita, kama baadhi ya Marabbi wa Kiyahudi, Mapadri wa Kikristo na Mahasusi wa Sabian.

Imam Ahmad رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Iyadh bin Himar Al-Mujash رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alitoa hutuba siku moja kwa kusema,

«وَإِنَّ رَبِّي أَمَرَنِي أَنْ أَعْلَمَكُم مَّا جَهِلْتُمْ مِمَّا عَلَّمَنِي فِي يَوْمِي هَذَا، كُلُّ مَا لِي نَحَلْتُهُ عِبَادِي حَلَالٌ، وَإِنِّي خَلَقْتُ عِبَادِي خُنَفَاءَ كُلُّهُمْ، وَإِنَّ الشَّيَاطِينَ أَتَتْهُمْ فَأَصْلَتْهُمْ عَنْ دِينِهِمْ، وَحَرَمْتُ عَلَيْهِمْ مَا أَخَلَلْتُ لَهُمْ، وَأَمَرْتُهُمْ أَنْ يُشْرِكُوا بِي مَا لَمْ أَنْزَلْ بِهِ سُلْطَانًا، ثُمَّ إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ نَظَرَ إِلَى أَهْلِ الْأَرْضِ فَمَقَّتَهُمْ عَرَبِيَّتَهُمْ وَعَجَمَتَهُمْ، إِلَّا

¹ Fat'hul Al-Bari 6:550.

بَقَايَا مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ، وَقَالَ: إِنَّمَا بَعَثْتُكَ لِأَبْتَلِيكَ وَأَبْتَلِي بِكَ، وَأَنْزَلْتُ عَلَيْكَ كِتَابًا لَا يَغْسِلُهُ الْمَاءُ، تَقْرَأُهُ نَائِمًا وَيَقْظَانَ، ثُمَّ إِنَّ اللَّهَ أَمَرَنِي أَنْ أُحْرَقَ فُرَيْنَا فَقُلْتُ: يَا رَبِّ إِذْ بِنْتُكَ وَأَسِي، فَيَدْعُوهُ خَيْرَةً، فَقَالَ: اسْتَخْرِجْهُمْ كَمَا اسْتَخْرِجُوكَ، وَاعْزُهُمْ نُعْرَكَ، وَأَنْفِقْ عَلَيْهِمْ فَسَتُنْفِقَ عَلَيْكَ، وَابْعَثْ جَيْشًا تَبَعَتْ خَمْسًا أَمْثَالَهُ، وَقَاتِلْ بِمَنْ أَطَاعَكَ مِنْ عَصَاكَ، وَأَهْلُ الْجَنَّةِ ثَلَاثَةٌ: ذُو سُلْطَانٍ مُقْسِطٌ مُوَفَّقٌ مُتَّصِدٌ، وَرَجُلٌ رَجِيمٌ رَقِيقُ الْقَلْبِ بِكُلِّ ذِي قُرْبَى وَمُسْلِمٍ، وَرَجُلٌ عَفِيفٌ فَقِيرٌ ذُو عِيَالٍ [مُتَّصِدٌ]. وَأَهْلُ النَّارِ خَمْسَةٌ: الضَّعِيفُ الَّذِي لَا دِينَ لَهُ، وَالَّذِينَ هُمْ فِيكُمْ نَجَسٌ أَوْ نَجَسًا - سَكَ يَحْيَى - لَا يَتَّقُونَ أَهْلًا وَلَا مَالًا، وَالْحَايِنُ الَّذِي لَا يَخْفَى لَهُ طَمَعٌ وَإِنْ دَقَّ إِلَّا خَاتَمَهُ، وَرَجُلٌ لَا يُضِيحُ وَلَا يُنْسِي إِلَّا وَهُوَ يُخَادِعُكَ عَنْ أَهْلِكَ وَمَالِكَ - وَذَكَرَ النَّبِيْلَ أَوْ الْكَذَّابَ - وَالسُّنْظِيرَ: الْفَاجِسَ»

"Mola wangu Ameniamuru nikufundisheni msiyoyajua ambayo kwayo Amenifundisha leo, "Utajiri wote niliowapa waja Wangu ni halali. Niliwaumba waja Wangu wote Hunafaa. Lakini shetani aliwajia na akawatoa katika Dini yao, akawaharamishia Niliyo wahalilisha, na akatoa ruksa. Na akawaamuru wanishirikishe Mimi kwa jambo ambalo Sikulieleza kabisa kwao wao. Waarabu na wasio Waarabu miongoni mwao, isipokuwa wachache miongoni mwa Wana wa Israil. Allah Akaniambia! Nilikupelekea ili kukujaribu na kuwa mtihani kwako. Nilikupelekea Kitabu ambacho hakiwezi kukoshwa na maji (ni cha milele, na utakisoma ukiwa macho na ukiwa umelala! Allah pia Alimuamuru niwachome (kuwaangamiza) Quraysh. Hivyo nikasema, 'Ewe mola! Watakata kichwa changu na kukiacha kama kipande cha mkate.' Akasema, 'Nitawatoa katika mji kama walivyokutoa, na utakapowavamia Tutakusaidia. Watumie masahaba zako na sisi Tutatumia kwa ajili yako, peleka jeshi na sisi Tutapeleka majeshi mara tano kama hayo (kuwapa usaidizi). Pigana pamoja na wale wanaokutii, dhidi ya wale wanaokuasi. Na wakazi wa peponi ni wa aina tatu: Kiongozi muadilifu aliyefuzu, mkarimu na mkweli; Mtu mrehemevu, msamehevu, mwenye moyo mkunjufu kwa jamaa na kila Muislamu; na mtu masikini mwenye watu wanaomtegemea naye ni mwenye kuwasaidia. Na wakazi wa Motoni ni watano, dhaifu asiye na dini, wale wanaofuata watu sikwa sababu

za kifamilia wala utajiri, na tapeli ambaye haachi utapeli wake hata kwa mambo madogo, na mtu anayekuja kila asubuhi na jioni, anaidanganya familia yako au kupata mali yako kwa njia ya dhulma. Na akamtaja mzushi au muongo, na mtu mwenye mdomo mchafu.”¹

Kwa hiyo, Hadithi inaeleza kuwa Allah تعالی Aliwaangalia watu wa dunia na akawachukia wote, waarabu na wasio waarabu, miongoni mwao, isipokuwa wachache miongoni mwa wana wa Israil au wachache miongoni mwao watu wa kitabu kama alivyorekodi Muslim.² Dini ilipotoshwa na ilibadilishwa kwa watu wa dunia mpaka Allah تعالی Alipomtuma Muhammad ﷺ, na Allah تعالی kwa sababu hiyo, Aliwaongoza viumbe na Akawatoa kwenye kiza na Kuwaingiza kwenye mwanga na Akawawekea njia iliyo sawa na sharia takatifu. Allah تعالی Amesema,

أَنْ تَقُولُوا مَا جَاءَنَا مِنْ بَشِيرٍ وَلَا نَذِيرٍ

“Msije mkasema: Hakufika kwetu mbashiri wala mwonyaji.”

Maana: Wasije kujenga hoja na kusema ya kuwa: “Enyi ambao mmeibadilisha dini yenu: Hatukujia sisi Mtume anayehubiria katika kheri na kutuonya shari.” Hivyo amekuja kwenu mleta habari njema na muonyaji, ambaye ni Mtume Muhammad ﷺ,

وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Na Mwenyezi Mungu Anao uweza wa kila kitu.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالی amesema, “Nina uwezo wa Kuwaadhibu wanaoniasi Mimi na Kuwalipa wale wanonitii Mimi.”¹



¹ Ahmad 4:162, na Muslim, kama ilivyooneshwa hapa chini.

² Muslim 4:2197.

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ يَنْقُورِ ادْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِيكُمْ أَنْبِيَاءَ وَجَعَلَكُمْ مُلُوكًا وَآتَاكُمْ مَا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿٢٠﴾ يَنْقُورِ ادْخُلُوا الْأَرْضَ الْمُقَدَّسَةَ الَّتِي كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَرْتَدُّوا عَلَىٰ أَدْبَارِكُمْ فَتَنْقَلِبُوا خَاسِرِينَ ﴿٢١﴾ قَالُوا يَمْوَسَىٰ إِنَّ فِيهَا قَوْمًا جَبَّارِينَ وَإِنَّا لَنَنْدُخُلُهَا حَتَّىٰ تَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِن يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِنَّا دَاخِلُونَ ﴿٢٢﴾ قَالُوا لَنْ نَدْخُلَهَا حَتَّىٰ يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِن يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِنَّا دَاخِلُونَ ﴿٢٣﴾ قَالُوا لَنْ نَدْخُلَهَا أَبَدًا مَا دَامُوا فِيهَا ۗ فَاذْهَبْ أَنتَ وَرَبُّكَ فَقَتِيلًا إِنَّا هَاهُنَا قَاعِدُونَ ﴿٢٤﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي لَا أَمْلِكُ إِلَّا نَفْسِي وَأَخِي ۗ فَافْرُقْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٥﴾ قَالَ فَإِنَّهَا مُخِرمَةٌ عَلَيْنَ ۗ أَرْبَعِينَ سَنَةً ۗ يَتِيهُونَ فِي الْأَرْضِ ۗ فَلَا تَأْسَ عَلَى الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٦﴾

* وَأَتْلُ عَلَيْنَ نَبَأَ ابْنِي آدَمَ بِالْحَقِّ إِذْ قَرَّبَا قُرْبَانًا فَتُقْبِلَ مِنْ أَحَدِهِمَا وَلَمْ يُتَقَبَلْ مِنَ الْآخَرِ قَالَ لَأَقْتُلَنَّكَ ۗ قَالَ إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٢٧﴾ لَئِن بَسَطْتَ إِلَيَّ يَدَكَ لِتَقْتُلَنِي مَا أَنَا بِبَاسِطِ يَدَيْ إِلَيْكَ لِأَقْتُلَنَّكَ ۗ إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٨﴾ إِنِّي أُرِيدُ أَنْ نَبُوءَ بِإِثْمِي وَإِثْمِكَ فَتَكُونَ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ ۗ وَذَلِكَ جَزَاءُ الظَّالِمِينَ ﴿٢٩﴾ فَطَوَّعَتْ لَهُ نَفْسُهُ قَتْلَ أَخِيهِ فَقَتَلَهُ ۗ فَأَصْبَحَ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٣٠﴾ فَجَعَلَ اللَّهُ غُرَابًا يَبْحَثُ فِي الْأَرْضِ لِيُرِيَهُ كَيْفَ يُورِي سَوَاءَ أَخِيهِ ۗ قَالَ يَتُولَّيْنِي أُعْجِزْتُ أَنَّ أَكُونَ مِثْلَ هَذَا الْغُرَابِ فَأُوْرِي سَوَاءَ أَخِي ۗ فَأَصْبَحَ مِنَ النَّادِمِينَ ﴿٣١﴾

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يَنْقُورِ ادْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِيكُمْ أَنْبِيَاءَ وَجَعَلَكُمْ مُلُوكًا وَآتَاكُمْ مَا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿٢٠﴾ يَنْقُورِ ادْخُلُوا الْأَرْضَ الْمُقَدَّسَةَ الَّتِي كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَرْتَدُّوا عَلَىٰ أَدْبَارِكُمْ فَتَنْقَلِبُوا خَاسِرِينَ ﴿٢١﴾ قَالُوا يَمْوَسَىٰ إِنَّ فِيهَا قَوْمًا جَبَّارِينَ وَإِنَّا لَنَنْدُخُلُهَا حَتَّىٰ يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِن يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِنَّا دَاخِلُونَ ﴿٢٢﴾ قَالُوا لَنْ نَدْخُلَهَا حَتَّىٰ يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِن يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِنَّا دَاخِلُونَ ﴿٢٣﴾ قَالُوا لَنْ نَدْخُلَهَا أَبَدًا مَا دَامُوا فِيهَا ۗ فَاذْهَبْ أَنتَ وَرَبُّكَ فَقَتِيلًا إِنَّا هَاهُنَا قَاعِدُونَ ﴿٢٤﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي لَا أَمْلِكُ إِلَّا نَفْسِي وَأَخِي ۗ فَافْرُقْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٥﴾ قَالَ فَإِنَّهَا مُخِرمَةٌ عَلَيْنَ ۗ أَرْبَعِينَ سَنَةً ۗ يَتِيهُونَ فِي الْأَرْضِ ۗ فَلَا تَأْسَ عَلَى الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٦﴾

20. Na pale Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, Alipowateuwa Manabii kati yenu, na Akakufanyeni watawala, na Akakupeni ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu.

21. Enyi watu wangu! Ingieni katika nchi takatifu ambayo Mwenyezi Mungu Amekuandikieni. Wala msirudi nyuma, msije mkawa wenye kukhasirika.

22. Wakasema: Ewe Musa! Huko wako watu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka wao watoke humo. Wakitoka humo hapo tutaingia.

23. Watu wawili miongoni mwa wachamungu ambao Mwenyezi Mungu Amewaneemesha, walisema: Waingilieni kwa mlangoni. Mtakapowaingilia basi kwa yakini nyinyi mtashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini.

24. Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa.

25. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu. Basi tutenge na hawa watu wapotovu.

26. (Mwenyezi Mungu) Akasema: Basi nchi hiyo wameharimishiwa muda wa miaka arubaini, watakuwa wakitanga-tanga katika ardhi. Basi wewe usiwasikitikie watu wapotovu.

Musa عليه السلام Anawakumbusha watu wake Fadhila za Allah تعالى na Kuwaamuru wao kuingia Ardhi Tukufu.

Allah تعالى Anaeleza kuwa mja Wake, Nabii ambaye Alizungumza naye moja kwa moja, Musa bin Imran عليه السلام, aliwakumbusha watu wake fadhila wanazopewa na Allah تعالى, kwa kuwapa mazuri yote ya maisha ya duniani na Akhera, endapo watabakia katika uongofu na njia iliyonyooka. Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 10:158.

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يُقَوْمِ أَدْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِيكُمْ أَنْبِيَاءَ

“Na pale Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, Alipowateuwa Manabii kati yenu,”

Kwani kila alipofariki dunia Mtume, aliletwa Mtume mwingine katika uzao wa baba yenu Ibrahim عليه السلام na waliomfuata yeye.

Kuna Mitume wengi miongoni mwa wana wa Israel walihubiri kwa Allah تعالى na wakionya dhidi ya adhabu Yake, mpaka Isa عليه السلام alipotumwa kuwa Mtume wa mwisho kutoka kwa wana wa Israel. Kisha Allah تعالى Akashusha wahyi kwa Mtume wa mwisho na Mjumbe wake, Muhammad ﷺ, mwana wa Abdullah, kutoka kizazi kitukufu cha Ismail عليه السلام, mwana wa Ibrahim عليه السلام. Muhammad ﷺ ni Mtume mwenye heshima kubwa kwa Mitume wote. Allah تعالى Amenena baadaye,

وَجَعَلَكُمْ مَلُوكًا

“Na Akakufanyeni watawala,...”

Abdur-Razzaq aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo; “Kuwa na mtumishi, mke na nyumba.”¹ Katika Mustadrak wake Al-Hakim alirekodi kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “mke na mjakazi.”

وَأَتَانَكُمْ مَا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ

“Na Akakupeni ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu.”

Maana: ‘Wakati wa zama zao.’² Al-Hakim alisema, “Sahihi kwa mujibu wa kigezo cha sahihi mbili, lakini hawakuikusanya.’ Qatadah alisema, “Walikuwa watu wa mwanzo kuchukua wajakazi.”³ Hadithi inaeleza,

«مَنْ أَصْبَحَ مِنْكُمْ مُعَافَىٰ فِي جَسَدِهِ، آيِنًا فِي سِرْبِهِ، عِنْدَهُ قُوَّةٌ يَّوْمِهِ، فَكَأَنَّمَا حَبِيزَتْ لَهُ الدُّنْيَا بِحَدَائِفِهَا»

“Yule miongoni mwenu ambaye ameamka asubuhi hali ya kuwa ni

¹ Abdur-Razzaq 1:187.

² Al-Hakim 2:312.

³ At-Tabari 10:163.

*mwenye siha katika mwili wake, ana amani katika familia yake na akawa na chakula cha siku ile; ni kama vile dunia na vyote vilivyomo ndani yake vilikusanywa kwa ajili yake.*¹

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَتَانَكُمْ مَا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ

“Na Akakupeni ambayo Hakuwapa wowote katika walimwengu.”

Maana: Wakati wa zama zenu, kama Tulivyodhukuru. Wana wa Israel walikuwa watukufu zaidi miongoni mwa watu wa zama zao, wakilinganishwa na Wagiriki, na binadaamu wote. Allah تعالى Amesema katika Aya nyengine,

وَلَقَدْ آتَيْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ وَرَزَقْنَاهُمْ مِّنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى
الْعَالَمِينَ ﴿١٦﴾

“Na hakika Tuliwapa Wana wa Israili Kitabu na hukumu na Unabii, na Tukawaruzuku vitu vizuri vizuri, na Tukawafadhilisha kuliko walimwengu wote.” (45:16)

Allah تعالى Amesema:

قَالُوا يَمْؤُوسَىٰ اجْعَلْ لَنَا إِلَهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ ﴿١٧﴾ إِنَّ هَٰؤُلَاءِ
مُتَّبِعُونَ مَا هُم فِيهِ وَيَنْطَلِقُونَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٨﴾ قَالَ أَغَيَّرَ اللَّهُ أَبْغَيْكُمْ إِلَهًا وَهُوَ
فَضَّلَكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٩﴾

“Wakasema: Ewe Musa! Hebu tufanyie na sisi miungu kama hawa walivyokuwa na miungu. Musa akasema: Hakika nyinyi ni watu msiojua kitu. Hakika haya waliyonayo watu hawa yatakuja angamia, na hayo waliyokuwa wakiyafanya yamepotea bure. Akasema: Je, nikutafutieni mola asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na Yeye Ndiye Aliyekufadhilisheni juu ya viumbe vyote?” (7:138-140)

Kwa hiyo, walikuwa bora zaidi miongoni mwa watu wa zama zao. Ummah wa Kiislamu umeheshimiwa na kutukuzwa zaidi mbele ya Allah تعالى, na una sheria

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 7:11.

zilizotimia na mfumo kamili wa maisha, una Mtume Mtukufu zaidi, dola kubwa, vyakula vingi, utajiri na watoto, himaya kubwa, furaha ya kudumu kuliko wana wa Israel. Allah تعالى Amesema.

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ

“Na vivyo hivyo Tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu,...” (2:143)

Tulitaja hadithi *Mutawatir* kuhusu heshima ya Ummah huu na hadhi na utukufu wake kwa Allah تعالى, tulipoeleza Kauli ya Allah تعالى katika Surah Al-Imran (3),

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

“Nyinyi mmekuwa bora ya umma waliotolewa kwa watu,...” (3:110)

Allah تعالى Anaeleza baadaye kuwa Musa عليه السلام aliwashajiisha wana wa Israel kupigana Jihad na kuingia Jerusalem, ambayo ilikuwa chini ya himaya yao zama za baba yao Yaqub عليه السلام. Yaqub عليه السلام na watoto waliohamia Misri wakati wa Nabii Yusuf عليه السلام. Watoto wake walisalia Misri mpaka wakati wa mapambano yao na Musa عليه السلام. Waliwakuta watu wababe na wenye nguvu Jerusalem ambao waliichukua baadaye. Musa عليه السلام, Nabii wa Allah تعالى, aliwaamuru wana wa Israel kuingia Jerusalem na kuwapiga adui yao, na aliwaahidi ushindi juu ya watu wenye nguvu kama wangelifanya hivyo, walikataa, waliasi na wakapinga amri yake. Hivyo, waliadhibiwa kwa miaka arobaini kwa kupotea na kuhangaika katika ardhi bila kujua mahali pa kwenda. Hii ilikuwa adhabu yao kwa kukataa Amri ya Allah تعالى,

Allah تعالى Amesema kuwa Musa عليه السلام aliwaamuru kuingia Ardhi Tukufu,

الَّتِي كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ

“Ambayo Mwenyezi Mungu Amekuandikieni.”

Maana: Ambayo Allah تعالى Aliwaahidi kwa maneno ya baba yenu Israil, kuwa ni Urithi kwa wale wanaoamini.

وَلَا تَرْتَدُوا عَلَىٰ أَذْبَارِكُمْ

“Wala msirudi nyuma,...” Maana: Wala msisite kupigana Jihad.

فَتَنقَلِبُوا حَسْرِينَ ﴿٢٠﴾ قَالُوا يَمْوَسَىٰ إِنَّ فِيهَا قَوْمًا جَبَّارِينَ وَإِنَّا لَن نَدْخُلُهَا حَتَّىٰ نَخْرُجُوا
مِنْهَا فَإِن نَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِنَّا دَاخِلُونَ ﴿٢١﴾

“Msije mkawa wenye kukhasirika. Wakasema: Ewe Musa! Huko wako watu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka wao watoke humo. Wakitoka humo hapo tutaingia.”

Kisingizio chao kilikuwa hiki, katika mji huu uliotuamrisha tuingie na kuwapiga watu wake, kuna watu majabari, wenye nguvu, watu waovu wenye maumbile ya kutisha na uwezo wa kimwili. Kwa hiyo wakasema, hatuna uwezo wa kuingia mji huu madhali bado wapo ndani yake, lakini wakitoka, nasi tutaingia, vinginevyo, hatuwezi kamwe kuwakabili.

Hotuba za Yuwsha (Joshua) na Kalib (Caleb):

Allah تعالی Amesema:

قَالَ رَجُلَانِ مِنَ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَن نَّمُوتَ اللَّهُ عَلَيْهِمَا

“Watu wawili miongoni mwa wachamngu ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha, walisema...”

Wana wa Israil walipokataa kumkiri Allah تعالی na kumfuata Mjumbe Wake Musa عليه السلام, wachamungu wawili miongoni mwao, ambao Allah تعالی Aliwapa fadhila nyingi na ambao wakimuhofu Allah تعالی na wakiihofu adhabu Yake, waliwashajiisha kusonga mbele. Pia ilisemwa kuwa Ayah inasomeka katika njia ambayo ina maana kuwa watu hao, waliheshimiwa na kutukuzwa na watu wao. Watu hao wawili walikuwa Yuwsha, mwana wa Nun; na Kalib, mwana wa Yufna, kama Ibn Abbas رضي الله عنهما, Mujahid, Ikrimah, Aliyyah, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas na *Salaf* wengine na wanazuoni wa karibuni walivyosema.¹ Watu hao wawili waliwaambia watu wao,

أَدْخُلُوا عَلَيْهِمُ الْبَابَ فَإِذَا دَخَلْتُمُوهُ فَإِنَّكُمْ عَلَيْهِونَ وَعَلَىٰ اللَّهُ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Waingilieni kwa mlangoni. Mtakapowaingilia basi kwa yakini nyinyi mtashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini.”

¹ At-Tabari 10:176-178.

Kwa hiyo, walisema, kama mnategemea kumuamini Allah تعالى, fuateni amri na mumtii Mjumbe Wake, kisha Allah تعالى Atawapeni ushindi dhidi ya maadui zenu na Atawapeni ukuu juu yao. Hivyo mtauteka Mji ambao Allah تعالى Aliwaahidi. Ushauri huu haukuwasaidia hata kidogo.

قَالُوا يَنْمُوسَىٰ إِنَّ لَكَ لَأَجْرًا غَيْرَ الْمَوْتِ فَقَالَ أَتَدْرُونَ
قَالُوا بَلَىٰ إِنْ كُنَّا بِعِلْمِ رَبِّنَا لَسَاءُ لِلَّذِينَ اتَّخَذُوا دُونَهُ مَوْتًا مَّا دَامُوا فِيهَا فَادَّهَبَ عَنْتَ وَرَبِّكَ فَقَتَلْنَا إِنَّا هَاهُنَا

“Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa.”

Hivi ndivyo walivyokataa kujiunga na Jihad, wakamkiuka Nabii wao, na wakakataa kumpiga adui yao.

Muitikio Mzuri wa Masahaba Wakati wa Vita ya Badr:

Hakuna jibu zuri kama ambalo Masahaba walimpa Mtume ﷺ wakati wa vita vya Badr, alipowataka shauri juu ya kupigana na jeshi la Quraysh, ambalo lilikuja kuhami msafara ulioongozwa na Abu Sufyan. Jeshi la Waislamu lilipoukosa msafara na jeshi la Quraysh lililokuwa na askari wenye nguvu mia tisa au elfu moja, waliposogea karibu, Abubakar رضي الله عنه alisimama na kusema jambo zuri. Na Muhajiri kadhaa walizungumza, wakati huo Mtume ﷺ alisema,

«أَشِيرُوا عَلَيَّ أَيُّهَا الْمُسْلِمُونَ»

“Nishaurini Enyi Waislamu!”

Mtume ﷺ akimaanisha Ansar ambao waliokuwa wengi wakati huo. Sa’d bin Mu’adh رضي الله عنه alisema, “Inaelekea kama unatukusudia sisi, Ewe Mjumbe wa Allah! Kwa jina la Yule Aliyekutuma na Ukweli! Kama unakusudia kukatisha bahari na kuingia ndani yake, tutakufuata na hapana kati yetu atakayebaki nyuma. Hatutachukia kukufuata na kukabiliana na adui yetu kesho. Tuna subira katika vita, umakini katika mapambano. Allah تعالى Akuwezeshe kushuhudia juhudi zetu, zitakufariji. Kwa hiyo, songa mbele na Rehema za Allah تعالى.” Mtume ﷺ aliridhika kwa maneno ya Sa’d رضي الله عنه na alishajiishwa kusonga mbele.¹

¹ At-Tabari 13:399.

Abubakar bin Marduwayh رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa alisema Mtume ﷺ alipokwenda kwenye vita vya Badr, aliomba ushauri kwa Waislamu. Na Umar رضي الله عنه akamshauri, “Enyi Ansar! Mtume anataka kusikia kutoka kwenu.” Wakajibu, “Hatutasema kama Wana wa Israil walivyomuambia Musa عليه السلام,

فَأَذْهَبَ أَنْتَ وَرَبُّكَ فَقَتِيلًا إِنَّا هَاهُنَا قَاعِدُونَ.

“Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa.”

Kwa Jina la Yule Aliyekutuma na Ukweli! Iwapo utachukua ngamia na kuwapeleka Bark Al-Ghamad (Jirani na Makkah) tutakufuata. Imam Ahmad, An-Nasai na Ibn Hibban,¹ pia wameinukuu Hadithi hii.

Katika Kitabu cha *Al-Maghazi* na *At-Tafsir*, Bukhari alinukuu kuwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema, “Katika siku ya Badr, Al-Miqdadi alisema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Hatutosema maneno walivyoyasema Wana wa Israil kumuambia Musa عليه السلام,

فَأَذْهَبَ أَنْتَ وَرَبُّكَ فَقَتِيلًا إِنَّا هَاهُنَا قَاعِدُونَ.

“Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa.”

Bali songa mbele nasi tutakuwa nawe.” Mtume ﷺ alifurahishwa baada ya kusikia kauli hii.”²

Musa عليه السلام Anaomba Dua kwa Allah تعالى Dhidi ya Mayahudi

Musa عليه السلام alisema,

قَالَ رَبِّ إِنِّي لَا أَمْلِكُ إِلَّا نَفْسِي وَأَخِي ۖ فَافْرِقْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْفَاسِقِينَ ﴿٦٥﴾

“Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu. Basi tutenge na hawa watu wapotovu.”

¹ Ahmad 3:105, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:334 na Ibn Hibban 7:109. Silsila ya riwaya hii si sahihi, lakini sehemu yake inaungwa mkono na riwaya inayofuata na ya kabla yake.

² Al-Bukhari na. 4609.

Wana wa Israil walipokataa kupigana, Musa عليه السلام aliwakasirikia sana na akaomba dua kwa Allah تعالى dhidi yao,

رَبِّ إِنِّي لَأَمْلِكُ إِلَّا نَفْسِي وَأَخِي^ط

“Mola wangu Mlezi! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu.”

Maana: Mimi na ndugu yangu Harun عليه السلام tu ndio tutakutii, kutekeleza Amri za Allah تعالى na kuitika wito,

فَأَفْرِقْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ

“Basi tutenge na hawa watu wapotovu.”

Al-Awfi aliarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Ina maana tuhukumu baina yetu na wao.”² Ali bin Abi Talhah aliarifu vivyo hivyo kutoka kwao.³ Adh-Dhahhak alisema kuwa Aya hiyo ina maana, “Tuhukumu na uamue baina yetu na wao.”⁴ Wanazuoni wengine walisema kuwa Aya inamaanisha, “Tutenganishe na wao.”

Kuzuiwa Mayahudi Kuingia Ardhi Takatifu kwa Miaka Arobaini:

Allah تعالى Amesema,

فَإِنَّهَا مُحَرَّمَةٌ عَلَيْهِمْ أَرْبَعِينَ سَنَةً يَتِيهُونَ فِي الْأَرْضِ^ع

“Basi nchi hiyo wameharimishiwa muda wa miaka arubaini, watakuwa wakitanga-tanga katika ardhi.”

Musa عليه السلام alipoomba dua dhidi ya Mayahudi kwa kukataa kupigana Jihad, Allah تعالى Aliwazuia kuingia ardhi takatifu kwa miaka arobaini, wakihangaika, walipopotea katika ardhi ya At-Tih, bila kujua njia ya kutokea. Wakati huo, miujiza mikubwa ilitokea, kama vile mawingu yaliyowafunika na *manna* na ndege (*salwa*) vilivyoteremshiwa na Allah تعالى. Allah تعالى Awatolea maji kutoka majabali, na miujiza mingine Aliyomsaidia nayo Musa bin Imran عليه السلام.

¹ At-Tabari 10:188.

² At-Tabari 10:189.

³ At-Tabari 10:189.

Wakati huo, Taurati iliteremshwa na Sharia iliwekwa kwa Wana wa Israil, na tebanakulo la kuabudia lilijengwa.

Ufunguzi wa Baitul Makdisi (Ardhi Takatifu)

Kauli ya Allah تعالى،

أَرْبَعِينَ سَنَةً

“Miaka arubaini,” Inaeleza,

يَتِيمُهُمْ فِي الْأَرْضِ

“Watakuwa wakitanga-tanga katika ardhi.”

Miaka hiyo ilipokwisha, Yuusha bin Nun aliwaongoza wale waliosalia miongoni mwao na kizazi cha pili, na wakaizingira ardhi takatifu - Baitul - Makdisi na kuiteka siku ya Ijumaa mchana. Jua lilipokuribia kuchwa na Yuusha aliogopa kuwa Sabato ingeanza, aliliambia (jua), “Unaamrisha na nimeamrisha vile vile – Ewe Allah! Lisimamishe lisizame kwa ajili yangu.” Allah تعالى Alilizuia jua lisichwe mpaka Yuusha bin Nun alipoiteka Ardhi takatifu Baitul Makdisi. Baadaye Allah تعالى Alimuamuru Yuusha awaamuru Wana wa Israil kuingia Ardhi takatifu Baitul Makdisi kupitia lango lake huku wameinama wakisema *Hittah* yaani ‘tufutie dhambi zetu.’ Hata hivyo walibadilisha walivyoamriwa waliingia wakijiburuta kwa mgongo huku wakinena, *Habbah* (mbegu) ndani ya *Shaarah* (unywele)’. Tuliyaeleza yote haya katika *Tafsir ya Surat Al-Baqarah*. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo,

فَإِنَّهَا مُحَرَّمَةٌ عَلَيْهِمْ أَرْبَعِينَ سَنَةً يَتِيمُهُمْ فِي الْأَرْضِ

“Basi nchi hiyo wameharimishiwa muda wa miaka arubaini, watakuwa wakitanga-tanga katika ardhi.”

Walizurura katika ardhi kwa miaka arobaini, katika kipindi ambacho Musa عليه السلام na Harun عليه السلام walifariki dunia, na kila mtu aliyekuwa na umri juu ya miaka arubaini. Miaka arobaini ilipotimia, Yuusha mwana wa Nun alichukua uongozi na baadaye akaiteka Ardhi takatifu Baitul Makdisi.¹ Yuusha

¹ Toleo sawa na hilo limeandikwa na At-Tabari 10:193.

alipokumbushwa kuwa siku ile ilikuwa Ijumaa na jua lilikaribia kuchwa, ambapo walikuwa bado wanashambulia Ardhi takatifu Baitul Makdisi, alichelea kuwa Sabato ingeanza. Kwa hiyo akaliambia jua, 'Nimeamrisha nawe umeamrisha.' Allah تعالی Alifanya jua lizame na Mayahudi wakaiteka Ardhi takatifu Baitul Makdisi na walikuta utajiri ambao hawakuwahi kuuona kabla. Walitaka moto uteketeze ngawira lakini moto haukufanya hivyo. Yuusha alisema, 'Baadhi yenu mmeiba kutokana na ngawira.' Kwa hiyo aliwaita viongozi wa makabila kumi na mawili na akachukua ahadi kutoka kwao. Kisha mkono wa mmoja wao ulikwama katika mkono wa Yuusha na Yuusha akasema, "Uliiba, hivyo rejeshwa ulivyoiba.' Hivyo mtu yule alileta kichwa cha Ng'ombe kilichotengenezwa kwa dhahabu na macho mawili yaliyotengenezwa kwa mawe ya thamani na meno yaliyotengenezwa kwa lulu. Yuusha alipoiongeza kwenye ngawira, moto uliita, kwanini walikatazwa kuweka ngawira. Kuna ushahidi unaounga mkono haya yote katika sahih.

Allah تعالی Anamfariji Musa عليه السلام.

Katika kumfariji Nabii Musa عليه السلام, Allah تعالی Alisema:

فَلَا تَأْسَ عَلَى الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ

"Basi wewe usiwasikitikie watu wapotovu."

Allah تعالی Alimuwambia usijihisi huzuni juu ya Hukumu Yangu dhidi yao, kwani wanastahili hukumu hiyo.

Kisa hiki kinawatia adabu Mayahudi, kinadhihirisha kumuasi kwao Allah تعالی na Mjumbe Wake, na kukataa kwao kutii amri ya Jihadi. Walikuwa dhaifu na hawakuipokea fikra ya kupambana na adui yao, kwa kuwa ngangari na kubeba sifa ya ushujaa wa kupigana na adui yao. Haya yalijiri huku wakiwa na Mtume miongoni mwao ambaye Allah تعالی Alizungumza naye, na alikuwa kiumbe bora zaidi wa Allah تعالی, kwa wakati ule. Mtume wao aliwaahidi ushindi dhidi ya maadui wao. Kadhalika walishuhudia maangamivu na adhabu ya kugharikishwa ambayo Allah تعالی Aliwaadhibu adui wao Firauni na wanajeshi wake, kiasi kwamba macho yao yaliridhishwa na kufarajiwa. Haya hayakutukia muda mrefu uliopita, lakini walikataa kufanya Jihadi dhidi ya watu ambao walikuwa na nguvu iliyokuwa chini zaidi ya moja ya kumi ya waliyokuwa nayo wamisri.

Kwa hivyo, uovu wa Wayahudi ulianikwa kwa kila mmoja, kuanikwa kulikokuwa kukubwa kiasi kwamba usingeweza kumaliza athari zake. Pia walipofushwa na ujinga na urukaji wao wa mipaka. Kwa hivyo, wakaghadhibikiwa na Allah تعالى na wakawa maadui Wake. Bado wanadai kuwa wao ni wana wa Mwenyezi Mungu na wapenzi Wake! Allah تعالى Azilaani nyuso zao zilizogeuzwa na kuwa na sura za nguruwe na nyani. Laana za Allah تعالى ziwaandame mpaka waingie kwenye Moto wenye hasira kali. Allah تعالى Awajaalie wakae Motoni milele, na Alishapitisha hilo, kila Sifa Njema Anazistahiki Yeye.

* وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ ابْنَيْ آدَمَ بِالْحَقِّ إِذْ قَرَّبَا قُرْبَانًا فَتُقْبِلَ مِنْ أَحَدِهِمَا وَلَمْ يُتَقَبَلْ مِنْ
 الْآخَرِ قَالَ لَأَقْتُلَنَّكَ ۗ قَالَ إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٢٠﴾ لَئِنْ بَسَطْتَ إِلَيَّ يَدَكَ
 لِتَقْتُلَنِي مَا أَنَا بِبَاسِطٍ يَدِيَ إِلَيْكَ لِأَقْتُلَنَّكَ ۗ إِنَّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿٢١﴾ إِنِّي أُرِيدُ
 أَنْ تَبُوءَ بِإِذْنِي وَإِيمَانِكَ فَتَكُونُ مِنَ أَصْحَابِ النَّارِ ۗ وَذَلِكَ جَزَاءُ الظَّالِمِينَ ﴿٢٢﴾ فَطَوَّعَتْ
 لَهُ نَفْسُهُ قَتْلَ أَخِيهِ فَقَتَلَهُ فَأَصْبَحَ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٢٣﴾ فَبَعَثَ اللَّهُ غُرَابًا يَبْحَثُ فِي
 الْأَرْضِ لِيُرِيَهُ كَيْفَ يُورِي سَوْءَةَ أَخِيهِ ۗ قَالَ يَوَيْلَئِي أَعَجَزْتُ أَنْ أَكُونَ مِثْلَ هَذَا
 الْغُرَابِ فَأُورِي سَوْءَةَ أَخِي ۗ فَأَصْبَحَ مِنَ النَّادِمِينَ ﴿٢٤﴾

27. Na wasomee khabari za wana wawili wa Adam kwa kweli. Walipotoa mhanga, ukakubaliwa wa mmoja wao, na wa mwengine haukukubaliwa. Akasema: Nitakuuwa. Akasema mwengine: Mwenyezi Mungu Huwapokelea wachamngu.

28. Ukininyooshea mkono wako kuniua, mimi sitakunyooshea mkono wangu kukuua. Hakika mimi namuogopa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.

29. Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako, kwani wewe utakua miongoni mwa watu wa Motoni. Na hayo ndiyo malipo ya wenye kudhulumu.

30. Basi nafsi yake ikampelekea kumuua nduguye, akamuua na akawa miongoni mwa wenye kukhasirika.

31. Hapo Mwenyezi Mungu Akamleta kunguru anayefukua katika ardhi ili amuaneshe vipi kumsitiri nduguye. Akasema: Ole wangu! Nimeshindwa kuwa kama kunguru huyu nikamsitiri ndugu yangu? Basi akawa miongoni mwa wenye kujuta.

Kisa cha Habil (Abel) na Qabil (Cain):

Allah تعالى Anaelezea mwisho mbaya na matokeo ya kuchupa mipaka, wivu, na kutotenda haki kupitia kisa cha watoto wawili wa Adam عليه السلام, Habil na Qabil. Jinsi mmoja alivyopituka mipaka ya uadui na akamuua mwenzake kwa sababu ya wivu na husuda, kutokana na mali aliyopewa na Allah تعالى na kwa sababu ya kafara aliyotoa kwa Allah تعالى haikukubaliwa. Ndugu aliyeuawa alisamehewa dhambi zake na aliingizwa Peponi, ambapo muuaji alikhasirika katika maisha ya duniani na akhera. Allah تعالى Amesema,

وَأْتَلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ ابْنَيْ آدَمَ بِالْحَقِّ

“Na wasomee khabari za wana wawili wa Adam kwa kweli.”

Maana: Waambie hao wenye wivu, watu dhalimu, ndugu wa nguruwe na manyani, miongoni mwa Mayahudi na wanadamu wenye kufanana nao, kisa cha watoto wawili wa Adam عليه السلام, Habil na Qabil, kama ambavyo wanazuoni wengi miongoni mwa *Salaf* na vizazi vyao vya baadaye walivyosema. Kauli ya Allah تعالى,

بِالْحَقِّ

“Kwa kweli.” Ina maana, iliyo wazi pasi na utata au kubadilishwa, au kugeuzwa na kuongezwa au kufutwa. Allah تعالى Amesema katika Aya nyengine

إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْقَصَصُ الْحَقُّ

“Hakika haya ndiyo maelezo ya kweli.”

مَنْ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ

“Sisi Tunakusimulia khabari zao kwa kweli.” (18:13) na

ذَلِكَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ قَوْلَ الْحَقِّ

“Huyo ndiye Isa mwana wa Maryamu. Ndiyo kauli ya haki...” (19:34)

Wanazuoni wengi miongoni mwa *Salaf* na vizazi vilivyofuatia walisema kuwa Allah تعالى Alimruhusu Adam عليه السلام kuwaozesha binti zake kwa kaka zao kwa sababu ya haja ya kitendo hicho. Aidha walisema kuwa kwa kila mimba, Adam عليه السلام alipewa pacha, mvulana na msichana, na alikuwa akimuozesha msichana wa pacha moja kwa mvulana wa pacha nyingine. Dadake Habil hakuwa mzuri wa sura, ambapo dadake Qabil alikuwa mzuri wa sura, ikampelekea Qabil kumtaka yeye mwenyewe, badala ya kaka yake. Adam عليه السلام alikataa mpaka wote watakapotoa kafara, na yule ambaye kafara yake ingekubaliwa, atamuoa dadake Qabil. Kafara la Habil lilikubaliwa, ambapo la Qabil lilikataliwa, na hivyo lile tuliloambiwa na Allah تعالى lilitokea.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa katika zama za Adam عليه السلام, "Mwanamke hakuruhusiwa kuolewa na pacha wake wa kiume, lakini Adam عليه السلام aliamrisha kumuozesha kwa kaka wengine. Kwa kila mimba, Adam عليه السلام alipata pacha, mwanamume na mwanamke. Wakati mmoja alizaliwa binti mzuri na wakati mwingine sio mzuri. Hivyo kaka wa pacha wa msichana mwenye sura mbaya alisema, "Niozeshe dada yako nami nitakuozesha dada yangu." Akasema hapana, kwani nina haki zaidi kwa dada yangu. Hivyo wote walitoa kafara. Kafara la yule aliyetoa kondoo lilikubaliwa ambapo kafara la yule mwenziwe (pacha wa dada mzuri), ambalo lilikuwa na mazao, halikukubaliwa. Hivyo huyu wa pili alimua kaka yake. Kisa hiki kina isnadi bora.¹ Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ

"Mwenyezi Mungu Huwapokelea wachamungu."

Wanaomcha Allah تعالى kwa matendo – Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Abu Ad-Darda' رضي الله عنه alisema, "Kama ningekuwa na uhakika kuwa Allah تعالى Ameridhia Sala yangu moja, ingelikuwa bora kwangu kuliko maisha ya dunia na vyote vilivyomo. Kwa sababu Allah تعالى Anasema,

إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ

"Mwenyezi Mungu Huwapokelea wachamungu."

¹ At-Tabari 10:223.

لَيْنُ بَسَطَتْ إِلَيَّ يَدَكَ لِتَقْتُلَنِي مَا أَنَا بِبَاسِطٍ يَدِيَ إِلَيْكَ لِأَقْتُلَكَ ۗ إِنَّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ
 الْعَالَمِينَ ﴿٢٠﴾

“Ukininyooshea mkono wako kuniua, mimi sitakunyooshea mkono wangu kukuua. Hakika mimi namuogopa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.”

Kaka yake Qabil, mtu mchamungu ambaye kafara lake lilikubaliwa kwa sababu ya uchamungu wake, alimuambia kaka yake, aliyemtishia kumuua bila uhalali wowote.

لَيْنُ بَسَطَتْ إِلَيَّ يَدَكَ لِتَقْتُلَنِي مَا أَنَا بِبَاسِطٍ يَدِيَ إِلَيْكَ لِأَقْتُلَكَ ۗ

“Ukininyooshea mkono wako kuniua, mimi sitakunyooshea mkono wangu kukuua.”

Sitotenda uovu unaotishia kuufanya, ili nisije nikapata dhambi kama wewe,

إِنَّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ

“Mimi namuogopa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.”

Na kwa sababu hiyo, sitofanya kosa ulilolitishia kulifanya. Bali nitasubiri na kuvumilia.

Abdullah bin Amr alisema, “Wallah! Habil alikuwa na nguvu zaidi ya mwenzake. Lakini uchaji Mungu wake ulizuia mkono wake.” Mtume ﷺ alisema katika Hadithi iliyonukuliwa ndani ya Sahih Mbili,

«إِذَا تَرَاخَا الْمُسْلِمَانِ بَيْنَهُمَا فَالْقَاتِلُ وَالْمَقْتُولُ فِي النَّارِ»

“Watakapokabiliana Waislamu na kila mmoja akiwa na upanga, wote muuaji na muuliwa watatupwa Motoni.”

Walisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Ni sahihi kwa muuaji, lakini vipi aliyeuawa?” Mtume ﷺ alijibu,

«إِنَّهُ كَانَ حَرِيصًا عَلَى قَتْلِ صَاحِبِهِ»

“Kwa hakika alikuwa na nia ya kumuua nduguye.”¹

¹ Fat’hul Al-Bari 13:35, Muslim 4:2214.

Imam Ahmad alinukuu kuwa, Sa'ad bin Abi Waqqasi رضي الله عنه alisema mwanzoni mwa maafa yaliyomsibu Uthman رضي الله عنه, "Nashuhudia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّهَا سَتَكُونُ فِتْنَةً الْقَاعِدُ فِيهَا خَيْرٌ مِنَ الْقَائِمِ، وَالْقَائِمُ خَيْرٌ مِنَ الْمَاشِي، وَالْمَاشِي خَيْرٌ مِنَ السَّاعِي»

"Itakuwepo fitna, na atakayekaa kitako ni bora kuliko atakayesimama, na atakayesimama ni bora kuliko atakayetembea, na atakayekuwa anatembea ni bora kuliko atakayekuwa anakimbia."

Alipoulizwa, 'Itakuwaje iwapo mtu atakapoingia nyumbani kwangu na akaingiza mkono kutaka kuniua?' Akajibu,

«كُنْ كَابْنِ آدَمَ»

*"Kuwa kama mtoto (mchamungu) wa Adam."*¹

At-Tirmidhi pia ilinukuu hivi, na akasema, "Hadithi hii ni Hasan, na sawa na hiyo iliripotiwa juu ya somo hili kutoka kwa Abu Hurayrah, Khabab bin Al-Arat, Abubakar, Ibn Mas'ud, Abu Waqid na Abu Musa رضي الله عنهم."²

Qur'an inaendelea,

إِنِّي أُرِيدُ أَنْ تَبُوءَ بِإِثْمِي وَإِثْمِكَ فَتَكُونَ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ ۗ وَذَلِكَ جَزَاءُ الظَّالِمِينَ ﴿٥٦﴾

"Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako, kwani wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni. Na hayo ndiyo malipo ya wenye kudhulumu. "

Ibn 'Abbas, Mujahid, Adh-Dhahhak, As-Suddi na Qatadah رضي الله عنهم waliyasema hayo.

إِنِّي أُرِيدُ أَنْ تَبُوءَ بِإِثْمِي وَإِثْمِكَ

"Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako,..."

¹ Ahmad 1:85.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:436.

Maana yake, dhambi ya kuniua mimi, ni ziada ya madhambi ya awali, Ibn Jarir رحمته الله تعالى aliiandika hii.¹ Kauli ya Allah تعالى,

فَطَوَّعَتْ لَهُ نَفْسُهُ قَتْلَ أَخِيهِ فَقَتَلَهُ فَأَصْبَحَ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٢٠﴾

“Basi nafsi yake ikampelekea kumuua nduguye, akamuua na akawa miongoni mwa wenye kukhasirika.”

Maana: Dhamira yake ilimsukuma kumuua nduguye kwa kulifanya lionekane kama jambo la maana kufanywa, hivyo akamuua, hata pale kaka, yake alipomrudi. Ibn Jarir رحمته الله تعالى alisema, “Alipotaka kumuua kaka yake alianza kumsongea shingo yake. Hivyo shetani alimchukua mnyama na akaweka kichwa chake juu ya jiwe, kisha akachukua jiwe jengine, na akakipiga kichwa chake mpaka akamuua na mtoto wa Adam عليه السلام alikuwa akitazama. Hivyo akamfanyia kaka yake vivyo hivyo.² Ibn Abi Hatim رحمته الله تعالى pia aliirekodi hadithi hii. Abdullah bin Wahb alisema kuwa Abdur – Rahman bin Zayd bin Aslam alisema kuwa baba yake alisema, “Qabil alimshika kichwa Habil ili amuue, hivyo Habil alilala chini na Qabil akaanza kumsongoa kichwa chake, bila kujua jinsi ya kumuua. Shetani alimjia Qabil na kumuuliza, ‘Unataka kumuua?’ Akajibu, ‘Ndiyo!’ Shetani akamuambia, “chukua jiwe lile na umpige nalo kichwani.’ Hivyo Qabil akachukua jiwe na akampiga nalo kaka yake kichwani. Kisha shetani akaenda mbio kwa Bi. Hawwa na akamuambia, ‘Ewe Hawwa! Qabil amemuua Habil!’ Akamuuliza, “Huzuni kubwa! kua maana yake nini?’ Akasema, “Hatokula tena, kunywa au kutikisika.’ Akasema, ‘Na hicho ndio kifo?’ Akajibu “Ndio chenyewe.’ Hivyo akaanza kulia mpaka Adam عليه السلام alipokuja akiwa analia na akasema, “Una jambo gani lililokusibu?’ Hakujiibu. Akamuuliza mara mbili, lakini hakujiibu. Hivyo akamuambia, ‘Wewe na mabinti zako mtarithi tabia ya kulia, ambapo mimi na watoto wangu wa kiume tutakuwa mbali na tabia hiyo.” Ibn Abi Hatim رحمته الله تعالى alinukuu maelezo hayo.

فَأَصْبَحَ مِنَ الْخَاسِرِينَ

“...na akawa miongoni mwa wenye kukhasirika.”

Duniani na akhera na hasara gani iliyo kubwa kuliko hii? Imam Ahmad amenukuu kuwa Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ At-Tabari 10:215-216.

² At-Tabari 4:536.

«لَا تُقْتَلُ نَفْسٌ ظُلْمًا إِلَّا كَانَتْ عَلَى ابْنِ آدَمَ الْأَوَّلِ كَيْفَلٌ مِنْ ذِمَّتِهَا، لِأَنَّهُ كَانَ أَوَّلَ مَنْ
سَنَّ الْقَتْلَ»

“Kwa Roho yeyote itakayotolewa kinyume cha sheria, isipokuwa mwana wa Adam atabeba mzigo wa kumwaga damu, kwani alikuwa wa kwanza kutenda kosa la kuua.”¹

Kundi ukimtoa Abu Dawud waliirekodi Hadithi hii.² Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliandika kuwa Abdullah bin Amr alikuwa akisema, “Mwana wa Adam aliyemuua nduguye ni muovu zaidi ya watu. Hapana umwagaji damu utakaotokea mpaka siku ya Kufufuliwa, ila atabeba mzigo huo, kwa kuwa alikuwa mtu wa kwanza kuua.”³

Allah تعالى Amesema:

فَبَعَثَ اللَّهُ غُرَابًا يَبْحَثُ فِي الْأَرْضِ لِيُرِيَهُ كَيْفَ يُورِي سَوْءَةَ أَخِيهِ ۗ قَالَ يَتُولَتِي
أَعْجَزْتُ أَنْ أَكُونَ مِثْلَ هَذَا الْغُرَابِ فَأُوْرِي سَوْءَةَ أَخِي ۗ فَأَصْبَحَ مِنَ النَّادِمِينَ ﴿٦٠﴾

“Hapo Mwenyezi Mungu Akamleta kunguru anayefukua katika ardhi ili amuoneshe vipi namna ya kumsitiri nduguye. Akasema: Ole wangu! Nimeshindwa kuwa kama kunguru huyu nikamsitiri ndugu yangu? Basi akawa miongoni mwa wenye kujuta.”

As-Sudi alisema kuwa Masahaba walisema, “Kaka yake alipokufa, Qabil alimuacha juu ya ardhi na hakujua namna ya kumzika. Allah تعالى Aliwatuma kunguru wawili, ambao walipigana mpaka mmoja wao akauawa. Hivyo akachimba shimo na akarusha mchanga juu ya maiti aliyemtia ndani ya shimo.” Qabil alipoona vile alisema:

يَتُولَتِي ۗ أَعْجَزْتُ أَنْ أَكُونَ مِثْلَ هَذَا الْغُرَابِ فَأُوْرِي سَوْءَةَ أَخِي ۗ

“Ole wangu! Nimeshindwa kuwa kama kunguru huyu nikamsitiri ndugu yangu?”⁴

¹ Ahmad 1:383.

² Fat'hul Al-Bari 12:198, Muslim 3:1303, Tuhfat Al-Ahwadhi 7:436, An-Nasai katika Al-Kubra 6:334, Ibn Majah 2:873.

³ At-Tabari 10:219.

⁴ At-Tabari 10:225.

Ali bin Abi Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kunguru alikuja kwa maiti ya kunguru mwingine na akamrushia udongo mpaka akafukiwa na ardhi.” Yule aliyemuua kaka yake akasema¹,

يَوَيْلَتِي أَعَجَزْتُ أَنْ أَكُونَ مِثْلَ هَذَا الْغُرَابِ فَأَوْرِي سَوْءَةَ أَخِي^ط

“Ole wangu! Nimeshindwa kuwa kama kunguru huyu nikamsitiri ndugu yangu?”²

Al-Hasan Al-Basri رحمته الله تعالى aliyatolea melezo maneno hayo,

فَأَصْبَحَ مِنَ النَّدِيمِ

“Basi akawa miongoni mwa wenye kujuta.”

Allah تعالى Amemfanya awe na majuto baada ya kuona hasara aliyoipata.

Adhabu Kali kwa Wanaochupa Mipaka na Kukataa Udugu wa Kuzaliwa:

Hadithi inasema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا مِنْ ذَنْبٍ أَجْدَرُ أَنْ يُعَجَلَ اللَّهُ عُقُوبَتَهُ فِي الدُّنْيَا مَعَ مَا يَدَّخِرُ لِصَاحِبِهِ فِي الْآخِرَةِ
مِنَ الْبُغْيِ وَقَطِيعَةِ الرَّحِمِ»

“Hapana dhambi inayostahili kuharakishiwa adhabu kali na Allah hapa duniani, ikiwa ni nyongeza ya ile Aliyoiweka kwa wahalifu kesho kiyama, kuliko dhambi ya kuchupa mipaka katika uovu na kukata udugu wa kuzaliwa.”²

Kitendo cha Qabil kilijumuisha yote haya. Sisi ni wa Allah تعالى na Kwake tutarejea.



¹ At-Tabari 10:226.

² Abu Dawud 5:208.

مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ كَتَبْنَا عَلَى بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُمْ مَنْ قَتَلَ
 نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ
 النَّاسَ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا
 وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِنْهُمْ بَعَدَ
 ذَلِكَ فِي الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ ﴿٣٢﴾ إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ
 يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَنْ
 يُقْتَلُوا أَوْ يُصَلَّبُوا أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِنْ خَلْفٍ أَوْ
 يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ ذَلِكَ لَهُمْ جِزَاءٌ فِي الدُّنْيَا وَلَهُمْ
 فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٣٣﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ قَبْلِ
 أَنْ تَقْدِرُوا عَلَيْهِمْ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣٤﴾

32. Kwa sababu ya hayo Tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliyemuua mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote. Na hakika waliwajia Mitume Wetu na hoja zilizowazi. Kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi.

33. Basi malipo ya wale wanaompiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na

wakawania kufanya uchafuzi katika nchi, ni kuuwawa, au kusulubiwa, au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kutolewa nchi. Hii ndiyo hizaya yao katika dunia; na katika Akhera watapata adhabu kubwa.

مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ كَتَبْنَا عَلَى بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُمْ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ
 نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا
 وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا وَلَقَدْ
 جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِنْهُمْ بَعَدَ
 ذَلِكَ فِي الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ ﴿٣٢﴾ إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ
 يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَنْ
 يُقْتَلُوا أَوْ يُصَلَّبُوا أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِنْ
 خَلْفٍ أَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ ذَلِكَ لَهُمْ جِزَاءٌ فِي الدُّنْيَا
 وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٣٣﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ قَبْلِ
 أَنْ تَقْدِرُوا عَلَيْهِمْ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ

رَحِيمٌ ﴿٣٤﴾

34 . Isipokuwa wale waliotubu kabla hamjawatia nguvuni. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghufira na Mwenye Kurehemu.

Binadamu ni Wajibu Kuheshimu Utukufu wa Binadamu Wenzao:

Allah تعالى Anasema, kwa sababu mtoto wa Adam عليه السلام alimuua kaka yake kwa kuchupa mipaka na ugomvi,

كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ

“...Tuliwaandikia Wana wa Israili...”

Maana yake, Tuliwawekea sheria na kuwafahamisha,

أَنَّهُمْ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا

“...ya kwamba aliyemuua mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote.”

Aya inaeleza, anayeua nafsi bila uhalali – kama vile kulipizia uuaji au kwa kusababisha ufisadi juu ya ardhi – itakuwa kama amewaua binadamu wote, kwa sababu hapana tofauti kati ya maisha ya mtu mmoja na mwingine.

وَمَنْ أَحْيَاهَا

“Na mwenye kumuokoa mtu na mauti...”

Kwa kuzuia damu yake isimwagike na kuamini juu ya utukufu wake, hakika watu wote wamesalimika naye,

فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا

“Kama amewaokoa watu wote.”

Al-A'Mashi na wengineo walisema kuwa Abu Salih, alisema kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Niliingia kwa Uthman رضي الله عنه alipokuwa amezingirwa katika nyumba yake na nikamuambia, “Nimekuja kukusaidia sasa inafaa kupigana (kukuhami). Ewe kiongozi wa Waumini!’ Akasema, “Ewe Abu Hurayrah! Inakupendeza kuuwa watu wote pamoja na mimi.’ Nikasema,

'Hapana.' Akasema, 'Ukiua mtu mmoja, ni kama umeua watu wote. Hivyo nakuomba urejee kwa ruhusa yangu bila ya kubeba dhambi.' Hivyo nilirejea na sikupigana." Ali bin Abi Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Na kama alivyosema Allah تعالى,

مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا
فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا

"...aliyemuwa mtu bila ya yeye kuua, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote."

Na kuiokoa nafsi ni kuacha kuua nafsi aliyoiharamisha Allah تعالى, isipokuwa kwa haki ya kisharia. Hii ndio maana ya kuokoa maisha ya binadamu wote, kwani, yeyote anayezuia kuua nafsi bila uhalali, maisha ya watu wote yatasalimika kutoka kwake."¹

Sawa na hiyo ilinenwa na Mujahid,

وَمَنْ أَحْيَاهَا

"Na mwenye kumuokoa mtu..." Maana: Anajizuia kuua nafsi.²

Al-Awfi aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا

"Kama amewauwa watu wote."

Muradi wake ni kuwa, "Yeyote anayeuua nafsi ambayo kwayo Allah تعالى Ameiharamisha, ni sawa na yule auaye binadamu wote."³ Said bin Jubayr alisema: "Yeyote anayeruhusu kumwaga damu ya Muislamu, ni kama yule anayeruhusu kumwagwa damu ya watu wote. Yeyote anayezuia kumwagwa damu ya Muislamu mmoja, ni sawa na azuiaye kumwagwa kwa damu ya watu wote." Kwa ziada, Ibn Jurayj alisema kuwa Al-Araj alisema kuwa Mujahid aliitolea maelezo Aya hii,

¹ At-Tabari 10:235.

² At-Tabari 10:236.

³ At-Tabari 10:233.

فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا

“...ni kama amewaua watu wote.”

Yeyote anayeua nafsi kwa kudhamiria, Allah تعالى Huufanya Moto wa Jahanam kuwa makazi yake, Atamghadhikikia na Atamlaani, na Amemuandalia adhabu kali, sawa na kama aliua watu wote, adhabu yake itakuwa ile ile.”

Ibn Jurayj alisema kuwa Mujahid alisema kuwa Aya,

وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا

“Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote.”

Maana: “Yule asiyemuua yeyote, basi maisha ya watu yamesalimika naye.”¹

Maonyo kwa Wafanyao Uharibifu:

Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَاتِ

“Na hakika waliwajia Mitume wetu na hoja zilizowazi.”

Maana: Ushahidi ulio wazi, dalili na uthibitisho,

ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ بَعْدَ ذَلِكَ فِي الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ

“Kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi.”

Aya hii inawakemea na kuwakosoa wanaofanya yaliyokatazwa, baada ya kujua kuwa yameharamishwa kuyafanya. Mayahudi wa Al-Madinah kama vile Banu Quraydha, An-Nadhir na Qaynuqa walikuwa wakipigana bega kwa bega na ima Khazraj au Aws, vita ilipotokea kati yao zama za Jahiliyyah. Vita hivyo vilipokwisha, Mayahudi huwafidia wale waliotekwa na kulipia dia kwa wale waliouawa. Allah تعالى Anawasema kwa tabia hii katika Surat Al-Baqarah.

¹ At-Tabari 10:235.

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ لَا تَسْفِكُونَ دِمَاءَكُمْ وَلَا تَخْرِجُونَ أَنْفُسَكُمْ مِنْ دِينِكُمْ ثُمَّ أَقْرَرْتُمْ
 وَأَنْتُمْ تَشْهَدُونَ ﴿٣٢﴾ ثُمَّ أَنْتُمْ هَتُّوْا لَهُ تَقْتُلُونَ أَنْفُسَكُمْ وَتَخْرِجُونَ فَرِيقًا مِنْكُمْ مِنْ
 دِينِهِمْ تَنْظَهُرُونَ عَلَيْهِمْ بِالْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَإِنْ يَأْتُوكُمْ أُسْرَى تَفْذَرُوهُمْ وَهُوَ مُحْرَمٌ
 عَلَيْكُمْ إِخْرَاجُهُمْ أَفْتُونُونَ بَعْضُ الْكُتُبِ وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضٍ فَمَا جَزَاءُ مَنْ يَفْعَلُ
 ذَلِكَ مِنْكُمْ إِلَّا خِزْيٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يُرَدُّونَ إِلَىٰ أَشَدِّ الْعَذَابِ وَمَا
 اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٣٤﴾

“Na Tulipochukua agano lenu kuwa hamtamwaga damu zenu, wala hamtatoana majumbani mwenu; nanyi mkakubali nanyi mnashuhudia. Kisha nyinyi kwa nyinyi mnauwana, na mnawatoa baadhi yenu majumbani kwao, mkisaidiana kwa dhambi na uadui. Na wakikujieni mateka mnawakomboa, na hali kuwatoa mmekatazwa. Je! Mnaamini baadhi ya Kitabu na mnakataa baadhi yake? Basi hana malipo mwenye kutenda hayo miongoni mwenu ila hizaya katika maisha ya duniani, na Siku ya Kiyama watapelekwa kwenye adhabu kali kabisa. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda.” (2:84-85)

Adhabu ya Wasababishao Uharibifu Juu ya Ardhi:

Baadaye Allah تعالى Amesema,

إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَنْ يُقَتَّلُوا أَوْ يُصَلَّبُوا
 أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِنْ خَلْفِهِمْ أَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ ۗ

“Basi malipo ya wale wanaompiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawania kufanya uchafuzi katika nchi, ni kuuwawa, au kusulubiwa, au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kutolewa nchi.”

“Upigaji vita unaokusudiwa katika aya hii, ni kwenda kinyume na kupinga jambo, na hili linasadifiana na ukafiri, uporaji na uhalifu katika njia. Kadhalika ufisadi katika Ardhi hujumuisha aina mbalimbali za maovu. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ikrimah na Al-Hasan Al-Basri walisema kuwa Aya hizi,

إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“Basi malipo ya wale wanaompiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake...” mpaka,

أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira na Mwenye Kurehemu.”

Iliteremshwa kuhusu washirikina. Hivyo, Aya inaamuru kuwa atakayetubia kabla hujamkamata, basi huna haki ya kumuadhibu. Aya hii haimuondoi Muislamu na adhabu iwapo ataua, atasababisha uharibifu juu ya ardhi au kupambana dhidi ya Allah تعالى na Mjumbe wake na kisha akajiunga na makafiri, kabla ya Waislamu hawajamkamata. Bado atastahili adhabu kwa makosa aliyoyafanya.”¹

Abu Dawood na An-Nasai walirekodi kutoka kwa Ikrimah kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya hii,

إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا

“Basi malipo ya wale wanaompiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawania kufanya uchafuzi katika nchi...”

Iliteremshwa kuhusu washirikina, wale miongoni mwao kabla hawajakamatwa, watakuwa bado wanastahili adhabu kwa makosa waliyoyatenda”²

Rai sahihi ni kuwa Ayah hii, ina maana ya jumla na inawajumuisha washirikina wote na wale wote wanaofanya uhalifu uliotajwa katika Ayah. Bukhari na Muslim walirekodi kuwa Abu Qilabah, jina lake ni Abdullah bin Zayd Al-Jirmi Al-Basri, alisema kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, “Watu wanane kutoka kabila la Ukl walikuja kwa Mtume ﷺ na wakampa ahadi ya kufuata Uislamu. Hali ya hewa ya Madina haikuwafaa wakaugua na wakamlalamikia Mtume ﷺ. Hivyo akawaambia,

¹ At-Tabari 10:244.

² Abu Dawud 4:536, An-Nasa 7:101.

«أَلَا تَخْرُجُونَ مَعَ رَاعِيِنَا فِي إِيْلِهِ، فَتُصِيبُوا مِنْ أَبْوَالِهَا وَأَلْبَانِهَا»

“Nendeni na wachungaji wetu ili mtibiwe kwa maziwa na mkojo wa ngamia.”

Hivyo walikwenda kama walivyoelekezwa, na baada ya kunywa maziwa na mkojo wa ngamia walipona, na wakamuua mchungaji na wakawaiwa wale ngamia wakaondoka nao. Habari zilimfikia Mtume ﷺ na aliwatuma wanaume wawafuate wale watu na wakawakamata. Aliamrisha mikono na miguu yao ikatwe (na ilifanyika hivyo), na macho yao yalitiwa alama kwa chuma cha moto. Baada ya hapo walianikwa juani mpaka wakafa.” Hadithi hii ni kwa mujibu wa Muslim. Katika masimulizi mengine ya Hadithi hii, ilitajwa kuwa watu hao ni wa kabila la Ukl au Uraynah. Simulizi nyingine iliripotiwa kuwa watu hao waliwekwa eneo la Hurrah (Madinah), na walipoomba maji hawakupewa.¹

Allah تعالى Amesema,

أَنْ يُقْتَلُوا أَوْ يُصَلَّبُوا أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِنْ خَلْفٍ أَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ^٢

“Kuuwawa, au kusulubiwa, au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kutolewa nchi.”

Ali bin Abi Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alizungumzia Aya hii, “Yeyote anayechukua silaha katika ardhi ya Waislamu na akaeneza woga katika njia za kuingilia mjini na akakamatwa, Kiongozi wa Waislamu ana hiari kuamrisha auawe, asulubiwe au akatwe mikono na miguu.”²

Vivyo hivyo alinena Said bin Al-Musayyib, Mujahid, Ata, Al-Hasan Al-Basri, Ibrahim An-Nakhai na Adh-Dhahhak, kama alivyorekodi Abu Jafar Ibn Jarir رحمه الله تعالى.³

Rai hii inaungwa mkono kwa kuwa neno Aw (au) linaonesha hiari (uchaguzi) kama Allah تعالى Alivyosema,

¹ Fat’hul Al-Bari 12:114, Muslim 3:1296.

² At-Tabari 10:263.

³ At-Tabari 10:262-263.

فَجَزَاءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعْمِ مُحْكَمٌ بِهِ ذَوْا عَدَلٍ مِّنكُمْ هَدِيًّا بَلِغَ الْكَعْبَةِ أَوْ كَفَرَةٌ
طَعَامٌ مَّسْكِينٍ أَوْ عَدْلٌ ذَٰلِكَ صِيَامًا

“...basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilicho sawa na alichokiua, katika mifugo, kama wanavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu. Mnyama huyo apelekwe kwenye Al Kaaba, au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini; au badala ya hayo ni kufunga,...” (5:95)

Allah تعالى Amesema,

فَمَنْ كَانَ مِنكُمْ مَّرِيضًا أَوْ بِهِ أَذًى مِّن رَّأْسِهِ فَفِدْيَةٌ مِّن صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٌ أَوْ ذُكْوٰٓءٌ

“Na atakayekuwa mgonjwa au ana vya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidiya kwa kufunga au kwa kutoa sadaka au kuchinja wanyama.”

فَكَفَّرْتُمُوهُ إِطْعَامٌ عَشْرَةَ مَسْكِينٍ مِّنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعَمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْوَتُهُمْ
أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ

“Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnachowalisha ahali wenu, au kuwavisha, au kumkomboa mtumwa.”

Aya zote hizo zimeruhusu kuchagua, kama ilivyo Aya hapo juu. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

أَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ

“...au kutolewa nchi...” Baadhi yao wamesema kuwa atafutwe mpaka akamatwe na kisha kupewa adhabu stahiki, au vinginevyo afukuzwe kutoka ardhi ya Waislamu. Kauli hii wameisema Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, Anas bin Malik, Said bin Jubayr, Adh-Dhahhak, Ar-Rabi bin Anas, Az-Zuhr, Al-Layth bin Sa'd na Malik bin Anas رضي الله عنهم. Vilevile badhi yao wamesema kuwa Ayah ina maana watu hawa watahamishiwa ardhi nyingine, au kwenye taifa jingine la Waislamu.¹

¹ At-Tabari 10:268-270.

Said bin Jubayr, Abu Ash-Shatha, Al-Hasan, Az-Zubayr, Adh-Dhahhak na Muqatil bin Hayyan walisema kuwa atapotezwa, lakini siyo nje ya ardhi ya Waislamu, wengine wanasema anatakiwa afungwe jela.

Kauli ya Allah تعالى،

ذَلِكَ لَهُمْ خِزْيٌ فِي الدُّنْيَا وَلَهُمْ فِي الآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ

“Hii ndiyo hizaya yao katika dunia; na katika Akhera watapata adhabu kubwa.”

Maana: Adhabu Tuliyoandika, kwa hawa wavamizi, kuwasulubu, kuwakata mikono na miguu inayokabiliana, na kuwafukuza katika nchi ni fedheha kwao miongoni mwa binadamu hapa duniani, pamoja na adhabu kali ya Allah تعالى Aliyowaandalia siku ya kiyama. Rai hii inakubaliana na rai ya Aya hizi zilizoteremshwa kwa ajili ya washirikina. Ama kwa Waislamu, Muslim katika Sahihi yake alirekodi kuwa Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alichukua ahadi kutoka kwetu na pia kutoka kwa wanawake: Kuwa hatumshirikishi Allah تعالى na chochote katika ibada, hatuibi, hatuzini, na hatuwai watoto wetu, na kuwa hatuenezi uzushi juu yetu wenyewe.” Alisema kwamba, ‘Yule anayetimiza ahadi, atalipwa na Allah تعالى. Yule anayekosea na kuadhibiwa hiyo itakuwa fidia kwake. Na wale ambao makosa yao yalihifadhiwa na Allah تعالى, basi mambo yao ni kwa Allah تعالى. Kama Ataridhia, Atawaadhibu na Akipenda, Atawasamehe.”¹

Ali رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ أَدْنَبَ ذَنْبًا فِي الدُّنْيَا فَعُوقِبَ بِهِ، فَاللهُ أَغْدَلُ مِنْ أَنْ يُنْتَبَى عُقُوبَتُهُ عَلَى عِبْدِهِ، وَمَنْ أَدْنَبَ ذَنْبًا فِي الدُّنْيَا فَسْتَرَهُ اللهُ عَلَيْهِ وَعَفَا عَنْهُ، فَاللهُ أَكْرَمُ مِنْ أَنْ يَعودَ عَلَيْهِ فِي شَيْءٍ قَدْ عَفَا عَنْهُ»

“Yeyote atakayefanya dhambi hapa duniani na akaadhibiwa kwa hilo, basi Allah ni Muadilifu zaidi kuchanganya adhabu mbili kwa mja wake. Yeyote anayefanya kosa hapa duniani na Allah Akamsitiri kosa lake na Akamsemehe; hivyo Allah ni Mkarimu sana kiasi cha Kutomuadhibu mja kwa jambo ambalo Ameshamsamehe.”

¹ Muslim 3:1333.

Imenukuliwa na Ahmad, Ibn Majah na At-Tirmidh ambaye alisema ni "Hasan Gharib."¹ Al-Hafiz Ad-Daraqutni رحمه الله تعالى aliulizwa juu ya Hadithi hii, na akasema kuwa ilipokelewa kutoka kwa Mtume ﷺ katika baadhi ya masimulizi, na ilisimuliwa na baadhi ya Masahaba katika Hadithi nyingine, kutoka kwa Mtume ﷺ ni sahihi.²

ذَلِكَ لَهُمْ خِزْيٌ فِي الدُّنْيَا

"Hii ndiyo hizaya yao katika dunia;"

Maana yake: Aibu, idhilali, adhabu, twezo na mateso hapa duniani kabla ya Kiyama.

وَلَهُمْ فِي الآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ

"Na katika Akhera watapata adhabu kubwa."

Ikiwa hawatatubu madhambi haya hadi kifo kiwakute. Katika hali hii, AKhera watastahili adhabu, licha ya adhabu na mateso ambayo Nimewapa duniani,

عَذَابٌ عَظِيمٌ

"Adhabu kubwa." "Katika moto wa Jahanamu."³

Adhabu ya Wale Wanaompiga vita Allah تعالى na Mjumbe Wake Inafutwa Wakitubu kabla ya Kuwatia nguvuni:

Allah تعالى Amesema,

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِن قَبْلِ أَن تَقْدِرُوا عَلَيْهِمْ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٥٠﴾

"Isipokuwa wale waliotubu kabla hamjawatia nguvuni. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira na Mwenye Kurehemu."

Aya hii iko wazi katika kuashiria kuwa inawahusu washirikina. Kwa Waislamu wanaofanya makosa ya jinai na wakatubu kabla ya kutiwa mbaroni, adhabu ya kuuawa, kusulubiwa na kukatwa mikono itafutwa. Mwenendo wa Masahaba katika suala hili ni kuwa Waislamu na washirikina katika kadhia hii wakileta toba watasamehewa, kama ilivyo wazi katika maneno ya Ayah.

¹ Ahmad 1:159, Tuhfat Al-Ahwadhi 7:377, Ibn Majah2:868.

² Ad-Daraqutni 3:215.

³ At-Tabari 10:276.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alirekodi kuwa Ash-Shabi alisema, “Harithal bin Badri At-Tamini alikuwa akiishi Al-Basrah, na alifanya kosa la uharibifu katika ardhi. Hivyo alizungumza na baadhi ya wanaume wa Kiquraish, kama vile Al-Hasan bin Ali, Ibn Abbas na Abdullah bin Ja’far رضي الله عنهم, na walizungumza na Ali رضي الله عنه kumhusu yeye ili aweze kumpa hifadhi, lakini Ali رضي الله عنه alikataa.

Hivyo Harithah alikwenda kwa Said bin Qays Al-Hamadani ambaye alimuacha nyumbani kwake na akaenda kwa Ali رضي الله عنه huku akisema, “Ewe kiongozi wa Waumini! Unasemaje juu ya wale wanaompiga vita Allah تعالى na Mjumbe Wake na wakafanya uharibifu duniani?” Hivyo alisoma Aya hii mpaka alipofikia,

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِن قَبْلِ أَن تَقْدِرُوا عَلَيْهِمْ

“Isipokuwa wale waliotubu kabla hamjawatia nguvuni.” Akasema: Hivyo basi Ali رضي الله عنه aliandika waraka uliohakikisha usalama, na Said bin Qays alisema, ‘Hii ni kwa ajili ya Harithah bin Badr.’ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alirekodi Hadithi hii.¹

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alirekodi kuwa Amir Ash-Sha’bi alisema, “Mtu kutoka Murad alikuja kwa Abu Musa, alipokuwa gavana wa Kufah wakati wa utawala wa Uthman رضي الله عنه na alimuambia baada ya kusali faradhi, ‘Ewe Abu Mussa! Naomba msaada wako. Mimi ni fulani bin fulani kutoka Murad na nilifanya vita dhidi ya Allah تعالى na Mjumbe wake ﷺ na nikasababisha uharibifu juu ya ardhi. Niliomba toba kabla hujawa na mamlaka juu yangu.” Abu Musa alitangaza, “Huyu ni fulani bin fulani alipigana vita dhidi ya Allah تعالى na Mjumbe Wake na akasababisha uharibifu juu ya ardhi, na alitubia kabla hatujawa na mamlaka juu yake. Kwa hiyo, yeyote atakayekutana naye, aamiliane naye vizuri. Kama anasema kweli, basi hii ndio njia ya wasemao ukweli. Iwapo anaongopa, dhambi zake zitamuangamiza.” Hivyo mtu yule alitulia kwa muda kama Allah تعالى Alivyotaka, lakini baadaye alifanya matata kwa viongozi na Allah تعالى Alimuadhibu kwa makosa yake na aliuawa.” Ibn Jarir رحمه الله تعالى alirekodi kuwa Musa bin Is-haq Al-Madani alisema kuwa Ali Al-Asadi alianzisha vita, akaweka vizuizi barabarani, akaogopesha njia na akamwaga damu na kuharibu mali. Viongozi na watu sawia walitaka kumkamata, lakini hawakuweza kufanya hivyo mpaka alipokuja baada ya kuomba toba, baada ya kumsikia mtu akisoma Aya,

¹ At-Tabari 10:280.

يَعْبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ
 جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٣٩﴾

“Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”(39:53)

Hivyo akamuambia mtu yule, “Ewe mja wa Allah! Soma tena.” Akasoma tena, na Ali al-Asadi aliweka chini upanga wake na alikwenda Madinah kutubia, aliwasili usiku. Alikoga na akaenda Masjid ya Mtume ﷺ na alisali Alfajiri. Alikaa karibu na Abu Hurayra رضي الله عنه kati ya wafuasi wake. Asubuhi, watu walimtambua na wakamfuata. Akasema, “Hamna njia dhidi yangu, nimekuja kuomba toba kabla hamjawa na mamlaka juu yangu.” Abu Hurayra رضي الله عنه alisema, “Amesema ukweli, na alimshika mkono na akaenda naye kwa Marwan bin Al-Hakam, aliyekuwa gavana wa Madinah wakati wa utawala wa Muawiyah رضي الله عنه. Abu Hurayra رضي الله عنه alisema, “Huyu ni Ali na amekuja kutubia nyinyi hamna njia ya Allah تعالى dhidi yake, wala hamuwezi kumuua.” Hivyo Ali al-Asadi alifutiwa adhabu, akaleta toba na akaenda baharini kupigana Jihad katika Njia ya Allah تعالى. Waislamu walikabiliana na Warumi katika vita, na Waislamu walileta mali, Ali alikuwemo katika moja ya meli za Warumi na Ali alikatisha kwenye meli hiyo na Warumi walimtoroka kwa upande wa pili wa meli, na meli ilipinduka na wote walizama.”

* * *

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَابْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ
 وَجَاهِدُوا فِي سَبِيلِهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣٥﴾ إِنَّ الَّذِينَ
 كَفَرُوا لَوَ أَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ
 لَيَفْتَنُوا بِهِ مِنْ عَذَابِ يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَا تُقْبَلُ مِنْهُمْ
 وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٣٦﴾ يُرِيدُونَ أَنْ يُخْرِجُوا مِنَ النَّارِ
 وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنْهَا ۗ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٣٧﴾
 وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا جَزَاءً بِمَا كَسَبَا
 نَكَالًا مِّنْ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٣٨﴾ فَمَنْ تَابَ مِنْ بَعْدِ
 ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللَّهَ يَتُوبُ عَلَيْهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ
 رَّحِيمٌ ﴿٣٩﴾ أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ يُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ وَيَغْفِرُ لِمَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ
 كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٠﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ
 وَابْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ وَجَاهِدُوا فِي
 سَبِيلِهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣٥﴾
 إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوَ أَنَّ لَهُمْ مَا
 فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ
 لَيَفْتَنُوا بِهِ مِنْ عَذَابِ يَوْمِ
 الْقِيَامَةِ مَا تُقْبَلُ مِنْهُمْ وَهُمْ عَذَابٌ
 أَلِيمٌ ﴿٣٦﴾ يُرِيدُونَ أَنْ يُخْرِجُوا
 مِنَ النَّارِ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنْهَا ۗ
 وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٣٧﴾

35. Enyi mlioamini! Mcheni
 Mwenyezi Mungu, na
 tafuteni njia ya kumfikia.
 Na piganeni Jihadi kwa ajili
 Yake ili mpate kuokoka.

36. Hakika waliokufuru lau wangukuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya Siku ya Kiyama, yasingelipokelewa kwao; na watapata adhabu chungu.

37. Watataka watoke Motoni, lakini hawatatoka humo, na watakuwa na adhabu inayodumu.

Amri ya kumcha Allah تعالى, Kutafuta Njia ya Kufika Kwake Pamoja na Kupigana Jihad

Allah تعالى Anawaamuru waja Wake wema kumcha Yeye, uchaji ambao umetajwa pamoja na vitendo vya utiifu, ina maana kujizuia na yaliyo haramishwa na kuacha yaliyokatazwa. Baadaye Allah تعالى Amesema,

وَأَبْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ

"...na tafuteni njia ya kumfikia."

Safyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisema, ametuhadithia kutoka kwa Talhah kutoka kwa Ata alisema; Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa *Wasilah* ina maana, "Njia ya kuliendea jambo."²

Kauli kama hii pia imesemwa na Mujahid, Abu Wail, Al-Hassan, Qatadah, Abdullah bin Kathir. Qatadah upande wake amesema Aya ina maana. "Tafuta njia ya kuliendea jambo Kwake kwa kumtii Yeye na kufanya mambo yanayo mridhisha Yeye."³

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ

"Hao wanaowaomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kwendea kwa Mola wao Mlezi..." (17:57)

Wasilah ni aina ya njia ya kupata kitu, na pia inatumika kwa maana ya daraja ya juu peponi, na ni daraja ya Mtume ﷺ na daraja hilo lipo karibu peponi na Arshi ya Allah تعالى. Bukhari amenukuu kutoka kwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ قَالَ جِئِنِ بِسْمِ اللَّهِ النَّدَاءِ: اللَّهُمَّ رَبِّ هَذِهِ الدَّعْوَةُ التَّامَّةُ، وَالصَّلَاةُ الْقَائِمَةُ، آتِ مُحَمَّدًا الْوَسِيلَةَ وَالْفَضِيلَةَ، وَابْعَثْهُ مَقَامًا مَحْمُودًا الَّذِي وَعَدْتَهُ، إِلَّا حَلَّتْ لَهُ الشَّفَاعَةُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

"Yeyote baada ya kusikia Adhana akasema, Ewe Allah! Bwana wa ulinganio huu uliotimia na Sala inayosimamishwa! Mpe Muhammad

¹ At-Tabari 10:284.

² At-Tabari 10:291.

³ At-Tabari 10:291.

*wasila na fadhila na Umpe siku ya hesabu wadhifa unaoheshimika ambao Ulimuahidi.' Isipokuwa mtu huyo hupata maombezi siku ya kiama.*¹

Muslim alirekodi kuwa Abdullah bin Amr bin Al-'As رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِذَا سَمِعْتُمُ الْمُؤَذِّنَ فَقُولُوا بِمِثْلِ مَا يَقُولُ، ثُمَّ صَلُّوا عَلَيَّ، فَإِنَّهُ مَنْ صَلَّى عَلَيَّ صَلَاةً صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ عَشْرًا، ثُمَّ سَلُّوا لِي الْوَسِيلَةَ، فَإِنَّهَا مَسْرُورَةٌ فِي الْجَنَّةِ لَا تَنْبَغِي إِلَّا لِعَبْدٍ مِنْ عِبَادِ اللَّهِ، وَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَنَا هُوَ، فَمَنْ سَأَلَ لِي الْوَسِيلَةَ حَلَّتْ عَلَيْهِ الشَّفَاعَةُ»

*"Utakapomsikia Muadhini, yarejee aliyoyasema kisha niombe. Hakika aniombaye rehema mara moja, Allah Atampa Rehema Zake mara kumi. Kisha mniombe wasilah, kwani ni daraja peponi ambayo ni mja mmoja tu wa Allah Anayestahiki kuipata, na ninataraji kuwa mimi ndiye mja mwenyewe. Kwa hakika anayeniombea wasilah kwa Allah, atapata haki ya kuombewa nami.*²

Allah تعالى Amesema,

وَجَاهِدُوا فِي سَبِيلِهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ

"Na piganeni Jihadi kwa ajili Yake ili mpate kuokoka."

Baada ya Allah تعالى Kuwaamuru Waislamu wajiepushe na yaliyokatazwa na wajitahidi kuwa watiifu, Aliwaamuru wapigane dhidi ya adui yao, makafiri, na washirikina walioacha njia iliyonyooka na wakaacha Dini sahihi.

Allah تعالى Aliwashajiisha waumini kwa Kuwakumbusha ufanisi usio na kikomo na furaha kuu Aliyowaandalia siku ya kiyama, ambayo haitobadilika au kupungua kwa wale waliojiunga na Jihad katika njia ya Allah تعالى. Watasalia ndani ya vyumba vya peponi ambavyo ni salama na vizuri. Wale wanaoishi katika makazi haya watakuwa katika starehe na hawatopata taabu, wataishi milele, hawatakufa, na nguo zao hazitokuwa ndogo, wala ujana wao hautoisha.

¹ Fat'hul Al-Bari 8:251.

² Muslim 1:288

Hapana Fidia Itakayokubaliwa Kutoka kwa Makafiri Siku ya Kiyama na Watabaki Motoni.

Kisha Allah تعالى Anaelezea mateso na adhabu iumizayo Anayowaandalia maadui zake wasiokuwa na imani siku ya kiyama. Allah تعالى Amesema

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ أَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ لَيَفْتَدُوا بِهِ مِنْ
عَذَابِ يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَا تُقْبَلُ مِنْهُمْ^ط وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٣٥﴾

“Hakika waliokufuru lau wangekuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya Siku ya Kiyama, yasingelipokelewa kwao; na watapata adhabu chungu.”

Hivyo iwapo kafiri angeleta ardhi imejaa dhahabu mara mbili ya kiasi kilichopo siku ya kiyama ili kujikomboa kutokana na adhabu ya Allah تعالى iliyomzingira. Hakika ataadhibiwa na wala haitokubaliwa mali hiyo. Bali hapatakuwa na mwanya wa kukwepa adhabu, na hatoweza kujiokoa kutokana nayo. Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema,

وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Na watapata adhabu chungu.”Maana: Inayoumiza.

يُرِيدُونَ أَنْ يُخْرِجُوا مِنَ النَّارِ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنْهَا^ط وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٣٦﴾

“Watataka watoke Motoni, lakini hawatatoka humo, na watakuwa na adhabu inayodumu.”

Katika Aya nyingine, Allah تعالى Amesema,

كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يُخْرِجُوا مِنْهَا مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا فِيهَا

“Kila wakitaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo.”

Kwa hiyo, wangelipenda kuondoka kwenye adhabu kwa sababu ya uchungu utakaosababishwa na mateso hayo. Hawatakuwa na njia ya kuitoroka. Jinsi miale ya moto itakavyowanyanyua sehemu ya juu ya Motoni, ndivyo malaika wa adhabu watakvowapinga kwa vyuma na watarudishwa chini,

وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّهِمٌ

“Na watakuwa na adhabu inayo dumu.” Maana: Milele, na hawatoweza kutoka au kukwepa. Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يُؤْتَى بِالرَّجُلِ مِنْ أَهْلِ النَّارِ فَيَقَالُ لَهُ: يَا ابْنَ آدَمَ! كَيْفَ وَجَدْتَ مَضْجَعَكَ؟ فَيَقُولُ: سَرٌّ مَضْجَعٌ، فَيَقَالُ: هَلْ تَنْتَدِي بِقُرَابِ الْأَرْضِ ذَهَبًا؟ قَالَ: فَيَقُولُ: نَعَمْ يَا رَبِّ! فَيَقُولُ اللَّهُ: كَذَبْتَ، قَدْ سَأَلْتِكَ أَقَلَّ مِنْ ذَلِكَ فَلَمْ تَفْعَلْ، فَيُؤَمَّرُ بِهِ إِلَى النَّارِ»

“Atakuja mtu katika watu wa Motoni na ataambiwa, “Ewe mwana wa Adam! Umeyaonaje makazi yako?” Atajibu, “Makazi mabaya.” Ataambiwa, ‘Utajikomboa kwa dunia iliyojaa dhahabu?’ Atasema, ‘Ndiyo, Ewe Mola.’ Allah Atamuambia, ‘Umesema uongo. Nilikutaka Jambo dogo kuliko hilo na hukuweza kulifanya, na ataamrisha kuingia motoni.” Muslimu na An-Nasai waliirekodi Hadith hii.¹

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا جِزَاءً بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَزِيزٌ
حَكِيمٌ ﴿٣٨﴾ فَمَنْ تَابَ مِنْ بَعْدِ ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللَّهَ يَتُوبُ عَلَيْهِ إِنَّ اللَّهَ
غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣٩﴾ أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يُعَذِّبُ مَنْ
يَشَاءُ وَيَغْفِرُ لِمَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٠﴾

38. Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao, hayo ni malipo ya waliyoyachuma, ndiyo adhabu ya mfano itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.

39. Lakini mwenye kutubia baada ya dhulma yake, na akatengenea, basi Mwenyezi Mungu Atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira na Mwenye Kurehemu.

40. Hujui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anao Ufalme wa mbingu na ardhi? Humuadhibu Amtakaye, na Humsamehe Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

¹ Muslim 4:2162 na An-Nasai 6:36.

Amri ya Kukata Mkono wa Mwizi

Allah تعالى Aameamuru na Kuweka sheria kuwa mkono wa mwizi mwanaume au mwanamke ukatwe. Wakati wa Jahiliyyah, hii ilikuwa adhabu kwa mwizi. Na Uislamu umeiendeleza adhabu hii. Katika Uislamu kuna masharti kadhaa kabla ya kutimizwa adhabu hiyo, kama tutakavyofahamisha.

Ni Wakati Gani Mkono wa Mwizi Unafaa Ukatwe?

Imerikodiwa katika sahihi mbili kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَعَنَ اللَّهُ السَّارِقَ يَسْرِقُ الْبَيْضَةَ فَتَقَطُّعُ يَدُهُ، وَيَسْرِقُ الْحَبْلَ فَتَقَطُّعُ يَدُهُ»

“Allah تعالى Amlaani mwizi anayeiba yai na ukakatwa mkono wake, na anayeiba kamba na akakatwa mkono wake.”¹

Bukhari na Muslim waliirikodi Hadithi hii kutoka kwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«تُقَطُّعُ يَدُ السَّارِقِ فِي رُبْعِ دِينَارٍ فَصَاعِدًا»

“Mkono wa mwizi hukatwa kwa kuiba robo ya Dinari au zaidi.”²

Muslim walirekodi kutoka kwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا تُقَطُّعُ يَدُ السَّارِقِ إِلَّا فِي رُبْعِ دِينَارٍ فَصَاعِدًا»

“Mkono wa mwizi hukatwa kwa kuiba robo Dinari au zaidi.”³

Hadithi hii ndio msingi wa suala hili kwa kuwa inaainisha kima ambacho ni halali mwizi kukatwa mkono, nacho ni robo Dinari.

Hivyo Hadithi hii inaweka kiwango. Na kusema kuwa ni Dirham tatu hakuleti mkanganyiko. Kwa sababu Dinar inayosemwa wakati huo ilikuwa sawa na Dirham kumi na mbili. Kwa hiyo Dirham tatu ni sawa na robo Dinar.

¹ Fat'hul Al-Bari 12:83, Muslim 3:1314.

² Fat'hul Al-Bari 12:99, Muslim 3:1312.

³ Muslim 4:1313.

Hii ndio rahisi kupatanisha rai mbili hizi. Maoni haya yalipokelewa kutoka kwa Umar bin Al-Khattab, Uthman bin Affan, Ali bin Ab-Talib رضي الله عنهم na hii ndio rai ya Umar bin Abdul-Aziz, Allayth bin Saa'd Al-Awzaq, na Ash-Shafii na wafuasi wake رضي الله عنهم. Hii pia ni rai ya Imam Ahmad bin Hanbal na Is-haq bin Rahwayh katika moja ya simulizi zake. Pia Abu Thawr, na Dawud bin Ali Az-Zahri رضي الله عنهم.

Imam Ahmad na Is-hak bin Raabiwayh wamesema riwaya nyingine ya kuwa, kila kiwango kimoja kati ya robo Dinari na Dirham tatu kimepokewa na sharia. Mtu yeyote atakayeiba katika moja ya viwango viwili hivyo, au kinacholingana na hivyo atakatwa mkono wake.

Ama Imam Abu Hanifah na wanafunzi wake Abu Yusuf, Muhammad na Zufar, pamoja na Sufyan Ath-Thawri, walisema kuwa kiwango cha chini cha wizi kinachostahili kukatwa mkono ni Dirham kumi, ambapo Dinar ilikuwa Dirham kumi na mbili zama zile.

Hukumu ya kwanza ni sahihi, kuwa kiwango cha chini cha wizi ni robo ya Dinar au zaidi. Kiwango hiki kidogo kiliwekwa kama kikomo cha kukata mkono, ili watu waache kuiba, na huu ni uamuzi wa busara kwa wale wenye akili timamu. Kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema,

جَزَاءُ بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِّنَ اللَّهِ وَأَلَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

"Hayo ni malipo ya waliyoyachuma, ndiyo adhabu ya mfano itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima."

Hii ndio adhabu iliyopangwa kwa kitendo kibaya walichofanya, kwa kuiba mali ya watu wengine kwa mikono yao. Kwa hiyo, Inastahili, zana waliyotumia kuibia mali ya watu ikatwe kama adhabu kutoka kwa Allah تعالى kwa kutenda kosa hilo.

وَأَلَّهُ عَزِيزٌ

"Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu..." Kwenye adhabu,

حَكِيمٌ

"...na Mwenye Hikima." Katika Amri Yake, Makatazo Yake, Sharia Yake na Uwezo Wake.

Toba ya Mwizi Inakubaliwa:

﴿فَمَنْ تَابَ مِنْ بَعْدِ ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللَّهَ يَتُوبُ عَلَيْهِ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾

“Lakini mwenye kutubia baada ya dhulma yake, na akatengenea, basi Mwenyezi Mungu Atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira na Mwenye Kurehemu.”

Kwa hiyo, yeyote anayetubia na akarejea kwa Allah تعالى baada ya kuiba, basi Allah تعالى Atamsamehe. Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abdullah bin Amr رضي الله عنه kuwa alisema kuwa mwanamke aliiba wakati wa Mtume ﷺ na wale aliowaibia walimleta na kusema, “Ewe Mjumbe wa Allah! mwanamke huyu ametuibia.” Jamaa zake wakasema, “Tunamlipia fidia,” Mtume ﷺ alisema,

﴿اقْطَعُوا يَدَهَا﴾

“Ukateni mkono wake.”

Wakasema, “Tunamlipia fidia Dinari mia moja.” Mtume ﷺ akasema:

﴿اقْطَعُوا يَدَهَا﴾

“Ukateni mkono wake.”

Mkono wake wa kulia ulikatwa na yule mwanamke aliuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Ninayo fursa ya kutubia?” Akasema,

﴿نَعَمْ أَنْتِ الْيَوْمَ مِنْ خَطِيئَتِكَ كَيَوْمَ وَلَدْتِكِ أَمْكِ﴾

“Ndiyo, leo huna dhambi tena kama siku uliyozaliwa na mama yako.”

Allah تعالى Aliteremsha ayah katika Surat Al-Maidah,

﴿فَمَنْ تَابَ مِنْ بَعْدِ ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللَّهَ يَتُوبُ عَلَيْهِ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾

“Lakini mwenye kutubia baada ya dhulma yake, na akatengenea, basi Mwenyezi Mungu Atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira na Mwenye Kurehemu.”

¹ Ahmad 2:177.

Mwanamke huyu alikuwa wa kabila la Makhzum. Kisa chake kilisimuliwa ndani ya Sahih Mbili kutoka kwa Az-Zuhri kutoka kwa Urwah kutoka kwa Aishah رضي الله عنها, Kadhia hii iliwashughulisha Maquraish baada ya kuiba wakati wa vita ya Kuiteka (Makkah). Walisema, "Nani anayeweza kuzungumza na Mtume ﷺ kuhusu suala hili?" Kisha wakasema, "Nani anathubutu kuzungumza naye juu ya kadhia hiyo zaidi ya Usamah bin Zayd رضي الله عنه, kipenzi chake." Mwanamke alipoletwa kwa Mtume ﷺ, Usamah bin Zayd رضي الله عنه alizungumza naye juu ya yule mwanamke na uso wa Mtume ﷺ ulibadilika rangi (kwa sababu ya hasira) na akasema,

«أَتَشْفَعُ فِي حَدِّ مِنْ حُدُودِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ؟»

"Unaleta maombi kwa adhabu iliyotolewa na Allah?"

Usamah alimuambia, "Muombe Allah تعالى Anisamehe, Ewe Mjumbe wa Allah!" Usiku ule, Mtume ﷺ alisimama na akatoa hotuba na akamshukuru Allah تعالى kama Anavyostahiki. Kisha akasema,

«أَمَّا بَعْدُ فَإِنَّمَا أَهْلَكَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ أَنَّهُمْ كَانُوا إِذَا سَرَقَ فِيهِمُ الشَّرِيفُ تَرَكُوهُ، وَإِذَا سَرَقَ فِيهِمُ الضَّعِيفُ أَقَامُوا عَلَيْهِ الْحَدَّ، وَإِنِّي وَالَّذِي تَقْسِي بِيَدِهِ لَوْ أَنَّ فَاطِمَةَ بِنْتَ مُحَمَّدٍ سَرَقَتْ لَقَطَعْتُ يَدَهَا»

"Ama baada ya yaliyotangulia, hakika si vingine, Ummah zilizotangulia ziliangamizwa kwa sababu mtu mwenye heshima alipoiba, walimuachia. Lakini masikini alipoiba walitekeleza hukumu na adhabu dhidi yake. Kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Endapo Fatmah binti Muhammad angeliiba, ningelimkata mkono wake."

Mtume ﷺ aliamuru mkono wa mwanamke aliyeiba ukatwe, ukakatwa. Aisha رضي الله عنها alisema, 'Toba yake ilikuwa ya kweli; baadaye aliolewa na alikuwa akinijia ili niwasilishe maombi yake kwa Mtume ﷺ."¹ Haya ndio maneno aliyokusanya Muslim, na katika mapokezi mengine ya Muslim, Aisha رضي الله عنها alisema, "Alikuwa mwanamke wa kabila la Makhzum aliyekuwa akiazima vitu na kisha akikana kuwa alivichukua. Mtume ﷺ akaamrisha mkono wake ukatwe."²

¹ Fat'hul Al-Bari 7:619, Muslim 3:1315.

² Muslim 4:1316.

Kisha Allah تعالى Amesema,

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Hujui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anao Ufalme wa mbingu na ardhi?”

Anamiliki kila kitu na Anaamua Atakavyo na hapana awezaye kuzuia Hukumu Yake,

وَيَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٥﴾

“...na Humsamehe Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”

* * *

* يَتَأْتِيهَا الرُّسُولُ لَا تَحْزَنْكَ الَّذِينَ
 مِنْ الَّذِينَ قَالُوا ءَامَنَّا بِأَفْوَاهِهِمْ وَلَمْ تُؤْمِن قُلُوبُهُمْ
 وَمِنَ الَّذِينَ هَادُوا سَمَّعُوا لِلْكَذِبِ سَمْعًا
 لِقَوْمٍ ءَاخِرِينَ لَمْ يَأْتُواكَ^ط بِحُجُوبٍ الْكَلِمَ مِنْ بَعْدِ
 مَوَاضِعِهِ يَقُولُونَ إِنْ أُوتِيتُمْ هَذَا فَخُذُوهُ وَإِن لَّمْ تَأْتَوْهُ
 فَاحْذَرُوا وَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ فِتْنَتَهُ فَلَنْ تَمْلِكَ لَهُ مِنَ اللَّهِ
 شَيْئًا أُولَئِكَ الَّذِينَ لَمْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يُطَهِّرَ قُلُوبَهُمْ هُمْ فِي
 الدُّنْيَا خِزْيٌ وَلَهُمْ فِي الآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٤١﴾
 سَمَّعُوا لِلْكَذِبِ أَكْثَرُونَ لِلسَّخْتِ فَإِن جَاءُوكَ
 فَاحْكُم بَيْنَهُمْ أَوْ أَعْرِضْ عَنْهُمْ وَإِن تُعْرِضْ عَنْهُمْ فَلَنْ
 يَضُرُّوكَ شَيْئًا وَإِن حَكَمْتَ فَاحْكُم بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ إِنَّ
 اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٤٢﴾ وَكَيْفَ تُحْكُمُونَكَ وَعِنْدَهُمُ
 الْقَوْلُ فِيهَا حُكْمُ اللَّهِ لَمَّا يَتَوَلَّوْنَ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَمَا
 أُولَئِكَ بِالْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٣﴾ إِنَّا أَنْزَلْنَا الْقُرْآنَ فِيهَا هُدًى
 وَنُورًا لِّحُكْمِهَا الْيَسُورَ الَّذِينَ اسْلَمُوا لِلَّذِينَ هَادُوا
 وَالرَّيْبِيِّونَ وَالْأَحْبَابُ بِمَا اسْتُخْفِظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ
 وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءَ فَلَا تَخْشَوُا النَّاسَ وَآخِشُوهُنَّ وَلَا
 تَشْتَرُوا بِمَا بَيْنَ يَدَيْ نَمَّا قَلِيلًا وَمَنْ لَمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ
 فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٤٤﴾ وَكَبَبْنَا عَلَيْهِمْ فِيهَا أَنَّ النَّفْسَ
 بِالنَّفْسِ وَالْعَيْنَ بِالْعَيْنِ وَالْأَنْفَ بِالْأَنْفِ وَالْأُذُنَ
 بِالْأُذُنِ وَالسِّنَّ بِالسِّنِّ وَالْجُرُوحَ قِصَاصًا فَمَنْ تَصَدَّقَ
 بِهِ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَهُ وَمَنْ لَمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ
 فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٤٥﴾

* يَتَأْتِيهَا الرُّسُولُ لَا تَحْزَنْكَ الَّذِينَ
 يُسْرِعُونَ فِي الْكُفْرِ مِنَ الَّذِينَ
 قَالُوا ءَامَنَّا بِأَفْوَاهِهِمْ وَلَمْ تُؤْمِن
 قُلُوبُهُمْ وَمِنَ الَّذِينَ هَادُوا
 سَمَّعُوا لِلْكَذِبِ سَمْعًا
 لِقَوْمٍ ءَاخِرِينَ لَمْ يَأْتُواكَ^ط بِحُجُوبٍ
 الْكَلِمَ مِنْ بَعْدِ مَوَاضِعِهِ يَقُولُونَ
 إِنْ أُوتِيتُمْ هَذَا فَخُذُوهُ وَإِن لَمْ
 تَأْتَوْهُ فَاحْذَرُوا وَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ فِتْنَتَهُ
 فَلَنْ تَمْلِكَ لَهُ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا
 أُولَئِكَ الَّذِينَ لَمْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يُطَهِّرَ
 قُلُوبَهُمْ هُمْ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ وَلَهُمْ
 فِي الآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٤١﴾
 سَمَّعُوا لِلْكَذِبِ أَكْثَرُونَ
 لِلسَّخْتِ فَإِن جَاءُوكَ فَاحْكُم بَيْنَهُمْ
 أَوْ أَعْرِضْ عَنْهُمْ وَإِن تُعْرِضْ عَنْهُمْ
 فَلَنْ يَضُرُّوكَ شَيْئًا وَإِن حَكَمْتَ
 فَاحْكُم بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ
 الْمُقْسِطِينَ ﴿٤٢﴾ وَكَيْفَ تُحْكُمُونَكَ
 وَعِنْدَهُمُ الْقَوْلُ فِيهَا حُكْمُ اللَّهِ لَمَّا

يَتَوَلَّوْنَ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَمَا أُولَئِكَ بِالْمُؤْمِنِينَ ﴿٤١﴾ إِنَّا أَنْزَلْنَا التَّوْرَةَ فِيهَا
هُدًى وَنُورٌ مَحْكُمٌ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا لِلَّذِينَ هَادُوا وَالرَّبَّيِّنُونَ وَالْأَحْبَابُ بِمَا
أَسْتَحْفِظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءَ ۚ فَلَا تَخْشَوُا النَّاسَ وَاخْشَوْنِ وَلَا تَشْتَرُوا
بِعَائِي ثَمَنًا قَلِيلًا ۚ وَمَنْ لَمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٤٢﴾

41. "Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wafanyao haraka kukufuru, miongoni mwa wanaosema kwa vinywa vyao: Tumeamini, na hali nyoyo zao hazikuamini, na miongoni mwa Mayahudi, wanaosikiliza kwa ajili ya uwongo, wanaosikiliza kwa ajili ya watu wengine wasiokufikia. Wao huyabadilisha maneno kutoka pahala pake. Wanasema: Mkipewa haya basi yashikeni, na msipopewa haya tahadharini. Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu Anataka kumfitini huwezi kuwa na madaraka naye mbele ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo zao. Watakuwa na hizaya duniani, na Akhera watakuwa na adhabu kubwa."

42. "Hao ni wasikilizaji kwa ajili ya kusema uwongo, na ni walaji mno vya haramu! Basi wakikujia, wahukumu baina yao au jipuuze nao. Na ukijipuuza nao, basi wao hawatakudhuru kitu. Na ukiwahukumu, basi hukumu baina yao kwa uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda waadilifu."

43. Na huwaje wakufanye wewe hakimumu nao wanayo Taurati yenye hukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanageuka. Na hao si wenye kuamini.

44. "Hakika Sisi Tuliteremsha Taurati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii walionyenyeka Kiislamu, na wachamungu, na wanazuoni, waliwahukumu Mayahudi; kwani walikabidhiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Nao wakawa ni mashahidi juu yake. Basi msiwaogope watu, bali niogopeni Mimi. Wala msibadilishe Aya Zangu kwa thamani chache. Na wasiohukumu kwa aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri."

Usiwe na Majonzi kwa Sababu ya Tabia ya Mayahudi na Wanafiki:

Aya hizi tukufu zilliteremshwa kuhusu wale wanaoendelea kwenye ukafiri, wenye kutoka nje ya utii wa Allah تعالى na Mtume Wake, wakizipa kipaumbele rai zao na utashi wao dhidi ya Allah تعالى na sharia za Allah تعالى.

مِنَ الَّذِينَ قَالُوا ءَامَنَّا بِأَفْوَاهِهِمْ وَلَمْ تُؤْمِن قُلُوبُهُمْ^٤

“...miongoni mwa wanaosema kwa vinywa vyao: Tumeamini, na hali nyoyo zao hazikuamini...”

Watu hawa walidai ni waumini kwa ndimi zao, lakini nyoyo zao hazina chembe ya imani, na wao ni wanafiki.

وَمِنَ الَّذِينَ هَادُوا^٥

“...na miongoni mwa Mayahudi...”

Maadui wa Uislamu na Waislamu, wao na wanafiki wote,

سَمَّعُونَ لِلْكَذِبِ

“...wanaosikiliza kwa ajili ya uwongo...”

Wanaukubali uongo na kujishughulisha nao,

سَمَّعُونَ لِقَوْمٍ ءَاخِرِينَ لَمْ يَأْتُوكَ

“...wanaosikiliza kwa ajili ya watu wengine wasiokufikia...”

Maana: Wanawafuata watu wengine hawaji kwenye baraza yako Ewe Muhammad. Pia husemwa, Aya inaweza kuwa na maana, wanasikiliza unayoyasema na kuyawasilisha kwa maadui zako ambao hawahudhuria baraza yako.

Mayahudi Wanabadilisha Sheria, Kama Vile Kurujumu Waziwazi

تُخَرِّفُونَ الْكَلِمَ مِنْ بَعْدِ مَوَاضِعِهِ^٦

“Wao huyabadilisha maneno kutoka pahala pake.”

Kwa kubadilisha maana zake na wakijua kuwa wanapotosha baada ya kufahamu.

يَقُولُونَ إِنَّ أُوتِيئْتُمْ هَذَا فَخُذُوهُ وَإِن لَّمْ تَأْتَوْهُ فَاحْذَرُوا

“Wanasema: Mkipewa haya basi yashikeni, na msipopewa haya tahadharini.”

Iliarifiwa kuwa sehemu ya Ayah hii iliteremshwa kuwahusu baadhi ya Mayahudi ambao waliua na wakasema, “Tumuombe Muhammad ﷺ awe hakimu wetu, na akitoa shauri tulipe Diyah, turidhie hukumu yake. Endapo atatoa adhabu kali msikubali hukumu yake.”

Rai sahihi ni kuwa Ayah hii iliteremshwa juu ya Mayahudi waliozini.

Mayahudi walibadilisha sheria waliyokuwa nayo katika Kitabu kutoka kwa Allah تعالیٰ kwa masuala ya adhabu ya uzinzi, kutoka kupiga mawe mpaka kufa, kuwa bakora mia moja, na kumpandisha na kumpaka masinzi usoni mwanamke mhalifu juu ya Punda na kumtangaza.

Suala hili la kiasherati lilitokea baada ya Hijrah, waliambizana, “Twendeni kwa Muhammad ﷺ ili atuamulie. Endapo atatoa hukumu ya kutandikwa viboko na kupakwa masinzi usoni, tekelezeni uamuzi wake na mfanye ni ushahidi kwenu na Allah تعالیٰ. Kwa njia hii moja. Lakini atakapoamua kuwa adhabu itakuwa kurujumiwa mpaka kufa, basi msiridhie hukumu yake.”

Kuna Hadithi nyingi zilizotaja kadhia hii. Malik رحمه الله تعالیٰ alisimulia kutoka kwa Abdullah bin Umar رضي الله عنهما alisema, “Mayahudi walimuendea Mtume ﷺ na wakataja kuwa mwanaume na mwanamke miongoni mwao walizini.

Mtume ﷺ akawaambia,

«مَا تَجِدُونَ فِي التَّوْرَةِ فِي سَأْنِ الرَّجْمِ؟»

“Hamuoni hukumu inayohusu kurujumu ndani ya Taurati?”

Wakajibu, “Tunaona watafedheheshwa kisha watatandikwa viboko.” Abdullah bin Salam akasema, ‘Mnaongopa. Taurati inataja *rajmi*, hivyo iletene Taurati.”

Walileta Taurati na wakaifunua lakini mmoja wao aliificha Aya inayohusu kurujumiwa akasoma maandiko yaliyo kabla na baada ya aya hiyo. Abdullah bin Salam akamuambia, Ondosha mkono wako, hivyo ikawa wazi ile Aya inayohusu kurujumiwa.

Hivyo wakasema ukweli, 'Ewe Muhammad! Aya hiyo ipo.' Mtume ﷺ aliamua wale wazinifu warujumiwe mpaka wafe na amri ilitekelezwa. Nilimuona yule mwanaume akijificha kwa mwanamke na kumfanya yeye kinga na mawe."

Bukhari na Muslim pia waliikusanya Hadithi hii na haya ni maneno yaliyokusanywa na Bukhari. Katika mapokezi mengine ya Bukhari, Mtume ﷺ aliwaambia Mayahudi.

«مَا تَضُنُّونَ بِهِمَا؟»

"Mtafanyaje katika hali hii?"

Wakasema, "Tutawakashifu na kuwaaziri." Mtume ﷺ alisoma Aya

فَاتُوا بِالتَّوْرَةِ فَاتْلُوهَا إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ

"Leteni Taurati muisome ikiwa nyinyi ni wasema kweli."

Walimleta mtu mmoja mlemavu na aliyeheshimiwa miongoni mwao na wakamuambia, "Soma Taurati." Alisoma mpaka alipofikia aya fulani aliifunika kwa mkono wake. Aliambiwa, "Ondoa mkono wako." Na ilikuwa aya inayohusu kurujumu.

Yule mtu akasema, "Ewe Muhammad! Hii ni Aya juu ya kurujumu; na tuliificha isifahamike miongoni mwetu. Hivyo Mtume ﷺ aliamuru wale wazinzi wawili wapigwe mawe, na walipigwa mawe."¹ Muslimu alirekodi kuwa mwanaume na mwanamke wa kiyahudi waliletwa mbele ya Mtume ﷺ kwa sababu walizini. Mtume ﷺ alikwenda kwa mayahudi na kuwauliza,

«مَا تَجِدُونَ فِي التَّوْرَةِ عَلَى مَنْ زَنَى؟»

"Kuna hukumu gani ndani ya Tawrat juu ya zina?"

Wakasema, 'Tunazipaka nyuso zao kwa masinzi, kisha tunawaweka juu ya Punda huku wameelekea nyuma na kuwatembeza mitaani.' Mtume ﷺ alisoma

فَاتُوا بِالتَّوْرَةِ فَاتْلُوهَا إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ

"Leteni Taurati muisome ikiwa nyinyi ni wasema kweli."

¹ Al-Bukhari na. 4556.

Hivyo walileta Tawrati na wakasoma mpaka msomaji alipofika katika Aya ya kurujumiwa. Kisha akaweka mkono wake juu ya Aya na akasoma kilichokuwa kabla yake na baada yake. Abdallah bin Salam ambaye alikuwa na Mtume ﷺ alisema, “Muambie aondoe mkono wake.” Na aliondoa mkono wake na chini yake ilikuwepo Aya inayohusu kupigwa mawe kwa mzinifu. Hivyo Mtume ﷺ aliamuru wazinzi warujumiwe, na walifanyiwa hivyo. Abdullah bin Umar رضي الله عنهما alisema, “Nilikuwa miongoni mwa wale waliowapiga mawe na nilimuona mwanaume akimkinga mwanamke na mawe kwa mwili wake.”¹ Abu Dawud aliandika kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, ‘Baadhi ya Mayahudi walikuja kwa Mtume ﷺ na wakamualika kwenda eneo la Quff. Hivyo alikwenda nyumba ya Al-Midras na walisema, “Ewe Aby Al-Qasim? Mwanaume miongoni mwetu amezini na mwanamke, tunaomba ukate shauri. Walimletea Mtume ﷺ mto wa kukalia. Mtume ﷺ akakaa juu yake, kisha akasema,

«اٰتُونِي بِالْتَّوْرٰةِ»

“Nileteeni Taurati,”

Aliletewa Taurati aliondoa mto alioukalia na akaiweka Taurati juu yake huku akisema,

«اٰمَنْتُ بِكَ وَبِمَنْ اَنْزَلْتِكَ»

“Nimekuamini Ewe Taurati na nimemuamini Mtume aliyeteremshiwa.”

Halafu akasema,

«اٰتُونِي بِاٰغْلِيْحِكُمْ»

“Nileteeni mwanazuoni wenu.”

Hivyo aliletwa kijana. Kisha alieleza kisa chote cha *rajmi* kama Malik alivyopokea kutoka kwa Nafi.² Hadithi hizi zinaelezea kuwa Mtume ﷺ alitoa hukumu iliyo ndani ya Taurati na hakuenzi walichoamini Mayahudi kwani Mayahudi waliamrisha kufuata sharia za Muhammad ﷺ pekee. Bali Mtume ﷺ alifanya hivyo kwa sababu Allah تعالى Alimuamuru kufanya hivyo. Aliwauliza kuhusu hukumu ya kurujumu ndani ya Taurati ili wakiri yaliyomo ndani ya Taurati na waliyoshirikiana kuyaficha pamoja na kukanusha na wakaacha

¹ Muslim 3:1326.

² Abu Dawud 4:597.

kuyatekeleza wakati wote. Walikiri kwa yale waliyoyatenda, japokuwa waliyafanya huku wakijua ukweli wa hukumu sahihi. Kilichowafanya kwenda kwa Mtume ﷺ kuhukumiwa katika kadhia hii ni utashi wao, sio kwamba walikubaliana na usahihi wa hukumu yake. Kwa sababu hii walisema,

إِنْ أُوتِيتُمْ هَذَا

"Mkipewa haya..."

Maana: Kupiga viboko, na kupakwa masinzi usoni,

وَإِنْ لَمْ تَوْتَوْهُ فَأَحْذَرُوا

"Na msipopewa haya tahadharini."

Na msikubali kumfuata. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ فِتْنَتَهُ فَلَنْ تَمْلِكَ لَهُ مِنْ أَلَيْسَ شَيْئًا أُولَئِكَ الَّذِينَ لَمْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يُطَهِّرَ قُلُوبَهُمْ هُمْ فِي الدُّنْيَا حِزْبٌ وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٥١﴾ سَمْعُونَ لِلْكَذِبِ أَكْثَلُونَ لِلشَّحْتِ

"Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu Anataka Kumfitini huwezi kuwa na madaraka naye mbele ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo zao. Watakuwa na hizaya duniani, na Akhera watakuwa na adhabu kubwa. Hao ni wasikilizaji kwa ajili ya kusema uwongo, na ni walaji mno vya haramu!"

Suht maana yake ni hongo, kama Ibn Mas'ud رضي الله عنه na wengine walivyoeleza.¹ Aya inaelezea endapo mmoja wenu yuko hivi, ni vipi Allah تعالى Atatakas moyo wake na kukubali dua yake?

Allah تعالى Alimuambia Mtume wake

فَإِنْ جَاءُوكَ

"Basi wakikujia,..." ili uwahukumu baina yao,

¹ At-Tabari 10:319.

فَأَحْكُم بَيْنَهُمْ أَوْ أَعْرِضْ عَنْهُمْ وَإِنْ تُعْرِضْ عَنْهُمْ فَلَنْ يَضُرُّوكَ شَيْئًا

“Wahukumu baina yao au jipuuzo nao. Na ukijipuuzo nao, basi wao hawatakudhuru kitu.”

Maana: Hapana madhara kama hutowahukumu baina yao. Hii ni kwa sababu walipokuja kutaka kuamuliwa baina yao, hawakutaka kufuata ukweli, lakini walifanya hivyo kwa yale yanayowafikiana na utashi wao. Yapasa tutaje hapa kuwa Ibn Abbas, Mujahid, Ikrimah, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi, Zayd bin Aslam. Ata Al-Khurasan, na wengineo رضي الله عنهم walisema kuwa sehemu hii ya Aya ilifutwa na kauli ya Allah تعالى ifuatayo,

وَأَنْ أَحْكُم بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ

“Na hukumu baina yao kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu.”¹

وَإِنْ حَكَمْتَ فَأَحْكُم بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ

“Na ukiwahukumu, basi hukumu baina yao kwa uadilifu.”

Haki na uadilifu. Japokuwa Mayahudi si waadilifu na wako nje ya njia iliyo sahihi,

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda waadilifu.”

Ukaripiaji wa Malengo Mabaya ya Mayahudi, na Kusifia Kitabu Chao cha Taurati.

Kisha Allah تعالى Anachukizwa na Mayahudi kwa fikra zao potofu na Malengo yao Mabaya ya kuacha waliyoyaamini kwa kweli kutoka katika kitabu chao, na ambacho kipo mkononi mwao. Ambacho hudai kuwa wameamrisha kukifuata.

Hata hivyo hawaifuati Taurati, bali wanataka sheria nyingine, japokuwa wanaamini kuwa sheria nyingine sio sahihi na haziwahusu.

Allah تعالى Amesema:

¹ At-Tabari 10:330-332.

وَكَيْفَ يُحْكِمُونَكَ وَعِنْدَهُمُ التَّوْرَةُ فِيهَا حُكْمُ اللَّهِ ثُمَّ يَتَوَلَّوْنَ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَمَا أُولَئِكَ بِالْمُؤْمِنِينَ ﴿٤١﴾

“Na huwaje wakufanye wewe hakimu nao wanayo Taurati yenye hukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanageuka. Na hao si wenye kuamini.”

Baadaye Allah تعالى Anaisifu Taurati kuwa Aliiteremsha kwa mjumbe Wake Musa عليه السلام, mwana wa Imran,

إِنَّا أَنْزَلْنَا التَّوْرَةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ تَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا لِلَّذِينَ هَادُوا

“Hakika Sisi Tuliteremsha Taurati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii walionyenyeka Kiislamu, waliwahukumu Mayahudi,”

Na hawa Mitume hawakukengeuka kutoka katika sheria ya Taurati au kuibadilisha,

وَالرَّابِّيُونَ وَالْأَحْبَارُ

“Na wachamngu, na wanazuoni,...” Hapa Rabhaniyyun ina maana ya wanazuoni wafanyao ibada ambao wana elimu na watu wa dini, na Ahbar ina maana ya wanazuoni,

بِمَا اسْتُحْفِظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ

“Kwani walikabidhiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu.” Muradi wake, walikabidhiwa kitabu cha Allah تعالى, na wakaamrisha kukifuata na wasifiche chochote,

وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءَ فَلَا تَخْشَوُا النَّاسَ وَآخِشُوا وَلَا تَنْتَرُوا بِعَابَتِي ثَمَنًا قَلِيلًا وَمَنْ لَمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

“...Nao wakawa ni mashahidi juu yake. Basi msiwaogope watu, bali Niogopeni Mimi. Wala msibadilisha Aya Zangu kwa thamani chache. Na wasiohukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.”

Kuna njia mbili za kuelezea Aya hii tutazielezea baadaye.

Sababu Nyingine ya Kuteremshwa Aya Hizi Tukufu

Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, Allah تعالى Aliteremsha Aya,

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

“Na wasiohukumu kwa aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.”

فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

“...Hao ndio madhalimu.” na

فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

“...Hao ndio mafasiki.” Ibn Abbasi رضي الله عنهما amesema: Allah تعالى Aliteremsha Aya hizo kuhusu makundi mawili ya Mayahudi, katika enzi za Jahiliyyah, kundi moja lilishinda jengine kutokana na sababu hiyo, walifunga mkataba kuwa kundi dhalili akiuliwa mtu wao wangepewa diya inayofikia wasaq hamsini. Na kila mtu aliyeuawa kutoka kundi la watukufu yake ilikuwa waski mia moja. Mkataba huu ulibaki hivyo mpaka Mtume ﷺ alipokuja Madina na makundi yote hayo yakawa chini ya utii wa Mtume ﷺ. Bado kundi lenye nguvu lilipeleka ujumbe likidai Wasaq mia moja kutoka kundi dhaifu. Hivyo kundi dhaifu lilisema, “Itakuwaje makundi mawili yenye dini sawa, nasaba moja na raia wa nchi moja, kuwe na Diya ambayo kwa baadhi ni nusu ya ile walipayo wengine?”

Tulikubaliana nayo kwa sababu mlitukandamiza na tuliwaogopeni. Kwa kuwa Muhammad ﷺ amekuja, hatutokupeni mlichotaka. Hivyo vita vilikuwa karibu kulipuka baina yao, kundi lenye nguvu (lilisemezana), wao kwa wao, ‘Wa Llah! Muhammad ﷺ hatowapeni Diya maradufu ambayo mnapewa mkilinganisha na ile mnayowalipa wao. Wamesema kweli, kwani walituma kiwango hiki kwa sababu tuliwakandamiza na kuwazidi nguvu. Kwa hiyo mpeleke mtu kwa Muhammad ﷺ atakayebaini hukumu yake katika shauri hili. Iwapo atakubali kuwapeni mnachodai, kubalini hukumu yake, na asipowapeni mnachotaka, msiende kwake kutatua shauri hilo!” Hivyo, walikwenda baadhi ya wanafiki kwa Mtume ﷺ ili kujaribu na kufahamu hukumu yake Mtume ﷺ. Walipokuja kwa Mjumbe ﷺ, Allah تعالى Alimueleza juu suala lile na njama zao. Allah تعالى Aliteremsha,

يَتَأْتِيهَا الرَّسُولُ لَا مَحْزَنَ الَّذِينَ يُسْرِعُونَ فِي الْكُفْرِ

“Ewe Mtume! Wasikuhuzunisha wa fanyao haraka kukufuru.” mpaka

الْفٰسِقُوْنَ

“...*mafasiki*.” Wa Llah! Ni kwa sababu ya matatizo yao ndipo Allah تعالى Akashusha Aya hizi, na wao ndio waliokusudiwa na Allah تعالى.”¹ Abu Dawud alikusanya masimulizi sawa na Hadithi hii.”² Abu Jafar Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa Ayah zilizopo kwenye Surat Al-Maidah,

فَاَحْكُم بَيْنَهُمْ اَوْ اَعْرَضْ عَنْهُمْ

“...*wahukumu baina yao au jipuuze nao*,...” hadi Kauli Yake

الْمُقْسِطِيْنَ

“...*waadilifu*.” Iliteremshwa kuhusu tatizo la Diya kati ya Bani An-Nadhir na Bani Quraydhah. Maiti wa Bani An-Nadhir walikuwa wakipewa heshima zaidi na walilipwa kiwango kamili cha Diya, ambapo Bani Quraydhah, Walipata nusu ya Diya kwa maiti wao. Hivyo walipeleka mashitaka yao kwa Mtume ﷺ ili waamuliwe na Allah تعالى Aliteremsha Ayat hizi kuwahusu. Mtume ﷺ aliwataka wafuate hukumu sahihi ya kadhia hii na alifanya kiwango cha Diyah sawa kwa makundi yote na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi katika suala hili.”³ Ahmad, Abu Dawud na An-Nasai⁴ pia waliipokea Hadithi hii kutoka kwa Abu Is-haq. Al-Awfi na Ali bin Abi Talhah waliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya hizi ziliteremshwa juu ya Mayahudi wawili ambao walizini, na tuliitaja Hadithi juu ya kisa hiki kabla. Inaelekea matukio hayo mawili ni yote sababu zilizopelekea kuteremshwa Aya hizi, na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Kwa sababu hii Allah تعالى Alisema baadaye,

وَكَتَبْنَا عَلَيْهِمْ فِيهَا اَنْ النَّفْسَ بِالنَّفْسِ وَالْعَيْنَ بِالْعَيْنِ

“*Na Tuliwaandikia ndani yake kuwa nafsi kwa nafsi na jino kwa jino.*”

Mpaka mwisho wa Aya, ambayo inaipa nguvu rai ya kisa cha Diya kuwa ndio sababu ya kushuka Aya kama tulivyo dhukuru hapo juu. Allah تعالى Anajua Zaidi. Allah تعالى Amesema,

¹ Ahmad 1:246.

² Abu Dawud 4:7.

³ At-Tabari 10:326.

⁴ Ahmad 1:363, Abu Dawud 4:16 na An-Nasai 8:19.

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

“Na wasiohukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.”

Al-Barau bin Azib, Hudhayfah bin Al-Yaman, Ibn Abbas, Abu Mijlz, Abu Rajah Al-Utarid, Ikrimah, Ubaydullah bin Abdullah, Al-Hassan Al-Basri na wengine رضي الله عنهم walisema kuwa Ayah hii iliteremshwa juu ya Watu wa Kitabu.¹ Al-Hassan Al-Basri رحمه الله تعالى aliongeza kuwa Ayah hii inatuhusu sisi pia.² Abdur-Razaq kutoka kwa Sufiani Ath - Thawri kutoka kwa Mansur kutoka kwa Ibrahim alisema kuwa Aya hizi, “Ziliteremshwa kuwahusu Wana wa Israil, na Allah تعالى Aliwakubalia kwa Ummah huu.” Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliandika kauli hii.³

Ali bin Abi Talhah pia alieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alieleza juu ya kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

“Na wasiohukumu kwa aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.”

“Yeyote anayekana yaliyoteremshwa na Allah تعالى, atakuwa amekufuru, na yeyote anayeridhia yaliyoteremshwa na Allah تعالى, lakini hakutawala kwalo, ni Dhalimu na Fasiq.” Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliandika kauli hii.⁴

“Abdur-Razaq alisema, ‘Ma’mar alitusimulia kuwa Tawas alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliulizwa kuhusu kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ

“Na wasiohukumu...” Alisema ni kitendo cha ukafiri. Ibn Tawus aliongezea, ‘Si sawa na wale wanaomkufuru Allah تعالى, Malaika Wake, Vitabu Vyake na Mitume Wake!’ Ath –Thawri alisimulia kuwa Ibn Jurayj alisema kuwa Ataa alisema, ‘Kuwa ni ukafiri mdogo, udhalimu mdogo na ufuska mdogo.’⁵ Waki alisema kuwa Said Al-Makki,

¹ At-Tabari 10:347-357.

² At-Tabari 10:357.

³ At-Tabari 10:356.

⁴ At-Tabari 10:597.

⁵ ‘Abdur-Razaq 1:191, At-Tabari 10:595.

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

“Na wasiohukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.”

“Huo sio ukafiri unaomtoa mtu katika Dini.”¹

وَكَتَبْنَا عَلَيْهِمْ فِيهَا أَنَّ النَّفْسَ بِالنَّفْسِ وَالْعَيْنَ بِالْعَيْنِ وَالْأَنْفَ بِالْأَنْفِ وَالْأَذْنَ بِالْأُذُنِ وَالسِّنَّ بِالسِّنِّ وَالْجُرُوحَ قِصَاصٌ فَمَنْ تَصَدَّقَ بِهِ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَهُ وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٤٥﴾

45. “Na humo Tuliwaandikia ya kwamba roho kwa roho, na jicho kwa jicho, na pua kwa pua, na sikio kwa sikio, na jino kwa jino, na kwa majaraha kisasi. Lakini atakayesamehe basi itakuwa ni kafara kwake. Na wasiohukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu.”

Aidha Aya hii inawafedhehesha na kuwasimbulia Mayahudi, kwa sababu ndani ya Taurati, wanasheria ya nafsi kwa nafsi. Hata hivyo waliifasiri sheria hiyo kwa lengo la kukengeuka na kuasi. Walikuwa wakiitumia sheria hii pale mtu wa Bani Nadhir alipouawa na mtu wa Quraydha, lakini hilo halikujiri lilipotokea kinyume chake. Bali, wangelirejea kwenye Diyah katika hali hii. Pia walifasiri ndani ya Taurati hukumu ya kurujumu wazinzi na badala yake wakaanzisha aina yao ya adhabu, kupiga viboko, kuwapaka masinzi na kuwatembeza hadharani, Kwa sababu hii Allah تعالی Amesema katika Aya iliyopita,

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

“Na wasiohukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu.”

Kwa sababu walikataa amri ya Allah تعالی kwa kudhamiria na kwa kuchupa mipaka na kuasi makusudi. Katika Aya hii Allah تعالی Amesema,

فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

“Basi hao ndio madhaalimu.”Kwani hawakudai haki ya mkandamizwaji kutoka kwa mkandamizaji katika aliloamrisha Allah تعالی kuwa wote watendewe haki. Badala yake walivunja amri hiyo, wakadhulumu na wakakoseana wao kwa wao.

¹ At-Tabari 10:355.

Mwanaume Huuawa kwa Kuuu Mwanamke:

Imam Abu Nasr As-Sabbagh رحمه الله تعالى alieleza katika Kitabu chake, "Ash – Shamil" kuwa wanazuoni wanakubaliana katika Ayah hii (5:45) kuwa ni uthibitisho na hoja juu ya yale tuliyoyaeleza huko nyuma. Maimamu wanakubaliana kuwa mwanaume anauawa kwa kumuua mwanamke, kwa mujibu wa dalili za jumla za Ayah hii. Hadithi aliyoirikodi An-Nasai¹ inaeleza kuwa Mtume ﷺ aliandika kauli hii katika barua yake aliyompa Amr bin Hazm,

«أَنَّ الرَّجُلَ يُقْتَلُ بِالنِّمْرَةِ»

"Mwanaume huuawa kwa kumuua mwanamke."

Katika Hadithi nyingine, Mtume ﷺ amesema,

«الْمُسْلِمُونَ تَتَكَافَأُ دِمَاؤُهُمْ»

"Waislamu ni sawa kwa mujibu wa utukufu wa damu zao."²

Hii pia ni rai ya wanazuoni wengi.

Kauli ya Assabbagh رحمه الله تعالى inayosema kuwa Aya hii ni hoja ya nguvu katika shauri lililopita, inapewa nguvu na Hadithi ya Mtume ﷺ iliyothibiti katika shauri hilo kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa alisema, Ar-Rabi (shangazi yake) alivunja jino la msichana, na nduguze Ar-Rabi waliomba kwa nduguze msichana kumsamehe (mkosaji), lakini walikataa. Hivyo walikwenda kwa Mtume ﷺ ambaye aliwaamuru walipize kisasi. Anas bin An-Badhr, kaka yake, aliuliza 'Ewe Mjumbe wa Allah! Je jino la Ar-Rabi litavunjwa?' Mtume ﷺ alisema, 'Ewe Anas! Kitabu cha Allah تعالى kinazungumzia kulipiza kisasi!' Anas رضي الله عنه akasema, 'Hapana, kwa Jina la Yule Aliyekutuma na ujumbe wa kweli meno yake hayatovunjwa. Baadaye jamaa wa msichana walikubali kumsamehe Ar-Rabi na wakaacha haki ya kulipiza kisasi." Mtume ﷺ alisema,

«إِنْ مِنْ عِبَادِ اللَّهِ مَنْ لَوْ أَقْسَمَ عَلَى اللَّهِ لِأَبْرِهِ»

"Kuna baadhi ya Waja wa Allah تعالى ambao wanapoapa kwa Jina la Allah تعالى, Basi hukubaliwa kiapo chao."³

Iliandikwa ndani ya Sahih Mbili.

¹ An-Nasai 8:58.

² Ibn Majah 2:895.

³ Ahmad 3:167.

Kulipiza Kisasi kwa Majeraha

Allah تعالى Amesema,

وَأَلْجُرُوحَ قِصَاصٍ

“Na kwa majaraha kisasi.”

Ali bin Abi Talha aliripoti kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, ‘Uhai kwa uhai, jicho kwa jicho, pua ikikatwa kwa pua, jino lililovunjwa kwa jino na jeraha kwa jeraha.’² Waislamu huru, wanaume kwa wanawake wako sawa katika masuala haya. Na watumwa wao, wanaume na wanawake, wako sawa katika suala hili. Na sheria hii ni kwa kukusudia nafsi na chini ya nafsi, kama Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى walivyorikodi.

Hukumu Muhimu:

Kulipiza Kisasi kwa jeraha kusitekelezwe mpaka kidonda cha muathirika kipone. Iwapo ulipizaji kisasi utafanywa kabla ya kupona kidonda halafu kidonda kikazidi, muathirika hatokuwa na haki za ziada katika kadhia hii. Ushahidi wa hukumu ya suala hili ni vile Imam Ahmad alivyopokea kutoka kwa Amr bin Shuaib, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake kuwa kuna mtu alimchoma mwenziwe mguuni kwa pembe. Muathirika alikuja kwa Mtume ﷺ akidai kisasi, na Mtume ﷺ alisema,

«حَتَّى تَبْرَأَ»

“Hapana mpaka upone.”

Yule mtu alirejea tena kwa Mtume ﷺ na akamtaka kufanyika usawa katika kulipiza kisasi na Mtume ﷺ aliliruhusu hilo. Baadaye yule mtu alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! ‘Sasa ninachechemea.’ Mtume ﷺ alisema,

«فَدَنْتُكَ فَعَصَيْتَنِي، فَأَبْعَدَكَ اللَّهُ وَبَطَلَ عَرَجُكَ»

“Nilikutaka usubiri, lakini hukunitii. Kwa hiyo, Allah Akutupilie mbali na kuchechemea kwako hakuna fidia.”

Baadaye, Mtume ﷺ alipiga marufuku jeraha kulipiziwa kisasi mpaka lipone.³

¹ Fat’hul Al-Bari 8:124, Muslim 3:1302.

² At-Tabari 10:360.

³ Ahmad 2:217.

Endapo muathirika ataruhusiwa kulipiza kisasi kwa jeraha lililosababishwa na mshari, na matokeo yake akafariki dunia, hapana fidia katika hali hii, kwa mujibu wa Masahaba wengi na wafuasi wao.

Kusamehe Kunafuta Dhambi

Allah تعالى Amesema, **فَمَنْ تَصَدَّقَ بِهِ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَهُ**^١

“Lakini atakayesamehe basi itakuwa ni kafara kwake.”

Ali bin Abi Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo kuwa,

فَمَنْ تَصَدَّقَ بِهِ

“Lakini atakayesamehe...” Maana yake: “Iwapo mmoja wenu alisamehe kwa njia ya sadaka inakuwa ni kafara kwa aliyejeruhi, hatoadhibiwa huko Akhera. Na ni malipo kwa aliyejeruhiwa.”¹ Sufiani Athauri رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Atwaa bin Assaib, kutoka kwa Said bin Jubair, kutoka kwa bin Abbaasi رضي الله عنهما: ‘Yeyote yule atayetoa sadaka kwa njia ya kusamehe inakuwa kwake kafara ya kuandikiwa dhambi kwa aliyejeruhi. Na malipo ya aliyejeruhiwa yapo juu ya Allah تعالى.” Haya ameyapokea bin Abuu Hatim رحمه الله تعالى. Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

فَمَنْ تَصَدَّقَ بِهِ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَهُ^٢

“Lakini atakayesamehe basi itakuwa ni kafara kwake.”

“Kwa muathirika.” Hii pia ni rai ya Al-Hasan Al-Basri, Ibrahim An-Nakhai na Abu Is-haq Al-Hamdani. Imam Ahmad aliandika kuwa Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه alisema Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«مَا مِنْ رَجُلٍ يُجْرَحُ مِنْ جَسَدِهِ جِرَاحَةً فَيَتَصَدَّقُ بِهَا، إِلَّا كَفَّرَ اللَّهُ عَنْهُ مِثْلَ مَا تَصَدَّقَ بِهِ»

“Mtu yeyote anayejeruhiwa kwenye mwili wake na akasamehe kulipiza kisasi kama sadaka yake, basi Allah تعالى Atamsamehe sawa na kile alichokisamehe.”³

¹ At-Tabari 10:367.

² At-Tabari 10:326.

³ Ahmad 5:316.

An-Nasai¹ na Ibn Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى waliandika Hadithi hii. Kauli ya Allah تَعَالَى،

وَمَنْ لَّمْ يَتَّخِذْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٤١﴾

“Na wasiohukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu.”

Mapema tulichukuwa kauli ya Ata na Tawus kuwa ni ukafiri mdogo, dhuluma mdogo na ufasiki mdogo.

* * *

¹ An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:335 na Ibn Jarir At-Tabari 10:364. Maana ya Hadithi hii inaungwa mkono na vitabu vingine.

وَقَفَيْنَا عَلَىٰ آثَرِهِمْ بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ
 مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرَةِ ۗ
 وَءَاتَيْنَاهُ الْإِنجِيلَ فِيهِ هُدًى
 وَنُورٌ وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ
 التَّوْرَةِ ۗ وَلِيَحْكُمَ أَهْلَ
 الْإِنجِيلِ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فِيهِ ۗ
 وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ
 الْفَاسِقُونَ ۖ
 وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ
 لِيُبَيِّنَ لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ
 الْكِتَابِ وَمُهَيِّمًا عَلَيْهِ ۗ فَاحْكُم
 بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ ۗ وَلَا تَتَّبِعْ
 أَهْوَاءَهُمْ عَمَّا جَاءَكَ مِنَ الْحَقِّ ۗ لِكُلِّ
 جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَاجًا ۗ وَلَوْ
 شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً
 وَاحِدَةً وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَكُمْ فِي مَا
 آتَيْنَاكُمْ ۗ فَاسْتَقِيمُوا الصِّرَاطَ
 إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا ۗ فَيُنَبِّئُكُمْ
 بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ۗ وَأَنْ
 أَحْكَمَ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ ۗ وَلَا
 تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ ۗ وَأَحْذَرَهُمْ أَنْ
 يَفْتِنُوكَ عَنْ بَعْضِ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ
 إِلَيْكَ ۗ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَاعْلَمْ أَنَّنَا
 يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُصِيبَهُمْ بِبَعْضِ
 ذُنُوبِهِمْ ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا مِنَ
 النَّاسِ لَفَاسِقُونَ ۖ أَفَحُكْمَ
 الْجَبَلِيَّةِ يَبْتَغُونَ ۗ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ
 اللَّهِ حُكْمًا لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ ۗ

وَقَفَيْنَا عَلَىٰ آثَرِهِمْ بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ
 مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرَةِ ۗ
 وَءَاتَيْنَاهُ الْإِنجِيلَ فِيهِ هُدًى وَنُورٌ
 وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرَةِ
 وَهُدًى وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ۖ
 وَلِيَحْكُمَ أَهْلَ الْإِنجِيلِ بِمَا أَنْزَلَ
 اللَّهُ فِيهِ ۗ وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ
 اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ۖ

46. Na Tukawafuatishia hao Isa bin Maryamu kuya-hakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na Tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongofu, na nuru na inayosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na uwongofu na mawaidha kwa wachamungu.

47. Na wahukumu Watu wa Injili kwa yale Aliyotemsha Mwenyezi Mungu ndani yake. Na wasiohukumu kwa yale Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu.

Allah تعالى Amemtaja Isa عليه السلام na habari ya Mtume ﷺ na Kuisifia Injili

Allah تعالى Amesema,

وَقَفَيْنَا

“Na Tukawafuatishia...” Maana yake: Tukawaambatanishia,

عَلَىٰ آثَرِهِمْ

“Nyuma yao.” Maana yake: Kwa Mitume wa Wana wa Israil,

بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرَةِ^ط

“Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati...”

Muongozo kwa maana ya kuiamini na kuifanyia kazi,

وَأَتَيْنَهُ الْإِنجِيلَ فِيهِ هُدًى وَنُورٌ

“Na Tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongofu, na nuru...”

Uongofu wenye kumuongoza kwenda kwenye ukweli; na nuru inayoondoa mashaka na kusuluhisha migongano,

وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرَةِ

“Na inayosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati...”

Maana: Uliizingatia Taurati isipokuwa kwa matukio machache ambayo yaliyoweka wazi kweli ambapo Wana wa Israil walitofautiana. Allah تعالى Anaeleza katika Aya nyingine kuwa Isa عليه السلام aliwaambia Wana wa Israil,

وَلِأَجْلِ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي حُرِّمَ عَلَيْكُمْ^ع

“Na ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mlioharimishiwa.”

Hivyo wanazuoni wanasema kuwa Injili ilifuta baadhi ya hukumu za Taurati. Kauli ya Allah تعالى

وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ

“Na mawaidha kwa wachamungu.”

Maana: Tuliifanya Injili ni muongozo na kemeo linalozuia kufanya dhambi na makosa, kwa wenye Taqwa kwa Allah تعالى na wanaogopa Makatazo Yake na Adhabu Zake.

Baadaye Allah تعالى Amesema,

وَلِيَحْكُمَ أَهْلُ الْإِنجِيلِ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فِيهِ^ع

“Na wahukumu Watu wa Injili kwa yale Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu ndani yake.”

Maana yake: Ili awahukumu kwa Injili katika watu wa zama zao. Au Ayah ina mana, ili waamini yote yaliyomo na kushikamana na maamrishi yake, ikiwa ni pamoja na habari kuhusu kuja kwa Muhammad ﷺ na amri ya kuamini na kumfuata alipotumwa. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

قُلْ يَا هَلْ أَكْتَبَ لَسْتُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ حَتَّىٰ تُقِيمُوا التَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ
مِّن رَّبِّكُمْ

“Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Hamna lenu jambo mpaka muishike Taurati na Injili na yote mlioteremshiwa kutokana na Mola wenu Mlezi.”

Na Allah تعالى Amesema,

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ

“Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiyesoma wala kuandika, wanayemkuta kaandikwa kwao katika Taurati...” Mpaka

الْمُفْلِحُونَ

“Wenye kufanikiwa.” Hapa Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

“Na wasiohukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu.”

Maana yake: Kumuasi Allah تعالى na kukhitari upotofu na kuacha ukweli. Tulishasema mapema kuwa Aya hii iliteremshwa juu ya Wakristo, na hili limethibitishwa na muktadha wa Aya.

وَأُنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ وَمُهَيِّمًا عَلَيْهِ
فَأَحْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ عَمَّا جَاءَكَ مِنَ الْحَقِّ لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ
شِرْعَةً وَمِنْهَا جَاةٌ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَيْنَاكُمْ
فَأَسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٠﴾ وَأَنْ
أَحْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ وَأَحْذَرَهُمْ أَنْ يَفْتِنُوكَ عَنْ بَعْضِ مَا أُنزَلَ

اللَّهُ إِلَيْكَ ط فَإِنْ تَوَلَّوْا فَاَعْلَمَ أَنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَن يُصِيبَهُمْ بِبَعْضِ ذُنُوبِهِمْ ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ
لَفَاسِقُونَ ﴿٤٨﴾ أَفَحُكْمَ الْجَهَنَّمِيَّةِ يَبْتَغُونَ ۖ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٤٩﴾

48 Na Tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda. Basi hukumu baina yao kwa aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamano yao ukaacha Haki iliyokujia. Kila mmoja katika nyinyi Tumemuwekea sharia yake na njia yake. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka Angekufanyeni nyote umma mmoja, lakini ni kukujaribuni kwa Aliyokupeni. Basi shindaneni kwa mambo ya kheri. Kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo yenu nyote, na Atakuja kuwaambieni yale mliyokuwa mkikhitalifiana."

49. Na wahukumu baina yao kwa Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamano yao. Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaacha baadhi ya Aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka, basi jua kwamba hakika Mwenyezi Mungu Anataka kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao. Na hakika wengi wa watu ni wapotofu."

50. "Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?"

Kuisifu Qur'an na Amri ya Kutumia Sharia Yake.

Allah تعالیٰ Ameitaja Tawrat ambayo Alimteremshia Mtume Wake Musa عليه السلام, ambaye Alizungumza naye moja kwa moja, Akaitukuza, na Kuamrisha ifuatwe. Kisha Allah تعالیٰ Anaitaja Injili, Anaisifu na Anawamuru watu wake kuifuata na kudumu nayo, kama tulivyoeleza. Kisha Qur'an Takatifu ambayo Alimteremshia mtumishi Wake bora na Mtume Wake ﷺ. Allah تعالیٰ Amesema,

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ

"...Tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi..."

Inamaanisha, pamoja na ukweli usio na shaka kuwa vinatoka kwa Allah تعالیٰ,

مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ

“Kinacho sadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Vitabu...”

Maana: Vitabu vitakatifu vilivyoteremshwa ambavyo vimeisifu Qur’an, na vikataja kuwa kitateremshwa kutoka kwa Allah تعالى kwenda kwa mja wake na Mtume wake Muhammad ﷺ. Qur’an iliteremshwa kama ilivyotabiriwa na maandiko yaliyotangulia. Ukweli huu uliongeza imani katika Vitabu vilivyo tangulia kwa uaminifu kwa wale wenye kujua maandiko haya, wale wanaoshikamana na amri na sharia za Allah تعالى na walioamini Mitume Yake. Allah تعالى Amesema,

قُلْ ءَامِنُوا بِمَآءِ أَوْ لَا تُؤْمِنُوا إِنَّا الَّذِيْنَ أُوْتُوا الْعِلْمَ مِنْ قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ
يَخْرُؤْنَ لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا ﴿١٠٧﴾ وَيَقُولُونَ سُبْحٰنَ رَبِّنَا إِن كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿١٠٨﴾

“Sema: laminini au msiiamini. Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake, wanaposomewa hii, huanguka kifudifudi wanasujudu. Na wanasema: Subhana Rabbina, Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika ahadi ya Mola wetu Mlezi lazima itimizwe!” (17:107-108)

Maana: Wanasema kuwa ahadi ya Mola wetu kuhusu kuja kwa Muhammad ﷺ kwa maneno ya Mitume Wake waliotangulia, bila shaka itatimizwa.

Kauli ya Allah تعالى,

وَمُهَيِّمًا عَلَيْهِ

“Na Kuyalinda juu yake...”

Maana: Iliyopewa dhamana juu yake. Sufian Ath-Thaur رحمه الله تعالى na wengineo wamepokea kutoka kwa Abu Is-hak kutoka kwa At-Tamimi kutoka kwa Ibin Abbass رضي الله عنهما kwa maana ya kusadikisha juu yake. Naye,¹ Ali bin Talhah aliripotiwa kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Muhaymin ni “uaminifu.” Qu’ran inaaminika juu ya kila kitabu kitakatifu kilichotangulia.”² Hii ilipokewa kutoka kwa Ikrima, Said bin Jubayr, Mujahid, Muhammad bin Ka’b, Atiyyah, Al-Hasan, Qatadah, Ata Al-Khurasani, As-Suddi na Ibn Zayd.³ Ibn Jarir رحمه الله تعالى

¹ At-Tabari 10:378.

² At-Tabari 10:379.

³ At-Tabari 10:377-380.

alisema, 'Qur'an imesadikishwa na vitabu vilivyotangulia. Kwa hiyo chochote kinachokubaliana na Qur'an ni kweli na kile kinachopingana na Qur'an ni batili.' Al-Wali amesimulia kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, "Muhaimin ina maana ya Shahidi."¹ Mujahidi, Qatadah na As-suddi walisema vivyo hivyo. Al-Awfi amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, "Muhaymini maana yake kimezidi kimaandiko vitabu vili vyotangulia."² Maana hizi ni sawa, kwa vile neno Muhaymin inajumuisha yote. Hivyo Qur'an inaaminika, ni shahidi, na imezidi kila Andiko lililotangulia. Kitabu hiki kitakatifu, Alichoteremsha Allah تعالى kuwa cha mwisho, na kilichokusanya kila kitu, kitakatifu na sahihi kwa zama zote. Qur'an imejumuisha mambo mazuri ya maandiko yaliyotangulia na nyongeza ya maandiko ambayo hayakuwemo katika vitabu vilivyotangulia. Kwa ajili hiyo alikifanya kuaminika, shahidi na kuwa muongozo wa vitabu vyote. Allah تعالى Aliahidi kuwa Atailinda Qur'an na Akaapa kwa Utukufu Wake Binafsi

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٥٠﴾

"Hakika Sisi ndio Tulioteremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio Tutaoulinda."

Allah تعالى Amesema.

فَأَحْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ ط

"Basi hukumu baina yao kwa Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu..."

Aya inaamrisha: Ewe Muhammad kuwa hakimu baina ya watu, waarabu na wasio waarabu, wanaojua kusoma na wasiojua, kwa yale Allah تعالى Aliyokuteremshia ndani ya hiki kitabu kitakatifu na yale yaliyothibitishwa kwako katika sheria ya Mitume waliotangulia - kama Ibn Jarir رحمه الله تعالى alivyosema.³ "Ibn Abu Hatim amesimulia kuwa bin Abbas رضي الله عنهما amesema: "Mtume alikuwa na khiari kuwahukumu kati yao au kutowasikiliza. Hivyo akawarejesha kwenye sheria zao. Ikateremshwa Aya,

وَأِنْ أَحْكَم بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ

"Na wahukumu baina yao kwa Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuute matamano yao."

¹ At-Tabari 10:377.

² At-Tabari 10:379.

³ At-Tabari 10:382.

Na aliamrisha Mtume ﷺ kuwahukumu kwa kitabu chetu.”¹ Kauli ya Allah تعالی،

وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ

“Wala usifuate matamaniao yao.”

Maana yake: Fikra wanazozindeleza ni kwa kuwa walikengeuka yale Allah تعالی Aliyomteremshia Mtume wake. Kwa sababu hii Allah تعالی Amesema

وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ

“Wala usifuate matamaniao yao.”

Aya inaamrisha: msitoke kwenye ukweli ambao Allah تعالی Amewafaradhisia, Mkafuata utashi wa watu waovu na wajinga. Kauli ya Allah تعالی،

لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَا جَاءَ

“Kila mmoja katika nyinyi Tumemuwekea sharia yake na njia yake.”

Abuu Hatim رضي الله عنهما amepokea kutoka kwa Ibn Abbasi رحمه الله تعالی،

لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً

“Kila mmoja katika nyinyi Tumemuwekea sharia...”

Amesema, maana yake, njia.²

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka Angekufanyeni nyote umma mmoja...”

Hili ni tangazo la jumla kwa mataifa yote likifahamisha Uweza wa Allah تعالی usio na kifani. Iwapo Allah تعالی Akitaka, Atawafanya binadamu wote kufuata dini moja na sharia moja, ambayo haitofutwa kamwe. Allah تعالی Aliamua kila Mtume awe na sharia yake mahsusi, ambayo baadaye hufutwa, sehemu yake yote na sheria ya Mtume atakayefuatia. Baadaye sheria zote ziliizotangulia zilifutwa na sheria aliyomtuma nayo Muhammad ﷺ Mjumbe na mja wake, ambaye Allah تعالی Alimtuma kwa watu wa duniani kama Mtume wa mwisho. Allah تعالی Amesema,

¹ At-Tabari 10:332.

² At-Tabari 10:387.

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَكِنْ لَيَبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka Angekufanyeni nyote umma mmoja, lakini ni Kukujaribuni kwa Aliyokupeni.”

Aya hii ina maana kuwa Allah تعالى Aliweka sheria tofauti ili kuwaita utiifu waja Wake katika kuzifuata sheria hizo. Hivyo Huwalipa au Huwaadhibu kwa mujibu wa amali zao na yale wanayoyadhamiria. Abdullah bin Kathir رحمه الله تعالى alisema kuwa Ayah hii ina maana.

فِي مَا آتَاكُمْ

“Kwa Aliyokupeni.”Maana yake: “Ya Kitabu.” Baadaye, Allah تعالى Anawahimiza kupupia kufanya amali njema.

فَأَسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ

“Basi shindaneni kwa mambo ya kheri.” Ambayo ni kumtii Allah تعالى, kufuata sharia Zake ambazo zilifuta sharia zilizotangulia, na kuamini kitabu Chake, Qur’an, ambacho ni kitabu cha mwisho Alichokiteremsha. Kisha Allah تعالى Amesema,

إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ

“Kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo yenu nyote...”

Kwa hiyo enyi watu, marejeo yenu na kituo chenu cha mwisho ni kwa Allah تعالى siku kiyama.

فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ

“Na Atakuja Kuwaambieni yale mliyokuwa mkikhitalifiana.”

Allah تعالى Atawafahamisheni kuhusu ukweli ambao mlikuwa mkitofautiana na Atawalipa watiifu kama jaza na Atawaadhibu wasioamini. Waasi wanakana ukweli na kufuata njia nyingine bila ushahidi, wakihalalisha matendo yao. Bali wamekana ushahidi uliodhahiri, dalili zisizo na shaka na zilizothibitishwa. Adh-Dhahak alisema kuwa,

فَأَسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ

“Basi shindaneni kwa mambo ya kheri.”

Ilielekezwa kwa Ummah wa Muhammad ﷺ lakini rai ya kwanza ni dhahiri zaidi. Kauli ya Allah تعالى.

وَأَنِ احْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ

“Na wahukumu baina yao kwa aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamano yao.”

Katika hali ya kuifafanua amri hii na kukataza suala la kuipuuza.

وَاحْذَرَهُمْ أُنْ يَفْتِنُوكَ عَنْ بَعْضِ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ إِلَيْكَ

“Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaacha baadhi ya Aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu.”

Muradi wake: Jihadhari na Mayahudi, maadui zenu, wasije kupotosha ukweli katika wanayokuambieni. Kwa hiyo msihadaiwe nao, kwani wao ni waongo, wapotoshaji na makafiri.

فَإِنْ تَوَلَّوْا

“Na wakigeuka,...” Katika hukumu unazozipitisha katika migogoro yao, na kukataa sharia ya Allah تعالى.

فَاعَلِمَ أَنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُصِيبَهُمْ بِبَعْضِ ذُنُوبِهِمْ

“Basi jua kwamba hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao.”

Maana yake: Jua kwamba litajiri kwa mujibu wa Amri ya Allah تعالى na kwa sababu ya Hikima Yake wamekengeuka ukweli, na kwa sababu ya makosa yao yaliyotangulia,

وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ لَفَنَسِفُونَ

“Na hakika wengi wa watu ni wapotofu.”

Kwa hiyo binadamu walio wengi wanamuasi Mola wao. Wanaacha ukweli na wanakuwa mbali nao. Allah تعالى Amesema katika Aya nyengine,

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٥٠﴾

“Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi...” Na,

وَإِنْ تَطَّعَ أَكْثَرُ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

“Na ukiwatii wengi wa walio ardhini watakupoteza mbali na njia ya Mwenyezi Mungu.”

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Kaa'b bin Assad, Ibn Saluba, Abdullah bin Sirya na Shas bin Qays waliambizana, 'Twendeni kwa Muhammad tukajaribu kupotosha katika dini.' Hivyo wakaenda kwa Muhammad ﷺ na wakamuambia, 'Ewe Muhammad unajua kuwa sisi ni wanazuoni, na viongozi wa Mayahudi. Iwapo tutakufuata na Mayahudi watakufuata na hawatapigana nasi. Lakini upo uadui baina yetu na baadhi ya watu wetu, kwa hiyo tutakuletea shauri hilo uwe muamuzi kati yetu lakini uwe upande wetu nasi tutakuamini.' Mtume ﷺ alikataa ahadi ile na Allah تعالى Akateremsha Aya juu yao,

وَأَنْ أَحْكَمَ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ وَاحْذَرْهُمْ أَنْ يَفْتِنُوكَ عَنْ بَعْضِ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ إِلَيْكَ

“Na wahukumu baina yao kwa Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamano yao. Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaacha baadhi ya aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu.”

mpaka

لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ

“Kwa ajili watu wenye yakini.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى¹ na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى waliandika Hadithi hii. Allah تعالى Anaendelea,

أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْتَغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنْ اللَّهِ حُكْمًا لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٥٠﴾

“Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliyemwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?”

Allah تعالى Anawachagiza wale wanaopuuza amri za Allah تعالى, ambazo zinajumuisha kila aina ya amali njema na kukataza kila aina ya uovu, lakini wanarejea kwenye maoni, utashi na desturi walizobuni watu wenyewe, yote hayo hayana misingi katika Dini ya Allah تعالى. Katika zama za Jahiliyyah, watu walikuwa wakifuata upotofu wa ujinga walioubuni kwa mawazo na hawaa. Tatar (Mongolis) walifuata sheria walizorithi kutoka kwa Mfalme wao Gengis Khan aliyewaandikia Al-Yasaq. Kitabu chenye sheria zilizotokana na dini mbalimbali kama vile Uyahudi, Ukristo na Uislamu. Sheria nyingi zilitokana

¹ At-Tabari 10:393.

na maoni na utashi wake. Baadaye, sharia hizo zilifuatwa na watoto wake, wakizipendelea kuliko sheria za kitabu cha Allah تعالى na Sunnah ya Mjumbe Wake.

Hivyo, anayefanya hivyo, ni kafiri anayestahili kupigwa vita, mpaka atakaporejea kwa Allah تعالى na Mjumbe Wake, hivyo hapana sharia iwe ndogo au kubwa itakayo rejelewa kwa isiyokuwa Sharia Yake. Allah تعالى Amesema,

أَفْحَكَمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَتْفُونَ^١

“Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya?”

Maana yake: Wanapendelea haya na kudharau hukumu ya Allah تعالى.

وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِقَوْمٍ يُوفُونَ^٢

“Na nani aliyemwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?”

Nani aliye muadilifu zaidi katika maamuzi zaidi ya Allah تعالى kwa wale wanaolewa sharia ya Allah تعالى, ambao wana uhakika kuwa Allah تعالى ni Mbora zaidi miongoni mwa wale wanaotoa maamuzi na kuwa Yeye ni Mwenye Huruma zaidi kwa viumbe Wake kuliko mama na watoto wake? Allah تعالى Anajua kila kitu kwa uhakika, ni Muweza wa kufanya kila kitu, na Yeye ni Muadilifu katika mambo yote.

Al-Hafiz Abu Al-Qasim At-Tabarani رحمه الله تعالى aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَبْغَضُ النَّاسِ إِلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ، مَنْ يَبْتَغِي فِيهِ الْإِسْلَامَ سُنَّةَ الْجَاهِلِيَّةِ، وَطَالِبُ دَمِ
امْرِئٍ بِغَيْرِ حَقٍّ لِيُرِيَقَ دَمَهُ»

“Mtu anayechukiza zaidi kwa Allah ni Muislamu anayefuata njia za Jahiliya na yule anayependa kumwaga damu ya mtu bila ya haki.”¹

Al-Bukhari alirekodi kuwa Abu Al-Yaman alisimulia Hadithi sawa na hiyo yenye nyongeza.²

¹ At-Tabarani 10:374

² Fat'hul Al-Bari 12:219.

* يَتَّيِبُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصْرَىٰ أَوْلِيَاءَ ۚ
 بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ
 اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٥١﴾ فَتَرَى الَّذِينَ فِي
 قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يُسْرِعُونَ فِيهِمْ يَقُولُونَ خَشْيَ أَنْ تُصِيبَنَا
 دَآئِرَةٌ ۗ فَعَسَىٰ اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَ بِالْفَتْحِ أَوْ أَمْرٍ مِّنْ عِنْدِهِ
 فَيُضْبِحُوا عَلَىٰ مَا أَسْرُوا فِي أَنفُسِهِمْ نَادِمِينَ ﴿٥٢﴾
 وَيَقُولُ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَهْتُولَاءِ الَّذِينَ أَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ
 أَيْمَانِهِمْ ۗ إِنَّهُمْ لَمَعَكُمْ ۗ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فَأَصْبَحُوا خَسِيرِينَ
 ﴿٥٣﴾ يَتَّيِبُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَن يَرْتَدَّ مِنكُمْ عَن دِينِهِ
 فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ حَسْبِهِمْ وَيُخَيِّبُونَهُمْ أَذًى عَلَى الْمُؤْمِنِينَ
 أَعِزَّةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ
 لَوْمَةَ لَآئِمٍ ۗ ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ وَاسِعٌ
 عَلِيمٌ ﴿٥٤﴾ إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا الَّذِينَ
 يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ ﴿٥٥﴾ وَمَنْ
 يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ
 الْغَالِبُونَ ﴿٥٦﴾ يَتَّيِبُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ
 اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُزُوعًا وَلَعِبًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ
 قَبْلِكُمْ وَالْكَافِرَ أَوْلِيَاءَ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ كُفْرَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾
 وَإِذَا نَادَيْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ اتَّخَذُوهَا هُزُوعًا وَلَعِبًا ۗ ذَٰلِكَ
 بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٥٨﴾

* يَتَّيِبُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ
 وَالنَّصْرَىٰ أَوْلِيَاءَ ۚ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ
 ۚ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٥١﴾ فَتَرَى
 الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يُسْرِعُونَ
 فِيهِمْ يَقُولُونَ خَشْيَ أَنْ تُصِيبَنَا
 دَآئِرَةٌ ۗ فَعَسَىٰ اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَ بِالْفَتْحِ أَوْ أَمْرٍ مِّنْ
 عِنْدِهِ فَيُضْبِحُوا عَلَىٰ مَا أَسْرُوا فِي
 أَنفُسِهِمْ نَادِمِينَ ﴿٥٢﴾ وَيَقُولُ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا أَهْتُولَاءِ الَّذِينَ أَقْسَمُوا بِاللَّهِ
 جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ ۗ إِنَّهُمْ لَمَعَكُمْ ۗ حَبِطَتْ
 أَعْمَالُهُمْ فَأَصْبَحُوا خَسِيرِينَ ﴿٥٣﴾

**51. Enyi mlio amini!
 Msiwafanye Mayahudi na
 Wakristo kuwa ni marafiki.
 Wao ni marafiki wao kwa
 wao. Na miongoni mwenu
 mwenye kufanya urafiki
 nao, basi huyo ni katika
 wao. Hakika Mwenyezi
 Mungu Hawaongoi watu
 wenye kudhulumu.**

**52. Utawaona wale wenye
 maradhi nyoyoni mwao
 wanakimbilia kwao waki-**

sema: Tunakhofu yasisibu mabadiliko. Huenda Mwenyezi Mungu Akaleta ushindi au jambo jingine litokalo Kwake wakawa wenye kujuta kwa waliyoficha katika nafsi zao.

53. Na walioamini watasema: Hivyo hawa ndio wale walioapa ukomo wa viapo vyao kuwa wao wa pamoja nanyi? Vitendo vyao vitapotea bure, na wataamkia kuwa wenye kukhasirika.

Kuharamishwa Kuwafanya Mayahudi, Wakristo na Maadui wa Uislamu kuwa Marafiki:

Allah تعالیٰ Anawazuia waja wake waumini kutowafanya marafiki Mayahudi na Wakristo kwa sababu ni maadui wa Uislamu na Waislamu, Allah تعالیٰ Awalaani. Kisha Akaeleza kuwa ni marafiki wao kwa wao na Anawaonya wanaofanya hivyo,

وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ

“Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao.”

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Umar رضي الله عنه alimuamrisha Abu Musa Al-Ashari رضي الله عنه ampelekee Ankara inayoonesha alichochukua na alichotumia. Abu Musa رضي الله عنه wakati huo alikuwa na Karani Mkristo, na hivyo akaweza kutimiza matakwa ya Umar رضي الله عنه. Umar رضي الله عنه alipenda alichooona na akasema, ‘Karani huyu ni makini. Utatusomea hapa Msikitini barua iliyotufikia kutoka Sham?’ Abu Musa رضي الله عنه akasema: ‘Lakini karani wangu hatuingia msikitini.’ Umar رضي الله عنه akasema, “Kwani si tohara?” Abu Musa رضي الله عنه akasema, “Hapana, ila yeye ni Mkristo.” Abu Musa رضي الله عنه akasema, “Hivyo, Umar رضي الله عنه akanishutumumu na akanipiga katika mapaja yangu, huku akisema, “Mtoe nje (ya Al-Madinah).” Kisha akasoma,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ

“Enyi mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki.”¹

Kisha alitoa taarifa kuwa Abdullah bin Utbah alisema, “Kila mmoja wenu achukue tahadhari kuwa anaweza kuwa Yahudi au Mkristo, bila kutambua.” Msimulizi wa kisa hiki alisema, “Tulidhani kuwa alikuwa anarejea Aya

¹ Ad-Dur Al-Manthur 3:100.

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ

“Enyi mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki.”¹ Allah تعالى Alisema,

فَتَرَى الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ

“Utawaona wale wenye maradhi nyoyoni mwao...”

Ugonjwa wa wasiwasi, kusita na unafiki

يُسْرِعُونَ فِيهِمْ

“Wanakimbilia kwao...” Maana: Wanapupia kuwafanya marafiki na wenza katika faragha na hadharani,

يَقُولُونَ خَشْيَةَ أَنْ تُصِيبَنَا دَآئِرَةٌ

“...wakisema: Tunakhofu yasitusibu mabadiliko.”

Hivyo wanatoa udhuru huu kwa urafiki wao na utiifu wao kwa makafiri, huku wakisema kuwa wanachelea kuwa makafiri wanaweza kuwapiga Waislamu, hivyo wanataka fadhila za Mayahudi na Wakristo ili watumie hisani yao, kwa manufaa yao. Hivyo Allah تعالى Alijibu,

فَعَسَىٰ أَلَّهُ أَنْ يَأْتِيَ بِالْفَتْحِ

“Huenda Mwenyezi Mungu Akaleta ushindi...” Akikusudia kutekwa kwa Makkah kwa mujibu wa As-Suddi.²

أَوْ أَمْرٍ مِّنْ عِنْدِهِ

“...au jambo jingine litokalo Kwake...” kuwataka Mayahudi na Wakristo kulipa Jizyah kama alivyoeleza As-Suddi.

فَيُصِصِحُوا

“...wakawa...” Maana: Wanafiki waliofanya urafiki na Mayahudi na Wakristo watakuwa,

عَلَىٰ مَا أَسْرُوا فِي أَنْفُسِهِمْ

“Wenye kujuta kwa waliyoyaficha katika nafsi zao.”

¹ Ibn Abu Hatim: 4:1156.

² At-Tabari 10:405.

تَنْذِيرَاتٍ

“...wenye kujuta...” Kwa ushuba wao na Mayahudi na Wakristo ambao haukuwafaa wala kuwalinda na madhara yoyote, si chochote bali madhara, kama Allah تعالى Alivyodhihirisha uhalisi wao kwa Waja Wake watiifu hapa duniani, japokuwa walijaribu kuuficha. Unafiki wao ulipoanza kuonekana dhidi yao, kadhia yao ikawa wazi kwa waja watiifu wa Allah تعالى. Waumini wakashangazwa na wanafiki hao waliojifanya waumini, wakila viapo vya uaminifu, hata hivyo madai yao yalikuwa uongo na uzandiki. Ndio maana Allah تعالى Akasema,

وَيَقُولُ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَهْتُوا لِمَا الَّذِينَ أَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ ۖ إِنَّهُمْ لَمَعَكُمْ ۚ حَبِطَتْ
أَعْمَالُهُمْ فَأَصْبَحُوا خَسِرِينَ ﴿٥٨﴾

“Na walioamini watasema: Hivyo hawa ndio wale walioapa ukomo wa viapo vyao kuwa wao wa pamoja nanyi? Vitendo vyao vitapotea bure, na wataamkia kuwa wenye kukhasirika.”

Sababu ya Kuteremka Aya

Muhammad bin Is'haq رحمه الله تعالى amesema: kabila la Kiyahudi la Banuu Qainukaa, ndio lilikuwa la kwanza kuvunja makubaliano kati ya Mtume ﷺ na wao. Asim amenisimulia kutoka kwa bin Umar رضي الله عنه kutoka kwa Qatada رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ akawatia kizuizini hadi wakasalimu amri. Hivyo, Abdillahi bin Ubayyi bin Saluli alisimama na kumuwendea Mtume ﷺ. Akasema: ‘Ewe Muhammad: Nakuomba ufanye hisani kwa washirika wangu Banuu Qainukaa, walikuwa huko nyuma ni washirika wa kabila la Khazraji.’ Mtume ﷺ hilo akaliona ni jambo zito, hivyo akasita kufanya maamuzi ya haraka, Abdullah bin Ubayyi bin Saluli akasema: ‘Nakuomba uwaachie huru washirika wangu.’ Mtume ﷺ akapinga kufanya hivyo. Hivyo Bin Salul akaingiza mkono wake katika nguo za Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akamuambia “Naomba uniachie!” Mtume ﷺ alikasirika hadi alama za mikunjo ya uso wake ikaonekana. Kisha akasema: “Tafadhali naomba uniachie!” Bin Salul akasema: “Naapa sikuachii hadi uwaachie washirika wangu ambao idadi yao ni (400) na diraya zao (300). Hakika wao walinihami na shari ya watu wekundu na weusi. Yaani hivi hivi tu. Mara moja unawafilisi? Hakika mimi ni mtu ninayehofia siku mambo yanaweza

geuka yakawa upande wangu.” Hivyo, Mtume ﷺ akasema: “Nimewaachia washirika wako”. Muhammad bin Is’haq رحمه الله تعالى amesema; Abuu Is’haq bin Yasaar amenisimulia kutoka kwa Ubada bin Walid bin Ubada bin Swamiti رضي الله عنه, kuwa amesema: Wakati Banuu Qainukaa walipompiga vita Mtume ﷺ. Bin Salul aliungana nao. Ama Ubada bin Samit رضي الله عنه alikuwa kinyume na wao. Alikuwa yeye ni sehemu ya Banuu Awf katika kabila la Khazraji ambao walikuwa na ushiriki na Banuu Qainukaa. Hivyo Ubada رضي الله عنه alienda kwa Mtume ﷺ akajivua na ushirika wao. Na akafadhilisha upande wa Allah تعالى na Mtume wake kuliko ushirika wao. Akasema: ‘Ewe Mtume ﷺ, mimi nipo pamoja na Allah تعالى na Mtume wake ﷺ na ninakana ushirika wao.” Hivyo, na Ubada bin Saamit رضي الله عنه na Abdillah bin Ubayy Aya hii ndio ikashuka katika Sura ya Maida.

﴿ يَتَّيِبُهُمُ اللَّهُ وَيُؤْتِيهِمُ اللَّهُ أَجْرًا كَثِيرًا ۖ وَلِيُخَيِّبَ اللَّهُ الْقَوْمَ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ۝٥١﴾

“Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao.” (5:51) Mpaka

﴿ وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْغَالِبُونَ ۝٥٢﴾

“Na atakayefanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda.” (5:56)¹

﴿ يَتَّيِبُهُمُ اللَّهُ وَيُؤْتِيهِمُ اللَّهُ أَجْرًا كَثِيرًا ۖ وَلِيُخَيِّبَ اللَّهُ الْقَوْمَ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ۝٥١﴾
 ﴿ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعْرَاجٌ عَلَى الْكٰفِرِينَ مُجْنَهْدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ ۚ ۝٥٢﴾
 ﴿ ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ۝٥٣﴾
 ﴿ إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ ۝٥٤﴾
 ﴿ وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْغَالِبُونَ ۝٥٥﴾

54. Enyi mlioamini! Atakayeiacha miongoni mwenu Dini yake, basi Mwenyezi Mungu Atakujaleta watu anaowapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa Waumini na wenye nguvu juu ya makafiri, wanapigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu,

¹ Ibn Hisham 3:52.

wala hawaogopi lawama ya anayelaumu. Hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu, Humpa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu na Mwenye kujua.

55. Hakika rafiki yenu mlinzi ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini, ambao hushika Sala na hutoa Zaka, nao wananyenyekea.

56. Na atakayefanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda.

Miongoni mwa Sifa za Wapenzi wa Allah تعالی na Anayewapinga wao Miongoni mwa Wanafiki.

Allah تعالی Anatilia mkazo Uwezo Wake Mkubwa na Anaeleza kuwa yeyote anayeacha kuitetea Dini Yake na kusimamisha Sharia Yake, basi Allah تعالی Ataleta badala yao ambao ni bora zaidi, wenye nguvu zaidi na waadilifu zaidi kwa Dini ya Allah تعالی na Sharia. Allah تعالی Amesema katika Aya nyingine,

وَإِن تَتَوَلَّوْا يَسْتَبَدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَلَكُمْ

“Na mkigeuka Atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi.” (47:38) na

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ ۚ إِنَّ يَشَأُ يَذْهَبِكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٩﴾
وَمَا ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ ﴿٢٠﴾

“Huoni kuwa Mwenyezi Mungu Ameziumba mbingu na ardhi kwa Haki? Akitaka Atakuondoeni na Alete viumbe wapya! Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si jambo gumu.” (14:19-20)

Kwa hakika hili sio muhali au gumu kwa Allah تعالی . Allah تعالی Anasema hapa,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَن يَرْتَدَّ مِنكُمْ عَن دِينِهِ

“Enyi mlio amini! Atakayeiacha miongoni mwenu Dini yake,...”

Na anauacha ukweli na kufuata upotofu, kuanzia sasa mpaka mwanzo wa Kiama. Kauli ya Allah تعالی ,

أَذِلَّةٌ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ

“...wanyenyekvu kwa Waumini na wenye nguvu juu ya makafiri...”

Hizi ndizo sifa za waumini kwa kuwa wanyenyekvu kwa ndugu zao na washirika wao, wakali kwa adui zao na mahasimu wao. Katika Aya, Allah تعالى Amesema,

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ ؑ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ

“Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao.”

تُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا تَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ ؑ

“...wanapigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anayelaumu.”

Hapana kinachowazuia kumtii Allah تعالى, kusimamisha Sharia Yake, kuwapiga maadui Zake, kuamrisha mema na kukataza maovu. Kwa hakika, hapana kinachowazuia kufuata njia hii, wala anayekusudia kuwazuia, kuwalaumu au kuwashutumumu. Imam Ahmad alirekodi kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema, “*Khalil Wangu* (rafiki mwandani, Mjumbe) ameniamrisha kufanya mambo saba. Aliniamrisha kuwapenda masikini na kuwa karibu nao. Aliniamrisha kuwaangalia walio chini yangu na si walio juu yangu. Aliniamrisha kuendeleza udugu wa kuzaliwa, hata kama wataukata. Aliamrisha kutomuomba mtu kitu, kusema kweli hata kama ni chungu, na kutoogopa lawama ya yeyote kwa ajili ya Allah تعالى. Aliniamrisha kila mara kusema, “*La hawla wa Quwwata illa billah* (Hapana nguvu au uwezo isipokuwa kutoka kwa Allah تعالى), kwa kuwa maneno haya ni hazina chini ya Arshi (ya Allah تعالى).”¹ Imethibitishwa ndani ya Sahih,

«مَا يَنْبَغِي لِلْمُؤْمِنِ أَنْ يُذِلَّ نَفْسَهُ»

“Muumini hatakiwi kujidhuru mwenyewe.” Akaulizwa; “Inakuwaje mtu kujidhuru mwenyewe, Ewe Mjumbe wa Allah?” Hivyo yeye alijibu,

«يَتَحَمَّلُ مِنَ الْبَلَاءِ مَا لَا يُطِيقُ»

“Anajibebesha mizigo asiyoimudu.”²

¹ Ahmad 5:405, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:531, na Ibn Majah 2:1332.

² Ahmad 5:159.

ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ

“Hiyo ndiyo Fadhila ya Mwenyezi Mungu, Humpa Amtakaye.”

Maana yake: Wote wenye sifa hizi, wanazipata kwa fadhila na ihsani ya Allah تعالى na kwa sababu Aliwapa sifa hizi.

وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu na Mwenye kujua.” Fadhila Zake hazina kikomo, na Anajua Wale wanaostahili au wasiostahili Fadhila na Ukarimu Wake. Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا

“Hakika rafiki yenu na Mlinzi ni Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na walioamini.”

Maana yake: Mayahudi sio rafiki zako. Bali, utii wako ni kwa Allah تعالى, Mjumbe Wake na waumini waaminifu.

الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ

“...ambao hushika Sala na hutoa Zaka nao wananyenyekea.”

Inakusudiwa waumini ambao wana sifa hizi na wanasimamisha Sala, ambayo ni moja ya nguzo muhimu za Uislamu, ambayo inahusisha kumuabudu Allah تعالى Pekee bila washirika. Wanatoa Zakah, ambayo ni haki ya viumbe na aina ya msaada kwa wahitaji na masikini. Ama kwa Kauli ya Allah تعالى,

وَهُمْ رَاكِعُونَ

“...nao wananyenyekea.” Maana yake: Wanahudhuria Sala za jamaa Msikitini na wanatumia kwa njia ya sadaka kwa kukidhi haja mbalimbali za Waislamu.

Sababu ya Kushuka Aya hizi.

Imetangulia huko nyuma kuwa Aya hizi zilishuka kwa Ubada bin Saamit رضي الله عنه. Wakati alipoukana ushirika wa Kiyahudi, na akaridhia ushirika wa Allah تعالى na Mtume Wake na waumini. Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema baada ya yote haya. Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُغْلِبُونَ ﴿٥٦﴾

“Na atakayefanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walioamini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda.” (5:56)

Pia Allah تعالى Amesema,

كَتَبَ اللَّهُ لِلَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ أَنْ يَتَذَكَّرُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَأَنْ يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أُولَئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُمْ بِرُوحٍ مِنْهُ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ أُولَئِكَ حِزْبُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥٧﴾

“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda. Huwakuti watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao Ameandika katika nyoyo zao Imani, na Amewapa nguvu kwa Roho itokayo Kwake. Na Atawaingiza katika bustani yapitayo mito kati yake. Humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu Awe radhi nao, na wao wawe radhi Naye. Hao ndio Hizbullahi, Kundi la Mwenyezi Mungu. Hakika Kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufanikiwa.”

Hivyo, wanaoridhia twaa ya Allah تعالى – Mjumbe Wake ﷺ na waumini Wake waaminifu – watafanikiwa duniani na Akhera.

Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema;

وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُغْلِبُونَ ﴿٥٦﴾

“Na atakayefanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na walioamini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda.”

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُزُؤًا وَلَعِبًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا
 الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَالْكَفَّارَ أَوْلِيَاءَ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ كُنتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾ وَإِذَا نَادَيْتُمْ إِلَى
 الصَّلَاةِ اتَّخَذُوهَا هُزُؤًا وَلَعِبًا ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٥٨﴾

57. Enyi mlioamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia kejeli na mchezo Dini yenu miongoni mwa waliopewa Kitabu kabla yenu, na makafiri wengine. Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini.

58. Na mnapoadhinia Sala wao wanaichukulia maskhara na mchezo. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.

Kuharamishwa Kuwafanya Marafiki Makafiri:

Ayah hii inazuia na kukataza kufanya urafiki na maadui wa Uislamu na watu wake, kama vile Watu wa Kitabu na washirikina. Makafiri hawa wanafanyia istihizai matendo muhimu ambayo yatatendwa na mtu, matukufu, matendo safi ya Uislamu ambayo ni pamoja na yote mazuri ya duniani na Akhera. Wanavifanyia masikhara vitendo hivyo na wanafanya ni mambo ya mchezo na istihzai, kwa sababu vitendo hivyo wanafikiri ni mchezo katika mtazamo wao potofu na fikra zao zilizovia. Allah تعالى Amesema,

مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَالْكَفَّارَ

“...miongoni mwa waliopewa Kitabu kabla yenu, na makafiri wengine.”

Hii ni kuweka wazi ubainifu na ufafanuzi. Kama Allah تعالى Alivyosema,

فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ

“Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu,...” 22:30

لَا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُزُؤًا وَلَعِبًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ

“Msiwafanye marafiki wale walioifanyia kejeli na mchezo Dini yenu miongoni mwa waliopewa Kitabu kabla yenu,...”

Kadhhalika maana haya yamejiri katika usomaji wa Ibin Masoud رضي الله عنهما kwa mujibu wa simulizi ya Ibn Jariri رحمه الله تعالى:

(لَا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُزُؤًا وَلَعِبًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ
وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا)

“Msiwafanye marafiki wale walioifanyia kejeli na mchezo dini yenu miongoni mwa waliopewa kitabu kabla yenu na washirikina.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ كُنتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini.”

Ina maana, mche Allah تعالى na usiwafanye marafiki maadui zenu na wa Dini yenu, kama kweli mnaamini Sharia za Allah تعالى na Dini Yake, ambayo waliifanyia Istihizai na mchezo.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine.

لَا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِن دُونِ الْمُؤْمِنِينَ وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ
اللَّهِ فِي شَيْءٍ إِلَّا أَن تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقَنَّةً وَيُحَذِّرْكُمْ اللَّهُ نَفْسَهُ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٥٦﴾

“Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.

Makafiri Wanakebehi Sala na Adhana:

Allah تعالى Amesema،

وَإِذَا نَادَيْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ اتَّخَذُوهَا هُزُؤًا وَلَعِبًا

“Na mnapoadhini kwa ajili ya Sala wao wanaichukulia maskhara na mchezo.”

¹ At-Tabari 10:430.

Mnaponadi Adhana kwa ajili ya Sala, ambacho ni kitendo kizuri, kwa wale wenye akili timamu na mazingatio mazuri,

أَتَّخِذُوهَا

“...wao wanaichukulia...” pia

هُزُؤًا وَلَعِبًا ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ

“...maskhara na mchezo. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.”

Kwa maana hufanya masihara katika ibada na Sharia za Allah تعالى. Hizi ni sifa za wafuasi wa shetani ambao, pindi mmoja wao:

«إِذَا سَمِعَ الْأَذَانَ أَدْبَرَ وَلَهُ حُصَاصٌ، أَيْ صُرَاطًا، حَتَّى لَا يَسْمَعَ التَّأْدِينَ فَإِذَا قُضِيَ التَّأْدِينُ، أَقْبَلَ فَإِذَا تَوَبَّ لِلصَّلَاةِ أَدْبَرَ، فَإِذَا قُضِيَ التَّوْبُّ أَقْبَلَ حَتَّى يَخْطُرَ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ، فَيَقُولُ: اذْكَرُ كَذَا اذْكَرُ كَذَا، لِمَا لَمْ يَكُنْ يَذْكَرُ حَتَّى يَظَلَّ الرَّجُلُ لَا يَدْرِي كَمْ صَلَّى، فَإِذَا وَجَدَ أَحَدَكُمْ ذَٰلِكَ، فَلْيَسْجُدْ سَجْدَتَيْنِ قَبْلَ السَّلَامِ»

“Anaposikia Adhana, shetani hukimbia na kutoa upepo ili asisikie Adhana. Adhana ikimalizika hurejea, na Iqama ikisomwa, shetani hukimbia tena. Iqama ikisha hurudi tena na hujaribu kupenya katika mawazo ya mtu na anasema, ‘Kumbuka hili na lile, ambalo hakulifikiria kabla ya Sala, mpaka anayesali kutojua raka alizo sali. Iwapo mmoja wenu hatokumbuka, basi ataleta sijda sahu kabla ya kutoa salamu.”¹

Hadithi hii imekubaliwa. Az-Zuhri alisema “Allah تعالى Ametaja Adhana ndani ya Kitabu Chake,

وَإِذَا نَادَيْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ اتَّخِذُوهَا هُزُؤًا وَلَعِبًا ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٥١﴾

“Na mnapoadhini kwa ajili ya Sala wao wanaichukulia maskhara na mchezo. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.”

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alirekodi kauli hii,²

¹ Al-Bukhari na. 608, 1222, 1231 na Muslim 1:291, 398.

² Ibn Abi Hatim 4:1164.

قُلْ يَا هَلْ أَكْتَسِبَ هَلْ تَنْقِمُونَ مِنَّا إِلَّا أَنْ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا
 أَنْزَلَ إِلَيْنَا وَمَا أَنْزَلَ مِن قَبْلُ وَأَنْ أَكْثَرْتُمْ فَنَسِقُونَ ﴿٥٩﴾ قُلْ
 هَلْ أَنْبِئُكُمْ بِشَرِّ مِمَّنْ ذَلِكَ مَثُوبَةٌ عِنْدَ اللَّهِ مَنْ لَعَنَهُ اللَّهُ
 وَعَظِبَ عَلَيْهِ وَجَعَلَ مِنْهُمْ الْفِرْدَةَ وَالْحَتَّازِيرَ وَعَبَدَ
 الطُّبُغُوتَ^٤ أُولَئِكَ شَرٌّ مَكَانًا وَأَضَلُّ عَن سَوَاءِ السَّبِيلِ ﴿٦٠﴾
 وَإِذَا جَاءُوكُمْ قَالُوا ءَامَنَّا وَقَدْ دَخَلُوا بِالْكَفْرِ وَهُمْ قَدْ
 خَرَجُوا بِهِ^٥ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا كَانُوا يَكْتُمُونَ ﴿٦١﴾ وَتَرَى
 كَثِيرًا مِّنْهُمْ يُسْرِعُونَ فِي الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَأَكْلِهِمْ
 الشُّحْتَ^٦ لَيْسَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٦٢﴾ لَوْلَا يَنْهَاهُمْ
 الرَّبِّيْبِيُّونَ وَالْأَحْبَابُ^٧ عَن قَوْلِهِمُ الْإِثْمَ وَأَكْلِهِمُ الشُّحْتَ^٨
 لَيْسَ مَا كَانُوا يَصْنَعُونَ ﴿٦٣﴾

59. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Hivyo mnatuchukia kwa kuwa tumemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyo teremshiwa na yaliyoteremshwa kabla, na kwa kuwa wengi katika nyinyi ni wapotofu?

60. Sema: Je! Nikuwambieni yule ambaye ni mwenye malipo mabaya zaidi kuliko hayo mbele ya Mwenyezi Mungu? Ni yule ambaye Mwenyezi Mungu Amemlaani na Amemka-sirikia, na Amewafanya miongoni mwao manyani na nguruwe, na wakamuabudu Shetani. Hao ndio wenye mahali pabaya na wamepotea zaidi njia iliyo sawa.

قُلْ يَا هَلْ أَكْتَسِبَ هَلْ تَنْقِمُونَ مِنَّا
 إِلَّا أَنْ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أَنْزَلَ إِلَيْنَا وَمَا
 أَنْزَلَ مِن قَبْلُ وَأَنْ أَكْثَرْتُمْ فَنَسِقُونَ
 ﴿٥٩﴾ قُلْ هَلْ أَنْبِئُكُمْ بِشَرِّ مِمَّنْ ذَلِكَ
 مَثُوبَةٌ عِنْدَ اللَّهِ مَنْ لَعَنَهُ اللَّهُ
 وَعَظِبَ عَلَيْهِ وَجَعَلَ مِنْهُمْ الْفِرْدَةَ
 وَالْحَتَّازِيرَ وَعَبَدَ الطُّبُغُوتَ^٤ أُولَئِكَ
 شَرٌّ مَكَانًا وَأَضَلُّ عَن سَوَاءِ السَّبِيلِ
 ﴿٦٠﴾ وَإِذَا جَاءُوكُمْ قَالُوا ءَامَنَّا وَقَدْ
 دَخَلُوا بِالْكَفْرِ وَهُمْ قَدْ خَرَجُوا بِهِ^٥
 وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا كَانُوا يَكْتُمُونَ ﴿٦١﴾
 وَتَرَى كَثِيرًا مِّنْهُمْ يُسْرِعُونَ فِي الْإِثْمِ
 وَالْعُدْوَانِ وَأَكْلِهِمْ الشُّحْتَ^٦
 لَيْسَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٦٢﴾
 لَوْلَا يَنْهَاهُمْ الرَّبِّيْبِيُّونَ وَالْأَحْبَابُ
 عَن قَوْلِهِمُ الْإِثْمَ وَأَكْلِهِمْ الشُّحْتَ^٨
 لَيْسَ مَا كَانُوا يَصْنَعُونَ ﴿٦٣﴾

61. Na wanapokujieni husema: Tumeamini. Lakini hakika wao wameingia na ukafiri wao, na wametoka nao pia. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi kabisa wa yote wanayoyaficha.

62. Na utawaona wengi katika wao wanakimbilia kwenye dhambi, na uadui, na ulaji wao vya haramu. Ni maovu mno hayo wayatendayo!

63. Mbona hao wanazuoni na makuhani wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi, na ulaji wao vya haramu? Ni maovu mno hayo wayafanyayo!

Watu wa Kitabu Wanawachukia Waumini kwa Sababu ya Kumuamini Allah
تعالى.

Allah تعالى Anaamrisha: “Sema Ewe Muhammad, kuwaambia wanaodhihaki na kuicheza shere Dini yako miongoni mwa watu waliopewa Kitabu.”

هَلْ تَنْقِمُونَ مِنَّا إِلَّا أَنْ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْنَا وَمَا أُنزِلَ مِن قَبْلُ

“Hivyo mnatuchukia kwa kuwa tumemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyoteremshiwa na yaliyoteremshwa kabla,...”

Je, unayo lawama juu yetu zaidi ya hizi? Hii kwa hakika sio sababu ya lawama.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyengine.

وَمَا نَقْمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَنْ يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٨٥﴾

“Nao hawakuona baya lolote kwao ila kuwa wakimuamini Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Msifiwa.” (85:8)

Na Allah تعالى Amesema:

وَمَا نَقْمُوا إِلَّا أَنْ أَغْتَابَهُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ مِن فَضْلِهِ ۗ

“Na hawakuchukia ila kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake Amewatajirisha kutokana na Fadhila Zake.” (9:74)

Ni Hadithi iliyokubaliwa na wengi. Mtume ﷺ alisema,

«مَا يَنْفَعُ ابْنَ جَبِيلٍ إِلَّا أَنْ كَانَ فَاقِرًا فَاتَّعَاهُ اللَّهُ»

“Ni jambo gani lililomfanya Ibn Jamil kukataa kutoa Zakat japokuwa alikuwa masikini na Allah Akamfanya tajiri?”¹

Kauli ya Allah تعالى، وَأَنْ أَكْثَرُكُمْ فَاسِقُونَ

“Na kwa kuwa wengi katika nyinyi ni wapotofu?”

Imeunganishwa na,

أَنْ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْنَا وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلُ

“...kwa kuwa tumemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyoteremshiwa na yaliyoteremshwa kabla...”

Kwa hiyo maana ya sehemu hii ya Ayah ni: Pia tunaamini wengi wenu ni waasi na mmekengeuka kutoka njia iliyonyooka.

Watu wa Kitabu Wanastahili Adhabu Kali Siku ya Kufufuliwa:

Allah تعالى Amesema,

قُلْ هَلْ أَنْتُمْ بِشَرٍّ مِنْ ذَلِكَ مَثُوبَةً عِنْدَ اللَّهِ

“Sema: Je! Nikuwambieni yule ambaye ni mwenye malipo mabaya zaidi kuliko hayo mbele ya Mwenyezi Mungu?”

Aya inamuamuru Mtume ﷺ asema: Je, nikupeni taarifa ya watu waovu mbele ya Allah تعالى siku ya Kiyama kuliko unavyotudhania sisi? Nyie mna sifa bainifu hizi,

مَنْ لَعَنَهُ اللَّهُ

“...Ni yule ambaye Mwenyezi Mungu Amemlaani...”

Wameepushwa mbali na Rehema Zake.

وَعَضِبَ عَلَيْهِ

“...na Amemkasirikia...”

Na hasira baada ya hapo, Hatokuwa radhi naye.

¹ Fat'hul Al-Bari 3:388, Muslim 2:676.

وَجَعَلَ مِنْهُمْ الْقِرَدَةَ وَالْخَنَازِيرَ

“...na Amewafanya miongoni mwao manyani na nguruwe...”

Kama tulivyotaja ndani ya Surat Al-Baqarah (2) na kama tutakavyo taja katika Surat Al-Araf (7). Sufyan Ath-Thawria رحمه الله تعالى lisimulia kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ aliulizwa iwapo kima na nguruwe wa leo ndio wale Allah تعالى Aliowabadilisha.” Akasema,

«إِنَّ اللَّهَ لَمْ يَهْلِكْ قَوْمًا، أَوْ لَمْ يَمْسَخْ قَوْمًا فَيَجْعَلْ لَهُمْ نَسْلًا وَلَا عَقِبًا، وَإِنَّ الْقِرَدَةَ وَالْخَنَازِيرَ كَانَتْ قَبْلَ ذَلِكَ»

“Allah Hajapata Kuwaangamiza watu kwa Kuwabadilisha na vizazi vingine. Kima na nguruwe walikuwepo kabla ya hapo.”¹

Hadithi iliandikwa pia na Muslim,²

Allah تعالى Amesema,

وَعَبَدَ الطَّغُوتَ

“...na wakamuabudu Shetani.”

Na Akajaalia wanamtumikia shetani. Maana ya Ayah ni: ‘Nye, Enyi Watu wa Kitabu, mliofanyia utani Dini yetu, ambayo ina Tawhid ya Allah تعالى, na kumpwekesha Yeye katika kumuabudu bila kumshirikisha, vipi mnaweza kutufanyia mzaha ambapo hizi ndio sifa zenu?’

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

أُولَئِكَ شَرٌّ مَكَانًا

“...Hao ndio wenye mahali pabaya...”

Kuliko hivyo wanavyotudhania sisi,

وَأَضَلُّ عَنْ سَوَاءِ السَّبِيلِ

“...na wamepotea zaidi njia iliyo sawa.”

¹ Mishkat Al-Athar 4:275.

² Muslim 4:2051.

Zaidi, katika Ayah haina maana kuwa kundi jingine halijapotoka mno, lakini ina maana kuwa Watu wa Kitabu wamepotea sana. Katika Aya nyingine, Allah تعالی Amesema,

أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقَرًّا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا ﴿٥٩﴾

“Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makaazi bora na mahali penye starehe nzuri.”

Wanafiki Wanajifanya Waumini Lakini Wanaficha Ukafiri Wao:

Allah تعالی Amesema,

وَإِذَا جَاءُوكُمْ قَالُوا ءَامَنَّا وَقَدْ دَخَلُوا بِالْكَفْرِ وَهُمْ قَدْ خَرَجُوا بِهِ^ع

“Na wanapokujieni husema: Tumeamini. Lakini hakika wao wameingia na ukafiri wao, na wametoka nao pia.”

Hii ni sifa bainifu ya wanafiki, kwani wanajifanya waumini ambapo mioyo yao inaficha Kufuru. Hivyo Allah تعالی Amesema,

وَقَدْ دَخَلُوا

“...wao wameingia...” kwako, Ewe Muhammad,

بِالْكَفْرِ

“...na ukafiri...” Hakika nyoyo zao zimeambatana na ukafiri, na kwa sababu hii hawanufaiki na elimu wanayoisikia kutoka kwako, wala ushauri na ukumbusho. Hivyo,

وَهُمْ قَدْ خَرَجُوا بِهِ^ع

“...na wametoka nao pia...” Yaani, wao peke yao,

وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا كَانُوا يَكْتُمُونَ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi kabisa wa yote wanayoyaficha.”

Allah تعالی Anajua siri zao na yaliyofichikana nyoyoni mwao, hata kama wanajidai kuwa vinginevyo kwa viumbe Vyake, na kujifanya kuwa wasivyokuwa. Allah تعالی, ambaye Ana elimu thabiti ya vinavyoonekana na visivyoonekana, Anawajua zaidi wanafiki kuliko Viumbe wake wanavyowajua na Atawalipa stahili yao. Kauli ya Allah تعالی,

وَتَرَى كَثِيرًا مِّنْهُمْ يُسْرِعُونَ فِي الْأَثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَأَكْلِهِمُ السُّحْتُ

“Na utawaona wengi katika wao wanakimbilia kwenye dhambi, na uadui, na ulaji wao vya haramu.”

Wanakwenda mbio kufanya yaliyokatazwa na kuharamishwa, huku wakienda kinyume na watu, wakila mali zao kupitia rushwa na riba,

لَيْسَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Ni maovu mno hayo wayafanyayo!”

Kwa hakika, mambo maovu ni yale waliyokuwa wakiyafanya na kuchupa mipaka walikofanya.

Kukaripiwa kwa Wanazuoni na Wasomi Wao kwa Kukata Tamaa Kukataza Maovu:

Allah تعالى Amesema,

لَوْلَا يَنْهَاهُمُ الرَّبَّيُّونَ وَالْأَحْبَارُ عَنْ قَوْلِهِمُ الْآثِمَ وَأَكْلِهِمُ السُّحْتُ لَيْسَ مَا كَانُوا
يَصْنَعُونَ

“Mbona hao wanazuoni na makohani wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi, na ulaji wao vya haramu? Ni maovu mno hayo wayafanyayo!”

Maana yake: Kwa nini wanazuoni wao hawawakatazi kufanya maovu? *Rabbaniyyun* ni wanazuoni ambao wana mamlaka, ambapo *Ahbar* ni wanazuoni wa kawaida.

لَيْسَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Ni maovu mno hayo wayafanyayo!”

Akiwakusudia *Rabbaniyyun*, kama Ali bin Abi Talhah alivyopokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, kwa Sababu waliacha kukataza maovu. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما¹ kuwa alisema, “Hapana Ayah ndani ya Qur’an ambayo ina adhabu kali kuliko Ayah hii,

¹ At-Tabari 10:450.

لَوْلَا يَنْهَاهُمُ الرَّبَّيُّونَ وَالْأَحْبَابُ عَنْ قَوْلِهِمُ الْإِنَّمَا أَكَلِمَةٌ لَيْسَ مَا كَانُوا

يَصْنَعُونَ ﴿٦٣﴾

“Mbona hao wanazuoni na makuhani wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi, na ulaji wao vya haramu? Ni maovu mno hayo wayafanyayo!”¹

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Yahya bin Ya'mar alisema, “Ali bin Abi Talib رضي الله عنه wakati mmoja alitoa hotuba, ambayo alianza kwa kumtukuza Allah تعالى na Kumshukuru. Kisha alisema, ‘Enyi Watu! Wale waliowatangulia waliangamizwa kwa sababu walifanya makosa na wanazuoni wao hawakuwakanya kutenda maovu. Maasi yalipozidi adhabu iliwaangamiza. Tambueni kuwa kuamrisha mema na kukataza maovu hakupunguzi riziki au umri.”² Imam Ahmad رحمه الله تعالى alirekodi kutoka kwa Jarir alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا مِنْ قَوْمٍ يَكُونُ بَيْنَ أَظْهُرِهِمْ مَنْ يَعْمَلُ بِالْمَعَاصِي هُمْ أَعَزُّ مِنْهُ وَأَمْنَعُ، وَلَمْ يُعَيِّرُوا إِلَّا أَصَابَهُمُ اللَّهُ مِنْهُ بِعَذَابٍ»

“Hapana mtu anayeishi na miongoni mwao wapo wanaofanya madhambi, ambapo waliosalia wana nguvu na uwezo zaidi ya wakosaji, hata hawawazuilii, bali Allah Atawapelekea adhabu.”³

Ahmad pekee ndiye aliyepokea kwa isnadi hii.⁴ Pia Abu Dawud aliandika. Katika masimulizi yake Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Nilimsikia Mtume ﷺ alisema,

«مَا مِنْ رَجُلٍ يَكُونُ فِي قَوْمٍ يَعْمَلُ فِيهِمْ بِالْمَعَاصِي، يَقْدِرُونَ أَنْ يُعَيِّرُوا عَلَيْهِ، فَلَا يُعَيِّرُوا إِلَّا أَصَابَهُمُ اللَّهُ بِعِقَابٍ قَبْلَ أَنْ يَمُوتُوا»

“Hapana mtu anayeishi miongoni mwa watu wanatenda maovu kati yao, na wasimkanye, hali wana uwezo wa kufanya hivyo, Allah Atawadhibu (wote) kabla hawajafa.”

Vile vile Ibn Majah⁵ aliandika Hadithi hii.

¹ At-Tabari 10:449.

² Kanz Al-Ummal 3:683.

³ Abu Dawud 4:510.

⁴ Ahmad 4:363.

⁵ Ibn Majah 2:1329.

kutoka kwa Mola wako Mlezi yatawazidisha wengi katika wao uasi na kufuru. Na Sisi Tumewatilia uadui na chuki baina yao mpaka Siku ya Kiyama. Kila mara wanapowasha moto wa vita, Mwenyezi Mungu Anauzima. Na wanajitahidi kuleta uharibifu katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu Hawapendi waharibifu.

65. Na lau kuwa Watu wa Kitabu wangeliamini na wakachamungu hapana shaka Tungeliwafutia makosa yao, na Tungeliwaingiza katika Bustani zenye neema.

66. Na lau kuwa wangeliishika Taurati na Injili na yote waliyoteremshiwa kutokana na Mola wao Mlezi, basi hapana shaka wangelikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao. Wapo watu miongoni mwao walio sawa, lakini wengi wao wanayoyafanya ni mabaya mno.

Mayahudi Wanasema Kuwa Mikono ya Allah Imefungwa!

Allah تعالی Anaendelea kuwalaani Mayahudi pamoja na vizazi vyao mpaka siku ya kiyama, wanamuelezea Allah تعالی kuwa ni bakhili, Allah تعالی ni Mtakatifu mno kuliko sifa wanazomnasibisha nazo. Aidha Mayahudi wanadai kuwa Allah تعالی ni masikini, ambapo wao ni wakwasi. Ali bin Abi Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliyatolea maelezo maneno ya Allah تعالی,

وَقَالَتِ الْيَهُودُ يَدُ اللَّهِ مَغْلُولَةٌ

“Na Mayahudi walisema: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba.”

“Hawana maana kuwa Mkono wa Allah تعالی Umefungwa bali wana maana ya kuwa ni bakhili na hatumii katika vile Anavyovimiliki. Allah تعالی ni Mtakatifu kuliko sifa wanazompa.”¹ Habari sawa na hizi ziliripotiwa kutoka kwa Mujahid, Ikrimah, Qatadah, As-Suddi na Adh-Dhahhak.² Allah تعالی Amesema katika Aya nyingine,

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٦٤﴾

“Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi”.

¹ At-Tabari 10:452.

² At-Tabari 10:453.

Katika Aya hii, Allah تعالى Amekataza ubahili na ufujaji mali, ambayo ni pamoja na matumizi yasiyo ya lazima. Allah تعالى Anaelezea ubahili kwa kusema,

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ

“Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako.”

Kwa hiyo, hii ndio maana waliyokusudia Mayahudi, laana ya Allah تعالى iwashukie. Ikrimah alisema kuwa Aya hii iliteremshwa juu ya Finhas, mmoja wa Mayahudi,¹ Allah تعالى Amlaani. Tuliitaja kabla kuwa Finhas alisema,

إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ

“Mwenyezi Mungu ni masikini, na sisi ni matajiri.

Allah تعالى Amekanusha kile walichomzushia Mayahudi na Akawalaani kwa sababu ya uongo na uzushi wao kumhusu Yeye. Allah تعالى Amesema,

غُلَّتْ أَيْدِيهِمْ وَلُعِنُوا بِمَا قَالُوا

“Mikono yao ndiyo iliyofumba, na wamelaaniwa kwa sababu ya waliyoyasema.”

Alichosema Allah تعالى kilitokea, kwa hakika Mayahudi ni mabakhili, wana wivu, woga na madhalili sana. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

أَمْ لَهُمْ نَصِيبٌ مِّنَ الْمَلِكِ فَإِذَا لَا يُؤْتُونَ النَّاسَ نَقِيرًا ﴿٥٤﴾ أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا ءَاتَاهُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ ۖ فَقَدْ ءَاتَيْنَا آلَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَءَاتَيْنَاهُم مَّلَكًا عَظِيمًا ﴿٥٥﴾

“Au wanayo sehemu ya utawala? Basi hapo wasingewapa watu hata tundu ya kokwa ya tende. Au wanawahusudu watu kwa yale Aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa Fadhila Yake? Basi Tuliwapa ukoo wa Ibrahim Kitabu na hikima na Tukawapa utawala mkubwa.” (4:53-54) na,

وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ

“...wakapigwa na unyonge...” (2:61),

¹ At-Tabari 10:153.

Mikono ya Allah تعالى ni Mikunjufu

Allah تعالى Amesema,

بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ يُنفِقُ كَيْفَ يَشَاءُ

“Bali Mikono Yake Iwazi. Hutoa Apendavyo.”

Neema za Allah تعالى ni nyingi, Rehema Zake hazina kikomo, kwa kuwa Anamiliki hazina ya kila kitu. Mazuri yote wayapatayo waja Wake ni kutoka Kwake Pekee, bila washirika. Ameumba kila kitu tunachokihitajia usiku na mchana, tuwapo safarini au nyumbani na katika hali zote.

Allah تعالى Amesema,

وَأَتَانَكُمْ مِّنْ كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّهِ لَا تَحْصُوهَا إِنَّ الْإِنسَانَ لَظَلُومٌ كَفَّارٌ ﴿١٤٣﴾

“Na Akakupeni kila mlichomuomba. Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu hamuwezi kuzidhibiti. Hakika mwanaadamu ni dhaalimu mkubwa, mwenye kuzikufuru neema.” (14:34)

Zipo Aya nyingine juu ya somo hili. Imam Ahmad bin Hanbal رحمه الله تعالى alisema kuwa Abdur-Razzaq alisimulia kuwa Maamar alisema kuwa Hammam bin Munabbih alisema, “Haya ndio aliyotusimulia Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ يَمِينَ اللَّهِ مَلَأَى، لَا يَبْغِضُهَا نَفَقَةً، سَحَاءَ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ، أَرَأَيْتُمْ مَا أَنْفَقَ مِنْذُ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، فَإِنَّهُ لَمْ يَبْغِضْ مَا فِي يَمِينِهِ - قال - : وَعَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ، وَفِي يَدِهِ الْأُخْرَى الْقَبْضُ يَرْفَعُ وَيَخْفِضُ»

“Mkono wa Kulia wa Allah Umejaa, na hapana matumizi yatakayopunguza Alichonacho, japokuwa Anatumia usiku na mchana. Fikirini kiasi gani Allah Ametumia toka Alipoumba mbingu na Ardhi? Pamoja na hayo haijapunguza Alichonacho katika Mkono Wake wa Kulia, Arshi Yake iko juu ya maji, na Mkono Wake Mwingine ni wa Kukamatia, Huinua na Kuteremsha”

Pia Allah تعالى Anasema katika hadithi Qudsi,

أَنْفِقْ، أَنْفِقْ عَلَيْكَ،

“Tumia Nami nitakulipa.”¹ Hadithi hii iliandikwa katika sahihi mbili.²

Ufunuo Unaoshuka kwa Waislamu Huzidisha Uasi na Ukafiri kwa Mayahudi

Allah تعالى Amesema,

وَلَيَزِيدَنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ طُغْيَانًا وَكُفْرًا^٤

“Yatawazidisha wengi katika wao uasi na kufuru.”

Maana yake: Neema zinazokuja, Ewe Muhamad ﷺ, ni maafa kwa maadui zako, Mayahudi na watu wa aina yao. Jinsi imani ya waumini, amali njema na elimu yenye manufaa inavyoongezeka, ndivyo makafiri wanapozidisha wivu kwako na kwa Ummah wako, na kuongeza *Tughyan* ambayo ni kuvuka mipaka iliyowekwa- na katika ukafiri-yaani kukukana Wewe. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ آمَنُوا هُدًى وَشِفَاءً^٥ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي آذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى^٦ أُولَٰئِكَ يُنَادَوْنَ مِنْ مَّكَانٍ بَعِيدٍ

“Sema: Hii Qur’ani ni uwongofu na poza kwa wenye kuamini. Na wasioamini umo uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni. Hao wanaitwa nao wako pahala mbali.” Na

وَنُنزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ^٧ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٨﴾

“Na Tunateremsha katika Qur’ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila khasara.” (17:82).

Baadaye Allah تعالى Amesema,

وَأَلْقَيْنَا بَيْنَهُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ^٩

“Na Sisi Tumewatilia uadui na chuki baina yao mpaka Siku ya Kiyama.”

¹ Ahmad 2:313.

² Fat’hul Al-Bari 13:415, Muslim 2:691.

Kwa hiyo mioyo yao haiungani. Bali, makundi yao tofauti na madhehebu yatakuwa na uadui na kuchukiana wao kwa wao, kwa sababu hawakubaliani katika ukweli, na kwa sababu walikupinga na kukukana. Kauli ya Allah تعالى،

كُلَّمَا أَوْقَدُوا نَارًا لِّلْحَرْبِ أَطْفَأَهَا اللَّهُ

“Kila mara wanapowasha moto wa vita, Mwenyezi Mungu Anauzima.”

Maana: Kila mara wanakufanyia njama na kuwasha moto wa vita, Allah تعالى Anauzima na Anafanya njama zao ziwageukie. Hivyo njama zao kuwadhuru wao.

وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ

“Na wanajitahidi kuleta uharibifu katika ardhi.”

Ni desturi yao siku zote kufanya uharibifu juu ya ardhi na Allah تعالى Hawapendi wenye mwendo huo.

Watu wa Kitabu Wangufuata Kitabu Chao, Wangukata Mazuri Hapa Duniani na Akhera

Allah تعالى Amesema,

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْكِتَابِ ءَامَنُوا وَاتَّقَوْا

“Na lau kuwa Watu wa Kitabu wanguamini na wakamchamungu...”

Vivyo hivyo, lau watu wa kitabu wanguamini Allah تعالى na Mjumbe wake na wakajiepusha na madhambi na yaliyokatazwa,

لَكَفَرْنَا عَنْهُمْ سِيَئَاتِهِمْ وَلَأَدْخَلْنَاهُمْ جَنَّاتِ النَّعِيمِ

“...Tungeliwafutia makosa yao, na Tungeliwaingiza katika Bustani zenye neema.”

Maana yake: ‘Tungeliwaondolea vikwazo na Tukawapa matilaba yao.’

وَلَوْ أَنَّهُمْ أَقَامُوا التَّوْرَةَ وَالْإِنجِيلَ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِمْ مِن رَّبِّهِمْ

“Na lau kuwa wanguamini Taurati na Injili na yote waliyoteremshiwa kutokana na Mola wao Mlezi...”

Maana yake: Qur’an, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na wengine,

لَأَكُلُوا مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ أَرْجُلِهِمْ^ع

“...wangelikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao.”

Wangelishikamana na vitabu walivyokuwa navyo ambavyo walivirithi kutoka kwa Mitume bila kuvifanyia mabadiliko vitabu hivyo, vingewaeleza kufuata ukweli na kutekeleza wahyi Aliompelekea Muhammad ﷺ. Vitabu hivi vinathibitisha ukweli wa Mtume ﷺ na maamrishi ambayo yanatakiwa kufuatwa. Kauli ya Allah تعالى،

لَأَكُلُوا مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ أَرْجُلِهِمْ^ع

“...wangelikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao.”

Ina maana vyakula vingi na vizuri vingeshushwa kutoka mawinguni na kukuzwa juu ya ardhi kwa ajili yao. Allah تعالى Amesema katika Aya nyengine،

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ ءَامَنُوا وَأَتَّقَوْا لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

“Na lau kuwa watu wa miji wangeliamini na wakamchamungu, kwa yakini Tungeliwafungulia baraka kutoka mbinguni na katika ardhi.”

Kauli ya Allah تعالى،

مِّنْهُمْ أُمَّةٌ مُّقْتَصِدَةٌ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ سَاءَ مَا يَعْمَلُونَ

“Wapo watu miongoni mwao walio sawa, lakini wengi wao wanayoyafanya ni mabaya mno.”

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى،

وَمِن قَوْمِ مُوسَىٰ أُمَّةٌ يَّهْدُونَ بِالْحَقِّ وَبِهِ يَعْدِلُونَ ﴿١٥٩﴾

“Na katika kaumu ya Musa lipo kundi linaowaongoa watu kwa haki na kwa haki wanafanya uadilifu.” (7:159)

Na Kauli Yake kuhusu wafuasi wa ‘Isa عليه السلام

فَقَاتِلْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْهُمْ أَجْرَهُمْ^ط

“Basi wale walioamini katika wao Tuliwapa ujira wao.”

Kwa hiyo, Allah تعالی Aliwapa daraja la juu la kipato “Iqtisad” ambalo ni tabaka la kati walilopewa Ummah huu. Juu yao kuna daraja la waliotangulia “Sabiqun” kama Allah تعالی Alivyoelezea katika Kauli Yake,

ثُمَّ أَوْرَثْنَا الْكِتَابَ الَّذِينَ اصْطَفَيْنَا مِنْ عِبَادِنَا فَمِنْهُمْ ظَالِمٌ لِنَفْسِهِ وَمِنْهُمْ مُقْتَصِدٌ وَمِنْهُمْ سَابِقٌ بِالْخَيْرَاتِ إِذْ قَالَ اللَّهُ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الْكَبِيرُ ﴿٣٢﴾
 جَنَّتٌ عَدْنٌ يَدْخُلُونَهَا يُحَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا ۗ وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٣٣﴾

“Kisha Tumewarithisha Kitabu hao ambao Tuliwateuwa miongoni mwa waja Wetu. Kati yao yupo aliyejidhulumu nafsi yake, na yupo wa katikati, na yupo aliyetangulia katika mambo ya kheri, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo fadhila kuu. bustani za milele wataingia. Huko watavikwa vikuku vya dhahabu, na lulu, na nguo zao humo ni za hariri.” (35:32:33)

* يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۗ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ ۗ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٤﴾

67. Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe Wake. Na Mwenyezi Mungu Atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu makafiri.

Ahadi ya Kufikisha Ujumbe wa Allah تعالی, na Ahadi ya Kupewa Ulinzi

Allah تعالی Anamtaja mja Wake na Mjumbe Wake Muhammad ﷺ kwa cheo cha “Mjumbe” na Anamuamuru afikishe yote Aliyomteremshia, amri ambayo Mtume ﷺ aliitekeleza kwa uadilifu mkubwa. Bukhari aliandika kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Yeyote atakayekuambieni kuwa Muhammad ﷺ alificha sehemu ya yale Aliyoteremshiwa na Allah تعالی, basi anasema uongo.” Allah تعالی Amesema

يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۗ

“Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi.”¹

¹ Fat’hul Al-Bari 8:124.

Bukhari aliikusanya Hadithi hii kwa ufupi, lakini akaitaja kwa urefu katika sehemu nyingine ya kitabu chake. Pia Muslim katika Kitabu cha Imani,¹ At-Tirmidhi na An-Nasai ndani ya Kitabu *Tafsir ya Sunan zao*.² Ndani ya *Sahih Mbili* kuna Hadithi kuwa 'Aishah رضي الله عنها alisema, "Kama Muhammad ﷺ angeficha chochote katika Qu'ran, basi angeficha Aya hii,

وَتَخْفَى فِي نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَاهُ

***"Na ukaficha nafsini mwako Aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyafichua, nawe ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye haki zaidi kumchelea."* (33:37)³**

Bukhari aliandika kuwa Az-Zuhri alisema, "Ujumbe unakuja kutoka kwa Allah تعالى, na mjumbe wajibu wake ni kuufikisha, na sisi ni juu yetu kuupokea. Ummah wa Muhammad ﷺ umethibitisha kuwa amewasilisha Ujumbe na amefikisha amana, alipowauliza katika mkutano mkubwa katika hotuba yake katika Hajj ya kuaga. Wakati huo, hawakuwepo zaidi ya arobaini elfu." Muslim alirekodi kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alimuambia Mtume ﷺ katika hotuba yake siku hiyo,

«أَبِيهَا النَّاسُ إِنَّكُمْ مَنْزُورُونَ عَنِّي، فَمَا أَنْتُمْ قَائِلُونَ؟»

"Enyi watu mtaulizwa juu yangu, hivyo mtajibu nini?"

Wakasema, "Tunashuhudia kuwa umefikisha Ujumbe, umetimiza (amana) na umetoa ushauri maridhawa." Mtume ﷺ akawanyooshea, huku akisema

«اللَّهُمَّ هَلْ بَلَّغْتُ؟ اللَّهُمَّ هَلْ بَلَّغْتُ؟»

"Ewe Allah! Nimefikisha? Ewe Allah! Nimefikisha?"⁴

Kauli ya Allah تعالى,

وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ

"Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake."

¹ Muslim 1:159.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:441 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:315.

³ *Fat'hul Al-Bari* 13:415, Muslim 1:160.

⁴ Muslim 2:886.

Muradi wake: Iwapo hutofikisha kwa watu ujumbe Niliokutuma basi utakuwa hujafikisha ujumbe Wangu. Maana: Mtume ﷺ anajua matokeo ya kushindwa huko. Ali bin Abi Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alielezea Ayah hii,

وَاللَّهُ يَعَصْمُكَ مِنَ النَّاسِ¹

“Mwenyezi Mungu Atakulinda dhidi ya watu.”¹

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu makafiri.”

Maana yake: Fikisha Ujumbe Wangu na Nitakulinda, Kukusaidia na Kukuunga mkono dhidi ya maadui zako na Nitakuhakikishia ushindi kwa maadui wako. Kwa hiyo, usiwe na woga au mwenye huzuni, kwani hapana hata mmoja wao atakayeweza kukudhuru. Kabla ya kuteremshwa Aya hii Mtume ﷺ alikuwa akilindwa, kama Imam Ahmed alivyorekodi kuwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alikuwa macho usiku mmoja, alikuwa pembeni yake akamuuliza, ‘Kuna jambo gani, Ewe Mjumbe wa Allah?’ Alijibu,

«لَيْتَ رَجُلًا صَالِحًا مِنْ أَصْحَابِي يَخْرُسُنِي اللَّيْلَةَ»

“Natamani mtu mchamungu miongoni mwa masahaba zangu anilinde usiku!”

Akasema, “Ghafla tulisikia sauti ya silaha.” Mtume ﷺ akauliza,

«مَنْ هَذَا؟»

“Nani huyu?” Yule (mlinzi mpya) akajibu, “Mimi ni Said bin Malik (Said bin Abi Waqqas).” Mtume ﷺ aliuliza,

«مَا جَاءَ بِكَ؟»

“Jambo gani limekuleta hapa?” Akajibu, “Nimekuja kukulinda Ewe Mjumbe wa Allah!” Aisha رضي الله عنها akasema, “Hivyo, Mtume ﷺ alilala usiku ule na akasikia sauti ya kukoroma.”² Hadithi hii imenukuliwa katika sahihi mbili.³

¹ At-Tabari 10:468.

² Ahmad 6:141.

³ Fat’hul Al-Bari 13:232, Muslim 4:1875.

Mapokezi mengine ya Hadithi hii ni kama ifuatavyo, “Mtume ﷺ alikuwa macho usiku mmoja baada ya kuja Madina...”¹ na baada ya Mtume ﷺ kukamilisha ndoa yake na Aisha رضي الله عنها, mwaka wa pili wa Hijrah.²

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Mtume ﷺ alikuwa akilindwa mpaka Aya hii iiliposhushwa,

وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ³

“Na Mwenyezi Mungu Atakulinda na watu.”

Aliongeza, Mtume ﷺ aliinua kichwa chake kutoka chumbani na kusema,

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ! انصِرُّوا فَقَدْ عَصَيْتَنِي اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ»

“Enyi watu! Nendeni, kwani Allah Atanilinda.” At-Tirmidhi aliandika na kusema, “Hadithi hii ni Gharib”³ Iliandikwa na Jarir رحمه الله تعالى⁴ na Al-Hakim katika Mustaadrak, ambapo alisema, “Isnadi yake ni sahihi, lakini Hawakuiandika” Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu makafiri.”

Maana yake, “Ewe Muhammad ﷺ, ulifikisha, na Allah تعالى Humuongoza Amtakaye, na Humpotosha Amtakaye. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Amesema,

لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ⁴

“Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humuwongoa Amtakaye.” (2:272) na

فَاذْمًا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ

“...juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hisabu.” (13:40)

¹ Fat’hul Al-Bari 6:95, Muslim: 4:1875.

² Rai sahihi ni kuwa, Mtume ﷺ alitamiliza ndoa yake na ‘Aishah رضي الله عنها, katika mwaka wa kwanza wa Hijra.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:410.

⁴ At-Tabari 10:469 na Al-Hakim 2:313.

Usihuzunike au kurudishwa nyuma na ukafiri wao. Allah تعالى Amesema

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا

"Hakika walioamini," Inawahusu waislamu.

وَالَّذِينَ هَادُوا

"...na Mayahudi..." Waliopewa Taurat.

وَالصَّابِقُونَ

"...na Masabii..." Ni kikundi katika wakristo na majusi ambao hawakufuata dini yoyote mahususi, kama alivyoeleza Mujahid. Ama Wakristo inafahamika walipewa Injili. Hapa inamaanisha kuwa kila kundi katika haya lililomuamini Allah تعالى na Akhera, ambayo ni siku ya hukumu na Hesabu, na likatenda mema. Na kufanya hivyo pekee haitoshi, hadi amali hio iafikiane na sheria ya Muhammad ﷺ, aliyetumwa kwa binadamu wote na majini. Iwapo moja ya makundi yalioamini yatakuwa na sifa hii, basi hawatakuwa na woga na yatakayojiri huko mbele, wala huzuni kwa waliyoyapoteza huko nyuma, wala majonzi hayatowapata.

Tulijadili Aya kama hii kabla katika Suratul Baqara. Hakuna haja ya kurudia tena hapa.

* * *

لَقَدْ أَخَذْنَا مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَأَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ رَسُولًا^ط
 كَمَا جَاءَهُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنفُسُهُمْ فَرِيقًا
 كَذَّبُوا وَفَرِيقًا يَقْتُلُونَ ﴿٧٠﴾ وَحَسِبُوا أَلَّا تَكُونَ فِتْنَةً
 فَعَمُوا وَصَمُوا ثُمَّ تَابَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ ثُمَّ عَمُوا وَصَمُوا
 كَثِيرٌ مِّنْهُمْ ؕ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿٧١﴾ لَقَدْ كَفَرَ
 الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ^ط وَقَالَ
 الْمَسِيحُ ابْنُ بَنِي إِسْرَائِيلَ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ^ط إِنَّهُ مَن
 يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ^ط وَمَا
 لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنْصَارٍ ﴿٧٢﴾ لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا
 إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا إِلَهٌ وَاحِدٌ وَإِن لَّمْ
 يَنْتَهُوا عَمَّا يَقُولُونَ لَيَمَسَّنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ
 عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٣﴾ أَفَلَا يَتُوبُونَ إِلَى اللَّهِ
 وَيَسْتَغْفِرُونَ^ع وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧٤﴾ مَا الْمَسِيحُ ابْنُ
 مَرْيَمَ^ط إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ^ط
 كَانَا يَأْكُلَانِ الطَّعَامَ ؕ أَنْظِرْ كَيْفَ نُبَيِّنُ لَهُمُ
 الْآيَاتِ ثُمَّ أَنْظِرْ أَنِّي يُؤْفَكُونَ ﴿٧٥﴾

لَقَدْ أَخَذْنَا مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ
 وَأَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ رَسُولًا^ط كَمَا جَاءَهُمْ
 رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنفُسُهُمْ فَرِيقًا
 كَذَّبُوا وَفَرِيقًا يَقْتُلُونَ ﴿٧٠﴾
 وَحَسِبُوا أَلَّا تَكُونَ فِتْنَةً فَعَمُوا
 وَصَمُوا ثُمَّ تَابَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ ثُمَّ
 عَمُوا وَصَمُوا كَثِيرٌ مِّنْهُمْ ؕ وَاللَّهُ
 بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿٧١﴾

70. Tulifanya agano na Wana wa Israili, na Tuka-watumia Mitume. Kila alipowajia Mtume kwa wasioyapenda nafsi zao wengine waliwakanusha na wengine wakawaua.

71. Na wakadhani kuwa hapatakuwa majaribio; basi wakawa vipofu na viziwi. Kisha Mwenyezi Mungu Akawapokelea toba zao. Kisha tena wengi katika wao wakawa vipofu na

viziwi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona hayo wayatendayo.

Allah تعالى Anatukumbusha kuwa Alichukua ahadi na agano kutoka kwa Wana wa Israel kumsikiliza na kumtii Yeye na Mjumbe Wake. Walivunja ahadi na maagano hayo na wakafuata utashi wao badala ya sheria, Na sharia

iliyoafikiana na utashi wao waliikubali, na ambayo haikuendana na utashi wao waliipinga. Kwa ajili hiyo Allah تعالى Alisema,

كَمَا جَاءَهُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنفُسُهُمْ فَرِيقًا كَذَّبُوا وَفَرِيقًا يَقْتُلُونَ ﴿٧٠﴾
وَحَسِبُوا أَنَّا لَنَكُونَنَّ فِتْنَةً فَعَمُوا وَصَمُوا

"Kila alipowajia Mtume kwa wasioyapenda nafsi zao wengine waliwakanusha na wengine wakawaua. Na wakadhani kuwa hapatakuwa majaribio; basi wakawa vipofu na viziwi."

Wakidhani kuwa hawatoadhibiwa kwa maovu waliyotenda. Ikawa bado, hawauoni ukweli na wakawa viziwi, wasiosikia ukweli. Kwa sababu hizi hawakuweza kuongozwa kwao. Allah تعالى Alisema hayo, kisha

فَعَمُوا وَصَمُوا

"...wakawa vipofu na viziwi."

كَثِيرٌ مِّنْهُمْ ۗ وَاللَّهُ بِصِيرٍ بِمَا يَعْمَلُونَ

"...wengi katika wao...na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona hayo wayatendayo."

Ana elimu timilifu kwa yale wayafanyao na miongoni mwao wanaostahili muongozo na wanastahili upotofu.

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ ۗ وَقَالَ الْمَسِيحُ بَنِيَّ إِسْرَائِيلَ آعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۗ إِنَّهُ مَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ ۗ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن أَنْصَارٍ ﴿٧١﴾ لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ ۗ وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا إِلَهُ وَاحِدٌ ۗ وَإِن لَّمْ يَنْتَهُوا عَمَّا يَقُولُونَ لَيَمَسَّنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٢﴾ أَفَلَا يَتُوبُونَ إِلَى اللَّهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لَهُ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧٣﴾ مَا الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ ۗ كَانَا يَأْكُلَانِ الطَّعَامَ ۗ أَنْظِرْ كَيْفَ نُنِيبُ ۗ لَهُمُ الْآيَاتِ ثُمَّ أَنْظِرْ أَنِّي يُؤْفَكُونَ ﴿٧٤﴾

72. Hakika wamekufuru waliosema: Mwenyezi Mungu ni Masihi mwana wa Maryamu! Na hali Masihi mwenyewe alisema: Enyi

Wana wa Israili! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu Atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na waliodhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru.

73. Kwa hakika wamekufuru waliosema: Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa Utatu. Hali hakuna mola ila Mungu Mmoja. Na ikiwa hawaachi hayo wanayoyasema, kwa yakini itawakamata adhabu chungu wale wanaokufuru.

74. Je! Hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na wakamuomba msamaha? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghufira na Mwenye Kurehemu.

75. Masihi mwana wa Maryam si chochote ila ni Mtume. Wamekwisha pita Mitume kabla yake. Na mama yake ni mwanamke mkweli. Wote wawili walikuwa wakila chakula. Angalia jinsi Tunavyowabainishia Aya, kisha angalia vipi wanavyogeuzwa.

Ukafiri wa Wakristo; Isa عليه السلام Alilingania katika Kumpwekesha Mungu Mmoja (Tawhid).

Allah تعالى Anaelezea kuwa madhehebu ya Wakristo kama vile ya Utawa, Jacobite na Nestorite ni makafiri, wale miongoni mwao wanaosema kuwa Isa عليه السلام ni Allah تعالى. Allah تعالى ni Mtukufu sana kuliko sifa wanazomhusisha Isa عليه السلام. Isa عليه السلام ni mja na Mtume ﷺ. Maneno aliyoyatamka Isa عليه السلام alipokuwa katika susu (kitanda cha mtoto mchanga) Ni, ***“Mimi ni Abdullah (mtumishi wa Allah).”*** Hakusema kuwa, “Mimi ni Allah” au “Mimi ni mtoto wa Allah” Bali alisema,

إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ ءَاتَنِي الْكِتَابَ وَجَعَلَنِي نَبِيًّا

“Hakika mimi ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu. Amenipa Kitabu, na Amenifanya Nabii”. (19:30). Mpaka,

وَإِنَّ اللَّهَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَأَعْبُدُوهُ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٣٦﴾

“Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi, na Mola wenu Mlezi. Basi muabuduni Yeye. Hii ndiyo njia iliyo nyooka”. (19:36)

Pia alitangaza alipokuwa mtu mzima, baada ya kupewa utume, akiwaamrisha kumuabudu Mola wake na Mola wao pekee bila washirika,

وَقَالَ الْمَسِيحُ يَبْنِي إِسْرَائِيلَ أَعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ^ط إِنَّهُ مَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ

“Masih mwenyewe alisema: Enyi Wana wa Israili! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu,...” katika ibada,

فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ ^ط

“Hakika Mwenyezi Mungu Atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni.”

Atawatupa motoni na kuwanyima pepo. Aidha Allah تعالى Amesema

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَن يَشَاءُ ^ط

“Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehe kushirikishwa, na Husamehe yaliyo duni ya hilo kwa Amtakaye.” (4:116) na

وَنَادَى أَصْحَابُ النَّارِ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَنْ أَفِيضُوا عَلَيْنَا مِنَ الْمَاءِ أَوْ مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ ^ط

قَالُوا إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَهُمَا عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٥٠﴾

“Na watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi: Tumimieni maji, au chochote Alichokuruzukuni Mwenyezi Mungu. Nao watasema: Hakika Mwenyezi Mungu Ameviharimisha hivyo kwa makafiri.”

Imerekodiwa ndani ya Sahihi¹ kuwa Mtume ﷺ alimtuma mtu mmoja kuwatangazia watu,

«إِنَّ الْجَنَّةَ لَا يَدْخُلُهَا إِلَّا نَفْسٌ مُّسْلِمَةٌ»

“Nafsi ya Muislamu tu ndio itaingizwa peponi.” Katika mapokezi mengine,

«مُؤْمِنَةٌ»

“Waumini tu.”

“Kwa sababu hiyo ndio maana Isa عليه السلام aliwaambia wana wa Israel,

¹ Fat'hul Al-Bari 6:207.

إِنَّهُ مَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَهُ النَّارُ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنْصَارٍ

“Kwani anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu Atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru.”

Hapana msaada kutoka kwa Allah تعالى, Wala hapana atakayemsaidia au kumhami katika hali watakuwemo. Kauli ya Allah تعالى,

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ

“Kwa hakika wamekufuru waliosema: Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa Utatu.”

Mujahid na wengineo walisema kuwa Aya hii iliteremshwa kuwahusu Wakristo tu. As-Suddi na wengineo walisema kuwa Aya hii iliteremshwa kuhusu kumfanya Isa عليه السلام na mama yake miungu pamoja na Allah تعالى, hivyo kumfanya Allah تعالى ni wa tatu katika utatu mtakatifu.¹ As-Suddi alisema, Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى mwisho wa sura,

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَعْيسَى ابْنُ مَرْيَمَ ءَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمَّيَ إِلَهَيْنِ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۗ قَالَ سُبْحَانَكَ

“Na pale Mwenyezi Mungu atakaposema: Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu? (Na Isa) atasema: Subhanaka...” (5:116)² Allah تعالى Akajibu,

وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا إِلَهُ وَاحِدٌ

“Hali hakuna mola ila Mungu Mmoja.” Maana: Hapana wanaostahili kuabudiwa isipokuwa Yupo Mungu Mmoja asiye na washirika, na Yeye ni Bwana wa viumbe vyote vinavyoishi. Kisha Allah تعالى Akasema, huku Akiwatisha na Kuwaonya,

وَإِنْ لَمْ يَنْتَهُوا عَمَّا يَقُولُونَ

“Na ikiwa hawaachi hayo wanayoyasema...”

¹ At-Tabari 10:483.

² At-Tabari 10:483.

Uongo wao na madai batili, kiyama watafungwa pingu za kuteswa.

لَيَمَسَّنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“...kwa yakini itawakamata adhabu chungu wale wanaokufuru.”

Kisha Allah تعالى Anasema,

أَفَلَا يَتُوبُونَ إِلَى اللَّهِ وَيَسْتَغْفِرُونََهُ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٧٥﴾

“Je! Hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na wakamuomba msamaha? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira na Mwenye Kurehemu.”

Hii inaonesha Ukarimu, Wema na Huruma ya Allah تعالى kwa waja Wake, Japokuwa walitenda dhambi kubwa na wakazua mambo na tuhuma za uongo. Pamoja na hayo yote, Allah تعالى Anawataka watubie ili apate Kuwasamehe, kwani Allah تعالى Huwasamehe wale wanaoleta toba ya kweli kweli.

Isa عليه السلام ni Mtumwa wa Allah تعالى na Mama Yake ni Muumini wa kweli

Allah تعالى Amesema,

مَا الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ

“Masihi mwana wa Maryam si chochote ila ni Mtume. Wamekwisha pita Mitume kabla yake.”

Isa عليه السلام ni kama Mitume waliopita, na ni mmoja wa watumishi wa Allah تعالى na mmoja wa Mitume wake watukufu. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

إِنَّ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٦٦﴾

“Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa Tuliemneemesha na Tukamfanya ni mfano kwa Wana wa Israili.”

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ ﴿١٦٧﴾

“Na mama yake ni mwanamke mkweli.” Alimuamini Allah تعالى kwa uaminifu mkubwa kwake. Hili ni daraja la juu alilopewa, ambayo inathibitisha kuwa hakuwa Mtume. Kisha Allah تعالى Amesema,

كَأَنَّا يَاكُلَانِ الطَّعَامَ

“Wote wawili walikuwa wakila chakula.”

Wanakula mlo na kutoa uchafu. Hivyo walikuwa waja sawa na wengine, si miungu kama walivyodai wafuasi wa baadhi ya madhehebu za kikristo, Allah تعالیٰ Aendelee kuwalaani mpaka siku ya kiama. Kisha Akasema,

أَنْظِرْ كَيْفَ نُبَيِّنُ لَهُمُ الْآيَاتِ

“Angalia jinsi Tunavyowabainishia Aya...”

Tumeifanya wazi kabisa,

ثُمَّ أَنْظِرْ أَنِّي يُؤَفِّكُونَ

“Kisha angalia vipi wanavyogeuzwa.”

Angalia maoni, fikra potofu, na madai wanayoshikilia, hata baada ya ufafanuzi wetu na maelezo yaliyowazi.

* * *

قُلْ أَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا
 وَلَا نَفْعًا ۗ وَاللَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٧٦﴾ قُلْ يَتَاهَلْ
 الْكِتَابِ لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ غَيْرَ الْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعُوا
 أَهْوَاءَ قَوْمٍ قَدْ ضَلُّوا مِن قَبْلُ وَأَضَلُّوا كَثِيرًا وَضَلُّوا عَن
 سَوَاءِ السَّبِيلِ ﴿٧٧﴾ لُعِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن بَنِي
 إِسْرَائِيلَ عَلَى لِسَانِ دَاوُدَ وَعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ ۗ ذَلِكَ بِمَا
 عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿٧٨﴾ كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ
 عَن مُّكْرٍ فَعَلُوهُ ۗ لَبِئْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٧٩﴾
 تَرَىٰ كَثِيرًا مِّنْهُمْ يَتَوَلَّوْنَ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ لَبِئْسَ مَا
 قَدَّمَتْ لَهُمْ أَنفُسُهُمْ أَن سَخِطَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَفِي الْعَذَابِ هُمْ
 خَالِدُونَ ﴿٨٠﴾ وَلَوْ كَانُوا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ
 الْآخِرِ مَا اخْتَدَوْهُمُ أَوْلِيَاءَ ۗ وَلَٰكِن كَثِيرًا مِّنْهُمْ
 فَسِقُونَ ﴿٨١﴾

قُلْ أَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا
 لَا يَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا ۗ وَاللَّهُ
 هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٧٦﴾ قُلْ يَتَاهَلْ
 الْكِتَابِ لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ غَيْرَ
 الْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعُوا أَهْوَاءَ قَوْمٍ قَدْ
 ضَلُّوا مِن قَبْلُ وَأَضَلُّوا كَثِيرًا
 وَضَلُّوا عَن سَوَاءِ السَّبِيلِ ﴿٧٧﴾

76. Sema: Je! Mnawa-abudu, badala ya Mwenyezi Mungu, wale ambao hawawezi kukudhuruni wala kukufaeni? Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.

77. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu bila ya haki. Wala

msifuate matamaniao ya watu waliokwishapotea tangu zamani, na wakawapoteza wengi, na wenyewe wakapotea njia iliyo sawa.

Kukatazwa (Ushirikina) na Kupetuka Mpaka katika Dini.

Allah تعالیٰ Anawakaripia wenye kumuwekea washindani na kuabudu masanamu na miungu bandia. Anaeleza kuwa miungu hiyo bandia haina kiasi chochote cha uungu. Allah تعالیٰ Amesema,

قُلْ

“Sema...” Ewe Muhammad, kuwaambia wana wa Adam عليه السلام, kama vile Wakristo, wanaomuabudu asiyekuwa Allah تعالیٰ,

أَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا

“Je! Mnawaabudu, badala ya Mwenyezi Mungu, wale ambao hawawezi kukudhuruni wala kukufaeni?”

Maana: Wasioweza kuzuia madhara yasikufikie wala kukunufaisheni,

وَاللَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua”

Anasikia Anachosema mja Wake na Anajua kila kitu. Kwa hiyo, vipi mnaabudu visivyo hai, visivyosikia, kuona wala kujua chochote – visivyo na uwezo wa kujidhuru wala kujinufaisha vyenyewe, achilia mbali kwa wengine – badala ya kumuabudu Allah.

Kisha Allah تعالى Akasema,

قُلْ يَتَأَهَّلَ الْكِتَابَ لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ غَيْرَ الْحَقِّ

“Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu bila ya haki.”

Maana yake: Msivuke mipaka kuhusu ukweli na kuzidisha mno katika kumsifu yule mliyeamrisha kumtukuza. Kumkithirishia mnakofanya na kumnyanyua kutoka katika daraja la utume kwenda daraja la uungu. Mlimfanyia hayo 'Isa عليه السلام, ambaye alikuwa Mtume, tena mkadai kuwa alikuwa mungu pamoja na Allah تعالى. Kosa hili lilitokea kwa sababu mliwafuata mafarisayo wenu, ambao walikuwa wapotevu kabla yenu hapo zamani,

وَأَضَلُّوا كَثِيرًا وَضَلُّوا عَن سَوَاءِ السَّبِيلِ

“...na wakawapoteza wengi, na wenyewe wakapotea njia iliyo sawa.”

Waliacha njia iliyonyooka, na kufuata njia ya upotofu:

لُعِبَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَى لِسَانِ دَاوُدَ وَعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ ذَلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿٧٦﴾ كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَن مُنْكَرٍ فَعَلُوهُ لَبِئْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٧٧﴾ تَرَى كَثِيرًا مِّنْهُمْ يَتَوَلَّوْنَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَبِئْسَ مَا

قَدَمَتْ هُمْ أَنْفُسَهُمْ أَنْ سَخِطَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَفِي الْعَذَابِ هُمْ خَالِدُونَ ﴿٧٦﴾ وَلَوْ كَانُوا
يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مَا آتَّخَذُوهُمْ أَوْلِيَاءَ وَلَكِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ
فَنَسِقُونَ ﴿٧٧﴾

78. Walilaaniwa waliokufuru miongoni mwa Wana wa Israili kwa ulimi wa Daud na wa Isa mwana wa Maryamu. Hayo ni kwa sababu waliasi na wakawa wanapindukia mipaka.

79. Walikuwa hawakatazani maovu waliyokuwa wakiyafanya. Hakika ni maovu yalioje mambo waliyokuwa wakiyafanya!

80. Utawaona wengi wao wanafanya urafiki na waliokufuru. Hakika ni maovu yaliyotangulizwa na nafsi zao hata Mwenyezi Mungu Amewakasirikia, nao watadumu katika adhabu.

81. Na lau wangelikuwa wanamuamini Mwenyezi Mungu, na huyu Nabii, na yaliyoteremshwa kwake, wasingeliwafanya hao marafiki. Lakini wengi katika wao ni wapotofu.

Laana ya Mwenyezi Mungu kwa Wana wa Israil.

Allah تعالی Anaelezea kuwa Aliwalaani makafiri miongoni mwa wana wa Israil, muda mrefu uliopita, katika aliomteremshia Mtume wake Dawud عليه السلام na kwa ulimi wa Isa mwana wa Maryam عليه السلام. kwa sababu ya kumuasi kwao Mwenyezi Mungu na kufanya kwao uadui kwa viumbe wake.

Al-Awf amepokea toka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kuwa: 'Walilaaniwa katika Taurati, Injili, Zaburi na Furqan (Qur'an)."

Kisha Allah تعالی Akabainisha hali yao katika waliokuwa wakiyategemea katika zama zao,

كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَنْ مُنْكَرٍ فَعَلُوهُ

"...Walikuwa hawakatazani maovu waliyokuwa wakiyafanya."

Maana yake: Ilikuwa hawakatazani wao kwa wao katika kufanya madhambi na maharamisho, kisha Allah تعالی Akawakosoa kwa hilo ili kuhadharisha kufanywa mfano wa walioyafanya, Akasema:

لَيْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٧٦﴾

"Hakika ni maovu yalioje mambo waliyokuwa wakiyafanya!"

Hadithi Zinzoelezea Kuamrisha Mema na Kukataza Machafu.

Hadithi katika kuamrisha mema na kukataza maovu ni nyingi mno, tutaje katika zinazonasibiana na maudhui haya.

Imam Ahmad alinukuu toka kwa Hudhayfah bin Al-Yamaan رضى الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَتَأْمُرُنَّ بِالْمَعْرُوفِ، وَلَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ، أَوْ لَيُوشِكَنَّ اللَّهُ أَنْ يَنْتَعِتَ عَلَيْكُمْ عِقَابًا مِنْ عِنْدِهِ، ثُمَّ لَتَدْعُهُنَّ فَلَا يَسْتَجِيبُ لَكُمْ»

*"Naapa kwa Yule ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake, mtaamrisha mema na mtakataza mabaya, vinginevyo Allah Atakupelekeeni adhabu kutoka Kwake, kisha mtamuomba hatajibu dua yenu."*¹

At Tirmidhi pia aliipokea na kusema, 'Hadithi hii ni Hasan.'²

Katika sahihi ya Muslim amepokea toka kwa Abu Said Al-Khudriy رضى الله عنه, amesema: Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ رَأَى مِنْكُمْ مُنْكَرًا فَلْيُغَيِّرْهُ بِيَدِهِ، فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِلِسَانِهِ، فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِقَلْبِهِ، وَذَلِكَ أَضْعَفُ الْإِيمَانِ»

*"Mwenye kuona ovu miongoni mwenu alizuie kwa mkono wake, kama hatoweza, basi kwa ulimi wake, kama hatoweza, basi kwa moyo wake na huo ni udhaifu zaidi wa imani."*³

Abu Dawuud amepokea toka kwa Ursi, maana Ibnu Amiirah رضى الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا عُمِلَتِ الْخَطِيئَةُ فِي الْأَرْضِ كَانَ مَنْ شَهِدَهَا فَكْرِهَهَا، - وَقَالَ مَرَّةً فَأَنْكَرَهَا - كَانَ كَمَنْ غَابَ عَنْهَا، وَمَنْ غَابَ عَنْهَا فَرَضِيهَا كَانَ كَمَنْ شَهِدَهَا»

¹ Ahmad 5:388.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:391.

³ Muslim: 1:69.

"Inapofanywa dhambi juu ya ardhi, basi inakuwa kwa aliyeona akakarihika, - mara nyingine Mtume alisema: na akachukia- atakuwa kama wale ambao hawakushuhudia; na asiye kuwepo akaridhia, atakuwa sawa na walioshuhudia."

Abu Dawud peke yake ndiye aliyepokea Hadithi hii.¹ Abu Dawud amepokea toka kwa watu miongoni mwa Masahaba wa Mtume ﷺ, kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَنْ يَهْلِكَ النَّاسُ حَتَّى يُعْذِرُوا أَوْ يُعَذِّرُوا مِنْ أَنْفُسِهِمْ»

"Watu hawataangamia mpaka aibu zao zitakapokuwa nyingi au watakapozidisha madhambi katika nafsi zao."

Ibn Majah amepokea toka kwa Abu Saidi Al-Khudriy رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ alitoa hutuba, katika aliyoyasema yalikuwa ni:

«أَلَا لَا يَمْنَعَنَّ رَجُلًا هَيْبَةُ النَّاسِ أَنْ يَقُولَ الْحَقَّ إِذَا عَلِمَهُ»

"Tahadhari! Kuwaogopa watu, kusimzuie mtu kusema ukweli, kama anaujua."

Abu Said رضي الله عنه alilia na kusema, "Wa Llaahi tumeona mambo tukaogopa."²

Hadithi nyingine toka kwa Abu Said رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema,

«أَفْضَلُ الْجِهَادِ كَلِمَةٌ حَقٌّ عِنْدَ سُلْطَانٍ جَائِرٍ»

"Jihad bora ni neno la haki mbele ya mfalme jeuri."

Ameipokea Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibnu Majah,³ na At-Tirmidhi amesema ni "*Hasan Gharib*" katika njia ya upokezi huu.

Imam Ahmad amepokea kuwa Hudhayfah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا يَتَّبِعِي لِمُسْلِمٍ أَنْ يُدِلُّ نَفْسَهُ»

"Haitakikani kwa Muislam kuidhalilisha nafsi yake."

¹ Abu Dawud: 4347.

² Ibn Majah: 4007.

³ Abu Dawud 4:514, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:395, na Ibn Majah 2:1239.

Wakasema, “Inakuwaje mtu akaidhalilisha nafsi yake?” Akasema,

«يَتَعَرَّضُ مِنَ الْبَلَاءِ لِمَا لَا يُطِيقُ»

“Anajitia katika mabalaa asiyoyaweza.”¹

Kama hivi imepokewa na At-Tirmidhi na Ibnu Majah, Tirmidhi amesema, “Hadithi hii ni Hasan Sahih Gharib”.²

Kuwakosoa Wanafiki.

Allah تعالی Amesema:

تَرَى كَثِيرًا مِّنْهُمْ يَتَوَلَّوْنَ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Utawaona wengi wao wanafanya urafiki na waliokufuru.”

Mujahid amesema: Aya hii inawahusu wanafiki, na Kauli ya Allah تعالی

لَيْسَ مَا قَدَّمَتْ هُمْ أَنْفُسُهُمْ

“Hakika ni maovu yaliyotangulizwa na nafsi zao.”

Maana yake: Kwa huko kuwatawalisha kwao makafiri na kuacha kwao kuwatawalisha waumini, ambako kuliwafanya wawe na unafiki ndani ya mioyo yao na kumkasirisha Allah تعالی, hasira inayodumu mpaka siku ya marejeo yao. Allah تعالی Amesema:

أَنْ سَخِطَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ

“Hata Mwenyezi Mungu Amewakasirikia.”

Imefasiriwa kuwa ni katika yale Aliyowakosoa nayo. Kisha Allah تعالی Akaeleza kuwa:

وَفِي الْعَذَابِ هُمْ خَالِدُونَ

“...nao watadumu katika adhabu.”

وَلَوْ كَانُوا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالنَّبِيِّ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مَا اتَّخَذُوهُمْ أَوْلِيَاءَ

“Na lau wangelikuwa wanamuamini Mwenyezi Mungu, na huyu Nabii, na yaliyoteremshwa kwake, wasingeliwafanya hao marafiki.”

¹ Ahmad 5:1405.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:531, na Ibn Majah 2:1332.

Maana kama wangemuamini Allah تعالى kwa yakini, Mjumbe Wake na Qur'an, wasingelifanya maovu ya kuwaunga mkono makafiri kwa siri na kuwafanyia uadui wale waumini, Allah تعالى, Mtume ﷺ na yale aliyoteremshiwa,

وَلَيْكِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ فَسِقُونَ

“Lakini wengi katika wao ni wapotofu.”

* * *

* لَتَجِدَنَّ أَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِلَّذِينَ ءَامَنُوا الْيَهُودَ
 وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا ۗ وَلَتَجِدَنَّ أَقْرَبَهُم مَّوَدَّةً لِلَّذِينَ ءَامَنُوا
 الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصْرِيَّ ۚ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَتَلُوا
 وَرَهْبَانًا وَأَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٨٢﴾ وَإِذَا سَمِعُوا مَا أُنزِلَ
 إِلَى الرَّسُولِ تَرَىٰ أَعْيُنُهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ مِمَّا عَرَفُوا
 مِنَ الْحَقِّ ۖ يَقُولُونَ رَبَّنَا ءَامَنَّا فَكُتِبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ ﴿٨٣﴾
 وَمَا لَنَا لَا نُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا جَاءَنَا مِنَ الْحَقِّ وَنَطْمَعُ أَنْ
 يُدْخِلَنَا رَبُّنَا مَعَ الْقَوْمِ الصَّالِحِينَ ﴿٨٤﴾ فَأَنْتَبَهُمُ اللَّهُ بِمَا
 قَالُوا جَنَّتٍ نَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ
 وَذَلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٥﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا
 بِعَآيِنِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿٨٦﴾ يَتَأَيَّمُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا
 لَا تُخَرِّمُوا طَيِّبَتِ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ
 لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿٨٧﴾ وَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَلًا
 طَيِّبًا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَنْتُمْ بِهِ مُؤْمِنُونَ ﴿٨٨﴾ لَا
 يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَٰكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا
 عَقَدْتُمُ الْأَيْمَانَ ۖ فَكَفَرْتُمْ ۖ إِطْعَامَ عَشْرَةِ مَسْكِينٍ مِنْ
 أَوْسَطِ مَا تُطْعَمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْفَتُهُمْ أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ ۖ
 فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ ۚ ذَلِكَ كَفْرَةٌ أَيْمَانِكُمْ إِذَا
 حَلَفْتُمْ ۚ وَاحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ ۚ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ ءَايَاتِهِ
 لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٨٩﴾

* لَتَجِدَنَّ أَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِلَّذِينَ
 ءَامَنُوا الْيَهُودَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا ۗ
 وَلَتَجِدَنَّ أَقْرَبَهُم مَّوَدَّةً لِلَّذِينَ
 ءَامَنُوا الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصْرِيَّ ۚ
 ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَتَلُوا
 وَرَهْبَانًا وَأَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٨٢﴾
 وَإِذَا سَمِعُوا مَا أُنزِلَ إِلَى الرَّسُولِ
 تَرَىٰ أَعْيُنُهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ
 مِمَّا عَرَفُوا مِنَ الْحَقِّ ۖ يَقُولُونَ
 رَبَّنَا ءَامَنَّا فَكُتِبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ ﴿٨٣﴾
 وَمَا لَنَا لَا نُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا جَاءَنَا
 مِنَ الْحَقِّ وَنَطْمَعُ أَنْ يُدْخِلَنَا
 رَبُّنَا مَعَ الْقَوْمِ الصَّالِحِينَ ﴿٨٤﴾
 فَأَنْتَبَهُمُ اللَّهُ بِمَا قَالُوا جَنَّتٍ
 نَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ
 وَذَلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٥﴾
 وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِعَآيِنِنَا
 أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿٨٦﴾

82. Hakika utawakuta
 walioshadidi kuliko watu

wote katika uadui kwa walioamini ni Mayahudi na washirikina. Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanaosema: Sisi ni Manasara. Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki, na kwa sababu wao hawafanyi kiburi.

83. Na wanapo sikia yaliyoteremshwa kwa Mtume utaona macho yao yanachururika machozi kwa sababu ya Haki waliyoitambua. Wanasema: Mola wetu Mlezi! Tumeamini. Basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia.

84. Na kwa nini tusimuamini Mwenyezi Mungu na Haki iliyotujia, na hali tunatumai Mola wetu Mlezi Atuingize pamoja na watu wema?

85. Basi Mwenyezi Mungu Atawalipa, kwa yale waliyoyasema, Bustani zipitazo mito kati yake; humo watadumu. Na haya ndiyo malipo ya wafanyao wema.

86. Na wale waliokufuru na wakazikanusha Ishara Zetu, hao ndio watu wa Motoni.

Kubainisha Sababu za Kushuka Aya Hizi.

Said bin Jabayr, As -Suddi na wengineo wamesema kuwa Aya hizi zilishushwa kwa ujumbe ambao An-Najaash (Mfalme wa Ethiopia) alituma kwa Mtume ﷺ ili kusikia maneno yake na kujua sifa zake, walipomuona na kuwasomea Qur'ani, walisilimu, walilia na kunyenyekea. Kisha walirejea kwa Najashi wakamueleza yaliyojiri.¹ Ataa bin Abi Rabaah alisema: "Wao walikuwa Wahabeshi waliosilimu wakati Waislamu walipohamia Ethiopia waliishi nao." Qatadah alisema, "Walikuwa wafuasi wa dini ya Isa عليه السلام, mwana wa Maryamu, ambao walipowaona Waislamu na kuisikia Quran, waliukubali Uislamu bila kusita."²

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema kuwa Aya hizi ziliteremshwa kwa watu wenye sifa hizi ni sawa walitoka Ethiopia au vinginevyo. Kauli Yake Allah تعالى:

¹ At-Tabari 10:499, 500.

² At-Tabari 10:501.

لَتَجِدَنَّ أَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِلَّذِينَ ءَامَنُوا الْيَهُودَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا^ط

“Hakika utawakuta walioshadidi kuliko watu wote katika uadui kwa walioamini ni Mayahudi na washirikina.”

Haikuwa hivyo isipokuwa ni kuwa ukafiri wa Mayahudi ni ukafiri wa inadi na kupinga na kuikanusha haki, kuwadharau watu na kuwavunjia heshima wanazuoni.

Kwa sababu hii Mayahudi laana ya Allah تعالى iendelee kuwashukia mpaka Siku ya Kiyama waliwaua Mitume wao wengi na walijaribu kumuua Mtume ﷺ mara kadhaa, vile vile kumfanyia mambo ya uchawi na kumtilia sumu. Pia waliwachochea watu wa aina yao miongoni mwa washirikina dhidi ya Mtume ﷺ. Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَلَتَجِدَنَّ أَقْرَبَهُم مَّوَدَّةً لِلَّذِينَ ءَامَنُوا الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصْرِي^ع

“Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanaosema: Sisi ni Manasara.”

Maana yake: Ambao wamedai kuwa wao ni Wakristo, wanaofuata dini ya Masihi na mafundisho ya Injili yake. Ndani yake kuna mapenzi kwa Uislamu na watu wake kwa ujumla. Na hilo ni kwa sababu ya huruma na ukarimu ambao umo ndani ya nyoyo zao, kwa kuwa wao wako katikia dini ya Masihi yenye ulaini na upole. Kama Allah تعالى Alivyosema:

وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ رَأْفَةً وَرَحْمَةً وَرَهَابَانِيَّةً

“Na Tukajaalia katika nyoyo za waliomfuata upole na rehema. Na umonaki (utawa wa mapadri)...” (57:27)¹

Katika kitabu chao kuna msemu; “Yule akupigae kofi shavu la kulia, mgeuzie shavu la kushoto.” Na kupigana kuliharamishwa katika imani yao, kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

¹ Ibn Kathir ameitaja sehemu hii tu ya Aya, na alichokidhamiria lazima kiwe dhahiri kwa msomaji. Hata hivyo sehemu iliyobakia ya Aya hiyo ambayo inatafsirika hivi: “...*(utawa wa mapadri) wameuzua wao. Sisi hatukuwaandikia hayo...*” (ikizungumzia umonaki) waziwazi inakhitilafiana na lengo la Ibn Kathir hapa. Yeye mwenyewe analizungumzia jambo hili baadaye kidogo, pia hata mwishoni mwa Tafsiri ya Surat Al-Hadid.

ذَٰلِكَ بِأَنَّ مِنْهُمْ قِسِيَسِينَ وَزُهَبَانَا وَأَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ

“Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki, na kwa sababu wao hawafanyi kiburi.”

Maana yake: Wanapatikana miongoni mwao makasisi nao ni wahubiri wao na wanazuoni wao. Amepokea Ibnu Abi Hatimi رحمه الله تعالى toka kwa Hamiya bin Riaab amesema: Nilimsikia Salmaan رضي الله عنه akiulizwa kuhusu Kauli Yake

تعالى:

ذَٰلِكَ بِأَنَّ مِنْهُمْ قِسِيَسِينَ وَزُهَبَانَا وَأَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ

“Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki, na kwa sababu wao hawafanyi kiburi.”

Inadhamini wasifu wao kuwa ni watu wenye elimu, wafanya ibada na wanyenyekevu. Kisha akawasifu kwa kunyenyekeka haki na kufuata usawa, Akasema:

وَإِذَا سَمِعُوا مَا أُنزِلَ إِلَى الرَّسُولِ تَرَىٰ أَعْيُنُهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ مِمَّا عَرَفُوا مِنَ الْحَقِّ

“Na wanaposikia yaliyoteremshwa kwa Mtume utaona macho yao yanachururika machozi kwa sababu ya Haki waliyoitambua.”

Maana yake: Kwa kuwa tayari wanayo elimu ya ubashiri wa kutumwa Mtume Muhammad ﷺ,

يَقُولُونَ رَبَّنَا ءَامَنَّا فَاكْتُبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ

“Wanasema: Mola wetu Mlezi! Tumeamini. Basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia.”

Pamoja na wenye kushuhudia usahihi wake na wanaomuamini.

وَمَا لَنَا لَا نُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا جَاءَنَا مِنَ الْحَقِّ وَنَطْمَعُ أَنْ يُدْخِلَنَا رَبُّنَا مَعَ الْقَوْمِ

الصَّالِحِينَ ﴿٨٥﴾

“Na kwa nini tusimuamini Mwenyezi Mungu na Haki iliyotujia, na hali tunatumai Mola wetu Mlezi Atuingize pamoja na watu wema?”

Aina hii ya Manaswara wao ndio waliotajwa katika Kauli Yake Allah تعالى,

وَأَنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِمْ خَشِعِينَ لِلَّهِ

“Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu wapo wanaomuamini Mwenyezi Mungu na yaliyoteremshwa kwenu na yaliyoteremshwa kwao, wakimnyenyekea Mwenyezi Mungu.” (3:199) na,

الَّذِينَ ءَاتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِهِ هُمْ بِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿١٩٩﴾ وَإِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ قَالُوا ءَأَمَّا بِيَمِينِنَا إِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلِهِ مُسْلِمِينَ ﴿٢٠٠﴾

“...Wale Tuliowapa Kitabu kabla yake wanakiamini hiki. Na wanaposomewa wanasema: Tunaiamini. Hakika hii ni Haki inayotoka kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa ni Waislamu, tulionyenyekea.” (28:52-53) mpaka

لَا تَتَّبِعِ الْجَاهِلِينَ

“Sisi hatutaki kujibizana na wajinga.” (28:55)

Kwa ajili hiyo ndipo Aliposema Allah تعالى hapa:

فَأْتَبَهُمْ اللَّهُ بِمَا قَالُوا

“Basi Mwenyezi Mungu Atawalipa,...”

Maana yake: “Akawalipa kwa sababu ya imani yao ya kukubali, na kuitambua kwao haki.”

جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا

“Bustani zipitazo mito katikati yake; humo watadumu.”

Maana yake: Watakaa humo milele hawabadiliki wala hawaondoki.

وَذَٰلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ

“Na haya ndiyo malipo ya wafanyao wema.”

Maana: Katika kufuata kwao haki na kuinyenyekea popote walipo, jinsi walivyo na pamoja na watu wowote walionao. Kisha Akaelezea kuhusu hali ya waovu, Akasema:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا

“Na wale waliokufuru na wakazikanusha Ishara Zetu,...”Maana: Wamezipinga na kuzikhalifu.

أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ

“Hao ndio watu wa Motoni.”Maana: Wao ni watu wake na ndio wenye kuingia humo.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُخْرِمُوا طَيِّبَتِ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ
 الْمُعْتَدِينَ ﴿٨٧﴾ وَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَالًا طَيِّبًا ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَنتُمْ بِهِ
 مُؤْمِنُونَ ﴿٨٨﴾

87. Enyi mlioamini! Msiharimishe vizuri Alivyokuhalalishieni Mwenyezi Mungu, wala msikiuke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wakiukao mipaka.

88. Na kuleni katika Alivyokuruzukuni Mwenyezi Mungu, halali na vizuri. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mnamuamini.

Hapana Utawa katika Uislamu.

Ali bin Abi Talhah amesema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, Aya hii iliteremshwa ikiwahusu baadhi ya Masahaba wa Mtume ﷺ ambao walisema, “Inabidi tuzikate dhakari zetu, tuache matamania ya dunia, na kusafiri sehemu mbali mbali kama wafanyavyo watawa.” Hilo likamfikia Mtume ﷺ, akawaita na kuwauliza kutokana na kauli yao hio, walijibu: “Ndiyo.” Mtume ﷺ akasema:

«لِكِنِّي أَصُومُ وَأُفْطِرُ، وَأَصَلِّي، وَأَنَامُ، وَأُنْكِحُ النِّسَاءَ، فَمَنْ أَخَذَ بِسُتِّي فَهُوَ مِنِّي،
 وَمَنْ لَمْ يَأْخُذْ بِسُتِّي فَلَيْسَ مِنِّي»

“Lakini mimi ninafunga na kufungua, ninasali na kulala, na ninaoa wanawake, Yeyote anayechukua suna yangu yu pamoja nami, na yeyote anayechukua Sunnah yangu si pamoja nami.”¹

¹ At-Tabari 10:518. Masimulizi sawa na haya ya sababu ya kushushwa Aya yalinukuliwa na Al-Bukhari.

Ameipokea Ibnu Abi Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى.

Ibn Mardawayh رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى amepokea toka kwa Al-Awfi toka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما mfano wa tukio hili. Katika sahihi mbili imepokewa toka kwa Aishah رضي الله عنها kuwa watu katika Masahaba wa Mtume ﷺ waliwauliza wakeze Mtume ﷺ kuhusu ibada zake za siri, mmoja wao akasema, "Sitokula nyama", mwingine akasema, "Sitooa" wa tatu alisema, "Sitolala kitandani". Mtume ﷺ aliposikia kauli hii alisema,

«مَا بَالُ أَقْوَامٍ يَقُولُ أَخَذْتُمْ كَذَا وَكَذَا، لَكِنِّي أَصُومُ وَأَفْطِرُ، وَأَنَا مُ وَأَقُومُ، وَأَأْكُلُ
اللَّحْمَ، وَأَتَزَوَّجُ النِّسَاءَ، فَمَنْ رَغِبَ عَنِّي فَلَيْسَ مِنِّي»

*"Wanalipi watu waliosema kadha wa kadha? Ninafunga na ninafuturu ninalala na ninasimama kusali, nakula nyama, na ninaoa wanawake. Basi mwenye kuchukia suna yangu si katika mimi."*¹

Kauli ya Allah تَعَالَى،

وَلَا تَعْتَدُوا

"Wala msikiuke mipaka."

Maana: Msizidishe katika kuzitia dhiki nafsi zenu kwa kujiharamishia vilivyo halalishwa, msichupe mipaka kwa kufanya isirafu katika mambo yaliyo halalishwa, tumieni kwa kadiri ya haja, wala msivuke mipaka ndani yake, kama alivyosema katika aya nyingine,

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا

"Na kuleni na kunyweni wala msifanye isirafu." (7:31) na

وَالَّذِينَ إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ ذَلِكَ قَوَامًا ﴿٦٧﴾

"Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo." (25:67)

¹ Fat'hul Al-Bari 9:5, Muslim 2:1020.

Hivyo Allah تعالی Amefaradhisha njia ya kati na kati baina ya wafanyao isirafu na wale wenye kujibana, na hairuhusu matumizi ya fujo, wala kujibana kupita kiasi. Ndio maana Allah تعالی Amesema,

لَا تُحْرَمُوا طَيِّبَاتِ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ

“Msiharimishe vizuri Alivyokuhalalishieni Mwenyezi Mungu, wala msikiuke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wakiukao mipaka.”

Kisha Akasema,

وَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَالًا طَيِّبًا

“Na kuleni katika Alivyokuruzukuni Mwenyezi Mungu, halali na vizuri.”

Kuleni visafi na halali kwenu,

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“...Na mcheni Mwenyezi Mungu...”

Katika mambo yenu yote, mtiini Yeye, na mtafute radhi Zake, na wakati huo huo mjiweke mbali na kuhalifu na kutomtii Allah تعالی,

وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَنْتُمْ بِهِ مُؤْمِنُونَ

“...Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mnamuamini.”

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا عَقَدْتُمُ الْأَيْمَانَ فَكَفَرْتُمْ

إِطْعَامَ عَشْرَةِ مَسْكِينٍ مِنْ أَوْسَطِ مَا تَطْعَمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْوَتُهُمْ أَوْ تَخْرِيرُ رَقَبَةٍ فَمَنْ

لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ ذَلِكَ كَفْرَةُ أَيْمَانِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ وَأَحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ كَذَلِكَ

يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٨٩﴾

89. “Mwenyezi Mungu Hatakushikeni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini Atakushikeni kwa mnavyoapa kweli kweli kwa makusudio. Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnachowalisha ahali zenu, au kuwavisha, au kumkomboa

mtumwa. Asiyepata hayo, basi afunge siku tatu. Hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapoapa. Na hifadhini yamini zenu. Namna hivyo Mwenyezi Mungu Anakubainishieni Aya zake ili mpate kushukuru."

Viapo Visivyodhamiriwa

Tulitaja somo la viapo visivyodhamiriwa ndani ya Surat Al-Baqarah, Sifa na Shukrani zote zinamstahiki Allah تعالى, na wala hatuhitaji kurudia tena hapa.

Aidha tulitaja kuwa: "*Al-Laghwu Al-Yamiin*" Ni kiapo kinachosemwa katikati ya maneno pindi mtu anapoongea bila hata ya kuazimia.

Mfano mtu kusema, 'hapana naapa kwa Allah تعالى' au kusema, 'ndio naapa kwa Allah تعالى.'

Adhabu kwa Kuvunja Kiapo

Allah تعالى Amesema,

وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا عَقَّدْتُمُ الْأَيْمَانَ^٥

"...lakini Atakushikeni kwa mnavyoapa kweli kweli kwa makusudio."

Kwa kurejea kwenye viapo mliyovikusudia ndani ya mioyo yenu,

فَكَفَّرْتُمُوهُنَّ إِطْعَامَ عَشْرَةِ مَسْكِينٍ

"...Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi..."

Ni wahitaji, wasioweza kujikimu kimaisha. Kauli ya Allah تعالى,

مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعَمُونَ أَهْلِيكُمْ

"...kwa chakula cha wastani mnachowalisha ahali wenu..."

Maana yake: Wastani wa mnachotumia kulisha familia zenu, kwa mujibu wa Ibn Abbas, Said bin Jubayr na Ikrimah رضي الله عنهم¹. Ata Al-Kharasani aliitolea maelezo Aya hii, "Kutokana na vizuri mnavyolisha familia zenu."²

¹ At-Tabari 10:541.

² At-Tabari 10:531.

Kauli ya Allah تعالى،

أَوْ كَسَوْتُهُمْ

“...au kuwavisha...”

Muradi wake ni kumpa kila mmoja kati yao nguo zifaazo kusalia, ima masikini huyo alikuwa mwanamume au mwanamke. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Al-Awaf alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema Aya ina maana ya joho au kanzu kwa kila masikini (miongoni mwa kumi).¹

Aidha Mujahid alisema kuwa, nguo ya chini kabisa kwa mujibu wa Aya, ni kanzu, na ya juu kwa utashi wa mtu.

Al-Hasan, Abu Jaafar Al-Baqir, Ata, Tawus, Ibrahim An-Nakhai, Hamad bin Abi Suleyman na Abu Malik walisema kuwa ina maana (kumpa kila mmoja kati ya masikini kumi) kanzu.³

Kauli ya Allah تعالى،

أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ

“...au kumkomboa mtumwa...”

Maana yake: Kumuwacha huru mtumwa Muislamu. Katika Muwatta ya Malik, Musnadi ya Shafii na Sahihi ya Muslim, Hadithi ndefu ilinukuliwa kuwa Umar bin Al-Hakam Al-As-Salami رضي الله عنه alisema kuwa kuna wakati alikuwa amuwache huru mtumwa (kama adhabu) na alimleta mjakazi mweusi mbele ya Mtume ﷺ ambaye alimuuliza,

«أَيْنَ اللهُ؟»

“Yuko wapi Allah?”

Akajibu, ‘Juu ya mbingu.’ Akasema,

«مَنْ أَنَا؟»

“Mimi ni nani?”

¹ At-Tabari 10:547.

² At-Tabari 10:545.

³ At-Tabari 10:545, 546.

Akajibu 'Mtume ﷺ." Akasema,

«أَعِظْهَا فَإِنَّهَا مُؤْمِنَةٌ»

*"Muuache huru, kwani ni muumini."*¹

Kuna aina tatu za adhabu kwa kuvunja kiapo kwa makusudi, na yoyote kati ya hizo inafaa, kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni.

Allah تعالى Ameanza na iliyo nyepesi, kisha ngumu, ambapo kisha ni rahisi kuliko kutoa nguo; na kutoa nguo, ni rahisi kuliko kuacha huru mtumwa.

Endapo mtu atashindwa kutimiza yaliyoamrisha, basi afunge siku tatu kwa kulipia kosa.

Kama Allah تعالى Alivyosema,

فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ

"...Asiyepata hayo, basi afunge siku tatu..."

Ubayy bin Ka'b, Ibn Masudi na wanafunzi wao رضي الله عنهم walisoma Aya hii na kutafsirika hivi, "Kisha lazima afunge siku tatu mutawalia."²

Hata kama kauli hii isingelizwa kwetu kuwa ni sehemu ya Qur'an, kwa masimilizi ya *Mutawatir*, bado yatakuwa ni maelezo ya Qur'ani na Masahaba ambao walipokea kutoka kwa Mtume ﷺ.

Kauli ya Allah تعالى,

ذَلِكَ كَفَّارَةٌ لِّأَيْمَانِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ

"...Hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapo apa..." (5:89)

Maana: Hii ni njia ya kufuata kiapo cha kisharia, kwa mujibu wa maana iliyotolewa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.³

¹ *Al-Muwata'* 2:776, *Ar-Risalah* na. 75, Muslim 1:38.

² At-Tabari 5:31.

³ At-Tabari 10:560, 562.

وَأَحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ

“...Na hifadhini yamini zenu...”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema: Maana yake, msiache viapo vyenu bila ya kulipa kafara.¹

كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ

“...Namna hivyo Mwenyezi Mungu Anakubainishieni Aya zake...”

Na Anakuelezeni,

لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“... ili mpate kushukuru...”

* * *

¹ At-Tabari 10:560, 562.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْحَمْرُ
 وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ
 مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ
 تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ
 أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ
 وَالْبَغْضَاءَ فِي الْحَمْرِ وَالْمَيْسِرِ
 وَالْأَنْصَابِ وَيَصُدَّكُمْ عَنْ ذِكْرِ
 اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ فَهَلْ أَنْتُمْ
 مُنْتَهُونَ ﴿٩١﴾ وَأَطِيعُوا اللَّهَ
 وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأَحْذَرُوا
 فِيمَا كُنْتُمْ تَوَلَّيْتُمْ فَأَعْلَمُوا
 أَنَّ مَا اتَّقَوْا وَءَامَنُوا وَعَمِلُوا
 الصَّالِحَاتِ جُنَاحٌ فِيمَا طَعِمُوا
 إِذَا مَا اتَّقَوْا وَءَامَنُوا وَأَحْسَنُوا
 وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿٩٢﴾
 يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِيَبْتَلُوكُمْ
 اللَّهُ بِشَيْءٍ مِّنَ الصَّيْدِ تَنَالَهُ
 أَيْدِيكُمْ وَرِمَاحُكُمْ لِيَعْلَمَ اللَّهُ
 مَن يَخَافُهُ بِالْغَيْبِ فَمَن أَعْتَدَى
 بَعْدَ ذَلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ
 أَلِيمٌ ﴿٩٣﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا
 لَا تَقْتُلُوا الصَّيْدَ وَأَنْتُمْ حُرْمٌ
 وَمَن قَتَلَهُ مِنكُم مُّتَعَمِّدًا
 فَجَزَاءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعْمِ
 تَحْكُمُ بِهِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ
 هَدْيًا بَلِغِ الْكَعْبَةِ أَوْ كَفَرَةً
 طَعَامٌ مَّسْكِينٍ أَوْ عَدْلٌ ذَلِكِ
 صِيَامًا لِيَذُوقَ وَبَالَ أَمْرِهِ
 عَفَا اللَّهُ عَمَّا سَلَفَ وَمَنْ عَادَ
 فَيَنْتَقِمُ اللَّهُ مِنْهُ وَاللَّهُ عَزِيزٌ
 ذُو انْتِقَامٍ ﴿٩٤﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْحَمْرُ
 وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ
 مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ
 تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ
 أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ
 وَالْبَغْضَاءَ فِي الْحَمْرِ وَالْمَيْسِرِ
 وَالْأَنْصَابِ وَيَصُدَّكُمْ عَنْ ذِكْرِ
 اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ فَهَلْ أَنْتُمْ
 مُنْتَهُونَ ﴿٩١﴾ وَأَطِيعُوا اللَّهَ
 وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأَحْذَرُوا
 فِيمَا كُنْتُمْ تَوَلَّيْتُمْ فَأَعْلَمُوا
 أَنَّ مَا اتَّقَوْا وَءَامَنُوا وَعَمِلُوا
 الصَّالِحَاتِ جُنَاحٌ فِيمَا طَعِمُوا
 إِذَا مَا اتَّقَوْا وَءَامَنُوا وَأَحْسَنُوا
 وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿٩٢﴾

90. Enyi mlioamini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu

katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa.

91. Hakika Shetani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na

kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mmeacha?

92. Na mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume, na tahadharini. Na ikiwa mtageuka basi jueni ya kuwa juu ya Mtume wetu ni kufikisha ujumbe tu ulio wazi.

93. Si dhambi juu ya walioamini na wakatenda mema kwa walivyo vila (zamani) maadamu wakichamungu na wakiamini na wakitenda mema, kisha wakachamungu, na wakaamini, kisha wakachamungu na wakafanya mazuri. Na Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao mazuri.

Kuharamishwa Ulevi na Kamari

Allah تعالی Anawakataza waja Wake waumini kutumia ulevi na kucheza Kamari ambayo ni haramu. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی alinukuu kutoka kwa Ali bin Abi Talib رضي الله عنه, kiongozi wa Waumini, alisema kuwa chesi (saratnji) ni aina ya kamari.¹ Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی alirekodi kuwa Ata, Mujahid na Tawus, au wawili kati yao, walisema kuwa kila aina ya michezo ya kubahatisha, ikiwa ni pamoja na watoto kuchezea michezo ya bahati nasibu kama vile korokoro au michezo ya kubeti.² Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa *Al-Maysir* ina maana kucheza kamari.³ Na kauli hii ni sawa na ya Adh-Dhahak aliyoipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما⁴ ambaye aliongeza, "Walikuwa wakicheza kamari katika enzi za Jahiliyyah, mpaka Uislamu ulipokuja. Kisha Allah تعالی Akaharamisha tabia hii mbaya."

Maana ya Kuabudu Sanamu na Kupiga Ramli.

Al-Ansab yalikuwa mawe ya madhabahu, makafara yalifanywa katika viunga vyake (zama za Jahiliyyah) kwa mujibu wa Ibn Abbas, Mujahid, Ata Said bin Jubayr na Al-Hasan رضي الله عنهم. Wao pia walisema kuwa *Al-Azlam* ilikuwa mishale waliyokuwa wakitumia kubahatisha ili kupata majibu, kama Abi Hatim رحمه الله تعالی alivyosimulia. Allah تعالی Amesema,

¹ Maneno hayo, kupitia isnadi zote, yamenasibishwa naye pasi na usahihi.

² At-Tabari 4:322, 323.

³ At-Tabari 4:325.

⁴ At-Tabari 4: 324.

رَجَسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ

“...ni uchafu katika kazi ya Shetani. ...”

Maana: Yanayochukiza miongoni mwa kazi za shetani, kwa mujibu wa Ali bin Abi Talhah aliyepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,¹ Said Bin Jubayr alisema kuwa *Rijs* maana yake ‘dhambi’;² ambapo Zayd bin Aslam alisema, “ni uchafu katika kazi ya Shetani.”³

فَاجْتَنِبُوهُ

“Basi jiepusheni navyo,...” Kwa maana iacheni. Baadaye Allah تعالى Amesema:

لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُونَ ﴿٢١٠﴾

“...ili mpate kufanikiwa...” Hii ni Kauli ya kutia moyo. Kisha Allah تعالى Akasema:

إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ ۗ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ ﴿٢١١﴾

“Hakika Shetani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mmeacha?” Hili ni tishio na onyo.

Kutaja Hadithi Zinazoharamisha *Khamr* (Vilevi).

Imam Ahmad aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, ‘Kulikuwa na hatua tatu za kuharamisha vilevi. Mtume ﷺ alipohamia Madinah, watu walikuwa wanakunywa pombe na kucheza kamari, hivyo walimuuliza Mtume ﷺ juu ya mambo haya, Allah تعالى Aliteremsha,

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ

“Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa...” (2:219)

¹ At-Tabari 10: 565.

² At-Tabari 4:330.

³ At-Tabari 10:565.

Mpaka mwisho wa Aya, watu wakasema, "Hivyo vilevi na kamari haviku-haramishwa kwetu. Allah تعالى Alisema,

فِيهِمَا إِنَّمَا كَبِيرٌ وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ

"Katika hivyo zipo dhambi kubwa na manufaa kwa watu."

Waliendelea kunywa pombe mpaka siku moja, Mtu mmoja miongoni mwa *Muhajirun* alikuwa akiwasalisha wenzake katika Sala ya Magharibi akachanganya aya katika kusoma kwake. Baada ya hapo, Allah تعالى Aliteremsha Kauli kali zaidi,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرَبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ

"Enyi mlioamini! Msikaribie Sala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayoyasema,..."

Kuanzia hapo watu walikuwa wanakunywa baada ya Sala ili wasali wakiwa na akili timamu. Aya kali zaidi iliteremshwa baadaye,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ
فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٥﴾

"Enyi mlioamini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa."

Wakasema: "Tumekoma Ewe Mola." Na watu wakasema; "Ewe Mjumbe wa Allah, kuna watu waliouliwa katika mapambano ya kuuhami Uislamu. Na wapo waliokufa juu ya vitanda vyao, walikuwa wakinywa pombe na kula chumo la kamari na hali ya kuwa Allah تعالى Amevifanya vitendo hivyo kuwa ni vya shetani?"

Allah تعالى Akateremsha,

لَيْسَ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جُنَاحٌ فِيمَا طَعِمُوا

"Si dhambi juu ya walioamini na wakatenda mema kwa walivyo vila (zamani)..."

Mpaka mwisho wa Aya. Mtume ﷺ alisema,

«لَوْ حُرِّمَ عَلَيْهِمْ لَتَرَكُوهُ كَمَا تَرَكَتُمْ»

“Lau kama wangeliharamishiwa, wangeacha kama mlivyoacha.”¹

Ahmad aliandika Hadithi hii. Imam Ahmad aliandika kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema “Ewe Allah! Elezea kwa uwazi hukumu kuhusu ulevi.” Aya hiyo katika *Surat Al-Baqarah* ikateremshwa,

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ

“Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa...” (2:219)

Umar رضي الله عنه aliitwa na alisomewa Aya hii, lakini bado alinena, “Ewe Allah! Tuwekee wazi hukumu ya *Khamr*.” Kisha Aya katika *Surat An-Nisaa* ilishushwa,

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرَبُوا الصَّلَاةَ وَأَنتُمْ سُكَرَىٰ

“Enyi mlio amini! Msikaribie Sala, hali mmelewa,...” (4:43)

Baada ya hapo Mtume ﷺ alimuona mtu amelewa wakati wa Sala umeingia, “Wote waliolewa hawaruhusiwi kukaribia Sala.” Umar رضي الله عنه aliitwa tena na alisomewa, lakini bado alisema, “Ewe Allah! Toa hukumu iliyo wazi kuhusu Pombe.” Kisha Aya ndani ya *Surat Al-Maidah* (5:91) ilishuka, na Umar رضي الله عنه aliitwa na alisomewa, alipofika sehemu ya Aya inayosomeka,

فَهَلْ أَنتُمْ مُنْتَهُونَ

“Basi je, mmeacha?” Umar رضي الله عنه alisema, “Tumeacha,² Tumeacha.” Abu Dawud, At-Tirmidhi na ‘An-Nasai³ waliandika Hadithi hii. Ali bin Al-Madini na At-Tirmidhi waliipa daraja la Sahihi. Imenukuliwa ndani ya Sahihi mbili, kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema katika hotuba yake; akiwa amesimama juu ya Mimbar ya Mtume ﷺ (ndani ya Msikiti wa Mtume ﷺ, katika mji wa Madina), “Enyi watu! Kuharamishwa kwa Pombe kumefafanuliwa; na Pombe inazalishwa kutoka katika vitu vitano, kutokana na zabibu, tende, asali, ngano

¹ Ahmad 2:351.

² Ahmad 1:53.

³ Abu Dawud 4:79, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:417, An-Nasai 8:286.

na shayiri. Pombe ndiyo inayoleweshwa akili.”¹ Bukhari alirekodi kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, ‘Pombe iliharamishwa wakati kulikuwa na aina tano ya vilevi Madinah, ukiacha vilivyokuwa vikitengenezwa kutokana na zabibu.”²

Hadithi Nyingine.

Imam Ahmad alirekodi kuwa Anas رضي الله عنه alisema, “Wakati mmoja nilikuwa nikiwapa vinywaji vyenye kilevi akina Abu Ubaydah bin Al-Jarrah, Ubayy bin Ka’b, Suhaili bin Bayda na marafiki zao waliokuwa wamekutana ndani ya nyumba ya Abu Talhah. Walipokaribia kulewa, baadhi ya Waislamu walifika na kuwaambia, “Mnajua kuwa Pombe imeharamishwa?” Walisema, ‘Tutasubiri na kuuliza!” Kisha wakasema, ‘Ewe Anas, Mimina pombe iliyobaki ndani ya chombo chako! Wallah! Hawakunywa tena, na Pombe yao zama hizo ilitengenezwa kwa tende mbichi na za kawaida.”³ Hii pia (ilirekodiwa katika ‘sahihi mbili. Katika masimulizi mengine ya Anas رضي الله عنه, “Nilikuwa mgawaji wa vinywaji kwa watu ndani ya nyumba ya Talhah wakati Pombe ilipoharamishwa na katika siku hizo Pombe ilitengenezwa kutokana na tende mbichi au za kawaida. Mlinganiaji alinadi, na Abu Talhah aliniamuru nikatazame yaliyojiri. Hivyo nikamkuta mtu akitangaza kuwa vinywaji vinavyoleweshwa vimeharamishwa, Abu Talhah alinituma nikamwage mvinyo nje. Nilikwenda nje na nikaimwaga, na ilitiririka katika mji wa Madinah. Baadhi ya watu walisema, “kuna watu waliokufa na mvinyo ukiwa matumboni mwao.” Baadaye wahyi kutoka kwa Allah تعالى ulishuka,

لَيْسَ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جُنَاحٌ فِيمَا طَعَمُوا

“Si dhambi juu ya walioamini na wakatenda mema kwa walivyo vila (zamani)...” (5:93)⁴

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, “Nilikuwa nikiwahudumia Abu Talhah, Abu Ubaydah bin Al-Jarrah, Abu Dujanah, Muadh bin Jabal na Suhaili bin Bayda, mpaka walipwewa kutokana na mvinyo uliotengezwa kwa mchanganyiko wa zabibu mbichi na za kawaida. Kisha nikamsikia mtu akitangaza, ‘Pombe imeharamishwa.” Hivyo hapana mtu aliyeingia au kutoka nje mpaka tulipomwaga Pombe na tukapasua mapipa

¹ Fat’hul Al-Bari 8: 126, Muslim: 4:2322.

² Fat’hul Al-Bari 8:126.

³ Ahmad 3:181.

⁴ Fat’hul Al-Bari 5:133, Muslim 3:1570.

yake. Baada ya hapo baadhi yetu tulitawadha na wengine wakakoga na tukajitia manukato. Kisha tukaenda zetu Masjid wakati Mtume ﷺ alikuwa akisoma,

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا أَحْمَرُوا وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ
الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ

“Enyi mliaoamini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo...” (5:90) mpaka,

فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ

“Basi je, mmeacha? (5:91)

Mtu aliuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Itakuwaje kwa wale waliokufa huku wakinywa?” Allah تعالى Aliteremsha Aya hii,

لَيْسَ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جُنَاحٌ فِيمَا طَعُمُوا

“Si dhambi juu ya walioamini na wakatenda mema kwa walivyo vila (zamani)...” (5:93)¹

Hadithi Nyingine:

Imam Ahmad aliandika kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

لُعِنَتِ الْخَمْرُ عَلَى عَشْرَةِ أَوْجِهٍ: لُعِنَتِ الْخَمْرُ بِعَيْنِهَا، وَشَارِبِهَا، وَسَاقِيهَا،
وَبَائِعِهَا، وَمُبْتَاعِهَا، وَعَاصِرِهَا، وَمُعْتَصِرِهَا، وَحَامِلِهَا، وَالْمَحْمُولَةَ إِلَيْهِ، وَآكِلُ
ثَمَرِهَا

“Mambo kumi yanayohusiana na Pombe yalilaaniwa. Pombe yenyewe ililaaniwa, kwa anayekunywa, mhudumu, muuzaji, mnunuzi, mtengenezaji, anayetuma kutengenezewa, mbebaji, anayepelekewa na anayekula fedha zitokanazo na Pombe.”²

Abu Dawud na Ibn Majah³ waliirekodi Hadithi hii.

¹ At-Tabari 10: 578.

² Ahmad 2:25.

³ Abu Dawud na. 2674, Ibn Majah na. 3380.

Ahmad alinukuu kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, “Mtume ﷺ alitoka kuelekea (Al-Mirbad) nikaongozana naye, na nilikuwa upande wake wa kulia, lakini alikuja Abubakar رضي الله عنه na nikampisha, na Abubakar رضي الله عنه akawa upande wa kulia wa Mtume ﷺ, ambapo mimi nilikuwa upande wa kushoto. Kisha Umar رضي الله عنه akajiunga nasi nikampisha akawa upande wa kushoto wa Mtume ﷺ. Mtume ﷺ aliona mfuko wa ngozi ukining’inia ukiwa na pombe, aliomba kisu na akaamuru ule mfuko upasuliwe; kisha akasema

«لُعِنَتِ الْخَمْرُ وَشَارِبُهَا، وَسَاقِيهَا، وَبَائِعُهَا، وَمُبْتَاعُهَا، وَحَاطِلُهَا، وَالْمَحْمُولَةُ إِلَيْهِ،
وَعَاصِرُهَا وَمُعْتَصِرُهَا، وَأَكِلُ ثَمَرِهَا»

“Pombe imelaaniwa na pia wanywaji, wahudumu, wauzaji, wanunuzi, wanaopelekewa, watengenezaji, wanaotengenezewa, na wanaokula thamani yake zitokanazo na pombe.”¹

Hadithi Nyingine:

Al-Hafiz Abu Bakar Al-Bayhaqi رحمه الله تعالى amepokea kuwa Sa’d رضي الله عنه alisema, “Kuna Aya nne zilizoteremshwa kuhusu Pombe.” Kisha akasema, “Mtu mmoja kutoka Ansar alipika chakula na akatualika. Tulikunywa Pombe kabla ya kuharamishwa na tulilewa, na tukaanza kujisifu kwa hali zetu. Ansar wakasema kuwa wao ni bora, ambapo Maquraish (Muhajirina) wakasema kuwa wao ni bora. Mmoja wa Ansar alichukua kipande cha mfupa akampiga nacho Sa’d رضي الله عنه kwenye pua na kukawa na jeraha. Toka siku hiyo pua ya Sa’d رضي الله عنه ikawa na kovu. Aya kashuka,

إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ

“Bila ya shaka ulevi, na kamari.” mpaka

فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ

“Basi je, mmeacha?” Iliteremshwa baadaye. Muslim aliandika hadithi hii.²

Hadithi Nyingine:

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Abdullah bin Amr رضي الله عنه alisema, Hakika Aya hii ndani ya Qur’ani,

¹ Ahmad 2:71.

² Al-Bayhaqi 8:285, Muslim na. 1748.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْحَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ
فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٥﴾

“Enyi mlilo amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa.”

Alisema: Iliku wemo kadhalika ndani ya Taurati, ‘Allah تعالی Aliteremsha ukweli ili kufuta batili. Kadhalika kuondosha pumbao za kipuuzi, filimbi au ala za mziki, dansa, gita, kinubi na shairi au tenzi zenye kuhamasisha mapenzi. Na pombe ni chungu kwa waionjao. Allah تعالی Ameapa kwa utukufu na nguvu zake, “Yeyote atakayeinywa baada ya Kuiharamisha, Nitamfanya awe na kiu siku ya Kiyama. Atakayeichacha baada ya Kuiharamisha, Nitamnywesha yeye Peponi.” Isnadi yake ni Sahih.¹

Hadithi Nyingine:

Ash-Shafii رحمه الله تعالی alisimulia toka kwa Malik toka kwa Naafi toka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ شَرِبَ الْخَمْرَ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ لَمْ يُبْ مِنْهَا حُرْمَتَهَا فِي الْآخِرَةِ»

“Yeyote anayekunywa Pombe hapa duniani na asitubie, atanyimwa kesho Kiyama.”

Bukhari na Muslim waliipokea Hadithi hii,² Muslim aliipokea toka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«كُلُّ مُسْكِرٍ خَمْرٌ، وَكُلُّ مُسْكِرٍ حَرَامٌ، وَمَنْ شَرِبَ الْخَمْرَ فَمَاتَ وَهُوَ يُدْبِنُهَا وَلَمْ يُبْ مِنْهَا، لَمْ يَشْرَبْهَا فِي الْآخِرَةِ»

“Kila kinacholevya ni Pombe na kila kilevi ni haramu. Yeyote anayekunywa Pombe na akifa na huku imemtawala, bila kutubia kwa kunywa, hatoinywa siku ya Kiyama.”³

¹ Ibn Abu Hatim 4:1196.

² Musnad Ash-Shafi na 1763, Al-Bukhari na 5575, Muslim 2003.

³ Muslim na. 2003.

Abdur-Rahman bin Harith bin Hisham alisema kuwa alimsikia Uthman bin Affan رضي الله عنه akisema, “Epukeni Pombe, kwani ni mama wa madhambi yote. Alikuwapo mtu kabla ya zama zenu ambaye alikuwa akimuabudu Allah تعالى na akajitenga na watu. Baadaye mwanamke muovu alimpenda na akamtuma mtumishi wake wa kike akamuambia kuwa walimtaka aje ashuhudie jambo. Hivyo akafuatana na mtumishi yule. Kila walipopita kwenye mlango mtumishi yule aliukomea, mpaka alipomkuta mwanamke mzuri akiwa na mtumishi wa kiume na chombo chenye Pombe. Alimuambia, “Wa Llah! Sikukualika kushuhudia lolote, bali kumzini, au kumuua huyu kijana au kunywa Pombe hii! Hivyo akanywa pombe, na akawa anataka zaidi mpaka akalewa, hivyo hakufikiria jambo jingine ila kumzini mwanamke yule na kumuua mtumishi wake. Kwa hiyo, epuka Pombe, kwa sababu haikai pamoja na Imani, bali kimojawapo hufukuza kingine (kutoka moyoni).” Hadithi hii ilipokewa na Bayhaqi.¹ Kauli hii ina isnadi ya uhakika. Abu Bakar bin Abi Ad-Duniya alinukuu kauli hii ndani ya kitabu chake juu ya kuharamishwa vilevi, lakini mapokezi yake ni kutoka kwa Mtume ﷺ. Kuinasibisha na Uthman رضي الله عنه ni sahihi zaidi na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Ahmad bin Hanbal alirekodi kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Pombe ilipoharamishwa, baadhi ya watu walisema, “Ewe Mtume! Itakuwaje kwa ndugu zetu waliokufa na huku wakinywa *Khamr*?” Allah تعالى Aliteremsha Aya hii.

لَيْسَ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جُنَاحٌ فِيمَا طَعَمُوا

“Si dhambi juu ya walioamini na wakatenda mema kwa walivyo vila (zamani)...”

Muwelekeo wa *Qiblah* ulipobadilishwa kutoka Baitul Makdisi kuwa Makkah, baadhi ya watu waliuliza, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Kuna hukumu gani kwa ndugu zetu waliokufa na huku wakisali kuelekea Baitul Makdisi?’ Allah تعالى Alishusha Aya hii,

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ

“Na Mwenyezi Mungu Hakuwa mwenye kuipoteza Imani yenu.”
(2:143)²

Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema Aya hii ilipotemshwa,

¹ Al-Bayhaqi 8:287, 288.

² Ahmad 1:295.

لَيْسَ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جُنَاحٌ فِيمَا طَعِمُوا إِذَا مَا اتَّقَوْا وَءَامَنُوا

“Si dhambi juu ya walio amini na wakatenda mema kwa walivyo vila (zamani) maadamu wakichamungu na wakiamini.”

Ilipoteremshwa,

«قِيلَ لِي: أَنْتَ مِنْهُمْ»

“Niliambiwa wewe ni miongoni mwao”.

Hadithi ilikusanywa na Muslim, At – Tirmidhi na An-Nasai.¹

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَيَبْلُوكَنَّكُمْ اللَّهُ بِشَيْءٍ مِّنَ الصَّيْدِ تَنَالَهُ أَيْدِيكُمْ وَرِمَاحُكُمْ لِيَعْلَمَ اللَّهُ مَن يَخَافُهُ بِالْغَيْبِ ۚ فَمَنِ اعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٩٤﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْتُلُوا الصَّيْدَ وَأَنْتُمْ حُرْمٌ ۚ وَمَن قَتَلَهُ مِنكُم مُّتَعَمِّدًا فَجَزَاءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعَمِ سَحْكُمُ بِهِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ هَدْيًا بَلِغَ الْكَعْبَةِ أَوْ كَفَّرَةٌ طَعَامُ مَسْكِينٍ أَوْ عَدْلٌ ذَلِكِ صِيَامًا لَّيَذُوقُوا وَنَالَ أَمْرَهُ ۗ عَفَا اللَّهُ عَمَّا سَلَفَ ۚ وَمَن عَادَ فَيَنْتَقِمُ اللَّهُ مِنْهُ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ ذُو انْتِقَامٍ ﴿٩٥﴾

94. Enyi mlioamini! Mwenyezi Mungu Atakujaribuni kidogo kwa wanyama wa kuwinda inayowafikia mikono yenu na mikuki yenu, ili Mwenyezi Mungu Amjue nani anayemkhofu kwa ghaibu. Basi atakayeruka mipaka baada ya hayo atapata adhabu kali.

95. Enyi mlioamini! Msiue wanyama wa kuwinda nanyi mmeharimia katika Hija. Na miongoni mwenu atakayemuua kwa makusudi, basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilichosawa na alichokiua, katika mifugo, kama wanavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu. Mnyama huyo apelekwe kwenye Al Kaaba, au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini; au badala ya hayo ni kufunga, ili aonje ubaya wa jambo lake hili. Mwenyezi Mungu Amekwishayafuta yaliyopita; lakini atakayefanya tena Mwenyezi Mungu Atampa adhabu. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye Kuadhibu.

¹ Muslim 4:1910, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:419, An-Nasai katika Al-Kubra 6:337.

Kuharamishwa Kuwinda Wanyama Pori Katika Maeneo Matakatifu na Wakati wa Kuwa Katika Ihramu

Al-Walibi alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

لَيَبْلُغَنَّكُمْ اللَّهُ بِشَيْءٍ مِّنَ الصَّيْدِ تَنَالَهُ أَيْدِيكُمْ وَرِمَاحُكُمْ

“Mwenyezi Mungu Atakujaribuni kidogo kwa wanyama wa kuwinda inayowafikia mikono yenu na mikuki yenu...” (5:94)

Inahusu, “Wanyama pori dhaifu na wachanga. Allah تعالى Anawatahini waja wake na wanyama pori hao wakiwa katika *Ihram*, kuwa kama wanataka waweza kuwashika kwa mikono yao. Allah تعالى Amewaamuru kuepuka kuwakamata.”¹ Mujahid alisema kuwa,

تَنَالَهُ أَيْدِيكُمْ

“...inayowafikia mikono yenu...” Inahusu mnyama pori mchanga na kindi.

وَرِمَاحُكُمْ

“...na mikuki yenu...”

Ambapo inahusu mnyama pori aliyekomaa.² Muqatil bin Hayyan alisema kuwa Aya hii iliteremshwa wakati wa Umrah ya Al-Hudaybiyyah, wakati wanyama pori na ndege walikuwa wakifuata Misafara ya Waislamu, ambapo hawajapata kuona mfano wake kabla. Allah تعالى Aliwaharamishia kuwawinda wanyama pori wawapo ndani ya ibada ya Hijja au Umra,

لِيَعْلَمَ اللَّهُ مَن تَخَافُهُ بِالْغَيْبِ³

“Mwenyezi Mungu Amjue nani anayemkhofu kwa ghaibu.”³

Kwa hiyo, Allah تعالى Anawajaribu waja Wake na wanyama pori wanaokaribia makazi yao, kama wanapenda, wanaweza kuwashika kwa mikono yao au mikuki hadharani au kwa siri. Hivi ndivyo utiifu wa wale wanaomtii Allah تعالى hadharani na kwa siri inakuwa wazi na inatahiniwa.

¹ At-Tabari 10:584.

² At-Tabari 10:583.

³ Ad-Durr Al-Manthur 3:185.

Katika Aya nyingine Allah تعالى Amesema,

إِنَّ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿٩٠﴾

“Hakika wanaomuogopa Mola wao Mlezi kwa ghaibu, watapata maghfira na ujira mkubwa.”

Allah تعالى Amesema tena,

فَمَنْ أَعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَلِكَ

“Basi atakayeruka mipaka baada ya hayo.”

Baada ya onyo na kitisho, kwa mujibu wa As-Suddi kisha,

فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“...atapata adhabu kali.” Kwa kukataa Amri ya Allah تعالى na yale Aliyoamrisha, baada ya hapo Allah تعالى Amesema,

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْتُلُوا الصَّيْدَ وَأَنْتُمْ حُرْمٌ

“Enyi mlioamini! Msiue wanyama wa kuwinda nanyi mmehirimia katika Hija.”

Aya hii inaharamisha kuua wanyama pori katika hali ya *Ihram*, isipokuwa kwa vile vilivyosamehewa kama ilivyopokewa ndani ya “Sahih mbili, Aishah رضي الله عنها alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«خَمْسٌ فَوَاسِقٌ يُقْتَلْنَ فِي الْجِلِّ وَالْحَرَمِ: الْغُرَابُ، وَالْجِدَاةُ، وَالْعُقْرَبُ، وَالْفَأْرَةُ، وَالْكَلْبُ الْعَقُورُ»

“Vitano ni uchafu vinaweza kuuawa ukiwa katika ihram au hapana; kunguru, ng'e, panya, mwewe na mbwa mwenye kichaa.”¹

Ibn Umar رضي الله عنهما alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«خَمْسٌ مِنَ الدَّوَابِّ لَيْسَ عَلَى الْمُحْرِمِ فِي قَتْلِهَا جُنَاحٌ: الْغُرَابُ، وَالْجِدَاةُ، وَالْعُقْرَبُ، وَالْفَأْرَةُ، وَالْكَلْبُ الْعَقُورُ»

¹ Al-Bukhari na. 3314, Muslim na. 1198.

“Si haramu uwapo ndani ya ibada ya Hijja au Umra kuua aina tano za wanyama, kunguru, kipanga, ng’e, panya na mbwa mwenye kichaa.”¹

Hadithi hii imepokewa ndani ya Sahih mbili.² Ayyub alisimulia kuwa Nafi alisimulia maneno kama yaliyo katika Hadithi hii kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما.³ Ayyub alisema, “Hivyo nilisema kwa Nafi, “Vipi nyoka?” Akasema, “Hapana shaka kuwa kumuua nyoka inaruhusiwa.”⁴ Hukumu juu ya mbwa mwenye kichaa pia inawahusu, mbweha, simba, chui na mfano wake, kwa kuwa wao ni hatari zaidi kuliko mbwa mwenye kicha au kwa sababu neno *kalb* (mbwa) linawahusu wote. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Abu Said رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ aliulizwa juu ya wanyama ambao mtu aliye katika Ibada ya Hijja na Umra “*Muhrim*” anaruhusiwa kuwaua na alisema,

«الْحَيَّةُ، وَالْعَقْرَبُ، وَالْفُؤَيْسِقَةُ، وَيَزِيمِي الْغُرَابَ وَلَا يُقْتَلُهُ، وَالْكَلْبُ الْعَقُورُ،
وَالْحِدَاةُ، وَالسَّبُعُ الْعَادِي»

“Nyoka, ng’e, panya na kunguru – ambaye anapigwa sio kumuua – mbwa mwenye kichaa, mwewe na wanyama Mbuaji.”

Abu ‘Dawud amepokea Hadithi hii, kama alivyofanya At-Tirmidhi, aliyesema kuwa ni “Haram” na Ibn Majah.⁵

Adhabu ya Kuua Mnyama Pori katika Maeneo Matakatifu au Katika Hali ya *Ihram* (Katika Ibada ya Hija na Umra).

Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ قَتَلَهُ مِنْكُمْ مُتَعَمِّدًا فَجَزَاءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعَمِ

“Na miongoni mwenu atakayemuua kwa makusudi, basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilichosawa na alichokiua,”

¹ Al-Muwatta’ 1:356.

² Fat’hul Al-Bari 4:42, Muslim 2:858.

³ An-Nasai 5:190.

⁴ Fat’hul Al-Bari 6:44.

⁵ Abu Dawud 2:424, Tuhfat Al-Ahwadhi 3:576, Ibn Majah 2:1032.

Mujahid bin Jabir alisema, “Maana ya kudhamiria hapa ni kuwa mtu anakusudia kuua mnyama pori huku akisahau kuwa yumo katika *Ihram*. Yeyote aliyeua mnyama pori kwa kudhamiria wakati alijua yuko katika *Ihram* hivyo kosa hili ni kubwa sana na halina fidia (inabatilika Ihramu yake).”¹ Kauli hii ni ngeni. Kauli ya walio wengi ya jopo la wanazuoni “Jamhuri” ni kuwa watalipa fidia kwa kuua mnyama pori ima wamesahau kuwa wako katika *Ihram* au vinginevyo. Az-Zuhri رحمه الله تعالى alisema, “Kitabu (Qur’an) kinasisitiza kutolewa fidia kwa kuua kwa kudhamiria na Sunnah imewajumuisha waliosahau pia.”² Maana ya Kauli hii ni kuwa Qur’an imetaja kutoa fidia kwa madhambi kwa wanaoua wanyama pori kwa makusudi.

لِيَذُوقَ وَبَالَ أَمْرِهِ ۗ عَفَا اللَّهُ عَمَّا سَلَفَ ۗ وَمَنْ عَادَ فَيَنْتَقِمُ اللَّهُ مِنْهُ ۗ

“...ili aonje ubaya wa jambo lake hili. Mwenyezi Mungu Amekwishayafuta yaliyopita; lakini atakayefanya tena Mwenyezi Mungu Atampa adhabu.”

Allah تعالى Atamuadhibu. Sunnah inayojumuisha hukumu iliyotolewa na Mtume ﷺ na Masahaba wake imeonesha ulazima wa kutoa fidia kwa kuua mnyama bila kudhamiria. Qur’an imeamuru fidia kwa kuua kwa kudhamiria. Kuua mnyama pori ni aina ya uharibifu, ambao unahitaji fidia ikiwa imedhamiriwa au haikudhamiriwa, ingawa wale waliodhamiria wamefanya dhambi kuliko wale waliofanya kosa kwa bahati mbaya. Kauli ya Allah تعالى,

فَجَزَاءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعْمِ

“Basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilicho sawa na alichokiua,...”

Basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilicho sawa na alichokiua, inadhihirisha ulazima wa kutoa mnyama badala ya yule aliyeuawa na *Muhrim* aliye katika Ibada ya Hija na Umra. Masahaba walitoa hukumu kuwa ngamia, kwa mfano, ni sawa na mbuni, na ng’ombe sawa na nyumbu, na mbuzi kwa swala. Katika hali ambayo hapana m-badala wa mnyama pori aliyeuawa, Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa watoe fedha Makkah kama sadaka, kama alivyopokea Bayhaqi. Kauli ya Allah تعالى (5:95),

¹ At-Tabari 11:8.

² At-Tabari 11:11.

تَحْكُمُ بِهِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ

“Kama wanavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu.”

Maana yake, ‘Wanaume wawili Waislamu waadilifu wakadirie mnyama sawa na mnyama pori aliyeuawa au thamani yake.’ Ibn Jarir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Abu Jarir Al-Bajali alisema, “Nilimuua swala nilipokuwa katika *Ihram* na nikamueleza swali hilo Umar رضي الله عنه, ambaye alisema, waendee nduguzo wawili ili wakuhukumu. Nikaenda kwa Abdur-Rahman na Sa’d رضي الله عنهما nao wakasema nitoe kondoo wa kiume.”¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliandika kuwa Tariq alisema “Arbid alimuua swala akiwa katika *Ihram* na alikwenda kwa Umar رضي الله عنه ili ahukumiwe. Umar رضي الله عنه alimuambia, sitokuhukumu na wakakata shauri kuwa Arbad lazima atoe mbuzi ambaye alilishwa kwa kupewa maji na nyasi nyingi. Umar رضي الله عنه alitoa maelezo,

تَحْكُمُ بِهِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ

“Kama wanavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu.”²

Kauli ya Allah تعالى،

هَدِيًّا بَلِغَ الْكَعْبَةِ

“Mnyama huyo apelekwe kwenye Al-Kaaba,...”

Inaashiria kuwa mnyama huyu wa fidia lazima apelekwe Ka’bah, yaani, eneo takatifu, ambapo atachinjwa na nyama yake igaiwe kwa masikini wa Eneo Takatifu. Kuna makubaliano ya wanazuoni kuhusu hukumu hii. Allah تعالى Amesema,

أَوْ كَفِّرَةٌ طَعَامُ مَسْكِينٍ أَوْ عَدْلٌ ذَلِكَ صِيَامًا

“...au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini; au badala ya hayo ni kufunga...”

Maana yake: Endapo aliye katika Ibada ya Hijja na Umra - *Muhrim* - hakupata badala sawa na alichokiua au mnyama aliyewindwa hana mbadala wake. Ali bin Abi Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alielezea Aya hii,

¹ At-Tabari 11:27.

² At-Tabari 11:26.

هَدِيًّا بَلِغَ الْكَعْبَةِ أَوْ كَفَّرَةً طَعَامٌ مَسْكِينٍ أَوْ عَدْلٌ ذَلِكِ صَيَّامًا

“...Mnyama huyo apelekwe kwenye Al Kaaba, au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini; au badala ya hayo ni kufunga...”

Iwapo “*Muhrim*” aliye katika lbada ya Hija na Umra alimuua mnyama pori, hukumu yake ni kutoa badala. Akimuua swala, atatoa kondoo atakayechinjwa Makka. Kama hawezi atawalisha masikini sita, vingine afunge siku tatu. Kama atamuua mbawala atatoa ng’ombe. Akishindwa atawalisha masikini ishirini au akishindwa atafunga siku ishirini. Iwapo atamuua Mbuni au Punda milia, atatoa ngamia, au kulisha masikini thelathini au kufunga siku thelathini. Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى wamepokea kauli hii, Ibn Jarir رحمه الله تعالى amezidisha, ‘Anaweza kutoa chakula, kipimo cha Kibaba kitakachowashibisha kila mmoja katika masikini.’¹ Kauli ya Allah تعالى,

لِيَذُوقَ وَبَالَ أَمْرِهِ

“...ili aonje ubaya wa jambo lake hili.”

Maana: Tumemuajibisha alipe fidia ili aonje adhabu ya kosa lake alilolifanya.

عَفَا اللَّهُ عَمَّا سَلَفَ

“Mwenyezi Mungu Amekwisha yafuta yaliyo pita.”

Zama za Jahiliyyah, madhali mtu anakuwa Muislamu mzuri na anafuata sheria za Allah تعالى, na wakati huo huo akijiepusha na makosa. Kisha Allah تعالى Akasema:

وَمَنْ عَادَ فَيَنْتَقِمُ اللَّهُ مِنْهُ

“Atakayefanya tena Mwenyezi Mungu Atampa adhabu.”

Maana: Afanyaye baada ya kuwa imeharamishwa katika Uislamu na kufahamu kuwa imeharamishwa. Ibn Jarayj alisema, “Nilisema kwa Ata, nini maana ya “Allah تعالى Amekwishayafuta yaliyopita;” Alisema, “Ina maana wakati wa enzi za Jahiliyaah.” Nikauliza kuhusu Kauli Yake, “Yeyote aliyefanya kosa hili katika Uislamu Allah تعالى Atamuadhibu naye atalipa fidia.” Nikauliza, “Kuna adhabu

¹ At-Tabari 11:31.

katika kurejea kosa hili uijuayo?" Akasema, "Hapana." Nikasema, "Unadhani mamlaka zina haki gani ya kumuwadhibu?" Akasema, "Hapana kwani ni dhambi alilofanya kati yake na Allah تعالى. Lazima alipe fidia."¹ "Ibn Jarir رحمه الله تعالى amepokea kauli hii.

Ilisemekana kuwa Allah تعالى Atawaadhibu inaashiria kutoa fidia kwa mujibu wa Sa'd bin Jubayr, Ata na wengi miongoni mwa vizazi vya mwanzo na vilivyofuatia.² Walisema kuwa *Muhrim* mtu aliye katika Ibada ya Hijja au Umra anapoua mnyama pori, fidia huwa lazima, bila kujali kuwa lilikuwa kosa la kwanza, la pili au la tatu, na ima ni kwa kudhamiria au kwa makosa. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى,

وَاللَّهُ عَزِيزٌ ذُو انْتِقَامٍ

"Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye Kuadhibu."

Allah تعالى Amesema kuwa Yeye Haonekani katika Udhibiti Wake, hapana awezaye kushindana Naye, au kumzuia kumuadhibu yeyote. Hii ni kwa sababu vitu vyote vilivyoumbwa ni viumbe Vyake na Uamuzi ni Wake, Yeye Ndiye Muweza, na Yeye Ndiye Mdhibiti. Kauli Yake,

ذُو انْتِقَامٍ

"...Mwenye Kuadhibu."

Maana yake: Huwaadhibu wale wanaomuasi kwa kumuasi Yeye.³

* * *

¹ At-Tabari 11:48.

² At-Tabari 11:50.

³ At-Tabari 11:57.

أُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ وَطَعَامُهُ مَتَعًا لَكُمْ وَلِلسَّيَّارَةِ
 مَتَعًا لَكُمْ وَلِلسَّيَّارَةِ وَحُرْمَ عَلَيْكُمْ
 صَيْدُ الْبَرِّ مَا دُمْتُمْ حُرْمًا ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ
 الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٩٦﴾ * جَعَلَ اللَّهُ الْكَعْبَةَ الْبَيْتَ
 الْحَرَامَ قِيَمًا لِلنَّاسِ وَالشَّهْرَ الْحَرَامَ وَاهْدَى
 وَالْقَلْتَيْدَ ۗ ذَلِكَ لِنَتَلَمَّوْا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي
 السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٩٧﴾
 أَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ وَأَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٨﴾
 مَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلْغُ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ ﴿٩٩﴾
 قُلْ لَا يَسْتَوِي الْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْخَبِيثِ ۗ
 فَاتَّقُوا اللَّهَ يَأْتِيُوا اللَّهَ يَتَأَوَّلِي الْأَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُونَ ﴿١٠٠﴾
 يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ إِنْ تُبَدَّ لَكُمْ تَسْؤُكُمْ
 وَإِنْ تَسْأَلُوا عَنْهَا حِينَ يُنزَّلُ الْقُرْآنُ تُبَدَّ لَكُمْ عَفَا اللَّهُ عَنْهَا
 ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿١٠١﴾ قَدْ سَأَلَهَا قَوْمٌ مِّن قَبْلِكُمْ ثُمَّ
 أَصْبَحُوا بِهَا كَافِرِينَ ﴿١٠٢﴾

أُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ وَطَعَامُهُ مَتَعًا لَكُمْ
 وَلِلسَّيَّارَةِ مَتَعًا لَكُمْ وَحُرْمَ عَلَيْكُمْ
 صَيْدُ الْبَرِّ مَا دُمْتُمْ حُرْمًا ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ
 الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٩٦﴾ * جَعَلَ اللَّهُ الْكَعْبَةَ الْبَيْتَ
 الْحَرَامَ قِيَمًا لِلنَّاسِ وَالشَّهْرَ الْحَرَامَ وَاهْدَى
 وَالْقَلْتَيْدَ ۗ ذَلِكَ لِنَتَلَمَّوْا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي
 السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ
 عَلِيمٌ ﴿٩٧﴾ أَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ وَأَنَّ
 اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٨﴾ مَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا
 الْبَلْغُ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ ﴿٩٩﴾

96. Nyinyi mmehalalishiwa kuvua vinyama vya baharini na kuvila, kwa faida yenu na kwa wasafiri. Na mmeharimishiwa mawindo

ya wanyama wa bara maadamu mmeharimia Hija. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mtakusanywa kwake.

97. Mwenyezi Mungu Ameifanya Al Kaaba, hii Nyumba Tukufu, ni simamio la watu, na kadhaalika Miezi Mitukufu, na wanyama wa dhabihu, na vigwe. Hayo ili mje ya kwamba Mwenyezi Mungu Anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo katika ardhi, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

98. Jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira, na Mwenye Kurehemu.

99. Haimlazimu Mtume ila kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu Anajua mnachokidhihirisha na mnachokificha.

Wanyama wa Majini ni Halali kwa Aliye katika Ibada ya Hijja

Sa'd bin Al-Musayyib, Said bin Jubayr na wengineo walitoa ufafanuzi juu ya Kauli ya Allah تعالى،

أُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ

“Nyinyi mmehalalishiwa kuvua vinyama vya baharini.”

Hii ina maana, kinachovuliwa kutoka humo,

وَطَعَامُهُ

“...**kuvila**...” Na kuvila vikiwa vikavu na vimetiwa chumvi.¹ Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa wanyama wa majini ni kivuliwacho kutoka majini kikiwa hai,

وَطَعَامُهُ

“...**kuvila**...” Inahusu kinachotupwa ufukweni kikiwa kimekufa. Kauli sawa na hizo zilipokewa kutoka kwa Abubakar As-Siddiq, Zaid bin Thabit, Abdullah bin Amr, Abu Ayyub Al-Ansari, Ikrimah, Abu Salamah bin Abdur-Rahman, Ibrahim An-Nakhai na Al-Hasan Al-Basri رضي الله عنهم. Kauli ya Allah تعالى،

مَتَّعًا لَكُمْ وَلِلسَّيَّارَةِ

“...**kwa faida yenu na kwa wasafiri**...” Yaani, ni manufaa na chakula kwenu.

وَلِلسَّيَّارَةِ

“...**na kwa wasafiri**...” Ni kwa wasafiri walio baharini na wanaosafiri kando kando ya bahari, hayo ameyasema Ikrimah.² Wanazuoni wengine wamesema kuwa wanyama wa majini ni halali kwa wale wanaowavua kutoka baharini, vivyo hivyo inapotiwa chumvi na kutumiwa kama chakula kwa wasafiri wa nchi kavu. Kauli sawa na hiyo ilipokelewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na As-Suddi na wengineo.³

¹ At-Tabari 11:59.

² At-Tabari 11:71.

³ At-Tabari 11:72, 73.

مَتَّعًا لَكُمْ وَلِلسَّيَّارَةِ^ط

“...*kwa faida yenu na kwa wasafiri...*” Na kwa wasafiri kama chakula na riziki kwenu,

وَلِلسَّيَّارَةِ^ط

“...*na kwa wasafiri...*” Na kwa wasafiri walio baharini na wanaosafiri kando kando ya bahari, amesema Ikrimah.¹ Wanazuoni wengine wamesema kuwa wanyama wa majini ni halali kwa wale wanaowavua kutoka baharini. Vivyo hivyo inapotiwa chumvi na kutumiwa kama chakula kwa wasafiri na nchi kavu. Kauli sawa na hiyo ilipokelewa kutoka kwa Ibn Abbas, Mujahid na As-Suddi na wengineo رضي الله عنهم.² Imam Malik bin Anas amepokea kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alipeleka jeshi upande wa pwani na alimteua Abu Ubaydah bin Al-Jarrah رضي الله عنه kuwa kamanda, na jeshi lilikuwa na watu mia tatu, pamoja nami. Tulitembea mpaka tukafika pahala na chakula chetu kilikaribia kuisha. ‘Abu Ubaydah رضي الله عنه alituamuru kuandaa chakula kwa ajili ya safari, na kilitiwa ndani ya mifuko miwili. Abu Ubaydah رضي الله عنه alikuwa akitugawia sehemu ndogo mpaka kilipoisha. Kila mmoja wetu alipewa tende moja tu.” Mimi (mmoja wa wapokezi kutoka kwa Jabir) nilisema, “Tende moja ilikutoshaje?” Jabir رضي الله عنه alijibu, “Tulijua thamani yake ilipokwisha.” Jabir رضي الله عنه aliongeza, “Tulipofika ufukweni wa bahari tuliona samaki mkubwa kama kilima. Jeshi lilimla kwa siku kumi na nane. Kisha Abu Ubaydah رضي الله عنه aliamuru mbavu mbili za mnyama huyo zitandikwe juu ya ardhi. Kisha akaamuru ngamia wa kike apitishwe chini ya mbavu hizo mbili (ili kufanya tao) na akapita bila kuzigusa.”³ Hadithi ilikusanywa pia ndani ya Sahih Mbili.⁴ Malik amepokea kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Mtu mmoja alimuuliza Mtume ﷺ, ‘Ewe Mjumbe wa Allah, Tunapoenda baharini huchukua maji kidogo na huyatumia kwa udhu, na tunapata kiu. Je, tunaweza kutumia maji ya bahari kwa ajili ya Udhu?’ Mtume ﷺ akajibu,

«مَنْ الطَّهْرُ مَاؤُهُ الْجِلُّ مَيْتُهُ»

“Maji yake ni yenye kutoharisha na vilivyo kufa katika bahari ni halali.”⁵

¹ At-Tabari 11:71.

² At-Tabari 11:72, 73

³ Al-Muwata’ 2:930.

⁴ Fat’hul Al-Bari 5:152, Muslim 3:1535.

⁵ Al-Muwatta’ 1:22.

Maimamu wawili, Ash-Shafii na 'Ahmad bin Hanbal waliandika Hadithi hii, pamoja na wakusanyaji wane wa *Sunan*. Al-Bukhari, At-Tirmidhi na Ibn Hibban waliipa daraja la Sahih. Hadithi hii imepokewa pia kutoka kwa Mtume ﷺ na Masahaba wengine.¹

Kuwinda Wanyama wa Bara ni Haramu kwa Mwenye Kuhiji

Allah تعالیٰ Amesema:

وَحُرْمَ عَلَيْكُمْ صَيْدُ الْبَرِّ مَا دُمْتُمْ حُرْمًا

“Na mmeharimishiwa mawindo ya wanyama wa bara maadamu mmeharimia Hija.”

Kuwinda wanyama ni haramu kwa mtu aliye katika Ibada ya Hijja, na kama atawinda, atalazimika kutoa fidia, na ataandikiwa madhambi iwapo atafanya kwa makusudi. Kama atawinda kimakosa, atatakiwa kulipa fidia na hatoruhusiwa kula nyama yake, kwa sababu aina hii ya mnyama kwake yeye ni sawa na nyamafu, kadhalika na walio katika Ibada ya Hija. Iwapo mtu asiye katika Ibada ya Hijja atawinda na kumpa chakula *Muhrim*, *Muhrim* haruhusiwi kula nyama hiyo iwapo aliwinda kwa ajili yake. As-Sa'b bin Jaththamah رضي الله عنه alisema kuwa alimpa pundamilia Mtume ﷺ kama zawadi katika eneo la Waddan au Ab'wa, Mtume ﷺ aliirudisha. Mtume ﷺ alipoona athari ya kurudisha kwake zawadi kwenye uso wa As-Sa'b رضي الله عنه alisema,

«إِنَّا لَم نَرِدُّهُ عَلَيْكَ إِلَّا أَنَا حُرْمٌ»

“Tumekurejeshea kwa sababu tuko katika Ibada ya Hijja.”²

Imepokewa katika Sahih Mbili. Mtume ﷺ alidhani kuwa As-Sa'b aliwinda Punda milia kwa ajili yake, akakataa kuipokea. Vinginevyo, mwenye kuhiji anaruhusiwa kula nyama iliyowindwa na asiyehiji. Kwani Abu Qatadah alipowinda punda milia wakati hakuwa ni mwenye kuhiji na aliwapa waliokuwa katika ibada ya Hijja, wakasita kula. Wakamuuliza Mtume ﷺ, naye aliwajibu,

¹ *Musnad Ash-Shafi* na. 25, Ahmad 2:2387, Abu Dawud na. 83, At-Tirmidhi na. 69, An-Nasai 1:50, Ibn Majah na. 386, Ibn Khuzaymah na. 111, Ibn Hibban na. 119.

² Al-Bukhari na. 1825, 2573, Muslim 2:850.

«هَلْ كَانَ مِنْكُمْ أَحَدٌ أَشَارَ إِلَيْهَا أَوْ أَعَانَ فِي قَتْلِهَا؟»

“Kuna mmoja wenu aliyemuonesha au alisaidia kumuwinda?” Walijibu, “Hapana.” Alisema,

«فَكُلُّوا»

“Kuleni.” Naye akala. Hadithi hii pia imo katika Sahih Mbili kwa maneno tofauti.¹

وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشُرُونَ ﴿٩٦﴾

“Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mtakusanywa Kwake.”

Allah تعالى Anasema, “Mcheni Allah تعالى, Enyi watu, na mfahamu Uwezo Wake, kwa kutii amri Zake na kujiepusha na Anayowakataza, katika ‘Aya zilizoteremshwa kwa Mtume ﷺ zinazokataza pombe, kucheza kamari, kutambika masanamu na kupiga ramli, pamoja na kuwinda mnyama pori na kuwaua mkiwa katika Ibada ya Hija. Kwa Allah تعالى mtarejea Kwake na Atawaadhibu kwa kutomtii Yeye na Atawalipa kwa kumtii.”

جَعَلَ اللَّهُ الْكَعْبَةَ الْبَيْتَ الْحَرَامَ قِيَمًا لِلنَّاسِ

“Mwenyezi Mungu Ameifanya Al Kaaba, hii Nyumba Tukufu, ni simamio la watu...”

Allah تعالى Anasema, Ameifanya Ka’bah kuwa nyumba Takatifu yenye hifadhi na salama, kwa watu wasio na kiongozi, kuwazuia wenye nguvu kuchupa mipaka dhidi ya watu dhaifu, waovu dhidi ya wema, na wakandamizaji dhidi ya wakandamizwaji.

وَالشَّهْرَ الْحَرَامَ وَالْهَدْيَ وَالْقَلْبَيْدَ

“Na kadhaalika Miezi Mitukufu, na wanyama wa dhabihu, na vigwe.”

Allah تعالى Anasema kuwa alifanya dhana hizo kama hifadhi ya amani kwa watu, kama alivyowafanyia Ka’bah hifadhi salama ili atofautishe kati yao,

¹ Fat’hul Al-Bari 9:528, Muslim 2:362. Ibn Kathir ametaja Aya nne tu kuanzia Aya 96 mpaka 99 na akaeleza vyema sehemu ya Aya nambari 96, lakini hakuelezea sehemu iliyobakia ya Aya nyingine (97-99). Hali hii ipo katika nakala ya Tafsiri yake, na huenda alisahau kufanya hivyo, kwani hayumkini kuwa wale walio na kitabu hiki walisahau kunakili sehemu hii tu. Hivyo tulitumia muhtasari wa Tafsiri ya Aya hizi kutoka kwa Imam wa Tafsiri, Ibn Jarir ‘At Tabari kikomo cha uwezo wetu, kwa msaada wa Allah تعالى.

kwani hiyo ni hifadhi na alama ya maisha na dini yao. Allah تعالى Alifanya Ka'bah, Mwezi Mtukufu, wanyama wa dhabihu, waliovishwa vigwe kama alama kuwa ni hifadhi salama kwa Waarabu waliokuwa wakizona alama hizo huwa takatifu. Hivyo, alama hizo zilikuwa sawa na chifu (kiongozi) anayotiiwa na wafuasi wake, na anayetunza utulivu na usalama wa raia. Ama kuhusu Ka'bah inajumuisha mipaka yote. Allah تعالى Ameziita "Haram" kwa sababu aliharamisha kuwindwa wanyama wake na kuharibu miti au majani yake. Vivyo hivyo, Ka'bah, Mwezi Mtukufu, wanyama wa dhabihu na wanyama waliovishwa vigwe zilikuwa alama katika ustawi wa maisha ya Waarabu. Alama hizo zilikuwa takatifu katika zama za Jahiliyyah. Baada ya kuja Uislamu zikawa alama za matukufu ya Hajj, ibada zao nyingine na Qibla ya Sala.

ذَلِكَ لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٩٦﴾

"Hayo ili mjue ya kwamba Mwenyezi Mungu Anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo katika ardhi, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

Allah تعالى Amesema, "Enyi watu, Nilifanya alama hizi kuwa hifadhi yenu, ili mumjue Aliyefanya alama hizo ambazo zina faida katika maisha yenu, Anayewapa ulinzi, pia Anajua kila kitu mbinguni na ardhini ambavyo vinawaletea faida sasa au baadaye. Jua kwamba Anafahamu kila kitu na kuwa hapana amali au jambo lolote linalopita bila ya Kulihifadhi, ili Awalipe wale watendao mema kwayo na wale waliotenda maovu."

أَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ وَأَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٧﴾

"Jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghira, na Mwenye Kurehemu."

Allah تعالى Anasema, jueni kuwa Mola wenu ambaye Anafahamu kila kilichomo mbinguni na ardhini, na Asiyepitwa na amali zenu za dhahiri au siri ni Mkali wa Kuadhibu kwa wanaomuasi na kumkengeuka. Pia Anasamehe madhambi ya wale wanaotii na kutubia Kwake, Anawarehemu zaidi kuliko Kuwaadhibu kutokana na dhambi walizotubu.

مَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلَاغُ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ ﴿٩٨﴾

"Haimlazimu Mtume ila kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu

Anajua mnachokidhihirisha na mnachokificha."

Hilo ni onyo la Allah تعالیٰ kwa waja wake. Anasema, Mjumbe wetu, Tuliye mtuma kwenu, alitakiwa kukufikishieni ujumbe wetu ambapo kulipa utiifu na kuadhibu waasi ni juu Yetu. Utiifu wa wanaokubali Ujumbe Wetu haujifichi Kwetu, kama ilivyo kwa wanaoasi na kukataa Ujumbe Wetu. Tunajua kila mmoja wenu afanyalo, alilolidhihirisha, analotangaza na analotamka kwa ulimi wake, na mnachoficha nyoyoni mwenu, ima imani, kutoamini, yakini, shaka au unafiki. Yeye ni Muweza, na hapana kinachofichwa nyoyoni, wala vitendo dhahiri vya roho mbinguni na ardhini vilivyoweza kukwepa ufahamu Wake. Mkononi Mwake Pekee, kuna malipo na adhabu na Anastahiki kuogopwa, kutiwa na kutoasiwa,

قُلْ لَا يَسْتَوِي الْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْخَبِيثِ ۚ فَاتَّقُوا اللَّهَ يَا أُولِي الْأَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٦﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنَ أَشْيَاءَ إِن تَبَدَّلَ لَكُمْ مَنُومٌ وَإِن تَسْأَلُوا عَنْهَا حِينَ يُنزَلُ الْقُرْءَانُ تُبَدَّلَ لَكُمْ ءَعَفَا اللَّهُ عَنْهَا ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿٩٧﴾ قَدْ سَأَلَهَا قَوْمٌ مِّن قَبْلِكُمْ ثُمَّ أَصْبَحُوا بِهَا كَافِرِينَ ﴿٩٨﴾

100. Sema: Haviwi sawa viovu na vyema ujapo kupendeza wingi wa viovu. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili, ili mpate kufanikiwa.

101. Enyi mliaoamini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni. Na mkiyauliza inapoteremshwa Qur'ani mtabainishiwa. Mwenyezi Mungu Amesamehe hayo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira Mpole.

102. Waliyauliza hayo watu wa kabla yenu, kisha wakawa wenye kuyakataa.

Allah تعالیٰ Anamuambia Mjumbe wake ﷺ,

قُلْ "Sema..."ewe Muhammad,

لَا يَسْتَوِي الْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ

"...Haviwi sawa viovu na vyema ujapo kupendeza..."Ewe mwanaadamu,

كَثْرَةُ الْخَبِيثِ ۚ

"Wingi wa viovu." Wengi wa uovu. Aya hii ina maana, kidogo kilicho halali

kilichonufaisha ni bora kuliko kingi kiovu chenye kudhuru. Kama ilivyokuja katika Hadithi: kilicho kidogo na kunufaisha ni bora kuliko kilicho kingi kikapumbaza.

فَاتَّقُوا اللَّهَ يَتَأْتِي آلَآبَابِ

“Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili,...” Wenye akili timamu, kuepuka na kuacha vilivyokatazwa, na mridhike na vile mlivyoruhusiwa kufanya.

لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُونَ

“...Ili mpate kufanikiwa...” Hapa duniani na kesho akhera.

Kuuliza Kusiko kwa Lazima Kumekatazwa

Allah تعالى Amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ إِن تُبَدَ لَكُمْ تَسْؤُكُمْ

“Enyi mlioamini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni.”

Aya hii inahusu Allah تعالى Kuwafundisha mwenendo mwema waja wake waumini, kwa Kuwakataza kuuliza mambo yasiyo na maana. Kwa kuwa wakipata majibu wanayoyatafuta, yanaweza kuwaletea matatizo ambayo itakuwa magumu pindi wanapoyasikia. Al Bukhari amepokea kuwa Anas bin Malik alisema, “Mtume ﷺ alitoa hotuba tofauti na nilivyowahi kusikia kabla. Katika hotuba hiyo, alisema,

«لَوْ تَعْلَمُونَ مَا أَغْلَمُ، لَضَحِكْتُمْ قَلِيلًا، وَلَبَكَيْتُمْ كَثِيرًا»

“Kama mngelijua ninayoyajua, mngelicheka kidogo na kulia sana.”

Masahaba wa Mtume ﷺ walifunika nyuso zao na sauti ya kilio ilikuwa inatokea kwenye vifua vyao. Mmoja wao aliuliza, “Baba yangu ni nani?” Mtume ﷺ alisema, “Fulani bin fulani.” Aya hii iliteremshwa baadaye:

لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ

“..Msiulize mambo..”¹ Muslim, Ahmad, At-Tirmidhi na An-Nasai waliiandika Hadithi hii.² Ibn Jarir رحمه الله تعالى amepokea kuwa ‘Qatadah aliitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى

¹ Fat’hul Al-Bari 8:130

² Fat’hul Al-Bari 11:326, Muslim 4:1832, Ahmad 3:180, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:421, Tuhfat Al-Ashraf 1:413.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ إِن تُبَدَّ لَكُمْ تَسْؤُكُمْ

“Enyi mlioamini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni.”

Anas bin Malik aliisimulia, mara moja watu walikuwa wakimsaili Mtume ﷺ mpaka wakamkasirisha. Hivyo alipanda juu ya Mimbar na kusema,

«لَا تَسْأَلُونِي النَّيْمَ عَنْ شَيْءٍ إِلَّا يَبِيْتُهُ لَكُمْ،

“Mtakachoniuliza chochote leo, nitawabainishia!”

Masahaba wa Mtume ﷺ wakaogopa kuwa huo ulikuwa mwanzo wa tukio kubwa, nikaangalia upande wa kulia na kushoto kwangu, nikawaona watu wameziba nyuso zao, wakilia. Mtu mmoja mbishi anayesemekana kuwa na baba mwingine, si baba yake hasa aliuliza, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Baba yangu nani?’ Mtume ﷺ akamjibu, ‘Baba yako ni Hudhafa.’ Umar رضي الله عنه alisimama alipoona hasira ya Mtume usoni mwake na akasema, “Tunamkubali Allah تعالى kama Mola, Uislamu kama Dini yetu na Muhammad ﷺ kama Mjumbe wetu, tunamkimbilia Allah katika kujikinga na uovu na fitna (Fitan).” Mtume ﷺ alisema,

«لَمْ أَرْ فِي الْخَيْرِ وَالشَّرِّ كَالْيَوْمِ قَطُّ، صُورَتْ لِي الْجَنَّةُ وَالنَّارُ حَتَّى رَأَيْتُهُمَا دُونَ الْحَاظِ،

“Sijashuhudia wema na uovu kama ilivyo leo. “Pepo na Moto vimeoneshwa kwangu hadi nikazona kuwa zipo bila kizuizi chochote.”¹

Hadithi hii imepokewa ndani ya Sahih Mbili kutoka kwa Sa’id.²

Al-Bukhari amepokea toka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, ‘Baadhi ya watu walikuwa wakimuuliza Mtume ﷺ kwa istihzai. Mmoja wao aliuliza, “Baba yangu nani?’ Ambapo mwingine aliuliza, “Ngamia wangu yuko wapi?”, alipopoteza ngamia wake. Allah تعالى Aliteremsha Aya hii juu yao,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ إِن تُبَدَّ لَكُمْ تَسْؤُكُمْ

“Enyi mlioamini! Msiulize mambo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni.”³

¹ At-Tabari 11:100.

² Fat’hul Al-Bari 13:47, Muslim 4:1834.

³ Fat’hul Al-Bari 8:130.

Imam Ahmad amepokea kuwa Ali رضي الله عنه alisema, "Aya hii ilipotremshwa

وَاللَّهُ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا

"Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kuwendea."

Na kwa ajili ya Allah تعالى imewawajibikia watu kuhiji nyumba hiyo waliuliza, 'Ewe Mjumbe wa Allah? Inatakiwa kila mwaka?' Hakuwajibu, nao wakauliza tena, "Ni kila mwaka?' Hakuwajibu, hivyo waliuliza tena, 'Ni kila mwaka?' Alisema,

«لَا، وَلَوْ قُلْتُ: نَعَمْ لَوَجِبْتُ وَلَوْ وَجِبْتُ لَمَا اسْتَطَعْتُمْ»

"Hapana na ningelisema "Ndiyo' ingelifaradhishwa na kama ingelifaridhishwa, msingeliweza kuitekeleza."

Allah تعالى Aliteremsha,

يَتَأْتِيَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ إِن تُبَدَّ لَكُمْ تَسْؤُكُمْ

"Enyi mlio amini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni."

At-Tirmidhi na Ibn Majah nao wamepokea Hadithi hii.¹ Maneno yaliyo wazi ya Aya hii yanaonesha kuwa tumekatazwa kuuliza mambo ambayo tukijua ukweli wake tutajuta kuuliza. Hivyo ni aula zaidi kuepuka maswali ya aina hiyo.

وَإِن تَسْأَلُوا عَنْهَا حِينَ يُنزَلُ الْقُرْءَانُ تُبَدَّ لَكُمْ

"Na mkiyauliza inapo teremshwa Qur'ani mtabainishiwa."

Maana yake: Mkiuliza yale mliyokatazwa kuulizia, wahyi utakapomshukia Mtume ﷺ mtawekewa wazi.

وَذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

"Na Hilo kwa Mwenyezi Mungu ni jepesi."

عَفَا اللَّهُ عَنْهَا

"Mwenyezi Mungu Amesamehe hayo." Mlichofanya kabla ya hili,

¹ Ahmad 1:113, At-Tirmidhi na. 3055, Ibn Majah na. 2884.

وَاللَّهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira Mpole.”

Msiulize juu ya mambo yasiyo na hukumu, kwani kutokana na maswali yenu, hukumu nzito inaweza kuwekwa. Hadithi inasema:-

«أَعْظَمُ الْمُسْلِمِينَ جُرْمًا مَنْ سَأَلَ عَنْ شَيْءٍ نَهَى يُحْرَمُ، فَحُرِّمَ مِنْ أَجْلِ مَسْأَلَتِهِ»

“Kosa kubwa kwa Muislamu ni yule anayeuliza jambo fulani lisiloharamishwa, hivyo likaharamishwa kwa sababu ya kuuliza kwake juu ya jambo hilo.”¹

Imepokewa ndani ya Sahih kuwa Mtume ﷺ alisema,

«ذَرُونِي مَا تَرَكْتُكُمْ، فَإِنَّمَا أَهْلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ كَثْرَةَ سؤَالِهِمْ وَاخْتِلَافُهُمْ عَلَى أَنْبِيَائِهِمْ»

“Niwachieni kama nilivyowaachia, wa kabla yenu waliangamizwa kwa kuuliza maswali mengi na kubishana na Mitume wao.”²

Hadithi ya kuaminika pia inaeleza,

«أَنَّ اللَّهَ تَعَالَى فَرَضَ فَرَائِضَ فَلَا تُضَيُّوهُمَا، وَحَدَّ حُدُودًا فَلَا تَعْتَدُوهَا، وَحَرَّمَ أَشْيَاءَ فَلَا تُنْتَهِكُوهَا، وَسَكَتَ عَنْ أَشْيَاءَ رَحِمَهُ بِكُمْ غَيْرَ نَسْيَانٍ فَلَا تَسْأَلُوا عَنْهَا»

“Allah, Aliyetukuka, amefaradhisha baadhi ya mambo ya wajibu, basi msiyadharau; Ameweka mipaka, basi msiichupe; Ameharamisha baadhi ya vitu, basi msiyafanye; na Ameyaacha baadhi ya mambo bila kuyawekea sheria, kama rehema kwenu, na sio kuwa Aliyasahau, basi msiulize juu yake.”³

Baada ya hapo Allah تعالى Amesema,

قَدْ سَأَلَهَا قَوْمٌ مِّن قَبْلِكُمْ ثُمَّ أَصْبَحُوا بِهَا كَافِرِينَ ﴿٩٦﴾

“Waliyauliza hayo watu wa kabla yenu, kisha wakawa wenye kuyakataa.”

¹ Al-Bukhari na. 7289, Muslim na. 2358.

² Muslim 4:1831.

³ Al-Bukhari 4623 na Muslim 2856.

Maana yake: Watu wa kabla yenu waliuliza maswali ya aina hiyo na walijibiwa. Hawakutumia majibu hayo, wakawa makafiri kwa ajili hiyo. Haya yalijiri kwa sababu waliwekewa wazi hukumu, lakini hawakufaidika, kwani waliuliza juu ya mambo hayo si kwa kupata uongozi, lakini kwa kufanya istihizai na inadi.



مَا جَعَلَ اللَّهُ مِنْ حَيْرَةٍ وَلَا سَابِيَةٍ وَلَا وَصِيْلَةٍ وَلَا حَامِرٍ
 وَلِيَكِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَأَكْثَرُهُمْ لَا
 يَعْقِلُونَ ﴿١٠٣﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَإِلَىٰ
 الرَّسُولِ قَالُوا حَسْبُنَا مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ ءِآبَاءَنَا ؕ أُولَٰئِكَ كَانَ
 ءِآبَاؤُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ ﴿١٠٤﴾ يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا عَلَيْهِمْ أَنْفُسَهُمْ ۖ لَا يَضُرُّهُمْ مَن ضَلَّ إِذَا اهْتَدَيْتُمْ ۗ
 إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾
 يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا شَهَادَةً بَيْنَهُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ
 الْمَوْتُ حِينَ الْوَصِيَّةِ اثْنَانِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ أَوْ ءَاخِرَانِ
 مِمَّنْ غَيْرُكُمْ إِن تَنَزَّضْتُمْ فِي الْأَرْضِ فَأَصْبَحْتُمْ مَصِيبَةً
 الْمَوْتُ نَحْسُونَهُمَا مِنْ بَعْدِ الْوَصِيَّةِ فَيُقْسِمَانِ بِاللَّهِ إِن
 أَرْتَبْتُمْ لَا نَشْتَرِي بِهِ ثَمَنًا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ وَلَا نَكْتُمُ
 شَهَادَةَ اللَّهِ إِنَّا إِذًا لَّعَمَلُ الْآثِمِينَ ﴿١٠٦﴾ فَإِن عُرِيَ عَلَىٰ أَنَّهُمَا
 اسْتَحَقَّ إِثْمًا فَاخْرَجَانِ يَفُومَانِ مَقَامَهُمَا مِنَ الَّذِينَ
 اسْتَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْأَوْلِيَيْنِ فَيُقْسِمَانِ بِاللَّهِ لَشَهَدْنَا أَحَقَّ
 مِنَ شَهَادَتِهِمَا وَمَا أَعْتَدْنَا إِنَّا إِذًا لَّعَمَلُ الظَّالِمِينَ ﴿١٠٧﴾
 ذَلِكَ أَدَّتْ أَنْ يَأْتُوا بِالشَّهَادَةِ عَلَىٰ وَجْهَيْهَا أَوْ خَافُوا أَنْ
 تُرَدَّ أَمْنٌ بَعْدَ أَيْمَانِهِمْ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَسْمَعُوا ۗ وَاللَّهُ لَا
 يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿١٠٨﴾ * يَوْمَ يَجْمَعُ اللَّهُ الرَّسُلَ
 فَيَقُولُ مَاذَا أُجِبْتُمْ ۗ قَالُوا لَا عِلْمَ لَنَا ؕ إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّمُ
 الْغُيُوبِ ﴿١٠٩﴾

مَا جَعَلَ اللَّهُ مِنْ حَيْرَةٍ وَلَا سَابِيَةٍ
 وَلَا وَصِيْلَةٍ وَلَا حَامِرٍ ۗ وَلِيَكِنَّ الَّذِينَ
 كَفَرُوا يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ ۗ
 وَأَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٠٣﴾ وَإِذَا قِيلَ
 لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَإِلَىٰ
 الرَّسُولِ قَالُوا حَسْبُنَا مَا وَجَدْنَا
 عَلَيْهِ ءِآبَاءَنَا ؕ أُولَٰئِكَ كَانَ
 ءِآبَاؤُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ ﴿١٠٤﴾

103. Mwenyezi Mungu Hakujaalia uharamu wowote juu ya "Bahira" wala "Saiba" wala "Wasila" wala "Hami". Lakini waliokufuru humzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na wengi wao hawatumii akili.

104. Na wanapoambiwa: Njooi kwenye yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, na kwa Mtume, husema: Yanatutosha tuliyouwakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka?

Tafsiri ya Wanyama Waliotajwa.

Al-Bukhari amepokea kuwa Said bin Al-Musayyib alisema, "Bahira" ni ngamia wa kike ambaye maziwa yake yaliachwa kwa ajili ya miungu na masanamu na hapana aliyeruhusiwa kumkama. "Saiba" ni ngamia wa kike aliyeachwa huru kulishwa kwa ajili ya miungu na masanamu, na hakuruhusiwa kubebeshwa kitu. Abu Harayrah عنه رضي الله alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«رَأَيْتُ عَمْرَو بْنَ عَامِرِ الْخُزَاعِيَّ يَجْرُ قُضْبَهُ فِي النَّارِ، وَكَانَ أَوَّلَ مَنْ سَيَّبَ
السَّوَابِ»

*"Nilimuona Amr bin Amir Al-Khuzaiyyi akivuta matumbo yake ndani ya moto, na alikuwa wa mwanzo kuanzisha itikadi ya "Saibah."*¹

Ama kuhusu *Wasilah* ni ngamia wa kike aliyeachwa huru kwa ajili ya miungu wa kisanamu, kwa sababu alizaa ndama jike katika mimba ya pili. Walikuwa wakiwaacha huru aina hiyo ya ngamia kama alizaa ngamia wawili majike bila kuwapo dume kati yao. Ama huhusu *Haam*, ni ngamia dume ambaye ataachwa huru bila kufanya kazi kwa ajili ya miungu wa kisanamu, baada ya kumaliza kazi yake aliyopangiwa. Ngamia dume aliyeachwa huru kufanya kazi katika hali hii anaitwa *Haami*.² Muslim na An-Nasai³ walipokea Hadithi hii. Imam Ahmad amepokea kuwa Abdullah bin Mas'ud عنه رضي الله alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ أَوَّلَ مَنْ سَيَّبَ السَّوَابِ وَعَبَدَ الْأَضْنَامَ أَبُو خُزَاعَةَ عَمْرُو بْنُ عَامِرٍ، وَإِنِّي رَأَيْتُهُ
يَجْرُ أَمْعَاءَهُ فِي النَّارِ»

*"Mtu wa mwanzo kuanzisha ada ya Saibah na kuabudu masanamu alikuwa Abu Khuzah, Amr bin Amir. Nilimuona akiburuzi matumbo yake ndani ya moto."*⁴

Amr aliyetajwa katika Hadithi ya hapo juu ni mtoto wa Luhay bin Qamah, mmoja wa machifu wa kabila la Khuzaah ambao walikuwa waangalizi wa nyumba ya Allah تعالى baada ya kabila la Jurhum. Alikuwa wa mwanzo kubadilisha dini ya Ibrahimu (*Al-Khalil* – Makkah) عليه السلام alileta ibada za masanamu katika eneo la Hijaz. Na akawawekea watu sharia za Kijamii za

¹ Al-Bayhaqi 10:12.

² *Fat'hul Al-Bari* 8:133.

³ Muslim 4:2192, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:338.

⁴ Ahmad 1:446.

kuabudu masanamu na kuwachinjia wanyama. Allah تعالى Amesema katika Surat Al-An'am,

وَجَعَلُوا لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ مِنَ الْحَرْثِ وَالْأَنْعَامِ نَصِيبًا

“Na wamemuwekea sehemu Mwenyezi Mungu katika mimea na wanyama Alioumba...” (6:136)

Ama *Bahirah*, Ali Bin Abi Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Ni ngamia wa kike ambaye amezaa mara tano. Baada ya hapo, waliangalia aliyezaliwa watano, kama alikuwa dume, wangelimchinja na kuliwa na wanaume tu bila wanawake. Kama alikuwa wa kike, wangelimkata masikio yake. Huyu ndiye *Bahirah* (hapana aruhusiwaye kumkama).¹ As-Suddi na wenzake walitaja kauli kama hiyo.² Ama *Saibah*, Mujahid alisema kuwa ni kondoo, na alitaja maana sawa na hiyo kwa *Bahirah*. Alisema anazaa majike sita na anakuwa katika hali yake, pindi tu anapozaa wa saba na akawa dume, jike au madume mawili humchinja na nyama yake huliwa na wanaume tu.³

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema kuwa *Saibah* ni ngamia jike ambaye amezaa majike kumi, bila kuzaa dume katikati yao; watamuacha huru na haikuwa ruhusa kumpanda, kukata manyoya yake au kumkama isipokuwa kwa ajili ya wageni tu. Abu Rawq alisema, “*Saibah* - ni pale mtu anapofanikiwa jambo lake hutoa katika mali yake Ngamia au kitu kingine, na atamuacha huru Ngamia huyo jike kwa masanamu (kushukuru kwa mafanikio). Baada ya hapo kila alichozaa kiliachwa huru kwa ajili ya miungu ya masanamu.” As-Suddi alisema, “Wakati mtu anapofanikisha mambo yake au alipona, au mali yake iliongezeka, aliitoa mali yake kwa ajili ya miungu ya masanamu. Wale waliojaribu kutwaa mali ya *Saibah* waliadhibiwa hapa duniani.

Ama kuhusu *Wasilah*, Ali bin Abi Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Ni kondoo anayezaa mara saba, iwapo atazaa dume katika mimba yake ya saba, wanaume tu ndio watakula nyama yake. Iwapo atazaa jike au jike na dume, wataachwa huru, wakitangaza (kuhusu dume), pacha mwenzake jike amemfanya asiweze kuchinjwa na kuliwa na wao.” Ibn Abi Hatim amepokea kauli hii.⁴ Abdur Razzaq alisimulia kutoka kwa Ma'mar kutoka kwa Az Zuhri alisema kuwa Said bin Al-Musayyab alisema,

¹ At-Tabari 11:129.

² At-Tabari 11:130.

³ At-Tabari 11:128.

⁴ Ibn Abu Hatim 4:1222.

وَلَا وَصِيْلَةٌ

“**Wala wasilah**” (5:103). “Ni ngamia jike anayezaa jike na kisha jike jengine katika mimba ya pili. Aina hiyo ya ngamia ataitwa *Wasilah* wakidai kuwa ana (*Wassalat*) kwa lugha ya kiarabu, kwa maana anaunganisha kati ya majike wawili bila kuzaa dume kati ya wawili hao. Walikuwa wakikata masikio (yao) *Wasilah* na kumuacha huru ale kwa ajili ya masanamu yao.”¹ Maelezo kama hayo yalipokelewa kutoka kwa Imam Malik bin Anas رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى. Muhammad bin Is-haq رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى alisema, Kondoo wa ‘*Wasilah*’ ni yule anayezaa majike kumi kwa mimba tano, akizaa majike mawili kwa kila mimba. Kondoo huyu ataitwa *Wasilah* na ataachwa huru. Chochote atakachozaa kondoo huyu, dume au jike watapewa wanaume na si wanawake, lakini akizaa kiokotwa mtoto aliyekufa, wanaume na wanawake watashirikiana.

Ama *Haami*, Al-Awf amesema kutoka kwa Ibn Abbas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا, “Ngamia dume akimpanda jike mara kumi, watamuita *Ham*, na humuacha huru.”² Ilipokelewa kutoka kwa Abu R’awq na Qatadah. Ali bin Abi Talhah amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا alisema, “*Ham* ni ngamia dume ambaye wanawe wamezaa wana wao, kisha watatangaza, ngamia huyu ni *Haami* (ameuhami) mgongo wake. Kwa hiyo, hawatom-bebesha chochote ngamia huyo, wala kukata manyoya yake, wala hawatamzuia kulishwa popote, au kunywa katika hodhi yoyote, hata kama hodhi hiyo si ya mmiliki wa Ngamia huyo.”³ Ibn Wahb alisema, “Nilimsikia Malik akisema, “Ama *Ham*, ni ngamia wa kiume ambaye hupangiwa idadi ya kupanda majike, na amalizapo kupandisha idadi hiyo huwekewa manyoya ya tausi na ataachwa huru.” Maoni mengine yalitolewa kuelezea Aya hii.

Kuna Hadithi juu ya somo hili aliyopokea Ibn Abi Hatim kutoka kwa Abi Is-haq As-Sabiyyi kutoka kwa Al-Ahwas Al-Jushami kutoka kwa baba yake Malik bin Nadhlah ambaye alisema, “Nilikuja kwa Mtume ﷺ nimevaa nguo kuukuu. Akaniambia,

«هَلْ لَكَ مِنْ مَالٍ؟»

“Je, Una mali yoyote?” Nikamjibu, “ndiyo” Akaniuliza,

¹ Abdur-Razzaq 1:196.

² At-Tabari 11:129.

³ Ibn Abu Hatim 4:1225.

«مِنْ أَيِّ الْمَالِ؟»

“Aina gani?” Nikasema, “Aina zote, ngamia, kondoo, farasi na watumwa.” Akasema,

«فَإِذَا آتَاكَ اللَّهُ مَالًا فَلْيَرَّ عَلَيْكَ»

“Iwapo Allah Amekupa utajiri, basi uonekane kwako”. Kisha akauliza,

«تُتَبِّحُ إِلَيْكَ وَاقِيَةَ أَذَانِهَا؟»

“Je, ngamia wako wanazaa ndama wenye masikio kamili?”

Nikasema, ‘Ndiyo. Ngamia wangu wanazaa ndama waliotimia viungo.’ Akasema,

«فَلَمَّا تَأْخُذُ الْمَوْسَىٰ نَقْطَعَ آذَانَ طَائِفَةٍ مِنْهَا وَتَقُولُ: هَذِهِ بِحِيرَةٌ، تَسْئَلُ آذَانَ طَائِفَةٍ مِنْهَا وَتَقُولُ: هَذِهِ حُرْمٌ»

“Huenda ukachukua kisu na kukata masikio ya baadhi yao nakusema, “Huyu ni Bahirah na kupasua masikio ya baadhi yao na kunadi, “Huyu ni Mtakatifu?” Nikasema, ‘Ndiyo.’ Akasema,

«فَلَا تَفْعَلْ إِنَّ كُلَّ مَا آتَاكَ اللَّهُ لَكَ حِلٌّ»

“Kwa hiyo usifanye hivyo, kwani utajiri uliopewa na Allah ni halali kwa ajili yako.” Kisha akasema,

«مَا جَعَلَ اللَّهُ مِنْ حَيْرَةٍ وَلَا سَابِيَةٍ وَلَا وَصِيَلَةٍ وَلَا حَامٍ»

“Mwenyezi Mungu Hakujaalia uharamu wowote juu ya “Bahira” wala “Saiba” wala “Wasila” wala “Hami.”

Ama kuhusu ‘Bahirah’, ni mnyama ambaye masikio yake yalikatwa, na mmiliki wa mnyama huyo, au mke wake, mabinti wake au watu wa nyumbani kwake hawaruhusiwi kufaidika na manyoya (sufu) au maziwa yake. Lakini akifa watashiriki kumla. Ama kuhusu ‘Saiba’ ni Ngamia wanaowatoa kama tambiko kwa miungu yao. Ama ‘Wasilah’ ni kondoo anayezaa matumbo sita. Alipozaa kwa mara ya saba, wanamkata masikio na Pembe, wakisema, amefikia kusudio na hawatomchinja, kumpiga au kumzuia kunywa katika bwawa.¹ Hadithi hii iisimuliwa na maelezo ya ziada. Katika mapokezi mengine ya Hadithi hii kutoka

¹ Ibn Abu Hatim 4:1220.

kwa Abu Is'haq kutoka kwa Abu Al-Ahwas, Awf bin Malik alitumia maneno yake mwenyewe (yaani aliyaelezea maneno haya si kama sehemu ya Hadithi yenyewe) na hii ni sahihi zaidi. Imam Ahmad alipokea Hadithi hii kutoka kwa Sufyan bin Uyaynah, kutoka kwa Aba Az-Zaaraa Amr bin Amir kutoka kwa ami yake Abu Al-Ahwas Awaf bin Malik bin Nadlah,¹ kutoka kwa baba yake, Malik bin Nadlah. Mapokezi haya hayana maelezo ya *Bahirah*, *Hamnk*. Yaliyoongezwa kwenye Hadithi hapo juu, na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Kauli ya Allah تعالى،

وَلَكِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَأَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ

“Lakini walio kufuru humzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na wengi wao hawatumii akili.”

Allah تعالى Hakuamrisha hivi vitendo vilivyozushwa na havihesabiki kama vitendo vya utiifu Kwake. Bali, ni washirikina waliozifanya kuwa ibadah na vitendo vya ibada vilivyokuwa vikiwakurubisha kwa Allah تعالى. Lakini wala havikuwasaida kuwa karibu Naye, bali hizi bidaa zitawadhuru.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنزَلَ اللَّهُ وَإِلَىٰ الرَّسُولِ قَالُوا حَسْبُنَا مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا

“Na wanapoambiwa: Njooi kwenye yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, na kwa Mtume, husema: Yanatutosha tuliyowakuta nayo baba zetu.”

Maana yake: Wanapoitwa kwenye Dini ya Allah تعالى, Sharia na Amri na kuacha Aliyoyaharamisha, wanasema, “Waliyokuwa wakiyafanya baba na babu zetu ni mazuri kwetu.” Allah تعالى Amesema,

أُولَٰئِكَ كَانَ أَبَاؤُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ شَيْئًا

“Je? Hata ikiwa baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka”

Maana yake: Hata kama baba zao hawakufahamu au hawakutambua ukweli au kujua njia. Kwa hiyo, naye atawafuata tu, ikiwa ndio hivi, vipi watawafuata wao, hawafuati wao isipokuwa mjinga na aliyopotea njia na waliopotoshwa kuliko walivyokuwa?

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا عَلَيْكُمْ أَنفُسَكُمْ لَا يَضُرُّكُمْ مِّنْ ضَلَّ إِذَا أِهْتَدَيْتُمْ إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ

جَمِيعًا فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٦﴾

¹ Ahmad 4:136.

105. Enyi mlioamini! Kilicho lazima juu yenu ni nafsi zenu. Hawakudhuruni waliopotoka ikiwa nyinyi mmeongoka. Ni kwa Mwenyezi Mungu ndio marudio yenu nyote; basi Atakuwambieni yale mliyokuwa mkiyatenda.

Amri ya Kutaka Mtu Ajirekebishe Nafsi Yake Kwanza

Allah تعالى Anawamuru waja wake waumini kujirekebisha wenyewe na kufanya amali njema kwa wingi kama inavyoyamkinika. Pia Anawaeleza kuwa yeyote atakayejirekebisha, hatodhuriwa na ubaya wa watu waovu, ima ni jamaa zake au vinginevyo. Imam Ahmad amepokea kuwa Qaisi alisema, "Abubakar As-Siddiq رضي الله عنه alisimama, alimshukuru Allah تعالى na akamtukuza na kisha akasema, "Enyi watu! Hakika nyinyi mnasoma Aya hii (someni),

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا عَلَيْكُمْ أَنفُسَكُمْ لَا يَضُرُّكُمْ مِّنْ ضَلَّ إِذَا أِهْتَدَيْتُمْ^٤

"Enyi mlioamini! Kilicho lazima juu yenu ni nafsi zenu. Hawakudhuruni waliopotoka ikiwa nyinyi mmeongoka."

Hakika nyinyi mnaiweka aya hii katika mahali pasipo pake. Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنَّ النَّاسَ إِذَا رَأَوْا الْمُنْكَرَ وَلَا يُغَيِّرُونَهُ، يُوشِكُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ أَنْ يَعْمَهُمْ بِعِقَابِهِ»

"Iwapo watu wataona uovu na wasiubadilisha, basi Allah Atawapelekea adhabu ambayo itawaenea wote."

Mimi (Qays) pia nilimsikia Abubakar رضي الله عنه akisema, "Enyi watu, jiepusheni kusema uongo kwani uongo unapingana na imani."¹

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا شَهَادَةٌ بَيْنَكُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمْ الْمَوْتُ حِينَ الْوَصِيَّةِ اثْنَانِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ أَوْ آخَرَانِ مِّنْ غَيْرِكُمْ إِنْ أَنتُمْ ضَرَبْتُمْ فِي الْأَرْضِ فَأَصَابَتْكُمْ مُصِيبَةُ الْمَوْتِ تَحْبِسُونَهُمَا مِنْ بَعْدِ الصَّلَاةِ فَيُقْسِمَانِ بِاللَّهِ إِنْ آرْتَبْتُمْ لَا نَشْتَرِي بِهِ ثَمَنًا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ وَلَا نَكْتُمُ شَهَادَةَ اللَّهِ إِنَّا إِذًا لَّمِنَ الْآثِمِينَ ﴿١٠٦﴾ فَإِنْ عُرِيَ عَلَىٰ أَنَّهُمَا اسْتَحَقَّا إِثْمًا فَآخَرَانِ يُقِيمَانِ مَقَامَهُمَا مِنَ الَّذِينَ اسْتَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْأَوْلَئِينَ فَيُقْسِمَانِ بِاللَّهِ لَشَهِدْتُنَا أَحَقُّ مِنْ شَهِدَتَيْهِمَا وَمَا أَعْتَدَيْنَا إِنَّا إِذًا لَّمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠٧﴾ ذَلِكَ أَدَّىٰ أَنْ يَأْتُوا

¹ Ahmad 1:5.

بِالشَّهَادَةِ عَلَىٰ وَجْهَيْهَا أَوْ تَخَافُوهَا أَنْ تُرَدَّ أَلْمَانُ بَعْدَ أَيَّمَانِهِمْ ۗ وَأَتَّقُوا اللَّهَ وَأَسْمَعُوا ۗ وَاللَّهُ لَا
يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿١٠٦﴾

106. Enyi mlioamini! Yanapomfikia mauti mmoja wenu na akataka kutoa wasia, basi wawepo mashahidi wawili miongoni mwenu ambao ni waadilifu. Na mnapokuwa safarini, na msiba wa mauti ukakusibuni, basi washuhudie wengineo wawili wasiokuwa katika nyinyi. Mtawazuia wawili hao baada ya Sala na waape kwa Mwenyezi Mungu, mkitilia shaka, wakisema: Hatutopokea thamani yoyote kwa haya hata kwa ajili ya jamaa; na wala hatutaficha ushahidi wa Mwenyezi Mungu; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye dhambi.

107. Ikgundulikana kuwa wawili hao wamestahiki dhambi, basi wawili wengineo kutokana na warithi wenye kudai haki washike makamo ya wa mwanzo. Nao waape kwa Mwenyezi Mungu wakisema: Hakika ushahidi wetu ni wa haki zaidi kuliko ushahidi wa wale. Na sisi hatujafanya dhambi; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa waliodhulumu.

108. Hivi inaelekea zaidi ya kwamba watatoa ushahidi ulio sawa au wataogopa visije vikaletwa viapo vingine baada ya viapo vyao. Na mcheni Mwenyezi Mungu na msikie. Na hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi wapotofu.

Ushahidi wa Mashahidi Wawili Waadilifu kwa Wosia.

Aya hii Tukufu ina Amri Takatifu kutoka kwa Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى،

يَتَأَيُّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا شَهَادَةَ بَيْنِكُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ حِينَ الْوَصِيَّةِ اثْنَانِ

“Enyi mlioamini! Yanapomfikia mauti mmoja wenu na akataka kutoa wasia, basi wawepo mashahidi wawili miongoni mwenu .”

Lazima wawepo mashahidi wawili katika masuala kama hayo ambao ni waadilifu,

ذَوَا عَدَلٍ

“...ambao ni waadilifu.” Hivyo kuwaelezea kuwa ni waadilifu.

مِنْكُمْ

“*Miongoni mwenu*”. Waislamu.

أَوْءَاخْرَانَ مِنْ غَيْرِكُمْ

“...*au washuhudie wengine wasiokuwa katika nyinyi*...” Wasiokuwa Waislamu yaani watu wa kitabu, kwa mujibu wa Ibn Abbas رضي الله عنهما kama Ibn Hatim رحمه الله تعالى alivyopokea.¹ Kisha Allah تعالى Akasema,

إِنْ أَنْتُمْ صَرَّيْتُمْ فِي الْأَرْضِ

“*Na mnapokuwa safarini,...*”

فَأَصَبْتَكُمْ مُصِيبَةً الْمَوْتِ

“*Na msiba wa mauti ukakusibuni,...*” Kuna masharti mawili kuhusu kuwatumia wasio Waislamu miongoni mwa *Dhimmi* kuwa mashahidi wakati hapana Waislamu. Mtu akiwa safarini na anahitaji kuandika wosia, kama Shuraih Al-Qadhi رحمه الله تعالى alivyosema. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alieleza, Shuraih alisema, “Ushahidi wa Mayahudi na Wakristo haukubaliki isipokuwa safarini na hata hivyo ushahidi wao ni katika wosia tu.”² Kauli ya Allah تعالى,

تَحْسِبُونَهُمَا مِنْ بَعْدِ الصَّلَاةِ

“*Mtawazuia wawili hao baada ya Sala*.” Inakusudiwa Sala ya Alasiri, kwa mujibu wa Al-Awfi aliyepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.³ Maelezo haya ni sawa na yaliyopokelewa kutoka kwa Said bin Jubayr, Ibrahim An-Nakhai, Qatadah, Ikrimah na Muhammad bin Sirin. Ama Az-Zuhri, alisema wanatiwa korokoroni baada ya Sala ya Waislamu (yaani ya jamaa). Kwa hiyo, mashahidi hao wawili watatiwa ndani baada ya Sala ya jamaa.⁴

فَيُقْسِمَانِ بِاللَّهِ إِنَّ آرْتَبْتُمْ

“*Na waape kwa Mwenyezi Mungu mkitilia shaka,...*” Iwapo mtashuku kuwa watasaliti au kufanya hiana, basi waape kwa Jina la Allah تعالى,

¹ Ibn Abu Hatim 4:1229.

² At-Tabari 11:163, 164.

³ At-Tabari 11:172.

⁴ At-Tabari 11:174.

لَا نَشْتَرِي بِهِ

“Hatutopokea.” Katika viapo vyetu, kwa mujibu wa Muqatil bin Hayyan.

ثُمَّنَا

“Thamani.” Kwa sasa mpaka mwisho wa maisha.

وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ

“Hata kwa ajili ya jamaa;...” Maana yake, iwapo wafaidika ni jamaa zetu, bado hatutaacha ukweli.

وَلَا نَكْتُمُ شَهَادَةَ اللَّهِ

“...na wala hatutaficha ushahidi wa Mwenyezi Mungu...”

Hivyo kueleza kuwa ushahidi ni wa Allah تعالى, kama njia ya kuheshimu na kuthamini umuhimu wake.

إِنَّا إِذَا لَمِنَ الْأَثَمِينَ

“...hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye dhambi...”

Endapo tutaoharibu ushahidi au kuubadili au kuuficha kabisa. Allah تعالى Amesema tena,

فَإِنَّ عُرْيَرَ عَلَىٰ أَنَّهُمَا اسْتَحَقَّا إِثْمًا

“...ikigundulika kuwa wao wamestahiki dhambi...”

Ikiwa mashahidi wawili watapatikana wamefanya udanganyifu, au wameiba kutoka katika mali ambayo wosia umeandikwa kuihusu,

يَقُومَانِ مَقَامَهُمَا مِنَ الَّذِينَ اسْتَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْأَوْلَادِينَ

“...washike makamo ya wa mwanzo.”

Aya hii inaonesha kuwa iwapo itabainika hiana kwa mashahidi wawili, basi watu wawili katika warithi wawe mashahidi badala.

فَيَقْسِمَانِ بِاللَّهِ لَشَهَدَتُنَا أَحَقُّ مِن شَهَدَتَيْهِمَا

“...Nao waape kwa Mwenyezi Mungu wakisema: Hakika ushahidi wetu ni wa haki zaidi kuliko ushahidi wa wale.”

Maana yake, wasia wetu ambao wameufanyia udanganyifu ni wa ukweli zaidi kuliko wasia walioutoa.

وَمَا أَعْتَدْنَا

“Na sisi hatujafanya dhambi...” Tulipowashutumu kwa udanganyifu,

إِذَا لَمِنَ الظَّالِمِينَ

“...hakika hapo tutakuwa miongoni mwa waliodhulumu.” Kama tulidanganya kwayo. Hiki ni kiapo cha warithi na kauli yao hupewa kipaumbele. Kama ilivyo kwa kiapo cha ndugu wa mtu aliyeuawa, iwapo atajaribu aliyeya kuficha kadhia hiyo. Hivyo familia yake itakula kiapo kwa kutaka heshima yake.

Hili limejadiliwa katika maudhui ya viapo katika vitabu vya hukumu na sharia ya Kiislamu. Kauli ya Allah تعالى,

ذَلِكَ أَذَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِالشَّهَادَةِ عَلَىٰ وَجْهَهَا

“Hivi inaelekea zaidi ya kwamba watatoa ushahidi ulio sawa...”

Yaani, hukumu inayowataka mashahidi Dhimmi wawili wale kiapo, kama kuna wasiwasi juu ya ukweli wao, inaweza kuwalazimisha kukiri wasia katika ukweli wake. Kauli ya Allah تعالى,

أَوْ يَخَافُونَ أَنْ تُرَدُّ أَلْمَنُ بَعْدَ أَيْمَانِهِمْ

“...au wataogopa visije vikaletwa viapo vingine baada ya viapo vyao.”

Ina maana, kuwataka wale kiapo kwa Jina la Allah تعالى kunaweza kuwashajiisha kukubali wasio sahihi kwa sababu wanaheshimu kiapo kwa Jina la Allah تعالى na wanamtukuza na wanamheshimu. Aidha wanaogopa kubainika iwapo warithi wa marehemu watatakiwa kula kiapo badala yao. Katika hali hii, warithi wataapa na kustahiki mirathi ambayo mashahidi wawili walishindwa kuitangaza. Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema,

أَوْ يَخَافُونَ أَنْ تُرَدُّ أَلْمَنُ بَعْدَ أَيْمَانِهِمْ

“...au wataogopa visije vikaletwa viapo vingine baada ya viapo vyao.” halafu,

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“...na mcheni Allah...” katika masuala yenu yote,

وَأَسْمَعُوا^ط

“Msikie.” Na mumtii

وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

“Na hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi wapotofu.”

Wasiomtii au kufuata Dini Yake.

* يَوْمَ يَجْمَعُ اللَّهُ الرُّسُلَ فَيَقُولُ مَاذَا أُجِبْتُمْ قَالُوا لَا عِلْمَ لَنَا إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّمُ الْغُيُوبِ ﴿١٠٩﴾

109. Ile siku ambayo Mwenyezi Mungu Atapowakusanya Mitume awaambie: Mlijibiwa nini? Watasema: Hatuna ujuzi; hakika Wewe Ndiye Mjuzi Mkubwa wa yote yaliyofichikana.

Mitume Wataulizwa Kuhusu Mataifa Yao.

Allah تعالى Ameeleza kuwa Siku ya Kiyama, Atawauliza Mitume kuhusu mataifa yao, Aliyowapeleka kwayo, walivyoyapokea mafundisho yao. Allah تعالى Amesema,

فَلَنَسْأَلَنَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْأَلَنَّ الْمُرْسَلِينَ ﴿١١٠﴾

“Na kwa yakini Tutawauliza wale waliopelekewa Ujumbe, na pia Tutawauliza hao Wajumbe.” Na

فَوَرَبِّكَ لَنَسْأَلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١١١﴾ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٢﴾

“Basi Naapa kwa Mola wako Mlezi! Tutawahoji wote, Kwa waliyokuwa wakiyatenda.” 15:92-93)

Na kauli ya Mitume hapa.

لَا عِلْمَ لَنَا^ط

“...hatuna ujuzi.”

Ni matokeo ya hofu ya siku hiyo, kwa mujibu wa Mujahid, Al-Hasan Al-Basri na As Suddi,¹ Abdul Razzaq alisimulia kutoka kwa Athawri alisema kuwa Al-Amash alisema kuwa Mujahid aliizungumzia,

¹ At-Tabari 11:210.

يَوْمَ تَجْمَعُ اللَّهُ الرُّسُلَ فَيَقُولُ مَاذَا أُجِبْتُمْ^ط

“Ile siku ambayo Mwenyezi Mungu Atapowakusanya Mitume awaambie: Mlijibiwa nini?”²

Wataogopa na kujibu,

لَا عَلِمْنَا^ط

“Hatuna ujuzi.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى¹ na Ibn Abii Hatim رحمه الله تعالى nao walirikodi maelezo haya. Ali bin Abi Talha alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliielezea Aya hii,

* يَوْمَ تَجْمَعُ اللَّهُ الرُّسُلَ فَيَقُولُ مَاذَا أُجِبْتُمْ قَالُوا لَا عَلِمْنَا^ط إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّمْتَ الْغُيُوبَ ﴿١٠٣﴾

“Ile siku ambayo Mwenyezi Mungu Atapowakusanya Mitume Awaambie: Mlijibiwa nini?” Watasema: Hatuna ujuzi; hakika Wewe Ndiye Mjuzi Mkubwa wa yote yaliyofichikana.”

“Watasema kwa Mola, mwenye daraja la juu, “Hatuna elimu zaidi ya yale tunayoyafahamu, na hata hivyo, Unajua zaidi yetu.”² Jibu hili ni Kumtukuza Mola, Mtukufu, inamaanisha, hatuna elimu inayolingana na Elimu Yako iliyoenea. Kwa hiyo, ufahamu wetu ni mwenendo wa watu hawa uliodhahiri, na sio siri zilizomo nyoyoni mwao. Wewe Unajua kila kitu, na Una ufahamu ulioenea kila kitu, na elimu yetu ikilinganishwa na Yako ni sawa na kutokuwa na elimu yeyote, kwani,

إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّمْتَ الْغُيُوبَ

“Wewe Ndiye Mjuzi Mkubwa wa yote yaliyofichikana.”

* * *

¹ At-Tabari 11:210.

² At-Tabari 11:211.

إِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ اذْكُرْ نِعْمَتِي عَلَيْكَ
 وَعَلَىٰ وَالِدَتِكَ إِذْ اٰتٰتُكَ بِرُوْحِ الْقُدُسِ تُكَلِّمُ النَّاسَ
 فِي الْمَهْدِ وَكَهَلًا ۗ وَاِذْ عَلَّمْتُكَ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ
 وَالتَّوْرَةَ وَالْاِنْجِيْلَ ۗ وَاِذْ تَخْلُقُ مِنَ الطِّيْنِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ
 بِاِذْنِي فَتَنفُخُ فِيهَا فَتَكُوْنُ طَيْرًا بِاِذْنِي ۗ وَتُبْرِئُ الْاَكْمَةَ
 وَالْاَبْرَصَ بِاِذْنِي ۗ وَاِذْ تُخْرِجُ الْمَوْتٰى بِاِذْنِي ۗ وَاِذْ
 كَفَفْتُ بَنِي إِسْرٰءِيْلَ عَنكَ اِذْ جِئْتَهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ
 فَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْهُمْ اِنْ هٰذَا اِلَّا سِحْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿١١٠﴾
 وَاِذْ اُوْحِيْتُ اِلَى الْاَحْوَارِيْنَ اَنْ ءَامِنُوْا بِ وِبِرْسُوْلِيْ
 قَالُوْا ءَاْمَنَّا وَاَشْهَدُ بِاَنْتَا مُسْلِمُوْنَ ﴿١١١﴾

إِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ اذْكُرْ
 نِعْمَتِي عَلَيْكَ وَعَلَىٰ وَالِدَتِكَ إِذْ
 اٰتٰتُكَ بِرُوْحِ الْقُدُسِ تُكَلِّمُ النَّاسَ
 فِي الْمَهْدِ وَكَهَلًا ۗ وَاِذْ عَلَّمْتُكَ
 الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ وَالتَّوْرَةَ
 وَالْاِنْجِيْلَ ۗ وَاِذْ تَخْلُقُ مِنَ الطِّيْنِ
 كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ بِاِذْنِي فَتَنفُخُ فِيهَا
 فَتَكُوْنُ طَيْرًا بِاِذْنِي ۗ وَتُبْرِئُ
 الْاَكْمَةَ وَالْاَبْرَصَ بِاِذْنِي ۗ وَاِذْ
 تُخْرِجُ الْمَوْتٰى بِاِذْنِي ۗ وَاِذْ
 كَفَفْتُ بَنِي إِسْرٰءِيْلَ عَنكَ اِذْ
 جِئْتَهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ فَقَالَ الَّذِيْنَ
 كَفَرُوْا
 مِنْهُمْ اِنْ هٰذَا اِلَّا سِحْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿١١٠﴾

وَاِذْ اُوْحِيْتُ اِلَى الْاَحْوَارِيْنَ اَنْ ءَامِنُوْا بِ وِبِرْسُوْلِيْ قَالُوْا ءَاْمَنَّا وَاَشْهَدُ بِاَنْتَا مُسْلِمُوْنَ ﴿١١١﴾

110. Na pale Mwenyezi Mungu Ataposema: Ewe Isa bin Maryamu! Kumbuka Neema Yangu juu yako, na juu ya mama yako, Nilipokutia nguvu kwa Roho Takatifu, ukazungumza na watu katika utoto na utuuzimani. Na Nilivyokufunza kuandika na hikima na Taurati na Injili. Na ulipotengeneza udongo sura ya ndege, kwa Idhini Yangu, kisha ukapuliza ikawa ndege kwa Idhini Yangu; na ulipowaponesha vipofu na wakoma kwa Idhini Yangu; na ulipowafufua wafu kwa Idhini Yangu; na nilipokukinga na Wana wa Israili ulipowajia na hoja zilizowazi, na wakasema waliokufuru miongoni mwao: Haya si lolote ila ni uchawi mtupu!

111. Na Nilipowafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume Wangu, wakasema: Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu.

Isa عليه السلام **Anakumbushwa Neema Alizopewa na Allah تعالى.**

Allah تعالى Anaeleza jinsi Alivyomneemesha mja Wake na Mtume Wake Isa عليه السلام, mwana wa Maryamu, kwa Kumpa miujiza na vitendo visivyo vya kawaida.

Allah تعالى Amesema,

أَذْكُرُ نِعْمَتِي عَلَيْكَ

“Kumbuka Neema Yangu juu yako,...”

Nilipokuumba kutokana na mama yako, bila kuingiliwa na mwanaume, Nami Nikakufanya dalili na ushahidi wa wazi na Nguvu Zangu juu ya vitu vyote.

وَعَلَىٰ وَالِدَتِكَ

“Na juu ya mama yako,...”

Nilipokufanya wewe ni ushahidi wa kuwa yeye ni mwanamke msafi, kutokana na tuhuma chafu walizomzushia madhalimu na wajinga.

إِذْ أَيْدِيكَ بِرُوحِ الْقُدُسِ

“Nilipokutia Nguvu kwa Roho Takatifu,...”

Malaika Jibril عليه السلام na kukufanya kuwa ni Mtume, ukilingania kwa Allah تعالى ukiwa mdogo na ukubwani. Nilikufanya uzungumze ndani ya susu, na ukashuhudia kuwa mama yako hakuwa na mwenendo m-baya, na ukanadi kuwa unaniabudu. Pia ulifikisha habari za Ujumbe Wangu na ukawalingania kuniabudu.

تُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا ط

“Ukazungumza na watu katika utoto na utuuzimani.”

Nikakufanya Nabii na Mlinganiaji tangu utotoni. Maana yake, uliwalingania watu kumuabudu Allah تعالى kuanzia utotoni hadi utu-uzima. Na neno “tukallim” ina maana kulingania, kwa sababu kuzungumza na watu akiwa mtoto ni jambo geni.

وَإِذْ عَلَّمْنَاكَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ

“Na Nilivyokufunza kuandika na hikima.”

Uwezo wa kuandika na kuelewa.

وَالْتَوْرَةَ

“...na Taurati...”

Iliyoteremshwa kwa Musa عليه السلام, mwana wa Imran, aliyezungumza na Allah تعالى moja kwa moja. Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذْ تَخْلُقُ مِنَ الطِّينِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ بِإِذْنِي فَتَنفُخُ فِيهَا فَتَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِي

“Na ulipotengeneza udongo sura ya ndege, kwa Idhini Yangu, kisha ukapuliza akawa ndege kwa Idhini Yangu.”

Maana yake: Uliufinyanga katika umbile la ndege kwa ruhusa Yangu; ili awe ndege kwa ruhusa Yangu, ulipoipulizia. Kisha akawa ndege anayeruka akiwa na roho kwa Idhini ya Allah تعالى. Allah تعالى Amesema

وَتُبْرِئُ الْأَكْمَهَ وَالْأَبْرَصَ بِإِذْنِي

“Na ulipowaponesha vipofu na wakoma kwa Idhini Yangu;...”

Maelezo haya yalishatolewa katika Surat Al-Imran na hatuhitaji kuyarejea hapa. Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذْ تُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِي

“Na ulipowafufua wafu kwa Idhini Yangu;...”

Muradi wake, uliwaita na wakatoka ndani ya makaburi yao kwa Idhini ya Allah تعالى, Uwezo na Utashi Wake.

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَإِذْ كَفَفْتُ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَنْكَ إِذْ جِئْتَهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ إِنْ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ

“Na nilipokukinga na Wana wa Israili ulipowajia na hoja zilizowazi, na wakasema waliokufuru miongoni mwao: Haya si lolote ila ni uchawi mtupu!”

Maana yake: Kumbuka Fadhila Zangu, nilipowazuia Wana wa Israel kukudhuru, ulipowaletea dalili na ushahidi ulio wazi, ukiwathibitishia utume wako na Ujumbe Wangu kwao. Walikukataa na wakakushutumumu kuwa ni mchawi na wakajaribu kukuua na kutaka kukusulubu, lakini Nilikuokoa, Nikakuinua Kwangu, Tulikusafisha kutokana na ushenzi wao, na Tukakulinda na shari zao.

Lugha iliyotumika katika Aya hii inaonesha kuwa Isa عليه السلام atakumbushwa fadhila hizi Siku ya Ufufuo.

Allah تعالى Ametumia wakati uliopita katika Aya hizi kuonesha kuwa ni jambo ambalo bila shaka litatokea.

Aya hii pia ina baadhi ya siri za ghaibu ambazo Allah تعالى Alimfunulia Mjumbe Wake Muhammad ﷺ.

Allah تعالى Amesema,

وَإِذْ أَوْحَيْتُ إِلَى الْحَوَارِيِّينَ أَنْ آمِنُوا بِي وَبِرَسُولِي

“Na Nilipowafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume wangu,...”

Aidha huu ni ukumbusho wa Fadhila za Allah تعالى kwa Isa عليه السلام kwa Kumpa wafuasi na masahaba. Maana ya Wahyi katika Aya hii, ni Ilhamu na wala si ufunuo wa moja kwa moja.

وَإِذْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ أُمِّ مُوسَىٰ أَنْ أَرْضِعِيهِ

“Tulimfunulia mama yake Musa kwa kumuambia: mnyonyeshe.” (228:7)

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَإِذْ أَوْحَىٰ رَبُّكَ إِلَى النَّعْلِ أَنْ اتَّخِذِي مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا وَمِنَ الشَّجَرِ وَمِمَّا يَعْرِشُونَ ﴿٦٨﴾ ثُمَّ كَلَّمْنَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ فَأَتَسَلَّتْهُنَّ سُبُلَ رَبِّكِ ذُلُلًا

“Na Mola wako mlezi Amemfunulia nyuki jitengezee majumba yako katika milima na katika miti na katika majumba wanayojenga watu kisha kula kila matunda na upite njia za Mola Wako mlezi zilizofanywa nyepesi kuzipita.” (16:68-69)

Al-Hasan Al-Basri رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى alitoa maelezo kuhusu *Hawariyyin*, "Allah تَعَالَى Aliwafunulia...", ambapo As-Suddi alisema "Aliingiza katika nyoyo zao."

ءَامِنَّا وَأَشْهَدُ بِأَنَّنا مُسْلِمُونَ

"Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu."

* * *

إِذْ قَالَ الْحَوَارِثُوتَ يَبْعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ هَلْ يَسْتَطِيعُ
 رَبُّكَ أَنْ يُنْزِلَ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ ۗ قَالَ اتَّقُوا اللَّهَ
 إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١١٢﴾ قَالُوا نُرِيدُ أَنْ نَأْكُلَ مِنْهَا
 وَتَطْبِخَنَّ قُلُوبُنَا وَنَعْلَمَ أَنْ قَدْ صَدَقْتُنَا وَنَكُونُ عَلَيْهَا مِنَ
 الشَّاهِدِينَ ﴿١١٣﴾ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا أَنْزِلْ
 عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ تَكُونُ لَنَا عِيدًا لِأَوَّلِنَا وَآخِرِنَا
 وَءَايَةً مِنْكَ ۗ وَأَرْزُقْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّزُقِينَ ﴿١١٤﴾ قَالَ اللَّهُ إِنِّي
 مُنْزِلُهَا عَلَيْكُمْ ۗ فَمَنْ يَكْفُرْ بَعْدَ مِنْكُمْ فَإِنِّي أُعَذِّبُهُ عَذَابًا
 لَا أُعَذِّبُهُ أَحَدًا مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿١١٥﴾ وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَبْعِيسَى
 ابْنَ مَرْيَمَ ءَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمَّي إِلَهَيْنِ مِنْ دُونِ
 اللَّهِ ۗ قَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقِّ
 إِنْ كُنْتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ ۗ تَعَلَّمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ
 مَا فِي نَفْسِكَ ۗ إِنَّكَ أَنْتَ عَالِمُ الْغُيُوبِ ﴿١١٦﴾ مَا قُلْتُ هُمْ
 إِلَّا مَا أَمَرْتَنِي بِهِ ءَأِنْ عَبَدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۗ وَكُنْتُ عَلَيْهِمْ
 شَهِيدًا ۗ مَا دُمْتُ فِيهِمْ ۗ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتُ أَنْتَ الرَّقِيبَ
 عَلَيْهِمْ ۗ وَأَنْتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿١١٧﴾ إِنْ تُعَذِّبْهُمْ فَإِنَّهُمْ
 عِبَادُكَ ۗ وَإِنْ تَغْفِرْ لَهُمْ فَإِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١١٨﴾
 قَالَ اللَّهُ هَذَا يَوْمُ يَنْفَعُ الصَّادِقِينَ صِدْقُهُمْ ۗ هُمْ جَنَّتٌ
 تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ
 وَرَضُوا عَنْهُ ۗ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾ لِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ
 وَالْأَرْضِ وَمَا فِيهِنَّ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٢٠﴾

إِذْ قَالَ الْحَوَارِثُوتَ يَبْعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ هَلْ يَسْتَطِيعُ
 رَبُّكَ أَنْ يُنْزِلَ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ ۗ قَالَ اتَّقُوا
 اللَّهَ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١١٢﴾ قَالُوا نُرِيدُ أَنْ نَأْكُلَ مِنْهَا
 وَتَطْبِخَنَّ قُلُوبُنَا وَنَعْلَمَ أَنْ قَدْ صَدَقْتُنَا وَنَكُونُ عَلَيْهَا
 مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿١١٣﴾ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا أَنْزِلْ
 عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ تَكُونُ لَنَا عِيدًا لِأَوَّلِنَا
 وَآخِرِنَا وَءَايَةً مِنْكَ ۗ وَأَرْزُقْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّزُقِينَ
 ﴿١١٤﴾ قَالَ اللَّهُ إِنِّي مُنْزِلُهَا عَلَيْكُمْ ۗ فَمَنْ يَكْفُرْ بَعْدَ
 مِنْكُمْ فَإِنِّي أُعَذِّبُهُ عَذَابًا لَا أُعَذِّبُهُ أَحَدًا مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿١١٥﴾

112. "Wanafunzi walipo-
 sema: Ewe Isa bin Maryamu!
 Je, Mola wako Mlezi Ana-
 weza kututemshia chakula
 kutoka mbinguni?"

113. Wakasema: Tunataka
 kukila chakula hicho, na
 nyoyo zetu zitue, na tujue
 kwamba umetuambia

kweli, na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia.

114. Akasema Isa bin Maryamu: Ewe Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wetu! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe Sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe ni Ishara itokayo Kwako. Basi turuzuku, kwani Wewe Ndiye Mbora wa wanao- ruzuku.

115. Mwenyezi Mungu Akasema: Hakika Mimi Nitakuteremshieni hicho. Lakini yeyote katika nyinyi atakayekana baadae, basi hakika Mimi Nitampa adhabu Nisiyopata Kumpa yeyote katika walimwengu.

Kushushwa kwa Meza ya Chakula Kutoka Mbinguni

Hiki ni kisa cha “Maidah” meza ya chakula iliyoshushwa kutoka mbinguni, ambapo imepewa Surah hii, “Surat Al-Maidah.” Hizi pia ni Fadhila ambazo Allah تعالى Alimpa mja Wake na Mtume Wake, Isa عليه السلام, akikubali ombi lake la kuteremshwa Maidah, na kufanya hivyo kama ushahidi wa wazi usio na utata.

Allah تعالى Amesema,

إِذْ قَالَ آلْحَوَارِيُّونَ

“Wanafunzi waliposema...”

Wanafunzi wa ‘Isa عليه السلام walisema,

يَعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ هَلْ يَسْتَطِيعُ رَبُّكَ أَنْ يُنَزِّلَ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ

“Wanafunzi waliposema: Ewe Isa bin Maryamu! Je, Mola wako Mlezi Anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni?”

Maidah ni meza iliyo na chakula juu yake. Baadhi ya wanazuoni walisema kuwa wanafunzi waliomba meza hiyo kwa sababu walikuwa masikini na wenye kuhitaji. Hivyo wakamuomba Isa عليه السلام kuomba dua kwa Allah تعالى Kuwateremshia meza ya chakula ili wale kila siku na hivyo waweze kuabudu. Akasema,

قَالَ اتَّقُوا اللَّهَ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Akasema: mcheni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni waumini...”

Isa عليه السلام aliwajibu, “Mcheni Allah تعالى! Na msiombe hili kwani unaweza kuwa mtihani kwenu, bali muaminini Allah تعالى katika utafutaji wa riziki, kama ni waumini wa kweli.”

قَالُوا نُرِيدُ أَنْ نَأْكُلَ مِنْهَا

“Wakasema: Tunataka kukila chakula hicho,...”

Tunataka tukile,

وَتَطْمِئِنُّ قُلُوبُنَا

“...na nyoyo zetu zitue,...”

Tutakapoona kikishuka kutoka mbinguni kwa ajili yetu,

وَنَعْلَمَ أَنْ قَدْ صَدَقْتَنَا

“...na tujue kwamba umetuambia kweli,...”

Kuhusu Ujumbe na imani yetu kwako itaongezeka, kadhalika na elimu yetu.

وَتَكُونَ عَلَيْهَا مِنَ الشَّاهِدِينَ

“...na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia.”

Tukithibitisha kuwa ni alama kutoka kwa Allah تعالى, inayoshuhudia kuwa wewe ni Mtume, na kuthibitisha ukweli uliotuletea na tuwe katika wanaoshuhudia

قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا أَنْزِلْ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ تَكُونُ لَنَا عِيدًا لِأَوَّلِنَا

وَأٰخِرِنَا

“Akasema Isa bin Maryamu: Ewe Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wetu! Tuteremshia chakula kutoka mbinguni ili kiwe Sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu,...”

As-Suddi alieleza kuwa Aya ina maana, “Tutaichukulia siku ilipotemshwa iwe siku ya kusherehekea ambapo sisi na watakaokuja baada yetu wataifanya

takatifu.”¹ Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisema kuwa ina maana, “Siku ya maombi.”²

وَأَيَّةٌ مِّنكَ

“Na kiwe ni Ishara itokayo Kwako.”

Ikithibitisha kuwa Unaweza Kufanya kila kitu na kuitikia ombi langu, ili wakubali nilichowafikishia kutoka Kwako,

وَأَرْزُقْنَا

“Basi turuzuku,…”

Chakula kitamu kisichohitaji juhudi au kazi ngumu.

وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّزُقِينَ ﴿٤٤﴾ قَالَ اللَّهُ إِنِّي مَتْرَلُهَا عَلَيْكُمْ فَمَنْ يَكْفُرْ بَعْدَ مِنْكُمْ

“Kwani Wewe Ndiye Mbora wa wanaoruzuku. Mwenyezi Mungu Akasema: Hakika Mimi Nitakuteremshieni hicho. Lakini yeyote katika nyinyi atakayekana baadae,…”

Kwa kuikataa dalili hii na kukataa kuingia lawamani,

فَلِيَّ أَعْدِبُهُ عَذَابًا لَّا أَعْدِبُهُ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ

“Basi hakika Mimi Nitampa Adhabu Nisiyopata Kumpa yeyote katika walimwengu.”

Miongoni mwa watu wa zama zako. Allah تعالى Alisema katika Aya sawa na hii.

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾

“Na itapofika Saa ya Kiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!” (40:46) na,

¹ At-Tabari 11:225.

² At-Tabari 11:225.

إِنَّ الْمُنْفِقِينَ فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ وَلَنْ يَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا ﴿١٤٥﴾

“Hakika wanaafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa Motoni,...” (4:145)

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa “Abdullah bin Amr alisema, “Wale watakaopata adhabu kali kabisa Siku ya Hesabu ni watatu: Wanafiki, waliokana baada ya kuteremshiwa chakula kutoka mbinguni, na waliokanushana katika watu wa Firauni.”¹

Ibn Abi Hatim alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Walimuambia Isa عليه السلام mwana wa Maryam, ‘Tuombe kwa Allah تعالى Atuteremshie kutoka mbinguni, meza ikiwa na samaki saba na vipande saba vya mkate; na ikawekwa mbele yao. Kikundi cha mwisho kilikula kama kikundi cha kwanza.”²

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amepokea kuwa Is-haq bin Abdullah alisema kuwa meza ya chakula iliteremshwa kwa Isa عليه السلام mwana wa Maryam ikiwa na vipande saba vya mkate na samaki saba, na wakala kama walivyoweza. Lakini walipoiba sehemu ya chakula, wakisema, “Pengine kesho hakitaletwa.” Meza ikainuliwa juu.³

Kauli hizi zinathibitisha kuwa meza iliteremshwa kwa Wana wa Israel wakati wa Isa عليه السلام mwana wa Maryam, ikiwa ni jibu la Allah تعالى kwa dua aliyoomba. Kama mtiririko wa Aya hizi unavyodhihirisha wazi katika Qur’an Tukufu.

Allah تعالى Akasema:

قَالَ اللَّهُ إِنِّي مَبْرَأٌ مِنْ آلِهَا وَآلِهَا عَلَيْهِمُ الْعَذَابُ

“Mwenyezi Mungu Akasema: Hakika Mimi Nitakuteremshieni hicho.” (5:115)

¹ At-Tabari 11:233.

² At-Tabari 5:132, Ibn Abu Hatim 4:1246

³ At-Tabari 5:134.

Tukio la Kihistoria la Kushangaza.

Wanahistoria wametaja ya kuwa Musa bin Nuswair Mwaklishi wa Dola ya Banii Umayya katika ufunguzi wa miji ya Maghribi (Morocco). Alikuta katika miji hiyo meza iliyonakishiwa kwa mapambo na aina mbalimbali za vito. Akaipeleka meza hiyo kwa Mtawala wa Waislamu enzi hizo Walid bin Abdil Malik aliyejenga Msikiti wa Damascus. Na Amir Walid alikufa kabla ya meza hiyo kumfikia. Hivyo, ikafika meza hiyo katika kipindi cha Ukhalifa wa ndugu yake Salman bin Abdil Malik watu walipoiona walishangazwa sana, kwa kuwa ilinakishiwa kwa vito na mapambo ya thamani. Na husemwa; 'Meza hii ilikuwa ni ya Suleiman bin Daudi عليه السلام.' Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ ءَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيٰ إِلَهَيْنِ مِن دُونِ
 اللَّهِ ۗ قَالَ سُبْحٰنَكَ مَا يَكُونُ لِيٰ أَن أَقُولَ مَا لَيْسَ لِيٰ بِحَقِّ ۗ إِن كُنتُ قُلْتُهُ فَقَدْ
 عَلِمْتَهُ ۗ تَعَلَّمْ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ ۗ إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّمُ الْغُيُوبِ ﴿١١٦﴾
 مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَا أَمَرْتَنِي بِمَآ أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۗ وَكُنتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا
 مَّا دُمْتُ فِيهِمْ ۗ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنتَ أَنْتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ ۗ وَأَنْتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ
 ﴿١١٧﴾ إِن تَعَدَّيْتَهُمْ فَلْيَأْمُرْ عِبَادَكَ ۗ وَإِن تَغْفِرْ لَهُمْ فإِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١١٨﴾

116. Na pale Allah Atakaposema: Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Allah? (Na Isa) atasema: Wewe Umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa nilisema basi bila ya shaka Umekwisha yajua. Wewe Unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yaliyo katika Nafsi Yako. Hakika Wewe Ndiye Mjuzi Mkubwa wa yaliyofichikana.

117. Sikuwaambia lolote ila Uliyoni amrisha, nayo ni: Muabuduni Allah, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao. Na Uliponichukua mimi (kwa kunirufaisha) Ukawa Wewe Ndiye Muangalizi juu yao. Na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu.

118. Ukiwaadhibu basi hao ni waja wako. Na Ukiwasamehe basi Wewe Ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.

Isa عليه السلام **Akataa Ushirikina na Athibitisha Ibada ya Mungu Mmoja (Tawhiid).**

Allah تعالى Atamuambia mja Wake na Mtume Wake, Isa bin Maryam عليه السلام, Atamuambia Siku ya Kiama mbele ya waliomuabudu Isa na mama yake kama miungu asiyekuwa Allah تعالى.

يٰٓيٰعِيسَىٰ ابْنَ مَرْيَمَ ءَاَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُوْنِي وَاٰمِيْٓ اِلٰهَيْنِ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ

“...Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu?”

Hili ni karipio na onyo kwa Wakristo akiwatahadharisha hadharani, kama alivyosema Qatadah na wenzake, na Qatadah aliitaja Ayah hii kama ushahidi,

هٰذَا يَوْمَ يَنْفَعُ الصّٰدِقِيْنَ صِدْقُهُمْ

“Hii ni siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao.” (5:119)

Kauli ya Allah,

سُبْحٰنَكَ مَا يَكُوْنُ لِيْ اَنْ اَقُوْلَ مَا لَيْسَ لِيْ بِحَقِّكَ

“Subhannak Wewe Umetakasika hainifaiki mimi kusema ambayo si haki.”

Haya ni maelekezo kwa Isa عليه السلام kutoka kwa Allah تعالى ili atamke majibu sahihi na yenye adabu ndani yake. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Abuu Harayrah رضي الله عنه alisema, “Isa عليه السلام atafundishwa hoja ikiwa ni majibu kwa Atakayoulizwa na Allah تعالى.”

وَإِذْ قَالَ اللّٰهُ يٰعِيسَىٰ ابْنَ مَرْيَمَ ءَاَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُوْنِي وَاٰمِيْٓ اِلٰهَيْنِ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ

“Na pale Mwenyezi Mungu Atakaposema: Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu?”

Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia: Mtume ﷺ alisema kuwa Allah تعالى Alimfundisha Isa عليه السلام kusema.

سُبْحٰنَكَ مَا يَكُوْنُ لِيْ اَنْ اَقُوْلَ مَا لَيْسَ لِيْ بِحَقِّكَ

“(Na Isa) atasema: Subhanaka, Wewe Umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu.”

¹ Ibn Abu Hatim 4:1253.

Ath-Thawri رحمه الله تعالى alipokea Hadithi hii kutoka kwa Ma'amar kutoka kwa Tawus.

Kauli ya Isa عليه السلام،

إِنْ كُنْتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ^ع

“Ikiwa nilisema basi bila ya shaka umekwishajua.”

Maana yake: Kama ningelisema, Wewe, Mola Wangu Ungelijua, kwani hapana kikwepacho ufahamu Wako. Bali sijasema maneno haya wala sijafikiri akilini mwangu, ndio maana akasema,

تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّمُ الْغُيُوبِ ﴿٥١﴾ مَا قُلْتُ هُمْ إِلَّا
مَا أَمَرْتَنِي بِهِ

“...Wewe Unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yaliyo katika Nafsi Yako. Hakika Wewe Ndiye Mjuzi Mkubwa wa yaliyofichikana. Sikuwaambia lolote ila Uliyoniambisha...”

Na kufikisha,

أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ^ع

“...nayo ni muabuduni Mwenyezi Mungu Mola wangu na Mola wenu.”

Niliwalingania yale Uliyoniipeleka nayo na Ukaniamuru niwafikishie,

أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ^ع

“...nayo ni muabuduni Mwenyezi Mungu Mola wangu na Mola wenu.”

Ndiyo niliyowafikishia,

وَكُنْتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَا دُمْتُ فِيهِمْ^ع

“Na nilikuwa juu yao shahidi nilipokuwa nao...”

Nilikuwa shahidi juu yao juu ya walichokifanya wakati nilipokuwa miongoni mwao.

فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتَ أَنْتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ وَأَنْتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

“Na Uliponichukua mimi (kwa kunirufaisha na kunipeleka mbinguni kamilifu hali nikiwa hai), Ukawa Wewe Ndie Muangalizi juu yao na Wewe ni shahidi juu yao ya kila kitu.”

Abu Dawud At-Tayalisi alirekodi kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Mtume ﷺ alisimama wima mara moja na alitoa hotuba na kusema,

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ! إِنَّكُمْ مَخْشُورُونَ إِلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ حُفَاةً، عُرَاةً، غُرْلًا»

"Enyi watu! Mtakusanywa kwa Allah mkiwa miguu mitupu, uchi na hamjatahiriwa,

كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ نُعِيدُهُ

"...Kama Tulivyoanza umbo la mwanzo Tualirudisha tena..."(21:104)

«وَإِنَّ أَوَّلَ الْخَلَائِقِ يُكْسَى يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِبْرَاهِيمَ، أَلَا وَإِنَّهُ يُجَاءُ بِرِجَالٍ مِنْ أُمَّتِي فَيُؤْخَذُ بِهِمْ ذَاتَ السَّمَالِ، فَأَقُولُ: أَصْحَابِي، فَيَقَالُ: إِنَّكَ لَا تَدْرِي مَا أَخَذْتُوا بَعْدَكَ، فَأَقُولُ كَمَا قَالَ الْعَبْدُ الصَّالِحُ»

"Kwa hakika viumbe wa kwanza kufunikwa nguo siku ya kiyama ni Ibrahim. Baadhi ya watu katika Ummah wangu wataletwa na kupelekwa kushoto (kwenye Moto) na nitapiga kelele, "Hawa ni wafuasi wangu! Kutasemwa, "Hujui waliyozua baada yako (katika Dini)." Hivyo nitasema kama mja mwema (Isa) alivyosema."

وَكُنْتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَا دُمْتُ فِيهِمْ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتُ أَنْتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ وَأَنْتَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ۖ إِنَّ تَعَذِّبَهُمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ وَإِن تَغْفِرَ لَهُمْ فإِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١١٦﴾

"Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao. Na Uliponichukua mimi (kwa kunirufaisha na kunipeleka mbinguni kamilifu hali nikiwa hai), Ukawa Wewe Ndiye Muangalizi juu yao. Na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu. Ukiwaadhibu basi hao ni waja Wako. Na Ukiwasamehe basi Wewe Ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima."

«فَيَقَالُ: إِنَّ هَؤُلَاءِ لَمْ يَزَالُوا مُرْتَدِّينَ عَلَيَّ أَعْقَابِهِمْ مُنْذُ فَارَقْتَهُمْ»

Aidha itasemwa, "watu hawa walikuwa wakirejea nyuma kwa miguu yao baada ya kuwaacha."¹

Al-Bakhari² pia aliandika Hadithi hii katika maelezo ya Aya hii. Allah تعالى Amesema

¹ Musnad At-Tayalisi na. 343.

² Fat'hul Al-Bari 8:135.

إِنْ تُعَذِّبِهِمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ ۖ وَإِنْ تَغْفِرَ لَهُمْ فإِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١١٦﴾

“Ukiwaadhibu basi hao ni waja Wako. Na Ukiwasamehe basi Wewe Ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.”

Masuala yote yanarejea kwa Allah تعالى, kwani Anafanya Anavyoridhia na hapana wa kusaili Ayafanyayo, ambapo Yeye Atawauliza. Pia Aya hii inaonesha uovu wa Wakristo waliomzulia uongo Allah تعالى na Mjumbe Wake, hivyo wakamnasibisha Allah تعالى kuwa na mshirika, mke na mwana. Allah تعالى Ametukuka katika hilo, Yuko baidi na hayo wanayomshirikisha nayo. Hivyo Ayah hii (5:118) ina thamani kubwa na inatoa habari za pekee. Na imekuja katika Hadithi kwamba Mtume siku moja alisimama usiku mzima hadi asubuhi huku akiikariri Aya hii.

قَالَ اللَّهُ هَذَا يَوْمُ يَنْفَعُ الصَّالِحِينَ صِدْقُهُمْ ۗ لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۖ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ۗ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١٦﴾ لِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا فِيهِنَّ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١١٧﴾

119. Mwenyezi Mungu Atasema: Hii ndiyo Siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata Bustani zipitazo mito kati yake. Humo watadumu milele. Mwenyezi Mungu Amewawia radhi, nao wawe radhi Naye. Huku ndiko kufuzu kukubwa.

120. Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo. Naye ni Muweza wa kila kitu.

Ni Ukweli Pekee Utakuwa na Faida Siku ya Kiyama.

Allah تعالى Anamjibu mja Wake na Mjumbe Wake Isa عليه السلام, mwana wa Maryam, baada ya kuwakana Wakristo walioongopa kuhusu Allah تعالى na Mjumbe Wake, Allah تعالى Akamtaka akae mbali na wakristo wapingaji wanao muongopea Allah تعالى na Mtume Wake. Isa عليه السلام aliwaelekeza kuhusu mwisho wao na Utashi wa Mola wao. Na aliwataka wafuate mafundisho ya Mola wao Mlezi. Hivyo Allah تعالى Anasema,

هَذَا يَوْمُ يَنْفَعُ الصَّالِحِينَ صِدْقُهُمْ ۗ

“...hii ndio siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao.”

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo, "Hii ndiyo siku ambayo itawanufaisha watu wanaompwekesha Allah تعالى wa Pekee katika ibada."

هُمَّ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا

"Wao watapata Bustani zipitazo mito kati yake. Humo watadumu milele."

Hawatatolewa humo,

رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ

"Mwenyezi Mungu Amewawia radhi..."

Kama Allah تعالى Alivyosema

وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ أَكْبَرُ

"Na Radhi za Mwenyezi Mungu ndio kubwa kuliko yote." (9:72)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

"Huku ndiko kufuzu kukubwa."

Maana yake: Ni mafanikio makubwa yasiyo na mfano. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine.

لِمَثَلٍ هَذَا فَلَيعْمَلِ الْعَمَلُونَ ﴿٦١﴾

"Kwa mfano wa haya na watende watendao." (37:61) na,

وَفِي ذَلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ الْمُتَنَافِسُونَ

"Na katika hayo washindanie wenye kushindana." (83:26)

Na Kauli Yake,

لِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا فِيهِنَّ ۚ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٠﴾

"Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo. Naye ni Muweza wa kila kitu."

Maana yake: Aliumba kila kitu, Anamiliki kila kitu, Anatawala yote na Ana uwezo wa kila kitu. Hivyo, kila kitu na kila mtu yuko katika Milki Yake na chini ya Uweza na Utashi Wake. Hapana mfano Wake, wala mshindani Wake, wala anayelingana Naye, Hana baba wala mtoto, wala Swahiba, Hana mola au mungu mwingine. Ibn Wahab alisema kuwa alimsikia Huyay bin Abdullah akisema kuwa Abu Abdur-Rahman kutoka kwa Abuu Abdurrahmani Al-Hubuliyi Abdullah bin Amr alisema, "Surah ya mwisho kuteremshwa ni *Surat Al-Maidah*."¹



¹ At-Tirmidhi na. 3063.

Tafsiri ya Suratul - An'am

Sura ya 6

Iliteremshwa Makkah

Fadhila za *Suratu Al-An'am* na Kipindi cha Kuteremshwa Kwake.

Al-'Awfi, 'Ikrimah, na 'Ata wamesema Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: "*Suratu Al-An'am* iliteremshwa Makkah"¹.

At-Tabarani alinukuu kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: "Surah nzima ya *Al-An'am* iliteremshwa Makkah wakati wa usiku, yote kwa pamoja, huku ikiwa imefuatana na malaika elfu sabini wakiwa wananyanyua sauti zao kwa *Tasbihi* (kumtumkuza Allah تعالى)"².

As-Suddi amesema kutoka kwa Murrah amesema: 'Abdullah alisema, "*Surat Al-An'am* iliteremshwa huku ikisindikizwa na malaika elfu sabini"³.



¹ Ad-Dur Al-Manthur 3:243.

² At-Tabarani 12:215.

³ Ad-Dur Al-Manthur 3:243.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْأَنْعَامِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ ۗ ثُمَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ ﴿١﴾ هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ طِينٍ ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا ۗ وَأَجَلٌ مُّسَمًّى عِنْدَهُ ۗ ثُمَّ أَنْتُمْ تَمْتَرُونَ ﴿٢﴾ وَهُوَ اللَّهُ فِي السَّمَوَاتِ وَفِي الْأَرْضِ ۗ يَعْلَمُ سِرَّكُمْ وَجَهْرَكُمْ وَيَعْلَمُ مَا تَكْسِبُونَ ﴿٣﴾ وَمَا تَأْتِيهِمْ مِنْ آيَةٍ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِمْ إِلَّا كَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ ﴿٤﴾ فَقَدْ كَذَّبُوا بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ ۗ فَسَوْفَ يَأْتِيهِمْ أَنْبَتُ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٥﴾ أَلَمْ يَرَوْا كَمَا أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ قَرْنٍ مَكَّنَّهِمْ فِي الْأَرْضِ ۗ مَا لَمْ نُمَكِّنْ لَهُمْ لَكُمْ وَأَرْسَلْنَا السَّمَاءَ عَلَيْهِمْ مِدْرَارًا وَجَعَلْنَا الْأَنْهَارَ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمْ فَأَهْلَكْنَاهُمْ بِذُنُوبِهِمْ وَأَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قَوْمًا آخَرِينَ ﴿٦﴾

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ ۗ ثُمَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ ﴿١﴾ هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ طِينٍ ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا ۗ وَأَجَلٌ مُّسَمًّى عِنْدَهُ ۗ ثُمَّ أَنْتُمْ تَمْتَرُونَ ﴿٢﴾ وَهُوَ اللَّهُ فِي السَّمَوَاتِ وَفِي الْأَرْضِ ۗ يَعْلَمُ سِرَّكُمْ وَجَهْرَكُمْ وَيَعْلَمُ مَا تَكْسِبُونَ ﴿٣﴾

1. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliye-umba mbingu na ardhi na Akafanya giza na mwan-gaza. Tena baada ya haya waliokufuru wanawafanya wengine sawa na Mola wao Mlezi.

2. Yeye Ndiye Aliyeku-umbeni kwa Udongo, kisha

Akakuhukumieni ajali, na muda maalumu uko Kwake tu. Tena baada ya haya nyinyi mnatia shaka.

3. Na Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhini. Anayajua ya ndani yenu na ya nje yenu. Na Anayajua mnayoyachuma”.

Sifa Njema ni za Allah Juu ya Kudura Zake na Ukubwa wa Mamlaka Yake.

Allah تعالى Anasifia Nafsi Yake Tukufu na Anajifaharisha kwa Kuumba mbingu na ardhi kuwa makazi ya waja Wake, na kwa Kujaalia kiza na mwangaza ili Kuwanufaisha waja hao usiku na mchana.

Katika Aya hii, Allah تعالى Anazungumzia kiza kwa wingi, *Dhulumat* (umoja wake ni *Dhulumah*), na Akazungumzia mwangaza kwa umoja, *An-Nur*, kwa sababu *An-Nur* ni Adhimu zaidi. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Ametumia neno la umoja Kueleza upande wa kulia, na neno la wingi katika Kueleza upande wa kushoto. Alisema;

عَنِ الَّتِيْمِيْنَ وَالشَّمَايِلِ

"...kulia na kushotoni". (16:48)

Ni kama Alivyosema mwishoni mwa Surah hii;

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ فَاتَّبِعُوهُ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ

"Basi kwa hakika hii ndiyo njia Yangu iliyonyooka, basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na njia Yake". (6:153)

Kisha Allah Akasema;

ثُمَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ

"Tena baada ya haya waliokufuru wanawafanya wengine sawa na Mola wao Mlezi".

Maana yake: Pamoja na yote haya, baadhi ya waja Wake wamemkufuru Yeye, na wakamfanyia washirika na washindani, na wakadai wanayomsingizia kwayo.

Kauli ya Allah تعالى;

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِّن طِينٍ

"Yeye Ndiye Aliyekuumbeni kwa Udongo".

Inamaanisha baba yao Adam عليه السلام, ambaye ndiye asili yao, na kutokana naye wameongezeka na kuenea pande za Mashariki na Magharibi.

Na Kauli Yake;

ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا وَأَجَلٌ مُّسِيٌّ عِنْدَهُ

“...kisha Akakuhukumieni ajali, na muda maalumu uko Kwake tu”.

Said bin Jubayr amesema Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa Kauli ya Allah تعالیٰ:

ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا

“...kisha Akakuhukumieni ajali”.

Maana yake ni mauti, na;

وَأَجَلٌ مُّسِيٌّ عِنْدَهُ

“...na muda maalumu uko Kwake tu”.

Maana yake ni Akhera.¹ Maelezo kama haya yalitolewa na Mujahid, ‘Ikrimah, Sa’id bin Jubayr, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahhak, Zayd bin Aslam, ‘Atiyyah, As-Suddi, Muqatil bin Hayyan na wengine². Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na Mujahid wamesema;

ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا

“...kisha Akakuhukumieni ajali”.

Maana yake: Ni muda wa dunia.

ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا وَأَجَلٌ مُّسِيٌّ عِنْدَهُ

“...kisha Akakuhukumieni ajali, na muda maalumu uko Kwake tu”.

Maana yake ni umri wa mwanadamu mpaka wakati wa kufa kwake. Ni kana kwamba maana hii imechukuliwa kutokana na Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّنَكُمْ بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ بِالنَّهَارِ

“Naye Ndiye Anayekufisheni usiku na Anakijua mlichofanya mchana”. (6:60)

¹ At-Tabari 11:257.

² At-Tabari 11:256-258.

³ At-Tabari 11:256.

عِنْدَهُ^ط

"...uko Kwake tu". Ni, hapana ajuaye itatukia lini, isipokuwa Yeye tu. Ni sawa na Kauli Yake, katika Aya nyingine;

إِنَّمَا عَلَّمَهَا عِنْدَ رَبِّي لَا يُجَلِّبُهَا لَوْ قَتَبَا إِلَّا هُوَ^ط

"Kuijua Kwake kuko kwa Mola Mlezi wangu. Haidhihirishi hiyo kwa wakati wake ila Yeye".

Pia ni sawa na Kauli Yake تعالى:

يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسِلُهَا ۚ قُلْ إِنَّمَا أَعْلَمُهَا إِلَهُي ۚ وَمَا يُغْنِي عَنْكَ الْعِلْمُ إِن كُنْتَ تَتَذَكَّرُ إِلَّا نَذِيرًا ۚ إِلَىٰ رَبِّكَ مُتَبِعُهَا ۚ

"Wanakuuliza Saa (ya Kiyama) itakuwa lini? Una nini wewe hata uitaje? Kwa Mola wako Mlezi ndio mwisho wake".

Na Kauli ya Allah تعالى:

ثُمَّ أَنتُمْ تَمْتَرُونَ

"Tena baada ya haya nyinyi mnatia shaka".

Maana yake: Mnalitilia mashaka jambo la Kiyama. Ni kwa mujibu wa As-Suddi¹.

Na Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ اللَّهُ فِي السَّمَوَاتِ وَفِي الْأَرْضِ ۚ يَعْلَمُ سِرُّكُمْ وَجَهْرُكُمْ وَيَعْلَمُ مَا تَكْسِبُونَ ۚ

"Na Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhini. Anayajua ya ndani yenu na ya nje yenu. Na Anayajua mnayoyachuma."

Maana yake: Yeye Ndiye Aitwaye Allah تعالى mbinguni na ardhini. Yaani, Yeye Ndiye Aabudiwaye, Apwekeshwaye; na Ungu Wake wanaukiri wale walio mbinguni na ardhini. Wanamuita Allah تعالى, na wanamuomba Yeye katika hali za hofu na matumaini, isipokuwa waliokufuru, miongoni mwa wanadamu na majini. Ni sawa na Kauli Yake katika Aya nyingine;

وَهُوَ الَّذِي فِي السَّمَاءِ إِلَهُهُ وَفِي الْأَرْضِ إِلَهُهُ

"Na Yeye Ndiye Mungu Mbinguni na Ndiye Mungu Katika Ardhi".

(43:84)

¹ At-Tabari 11:260.

Maana yake: Yeye ni Mungu wa yeyote aliye mbinguni na aliye ardhini. Na Yeye Anazijua siri zenu na mnayoyadhihirisha. Na Kauli ya Allah تعالى:

وَيَعْلَمُ مَا تَكْسِبُونَ

“Na Anayajua mnayoyachuma”.Maana yake: Matendo yenu yote mnayoyafanya, ya kheri na ya shari.

وَمَا تَأْتِيهِمْ مِنْ آيَةٍ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِمْ إِلَّا كَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ ﴿٦﴾ فَقَدْ كَذَّبُوا بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ ۖ فَسَوْفَ يَأْتِيهِمْ أَنْبُؤُهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٧﴾ أَلَمْ يَرَوْا كَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ قَرْنٍ مَكَّنَّهِمْ فِي الْأَرْضِ مَا لَمْ يُمْكِنْ لَكُمْ وَأَرْسَلْنَا السَّمَاءَ عَلَيْهِمْ مِدْرَارًا وَجَعَلْنَا الْأَنْهَارَ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمْ فَأَهْلَكْنَاهُمْ بِدُنُوبِهِمْ وَأَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قَرْنًا آخَرِينَ ﴿٨﴾

4. Na haiwafikii hata ishara moja katika ishara za Mola wao Mlezi ila wao huwa wenye kuipa nyongo.

5. Wameikanusha Haki ilipowajia. Basi zitawajia khabari za yale waliyokuwa wakiyakejeli.

6. Je, hawaoni vizazi vingapi Tulivyoviangamizo kabla yao? Tuliwaweka katika nchi Tusivyokuwekeni nyinyi; Tukawapelekea mvua nyingi na Tukaifanya mito inapita chini yao. Mwishowe Tukawaangamiza kwa madhambi yao; na Tukaanzisha baada yao kizazi kingine.

Ukaidi wa Washirikina na Onyo Kwao.

Allah تعالى Anawazungumzia washirikina wakadhibishaji, wakaidi, wao huipa mgongo kila Aya, yaani dalili, muujiza na hoja juu ya Upweke wa Allah تعالى na ukweli wa Mitume Wake watukufu. Hawatafakari wala hawajali. Allah تعالى Amesema;

فَقَدْ كَذَّبُوا بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ ۖ فَسَوْفَ يَأْتِيهِمْ أَنْبُؤُهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٦﴾

“Wameikanusha Haki ilipowajia. Basi zitawajia khabari za yale waliyokuwa wakiyakejeli”.

Hili ni tishio kwao na onyo kali kwa kuikadhibisha haki. Kwa hakika, wataupata ukweli ambao walikuwa wakiukadhibisha na watapata ladha ya mwisho

mbaya. Kisha Allah تعالی Akawapa Waadhi na Kuwahadharisha, wajiepushe na adhabu na huzuni za kidunia kama zilizowakumba waliokuwa kama wao, katika vizazi vilivyopita, ambao walikuwa na nguvu zaidi yao, walikuwa wengi, walimiliki mali nyingi na walizaa watoto wengi, walijinufaisha sana na ardhi na walikuwa na majumba. Kisha Akasema;

أَلَمْ يَرَوْا كَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ قَرْنٍ مَكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ مَا لَمْ نُمَكِّنْ لَهُمْ

***“Je, hawaoni vizazi vingapi Tulivyoviangamizo kabla yao?
Tuliwaweka katika nchi Tusivyokuwekeni nyinyi”.***

Maana yake: Mali, watoto, majengo, vyakula vingi, utajiri na maaskari. Na kwa ajili hii, Amesema;

وَأَرْسَلْنَا السَّمَاءَ عَلَيْهِمْ مِدْرَارًا

“...Tukawapelekea mvua nyingi”.

Kipindi baada ya kipindi.

وَجَعَلْنَا الْأَنْهَارَ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمْ

“...na Tukaifanya mito inapita chini yao”.

Maana yake: Tuliwapelekea mvua kwa wingi na chemchem zikawa nyingi, yaani kwa ajili ya kuwavuta kidogo kidogo na kuwapa muda mfupi.

فَأَهْلَكْنَاهُمْ يَوْمَهُمْ

“Mwishowe Tukawaangamiza kwa madhambi yao”.

Maana yake: Kutokana na makosa na maovu yao waliyoyatenda.

وَأَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قَرْنًا آخَرِينَ

“...na Tukaanzisha baada yao kizazi kingine”.

Maana yake: Vizazi hivi vilivyotangulia viliondoka na vikawa kama vielelezo na simulizi.

وَأَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قَرْنًا آخَرِينَ

“...na Tukaanzisha baada yao kizazi kingine”.

Maana yake: Kizazi kingine, ili nacho Tukijaribu. Nao walifanya kama vitendo vyao, nao wakaangamia kama wale waliotangulia. Kwa hivyo, “Enyi

mnaoambiwa haya jihadharisheni yasiye yakawapata kama yaliyo wasibu hao, kwani nyinyi hamkuwa wapenzi zaidi kwa Allah تعالیٰ kuliko Mitume wao. Hivyo basi, nyinyi mnastahiki zaidi kupewa adhabu na kuharakishiwa mateso kuliko wao, kama isingelikuwepo huruma Yake na hisani".



وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَابًا فِي قِرْطَاسٍ
 فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ لَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا
 إِن هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٧﴾ وَقَالُوا لَوْلَا
 أَنْزَلَ عَلَيْهِ مَلَكٌ ۖ وَلَوْ أَنْزَلْنَا مَلَكًا
 لَقُضِيَ الْأَمْرُ ثُمَّ لَا يُنظَرُونَ ﴿٨﴾
 وَلَوْ جَعَلْنَاهُ مَلَكًا لَجَعَلْنَاهُ رَجُلًا
 وَلَلَبَسْنَا عَلَيْهِمْ مَا يَلْبَسُونَ ﴿٩﴾
 وَلَقَدْ آسْتَفِزُوا بِنُوحٍ إِذْ أَوْسَىٰ أُولَئِكَ
 بِالذِّكْرِ لَئِن كَانُوا بِآيَاتِنَا لَشَاقِقِينَ ﴿١٠﴾
 وَإِن جَعَلْنَاهُ نَارًا لَّخَالِدًا نُّورًا
 وَإِن جَعَلْنَاهُ سَمَكًا لَّيَلْبَسُنَّ أَفْئِدَتَهُمْ
 وَإِن جَعَلْنَاهُ جَنًّا لَيَلْبَسُنَّ أَفْئِدَتَهُمْ
 وَإِن جَعَلْنَاهُ نَجًّا لَيَضْحَكُنَّ مِنْكَ
 وَالنَّجَّاتُ الْيَتِيمَ إِذْ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ لَمَّا
 كُنْتُمْ نَاجِيَةً سَائِرِينَ فِي الْبَحْرِ وَكَانَ
 عَصَىٰ اللَّهِ لِلْكَافِرِينَ عَاقِبَةً مُّكْذِبِينَ ﴿١١﴾
 قُل لِّمَن مَّا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ
 قُل لِّلّٰهِ كَتَبَ عَلٰى نَفْسِهٖ الرَّحْمَۃَ لِيَجْمَعَنَّكُمْ
 اِلٰى يَوْمٍ ۗ لَّا رَيْبَ فِيْهِ ۗ الَّذِيْنَ حَسِبُوْا
 اَنْفُسَهُمْ فَهْمًا ۗ لَّا يُؤْمِنُوْنَ ﴿١٢﴾ * وَلَهُ مَا
 سَكَنَ فِي الْاٰلِ وَالنَّهَارِ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ
 الْعَلِيْمُ ﴿١٣﴾ قُلْ اَعْتَدَ اللّٰهُ لِيَّوْلٰىا فَاَطِرِ
 السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَهُوَ يُطْعِمُهُمْ وَلَا يُطْعَمُ
 مِنْ اِيْنِيْ ۗ اَمْرًا ۗ اَنْ اَكُوْنَ اَوَّلَ مَنْ اَسْلَمَ ۗ وَلَا
 تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿١٤﴾ قُلْ اِنِّيْ اَخَافُ
 اِنْ عَصَيْتُ رَبِّيْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ﴿١٥﴾
 مَنْ يُصْرَفْ عَنْهُ يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمْنَاهُ
 وَذٰلِكَ الْفَوْزُ الْاَمِيْنُ ﴿١٦﴾

وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَابًا فِي قِرْطَاسٍ
 فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ لَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا
 إِن هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٧﴾ وَقَالُوا لَوْلَا
 أَنْزَلَ عَلَيْهِ مَلَكٌ ۖ وَلَوْ أَنْزَلْنَا مَلَكًا
 لَقُضِيَ الْأَمْرُ ثُمَّ لَا يُنظَرُونَ ﴿٨﴾
 وَلَوْ جَعَلْنَاهُ مَلَكًا لَجَعَلْنَاهُ رَجُلًا
 وَلَلَبَسْنَا عَلَيْهِمْ مَا يَلْبَسُونَ ﴿٩﴾
 وَلَقَدْ آسْتَفِزُوا بِنُوحٍ إِذْ أَوْسَىٰ أُولَئِكَ
 بِالذِّكْرِ لَئِن كَانُوا بِآيَاتِنَا لَشَاقِقِينَ ﴿١٠﴾
 وَإِن جَعَلْنَاهُ نَارًا لَّخَالِدًا نُّورًا
 وَإِن جَعَلْنَاهُ سَمَكًا لَيَلْبَسُنَّ أَفْئِدَتَهُمْ
 وَإِن جَعَلْنَاهُ جَنًّا لَيَلْبَسُنَّ أَفْئِدَتَهُمْ
 وَإِن جَعَلْنَاهُ نَجًّا لَيَضْحَكُنَّ مِنْكَ
 وَالنَّجَّاتُ الْيَتِيمَ إِذْ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ لَمَّا
 كُنْتُمْ نَاجِيَةً سَائِرِينَ فِي الْبَحْرِ وَكَانَ
 عَصَىٰ اللَّهِ لِلْكَافِرِينَ عَاقِبَةً مُّكْذِبِينَ ﴿١١﴾

7. Na lau Tungelikute-remshia kitabu cha karatasi, wakakigusa kwa mikono yao, wangelisema waliokufuru: Haya si chochote ila ni uchawi dhahiri.

8. Na wao husema: Mbona hakuteremshiwa Malaika?

Na kama Tungeliteremsha Malaika, basi bila ya shaka ingeshahukumikiwa Amri, tena hapo wasingelipewa muhula.

9. Na kama Tungelimfanya Malaika bila ya shaka Tungelimfanya kama binadamu, na Tungeliwatilia matatizo yale wanayoyatatiza wao.

10. Na hakika Mitume walio kabla yao walifanyiwa kejeli, lakini walio wafanyia kejeli wakaja kuzungukwa na yale yale waliyokuwa wao wanayafanyia kejeli.

11. Sema: Tembeeni ulimwenguni, kisha mtazame ulikuwaje mwisho wa wanaokanusha.

Karipio kwa Wakaidi na Kukataa Kwao Mwanadamu Kuwa Mtume.

Allah تعالى Anaeleza ukaidi wa washirikina na kuikana kwao haki na kuifanyia upinzani.

وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَابًا فِي قِرْطَاسٍ فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ

“Na lau Tungelikuteremshia kitabu cha karatasi, wakakigusa kwa mikono yo”.

Maana yake ni, kama wangeuona ujumbe huu ukishuka na wakaushuhudia kwa macho yao.

لَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ

“...wangelisema waliokufuru: Haya si chochote ila ni uchawi dhahiri”.

Hii inalingana na Alivyosema Allah تعالى kuhusu ufidhuli wao dhidi ya jambo la kweli na uhakika;

وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا مِّنَ السَّمَاءِ فَظَلُّوا فِيهِ يَعْرُجُونَ ﴿١٤﴾ لَقَالُوا إِنَّمَا سُكَّرَتْ أَبْصَارُنَا
بَلْ نَحْنُ قَوْمٌ مَّسْحُورُونَ ﴿١٥﴾

“Na lau Tungeliwafungulia mlango wa mbingu, wakawa wanapanda. Basi wangelisema: Macho yetu yamelevywa, bali sisi wenyewe tumerogwa”. (15:14-15) na,

وَإِن يَرَوْا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ سَاقِطًا يَقُولُوا سَحَابٌ مَّرْكُومٌ ﴿٤٤﴾

“Na hata wangeona pande linatoka mbinguni linaanguka wangesema: Ni mawingu yaliyobebana”. (52:44)

وَقَالُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ مَلَكٌ

“Na wao husema: Mbona hakuteremshiwa Malaika?” Maana yake: Ili awepo Mwonyaji mwingine pamoja naye. Allah تعالى Amesema;

وَلَوْ أَنْزَلْنَا مَلَكًا لَقُضِيَ الْأَمْرُ ثُمَّ لَا يُنظَرُونَ

“Na kama Tungeliteremsha Malaika, basi bila ya shaka ingeshahukumiwa Amri, tena hapo wasingelipewa muhula”.

Maana yake: Kama Malaika wangeteremshwa juu ya yale waliyo nayo, basi adhabu kutoka kwa Allah تعالى ingewajia. Ni kama Alivyosema katika Aya nyingine;

مَا نُنزِلُ الْمَلٰٓئِكَةَ اِلَّا بِالْحَقِّ وَمَا كَانُوْا اِذَا مُنظَرِيْنَ ﴿٨﴾

“Sisi Hatuwateremshi Malaika ila kwa sababu ya haki, na hapo hawatapewa muhula”. (15:8)

Pia na Kauli Yake;

يَوْمَ يَرَوْنَ الْمَلٰٓئِكَةَ لَا بُشْرٰى يَوْمَئِذٍ لِلْمُجْرِمِيْنَ

“Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wakosefu”. (25:22)

Kauli ya Allah تعالى;

وَلَوْ جَعَلْنٰهُ مَلَكًا لَّجَعَلْنٰهُ رَجُلًا وَلَلَبَسْنَا عَلَيْهِمْ مَا يَلْبَسُوْنَ ﴿٩﴾

“Na kama Tungelimfanya Malaika bila ya shaka Tungelimfanya kama binadamu, na Tungeliwatilia matatizo yale wanayoyatatiza wao”.

Maana yake ni kuwa, kama Tungelinteremsha Malaika pamoja na Mtume wa kibinadamu ili waweze kuzungumza naye na kunufaika na mafundisho yake. Hata katika hali hii, (ya Malaika kuwa katika umbo la kibinadamu) naye anaweza kusababisha utatanishi baina yao kama vile walivyokosa kuelewana juu ya kuukubali Utume wa mwanadamu. Allah تعالى Amesema;

قُلْ لَوْ كَانَ فِي الْاَرْضِ مَلٰٓئِكَةٌ يَّمشُوْنَ مُطْمَئِنِّيْنَ لَنَزَلْنَا عَلَيْهِمْ مِنَ السَّمٰوٰتِ

مَلٰٓئِكًا رُّسُوْلًا ﴿١٠﴾

“Sema: Ingelikuwa duniani wapo Malaika wanatembea kwa utulivu wao, basi bila ya shaka Tungeliwateremshia Malaika kuwa ni Mtume wao”. (17:95)

Ni kutokana na rehema za Allah تعالى kwa viumbe wake, Yeye Huwapelekea wao Mtume anayetokana na jinsi yao, ili iwezekane kwake kuwalingania, ili

baadhi yao wanufaike kutokana na Alivyosema Allah تعالى:

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ ءَايَاتِهِ
وَيُزَكِّيهِمْ

“Hakika Mwenyezi Mungu Amewafanyia wema mkubwa Waumini vile Alivyowaletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, anayewasomea Aya Zake, na anawatakasa”. (3:164)

Adh-Dhahhak amesema Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Ayah hii (6:9), “Kama Malaika angetumwa kwao, angekwenda akiwa katika umbo la mtu, kwa sababu wao wasingeweza kumtazama Malaika kwa sababu ya nuru.”¹

وَلَكَبَسْنَا عَلَيْهِم مَّا يَلِيْسُونَ

“...na Tungeliwatilia matatizo yale wanayoyatatiza wao”.

Maana: Tungeliwatatiza wao juu ya wanayotatizana nayo. Al-Walibi amesimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Tungeliwatatiza juu yao”.

وَلَقَدْ آسَفْنَاهُ بِرُسُلِهِ مِّن قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالذِّكْرِ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ

“Na hakika Mitume walio kabla yao walifanyiwa kejeli, lakini waliowafanyia kejeli wakaja kuzungukwa na yale yale waliyokuwa wao wanayafanyia kejeli”.

Huku ni kumfariji Mtume kutokana na baadhi ya watu kumkadhibisha. Pia ni kumuahidi yeye na Waumini kuhusu Nusura ya Allah تعالى, na mwisho mwema duniani na Akhera. Kisha Allah تعالى Akasema:

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ ثُمَّ أَنْظِرُوا كَيْفَ كَانَ عَنقِبَةُ الْمُكذِبِينَ

“Sema: Tembeeni ulimwenguni, kisha mtazame ulikuwaje mwisho wa wanaokanusha”.

Maana yake: Jifikirieni nyinyi wenyewe, na mfanye taamuli kuhusu adhabu ambazo Allah تعالى Aliwapatia mataifa yaliyotangulia, ambao waliwakadhibisha Mitume wao, wakawafanyia ukaidi. Allah تعالى Aliwapelekea adhabu, huzuni na madhila humu duniani, pamoja na kuwawekea adhabu iumizayo huko Akhera. Wakati huo huo Aliwaokoa Mitume Wake na waja Wake Waumini.

¹ At-Tabari 11:268.

قُلْ لِمَنْ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ قُلْ لِلَّهِ ۗ كَتَبَ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ۗ
 لِيَجْمَعَنَّكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ ۗ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ۝
 ۝ * وَلَهُ مَا سَكَنَ فِي اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ۝ قُلْ أَعْيَرَ اللَّهُ اتَّخَذُ
 وَلِيًّا فَاطِرِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ يُطْعِمُ وَلَا يُطْعَمُ ۗ قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ
 أَوَّلَ مَنْ أَسْلَمَ ۗ وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ۝ قُلْ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي
 عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ۝ مَنْ يُصْرَفْ عَنْهُ يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمَهُ ۗ وَذَٰلِكَ الْفَوْزُ لِلْمُؤْمِنِينَ ۝

**12. Sema: Ni vya nani vilivyomo katika mbingu na katika ardhi?
 Sema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Yeye Amejilazimisha Nafsi Yake
 Kurehemu. Hakika Atakukusanyeni Siku ya Kiyama isiyokuwa na
 shaka. Waliojikhasiri wenyewe hawaamini.**

**13. Na ni Vyake vilivyotulia usiku na mchana. Naye Ndiye Mwenye
 Kusikia na Mwenye kujua.**

**14. Sema: Je, nimchukue rafiki mlinzi asiyekuwa Mwenyezi Mungu,
 Ambaye Ndiye Muumba mbingu na ardhi, Naye Ndiye Anayelisha
 wala Halihi? Sema: Mimi nimeamrisha niwe wa kwanza wa
 wenye kusilimu. Na wala kabisa usiwe miongoni mwa washirikina.**

**15. Sema: Mimi naogopa adhabu ya Siku kubwa hiyo ikiwa
 nitamuasi Mola wangu Mlezi.**

**16. Atakayepushwa nayo adhabu hiyo katika siku hiyo atakuwa
 Mwenyezi Mungu Amemrehemu. Na huko ndiko kufuzu kuliko
 wazi".**

Allah تعالیٰ Ndiye Muumbaji na Mtoaji Riziki, ni Wajibu Kumtii.

Allah تعالیٰ Anaeleza kuwa Yeye Ndiye Mwenye Kuzimiliki Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake, na kwamba Ameandikia Nafsi Yake Tukufu Rehema.

Ni kama ilivyothibitishwa katika *Sahih* Mbili, kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ اللَّهَ لَمَّا خَلَقَ الْخَلْقَ، كَتَبَ كِتَابًا عِنْدَهُ فَوْقَ الْعَرْشِ، إِنَّ رَحْمَتِي تَغْلِبُ غَضَبِي»

"Allah Alipowaumba viumbe, Aliandika katika Kitabu Alichonacho katika 'Arsh; "Kwa hakika, Rehema Zangu zinaishinda Ghadhabu Yangu."¹

لَيَجْمَعَنَّكُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ^٥

"Hakika Atakukusanyeni Siku ya Kiyama isiyokuwa na shaka".

Ameapa kwa Nafsi Yake Tukufu kuwa Atawakusanya waja Wake.

إِلَى مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ

"kwa wakati wa siku maalumu". (56:50)

Nayo ni siku ya Kiyama ambayo haina shaka kwa waja Wake Waumini kuhusu uhakika wake. Ama wale wanaomkataa na kukadhibisha, wapo katika mashaka na vurugu. Na Kauli Yake;

الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ

"Waliojikasiri nafsi zao". Maana yake: Katika Siku ya Kiyama.

فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ

"...wenyewe hawaamini".

Maana yake: Hawayasadiki marejeo, wala hawayahofii matatizo ya siku hiyo. Kisha Allah تعالى Akasema;

وَلَهُ مَا سَكَنَ فِي اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ^٦

"Na ni Vyake vilivyotulia usiku na mchana".

Maana yake: Kila kitu kilichopo mbinguni na ardhini ni mja na ni kiumbe Wake Yeye, na yuko chini ya Mamlaka, Nguvu na Utashi Wake, hapana mola aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye.

وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

"Naye Ndiye Mwenye Kusikia na Mwenye Kujua".

¹ Fat'hul Al-Bari 13:395 na Muslim 4:2107.

Anazisikia kauli za waja Wake, Anayajua matendo yao, dhamira na siri zao. Halafu Allah تعالى Akamuambia mja na Mjumbe Wake, Muhammad ﷺ ambaye Alimtuma kwa *Tawhid* halisi na Dini nyoofu na Akamuamuru awalinganie watu katika njia iliyonyooka.

قُلْ أَغَيَّرَ اللَّهُ إِلَهُمُ الَّذِي قَدَّمُوا فَاطِرِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Sema: Je, nimchukue rafiki mlinzi asiyekuwa Mwenyezi Mungu, Ambaye Ndiye Muumba wa mbingu na ardhi”.

Ni sawa na Kauli Yake;

قُلْ أَفَغَيَّرَ اللَّهُ تَأْمُرُونَ أَعْبُدُ أَيُّهَا الْجَاهِلُونَ ﴿٦١﴾

“Sema: Je, mnaniamrisha nimuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, enyi majahili?”

Maana yake hapa ni kuwa sitamfanya yeyote kuwa mlezi wangu isipokuwa Allah تعالى Peke Yake, Hana mshirika, kwani Yeye Ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi, Aliyeianzisha pasi na kuwepo mithili kabla yake.

وَهُوَ يُطْعِمُ وَلَا يُطْعَمُ

“...Naye Ndiye Anayelisha wala Halishwi?”

Maana; Yeye Huwakimu viumbe Wake pasi na kuwa na haja kwao. Kama Alivyosema Allah تعالى;

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

“Nami Sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi”. (51:56)

Baadhi ya wanazuoni husoma;

وَهُوَ يُطْعِمُ وَلَا يُطْعَمُ

“Naye Hulisha wala Hali”

Kwamba Allah تعالى Hali. Na katika Hadithi aliyoisimulia Abu Hurayrah رضي الله عنه, Mtu mmoja katika Al-Ansar kutoka sehemu za Qubah alimualika Mtume ﷺ kwa ajili ya chakula, nasi tukaenda pamoja naye. Mtume ﷺ alipomaliza kula na kuosha mikono yake, alisema;

«الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي يُطْعِمُ وَلَا يُطْعَمُ، وَمَنْ عَلَيْنَا فِهْدَانًا وَأَطْعَمَنَا، وَسَقَانَا مِنَ الشَّرَابِ، وَكَسَانَا مِنَ الْعُرْيِ، وَكُلَّ بَلَاءٍ حَسَنٍ أَبْلَانَا، الْحَمْدُ لِلَّهِ غَيْرَ مُؤَدَّعٍ رَبِّي وَلَا مُكَافَأٍ وَلَا مَكْفُورٍ، وَلَا مُسْتَعْنَى عَنْهُ، الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَطْعَمَنَا مِنَ الطَّعَامِ، وَسَقَانَا مِنَ الشَّرَابِ، وَكَسَانَا مِنَ الْعُرْيِ، وَمَدَانَا مِنَ الضَّلَالِ، وَبَصَّرَنَا مِنَ الْعَمَى، وَفَضَّلَنَا عَلَى كَثِيرٍ مِمَّنْ خَلَقَ تَفْضِيلًا، الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ»

“Namshukuru Allah Ambaye Hulisha wala Hali shwi, Ametu neemesha na Ametuhidi na Kutulisha, Akatupatia kinywaji, Akatusitiri kwa Kutuvisha hali ya kuwa tulikuwa uchi, Na kila neema Ametujaribu. Namshukuru Allah kwa Neema Zake zisizoachwa, wala kurudishwa, wala kukanushwa. Au (mtu kuweza) kujitosheleza bila ya kuhitajia neema za Allah. Namshukuru Allah Ambaye Ametulisha chakula, Akatupatia kinywaji, Akatuvisha dhidi ya kuwa uchi, Akatuongoa dhidi ya upotofu, Akatupatia uoni dhidi ya upofu na Akatunyanyua hadhi juu ya viumbe Wake wengi. Namshukuru Allah, Mola wa walimwengu wote.”¹

قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَسْلَمَ

“Sema: Mimi nimeamrisha niwe wa kwanza wa wenye kusilimu”.

Maana yake: Katika umma huu.

وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٦٤﴾ قُلْ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٦٥﴾

“Na wala kabisa usiwe miongoni mwa washirikina. Sema: Mimi naogopa adhabu ya Siku kubwa hiyo ikiwa nitamuasi Mola wangu Mlezi”. (6:14-15)

Maana yake: Siku ya Kiyama.

مَنْ يُصِرْفَ عَنْهُ

“...yule atakayeepushwa nayo”.

Maana: Adhabu.

¹ An-Nasai katika Al-Kubra 6:82.

فَقَدْ رَجِمَهُ^ع

"...katika siku hiyo atakuwa Mwenyezi Mungu Amemrehemu".

Maana yake: Amekuwa na huruma naye.

وَدَلِكِ الْفَوْزُ الْمُبِينُ

"Na huko ndiko kufuzu kuliko wazi".

Kama katika Kauli Yake nyingine;

فَمَنْ زُحِرَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ^ه وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿١٨٥﴾

"Na Atakayeepushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu". (3:185)

Kufaulu kunaleta faida na kuondosha hasara.

* * *

وَإِن يَمَسُّكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ ۗ وَإِن
 يَمَسُّكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٧﴾ وَهُوَ الْقَاهِرُ
 فَوْقَ عِبَادِهِ ۗ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ ﴿٨﴾ قُلْ أَيُّ شَيْءٍ أَكْبَرُ
 شَهَادَةً ۗ قُلِ اللَّهُ ۗ شَهِدْتُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۗ وَأُوحِيَ إِلَيَّ هَذَا
 الْقُرْآنُ لِأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ ۗ أَلَيْسَ لَكُمْ لَشَهِدُونَ أَنْ
 مَعَ اللَّهِ إِلَهَةٌ أُخْرَىٰ ۗ قُلْ لَا أَشْهَدُ ۗ قُلْ إِنَّمَا هُوَ إِلَهُهُ وَاحِدٌ
 وَإِنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٩﴾ الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ
 يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ آبَاءَهُمْ ۗ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ
 فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠﴾ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ
 كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾
 وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا أَيْنَ شُرَكَائُكُمْ
 الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿١٢﴾ ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فَتَنْتَهُمْ إِلَّا أَنْ
 قَالُوا وَاللَّهِ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿١٣﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ كَذَبُوا
 عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ ۗ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿١٤﴾ وَوَيْهِمْ
 مَنْ يَسْتَمِعُ إِلَيْكَ ۗ وَجَعَلْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَنْ يَفْقَهُوهُ وَفِي
 آذَانِهِمْ وَقْرًا ۗ وَإِنْ يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَا يُؤْمِنُوا بِهَا ۗ حَتَّىٰ إِذَا
 جَاءُوكَ مُجْتَدِلُونَكَ يَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ هَذَا إِلَّا أَسْطِيرٌ
 الْأُولِينَ ﴿١٥﴾ وَهُمْ يَتَّبِعُونَ عَنَتَهُ وَيَتَّبِعُونَ عَنَتَهُ ۗ وَإِن
 يُهْلِكُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿١٦﴾

وَإِن يَمَسُّكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ
 لَهُ إِلَّا هُوَ ۗ وَإِن يَمَسُّكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ
 عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٧﴾ وَهُوَ
 الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ ۗ وَهُوَ الْحَكِيمُ
 الْخَبِيرُ ﴿٨﴾ قُلْ أَيُّ شَيْءٍ أَكْبَرُ
 شَهَادَةً ۗ قُلِ اللَّهُ ۗ شَهِدْتُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۗ
 وَأُوحِيَ إِلَيَّ هَذَا الْقُرْآنُ لِأُنذِرَكُمْ
 بِهِ وَمَنْ بَلَغَ ۗ أَلَيْسَ لَكُمْ لَشَهِدُونَ
 أَنْ مَعَ اللَّهِ إِلَهَةٌ أُخْرَىٰ ۗ قُلْ لَا
 أَشْهَدُ ۗ قُلْ إِنَّمَا هُوَ إِلَهُهُ وَاحِدٌ وَإِنِّي
 بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٩﴾ الَّذِينَ
 آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا
 يَعْرِفُونَ آبَاءَهُمْ ۗ الَّذِينَ خَسِرُوا
 أَنفُسَهُمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠﴾
 وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ
 كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ
 الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾

17. Na ikiwa Mwenyezi
 Mungu Akikugusisha
 madhara, basi hapana wa
 kukuondolea hayo ila Yeye.
 Na ikiwa Akikugusisha

kheri, basi Yeye Ndiye Mwenye Uweza wa kila kitu. Naye Ndiye Mwenye Uweza wa kila kitu.

18. Naye Ndiye Mwenye Nguvu juu ya waja Wake, na Ndiye Mwenye Hikima na Mwenye khabari zote.

19. Sema: Kitu gani ushahidi wake mkubwa kabisa? Sema: Mwenyezi Mungu. Yeye Ndiye Shahidi baina yangu na nyinyi. Na nimefunuliwa Qur'an hii ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia. Ati kweli nyinyi mnashuhudia kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu wapo miungu wengine? Sema: Mimi sishuhudii hayo. Sema: Hakika Yeye ni Mungu Mmoja tu, nami ni mbali na mnaowashirikisha.

20. Wale Tuliowapa Kitabu wanayajua haya kama wanavyowajua watoto wao. Wale waliozikhasiri nafsi zao hawaamini.

21. Na nani dhalimu zaidi kuliko anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu, au akazikanusha Ishara Zake? Hakika madhalimu hawafanikiwi".

Allah تعالیٰ Ndiye Mnufaishaji, Mwenye Kuleta Madhara, Mwenye Nguvu.

Allah تعالیٰ Anaeleza Yeye Pekee Ndiye Mmiliki wa madhara na manufaa na Yeye Hufanya vile Atakavyo kwa waja Wake, hapana mwenye kuthubutu kuikinza hukumu wala kulizuia Analoliamua.

وَإِنْ يَمْسَسْكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ ۗ وَإِنْ يَمْسَسْكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ

قَدِيرٌ ﴿٦١﴾

"Na ikiwa Mwenyezi Mungu Akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye. Na ikiwa Akikugusisha kheri, basi Yeye Ndiye Mwenye Uweza wa kila kitu.

Ni sawa na Kauli Yake nyingine;

مَا يَفْتَحِ اللَّهُ لِلنَّاسِ مِنْ رَحْمَةٍ فَلَا مُمْسِكَ لَهَا ۗ وَمَا يُمْسِكُ فَلَا مُرْسِلَ لَهُ مِنْ بَعْدِهِ ۗ

“Rehema ambayo Mwenyezi Mungu Anawafungulia watu hapana wa kuizuia. Na Anayoizuia hapana wa kuipeleka isipokuwa Yeye”. (35:2)

Katika Sahih imenukuliwa Mtume ﷺ alikuwa akisema;

«اللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أُعْطِيَتْ وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ»

“Ewe Allah, hapana mwenye kuyazuia Uliyoyatoa, wala mwenye kutoa Uliyoyazuia, wala hakuna bahati yoyote dhidi yako itakayomnufaisha mwenye sudi”¹.

Kwa ajili hii Allah تعالیٰ Amesema;

وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ

“Naye Ndiye Mwenye Nguvu juu ya waja Wake.” Maana: Yeye Ndiye Ambaye shingo humnyenyekea, na madikteta huwa dhalili Kwake na Ana Nguvu juu ya kila kitu. Viumbe hawana thamani Kwake na wako chini ya Utukufu Wake, Kiburi Chake, Ukuu Wake na Uweza Wake wa mambo yote. Vyote ni vyenye kunywea mbele Yake na viko chini ya Nguvu na Uamuzi Wake.

وَهُوَ الْحَكِيمُ

“...na Ndiye Mwenye Hikima”. Katika Matendo Yake yote.

الْخَبِيرُ

“Mwenye khabari zote”. Kwa Kuviweka vitu mahali vinapostahili, na wala hampatii yeyote isipokuwa Anayestahiki. Kisha Allah تعالیٰ Akasema;

قُلْ أَىُّ شَىْءٍ أَكْبَرُ شَهَادَةً

“Sema: Kitu gani ushahidi wake mkubwa kabisa?”

Maana yake: Ni kitu gani chenye ushahidi mkubwa zaidi.

قُلْ اللَّهُ شَهِدٌ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ

“Sema: Mwenyezi Mungu. Yeye Ndiye Shahidi baina yangu na nyinyi”.

Kwani Anakijua vyema nilichokuleteeni, na juu ya yale mnayoyasema kunihusu.

¹ Fat’hul Al-Bari 2:379.

وَأُوحِيَ إِلَيَّ هَذَا الْقُرْآنُ لِأُنذِرْكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

“Na nimefunuliwa Qur’an hii ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia”.

Maana: Qur’an hii ni yenye kumuonya kila inayemfikia. Ni kama katika Kauli nyingine ya Allah;

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَالِنَارُ مَوْعِدُهُ

“...na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao”. (11:17)

Ar-Rabi’ bin Anas alisema, “Wale wanaomfuata Mtume ﷺ wanatakiwa walinganie sawa na alivyoonya.” Na Kauli Yake;

أَيُّكُمْ لَتَشْهَدُونَ

“Ati kweli nyinyi mnashuhudia”. Enyi washirikina.

أَنْتَ مَعَ اللَّهِ ءِالِهَةً أُخْرَى قُلْ لَا أَشْهَدُ

**“...kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu wapo miungu wengine?
Sema: Mimi sishuhudii hayo”.** Na katika Aya nyingine, Alisema;

فَإِنْ شَهِدُوا فَلَا تَشْهَدْ مَعَهُمْ

“Basi wakishuhudia, wewe usishuhudie pamoja nao”. (6:150)

قُلْ إِنَّمَا هُوَ إِلَهُهُ وَاحِدٌ وَإِنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ

“Sema: Hakika Yeye ni Mungu Mmoja tu, nami ni mbali na mnaowashirikisha”.

Watu wa Kitabu Wanamjua Mtume Kama Wawajuavyo Watoto Wao.

Baada ya maelezo hayo, Allah تعالی Alielezea kuhusu watu waliopewa Kitabu: kuwa wao wanakifahamu ulichowaletea, kama wanavyowajua watoto wao kwa sababu wanazo khabari kutoka kwa wajumbe na Mitume waliotangulia. Mitume wote walitoa bishara za ujio wa Muhammad ﷺ na sifa na wasifu wake, mji wake, kuhama kwake na sifa za umma wake. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema;

الَّذِينَ حَسِبُوا أَنفُسَهُمْ

“Wale waliozikhasiri nafsi zao”. Na kwa hivyo walipata hasara kubwa zaidi.

فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٧﴾

"...*hawaamini*" Ni kuhusu jambo hili lililo dhahiri shahiri ambalo lilibashiriwa na Mitume na ni jambo lililotukuzwa sana hapo zamani na wakati huu. Allah تعالى Akasema tena;

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ

"Na nani dhalimu zaidi kuliko anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu, au akazikanusha Ishara Zake?"

Maana: Hapana dhalimu zaidi kuliko aliyemzulia urongo Allah تعالى, akadai kuwa eti Allah تعالى amemtuma, na hali hakumtuma, kisha hakuna dhalimu zaidi kuliko aliyekadhibisha Aya, hoja, ushahidi na dalili za Allah تعالى.

إِنَّهُ لَا يَفْلِحُ الظَّالِمُونَ

"Hakika madhalimu hawafanikiwi".

Kwa hakika, watu wa namna mbili, hawatafuzu, mzushi na mkadhibishaji.

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا آيِنَ شُرَكَائِكُمْ الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿١٧﴾
 ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فَتَنْتُهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا وَاللَّهِ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿١٨﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ كَذَبُوا
 عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ ۖ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿١٩﴾ وَمِنْهُمْ مَّنْ يَسْتَمِعُ إِلَيْكَ ۗ وَجَعَلْنَا
 عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَنْ يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۖ وَإِنْ يَرَوْا كَلًّا ۖ آيَةً لَا يُؤْمِنُونَ
 بِهَا حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوكَ مُجِدِّدُونَكَ يَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ هَذَا إِلَّا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٠﴾
 وَهُمْ يَنْهَوْنَ عَنْهُ وَيَنْتَوِبُونَ عَنْهُ ۖ وَإِنْ يُهْلِكُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٢١﴾

22. Siku Tutapowakusanya wote pamoja, kisha Tuwaambie walioshirikisha: Wako wapi washirikishwa wenu mliokuwa mnadai?

23. Kisha hautakuwa udhuru wao ila ni kusema: Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.

24. Tazama jinsi wanavyojisemea uwongo wenyewe. Na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua.

25. Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza; na Tumezitia pazia nyoyo zao wasije kuyafahamu. Na upo uziwi masikioni mwao, na wakiona kila Ishara hawaiamini. Hata wakikujia kwa kujadiliana nawe, wanasema waliokufuru: Hizi si chochote ila hadithi za watu wa kale.

26. Nao huwazuia watu, na wao wenyewe wanajitenga nayo. Nao hawaangamizi ila nafsi zao tu, wala wao hawatambui.

Washirikina Wanahojiwa Kuhusu Ushirikina Wao.

Kuhusu Washirikina, Allah تعالى Amesema:

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا

“Siku Tutapowakusanya wote pamoja”. Katika Siku ya Kiyama, kisha Atawahoji kuhusu masanamu na washindani waliowaabudu badala ya Yeye. Allah تعالى Atawaambia;

أَيْنَ شُرَكَائِكُمُ الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ

“Wako wapi washirikishwa wenu mliokuwa mnadai?”

Ni sawa na Kauli Yake katika Surat Al-Qasas;

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ أَيْنَ شُرَكَائِيَ الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٦٢﴾

“Na siku Atakapowaita na Akasema: Wako wapi mliokuwa mkidai ni washirika Wangu?” (28:62)

Kauli ya Allah تعالى,

ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فِتْنَتُهُمْ

“Kisha hautakuwa udhuru wao”. Maana, hoja. ‘Ata Al-Khurasani amesema;

ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فِتْنَتُهُمْ

“Kisha hautakuwa udhuru wao”. Katika mateso watakayopatiwa.

إِلَّا أَنْ قَالُوا وَاللَّهِ رَبَّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ

“...ila ni kusema: Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina”¹.

¹ At-Tabari 11:299.

Allah تعالی Amesema;

أَنْظِرْ كَيْفَ كَذَبُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ ۖ وَصَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٦٤﴾

“Tazama jinsi wanavyojisemea uwongo wenyewe. Na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua”.

Hii ni sawa na Kauli Yake nyingine;

ثُمَّ قِيلَ لَهُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ تُشْرِكُونَ ﴿٦٥﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۗ قَالُوا ضَلُّوا عَنَّا بَلْ لَمْ نَكُنْ نَدْعُوا مِنْ قَبْلُ شَيْئًا ۚ كَذَلِكَ يَضِلُّ اللَّهُ الْكَافِرِينَ ﴿٦٦﴾

“Tena wataambiwa: Wako wapi mliokuwa mkiwashirikisha. Badala ya Allah? Watasema: Wametupotea, bali tangu zamani hatukuwa tukiomba kitu! Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Anawaachia makafiri wapotelee mbali”. (40:73-74)

Muovu Hanufaiki na Qur'an.

Kauli ya Allah تعالی Amesema;

وَمِنْهُمْ مَنْ يَسْتَمِعُ إِلَيْكَ ۗ وَجَعَلْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَنْ يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۚ وَإِنْ يَرَوْا كُلًّا ءَابَيْتُمْ لَا يُؤْمِنُوا بِهَا ۚ

“Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza; na Tumezitia pazia nyoyo zao wasije kuyafahamu. Na upo uziwi masikioni mwao, na wakiona kila Ishara hawaiamini”.

Maana yake, wanakuja (kwako, ewe Muhammad ﷺ) kukusikiliza kisomo chako, lakini hawanufaiki nacho kwani Allah تعالی Amejaalia, pazia nyoyo zao. Maana, vifuniko ili wasiielewe Qur'an.

وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۚ

“Na upo uziwi masikioni mwao”. Unawazuia kuyasikia ya kuwanufaisha. Katika Aya hii nyingine, Allah تعالی Amesema;

وَمَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا كَمَثَلِ الَّذِي يَنْعِقُ بِمَا لَا يَسْمَعُ إِلَّا دُعَاءً وَنِدَاءً ۚ

“Na mfano wa waliokufuru ni kama mfano wa anayempigia kelele asiyesikia ila wito na sauti tu”. (2:171)

وَأِنْ يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَا يُؤْمِنُوا بِهَا^ع

“...na wakiona kila Ishara hawaiamini”.

Maana: Aya, hoja, ushahidi wa wazi na alama zozote wanazoziona hawaiamini, hawana ufahamu halisi wala Uamuzi safi. Ni kama Alivyosema katika Kauli Yake nyingine;

وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَأَسْمَعَهُمْ^ط

“Na Mwenyezi Mungu Angelijua wema wowote kwao Angeliwa-sikilizisha”. (8:23)

Na Kauli Yake;

حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوكَ تُجَادِلُونَكَ

“Hata wakikujia kwa kujadiliana nawe.”

Wanasailiana nawe na kukufanyia mdahalo kutumia batili dhidi ya haki.

يَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّا هَذَا إِلَٰهٌ آسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ

“...wanasema waliokufuru: Hizi si chochote ila hadithi za watu wa kale”.

Maana: Haya uliyokuja nayo si lolote, bali yamenakiliwa kutoka katika vitabu vilivyotangulia. Na Kauli Yake;

وَهُمْ يَنْهَوْنَ عَنْهُ وَيَنْعَوْنَ عَنْهُ^ط

“Nao huwazuia watu, na wao wenyewe wanajitenga nayo”.

Ni kuwa, wanawakataza watu kuifuata haki ya kumfuata Mtume na kuitii Qur'an.

وَيَنْعَوْنَ عَنْهُ^ط

“...na wao wenyewe wanajitenga nayo”.

Maana: Pia wanawabaidisha nayo, na kwa ajili hiyo wanatenda maovu mawili kwa pamoja, hawanufaiki wala hawamuwachii yeyote anufaika naye. Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema;

وَهُمْ يَنْهَوْنَ عَنْهُ

“Nao huwazuia watu”.

Wanawazuia watu ili wasimuamini Muhammad ﷺ¹.

Na Muhammad bin Al-Hanafiyyah رحمه الله تعالى alisema, “Makafiri wa Kikuraishi walikuwa wakimuepuka Muhammad ﷺ na waliwazuilia watu wengine kumuendea².”

Hayo pia yalisemwa na Qatadah, Mujahid, Adh-Dhahhak na wengine³.

وَأِنْ يُّهْلِكُونِ إِلَّا أَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ

“Nao hawaangamizi ila nafsi zao tu, wala wao hawatambui”.

Kwa maana: kwa kitendo hiki, hawamuangamizi mwingine yeyote isipokuwa nafsi zao na madhila yake yatawakumba wao wenyewe, na wao hawalitambui hili.

* * *

¹ At-Tabari 11:311.

² At-Tabari 11:311.

³ At-Tabari 11:312.

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وَقَفُوا عَلَى النَّارِ فَقَالُوا يَلَيْتَنَا زُرُّدٌ وَلَا نُكَذِّبُ
 بِغَايَتِ رَبِّنَا وَنَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٧﴾ بَلْ بَدَأَ هُمْ مَا
 كَانُوا يُخْفُونَ مِنْ قَبْلُ ۗ وَلَوْ رُدُّوا لَعَادُوا لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ
 لَكَاذِبُونَ ﴿٢٨﴾ وَقَالُوا إِن هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا وَمَا نَحْنُ
 بِمَبْعُوثِينَ ﴿٢٩﴾ وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وَقَفُوا عَلَى رَبِّهِمْ ۖ قَالَ أَلَيْسَ
 هَذَا بِالْحَقِّ ۗ قَالُوا بَلَىٰ وَرَبِّنَا ۗ قَالَ فَذُقُوا الْعَذَابَ بِمَا
 كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٠﴾ قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِلِقَاءِ اللَّهِ حَتَّىٰ
 إِذَا جَاءَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً قَالُوا يَسْحَرَتْنَا عَلَىٰ مَا فَرَطْنَا
 فِيهَا وَهُمْ يَحْمِلُونَ أَوْزَارَهُمْ عَلَىٰ ظُهُورِهِمْ ۗ أَلَا سَاءَ مَا
 يَزُرُونَ ﴿٣١﴾ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَعِبٌ وَلَهُوَ ۗ وَلِلْآخِرَةِ
 الْآخِرَةُ خَيْرٌ لِّذِينَ يُتَّقُونَ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٣٢﴾ قَدْ نَعَلِمُ
 إِنَّهُ لَيَخْزُنكَ الَّذِي يَقُولُونَ ۗ فَإِنَّهُمْ لَا يُكَذِّبُونَكَ وَلَئِنَّ
 الظَّالِمِينَ بِغَايَتِ اللَّهِ يَحْجِدُونَ ﴿٣٣﴾ وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ
 مِنْ قَبْلِكَ فَصَبَرُوا عَلَىٰ مَا كُذِّبُوا وَأَوَدُّوا حَتَّىٰ أَنهَمُ نَصْرَتْنَا
 ۗ وَلَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۗ وَلَقَدْ جَاءَكَ مِنْ نَبِيِّنَا
 الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٤﴾ وَإِنْ كَانَ كَبُرَ عَلَيْكَ إِعْرَاضُهُمْ فَإِنْ
 اسْتَطَعْتَ أَنْ تَبْتَغِيَ نَفَقًا فِي الْأَرْضِ أَوْ سُلَّمًا فِي السَّمَاءِ
 فَتَأْتِيَهُمْ بِغَايَةِ ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَمَعَهُمْ عَلَى الْهَدْيِ ۗ فَلَا
 تَكُونَنَّ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٣٥﴾ * إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ
 يَسْمَعُونَ وَالْمَوْتَىٰ يَجْعَلُهُمُ اللَّهُ ثُمَّ إِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٣٦﴾

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وَقَفُوا عَلَى النَّارِ فَقَالُوا
 يَلَيْتَنَا زُرُّدٌ وَلَا نُكَذِّبُ بِغَايَتِ رَبِّنَا
 وَنَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٧﴾ بَلْ بَدَأَ
 هُمْ مَا كَانُوا يُخْفُونَ مِنْ قَبْلُ ۗ وَلَوْ
 رُدُّوا لَعَادُوا لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ
 لَكَاذِبُونَ ﴿٢٨﴾ وَقَالُوا إِن هِيَ إِلَّا
 حَيَاتُنَا الدُّنْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ
 ﴿٢٩﴾ وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وَقَفُوا عَلَى رَبِّهِمْ
 ۖ قَالَ أَلَيْسَ هَذَا بِالْحَقِّ ۗ قَالُوا بَلَىٰ
 وَرَبِّنَا ۗ قَالَ فَذُقُوا الْعَذَابَ بِمَا
 كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٠﴾

**27. Na ungeona wataka-
 posimamishwa kwenye
 Moto, wakawa wanasema:
 Laiti tungelirudishwa, wala
 hatutakanusha tena Ishara
 za Mola wetu Mlezi, na
 tutakuwa miongoni mwa
 Waumini.**

**28. Bali yamewadhihirikia
 waliyokuwa wakiyaficha
 zamani. Na kama wangeli-
 rudishwa bila ya shaka
 wangeparejea yale yale
 waliyokatazwa. Na hakika
 hao ni waongo.**

29. Na walisema: Hakuna mengine ila maisha yetu haya ya duniani, wala sisi hatutafufuliwa.

30. Na lau ungeliona watavyosimamishwa mbele ya Mola wao Mlezi. Je, si kweli haya. Na wao watasema: Kwani? Tunaapa kwa Mola Mlezi wetu ni kweli. Yeye Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya vile mlivyokuwa mnakataa.

Matumaini na Utashi Havitamnufaisha Yeyote Mara Atakapoiona Adhabu.

Allah تعالى Anaitaja hali ya makafiri watakaposimamishwa mbele ya Moto katika Siku ya Kiyama na wakaiona minyororo yake na pingu, pamoja na kuyashuhudia kwa macho mambo hayo ya kutisha na ya nguvu. Basi hapo, watasema;

يَلَيَّتْنَا نُرْدُ وَلَا نُكْذِبُ بِآيَاتِ رَبِّنَا وَنَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

“Laiti tungelirudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni mwa Waumini”.

Wanatamani warejeshwe katika maisha ya duniani ili waweze kufanya amali njema, na ili wasizikadhibishe Aya za Mola wao na ili wawe miongoni mwa Waumini.

بَلْ بَدَأَ هُمْ مَّا كَانُوا يُخْفُونَ مِن قَبْلُ

“Bali yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani”.

Maana: Bali wakati huo yatawadhihirikia yale waliyokuwa wakiyaficha katika ukafiri, ukadhibishaji na ukaidi. Hayo yatawakumba hata kama watayakana duniani au Akhera.

Kama hapo nyuma kidogo, Allah تعالى Alivyosema;

نُرِّمُ لَمْ تَكُنْ فِتْنَتُهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا وَاللَّهِ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿٦٣﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ كَذَّبُوا عَلَيَّ أَنْفُسِهِمْ ۖ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٦٤﴾

“Kisha hautakuwa udhuru wao ila ni kusema: Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina. Tazama jinsi wanavyojisemea uwongo wenyewe. Na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua”.
(6:23-24)

Pia maana yake hapa yaweza kuwa watadhihirikiwa na ukweli ambao walikuwa wakiujua katika nafsi zao, kama vile ukweli wa yale waliyokuja nayo Mitume duniani, ingawa walikuwa wakiwaonyesha wafuasi wao kinyume cha hivyo.

Ni kama katika Kauli Yake Alipomzungumzia Nabii Musa عليه السلام, kuwa alimuambia Firauni;

لَقَدْ عَلِمْتِ مَا أَنْزَلَ هُنَا ۖ إِلَّا رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ بِصَآئِرٍ

“Wewe unajua bila ya shaka kuwa haya hakuyateremsha ila Mola Mlezi wa mbingu na ardhi ili kuwa ni ushahidi wa kuonekana”.
(17:102)

Pia kauli ya Allah تعالى Akitoa khabari za Firauni na kaumu yake;

وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا

“Na wakazikataa kwa dhuluma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo”. (27:14)

بَلْ بَدَأَ هُمْ مَّا كَانُوا مُخْتَفُونَ مِنْ قَبْلُ

“Bali yamewadhahirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani”.

Kwa hakika, hawakutaka kurejea duniani kwa kutaka na kupenda kuwa na Imani, bali ni kwa sababu ya kuiogopa adhabu wanayoishuhudia, ikiwa ni malipo ya yale waliyokuwa nayo katika ukafiri.

Kwa ajili hiyo wanaomba warejee duniani, ili waweze kujiokoa dhidi ya waliyoyaona motoni.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema;

وَلَوْ رُدُّوا لَعَادُوا لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ

“Na kama wangelirudishwa bila ya shaka wangeyarejea yale yale waliyokatazwa. Na hakika hao ni waongo”.

Maana: kule kutamani kwao kurudi kwa kuitaka na kuipenda Imani. Kisha Akatoa maelezo yanayowahusu hao kuwa, ***“...kama wangelirudishwa”*** duniani ***“...bila ya shaka wangeyarejea yale yale waliyokatazwa”***. Ukafiri na uasi.

وَلَهُمْ لَكُذِبُونَ

“Na hakika hao ni waongo”.

Maana: kuhusu kusema kwao,

يَلِيَّتَنَا نُرُدُّ وَلَا نُكْذِبُ بِعَايَتِ رَبِّنَا وَنَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٧﴾

“Laiti tungelirudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni mwa Waumini.”

Maana: wangeyarejea yale waliyokatazwa kuyafanya na wangesema;

إِنَّ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا أَلْدُنْيَا

“Hakuna mengine ila maisha yetu haya ya duniani.”

Maana: Hakuna lolote, bali ni maisha haya haya ya duniani tu, hakuna tena kurejea baada yake. Ndio maana Akasema;

وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ

“...wala sisi hatutafufuliwa.”

Kisha Allah تعالى Akasema;

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وُقِفُوا عَلَىٰ رَبِّهِمْ

“Na lau ungeliona watavyosimamishwa mbele ya Mola wao Mlezi”.

Maana: Wakiwa wamesimamishwa mbele Yake, na kuwaambia;

أَلَيْسَ هَذَا بِالْحَقِّ

“Je, si kweli haya?” Maana: je, marejeo haya si ya kweli? Wala si ya uwongo, kama mlivyokuwa mkidhani.

قَالُوا بَلَىٰ وَرَبِّنَا قَالَ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ

“Na wao watasema: Kwani? Tunaapa kwa Mola Mlezi wetu ni kweli. Yeye Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya vile mlivyokuwa mnakataa”.

Maana: Kutokana na kule kuyakadhibisha kwenu, basi leo onjeni adhabu yake.

أَفَسِحْرٌ هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تُبْصِرُونَ ﴿٣١﴾

"Je! Huu ni uchawi, au hamuoni tu?"

قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِلِقَاءِ اللَّهِ ^ط حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً قَالُوا يَنْحَسِرْتَنَا
عَلَىٰ مَا فَرَّطْنَا فِيهَا وَهُمْ يَحْمِلُونَ أَوْزَارَهُمْ عَلَىٰ ظُهُورِهِمْ ^ع أَلَا سَاءَ مَا يَزِرُونَ ﴿٣٢﴾
وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَعِبٌ وَلَهُوَ ^ط وَلِلدَّارِ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِلَّذِينَ يُتَّقُونَ ^ط أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٣٣﴾

31. Hakika wamekhasirika waliokanusha kukutana na Mwenyezi Mungu, mpaka ilipowajia Saa kwa ghafla, wakasema: Ole wetu kwa tuliyo yapuuza! Nao watabeba mizigo yao juu ya migongo yao. Ni maovu hayo wanayoyabeba.

32. Na maisha ya dunia si chochote ila ni mchezo na pumbao tu. Na hakika nyumba ya Akhera ni bora zaidi kwa wanaomcha Mungu. Basi, je, hamtii akilini?"

Allah تعالى Anaeleza majuto ya makafiri watakapokabliana Naye, na kukata kwao tamaa mara Saa itakapowafikia kwa ghafla, pamoja na huzuni zao kwa kupuuza kwao amali njema na kwa maovu yao. Kwa ajili hii, Alisema:

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً قَالُوا يَنْحَسِرْتَنَا عَلَىٰ مَا فَرَّطْنَا فِيهَا

"...mpaka ilipowajia Saa kwa ghafla, wakasema: Ole wetu kwa tuliyo yapuuza!"

Makusudio ya neno "...tuliyo yapuuza" Kiwakilishi hapa chaweza kurejeshwa katika maisha ya duniani, na juu ya amali na mambo ya Akhera. Na Kauli ya Allah تعالى:

وَهُمْ يَحْمِلُونَ أَوْزَارَهُمْ عَلَىٰ ظُهُورِهِمْ ^ع أَلَا سَاءَ مَا يَزِرُونَ

"Nao watabeba mizigo yao juu ya migongo yao. Ni maovu hayo wanayoyabeba".

Amesema Asbat kuwa As-Suddi alisema, "Mtu dhalimu akiingia tu kaburini kwake, hujiwa na mtu mwenye sura mbaya, mweusi mwenye kunuka vibaya

akiwa amevaa nguo chafu, na ataingia kaburini pamoja naye. Akimuona atasema, "Uso wako ni mbaya mno". Atajibu, "Hata amali zako zilikuwa mbaya". Atasema tena, "Unanuka vibaya sana". Atamjibu, "Amali zako nazo zilikuwa zinanuka vibaya". Atamuambia, "Nguo zako ni chafu mno". Atamjibu, "Amali zako zilikuwa chafu". Atamsaili, "Wewe ni nani?" Atamjibu, "Amali Zako". Atakuwa pamoja naye kaburini mwake, na atakapofufuliwa katika Siku ya Kiyama atamuambia, "Mimi nilikuwa duniani nikikuchukua katika vitamu na vya matamano, sasa wewe, utanibeba leo". Kisha Atapanda mgongoni mwake, na atamswaga mpaka amuingize Motoni. Kwa hivyo, Allah تعالى Amesema;

وَهُمْ يَحْمِلُونَ أَوْزَارَهُمْ عَلَى ظُهُورِهِمْ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَزُرُونَ

"Na watabeba mizigo yao juu ya migongo yao. Ni maovu hayo wanayoyabeba"¹.

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَعِبٌ وَلَهْوٌ ۗ

"Na maisha ya dunia si chochote ila ni mchezo na pumbao tu".

Maana: Sehemu kubwa sana ni mambo hayo;

وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِّلَّذِينَ يَتَّقُونَ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ

"Na hakika nyumba ya Akhera ni bora zaidi kwa wanao mcha Mungu. Basi, je, hamtii akilini?"

قَدْ نَعْلَمُ إِنَّهُمْ لَيَخُزْنُكَ الَّذِي يَقُولُونَ فَإِنَّهُمْ لَا يَكْذِبُونَكَ وَلَكِنَّ الظَّالِمِينَ بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبَرُوا عَلَىٰ مَا كُذِّبُوا وَأَوْدُوا حَتَّىٰ أَتَتْهُمْ نَصْرُنَا وَلَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۗ وَلَقَدْ جَاءَكَ مِن نَّبِيِّ الْمُرْسَلِينَ ﴿٦٧﴾ وَإِن كَانَ كِبَرَ عَلَيْكَ إِعْرَاضُهُمْ فَإِنِ اسْتَطَعْتَ أَن تَبْتَغِي نَفَقًا فِي الْأَرْضِ أَوْ سُلْمًا فِي السَّمَاءِ فَتَأْتِيَهُمْ بِآيَةٍ ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَمَعَهُمْ عَلَى الْهَدْيِ ۗ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٦٨﴾ * إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ يَسْمَعُونَ ۗ وَالْمَوْتَىٰ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ ثُمَّ إِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٦٩﴾

¹ At-Tabari 11:328.

33. Tunajua ya kwamba yanakuhuzunisha wanayoyasema. Basi hakika wao hawakukanushi wewe, lakini hao madhalimu wanazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu.

34. Na hakika walikanushwa Mitume wa kabla yako. Nao wakavumilia kule kukanushwa, na kuudhiwa, mpaka ilipowafikia nusura yetu. Na hapana wa kubadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu. Na bila ya shaka zimekuja baadhi ya khabari za Mitume hao.

35. Na ikiwa ni makubwa kwako huku kukataa kwao, basi kama unaweza kutafuta njia ya chini kwa chini ya ardhi, au ngazi kwendea mbinguni ili uwalettee Ishara – Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angependa Angeliwakusanya kwenye uwongofu. Basi usiwe miongoni mwa wasiojua.

36. Hakika wanaokubali ni wale wanaosikia. Na ama wafu Mwenyezi Mungu Atawafufua, na kisha Kwake Yeye ndio watarejeshwa.

Kumfariji Mtume ﷻ.

Allah تعالى Anamfariji Mtume ﷻ kutokana na huzuni yake juu ya watu kumkadhibisha na kumuasi.

قَدْ نَعْلَمُ إِنَّهُ لَيَحْزُنُكَ الَّذِي يَقُولُونَ^ط

“Tunajua ya kwamba yanakuhuzunisha wanayoyasema”.

Ikiwa na maana kuwa, ‘Tunajua kuhusu kukukadhibisha kwao na kuwahuzunikia na kuwasitikia kwako.’

Ni kama katika Kauli Yake nyingine,

فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسْرَاتٍ^ع

“Basi nafsi yako isijihiliki kwa kuwasikitikia”. (35:8)

Allah تعالى Amesema tena katika Aya nyingine;

لَعَلَّكَ بَخِيعٌ نَفْسِكَ أَلَّا يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٣٦﴾

“Huenda labda ukajikera nafsi yako kwa kuwa hawawi Waumini”.

(26:3) na;

فَلَعَلَّكَ بَخِيعٌ نَفْسِكَ عَلَىٰ ءَاثَرِهِمْ إِن لَّمْ يُؤْمِنُوا بِهَذَا الْحَدِيثِ أَسَفًا ﴿٦﴾

“Huenda ukajihiliki nafsi yako kwa ajili yao, kuwasikitikia kwa kuwa hawayaamini mazungumzo haya!” (18:6)

Kauli ya Allah;

فَأَيُّهُمْ لَا يُكَذِّبُونَكَ وَلَٰكِنَّ الظَّالِمِينَ بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ

“Basi hakika wao hawakukanushi wewe, lakini hao madhalimu wanazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu”.

Maana: Si wewe wanayekuzushia uongo, kwa jinsi jambo lenyewe lilivyo.

وَلَٰكِنَّ الظَّالِمِينَ بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ

“...lakini hao madhalimu wanazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu”.

Ni ukweli ndio wanaoukana, na wanauzuia kwa vifua vyao. Muhammad bin Is-haq ametaja kuwa Az-Zuhri alikizungumzia kisa cha Abu Jahl, Abu Sufyan Sakhr bin Harb na Akhnas bin Shariq alipokuja kumsikiliza Mtume ﷺ akisoma Qur'an usiku. Lakini kila mmoja wao hakutambua habari ya kuwepo kwa mwenzake yeyote. Wakaisikiliza hadi asubuhi, kisha wakaondoka wote wakakutana njiani wakiwa wanarejea majumbani kwao. Kila mmoja wao akamwambia mwenzake; “Ni nini kilichokuleta?” akamtajia yaliyomleta, halafu wakaagana kwamba wasirudie tena kufanya hivyo kuchelea vijana wa Kikuraishi wasije wakawang'amua jambo lao hili na kuamua kuwaiga. Ulipowadia usiku wa siku iliyofuata, kila mmoja wao alikuja kwa kudhani kwamba wenzake wawili si wenye kuja, kutokana na ahadi waliyowekeana. Asubuhi ilipowadia wakakutana tena njiani. Wakalaumiana, halafu wakaahidiana tena juu ya kutokurejea. Ulipoingia usiku wa siku ya tatu, walikuja tena. Asubuhi wakaapiana kama hapo mwanzoni, kisha kila mmoja akaondoka kivyake. Asubuhi hiyo, Akhnasi bin Shariq alichukua fimbo yake, akamuendea Abu Sufyan bin Harb nyumbani kwake, akamuambia, “Ewe Abu Handhwalah! Niambie maoni yako kuhusu uliyoyasikia kutoka kwa

Muhammad". Akajibu, "Ewe Abu Tha'labah! Wallahi! Nimeyasikia maneno ninayoyajua, na ninazijua athari zake. Pia nimeyasikia mambo ambayo siyajui wala sizijui athari zake." Al-Akhnas akasema, "Nami vivyo hivyo, kwa jina la huyo uliyemuapia". Kisha akatoka kwake na akaenda kwa Abu Jahl, akaingia nyumbani kwake akasema, "Ewe Abul-Hakam! Una rai gani kuhusu yale uliyoyasikia kutoka kwa Muhammad? Ulisikia nini?" Akasema, "Sisi na Banu 'Abd Manaf (ukoo wa Mtume) tulishindana, kwa hiyo walilisha pale tulipolisha, wakachukua tulipochukua na wakatoa tulipotoa. Mpaka wakachukua tulipochukua na wakatoa tulipotoa. Mpaka tulipokaribiana mno, tukawa kama farasi wawili walio katika mashindano ya kwenda mbio, wakasema, "Sisi tunaye Mtume atokanaye na sisi, ambaye anapata wahyi kutoka mbinguni". Basi ni kwa namna gani tutaweza kuwashinda katika hili? Wallahi! Hatutamuamini bilikuli! Wala hatutamsadiki". Hapa ndipo Al-Akhnas aliposimama na kumuacha."¹. Kauli Yake *تعالى*;

وَلَقَدْ كَذَّبْتَ رَسُولٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبْرُوا عَلَىٰ مَا كَذَّبُوا وَأَوْدُوا حَتَّىٰ أَنَّهُمْ نَصَرُنَا

"Na hakika walikanushwa Mitume wa kabla yako. Nao wakavumilia kule kukanushwa, na kuudhiwa, mpaka ilipowafikia Nusura Yetu".

Hii inamfariji Mtume ﷺ kutokana na baadhi ya watu wake waliomkadhibisha. Pia Allah *تعالى* Anamuamuru awe na subira kama vile Mitume wetu wakuu walivyofanya. Tena Alimuahidi ushindi kama walivyokuwa washindi (Mitume hao) na wakawa na mwisho mwema, baada ya kukadhibishwa na udhia mkubwa uliofanywa na kaumu zao. Baadaye wakapata ushindi duniani, kama ulivyo ushindi wao huko Akhera. Ndipo Aliposema;

وَلَا مَبْدَلَ لِكَلِمَاتِ اللَّهِ

"Na hapana wa kubadilisha Maneno ya Mwenyezi Mungu".

Inahusu hukumu Yake ya uwepo ushindi kwa waja Wake Waumini, duniani na Akhera.

Ni sawa na Alivyosema;

¹ Ibn Hisham 1:337 kutokana na mlolongo wa wasimulizi mbalimbali. Hadithi hii si *Sahih*.

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَلِمَتُنَا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿٢٧﴾ إِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنْصُورُونَ ﴿٢٨﴾ وَإِنْ جُنَدَنَا لَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٢٩﴾

“Na bila ya shaka Neno Letu lilikwishatangulia kwa waja Wetu waliotumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakaonusuriwa. Na kwamba jeshi Letu ndilo litakaloshinda”.

Allah تعالیٰ Amesema;

كَتَبَ اللَّهُ لَأَعْلَبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ۚ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٨﴾

“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda”. (58:21)

Allah تعالیٰ Amesema;

وَلَقَدْ جَاءَكَ مِنْ نَبِيِّنَا الْمُرْسَلِينَ ۚ

“Na bila ya shaka zimekuja baadhi ya khabari za Mitume hao”.

Ni khabari kuhusu namna walivyofanywa kuwa washindi na jinsi walivyosaidiwa na kuwashinda wale waliowakadhibisha wao kutoka katika kaumu zao.

Kwa hivyo, una mfano mzuri kutoka kwao. Halafu Allah تعالیٰ Akasema;

وَإِنْ كَانَ كَبُرَ عَلَيْكَ إِعْرَاضُهُمْ

“Na ikiwa ni makubwa kwako huku kukataa kwao”.

Ina maana, ikiwa imekuwia vigumu kuvumilia jambo la kukukataa kwao.

فَإِنْ أَسْتَطَعْتَ أَنْ تَبْتَغِيَ نَفَقًا فِي الْأَرْضِ أَوْ سُلَّمًا فِي السَّمَاءِ

“...basi kama unaweza kutafuta njia ya chini kwa chini ya ardhi, au ngazi kuendea mbinguni”.

Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: Neno *An-Nafaq* limetumika kumaanisha njia inayopita nchi kavu au majini katika uso wa dunia. Katika ayah, linamaanisha, “Ikiwa unaweza kuipata njia, **“...ili uwalettee Ishara”.** Au ujifanyie ngazi kwa ajili ya kukwea mpaka mbinguni, na

uwalettee ishara, iliyo bora kuliko nilizowaletea wao, basi fanya hivyo"¹. Na hivi ndivyo alivyosema Qatadah, As-Suddi na wengine². Kauli ya Allah تعالى;

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَمَعَهُمْ عَلَى الْهُدَىٰ ۚ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْجَاهِلِينَ

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angependa Angeliwakusanya kwenye uwongofu. Basi usiwe miongoni mwa wasiojua”

Ni kama Kauli Yake;

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي الْأَرْضِ كُلَّهُمْ جَمِيعًا

“Angelitaka Mola wako Mlezi wangeliamini wote waliomo katika ardhi”. (10:99)

Ali bin Abu Twalhah alieleza kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَمَعَهُمْ عَلَى الْهُدَىٰ ۚ

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angependa Angeliwakusanya kwenye uwongofu”³.

Akasema, “Kwa hakika, Mtume ﷺ alikuwa na hamu kubwa watu wote wawe Waumini na wamfuata yeye katika uwongofu. Allah تعالى Akamjulisha kuwa ni wale tu ambao waliandikiwa kuwa wema katika *Dhikr* (kumbu kumbu) ya kwanza watakaoamini”. Na Kauli Yake;

إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ يَسْمَعُونَ

“Hakika wanaokubali ni wale wanaosikia”.

Maana yake, kwa hakika wataitikia wito wako ewe Muhammad ﷺ wenye kuyasikia maneno, kuyafahamu na kuyaelewa. Katika Ayah nyingine, Allah تعالى Amesema;

لِيُنذِرَ مَنْ كَانَ حَيًّا وَيَحِقِّ الْقَوْلُ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٣٦﴾

“Ili imuonye aliye hai, na neno litimie juu ya makafiri.” (36:40)

¹ At-Tabari 11:338.

² At-Tabari 11:338.

³ At-Tabari 11:340. Maana yake, wale aliohukumu kwamba wawe Waumini.

Na Kauli Yake;

وَالْمَوْتَىٰ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ ثُمَّ إِلَيْهِ يُرْجَعُونَ

“Na ama wafu Mwenyezi Mungu Atawafua, na kisha Kwake Yeye ndio watarejeshwa”.

Inamaanisha makafiri, kwa sababu nyoyo zao zimekufa, basi Allah تعالى Akawashabihisha na miili iliyokufa kwa Kusema;

وَالْمَوْتَىٰ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ ثُمَّ إِلَيْهِ يُرْجَعُونَ

“Na ama wafu Mwenyezi Mungu Atawafua, na kisha Kwake Yeye ndio watarejeshwa”.

Hii ni katika njia ya kuwakatisha tamaa na kuwadhalilisha.

* * *

وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِنْ رَبِّهِ ۚ
 قُلْ إِنَّ اللَّهَ قَادِرٌ عَلَىٰ أَنْ يُنَزِّلَ
 آيَةً وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٧﴾
 وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ
 أَمْثَالُكُمْ ۚ مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ ۚ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ
 يُحْشَرُونَ ﴿٣٨﴾ وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا صُمٌّ وَبُكْمٌ فِي
 الظُّلُمَاتِ ۚ مَنْ يَشِئِ اللَّهُ يَضِلَّهُ وَمَنْ يَشَأْ يَجْعَلْهُ عَلَىٰ
 صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٣٩﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَنْتُمْ عَدَابِ
 اللَّهِ أَوْ أَنْتُمْ السَّاعَةُ أَعْيَرَ اللَّهُ تَدْعُونَ إِنْ كُنْتُمْ
 صَادِقِينَ ﴿٤٠﴾ بَلْ إِيَّاهُ تَدْعُونَ فَيَكْشِفُ مَا تَدْعُونَ
 إِلَيْهِ إِنْ شَاءَ وَتَنْسَوْنَ مَا تُشْرِكُونَ ﴿٤١﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا
 إِلَىٰ أُمَمٍ مِنْ قَبْلِكَ فَأَخَذْنَاهُمْ بِالْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ لَعَلَّهُمْ
 يَتَضَرَّعُونَ ﴿٤٢﴾ فَلَوْلَا إِذْ جَاءَهُمْ بَأْسُنَا تَضَرَّعُوا وَلَٰكِنْ
 قَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ مَا كَانُوا
 يَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾ فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ فَتَحْنَا
 عَلَيْهِمْ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا
 أَخَذْنَاهُمْ بَغْتَةً فَإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ ﴿٤٤﴾ فَقَطَّعَ دَابِرَ
 الْقَوْمِ الَّذِينَ ظَلَمُوا ۚ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٥﴾

وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِنْ رَبِّهِ ۚ
 قُلْ إِنَّ اللَّهَ قَادِرٌ عَلَىٰ أَنْ يُنَزِّلَ
 آيَةً وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ
 ﴿٣٧﴾ وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا
 طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُمْ ۚ
 مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ ۚ ثُمَّ
 إِلَىٰ رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ ﴿٣٨﴾ وَالَّذِينَ
 كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا صُمٌّ وَبُكْمٌ فِي
 الظُّلُمَاتِ ۚ مَنْ يَشِئِ اللَّهُ يَضِلَّهُ وَمَنْ
 يَشَأْ يَجْعَلْهُ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٣٩﴾

37. Na wamesema: Kwa nini Hakuteremshiwa muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Sema: Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa Kuteremsha muujiza. Lakini wengi wao hawajui.

38. Na hapana mnyama katika ardhi, wala ndege anayeruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi. Hatukupuza

Kitabuni kitu chochote. Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa.

39. Na waliokanusha Ishara Zetu ni Viziwi na mabubu waliomo gizani. Mwenyezi Mungu Humuachia kupotea Amtakaye, na Humuweka katika njia iliyonyooka Amtakaye”.

Washirikina Wanataka Muujiza.

Allah تعالى Anasema washirikina walikuwa wakisema; “Kwa nini (Muhammad) hatuletei Aya kutoka kwa Mola wake?” Wakimaanisha, muujiza kwa mujibu wa utashi wao. Wakati mwingine waliidiriki kusema;

لَنْ نُؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنْبُوعًا

“Hatutakuamini mpaka ututimbulie chemchem katika ardhi hii”.
(17:90)

قُلْ إِنَّ اللَّهَ قَادِرٌ عَلَىٰ أَنْ يُنَزِّلَ آيَةً وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

“Sema: Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa Kuteremsha muujiza. Lakini wengi wao hawajui”.

Hakika! Allah تعالى ni Muweza juu ya hilo, lakini kwa Hikima Zake Analiakhirisha, kwa kuwa Angelipeleka Aya kama walivyotaka Halafu wakaendelea kutokuamini, Angeliwaharakishia adhabu kama Alivyofanya kwa umma kadha zilizotangulia. Ni sawa na Alivyosema katika sehemu nyingine,

وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا الْأَوْلُونَ^٤ وَءَاتَيْنَا ثُمُودَ النَّاقَةَ مُبْصِرَةً فَظَلَمُوا بِهَا^٥ وَمَا نُرْسِلُ بِالْآيَاتِ إِلَّا تَخْوِيفًا ﴿١٧﴾

“Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha. Na Tuliwapa Wathamudi ngamia jike kuwa ni Ishara iliyo dhahiri, lakini walidhulumu kwayo. Nasi Hatupeleki ishara ila kwa ajili ya kuhadharisha”. (17:59)

Allah تعالى Anasema,

إِنْ دُشِيَ نُنَزِّلْ عَلَيْهِم مِّنَ السَّمَاءِ آيَةً فَظَلَّتْ أَعْنَاقُهُمْ لَهَا خَاضِعِينَ ﴿٢٦﴾

“Tungependa Tungeliwateremshia kutoka mbinguni Ishara zikanyenyekesha shingo zao”. (26:4)

Maana ya Umam.

Kauli ya Allah تعالى;

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُمْ

“Na hapana kiumbe katika ardhi, wala ndege anayeruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi”.

Mujahid amesema, “Maana yake, spishi zenye majina tofauti”¹. Qatadah amesema, “Ndege ni *Ummah*, wanadamu ni *Ummah* na majini ni *Ummah*”². As-Suddi amesema;

إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُمْ

“...ila ni umma kama nyinyi”.

Ila ni viumbe kama nyinyi³. Na Kauli Yake;

مَا فَرَطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ

“Hatukupuza Kitabuni kitu chochote”. Maana: Elimu ya vitu vyote Anayo Allah تعالى, na kamwe Haghafiliki na kiumbe wake yeyote wala riziki na mambo yao, iwe ni bara au baharini. Ni kama Kauli Yake;

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي كِتَابِ

مُبِينٍ ﴿٦﴾

“Na hakuna kiumbe yeyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye Anajua makao yake na mapito yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha”. (11:6)

Maana: Kuna taarifa ya majini, idadi, harakati zao na kutulia kwao. Pia amesema;

وَكَايْنٍ مِّنْ دَابَّةٍ لَا تَحْمِلُ رِزْقَهَا اللَّهُ يَرْزُقُهَا وَإِيَّاكُمْ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦﴾

“Na viumbe wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Mwenyezi Mungu Anawaruzuku hao na nyinyi pia. Na Yeye Ndiye Mwenye kusikia Mwenye Kujua”. (29:60)

¹ At-Tabari 11:345.

² At-Tabari 11:345.

³ At-Tabari 11:345.

Ibn Abu Hatim ameeleza kwamba bin 'Abbas رضي الله عنهما alieleza Kauli hiyo,

ثُمَّ إِلَى رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ

"Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa".

"Kifo kimewakusanya"¹. Imesemwa pia kwamba kukusanywa kwao ni katika Siku ya Ufufuo kwa sababu ya Kauli Yake nyingine;

وَإِذَا أَلْوَحُوشُ حُشِرَتْ

"Na wanyama wa mwituni wakakusanywa". (81:5)

Abdur-Razzaq amemnukuu Ibn 'Abas رضي الله عنهما kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

إِلَّا أُمَّةٌ أَمْثَالِكُمْ ۗ مَا فَرَقْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ ۚ ثُمَّ إِلَى رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ

"...ila ni umma kama nyinyi. Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa".

Alisema, "Viumbe wote watakusanywa katika Siku ya Kiyama, wanyama, ndege na kila kitu. Uadilifu wa Allah تعالى utakuwa wa hali ya juu mno katika siku hiyo, kiasi kondoo asiye na pembe atachukua haki yake kutoka kwa kondoo mwenye pembe aliyemjeruhi hapa duniani. Kisha Allah تعالى Atasema, "Kuweni mchanga" hapa ndipo kafiri atakaposema;

يَلِيَّتِي كُنْتُ تُرَابًا

"Laiti ningelikuwa udongo!" (78:40)²

Na hii imeelezwa na Mtume ﷺ katika Hadith kuhusu baragumu.

Makafiri ni Kama Viziwi na Mabubu Walio Kizani.

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا صُمُّوا وَنُكِّمُوا فِي الظُّلُمَاتِ

"Na waliokanusha Ishara Zetu ni Viziwi na mabubu waliomo gizani".

Kwa sababu ya ujinga wao, uhaba wa elimu na ukosefu wa uelewa ni kama kiziwi, ambaye hasikii. Pia ni bubu, ambaye hasemi. Pamoja na hayo yuko

¹ Ibn Abu Hatim 4:1286.

² At-Tabari 11:347.

kizani, haoni. Mtu kama huyu ataongokaje mpaka aweze kuipata njia au kujitoa katika hali hiyo. Allah تعالی Alisema katika Aya nyingine;

مَثَلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِي اسْتَوْقَدَ نَارًا فَلَمَّا أَضَاءَتْ مَا حَوْلَهُ ذَهَبَ اللَّهُ بِنُورِهِمْ وَتَرَكَهُمْ فِي ظُلْمَةٍ لَا يُبْصِرُونَ ﴿٦٧﴾ صُمُّ بَكْمٌ عُمَىٰ فَهُمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿٦٨﴾

“Mfano wao ni kama mfano wa aliyekoka moto, na ulipotanda mwangaza wake kote kote Mwenyezi Mungu Aliiondoa nuru yao na Akawaacha katika giza, hawaoni. Viziwi, mabubu, vipofu kwa hivyo hawatarejea”. (2:17-18)

Na Allah تعالی Anasema;

أَوْ كَظُلْمَتٍ فِي نَحْرِ لُجِّيٍّ يَغْشَاهُ مَوْجٌ مِّنْ فَوْقِهِ مَوْجٌ مِّنْ فَوْقِهِ سَحَابٌ ۗ ظَلَمْتُمْ بَعْضُهَا فَوْقَ بَعْضٍ إِذَا أَخْرَجَ يَدُهُ لَمْ يَكَدْ يَرَاهَا ۗ وَمَنْ لَّمْ يَجْعَلِ اللَّهُ لَهُ نُورًا فَمَا لَهُ مِن نُّورٍ ﴿٤٠﴾

“Au ni kama giza katika bahari kuu, iliyofunikwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu. Giza juu ya giza. Akiutoa mtu mkono wake ni vigumu kuuona. Na ambaye Mwenyezi Mungu Hakumjaalia kuwa na nuru hawi na nuru”. (24:40)

Kwa ajili hiyo, Allah تعالی Anasema;

مَنْ يَشَأِ اللَّهُ يُضِلَّهُ وَمَنْ يَشَأْ يُجْعَلْهُ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٦٩﴾

“Mwenyezi Mungu Humuachia kupotea Amtakaye, na Humuweka katika njia iliyonyooka Amtakaye”.

Kwa kuwa Yeye Hufanya vile Atakavyo kwa viumbe Wake.

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَتَيْتُمْ عَذَابَ اللَّهِ أَوْ أَتَيْتُمْ السَّاعَةَ أُغَيْرَ اللَّهُ تَدْعُونَ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧٠﴾ بَلْ إِيَّاهُ تَدْعُونَ فَيَكْشِفُ مَا تَدْعُونَ إِلَيْهِ إِنْ شَاءَ وَتَنْسَوْنَ مَا تُشْرِكُونَ ﴿٧١﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ فَأَخَذْنَاهُم بِالْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ لَعَلَّهُمْ يَتَضَرَّعُونَ ﴿٧٢﴾ فَلَوْلَا إِذْ جَاءَهُمْ بَأْسُنَا تَضَرَّعُوا وَلَكِنْ قَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٧٣﴾

﴿٤٠﴾ فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ فَتَحْنَا عَلَيْهِمُ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا أَخَذْنَاهُم بَغْتَةً فَإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ ﴿٤١﴾ فَقَطَّعَ دَابِرَ الْقَوْمِ الَّذِينَ ظَلَمُوا ۗ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٢﴾

40. Sema: Mwaonaje ikikujieni adhabu ya Mwenyezi Mungu, au ikakufikieni hiyo Saa – mtamuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi ni wa kweli?

41. Bali Yeye Ndiye mtakayemuomba, naye Atakuondoleeni mnachomuomba Akipenda. Na mtasahau hao mnaowafanya washirika wake.

42. Na kwa yakini Tulipeleka Mitume kwa kaumu zilizokuwa kabla yako, kisha Tukazitia katika dhiki na mashaka ili zipate kunyenyekea.

43. Kwa nini wasinyenyekee ilipowafikia adhabu yetu? Lakini nyoyo zao zilikuwa ngumu, na Shetani akawapambia waliyokuwa wakiyafanya.

44. Basi waliposahahu waliokumbushwa Tuliwafungulia milango ya kila kitu. Mpaka walipofurahia yale waliyopewa Tuliwashika kwa ghafla, na mara wakawa wenye kukata tamaa.

45. Ikakatwa mizizi ya watu waliodhulumu – na wa Kuhimidiwa ni Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote”.

Kusimamisha Hoja kwa Washirikina Kumuomba Kwao Allah تعالیٰ Peke Yake Wakati wa Adhabu.

Allah تعالیٰ Anaeleza Yeye Hufanya Ayatakayo kwa viumbe Wake na hakuna atakayethubu kugomea hukumu Yake wala kuiondoa kutoka kwa waja Wake. Bali Yeye Yu Mpweke, Hana mshirika, Ambaye Hujibu dua ya yeyote Amtakaye anayemuomba. Na kwa ajili hiyo Alisema;

قُلْ أَرَأَيْتَكُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُ اللَّهِ أَوْ أَتَتْكُمُ السَّاعَةُ أَغَيْرَ اللَّهِ تَدْعُونَ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

“Sema: Mnaonaje ikikujieni adhabu ya Mwenyezi Mungu, au ikakufikieni hiyo Saa – mtamuomba asiye kuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi ni wakweli?”

Maana yake, (nyinyi makafiri) hamtamuita mwingine kwa ajili ya kuyaondosha hayo, isipokuwa Allah تعالى na kwa hivyo Akaongeza kwa Kusema;

إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

"...ikiwa nyinyi ni wakweli?" Maana: Kwa kumshirikisha Yeye na miungu ya uwongo.

بَلْ إِيَّاهُ تَدْعُونَ فَيَكْشِفُ مَا تَدْعُونَ إِلَيْهِ إِنْ شَاءَ وَتَنْسَوْنَ مَا تُشْرِكُونَ ﴿٦٦﴾

"Bali Yeye Ndiye mtakayemuomba, naye Atakuondoleeni mnachomuomba Akipenda. Na mtasahau hao mnaowafanya washirika wake".

Katika nyakati za dharura, huwa mnamuomba Allah تعالى na mnayasahau masanamu na miungu wa uwongo. Ni kama katika Kauli Yake nyingine;

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِيَّاهُ

"Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu". (17:67)

Na Kauli Yake;

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ فَأَخَذْنَاهُم بِالْبَأْسَاءِ

"Na kwa yakini Tulipeleka Mitume kwa kaumu zilizokuwa kabla yako, kisha Tukazitia katika dhiki".

Maana: Ufakiri na dhiki ya kimaisha.

وَالضَّرَّاءِ

"...na mashaka". Maradhi ya namna mbalimbali na maumivu.

لَعَلَّهُمْ يَتَضَرَّعُونَ

"...ili Zipate kunyenyekea". Maana yake: Wanamuomba Allah تعالى na wanamnyenyekea. Allah تعالى Amesema;

فَلَوْلَا إِذْ جَاءَهُمْ بَأْسُنَا تَضَرَّعُوا

"Kwa nini wasinyenyekee ilipowafikia adhabu Yetu?"

Ikimaanisha kwamba: kwa nini hawaamini na kutunyenyekea Sisi pindi Tunapowajaribu kwa kuwapelekea maafa.

وَلَيْكِن قَسَتْ قُلُوبُهُمْ

“Lakini nyoyo zao zilikuwa ngumu”.

Maana: Hazikulainika wala kunyenyekea.

وَزَيْنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“...na Shetani akawapambia waliyokuwa wakiyafanya”.

Miongoni mwa mambo ya *ushirikina*, ufidhuli na maasi.

فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ

“Basi waliposahahu waliokumbushwa”.

Waliyakataa, wakayapuuzaa na wakayageuzia migongo.

فَتَحْنَا عَلَيْهِمُ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ

“Tuliwafungulia milango ya kila kitu”.

Makusudio ni, “Tuliwafungulia milango ya riziki katika kila walichokhitari. Na huku ni kuwavuta kidogo kidogo na kuwapa muda”. Tunajilinda kwa Allah تعالی dhidi ya mwisho huo. Ndiyo sababu Allah تعالی Alisema;

حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا

“Mpaka walipofurahia yale waliyopewa”.

Kama vile, mali, watoto na riziki.

أَخَذْنَاهُمْ بِغَتَّةٍ فَإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ

“...Tuliwashika kwa ghafla, na mara wakawa wenye kukata tamaa”..”

Maana yake: Bila ya kutarajia. Wakakosa matumaini ya kupata kheri yoyote. Al-Walabi amesema Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Maana ya neno *Mublis*, ni mwenye kukata tamaa”. Na Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالی alisema, “Aliyekunjuliwa riziki na Allah تعالی halafu asione huo ni mtihani aliopewa, basi ni mkosefu wa busara na yule aliyezuiwa halafu asione kwamba huo ni mtihani aliopewa, basi ni mkosefu wa busara. Kisha akasoma Aya;

فَلَمَّا دَسُّوا مَا دُكِّرُوا بِهِ فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا
أَخَذْنَاهُمْ بِغَتَّةٍ فَإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ ﴿٤٥﴾

“Basi waliposahahu waliokumbushwa Tuliwafungulia milango ya kila kitu. Mpaka walipofurahia yale waliyopewa Tuliwashika kwa ghafla, na mara wakawa wenye kukata tamaa”.

Halafu akasema, “Naapa kwa Jina la Mola wa Al-Ka’bah, Allah تعالى Aliwatia mchanga wa macho, watu walipewa haja zao kisha wakaadhibiwa”. Imepokewa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى (Ad-Durr Al-Manthur 3:270 na Ibn Abu Hatim 4:1291).

* * *

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَخَذَ اللَّهُ سَمْعَكُمْ
 وَأَبْصَرَكُمْ وَخَتَمَ عَلَى قُلُوبِكُمْ
 مِّنْ إِلَهِ غَيْرِ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِهِ
 أَنْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ
 الْآيَاتِ ثُمَّ هُمْ يَصْدِفُونَ ﴿٤٦﴾
 قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَتَيْتُمْ
 عَذَابَ اللَّهِ بَغْتَةً أَوْ جَهْرَةً
 هَلْ يُهْلِكُ إِلَّا الْقَوْمَ
 الظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾ وَمَا تُرْسِلُ
 الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ
 وَمُنذِرِينَ ۗ فَمَنْ ءَامَنَ وَأَصْلَحَ
 فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ
 يَحْزَنُونَ ﴿٤٨﴾ وَالَّذِينَ
 كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا يَمَسُّهُمُ
 الْعَذَابُ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٤٩﴾
 قُلْ لَا أَقُولُ لَكُمْ عِندِي
 خَزَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ
 الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ لَكُمْ إِنِّي
 مَلَكٌ ۗ إِن آتَيْتُ إِلَّا مَا
 يُوحَىٰ إِلَيَّ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي
 الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ ۗ أَفَلَا
 تَتَفَكَّرُونَ ﴿٥٠﴾ وَأَنْذِرْ
 بِهِ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَنْ
 تُخْشَوْا إِلَىٰ رَبِّهِمْ ۗ لَيْسَ
 لَهُمْ مِنْ دُونِهِ إِلَهٌ ۗ وَلَا
 شَافِعٌ لَهُمْ ۗ يُتَّقُونَ ﴿٥١﴾
 وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ
 رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ
 يُرِيدُونَ وَجْهَهُ ۗ مَا عَلَيْكَ
 مِنْ حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ وَمَا
 مِنْ حِسَابِكَ عَلَيْهِمْ مِنْ شَيْءٍ
 فَتَطْرُدَهُمْ فَتَكُونَ مِنَ
 الظَّالِمِينَ ﴿٥٢﴾ وَكَذَلِكَ
 فَتَنَّا بَعْضَهُم بِبَعْضٍ
 لِّيَقُولُوا أَهْتُوا لِمَنْ ۗ أَلَّهِ
 اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنْ بَيْنِنَا ۗ أَلَيْسَ
 اللَّهُ بِأَعْلَمَ بِالشَّاكِرِينَ ﴿٥٣﴾
 وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ
 بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلِّمْتُ عَلَيْكُمْ
 ۗ كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ
 الرَّحْمَةَ ۗ أَنَّهُ مِّنْ عَمَلٍ
 مِنْكُمْ سُوءًا يَجْهَلُونَ ثُمَّ
 تَابَ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَأَصْلَحَ
 فَأَنَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٥٤﴾

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَخَذَ اللَّهُ سَمْعَكُمْ
 وَأَبْصَرَكُمْ وَخَتَمَ عَلَى قُلُوبِكُمْ مِّنْ إِلَهِ
 غَيْرِ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِهِ أَنْظُرْ كَيْفَ
 نُصَرِّفُ الْآيَاتِ ثُمَّ هُمْ يَصْدِفُونَ ﴿٤٦﴾
 قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَتَيْتُمْ
 عَذَابَ اللَّهِ بَغْتَةً أَوْ جَهْرَةً هَلْ
 يُهْلِكُ إِلَّا الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾
 وَمَا تُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ
 وَمُنذِرِينَ ۗ فَمَنْ ءَامَنَ وَأَصْلَحَ فَلَا
 خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٤٨﴾
 وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا يَمَسُّهُمُ
 الْعَذَابُ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٤٩﴾

46. Sema: Mnaonaje
 Mwenyezi Mungu Aka-
 nyakua kusikia kwenu, na
 kuona kwenu, na Akazi-
 zibua nyoyo zenu, ni mungu
 gani Asiyekuwa Mwenyezi
 Mungu Atayekuleteni
 hayo tena? Angalia vipi
 Tunavyozieleza Ishara,
 kisha wao wanapuuza.

47. Sema: Mwaonaje,
 ikikufikieni adhabu ya
 Mwenyezi Mungu kwa

ghafila, au kwa dhahiri, je wataangamizwa isipokuwa walio-dhulumu?

48. Na hatuwatumi Mitume ila huwa ni wabashiri na waonyaji. Na wenye kuamini na wakatenda mema haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.

49. Na walio kanusha Ishara Zetu itawagusa adhabu kwa walivyokuwa wakipotoka”.

Allah تعالى Alimuambia Mjumbe Wake, Ewe Muhammad, Wanaambiwa hao mafedhuli wapingaji,

أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَخَذَ اللَّهُ سَمْعَكُمْ وَأَبْصَرَكُمْ

“Sema: Mwaonaje Mwenyezi Mungu Akanyakua kusikia kwenu, na kuona kwenu”.

Maana yake: Akavibwakua hivyo kutoka kwenu kama vile Alivyokupatieni. Katika aya nyingine, Alisema;

هُوَ الَّذِي أَذْشَأَكُمْ وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ

“Yeye Ndiye Aliyekuumbeni tangu mwanzo, na Akakupeni masikio na macho.”

Na inawezekana ikawa kunufaika na viungo hivyo ni kwa maana ya kisharia. Na kwa kuzingatia hilo Amesema,

وَحَتَمَ عَلَى قُلُوبِكُمْ

“...na Akatia muhuri nyoyoni mwenu”.

Katika Aya nyingine Amesema tena;

أَمْ يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ

“Au ni nani anayemiliki kusikia na kuona?” (10:31) Na,

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ

“Na Jueni kuwa Mwenyezi Mungu Huingia kati ya mtu na moyo wake”. (8:24) Na;

مَنْ إِلَهٌ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِهِ

“...ni mungu gani Asiyekuwa Mwenyezi Mungu Atayekuleteeni hayo tena?”

Maana: Je kuna mwingine asiyekuwa Allah تعالى Anayeweza kukurejesheni hivyo. Allah تعالى Akishakunyang'anyeni hayo, hakuna mwenye uwezo wa kukurudishieni isipokuwa Yeye tu.

أَنْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْأَبْتِ

“Angalia vipi Tunavyozieleza Ishara”.

Maana yake: Tunazibainisha, kuzifafanua na kuzitafsiri katika kuonesha kuwa hapana wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى, na kwamba wale wanaowaabudu kinyume na Yeye ni wa uwongo na wa upotevu.

ثُمَّ هُمْ يَصْدِفُونَ

“...kisha wao wanapuuza”.

Maana yake: Kisha wao baada ya ishara hizi wanapuuza. Pia ina Maana: Wanaipa mgongo haki na wanawazuia watu kumfuata. Na Kauli ya Allah;

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَنْتُمْ عَذَابُ اللَّهِ بَغْتَةً

“Sema: Mwaonaje, ikikufikieni adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa ghafla”.

Maana yake: Huku nyinyi hamtambui, ikakushutukizieni, tahamaki imekufikieni.

أَوْ جَهْرَةً

“...au kwa dhahiri”. Bayana.

هَلْ يَهْلِكُ إِلَّا الْقَوْمُ الظَّالِمُونَ

“...je wataangamizwa isipokuwa waliodhulumu?”

Adhabu hiyo inakumba madhalimu wanaomshirikisha Allah تعالى, ilhali wale waliomuabudu Allah تعالى Peke Yake bila kumshirikisha, hawatakuwa na khofu wala kuhuzunika.

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ

“Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhuluma”. (6:82)

Kauli Yake تعالیٰ:

وَمَا نُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ

“Na hatuwatumi Mitume ila huwa ni wabashiri na waonyaji”.

Maana yake: Wanatoa bishara ya kheri kwa waja wa Allah تعالیٰ, na wanatoa maonyo kwa wanaomkana Allah تعالیٰ juu ya Ghadhabu za Allah تعالیٰ na Adhabu Zake. Na kwa ajili hii, Alisema;

فَمَنْ ءَامَنَ وَأَصْلَحَ

“Na wenye kuamini na wakatenda mema”.

Maana yake: Mwenye kuamini moyoni mwake yale waliyokuja nayo Mitume na akatenda mema kwa kuwafuata wao.

فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ

“...haitakuwa khofu juu yao”. Kuhusu yajayo.

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ

“...wala hawatahuzunika”.

Kuhusu yale waliyoyakosa na kuyaacha nyuma yao, miongoni mwa mambo ya kidunia.

Kisha Allah تعالیٰ Akasema;

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا يَمَسُّهُمْ الْعَذَابُ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٨٤﴾

“Na waliokanusha Ishara Zetu itawagusa adhabu kwa walivyokuwa wakipotoka”.

Maana yake: Watapatwa na adhabu, kwa kukufuru kwao waliyokuja nayo Mitume, na wakatoka katika amri na twaa ya Allah تعالیٰ, na wakabobea katika Alivyokataza na Kuchupa mipaka Aliyoiweka.

قُلْ لَا أَقُولُ لَكُمْ عِنْدِي خَزَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ لَكُمْ إِنِّي مَلَكٌ ۗ إِن أَنْتُمْ
 إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ ۗ أَفَلَا تَتَفَكَّرُونَ ﴿٥٠﴾ وَأَنْذِرْ بِهِ
 الَّذِينَ يَخَافُونَ أَنْ يُمَحَّشَرُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ ۗ لَيْسَ لَهُمْ مِنْ دُونِهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ
 ﴿٥١﴾ وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ ۗ مَا عَلَيْكَ مِنْ
 حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ وَمَا مِنْ حِسَابِكَ عَلَيْهِمْ مِنْ شَيْءٍ فَتَطْرُدَهُمْ فَتَكُونَ مِنَ الظَّالِمِينَ
 ﴿٥٢﴾ وَكَذَلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لِيَقُولُوا أَهَؤُلَاءِ مَنِ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنْ بَيْنِنَا ۗ
 أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَعْلَمَ بِالشَّاكِرِينَ ﴿٥٣﴾ وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلِّمٌ
 عَلَيْكُمْ ۗ كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ۗ أَنَّهُ مَنْ عَمِلَ مِنْكُمْ سُوءًا بِجَهْلَةٍ ثُمَّ تَابَ مِنْ
 بَعْدِهِ وَأَصْلَحَ فَأَنَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٤﴾

50. Sema: Mimi sikuambii kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu. Wala Sijui mambo yaliyofichikana. Wala siwaambii kuwa mimi ni Malaika. Mimi sifuati ila yanayofunuliwa kwangu. Sema: Je wanakuwa sawa kipofu na mwenye kuona. Basi hamfikiri?

51. Na waonye kwayo wanaogopa kuwa watakusanywa kwa Mola wao Mlezi, hali ya kuwa hawana mlinzi wala muombezi isipokuwa Yeye, ili wapate kuchamungu.

52. Wala usiwafukuze wanaomuomba Mola Mlezi wao asubuhi na jioni wakitaka radhi Yake. Si juu yako hesabu yao hata kidogo, wala hesabu yako si juu yao hata kidogo, hata uwafukuze na uwe miongoni mwa wenye kudhulumu.

53. Na hivi ndivyo Tunavyowajaribu wao kwa wao, ili wasiseme: Ni hao ndio Mwenyezi Mungu Amewafadhilisha miongoni mwetu? Kwani Mwenyezi Mungu Hawajui wanaoshukuru?

54. Na wanapokujia wanaoziamini Ishara Zetu waambie: Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu! Mola wenu Mlezi Amejilazimisha Rehema, ya kwamba atakayefanya uovu miongoni mwenu kwa

**ujinga, kisha akatubu baada yake na akategemea, basi hakika
Yeye ni Mwenye Maghufira Mwenye Kurehemu.**

Mtume ﷺ Hamiliki Hazina za Allah تعالى Wala Hajui Ghaibu.

Allah تعالى Alimuambia Mtume Wake;

قُلْ لَا أَقُولُ لَكُمْ عِنْدِي خَزَائِنُ اللَّهِ

“Sema: Mimi sikwambii kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu”.

Maan yake, similiki khazina za Allah تعالى wala sina mamlaka nazo.

وَلَا أَعْلَمُ الْغَيْبَ

“Wala Sijui mambo yaliyofichikana.”

Maana: Wala sikuambieni kuwa mimi nina elimu ya ghaibu kwani ujuzi wa hayo anao Allah تعالى, wala Sipati kutambua lolote isipokuwa lile Analonijulisha.

وَلَا أَقُولُ لَكُمْ إِنِّي مَلَكٌ

“Wala siwaambii kuwa mimi ni Malaika”.

Maana: Wala sidai kuwa mimi ni Malaika, kwa hakika, mimi ni kiumbe kama wengine, huwa napata Wahyi kutoka kwa Allah تعالى, Amenifadhilisha na kunineemesha kwa kunipa jukumu hilo. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema;

إِن أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ

“Mimi sifuati ila yanayofunuliwa kwangu”.

Maana yake: Sitoki nje ya Wahyi hata kwa kiasi cha shubiri au chini ya hapo.

قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ

“Sema: Je wanakuwa sawa kipofu na mwenye kuona”.

Inamaanisha, je anayefuata haki na ikamuongoa analingana na aliyepotea?

أَفَلَا تَتَفَكَّرُونَ

“Basi hamfikiri?” Hii inafanana na Kauli Yake,

﴿ أَفَمَن يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ الْحَقُّ كَمَن هُوَ أَعْمَىٰ ۚ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴾

“Je! Anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako Mlezi ni Haki ni sawa na aliye kipofu? Wenye akili ndio wanaozingatia”. (13:19)

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَنْذِرْ بِهِ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَن يُحْشَرُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ لَيْسَ لَهُم مِّنْ دُونِهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ

“Na waonye kwayo wanaoogopa kuwa watakusanywa kwa Mola wao Mlezi, hali ya kuwa hawana mlinzi wala mwombezi”.

Maana: Uwaonye kwa kuwasomea Qur'an hii ewe Muhammad ﷺ.

الَّذِينَ هُمْ مِّنْ حَشِيَّةٍ رَّبِّهِمْ مُّشْفِقُونَ

“Kwa hakika hao ambao kwa kumuogopa Mola wao Mlezi wanamnyenyekea”. (23:57) Na ambao,

وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ سُوءَ الْحِسَابِ ﴿٢١﴾

“...wanamuogopa Mola wao, na wanaikhofu hesabu mbaya”. (13:21)

الَّذِينَ يَخَافُونَ أَن يُحْشَرُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ

“...wanaoogopa kuwa watakusanywa kwa Mola wao Mlezi”.

Katika Siku ya Kiyama.

لَيْسَ لَهُم مِّنْ دُونِهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ

“...hali ya kuwa hawana mlinzi wala mwombezi”.

Hawatakuwa na ndugu wala mwombezi dhidi ya adhabu Yake ikiwa Allah تعالى Atataka kumuadhibu.

لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

“...ili wapate kuchamungu”.

Kwa hivyo, onya kuhusu siku hii ambayo hakuna hakimu mwingine yeyote, isipokuwa Allah تعالى.

لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

"...ili wapate kuchamungu".

Basi wakawa wanafanya amali njema humu duniani ambazo zitawaokoa katika Siku ya Kiama dhidi ya Adhabu Yake, na kuwazidishia malipo.

Mtume ﷺ Akatazwa Kuwarudisha Masahaba Dhaifu, na Amri ya Kuwafanyia Wao Ukarimu Pindi Wanapokuja.

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ^ط

"Wala usiwafukuze wanaomuomba Mola Mlezi wao asubuhi na jioni kwa kutaka Radhi Yake".

Maana yake: Usiwafukuze wale wenye sifa hizi, bali uwafanye kuwa ndio wenzako katika kukaa na wenye kushirikiana nawe. Ni kama Kauli Yake tena;

وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ^ط وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا^ط وَلَا تُطِعْ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَن ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطًا ﴿٢٨﴾

"Na isubirisha nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka Radhi Yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia. Wala usimtii Tuliymghafilisha moyo wake asitukumbuke, na akafuata matamano yake yakawa yamepita mipaka". (18:28)

يَدْعُونَ رَبَّهُمْ

"...wanaomuomba Mola Mlezi".

Wanamuabudu na wanamuomba Yeye.

بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ

"...asubuhi na jioni".

Sa'id bin Al-Musayyab, Mujahid, Hasan na Qatadah walisema, Makusudio ni Sala za Faradhi. Hii ni kama Kauli Yake;

وَقَالَ رَبُّكُمْ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ

“Na Mola wenu Mlezi Anasema: Niombeni Nitakuitikieni”.

Maana: Nitakutakabalieni. Allah تعالى Akasema;

يُرِيدُونَ وَجْهَهُ

“...Wanataka Radhi Yake”.

Maana yake, Wanatafuta Radhi ya Allah تعالى kwa amali hizo na wao wanafanya ibada zao na twaa kwa ikhlasi. Na Kauli Yake;

مَا عَلَيْكَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ وَمَا مِنْ حِسَابِكَ عَلَيْهِمْ مِنْ شَيْءٍ

“Si juu yako hesabu yao hata kidogo, wala hesabu yako si juu yao hata kidogo”.

Ni kama kauli ya Nabii Nuh عليه السلام kuwajibu wale waliosema;

أَنْتُمْ لَكُمْ وَأَتَّبَعَكَ الْأَرْذَالُونَ

“Je! Tukuamini wewe, hali wanaokufuata ni watu wa chini?”

(26:111)

Nuh عليه السلام Aliwajibu;

وَمَا عَلَّمِي بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٢﴾ إِنَّ حِسَابَهُمْ إِلَّا عَلَىٰ رَبِّي لَو تَشْعُرُونَ ﴿١١٣﴾

“Akasema: Nayajuaje waliyokuwa wakiyafanya? Hisabu yao haiko ila kwa Mola wao Mlezi, laiti mmngelitambua!” (26:112-113)

Maana yake: Hesabu yao iko kwa Allah تعالى, wala haiko kwangu, kama ambavyo hesabu yangu haiko kwao.

Na Kauli ya Allah تعالى;

فَتَطْرُدْهُمْ فَتَكُونَ مِنَ الظَّالِمِينَ

“...hata uwafukuze na uwe miongoni mwa wenye kudhulumu”.

Maana yake: Ukifanya hivyo, basi hali ni kama hiyo, Kauli ya Allah تعالى;

وَكَذَلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُم بِبَعْضٍ

“Na hivi ndivyo Tunavyowajaribu wao kwa wao”.

Tuliwapima, Tuliwajaribu na Tukawafanyia mtihani wao kwa wao.

لَيَقُولُوا أَهْتُولَاءِ مَنْ بَلَّغَهُمُ اللَّهُ عَلَيْهِم مِّنْ بَيْنِنَا

“...ili wapate kusema: Ni hao ndio Mwenyezi Mungu Amewafadhilisha miongoni mwetu?”

Hii ndiyo sababu mwanzoni, wengi wa waliomfuata Mtume ﷺ walikuwa watu wanyonge katika wanaume na wanawake, watumwa na vijakazi, na wachache sana katika wakuu. Nuh عليه السلام pia aliambiwa na watu wake;

مَا نَزَّلَكَ إِلَّا بَشَرًا مِّثْلَنَا وَمَا نَزَّلَكَ إِلَّا الَّذِينَ هُمْ أَرَادُوا بِآدَىٰ الرَّأْيِ

“...wala hatukuoni wamekufuata ila wale waliokuwa kwetu watu duni, na hao wamekufuata bila Kutafakari”. (11:27)

Tena ni kama Heraclius, Mfalme wa Roma alivyomuuliza Abu Sufyan, “Watu wenye vyeo ndio wanaomfuata au wanyonge?” Akajibu, “Bali ni wanyonge wao”. Akasema, “Watu hao ndio wafuasi wa Mitume”.

Na makusudio hapa ni kwamba; washirikina wa kikuraishi walikuwa wakiwadhihaki wanyonge wao waliomuamini Muhammad ﷺ na hata kuwaadhibu baadhi ya waliowamudu. Na walikuwa wakisema, “Ni hao ndio Mwenyezi Mungu Amewafadhilisha miongoni mwetu?” Wakimaanisha kuwa Allah تعالى Asingewaongoa watu hawa kwenye kheri badala ya sisi, kama kungelikuwa na kheri kweli na kutuacha sisi, ni kama kauli yao;

لَوْ كَانَ خَيْرًا مَا سَبَقُونَا إِلَيْهِ

“Na lau ingelikuwa ni kheri basi wasingetutangulia”. (46:11) na,

وَإِذَا تَنَزَّلَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَيُّ الْفَرِيقَيْنِ خَيْرٌ مَّقَامًا

وَأَحْسَنُ نَدْبًا ﴿٧٣﴾

“Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, waliokufuru huwaambia walioamini: Lipi katika makundi mawili lenye cheo kizuri na lililobora barazani?” (19:73)

Katika kujibu hilo Allah تعالى Akasema;

وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّن قَرْنٍ هُمْ أَحْسَنُ أَثْنًا وَرِئِيًّا ﴿٧٤﴾

“Na kaumu ngapi Tuliziangamiza zilizokuwa na mapambo mazuri zaidi na wazuri zaidi kwa kuwatazama!” (19:74)

أَهْتَوُلَا مِّنْ أَلَلَّهِ عَلَيْهِمْ مِّنْ بَيِّنَاتٍ أَلَيْسَ أَلَلَّهُ بِأَعْلَمَ بِالشَّكِرِينَ

“Ni hao ndio Mwenyezi Mungu Amewafadhilisha miongoni mwetu? Kwani Mwenyezi Mungu Hawajui wanaoshukuru?”

Maana yake: Je Allah تعالى Hakuwa Ndiye Mjuzi zaidi kuhusu wanaomshukuru, kwa maneno na nia zao? Na kwa hivyo, Akawawafikisha na Kuwaongoa katika njia za amani, na kwa Idhini Yake Akawatoa gizani na Kuwapelekea katika nuru na Akawaongoza katika njia nyoofu. Katika Aya nyingine Allah تعالى Alisema;

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا وَإِنَّ أَلَلَّهُ لَمَعَ أَلْمُحْسِنِينَ ﴿٦٩﴾

“Na wanaofanya juhudi kwa ajili Yetu, Sisi Tutawaongoa kwenye njia Zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na watu wema”. (26:69)

Hadithi Sahih inaeleza,

إِنَّ أَلَلَّهُ لَا يَنْظُرُ إِلَى صُورِكُمْ وَلَا إِلَى أَلْوَانِكُمْ، وَلَكِن يَنْظُرُ إِلَى قُلُوبِكُمْ وَأَعْمَالِكُمْ،

“Hakika Allah Hatizami sura wala rangi zenu, bali Anatizama nyoyo na amali zenu”¹. Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ

“Na wanapokuja wanaoziamini Ishara Zetu waambie: Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu!”

Maana yake: Uwafanyie ukarimu kwa kuwaitikia maamkizi yao na uwape ishara kuhusu rehema kunjufu za Allah تعالى makhsusi kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema,

¹ Muslim 4:1987.

كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ

“Mola wenu Mlezi Ameilazimisha Rehema”.

Maana yake: Ameilazimisha Nafsi Yake Tukufu iwapatie Rehema, kama njia ya Fadhila Zake, Ihsan na Ukarimu.

أَنَّهُ مَن عَمِلَ مِنكُمْ سُوءًا بِجَهَالَةٍ

“...ya kwamba atakayefanya uovu miongoni mwenu kwa ujinga”.

Kila anayemuasi Allah تعالى ni jahili.

ثُمَّ تَابَ مِن بَعْدِهِ وَأَصْلَحَ

“...kisha akatubu baada yake na akategemea”.

Maana yake: Akayaacha maasi aliyokuwa akiyafanya, na akaazimia kutoyarejelea, na akafanya amali njema katika mustakabali wake.

فَأَنَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“...basi hakika Yeye ni Mwenye Maghufira Mwenye Kurehemu”.

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَمَّا قَضَىٰ اللَّهُ الْخَلْقَ كَتَبَ فِي كِتَابٍ فَهُوَ عِنْدَهُ فَوْقَ الْعَرْشِ: إِنَّ رَحْمَتِي غَلَبَتْ غَضَبِي»

“Allah Alipomaliza Kuwaumba viumbe, Aliandika katika Kitabu Alichu Nacho juu ya Arshi, “Rehema Yangu imeishinda Ghadhabu Yangu”¹.

Hadith hii imenukuliwa katika Sahih Mbili pia².

* * *

¹ Ahmad 2:313.

² Fat'hul Al-Bari 13:395, Muslim 4:2107.

وَكَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٥٥﴾
 قُلْ إِنِّي نُهِيتُ أَنْ أَعْبُدَ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ قُلْ
 لَا اتَّبِعُ أَهْوَاءَكُمْ قَدْ ضَلَلْتُ إِذًا وَمَا أَنَا مِنَ
 الْمُهْتَدِينَ ﴿٥٦﴾ قُلْ إِنِّي عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِنْ رَبِّي وَكَذَّبْتُمْ بِهِ
 مَا عِنْدِي مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ ۚ إِنَّ الْحُكْمَ إِلَّا لِلَّهِ
 يَقْضُ الْحَقَّ وَهُوَ خَيْرُ الْفَاصِلِينَ ﴿٥٧﴾ قُلْ لَوْ أَنَّ عِنْدِي
 مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ لَفُضِيَ الْأَمْرُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ وَاللَّهُ أَعْلَمُ
 بِالظَّالِمِينَ ﴿٥٨﴾ * وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا
 إِلَّا هُوَ ۚ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۚ وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ
 إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٌ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا
 يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٩﴾ وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّاكُم
 بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ بِالنَّهَارِ ۚ ثُمَّ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ لِيُقْضَىٰ
 أَجَلٌ مُّسَمًّى ۗ ثُمَّ إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ ثُمَّ يُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ
 تَعْمَلُونَ ﴿٦٠﴾ وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ ۗ وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ
 حَفَظَةً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَكُمْ الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ رُسُلُنَا وَهُمْ
 لَا يُفْرِطُونَ ﴿٦١﴾ ثُمَّ رُدُّوْا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمْ الْحَقَّ ۚ لَا لَهَ
 الْحُكْمُ وَهُوَ أَسْرَعُ الْحَاسِبِينَ ﴿٦٢﴾

وَكَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ
 سَبِيلُ الْمُجْرِمِينَ ﴿٥٥﴾ قُلْ إِنِّي نُهِيتُ
 أَنْ أَعْبُدَ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ
 اللَّهِ قُلْ لَا اتَّبِعُ أَهْوَاءَكُمْ قَدْ
 ضَلَلْتُ إِذًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُهْتَدِينَ
 ﴿٥٦﴾ قُلْ إِنِّي عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِنْ رَبِّي
 وَكَذَّبْتُمْ بِهِ ۚ مَا عِنْدِي مَا
 تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ ۚ إِنَّ الْحُكْمَ إِلَّا لِلَّهِ
 يَقْضُ الْحَقَّ وَهُوَ خَيْرُ الْفَاصِلِينَ
 ﴿٥٧﴾ قُلْ لَوْ أَنَّ عِنْدِي مَا
 تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ لَفُضِيَ الْأَمْرُ بَيْنِي
 وَبَيْنَكُمْ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِالظَّالِمِينَ
 ﴿٥٨﴾ * وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا
 يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ ۚ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ
 وَالْبَحْرِ ۚ وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ
 إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٌ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ
 وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ
 مُّبِينٍ ﴿٥٩﴾

55. Na ndio hivi Tunavyovieleza Ishara ili ibainike njia ya wakosefu. Sema: Mimi nimekatanzwa kuwaabudu hao mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu.

56. Sema: Mimi sifuati matamano yenu. Hivyo nitakuwa nimepotea, na sitakuwa miongoni mwa walioongoka.

57. Sema: Mimi nipo kwenye sharia iliyowazi itokayo kwa Mola Wangu Mlezi, nanyi, mnaikanusha. Mimi sinacho hicho mnachokihimiza. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu. Yeye Anasimulia yaliyo kweli; naye ni Mbora wa Kuhukumu kuliko wote.

58. Sema: Lau kuwa ninacho hicho mnachokihimiza, ingelikwishakatwa shauri baina yangu na nyinyi. Na Mwenyezi Mungu Anawashinda wote Kuwajua madhalimu.

59. Na ziko Kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye Anajua kilichoko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinachobainisha”.

Mtume ﷺ Ana Uhakika na Anachokilingania na Malipo Yako kwa Allah تعالى.

Allah تعالى Amesema, kama Tulivyobainisha hoja na dalili zinazothibitisha njia ya uwongofu na ubaya wa malumbano na ufidhuli.

كَذَلِكَ نَفْصَلُ الْآيَاتِ

“Na ndio hivi Tunavyozieleza Ishara”.

Zile ambazo wanaoambiwa wanahitaji ufafanuzi wake.

وَلَتَسْتَبِينَ سَبِيلُ الْمُجْرِمِينَ

“...ili ibainike njia ya wakosefu”.

Maana yake: Ili njia ya wenye madhambi wanaomkhalifu Mtume ﷺ idhihirike.

قُلْ إِنِّي عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي

“Sema: Mimi nipo kwenye sharia iliyo wazi itokayo kwa Mola wangu Mlezi”.

Maana yake: Nina ujuzi tosha wa Shariah ya Allah تعالى Aliyonifunulia.

وَكَذَّبْتُمْ بِهِ^ع

"...nanyi, mnaikanusha".

Hamuamini ukweli ulionifikia kutoka kwa Allah تعالى,

مَا عِنْدِي مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ^ع

"Mimi sinacho hicho mnachokihimiza". Maana yake: Adhabu.

إِنَّ الْحُكْمَ إِلَّا لِلَّهِ^ط

"Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu".

Maana yake: Kwa hakika, hukumu ya jambo hilo iko kwa Allah تعالى. Akitaka Atakuharakishieni adhabu. Na Akitaka Atakupeni muda na kukuakhirishieni, kutokana na Hekima Zake kubwa. Ndiyo sababu Allah تعالى Alisema;

يَقْضُ الْحَقُّ وَهُوَ خَيْرُ الْفَصْلِينَ^ط

"Yeye Anasimulia yaliyo kweli; naye ni Mbora wa Kuhukumu kuliko wote".

Maana yake: Yeye ni Mbora wa kutoa Hukumu baina ya waja Wake. Kauli Yake;

قُلْ لَوْ أَنَّ عِنْدِي مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ لَقُضِيَ الْأَمْرُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ^ط

"Sema: Lau kuwa ninacho hicho mnachokihimiza, ingelikwishakatwa shauri baina yangu na nyinyi".

Maana yake: Kama ningelikuwa na hayo mnayoyaomba, kwa hakika, Ningelikushushieni mnalolistahiki.

وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِالظَّالِمِينَ

"Na Mwenyezi Mungu Anawashinda wote Kuwajua madhalimu".

Ikiwa itaulizwa, nini maana ya Aya hii ikilinganishwa na Hadith iliyo katika Sahih Mbili? Kutoka kwa 'Aisha رضي الله عنها kuwa alimuuliza Mtume ﷺ, "Ewe Mjumbe wa Allah! Je umewahi kukumbana na siku ngumu kuliko siku ya (vita vya) Uhud?" Mtume ﷺ alisema,

«لَقَدْ لَقِيتُ مِنْ قَوْمِكَ، وَكَانَ أَشَدَّ مَا لَقِيتُ مِنْهُمْ يَوْمَ الْعَقَبَةِ، إِذْ عَرَضْتُ نَفْسِي عَلَى ابْنِ عَبْدِ يَالِيلَ بْنِ عَبْدِ كَلَّالِ، فَلَمْ يُجِئْنِي إِلَى مَا أَرَدْتُ، فَأَنْطَلَقْتُ وَأَنَا مَهْمُومٌ عَلَى وَجْهِ، فَلَمْ أَسْتَفِيقْ إِلَّا بِقَرْنِ الثَّعَالِبِ، فَرَفَعْتُ رَأْسِي، فَإِذَا أَنَا بِسَحَابَةٍ قَدْ ظَلَّلَتْنِي، فَنَظَرْتُ فَإِذَا فِيهَا جِبْرِيْلُ عَلَيْهِ السَّلَامُ، فَتَنَادَانِي فَقَالَ: إِنَّ اللَّهَ قَدْ سَمِعَ قَوْلَ قَوْمِكَ لَكَ، وَمَا رَدُّوا عَلَيْكَ، وَقَدْ بَعَثَ إِلَيْكَ مَلَكَ الْجِبَالِ، لِتَأْمُرَهُ بِمَا شِئْتَ فِيهِمْ، قَالَ: فَتَنَادَانِي مَلَكُ الْجِبَالِ وَسَلَّمْ عَلَيَّ، ثُمَّ قَالَ: يَا مُحَمَّدُ! إِنَّ اللَّهَ قَدْ سَمِعَ قَوْلَ قَوْمِكَ لَكَ، وَقَدْ بَعَثَنِي رَبُّكَ إِلَيْكَ، لِتَأْمُرَنِي بِأَمْرِكَ فِيمَا شِئْتَ، إِنْ شِئْتَ أَطَبَّقْتُ عَلَيْهِمُ الْأَخْشَبِينَ» فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «بَلْ أَرْجُو أَنْ يُخْرِجَ اللَّهُ مِنْ أَضْلَابِهِمْ، مَنْ يُعْبُدُ اللَّهَ لَا يُشْرِكُ بِهِ شَيْئًا»

“Watu wako walinipa wakati mgumu na zaidi ilikuwa katika siku ya ‘Aqabah, wakati nilipojipeleka mwenyewe kwa Ibn ‘Abd Yaaliyl bin ‘Abd Kulaal ambaye hakuitikia wito wangu. Kwa hiyo, Nikaondoka nikiwa na huzuni nyingi. Sikupumzika mpaka nilipofika Qarn Ath-Tha’aalib ambapo niliinua kichwa changu juu, mara nikaona mawingu yakinisitiri. Nikatizama na nikamuona Jibril, akaniita na kuniambia, “Kwa hakika, Allah Amesikia kauli yako kwa kaumu yako na walichokujibu na Amemtuma kwako malaika wa milima ili umuamuru lolote ulitakalo juu yao”. Malaika wa Milima akaniita na kuniambia. Halafu akasema, “Ewe Muhammad! Kwa hakika, Allah Amesikia namna watu wako walivyoichukulia kauli yako, na Mola wako Amenituma kwako ili uniamuru utakavyo. Ukitaka nitaachilia Al-Akshabain (milima miwili) iwaangukie”. Mtume ﷺ akasema, “Hapana, nina matumaini kwamba Allah Atajaalia wazae kizazi kitakachomuabudu Allah na hawatamshirikisha na chochote”¹.

Na hili ndilo tamko la Muslim. Jambo la kuadhibiwa kwa Makuraishi liliwekwa katika khiyari ya Mtume ﷺ, lakini aliamua kuwa na subira na akamuomba Allah تعالی, Awaakhirishie, kwani huenda Akawapatia uzao usiomshirikisha na chochote. Basi tutaikusanya vipi maana ya *Hadith* hii na Aya tukufu ifuatayo;

¹ Fath Al-Bari 6:360 na Muslim 3:1420.

قُلْ لَوْ أَنَّ عِنْدِي مَا تَسْتَعِجِلُونَ بِهِ لَقُضِيَ الْأَمْرُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۗ وَاللَّهُ أَعْلَمُ
بِالظَّالِمِينَ

“Sema: Lau kuwa ninacho hicho mnachokihimiza, ingelikwishakatwa shauri baina yangu na nyinyi. Na Mwenyezi Mungu Anawashinda wote Kuwajua madhalimu”.

Jawabu la swali hili ambalo Allah تعالی ni Mjuzi zaidi, ni kuwa, Aya hii imejulisha kuwa, kama adhabu waliyoiomba ilikuwa katika mamlaka ya Mtume ﷺ katika wakati walipokuwa wakiitaka, Angeliwapelekea.

Ama katika *Hadithi*, makafiri hawakumuomba Mtume ﷺ kuwa adhabu iwashukie.

Bali Malaika anayetumikishwa katika milima alimpa khiyari Mtume ﷺ kuwa kama akitaka Malaika watawabamiza kwa kuwafunika na milima miwili ambayo ipo kaskazini na kusini mwa mji wa Makkah.

Na katika hili, Mtume ﷺ hakutaka hayo yatokee, na akaomba wafanyiwe huruma.

Allah تعالی Ndiye Pekee Ajuaye Ghaibu.

Kauli ya Allah تعالی;

وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ

“Na ziko Kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu”.

Al-Bukhari amenukuu kuwa Salim bin ‘Abdullah alisema kuwa baba yake alisema kwamba Mtume ﷺ alisema;

«مَفَاتِحُ الْغَيْبِ خَمْسٌ لَا يَعْلَمُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ»

“Funguo za ghaibu ziko tano na hakuna azijuaye, isipokuwa Allah”.

إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُرْسِلُ الْغَيْثَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ ۗ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّاذَا

تَكْسِبُ غَدًا ۗ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿٦٢﴾

“Hakika kuijua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye Ndiye Anayeiteremsha mvua. Na Anavijua vilivyomo ndani ya matumbo ya uzazi. Na haijui nafsi yoyote itachuma nini kesho. Wala nafsi yoyote haijui itakufa nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujua, Mwenye Khabari” (31:34)¹.

Na Kauli Yake تعالى:

وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ

“Na Yeye Anajua kilichoko nchi kavu na baharini”.

Maana yake: Elimu Yake Tukufu imekizunguka kila kitu, cha bara na baharini, hakuna chochote katika hivyo, kilichofichikana, hata japo uzito wa atomu, kiwe ardhini ama mbinguni.

Na Kauli Yake:

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا

“Na halidondoki jani ila Analijua”.

Maana: Anajua mitikisiko mpaka ya vitu visivyo na uhai, sembuse wanyama, hasa wale waliowekewa sheria ya Dini, miongoni mwa majini na wanadamu?

Katika Aya nyingine, Amesema:

يَعْلَمُ خَائِبَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفِي الصُّدُورُ ﴿٥٥﴾

“(Mwenyezi Mungu) Anajua khiyana ya macho na yanayoficha vifua”.

وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّنَا بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ بِالنَّهَارِ ثُمَّ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ لِيُقْضَىٰ أَجَلٌ

مُسَمًّى ۗ ثُمَّ إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ ثُمَّ يُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥٦﴾ وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ ۗ

وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ حَفَظَةً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَكُمْ الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ رُسُلُنَا وَهُمْ لَا يُفْرِطُونَ ﴿٥٧﴾

ثُمَّ رُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقِّ ۗ أَلَا لَهُ الْحُكْمُ وَهُوَ أَسْرَعُ الْحَاسِبِينَ ﴿٥٨﴾

¹ Fat'hul Al-Bari 8:141.

60. Na Yeye Ndiye Anayekufisheni usiku, na Anakijua mlichofanya mchana. Kisha Yeye Hukufufueni humo mchana ili muda uliowekwa utimizwe. Kisha Kwake Yeye Ndiyo marejeo yenu, na tena Akwambieni mliyokuwa mkiyafanya.

61. Naye Ndiye Mwenye Nguvu za Kushinda, Aliye juu ya waja Wake. Na Hukupelekeeni waangalizi, mpaka mmoja wenu yakimjia mauti wajumbe Wetu humfisha, nao hawafanyi taksiri.

62. Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki. Hakika, hukumu ni Yake. Naye ni Mwepesi kuliko wote wanao hesabu".

Waja Wote Wako Chini ya Uangalizi wa Allah تعالى Kabla na Baada ya Mauti.

Allah تعالى Amesema kwamba Yeye Huwafisha waja Wake usingizini mwao usiku, kwani kulala ni kifo kidogo. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Alisema;

إِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَىٰ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ

"Pale Mwenyezi Mungu Aliposema: Ewe Isa! Mimi Nitakutimizia muda wako wa kuishi, na Nitakunyanyua Kwangu". (3:55) na;

اللَّهُ يَتَوَفَّى الْأَنفُسَ حِينَ مَوْتِهَا وَالَّتِي لَمْ تَمُتْ فِي مَنَامِهَا ۖ فَيُمْسِكُ الَّتِي قَضَىٰ عَلَيْهَا
الْمَوْتَ وَيُرْسِلُ الْأُخْرَىٰ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ

"Mwenyezi Mungu Huzipokea roho zinapokufa. Na zile zisiokufa wakati wa kulala kwake, Huzishika zilizohukumwiwa kufa, na Huzirudisha nyingine mpaka ufike wakati uliowekwa". (39:42)

Katika Aya hii, Ametaja kufa kwa namna mbili, kifo kikubwa na kidogo. Na hivi ndivyo Alivyotaja, Ametanguliza, kilicho kikubwa, kabla ya kidogo.

Kauli ya Allah تعالى;

وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّاكُم بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُم بِالنَّهَارِ

"Na Yeye Ndiye Anayekufisheni usiku, na Anakijua mlichofanya mchana".

Inamaanisha kuwa Anayajua matendo mnayoyafanya wakati wa mchana¹. Aya hii inajulisha Elimu Kamilifu ya Allah تعالى juu ya viumbe Wake kwa mchana na usiku na katika kutulia mienendo yao. Ni sawa na Kauli Yake;

سَوَاءٌ مِنْكُمْ مَنْ أَسْرَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿١٠﴾

“Ni sawa anayeficha kauli yake kati yenu na anayeidhihirisha, na anayejibanza usiku na anayetembea jahara mchana”. (13:10) na,

وَمِنْ رَحْمَتِهِ جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ

“Na ni katika rehema Zake Amekufanyieni usiku na mchana mpate kupumzika humo”. (28:73)

Maana yake: Wakati wa usiku.

وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ

“Na mtafute Fadhila Zake”.

Maana yake: Wakati wa mchana. Na kwa minajili hiyo Allah تعالى Akasema;

وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّنَكُمْ بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ بِالنَّهَارِ

“Na Yeye Ndiye Anayekufisheni usiku, na Anakijua mlichofanya mchana”.

Kama Alivyosema;

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ لِبَاسًا ﴿١٠﴾ وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ﴿١١﴾

“Na Tukafanya usiku ni nguo? Na Tukaufanya mchana ni wa kuchumia maisha?” (78:10-11)

ثُمَّ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ

“Kisha Yeye Hukufufueni humo”.

Maana yake: Wakati wa mchana, kwa mujibu wa Mujahid, Qatadah na As-Suddi. Kauli ya Allah تعالى;

¹ At-Tabari 5:212.

لِيُقْضَىٰ أَجَلٌ مُّسَيَّءٌ

"...ili muda uliowekwa utimizwe".

Inazungumzia kipindi cha maisha ya kila mtu.

ثُمَّ إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ

"Kisha Kwake Yeye Ndiyo marejeo yenu". Siku ya Kiyama.

ثُمَّ يُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

"..na tena Akwambieni mliyokuwa mkiyafanya".

Na Atakulipeni, malipo mema kwa wema na mabaya kwa ubaya.

Na Kauli Yake;

وَهُوَ الْغَافِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ

"Naye Ndiye Mwenye Nguvu za Kushinda, Aliye juu ya waja Wake".

Maana yake: Yeye Ndiye Anayekitenza nguvu kila kitu. Kila kitu ni kinyenyekevu katika Utukufu na Kiburi Chake.

وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ حَفَظَةً

"Na Hukupelekeeni waangalizi".

Malaika ambao ni waangalizi wa mwanadamu.

Ni kama Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لَهُمْ مُعَقِّبَاتٌ مِّنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ

"Kila mtu analo kundi la malaika mbele yake na nyuma yake linamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu". (13:11)

Wanaochunga amali zake na kuziandika. Kama katika Kauli Yake nyingine;

وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لِحَافِظِينَ

"Na hakika bila ya shaka wapo walinzi juu yenu". (82:10) na;

إِذْ يَتَلَقَى الْمُتَلَقِيَانِ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ قَعِيدٌ ﴿٥٧﴾ مَا يَلْفِظُ مِنْ قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿٥٨﴾

“Wanapopokea wapokeaji wawili, wanaokaa kuliani na kushotoni. Hatamki neno ila karibu yake yupo mwangalizi tayari”. (50:17-18)

Kauli ya Allah تعالى:

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدُكُمُ الْمَوْتُ

“...mpaka mmoja wenu yakimjia mauti”. Inakusudiwa kuwa muda wake wa kufariki ukishawadia.

تَوَفَّئَهُ رُسُلُنَا

“...wajumbe wetu humfisha”. Maana yake: Malaika wenye kuwajibika na kazi hii. Alisema Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na wengineo kuwa Malaika wa mauti anasaidiwa na Malaika wengine wanaoitoa roho kutoka katika kiwiliwili na kumkabidhi Malaika wa mauti pindi ifikiapo kooni¹. Na Kauli Yake;

وَهُمْ لَا يُفَرِّطُونَ

“...nao hawafanyi taksiri”. Katika kuihifadhi roho ya Aliyekufa, bali wanaichukua mpaka Anapopataka Allah تعالى. Ikiwa ni ya mja mwema, basi itakwenda Illiyyin, na ikiwa ni ya fidhuli, basi itakuwa katika Sijjin². Na Kauli Yake;

ثُمَّ رُدُّوْا إِلَى اللَّهِ مَوْلَهُمْ الْحَقَّ

“Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki”.

Imamu Ahmad amemnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ الْمَيِّتَ تَحْضُرُهُ الْمَلَائِكَةُ فَإِذَا كَانَ الرَّجُلُ الصَّالِحُ، قَالُوا: أَخْرُجِي أَيْتَهَا النَّفْسُ الطَّيِّبَةُ كَانَتْ فِي الْجَسَدِ الطَّيِّبِ، أَخْرُجِي حَمِيدَةً، وَأَبْشِرِي بِرَوْحٍ وَرِيحَانٍ، وَرَبِّ غَيْرِ غَضَبَانَ، فَلَا تَرَأَى لَهَا يُقَالُ لَهَا ذَلِكَ حَتَّى تَخْرُجَ، ثُمَّ يُعْرَجُ بِهَا إِلَى السَّمَاءِ، فَيَسْتَفْتَحُ لَهَا فَيُقَالُ مَنْ هَذَا؟ فَيُقَالُ: فُلَانٌ، فَيُقَالُ: مَرَحِبًا بِالنَّفْسِ الطَّيِّبَةِ، كَانَتْ فِي الْجَسَدِ الطَّيِّبِ، ادْخُلِي حَمِيدَةً وَأَبْشِرِي بِرَوْحٍ وَرِيحَانٍ وَرَبِّ غَيْرِ غَضَبَانَ، فَلَا تَرَأَى

¹ At-Tabari 11:410.

² Rejea Surat Al-Mutaffin, 83:7-9 na 18-21.

يَقَالُ لَهَا ذَلِكَ حَتَّى يُتْتَهَىٰ بِهَا إِلَى السَّمَاءِ الَّتِي فِيهَا اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ، وَإِذَا كَانَ الرَّجُلُ السُّوءَ، قَالُوا: اخْرُجِي أَيُّهَا النَّفْسُ الْخَبِيثَةُ كَأَنْتَ فِي الْجَسَدِ الْخَبِيثِ، اخْرُجِي ذَمِيمَةً وَأَبْشِرِي بِحَمِيمٍ وَعَسَاقِي، وَأَخْرَجَ مِنْ شَكْلِهِ أَزْوَاجَ، فَلَا تَزَالُ يُقَالُ لَهَا ذَلِكَ حَتَّى تَخْرُجَ، ثُمَّ يُعْرَجُ بِهَا إِلَى السَّمَاءِ، فَيُسْتَفْتَحُ لَهَا فَيُقَالُ: مَنْ هَذَا؟ فَيُقَالُ: فَلَانٌ، فَيُقَالُ: لَا مَرْحَبًا بِالنَّفْسِ الْخَبِيثَةِ كَأَنْتَ فِي الْجَسَدِ الْخَبِيثِ، اِرْجِعِي ذَمِيمَةً، فَإِنَّهُ لَا يَفْتَحُ لَكَ أَبْوَابَ السَّمَاءِ، فَتُرْسَلُ مِنَ السَّمَاءِ ثُمَّ تُصِيرُ إِلَى الْقَبْرِ، فَيَجْلِسُ الرَّجُلُ الصَّالِحُ، فَيُقَالُ لَهُ مِثْلُ مَا قِيلَ فِي الْحَدِيثِ الْأَوَّلِ، وَيَجْلِسُ الرَّجُلُ السُّوءُ فَيُقَالُ لَهُ مِثْلُ مَا قِيلَ فِي الْحَدِيثِ الثَّانِي،

*"Malaika humjia mtu anayekaribia kufa. Akiwa ni mwema, wao husema, "Ewe roho nzuri iliyo ndani ya mwili mzuri! Toka humo kwa heshima na upokee bishara ya kupata raha na manukato na Mola Akiwa Hana Ghadhabu. Wataendelea kumuambia hayo mpaka roho yake itakapotoka. Kisha wanapanda nayo mbinguni, na pataombwa mlango ufunguliwe kwa ajili ya roho hiyo. Pataulizwa, "Ni nani?" Jibu litatolewa, "Fulani" Patasemwa, "Karibu sana, roho nzuri iliyokuwa katika mwili mzuri. Ingia kwa heshima na upokee bishara ya kupata raha na manukato na Mola Akiwa Hana ghadhabu. Itaendelea kuambiwa hayo mpaka itakapofika katika mbingu Aliyomo Allah. Na kama Atakuwa ni mtu muovu, Malaika watasema, "Toka ewe roho chafu, kutoka katika mwili mchafu. Toka ukiwa mwenye fedheha, na upokee khabari za kinywaji kiovu cha maji ya moto na usaha, na kingine kilicho mchanganyiko. Wataendelea kuambiwa hivyo mpaka itakapotoka roho. Kisha wanapanda nayo mpaka mbinguni na pataombwa mlango ufunguliwe kwa ajili ya roho hiyo. Pataulizwa, "Ni nani?" Jibu litatolewa, "Fulani". Patasemwa, "Roho chafu haikaribishwi. Ondoka kwa fedheha, milango ya mbinguni haitafunguliwa kwa ajili yako". Basi, itafukuzwa huko mbinguni na kurejeshwa kaburini. Mtu yule mwema atakalishwa, na kuambiwa maneno kama ya hapo mwanzoni. Mtu mwovu naye atakalishwa na ataambiwa kama hapo mwanzoni"*¹

¹ Ahmad 2:364.

Pia inawezekana maana ya Kauli Yake;

ثُمَّ رُدُّوْا

“Kisha watarudishwa”.

Viumbe wote, kwa Allah تعالى katika Siku ya Kiyama, halafu Awahukumu kwa uadilifu. Ni kama Alivyosema katika Aya nyingine;

قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ﴿٥٦﴾ لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٥٧﴾

“Sema: Hakika wa zamani na wa mwisho. Bila ya shaka watakusanywa kwa wakati wa siku maalumu”. (56:49-50) Na;

وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا

“...na Tutawafufua – wala hatutamuacha hata mmoja kati yao”.

Hadi

وَلَا يَظَلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا

“Na Mola wako Hatomdhulumu yeyote”. (18:49)

Kwa ajili hiyo Allah تعالى Alisema;

ثُمَّ رُدُّوْا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقِّ ۗ أَلَا لَهُ الْحُكْمُ وَهُوَ أَسْرَعُ الْحَاسِبِينَ

“Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki. Hakika, Hukumu ni Yake. Naye ni Mwepesi kuliko wote wanao hesabu”. (6:62)

* * *

قُلْ مَنْ يُنَجِّبِكُمْ مِنْ ظُلُمَاتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ تَدْعُونَهُ تَضَرُّعًا
 وَخُفْيَةً لَئِنْ أَجَبْنَا مِنْ هَدِيهِ لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿٦٣﴾
 قُلِ اللَّهُ يُنَجِّبِكُمْ مِمَّا وَمِنْ كُلِّ كَرْبٍ ثُمَّ أَنْتُمْ
 تُشْرِكُونَ ﴿٦٤﴾ قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّنْ فَوْقِكُمْ أَوْ
 مِنْ تَحْتِ أَرْضِكُمْ أَوْ يَلْبِسَكُمْ شِيْعًا وَيُذِيقَ بَعْضَكُمْ بَأْسَ
 بَعْضٍ ۗ أَنْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُوْنَ ﴿٦٥﴾
 وَكَذَّبَ بِهِ قَوْمُكَ وَهُوَ الْحَقُّ ۗ قُلْ لَسْتُ عَلَيْكُمْ بِوَكِيلٍ
 ﴿٦٦﴾ لِكُلِّ نَبِيٍّ مُّسْتَقَرٌّ ۖ وَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾ وَإِذَا رَأَيْتَ
 الَّذِينَ يَخُوضُونَ فِي آيَاتِنَا فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ حَتَّىٰ يَخُوضُوا فِي
 حَدِيثٍ غَيْرِهِ ۗ وَإِمَّا يُنْسِيَنَّكَ الشَّيْطَانُ فَلَا تَقْعُدْ بَعْدَ
 الذِّكْرِىٰ مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٦٨﴾ وَمَا عَلَى الَّذِينَ
 يَتَّقُونَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ وَلَكِنْ ذِكْرِىٰ لَعَلَّهُمْ
 يَتَّقُونَ ﴿٦٩﴾ وَذَرِ الَّذِينَ أَخَذُوا دِيْنَهُمْ لَٰعِبًا وَلَهُمْ
 وَعَرَّتُهُمْ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا ۗ وَذَكَرَ بِهِمْ أَنْ تَبْسَلَ نَفْسٌ بِمَا
 كَسَبَتْ لَيْسَ لَهَا مِنْ دُوْرِ اللَّهِ وِلْيٌ وَلَا شَفِيعٌ ۚ وَإِنْ تَعَدَّلَ
 كُلٌّ عَدَلٍ لَّا يُؤْخَذُ مِنْهَا ۗ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ أُبْسِلُوا بِمَا
 كَسَبُوا ۗ لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا
 يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾

قُلْ مَنْ يُنَجِّبِكُمْ مِنْ ظُلُمَاتِ الْبَرِّ
 وَالْبَحْرِ تَدْعُونَهُ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً لَئِنْ
 أَجَبْنَا مِنْ هَدِيهِ لَنَكُونَنَّ مِنَ
 الشَّاكِرِينَ ﴿٦٣﴾ قُلِ اللَّهُ يُنَجِّبِكُمْ
 مِمَّا وَمِنْ كُلِّ كَرْبٍ ثُمَّ أَنْتُمْ
 تُشْرِكُونَ ﴿٦٤﴾ قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ
 أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّنْ فَوْقِكُمْ
 أَوْ مِنْ تَحْتِ أَرْضِكُمْ أَوْ يَلْبِسَكُمْ
 شِيْعًا وَيُذِيقَ بَعْضَكُمْ بَأْسَ بَعْضٍ ۗ
 أَنْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ
 يَفْقَهُوْنَ ﴿٦٥﴾

63. Sema: Ni nani anaye-
 kuokoeni katika giza la nchi
 kavu na baharini? Mnamu-
 omba kwa unyenyekevu na
 kwa siri, mkisema: Kama
 Akituokoa na haya bila ya
 shaka tutakuwa miongoni
 mwa wanao- shukuru.

64. Sema: Mwenyezi Mungu
 Hukuokoeni kutoka hayo,
 na kutoka kila mashaka, na
 kisha nyinyi mnamshi-
 rikisha!

65. Sema: Yeye Ndiye Muweza wa Kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu au
 kutoka chini ya miguu yenu, au Kukuleteeni fujo la mfarakano, na

Kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzenu. Tazama vipi Tunavyo zieleza Aya ili wapate kufahamu.

Kubainisha Fadhila, Ukarimu, Nguvu na Uwezo wa Allah تعالى.

Allah تعالى Anaeleza namna Anavyowapa fadhila waja Wake, kwa Kumuokoa mwenye dhiki katika kiza cha bara na baharini, maana wenye matatizo wakiwa bara, na katika vina vya baharini, pindi wanapokumbwa na dhoruba, basi wakati huo huwa wanamuomba Allah تعالى Peke Yake, bila washirika.

Katika Aya nyingine, Allah تعالى Anasema;

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَٰهًا

“Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu”. (17:67) na;

هُوَ الَّذِي يُسِيرُكُمُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ حَتَّىٰ إِذَا كُنْتُمْ فِي الْفُلِكِ وَجَرَبَ بِكُمْ بِرِيحٍ طَيِّبَةٍ وَفَرِحُوا بِهَا جَاءَتْهَا رِيحٌ عَاصِفٌ وَجَاءَهُمُ الْمَوْجُ مِنْ كُلِّ مَكَانٍ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ أُحِيطَ بِهِمْ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ لَئِن أُنجِيتَنَا مِنْ هَذِهِ لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿٦٧﴾

“Yeye Ndiye Anayekuendesheni bara na baharini. Hata mnapokuwa majahazini na yakawa yanakwenda nao kwa upepo mzuri wakaufurahia, upepo mkali ukawazukia, na yakawajia mawimbi kutoka kila upande, na wakaona wameshazongwa, basi hapo humuomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia niya: Ukituokoa na haya bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru”. (10:22) Na,

أَمْ يَهْدِيكُمْ فِي ظُلُمَاتٍ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَمَنْ يُرْسِلُ الرِّيَّحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ ۗ أَلَيْسَ اللَّهُ بِمَعِ اللَّهُ تَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٦٨﴾

“Au nani yule anayekuongoeni katika giza la bara na bahari, na akazipeleka pepo kuleta bishara kabla ya rehemu Zake? Je! Yupu Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ametukuka Mwenyezi Mungu juu ya wanaowashirikisha naye”. (27:63)

Na Amesema katika Aya hii tukufu;

قُلْ مَنْ يُنَجِّيكُمْ مِنَ ظُلُمَاتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ تَدْعُونَهُ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً

“Sema: Ni nani anayekuoeni katika giza la nchi kavu na baharini? Mnamuomba kwa unyenyekevu na kwa siri”.

Kwa siri na dhahiri.

لَيْنَ أُنَجِّينَا

“Kama Akituokoa”. Kutoka katika dhiki hii.

لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ

“...bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru”.

Baadae, Allah تعالى Alisema;

قُلِ اللَّهُ يُنَجِّيكُمْ مِنْهَا وَمِنْ كُلِّ كَرْبٍ ثُمَّ أَنْتُمْ تُشْرِكُونَ ﴿٦٤﴾

“Sema: Mwenyezi Mungu Hukuoeni kutoka hayo, na kutoka kila mashaka, na kisha nyinyi mnamshirikisha!”

Ikimaanisha na bado katika vipindi vya raha mnamshirikisha na miungu mingine.

Allah تعالى Alisema;

قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّنْ فَوْقِكُمْ أَوْ مِنْ تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ

“Sema: Yeye Ndiye Muweza wa Kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu”.

Aliyasema maneno haya baada ya kusema.

ثُمَّ أَنْتُمْ تُشْرِكُونَ

“...kisha nyinyi mnamshirikisha!” Allah تعالى Alisema tena;

قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا

“Sema: Yeye Ndiye Muweza wa Kukuleteeni adhabu”.

Maana yake: Baada ya kukuokoeni.

Ni sawa na Kauli Yake katika Surat Subhaan (Sura ya 17).

رَبُّكُمْ الَّذِي يُرِيحُ لَكُمْ الْفَلَاحَ فِي الْبَحْرِ لِيَتَّبِعُوا مِنْ فَضْلِهِ إِنَّهٗ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٦٦﴾ وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَاهُ فَلَمَّا نَجَّكُمْ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ وَكَانَ الْإِنْسَانُ كَفُورًا ﴿٦٧﴾ أَفَأَمِنْتُمْ أَنْ يَخْسِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْبَرِّ أَوْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ وَكِيلًا ﴿٦٨﴾ أَمْ أَمِنْتُمْ أَنْ يُعِيدَكُمْ فِيهِ تَارَةً أُخْرَى فَيُرْسِلَ عَلَيْكُمْ قَاصِفًا مِنَ الرِّيحِ فَيُغْرِقَكُم بِمَا كَفَرْتُمْ ۗ ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ عَلِيًّا بِهِ تَبِيعًا ﴿٦٩﴾

"Mola wenu Mlezi Ndiye Anayekuendesheni marikebu katika bahari ili mtafute katika fadhila Zake. Hakika Yeye ni Mwenye Kukurehemuni nyinyi. Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnao waomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu. Na Anapokuvueni mkafika nchi kavu, mnageuka. Ama mwanadamu ni mwingi wa kukanusha. Je! Mmeaminisha ya kuwa Hataku didimizeni upande wowote katika nchi kavu, au kwamba Hataku leteeni tufani la kokoto? Kisha msipate mtetezi. Hatakurudisheni humo mara nyingine na kukupelekeeni kimbunga cha upepo Akakuzamisheni kwa mlivyo kufuru, na kisha msipate wa kukunusuruni nasi". (17:66-69)

Al-Bukhari alieleza kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّن فَوْقِكُمْ أَوْ مِن تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ أَوْ يَلِيَسَكُمُ شَيْعًا وَيُدِيقَ بَعْضَكُم بَأْسَ بَعْضٍ ۗ أَنْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُوْنَ ﴿٦٧﴾

"Sema: Yeye Ndiye Muweza wa Kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu au Kukuleteeni fujo la mfarakano, na Kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzenu. Tazama vipi Tunavyozieleza Aya ili wapate kufahamu".

"Yalbisakum" Maana yake: Kukuleteeni machafuko, kwa kuwagawa katika makundi na madhehebu. Jabir bin 'Abdullah رضي الله عنه alieleza Ayah hii ilipotemshwa,

قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّن فَوْقِكُمْ

"Sema: Yeye Ndiye Muweza wa Kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu".

Mtume ﷺ alisema;

«أَعُوذُ بِرَوْحِكَ»

“Najilinda kwa Uso Wako.”

أَوْ مِنْ تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ

“...au chini ya miguu yenu”. Akasema tena Kauli hiyo,

أَوْ يَلِيْسِكُمْ شَيْعًا وُيَذِيقَ بَعْضُكُمْ بَأْسَ بَعْضٍ

“...au Kukuleteeni fujo la mfarakano, na Kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzenu”.

Mtume ﷺ akaendelea kusema;

«هَذِهِ أَخْرُونُ - أَوْ أُبْسَرُ»

“Huu ni mzigo mdogo au mwepesi zaidi”¹.

Bukhari aliinukuu tena Hadith hii katika kitabu cha *Tawhid* (ndani ya *Sahih*)². An-Nasai naye aliinukuu katika kitabu cha *Tafsir*³.

Hadith Nyingine.

Imamu Ahmad amenukuu kwamba Sa'd bin Abu Waqqas رضي الله عنه alisema, Tuliambatana na Mtume ﷺ na tukapita katika Msikiti wa Banu Mu'awiyah. Mtume ﷺ akaingia ndani na kusali rakaa mbili, sisi tukasali nyuma yake. Akamuomba Mola Wake dua ndefu, halafu akasema;

«سَأَلْتُ رَبِّي ثَلَاثًا: سَأَلْتُهُ أَنْ لَا يُهْلِكَ أُمَّتِي بِالْفَرْقِ فَأَعْطَانِيهَا، وَسَأَلْتُهُ أَنْ لَا يُهْلِكَ أُمَّتِي بِالسَّيِّئَةِ فَأَعْطَانِيهَا، وَسَأَلْتُهُ أَنْ لَا يَجْعَلَ بَأْسَهُمْ بَيْنَهُمْ فَمَنْعَنِيهَا»

“Nimemuomba Mola wangu mambo matatu, nimemuomba Asiuangamize umma wangu kwa gharika, na Akanipatia hilo. Nimemuomba pia Asiuangamize umma wangu kwa ukame, na Akanipatia hilo. Nikamuomba Asiwafanye wapate kivangaito cha wengine, lakini hilo Hakunipatia”. (Ahmad 1:175 na Muslim 2890)

¹ Fat'hul Al-Bari 8:141.

² Fat'hul Al-Bari 13:400.

³ An-Nasai katika Al-Kubra 6:340.

Hadith Nyingine.

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Khabbab bin Al-Arat, Mawla wa Banu Zuhrah, رضي الله عنه alipigana vita vya Badr pamoja na Mtume ﷺ, alisema; "Nilikutana na Mtume ﷺ katika usiku ambao alisali kucha mpaka alfajiri." Mtume ﷺ akatoa salamu ya kumaliza Sala yake, nilimuambia, "Ewe Mjumbe wa Allah! Usiku wa leo, umesali Sala ambayo Sijawahi kukuona ukiisali kama hivyo." Mtume ﷺ akasema;

«أَجَلٌ إِنَّهَا صَلَاةٌ رَّغِبٍ وَرَهْبٍ، سَأَلْتُ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ فِيهَا ثَلَاثَ خِصَالٍ، فَأَعْطَانِي
الثَّيْبَ وَمَتْنِي وَاجِدَةً، سَأَلْتُ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ أَنْ لَا يُهْلِكَنَا بِمَا أَهْلَكَ بِهِ الْأُمَّمَ قَبْلَنَا
فَأَعْطَانِيهَا، وَسَأَلْتُ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ أَنْ لَا يُظْهِرَ عَلَيْنَا عَدُوًّا مِنْ غَيْرِنَا فَأَعْطَانِيهَا،
وَسَأَلْتُ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ أَنْ لَا يَلْبَسَنَا شَيْءًا فَمَتَّنِيهَا»

"Amba! Ilikuwa ni Sala ya shauku na khofu. Katika Sala hiyo, nimemuomba Mola Wangu mambo matatu, akanipatia mawili na kunizuilia moja. Nimemuomba Mola Wangu Asituangamize kwa kile Alichowaangamizia umma uliotangulia, Akanikubalia. Nikamuomba Mola Wangu Asiwafanye maadui zetu watushinde, na Akanipatia hilo. Na nikamuomba Mola Wangu Asitufarakishe kwa kiwango cha kuwepo makundi makundi, Akanizuilia hilo"¹.

Wameinukuu An-Nasai, Ibn Hibban katika *Sahih* yake, na Tirmidhi katika kitabu juu ya *Al-Fitan* na akasema, "*Hasan Sahih*"². Kauli ya Allah تعالى:

أَوْ يَلْبَسَكُمْ شَيْئًا

"...au Kukuleteni fujo la mfarakano".

Maana yake: Atakufanyeni muwe katika ghasia na kugawanyika katika makundi yenye upinzani. Al-Walibi ('Ali bin Abu Twalhah) alisema Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema Aya hii inamaanisha matamano³. Vivyo hivyo alisema Mujahid na wengine⁴. Ilipokewa Hadith ya Mtume ﷺ kupitia isnadi za wapokezi mbalimbali kuwa alisema;

¹ Ahmad 1:175 na Muslim 2890.

² Ahmad 3:108.

³ An-Nasai 3:217, Ibn Hibban 9:179, Tufhat Al-Ahwadhi 6:397, Ahmad 5:108.

⁴ At-Tabari 11:420.

رَسْتَنْتَرُقُ هَذِهِ الْأُمَّةَ عَلَى ثَلَاثٍ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، كُلُّهَا فِي النَّارِ إِلَّا وَاحِدَةً

*"Umma huu utagawanyika katika makundi sabini na matatu, yote yataingia motoni isipokuwa moja"*¹.

Kauli ya Allah تعالى:

وَيُذِيقُ بَعْضَكُمْ بَأْسَ بَعْضٍ

"... na kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzenu".

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na wengine, wamesema maana yake Anawafanya mtesane na kuuana². Na Kauli Yake;

أَنْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ

"Tazama vipi Tunavyo zieleza Ayah".

Maana yake: Tunaziweka dhahiri shahiri na tunazifanua na kuzitafsiri.

لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُونَ

"...ili wapate kufahamu".

Maana yake: Wafahamu na wazingatie Aya, Uthibitisho na ushahidi wa Allah تعالى.

وَكَذَّبَ بِمِ قَوْمِكَ وَهُوَ الْحَقُّ قُلْ لَسْتُ عَلَيْكُمْ بِوَكِيلٍ ﴿٦٦﴾ لِكُلِّ نَبِيٍّ مُسْتَفْرَضٍ وَسَوْفَ

تَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾ وَإِذَا رَأَيْتَ الَّذِينَ يَخُوضُونَ فِي آيَاتِنَا فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ حَتَّى يَخُوضُوا فِي

حَدِيثِ غَيْرِهِ ؕ وَإِنَّمَا يُنْسِئُكَ الشَّيْطَانُ فَلَا تَقْعُدْ بَعْدَ الذِّكْرِى مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ

﴿٦٨﴾ وَمَا عَلَى الَّذِينَ يَتَّقُونَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ وَلَكِنْ ذِكْرٌ لَعَلَّهُمْ

يَتَّقُونَ ﴿٦٩﴾

66. "Na watu wako Wameikanusha, nayo ni Haki. Sema: Mimi sikuwakilishwa juu yenu.

¹ At-Tabari 11:419.

² Abu Dawud 5:5, Tufhat Al-Awadhi 7:399, Ibn Majah 2:1322.

67. Kila khabari ina kipindi chake. Nanyi mtakuja jua.

68. Na unapowaona wanaoziingilia Ayah Zetu, basi jitenge nao mpaka waingilie mazungumzo mengine. Na kama Shetani Akikusahaulisha, basi baada ya kutanabahi usikae pamoja na watu madhalimu.

69. Wala wamchao Mungu hawana jukumu lolote kwao, lakini ni kukumbusha, asaa wapate kujiepusha”.

Mahubiri (Daawa) ni Muongozo Usio na Kulazimishana.

Allah تعالى Anasema;

وَكَاذِبٌ بِهِ

“Wameikanusha”. Qur'an, uwongofu na maelezo yaliyo dhahiri, uliyokuja nayo (ewe Muhammad) kwao.

وَهُوَ الْحَقُّ

“...nayo ni Haki”. Ambayo haiko Haki nyingine nyuma yake.

قُلْ لَسْتُ عَلَيْكُمْ بِوَكِيلٍ

“Sema: Mimi sikuwakilishwa juu yenu”

Maana yake: Si mlinzi juu yenu, wala mimi si mwangalizi wenu. Ni sawa na Kauli Yake nyingine;

وَقُلِ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكُمْ ۗ فَمَنْ شَاءَ فَلْيُؤْمِنْ وَمَنْ شَاءَ فَلْيُكْفُرْ

“Na sema: Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae”.

Inamaanisha, majukumu yangu ni kuufikisha ujumbe, na wajibu kwenu ni kuusikiliza na ta'a. Watakaonifuata watafurahi duniani na Akhera. Watakaonikhalifu watakuwa wanyonge duniani na Akhera. Na kwa sababu hiyo Allah تعالى Alisema;

لِكُلِّ نَبِيٍّ مُّسْتَقَرٌّ

“Kila khabari ina kipindi chake”. Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na wengine wengi walisema kuwa maana yake ni kila habari ina uhakika, yaani kheri itatokea, hata kama ni baadaye. Allah تعالى Alisema katika Kauli Yake nyingine;

وَلَتَعْلَمَنَّ تَبَاهُ بَعْدَ حَيْبٍ ﴿٦٦﴾

“Na bila ya shaka Mtajua khabari zake baada ya muda”. (38:88)

na,

لِكُلِّ أَجَلٍ كِتَابٌ

“Kila kipindi kina hukumu yake”. (13:38)

Hili ni onyo na ahadi ambayo haina shaka itatukia. Kwa sababu hii Allah تعالى Alisema;

وَسَوْفَ تَعْلَمُونَ

“Nanyi mtakuja jua.” Na Kauli Yake:

وَإِذَا رَأَيْتَ الَّذِينَ يَخُوضُونَ فِي آيَاتِنَا

“Na unapowaona wanaoziingilia Aya zetu”. Maana yake: Kwa kukanusha na kudhihaki.

Marufuku ya Kukaa pamoja na Watu Wanaozikejeli Aya za Allah تعالى

فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ حَتَّىٰ يَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ ۗ

“...basi jitenge nao mpaka waingilie mazungumzo mengine”.

Maana yake: Mpaka waingie katika maneno yasiyokuwa yale waliyokuwa nayo katika kukadhibisha.

وَأِمَّا يُنَسِّئَنَّكَ الشَّيْطَانُ

“Na kama Shetani Akikusahaulisha”.

Na kusudio lake ni kila mmoja katika umma, kwamba asiketi pamoja na wakadhibishaji wanaobadili Ayah za Allah تعالى na kuziweka mahali pasipostahiki. Ikiwa mtu mmoja wapo atasahau na akakaa nao,

فَلَا تَقْعُدْ بَعْدَ الذِّكْرِ

“...basi baada ya kutanabahi usikae”. Baada ya kukumbuka.

مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ

“...pamoja na watu madhalimu”. Imepokewa *Hadith* kuhusu jambo hili.

رُفِعَ عَنِ أُمَّتِي الْخَطَأَ وَالنَّسْيَانَ وَمَا اسْتَكْرَهُوا عَلَيْهِ

“Umma wangu umesamehewa makosa yasiyo ya kukusudiwa, kusahau na waliyoshurutishwa”¹.

Aya hii (6:68) ndiyo iliyooneshwa katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَقَدْ نَزَّلَ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتَابِ أَنْ إِذَا سَمِعْتُمْ آيَاتَ اللَّهِ يُكْفَرُ بِهَا وَيُسْتَهْزَأُ بِهَا فَلَا تَعْبُدُوا
مَعَهُمْ حَتَّى تَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ ۚ إِنَّكُمْ إِذَا مِثَلْتُمْ^٤

“Naye Amekwisha Kuteremshieni katika Kitabu hiki ya kwamba mnaposikia Ayah za Mwenyezi Mungu zinakanushwa na zinafanyiwa kejeli, basi msikae pamoja nao, mpaka waingie katika mazungumzo mengine. Hivyo mtakuwa nanyi mfano wao hao”.
(4:140)

Maana yake: Iwapo mtakaa nao na mkawakubalia wanayoyasema, mtakuwa sawa nao katika hayo wanayoyasema. Na Kauli Yake;

وَمَا عَلَى الَّذِينَ يَتَّقُونَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ

“Wala wamchao Mungu hawana jukumu lolote kwao”.

Ina maana: Kama watajiepusha nao, kwa kutokukaa nao watakuwa wamejiweka salama dhidi yao, na wamejiokoa na dhambi zao. Kauli ya Allah تعالى:

وَلَكِنْ ذُكِّرُوا لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

“...lakini ni kukumbusha, asaa wapate kujiepusha”.

Maana yake: Bali Tulikuamuruni mjitenge nao kwa wakati huo ili kuwakumbusha makosa waliyo nayo, asaa wataiacha tabia hiyo na kukoma kufanya hivyo tena.

وَذَرِ الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَهُمْ لِبَآءٍ وَلَهُوَ أَلْحَقُهُمْ أَحْيَاؤُهُمُ الدُّنْيَا ۖ وَذُكِّرُوا بِمَا كَانُوا يُفْسِدُونَ ۚ بِمَا كَسَبَتْ لَيْسَ لَهَا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ ۚ وَإِنْ تَعَدَلْ كُلٌّ عَدْلًا لَأُتَّخَذَ مِنْهَا أُوتِيكَ الَّذِينَ أُبْسِلُوا بِمَا كَسَبُوا ۗ لَهُمْ شَرَابٌ مِنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٦٨﴾

﴿٦٨﴾ كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٦٨﴾

¹ Ibn Majah 1:659.

70. Waachilie mbali walioifanya dini yao ni mchezo na pumbao, na uhai wa dunia ukawaghuri. Nawe kumbusha kwayo, isije nafsi ikaangamizwa kwa sababu ya iliyoyachuma, nayo haina mlinzi wala mwombezi ila Mwenyezi Mungu. Na ingalitoa kila fidia haitakubaliwa. Hao ndio walioangamizwa kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Wao watapata kinywaji cha maji ya moto kabisa, na adhabu chungu kwa yale waliyokufuru”.

Allah تعالیٰ Anasema;

وَذَرِ الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَهُمْ لَعِبًا وَلَهْوًا وَعَرَّتْهُمْ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا

“Waachilie mbali walioifanya dini yao ni mchezo na pumbao, na uhai wa dunia ukawaghuri”.

Maana yake: Waachilie, uwape mgongo, wape muda, kwani muda mchache baadae, watapata adhabu kubwa. Kwa sababu hii, Alisema;

وَذَكِّرْ بِهِ

“Nawe kumbusha kwayo” Maana yake: Kuwakumbusha watu kwa kuitumia Qur'an hii, na uwaonye juu ya hasira ya Allah تعالیٰ na adhabu iumizayo, Siku ya Kiyama. Na Kauli Yake;

أَنْ تُبْسَلَ نَفْسٌ بِمَا كَسَبَتْ

“...isije nafsi ikaangamizwa kwa sababu ya iliyoyachuma”.

Adh-Dhahhak amesema kutoka kwa Ibn 'Abbas, Mujahid na 'Ikrimah, Hasan na As-Suddi رضي الله عنهم kuwa wamesema, *tubsala* maana yake “ijisalimishe”¹. Al-Walibi alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema maana yake ni, “iwekwe wazi”². Qatadah amesema maana yake, “imezuiliwa”³. Murrah na Ibn Zaid walisema, “kuchukuliwa”⁴. Al-Kalbi amesema, maana yake ni, “kulipwa fidia”⁵. Maneno na maelezo haya yote yana maana zinazokaribiana sana kwa kuwa yote yana maanisha ni kutaka amani dhidi ya kujiweka wazi kwa ajili ya

¹ At-Tabari 11:443.

² At-Tabari 11:443.

³ At-Tabari 11:443.

⁴ At-Tabari 11:443.

⁵ At-Tabari 11:444.

maangamizo, kutengwa na mambo ya kheri na kuwekewa kizuizi dhidi ya kupata matilaba. Ni sawa na Kauli Yake;

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ۖ إِلَّا أَسْحَبَ الَّتِي مِن ۖ

“Kila nafsi imo rahanini kwa mabaya iliyoyachuma. Isipokuwa watu wa kuliani”. (74:38-39)

Kauli Yake;

لَيْسَ هَآءَا مِن دُونِ اللَّهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ

“...nayo haina mlinzi wala mwombezi ila Mwenyezi Mungu”.

Allah تعالى Alisema;

وَإِن تَعَدَلْ كُلٌّ عَدْلٍ لَّا يُؤْخَذُ مِنْهَا

“Na ingalitoa kila fidia haitakubaliwa”.

Maana yake: Hata kama itatoa chochote, haitakubaliwa. Ni kama Kauli Yake nyingine;

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِمْ مِلَّةٌ الْأَرْضِ ذَهَبًا

“Hakika wale waliokufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangelitoa”. (3:91)

Hali kadhalika, Allah تعالى Alisema hapa;

أُولَئِكَ الَّذِينَ أُبْسِلُوا بِمَا كَسَبُوا لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ

“Hao ndio walioangamizwa kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Wao watapata kinywaji cha maji ya moto kabisa, na adhabu chungu kwa sababu ya kukufuru kwao”.

* * *

قُلْ أَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُنَا وَلَا يَضُرُّنَا وَتُرْدُ
 عَلَيَّ أَعْقَابِنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا اللَّهُ كَالَّذِي آسْتَهْوَتْهُ
 الشَّيَاطِينُ فِي الْأَرْضِ حَيْرَانَ لَهُ أَصْحَابٌ يَدْعُونَهُ إِلَى
 الْهُدَى آتَيْنَا قُلْ إِنَّ هُدَى اللَّهِ هُوَ الْهُدَى وَأْمُرْنَا
 لِنُسَلِّمَ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧١﴾ وَأَنْ أَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتَقُواهُ
 وَهُوَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٧٢﴾ وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ وَيَوْمَ يَقُولُ كُنْ
 فَيَكُونُ قَوْلُهُ الْحَقُّ وَلَهُ الْمُلْكُ يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ
 عِلْمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ﴿٧٣﴾ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ ﴿٧٤﴾ *
 وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ إِذْ أَرَّأْتَنِي تَعْبُدُ آلِهَةً
 دُونِ اللَّهِ وَقَوْمَكَ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٧٥﴾ وَكَذَلِكَ نُرِي
 إِبْرَاهِيمَ مَلَكُوتَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلِيَكُونَ مِنَ الْمُوقِنِينَ
 ﴿٧٦﴾ فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ اللَّيْلُ رَأَى كَوْكَبًا ﴿٧٧﴾ قَالَ هَذَا رَبِّي
 فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَا أُحِبُّ الْآفَلِينَ ﴿٧٨﴾ فَلَمَّا رَأَى الْقَمَرَ
 بَازِعًا قَالَ هَذَا رَبِّي فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَيْنَ لَمْ يَهْدِنِي رَبِّي
 لَأَكُونَنَّ مِنَ الْقَوْمِ الضَّالِّينَ ﴿٧٩﴾ فَلَمَّا رَأَى الشَّمْسَ
 بَازِعَةً قَالَ هَذَا رَبِّي هَذَا أَكْبَرُ فَلَمَّا أَفَلَتْ قَالَ يَنْفَوِّرُ
 إِنِّي بِرَبِّيٍّ مِمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٨٠﴾ إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي
 فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا ﴿٨١﴾ وَمَا أَنَا مِنَ
 الْمُشْرِكِينَ ﴿٨٢﴾

قُلْ أَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا
 يَنْفَعُنَا وَلَا يَضُرُّنَا وَتُرْدُ عَلَيَّ
 بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا اللَّهُ كَالَّذِي
 الشَّيَاطِينُ فِي الْأَرْضِ حَيْرَانَ لَهُ
 أَصْحَابٌ يَدْعُونَهُ إِلَى الْهُدَى
 قُلْ إِنَّ هُدَى اللَّهِ هُوَ الْهُدَى
 وَأْمُرْنَا لِنُسَلِّمَ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧١﴾
 وَأَنْ أَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتَقُواهُ
 وَهُوَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٧٢﴾
 وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ
 بِالْحَقِّ وَيَوْمَ يَقُولُ كُنْ فَيَكُونُ
 قَوْلُهُ الْحَقُّ وَلَهُ الْمُلْكُ يَوْمَ
 يُنْفَخُ فِي الصُّورِ عِلْمُ الْغَيْبِ
 وَالشَّهَادَةِ ﴿٧٣﴾ وَهُوَ الْحَكِيمُ
 الْخَبِيرُ ﴿٧٤﴾

**71. Sema: Je tumuombe
 asiyekuwa Mwenyezi
 Mungu ambae hatunufaishi
 Mungu ambaye hatudhuru, na turejee
 nyuma baada ya Mwenyezi
 Mungu kuishatuhidi? Tuwe
 kama ambao mashetani
 wamempumbaza katika
 ardhi, amebabaika? Anao**

marafiki wanaomuita aende kwenye uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu. Nasi tumeamrisha tusilimu kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote,

72. Na mshike Sala, na Mcheni Yeye, na Kwake Yeye ndiko mtakokusanywa.

73. Naye Ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi kwa Haki. Na siku Ataposema: Kuwa! Basi itakuwa. Kauli yake ni Haki. Na Ufalme wote ni Wake Siku litapopulizwa baragumu, Mjuzi wa yaliyofichikana na yanayoonekana. Naye Ndiye Mwenye Hikima na Mwenye Khabari”.

Mfano wa Mwenye Kurejea Kwenye Ukafiri Baada ya Kuwa na Imani na Matendo Mema.

As-Suddi alisema, “Baadhi ya washirikina waliwaambia Waislamu: “Ifuateni njia yetu na muitelekeze dini ya Muhammad”.

Allah تعالی Akateremsha;

قُلْ أَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُنَا وَلَا يَضُرُّنَا وَنُرَدُّ عَلَىٰ أَعْقَابِنَا

“Sema: Je tumuombe asiyekuwa Mwenyezi Mungu ambae hatufai wala hatudhuru, na turejee nyuma”

Maana yake: Katika ukafiri.

بَعْدَ إِذْ هَدَيْنَا اللَّهَ

“...baada ya Mwenyezi Mungu kuishatuhidi?”

Tukifanya hivyo, mfano wetu utakuwa ni wa ambaye mashetani wamempumbaza na akawa mzururaji ardhini.

Allah تعالی Anasema, mfano wenu iwapo mtakufuru baada ya kuamini, ni mfano wa mtu aliyetoka pamoja na watu njiani, akapotea njia, na mashetani wamempumbaza na kuwa mzururaji ardhini. Wakati huo huo jamaa zake walioko njiani, wakawa wanamuita na kumuambia, “Rudi, sisi tuko katika njia”. Na yeye akakataa kuwaendea. Mfano huo ndio unaopigwa kwa anayewafuata Makafiri baada ya kumtambua Muhammad ﷺ, na Muhammad ﷺ ndiye

anayewalingania waende katika njia, na njia hiyo ni Uislamu". Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliyanukuu maelezo haya¹. Na Kauli Yake;

كَالَّذِي أَسْتَهْوَتْهُ الشَّيَاطِينُ فِي الْأَرْضِ

"...kama ambao mashetani wamempumbaza katika ardhi".

Hayo ni mazimwi.

يَدْعُونَهُ

"...wanaomuita". Kwa jina lake na la baba au babu yake, naye anayafuata na kudhania kwamba yuko katika uwongofu. Hivyo, anaitikia wito wa mashetani. Asubuhi atajikuta kuwa wamemuangamiza, au pengine wamemla, au wanaweza kumtupa katika ardhi kame ambako ataangamia kwa kiu. Huu ndio mfano wa mwenye kuitikia miungu inayoabudiwa badala ya Allah تعالى. Ameinukuu Ibn Jarir رحمه الله تعالى². Na kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

قُلْ إِنْ هَدَىٰ اللَّهُ هُوَ الَّذِي هُوَ أَلْهَدَىٰ

"Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu".

Ni sawa na Kauli Yake nyingine;

وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُضِلٍّ

"Na ambaye Mwenyezi Mungu Anamuongoa hana wa kumpotoa".

Na,

إِنْ تَحَرَّصَ عَلَىٰ هُدَاهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ يُضِلُّ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿١٦﴾

"Hata ukiwa na pupa ya kutaka kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Hamuongoi yule anayeshikilia kupotea. Wala hawatapata wa kuwanusuru". (16:37)

Kauli ya Allah تعالى;

وَأْمُرْنَا لِنُسَلِّمَ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ

"Nasi tumeamrisha tusilimu kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote".

Tumuabudu kwa *Ikhlas* Yeye Peke Yake, Asiye na mshirika.

¹ At-Tabari 11:452.

² At-Tabari 11:452.

وَأَنْ أَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا زَكَاةَ

“Na mshike Sala, na Mcheni Yeye”.

Maana yake: Tumeamrisha kusimamisha Sala na kumtii Yeye katika hali zetu zote.

وَهُوَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ

“...na Kwake Yeye ndiko mtakokusanywa”.

Maana yake: Siku ya Kiyama.

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ

“Naye Ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi kwa Haki”.

Maana yake: Kwa uadilifu, basi Yeye Ndiye Aliyeziumba na Ndiye Mmiliki wa hivyo viwili, na ni Mwendeshaji wake na vilivyo baina yake.

Na Kauli Yake;

وَيَوْمَ يَقُولُ كُنْ فَيَكُونُ

“Na siku Ataposema: Kuwa! Basi itakuwa”.

Maana yake: Siku ya Kiyama ambayo Allah تعالى Ataposema, “Kuwa, basi itakuwa kwa Amri Yake kama kupepesa jicho tu, au kwa wepesi zaidi. Inaweza kukadiriwa kusema, “Na muiogope siku Ataposema kuwa, mara ikatukia”.

Ama kuhusu Kauli Yake;

خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ

“Aliyeziumba mbingu na ardhi”.

Maana yake: “Aliiumba” na siku Ataposema, “Kuwa”, na ikawa. Akataja mwanzo wa uumbaji na kurejea Kwake. Hii inanasibiana na kusema, na uikumbuke siku Ataposema, “kuwa” na ‘ikawa’.

Na Kauli Yake;

قَوْلُهُ الْحَقُّ وَلَهُ الْمُلْكُ

“Kauli Yake ni Haki. Na Ufalme wote ni Wake”.

Hizi ni sifa mbili za Mola Mlezi wa walimwengu wote.

Maelezo Kuhusu Kupulizwa Baragumu.

Kauli Yake Allah تعالیٰ;

يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ^٤**“Siku litapo pulizwa baragumu”.** Inaashiria Kauli Yake;وَيَوْمَ يَقُولُ كُن فَيَكُونُ^٥**“Na siku Ataposema: Kuwa! Basi itakuwa”.**

Pia inachukulika kwamba inamaanisha,

وَلَهُ الْمَلَأُ يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ^٤**“Na Ufalme wote ni Wake Siku litapo pulizwa baragumu”.**

Ni sawa na Kauli Yake nyingine;

لِمَنِ الْمَلِكُ الْيَوْمَ لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿٦﴾

“Ufalme ni wa nani leo? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mteza Nguvu”. (40:16) na,الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ لِلرَّحْمَنِ^٤ وَكَانَ يَوْمًا عَلَى الْكَافِرِينَ عَسِيرًا ﴿٦﴾**“Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema, na itakuwa siku ngumu kwa makafiri”.** (25:26)Neno *Sur*, lililotumika hapa lina maana ya baragumu ambalo Israafil عليه السلام atalipuliza. Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ إِسْرَافِيلَ قَدِ انْتَقَمَ الصُّورَ، وَحَتَّى جَبْهَتُهُ يَنْتَظِرُ مِنِّي يُؤَمِّرُ فَيَنْفَخُ»

“Israafil ameshalikamata baragumu mdomoni mwake, na ameliinamisha komo lake, anangojea muda atakapoamrisha, apulize”¹.Muslim ameinukuu katika *Sahih* yake². Imamu Ahmad alinukuu kwamba ‘Abdullah bin ‘Amr رضي الله عنه alisema, “Bedui aliuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Baragumu ni nini?” Akamjibu,¹ At-Tabari 5:238.² *Tufhat Al-Ahwadhi* 7:117 na Ahmad 2:162.

«قُرْآنٌ يُنْفَخُ فِيهِ»

“Ni mfano wa pembe ambayo itapulizwa ndani yake”.

* وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ ءَأَزَرَ أَتَتَّخِذُ أَصْنَامًا ءَالِهَةً إِنِّي أَرَأَيْتَ إِذْ أُرَاكَ وَقَوْمَكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٧٦﴾ وَكَذَلِكَ نُرَى إِبْرَاهِيمَ مَلَكُوتَ الْمَلَكُوتِ وَالْأَرْضِ وَلَيْكُونَ مِنَ الْمُوقِنِينَ ﴿٧٧﴾ فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ اللَّيْلُ رَأَى كَوْكَبًا ﴿٧٨﴾ قَالَ هَذَا رَبِّي فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَا أُحِبُّ الْآفَلِينَ ﴿٧٩﴾ فَلَمَّا رَأَى الْقَمَرَ بَازِعًا قَالَ هَذَا رَبِّي فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَيْنَ لَيْنَ لَمْ يَهْدِنِي رَبِّي لَأَكُونَنَّ مِنَ الْقَوْمِ الضَّالِّينَ ﴿٨٠﴾ فَلَمَّا رَأَى الشَّمْسَ بَازِعَةً قَالَ هَذَا رَبِّي هَذَا أَكْبَرُ فَلَمَّا أَفَلَتْ قَالَ يَنْفُورِ إِبْرَاهِيمُ مِمَّا تَتَّبِعُونَ ﴿٨١﴾ إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٨٢﴾

74. Na pale Ibrahim alipomuambia baba yake, Azar: Unayafanya masanamu kuwa ni miungu? Hakika mimi nakuona wewe na watu wako mmo katika upotofu uliowazi.

75. Na kadhalika Tulimuonesha Ibrahim Ufalme wa mbingu na ardhi, na ili awe miongoni mwa wenye yakini.

76. Na ulipomuingilia usiku akaona nyota, akasema: Huyu ni Mola Mlezi wangu. Ilipotua akasema: Siwapendi wanaotua.

77. Alipouona mwezi unachomoza akasema: Huyu Ndiye Mola Mlezi wangu. Ulipotua akasema: Kama Mola Mlezi wangu hakuniongoa, nitakuwa katika kaumu ya waliopotea.

78. Na alipoliona jua linachomoza akasema: Huyu Ndiye Mola Mlezi wangu. Huyu mkubwa kuliko wote. Lilipotua alisema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayoyafanyia ushirikina.

79. Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa kwa Aliyeziumba mbingu na ardhi, hanifan, wala mimi si miongoni mwa washirikina.

Waadhi wa Ibrahim عليه السلام kwa Baba Yake.

Kusudio ni kuwa Ibrahim عليه السلام alimnasihhi baba yake kuhusu ibada ya masanamu, akamzuia na kumkataza.

Kama Alivyosema Allah تعالى:

﴿ وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ ءَأَزَرَ أَتَّخِذُ أَصْنَامًا ءَالِهَةً ۗ ﴾

“Na pale Ibrahim alipomuambia baba yake, Azar: Unayafanya masanamu kuwa ni miungu?”

Maana yake: Unaabudu sanamu badala ya Allah تعالى?

﴿ إِنِّي أَرَأَيْتَ أَزْرَكَ وَقَوْمَكَ ﴾

“Hakika mimi nakuona wewe na watu wako”.

Wanaofuata njia yako.

﴿ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴾

“...mmo katika upotofu ulio wazi”.

Wanababaika hawapajui waendako, bali wapo katika visa na ujinga. Na jambo lenu kwamba liko katika ujinga na upotovu iko dhahiri kwa kila mwenye akili iliyosalimika.

Allah تعالى pia Alisema;

﴿ وَأَذْكُرُ فِي ٱلْكِتَآبِ إِبْرَاهِيمَ ءَ إِنَّهُ كَانَ صِدِّيقًا نَبِيًّا ۗ ﴾ ﴿٦٨﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ يَتَّبِعْتَنِي لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا

يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا ۗ ﴿٦٩﴾ يَتَّبِعْتَنِي قَدْ جَاءَنِي مِنَ ٱلْعِلْمِ مَا لَمْ

يَأْتِكَ فَاتَّبِعْنِي أَهْدِكَ صِرَاطًا سَوِيًّا ۗ ﴿٧٠﴾ يَتَّبِعْتَنِي لَا تَعْبُدِ ٱلشَّيْطَانَ إِنَّ ٱلشَّيْطَانَ كَانَ

لِلرَّحْمَنِ عَصِيًّا ۗ ﴿٧١﴾ يَتَّبِعْتَنِي أَنۢ أٰخَافُ أَنۢ يَمْسَكَ عَذَابِي مِنَ ٱلرَّحْمٰنِ فَتَكُونَ لِلشَّيْطٰنِ

وَلِيًّا ۗ ﴿٧٢﴾ قَالَ أَرَأَيْتَ إِنْ عَلَّمْتُكَ ٱلْحِكْمَةَ وَءَاتَيْتُكَ مَالًا كَثِيرًا وَءَسْرَفْتَهُ

﴿٧٣﴾ قَالَ سَلٰمٌ عَلَيْكَ ؕ سَأَسْتَغْفِرُ لَكَ رَبِّي إِنَّهُ كَانَ بِي حَفِيًّا ۗ ﴿٧٤﴾ وَأَعْتَرٰلَكُمْ وَمَا

تَدْعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ وَأَدْعُوا رَبِّي عَسَىٰٓ أَلَّا أَكُونَ بِدُعَآءِ رَبِّي شَقِيًّا ۗ ﴿٧٥﴾

“Na mtaje katika Kitabu Ibrahim. Hakika yeye alikuwa mkweli, Nabii. Alipomuambia baba yake: Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyokufaa chochote? Ewe baba yangu! Kwa yakini imenifikia ilimu isiyokufikia wewe. Basi nifuate mimi, nami nitakuongoza njia iliyo Sawa. Ewe baba yangu! Usimuabudu Shetani. Hakika Shetani ni mwenye kumuasi Mwingi wa Rehema. Ewe baba yangu! Hakika mimi naogopa isikupate adhabu inayotoka kwa Mwingi wa Rehema ukaja kuwa mwenziwe Shetani, (Baba) akasema: Unaichukia miungu yangu, ewe Ibrahim? Kama huachi, basi lazima nitakupiga mawe. Na niondokee mbali kwa muda! (Ibrahim) akasema: Salamun a’laika! Amani iwe juu yako! Mimi Nitakuombea msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye Ananihurumia sana. Nami najitenga nanyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Na ninamuomba Mola wangu Mlezi; asaa nisiwe mwenye kukosa bahati kwa kumuomba Mola wangu Mlezi”. (19:41-48)

Ibrahim عليه السلام aliendelea kumuombea maghufira kipindi chote cha uhai wa baba yake. Alipofariki akiwa katika ushirikina na lilipombainikia Ibrahim عليه السلام jambo hilo, aliacha kumuombea maghufira na akaacha kujihusisha naye.

Allah تعالى Alisema;

وَمَا كَانَ اسْتِغْفَارُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا عَنْ مَّوْعِدَةٍ وَعَدَّهَا إِيَّاهُ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ أَنَّهُ عَدُوٌّ
لِلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ ﴿١١٤﴾

“Wala haikuwa Ibrahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye. Lakini ilipombainikia kwamba yeye ni adui wa Mwenyezi Mungu, alijiepusha naye. Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, mnyenyekevu, mvumilivu”. (9:114)

Imethibiti katika Sahih kuwa Ibrahim عليه السلام atakutana na baba yake, Azar, Siku ya Kiyama. Azar Atamuambia: “Mwanangu! Leo sitakuasi”. Ibrahim عليه السلام atasema, “Ewe Mola wangu! Je Hukuniahidi kuwa Hutanifedhehesha Siku ya kufufuliwa? Na ni fedheha gani kubwa zaidi ya baba yangu aliyekuwa

mbali na neema?" Itasemwa, "Ewe Ibrahim! Angalia nyuma yako, mara (atamuona baba yake amegeuka na kuwa fisi dume) atakamatwa miguu yake na kutupwa katika Moto"¹.

Ishara za Upekee wa Allah تعالى; (Tawhid) Zamdhihirikia Ibrahim عليه السلام.

Kauli ya Allah تعالى;

وَكَذَلِكَ نُرَىٰ إِبْرَاهِيمَ مَلِكُوتَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

"Na kadhalika Tulimuonesha Ibrahim Ufalme wa mbingu na ardhi".
(6:75)

Maana yake: Tulimbainishia Ishara za Allah تعالى; katika Kutafakari kwake juu ya uumbaji wa mbingu na ardhi, Tulimuonesha Upweke wa Allah تعالى; katika Umiliki na Uumbaji Wake, na kwamba hakuna mola mwingine asiye kuwa Yeye, wala hakuna mola Mlezi, bali Yeye. Ni kama Kauli Yake Allah تعالى;

قُلْ أَنْظَرُوا مَاذَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

"Sema: Angalieni yaliyomo mbinguni na kwenye ardhi!" (10:101)
na;

أَفَلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ لَفَلَسَّ بِأَنْفُسِهِمْ
الْأَرْضَ أَوْ لَمْ يَنْظُرُوا إِلَىٰ مَا فِي السَّمَاءِ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّكُلِّ عَبْدٍ مُّنِيبٍ ﴿١٠١﴾

"Kwani hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao ya mbingu na ardhi? Tungelipenda Tungeliwadidimiza ndani ya ardhi, au Tungeliwateremshia juu yao vipande vya mbingu. Hakika katika haya zipo Ishara kwa kila mja aliyetubia". (34:9)

Kauli Yake Allah تعالى;

فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ اللَّيْلُ

"Na ulipomuingilia usiku". Ulipomfunika kwa giza na kumsitiri.

¹ Fat'hul Al-Bari 6:445. Kuna sababu nyingi zinazoelezewa kwa ajili ya tukio hili, mojawapo ni kwamba, Ibrahim عليه السلام hatojisikia fedheha kwa kumuona fisi aliyetapaa Kinyesi akitupwa Motoni, na kuwa haya yanamstahiki baba yake. Angalia rejea iliyotolewa kwa ajili ya maelezo zaidi.

رَأَى كَوْكَبًا^ط

"...akaona kaukab". Maana yake: Nyota.

قَالَ هَذَا رَبِّي^ط فَلَمَّا أَفَلَ

"...akasema: Huyu ni Mola Mlezi wangu. Ilipotua".

Maana yake: Ilipopotea, alisema;

لَا أَحِبُّ الْآفِلِينَ

"Siwapendi wanaotua".

Qatadah alisema, alijua kuwa Mola wake ni wa daima, na kamwe haondoki.¹

فَلَمَّا رَأَى الْقَمَرَ بَازِعًا قَالَ هَذَا رَبِّي^ط فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَئِن لَّمْ يَهْدِنِي رَبِّي لَأَكُونَنَّ مِنَ الْقَوْمِ الضَّالِّينَ ﴿٧١﴾ فَلَمَّا رَأَى الشَّمْسَ بَازِعَةً قَالَ هَذَا رَبِّي

"Alipouona mwezi unachomoza akasema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu. Ulipotua akasema: Kama Mola Mlezi wangu hakuniongoa, nitakuwa katika kaumu ya waliopotea. Na alipoliona jua linachomoza akasema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu".

Maana yake: Huyu Mwenye kutoa mwangaza na kupanda juu ndiye Mola wangu.

هَذَا أَكْبَرُ^ط

"Huyu mkubwa". Zaidi ya nyota na mwezi, tena ana mwangaza zaidi.

فَلَمَّا أَفَلَّتْ

"Lilipotua". Maana yake: Lilipozama.

قَالَ يَنْقُورُ إِنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٧٢﴾ إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ

"...alisema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayoyafanyia ushirikina. Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa".

Maana yake: Mimi nimeitakasa dini yangu na ibada zangu nimezifanya ziwe nyoofu.

¹ At-Tabari 11:480.

لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ

“...kwa Aliyeziumba mbingu na ardhi”.

Maana yake: Aliyeziumba na Akazianzisha bila ya kuwa na kigezo kilichosabiki.

حَنِيفًا

“...hanifan”. Katika hali ya kujiepusha na ushirikina na kushikamana na upekee wa Allah (Tauhidi) تعالى. Ndio sababu Akasema baadaye;

وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ

“...wala mimi si miongoni mwa washirikina”.

Huu Ulikuwa Mdahalo Kati ya Ibrahim عليه السلام na Watu wake, na Wala si Katika Kutafuta Uhakika wa Allah تعالى.

Wafasiri wa fani ya tafsiri ya Qur'an wametofautiana kuhusu mazungumzo ya Ibrahim عليه السلام na watu wake, je yalikuwa ni sehemu ya mtazamo wake binafsi au ni katika kuweka wazi mabaya yaliyokuwa yakifanywa na watu wake? Bin Jarir رحمه الله تعالى amesimulia kupitia njia ya Ali bin Abii Twalha kutoka kwa Ibn Abbas عليه السلام kuwa huu ulikuwa ni mtazamo binafsi wa Ibrahim عليه السلام. Na Ibn Jarir رحمه الله تعالى rai hii ameifadhilisha, kwa kutoa hoja ya Kauli Yake Allah تعالى pale aliposema, “Kama Mola Mlezi wangu Hakuniongoa.”

Ukweli ni kuwa, katika Ayah hizi, Ibrahim عليه السلام alikuwa akijadiliana na kaumu yake akijitahidi kuweka wazi, na kuwaeleza ubatilifu wa yale waliyokuwa nayo jamaa zake katika kuyaabudu masanamu na maumbile ya sayari za juu. Mwanzoni kabisa kwa baba yake, Ibrahim عليه السلام aliwaeleza watu wake kuhusu makosa yao katika kuyaabudu masanamu ya ardhini ambayo yana sura za Malaika wa mbinguni, ili wawaombe shufaa kwa Muumbaji Mkuu. Watu hao walidhani kwamba wao walikuwa dhalili mno kiasi cha kushindwa kumuabudu Allah تعالى moja kwa moja, ndiyo sababu ya kuwaabudu Malaika ili wawashufae kwa ajili ya riziki, nusura na mahitaji yao mengine. Kisha aliwaeleza makosa yao na upotevu wao katika kuyaabudu maumbile. Nazo ni sayari saba ambazo walisema kuwa ni Mwezi, Zebaki, Zuhura, Jua, Mars, Jupita na Zohari. Kati ya hizo, jua ndilo lilikuwa na mwangaza zaidi na lenye kuheshimiwa kuliko vingine, kisha mwezi, Halafu Zuhura. Mwanzoni kabisa, Ibrahim عليه السلام alithibitisha

kuwa sayari ya Zuhura haikufaa kuwa na sifa ya Uungu, kwa sababu ilikuwa ikitumika kwa kipindi na njia maalumu, haiwezi kupinda wala kuchepuka kulia wala kushoto kwa njia yake, wala haina mamlaka katika mambo yake, bali hiyo ni kiumbe chenye kutoa mwangaza Alichokiumba Allah تعالى kwa Hikima Yake kubwa. Nayo huwa inachomoza kutoka upande wa mashariki na inakwenda kwa kitambo baina ya hapo na magharibi, kisha inapotea machoni, Halafu inadhihiri katika usiku unaofuatia na kuendelea. Na hii haifai kuwa ni sifa ya Uungu. Kisha, Ibrahim عليه السلام akahamia katika kuuieleza mwezi kama alivyofanya kwa sayari. Halafu akahamia kwa suala la jua kama hivyo hivyo. Alipokamilisha uthibitisho kwamba vitu hivyo vitatu havikuwa miungu, ingawa ndivyo vitoavyo nuru inayolifikia jicho. Na Mtazamo huu unathibitishwa na hoja yenye nguvu ya aya hii.

قَالَ يَنْفَوْرٍ إِنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ

“Akasema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayoyafanyia ushirikina”. (6:78)

Maana yake: Mimi nimesalimika dhidi ya kuviabudu na dhidi ya kuwachukulia kwamba ni walinzi. Kama kweli ni waungu, basi kuleni njama dhidi yangu, wala msinicheleweshe.

إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٧٨﴾

“Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa kwa Aliyeziumba mbingu na ardhi, hanifan, wala mimi si miongoni mwa washirikina”.

Ina maana, kwa hakika, namuabudu Muumbaji wa vitu hivi, Aliyevisanii, Anayevitiisha, Anayevikadiria na Anayeviendesha Ambaye, Mkono Wake ndio Unaomiliki kila jambo, ni Muumbaji wa kila kitu, ni Mola, Mfalme na Mungu wa kila kitu. Katika Aya nyingine, Alisema;

إِنَّ رَبَّكُمْ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشَىٰ اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٩﴾

“Hakika Mola Mlezi wenu ni Mwenyezi Mungu Aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha Akakaa juu ya Kiti cha Enzi. Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua, na mwezi, na nyota zinazotumika kwa Amri Yake. Fahamuni! Kuumba na Amri ni Zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu. Mola Mlezi wa viumbe vyote”. (7:54)

Allah ﷻ Amesema kumhusu Ibrahim عليه السلام:

﴿ وَلَقَدْ آتَيْنَا إِبْرَاهِيمَ رُشْدَهُ مِن قَبْلُ وَكُنَّا بِمِمْ عَلِيمِينَ ﴿٥١﴾ إِذْ قَالَ لِأَيُّهُ وَقَوْمِهِ مَا

هَذِهِ التَّمَاثِيلُ الَّتِي أَنْتُمْ هَا عَنْكُمُونَ ﴿٥٢﴾

“Na hakika Tulikwishampa Ibrahim uwongofu wake zamani, na Tulikuwa tunamjua. Alipomuambia baba yake na watu wake: Ni nini haya masanamu mnayoyashughulikia kuyaabudu?”(21:51-52)

Kinachotiliwa nguvu katika Aya hizi ni kwamba, Ibrahim عليه السلام katika hali hizi alikuwa anawapa changamoto kaumu yake kuhusu mambo waliyokuwa nayo, miongoni mwa ushirikina, Na wala hakubuni mtazamo wake binafsi.

* * *

وَحَاجَّهُ قَوْمُهُ ۚ قَالَ أَتُحِبُّونِي فِي اللَّهِ وَقَدْ هَدَانِ ۗ وَلَا
 أَخَافُ مَا تُشْرِكُونَ بِهِ إِلَّا أَنْ يُشَاءَ رَبِّي شَيْئًا ۗ وَسِعَ رَبِّي
 كُلَّ شَيْءٍ ۗ عَلِمًا ۗ أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٨٠﴾ وَكَيْفَ أَخَافُ
 مَا أَشْرَكْتُمْ وَلَا تَخَافُونَ أَنَّكُمْ أَشْرَكْتُم بِاللَّهِ مَا لَمْ
 يُنَزَّلْ بِهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا ۚ فَأَيُّ الْفَرِيقَيْنِ أَحَقُّ بِالْأَمْنِ ۗ
 إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٨١﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا
 إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ ﴿٨٢﴾
 وَتِلْكَ حُجَّتُنَا ءَاتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَى قَوْمِهِ ۚ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ
 مَنْ نَشَاءُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٨٣﴾ وَوَهَبْنَا لَهُ
 إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۗ كُلًّا هَدَيْنَا ۗ وَنُوحًا هَدَيْنَا مِنْ قَبْلُ ۗ
 وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِ دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ وَمُوسَى
 وَهَارُونَ ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٤﴾ وَذَكَرْنَا وَيْحَ
 وَعِيسَى وَإِلْيَاسَ ۗ كُلًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٨٥﴾ وَإِسْمَاعِيلَ
 وَالْيَسَعَ وَيُوسُفَ وَلُوطًا ۗ وَكُلًّا فَضَّلْنَا عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٨٦﴾
 وَمِنَ ءَابَائِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَإِخْوَانِهِمْ ۗ وَاجْتَبَيْنَاهُمْ وَهَدَيْنَاهُمْ
 إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٨٧﴾ ذَلِكَ هُدَى اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَنْ
 يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَا كَانُوا
 يَعْمَلُونَ ﴿٨٨﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ ءَاتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَ
 وَالنَّبُوَّةَ ۗ فَإِنْ يَكْفُرْ بِهَا هُنَّ لِآءٍ فَفَدَّا بِهَا قَوْمًا لَّيْسُوا
 بِهَا بِكَافِرِينَ ﴿٨٩﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ فَبِهِدَّتْ لَهُمْ
 آفَاقُهُمْ ۗ قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۗ إِنَّ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ
 لِلْعَالَمِينَ ﴿٩٠﴾

وَحَاجَّهُ قَوْمُهُ ۚ قَالَ أَتُحِبُّونِي فِي اللَّهِ وَقَدْ هَدَانِ ۗ وَلَا
 أَخَافُ مَا تُشْرِكُونَ بِهِ إِلَّا أَنْ يُشَاءَ رَبِّي شَيْئًا ۗ وَسِعَ رَبِّي
 كُلَّ شَيْءٍ ۗ عَلِمًا ۗ أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٨٠﴾ وَكَيْفَ
 أَخَافُ مَا أَشْرَكْتُمْ وَلَا تَخَافُونَ أَنَّكُمْ أَشْرَكْتُم بِاللَّهِ مَا لَمْ
 يُنَزَّلْ بِهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا ۚ فَأَيُّ الْفَرِيقَيْنِ أَحَقُّ بِالْأَمْنِ ۗ
 إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٨١﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا
 إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ ﴿٨٢﴾
 وَتِلْكَ حُجَّتُنَا ءَاتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَى قَوْمِهِ ۚ نَرْفَعُ
 دَرَجَاتٍ مَنْ نَشَاءُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٨٣﴾

80. Na watu wake wakamhoji. Akasema: Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu, na hali Yeye Ameniongoa? Wala siogopi hao mnaowashirikisha naye, ila Mola wangu Mlezi Akipenda kitu. Mola

wangu Mlezi Amekusanya ilimu ya kila kitu. Basi je, hamkumbuki?

81. Na vipi nivikhofu hivyo mnavyovishirikisha, hali nyinyi hamkhofu kuwa nyinyi mmemshirikisha Mwenyezi Mungu na kitu ambacho hakukiteremshia uthibitisho. Basi kundi gani katika mawili haya lina haki zaidi kupata amani, kama nyinyi mnajua?

82. Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhuluma – hao ndio watakaopata amani na wao ndio walioongoka.

83. Na hizo ndizo hoja zetu Tulizompa Ibrahim kuhojiana na watu wake. Tunamnyanyua kwa vyeo Tumtakaye. Hakika Mola Mlezi wako ni Mwenye Hikima na Mwenye Ujuzi”.

Allah تعالى Anasema kwamba Khalil Wake, Mtume Ibrahim عليه السلام pindi watu wake walipomtajia shaka yao kuhusu Upweke wa Allah تعالى (Tauhidi) na wakamhoji, alisema;

أَتُحْجِرُونِي فِي آلِهِ وَقَدْ هَدَانِي

“Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu, na hali Yeye Ameniongoa?”

Maana yake: Mnahojiana nami kuhusu jambo la Allah تعالى, ilhali hapana mola wa haki wa kuabudiwa isipokuwa Yeye, na Amenionesha na Kuniongoza mpaka katika ukweli nami nikaufahamu?

Kwa hivyo, ninawezaje kuyafuata maelezo yenu yaliyopotoka na mashaka yenu batilifu?

Na Kauli ya Allah تعالى;

وَلَا أَخَافُ مَا تُشْرِكُونَ بِهِ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ رَبِّي شَيْئًا

“Wala siogopi hao mnaowashirikisha naye, ila Mola wangu Mlezi Akipenda kitu”.

Maana yake: Miongoni mwa dalili za ubatilifu wa maneno yenu ni kuhusu imani yenu, miungu yenu hii mnayoiabudu haina athari yoyote, wala mimi sikhofu wala sijali. Basi, ikiwa miungu hiyo inaweza kunidhuru, basi itumieni ushahidi dhidi yangu, wala msinikwaze, bali mniharakishie. Na kauli ya Ibrahim عليه السلام;

إِلَّا أَنْ يَشَاءَ رَبِّي شَيْعًا

"...ila Mola wangu Mlezi Akipenda kitu".

Maana yake: Allah تعالى Peke Yake Ndiye Anayesababisha manufaa na madhara.

وَسِعَ رَبِّي كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا

"Mola wangu Mlezi Amekusanya ilimu ya kila kitu".

Maana yake: Elimu ya Allah تعالى imekizunguka kila kitu, wala hakuna chochote kilichojiificha Kwake.

أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ

"Basi je, hamkumbuki?"

Yale niliyokuelezeeni, je hampati mazingatio kwamba miungu hii ni ya uwongo na kwa hivyo muache kuiabudu. Hoja hii ya Ibrahim عليه السلام inafanana na aliyoitoa Mtume Hud عليه السلام kwa watu wake, 'Ad. Allah تعالى Alilitaja tukio hili katika Kitabu Chake pindi Aliposema;

قَالُوا يَهُودُ مَا جِئْتَنَا بِبَيِّنَةٍ وَمَا نَحْنُ بِتَارِكِي آلِهَتِنَا عَنْ قَوْلِكَ وَمَا نَحْنُ لَكَ
بِمُؤْمِنِينَ ﴿٥٦﴾ إِنْ نَقُولُ إِلَّا اعْتَرْنَاكَ بِبَعْضِ آلِهَتِنَا بِسُوءٍ قَالَ إِنِّي أُشْهِدُ اللَّهَ وَآسَهِدُوكُمْ
أَنِّي بَرِيءٌ مِمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٥٧﴾ مِنْ دُونِهِ فَيَكِيدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ لَا تُنظِرُونَ ﴿٥٨﴾ إِنِّي تَوَكَّلْتُ
عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمْ ۚ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا ۚ إِنَّ رَبِّي عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٩﴾

"Wakasema: Ewe Hud! Hujatuletea dalili wazi. Wala sisi hatuiachi miungu yetu kwa kufuata kauli yako. Na wala sisi hatukuamini wewe. Sisi tunasema: Baadhi katika miungu yetu imekusibu kwa baa. Akasema: Hakika mimi namshuhudisha Mwenyezi Mungu, na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnaowafanya washirikina. Mkamuacha Yeye. Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi, na kisha msinipe muhula! Hakika mimi nimemtegemea Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye Anamuendesha Atakavyo. Hakika Mola wangu Mlezi yuko juu ya Njia Iliyonyooka".
(11:53-56)

Na kauli ya Ibrahim عليه السلام;

وَكَيْفَ أَخَافُ مَا أَشْرَكْتُمْ

“Na vipi nivikhofu hivyo mnavyovishirikisha”.

Maana: Ni kwa vipi niyakhofu masanamu haya mnavoyaabudu badala ya Allah تعالى.

وَلَا تَخَافُونَ أَنْتُمْ أَشْرَكْتُمْ بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا

“...hali nyinyi hamkhofu kuwa nyinyi mmemshirikisha Mwenyezi Mungu na kitu ambacho hakukiteremshia uthibitisho”.

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na wengine, miongoni mwa Salaf walisema, inamaanisha ushahidi¹.

Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى;

أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَعُوا لَهُمْ مِنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذُنْ بِهِ اللَّهُ

“Au hao wana miungu ya kishirikina waliowatungia dini asiyoitolea idhini Mwenyezi Mungu?” (42:21) na,

إِنْ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنْتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطَانٍ

“Hayo hayakuwa ila majina mliyowapa nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu Hakuleta uthibitisho wowote juu ya hayo”.
(53:40)

Kauli Yake;

فَأَيُّ الْفَرِيقَيْنِ أَحَقُّ بِالْأَمْنِ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

“Basi kundi gani katika mawili haya lina haki zaidi kupata amani, kama nyinyi mnajua?”

Maana yake: Ni kundi lipi lililo kwenye ukweli, wale wanaomuabudu Yule Ambaye Mkononi Mwake kuna madhara na manufaa, au wale wanaokiabudu kisichodhuru wala kunufaisha, bila ya kuwa na ithibati? Ni lipi kati ya makundi haya mawili linastahiki kusalimika dhidi ya adhabu katika Siku ya Kiyama?

¹ At-Tabari 11:491.

Allah تعالیٰ Amesema;

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ ﴿٨٧﴾

“Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhuluma – hao ndio watakaopata amani na wao ndio walioongoka”.

Maana yake: Hao wanaomuabudu Allah تعالیٰ Peke Yake bila kumshirikisha, ndio watakaosalimika katika Siku ya Kiyama, na ndio walioongoka humu duniani na Akhera.

Ushirikina Ndiyo Dhuluma Kubwa.

Al-Bukhari amemnuuu ‘Abdullah رضي الله عنه kuwa alisema, “Iliposhuka Aya,

وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ

“...na hawakuchanganya imani yao na dhuluma”.

Masahaba wa Mtume ﷺ walisema, “Ni nani katika sisi ambaye hajaidhulumu nafsi yake?” Basi Aya nyingine, ikateremka,

إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ

“Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhuluma iliyo kubwa”.¹

Imamu Ahmad amenukuu kwamba ‘Abdullah رضي الله عنه amesema, Aya,

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ

“Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhuluma”.

Ilipoteremshwa, iliwawia watu vigumu. Wakauliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Ni nani katika sisi ambaye hajaidhulumu nafsi yake?” Akawajibu;

إِنَّهُ لَيْسَ الَّذِي تَعْتَوْنَ، أَنْتُمْ تَسْمَعُوا مَا قَالَ الْعَبْدُ الصَّالِحُ

“Si hicho mnachokimaanisha, je hamjakisikia alichokisema mja (Luqman) mwema”.

¹ Fat’hul Al-Bari 8:144.

يَبْنِي لَا تُشْرِكْ بِاللَّهِ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ

“Ewe Mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu. Kwani hakika ushirikina ni dhuluma iliyo kubwa”. (31:13)¹.

Kauli ya Allah تعالى:

وَتِلْكَ حُجَّتُنَا آتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِ

“Na hizo ndizo hoja zetu Tulizompa Ibrahim kuhojiana na watu wake”.

Maana yake: Tulimuongoza kutoa hoja zake juu yao. Amesema Mujahid na wengine kwamba hilo la hoja linamaanisha Kauli ya Allah تعالى:

وَكَيْفَ أَخَافُ مَا أَشْرَكْتُمْ وَلَا تَخَافُونَ أَنَّكُمْ أَشْرَكْتُم بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ
عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا فَأَيُّ الْفَرِيقَيْنِ أَحَقُّ بِالْأَمْنِ

“Na vipi nivikhofu hivyo mnavyovishirikisha, hali nyinyi hamkhofu kuwa nyinyi mmemshirikisha Mwenyezi Mungu na kitu ambacho hakukiteremshia uthibitisho. Basi kundi gani katika mawili haya lina haki zaidi kupata amani².

Allah تعالى Alimsadikisha yeye ukweli na Akamthibitishia amani na uwongofu, Alisema;

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ

“Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhuluma – hao ndio watakaopata amani na wao ndio walioongoka”.

Baada ya hapo Akasema;

وَتِلْكَ حُجَّتُنَا آتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مِّنْ ذُنُوبِهِ

“Na hizo ndizo hoja Zetu Tulizompa Ibrahim kuhojiana na watu wake. Tunamnyanyua kwa vyeo Tumtakaye”.

¹ Ahmad 1:144.

² At-Tabari 11:505.

إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ

"Hakika Mola Mlezi wako ni Mwenye Hikima na Mwenye Ujuzi".

Yeye ni Mwenye Hikima katika Kauli na Matendo Yake, Mjuzi zaidi kuhusu wale Anaowaongoza au Kutowaongoza, hata kama zitatolewa hoja juu Yake au la. Ni sawa na Alivyosema;

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٨﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّى يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٦٩﴾

"Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwishathibitika juu yao, hawataamini. Ijapokuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyochungu". (10:96-97)

Kwa ajili hiyo, Amesema hapa;

إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ

"Hakika Mola Mlezi wako ni Mwenye Hikima na Mwenye Ujuzi".

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۗ كُلًّا هَدَيْنَا ۗ وَنُوحًا هَدَيْنَا مِنْ قَبْلُ ۗ وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِ دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ وَمُوسَى وَهَارُونَ ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٠﴾ وَزَكَرِيَّا وَيَحْيَىٰ وَعِيسَىٰ وَإِلْيَاسَ ۗ كُلًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٨١﴾ وَإِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَيُونُسَ وَلُوطًا ۗ وَكُلًّا فَضَّلْنَا عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٨٢﴾ وَمِنْ آبَائِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَإِخْوَانِهِمْ ۗ وَاجْتَبَيْنَاهُمْ وَهَدَيْنَاهُمْ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٨٣﴾ ذَلِكَ هُدَى اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٨٤﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَ وَالنَّبُوءَةَ ۗ فَإِن يُكْفَرْ بِهَا هَتُولَاءٍ ۗ فَفَقَدْ وَكَلْنَا بِهَا قَوْمًا لِّيَسُؤُوا بِهَا بِكُفْرِهِمْ ۗ أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ فَبُهْدَنُهُمْ فَقَتَلَهُ ۗ قُلْ لَّا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۗ إِن هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿٨٥﴾

84. Na Tukamtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaakub. Kila mmoja wao Tulimuongoa. Na Nuhu Tulimuongoza kabla. Na katika kizazi chake Tulimuongoza Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo Tunavyowalipa wafanyao wema.

85. Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas. Wote walikuwa miongoni mwa watu wema.

86. Na Ismail, na Al-Yasaa, na Yunus, na Lut'. Na wote Tuliwafadhilisha juu ya walimwengu wote.

87. Na kutokana na baba zao, na vizazi vyao na ndugu zao. Na Tukawateua na Tukawaongoa kwenye njia iliyonyooka.

88. Hiyo ni Hidaya ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo Humhidi Amtakaye katika waja Wake. Na lau wangelimshirikisha yangeli-waharibikia waliyokuwa wakiyatenda.

89. Hao ndio Tuliowapa Vitabu na hukumu na Unabii. Ikiwa hawa watayakataa hayo, basi Tumekwisha yawakilisha kwa watu wasioyakataa.

90. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu Amewahidi. Basi fuata hidaya yao. Sema: Mimi sikuombeni ujira. Haya hayakuwa ila ni mawaidha kwa walimwengu wote".

Ibrahim عليه السلام Anapokea Khabari za Kutunukiwa Is-haq عليه السلام na Yaqub عليه السلام Uzeeni Kwake.

Allah تعالى Anasema kuwa Yeye Alimtunuku Ibrahim عليه السلام (mtoto) Is-haq عليه السلام baada ya kufikia uzeeni na kukosa matumaini ya yeye na hata mkewe Sarah kuzaa. Malaika waliokuwa wakiwaendea kaumu ya Lut عليه السلام walimjia, na wakawajulisha khabari njema Ibrahim عليه السلام na mkewe kuhusu kumzaa Is-haq عليه السلام. Mke wa Ibrahim عليه السلام alishangazwa na khabari hiyo;

قَالَتْ يَوَيْلَئِيْ ءَا۟لِدُ وَاَنَا عَجُوْزٌ وَهٰذَا بَعْلِى شَيْخًا ۗ اِنَّ هٰذَا لَشَيْءٌ عَجِيْبٌ ﴿٧٦﴾

قَالُوْۤا اَتَعْجَبِيْنَ مِنْ اَمْرِ اللّٰهِ رَحِمْتُ اللّٰهَ وَبَرَكَتُهُ عَلٰىكُمْ اَهْلَ الْبَيْتِ ۗ اِنَّهٗ حَمِيْدٌ مَّجِيْدٌ ﴿٧٧﴾

"Akasema: Je, hivyo mimi nizae, na hali yangu ni kikongwe na mume wangu huyu ni kizee? Hakika haya ni mambo ya ajabu! Wakasema: Je, unastaajabia Amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye Ndiye Msafiwa wa Kutukuzwa". (11:72-73)

Wakamjulisha hilo pamoja na kupewa kwake Utume na watoto na Wajukuu. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Alisema;

وَدَشَّرْنَاهُ بِإِسْحَاقَ نَبِيًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿١١٢﴾

“Na Tukambashiria kuzaliwa Is-haq, naye ni Nabii miongoni mwa watu wema”. (37:112)

Na hii ni bishara kamilifu zaidi na ni fadhila kubwa, na Alisema;

بِإِسْحَاقَ وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ

“(kuzaliwa) Is-haq, na baada ya Is-haq ni Yaaqub”. (11:71)

Maana yake: Mtoto huyu naye atazaa wakati wa uhai wenu (Ibrahim na Sarah), ili macho yenu yapate kufarijika naye, kama yalivyotulia kwa baba yake. Hakika, furaha kwa ajili ya mjukuu ni kubwa, kwani hii inamaanisha kuendelea kwa kizazi. Pia, kwa kuwa vikongwe kupata watoto, ilidhaniwa kuwa hawataendelea kupata vizazi kutokana na udhaifu wao. Kwa sababu hii, Allah تعالى Akatoa bishara kwa Ibrahim عليه السلام na kwa mwanaye, kwa jina, Yaaqub عليه السلام, ambalo linamaanisha “mwenendo wa kizazi”. Haya yalikuwa ni malipo kwa Ibrahim عليه السلام ambaye aliwaacha watu wake na kuondoka kutoka kwao ili aweze kumuabudu Allah تعالى Peke Yake. Allah تعالى Akambadilishia na Kumpa watu waliokuwa bora kuliko kaumu na kabila lake, kwa Kumpatia watoto wake wenyewe walio wema na wafuasi wa dini yake, ili macho yake yafarijike nao. Ni kama Alivyosema katika Aya nyingine;

فَلَمَّا أَعْرَضَهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ وَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۗ كُلًّا جَعَلْنَا نَبِيًّا ﴿١١٣﴾

“Basi alipojitenga nao na yale waliyokuwa wakiyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu, Tulimpa Is-haq na Yaaqub, na kila mmoja Tukamfanya Nabii”. (19:49) Allah تعالى Alisema hapa;

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۗ كُلًّا هَدَيْنَا ۗ

“Na Tukamtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaakub. Kila mmoja wao Tulimuongoza”.

Na Kauli Yake;

وَنُوحًا هَدَيْنَا مِن قَبْلُ ۗ

“Na Nuhu Tulimuongoza kabla”.

Maana yake: Kabla yake Tulimuongoza Nuh عليه السلام kama Tulivyomuongoza Ibrahim عليه السلام na Tukampa kizazi chema.

Sifa Makhsusi za Nuh عليه السلام na Ibrahim عليه السلام.

Kila mmoja katika Mitume hawa wawili alikuwa na sifa kubwa makhsusi. Ama kuhusu Nuh عليه السلام pindi Allah تعالى Alipowagharikisha watu wa duniani, isipokuwa waliomuamini Nuh عليه السلام na wakawa pamoja naye katika Safina, Allah تعالى Alikijaalia kizazi chake ndicho kilichosalia, basi watu wote wanatokana na kizazi hicho. Ama kuhusu Al-Khalil Ibrahim عليه السلام, Allah Hakumpeleka Mtume yeyote baada yake, bali ni kutoka katika kizazi chake.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine;

وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

“Na Tukajaalia katika dhuriya zake Unabii na Kitabu”. (29:27) na;

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا وَإِبْرَاهِيمَ وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِمَا النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

“Na bila ya shaka Tulimtuma Nuhu na Ibrahim, na Tukaweka katika dhuriya zao Unabii na Kitabu”. (57:26) na,

أُولَئِكَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ مِنْ ذُرِّيَّةِ آدَمَ وَمِمَّنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ وَمِنْ ذُرِّيَّةِ
إِبْرَاهِيمَ وَإِسْرَائِيلَ وَمِمَّنْ هَدَيْنَا وَاجْتَبَيْنَا إِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُ الرَّحْمَنِ خَرُّوا سُجَّدًا

وَبُكْيًا ﴿٢٥﴾

“Hao ndio Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii katika uzao wa Adam, na katika uzao wa wale Tuliwapandisha pamoja na Nuhu, na katika uzao wa Ibrahim na Israil, na katika wale Tuliwaongoa na Tukawateua. Wanaposomewa Ayah za Mwingi wa Rehema huanguka kusujudu na kulia”. (19:58)

Na katika Aya hii tukufu, Alisema;

وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِ

“Na katika kizazi chake”. Maana yake: Na Tuliiongoza dhuria wake.

دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ

"...Tulimuongoza Daud na Suleiman".

Kutokana na dhuria wa Nuh عليه السلام, kwa mujibu wa Ibn Jarir رحمه الله تعالى¹. Pia inawezekana kuwa Aya inamtaja Ibrahim عليه السلام kwa sababu ni yeye ndiye anayezungumziwa kupata fadhila katika maneno yaliyotangulia, ingawa Lut عليه السلام si katika uzao wa Ibrahim عليه السلام, kwani alikuwa ni mtoto wa kaka yake, Maaran bin Azar. Inawezekana kusema kwamba Lut عليه السلام alitajwa katika dhuria wa Ibrahim عليه السلام kwa ajili ya majumuisho tu.

Kama vile Allah تعالى Alivyosema;

أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْمَوْتُ إِذْ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعْبُدُونَ مِنْ بَعْدِي قَالُوا نَعْبُدُ
إِلَهَكَ وَإِلَهَ آبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِلَهُهَا وَاحِدًا وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿٨٠﴾

"Je! Mlikuwapo yalipomfikia Yaqub mauti, akawaambia Wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is-haq, Mungu Mmoja tu, na sisi tunasilimu Kwake".

Hapa, Ismail عليه السلام, ami yake Yaqub عليه السلام ameingia katika mababa wa Yaqub عليه السلام katika majumuisho. Halikadhalika, Allah تعالى Alisema;

فَسَجَدَ الْمَلَائِكَةُ كُلُّهُمْ أَجْمَعُونَ ﴿٨١﴾ إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَى أَنْ يَكُونَ مَعَ السَّاجِدِينَ ﴿٨٢﴾

"Basi Malaika wote pamoja Walimsujudia. Isipokuwa Iblisi. Yeye alikataa kuwa pamoja na waliosujudu".

Iblisi ameingizwa katika Amri ya Allah تعالى kwa Malaika kusujudu na Akamtia adabu kwa kukhalifu kwake, kwa kuwa alishabihiana nao katika hilo la kuamrisha, hivyo alijumuishwa pamoja nao, ingawa alikuwa jini, na aliumbwa kutokana na moto, ilhali Malaika waliumbwa kutokana na nuru. Kutajwa kwa Isa عليه السلام katika dhuria wa Ibrahim عليه السلام au Nuh عليه السلام, kama ilivyotajwa hapo juu ni ushahidi kwamba Wajukuu watokanao na mabinti wa mtu pia wanaingia katika dhuria wa mtu. Hii ni kwa sababu Isa عليه السلام ameingizwa katika nasaba ya Ibrahim عليه السلام kupitia kwa mama yake, kwa kuwa hakuwa na baba.

¹ At-Tabari 11:507.

Ibn Abu Hatim amemnuuu Abu Harb bin Abu Al-Aswad, "Al-Hajjaj alituma ujumbe kwa Yahya bin Ya'mar, akisema, "Niliambiwa kwamba wewe unadai Al-Hasan na Al-Husayn ni katika dhuria wa Mtume ﷺ, uliyakuta hayo katika Kitabu cha Allah ﷻ? Nimekisoma tangu mwanzo mpaka mwishoni, wala sijalikuta hilo". Yahya alisema, "Hukuisoma *Surat Al-An'am*",

وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِ دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ

"Na katika kizazi chake Tulimuongoza Daudi na Suleiman". Mpaka,

وَيَحْيَىٰ وَعِيسَىٰ

"Na Yahya na Isa". Al-Hajjaj alisema, "Ndiyo". Yahya akasema, "Je, Isa عليه السلام hakuwa katika dhuria wa Ibrahim عليه السلام ingawa hakuwa na baba?" Akasema, "Umesema kweli"¹. Minajili hii, mtu anapousia dhuria wake au anapowapa waqfu au anapotoa zawadi, watoto wa mabinti nao huingia. Lakini mtu anapowapatia kitu watoto wa kiume au akaacha waqfu kwa ajili yao, waqfu huo utakuwa mahususi kwa Wanawe wa kiume au watoto wao wa kiume. Kauli ya Allah ﷻ:

وَمِنَ آبَائِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَإِخْوَانِهِمْ

"Na kutokana na baba zao, na vizazi vyao na ndugu zao". (6:87)

Alitaja kwamba baadhi ya Mitume wa hapo awali na waliokuja nyuma yao nao waliongozwa na kuteuliwa. Kwa ajili hii, Allah ﷻ Alisema;

وَأَجْتَبَيْنَاهُمْ وَهَدَيْنَاهُمْ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

"Na Tukawateua na Tukawaongoa kwenye njia iliyonyooka".

Ushirikina Hufuta Amali, Hata za Mitume.

Kisha Alisema;

ذَٰلِكَ هُدَىٰ اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ مِن عِبَادِهِ

"Hiyo ni Hidaya ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo Humhidi Amtakaye katika waja Wake".

Maana yake: Hili liliwatokea wao kwa kuwezeshwa na Allah ﷻ na Mwongozo Wake kwao.

¹ Ad-Durr Al-Manthur 3:311.

وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Na lau wangelimshirikisha yangeliwaharibikia waliyokuwa wakiyatenda”.

Hii inalikuza jambo la hatari la ushirikina na dhambi ya kuitenda. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Alisema;

وَلَقَدْ أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكَ لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ

“Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa waliokuwa kabla yako: Bila ya shaka, ikiwa utamshirikisha Mwenyezi Mungu amali zako zitaanguka”. (39:65)

Hapa, neno “ikiwa” linamaanisha sharti, lakini halikusudii kwamba litatokea. Ni sawa na katika Kauli Yake;

قُلْ إِنْ كَانَ لِلرَّحْمَنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعَبِيدِ

“Sema: Angelikuwa Ar-Rahmaan Ana mwana, basi mimi ningelikuwa wa kwanza kumuabudu”. (43:81)

Pia ni sawa na Kauli Yake nyingine;

لَوْ أَرَدْنَا أَنْ نَتَّخِذَ هَوًا لَآتَخَذَنَّهُ مِنْ لَدُنَّا إِنَّ كُفَّاءَ فَعِيلِينَ

“Kama Tungelitaka kufanya mchezo Tungejifanyia Sisi wenyewe, lau kwamba Tungelikuwa ni wafanyao mchezo”. (21:17)

Na nyingine;

لَوْ أَرَادَ اللَّهُ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا لَاصْطَفَىٰ مِمَّا خَلَقَ مَا يَشَاءُ ۚ سُبْحٰنَهُ ۗ هُوَ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ

“Lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka kuwa na mwana, basi bila ya shaka Angeliteua Amtakaye katika Aliowaumba. Subhanahu, Ametakasika na hayo! Yeye ni Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenda Atakalo”. (39:4)

Kauli ya Allah تعالى;

أُولَئِكَ الَّذِينَ ءَاتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَ وَالنُّبُوَّةَ

“Hao ndio Tuliowapa Vitabu na hukumu na Unabii”.

Maana yake: Tuliwapa fadhila hizo kama Rehma kwa waja Wake na Ukarimu Wetu kwa viumbe.

فَإِنْ يَكْفُرْ بِهَا

"Ikiwa hawa watayakataa hayo".

Inamaanisha Utume. Pia inawezekana ikawa inakusudia mambo hayo matatu, ambayo ni Kitabu, Hukumu na Utume. Na Kauli Yake;

هَؤُلَاءِ

"Hawa". Inamaanisha watu wa Makkah, kwa mujibu wa Ibn 'Abbas, Sa'id bin Al-Musayyab, Adh-Dhahhak, Qatadah na As-Suddi na wengine ¹رضي الله عنهم.

فَقَدْ وَكَلْنَا بِهَا قَوْمًا لَّيْسُوا بِهَا بِكَافِرِينَ

"...basi Tumekwisha yawakilisha kwa watu wasioyakataa".

Maana yake: Kama Makuraishi na wengine, Waarabu na wasio Waarabu, wasio na kitabu na waliopewa kitabu, miongoni mwa wakazi wa duniani watazikataa fadhila hizi, basi Sisi Tumekwishayawakilisha kwa watu wengine, yaani Muhajirun na Answar, na wafuasi wao mpaka Siku ya Kiyama.

قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا

"Sema: Mimi sikuombeni ujira."

Hawataikataa fadhila yoyote katika hizi, hata herufi moja, bali wataziamini zote kwa pamoja, hata zile zisizo dhahiri kwa baadhi yao. Tunamuomba Allah تعالى Atujaalie tuwe miongoni mwao, kwa fadhila, ukarimu na ihsani Yake. Akimuambia Mja na Mjumbe Wake, Muhammad ﷺ, Allah تعالى Alisema;

أَوْلِيَّتِكَ

"Hao". Maana: Mitume waliotajwa, pamoja na mababa, dhuria na ndugu.

الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ

"...ndio ambao Mwenyezi Mungu Amewahidi" Maana: Hao tu ndio wenye uwongofu, si wengine.

¹ At-Tabari 11:515, 516.

فِيهِدْنُهُمْ أَقْتَدِهِۦ

“Basi fuata Hidaya yao”.

Maana yake: Uige na ufuata. Hakika, amri hii kwa Mtume ﷺ inaingia mpaka kwa umma wake, wamfuata katika sheria na amri anazowapatia. Al-Bukhari alinukuu kuhusu Aya hii, kwamba Mujahid alimuuliza Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, “Kuna sehemu katika Surat Sad ambapo sijida imethibitishwa?” Alijibu, “Ndiyo”. Kisha akasoma;

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ

“Na Tukamtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaakub”. Mpaka,

فِيهِدْنُهُمْ أَقْتَدِهِۦ

“Basi fuata Hidaya yao”.

Kisha akasema, “Yeye (Mtume wetu Muhammad ﷺ) - alikuwa miongoni mwao”. katika Riwaya nyingine, Mujahid aliongeza kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mtume wenu, Muhammad ﷺ ni miongoni mwa wale ambao imeamriwa kuwafuata”¹. Kauli ya Allah تعالى;

قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا

“Sema: Mimi sikuombeni ujira”.

Maana yake: Sikuombeni malipo yoyote minajili ya kuifikisha Qur'an hii kwenu, wala sihitaji kitu kingine chochote.

إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ

“Haya hayakuwa ila ni mawaidha kwa walimwengu wote”.

Ili iwakumbushe na kuwaongoza kutoka katika upofu kwenda katika uwongofu na kutoka katika ukafiri kwenda katika Imani.

* * *

¹ Fat'hul Al-Bari 8:144. Rejea katika Surat Sad (38) ambapo kumetajwa kuwa Dawud alisujudu. Kwa kuwa Allah تعالى Aameamuru kufuata yale yalioongozwa ndani ya Ayah hizi za Surat Al-An'am, pia ni lazima tusujudu mahali palipotajwa sijida za Mitume, kwa mujibu wa Ibn 'Abbas.

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ إِذْ قَالُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَى بَشَرٍ مِّن شَيْءٍ ۗ قُلْ مَنْ أَنْزَلَ الْكِتَابَ الَّذِي جَاءَ بِهِ مُوسَىٰ نُورًا وَهُدًى لِّلنَّاسِ ۗ تَجْعَلُونَهُ قَرَاطِيسَ تُبْدُونَهَا وَتُخْفُونَ كَثِيرًا ۗ وَعَلِمْتُمْ مَا لَمْ تَعْلَمُوا أَنْتُمْ وَلَا آبَاؤُكُمْ ۗ قُلِ اللَّهُ ثُمَّ ذَرْهُمْ فِي خَوْضِهِمْ يَلْعَبُونَ ﴿٩١﴾ وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ مُّصَدِّقُ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَلِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا ۗ وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ يُؤْمِنُونَ بِهِ ۗ وَهُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٩٢﴾ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ قَالَ أُوحِيَ إِلَيَّ وَلَمْ يُوحَ إِلَيْهِ شَيْءٌ ۗ وَمَنْ قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ ۗ وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمْرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُوا أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنفُسَكُمُ ۗ الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنْتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٩٣﴾ وَلَقَدْ جِئْتُمُونَا فُرَادَىٰ كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ ۗ وَتَرَكْتُمْ مَا خَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ ۗ وَمَا نَرَىٰ مَعَكُمْ شُفَعَاءَكُمُ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَاءُ ۗ لَقَدْ تَقَطَّعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ عَنْكُمْ مَا كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٩٤﴾

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ إِذْ قَالُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَى بَشَرٍ مِّن شَيْءٍ ۗ قُلْ مَنْ أَنْزَلَ الْكِتَابَ الَّذِي جَاءَ بِهِ مُوسَىٰ نُورًا وَهُدًى لِّلنَّاسِ ۗ تَجْعَلُونَهُ قَرَاطِيسَ تُبْدُونَهَا وَتُخْفُونَ كَثِيرًا ۗ وَعَلِمْتُمْ مَا لَمْ تَعْلَمُوا أَنْتُمْ وَلَا آبَاؤُكُمْ ۗ قُلِ اللَّهُ ثُمَّ ذَرْهُمْ فِي خَوْضِهِمْ يَلْعَبُونَ ﴿٩١﴾ وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ مُّصَدِّقُ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَلِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا ۗ وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ يُؤْمِنُونَ بِهِ ۗ وَهُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٩٢﴾

91. Na hawakumkadiria Mwenyezi Mungu kwa haki ya Kadri Yake, waliposema: Mwenyezi Mungu Haku- mteremshia mwanadamu chochote. Sema: Nani aliyeteremsha Kitabu alichokuja nacho Musa, chenye nuru na uwongofu

kwa watu, mlichokifanya kurasa kurasa mkzionesha, na mengi mkiyaficha. Na mkafunzwa mliyokuwa hamyajui nyinyi wala baba zenu? Sema: Mwenyezi Mungu. Kisha waache wacheze katika porojo lao.

92. Na hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa, chenye kuhakikisha yaliyotangulia, na ili uuonye Mama wa Miji na walio pembezoni mwake. Na wenye kuamini Akhera wanakiamini kitabu hiki, nao wanazihifadhi Sala zao.

Ubinadamu wa Mtume na Kuteremshiwa Kitabu Juu Yake.

Allah تعالى Anasema wale waliomkadhibisha Mtume Wake ﷺ, hawakumtukuza Yeye inavyostahiki. Alisema Ibn 'Abbas, Mujahid na 'Abdullah bin Kathir رضي الله عنهم, kwamba Ayah hii iliteremshwa kuwahusu Makuraishi¹.

Pia ilisemwa kuhusu kikundi cha Mayahudi.

قَالُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَيَّ بَشِيرٍ مِّنْ شَيْءٍ^١

"...waliposema: Mwenyezi Mungu Hakumteremshia mwanadamu chochote".

Allah تعالى Alisema pia;

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَى رَجُلٍ مِّنْهُمْ أَنْ أَنْذِرِ النَّاسَ

"Je! Imekuwa ajabu kwa watu kwamba Tumemfunulia mmoja wao kuwa: Waonye watu". (10:2)

Pia katika Kauli Yake;

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَنْ يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَبَعَثَ اللَّهُ بَشَرًا رَسُولًا ﴿١٧٠﴾
 قُلْ لَوْ كَانَتْ فِي الْأَرْضِ مَلَائِكَةٌ يَّمشُونَ مُطْمَئِنِّينَ لَنزَلْنَا عَلَيْهِم مِّنَ السَّمَاءِ
 مَلَكًَا رَسُولًا ﴿١٧١﴾

"Na nini kilichowazuilia watu kuamini ulipowajia uwongofu isipokuwa walisema: Je! Mwenyezi Mungu Humtuma mwanadamu kuwa ni Mtume? Sema: Ingelikuwa duniani wapo Malaika wanatembea kwa utulivu wao, basi bila ya shaka Tungeliwateremshia Malaika kuwa ni Mtume wao". (17:94-95)

¹ At-Tabari 11:524.

Allah تعالی Alisema hapa;

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِمْ إِذْ قَالُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَيْنَا بَشِيرًا مِّنْ شَيْءٍ

“Na hawakumkadiria Mwenyezi Mungu kwa haki ya Kadri Yake, waliposema: Mwenyezi Mungu Hakumteremshia mwanadamu chochote”.

Allah تعالی Aliwajibu;

قُلْ مَنْ أَنْزَلَ الْكِتَابَ الَّذِي جَاءَ بِهِ مُوسَى نُورًا وَهُدًى لِّلنَّاسِ

“Sema: Nani aliyeteremsha Kitabu alichokuja nacho Musa, chenye nuru na uwongofu kwa watu”.

Maana: Sema ewe Muhammad ﷺ, kuwaambia hawa wanaokanusha kuwa Allah تعالی hakuteremsha chochote kutoka Kwake, kwa uthibitisho wa sehemu ya kadhia katika ukanushaji wao wa hoja kwa hoja.

Allah تعالی Amesema katika kuwajibu wao.

مَنْ أَنْزَلَ الْكِتَابَ الَّذِي جَاءَ بِهِ مُوسَى

“Nani aliyeteremsha Kitabu alichokuja nacho Musa”.

Nayo ni Taurat ambayo nyote mnajua kwamba Allah تعالی Aliiteremsha kwa Musa bin 'Imraan عليه السلام, iwe nuru na uwongofu kwa watu, ili itoe mwangaza katika majibu ya mambo mbalimbali yaliyokuwa na mushkeli na kutoa mwongozo kutoka katika kiza cha yaliyo ya mashaka.

Kauli ya Allah تعالی;

تَجَعَلُونَهُ قَرَاطِيسَ تُبْدُونَهَا وَتُخْفُونَ كَثِيرًا

“...mlichokifanya kurasa kurasa mkzionesha, na mengi mkiyaficha”.

Ina maana kuwa, mmeifanya Taurati katika karatasi mbalimbali ambazo mlizinukuu kutoka katika Kitabu halisi mlichokuwa nacho na mkayabadili mambo kadha, kisha mnasema, “Haya yanatoka kwa Allah تعالی”, ilhali hayatoki kwa Allah تعالی. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema;

تَجْعَلُونَهُ قَرَاطِيسَ تُبْدُونَهَا وَتُخْفُونَ كَثِيرًا^ط

“...mlichokifanya kurasa kurasa mkzionesha, na mengi mkiyaficha”.

Na Kauli Yake;

وَعَلَّمْتُم مَّا لَمْ تَعَلَّمُوا أُنْتُمْ وَلَا ءَابَاؤُكُمْ^ط

“Na mkafunzwa mliyokuwa hamyajui nyinyi wala baba zenu?”

Maana: Ni nani aliyeiteremsha Qur'an ambamo Allah تعالى Alikufundisheni khabari za wale waliokuwepo kabla yenu na pia zijazo ambazo si nyinyi wala baba zenu mlikuwa mkizijua. Kauli ya Allah تعالى:

قُلِ اللَّهُ^ط

“Sema: Mwenyezi Mungu”.

'Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Ina maana, 'Sema, Allah تعالى Ndiye Aliyeiteremsha”.

Allah تعالى Alisema;

ثُمَّ ذَرَهُمْ فِي خَوْضِهِمْ يَلْعَبُونَ

“Kisha waache wacheze katika porojo lao”.

Maana yake: Waache wacheze katika ujahili na upotevu wao, mpaka yakini kutoka kwa Allah تعالى iwajie. Halafu watajua kwamba, mwisho mwema ni wao ama ni wa waja wa Allah تعالى wachamungu.

Na Kauli Yake;

وَهَذَا كِتَابٌ

“Na hiki ni Kitabu”. Maana yake: Qur'an.

أَنْزَلْنَاهُ مَبَارَكٌ مُّصَدِّقُ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَلِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ

“Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa, chenye kuhakikisha yaliyotangulia, na ili uuonye Mama wa Miji”.

Maana yake: Makkah.

وَمَنْ حَوَّلَهَا

"...na walio pembezoni mwake".

Miongoni mwa Waarabu na mataifa mengine ya wanaadamu, Waarabu na wasio Waarabu. Ni kama Alivyosema katika Aya nyingine;

قُلْ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

"Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote".

(7:158) Na,

لَأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

"...ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia". (6:19) Na,

يَكْفُرُ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَأَلْتَارُ مَوْعِدُهُ

"...na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao". (11:17) Na,

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿٥١﴾

"Ametukuka Aliyeteremsha Furqani kwa mja Wake, ili awe Mwonyaji kwa walimwengu wote". (25:1) Na,

وَقُلْ لِلَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْأُمِّيِّينَ أَأَسْلَمْتُمْ ؕ فَإِنْ أَسْلَمُوا فَقَدِ اهْتَدَوْا وَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ ؕ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ

"Na waambie waliopewa Kitabu na wasio na kisomo: Je! Mmesilimu? Wakisilimu basi wameongoka. Na wakikengeuka basi juu yako ni kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja Wake". (3:20)

Sahih Mbili zimenukuu kuwa Mtume ﷺ alisema;

«أَعْطَيْتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ قَبْلِي»

"Nimepewa mambo matano ambayo hakupewa yeyote katika Mitume kabla yangu".

Mtume ﷺ alilitaja jambo mojawapo kati ya hayo matano,

«وَكَانَ النَّبِيُّ يَبْتِغِي إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً، وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً»

"Kila Mtume alikuwa akipelekwa kwa watu wake makhususi, mimi nimetumwa kwa watu wote"¹.

Na kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ يُؤْمِنُونَ بِهِ^ط

"Na wenye kuamini Akhera wanakiamini "

Maana yake: Wale wanaomuamini Allah تعالى na Siku ya Mwisho, wanakiamini Kitabu hiki kilichobarikiwa, Qur'an, ambayo Tulikuteremshia, ewe Muhammad.

وَهُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ

"...nao wanazihifadhi Sala zao".

Maana yake: Wanayatekeleza yale waliyofaradhishiwa, wanasali katika wakati wake uliopangwa.

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ قَالَ أُوحِيَ إِلَيَّ وَلَمْ يُوحَ إِلَيْهِ شَيْءٌ وَمَنْ قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَوْ تَرَى إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُوا أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنْفُسَكُمْ^ط الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنْتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٩٣﴾ وَلَقَدْ جِئْتُمُونَا فُرَادَى كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَتَرَكْتُمْ مَا خَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ^ط وَمَا نَرَى مَعَكُمْ شُفَعَاءَكُمُ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَؤُا^ط لَقَدْ تَقَطَّعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ عَنْكُمْ مَا كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٩٤﴾

93. Nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu, au anayesema: Mimi nimeletewa wahyi; na hali hakuletewa wahyi wowote. Na yule anayesema: Nitateremsha kama alivyoteremsha Mwenyezi Mungu. Na lau ungeliwaona madhalimu wanavyokuwa katika mahangaiko ya

¹ Fat'hul Al-Bari 519, Muslim 1:370.

mauti, na Malaika wamewanyooshea mikono wakiwaambia: Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyo ya haki, na mliyokuwa mkizifanyia kiburi Ishara Zake.

94. Nanyi mlitujia wapweke kama Tulivyokuumbeni mara ya kwanza. Na mkayaacha nyuma yenu yote Tuli yokupeni, na wala hatuwaoni hao waombezi wenu, ambao mlidai kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu kwenu. Yamekatika mahusiano baina yenu, na yamekupoteeni mliyokuwa mkidai.

Dhalimu Mkubwa Kushinda Wote ni Anayemzushia Allah تعالی, na Kudai Kushushiwa Wahyi.

Allah تعالی Anasema;

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا

“Nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu”.

Maana yake: Hapana aliye na udhalimu mkubwa kumzidi anayemkadhibisha Yeye kwa kudai kuwa Ana washirika au mtoto, au akadai kuwa yeye ni mtume ilhali si kweli. Na kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema;

أَوْ قَالَ أُوْحِيَٰٓ إِلَىٰٓ يُوْحَٓ إِلَيْهِ شَيْءٌ

“...au anayesema: Mimi nimeletewa wahyi; na hali hakuletewa wahyi wowote”.

‘Ikrimah na Qatadah walisema; Aya hii ilishushwa kuhusu jambo la Musaylamah Al-Kaddhab¹.

وَمَنْ قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ

“Na yule anayesema: Nitateremsha kama alivyoteremsha Mwenyezi Mungu”.

¹ At-Tabari 11:533-535. “Al-Kaddhab”, maana yake mwongo. Musaylamah alidai utume zama za uhai wa Mtume ﷺ, kisha akatubu. Baada ya kufariki Mtume ﷺ, imeelezwa kwamba alirudia madai hayo au yanayofanana na hayo.

Maana yake: Au anayedai kuwa uongo wake unashindana na Wahyi uliokuja kutoka kwa Allah تعالى. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Amesema;

وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا قَالُوا قَدْ سَمِعْنَا لَوْ نَشَاءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هَذَا^١

“Na wanaposomewa Aya Zetu, wao husema: tumesikia na lau tungelipenda tungesema kama haya”. (8:31)

Hali za Madhalimu Hawa Wakati wa Kifo na Siku ya Kiyama.

Kauli ya Allah تعالى;

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ

“Na lau ungelibaona madhalimu wanavyokuwa katika mahangaiko ya mauti”.

Maana yake: Ugumu, maumivu na mateso.

وَأَلْمَلَيْكَةَ بَاسِطُوا أَيْدِيهِمْ

“...na Malaika wamewanyooshea mikono yao”.

Maana yake: Kwa kuwapiga. Ni kama katika Kauli nyingine ya Allah تعالى;

لَيْنُ بَسَطْتَ إِلَىٰ يَدِكَ لِتَقْتُلَنِي

“Ukininyooshea mkono wako kuniua”. (5:28) Na,

وَيَبْسُطُوا إِلَيْكُمْ أَيْدِيهِمْ وَأَلْسِنَتِهِم بِالسُّوْءِ

“...na wanakunjulieni mikono yao na ndimi zao kwa uovu”. (60:2)

Adh-Dhahhak na Abu Swalih walisema, “Wanakunjulieni mikono yao, yaani kwa adhabu”¹. Pia ni kama Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ يَتَوَفَّى الَّذِينَ كَفَرُوا أَلْمَلَيْكَةَ يَصْرِيحُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَارَهُمْ

“Na laiti ungeliona Malaika wanapowafisha waliokufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao”. (8:50)

¹ At-Tabari 11:539.

Na kwa ajili hii, Alisema;

وَأَلْمَلَيْكَةَ بَاسِطُوا أَيْدِيَهُمْ

"...na Malaika wamewanyooshea mikono".

Maana yake: Kwa kuwapiga, mpaka roho zao ziondoke kutoka katika viwiliwili vyao. Na kwa sababu hii, Allah تعالى Alisema;

أَخْرِجُوا أَنْفُسَكُمْ

"Zitoeni roho zenu!"

Jambo hili ni kwamba, pindi kafiri anapokaribia kufa, Malaika humpa bishara ya kupewa adhabu, visasi, minyororo, Jahanamu, maji yachemkayo na Ghadhabu za Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Halafu roho yake itatawanyika ndani ya mwili wake na itaasi na kugoma kutoka. Kisha Malaika watawapiga, mpaka roho zao ziondoke kutoka katika viwiliwili vyao, huku wakiwaambia;

أَخْرِجُوا أَنْفُسَكُمْ الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ

"Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyo ya haki".

Maana yake: Leo mtafedheheshwa mpaka ukomo wake, kama mlivyokuwa mkimkadhibisha Allah تعالى na kiburi chenu cha kukataa kufuata ayah Zake na kuwafuata Mitume Wake. Kuna Hadithi *Mutawatir*¹ nyingi zinazoeleza kitu kinachowatokea Waumini na makafiri pindi wanapokufa, na tutazitaja Hadithi hizi tutakapoelezea kauli ifuatayo ya Allah تعالى;

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ

"Mwenyezi Mungu Huwathibitisha wenye kuamini kwa kauli thabiti katika maisha ya Dunia na katika Akhera." (14:27)

¹ Hadithi iliyosimuliwa kupitia njia kadha, ikiwa na wasimulizi wengi katika kila hatua ya isnadi.

Maana yake: Siku yao ya kurejea wataambiwa haya. Kama katika kauli Yake nyingine Alivyosema;

وَعَرِضُوا عَلَىٰ رَبِّكَ صَفًا لَّقَدْ جِئْتُمُونَا كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ ۗ

“Na wakahudhurishwa mbele ya Mola wako Mlezi kwa safu (wakaadhibiwa): Mmetujia kama Tulivyokuumbeni mara ya kwanza!” (18:48)

Maana yake: Kama Tulivyoanzisha Kukuumbeni, Tumekurudisheni, ingawa mlikuwa mnalikanusha hilo na kukataa uwezekano wake. Kwa hivyo hii ndiyo siku ya kufufuliwa. Na kuhusu Kauli Yake;

وَتَرَكْتُمْ مَا خَوَّلْتُمْ وِرَاءَ ظُهُورِكُمْ ۗ

“Na mkayaacha nyuma yenu yote Tuli yokupeni”. (6:94)

Miongoni mwa mali mbalimbali mlizojikusanyia katika maisha ya duniani, zote mmeziacha nyuma yenu. *Sahih* imenukuu kuwa Mtume ﷺ alisema;

«يَقُولُ ابْنُ آدَمَ مَالِي مَالِي وَهَلْ لَكَ مِنْ مَالِكَ إِلَّا مَا أَكَلْتَ فَأَنْتَيْتَ، أَوْ لَبِئْتَ فَأَبْلَيْتَ، أَوْ نَصَدَقْتَ فَأَمْضَيْتَ، وَمَا سِوَى ذَلِكَ فَذَاهِبٌ وَتَارِكُهُ لِلنَّاسِ»

“Mwanadamu anasema, “Mali yangu, mali yangu! Lakini una mali gani zaidi ya ile uliyoila na ukaimaliza, au ulichokivaa na kikachakaa, au ulichokitoa Sadaka na kikabakia (katika kumbukumbu za matendo mema)? Kisichokuwa sadaka, utapokufa, utawaachia watu”¹.

Hasan Al-Basr رحمه الله تعالى alisema, “Siku ya Kiyama, mwanadamu ataletwa akiwa dhalili kama mtoto wa kondoo. Allah تعالى Atasema, “Kiko wapi ulichokikusanya?” Atasema, “Ewe Mola wangu! Nimekikusanya na kukiacha kikiwa kamili kama kilivyokuwa”. Allah تعالى Atamuambia, “Ewe mwanadamu! Kiko wapi ulichojitangulizia nafsi yako?” Na hapo atajitambua kwamba hakujitangulizia chochote”.

Kisha Al-Hasan akasoma Aya ifuatayo;

¹ Muslim 4:2273.

وَلَقَدْ جِئْتُمُونَا فُرَادَىٰ كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَتَرَكْتُمْ مَا خَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ ۗ

“Nanyi mmetujia wapweke kama Tulivyokuumbeni mara ya kwanza. Na mkayaacha nyuma yenu yote Tuliyokupeni”.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى aliyanukuu maneno haya. Na Kauli Yake;

وَمَا نَرَىٰ مَعَكُمْ شُفَعَاءَكُمُ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَؤُا ۗ

“...na wala hatuwaoni hao waombezi wenu, ambao mlidai kuwa ni washirika”.

Huku ni kuwaadabisha na kuwakaripia makafiri juu ya yale waliyoyafanya duniani, miongoni mwa washindani wa Allah تعالى na masanamu, wakidhani kwamba hivyo vitawafaa maishani mwao na baada ya kufufuliwa kwao, ikiwa kufufuliwa kupo, kama fikra zao zilivyowatuma. Siku ya Kiyama hawatakuwa na udhuru, upotofu utawekwa dhahiri, na walivyovizua kuwa miungu vitawapotea. Allah تعالى Atawaita huku viumbe wengine wakisikiliza.

أَيْنَ شُرَكَاءِي الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ

“Wako wapi washirika Wangu ambao mlikuwa mkidai (kuwa washirika Wangu)?” (28:62)

Tena wataambiwa wao;

وَقِيلَ لَهُمْ أَنَّىٰ مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٩٢﴾ مِن دُونِ اللَّهِ هَلْ يَنْصُرُونَكُم أَوْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٩٣﴾

“Na wataambiwa: Wako wapi mlikuwa mkiwaabudu. Badala ya Mwenyezi Mungu? Je! Wanakusaidieni, au wanajisaidia wenyewe?” (26:92-93)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Aliwaambia;

وَمَا نَرَىٰ مَعَكُمْ شُفَعَاءَكُمُ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَؤُا ۗ

“...na wala hatuwaoni hao waombezi wenu, ambao mlidai kuwa ni washirika”.

Maana yake: Katika kuwaabudia. Kwa maana, nyinyi ni wabia katika ibada yao. Kisha Allah تعالى Akasema;

لَقَدْ تَقَطَّعَ بَيْنَكُمْ

"Yamekatika mahusiano baina yenu".

Pia, Aya hii husomwa kwa kumaanisha, mahusiano, ya kila namna na mafungamano yote yaliyokuwa baina yako na wao yamekatika.

وَصَلَّ عَنْكُمْ

"...na yamekupoteeni". Yameondoka.

مَا كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ

"...mliyokuwa mkidai".

Katika kuyatumaini masanamu na washindani. Ni kama Kauli nyingine ya Allah;

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأُوا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿١٦٦﴾
 وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا لَوْ أُرْسِلْنَا كَرَّةً فَنَتَّبِعُ آبَاءَ نَحْنُ كَذَلِكَ يُرِيهِمُ اللَّهُ
 أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ ۗ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ ﴿١٦٧﴾

"Waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata, na hali ya kuwa wamekwishaiona adhabu; na waliofuata watasema: Laiti tungeweza kurudi tukawakataa wao kama wanavyotukataa sisi! Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Atakavyowaonesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni". (2:166-167)

Na Amesema tena;

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠١﴾

"Basi litapolulizwa baragumu hapo hautakuwepo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana". (23:101)

Na Amesema pia;

إِنَّمَا أَخَذْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا مَّوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُ
 بَعْضُكُم بِبَعْضٍ ۗ وَبَلَّغْنَا بَعْضُكُم بَعْضًا وَمَأْوَأَتُكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُم مِّن نَّصِيرِينَ ﴿١٠٢﴾

“Hakika nyinyi mmeyashika masanamu badala ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yaliyo baina yenu katika uhai wa duniani. Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi, na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi. Na makazi yenu ni Motoni. Wala hamtapata wa kukunusuruni”. (29:25) Tena,

وَقِيلَ ادْعُوا شُرَكَاءَكُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ

“Na itasemwa: Waiteni hao miungu wa kishirikina wenu! Basi watawaita, lakini hawatawaitikia”. (28:64) pia;

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا

“Na siku Tutakapowakusanya wote, kisha Tutawaambia walioshirikisha”. (10:28)

Mpaka Kauli Yake;

وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ

“...na yote waliyokuwa wakiyazua yatawapotea”. (10:30)

* * *

* إِنَّ اللَّهَ فَالِقُ الْغَيْبِ وَالنَّوَى ^ط يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَمِيَّتِ
 وَيُخْرِجُ الْمَمِيَّتَ مِنَ الْحَيِّ ^ع ذَٰلِكُمْ اللَّهُ ^ط فَأَنَّى تُؤْفَكُونَ ﴿٩٥﴾
 فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ
 حُسْبَانًا ^ع ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٩٦﴾ وَهُوَ الَّذِي
 جَعَلَ لَكُمُ النُّجُومَ لِتَهْتَدُوا بِهَا فِي ظُلُمَاتِ اللَّيْلِ وَالْبَحْرِ ^ط قَدْ
 فَصَّلْنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٩٧﴾ وَهُوَ الَّذِي أَنشَأَكُم
 مِن نَفْسٍ وَاحِدَةٍ فَمُسْتَقَرٌّ وَمُسْتَوْدَعٌ ^ط قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ
 لِقَوْمٍ يَفْقَهُونَ ﴿٩٨﴾ وَهُوَ الَّذِي أَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً
 فَأَخْرَجْنَا بِهِ نَبَاتَ كُلِّ شَيْءٍ فَأَخْرَجْنَا مِنْهُ خَضِرًا يُخْرِجُ
 مِنْهُ حَبًّا مُتَرَاكِبًا وَمِنَ النَّخْلِ مِن طَلْعِهَا قِنْوَانٌ دَانِيَةٌ
 وَجَنَّاتٍ مِّنْ أَعْنَابٍ وَالزَّيْتُونَ وَالرُّمَّانَ مُشْتَبِهًا وَغَيْرَ
 مُتَشَبِهٍ ^ط أَنْظَرُوا إِلَى ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَيَنْعِهِ ^ع إِنَّ فِي ذَٰلِكُمْ
 لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٩٩﴾ وَجَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ آلِهِنَ
 وَخَلَقَهُمْ ^ط وَخَرَقُوا لَهُ بَنِينَ وَبَنَاتٍ بِغَيْرِ عِلْمٍ ^ع سُبْحٰنَهُ
 وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُصِفُونَ ﴿١٠٠﴾ بَدِيعُ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ^ط
 أَنَّىٰ يَكُونُ لَهُ وَلَدٌ وَلَمْ تَكُن لَّهُ صَاحِبَةٌ ^ط وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ ^ط
 وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٠١﴾

* إِنَّ اللَّهَ فَالِقُ الْغَيْبِ وَالنَّوَى ^ط
 يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَمِيَّتِ وَيُخْرِجُ
 الْمَمِيَّتَ مِنَ الْحَيِّ ^ع ذَٰلِكُمْ اللَّهُ ^ط فَأَنَّى
 تُؤْفَكُونَ ﴿٩٥﴾ فَالِقُ الْإِصْبَاحِ
 وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ
 وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ^ع ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ
 الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٩٦﴾ وَهُوَ الَّذِي
 جَعَلَ لَكُمُ النُّجُومَ لِتَهْتَدُوا بِهَا فِي
 ظُلُمَاتِ اللَّيْلِ وَالْبَحْرِ ^ط قَدْ فَصَّلْنَا
 الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٩٧﴾

95. Hakika Mwenyezi
 Mungu Ndiye Mpasuaji
 mbegu na kokwa, zika-
 chipua. Humtoa aliye hai
 kutoka maiti, naye ni
 Mtoaji maiti kutokana na
 aliye hai. Huyo Ndiye
 Mwenyezi Mungu. Basi vipi
 mnageuzwa?

96. Ndiye Anayepambazua
 mwangaza wa asubuhi; na
 Ameufanya usiku kuwa

mapumziko na utulivu, na jua na mwezi kwenda kwa hisabu. Hayo ndiyo
 makadirio ya Aliyetukuka Mwenye Nguvu, Mwenye Ujuzi.

97. Na Ndiye Aliye Kuwekeeni nyota ili mwongoke kwazo katika kiza cha bara na bahari. Hakika Tumezichambua Ishara hizi kwa watu wanaojua.

Kumjua Allah تعالى kwa Baadhi ya Ishara Zake.

Allah تعالى Anaeleza kwamba Yeye Ndiye Mpasuaji wa mbegu na kokwa, maana yake: Huipasua katika udongo, kisha mimea ya namna mbali mbali hutoka, kama vile nafaka na matunda, ya rangi tofauti tofauti, umbo na ladha.

Kwa ajili hii, Aya hii;

فَالِقُ الْخَيْبِ وَالنَّوَىٰ

“Ndiye Mpasuaji mbegu na kokwa”.

Imetafsiriwa na Kauli Yake Allah تعالى:

تُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ

“Humtoa aliye hai kutoka maiti, naye ni Mtoaji maiti kutokana na aliye hai”.

Maana yake: Yeye Hutoa mimea hai kutokana na nafaka na kokwa ambazo kama vile hazina uhai na zimekufa. Allah تعالى Alisema;

وَأَيُّهُمُ الْأَرْضُ الْمَيِّتَةُ أَحْيَيْنَاهَا وَأَخْرَجْنَا مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُونَ ﴿٣٣﴾

“Na ishara hiyo kwao – ardhi iliyokufa, nasi Tukaifufua, na Tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila!” (36:33)

Mpaka katika Kauli Yake;

وَمِنْ أَنْفُسِهِمْ وَمِمَّا لَا يَعْلَمُونَ

“...na katika nafsi zao, na katika wasivyovijua”. (36:36)

Na katika Kauli Yake;

وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ

“...naye ni Mtoaji maiti kutokana na aliye hai”.

Kuna maelezo ambayo huwa yanakaribiana katika maana, kama vile, Analeta yai kutokana na kuku, na kinyume chake. Wengine wamesema, Anamtoa mtoto

mwema kutoka kwa mtu mwovu, na kinyume chake. Na maana nyingine zinatokana na Aya.

Kisha Allah تعالى Alisema; ذَلِكُمْ اللَّهُ

“Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu”.

Maana yake: Anayeyafanya yote haya ni Allah تعالى.

فَأَنِّي تُؤفَكُونَ

“Basi vipi mnageuzwa?”

Maana yake: Ni kwa vipi mnaondoshwa katika ukweli na mnakwenda katika ubatilifu.

Kisha mnamshirikisha wengine pamoja na Allah تعالى katika ibada.

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا

“Ndiye Anayepambazua mwangaza wa asubuhi; na Ameufanya usiku kuwa mapumziko na utulivu”.

Inamaanisha kuwa Yeye Ndiye Aliyeumba mwangaza na kiza. Allah تعالى Alisema mwanzoni mwa Sura hii,

وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ

“...na Akafanya giza na mwangaza”.

Kwa hakika, Allah تعالى Huondoa giza la usiku na Kuwaletea nuru viumbe na Kuutia nuru upeo wa macho huku Akilitawanya giza na Kumaliza usiku wa giza lake nene na kuleta mchana na mwangaza wake na kung'aa kwake.

Allah تعالى Alisema; يُغْشَى اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا

“Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi”. (7:54)

Allah تعالى Anawakumbusha Uweza Wake wa kuumba vitu anuwai vyenye kutofautiana, katika kuonesha Ukuu Wake na Ukubwa wa Nguvu Zake. Ametaja kwamba Yeye Ndiye Mpasuaji wa mapambazuko na Akataja na kinyume chake, Aliposema;

وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا

"...na Ameufanya usiku kuwa mapumziko na utulivu".

Maana yake: Wenye kiza na kutanda, ili vitu vitulie. Kama Alivyosema sehemu nyingine;

وَالضُّحَىٰ ﴿١﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾

"Naapa kwa mchana! Na kwa usiku unapotanda". (93:1-2) Na,

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿١﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّىٰ ﴿٢﴾

"Naapa kwa usiku unapofunika! Na mchana unapodhihiri!" (92:1-2) Na,

وَالنَّهَارِ إِذَا جَلَّهَا ﴿٢﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا ﴿١﴾

"Na kwa mchana unapolidhihirisha! Na kwa usiku unapolifunika!" (91:3-4)

Kauli ya Allah تعالى:

وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا

"...na jua na mwezi kwenda kwa hisabu".

Maana yake: Jua na mwezi vina njia zao za kupita (mzingo) kulingana na kipindi kilichopangwa kwa utaratibu wenye usahihi wa hali ya juu, haibadiliki wala kugeuka, bali, vyote, jua na mwezi vina vituo mbalimbali vinavyopitia wakati wa kiangazi na kipupwe na kwa hivyo kuleta mabadiliko ya urefu wa usiku na mchana. Kama Alivyosema Allah تعالى:

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا وَقَدَرَهُ مَنَازِلَ

"Yeye Ndiye Aliyelijaalia jua kuwa na mwangaza na mwezi ukawa na nuru, na Akaupimia vituo". (10:5)

Pia ni sawa na Alivyosema;

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٤٠﴾

"Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupitia mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao". (36:40)

Amesema pia;

وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ وَالنُّجُومُ مَسْخَرَاتٌ بِأَمْرِهٖ

"...na jua na mwezi, na nyota zikutumikieni kwa Amri Yake". (16:12)

Kauli ya Allah تعالى;

ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ

"Hayo ndiyo makadirio ya Aliyetukuka Mwenye Nguvu, Mwenye Ujuzi".

Maana yake: Vyote vinakwenda kwa mujibu wa Amri na vipimo vya Allah تعالى. Ambaye hakuna wa kumkatalia wala kumkhalifu. Yeye ni Mjuzi wa kila kitu, na kamwe hakuna chochote kisicho katika Elimu Yake japo chenye uzito wa atomu ardhini na mbinguni. Mara nyingi Allah تعالى Anapotaja Kuumbwa kwa usiku. Mchana, jua na mwezi Anakhitimisha maelezo kwa Kutaja Utukufu Wake na Elimu Yake.

Ni kama Alivyofanya katika Aya ifuatayo;

وَأَيُّهُمُ اللَّيْلُ نَسَلَخُ مِنْهُ النَّهَارَ فَإِذَا هُم مُّظْلَمُونَ ﴿٣٧﴾ وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَّهَا

ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٣٨﴾

"Na usiku ni Ishara kwao. Tunauvua humo mchana, mara wao wanakuwa gizani. Na jua linakwenda kwa kiwango chake. Hayo ni makadirio ya Mwenye Nguvu, Mwenye Kujua". (36:37-38)

Na Alipotaja mbingu na vilivyomo, mwanzoni mwa Surat Ha-Mim As-Sajdah, Alisema;

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ النُّجُومَ لِتَهْتَدُوا بِهَا فِي ظُلُمَاتِ اللَّيْلِ وَالْبَحْرِ

"Na Ndiye Aliyekuwekeeni nyota ili mwongoke kwazo katika kiza cha bara na bahari".

Kauli Yake,

وَرَبَّنَا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصْصِيحٍ وَحِفْظٍ ۗ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ

"Na Tukaipamba mbingu ya chini kwa mataa na kwa ulinzi. Hichi ndicho kipimo cha Mwenyezi Mungu Mwenye Kujua". (41:12)

Baadhi ya *Salaf* walisema: Yeyote mwenye kuitakidi mambo yasiyokuwa matatu yafuatayo kuhusu nyota hizi, atakuwa amekosea na amemkadhibisha Allah تعالى. Kwamba Allah تعالى Alizijaalia ziwe pambo la mbingu, na vimondo vya kuwapigia mashetani, na ziwe mwongozo katika kiza cha bara na baharini.

Na Kauli Yake;

قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ

"Hakika Tumezichambua Ishara hizi".

Maana yaake: Tumezielezea na Kuzidhihirisha.

لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ

"...kwa watu wanaojua".

Maana yake: Wenye akili na wanajua haki na wanajiepusha na upotovu.

وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ فَمُسْتَقَرٌّ وَمُسْتَوْدَعٌ قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ
يَفْقَهُونَ ﴿٩٥﴾ وَهُوَ الَّذِي أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ نَبَاتَ كُلِّ شَيْءٍ
فَأَخْرَجْنَا مِنْهُ خَضِرًا نُخْرَجُ مِنْهُ حَبًّا كَثِيرًا وَمِمَّا كَسَبُوا وَنَاظُرُوكَ وَإِنَّا لَهُ لَنَاصِرُونَ
وَجَنَّاتٍ مِنْ أَعْنَابٍ وَالزَّيْتُونَ وَالزُّمَانُ مِثْلَيْهَا وَعِشْرَةَ مِثْلَيْهَا أَنْظُرُوا إِلَى ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ
وَيَنْعِمَ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكُمْ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٩٦﴾

98. Na Yeye Ndiye Aliyekuumbeni kutokana na nafsi moja. Pako pahali pa kutulia na pa kupita njia. Hakika Tumezichambua Ishara hizi kwa watu wanaofahamu.

99. Na Yeye Ndiye Anayeteremsha maji kutoka mbinguni; na kwayo Tunatoa mimea ya kila kitu. Kutokana na baadhi yao Tukatoa mimea ya kijani, Tukatoa ndani yake punje zilizopandana; na kutokana na mitende yakatoka kwenye makole yake mashada yaliyoinama, na Bustani za mizabibu na mizaituni, na makomamanga, yaliyofanana na yasiyofanana. Angalieni matunda yake yanapozaa na yakawiva. Hakika katika hayo pana Ishara kwa watu wanaoamini.

Allah تعالى Anasema;

وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ

“Na Yeye Ndiye Aliyekuumbeni kutokana na nafsi moja”.

Maana yake: Adam عليه السلام. Sawa na Alivyosema;

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَتَقْوَىٰ رَبِّكُمْ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً

“Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi Aliyekuumbeni kutokana na nafsi moja, na Akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na Akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi”. (4:1)

Kauli ya Allah تعالى;

فَمُسْتَقَرًّا وَمُسْتَوْدَعًا

“Pako pahali pa kutulia na pa kupita njia” Alisema Ibn Mas'ud, Ibn 'Abbas, Abu 'Abdur-Rahman As-Sulami, Qais bin Abu Hazim, Mujahid, 'Ata, Ibrahim An-Nakha'i, Adh-Dhahhak, Qatadah, As-Suddi, 'Ata Al-Khurasani na wengine رضي الله عنهم:

فَمُسْتَقَرًّا

“Pako pahali pa kutulia”. Maana: Ndani ya tumbo la uzazi. Wao au wengi kuliko hao, pia walisema kwamba;

وَمُسْتَوْدَعًا

“...na pa kupita njia”. Ina maana: “Katika uti wa mgongo”¹. Ibn Mas'ud رضي الله عنه na wengine wameeleza kinyume chake. Ibn Mas'ud رضي الله عنه na kundi lake tena wamesema kwamba *Mustaqar*, maana yake maisha ya humu duniani, ilhali, *Mustawda*”, maana yake ni mahali pa hifadhi baada ya kifo (kaburi). Baada ya hapo, Allah تعالى Alisema;

قَدْ فَصَّلْنَا آيَاتٍ لِقَوْمٍ يُفْقَهُونَ

“Hakika Tumezichambua Ishara hizi kwa watu wanaofahamu”.

Inarejea kwa wanaoyafahamu na kuyaelewa Maneno ya Allah تعالى na maana yake. Kauli ya Allah تعالى;

¹ At-Tabari 11:565-570.

وَهُوَ الَّذِي أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً

“Na Yeye Ndiye Anayeteremsha maji kutoka mbinguni”.

Maana yake: Kwa kipimo maalumu kama baraka na riziki kwa waja na kama njia ya Kuwaondolea dhiki na Kuyawezesha maisha ya viumbe, ni rehema ya Allah تعالیٰ kwa viumbe Wake. Kauli ya Allah تعالیٰ;

فَأَخْرَجْنَا بِهِ نَبَاتَ كُلِّ شَيْءٍ

“...na kwayo Tunatoa mimea ya kila kitu”. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالیٰ;

وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَاءِ كُلَّ شَيْءٍ حَيًّا

“Na Tukajaalia kwa maji kila kilicho hai?” (21:30)

فَأَخْرَجْنَا مِنْهُ خَضِرًا

“Tukatoa mimea ya kijani”. Maana yake: Mimea na miti ya chanikiwiti. Baada ya hapo Tunaumba ndani yake nafaka na matunda. Na kwa ajili hii, Allah تعالیٰ Alisema;

نَخْرُجُ مِنْهُ حَبًّا مُتَرَاكِبًا

“Tukatoa ndani yake punje zilizopandana”. Maana yake: Baadhi yake zimepandana na nyingine, kama vile mashuke na mfano wake.

وَمِنَ النَّخْلِ مِنْ طَلْعِهَا قِنْوَانٌ

“...na kutokana na mitende yakatoka kwenye makole yake mashada”.

Makole ya mitende.

دَائِنَةٌ

“...yaliyoinama”. Maana yake: Yako karibu na chini. Kama alivyosema ‘Ali bin Abu Twalhah Al-Walibi kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema;

قِنْوَانٌ دَائِنَةٌ

“...mashada yaliyoinama”. Maana ya mashada yaliyoinama ni mitende mifupi ambayo matawi yake yananing’inia karibu na ardhini¹. Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ aliyankuu maneno hayo. Kauli ya Allah تعالیٰ;

¹ At-Tabari 11:576.

وَجَنَّتٍ مِّنْ أَعْنَابٍ

"...na bustani za mizabibu". Maana yake: Tunatoa kutokana nayo, Bustani za mizabibu. Zabibu na tende ni matunda ya namna mbili ambayo yenye thamani kubwa kwa watu wa Al-Hijaz (Magharibi mwa Uarabuni) na pengine ndiyo yapendwayo sana duniani. Allah تعالى Amewakumbusha waja Wake kuhusu Fadhila Zake kwa Kuwapatia matunda haya ya namna mbili, ni pale Aliposema;

وَمِنْ ثَمَرَاتِ النَّخِيلِ وَالْأَعْنَابِ تَتَّخِذُونَ مِنْهُ سَكَرًا وَرِزْقًا حَسَنًا¹

"Na kutokana na matunda ya mitende na mizabibu mnatengeneza ulevi na riziki nzuri". (16:67)

Hii ilikuwa kabla ya kuharamishwa pombe. Na Amesema;

وَجَعَلْنَا فِيهَا جَنَّاتٍ مِّنْ نَّخِيلٍ وَأَعْنَابٍ

"Na Tukafanya ndani yake bustani ya mitende na mizabibu". (36:34)

وَالزُّمَّانَ مُشْتَبِهًا وَغَيْرَ مُتَشَبِهٍ²

"... na makomamanga, yaliyofanana na yasiyofanana".

Qatadah na wengine walisema, yanafanana katika majani na maumbo na yanatofautiana kwenye mnasaba wa matunda, maumbo, ladha na tabia¹.

أَنْظُرُوا إِلَى ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَيَنْعِمَهُ²

"Angalieni matunda yake yanapozaa na yakawiva".

Maana yake: Kupevuka kwa matunda. Hayo aliyasema Al-Baraa bin 'Azib, bin 'Abbas, Adh-Dhahhak, 'Ata Al-Khurasani, As-Suddi, Qatadah na wengine رضي الله عنهم². Ayah hii inamaanisha, fanyeni taamuli juu ya uwezo wa Muumbaji wa matunda hayo, Ambaye Alibadili kutokuwepo kwa matunda hayo na kuyafanya yawepo baada ya kwamba ilikuwa ni miti mikavu, na hatimaye zikawa zabibu na tende; hali kadhalika rangi mbali mbali, maumbo, ladha na harufu za kila kilichoumbwa. Ni sawa na Kauli Yake;

¹ At-Tabari 11:578.

² At-Tabari 11:582.

وَفِي الْأَرْضِ قِطْعٌ مُتَجَبَّرَةٌ وَجَنَّتْ مِّنْ أَعْتَابٍ وَرَزَعٌ وَخَيْلٌ صَيَّوَانٌ وَغَيْرُ صَيَّوَانٍ يُسْقَىٰ
بِمَاءٍ وَاحِدٍ وَنُفْضِلُ بَعْضَهَا عَلَىٰ بَعْضٍ فِي الْأَكْلِ^٤

“Na katika ardhi vimo vipande vilivyokaribiana, na zipo Bustani za mizabibu, na mimea mingine, na mitende yenye kuchipua kwenye shina moja na isiochipua kwenye shina moja, nayo inatiliwa maji yale yale. Na Tunaifanya baadhi yao bora kuliko mengine katika kula”. (13:4)

Kwa ajili hiyo Allah تعالى Alisema;

إِنَّ فِي ذَٰلِكُمْ

“Hakika katika hayo”. Enyi watu.

لَآيَاتٍ

“...pana Ishara”.

Maana yake: Dalili mbalimbali juu ya ukamilifu wa uwezo wa Muumbaji wa vitu hivi, Hekima na Rehema Zake.

لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

“...kwa watu wanao amini”.

Maana yake: Wanamuamini Allah تعالى na wanawafuata Mitume Wake.

وَجَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ الْجِنَّ وَخَلَقَهُمْ^٥ وَخَرَقُوا لَهُ بَنِينَ وَبَنَاتٍ بِغَيْرِ عِلْمٍ^٤ سُبْحٰنَهُ وَتَعٰلٰى
عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٥﴾

100. Bado wamemfanyia Mwenyezi Mungu majini kuwa washirika wake, na hali Yeye Ndiye Aliyewaumba. Na wakamzulia, bila ya ujuzi wowote, kuwa Ana wana wa kiume na wa kike. Subhanahu, Ametakasika na Ametukuka juu ya hayo wanayombandikiza nayo!.

Karipio kwa Washirikina.

Allah تعالى Anawajibu washirikina ambao wanamshirikisha katika ibada. Hao walimuabudu Allah تعالى kwa kumjumuisha na majini. Allah تعالى Ametakasika na shirki na kufuru zao. Kukisemwa, ni kwa namna gani waliwaabudu majini, ilhali wao waliabudu masanamu? Jawabu ni kwamba, wao hawakuyaabudu masanamu, bali kumetokana na utiifu kwa majini na kuwaamuru kwao hivyo. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنْ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ إِلَّا إِنْتَا وَإِنْ يَدْعُونَ إِلَّا شَيْطَانًا مَرِيدًا ﴿١١٧﴾ لَعَنَهُ اللَّهُ
وَقَالَ لَأَتَّخِذَنَّ مِنْ عِبَادِكَ نَصِيبًا مَفْرُوضًا ﴿١١٨﴾ وَلَا ضَلَّتْهُمْ وَلَا مَنِيْنَهُمْ وَلَا مَرْتَبَهُمْ
فَلْيَبْتَئِكُنَّ آذَانَ الْعَالَمِينَ وَلَا تُرَبِّهُمُ فَلْيَغَيِّرُنَّ خَلْقَ اللَّهِ وَمَنْ يَتَّخِذِ الشَّيْطَانَ وَلِيًّا
مِنْ دُونِ اللَّهِ فَقَدْ خَسِرَ خُسْرَانًا مُبِينًا ﴿١١٩﴾ يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيهِمْ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ
إِلَّا غُرُورًا ﴿١٢٠﴾

“Wao hawawaombi badala yake Yeye ila wanawake, wala hawamuombi ila Shetani aliyeasi. Mwenyezi Mungu Amemlaani. Naye Shetani alisema: Kwa yakini nitawachukua sehemu maalumu katika waja wako. Na hakika nitawapoteza na nitawatia matamania, na nitawaamrisha, basi watakata masikio ya wanyama, na nitawaamrisha, basi watabadili Aliyumba Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumfanya Shetani kuwa mlinzi wake badala ya Mwenyezi Mungu, basi huyo amekhasiri khasara ya dhahiri. Anawaahidi na anawatia tamaa. Na Shetani hawaahidi ila udanganyifu”. (4:117-120) na,

أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي

“Je! Mnamshika yeye na dhuriya wake kuwa marafiki badala Yangu”. (18:50)

Na Ibrahim عليه السلام alimuambia baba yake;

يَتَّابِتْ لَّا تَعْبُدِ الشَّيْطَانَ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلرَّحْمَنِ عَصِيًّا ﴿١٤﴾

“Ewe baba yangu! Usimuabudu Shetani. Hakika Shetani ni mwenye kumuasi Mwingi wa Rehema”. (19:44)

Ni sawa pia na Kauli ya Allah تعالى;

﴿ أَلَمْ أَعْهَدْ إِلَيْكُمْ يَبْنَىءَ آدَمَ أَن لَّا تَعْبُدُوا الشَّيْطَانَ ۖ إِنَّهُ لَكُرْمٌ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٦٦﴾ وَأَن أَعْبُدُونِي ۚ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦٧﴾ ﴾

“Je! Sikuagana nanyi, wanaadamu, kuwa msimuabudu shetani? Hakika yeye ni adui dhahiri kwenu. Na ya kwamba mniabudu Mimi? Hii ndiyo njia Iliyonyooka”. (36:60-61)

Malaika watasema katika Siku ya Kiyama;

﴿ سُبْحَانَكَ أَنْتَ وَلِيْنَا مِن دُونِهِمْ ۖ بَلْ كَانُوا يَعْبُدُونَ آلِجِنِّ أَكْثَرُهُم مِّنْ مُّؤْمِنُونَ ﴾

“Subhanak, Umetakasika. Wewe Ndiye kipenzi chetu si hao. Bali wao waikuwa wakiwaabudu majini; wengi wao wakiwaamini hao”. (34:41)

Kwa hivyo Alisema;

﴿ وَجَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ آلِجِنِّ وَخَلَقَهُمْ ﴾

“Bado wamemfanyia Mwenyezi Mungu majini kuwa washirika wake, na hali Yeye Ndiye Aliyewaumba”. (6:100)

Maana yake: Aliwaumba, kwa hivyo, Yeye Ndiye Muumbaji, Peke Yake wala hana mshirika, basi ni kwa vipi ghairi yake aabudiwe Naye pamwe? Ni sawa na kauli ya Nabii Ibrahim عليه السلام;

﴿ قَالَ أَتَعْبُدُونَ مَا تَنْحِتُونَ ﴿٦٧﴾ وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾ ﴾

“Akasema: Hivyo mnaviabudu vitu mnavyovichonga wenyewe? Na hali Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni nyinyi na hivyo mnavyovifanya!” (37:95-96)

Maana ya Aya ni kwamba, Allah تعالى Ndiye Muumbaji Pekee, na kwa hivyo, ni wajibu kumpwekesha katika ibada, Yeye Peke Yake pasi na mshirika. Kauli ya Allah تعالى;

وَحَرَقُوا لَهُم بَيْنَ وَبَيْنَ وَبَنَّتْ بِغَيْرِ عِلْمٍ

“Na wakamzulia, bila ya ujuzi wowote, kuwa Ana wana wa kiume na wa kike”.

Allah تعالى Anafahamisha kuhusu upotovu wa wapotovu kwa kusema Allah تعالى Ana mwana. Kama Wayahudi wanavyodai hayo kwa Uzayr, na maneno ya Wakristo kwa Isa عليه السلام, na yale waliyosema washirikina wa kiarabu juu ya Malaika ni wana wa Allah. Allah تعالى Yu mbali mno dhidi ya wanayoyasema. Na maana ya neno “kharqu” ni kwamba walibuni, wakazua, wakadai na wakaongopa, kwa mujibu wa wanazuoni wa *Salaf*. Na kwa ajili hii Allah تعالى Alisema;

سُبْحٰنَهُۥ وَتَعٰلٰى عَمَّا يَصِفُوۡنَ

“Subhanahu, Ametakasika na Ametukuka juu ya hayo wanayo mbandikiza nayo!”

Maana yake: Ametukuka na Ameenpukana mbali. Na Yeye ni Mkuu mno dhidi ya kuwa na wana, washindani, walinganifu na washirika kama wanavyodai hawa majahili wapotevu.

بَدِيعُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ اَنۢىۡ يَكُوۡنُ لَهُۥ وَلَدٌ وَّلَمْ تَكُنۡ لَّهٗۤ اَصْحٰبَةٌ وَّخَلَقَ كُلَّ شَيْۡءٍ ۭ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْۡءٍ عَلِيۡمٌ ﴿١٠١﴾

101. “Yeye Ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi bila ya ruwaza. Itakuwaje Awe na mwana Naye hakuwa na mke? Naye Ndiye Aliyeumba kila kitu”.

Maana ya Uumbaji Badi’

بَدِيعُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ

“Yeye Ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi”. Maana yake: Mbunifu, Muumbaji, Mwanzilishaji na Mzinduzi wake pasi na ruwaza, kwa mujibu wa Mujahid na As-Suddi. Na hii ndiyo asili ya neno linalotumika kutaja uzushi, *Bid’ah*, kwa sababu ni kitu kilichobuniwa kisichokuwa na mfano wa kuiga kwa waliotangulia.

أَنَّى يَكُونُ لَهُ وُلْدٌ وَلَمْ تَكُنْ لَهُ صَاحِبَةً

“Itakuwaje Awe na mwana Naye hakuwa na mke?”

Maana yake: Mtoto huwa anatokana na kuzaliwa na wanandoa wawili wenye kutangamana. Allah تعالى Hatangamani na kitu wala hakuna kiumbe Chake chochote kinachoshabihiana Naye, kwa sababu Yeye ni Muumbaji wa kila kitu, hivyo, Hana mke wala mwana. Sawa na Kauli Yake;

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا ﴿٨٨﴾

“Na wao ati husema kuwa Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema Ana mwana! Hakika mmeleta jambo la kuchusha mno!” (19:88-89)

Mpaka;

وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ﴿٩٥﴾

“Na kila mmoja katika wao Atamfikia Siku ya Kiyama peke yake”. (19:95)

وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“Naye Ndiye Aliyeumba kila kitu. Naye ni Mwenye Kujua kila kitu”.

Allah تعالى Amebainisha kwamba Yeye Ndiye Aliyekiumba kila kitu, na kwamba Yeye ni Mtambuzi wa kila kitu, basi Atakuwaje na mke wa kutangamana Naye? Allah تعالى Ametukuka mno dhidi ya kuwa na mwana.

* * *

ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ ۖ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۖ خَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ
 فَاعْبُدُوهُ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿١٠٢﴾ لَا تَدْرِكُهُ
 الْآبْصَارُ ۖ وَهُوَ يُدْرِكُ الْآبْصَرَ ۖ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ ﴿١٠٣﴾
 قَدْ جَاءَكُمْ بَصَائِرُ مِّن رَّبِّكُمْ ۖ فَمَن أَبْصَرَ فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَن
 عَمِيَ فَعَلَيْهَا ۗ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ ﴿١٠٤﴾ وَكَذَٰلِكَ
 نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لِيَقُولُوا دَرَسْتَ وَلِنُبَيِّنَهُ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ
 ﴿١٠٥﴾ اتَّبِعْ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِّن رَّبِّكَ ۖ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۖ
 وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٦﴾ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكُوا ۗ وَمَا
 جَعَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا ۖ وَمَا أَنتَ عَلَيْهِم بِوَكِيلٍ ﴿١٠٧﴾ وَلَا
 تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ فَيَسُبُّوا اللَّهَ عَدْوًا
 بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ كَذَٰلِكَ زَيْنَا لِكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلَهُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ
 مَرْجِعُهُمْ فَيُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٠٨﴾ وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ
 جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن جَاءَنَّهُمْ آيَةٌ لِّيُؤْمِنُوا بِهَا ۗ قُلْ إِنَّمَا
 الْآيَاتُ عِنْدَ اللَّهِ ۖ وَمَا يُشْعُرُكُمْ أَنهَآ إِذَا جَاءَتْ لَا يُؤْمِنُونَ
 ﴿١٠٩﴾ وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَرَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِآيَةِ
 مَرْقَةٍ وَنَذَرَهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ ۖ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۖ
 خَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَاعْبُدُوهُ ۗ وَهُوَ
 عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿١٠٢﴾ لَا
 تَدْرِكُهُ الْآبْصَارُ ۖ وَهُوَ يُدْرِكُ
 الْآبْصَرَ ۖ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ ﴿١٠٣﴾

102. "Huyo Ndiye Allah, Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu, hapana mungu ila Yeye, Muumba wa kila kitu. Basi muabuduni Yeye tu. Naye ni Mtegemewa wa kila kitu.

103. Macho hayamfikilii bali Yeye Anayafikilia macho. Naye ni Mjuzi, Mwenye Khabari".

Allah تعالى Ndiye Mola Wenu.

Allah تعالى Anasema;

ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ ۖ

"Huyo Ndiye Allah, Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu". Maana yake, Amekiumba kila kitu, wala Hana mwana wala mke.

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۖ خَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَاعْبُدُوهُ ۗ

"...hapana mungu ila Yeye, Muumba wa kila kitu. Basi muabuduni Yeye tu".

Yeye Peke Yake, pasi na mshirika, na kukiri Upweke na Tauhidi Yake, na kwamba hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, Hana mwana, wala mzazi, wala mithili, wala mlinganifu.

وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ

“Naye ni Mtegemewa wa kila kitu”.

Maana yake: Mwenye Kuhifadhi na Mlinzi, Anakiendesha kila kilicho ghairi yake, Anawakimu na Anawalinda usiku na mchana.

Kumuona Allah تعالى Huko Akhera.

لَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ

“Macho hayamfikilii”.

Maana yake: Hayamfikii duniani. Huko Akhera Yawezekana kumuona, kama Hadithi kadhaa kutoka kwa Mtume ﷺ zilivyothibitisha hilo, na zinapitia katika isnadi na *Sunan* za uhakika. Kama alivyosema Masruq kwamba ‘Aishah رضي الله عنها alisema, “Atakayedai kuwa Muhammad ﷺ alimuona Mola Wake atakuwa ameongopa”. Na katika Riwaya nyingine: imekuja (anaongopa dhidi ya Allah تعالى), kwani Allah تعالى Amesema;

لَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ

“Macho hayamfikilii bali Yeye Anayafikilia macho”¹.

Sahih Muslim imemnukuu Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ اللَّهَ لَا يَنَامُ وَلَا يَتَبَوَّأُ لَهُ أَنْ يَنَامَ، يَخْفِضُ الْقَسْطَ وَيَرْفَعُهُ، يُرْفَعُ إِلَيْهِ عَمَلُ النَّهَارِ قَبْلَ اللَّيْلِ، وَعَمَلُ اللَّيْلِ قَبْلَ النَّهَارِ، حِجَابُهُ الثُّورُ - أَوْ النَّارُ - نَوَّ كَشَفَهُ لِأَخْرَقَتْ سُبْحَاتُ رَجَبِهِ مَا انْتَهَى إِلَيْهِ بَصَرُهُ مِنْ خَلْقِهِ»

“Kwa hakika, Allah Huwa Halali wala Haimpasii Alale. Huwa Anateremsha chini Mizani (ya kila kitu) na Kuinyanyua. Amali za

¹ Fat'hul Al-Bari 8:472, Muslim 1:159, Tufhat Al-Ahwadhi 8:441, An-Nasai katika Al-Kubra 6335, Muslim 6:49.

mchana hupandishwa Kwake kabla ya za usiku, na amali za usiku kabla ya za mchana. Kizuizi Chake ni Nuru – au Moto – na lau kama Atakiondoa, Nuru ya Wajih Wake itateketeza kila kitu mpaka upeo wa Uoni Wake”¹.

Na katika Vitabu vilivyotangulia kuteremshwa kuna maelezo, “Allah تعالى Alimuambia Musa عليه السلام pindi alipoomba kumuona, “Ewe Musa! Hakika! Hakuna kiumbe hai kitakachomudu kuniona, isipokuwa kitakufa, wala kilicho kikavu, Ila hukiangamiza”. Na Alisema Allah تعالى;

فَلَمَّا تَخَلَّى رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكًّا وَخَرَّ مُوسَىٰ صَعِقًا فَلَمَّا أَفَاقَ قَالَ سُبْحَانَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُؤْمِنِينَ

“Basi Alipojionesha Mola Mlezi wake kwa mlima, Aliufanya uvurugike, na Musa akaanguka chini amezimia. Alipozindikana alisema: Subhanaka, Umetakasika! Natubu Kwako, na mimi ni wa kwanza wa Waumini”. (7:143)

Aya, Hadithi na maelezo haya hayakanushi ukweli kuwa Allah تعالى Ataonekana katika Siku ya Kiyama kwa waja Wake waumini kwa namna Atakayoamua Yeye, na Kuuhiifadhi Utukufu na Ukuu Wake kama Ulivyo. Ametukuka na kila jema na Ameepukana na kila upungufu, basi, kwa hakika macho hayamfikilii. Kwa ajili hii, Mama wa waumini, ‘Aishah رضي الله عنها alikuwa akithibitisha kuwa kutawezekana kumuona Allah تعالى huko Akhera, na akilikataa hilo kwa humu duniani, na aliitaja hii kama ushahidi;

لَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ

“Macho hayamfikilii bali Yeye Anayafikilia macho”.

Alichokikanusha mama Aisha رضي الله عنها, ni suala la uwezekano wa macho kumfikilia kwa maana ya kuuona Ukuu na Utukufu Wake, kama Alivyo. Hilo ni muhali kwa Malaika na viumbe wengine wote. Na kuhusu Kauli Yake;

وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ

“...bali Yeye Anayafikilia macho”

¹ Muslim 1:62.

Maana yake: Anayazingira yote na Ana Elimu kamilifu kuwahusu, kwa sababu Yeye Ndiye Aliyeumba viumbe vyote. Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine;

أَلَا يَعْلَمُ مَنْ خَلَقَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ ﴿١٠٢﴾

“Asijue Aliyeumba, Naye Ndiye Mjua Siri, Mwenye Khabari?” (67:14)

Pengine maana ya *Al-Abswaar* (macho) inarejea katika wenye kuona. Kama As-Suddi alivyoizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

لَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ

“Macho hayamfikilii bali Yeye Anayafikilia macho”.

“Hapana kinachomuona (humu duniani) lakini Yeye Anawaona viumbe wote”. Abu Al-'Aliyah ameizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ

“Naye ni Mjuzi, Mwenye Khabari”.

Kwa kusema, “Mjuzi” kwa Kuvileta vitu vyote, “Mwenye khabari” kuhusu mahali pao. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Haya ni kama Allah تعالى Alivyoizungumza Alipoeleza khabari kuhusu Luqman, juu ya aliyomuahidi mwanaye;

يَبْنِي إِبْرَاهِيمَ إِنَّ تَكُ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِنْ خَرْدَلٍ فَتَكُنْ فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي السَّمَوَاتِ أَوْ فِي الْأَرْضِ
يَأْتِ بِهَا اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿١٠٢﴾

“Ewe Mwanangu! Kikiwapo kitu cha uzito wa chembe ya khardali kikawa ndani ya jabali au ndani ya mbingu au ndani ya ardhi, basi Mwenyezi Mungu Atakileta. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyofichika, Mwenye Khabari za yote”. (31:160)

قَدْ جَاءَكُمْ بَصَائِرُ مِنْ رَبِّكُمْ ۖ فَمَنْ أَبْصَرَ فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ عَمِيَٰ فَعَلَيْهَا ۚ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِخَفِيظٍ ﴿١٠٤﴾ وَكَذَٰلِكَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ لِّدْرَسٍ ۚ وَلِتُبَيِّنَ لَهُ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿١٠٥﴾

104. Zimekwishakukujieni hoja wazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Basi anayeona ni kwa faida yake mwenyewe, na anayepofuka basi ni khasara yake. Nami si mtunzaji wenu.

105. Na namna hivyo Tunazisarifu Ayah, na wao wakwambie: Umesoma. Na ili Tuyabainishe kwa watu wanaojua.

Maana ya Al-Baswair.

Al-Baswair ni ushahidi na hoja zilizomo ndani ya Qur'an na ujumbe aliokuja nao Mtume ﷺ;

فَمَنْ أَبْصَرَ فَلِنَفْسِهِ

"Basi anayeona ni kwa faida yake mwenyewe". Sawa na Kauli Yake nyingine;

فَمَنْ آهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا

"Basi anayeongoka anaongoka kwa faida ya nafsi yake, na anayepotea anapotea kwa khasara ya nafsi yake". (10:108)

وَمَنْ عَمِيَ فَاعْلَيْهَا

"...na anayepofuka basi ni khasara yake".

Baada ya kutaja Al-Baswair, Allah تعالى Alisema;

فَإِنَّهَا لَا تَعْمَىٰ الْأَبْصُرُ وَلَكِن تَعْمَىٰ الْقُلُوبُ الَّتِي فِي الصُّدُورِ

"Kwani hakika si macho yanayopofuka, lakini zinazopofuka ni nyoyo zilizomo vifuani". (22:46)

وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ

"Nami si mtunzaji wenu". Maana yake: Si muhifadhi wala mlinzi, bali ni mfikishaji, na Allah تعالى Humhidi Amtakaye na Kumuacha apotee Amtakaye. Kauli Yake.

وَكَذَٰلِكَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ

"Na namna hivyo Tunazisarifu Ayah". (6:105)

Maana yake: Kama Tulivyofafanua Ayah mbalimbali za Sura hii katika kuelezea Tauhid, na kwamba hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, na hivi ndivyo Tunavyozidhihirisha, Tunazitafsiri na Kuzisherehi katika kila mahali ili kuondosha ujinga wa majahili, na ili washirikina na makafiri wakadhibishao waseme, "Darasta" - Ewe Muhammad umesoma na umejifunza kutoka kwa waliokuwa kabla yako miongoni mwa waliopewa Kitabu". Hivi ndivyo alivyosema Ibn 'Abbas, Mujahid, Sa'id bin Jubayr na Adh-Dhahhak na wengine

رضي الله عنهم¹. At-Tabarani ameeleza kuwa 'Amr bin Kaysan alisema alimsikia Ibn 'Abbas رضي الله عنهما². "Darasta, maana yake umesoma, umebishania, umejadiliana"². Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى katika Kuelezea ukadhibishaji na ufidhuli wao;

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّ هَذَا إِلَّا إِفْكٌ أُفْتَرْتَهُ وَأَعَانَهُ عَلَيْهِ قَوْمٌ آخَرُونَ فَقَدْ جَاءُوا ظُلْمًا
وَزُورًا ﴿٤﴾ وَقَالُوا أَسْطِيرُ الْأُولِينَ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّى عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٥﴾

"Na wamesema waliokufuru: Haya si chochote ila ni uzushi aliouzua, na wamemsaidia kwa haya watu wengine! Hakika hawa wamekuja na dhulma na uwongo. Na wakasema: Hivi ni visa vya watu wa kale alivyoviandikisha, anavyosomewa asubuhi na jioni".
(25:4-5)

Allah تعالى Anaelezea madai yao na uongo wao, Kauli ya Allah تعالى;

إِنَّهُ فَكَّرَ وَقَدَّرَ ﴿١٨﴾ فَقُتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿١٩﴾ ثُمَّ قُتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ نَظَرَ ﴿٢١﴾ ثُمَّ
عَبَسَ وَوَسَّسَ ﴿٢٢﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ وَاسْتَكْبَرَ ﴿٢٣﴾ فَقَالَ إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ يُؤْتَرُ ﴿٢٤﴾ إِنَّ هَذَا إِلَّا
قَوْلُ الْبَشَرِ ﴿٢٥﴾

"Kwani hakika yeye alifikiri na akapima. Basi ameangamia! Vipi alivyopima! Tena ameangamia! Vipi alivyopima! Kisha akatazama, kisha akakunja kipaji, na akanena. Kisha akaipa kisogo haki, na akatakabari. Na akasema: Haya si chochote ila ni uchawi ulionukuliwa. Haya si chochote ila kauli ya binadamu". (74:18-25)

Kauli Yake;

وَلْيُنَبِّئَنَّهُ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ

"Na ili Tuyabainishe kwa watu wanaojua". Maana yake: Na Tutayaweka waziwazi kwa watu wanaojua haki na kuifuata, na batili wanaiepuka. Hekima ya Allah تعالى ni kamili, Huwaachilia makafiri wapotee na Huwabainishia haki Waumini. Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

يُضِلُّ بِهِ كَثِيرًا وَيَهْدِي بِهِ كَثِيرًا

"Kwa mfano huu Huwapoteza wengi na Huwaongoa wengi". (2:26) Na;

¹ At-Tabari 12:27.

² At-Tabarani 11:137.

لِيَجْعَلَ مَا يُلْقَى الشَّيْطَانُ فِتْنَةً لِلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ وَالْقَاسِيَةِ قُلُوبُهُمْ

“Hayo ni ili Alifanye lile analoliitia Shetani liwe na fitna kwa wale wenye maradhi ndani ya nyoyo zao, na wale ambao nyoyo zao ni ngumu”. (22:53) Mpaka;

وَإِنَّ اللَّهَ لَهَادٍ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

“Na hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Anayewaongoa wenye kuamini kwenye njia Iliyonyooka”. (22:54) Na;

وَمَا جَعَلْنَا أَصْحَابَ النَّارِ إِلَّا مَلَائِكَةً وَمَا جَعَلْنَا عِدَّتَهُمْ إِلَّا فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا لِيَسْتَيْفِنَ
الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَيَزِدَّادَ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِيمَانًا وَلَا يَرْتَابَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ
وَالْمُؤْمِنُونَ وَلِيَقُولَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ وَالْكَافِرُونَ مَاذَا أَرَادَ اللَّهُ بِهَذَا مَثَلًا كَذَلِكَ
يُضِلُّ اللَّهُ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ وَمَا يَعْلَمُ جُنُودَ رَبِّكَ إِلَّا هُوَ

“Na Hatukuwafanya walinzi wa Motoni ila ni Malaika, wala Hatukuifanya idadi yao hiyo ila kuwatatanisha waliokufuru, wapate kuwa na yakini waliopewa Kitabu, na wazidi Imani wale walioamini, wala wasiwe na shaka waliopewa Kitabu na Waumini na wapate kusema wenye maradhi katika nyoyo zao na makafiri: Mwenyezi Mungu Amekusudia nini kwa mfano huu? Ndio kama hivyo Mwenyezi Mungu Humuacha apotee Amtakaye na Humuongoa Amtakaye. Na hapana yeyote Anayejua majeshi ya Mola wako Mlezi ila Yeye tu”. (74:31) Na;

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْءَانِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٨٢﴾

“Na Tunateremsha katika Qur'an yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishi madhalimu ila khasara”. (17:82) Na;

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءٌ ۗ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي ءَاذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ
عَلَيْهِمْ عَمًى ۗ أُولَٰئِكَ يُنَادَوْنَ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ

“Sema: Hii Qur’an ni uwongofu na poza kwa wenye kuamini. Na wasioamini umo uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni. Hao wanaitwa nao wako pahala mbali”. (41:44)

Zipo Aya nyingine zinazojulisha kuwa Allah تعالی Ameiteremsha Qur’an Kuwaongoza wachamungu, na kwamba Yeye Humuachilia apotee au Kumhidi Amtakaye.

أَتَّبِعْ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۗ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٦﴾
 وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكُوا ۗ وَمَا جَعَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيفًا ۗ وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ ﴿١٠٧﴾

106. Fuata uliyofunuliwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Hapana mungu ila Yeye. Na jitenge na washirikina.

107. Na lau Mwenyezi Mungu Angelipenda, wasingekuwa washirikina. Na Sisi Hatukukufanya wewe uwe mtunzaji wao. Wala wewe si mlinzi juu yao.

Amri ya Kufuata Wahyi.

Allah تعالی Anamuamuru Mjumbe Wake na wafuasi wa njia yake,

أَتَّبِعْ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ

“Fuata uliyofunuliwa kutoka kwa Mola wako Mlezi”. Maana: Ufuate na utende kulingana nao (Ufunuo), kwani unayofunuliwa kutoka kwa Mola wako ni kweli, hakuna shaka kwa sababu hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye.

وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ

“Na jitenge na washirikina”. Maana yake: Waachilie, stahamili udhia wao, mpaka Allah تعالی Akusaidie, Akunusuru na Akupe ushindi dhidi yao. Na ujue kwamba Allah تعالی Ana hekima katika Kuwaachilia wapotee, kwani Angelitaka Yeye Angeliwahidi watu wote, na Angelitaka Angeliwajumuisha wote katika Hidaya.

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكُوا

“Na lau Mwenyezi Mungu Angelipenda, wasingelikuwa washirikina”.

Ina maanisha kwamba, Utashi na Hekima vipo katika umiliki Wake, Haulizwi juu ya Analolifanya, ilhali wao ni wa kuulizwa. Kauli Yake;

وَمَا جَعَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا ط

“Na Sisi Hatukukufanya wewe uwe mtunzaji wao”. Maana: Msimamizi anayeangalia kauli na amali zao.

وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ

“Wala wewe si mlinzi juu yao”. Maana: Wa kuzichunga riziki na mambo yao, kwani wajibu wako ni kuufikisha Ujumbe tu. Sawa na Kauli Yake nyingine;

فَذَرِّزْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ﴿٨٨﴾ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ﴿٨٩﴾

“Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia”. (88:21-22)

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ

“Juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hisabu”. (13:40)

وَلَا تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَيَسُبُّوا اللَّهَ عَدْوًا بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ كَذَلِكَ زَيْنًا لِكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلُهُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ مَرْجِعُهُمْ فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٠﴾

108. Wala msiwatukane hao wanaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, wasije na wao wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua. Namna hivyo Tumepambia kila umma vitendo vyao. Kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao Mlezi, Naye Atawaambia waliyokuwa wakiyatenda.

Kukatazwa Kuitukana Miungu Batili ya Makafiri, Ili na Wao Wasije Wakamsubu Allah تعالیٰ.

Allah تعالیٰ Anamkataza Mjumbe Wake na Waumini kuisubu miungu ya washirikina, hata kama kuna maslahi ndani yake, kwani kufanya hivyo kunaweza kusababisha shari zaidi kuliko manufaa yake, kwani washirikina wanaweza kulikabili hilo kwa kumtukana Mola wa Waumini, Naye ni Allah تعالیٰ, Ambaye hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye. Kama alivyosema ‘Ali bin Abu Twalhah kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Aya hii. “(Makafiri) walisema, ‘Ewe Muhammad! Acha kuitukana miungu yetu, au tutamsubu Mola wako’. Baada ya hapo, Allah تعالیٰ Akawakataza Waumini kuyatukana masanamu yao.

فَيَسُبُّوا اللَّهَ عَدُوًّا بِغَيْرِ عِلْمٍ

"...wasije na wao wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua"¹.

'Abdur-Razzaq amemnukuu Ma'mar kwamba alipashwa na Qatadah kuwa, "Waislamu walikuwa wakiyatukana masanamu ya makafiri, basi makafiri wakawa wanalipa kisasi kwa kumsubu Allah تعالى pasi na elimu. Basi Allah تعالى Akateremsha;

وَلَا تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ

"Wala msiwatukane hao wanaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu"².

"Na katika shauri hili – la kuacha jambo la manufaa kwa ajili ya kuupeusha uovu mkubwa zaidi yake – ni maelezo yaliyokuwa katika Hadithi iliyonukuliwa katika *Sahih* kwamba Mtume ﷺ alisema;

«مَلْعُونٌ مَنْ سَبَّ وَالِدَيْهِ»

"Amelaaniwa anayewasubu Wazazi wake".

Wakamuuliza, "Ewe Mjumbe wa Allah! Ni vipi mtu anaweza kuwasubu Wazazi wake mwenyewe?" Akasema;

«يَسُبُّ أَبَا الرَّجُلِ فَيَسُبُّ أَبَاهُ وَيَسُبُّ أُمَّهُ فَيَسُبُّ أُمَّهُ»

"Mtu anamsubu baba wa mtu, na huyo naye anamsubu baba yake mtukanaji, na anamsubu mama yake, naye anamsubu mama yake"³.

Kauli ya Allah تعالى;

كَذَلِكَ زَيْنًا لِّكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلُهُمْ

"Namna hivyo Tumepambia kila umma vitendo vyao".

Maana yake: Kama jinsi Tulivyowapambia watu hao kuyapenda masanamu, kuyatetea na kuyalinda, ndivyo Tulivyoupambia amali zao kila umma miongoni mwa wale waliopotoka. Na Allah تعالى Ana hoja zisizopingika, na Hekima Timilifu kuhusu Anayoyataka na Anayoyakhitari.

¹ At-Tabari 12:34.

² Abdur-Razzaq 2:215.

³ Fat'hul Al-Bari 10417.

ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ مَرْجِعُهُمْ

"Kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao Mlezi". Kurejea kwao na makazi yao ya mwisho.

فَيُنزِّلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

"...naye Atawaambia waliyokuwa wakiyatenda". Maana yake: Anawalipa kwa amali zao, kheri kwa kheri na shari kwa shari.

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن جَاءَهُمْ آيَةٌ لِّيُؤْمِنُوا بِهَا ۗ قُلْ إِنَّمَا الْآيَاتُ عِنْدَ اللَّهِ وَمَا يُشْعِرُكُمْ أَنَّهَا إِذَا جَاءَتْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠٩﴾ وَتُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَرَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ ۗ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَنَدَّرَهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

109. Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu kwa ukomo wa viapo vyao, kuwa ikiwafikia Ishara wataamini. Sema: Ishara ziko kwa Mwenyezi Mungu. Na ni kitu gani kitakachokujulisheni nyinyi kwamba zitapokuja hawatoamini?

110. Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza, Tunawaacha katika maasi yao wakitangatanga.

Kudai Miujiza na Kuapa Kuiamini Iwapo Itatokea.

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu washirikina kuwa waliapa kwa kuvipa nguvu viapo vyao, yaani kwa kusisitiza kwamba,

لَئِن جَاءَهُمْ آيَةٌ

"...kuwa ikiwafikia Ishara". Maana yake: Miujiza au Shani.

لِّيُؤْمِنُوا بِهَا

"...wataamini". Maana yake: Watasadiki.

قُلْ إِنَّمَا الْآيَاتُ عِنْدَ اللَّهِ

"Sema: Ishara ziko kwa Mwenyezi Mungu". (6:109)

Maana: Sema ewe Muhammad ﷺ kuwaambia wale wanaokutaka ishara, kwa uasi, kufuru na ufidhuli, si katika njia ya Hidaya na kutaka kuongoka, kwamba,

“Kwa hakika, jambo la kuleta miujiza ni la Allah تعالى, Akitaka Atakuleteeni na Akitaka Atakupuuzeni”. Na Kauli Yake;

وَمَا يُشْعِرُكُمْ أَنَّهَا إِذَا جَاءَتْ لَا يُؤْمِنُونَ

“Na ni kitu gani kitakachokujulisheni nyinyi kwamba zitapokuja hawatoamini?”

Ilisemwa wanaaambiwa washirikina, kwa mujibu wa Mujahid. Ni kama vile Anawaambia hivi – nini kitakujulisheni kuhusu kusadiki kwenu katika kiapo hiki mnachoapa? Hii ina maana hata kama itakuja hiyo ishara wanayoitaka, hawatoamini. Pia ilisemwa Waumini ndio wanaoambiwa katika Kauli ya Allah تعالى, “Na ni kitu gani kitakachokujulisheni nyinyi” waumini kwamba wao wataamini? Katika mtazamo huu wa mwisho, hukadiriwa uthibitishaji wa habari na wala si ukanushaji, kama ilivyokuja katika Kauli nyingine ya Allah تعالى. Katika maelezo ya herufi ya “la” yenye maana ya uthibitishaji.

قَالَ مَا مَنَّكَ إِلَّا تَسْجُدَ إِذْ أَمَرْتُكَ

“Nini kilichokuzuia kumsujudia Nilipokuamrisha?” (7:12) na,

وَحَرَامٌ عَلَى قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا أَنَّهُمْ لَا يَرْجِعُونَ

“Na haiwi kwa wana – mji Tuliouangamiza, ya kwamba hawatarejea”. (21:95)

Inamaanisha: “Ni nini kilichokuzuia usisujudu pindi Nilipokuamuru”, “Na ni muhali kabisa kwamba wao watarejea” Na katika Aya ya sura hii hukadiriwa hivi: “Nini kitakujulisheni enyi Waumini mnaotamani sana hilo la kuamini kwao kwamba wakijiwa na ishara wataamini?” Kauli ya Allah تعالى;

وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَارَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ

“Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza”.

Al-'Awfi amesema Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Ayah hii, “Pindi washirikina walipoyapinga yale Allah تعالى Aliyoyateremsha, nyoyo zao hazikutulia katika jambo moja, bali walikataa kila jambo (la manufaa)”¹. Mujahid ameizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

¹ At-Tabari 12:44.

وَنُقَلِّبُ أَفْعَادَهُمْ وَأَبْصَرَهُمْ

“Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao”.

Tunawabadili kutoka katika Imani, kama Tulivyofanya hivyo hapo kabla. Hayo waliyasema 'Ikrimah na 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam. Na Ibn Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Allah تعالى Anasema watakachosema waja wake kabla hawajakisema, na watakachokifanya kabla hawajakifanya”. Allah تعالى Alisema;

وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثْلُ خَبِيرٍ

“Na hapana atakayekupa khabari vilivyo kama Yeye Mwenye khabari”. (35:14) na;

أَنْ تَقُولَ نَفْسٌ يَحْسَرُنِي عَلَى مَا فَرَّطْتُ فِي جَنْبِ اللَّهِ

“Isije ikasema nafsi: Ee majuto yangu kwa yale niliyopoteza upande wa Mwenyezi Mungu...”. (39:56) Hadi;

لَوْ أَنَّ لِي كَرَّةً فَأَكُونَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ

“Au ikasema inapoona adhabu: Lau ningelipata fursa nyingine, ningelikuwa miongoni mwa wafanya mema”. (39:58)

Basi, Allah تعالى Alitoa khabari, lau wangelirudishwa wasingelikuwa katika Hidayu. Na Amesema Allah تعالى,

وَلَوْ رُدُّوْا لَعَادُوْا لِمَا بُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُوْنَ

“Na kama wangelirudishwa bila ya shaka wangeyarejea yale yale waliyokatazwa. Na hakika hao ni waongo”. (6:28) na Amesema;

وَنُقَلِّبُ أَفْعَادَهُمْ وَأَبْصَرَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوْا بِمِآءِ أَوَّلَ مَرَّةٍ

“Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza”.

Na alisema, “Kama wangelirudishwa duniani wangelizuiliwa kupata Hidayu kama hapo mwanzoni, walipokuwa duniani.” Na Kauli Yake;

وَنَذَرُهُمْ

"...Tunawaacha".

Maana yake: Hatujishughulishi nao.

فِي طُعَيْنِهِمْ

"...katika maasi yao".

Ibn 'Abbas na As-Suddi wamesema: Maana yake, ukafiri. Abu Al-'Aliyah, Ar-Rabi' bin Anas na Qatadah walisema: Ina maana, "katika upotevu wao".

يَعْمَهُونَ

"...wakitangatanga".

Al-A'mash alisema, wakifanya mchezo. Ibn 'Abbas, Mujahid, Abu Al-'Aliyah, Ar-Rabi', Abu Malik na wengine walisema wakisusurika katika ukafiri wao.

* * *

* وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةَ
 وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَىٰ وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ
 شَيْءٍ قُبُلًا مَّا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ
 وَلٰكِن كَثَرْتُمْ يٰجَاهِلُونَ ﴿١١١﴾ وَكَذٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ
 عَدُوًّا شٰٓئِطِينَ الْاِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ اِلَىٰ بَعْضٍ
 زُخْرَفَ الْقَوْلِ غُرُورًا ۗ وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ ۗ فَذَرْهُمْ وَمَا
 يَفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾ وَلِتَصْغَىٰ اِلَيْهِ الْاَفِيْدَةُ الْاٰذِنِ لَا يُؤْمِنُوْنَ
 بِالْآخِرَةِ وَلَيَرْضَوْهُ وَلَيَقْتَرِفُوْا مَا هُمْ مُّقْتَرِفُوْنَ ﴿١١٣﴾
 اَفَغَيَّرَ اللّٰهُ اٰتِنِيْ حَكَمًا ۗ وَهُوَ الَّذِي۟ اَنْزَلَ اِلَيْكُمْ الْكِتٰبَ
 مُفَصَّلًا ۗ وَالَّذِي۟نَ اٰتَيْنَهُمُ الْكِتٰبَ يَعْلَمُوْنَ اَنَّهُۥ مُنْزَلٌ مِّنْ
 رَبِّكَ بِالْحَقِّ ۗ فَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِيْنَ ﴿١١٤﴾ وَتَمَّتْ
 كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا ۗ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمٰتِيْهِ ۗ وَهُوَ
 السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿١١٥﴾ وَاِنْ تُطِيعْ اَكْثَرُ مَنْ فِى الْاَرْضِ
 يُضِلُّوْكَ عَنۢ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۗ اِنْ يَتَّبِعُوْنَ اِلَّا الظَّنَّ وَاِنْ هُمْ اِلَّا
 يَخْرُصُوْنَ ﴿١١٦﴾ اِنَّ رَبَّكَ هُوَ اَعْلَمُ مَنۢ يَضِلُّ عَنۢ سَبِيْلِهِ ۗ
 وَهُوَ اَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِيْنَ ﴿١١٧﴾

* وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةَ
 وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَىٰ وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ
 شَيْءٍ قُبُلًا مَّا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا إِلَّا
 أَن يَشَاءَ اللَّهُ وَلٰكِن كَثَرْتُمْ
 يٰجَاهِلُونَ ﴿١١١﴾

**111. Na lau kuwa Tunge-
 liwateremshia Malaika, na
 maiti wakazungumza nao,
 na Tukawakusanyia kila
 kitu mbele yao, bado wasi-
 ngeliamini, ila Mwenyezi
 Mungu Atake. Lakini
 wengi wao wamo ujingani.**

Allah تعالى Anasema; “Kama
 Tuliwakubalia ombi lao hao
 walioapa kwa Allah تعالى
 viapo vya nguvu, kwamba
 wangeliijiwa na ishara,
 Tunge liwateremshia
 Malaika kuwapasha
 khabari za Ujumbe utokao
 kwa Allah تعالى kuwa

wawasadiki Mitume kama walivyoomba, wakasema;

أَوْ تَأْتِي بِلِلَّهِ وَالْمَلٰٓئِكَةِ قَبِيْلًا

“...au utuletee Mwenyezi Mungu na Malaika uso kwa uso”. (17:92)

na;

قَالُوْا لَنْ نُّؤْمِنَ حَتّٰى تُنَزَّلَ عَلَيْنَا مِثْلَ مَا اُنزِلَ عَلَيْنَا

“...wao husema: Hatutoamini mpaka tupewe mfano wa waliopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu”. (6:124) na;

﴿ وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْنَا آيَاتٌ مِّنْ سَمَوَاتِكُمْ أَوْ نَرَى رِيبًا لَقَدْ أَشْكَبُوا
فِي أَنْفُسِهِمْ وَغَتَوْا عُتُقًا كَبِيرًا ﴿٢١﴾ ﴾

“Na walisema wale wasiotaraji kukutana Nasi: Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika au hatumuoni Mola wetu Mlezi? Kwa yakini hawa wamejiona bora nafsi zao, na wamepanda kichwa vikubwa mno!” (25:21)

﴿ وَكَلَّمَهُمُ الْمُوتَىٰ ﴾

“...na maiti wakazungumza nao”. Maana yake: Wakawapa khabari juu ya kuyasadiki yale waliyokuja nayo Mitume.

﴿ وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَيْءٍ قُبُلًا ﴾

“...na Tukawakusanyia kila kitu mbele yao”.

Baadhi wamelisoma neno lilotafsiriwa, “Mbele yao” kwa, *Qibalan*, kwa maana ya kukutana ana kwa ana. Na wengine walisoma *Qubulan* kwa maana hiyo pia. Kwa mujibu wa ‘Ali bin Abu Twalhah na Al-‘Awfi walivyomnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما. Hali kadhalika, Qatadah na ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam walisema hivyo hivyo. Mujahid alisema, “Mbele yao” yaani, makundi kwa makundi ya watu². Ina maana umma wote, mmoja baada ya mwingine utakusanywa na kusadikisha juu ya ukweli wa yale waliyokuja nayo Mitume.

﴿ مَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ ﴾

“...bado wasingeliamini, ila Mwenyezi Mungu Atake”.

Maana yake: Hidaya inatoka kwa Allah تعالى, si kutoka kwao. Allah تعالى Humhidi Amtakaye na Kumuachilia Amtakaye apotee, na Yeye Hufanya Atakavyo.

﴿ لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ ﴾ ﴿٢٣﴾

“Yeye Hahojiwi kwa Ayatendayo, na wao ndio Wanahojiwa kwa wayatendayo”. (21:23)

¹ At-Tabari 12:49.

² At-Tabari 12:49, 50.

Kwa sababu ya Ujuzi Wake, Hekima, Nguvu, Mamlaka Yake ya juu na Ushindi Wake. Aya hii ni sawa na Kauli Yake تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١١١﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ
يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿١١٢﴾

“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini. Ijapo kuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu”. (10:96-97)

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطِينِ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ
زُخْرَفَ الْقَوْلِ غُرُورًا ۗ وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ ۗ فَذَرْهُمْ ۗ وَمَا يَفْتَرُونَ ﴿١١٣﴾ وَلِتَصْغَىٰ
إِلَيْهِ أَفئِدَةُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَلِيَرَوْهُ وَليَقْتَرِفُوا مَا هُمْ مُّقْتَرِفُونَ ﴿١١٤﴾

112. Na kadhalika Tumemfanyia kila Nabii maadui mashetani wa kiwatu, na kijini, wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba – pamba, kwa udanganyifu. Na Angelipenda Mola wako Mlezi wasingelifanya hayo. Basi waache na wanayoyazua.

113. Na ili nyoyo za wasioamini Akhera ziyaelekee hayo, nao wayaridhie na wayachume wanayoyachuma.

Kila Mtume Ana Maadui.

Allah تعالى Anasema, kama Tulivyojaalia uwe na maadui wanaokupinga na kukuasi, Tulijaalia maadui kwa kila Nabii kabla yako, basi usihuzunishwe na hilo. Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine;

وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبَرُوا عَلَىٰ مَا كُذِّبُوا وَأُوذُوا

“Na hakika walikanushwa Mitume wa kabla yako. Nao wakavumilia kule kukanushwa na kuudhiwa”. (6:34) na;

مَا يُقَالُ لَكَ إِلَّا مَا قَدْ قِيلَ لِلرُّسُلِ مِن قَبْلِكَ ۗ إِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ وَذُو عِقَابٍ أَلِيمٍ ﴿١١٥﴾

“Huambiwi ila yale yale waliyoambiwa Mitume wa kabla yako.

Hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka ni Mwenye Maghfira, na ni Mwenye Adhabu Chungu". (41:43) na;

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا مِّنَ الْمُجْرِمِينَ

"Na hivi hivi Tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wakosefu". (25:31)

Waraqah bin Nawfal alimuambia Mtume ﷺ, "Kwa hakika, hakuna aliyekuja na kile ulichokuja nacho, bali alifanyiwa uadui". Na kuhusu Kauli Yake تعالى;

شَيْطَانِ الْإِنْسِ

"...mashetani wa kiwatu". Badili ya,

عَدُوًّا

"...maadui". Maana: Wana maadui katika mashetani wa kiwatu na wa kijini. Maana ya *Shaytan* ni kila aliyezidi sana kwa kufanya shari. Na hapana anayethubutu kumfanyia uadui Mtume ﷺ, isipokuwa Shetani wa kiwatu na wa kijini, Allah تعالى Awaangamize na Awalaani. 'Abdur-Razzaq alisema: Ma'mar alitueleza kwamba Qatadah aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

شَيْطَانِ الْإِنْسِ

"...mashetani wa kiwatu, ...". Kwa kusema: Kutoka kwa majini na watu, mashetani hufundishana. Na Kauli Yake;

يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ زُخْرَفَ الْقَوْلِ غُرُورًا

"...wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba – pamba, kwa udanganyifu".

Inamaanisha, wanafundishana wao kwa wao maneno yaliyopambwa kwa udanganyifu. Yamepambwa ili yamghuri mjinga wa jambo hilo anapolisikia.

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ

"Na Angelipenda Mola wako Mlezi wasingelifanya hayo".

Maana yake: Na yote hayo ni kwa *Qadar*, Hukumu na Kutaka kwa Allah تعالى kwamba kila Nabii awe na maadui kutokana na hao.

فَذَرَهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ

"Basi waache na wanayoyazua". Maana yake: Wanayoyakadhibisha. Maana: Achana na udhia wao na utawakali kwa Allah تعالى juu ya huo uadui wao, kwani Yeye Anakutosha na Atakunusuru dhidi yao. Na Kauli Yake;

وَلْتَصَفَىٰ إِلَيْهِ

"Na ili ziyaelekee hayo". Kwa mujibu wa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, inamaanisha, "Ili ziyaendee hayo".

أَفئِدَةُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ

"...nyoyo za wasioamini Akhera ziyaelekee hayo".

Maana: Nyoyo, akili na masikio yao. As-Suddi alisema, ni nyoyo za makafiri.

وَلْيَرْضَوْهُ

"...nao wayaridhie". Maana: Wayapende na wawe na utashi nayo¹. Hayo wanayakubali asiyeamini Akhera. Sawa na Alivyosema Allah تعالى;

فَإِنْ كُمْرًا وَمَا تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾ مَا أَشْتَرُ عَلَيْهِ بِفَنَتَيْنِ ﴿٣٨﴾ إِلَّا مَنْ هُوَ صَالٍ الْجَحِيمِ ﴿٣٩﴾

"Basi hakika nyinyi na mnaowaabudu. Hamuezi kuwapoteza. Isipo kuwa yule atakayeingia Motoni. (37:161-163) na,

إِنْ كُمْرًا لَفِي قَوْلٍ مُّخْتَلِفٍ ﴿٤٠﴾ يُؤْفَكُ عَنْهُ مَنْ أُفِكَ ﴿٤١﴾

"Hakika nyinyi bila ya shaka mmo katika kauli inayokhitalifiana. Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa." (51:8-9)

Kauli ya Allah تعالى;

وَلْيَقْتَرِفُوا مَا هُمْ مُّقْتَرِفُونَ

"...na wayachume wanayoyachuma".

'Ali bin Abu Twalha alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa inamaanisha, "Wajipatie kipato chao"². As-Suddi na Ibn Zayd pia walisema, "Waache wafanye watakalolifanya"³.

¹ At-Tabari 12:59.

² At-Tabari 12:59.

³ At-Tabari 12:60.

أَفَغَيْرَ اللَّهِ أُبْتِغَىٰ حَكْمًا وَهُوَ الَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكُمُ الْكِتَابَ مُفَصَّلًا ۗ وَالَّذِينَ
 ءَاتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ يَعْلَمُونَ أَنَّهُ مُنَزَّلٌ مِّن رَّبِّكَ بِالْحَقِّ ۗ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿١١٤﴾
 وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا ۗ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١١٥﴾

114. Je, nimtafute hakimu ghairi ya Mwenyezi Mungu, Naye Ndiye Aliyekuteremshieni Kitabu kilichoelezwa waziwazi? Na hao Tuliowapa Kitabu wanajua ya kwamba kimeteremshwa na Mola wako Mlezi kwa Haki. Basi usiwe katika wanaotia shaka.

115. Na yametimia maneno ya Mola Mlezi wako kwa kweli na uadilifu. Hapana awezaye kuyabadilisha Maneno Yake. Na Yeye Ndiye Mwenye Kusikia na Mwenye Kujua.

Allah تعالى Anasema Kumuambia Mtume wake; Sema kuwaambia hawa wanaomshirikisha Allah تعالى, ambao huabudu asiyekuwa Allah تعالى.

أَفَغَيْرَ اللَّهِ أُبْتِغَىٰ حَكْمًا

“Je nimtafute hakimu ghairi ya Mwenyezi Mungu”. Maana: Kati yangu na nyie.

وَهُوَ الَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكُمُ الْكِتَابَ مُفَصَّلًا

“Naye Ndiye Aliye kuteremshieni Kitabu kilichoelezwa”. Maana: Kilichobainishwa.

وَالَّذِينَ ءَاتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ

“Na hao Tuliowapa Kitabu”. Mayahudi na Wakristo.

يَعْلَمُونَ أَنَّهُ مُنَزَّلٌ مِّن رَّبِّكَ بِالْحَقِّ

“...wanajua kwamba kimeteremshwa na Mola wako Mlezi kwa Haki”.

Inamaanisha, kutokana na bishara walizo nazo kutoka kwa Mitume waliotangulia ambazo zinakuhusu wewe.

فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ

“Basi usiwe katika wanaotia shaka”. Sawa na Kauli Yake nyingine.

فَإِنْ كُنْتَ فِي شَكٍّ مِّمَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ فَسْأَلِ الَّذِينَ يَفْرَهُونَ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكَ ۗ لَقَدْ

جَاءَكَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ ۗ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿١١٦﴾

“Na ikiwa unayoshaka katika Tuli yokuteremshia, basi waulize wasomao Kitabu kabla yako. Kwa yakini imekwishakujia Haki kutoka kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wenye shaka”. (10:94)

Hili ni sharti, na sharti huwa halina ulazima wa kutokea. Kauli ya Allah تعالى;

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

“Na yametimia Maneno ya Mola Mlezi wako kwa kweli na uadilifu”.

Qatadah alisema, “Ukweli wa Aliyoyasema, na Uadilifu katika Aliyoyahukumu.”¹ Allah تعالى Huwa Anatoa Khabari za Kweli na Uadilifu katika Amri Zake. Kwa hivyo, kila Alichokitolea khabari ni kweli, pasi na shaka hata kidogo, na kila Aliloliamuru ni la kiuadilifu ambalo hakuna lililo na uadilifu ghairi ya hilo, kila Alilolikataza ni la batili, kwani Yeye Hakatazi isipokuwa uovu. Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine;

يَأْمُرُهُم بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ

“...Anayewaamrisha mema na Anawakanya maovu”. (7:157)

Mpaka mwisho wa Aya.

لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ

“Hapana Awezaye kuyabadilisha Maneno Yake”.

Maana yake: Hakuna wa kuzuia Hukumu ya Allah تعالى, si duniani wala si Akhera.

وَهُوَ السَّمِيعُ

“Na Yeye Ndiye Mwenye Kusikia”.

Kauli za waja Wake.

الْعَلِيمُ

“...na Mwenye Kujua”

Shughuli na ukosefu wao wa kufanya shughuli, na Ndiye Anayemjazi kila mtenda kwa amali yake.

¹ At-Tabari 12:63.

وَأَن تَطْعَ أَكْثَرُ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۚ إِنَّ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَأَن هُمْ
إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿١١٦﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ مَن يَضِلُّ عَن سَبِيلِهِ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١١٧﴾

116. Na ukiwatii wengi katika hawa waliomo duniani watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawa hawaifuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kusema uwongo tu.

117. Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mjuzi wa Kushinda wote Kuwajua waliopotea njia Yake, na Ndiye Mjuzi Kushinda wote Kuwajua waliohidika.

Watu Wengi ni Wapotevu.

Allah تعالی Anaeleza hali za watu wengi wa duniani, kwamba wapo katika upotovu.

Sawa na Allah تعالی Alivyosema katika Aya nyingine;

وَلَقَدْ ضَلَّ قَبْلَهُمْ أَكْثَرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٣٧﴾

“Na bila ya shaka walikwisha potea kabla yao wengi wa watu wa zamani”. (37:71) Na;

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

“Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi”. (12:103)

Na katika upotevu wao hawana yakini na jambo lao, bali wapo katika dhana ya uongo na maono batili.

إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَأَن هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ

“Hawa hawaifuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kusema uwongo tu”.

Al-Khars ni kizuizi kama vile *Khars An-Nakhl* ambayo ni kizuizi cha tende zilizo katika mti huo. Na yote hayo ni kwa *Qadar* na Kutaka kwa Allah تعالی.

هُوَ أَعْلَمُ مَنْ يَضِلُّ عَنْ سَبِيلِهِ^ط

“Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mjuzi wa Kushinda wote Kuwajua waliopotea njia Yake”.

Basi Humrahisishia hilo.

وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ

“...na Ndiye Mjuzi Kushinda wote Kuwajua waliohidika”.

Naye Humrahisishia hilo. Kila mmoja hurahisishwa kwa ajili ya lile aliloumbiwa kwalo.

* * *

فَكُلُوا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ إِنْ كُنْتُمْ بِقَابِئِهِ مُؤْمِنِينَ ﴿١١٨﴾ وَمَا لَكُمْ أَلَّا تَأْكُلُوا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَقَدْ فَصَّلَ لَكُمْ مَا حَرَّمَ عَلَيْهِ إِذْ أَخْطَرْتُمْ إِلَيْهِ وَإِنْ كَثِيرًا لِيُضِلُّونَ بِأَهْوَابِهِمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ إِنْ رَبُّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِالْمُعْتَدِينَ ﴿١١٩﴾ وَذَرُوا ظَهْرَ الْإِثْمِ وَبَاطِنَهُ إِنَّ الَّذِينَ يَكْسِبُونَ الْإِثْمَ سَيَجْزَوْنَ بِمَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿١٢٠﴾ وَلَا تَأْكُلُوا مِمَّا لَمْ يُذْكَرِ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَإِنَّهُ لَفِسْقٌ وَإِنَّ الشَّيَاطِينَ لَيُوحُونَ إِلَيْكُمْ لِيجْعِدُوا لَكُمْ وَإِنْ أَطَعْتُمُوهُمْ إِنَّكُمْ لَمُشْرِكُونَ ﴿١٢١﴾ أَوْ مَن كَانَ مِتًّا فَأَحْيَيْنَاهُ وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِي بِهِ فِي النَّاسِ كَمَن مَّثَلُهُ فِي الظُّلُمَاتِ لَيْسَ بِخَارِجٍ مِّنْهَا كَذَلِكَ زُيِّنَ لِلْكَافِرِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢٢﴾ وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا فِي كُلِّ قَرْيَةٍ أَكْبَرًا مُّجْرِمِيهَا لِيَمْكُرُوا فِيهَا وَمَا يَمْكُرُونَ إِلَّا بِأَنْفُسِهِمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿١٢٣﴾ وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ حَتَّى نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلُ اللَّهِ اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ ﴿١٢٤﴾

فَكُلُوا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ إِنْ كُنْتُمْ بِقَابِئِهِ مُؤْمِنِينَ ﴿١١٨﴾ وَمَا لَكُمْ أَلَّا تَأْكُلُوا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَقَدْ فَصَّلَ لَكُمْ مَا حَرَّمَ عَلَيْهِ إِذْ أَخْطَرْتُمْ إِلَيْهِ وَإِنْ كَثِيرًا لِيُضِلُّونَ بِأَهْوَابِهِمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ إِنْ رَبُّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِالْمُعْتَدِينَ ﴿١١٩﴾

118. Basi kuleni katika walio somewa Jina la Mwenyezi Mungu, ikiwa mnaziamini Aya Zake.

119. Na kwa nini msile katika waliosomewa Jina la Mwenyezi Mungu, Naye Amekwisha kukubainishieni Alivyokuharamishieni, isipokuwa vile mnavyo lazimishwa? Na hakika wengi wanapoteza kwa matamaniao yao bila ya kuwa na ilimu. Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mjuzi Kushinda wote Kuwajua wanao-pindukia mipaka.

Kuruhusiwa Kilichochoinjwa kwa Jina la Allah تعالى

Hii ni ruhusa ya Allah تعالى kwa waja Wake, wale wanyama wanaochinjwa kwa kudhukuriwa Jina Lake, na inafahamika hapa, kuwa mnyama ambaye hakudhukuriwa Jina la Allah تعالى haruhusiwi kuliwa, kama makafiri wa kikuraishi walivyokuwa wakijihalalishia kwa kula nyamafu na wanyama waliochoinjwa kwa ajili ya sanamu na ghairi ya hao. Halafu Akatumainisha

ulaji wa nyama ya wanyama ambao Jina Lake lilitajwa wakati wa kudhabihu. Allah تعالى Alisema;

وَمَا لَكُمْ أَلَّا تَأْكُلُوا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَقَدْ فَصَّلَ لَكُمْ مَا حَرَّمَ عَلَيْكُمْ

“Na kwa nini msile katika waliosomewa Jina la Mwenyezi Mungu, Naye Amekwishakukubainishieni Alivyokuharamishieni”.

Maana: Ameshabainisha walioharamishwa kwenu na Akafafanua. Baadhi yao walisoma neno lililotafsiriwa, “Amekwisha Kubainishieni”, kwa shada, *faswala*, na wengine bila shada, *faswala*. Yote mawili yana maana moja, kwa maana ya kubainisha na kusherehi.

إِلَّا مَا اضْطُرِرْتُمْ إِلَيْهِ

“...isipokuwa vile mnavyolazimishwa?” Maana: Isipokuwa katika hali ya dharura, mnaruhusiwa mnyama mnyempata kumla. Kisha, Allah تعالى Alibainisha ujahili wa washirikina kuhusu rai zao potovu, kwa kujihalalishia kwao nyamafu, na aliyechinjwa kwa kutajwa jina lisilo la Allah تعالى. Alisema;

وَإِنَّ كَثِيرًا لَّمْ يَضِلُّوا بِأَهْوَابِهِمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِالْمُعْتَدِينَ

“Na hakika wengi wanapoteza kwa matamano yao bila ya kuwa na ilimu. Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mjuzi Kushinda wote Kuwajua wanaopindukia mipaka”.

Maana yake: Yeye Anajua urukaji wao mipaka, uwongo na uzushi wao.

وَذُرُوا ظَهَرَ الْإِثْمِ وَبَاطِنُهُ إِنَّ الَّذِينَ يَكْسِبُونَ الْإِثْمَ سَيُجْزَوْنَ بِمَا كَانُوا يَقْتَرِفُونَ ﴿١٢٠﴾

120. Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana. Hakika wanaochuma dhambi watalipwa kwa waliyokuwa wakiyachuma.

Mujahid alisema;

وَذُرُوا ظَهَرَ الْإِثْمِ وَبَاطِنُهُ

“Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana”. Maasi katika hadhara na ufichoni¹. Na amesema Qatadah,

وَذُرُوا ظَهَرَ الْإِثْمِ وَبَاطِنُهُ

“Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana”.

¹ At-Tabari 12:73.

Maana yake: Ya siri na ya dhahiri, machache au mengi¹. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّيَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ

“Sema: Mola Mlezi Wangu Ameharamisha mambo machafu ya dhahiri na ya siri”. (7:33)

Na kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema;

إِنَّ الَّذِينَ يَكْسِبُونَ آلَاءَنَا سَيُجْزَوْنَ بِمَا كَانُوا يَقْتَرِفُونَ

“Hakika wanaochuma dhambi watalipwa kwa waliyokuwa wakiyachuma”.

Maana yake: Ima yawe ya dhahiri ama ya siri, Allah تعالى Atawajazi. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kwamba An-Nawwas bin Sam'an alisema, “Nilimuuliza Mtume ﷺ kuhusu *Al-Ithm* (dhambi). Akasema;

«إِنَّمَا مَا حَاكَ فِي صَدْرِكَ وَكَرِهْتَ أَنْ يَطَّلِعَ النَّاسُ عَلَيْهِ»

*“Dhambi ni kila jambo lisilokupa raha moyoni mwako na hupendi watu walijue”.*²

وَلَا تَأْكُلُوا مِمَّا لَمْ يُذْكَرِ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَإِنَّهُ لَفِسْقٌ وَإِنَّ الشَّيَاطِينَ لَيُوحُونَ إِلَيْكَ

أُولِيَاءِ بِهِمْ لِيَجِدُوا لَكُمْ ط ۖ وَإِنْ أَطَعْتُمُوهُمْ إِنَّكُمْ لَمُشْرِكُونَ ﴿١٢١﴾

121. Wala msile katika wale wasiosomewa Jina la Mwenyezi Mungu. Kwani huo ni upotofu. Na kwa yakini mashetani wanawafunza marafiki zao kubishana nanyi. Na mkiwafuata basi hapana shaka nyinyi mtakuwa washirikina.

Kuharamishwa kwa Kilichochinjwa kwa Ghairi ya Jina la Allah تعالى.

Aya hii inajulisha kuwa dhabihu haihalaliki ikiwa Jina la Allah تعالى halijadhukuriwa wakati wa kumchinja, hata kama mchinjaji aliyechinja ni Muislamu.

Na Anasema katika Aya inayohusu masuala ya kuwinda,

¹ At-Tabari 12:72.

² Muslim 4:1980.

فَكُلُوا مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَاذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ^ط

“Basi kuleni walichokukamatieni, na mkisomee Jina la Mwenyezi Mungu”. (5:4)

Halafu Akasisitiza katika Aya hii kwa Kauli Yake;

وَإِنَّهُ لَفِسْقٌ

“Kwani huo ni upotofu”.

Ilisemwa kiwakilishi kinarejea katika kula. Na ilisemwa pia, inarudi katika kuchinja kwa ajili ya kilichoghairi ya Allah تعالى. Kuna Hadithi kadha za Mtume ﷺ zinazozungumzia jambo la kutaja Jina la Allah تعالى wakati wa kuchinja na kuwinda. Kama vile Hadithi mbili za ‘Adi bin Hatim na Abu Tha’labah رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ alisema;

«إِذَا أُرْسِلْتَ كَلْبِكَ الْمُعَلَّمِ وَذَكَرْتَ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ فَكُلْ مَا أَمْسَكَ عَلَيْكَ»

“Unapomtuma mbwa wako aliyepata mafunzo na ukalidhukuru Jina la Allah wakati wa kumuachilia, basi kula mnyama atakaye kukamatia”.

Hadithi hii ilikusanywa katika *Sahih Mbili*¹. Ar-Rafi’ bin Khadij رضي الله عنه amesimulia kwamba Mtume ﷺ alisema;

«مَا أَنْهَرَ الدَّمَ وَذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ فَكُلُوهُ»

“Mnyama aliyetolewa damu (kuchinjwa) na Jina la Allah Likatajwa wakati wa kufanya hivyo, kuleni”.

Hadithi hii nayo ilikusanywa katika *Sahih Mbili*². Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema kwamba Mtume ﷺ aliwaambia majini;

«لَكُمْ كُلُّ عَظْمٍ ذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ»

“(Chakula) chenu ni kila mfupa ambao Jina la Allah lilitajwa wakati wa kuchinja”.³

¹ Fat’hul Al-Bari 9:524 na 9:137 na Muslim 3:1529 na 3:1352.

² Fat’hul Al-Bari 9:546 na Muslim 3:1558.

³ Muslim 1:332.

Jundub bin Sufyan Al-Bajali رضى الله عنه alisema Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ دَبَّحَ قَبْلَ أَنْ يُصَلِّيَ فَلْيَذْبَحْ مَكَانَهَا أُخْرَى، وَمَنْ لَمْ يَكُنْ ذَبَّحَ، حَتَّى صَلَّيْنَا
فَلْيَذْبَحْ بِاسْمِ اللَّهِ»

“Aliyechinja kabla ya kusali, basi akachinje mnyama mwingine mahali badala ya huyo, na ambaye hakuchinja, hata tukasali, basi amchinje kwa kulidhukuru Jina la Allah”.

Sahih Mbili zilinukuu Hadithi hii¹.

Wahyi wa Shetani.

Kauli ya Allah تعالى;

وَإِنَّ الشَّيْطَانَ لِيُوحِيَ إِلَىٰ أَوْلِيَآئِهِمْ لِيُجَدِّدَ لَكُمْ

“Na kwa yakini mashetani wanawafunza marafiki zao kubishana nanyi”.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alimnukuu Abu Is-haq kwamba alisema, mtu mmoja kamuambia Ibn 'Umar رضى الله عنهما kuwa Al-Mukhtar anadai huwa anapata wahyi. 'Umar رضى الله عنه akamjibu, “Amesema kweli”. Kisha akaisoma Aya hii,

وَإِنَّ الشَّيْطَانَ لِيُوحِيَ إِلَىٰ أَوْلِيَآئِهِمْ

“Na kwa yakini mashetani wanawafunza marafiki zao”².

Abu Zamil alisema, “Nilikuwa nimekaa karibu ya Ibn 'Abbas رضى الله عنهما katika kipindi ambacho Al-Mukhtar bin 'Ubayd alifanya Hija. Mtu mmoja akaja kwa Ibn 'Abbas رضى الله عنهما na akasema, “Ewe Ibn 'Abbas! Abu Is-haq (Al-Mukhtar), anadai ameletewa Wahyi usiku huu”. Ibn 'Abbas رضى الله عنهما akasema, “Amesema ukweli”. Nikafedheheshwa, na nikasema, “Unasema amesema ukweli?” Ibn 'Abbas رضى الله عنهما akasema, “Kuna namna mbili za Wahyi, wa Allah تعالى na wa shetani. Wahyi wa Allah تعالى unakwenda kwa Muhammad ﷺ na wa shetani huwa unakwenda kwa marafiki wake”. Halafu akasoma;

وَإِنَّ الشَّيْطَانَ لِيُوحِيَ إِلَىٰ أَوْلِيَآئِهِمْ

“Na kwa yakini mashetani wanawafunza marafiki zao”³.

¹ Ibn Abu Hatim 4:1379.

² At-Tabari 12:86.

³ At-Tabari 12:81.

Tumekwishatangulia kutoa maelezo yanayofanana na haya katika tafsiri aliyoitoea 'Ikrimah kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا

"...wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba pamba, kwa udanganyifu".

Kauli ya Allah تعالى:

لِيُجَدِّدِلَكُمْ

"...kubishana nanyi".

Ibn Jarir رضي الله عنهما amemnuuu Ibn 'Abbas رحمه الله تعالى juu ya,

وَلَا تَأْكُلُوا مِمَّا لَمْ يُذَكَّرْ أَشْرُ اللَّهِ عَلَيْهِ

"Wala msile katika wale wasiosomewa Jina la Mwenyezi Mungu".

Mpaka katika Kauli Yake;

لِيُجَدِّدِلَكُمْ

"...kubishana nanyi". Akasema, mashetani huwa wanawafundisha marafiki zao kwa kuwaambia, "Mnakula wanyama mnaowaua nyinyi na si wanaokufa kwa Amri ya Allah تعالى (wanaokufa wenyewe)?" Na katika baadhi ya matamshi yake mengine ambayo pia alimnuuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, ni kwamba, "Wanyama mnaowaua ni wale mnaowachinja kwa kulidhukuru Jina la Allah تعالى na ambaye hakutajiwa Jina la Allah تعالى ndiye aliyekufa mwenyewe (nyamafu)"¹. Katika kuitafsiri Aya hii, As-Suddi alisema, "Baadhi ya washirikina waliwaambia Waislamu: "Mnadai vipi kwamba mnatafuta Radhi za Allah تعالى ilhali mnyama aliyefishwa na Allah تعالى hamli na mnakula mnayemchinja?" Allah تعالى Alisema;

وَأِنْ أَطَعْتُمُوهُمْ

"Na mkiwafuata basi". Na mkala nyamafu.

إِنَّكُمْ لَمُشْرِكُونَ

"...hapana shaka nyinyi mtakuwa washirikina"² Mujahid, Adh-Dhahhak na wanazuoni wengine wa *Salaf* walisema hivyo hivyo³.

¹ At-Tabari 12:81.

² At-Tabari 12:81.

³ At-Tabari 12:80.

Kufadhilisha Kauli ya Yeyote Badala ya Hukumu ya Allah تعالى ni Ushirikina.

Kauli ya Allah تعالى; وَإِنْ أَطَعْتُمُوهُمْ إِنَّكُمْ لَمُشْرِكُونَ

“Na mkiwafuata basi hapana shaka nyinyi mtakuwa washirikina”.

Maana: Mnaipa mgongo amri na hukumu ya Allah تعالى kwa kutanguliza kauli ya asiyekuwa Allah تعالى huu ni ushirikina. Sawa na Kauli Yake nyingine;

أَتَّخِذُوا أَحْبَابَهُمْ وَوَهَبْنَاهُمْ أَزْوَاجًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ

“Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu”. (9:31)

Katika maelezo ya Aya hii, At-Tirmidhi alinukuu kuwa ‘Adi bin Hatim alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Hawakuwaabudu”. Mtume ﷺ akasema;

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا اَحْلُوْا لَهُمُ الْحَرَامَ وَحَرِّمُوْا عَلَيْهِمُ الْحٰلَالَ فَاتَّبِعُوْهُمْ فَاِنَّكُمْ لَعِبَادَتُهُمْ
يٰۤاَيُّهَا

“Naam, waliwahalalishia vya haramu na wakawaharamishia vya halali, na wao wakawafuata. Huko ndiko kuwaabudu kwao”¹.

اَوْ مِّنْ كَانَ مِيْتًا فَاحْيِيْنٰهُ وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِيْ بِهٖ فِى النَّاسِ كَمَنْ مَّثَلُهٗ فِى الظُّلُمٰتِ
لَيْسَ بِخَارِجٍ مِّنْهَا كَذٰلِكَ زُوِيْنَا لِلْكَٰفِرِيْنَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٢٢﴾

122. Je, aliyekuwa maiti kisha Tukamhuisha, na Tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu, mfano wake ni kama aliyoko gizani akawa hata hawezi kutoka humo? Kama hivyo makafiri wamepambiwa waliyokuwa wakiyafanya.

Mfano wa Kafiri na Muumini.

Hii ni mithili Aliyoipiga Allah تعالى kwa Muumini aliyekuwa mfu, yaani akitangatanga katika maangamizo ya upotevu, basi Yeye Akamfufua, yaani Akauhuisha moyo wake kiimani, Akamhidi na Akamuwafikisha kuwafuata Mitume.

¹ Tufhat Al-Ahwadhi 8:492.

وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِي بِمِ فِي النَّاسِ

"...na Tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu".

Maana: Anaongozwa popote anapopita na namna ya kudumu katika njia sahihi. Nuru ni Qur'an, kwa mujibu wa Al-'Awafi na Ibn abu Twalhah walivyomnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما¹. As-Suddi alisema kuwa ni Uislamu². Maana zote mbili ni sahihi.

كَمَنْ مَثَلُهُ فِي الظُّلْمَتِ

"...mfano wake ni kama aliyoko gizani". La ujahili, matamanio na namna mbalimbali za upotevu.

لَيْسَ بِخَارِجٍ مِّنْهَا

"...akawa hata hawezi kutoka humo?" Inamaanisha kuwa hapati upenyo wa kumuongoza ili anusurike na kuondoka kutoka humo. Katika Musnad Imam Ahmad kuna Hadithi ya Mtume ﷺ kwamba alisema;

«إِنَّ اللَّهَ خَلَقَ خَلْقَهُ فِي ظُلْمَةٍ، ثُمَّ رَسَّ عَلَيْهِمْ مِنْ نُورِهِ، فَمَنْ أَصَابَهُ ذَلِكَ النُّورُ اهْتَدَى، وَمَنْ أَخْطَأَهُ ضَلَّ»

*"Allah تعالى Aliwaumba viumbe Wake gizani, kisha Akawanyunyizia Nuru Yake juu yao. Yule ambaye Nuru hiyo imemsibu huongoka, na ambaye imemkosa ni mpotevu"*³.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُمْ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُمْ مِنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

"Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Huwatoa gizani na Kuwaingiza mwangazani. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni Mashetani. Huwatoa kwenye mwangaza na kuwaingiza gizani. Hao ndio watu wa Motoni, na humo watadumu". (2:257) na,

¹ At-Tabari 12:91.

² At-Tabari 12:91.

³ Ahmad 2:176.

أَفَمَنْ يَمْشِي مُكِبًّا عَلَىٰ وَجْهِهِ أَهْدَىٰ أَمَّنْ يَمْشِي سَوِيًّا عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٦٧﴾

“Je! Anayekwenda akisinukia juu ya uso wake ni mwongofu zaidi, au yule anayekwenda sawa sawa katika njia lliyonyooka?” (67:22)
na,

* مَثَلُ الْفَرِيقَيْنِ كَالْأَعْمَىٰ وَالْأَصْمَىٰ وَالْبَصِيرِ وَالسَّمِيعِ ۗ هَلْ يَسْتَوِيَانِ مَثَلًا ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿١١﴾

“Mfano wa makundi mawili ni kama kipofu, kiziwi na mwenye kuona na anayesikia. Je, wawili hawa wanakuwa sawa kwa kufananishwa? Basi, je, hamfikiri?” (11:24)

وَمَا يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ ﴿١٢﴾ وَلَا الظُّلُمَاتُ وَلَا النُّورُ ﴿١٣﴾ وَلَا الظُّلُمُ وَلَا النُّورُ ﴿١٤﴾ وَمَا يَسْتَوِي الْأَحْيَاءُ وَلَا الْأَمْوَاتُ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُسْمِعُ مَن يَشَاءُ ۗ وَمَا أَنْتَ بِمُسْمِعٍ مَّن فِي الْقُبُورِ ﴿١٥﴾ إِنَّ أَنْتَ إِلَّا نَذِيرٌ ﴿١٦﴾

“Na kipofu na mwenye kuona hawalingani. Wala giza na mwangaza. Wala kivuli na joto. Wala hawalingani walio hai na maiti. Hakika Mwenyezi Mungu Humsikilizisha Amtakaye. Wala wewe si wa kuwasikilizisha walio makaburini. Hukuwa wewe ila ni Mwonyaji”. (35:19-23)

Kuna Aya nyingi kuhusu mada hii. Mnasaba wa kupiga mfano wa vitu viwili vilivyoasiki hapa. Nuru akisi yake ni neno giza ni kama ilivyotangulia hapo mwanzoni mwa Surah hii, katika kuielezea Aya,

وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ

“...na Akafanya giza na mwangaza”. (6:1)

Kauli ya Allah تعالى:

كَذَٰلِكَ نُزَيِّنُ لِلْكَافِرِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Kama hivyo makafiri wamepambiwa waliyokuwa wakiyafanya”.

Maana yake: Kuwapendezeshea ujinga na upotevu walio nao kwa Kudura na Hekima kubwa ya Allah تعالى, kwamba hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى Peke Yake, Asiyekuwa na mshirika.

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا فِي كُلِّ قَرْيَةٍ أَكْبَرًا مُجْرِمِيهَا لِيَمْكُرُوا فِيهَا ۗ وَمَا يَمْكُرُونَ إِلَّا
 بِأَنْفُسِهِمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿١١٨﴾ وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ حَتَّى نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ
 رُسُلُ اللَّهِ ۗ اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ
 وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ ﴿١١٩﴾

123. Kadhalika katika kila mji Tumewajaalia wakubwa wa wakosefu wao wafanye vitimbi ndani yake. Na wala hawafanyi vitimbi isipokuwa nafsi zao, nao hawatambui.

124. Na inapowajia Ishara, wao husema: Hatutoamini mpaka tupewe mfano wa waliopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi kuliko wote Kujua wapi Anaweka ujumbe Wake. Itawafikia hao waliokosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyokuwa wakivifanya”.

Wakuu wa Waovu, Hila Zao na Mwisho Wao.

Allah تعالیٰ Anasema: Kama Tulivyojaalia katika mji wako ewe Muhammad ﷺ, kuwepo kwa wakuu, viongozi wa waovu, na walinganiaji wa ukafiri, uzuiaji njia ya kwenda kwa Allah تعالیٰ, kukukhalifu na kukufanyia uadui, kadhalika, Mitume wa kabla yako walikuwa wakijaribiwa katika hilo, lakini hatimaye wakawa na mwisho mwema. Kama Alivyosema Allah تعالیٰ katika Aya nyingine,

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا مِّنَ الْمُجْرِمِينَ ۗ

“Na hivi hivi Tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wakosefu”. (25:31) na

وَإِذَا أَرَدْنَا أَنْ نُبْلِكَ قَرْيَةً أَمَرْنَا مُتْرَفِيهَا فَفَسَقُوا فِيهَا

“Na pindi Tukitaka Kuuteketeza mji Huwaamrisha wale wenye starehe na taanusi, lakini wao huendelea kutenda maovu humo”. (17:16)

Ilisemwa kuwa, maana yake, “Tuliwaamuru watutii Sisi, lakini wakakhalifu, Tukawaangamiza”. Ilisemwa pia maana yake ni, “Amran Qadariyyan -

Tuliwaamuru kulingana na *Qadar*", kama Alivyosema hapa;

لِيَمْكُرُوا فِيهَا ط

"...wafanye vitimbi ndani yake". Na Kauli Yake Allah تعالى،

أَكْبَرَ مُجْرِمِيهَا لِيَمْكُرُوا فِيهَا ط

"...wakubwa wa wakosefu wao wafanye vitimbi ndani yake".

أَكْبَرَ مُجْرِمِيهَا

"...wakubwa wa wakosefu wao". Amesema: Watukufu wa waovu wao, hivyo wakaasi pindi wanapofanya hivyo Tunawahilikisha kwa kuwatia Adabu.

وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِّنْ نَّذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ ﴿٣٤﴾ وَقَالُوا
نَحْنُ أَكْثَرُ أَمْوَالًا وَأَوْلَدًا وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِينَ ﴿٣٥﴾

"Na Hatukumtuma Mwonyaji yeyote kwenye mji, ila walisema waliojidekeza kwa starehe zao wa mji huo: Hakika sisi tunayakataa hayo mliyotumwa nayo. Na wakasema: Sisi tuna mali mengi zaidi na watoto, wala sisi hatutaadhibiwa". (34:34-35) Na,

وَكَذَلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِّنْ نَّذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ
أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ مُّقْتَدُونَ ﴿٣٦﴾

"Na kadhalika Hatukumtuma Mwonyaji kwenye mji wowote ila watu wake waliodeka kwa starehe walisema: Hakika sisi Tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi tunafuata nyayo zao". (43:23)

Na makusudio ya vitimbi katika Aya (6:123) ni ulinganijaji wao wa kuvutia katika upotevu kwa njia ya maneno na vitendo vya kupamba pamba. Kama Kauli Yake katika khabari za kaumu ya Nuh عليه السلام;

وَمَكُرُوا مَكْرًا كُبْرًا ﴿٧١﴾

"Na Wakapanga vitimbi vikubwa". (71:22) na,

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ مَوْتُوا فَوْتُونَ عِندَ رَبِّهِمْ يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلَ يَقُولُ
الَّذِينَ اسْتَضَعِفُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لَوْلَا أَنْتُمْ لَكُنَّا مُؤْمِنِينَ ﴿٧٢﴾ قَالَ الَّذِينَ

أَسْتَكْبِرُوا لِلَّذِينَ اسْتَضَعُّوهُمُ أَنْحَنُ صَدَدْنَا عَنْ آهْدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ ۗ بَلْ كُنْتُمْ
 مُجْرِمِينَ ﴿٣١﴾ وَقَالَ الَّذِينَ اسْتَضَعُّوهُمُ لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا
 أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ أَندَادًا ۗ

“Na ungeliswaona madhalimu wataposimamishwa mbele ya Mola wao Mlezi, wakirudishiana maneno wao kwa wao! Wanyonge wakiwaambia waliotakabari: Lau kuwa si nyinyi, bila ya shaka tungelikuwa Waumini sisi. Waliotakabari watawaambia wanyonge: Kwani sisi ndio tuliokuzuieni na uwongofu baada ya kukujieni? Bali nyinyi wenyewe ni wakosefu. Na wanyonge watawaambia waliotakabari: Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipokuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu, na Tumfanyie washirika”. (34:31-33)

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisema, baba yetu alituambia, Ibn Abi ‘Umar alituambia, Sufyan alitueleza, “Kitimbi chochote kilichotajwa ndani ya Qur’an kinaashiria amali”. Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا يَمْكُرُونَ إِلَّا بِأَنْفُسِهِمْ وَمَا يَشْعُرُونَ

“Na wala hawafanyi vitimbi isipokuwa nafsi zao, nao hawatambui”.

Maana: Madhara ya vitimbi vyao na jambo la kuwapotosha wale wanaowapotosha utawarudia wao wenyewe.

Sawa na Alivyosema katika Ayah nyingine.

وَلِيَحْمِلُوا أَثْقَالَهُمْ وَأَثْقَالًا مَعَ أَثْقَالِهِمْ ۗ

“Na hapana shaka wataibeba mizigo yao na mizigo mingine pamoja na mizigo yao”. (29:13) Na,

وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَزُرُونَ

“...na sehemu ya mizigo ya wale wanaowapoteza bila ya kujua. Angalia, ni maovu mno hayo wanayoyabeba!” (16:25)

Kauli ya Allah تعالى:

وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ حَتَّى نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلُ اللَّهِ

“Na inapowajia Ishara, wao husema: Hatutoamini mpaka tupewe mfano wa waliopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu”.

Inamaanisha, itakapowajia Ishara, Ushahidi na Hoja isiyopingika, wanasema;

لَنْ نُؤْمِنَ حَتَّى نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلُ اللَّهِ

“Hatutoamini mpaka tupewe mfano wa waliopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu”.

Maana: Hadi Malaika watakapotujia na Ujumbe utokao kwa Allah تعالى, kama unavyokuja kwa Mitume. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْنَا الْمَلٰٓئِكَةُ أَوْ نَرَىٰ رَبَّنَا

“Na walisema wale wasiotaraji kukutana Nasi: Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika au hatumuoni Mola wetu Mlezi?” (25:21)

Kauli ya Allah تعالى;

اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ

“Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi kuliko wote Kujua wapi Anaweka ujumbe Wake”.

Maana yake: Yeye Ndiye Anayejua hasa, ni wapi pa Kuuweka Ujumbe Wake, na pia Kumjua Anayestahiki kubeba jukumu Lake, miongoni mwa viumbe. Sawa na Kauli Yake;

وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ هٰذَا الْقُرْءَانُ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنَ الْفَرِيقَيْنِ عَظِيمٍ ﴿٣١﴾ أَهْمُ يَقْسُمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ

“Na walisema: Kwa nini Qur'an hii haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii? Kwani wao ndio wanaogawa rehema za Mola wako Mlezi?” (43:31-32)

Wanamaanisha, kwa nini Qur'an hii haikuteremshwa kwa mtu kiongozi, mkuu, Mheshimiwa machoni mwao.

مِّنَ الْفَرِيقَيْنِ

“..katika miji miwili hii?”

Maana: Makkah na Twaif. Hilo ni kwa kuwa wao – Allah تعالى Awaangamize – walikuwa wakimdhaliisha Mtume ﷺ kwa uasi, husda, ufidhuli na kiburi. Kauli nyingine ya Allah تعالى inaeleza khabari zao.

وَإِذَا رَأَوْكَ إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُؤًا أَهْذًا الَّذِي بَعَثَ اللَّهُ رَسُولًا ﴿٢٥﴾

“Na wanapokuona hawakuchukulii ila ni mzaha tu, na (wanasema): Ati ndiye huyu Mwenyezi Mungu Aliyemtuma kuwa Mtume?” (25:41) na,

وَإِذَا رَأَاكَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُؤًا أَهْذًا الَّذِي يَذْكُرُ آلِهَتَكُمْ
وَهُمْ بِذِكْرِ الرَّحْمَنِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٢٦﴾

“Na wakikuona waliokufuru hawakufanyi wewe ila ni kitu cha maskhara tu, (wakisema): Je! Ndiye huyu anaye itaja miungu yenu? Na hali wao wanakataa kumkumbuka Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema!” (21:36) na,

وَلَقَدْ أَسْتَجَبْنَا لِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٢٧﴾

“Na Mitume walio kabla yako walikwisha dhihakiwa. Kwa hivyo wale waliowafanyia maskhara yaliwafika yale waliyokuwa wakiyafanyia dhihaka”. (21:41)

Makafiri Wanakiri Juu ya Utukufu wa Nasaba ya Mtume ﷺ.

Makafiri waliyafanya haya huku wakijua fadhila, utukufu na ubora wa nasaba ya Mtume ﷺ; walijua utwahara wa nyumba yake, malezi na makuzi yake, Allah تعالى, Malaika Wake na Waumini wamsalie. Makafiri walikuwa wakimuita Al-Amin – Mwaminifu, hata kabla hajateremshiwa Wahyi. Kiongozi wa makafiri, Abu Sufyan, alikiri jambo hili pindi Heraclius, Mfalme wa Roma Alipomuuliza, “Iko vipi nasaba yake kwenu?” Akajibu, “Nasaba yake ni yenye kuheshimiwa nasi”. Akauliza, “Je mlikuwa mkimtumumu kuongopa kabla hajayasema (hayo ya Utume) aliyoyasema?” Akajibu, “Hapana”. Mazungumzo hayo kwa urefu wake wote yalimjulisha Mfalme wa Roma juu ya usafi wa sifa za Mtume ﷺ kuhusu ukweli wa Utume wake na usahihi wa aliyokuja nayo. Imam Ahmad alimnukuu Wathilah bin Al-Asqa رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ مِنْ وَلَدِ إِبْرَاهِيمَ إِسْمَاعِيلَ، وَاصْطَفَىٰ مِنْ بَنِي إِسْمَاعِيلَ بَنِي كِنَانَةَ
وَاصْطَفَىٰ مِنْ بَنِي كِنَانَةَ قُرَيْشًا وَاصْطَفَىٰ مِنْ قُرَيْشِ بَنِي هَاشِمٍ وَاصْطَفَانِي مِنْ بَنِي
هَاشِمٍ»

“Kwa hakika, Allah Alimchagua Ismail kutoka kwa wana wa Ibrahim; Banu Kinanah kutoka kwa wana wa Ismail, Quraysh kutoka kwa Banu Kinanah, Banu Hashim kutoka kwa Quraysh, na Ameniteua mimi kutoka kwa Banu Hashim”¹.

Muslim peke yake aliinukuu Hadithi hii². Bukhari alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema kwamba Mtume ﷺ alisema;

«بُعِثْتُ مِنْ خَيْرِ قُرُونِ بَنِي آدَمَ قَرْنَا فَقَرْنَا، حَتَّىٰ بُعِثْتُ مِنَ الْقَرْنِ الَّذِي كُنْتُ فِيهِ»

“Nimechaguliwa kutokana na mfuatano wa vizazi bora vya wanadamu, mpaka katika kizazi nilichokuwemo”³.

Kauli ya Allah تعالى;

سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ

“Itawafikia hao waliokosa, udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu”.

Hii ni ahadi ya uhakika Anayoitoa Allah تعالى, na tishio kali kwa wanaofanya kiburi dhidi ya kufuata Mitume wa Allah تعالى na kunyenyekea, waliyokuja nayo. Katika Siku ya Kiyama watu hao watapata adhabu na udhalili wa kudumu. Sababu ya kupewa adhabu ya udhalili katika Siku ya Kiyama ni kwa sababu walikuwa wenye kiburi duniani. Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

“Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhaliike”. (40:60)

Maana yake: Wakiwa duni, dhalili, hakiri. Kauli ya Allah تعالى;

¹ Ahmad 4:107.

² Muslim 4:1682.

³ Fat'hul Al-Bari 6:653.

وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ

“...na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyo kuwa wakivifanya”.

Mara nyingi, vitimbi ni vya uficho, na vinaambatana na hila na khadaa, makafiri watakabiliwa na adhabu kali kutoka kwa Allah تعالى, katika Siku ya Kiyama, ni malipo muwafaka.

وَلَا يَظْلِمُ رُبُّكَ أَحَدًا

“Na Mola wako Mlezi Hamdhulumu Yeyote”. (18:49)

Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine,

يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ ﴿٩﴾

“Siku zitakapo dhihirishwa siri”. (86:9)

Maana yake: Zitakapodhihiri siri, fikra zilizofichikana na dhamira. Katika Hadithi Sahih Mbili kumenukuliwa kuwa Mtume ﷺ alisema;

«يُنْصَبُ لِكُلِّ غَادِرٍ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ، فَيَقَالُ: هَذِهِ غَدْرَةُ فُلَانٍ بِنِ فُلَانٍ
بِنِ فُلَانٍ»

“Katika siku ya Kiyama, itanyanyuliwa bendera kwa kila mlaghai na kutasemwa, “Huu ni ulaghai wa fulani bin fulani bin fulani”¹.

Hikima ya jambo hili ni, kwa kuwa mpango wa ulaghai hufanywa kwa siri, na watu huwa hawana habari, basi, katika Siku ya Kiyama itakuwa ni jambo linalojulikana na hadhara juu ya waliofanya na walichokifanya.

* * *

¹ Fat'hul Al-Bari 6:327 na Muslim 4:1361.

فَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ ۗ وَمَنْ يُرِدْ
 أَنْ يُضِلَّهُ يَجْعَلْ صَدْرَهُ ضَيِّقًا حَرَجًا كَأَنَّمَا يَصَّعْدُ فِي
 السَّمَاءِ ۚ كَذَلِكَ يَجْعَلُ اللَّهُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِينَ لَا
 يُؤْمِنُونَ ﴿١٢٥﴾ وَهَذَا صِرَاطُ رَبِّكَ مُسْتَقِيمًا ۚ قَدْ فَصَّلْنَا
 الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَذَّكَّرُونَ ﴿١٢٦﴾ * هُمْ دَارَ السَّلَامِ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ
 وَهُوَ وَلِيُّهُم بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢٧﴾ وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا
 يَمْعَشَرِ الْجِنِّ قَدْ اسْتَكْبَرْتُمْ مِنَ الْإِنْسِ ۗ وَقَالَ أَوْلِيَاؤُهُمْ
 مِنَ الْإِنْسِ رَبَّنَا اسْتَمْتَعَ بَعْضُنَا بِبَعْضٍ وَوَلَعْنَا أَعْنَاقَنَا
 لِلَّذِي أَجَلَّتْ لَنَا ۚ قَالَ النَّارُ مَثْوَاكُمْ خَالِدِينَ فِيهَا إِلَّا مَا
 شَاءَ اللَّهُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٢٨﴾ وَكَذَلِكَ نُؤَلِّيُ بَعْضَ
 الظَّالِمِينَ بَعْضًا بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٢٩﴾ يَمْعَشَرِ الْجِنِّ
 وَالْإِنْسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنْكُمْ يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِي
 وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَذَا ۚ قَالُوا شَهِدْنَا عَلَىٰ أَنْفُسِنَا ۗ
 وَغَرَّبْتُهُمُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ أَنَّهُمْ كَانُوا
 كَافِرِينَ ﴿١٣٠﴾

فَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ
 صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ ۗ وَمَنْ يُرِدْ أَنْ
 يُضِلَّهُ يَجْعَلْ صَدْرَهُ ضَيِّقًا حَرَجًا
 كَأَنَّمَا يَصَّعْدُ فِي السَّمَاءِ ۚ
 كَذَلِكَ يَجْعَلُ اللَّهُ الرِّجْسَ عَلَى
 الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٢٥﴾

125. Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu Anataka Kumhidi Humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na Anayetaka Apotee Hukufanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hivi Mwenyezi Mungu Ana-jaalia uchafu juu ya wasioamini.

Allah تعالى Anasema;

فَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ
 صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ ۗ

“Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu Anataka Kumhidi Humfungulia kifua chake kwa Uislamu”.

Maana yake: Humrahisishia, Humpa nguvu na Kumsahilishia kwa ajili ya Uislamu, na hizi ni alama za kheri.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

أَفَمَنْ شَرَحَ اللَّهُ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ فَهُوَ عَلَىٰ نُورٍ مِّن رَّبِّهِ^٤

“Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu Amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?)” (39:22) na;

وَلَٰكِنَّ اللَّهَ حَبِيبٌ إِلَيْكُمْ أَلَا يَمَنَّ وَرَبُّنَا فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ^٥
أُولَٰئِكَ هُمُ الرَّشِدُونَ

“Lakini Mwenyezi Mungu Amekupendezeeni Imani, na Akaipamba katika nyoyo zenu, na Amekufanyeni muuchukie ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walioongoka”. (49:7)

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما تعالیٰ Kauli ya Allah

فَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ^٦

“Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu Anataka Kumhidi Humfungulia kifua chake kwa Uislamu”.

Kwa kusema, “Allah تعالیٰ Anasema Ataukunjua moyo wake kwa ajili ya Tauhidi na Imani Kwake”¹. Hii ni sawa na ilivyoielezwa na Abu Malik na wengine, nayo ni dhahiri. Kauli ya Allah تعالیٰ:

وَمَنْ يُرِدْ أَنْ يُضِلَّهُ تَجْعَلْ صَدْرَهُ ضَيِّقًا حَرَجًا

“Na Anayetaka apotee Hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana”.

Neno lililotafsiriwa, “kina dhiki”, husomwa *Dhwayqan* na baadhi ya wasomaji, huku wengine husoma *Dhwayyiqan*. Baadhi yao husoma neno lililotafsiriwa “Kimebana”, *Harijan*, na maana yake ni chenye dhambi, kwa mujibu wa As-Suddi, huku wengine husoma *Harajan*, kwa maana ya hakiruhusu jambo lolote la kumfanya aongoke, wala kitu chochote kinachohusu Imani hakiwezi kupenya ndani. ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alimuuliza bedui mmoja kutoka Mudlaj juu ya *Al-Harajah*, akasema, “Ni mti unaoota kati kati ya miti mingine. Haufikiwi na wanyama wachungwao wala wa mwituni wala kitu kingine”. ‘Umar رضي الله عنه akasema, “Moyo wa mnafiki nao ni hivyo hivyo, jambo jema halimfikii”².

¹ Ad-Dur Al-Manthur 3:356.

² At-Tabari 12:104.

كَأَنَّمَا يَصْعَدُ فِي السَّمَاءِ

"...kama kwamba anapanda mbinguni".

Kwa sababu ya uzito wake wa kupokea imani. Sa'id bin Jubayr alisema kuhusu kauli, "...kifua chake kina dhiki, kimebana". Kila njia ya kuingia moyoni mwake haipitiki¹. Al-Hakam bin Aban alisema 'Ikrimah alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akiizungumzia Aya,

كَأَنَّمَا يَصْعَدُ فِي السَّمَاءِ

"...kama kwamba anapanda mbinguni".

Kwamba inamaanisha, "Kama mwanadamu asivyoweza kupanda juu mbinguni, Tauhidi na imani havitaweza kuingia moyoni mwake, mpaka Allah تعالی Aviingize"².

Imamu Abu Ja'far Ibn Jarir رحمه الله تعالی alisema: Huu ni mfano Alioupiga Allah تعالی kwa moyo wa kafiri huyu juu ya dhiki kali aliyo nayo juu ya kumfikia imani. Anasema, mfano wa kujizuia kwake kuikubali imani na dhiki ya kutokufikiwa nayo ni kama kujizuia kwake kupanda juu mbinguni na kushindwa kwake kufanya hivyo, kwani hilo liko nje ya wasaa na uwezo wake"³. Pia Ameizungumzia Kauli ya Allah تعالی;

كَذَلِكَ تَجْعَلُ اللَّهُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ

"Namna hivi Mwenyezi Mungu Anajaalia uchafu juu ya wasio amini".

Kwamba Allah تعالی Anasema, "Kama ambavyo Allah تعالی Hujaalia kifua cha yeyote Anayetaka kumpotosha kibanwe na dhiki, ndivyo pia Humuachilia shetani amfuata mtu huyo na wengine kama yeye, katika waliokataa kumuamini Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ. Basi shetani humuhadaa dhidi ya njia za Allah تعالی"⁴. Ibn Abu Tualhah alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa neno *Ar-Rijs* (uchafu) linakusudia shetani⁵. Mujahid amesema, *Ar-Rijs* ni kila lisilo na kheri ndani yake⁶. 'Abdur-Rahman Ibn Zayd Ibn Aslam alisema kwamba *Ar-Rijs* maana yake, "adhabu".

¹ At-Tabari 12:105.

² Ad-Dur Al-Manthur 3:356.

³ At-Tabari 12:109.

⁴ At-Tabari 12:110.

⁵ At-Tabari 12:111.

⁶ At-Tabari 12:111.

وَهَذَا صِرَاطُ رَبِّكَ مُسْتَقِيمًا ۗ قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَذَّكَّرُونَ ﴿١٢٦﴾ * هُمْ دَارُ السَّلَامِ
عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ وَهُوَ وَلِيُّهُم بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢٧﴾

126. Na hii ndiyo njia ya Mola wako Mlezi Iliyonyooka. Tumezipambanua Aya kwa watu wanaokumbuka.

127. Hao watapata nyumba ya salama kwa Mola Mlezi wao. Naye Ndiye Rafiki Mlinzi wao kwa sababu ya waliyokuwa wakiyatenda.

Allah تعالی Alipoitaja njia ya walioikosa njia Yake huku wakiwazuia wengine kuifuata Alijulisha juu ya utukufu wa uongofu wa dini ya haki ambayo Aliyomtuma Mtume ﷺ kuifikisha, kisha Alisema;

وَهَذَا صِرَاطُ رَبِّكَ مُسْتَقِيمًا

“Na hii ndiyo njia ya Mola wako Mlezi Iliyonyooka”.

Maana yake: Dini hii Tuliyokuamrisha, ewe Muhammad ﷺ kwa Kukuteremshia hii Qur'an na ndio njia ya Allah تعالی, iliyonyooka.

قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ

“Tumezipambanua Aya”.

Maana yake: Tumezidhihirisha, Tumezibainisha na Tumezitaafsiri.

لِقَوْمٍ يَذَّكَّرُونَ

“...kwa watu wanaokumbuka”.

Maana yake: Kwa wenye kufahamu na kuelewa kile ambacho Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ wanachowajulisha.

هُمْ دَارُ السَّلَامِ

“Hao watapata nyumba ya salama”. Jannah.

عِنْدَ رَبِّهِمْ

“...kwa Mola Mlezi wao” Maana: Siku ya Kiama. Allah تعالی Ameiita Jannah kwa jina la Daru s-Salaam (nyumba ya salam) kwa sababu ya amani iliyomo

humu kwa kuwa wakazi wake wamepitia njia iliyonyooka inayolingana na mienendo ya Mitume na njia yao. Kama walivyosalimika na maradhi ya kwenda upogo, wamefika katika nyumba ya salama.

وَهُوَ وَلِيُّهُمْ

“Naye Ndiye Rafiki Mlinzi wao.”

Muhifadhi, Mlinzi na Mwenye Kuwasaidia.

بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“...kwa sababu ya waliyo kuwa wakiyatenda”.

Maana: Kama malipo kwa sababu ya amali zao njema, Allah تعالى Amewafadhili Amekuwa Mkarimu kwao, na Amewalipa *Jannah*.

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا يَمَعَشَرَ آجِلِينَ قَدْ أَسْتَكْتَرْتُمْ مِنَ الْإِنْسِ ط وَقَالَ أَوْلِيَاؤُهُمْ مِنَ الْإِنْسِ
رَبَّنَا أَسْتَمْتَعَ بَعْضُنَا بِبَعْضٍ وَبَلَّغْنَا أَجَلَنَا الَّذِي أَجَلْتَ لَنَا ؕ قَالَ النَّارُ مَثْوَاكُمْ خَالِدِينَ
فِيهَا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٢٨﴾

128. Na ile Siku Atapowakusanya wote Awaambie: Enyi makundi ya majini! Hakika nyinyi mmechukua wafuasi wengi katika wanadamu. Na marafiki zao katika wanadamu waseme: Mola Mlezi wetu! Tulinufaishana sisi na wao. Na Tumefikia ukomo wetu uliotuwekea. Basi Mwenyezi Mungu Atasema: Moto ndio makazi yenu, mtadumu humo, ila Apendavyo Mwenyezi Mungu. Hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Hikima, na Mwenye Kujua.

Allah تعالى Anasema, “Kumbuka, ewe Muhammad ﷺ, katika unayowaeleza na kuwaonya.”

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا

“Na ile Siku Atapowakusanya wote”.

Maana: Majini na wasaidizi wao katika wanadamu waliokuwa wakiwaabudu wao duniani, na wakajikinga kwao na kuwatii, na kufundishana wao kwa wao, maneno ya kupamba – pamba kwa udanganyifu.

يَمَعَشَرَ الْجِنِّ قَدْ اسْتَكْرَثْتُمْ مِنَ الْإِنْسِ^ط

“Enyi makundi ya majini! Hakika nyinyi mmechukua wafuasi wengi katika wanadamu”.

Maana: Kisha Allah تعالى Atasema, “Enyi makundi ya majini!” Na kuendelea. Kauli ya Allah تعالى;

قَدْ اسْتَكْرَثْتُمْ مِنَ الْإِنْسِ^ط

“...mmechukua wafuasi wengi katika wanadamu”.

Maana yake: Katika kuwapotosha na kuwapoteza. Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

* أَلَمْ أَعْهَدْ إِلَيْكُمْ يَبْنَىءَ آدَمَ أَن لَّا تَعْبُدُوا الشَّيْطَانَ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٦١﴾ وَأَنِ
 أَعْبُدُونِي ۗ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦٢﴾ وَلَقَدْ أَضَلَّ مِنْكُمْ جِبِلًّا كَثِيرًا أَفَلَمْ تَكُونُوا
 تَعْقِلُونَ ﴿٦٣﴾

“Je! Sikuagana nanyi, enyi wanadamu, kuwa msimuabudu shetani? Hakika yeye ni adui dhahiri kwenu. Na ya kwamba mniabudu Mimi? Hii ndiyo njia iliyonyooka. Na bila ya shaka yeye amekwihalipoteza kundi kubwa miongoni mwenu. Je, hamkuwa mkifikiri?” (36:60-62) na;

وَقَالَ أَوْلِيَاؤُهُمْ مِنَ الْإِنْسِ رَبَّنَا اسْتَمْتَعَ بَعْضُنَا بِبَعْضٍ

“Na marafiki zao katika wanadamu waseme: Mola Mlezi wetu! Tulinufaishana sisi na wao”.

Maana yake: Wanadamu wenye urafiki na majini watampa Allah تعالى jibu hili baada ya swali hilo.

Al-Hasan alisema, wala hawakunufaishana wao kwa wao, isipokuwa ni majini walitoa amri, wanadamu wakafanya (waliyo amrisha)¹. Ibn Jurayj alisema, ilikuwa katika zama za ujahili, mtu akipita katika sehemu, husema: “Najikinga kwa mkuu wa bonde hili”, na hivyo ndivyo walivyonufaishana, na ndio udhuru

¹ Ad-Durr Al-Manthur 3:357.

watakaoutoa Siku ya Kiyama”¹. Ama majini hunufaika vipi na watu ni kama tulivyokwishataja. Wanachopata majini ni namna watu wanavyowatukuza wao katika kuwaomba msaada, na wanasema, “Tumekuwa wakubwa wa watu na majini”.

وَبَلَّغْنَا أَجَلَنَا الَّذِي أَجَّلْتَ لَنَا

“Na tumefikia ukomo wetu uliotuwekea”.

Amesema As-Suddi, maana yake, mauti.

قَالَ النَّارُ مَتَّوْنُكُمْ

“Basi Mwenyezi Mungu Atasema: Moto ndio makazi yenu”.

Maana yake: Makazi yenu nyinyi, wao na marafiki zenu.

خَلْدَيْنَ فِيهَا

“...mtadumu humo”.

Maana yake, mtakaa humo milele, isipokuwa Atakapopenda Allah تعالى.

وَكَذَلِكَ نُؤَلِّي بَعْضَ الظَّالِمِينَ بَعْضًا بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٢٩﴾

129. Ndio kama hivi Tunawaelekeza madhalimu wapendane wao kwa wao kwa sababu ya waliyokuwa wakiyachuma.

Madhalimu Husaidiana Wao kwa Wao.

Ma'mar alimnukuu Qatadah katika kuitafsiri Aya hiyo, alisema, watafuatana mmoja baada ya mwingine katika kuingia Motoni².

Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

وَكَذَلِكَ نُؤَلِّي بَعْضَ الظَّالِمِينَ بَعْضًا

“Ndio kama hivi Tunawaelekeza madhalimu wapendane wao kwa wao”.

¹ At-Tabari 12:116.

² Abdur-Razzaq.

Kwamba inakusudia madhalimu wa kijini na wa kibinadamu"¹. Na Akasoma;

وَمَنْ يَعِشْ عَنْ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقِضْ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ ﴿١٢٥﴾

"Anayeyafanyia upotofu maneno ya Ar-Rahmani Tunamuwekea Shetani kuwa ndiye rafiki yake". (43:36)

Akasema kuwa ina maana, Tukawasakiza madhalimu wa kijini kwa madhalimu wa kibinadamu. Baadhi ya washairi walisema; "Hakuna mkono wowote ulio juu ya Mkono wa Allah تعالى, wala hakuna dhalimu yeyote isipokuwa atajaribiwa kwa dhalimu mwengine." Kwa hivyo, maana ya Aya Tukufu, "Kama Tulivyolifanya kundi hili la wanadamu wenye khasara kuwa na urafiki na kikundi cha wale waliwapotosha wao katika majini, kadhalika, ndivyo Tunavyowafanyia madhalimu, Tunawasakiza kulipizana visasi wao kwa wao. Na Tunawaangamiza baadhi yao kwa wengine, na Tunalipiza kisasi baadhi yao kwa wengine hali ya kuwa ni malipo ya udhalimu na madhambi yao".

يَمَعَشَرَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ ءَايَاتِي وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ
يَوْمِكُمْ هَذَا قَالُوا شَهِدْنَا عَلَىٰ أَنفُسِنَا ۗ وَغَرَّتُهُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ
أَنَّهُمْ كَانُوا كَافِرِينَ ﴿١٣٠﴾

130. Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakukujieni Mitume kutokana na nyinyi wenyewe wakikubainishieni ayah Zangu, na wakikuonyeni mkutano wa Siku yenu hii. Nao watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu. Na yaliwadanganya maisha ya dunia. Na watajishuhudia wenyewe ya kwamba walikuwa makafiri.

Majini na Wanadamu Kusailiwa Vikali na Kukiri Kuwa Allah تعالى Aliwatuma Mitume Kwao.

Hii nayo ni adhabu ambayo Allah تعالى Atawapa makafiri, katika majini na watu katika Siku ya Kiyama, Atakapowauliza, ilhali Yeye Ndiye Mjuzi zaidi, iwapo Mitume walifikisha Ujumbe Wake. Swali lenyewe ni hili,

¹ At-Tabari 12:119.

يَمْعَشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ

“Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakukujieni Mitume kutokana na nyinyi wenyewe”.

Maana: Nyote kwa ujumla wenu. Itambulike, Mitume walitokana na wanadamu tu, wala hawakutokana na majini, kama Mujahid, Ibn Jarir na Maimamu wa *Salaf* na waliokuwa nyuma walivyosema. Ushahidi kwamba Mitume walitokana na wanadamu tu, ni Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ^٤

“Hakika Sisi Tumekuletea wahyi wewe kama Tulivyowapelekea wahyi Nuhu na Manabii waliokuwa baada yake”. (4:163) Mpaka;

رُسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لَعَلَّ يُكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ

“Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume”. (4:165)

Na Kauli ya Allah تعالى Alipotoa khabari za Ibrahim عليه السلام؛

وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

“Na Tukajaalia katika dhuriya wake Unabii na Kitabu”. (29:27)

Basi, ikawa Utume na Kitabu vinapelekwa kupitia kwa dhuriya ya Ibrahim عليه السلام, wala hakuna hata mtu mmoja aliyesema, “Kulikuwepo utume kupitia kwa majini kabla ya Ibrahim *Al-Khalil* عليه السلام, Halafu ukakatika baada ya kutumwa yeye”. Pia, Allah تعالى Alisema;

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لَيَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَيَمْشُونَ فِي الْأَسْوَاقِ^٥

“Na Hatukuwatumia kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakienda masokoni”.

(25:20) Na;

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رَجَالًا نُوحِيَ إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَى^٦

“Na Hatukuwatumia Mitume kabla yako isipokuwa wanaume Tuliowafunulia miongoni mwa watu wa mijini...”. (12:109)

¹ At-Tabari 12:122.

Kwa hivyo, majini ni wenye kuwafuata wanadamu katika jambo la utume, ndiyo sababu Allah تعالی Aliizungumzia khabari zao.

وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوا أَنصِتُوا فَلَمَّا قُضِيَ وَلَوْ إِلَىٰ قَوْمِهِمْ مُنْذِرِينَ ﴿٦٠﴾ قَالُوا يَنْقُومَنَا إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا أُنزِلَ مِن بَعْدِ مُوسَىٰ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ وَإِلَىٰ طَرِيقٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٦١﴾ يَنْقُومَنَا أَجِيبُوا دَاعِيَ اللَّهِ وَءَامِنُوا بِهِ يَغْفِرَ لَكُمْ مِّن ذُنُوبِكُمْ وَيُجِرْكُمْ مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٦٢﴾ وَمَنْ لَا يُجِبْ دَاعِيَ اللَّهِ فَلَيْسَ بِمُعْجِزٍ فِي الْأَرْضِ وَلَيْسَ لَهُ مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءُ أُولَٰئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٦٣﴾

“Na wakati Tulipowaleta kundi la majini kuja kwako kuisikiliza Qur’an. Basi walipoihudhuria walisema: Sikilizeni! Na ilipokwishasomwa, walirudi kwa kaumu wao kwenda kuwaonya. Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi tumekisikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake, na kinachoongoza kwenye Haki na kwenye njia iliyonyooka. Enyi kaumu yetu! Mwitikieni Mwenye kuita kwa Mwenyezi Mungu, na muaminini, Mwenyezi Mungu Atakusameheni, na Atakuingeni na adhabu chungu. Na wasiomuitikia mitali wa Mwenyezi Mungu basi hao hawatashinda katika ardhi, wala hawatakuwa na walinzi mbele Yake. Hao wamo katika upotovu uliodhahiri”. (46:29-32)

Hadithi aliyoinukuu At-Tirmidhi na wengine inaeleza kuwa Mtume ﷺ aliwasomea majini Surat Ar-Rahman, na ndani yake kuna Kauli ya Allah تعالی;

سَنَفْرُغُ لَكُمْ أَيُّهَ الثَّقَلَانِ ﴿٦٤﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٥﴾

“Tutakuhisabuni enyi makundi mawili. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayoikanusha?” (55:31-32)¹

Katika Aya hii Tukufu, Allah تعالی Alisema;

¹ Tufhat Al-Ahwadhi 9:177.

يَمَعَشَرَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِي وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ
يَوْمِكُمْ هَذَا قَالُوا شَهِدْنَا عَلَىٰ أَنْفُسِنَا

“Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakukujieni Mitume kutokana na nyinyi wenyewe wakikubainishieni Aya Zangu, na wakikuonyeni mkutano wa Siku yenu hii. Nao watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu”.

Maana yake: Tumekiri kwamba Mitume walitufikishia Ujumbe Wako na wakatutahadharisha kukutana na Wewe, na kwamba Siku hii itatukia, haina shaka. Kauli ya Allah تعالى:

وَعَرَّتَهُمُ الْحَيَاةُ

“Na yaliwadanganya maisha ya dunia”.

Na wamepetuka mipaka katika maisha ya duniani na wakajiangamiza nafsi zao kwa kuwakadhibisha Mitume na kuikana miujiza yao. Haya ni kwa sababu walihadaika na uzuri wa mapambo na tamaa za maisha ya duniani.

وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ

“Na watajishuhudia wenyewe”.

Katika Siku ya Kiyama.

أَنَّهُمْ كَانُوا كَافِرِينَ

“...ya kwamba walikuwa makafiri”

Maana: Duniani, kwa kuyakataa yale waliyoletewa na Mitume, ziwaendee wao rehema na amani za Allah تعالى.

* * *

ذَلِكَ أَنْ لَمْ يَكُنْ رَبُّكَ مُهْلِكَ
 الْفُقَرَىٰ بِظُلْمٍ وَأَهْلُهَا غَفِلُونَ ﴿١٣١﴾
 وَلِكُلِّ دَرَجَةٍ مِّمَّا عَمِلُوا وَمَا رَبُّكَ
 بِغَفِيلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٢﴾ وَرَبُّكَ الْغَنِيُّ ذُو الرَّحْمَةِ
 إِنْ يَشَاءُ يُدْهِبْكُمْ وَيَسْتَخْلِفْ مِنْ بَعْدِكُمْ مَا يَشَاءُ كَمَا
 أَنْشَأَكُمْ مِنْ ذُرِّيَةِ قَوْمٍ ءَاخِرِينَ ﴿١٣٣﴾ إِنَّ مَا
 تُوعَدُونَ لَآتٍ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿١٣٤﴾ قُلْ يَتَقَوَّمِ
 أَعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَائِلٌ ۗ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَنْ
 تَكُونُ لَهُ عَقِيبَةُ الدَّارِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿١٣٥﴾
 وَجَعَلُوا لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ مِنَ الْحَرْثِ وَالْأَنْعَامِ نَصِيبًا فَقَالُوا
 هَذَا لِلَّهِ بِزَعْمِهِمْ وَهَذَا لِشُرَكَائِنَا ۗ فَمَا كَانَ
 لِشُرَكَائِهِمْ فَلَا يَصِلُ إِلَى اللَّهِ ۗ وَمَا كَانَ لِلَّهِ
 يَصِلُ إِلَىٰ شُرَكَائِهِمْ ۗ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿١٣٦﴾
 وَكَذَلِكَ زَيَّنَ لِكَثِيرٍ مِنَ الْمُشْرِكِينَ قَتْلَ
 أَوْلَادِهِمْ شُرَكَائِهِمْ لِيُرْدُوهُمْ وَلِيَلْبِسُوا عَلَيْهِمْ دِينَهُمْ ۗ
 وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا فَعَلُوهُ ۗ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ ﴿١٣٧﴾

ذَلِكَ أَنْ لَمْ يَكُنْ رَبُّكَ مُهْلِكَ
 الْفُقَرَىٰ بِظُلْمٍ وَأَهْلُهَا غَفِلُونَ ﴿١٣١﴾
 وَلِكُلِّ دَرَجَةٍ مِّمَّا عَمِلُوا وَمَا
 رَبُّكَ بِغَفِيلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٢﴾

131. Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola wako Mlezi hakuwa wa kuiangamiza miji kwa dhulma, hali wenyewe wameghafilika.

132. Na wote wana daraja mbali mbali kutokana na yale waliyoyatenda. Na Mola wako Mlezi si Mwenye Kughafilika na yale wanayoyatenda.

Allah تعالى Anasema:

ذَلِكَ أَنْ لَمْ يَكُنْ رَبُّكَ مُهْلِكَ
 الْفُقَرَىٰ بِظُلْمٍ وَأَهْلُهَا غَفِلُونَ ﴿١٣١﴾

“Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola wako Mlezi hakuwa wa Kuiangamiza

miji kwa dhulma, hali wenyewe wameghafilika”.

Maana yake: Tumewapeleka Mitume na Tumeteremsha Vitabu kwa namna mbili za viumbe, majini na wanadamu, ili hata mmoja asiwe na udhuru kwa makosa yake ikiwa hakufikiwa na wito. Hivyo, hatukuuadhibu umma wowote, isipokuwa baada ya kuwapelekea Mitume, ili wakose udhuru. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Alisema;

وَأَنْ مِنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ

"Na hapana umma wowote ila ulipata Mwonyaji kati yao". (35:24)

Na;

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ آعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطُّغُوتَ

"Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani". (16:36) Na;

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا

"Wala Sisi Hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume". (17:15) Na;

تَكَادُ تَمَيِّزُ مِنَ الْغَيْظِ كُلَّمَا أُلْقِيَ فِيهَا فَوْجٌ سَأَلْتَهُمْ خَزَنَتُهُ أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ﴿٦٦﴾ قَالُوا بَلَىٰ قَدْ جَاءَنَا نَذِيرٌ فَكَذَّبْنَا

"Kila mara likitupwa kundi humo walinzi wake huwauliza: Kwani hakukujieni Muonyaji? Watasema: Kwani! Ametujia Muonyaji, lakini tulimkadhibisha". (67:8-9)

Kuna Aya nyingi sana kuhusu mada hii. Kauli ya Allah تعالى;

وَلِكُلِّ دَرَجَةٍ مِمَّا عَمِلُوا

"Na wote wana daraja mbali mbali kutokana na yale waliyoyatenda".

Maana yake: Kila anayemtii Allah تعالى au kumuasi ana daraja na ngazi kulingana na amali yake, ambazo Allah تعالى Anawapa na Kuwalipa, wema kwa wema na shari kwa shari. Mimi nasema, inawezekana kuwa inarejea Kauli ya Allah تعالى;

وَلِكُلِّ دَرَجَةٍ مِمَّا عَمِلُوا

"Na wote wana daraja mbali mbali kutokana na yale waliyoyatenda".

Maana yake: Kafiri wa kijini au wa kibinadamu. Maana yake kila mmoja wao ana daraja yake Motoni kulingana na maovu yake. Sawa na Kauli Yake;

قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٌ

"Itakuwa kwenu nyote maradufu". (7:38) Na;

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ زِدْنَاهُمْ عَذَابًا فَوْقَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوا
يُفْسِدُونَ ﴿١٣٨﴾

“Wale waliokufuru na kuzuilia njia ya Mwenyezi Mungu Tutawazidishia adhabu juu ya adhabu, kwa walivyokuwa wakifisidi”. (16:88)

Allah تعالى Akasema;

وَمَا رُبُّكَ بَغْفِيلٌ عَمَّا يُعْمَلُونَ ﴿١٣٨﴾

**“Na Mola wako Mlezi si Mwenye Kughafilika na yale wanayo-
yatenda”.**

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema; “Amali zote hizi wanazozifanya, Ewe Muhammad ﷺ, walizitenda huku Mola wako Akizijua, Anazikusanya na Kuziandika Kwake Yeye, ili Awajazi watakapokutana Naye na kurejea Kwake”¹.

وَرُبُّكَ الْغَنِيُّ ذُو الرَّحْمَةِ ۚ إِن يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَسْتَخْلِفْ مِن بَعْدِكُم مَّا يَشَاءُ كَمَا
أَنشَأَكُم مِّن ذُرِّيَّةٍ قَوْمٍ ءَاخِرِينَ ﴿١٣٨﴾ ۚ إِن مَّا تُوْعَدُونَ لَأَتِيَنَّكُمْ
بِمُعْجِزَاتِنَا ۚ قُلْ يَنْقُورِ أَعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَامِلٌ ۗ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَن
تَكُونُ لَهُ عَنقِبَةُ الدَّارِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿١٣٩﴾

133. Na Mola wako Mlezi Ndiye Mkwasi, Mwenye Rehema. Akipenda Atakuondoeni na Awaweke wengine Awapendao badala yenu, kama vile Alivyokutoeni kutokana na uzazi wa watu wengine.

134. Bila ya shaka hayo mnayoahidiwa yatafika tu, wala nyinyi hamtaweza kuyaepuka.

135. Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni muwezayo, na hakika mimi nafanya. Mtakuja jua nani atakuwa na makazi mema mwishoni. Hakika madhalimu hawatafanikiwa.

¹ At-Tabari 12:125.

Karipio la Kuwaangamiza Kama Hawatatii.

Allah تعالى Anasema;

وَرَبُّكَ

“Na Mola wako Mlezi”. Ewe Muhammad ﷺ.

أَلْعَبَىٰ

“Ndiye Mkwasi”.

Maana yake: Yu Huru dhidi ya kuwahitaji viumbe Wake kwa namna yoyote, ilhali wao wanamhitaji Yeye katika hali zao zote.

ذُو الرِّحْمَةِ

“Mwenye Rehema”.

Maana yake: Pamoja na hayo, Yeye ni Rahimu kwao. Sawa na Alivyosema Allah تعالى;

إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرءُوفٌ رَّحِيمٌ

“Kwani Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watu na Mwenye Kuwarehemu”. (2:143)

إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ

“Akipenda Atakuondoeni”.

Mtakapo zikhalifu Amri Zake.

وَدَسْتَخَلَفَ مِنْ بَعْدِكُمْ مَا يَشَاءُ

“...na Awaweke wengine Awapendao badala yenu”.

Maana yake: Watu wengine ambao watakuwa Watiifu.

كَمَا أَنْشَأَكُمْ مِنْ ذُرِّيَةِ قَوْمٍ آخَرِينَ

“...kama vile Alivyo Kutoeni kutokana na uzazi wa watu wengine”.

Maana yake: Yeye Analiweza hilo, kwa urahisi na ni sahali Kwake. Kama Alivyoviondoa vizazi vya awali na Kuvileta vingine baada yao, Halikadhalika, Ana uwezo wa Kuwaondoa hao na Kuwaleta wengine.

Sawa na Alivyosema Allah تعالى;

إِنْ يَشَاءُ يُذْهِبْكُمْ أَيُّهَا النَّاسُ وَيَأْتِ بِآخَرِينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ ذَٰلِكَ قَدِيرًا ﴿١٣١﴾

“Akitaka Atakuondoeni, enyi watu! Na Awalete wengineo. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa hayo”. (4:133) na;

* يَتَأْتِيَا النَّاسُ أَنْتُمْ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٣٥﴾ إِنْ يَشَاءُ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿٣٦﴾ وَمَا ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ ﴿٣٧﴾

“Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujitoshwa, Msifiwa. Akitaka Atakuondoeni na Alete viumbe vipya. Na hilo si gumu kwa Mwenyezi Mungu”. (35:15-17) na;

وَاللَّهُ الْغَنِيُّ وَأَنْتُمُ الْفُقَرَاءُ ۗ وَإِن تَتَوَلَّوْا يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَلَكُمْ

“Na Mwenyezi Mungu si Mhitaji, na nyinyi ndio wahitaji. Na mkigeuka Atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi...”.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema kwamba Ya'qub bin 'Utbah alisema kuwa alimsikia Aban bin 'Uthman akiizungumzia Aya;

كَمَا أَنْشَأَكُمْ مِنْ ذُرِّيَّةِ قَوْمٍ آخَرِينَ

“...kama vile Alivyokutoeni kutokana na uzazi wa watu wengine”.

“Dhuriya wa mwanzoni wa asili na dhuriya wa watoto.”¹ Kauli ya Allah تعالى;

إِن مَّا تُوْعَدُونَ لَأَتِيَنَّكُمْ ۗ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿١٣٦﴾

“Bila ya shaka hayo mnayoahidiwa yatafika tu, wala nyinyi hamtaweza kuyaepuka”.

Maana: Waambie ewe Muhammad ﷺ, kuwa swala la kurejea wanakoahidiwa, litatukia na halina shaka.

¹ Ad-Dur Al-Manthur 3:361.

وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ

"...wala nyinyi hamtaweza kuyaepuka".

Maana yake, hamtamuepuka Allah تعالى, bali Yeye ni Muweza wa Kukurudisheni, hata kama mmegeuka vumbi na mifupa. Yeye ni Muweza, Hashindwi na chochote. Kauli ya Allah تعالى;

قُلْ يَاقَوْمِ أَعْمَلُوا عَلَيَّ مَكَاتِبِكُمْ إِنِّي عَامِلٌ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ

"Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni muwezayo, na hakika mimi nafanya. Mtakuja jua".

Hili ni tishio kali na karipio zito kuwa endeleeni katika njia na mwelekeo wenu ikiwa mnadhani kuwa nyinyi mko katika Hidayah, nami nitasalia katika njia na mwenendo wangu. Sawa na Kauli Yake;

وَقُلْ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ أَعْمَلُوا عَلَيَّ مَكَاتِبِكُمْ إِنَّا عَمِلُونَ ﴿١١١﴾ وَأَنْتُمْ مُنْتَظِرُونَ ﴿١١٢﴾

"Na waambie wale wasioamini: Fanyeni muwezavyo, nasi pia Tunafanya. Na ngojeni, na Sisi Tunangoja". (11:121-122)

'Ali bin Abu Twahlah alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akiizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

عَلَيَّ مَكَاتِبِكُمْ

"Fanyeni muwezavyo".

Kwamba maana yake ni, mwelekeo wenu¹.

فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَنْ تَكُونُ لَهُ عَنقَبَةُ الدَّارِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ

"Mtakuja jua nani atakuwa na makazi mema mwishoni. Hakika madhalimu hawatafanikiwa". (6:135)

Maana: Mtakuja kujua ikiwa mwisho mwema ni wangu (mimi Muhammad ﷺ) au wenu (nyinyi makafiri). Allah تعالى Ameitunza Ahadi Yake kwa Mtume Wake ﷺ na Akamnusuru Muhammad ﷺ awashinde waliomkhalifu. Allah تعالى Alimpatia Muhammad ﷺ ushindi wa Makkah dhidi ya kaumu yake

¹ At-Tabari 12:129.

waliomkadhishisha na kumfanyia uadui. Kwa hakika, jambo la Mtume ﷺ likazagaa katika maeneo mengine ya rasi ya Uarabuni, mpaka Yemen na Bahrain, na yote hayo zama za uhai wake. Baada ya kifo chake, ukapatikana ushindi katika ardhi na majimbo mengine zaidi katika kipindi cha Makhalifa wake. Sawa na Alivyosema Allah تعالى:

كَتَبَ اللَّهُ لِلَّهِ لِأَعْلِينَ أَنَا وَرُسُلِي إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢١﴾

“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda”. (58:21) na;

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٢١﴾ يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٢٢﴾

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi. Siku ambayo hautawafaa madhalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata makazi mabaya kabisa”. (40:51-52)

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ﴿١٠٥﴾

“Na hakika Tulikwishaandika katika Zaburi baada ya kumbukumbu, ya kwamba nchi watairithi waja Wangu walio wema”. (21:105)

وَجَعَلُوا لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ مِنَ الْحَرْثِ وَالْأَنْعَامِ نَصِيبًا فَقَالُوا هَذَا لِلَّهِ بِزَعْمِهِمْ وَهَذَا لِشُرَكَائِنَا فَمَا كَانَ لِشُرَكَائِهِمْ فَلَا يَصِلُ إِلَى اللَّهِ وَمَا كَانَ لِلَّهِ فَهُوَ يَصِلُ إِلَى شُرَكَائِهِمْ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿١٠٦﴾

136. Na wamemuwekea Mwenyezi Mungu katika Alivyoviumba, miongoni mwa mimea na wanyama, sehemu, nao husema: Hii ni sehemu ya Mwenyezi Mungu – kwa madai yao – na hii ni ya miungu tunaowashirikisha. Basi vile walivyowakusudia miungu yao havimfikii Mwenyezi Mungu, na vilivyokuwa vya Mwenyezi Mungu huwafikia miungu yao. Ni uovu kabisa hayo wanayoyahukumu.

Ubainifu wa Baadhi ya Amali za Kishirikina.

Hili ni Karipio la Allah تعالى kwa washirikina waliofanya bidaa, ukafiri na ushirikina na wakamfanya Allah تعالى kuwa sehemu ya viumbe Wake (kwa kumfanyia washiriki), ilhali Yeye Ndiye Muumbaji wa kila kitu, Utukufu ni Wake. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

وَجَعَلُوا لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ

“Na wamemuekea Mwenyezi Mungu katika Alivyoviumba”. Maana: Katika Alivyoviumba.

مِنَ الْحَرْثِ

“...miongoni mwa mimea”. Maana yake: mazao na matunda.

وَأَلَّا تَعْلَمَ نَصِيبًا

“...na wanyama, sehemu”. Maana yake: Kiasi fulani.

فَقَالُوا هَذَا لِلَّهِ بِزَعْمِهِمْ وَهَذَا لِشُرَكَائِنَا

“...nao husema: Hii ni sehemu ya Mwenyezi Mungu – kwa madai yao – na hii ni ya miungu tunaowashirikisha”. Kauli ya Allah تعالى;

فَمَا كَانَ لِشُرَكَائِهِمْ فَلَا يَصِلُ إِلَى اللَّهِ وَمَا كَانَ لِلَّهِ فَهُوَ يَصِلُ إِلَى شُرَكَائِهِمْ

“Basi vile walivyowakusudia miungu yao havimfikii Mwenyezi Mungu, na vilivyokuwa vya Mwenyezi Mungu huwafikia miungu yao”.

‘Ali bin Abu Twalhah na Al-‘Awfi walimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما katika kuitafsiri Aya hii, alisema, Maadui wa Allah تعالى, baada ya kuvuna mazao, walikuwa wakigawa fungu la kutoa kwa ajili ya Allah تعالى, fungu jingine kwa ajili ya sanamu. Walilihifadhi fungu la sanamu, iwe ni shamba, matunda au kitu chochote kilichotokana na mavuno walikitunza na kukizuia, kiasi kwamba Waliweza kukiokota kitu chochote kilichodondoka kutoka katika fungu lililotengwa kwa ajili ya As-swamad (Allah تعالى) na kuliongezea katika fungu lililotengwa kwa ajili ya sanamu. Ikiwa maji yaliyotengwa kwa ajili ya sanamu yaliwaelemea na kumwagikia kitu walichokitenga kwa ajili ya Allah تعالى na kikachanganyika na kile walichokitengea sanamu, basi walikifanya kwamba

ni cha sanamu, huku wakisema, huyu (sanamu) ni fakiri, wala hawakukirejesha katika fungu walilolifanya ni la Allah تعالى yaliyowaelemea walichokipanga kwamba ni cha sanamu, walikiacha kuwa ni cha sanamu. Pia walizifanya baadhi ya mali zao kuwa tukufu, kama vile *Bahirah, Saibah, Wasilah na Ham*, na wakaifanya kuwa ya sanamu, na kudai kuwa wanafanya hivyo kama njia ya kujisogeza karibu na Allah تعالى. Allah تعالى Alisema;

وَجَعَلُوا لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ مِنَ الْحَرْثِ وَالْأَنْعَامِ نَصِيبًا

“Na wamemuekea Mwenyezi Mungu katika Alivyoviumba, miongoni mwa mimea na wanyama, sehemu”¹.

Na hivi ndivyo alivyosema Mujahid, Qatadah, As-Suddi na wengine². ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam aliizungumzia Ayah hiyo, “Kila dhabihu aliyetengwa kwa ajili ya Allah تعالى hakuweza kuliwa katu, mpaka wataje pamoja na majina ya miungu, lakini dhabihu waliyemtenga kwa ajili ya miungu hiyo, Jina la Allah تعالى hawakulidhukuru”. Na akaisoma Aya mpaka akafikia,

سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ

“Ni uovu kabisa hayo wanayoyahukumu”³.

Maana: Ni ugawaji mbaya, kwani kwanza wamefanya makosa kuhusu jambo la kugawa, kwani Allah تعالى Ndiye Mola wa kila kitu, ni Mmiliki na Muumbaji Wake, kila kitu kimo katika Kudura na Kutaka Kwake, hapana ghairi Yake wa kuabudiwa kwa haki wala hapana mola mlezi isipokuwa Yeye. Na hata baada ya mgao waliodai wao, Ugawaji huu muovu, hawakudumu nao, bali walifanya udanganyifu. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَيَجْعَلُونَ لِلَّهِ الْآبِنَاتِ سُبْحَانَ اللَّهِ وَلَهُمْ مَا يَشْتَهُونَ

“Na wanamfanyia Mwenyezi Mungu ati Ana mabinti, Subhanahu, Aliyetakasika! Na wao wenyewe, ati ndio wawe na hayo wanayoyatamani”. (16:57) Na;

¹ At-Tabari 12:132.

² At-Tabari 12:133.

³ At-Tabari 12:134.

وَجَعَلُوا لَهُ مِنْ عِبَادِهِ جُزْءًا إِنَّ الْإِنْسَانَ لَكَفُورٌ مُّبِينٌ ﴿١٣١﴾

“Na wakamfanyia katika waja wake fungu. Kwa hakika mwanadamu ni mtovu wa fadhila aliye dhahiri”. (43:15) na;

أَلَمْ تَرَ أَتَىٰ الْكُفْرَ وَلَهُ الْأُنْتَىٰ ﴿١٣٢﴾ تِلْكَ إِذًا قِسْمَةٌ ضِيزَىٰ ﴿١٣٣﴾

“Je! Nyinyi mnao wana wanaume na Yeye ndio awe na wanawake? Huo ni mgawanyo wa dhulma!” (53:21-22)

وَكَذَٰلِكَ زَيْنَ لِكَثِيرٍ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ قَتَلَ أَوْلَادِهِمْ شُرَكَاءَهُمْ لِيُردُّوهُمْ وَلِيَلْبِسُوا عَلَيْهِمْ دِينَهُمْ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا فَعَلُوهُ ۗ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتُرُونَ ﴿١٣٧﴾

137. Na kadhalika hao washirika wao wamewapambia wengi katika washirikina kuwaua watoto wao ili kuwaangamiza na kuwavurugia dini yao. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelipenda wasingefanya hayo. Basi waache na hayo wanayoyazua.

Shetani Huwapambia Washirikina Wawaue Watoto Wao.

Allah تعالیٰ Anasema, kama Shetani alivyowapambia wanaomfanyia Allah تعالیٰ sehemu ya Alivyoviumba, katika mashamba na wanyama, kadhalika waliwapambia kuua watoto wao kwa kukhofia umasikini, na kuwazika mabinti wachanga kwa kuchelea aibu. ‘Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما akisema maana ya;

وَكَذَٰلِكَ زَيْنَ لِكَثِيرٍ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ قَتَلَ أَوْلَادِهِمْ شُرَكَاءَهُمْ

“Kadhalika hao washirika wao wamewapambia wengi katika washirikina kuwaua watoto wao”.

Maana yake: “Waliwafanyia kuwaua watoto wao ili liwe jambo la kuvutia kwao”¹. Mujahid alisema, “...**washirika wao**” ni mashetani wao ambao wanawaamuru wawaue watoto wao kwa hofu ya njaa”². As-Suddi alisema, mashetani wamewaamuru wao wawaue mabinti zao.

لِيُردُّوهُمْ

“...ili kuwaangamiza”. Kuwahilikisha au;

¹ At-Tabari 12:136.

² At-Tabari 12:136.

وَلْيَلْبِسُوا عَلَيْهِمْ دِينَهُمْ^ط

"...na kuwavurugia dini yao."¹

Kuwatibulia dini yao na mfano wake. Allah تعالى Alisema;

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا فَعَلُوهُ^ط

"Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelipenda wasingefanya hayo".

Maana: Kila kinachotokea ni kwa kuachiliwa na Allah تعالى, Kutaka na Kukhitari Kwake kwamba kitu hicho kiwe. Na Yeye Ana Hikima timilifu kuhusu hilo, na huwa Haulizwi Alifanyalo, ilhali wao ni wa kuulizwa.

فَذَرَهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ

"Basi waache na hayo wanayo yazua"

Maana: Usijishughulishe nao, na uepukane na waliyo nayo, na Allah تعالى Atahukumu baina yako na wao.

* * *

¹ At-Tabari 12:137.

وَقَالُوا هَذِهِمُ أَنْعَمُ وَحَرِّثُ حِجْرٌ لَا يَطْعَمُهَا إِلَّا مَنْ
 نَشَاءُ بِرِزْقِهِمْ وَأَنْعَمُوا حُرِّمَتْ ظُهُورُهَا وَأَنْعَمُوا لَا يَذْكُرُونَ
 أَسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا افْتِرَاءً عَلَيْهِ سَيَجْزِيهِمْ بِمَا كَانُوا
 يَفْتَرُونَ ﴿١٣٨﴾ وَقَالُوا مَا فِي بُطُونِ هَذِهِ الْأَنْعَمِ
 خَالِصَةً لِّذُكُورِنَا وَمُحْرَمٌ عَلَىٰ أَرْوَاجِنَا ۗ وَإِنْ يَكُن مِيتَةً
 فَهُمْ فِيهِ شُرَكَاءُ سَيَجْزِيهِمْ وَصَفَهُمْ ۗ إِنَّهُ حَكِيمٌ
 عَلِيمٌ ﴿١٣٩﴾ قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ قَتَلُوا أَوْلَادَهُمْ سَفَهًا بِغَيْرِ عِلْمٍ
 وَحَرَّمُوا مَا رَزَقَهُمُ اللَّهُ افْتِرَاءً عَلَى اللَّهِ قَدْ ضَلُّوا وَمَا
 كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١٤٠﴾ * وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَ جَنَّاتٍ
 مَعْرُوشَاتٍ وَغَيْرَ مَعْرُوشَاتٍ وَالنَّخْلَ وَالزَّرْعَ مُخْتَلِفًا أَكْلُهُ
 وَالزَّيْتُونَ وَالرُّمَّانَ مُتَشَابِهًا وَغَيْرَ مُتَشَابِهٍ ۗ كُلُوا مِنْ
 ثَمَرِهِمْ إِذَا أَثْمَرَ وَآتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ ۗ وَلَا تُسْرِفُوا
 إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴿١٤١﴾ وَمِمَّنْ آتَاكُمْ حُمُولَةٌ
 وَفَرَسًا ۗ كُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ
 الشَّيْطَانِ ۗ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿١٤٢﴾

وَقَالُوا هَذِهِمُ أَنْعَمُ وَحَرِّثُ حِجْرٌ
 لَا يَطْعَمُهَا إِلَّا مَنْ نَشَاءُ بِرِزْقِهِمْ
 وَأَنْعَمُوا حُرِّمَتْ ظُهُورُهَا وَأَنْعَمُوا
 لَا يَذْكُرُونَ أَسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا افْتِرَاءً
 عَلَيْهِ سَيَجْزِيهِمْ بِمَا كَانُوا
 يَفْتَرُونَ ﴿١٣٨﴾

138. Na husema: Wanyama hawa na mimea hii ni mwiko. Hawatokula ila wale tuwapendao – kwa madai yao tu. Na wanyama hawa imeharamishwa migongo yao kupandwa. Na wanyama wengine hawa-litaji Jina la Mwenyezi Mungu juu yao. Wana-mzulia uwongo tu Mwenyezi Mungu. Atawa-lipa kwa hayo wana-yomzulia.

Baadhi ya Mifugo Waliyojiharamishia Washirikina.

'Ali bin Abu Twahlh alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akisema neno Hijr (mwiko) katika Aya linakusudia walichokiharamisha, kama vile Al-Waswilah na mfano wake¹. Pia, Mujahid, Adh-Dhahhak, As-Suddi, Qatadah, 'Abdurrahman bin Zayd bin Aslam na wengine walisema hivyo hivyo². Qatadah alisema tena;

¹ At-Tabari 12:143.

² At-Tabari 12:143.

وَقَالُوا هَذِهِمُ أَنْعَمُوا وَعَحْرَثُ حِجْرٌ

“Na husema: Wanyama hawa na mimea hii ni mwiko.”

“Ni kuharamishwa ambako mashetani waliamua katika mali zao na namna ya kujiwekea uzito na kushadidisha, wala si kutoka kwa Allah تعالیٰ.”

Ibn Zayd bin Aslam naye alisema;

حِجْرٌ

“..ni mwiko.”

Waliojiwekea kwa ajili ya miungu wao¹. As-Suddi alisema kuhusu Aya;

لَا يَطْعُمَهَا إِلَّا مَنْ نَشَاءُ بِزَعْمِهِمْ

“Hawatokula ila wale tuwapendao – kwa madai yao tu”.

Wanasema: “Ni haramu kula isipokuwa wale tunaowataka (ndio watakaokula)”².

Na Aya hii Tukufu ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ;

قُلْ أَرَأَيْتُمْ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ لَكُمْ مِنْ رِزْقٍ فَجَعَلْتُمْ مِنْهُ حَرَامًا وَحَلَالًا قُلْ إِنَّ اللَّهَ أَدْبَرَ لَكُمْ

أَمْرًا عَلَى اللَّهِ تَفْتَرُونَ ﴿١٠٥﴾

“Sema! Je, Mwaonaye zile riziki alizokuteremshieni Mwenyezi Mungu nanyi mkafanya katika hizo nyingine haramu na nyingine halali. Sema: Je! Mwenyezi Mungu Amekuruhuni, au mnamzulia Mwenyezi Mungu tu?” (10:59) na;

مَا جَعَلَ اللَّهُ مِنْ نَجِيرَةٍ وَلَا سَائِبَةٍ وَلَا وَصِيلَةٍ وَلَا حَامٍ وَلَكِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يَفْتَرُونَ عَلَى

اللَّهِ الْكَذِبَ وَأَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٠٦﴾

“Mwenyezi Mungu Hakujaalia uharamu wowote juu ya “Bahira” wala “Saiba” wala “waswila” wala “Hami”. Lakini waliokufuru humzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na wengi wao hawatunii akili”. (5:103)

¹ At-Tabari 12:143.

² At-Tabari 12:143.

As-Suddi alisema, wanyama ambao waliharamishwa kubeba mizigo walikuwa *Al-Bahirah, As-Saibah, Al-Waswilah na Al-Ham na* mifugo ambayo Jina la Allah تعالی lilikuwa halitajwi na washirikina wakati wa kuchinja wala wakati wa kuzaliwa. Abu Bakr ibn 'Iyash alisema 'Asim bin An-Najud aliniambia, "Unajua maana ya Kauli ya Allah تعالی:

وَأَنْعَمَ حُرْمَتَ ظُهُورِهَا وَأَنْعَمَ لَا يَذْكُرُونَ أَسْمَاءَ اللَّهِ عَلَيْهَا

"Na wanyama hawa imeharamishwa migongo yao kupandwa. Na wanyama wengine hawalitaji Jina la Mwenyezi Mungu juu yao..."

Nikasema, "Hapana". Akasema, "Ni *Bahirah* ambaye hawakumtumia kwa ajili ya *Hijja* (ima kwa kumpanda au kumbebesha mizigo juu yao)"¹. Mujahid alisema, kulikuwa na baadhi ya ngamia ambao Jina la Allah تعالی lilikuwa hawalidhukuru wala kwa jambo lolote lililowahusu, kama wakiwapanda, wakiwakamua maziwa, wakibeba mizigo, kuwapandisha au kitendo kingine chochote².

أَفْتَرَاءً عَلَيْهِ

"Wanamzulia uwongo tu"

Allah تعالی kwa kulinasibisha ovu hili katika Dini na Sharia ya Allah تعالی kwani hakuwaruhusu kufanya hivyo wala kuwaridhia.

سَيَجْزِيهِمْ بِمَا كَانُوا يَفْتَرُونَ.

"Atawalipa kwa hayo wanayomzulia". Juu Yake na kumnasibisha nayo.

وَقَالُوا مَا فِي بُطُونِ هَذِهِ الْأَنْعَامِ خَالِصَةٌ لِّذُكُورِنَا وَمُحْرَمٌ عَلَىٰ أَرْوَاجِنَا ۗ وَإِن يَكُن مَّيْتَةً فَهُمْ فِيهِ شُرَكَاءُ ۗ سَيَجْزِيهِمْ وَصَفَهُمْ ۗ إِنَّهُرَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٣٩﴾

139. Na husema: Waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu, na wameharamishwa kwa wake zetu. Lakini ikiwa nyamafu basi wanashirikiana. Mwenyezi Mungu Atawalipa kwa maelezo yao hayo. Hakika Yeye ni Mwenye Hikima, Mwenye Kujua.

¹ At-Tabari 12:143.

² At-Tabari 12:145.

Abu Is-haqas-Subay' amesema 'Abdullah bin Abu Al-Hudhayl amemnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما juu ya Aya;

وَقَالُوا مَا فِي بُطُونِ هَذِهِ الْأَنْعَامِ خَالِصَةٌ لِّذُكُورِنَا

"Na husema: Waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu".

Akasema, ni maziwa¹. Al'Awfi alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa ayah;

وَقَالُوا مَا فِي بُطُونِ هَذِهِ الْأَنْعَامِ خَالِصَةٌ لِّذُكُورِنَا وَمُحَرَّمٌ عَلَىٰ أَزْوَاجِنَا

"Na husema: Waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu".

Inazungumzia maziwa ambayo walikuwa wakiwakataza wanawake na wanakunywa wanaume katika wao, na ilikuwa, mbuzi alipozaa mwanambuzi dume walimchinja huyo mzaliwa na kuliwa na wanaume tu, si wanawake. Na alipozaa jike aliachwa, hakuchinjwa. Na alipozaa mfu wakawa wanakula wote, Allah تعالى Akaikataza tabia hii². Na As-Suddi alisema hivyo hivyo³.

As-Sha'bi alisema, maziwa ya *Bahirah* hayanywiwi ila na wanaume tu, lakini mifugo yoyote ya *Bahirah* ilipokufa, ililiwa na wanaume na wanawake. Na hivi ndivyo alivyosema 'Ikrimah, Qatadah na 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam. Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

وَقَالُوا مَا فِي بُطُونِ هَذِهِ الْأَنْعَامِ خَالِصَةٌ لِّذُكُورِنَا وَمُحَرَّمٌ عَلَىٰ أَزْوَاجِنَا

"Na husema: Waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu, na wameharamishwa kwa wake zetu".

Kwa kusema, "Inarejea *Sa'ibah na Bahirah*"⁴. Abu Al-'Aliyyah, Mujahid na Qatadah walizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

سَيَجْزِيهِمْ وَصَفَهُمْ

"Mwenyezi Mungu Atawalipa kwa maelezo yao hayo...".

¹ At-Tabari 12:146.

² At-Tabari 12:147.

³ At-Tabari 12:148.

⁴ At-Tabari 12:148.

Maana: Kwa kuongopa kwao¹. Hili limeelezwa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَلَا تَقُولُوا لِمَا تَصِفُ أَلْسِنَتُكُمُ الْكَذِبَ هَذَا حَلَلٌ وَهَذَا حَرَامٌ لِّتَفْتَرُوا عَلَى اللَّهِ
الْكَذِبَ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿١١٦﴾

“Wala Msiseme uongo, kwa kuropokwa na ndimi zenu: Hichi halali na hichi haramu – mkimzulia uongo Mwenyezi Mungu. Hakika wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa”.
(16:116-117)

إِنَّهُ حَكِيمٌ

“Hakika Yeye ni Mwenye Hikima”. Katika Kauli, Matendo, Sharia na Qadari Yake.

عَلِيمٌ

“Mwenye Kujua”. Juu ya amali za kheri na za shari za waja Wake na Atawalipa malipo timilifu.

قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ قَتَلُوا أَوْلَادَهُمْ سَفَهًا بِغَيْرِ عِلْمٍ وَحَرَّمُوا مَا رَزَقَهُمُ اللَّهُ افْتِرَاءً عَلَى اللَّهِ قَدْ
ضَلُّوا وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١٤٠﴾

140. Hakika wamekhasirika wale ambao wamewaua watoto wao kwa upumbavu pasipokujua, na wakaharamisha Alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu kwa Kumzulia Mwenyezi Mungu. Hakika wamepotea, wala hawakuwa wenye kuongoka.

Allah تعالى Anasema waliofanya hayo, wamekhasirika duniani na Akhera. Ama duniani, walikhasirika kwa kuwaua watoto wao, wakadhikika na mali zao, na wakajiharamishia vitu kadha walivyovizua wao wenyewe. Ama Akhera wataishia katika makazi mabaya kabisa kwa kumkadhibisha Allah تعالى na kumzushia kwao. Ni sawa na Kauli Yake;

قُلْ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿١٤١﴾ مَتَّعٌ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ
إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿١٤٢﴾

“Sema: Hao wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo

¹ At-Tabari 12:152.

yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao". (10:69-70)

Katika kuitafsiri Aya hii Al-Hafidh Abu Bakr Ibn Marduwyah alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akisema, "Kama itakufurahisha kuujua ujinga wa Waarabu ulivyokuwa, basi, soma Aya zilizo baada ya ile ya mia na thelathini katika Surat Al-An'am.

قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ قَتَلُوا أَوْلَادَهُمْ سَفَهًا بِغَيْرِ عِلْمٍ وَحَرَّمُوا مَا رَزَقَهُمُ اللَّهُ افْتِرَاءً عَلَى اللَّهِ قَدْ ضَلُّوا وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿٦٩﴾

"Hakika wamekhasirika wale ambao wamewauwa watoto wao kwa upumbavu pasipokujua, na wakaharamisha Alivyo waruzuku Mwenyezi Mungu kwa kumzulia Mwenyezi Mungu. Hakika wamepotea, wala hawakuwa wenye kuongoka".

Pia, Al Bukhari alinukuu haya katika Sura mojawapo katika Sahih juu ya fadhila za Quraysh¹.

* وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَ جَنَّاتٍ مَعْرُوشَاتٍ وَغَيْرَ مَعْرُوشَاتٍ وَالنَّخْلَ وَالزَّرْعَ مُخْتَلِفًا أُكُلُهُ وَالزَّيْتُونَ وَالرُّمَانَ مُتَشَابِهًا وَغَيْرَ مُتَشَابِهٍ ۗ كُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَءَاتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ ۗ وَلَا تُسْرِفُوا ۗ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴿٧٠﴾ وَمِنَ الْأَنْعَامِ حَمُولَةٌ وَفَرَسَاتٌ ۗ كُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوتِ الشَّيْطَانِ ۗ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٧١﴾

141. Na Yeye Ndiye Aliyeziumba bustani zenye kutambaa juu ya chanja, na zisiotambaa, na mitende, na mimea yenye matunda mbali mbali, na mizaituni na makomamanga inayofanana. Kuleni matunda yake inapozaa, na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake. Wala msitumie kwa fujo. Hakika Yeye Hawapendi watumiao kwa fujo.

142. Na katika wanyama Amekujaalieni wenye kubeba mizigo na kutoa matandiko. Kuleni katika Alivyokuruzukuni Mwenyezi Mungu, wala msifuata nyayo za Shetani. Hakika yeye ni adui yenu dhahiri.

¹ Fat'hul Al-Bari 6:636.

Allah تعالی Ndiye Aliyeumba Matunda, Nafaka na Mifugo.

Allah تعالی Anasema kwamba Yeye Ndiye Muumbaji wa kila kitu, ikiwa ni pamoja, matunda na mifugo ambayo washirikina hawa wameingiza ndani yake mila na desturi zao potofu na kukakasimu na kugawa mafungu kwa kuhalalisha baadhi ya mafungu na kuharamisha mingine. Akasema;

وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَ جَنَّاتٍ مَّعْرُوشَاتٍ

“Na Yeye Ndiye Aliyeziumba bustani zenye kutambaa juu ya chanja, na zisiotambaa...”

‘Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما juu ya Kauli ya Allah تعالی, “zenye kutambaa juu ya chanja”. Inamaanisha zile ziizowekewa chanja, na katika nukuu nyingine, maana yake ni zile ambazo watu wameziwekea fito, “...na zisiotambaa” ni matunda yanayojiotea yenyewe katika nchi kavu na milimani¹. ‘Ata Al-Khurasani alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kwamba alisema, “...zenye kutambaa juu ya chanja” ni zabibu zilizowekewa fito, “...na zisiotambaa” ni zabibu zisizowekewa fito. Na hivyo ndivyo alivyosema As-Suddi. Ibn Jurayj alisema, “...inayofanana na isiyofanana”. Kwa maana ya, “...inayofanana” kwa namna inavyoonekana, “...isiyofanana” katika vyakula². Muhammad bin Ka'b alisema;

كُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ

“Kuleni matunda yake inapozaa”. Amesema, “(Kuleni) kutokana na tende mbichi na zabibu mbichi”³. Na Kauli ya Allah تعالی;

وَأَتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ

“...na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake”. Mujahid aliizungumzia Ayah hii, “Masikini wakikujia, wapeni kiasi”⁴. Na ‘Abdur-Razzaq alimnukuu Mujahid akiizungumzia Aya;

وَأَتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ

“...na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake”.

¹ At-Tabari 12:156.

² At-Tabari 12:157.

³ At-Tabari 12:157.

⁴ At-Tabari 12:163.

Kwa kusema, "Wakati wa kupanda, anatoa gao (la mbegu) na wakati wa mavuno, anatoa gao na anawaachia wachukue mabaki yaliyosalia katika eneo la mavuno"¹. Ath-Thawri alimnukuu Ibrahim An-Nakha'i kwamba alisema, "Atoe mithili ya nyasi kavu"². Ibn Al-Mubarak alimnukuu Sa'id bin Jubayr;

وَأَتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ^ط

"...na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake".

Kwamba alisema, "Jambo hili la kuwapa masikini gao (la mbegu na nyasi kavu) kwa wanyama wao, ilikuwa kabla ya kufaradhiwa Zakah". Allah تعالى Ameshawakemea wanaovuna, bila ya kutoa Sadaka, kama Alivyotaja kisa cha wamiliki wa bustani katika *Suratun-Nun*.

إِذْ أَقْسَمُوا لَيَصْرِمُنَّهَا مُصْبِحِينَ ﴿٧﴾ وَلَا يَسْتَنْتُونَ ﴿٨﴾ فَطَافَ عَلَيْهَا طَائِفٌ مِّن رَّبِّكَ وَهُمْ نَائِبُونَ ﴿٩﴾ فَأَصْبَحَتْ كَالصَّرِيمِ ﴿١٠﴾ فَتَنَادُوا مُصْبِحِينَ ﴿١١﴾ أَنِ اغْدُوا عَلَيَّ حَرْثِكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٢﴾ فَانطَلَقُوا وَهُمْ يَتَخَفَتُونَ ﴿١٣﴾ أَن لَّا يَدْخُلُهَا الْيَوْمَ عَلَيْكُمْ مَسْكِينٌ ﴿١٤﴾ وَغَدَوَا عَلَى حَرْدٍ قَدِيرِينَ ﴿١٥﴾ فَلَمَّا رَأَوْهَا قَالُوا إِنَّا لَضَالُونَ ﴿١٦﴾ بَلْ نَحْنُ مَحْرُومُونَ ﴿١٧﴾ قَالَ أَوْسَطُهُمْ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ لَوْلَا تُسَبِّحُونَ ﴿١٨﴾ قَالُوا سُبْحَانَ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿١٩﴾ فَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَلَومُونَ ﴿٢٠﴾ قَالُوا يَبُولْنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٢١﴾ عَسَى رَبِّنَا أَنْ يُبَدِّلَنَا خَيْرًا مِّنْهَا إِنَّا إِلَى رَبِّنَا رَاغِبُونَ ﴿٢٢﴾ كَذَلِكَ الْعَذَابُ ۖ وَالْعَذَابُ الْآخِرَةُ أَكْبَرُ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٢٣﴾

"Walipoapa kwamba watayavuna mazao yake itakapowadia asubuhi. Wala hawakusema: Mungu Akipenda! Basi lilitokea tukio juu yake kutoka kwa Mola wako Mlezi, nao wamelala! Likawa kama usiku wa giza. Asubuhi wakitana. Ya kwamba Nendeni kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna. Basi walikwenda na huku wakinong'onezana, Ya kuwa leo hata masikini mmoja asikuingilieni. Na walikwenda asubuhi, nao wameshikilia azimio hilo. Basi

¹ Abdur-Razzaq 2:219.

² At-Tabari 12:165.

walipoliona, wakasema: Hakika tumepotea! Bali tumenyimwa! Mbora wao akasema: Sikukuambieni, kwa nini hamumtakasi Mwenyezi Mungu? Wakasema: Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tulikuwa wenye kudhulumu. Basi wakakabilia kulaumiana wao kwa wao. Wakasema: Ole wetu! Tulikuwa tumeikiuka mipaka! Asaa Mola wetu Mlezi Akatubadilishia lililo bora kuliko hili. Hakika sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi. Namna hivi yanakuwa mateso, na bila ya shaka mateso ya Akhera ni makubwa zaidi, laiti wangelijua!” (68:18-33)

Ubainifu wa Kukatazwa Ufujaji.

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ

“Wala msitumie kwa fujo. Hakika Yeye Hawapendi watumiao kwa fujo”.

Imesemwa kuwa maana yake: Msifanye Israfu katika kutoa kwa kuzidi kiasi cha kawaida. Ibn Jurayj alisema, “Ayah hii iliteremshwa kumhusu Thabit bin Qais bin Shammash ambaye alikonyoa tende kadha kutoka katika miti yake, kisha akasema, “Leo hanijii yeyote bali nitamlisha”. Akawalisha mpaka jioni ikafika akiwa hana hata tende moja. Allah تعالى Akateremsha;

وَلَا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ

“Wala msitumie kwa fujo. Hakika Yeye Hawapendi watumiao kwa fujo”.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliinukuu kutoka kwa Thabit. Hata hivyo maana ya wazi ya Aya hii, Allah تعالى ni Mjuzi zaidi, ni kwamba;

كُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَآتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ وَلَا تُسْرِفُوا

“Kuleni matunda yake inapozaa, na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake. Wala msitumie kwa fujo...”.

Imerejea katika kula, maana yake, ‘Msifanye Israfu katika kula kwa kuwa husababisha madhara ya kiakili na kimwili.’ Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا

"...na kunyweni na wala Msifanye ubadhirifu". (7:31)

Katika Sahih Al-Bukhari kuna Hadithi ifuatayo iliyonukuliwa na isnadi ya wasimuliaji;

«كُلُوا وَاشْرَبُوا وَابْتَسُوا مِنْ غَيْرِ إِسْرَافٍ وَلَا مَخِيلَةٍ»

"Kuleni na kunyweni na vaeni pasi na kufanya ufujaji na kuwa na majivuno".

Manufaa ya Mifugo.

Kauli ya Allah تعالى;

وَمِنَ الْأَنْعَامِ حَمُولَةٌ وَفَرَشَاتٌ

"Na katika wanyama Amekujaalieni wenye kubeba mizigo na kutoa matandiko..."

Maana: Alikuumbieni mifugo ambayo baadhi yake hutumika kwa ajili ya kubeba mizigo na wengine ni *Farsh*. Ilisemwa kwamba kusudio la wabebao mizigo ni wanyama kama ngamia, na *Farsh* ni wadogo kuliko huyo. Hayo ni kwa mujibu wa nukuu ya Al-Hakim na akasema, "Isnadi yake ni Sahih lakini wote wawili hawakuinukuu"². 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema, "Wanyama wabebaji ni wale mnaopanda na *Farsh* ni wale mnaokula nyama zao na mnawakamua maziwa. Mbuzi huwa hawezi kubeba, bali Mnakula nyama yake na mnachukua sufu nyingi kwa ajili ya nguo na mabusati"³. Haya aliyoyasema 'Abdur-Rahman yana nguvu, na yanathibitishwa na Kauli ya Allah تعالى;

أُولَئِكَ يَرَوْنَ أَنَّا حَلَقْنَا لَهُمْ مِمَّا عَمِلَتْ أَيْدِينَا أَنْعَامًا فَهُمْ لَهَا مَلَائِكُونَ ﴿٧١﴾ وَذَلَّلْنَاهَا لَهُمْ

فَعَمِيَتْ رُكُوبُهُمْ وَمِنْهَا يَأْكُلُونَ ﴿٧٢﴾

"Je! Hawaoni kwamba Tumewaumbia kutokana na iliyofanya Mikono Yetu wanyama wa mifugo, na wao wakawa wenye kuwamiliki. Na Sisi Tukawadhalilisha. Basi baadhi yao wako wanaowapanda, na baadhi yao wanawala". (36:71-72) Na;

¹ Kitabu cha mavazi, sura ya kwanza, kukiwa na maneno tofauti kidogo. Ilinukuliwa na Ibn Majah, An-Nasai na wengine, kwa isnadi iliyo kamili.

² Al-Hakim 2:317.

³ At-Tabari 12:181.

وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً ۚ نُسْقِيكُمْ مِمَّا فِي بُطُونِهِمْ مِنْ بَيْنِ فَرْثٍ وَدَمٍ لَبَنًا خَالِصًا سَائِغًا
لِّلشَّارِبِينَ ﴿١٣٨﴾

“Na hakika katika wanyama hao nyinyi mna mazingatio. Tunakunywesheni katika vile viliomo matumboni mwao, vikatoka baina ya mavi na damu, maziwa safi mazuri kwa wanywao”. (16:66)
Mpaka Aliposema;

وَمِنْ أَصْوَابِهَا وَأَوْبَارِهَا وَأَشْعَارِهَا أَثْنَا وَمِئْتًا إِلَىٰ حِينٍ

“Na kutokana na sufi zao na manyoya yao na nywele zao mnafanya matandiko na mapambo ya kutumia kwa muda”. (16:80)

Kuleni Nyama za Wanyama Hawa, Wala Msizifuate Nyayo za Shetani.

Kauli ya Allah تعالى:

كُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ

“Kuleni katika Alivyokuruzukuni Mwenyezi Mungu”.

Maana: Matunda, Mazao na mifugo, wote wameumbwa na Allah تعالى na Akajaalia kuwa riziki yenu.

وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ۚ

“...wala msifuate nyayo za Shetani”.

Maana: Njia na amri zake, kama walivyomfuata washirikina ambao aliharamisha matunda na mazao waliyoruzukiwa na Allah تعالى kwa kumzulia Allah تعالى kwamba hilo lilitoka Kwake.

إِنَّهُ لَكُمْ

“Hakika yeye kwenu”.

Kwa hakika, enyi watu, shetani kwenu nyinyi.

عَدُوٌّ مُّبِينٌ

“...ni adui yenu dhahiri”. Uadui wake uko dhahiri. Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٦﴾

“Hakika Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui. Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni”. (35:6) Na;

يَبْنِيْءَ آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمْ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ مِنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْءَٰهُمَا

“Enyi wanadamu! Asije Shetani kukufitinini kama alivyowatoa Wazazi wenu Peponi, akawavua nguo zao kuwaonesha tupu zao”. (7:27)

Na Kauli nyingine;

أَفْتَتَحِدُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا ﴿٥٠﴾

Je! Mnamshika yeye na dhuriya wake kuwa marafiki badala Yangu, hali wao ni adui zenu? Ni uovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu”. (18:50)

Aya zinazohusu mada hii ziko nyingi ndani ya Qur'an.

* * *

تَمَيَّنِيَّةَ أَزْوَاجٍ مِّنَ الْأُنثَىٰ وَوَيْسَ الْأَمْعَرِ أُنثَىٰ ۗ
 قُلْ ۗ وَالذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ الْأُنثَىٰنِ ۗ أَمَا اشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ أَرْحَامٌ
 الْأُنثَىٰنِ ۗ نَبِّئُونِي بِعِلْمٍ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٤٣﴾ وَمِنَ
 الْإِبِلِ أُنثَىٰنِ ۗ وَمِنَ الْبَقَرِ أُنثَىٰنِ ۗ قُلْ ۗ وَالذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ
 الْأُنثَىٰنِ ۗ أَمَا اشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ أَرْحَامٌ الْأُنثَىٰنِ ۗ أَمْ كُنْتُمْ
 شُهَدَاءَ إِذْ وَصَّيْنَاكُم بِالْحَقِّ ۗ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ
 عَلَى اللَّهِ كَذِبًا لِّيُضِلَّ النَّاسَ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي
 الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٤٤﴾ قُلْ لَا أُجِدُ فِي مَا أُوحِيَ إِلَيَّ
 مُحَرَّمًا عَلَىٰ طَاعِمٍ يَطْعَمُهُ إِلَّا أَنْ يَكُونَ مِمَّنَّاءَ أَوْ دَمًا
 مَّسْفُوحًا أَوْ لَحْمَ خِزْيِيرٍ فَإِنَّهُ رِجْسٌ أَوْ فِسْقًا أُهْلًا لِّغَيْرِ
 اللَّهِ بِهِ ۗ فَمَنْ أَضْطَرُّ غَيْرِ مَا نَبَا ۗ وَلَا عَادٍ فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٌ
 رَّحِيمٌ ﴿١٤٥﴾ وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا كُلَّ ذِي ظُفْرِ
 ۗ وَمِنَ الْبَقَرِ وَالْغَنَمِ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُومَهُمَا إِلَّا مَا
 حَمَلَتْ ظُهُورُهُمَا أَوْ الْحَوَايَا أَوْ مَا اخْتَلَطَ بِعَظْمٍ ۗ ذَلِكَ

جَزَيْتَهُمْ بِغَيْرِهِمْ ۗ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿١٤٦﴾

تَمَيَّنِيَّةَ أَزْوَاجٍ مِّنَ الْأُنثَىٰنِ أُنثَىٰ ۗ
 وَمِنَ الْأَمْعَرِ أُنثَىٰ ۗ قُلْ
 ۗ وَالذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ الْأُنثَىٰنِ ۗ أَمَا
 اشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ أَرْحَامٌ الْأُنثَىٰنِ ۗ
 نَبِّئُونِي بِعِلْمٍ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ
 ﴿١٤٣﴾ وَمِنَ الْإِبِلِ أُنثَىٰنِ وَمِنَ
 الْبَقَرِ أُنثَىٰنِ ۗ قُلْ ۗ وَالذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ
 أَمِ الْأُنثَىٰنِ ۗ أَمَا اشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ
 أَرْحَامٌ الْأُنثَىٰنِ ۗ أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ
 إِذْ وَصَّيْنَاكُم بِالْحَقِّ ۗ فَمَنْ أَظْلَمُ
 مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا
 لِّيُضِلَّ النَّاسَ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا
 يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٤٤﴾

143. Amekuumbieni namna
 nane za wanyama: Wawili
 katika kondoo, na wawili

katika mbuzi. Sema: Je, Ameharamisha yote madume mawili au majike
 mawili, au waliomo matumboni mwa majike yote mawili? Niambieni kwa
 ilimu ikiwa nyinyi mnasema kweli.

144. Na wawili katika ngamia, na wawili katika ng'ombe. Sema: Je,
 Ameharamisha yote madume mawili au majike mawili, au waliomo
 matumboni mwa yote majike? Au Mlikuwapo Mwenyezi Mungu Alipokuusieni
 haya? Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule aliyemzulia Mwenyezi Mungu

uwongo kwa ajili ya kuwapoteza watu bila ya ilimu? Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongozi watu madhalimu.

Aya hizi zinaonesha ujinga wa Waarabu kabla ya Uislamu kwa namna walivyokuwa wameharamisha mifugo yao na kugawa katika namna kama *Bahirah, Saibah, Waswilah na Ham*, na mifugo mingine, matunda na mazao, miongoni mwa uzushi wao. Allah تعالی Akabainisha kwamba Yeye Aliumba Bustani zilizowekewa na zisizowekewa vichanja, na wanyama wa ubebaji na wa *Farsh*. Kisha Akaeleza aina mbali mbali za mifugo madume na majike, kama vile kondoo na mbuzi, ngamia na ng'ombe. Kwamba, Yeye Allah تعالی Hakuwaharamisha hao wala watoto wao, bali hao wote wameumbwa kwa ajili ya wanadamu, kwa Matumizi ya kula na kupanda, kubeba vitu, kukama maziwa na manufaa mengine.

Sawa na Kauli Yake nyingine;

وَأَنْزَلَ لَكُمْ مِنَ الْأَنْعَامِ ثَمَنِيَّةً أَزْوَاجٍ

"Na Akakuleteni wanyama wa mifugo jozi nane...". (39:6).

Kauli ya Allah تعالی;

أَمَا اسْتَمَلْتُمْ عَلَيْهِ أَرْحَامَ الْأُنثَىٰ

"...au waliomo matumboni mwa majike yote mawili?"

Hii inakanusha kauli ya washirikina;

مَا فِي بُطُونِ هَذِهِ الْأَنْعَامِ خَالِصَةٌ لِّذُكُورِنَا وَمُحَرَّمٌ عَلَيْنَا أَزْوَاجِنَا

"Waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu, na wameharamishwa kwa wake zetu".

Kauli ya Allah تعالی;

نَبِّئُونِي بِعِلْمٍ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ

"Niambieni kwa ilimu ikiwa nyinyi mnasema kweli".

Maana: Niambieni kutokana na elimu ya yakini, namna gani na lini Allah تعالی Aliharamisha *Bahirah, Saibah, Waswilah na Ham* na kama hao?

Al-'Awfi alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما juu ya Kauli ya Allah تعالی;

ثُمَّ نَبِيَّةٌ أَرْوَجُ مِنْ الْأَضْأَانِ أُنْتَيْنِ وَمِنْ أَلْمَعْرِزِ أُنْتَيْنِ^٤

"...namna nane za wanyama: Wawili katika kondoo, na wawili katika mbuzi".

Hizi ni jozi nne.

قُلْ ءَأَلذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ الْأُنثَيَيْنِ

"Sema: Je, Ameharamisha yote madume mawili au majike mawili".

Anasema, 'Sijaharamisha yoyote katika hao'.

أَمَّا أَشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ أَرْحَامُ الْأُنثَيَيْنِ^٥

"...au waliomo matumboni mwa majike yote mawili?"

Maana yake: Tumbo la uzazi halizai kingine zaidi ya kiume na kike, basi kwanini mnaharamisha baadhi na kuhalalisha wengine?

تَبَيَّنُونِي بِعِلْمٍ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

"Niambieni kwa ilimu ikiwa nyinyi mnasema kweli".

Allah تعالى Anasema; "Wote hawa wameruhusiwa"¹. Kauli ya Allah تعالى;

أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ وَصَلَكُمُ اللَّهُ بِهَذَا

"Au Mlikuwapo Mwenyezi Mungu Alipokuusieni haya?"

Kwa kuudhihaki uzushi wa washirikina, na uongo wao juu ya Allah تعالى Kuharamisha wanachokiona wao kuwa ni haramu katika hivyo.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا يُضِلُّ النَّاسَ بِغَيْرِ عِلْمٍ^٦

"Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule aliyemzulia Mwenyezi Mungu uwongo kwa ajili ya kuwapoteza watu bila ya ilimu?"

Maana yake: Hakuna dhalimu zaidi yao.

¹ At-Tabari 12:187.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu”.

Wa kwanza aliyeingia katika Aya hii ‘Amr bin Luhay bin Qum’ah kwa sababu ndiye aliyekuwa wa kwanza aliyeabadili dini ya Mitume na kubuni mambo ya Saibah, Waswilah na Ham, kama ilivyothibiti ndani ya Sahih¹.

قُلْ لَا أَجِدُ فِي مَا أُوحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّمًا عَلَى طَاعِمٍ يَطْعَمُهُ إِلَّا أَنْ يَكُونَ مَيْتَةً أَوْ دَمًا
مَسْفُوحًا أَوْ لَحْمَ خنزِيرٍ فَإِنَّهُ رِجْسٌ أَوْ فِسْقًا أُهْلًا لِعَٰبِ اللَّهِ بِهِ ۗ فَمَنْ أَضَلُّ مِمَّنْ
وَلَا عَادٍ فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٤٥﴾

145. Sema: Sioni katika yale niliyofunuliwa mimi kitu kilichoharamishwa kwa mlaji kukila isipokuwa kiwe ni nyamafu au damu inayomwagika, au nyama ya nguruwe, kwani hiyo ni uchafu; au kwa upotofu kimechinjwa kwa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Lakini mwenye kushikwa na dharura, bila ya kufanya uovu wala kupetuka mipaka, basi hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

Ubainifu wa Kubainisha Vitu Vilivyoharamishwa.

Allah تعالیٰ Anamuamuru mja na Mtume Wake ﷺ:

قُلْ

“Sema”. Ewe Muhammad! Kuwaambia hao walioharamisha vile walivyo - ruzukiwa na Allah تعالیٰ hali ya kuwa ni kumzulia Allah تعالیٰ uwongo.

قُلْ لَا أَجِدُ فِي مَا أُوحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّمًا عَلَى طَاعِمٍ يَطْعَمُهُ

“Sioni katika yale niliyofunuliwa mimi kitu kilichoharamishwa kwa mlaji kukila”.

Maana yake: Sikuti mnyama yoyote aliyaharamishwa, isipokuwa hawa waliotajwa hapa. Tunapenda kutaja hapa, vitu vilivyoharamishwa ambavyo

¹ Fat’hul Al-Bari 8:132.

vimetajwa katika Surat *Al-Maidah* na Hadithi zinazozungumzia mada hii zinaingia katika kujenga maana ya Aya hii.

أَوْ دَمًا مَّسْفُوحًا

“...au damu inayomwagika”.

Qatadah alisema, “Damu iliyomwagika Iliharamishwa, ama nyama ambayo imesalia damu ndani yake inaruhusiwa”¹. Al-Humaydi alisema, Sufyan alitueleza, ‘Umar bin Dinar alituhadithia, “Nilimuambia Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنه, “Wanadai kuwa Mtume ﷺ aliharamisha nyama za punda wakati wa vita vya Khaybar”. Akasema, ‘Al-Hakam bin ‘Amr alikuwa akiyasema hayo kutoka kwa Mtume ﷺ, lakini mwanazuoni huyo, akimkusudia Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alilikataa hilo, huku akisoma Aya;

قُلْ لَا أَجِدُ فِي مَا أُوحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّمًا عَلَى طَاعِمٍ يَطْعَمُهُ

“Sema: Sioni katika yale niliyofunuliwa mimi kitu kilichoharamishwa kwa mlaji kukila”².

Al-Bukhari na Abu Dawud waliinukuu Hadithi hii³.

Naye Abu Bakr bin Marduwyah na Al-Hakim katika *Mustadrak* yake, walinukuu kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Watu katika zama za Ujahiliya walikuwa wakila vitu na wakiviacha vingine kwa kuvikirahi. Basi, Allah تعالى Akamtuma Mjumbe Wake na Akateremsha Kitabu Chake, Akahalalisha baadhi ya vitu na Kuviharamisha vingine. Basi, Alivyovihalalisha vinaruhusiwa na Alivyoviharamisha ni mwiko, na Alivyovinyamazia, vimesamehewa.

Kisha akasoma Aya hii;

فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“basi hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”.

Hili ni tamko la Ibn Marduwyah. Abu Dawud aliinukuu pia. Al-Hakim akasema, Hadith hii ni *Hasan* yenye isnadi *Sahih* lakini hawakuinukuu, wote wawili⁴.

¹ At-Tabari 12:193.

² Al-Humaydi 2:379.

³ Fat’hul Al-Bari 9:570 na Abu Dawud 4:162.

⁴ Abu Dawud 3800 na Al-Hakim 4:115.

Imamu Ahmad alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, akisema, "Mbuzi wa Saudah bint Zam'ah رضي الله عنها alikufa, naye akasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Fulani amekufa, akimkusudia Mbuzi huyo". Mtume ﷺ akasema;

«فَلِمَ لَا آخَذْتُمْ مَسْكَهَا؟»

"Kwa nini hamkuichukua ngozi yake kuitumia?"

Akasema, "Tuitumie ngozi ya Mbuzi Aliyekufa?" Mtume ﷺ akasema;

«إِنَّمَا قَالَ اللَّهُ: ﴿قُلْ لَا آجِدُ فِي مَا أُوحِيَ إِلَيَّ مَعْرَمًا عَلَىٰ طَائِعٍ يَطْعَمُهُ، إِلَّا أَنْ يَكُونَ مَيْتَةً أَوْ دَمًا مَسْفُورًا أَوْ لَحْمَ خَيْزِرٍ﴾ وَإِنَّكُمْ لَا تَطْعَمُونَهُ أَنْ تَذَبُّوهُ فَتَتَّبِعُوا بِهِ»

"Kwa hakika, Allah Alisema; "Sema: Sioni katika yale niliyofunuliwa mimi kitu kilichoharamishwa kwa mlaji kukila isipokuwa kiwe ni nyamafu au damu inayomwagika, au nyama ya nguruwe". Hapo mtakuwa hamli Mbuzi huyo, iwapo mtaitengeneza ngozi yake na mkanufaika nayo".

Kwa hivyo, Bi Saudah رضي الله عنها aliagiza, kondoo akachunwa ngozi na ikatengenezwa na kufanywa kiriba cha maji na akakitunza mpaka kilipochakaa"¹. Al-Bukhari na an-Nasai waliikusanya Hadithi sawa na hii².

Kauli ya Allah تعالى;

فَمَنْ أَضْطَرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ

"Lakini mwenye kushikwa na dharura, bila ya kukusudia uovu wala kupetuka mipaka".

Maana yake: Atakayepatwa na dharura ya kulazimika kula katika Alivyoharamisha Allah تعالى katika Aya hii na huku hokusudii kufanya uovu au kuruka mipaka.

فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

"...basi hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu".

Maana yake: Ni Mwenye Kumsamehe tena Rahimu kwake. Tafsiri ya Aya hii

¹ Ahmad 1:327.

² Fat'hul Al-Bari 11:577 na An-Nasai 7:173.

ilikwisha tangulia katika *Surat Al-Baqarah* kwa kiasi cha kutosha. Ayah hii tukufu inawakanusha washirikina walipozusha waliyoyoyazusha kwa kujiharamishia wao wenyewe kwa rai zao potovu juu ya *Bahirah, Saibah, Wasilah, Ham* na mfano wa hao. Mtume ﷺ akaamriwa awapashe kuwa yeye hapati katika Wahyi alioletewa na Allah تعالى kwamba kuna uharamu huo. Bali vilivyoharamishwa ni vile vilivyotajwa na Aya hii ambavyo ni pamoja na nyamafu, damu iliyomwagika, nyama ya nguruwe na kilichochinjwa kwa jina lisilo la Allah تعالى. Hivyo, kisichokuwa katika hivyo hakijaharamishwa, bali kilichonyamaziwa kimesamehewa. Basi ni kwa namna gani nyinyi mnadai kwamba hivyo ni haramu na mnaharamisha kwa ushahidi upi ilhali Allah تعالى Hakuviharamisha?

وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا كُلَّ ذِي ظُفْرٍ ^ط وَمِنَ الْبَقَرِ وَالْغَنَمِ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُومَهُمَا إِلَّا مَا حَمَلَتْ ظُهُورُهُمَا أَوْ الْحَوَايَا أَوْ مَا اخْتَلَطَ بِعَظْمٍ ^ع ذَلِكَ جَزَيْنَهُمْ بِبَغْيِهِمْ ^ط وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿١٤٦﴾

146. Na wale waliofuata dini ya Kiyahudi Tumewaharamishia kila mwenye kucha. Na katika ng'ombe na kondoo na mbuzi Tumewaharamishia shahamu yao, isipokuwa ile iliyobeba migongo yao au matumbo yao, au iliyogandamana na mifupa. Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao. Na bila ya shaka Sisi ndio wasema kweli".

Vyakula vya Halali Walivyoharamishiwa Wayahudi kwa Sababu ya Uasi Wao.

Allah تعالى Anasema: Tuliwaharamishia Mayahudi kila ndege na mnyama mwenye kwato zisizokuwa na migawanyiko¹. Kama vile ngamia, mbuni, bata na bata bukini. Allah تعالى Anasema hapa;

وَمِنَ الْبَقَرِ وَالْغَنَمِ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُومَهُمَا

"Na katika ng'ombe na kondoo na mbuzi Tumewaharamishia shahamu yao".

¹ Angalia maelezo katika *Surat Al-'Imran* 3:93.

As-Suddi alisema, inamaanisha, mafuta ya kwenye utumbo (*Ath-Tharb*) na mafuta ya figo mbili. Wayahudi walikuwa wakisema Israil alikuwa akijiharamishia vitu hivyo, basi na wao wakajiharamishia. 'Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akiizungumzia Aya;

إِلَّا مَا حَمَلَتْ ظُهُورُهُمَا

“...isipokuwa ile iliyobeba migongo yao”.

Maana yake: Mafuta yanayopatikana migongoni mwao¹. Kauli ya Allah تعالى:

أَوِ الْحَوَايَا

“...au matumbo yao”. Imamu Abu Ja'far bin Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Neno *Al-Hawaya* ni wingi, na umoja ni *Hawiyaa* au *Hawiya* na *Hawwiyah*, nayo ni yale yaliyojikusanya na kujizungusha ndani ya tumbo. Nayo ni ‘yanayopatikana katika utumbo”. Na alisema, Maana ya maneno haya, **“Na katika ng'ombe na kondoo na mbuzi Tumewaharamishia shahamu yao, isipokuwa ile iliyobeba migongo yao au matumbo yao”** 'Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, *Hawaya* ni utumbo². Mujahid naye alisema kuwa *Hawaya* ni utumbo³. Sa'id bin Jubayr na Adh-Dhahhak walisema vivyo hivyo⁴. Kauli ya Allah تعالى:

أَوْ مَا آخَتَلَطَ بِعَظْمٍ

“...au iliyogandamana na mifupa...”.

Maana: Isipokuwa shahamu iliyogandamana mifupa, Tumekuhalalishieni. Ibn Jurayj alisema, “Ni shahamu ya makalioni iliyochanganyika na vifupa vya mkiani, hivyo, kila kitu kinachopatikana katika miguu, mbavu, kichwa, macho na kinachogandamana na mifupa yake kilihalalishwa”⁵. As-Suddi alisema vivyo hivyo⁶.

ذَلِكَ جَزَيْنَهُمْ بِبَعْثِهِمْ

“Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao...”.

¹ At-Tabari 12:202.

² At-Tabari 12:203.

³ At-Tabari 12:204.

⁴ At-Tabari 12:204.

⁵ At-Tabari 12:205.

⁶ At-Tabari 12:205.

Maana: Kuwapa dhiki huku Tuliwafanyia na Kuwalazimisha kwa ajili ya Kuwalipa uasi wao na kukhalifu kwao Amri Zetu. Na Kauli nyingine ya Allah تعالی;

فَيُظَلَمُونَ مِنَ الَّذِينَ هَادُوا حَرَمْنَا عَلَيْهِمْ طَيْبَاتٍ أُحِلَّتْ لَهُمْ وَبِصَدِّهِمْ عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ
كَثِيرًا

“Basi kwa dhuluma yao Mayahudi Tuliwaharamishia vitu vizuri walivyohalalishiwa. Na kwa sababu ya kuwazuilia kwao watu wengi na njia ya Mwenyezi Mungu”. (4:160)

Na Kauli ya Allah تعالی;

وَإِنَّا لَصَادِقُونَ

“Na bila ya shaka Sisi ndio wasema kweli.”

Maana yake: Sisi ni Waadilifu sana katika adhabu Tuliyoaadhibu. Ibn Jarir رحمة الله تعالی alisema, “Sisi ni Wakweli katika yale Tuliyojulisha, ewe Muhammad juu ya kuwaharamishia wao vyakula hivi. Sio kama walivyodai kwamba Israil alijiharamishia yeye mwenyewe (na wao wakamuiga)”¹.

Hila za Wayahudi na Laana ya Allah تعالی Juu Yao.

‘Abdullah bin ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, ilimfikia habari ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه kwamba Samurah aliuza pombe akasema, “Allah Amlaani Samurah! Hakujuu kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَعَنَ اللَّهُ الْيَهُودَ حُرِّمَتْ عَلَيْهِمُ الشُّحُومُ فَجَمَلُوهَا فَبَاغَوْهَا»

“Allah تعالی Awalaani Wayahudi, waliharamishiwa shahamu, wao waliziyeyusha na wakaziuza”.

Imenakiliwa katika *Sahih Mbili*². Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنه anasema, “Nilimsikia Mtume ﷺ katika mwaka wa ushindi wa Makkah akisema,

«إِنَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ حَرَّمَ بَيْعَ الْخَمْرِ وَالْمَيْتَةِ وَالْخِنْزِيرِ وَالْأَضْنَامِ»

“Allah تعالی na Mjumbe Wake wameharamisha uuzaji wa pombe, nyamafu, nguruwe na masanamu”.

¹ At-Tabari 12:106.

² Fat’hul Al-Bari 4:483 na Muslim 3:1207.

Pakasemwa, "Ewe Mjumbe wa Allah! Shahamu ya nyamafu je? Hutumika katika kutia rangi ngozi, kupaka rangi Safina na watu huitumia kwa ajili ya kupata mwangaza". Akasema;

«لَا هُوَ حَرَامٌ»

"Hapana, ni haramu".

Kisha Mtume ﷺ akasema katika hilo;

«قَاتَلَ اللَّهُ الْيَهُودَ إِنَّ اللَّهَ لَمَّا حَرَّمَ عَلَيْهِمْ سُحُومَهَا جَمَلَوْهُ ثُمَّ بَاعُوهُ وَأَكَلُوا نَمَتَهُ»

"Allah Awalaani Wayahudi, waliharamishiwa shahamu wao waliziyeyusha na wakaziuza na wakala thamani yake¹".

Al-Jamaa wameinukuu Hadithi hii².

* * *

¹ Fat'hul Al-Bari 4:495.

² Fat'hul Al-Bari 4:495, Muslim 3:1207, Abu Dawud 3:356, Tufhat Al-Ahwadhi 4:521, An-Nasai 7:309 na Ibn Majah 2:732.

فَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ رَبُّكُمْ ذُو رَحْمَةٍ وَاسِعَةٍ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُهُ عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٤٧﴾

147. Wakikukanusha basi wewe sema: Mola Mlezi wenu ni Mwenye Rehema iliyoenea. Wala hazizuiliki Adhabu Yake kwa watu wahalifu".

Allah تعالى Anasema, wakiku-kadhibisha, ewe Muham-mad ﷺ, hao washirikina na Wayahudi na mfano wake, hao wanaokukhalifu.

فَقُلْ رَبُّكُمْ ذُو رَحْمَةٍ وَاسِعَةٍ

"...sema: Mola Mlezi wenu ni Mwenye Rehema iliyoenea".

Huku ni kuwatia moyo katika kutafuta rehema kunjufu za Allah تعالى na kumfuata Mtume Wake ﷺ.

وَلَا يُرَدُّ بَأْسُهُ عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٤٧﴾

فَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ رَبُّكُمْ ذُو رَحْمَةٍ وَاسِعَةٍ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُهُ عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٤٧﴾ سَيَقُولُ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكْنَا وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَمْنَا مِنْ شَيْءٍ كَذَلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ حَتَّىٰ ذَاقُوا بَأْسَنَا قُلْ هَلْ عِنْدَكُمْ مِنْ عِلْمٍ فَتُخْرِجُوهُ لَنَا إِنْ تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ أَنْتُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ ﴿١٤٨﴾ قُلْ فَلِلَّهِ الْحُجَّةُ الْبَلِيغَةُ فَلَوْ شَاءَ لَهَدَيْتُكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٤٩﴾ قُلْ هَلُمْ شُهَدَاءُ كُمْ الَّذِينَ يَشْهَدُونَ أَنَّ اللَّهَ حَرَّمَ هَذَا فَإِنْ شَهِدُوا فَلَا تَشْهَدْ مَعَهُمْ وَلَا تَتَّبِعِ أَهْوَاءَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَهُمْ بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ ﴿١٥٠﴾ * قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِنْ إِمْلَاقٍ نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ وَلَا تَقْرَبُوا الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ذَٰلِكُمْ وَصَّيْتُكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١٥١﴾

"Wala haizuiliki Adhabu Yake kwa watu wahalifu".

Kuwapa vitisho kwa kumkhalifu kwao Mtume ﷺ ambaye ni Nabii wa mwisho. Mara nyingi, Allah تعالى Hukutanisha utiaji moyo na utoaji vitisho katika Qur'an. Sawa na Alivyosema Allah تعالى mwishoni mwa sura hii;

إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Hakika Mola Mlezi wako ni Mwepesi wa Kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu". (6:165) na;

وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ لِلنَّاسِ عَلَى ظُلْمِهِمْ وَإِنَّ رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ

"Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye msamaha kwa watu juu ya udhalimu wao. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mkali wa Kuadhibu". (13:6) na;

• نَبِيُّ عِبَادِي أَنِّي أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٤٧﴾ وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ

"Waambie waja Wangu ya kwamba Mimi Ndiye Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu. Na kwamba Adhabu Yangu Ndio Adhabu iliyochungu!"

عَافِرِ الذَّنْبِ وَقَابِلِ التَّوْبِ شَدِيدِ الْعِقَابِ

"Anayesamehe dhambi na Anayepokea toba, Mkali wa Kuadhibu". (40:3) Na;

إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١٤٨﴾ إِنَّهُ هُوَ يُبَدِّلُ وَيُعِيدُ ﴿١٤٩﴾ وَهُوَ الْغَفُورُ الْوَدُودُ

"Hakika kutesa kwa Mola wako Mlezi ni kukali. Yeye Ndiye Anayanzisha na Ndiye Anayerejeza tena, Naye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Mapenzi". (85:12-14)

Aya zinazohusu mada hii ni nyingi sana.

سَيَقُولُ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكْنَا وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَمْنَا مِنْ شَيْءٍ ؕ كَذَلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ حَتَّى ذَاقُوا بَأْسَنَا ؕ قُلْ هَلْ عِنْدَكُمْ مِنْ عِلْمٍ فَتُخْرِجُوهُ لَنَا ؕ إِنْ تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ أَنْتُمْ إِلَّا تُخْرِصُونَ ﴿١٥٠﴾ قُلْ فَلِلَّهِ الْحُجَّةُ الْبَالِغَةُ ؕ فَلَوْ شَاءَ لَهَدَيْتُكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٥١﴾ قُلْ هَلُمْ شُهَدَاءُكُمْ الَّذِينَ يَشْهَدُونَ أَنَّ اللَّهَ حَرَّمَ هَذَا ؕ فَإِنْ شَهِدُوا فَلَا تَشْهَدْ مَعَهُمْ ؕ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ كَذَبُوا بِبَايِعَتِنَا وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَهُمْ بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ ﴿١٥٢﴾

148. Watasema walioshirikisha: Lau kuwa Mwenyezi Mungu Angetaka tusingelishiriki sisi, wala baba zetu; wala tusinge haramishwa kitu chochote. Vipi hivi walikanusha waliokuwa kabla yao mpaka walipoorja adhabu Yetu. Sema: Je, nyinyi mnayo elimu mtutolee? Nyinyi hamfuati ila dhana. Wala hamsemi ila uwongo.

149. Sema: Basi Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye hoja ya kukata. Na kama Angelipenda Angelikuhidini wote.

150. Sema: Leteni mashahidi wenu wataoshuhudia kuwa Mwenyezi Mungu Ameharamisha hawa. Basi wakishuhudia, wewe usishuhudie pamoja nao. Wala usifuate matamano ya waliozikanusha Ishara Zetu, wala hawaiamini Akhera na ambao wanamlinganisha Mola Mlezi wao na wengine.

Fikra Potovu na Kukanushwa Kwake.

Huu ni mjadala Alioutaja Allah تعالى na Anakanusha fikra potovu waliyonayo washirikina katika ushirikina wao, kwamba, Allah تعالى Anayajua yale wayafanyayo kuhusu ushirikina wao na yale waliyojiharamishia wenyewe, na Allah تعالى Ana Uwezo wa Kuyabadilisha yote hayo kwa Kutuongoza katika Imani ya kweli, na Kuweka kizuizi kati yetu na ukafiri, lakini Hakuyabadili hayo. Kwa hivyo wakidai Allah تعالى Ndivyo Alivyotaka na Ameturidhia sisi kwa hayo. Kwa ajili hiyo, walisema;

لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكْنَا وَلَا ءَابَاؤُنَا وَلَا حَرَمْنَا مِنْ شَيْءٍ

“Lau kuwa Mwenyezi Mungu Angetaka tusingelishirikisha sisi, wala baba zetu; wala tusingeharamisha kitu chochote”.

Sawa na katika Kauli Yake nyingine;

وَقَالُوا لَوْ شَاءَ الرَّحْمَنُ مَا عَبَدْنَاهُمْ

“Angelipenda Mwingi wa Rehema tusingeliwaabudu wao”. (43:20)

Kadhhalika kama Aya iliyo katika Surat An-Nahl imeeleza sawa na hayo.

كَذَلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“Kama hivi walikanusha waliokuwa kabla yao”.

Maana yake: Kwa dhana hii, wapotevu wa kabla yao walipotea. Nayo ni fikra potofu isiyokuwa na nguvu, kwa sababu, kama ingelikuwa sahihi basi Allah تعالى Asingewadhuru na Kuwaangamiza, na Kuwasaidia Mitume Wake watukufu dhidi yao, na Akawaonjisha washirikina, adhabu iumizayo.

قُلْ هَلْ عِنْدَكُمْ مِّنْ عِلْمٍ

“Sema: Je, nyinyi mnayo elimu?”

Kwamba Allah تعالى Amekuwa radhi nanyi katika yale mliyo nayo.

فَتُخْرِجُوهُ لَنَا

“...mtutolee?”

Maana yake: Mlidhihirishe, mlibainishe na mliweke wazi.

إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ

“Nyinyi hamfuati ila dhana?”

Madanganyo na ghiliba na malengo ya neno *Dhwanna* (dhana) hapa ni fikra mbaya.

وَإِن أَنتُمُ إِلَّا تَخْرُصُونَ

“Wala hamsemi ila uwongo tu?”

Mnakadhibisha juu ya Allah تعالى katika madai mliyoyatoa. Kauli ya Allah تعالى;

قُلْ فَلِلَّهِ الْحُجَّةُ الْبَلِيغَةُ ۗ فَلَوْ شَاءَ لَهَدَيْتُكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٤٧﴾

“Sema: Basi Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye hoja ya kukata. Na kama Angelipenda Angelikuhidini nyote?”

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ;

قُلْ

“Sema”. Kuwaambia wao.

فَلِلَّهِ الْحُجَّةُ الْبَلِيغَةُ ۗ

“Basi Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye hoja ya kukata?”

Maana yake: Yeye Ndiye Mwenye Hikima timilifu na hoja yenye kukata katika Kumuongoza aliyeongoka na Kumpoteza aliyepotea.

فَلَوْ شَاءَ لَهَدَيْنَاكُمْ أَجْمَعِينَ

“Na kama Angelipenda Angelikuhidini nyote”.

Yote hayo ni kwa Kudura Yake, Kutaka na Kukhitari Kwake. Pamoja na hayo, Yeye ni Mwenye radhi kwa Waumini na Ana Ghadhabu kwa makafiri.

Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine;

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَمَعَهُمْ عَلَى الْهَدْيِ

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angependa Angeliwakusanya kwenye uongofu”. (6:35) Na;

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي الْأَرْضِ

“Angelitaka Mola wako Mlezi Wangeliamini wote waliomo katika ardhi”. (10:99) Na;

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً ۗ وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ۗ إِلَّا مَن رَّحِمَ رَبُّكَ ۗ وَلِذَلِكَ خَلَقَهُمْ ۗ وَتَمَّتْ كَلِمَةُ رَبِّكَ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ

“Na Mola wako Mlezi Angelipenda Angewafanya watu wote wakawa umma mmoja. Lakini hawaachi kukhitalifiana. Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi Amewarehemu; na kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu Amewaumba. Na litatimia Neno la Mola wako Mlezi: Kweli kweli Nitaijaza Jahannam kwa majini na watu pamoja”. (11:118 - 119)

Adh-Dhahhak alisema, “Mtu akimuasi Allah تعالى, huwa hana hoja, lakini Allah تعالى Ana hoja yenye kukata, kwa waja Wake.

Kauli ya Allah تعالى;

قُلْ هَلُمَّ شُهَدَاءَكُمْ

“Sema: Leteni mashahidi wenu”. Maana yake: Wawasilisheni mashahidi wenu.

الَّذِينَ يَشْهَدُونَ أَنَّ اللَّهَ حَرَّمَ هَذَا

“...wataoshuhudia kuwa Mwenyezi Mungu Ameharamisha hawa”.

Maana yake: Mlichokiharamisha na mlichokikadhibisha na mlichokizusha juu ya Allah تعالى:

فَإِنْ شَهِدُوا فَلَا تَشْهَدْ مَعَهُمْ

“Basi wakishuhudia, wewe usishuhudie pamoja nao”.

Maana yake: Kwa kuwa wao kwa hakika katika hali hii, ushahidi wao utakuwa si wa kweli, ni uongo.

وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ كَذَبُوا بِعَايِنِنَا وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَهُمْ بِرَبِّهِمْ
يَعْدِلُونَ

“Wala usifuat matamania ya waliozikanusha Ishara Zetu, wala hawaiamini Akhera na ambao wanamlinganisha Mola Mlezi wao na wengine”.

Maana yake: Wanamshirikisha na wanamzushia walinganifu Naye.

* قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبِّي عَلَيْكُمْ أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا
وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِمَّنْ إِمْلَقِي نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ وَلَا تَقْرَبُوا الْفَوَاحِشَ مَا
ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ذَٰلِكُمْ وَصَّيْتُكُمْ
بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١٥١﴾

151. Sema: Njoooni nikusomeeni Aliyokuharamishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na Wazazi wenu wafanyieni wema. Wala Msiwaue watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi Tunakuruzukuni nyinyi na wao. Wala msikaribie mambo machafu, yanayoonekana, na yanayofichikana. Wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Ameharamisha kuiua, ila ikiwa kwa haki. Hayo Amekuusieni ili myatie akilini.

Wasia Kumi.

Dawud Al-Awdy amenukuu kutoka kwa, Ash-Sha'bi, kutoka kwa 'Alqamah, kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema, "Anayetaka kuangalia wasia wa Mtume ﷺ amabo una muhuri wake, basi azisome aya hizo;

قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

"Sema: Njoooni nikusomeeni Aliyokuharamishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote".

Mpaka katika Kauli ya Allah تعالى:

لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

"Haya Amekusieni ili mpate kuchamungu". (6:53)¹

Katika kitabu chake cha *Mustadrak* yake, Al-Hakim alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, "Katika *Surat Al-An'am* kuna Ayah zilizo dhahiri, na ndizo mama wa Kitabu (Qur'an)". Kisha akasoma;

قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ

"Sema: Njoooni nikusomeeni Aliyokuharamishieni Mola wenu Mlezi".

Isnadi yake ni *Sahih* lakini hawakuinukuu².

Al-Hakim alinukuu pia (katika kitabu chake cha *Mustadrak*) kutoka kwa 'Ubadah bin As-Swamit رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alisema;

«أَبْكُمْ يُبَايِعُنِي عَلَى ثَلَاثٍ»

"Nani kati yenu atakayeniunga mkono katika mambo matatu?"

Kisha akasoma Aya ifuatayo,

قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ

"Sema: Njoooni nikusomeeni Aliyokuharamishieni Mola wenu Mlezi". Mpaka mwisho wa Aya hiyo, kisha akasema,

¹ Tufhat Al-Ahwadhi 8:446.

² Al-Hakim 2:317.

تَقَمَّنْ وَتَى فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ وَمَنْ انْتَقَصَ مِنْهُنَّ شَيْئًا فَأَذْرَكَهُ اللَّهُ بِهٖ فِي الدُّنْيَا كَانَتْ
عُقُوبَتُهُ، وَمَنْ آخَرَ إِلَى الْآخِرَةِ فَأَمْرُهُ إِلَى اللَّهِ إِنْ شَاءَ عَذَّبَهُ وَإِنْ شَاءَ عَفَا عَنْهُ

“Atakayetekeleza (bai'a hii) uungaji mkono huo, malipo yake ni juu ya Allah تعالى na atakayepunguza kitu katika hayo, Allah تعالى Akamuadhibu duniani, hiyo ndiyo itakuwa adhabu yake. Na Atakayemuakhirisha mpaka Akhera, basi hukumu yake ni kwa Allah تعالى, Akitaka Atamuadhibu na Akitaka Atamsamehe”.

Halafu akasema, “Isnadi yake ni *Sahih* lakini hawakuinukuu”¹.

Ama kuhusu tafsiri yake, Allah تعالى Anamuambia Nabii na Mtume Wake, Muhammad ﷺ: Ewe Muhammad! Waambie washirikina ambao wanaabudu ghairi ya Allah تعالى, wakaviharamisha Alivyowaruzuku na wakaua watoto wao na yote hayo waliyafanya kwa rai zao na hadaa za shetani kwao.

قُلْ

“Sema”. Uwaambie.

تَعَالَوْا

“Njooni”. Mje na msogee.

أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبِّيَ عَلَيْكُمْ

“...nikusomeeni Aliyokuharamishieni Mola wenu Mlezi”.

Inamaanisha: Nitakuambieni na kukujulisheni kuhusu Alivyoviharamisha Mola wenu juu yenu ni khabari ya kweli, na siyo ya kudhani, wala ya matamania ya nafsi bali ni Wahyi na Amri kutoka Kwake.

Wasia wa Kwanza: Kukataza Ushirikina.

أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

“...kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote”. Kana kwamba kuna maneno yaliyoachwa, kama ulivyo muktadha wa Aya hiyo na yanaweza kukadiriwa kuwa, ni Amekuusieni, **“Kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote”.**

¹ Al-Bukhari na. 1237 na Muslim 94.

Na kwa ajili hiyo, mwishoni mwa Aya Alisema;

ذَلِكُمْ وَصَّوْنَاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

“Hayo Amekuusieni ili myatie akilini”.

Katika Sahih Mbili, kuna Hadith ya Abu Dharr رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema;

«أَتَانِي جِبْرِيلُ فَبَسَّرَنِي أَنَّهُ مَنْ مَاتَ لَا يُشْرِكُ بِاللَّهِ شَيْئًا مِنْ أُمَّتِكَ دَخَلَ الْجَنَّةَ، قُلْتُ: وَإِنْ زَنَى وَإِنْ سَرَقَ؟ قَالَ: وَإِنْ زَنَى وَإِنْ سَرَقَ، قُلْتُ: وَإِنْ زَنَى وَإِنْ سَرَقَ؟ قَالَ: وَإِنْ زَنَى وَإِنْ سَرَقَ وَإِنْ شَرِبَ الْخَمْرَ»

*“Jibril alinjia na akanipa bishara kwamba, “Yeyote katika Umma wako anayekufa huku hajamshirikisha Allah تعالى na chochote, ataingia Janna”. Nikasema, “Hata akizini au akiiba?” Akasema: “Hata akizini au akiiba”. Nikasema, “Hata akizini au akiiba?” akasema: “Hata akizini au akiiba”. Nikasema, “Hata akizini au akiiba?” Akasema: “Hata akizini au akiiba au akinywa pombe”.*¹

Na katika baadhi ya isnadi na Sunan katika Hadithi ya Abu Dharr رضي الله عنه ni kuwa alisema, Mtume ﷺ alisema;

«يَقُولُ تَعَالَى: يَا ابْنَ آدَمَ إِنَّكَ مَا دَعَوْتَنِي وَرَجَوْتَنِي فَأِنِّي أَغْفِرُ لَكَ عَلَى مَا كَانَ مِنْكَ وَلَا أَبَالِي، وَلَوْ أَتَيْتَنِي بِقُرَابِ الْأَرْضِ خَطِيئَةً أَتَيْتَكَ بِقُرَابِهَا مَغْفِرَةً مَا لَمْ تُشْرِكْ بِي شَيْئًا، وَإِنْ أَخْطَأْتَ حَتَّى تَبْلُغَ خَطَايَاكَ عَنَانَ السَّمَاءِ ثُمَّ اسْتَغْفَرْتَنِي غَفَرْتُ لَكَ»

*“Allah تعالى Anasema, “Ewe mwanadamu! Kadiri unavyoniomba na ukawa na matarajio Kwangu, basi Mimi Nitakusamehe makosa yoyote utakayokuwa nayo wala sijali. Hata kama utanijia na dhambi za ujazo wa dunia. Nitakupa maghfira kwa ujazo huo maadamu haunishirikishi na kitu. Na hata kama utafanya madhambi mpaka yakafika mipaka ya anga, kisha ukaniomba msamaha, Nitakughufiria”.*²

¹ Ahmad 5:172 na Tufhat na Al-Ahwadhi kutoka kwa Anas 9:524.

² Muslim 1:94.

Hadithi hii ina ushahidi wa Aya katika Qur'an pia, Allah تعالى Aliposema;

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehi kushirikishwa na kitu. Lakini Yeye Husamehe yasiyokuwa hayo kwa Amtakaye”. (4:116)

Katika Sahih Muslim, Imenukuliwa kutoka kwa Ibn Masudi رضي الله عنه, Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ مَاتَ لَا يُشْرِكُ بِاللَّهِ شَيْئًا دَخَلَ الْجَنَّةَ»

“Yeyote anayekufa huku hajamshirikisha Allah na chochote ataingia Peponi”¹.

Kuna Aya na Hadithi nyingi kuhusu mada hii.

Wasia wa Pili: Amri ya Kuwafanyia Wema Wazazi Wawili.

Kauli ya Allah تعالى;

وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

“Na Wazazi wenu wafanyieni wema”.

Maana yake: Na Amekuusieni na Kukuamuruni kwamba muwafanyie ihsani Wazazi wenu, sawa na Kauli ya Allah تعالى;

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

“Na Mola wako Mlezi Aameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na Wazazi wawili muwatendee wema”. (17:23)

Na baadhi ya Ulamaa walisoma neno Waqadhwa katika Ayah hiyo kwa kuweka Wa was-Swaa badala yake, yaani na Mola wako Ameusia. Allah تعالى mara nyingi Analinganisha utiifu Wake na kuwafanyia wema Wazazi wawili. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلَوْلَا دَيْكَ إِلَى الْمَصِيرِ ﴿١٤٧﴾ وَإِنْ جَاهَدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۖ وَصَاحِبَيْهِمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۗ وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَيَّ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ مَرْجِعِكُمْ فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٤٨﴾

¹ At-Tabari 12:188.

“Nishukuru Mimi na Wazazi wako. Ni Kwangu Mimi ndiyo marudio. Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwatii. Lakini kaa nao kwa wema duniani, nawe ishike njia ya anayeelekea Kwangu. Kisha marejeo yenu ni Kwangu Mimi, na Mimi Nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda”. (31:14-15)

Hivyo Aameamuru kuwafanyia Ihsani hata kama walikuwa washirikina. Allah تعالى Alisema pia;

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ لَا تَعْبُدُونَ إِلَّا اللَّهَ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

“Na Tulipofunga agano na Wana wa Israili: Hamtamuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu; na muwafanyie wema Wazazi”. (2:83)

Kuna Aya nyingi kuhusu jambo hili. Katika Sahih Mbili kuna Hadithi ya Ibn Mas'ud رضي الله عنه, kwamba alisema, Nilimuuliza Mtume ﷺ, “Ni amali gani iliyo bora?” Akasema;

«الصَّلَاةُ عَلَى وَفْيِهَا»

“Sala katika wakati wake”. Nikasema, “Kisha ipi?” Akasema;

«بِرُّ الْوَالِدَيْنِ»

“Kuwafanyia wema wazazi wawili”. Nikasema, “Kisha ipi?” Akasema;

«الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

“Jihadi katika njia ya Allah”.

Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema: Hayo aliniambia Mtume ﷺ na kama ningeliongeza kumuuliza angelisema na mengine zaidi¹.

Wasia wa tatu: Katazo la Kuwaua Watoto Wadogo

Kauli ya Allah تعالى;

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِمَّنْ إِمْلَقِي نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ

“Wala Msiwaue watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi Tunakuruzukuni nyinyi na wao”.

¹ Fat'hul Al-Bari 2:12 na Muslim 1:89.

Baada ya Allah تعالى Kuusia kuwafanyia ihsani Wazazi na Wazazi wa Wazazi, Aliunganisha kwa Kuusia Kuwafanyia wema watoto na wajukuu. Allah تعالى Alisema;

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِمَّنْ إِمْلَقِي^ط

“Wala Msiwaue watoto wenu kwa sababu ya umasikini”.

Hilo la kuua watoto wao linatokana na ghiliba za mashetani. Wakawa wanawazika watoto wachanga wa kike wangali hai kwa kukhofia fedheha, na wakati mwingine waliwaua baadhi ya watoto wa kiume kwa kukhofia ufakiri. *Sahih* zimenukuu Hadithi ya ‘Abdullah bin Mas’ud رضى الله عنه kwamba alimuuliza Mtume ﷺ, “Ni dhambi gani iliyo kubwa?” Akasema;

«أَنْ نَجْعَلَ لِلَّهِ نِدَاءً وَهُوَ خَلَقَكَ»

“Kumfanyia Allah تعالى washindani, ilhali, Yeye Ndiye Aliyekuumba”.

Nikasema, “Kisha ipi?” Akasema;

«أَنْ نَقْتُلَ وَلَدَكَ خَشِيَةً أَنْ يَطْعَمَ مَعَكَ»

“Kumuua mwanao kwa kukhofia atashiriki nawe katika kula”.

Nikasema, “Kisha ipi?” Akasema;

«أَنْ تُزَانِي حَلِيلَةَ جَارِكَ»

“Kuzini na mke wa jirani yako”. Kisha Mtume ﷺ akasoma;

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُونَ^ع

“Na wale wasiomuomba mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawau nafsi Aliyoiharamisha Mwenyezi Mungu isipokuwa kwa haki, wala hawazini”. (25:68)¹

Kauli ya Allah تعالى;

مِمَّنْ إِمْلَقِي^ط

“...kwa sababu ya umasikini”.

¹ Fat’hul Al-Bari 8:350 na Muslim 1:98.

Ibn 'Abbas, Qatadah, As-Suddi na wengine رضي الله عنهم, walisema; Maana yake, ufakiri.¹ Maana: Msiwaue kwa sababu ya ufakiri wenu. Na Amesema katika Surat Israa,

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَاقٍ^ط

“Wala Msiwaue wana wenu kwa kuogopa umasikini”. (17:31)

Yaani, Msiwaue kwa kukhofia ufakiri hapo baadaye, kwa ajili hiyo, Akasema;

نَحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ^ط

“Sisi Tunakuruzukuni nyinyi na wao”. Alianza kwa riziki yao Wazazi, kwa sababu ndipo mahali mada ilipo, yaani, msichelee ufakiri wenu, kwani riziki yao ni juu ya Allah تعالى, na kwa kuwa ufakiri ni jambo lenye kupatikana, Allah تعالى Alisema;

نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ^ط

“Sisi Tunakuruzukuni nyinyi na wao”. Kwa kuwa ndio lenye umuhimu mkubwa hapa, Allah تعالى Ndiye Anayejua zaidi. Kauli ya Allah تعالى;

وَلَا تَقْرَبُوا أَلْفَوْاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ^ط

“Wala msikaribie mambo machafu, yanayoonekana, na yanayofichikana”.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّيَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ وَالْإِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَأَنْ تُشْرِكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْمُونَ ﴿٦٣﴾

“Sema: Mola Mlezi wangu Ameharamisha mambo machafu ya dhahiri na ya siri, na dhambi na uasi bila ya haki na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na asichokiletea uthibitisho, na Kumzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua”. (7:33)

Tafsiri yake imetangulia katika Kauli ya Allah تعالى;

وَذَرُوا ظَهَرَ الْإِثْمِ وَبَاطِنَهُ^ط

“Na acheni dhambi zilizodhahiri na zilizofichikana”. (6:120)

¹ At-Tabari 12:217

Katika *Sahihi* mbili kuna Hadithi ya Ibn Mas'ud رضى الله عنه alisema Mtume ﷺ:

«لَا أَحَدٌ أَغْيَرَ مِنَ اللَّهِ، مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ حَرَّمَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ»

*"Hakuna mwenye wivu zaidi ya Allah, kwa sababu hiyo, Aliharamisha maovu, ya dhahiri na ya ufichoni"*¹.

'Abdul-Malik ibn 'Umayr alisema, Warrad alisema, toka kwa mtumwa wake aliyemuachilia huru, kuwa Al-Mughirah alisema kwamba Sa'd bin 'Ubadah رضى الله عنه alisema, "Kama nitamuona mwanaume yeyote yuko pamoja na mke wangu (wakizini), nitampiga kwa upanga bila ya huruma". Habari hizo zikamfikia Mtume ﷺ na akasema;

«أَتَعْجِبُونَ مِنْ غَيْرَةِ سَعْدٍ؟ فَوَاللَّهِ لَأَنَا أَغْيَرُ مِنْ سَعْدٍ، وَاللَّهُ أَغْيَرُ مِنِّي، مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ حَرَّمَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ»

*"Mnaushangaa wivu wa Sa'd? Wallahi, mimi nina wivu kumshinda Sa'd, na Allah Ana wivu kunizidi mimi, kwa sababu hiyo, Aliharamisha maovu, ya dhahiri na ya ufichoni"*².

Imenukuliwa na *Sahihi* Mbili.

Wasia wanne: Katazo la Kuiua Nafsi Bila ya Haki.

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ

"Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Ameharamisha kuiua, ila ikiwa kwa haki".

Aya hii ni katika Aya ambazo Allah تعالى Anaeleza kwa msisitizo juu ya kukatazwa huko, ingawa imeingia katika Aya zinazokataza maovu ya dhahiri na ya ufichoni. Imeelezwa katika *Sahih* Mbili, kwamba Ibn Mas'ud رضى الله عنه alisema, kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَا يَجِلُّ دَمٌ أَمْرِي؛ مُسْلِمٌ يَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنِّي رَسُولُ اللَّهِ، إِلَّا يَأْخُذِي ثَلَاثٌ: الثَّيْبُ الرَّأْيِي، وَالنَّفْسُ بِالنَّفْسِ، وَالتَّارِكُ بَيْنِيهِ الْمَفَارِقُ لِلْجَمَاعَةِ»

¹ Fat'hul Al-Bari 8:146 na Muslim 4:2114.

² Fat'hul Al-Bari 13:411 na Muslim 2:1136.

“Si halali, damu ya Muislamu anayetoa shahada kuwa hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na kwamba mimi ni Mjumbe wa Allah, isipokuwa kwa moja katika mambo matatu. Mzinifu ambaye aliwahi kuidiriki ndoa, nafsi kwa nafsi na anayeritadi Dini na akaitenga jamaa (jamii ya waumini waaminifu).”¹

Kuna makatazo, makaripio na maonyo dhidi ya kumuua *Mua'ahid*, yaani, mtu asiye Muislamu ambaye amepewa mkataba wa hifadhi na Waislamu. Al-Bukhari amenukuu kuwa 'Abdullah bin 'Amr رضي الله عنه alisema Mtume ﷺ alisema;

«مَنْ قَتَلَ مُعَاهِدًا لَمْ يَرِحْ رَائِحَةَ الْجَنَّةِ، وَإِنَّ رِيحَهَا لَيُوجَدُ مِنْ مَسِيرَةِ أَرْبَعِينَ عَامًا»

“Atakayemuua mtu mwenye mkataba wa hifadhi na waislamu hatonusa harufu ya Pepo, na kwa hakika harufu ya pepo yake itakuwa kwa umbali wa mwendo wa miaka arubaini.”²

Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema Mtume ﷺ alisema;

«مَنْ قَتَلَ مُعَاهِدًا لَهُ ذِمَّةُ اللَّهِ وَذِمَّةُ رَسُولِهِ فَقَدْ أَخْفَرَ بِذِمَّةِ اللَّهِ، فَلَا يَرِحْ رَائِحَةَ الْجَنَّةِ، وَإِنَّ رِيحَهَا لَيُوجَدُ مِنْ مَسِيرَةِ سَبْعِينَ خَرِيفًا»

“Atakayemuua mtu mwenye hifadhi ya Waislamu, ambaye yuko katika hifadhi ya Allah na Mtume Wake, basi atakuwa ameichafua hifadhi ya Allah na Mtume Wake (kwa mtu huyo). Kwa hivyo, hatonusa harufu ya pepo, harufu ya pepo yake itakuwa umbali unaofikia mwendo wa miaka arubaini”.

Ibn Majah na At-Tirmidhi waliinukuu Hadithi hii, na At-Tirmidhi alisema, ni *Hasan Sahih*.³ Kauli ya Allah تعالى:

ذَلِكُمْ وَصَّيْنَاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

“Hayo Amekuusieni ili myatie akilini.”

Maana: Hayo ndiyo Aliyokuamrisheni ili mfahamu Amri Zake na Makatazo Yake.

¹ Fat'hul Al-Bari 12:209 na Muslim 3:1302.

² Fat'hul Al-Bari 12:370.

³ Tuhfatul Al-Ahwadhi 4:658 na Ibn Majah 2:896.

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ
 أَشُدَّهُ ۗ وَأَوْفُوا بِالْكَيْلِ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ ۗ لَا تَكْلِفُ
 نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۗ وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ
 وَبِعَهْدِ اللَّهِ أَوْفُوا ۗ ذَٰلِكُمْ وَصْنُكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿١٥٢﴾
 وَأَنْ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۗ وَلَا تَتَّبِعُوا
 السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ۗ ذَٰلِكُمْ وَصْنُكُمْ بِهِ
 لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٥٣﴾ ثُمَّ آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ تَمَامًا
 عَلَىٰ الَّذِي أَحْسَنَ وَتَفْصِيلًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً
 لَّعَلَّهُمْ بِلِقَاءِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ ﴿١٥٤﴾ وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ
 مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَأَتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٥٥﴾ أَنْ تَقُولُوا
 إِنَّمَا أَنْزَلَ الْكِتَابَ عَلَىٰ طَائِفَتَيْنِ مِن قَبْلِنَا وَإِنْ كُنَّا عَن
 دِرَاسَتِهِمْ لَغَافِلِينَ ﴿١٥٦﴾ أَوْ تَقُولُوا لَوْ أَنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْهِ
 الْكِتَابَ لَكُنَّا أَهْدَىٰ مِنْهُمْ ۗ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِّن
 رَبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ ۗ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن كَذَّبَ بِآيَاتِ
 اللَّهِ وَصَدَفَ عَنْهَا ۗ سَنَجْزِي الَّذِينَ يَصْدِفُونَ عَنَّا آيَاتِنَا
 سُوءَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوا يَصْدِفُونَ ﴿١٥٧﴾

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ
 أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۗ وَأَوْفُوا
 بِالْكَيْلِ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ ۗ لَا
 تُكْلِفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۗ وَإِذَا قُلْتُمْ
 فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ وَبِعَهْدِ
 اللَّهِ أَوْفُوا ۗ ذَٰلِكُمْ وَصْنُكُمْ بِهِ
 لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿١٥٢﴾

152. Wala msizikaribie mali za yatima ila kwa njia ya wema kabisa, mpaka afikilie utu uzima. Na timizeni vipimo na Mizani kwa uadilifu. Sisi Hatu-mkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Na msemapo semeni kwa uadilifu, ingawa ni jamaa. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni. Hayo Amekuusieni ili mpate kukumbuka.

Wasia wa Tano: Kuharamishwa Kula Mali ya Yatima.

'Ata bin As-saib alisema kutoka kwa Sa'd bin Jubayr kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, pindi Allah تعالي Alipotereisha;

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

“Wala msiyakaribie mali ya yatima ila kwa njia ya wema kabisa...”. Na;

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا

“Hakika wanaokula mali ya mayatima kwa dhulma...” (4:10)

Waliposikia Aya hii masahaba waliokuwa walezi wa yatima walianza kutenganisha baina ya vyakula na vinywaji vyao na vile vya yatima. Wakawa wanahifadhi chakula cha yatima pindi kiliposalia, mpaka atakapokula au kitakapoharibika. Hili likawawia vigumu masahaba, wakamtajia hilo Mtume ﷺ. Allah تعالى Akateremsha;

وَسَأَلُونَكَ عَنِ الْيَتَامَىٰ قُلْ إِصْلَاحٌ لَهُمْ خَيْرٌ وَإِنْ تُخَالِطُوهُمْ فَارْحَمُوا

“Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: Kuwatengenezea ndio kheri. Na mkichanganyika nao basi ni ndugu zenu...” (2:220)

Baada ya hapo, walichanganya vyakula na vinywaji vyao na vile vya mayatima. Abu Dawud ameinukuu kauli hii¹. Kauli ya Allah تعالى;

حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ

“...mpaka afikilie utu uzima”. Ash-Shabi, Malik na wengine kadha katika *Salaf* walisema, maana yake, ni mpaka abaleghe².

Wasia wa sita: Amri Juu ya Kukamilisha Vipimo na Mizani.

Kauli ya Allah تعالى,

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ

“Na timizeni vipimo na Mizani kwa uadilifu...”

Allah تعالى Anaamuru kuwepo uadilifu katika jambo la kuchukua na kutoa. Pia, Ametoa onyo dhidi ya kuacha kuitekeleza amri hii, katika Kauli Yake;

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿٦١﴾ الَّذِينَ إِذَا أَكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ ﴿٦٢﴾ وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٦٣﴾ أَلَا يَظُنُّ أُولَٰئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ ﴿٦٤﴾ لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٦٥﴾ يَوْمَ يَقُومُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٦﴾

¹ Abu Dawud 3:291.

² At-Tabari 12:223.

“Ole wao hao wapunjao! Ambao wanapojipimia kwa watu hudai watimiziwe. Na wao wanapowapimia watu kwa kipimo au Mizani hupunguza. Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa. Katika siku iliyokuu. Siku watapomsimamia watu Mola Mlezi wa walimwengu wote?” (83:1-6)

Allah تعالی Aliuangamiza umma mzima uliokuwa na Desturi ya kupunguza Mizani na vipimo¹. Kauli ya Allah تعالی:

لَا تُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا^ط

“Sisi Hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake”.

Maana: Atakayejitahidi kutekeleza haki na katika kuipokea, na kama atafanya makosa baada ya kutumia fursa na akafanya juhudi zake, basi hana madhambi.

Wasia wa saba: Amri ya Kutoa Ushahidi Adilifu.

Kauli ya Allah تعالی: وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ^ط

“Na msemapo semeni kwa uadilifu, ingawa ni jamaa”.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُفُونًا قَوْمِينَ ۚ لِلَّهِ شُهَدَاءُ بِالْقِسْطِ^ط

“Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkatoa ushahidi kwa haki”. (5:8)

Na kuna Aya inayoshabihiana nayo katika Surat An-Nisaa. Allah تعالی Anaamuru uadilifu katika matendo na kauli kwa walio karibu na wa mbali. Allah تعالی Anaamuru uadilifu kwa kila mmoja, wakati wote na katika kila hali.

Wasia wa nane: Amri ya Juu ya Kutekeleza Ahadi ya Allah تعالی.

Kauli ya Allah تعالی: وَيَعْهَدِ اللَّهُ أَوْفُوا^ط

“Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni”. Ibn Jarir رحمه الله تعالی alisema, “Allah تعالی Anaamuru: Na wasia Allah تعالی ambao Amekuusieni utekelezeni.

¹ Yaani fikra ya Mtume Shu'ayb عليه السلام, angalia Surat Al-A'raf 7:85-92.

Na kuutekeleza wasia huo, ni kumtii Yeye katika yale Aliyowaamuru na kuacha Aliyokukatazeni na mshikamane na Kitabu Chake na Sunna za Mtume Wake ﷺ. Huko ndiko kutekeleza ahadi za Allah تعالى.

ذَالِكُمْ وَصَّيْنَكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

“Hayo Amekuusieni ili mpate kukumbuka”. Allah تعالى Anasema, hayo Amekuagizeni na Kukuamrisheni na Akakusisitizieni.

لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

“...ili mpate kukumbuka”. Maana yake: Mnawaidhiwa na kwa hivyo mviache mliyokuwa mkivifanya kabla ya hivi¹.

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ذَٰلِكُمْ وَصَّيْنَكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٥٣﴾

153. Na kwa hakika hii ndiyo njia Yangu Iliyonyooka. Basi ifuateni, wala msifuata njia nyingine, zikakutengeni na njia Yake. Haya Amekuusieni ili mpate kuchamungu.

Wasia wa Tisa na wa Kumi: Amri ya Kuifuata Njia ya Allah تعالى Iliyonyooka na Kuziacha Njia Nyingine Zote.

‘Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما akiizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ

“...wala msifuata njia nyingine, zikakutengeni na njia Yake”.

Na Kauli nyingine;

أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ

“Kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo”. (42:13)

Na Ayah nyingine kama hii katika Qur’an, “Allah تعالى Aliwaamuru Waumini juu ya *Jama’ah* na Akawakataza kutofautiana na mfarakano, na Akawajulisha kwamba waliokuwa kabla yao waliangamizwa kwa sababu ya mabishano na ugomvi katika Dini ya Allah تعالى². Kauli kama hiyo ilitolewa na Mujahid na wengine³.

¹ At-Tabari 12:225.

² At-Tabari 12:229.

³ At-Tabari 12:229.

Imamu Ahmad bin Hanbal رضي الله عنه alimnukuu 'Abdullah bin Mas'ud رحمه الله تعالى akisema, "Mtume ﷺ akichora mistari kwa mkono wake (chini) na akasema;

«هَذَا سَبِيلُ اللَّهِ مُسْتَقِيمًا»

"Hii ni njia ya Allah iliyonyooka".

Kisha akachora mistari mingine inayokwenda kulia na kushoto mwa mstari huo, na akasema;

«هَذِهِ السُّبُلُ لَيْسَ مِنْهَا سَبِيلٌ إِلَّا عَلَيْهِ شَيْطَانٌ يَدْعُو إِلَيْهِ»

"Hizi ni njia nyingine ambapo hapana hata moja isiyokuwa na shetani anayelingania kuifuata".

Kisha Akasoma;

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ^٤

"Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu Iliyonyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na njia Yake." (6:153)¹

Al-Hakim pia aliinukuu Hadithi hii na akasema, "Isnadi yake ni Sahih, lakini hawakuinukuu"².

Imamu Ahmad na 'Abdi bin Humayd waliinukuu, kutoka kwa Jabir رضي الله عنه, na tamko hili ni la Ahmad, kwamba Jabir رضي الله عنه alisema, "Tulikuwa tumekaa pamoja na Mtume ﷺ akachora mstari mmoja mbele yake, Halafu akasema;

«هَذَا سَبِيلُ اللَّهِ»

"Hii ni njia ya Allah".

Kisha akachora mistari mingine miwili kuelekea kulia na mingine miwili kuelekea kushoto, na akasema,

«هَذِهِ سُبُلُ الشَّيْطَانِ»

"Hizi ni njia za Shaytan".

Kisha akaweka mkono wake katika njia ya katikati na akasoma Ayah hii;

¹ Ahmad 1:465.

² Al-Hakim 2:318.

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ۚ ذَٰلِكُمْ
 وَصَّيْنَاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٥٦﴾

“Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu Iliyonyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na njia Yake. Haya Amekuusieni ili mpate kuchamungu”¹.

Imamu Ahmad, Ibn Majah, katika Kitabu cha Sunnah ndani ya *Sunan* yake, na Al-Bazzar alilikusanya *Hadith* hii². Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kwamba mtu mmoja alimuambia Ibn Mas'ud رضي الله عنه, “Ni nini *As-Swiratwal-Mustaqim* (njia iliyonyooka)?” Ibn Mas'ud رضي الله عنه akasema, Muhammad ﷺ alituacha tukiwa katika ncha yake ya chini na ncha yake nyingine iko peponi. Kuumeni kwa njia hii na kushotoni kwake kuna njia nyinginezo, na katika njia hizo kuna watu wanaowalingania karibu yao. Atakayekwenda katika njia hizo ataishia Motoni na atakayefuata njia iliyonyooka ataingia peponi”. Kisha Ibn Mas'ud رضي الله عنه akasoma;

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ۚ

“Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu Iliyonyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na njia Yake”³.

Imamu Ahmad alinukuu kwamba, An-Nawwas bin Sam'ah رضي الله عنه alisema Mtume ﷺ alisema;

«ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا، وَعَنْ جَنبَيْهِ الصِّرَاطِ سُرُورَانِ فِيهِمَا أَبْوَابٌ مُنْفَتِحَةٌ، وَعَلَى الْأَبْوَابِ سُورٌ مُرْخَاةٌ وَعَلَى بَابِ الصِّرَاطِ دَاعٍ يَدْعُو: يَا أَيُّهَا النَّاسُ هَلُمُّوا اذْخُلُوا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا وَدَاعٍ يَدْعُو مِنْ فَوْقِ الصِّرَاطِ فَإِذَا أَرَادَ الْإِنْسَانُ أَنْ يَفْتَحَ شَيْئًا مِنْ تِلْكَ الْأَبْوَابِ قَالَ وَيَحَكُّ لَا تَفْتَحُهُ فَإِنَّكَ إِنْ فَتَحْتَهُ تَلَجَّهُ فَالصِّرَاطُ الْإِسْلَامُ وَالسُّورَانِ حُدُودُ اللَّهِ وَالْأَبْوَابُ الْمُنْفَتِحَةُ مَحَارِمُ اللَّهِ وَذَلِكَ الدَّاعِي عَلَى رَأْسِ الصِّرَاطِ كِتَابُ اللَّهِ، وَالدَّاعِي مِنْ فَوْقِ الصِّرَاطِ وَاعِظُ اللَّهِ فِي قَلْبِ كُلِّ مُسْلِمٍ»

“Allah Alipiga mfano wa njia iliyonyooka na pembeni mwa njia hiyo kuna kuta mbili ambazo zina milango iliyokuwa wazi. Katika milango

¹ Ahmad 3:397 na 'Abd bin Humayd na. 345.

² Ibn Majah 11.

³ At-Tabari 12:230.

kuna mapazia yaliyoning'inizwa mpaka chini. Katika njia kuna mlinganiaji anayenadi: "Enyi watu! Njoooni nyote muingie katika njia iliyonyooka, wala msifarakane". Na kuna mlinganiaji anayenadi kutoka juu ya njia. Mwanadamu anapotaka kufungua mlango wowote uliopo, humuambia, "Ole wako! Usiufungue, kwani kama utaufungua utaingia". Njia ni Uislamu, kuta mbili ni mipaka ya Allah, milango iliyo wazi ni matendo yaliyoharamishwa, mlinganiaji katika lango la njia ni Kitabu cha Allah, na mlinganiaji aliye juu ya njia ni maonyo ya Allah katika moyo wa kila Muislamu"¹.

At-Tirmidhi na An-Nasai pia waliinukuu Hadithi hii na At-Tirmidhi alisema, Hasan Gharib"².

فَاتَّبِعُوهُ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ

"Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine". Allah تعالى Aliitaja njia Yake kwa neno la umoja (Sswiratal Mustaqim) kwa sababu haki ni moja tu, na Anazieleza njia nyinginezo kwa neno la wingi (Subulu), kwa sababu ni nyingi na zimegawanyika. Allah تعالى Alisema katika Aya nyingine;

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا ءَٰوِيَاءُهُمُ
الطُّغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ ۗ ءَٰوَلَيْكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا
خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

"Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Huwatoa gizani na Kuwaingiza mwangazani. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni Mashetani. Huwatoa kwenye mwangaza na Kuwaingiza gizani. Hao ndio watu wa Motoni, na humo watadumu". (2:257)

ثُمَّ ءَاتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ تَمَامًا عَلَى الَّذِي أَحْسَنَ وَتَفْصِيلًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً
لِّعَلَّهُمْ بِلِقَاءِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ ﴿٢٥٨﴾ وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ
تُرْحَمُونَ ﴿٢٥٩﴾

154. Tena Tulimpa Musa Kitabu kwa kumtimizia (neema)

¹ Ahmad 4:182.

² Tuhfatul Al-Ahwadhi 8:152 na An-Nasai katika Al-Kubra 6:231.

aliyefanya wema, na kuwa ni maelezo ya kila kitu, na uwongofu na rehema, ili wapate kuamini mkutano wao na Mola wao Mlezi.

155. Na hichi ni Kitabu Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa. Basi kifuateni, na mchenimungu, ili mrehemewe.

Kuisifia Qur'an na Taurati.

Baada ya Allah تعالیٰ Kuizungumzia Qur'an kwa kusema;

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ^ط

“Na kwa hakika hii ndiyo njia Yangu iliyonyooka. Basi ifuateni...”.

Kisha Aliisifia Taurati na Mtume Wake ﷺ. Alisema;

ثُمَّ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ

“Tena Tulimpa Musa Kitabu”. Mara kwa mara, Allah تعالیٰ Alikutanisha Kuitaja Qur'an na Taurati. Sawa na Kauli ya Allah تعالیٰ;

وَمِن قَبْلِهِ كِتَابَ مُوسَى إِمَامًا وَرَحْمَةً^ط وَهَذَا كِتَابٌ مُّصَدِّقٌ لِّسَانِ عَرَبِيًّا

“Na kabla yake kilikuwapo Kitabu cha Musa, kuwa chenye uwongozi na rehema. Na hichi ni Kitabu cha kusadikisha na kilichokuja kwa lugha ya Kiarabu”. (46:12)

Na Kauli Yake nyingine mwanzoni mwa Sura hii;

قُلْ مَنْ أَنْزَلَ الْكِتَابَ الَّذِي جَاءَ بِهِ مُوسَى نُورًا وَهُدًى لِّلنَّاسِ^ط تَجْعَلُونَهُ قَرَاطِيسَ تُبْدُونَهَا وَتُخْفُونَ كَثِيرًا^ط

“Sema: Nani aliyeteremsha Kitabu alichokuja nacho Musa, chenye nuru na uwongofu kwa watu, mlichokifanya kurasa kurasa mkizionesha, na mengi mkiyaficha”. (6:91) Na baada yake;

وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مَبَارَكٌ

“Na hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa...”. (6:92)

Katika kutujulisha khabari za washirikina, Allah تعالیٰ Alisema;

فَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوا لَوْلَا أُوتِيَ مِثْلَ مَا أُوتِيَ مُوسَىٰ

"Ilipowajia Haki kutoka Kwetu walisema: Mbona hakupewa kama aliyopewa Musa?..." (28:48)

Allah تعالی Alisema;

أَوَلَمْ يَكْفُرُوا بِمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ مِنْ قَبْلُ قَالُوا سِحْرَانِ تَظَاهَرَا وَقَالُوا إِنَّا بِكُلِّ كَافِرٍ

"Je! Kwani wao hawakuyakataa aliyopewa Musa zamani? Walisema: Ni wachawi wawili wanasaidiana. Na wakasema: Hakika Sisi Tunawakataa wote". (28:48)

Allah تعالی Alitueleza khabari za majini kwamba walisema;

يَنْفَوْمَنَا إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا أُنزِلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَىٰ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ

"Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi Tumesikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake, na kinachoongoza kwenye Haki...". (46:30)

Kauli ya Allah تعالی;

تَمَامًا عَلَى الَّذِي أَحْسَنَ وَتَفْصِيلًا

"kwa kumtimizia (neema) aliyefanya wema, na kuwa ni maelezo...".

Ina maana, "Tulimpa Kitabu Tulichokiteremsha kikiwa kitimilifu, kikamilifu na kilichokusanya yale yanayohitajiwa katika sharia Yake". Sawa na Kauli ya Allah

تعالی;

وَكَتَبْنَا لَهُ فِي الْأَلْوَابِ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ

"Na Tukamuandikia katika mbao kila kitu...". (7:145)

Kauli ya Allah تعالی;

عَلَى الَّذِي أَحْسَنَ

"...aliye fanya wema...". Maana yake: Hali ya kuwa ni malipo ya ihsani yake katika utendaji na kutekeleza Amri Zetu kwa usahihi na utii wake Kwetu. Sawa na Kauli ya Allah تعالی;

هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَنِ إِلَّا الْإِحْسَانُ ﴿٥٥﴾

"Ati yaweza kuwa malipo ya ihsani ila ihsani?" (55:60)

Na Kauli Yake:

﴿ وَإِذْ أَبْتَأْتَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۗ قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ۗ ﴾

“Na Mola wake Mlezi Alipomjaribu Ibrahim kwa Kumpa amri fulani, naye akatimiza, Akamuambia: Hakika Mimi nitakufanya uwe mwongozi wa watu”. (2:124) Na;

﴿ وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ أَئِمَّةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا صَبَرُوا ۖ وَكَانُوا بِعَٰيَتِنَا يُوقِنُونَ ﴾

“Na Tukawafanya miongoni mwao waongozi wanaoongoa watu kwa Amri Yetu, waliposubiri na wakawa na yakini na Ishara Zetu”. (32:24)

Kauli ya Allah تعالى:

﴿ وَتَفْصِيلًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً ۗ ﴾

“...na kuwa ni maelezo ya kila kitu, na uwongo fu na rehema”.

Ndani yake, kuna maelezo ya kukisifu Kitabu Chake Alichomteremshia (Musa عليه السلام).

﴿ لَعَلَّهُمْ يُلْقَآءَ رَبَّهُمْ يُؤْمِنُونَ ﴾ ﴿ وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴾

“...ili wapate kuamini mkutano wao na Mola wao Mlezi. Na hichi ni Kitabu Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa. Basi kifuateni, na mchenimungu, ili mrehemewe”.

Ndani ya Aya hizi kuna wito wa kuifuata Qur'an. Allah تعالى Anawatia moyo waja Wake wakifuata Kitabu Chake na Anawaamuru wakizingatie na kukifanyia kazi na walinganie kukizingatia na kukiendea, na Akakielezea kwamba ni chenye baraka kwa watakaokifuata na kukifanya mwongozo katika maisha ya duniani na Akhera kwa sababu ndiyo kamba madhubuti ya Allah تعالى.

﴿ أَنْ تَقُولُوا إِنَّمَا أَنْزَلَ إِلَهُكُمُ عَلَىٰ طَائِفَتَيْنِ مِنَ قَبْلِنَا وَإِنْ كُنَّا عَنْ دِرَاسَتِهِمْ لَغَافِلِينَ ﴾ ﴿ أَوْ تَقُولُوا لَوْ أَنَّا أُنزِلَ عَلَيْنَا الْكِتَابُ لَكُنَّا أَهْدَىٰ مِنْهُمْ ۗ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةً ۗ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن كَذَّبَ بِعَٰيَاتِ اللَّهِ وَصَدَفَ عَنْهَا ۗ سَنَجْزِي الَّذِينَ يَصْدِفُونَ عَنْ ءَايَاتِنَا سُوءَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوا يَصْدِفُونَ ﴾

156. Msije mkasema: Hakika mataifa mawili kabla yetu yameteremshiwa Kitabu; na sisi tulikuwa hatuna khabari ya waliyokuwa wakiyasoma.

157. Au mkasema: Lau kuwa tumeteremshiwa sisi Kitabu tungelikuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu na rehema. Basi nani aliye dhalimu mkubwa zaidi kuliko yule anayekanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, na akajitenga nazo? Tutawalipa wanaojitenga na Ishara Zetu adhabu kali kabisa kwa sababu ya kujitenga kwao.

Qur'an ni Hoja ya Allah تعالیٰ Juu ya Viumbe Wake.

Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ alisema, maana yake ni Kitabu hiki Tumekiteremsha ili msije mkasema;

إِنَّمَا أَنْزَلَ الْأَكْتَابَ عَلَىٰ طَائِفَتَيْنِ مِنْ قَبْلِنَا

“Hakika mataifa mawili kabla yetu yameteremshiwa Kitabu...”.

Maana yake: Ili udhuru wenu ukatike. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ;

وَلَوْلَا أَنْ تُصِيبَهُمْ مُصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ فَيَقُولُوا رَبَّنَا لَوْلَا أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا
فَتَتَّبَعْنَا آيَاتِكَ

“Na usije kuwasibu msiba kwa iliyotanguliza mikono yao, wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Mbona hukututumia Mtume nasi, tukafuata Ishara zako”. (28:47)¹

Na Kauli Yake;

عَلَىٰ طَائِفَتَيْنِ مِنْ قَبْلِنَا

“...mataifa mawili kabla yetu...”. ‘Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما akisema kwamba hao ni Wayahudi na Wakristo². Na hivi ndivyo alivyosema Mujahid, As-Suddi, Qatadah na wengine kadhaa³. Kauli Yake;

وَإِنْ كُنَّا عَنْ دِرَاسَتِهِمْ لَغَفْلِينَ

“...na sisi tulikuwa hatuna khabari ya waliyokuwa wakiyasoma...”.

¹ At-Tabari 12:239.

² At-Tabari 12:240.

³ At-Tabari 12:241.

Maana yake: Hatukuwa tukiyaelewa waliyokuwa wakiyasema, kwa sababu hayakuwa katika lugha yetu, nasi tulikuwa na kazi nyingine na tukaghafilika juu ya yale waliyokuwa wakishughulika nayo. Kauli ya Allah تعالى;

أَوْ تَقُولُوا لَوْ أَنَّا أُنزِلَ عَلَيْنَا الْكِتَابُ لَكُنَّا أَهْدَىٰ مِنْهُمْ ۗ

“Au mkasema: Lau kuwa tumeteremshiwa sisi Kitabu tungelikuwa waongofu zaidi kuliko wao...”.

Na tuliukata udhuru wenu huu, ili msije mkasema, “Kama Kitabu tungeliteremshiwa kama walivyoteremshiwa, tungeliongoka zaidi kuliko wao”. Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن جَاءَهُمْ نَذِيرٌ لَّيَكُونُنَّ أَهْدَىٰ مِنْ إِحْدَى الْأُمَمِ ۗ

“Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa kuapa kwao, kwamba akiwaja Mwonyaji bila ya shaka watakuwa waongofu zaidi kuliko taifa jingine lolote...”. (35:42)

Hapa pia Allah تعالى Alisema;

فَقَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ ۗ

“Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu na rehema”.

Allah تعالى Anasema, Imekujieni Qur'an tukufu, kutoka kwa Allah تعالى kupitia ulimi wa Muhammad ﷺ, Mtume mwarabu, ndani yake imebainishwa halali na haramu na uongofu wa yaliyo nyoyoni, na pia ni rehema kutoka kwa Allah تعالى kwa waja Wake wanaokifuata na kuyatumia yaliyomo. Kauli ya Allah تعالى;

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن كَذَبَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَصَدَفَ عَنْهَا ۗ

“Basi nani aliye dhalimu mkubwa zaidi kuliko yule anayekanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, na akajitenga nazo?”

Maana yake: Hakujuinufaisha na yale aliyokuja nayo Mtume ﷺ wala hakufuata kile alichotumwa nacho, wala hakuwaacha wengine wazifuate, bali aliwakitisha tamaa na aliwazuia watu dhidi ya kuzifuata ishara za Allah تعالى. Hayo ni kwa mujibu wa As-Suddi, ama Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na Qatadah walisema maana ya *Sadafa 'anha* ni alizipa mgongo ishara za Allah تعالى. Allah تعالى Anasema;

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ أَوْ يَأْتِيَ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ يَوْمَ يَأْتِي بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِنْ قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيْمَانِهَا خَيْرًا ۗ قُلِ أَنْتَظِرُوا إِنَّا مُنْتَظِرُونَ ﴿١٥٨﴾ إِنَّ الَّذِينَ فَرَقُوا دِيْنَهُمْ وَكَانُوا شَيْعًا لَسْتَ مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ ۚ إِنَّمَا أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُمْ بِمَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿١٥٩﴾ مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرٌ أَمْثَالِهَا ۗ وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَى إِلَّا بِمِثْلِهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦٠﴾ قُلْ إِنِّي هَدَيْتُ رَبِّي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ دِيْنًا قِيَمًا مِْلَةً إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۚ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٦١﴾ قُلْ إِنْ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾ لَا شَرِيكَ لَهُ ۚ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾ قُلْ أَعْيَرَ اللَّهُ أَبْنِي رَبًّا وَهُوَ رَبُّ كُلِّ شَيْءٍ ۗ وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ إِلَّا عَلَيْهَا ۗ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَى ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ مَرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿١٦٤﴾ وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ خُلُقِيْنَ الْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِيُبْلُوَكُمْ فِي مَا ءَاتَاكُمْ ۗ إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ الْعَقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٦٥﴾

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ أَوْ يَأْتِيَ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ يَوْمَ يَأْتِي بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِنْ قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيْمَانِهَا خَيْرًا ۗ قُلِ أَنْتَظِرُوا إِنَّا مُنْتَظِرُونَ ﴿١٥٨﴾

158. Wanangoja jengine ila wawafikie Malaika, au awafikie Mola wako Mlezi au zifike baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi? Siku zitakapofika baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi, kuamini hapo hakutumfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake, au amefanya kheri katika Imani yake. Sema: Ngojeni, nasi pia tunangoja.

Onyo kwa Kila Acheleweshae Imani Yake na Toba Yake.

Allah تعالى Anawaonya wanaomkufuru, wanaomkhalifu Mtume Wake ﷺ, wakadhibishao ishara Zake na wanaozuilia watu dhidi ya njia Yake, kwa Kusema;

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ

“Wanangoja jengine ila wawafikie Malaika, au Awafikie Mola wako Mlezi”.

Hilo litatukia katika Siku ya Kiyama.

أَوْ يَأْتِيَنَّ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ يَوْمَ يَأْتِي بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا

“...au zifike baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi? Siku zitakapofika baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi, kuamini hapo hakutomfaa mtu kitu”.

Hayo ni yenye kutokea kabla ya kufika Siku ya Kiyama zitapojitokeza alama na ishara za Kiyama na pindi watakapoziona baadhi yake, kama Al-Bukhari alivyomnukuu Abu Hurayrah عنه رضي الله عنہ kuhusu tafsiri ya Aya hii, kwamba Mtume ﷺ alisema;

«لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى تَطْلُعَ الشَّمْسُ مِنْ مَغْرِبِهَا فَإِذَا رَأَاهَا النَّاسُ آمَنَ مَنْ عَلَيْهَا فَذَلِكَ جِبِينٌ»

“Kiyama hakitosimama mpaka jua lichomoze kutokea upande wa magharibi yake. Watu wakishaliona, waliomo duniani wataamini”.

Basi huo ndio wakati ambapo;

لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِنْ قَبْلُ

“...hakutomfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake”¹.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Abu Hurayrah عنه رضي الله عنہ kuwa alisema Mtume ﷺ alisema;

«ثَلَاثٌ إِذَا خَرَجْنَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ آمَنَتْ مِنْ قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيمَانِهَا خَيْرًا، طُلُوعُ الشَّمْسِ مِنْ مَغْرِبِهَا وَالذَّجَالُ وَدَابَّةُ الْأَرْضِ»

“Matatu yatakapotokea, haitaifaa nafsi imani yake iwapo haikuwa imeamini au kunufaika na imani hiyo hapo kabla, kuchomoza jua kutokea upande wa magharibi yake, Dajjal na mnyama wa ardhi”².

Alimnukuu Ahmad, na katika nukuu yake ni kuwa Mtume ﷺ pia alitaja moshi³.

Imamu Ahmad alimnukuu 'Amr bin Jarir kuwa alisema, “Watu watatu Waislamu walikaa pamoja na Marwan huko Madinah, wakamsikia akizungumzia ishara za Siku ya Kiyama, akisema kwamba ya mwanzo ni Dajjal. Watu hawa wakaenda

¹ Fat'hul Al-Bari 8:147.

² At-Tabari 12:265.

³ Ahmad 2:445.

kwa 'Abdullah bin 'Amr na wakamueleza waliyoambiwa na Marwan kuhusu alama za Kiyama. Naye akasema, Marwan hajasema kitu, mimi ninakumbuka nilimsikia Mtume ﷺ akisema;

«إِنَّ أَوَّلَ الْآيَاتِ خُرُوجًا طُلُوعُ الشَّمْسِ مِنْ مَغْرِبِهَا وَخُرُوجُ الدَّابَّةِ ضَحَى فَأَيُّهُمَا
كَانَتْ قَبْلَ صَاحِبِهَا فَالْآخَرَى عَلَى أَثَرِهَا»

“Alama ya mwanzo kutokea, ni kuchomoza jua kutokea upande wa magharibi yake na kuchomoza mnyama wakati wa dhuha, chochote kati ya viwili hivi kikitokea, basi chenzake kitafuatia”¹.

Kisha, 'Abdullah ambaye alikuwa akisoma vitabu, akasema, na ninadhani alama ya mwanzo kutokea ni jua kuchomoza kutoka upande wa Magharibi na hiyo ni kwa sababu, kila linapokuchwa, linakwenda chini ya Arshi, linasujudu na linaomba idhini ya kurejea upande wa Mashariki na linaruhusiwa, mpaka Allah تعالی Atakapolitaka lichomoze kutokea upande wa Magharibi. Kwa hivyo litafanya kama kawaida yake, litakwenda chini ya Arshi, litasujudu, litaomba idhini ya kurejea, lakini halitapewa jibu lolote, mpaka ufike muda wa usiku kwa kiasi Atakachotaka Allah تعالی, na litajua kwamba kama litaruhusiwa kurejea, halitaweza kuwahi upande wa Mashariki. Litasema, “Ewe Mola wangu! Upande wa Mashariki ni mbali, nitakuwa na uzuri gani kwa watu?” Mpaka upeo wa macho utaonekana kama mzunguko (usio na rangi), litaomba idhini ya kurejea na litaambiwa, “Chomoza kutokea mahali ulipo”. Basi hapo litachomozea watu kutokea upande wa machweo yake”. Kisha Abdallah alisema;

لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِنْ قَبْلُ

“...hakutomfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake...”.

Hadithi hii ilinukuliwa pia na Muslim katika *Sahih* yake na Abu Dawud na Ibn Majah katika *Sunan* zao². Kwa hiyo, Kauli ya Allah تعالی;

لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِنْ قَبْلُ

“...hakutomfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake”.

¹ Ahmad 2:201.

² Muslim 4:2260, Abu Dawud 4:490 na Ibn Majah 2:1335. Maneno yote kwa ukamilifu wake, yapo kwa Ahmad. Hadithi ipo kwa Muslim, sentensi ya kwanza inatoka kwa 'Abdullah ipo kwa wengine.

Maana yake: Ikiwa kafiri ataanza kuwa na imani kuanzia siku hiyo, hatakubaliwa, lakini ambaye alikuwa muumini kabla ya hapo na akawa mtenda mema katika amali zake, atakuwa katika kheri kubwa, na kama hakuwa mtenda mema, na akafanya toba katika Siku hiyo, haitakubaliwa. Ni sawa na ilivyojulishwa na Hadithi zilizotangulia. Hivyo ndiyo tafsir ya Kauli ya Allah تعالى:

أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيمَانِهَا خَيْرًا

"...au amefanya kheri katika Imani yake". Maana yake: Wala haitakubaliwa amali njema ikiwa haikufanywa kabla ya hapo. Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ أَنْتَظِرُونَ إِنَّا مُنتَظِرُونَ

Sema: Ngojeni, nasi pia tunangoja".

Hili ni onyo kali kwa makafiri, pia ni ahadi iliyosisitizwa dhidi ya mwenye kuichelewesha imani na toba yake mpaka katika wakati ambao hilo halitamnufaisha. Na hukumu hii ni baada ya jua kuchomoza kutokea upande wa Magharibi kwa sababu ya kukaribia Kiyama na kudhihiri ishara Zake. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَهَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَنْ تَأْتِيَهُمْ بَغْتَةً ۖ فَقَدْ جَاءَ أَشْرَاطُهَا ۗ فَأَنَّى لَهُمْ إِذَا جَاءَهُمْ
ذِكْرُهُمْ ﴿١٥٨﴾

"Kwani wanangojea jengine isipokuwa iwafikie Saa (ya Kiyama) kwa ghafla? Na hakika alama zake zimekwisha kuja. Na itapowajia kutawafaa wapi kukumbuka hapo?" (47:18) Na;

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَحَدَّهُدُ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ ﴿١٥٩﴾ فَلَمَّا يَكُ
يَنْفَعُهُمْ إِيمَانُهُمْ لَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا ۗ

"Walipoiona Adhabu Yetu walisema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni wa pekee, na tunaikataa miungu tuliyokuwa tukiishirikisha naye. Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa kitu wakati ambao wamekwishaiona Adhabu Yetu". (40:84-85)

إِنَّ الَّذِينَ فَرَقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيعًا لَسْتَ مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ ۗ إِنَّمَا أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُمْ بِمَا
كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿١٦٥﴾

159. Hakika walioigawa Dini yao na wakawa makundi makundi, huna uhusiano nao wowote. Bila ya shaka shauri lao liko kwa Mwenyezi Mungu; kisha Atawaambia yale waliyokuwa wakiyatenda". (6:159)

Shutuma Dhidi ya Mifarakano Katika Dini.

Mujahid, Qatadah, Adh-Dhahhak na As-Suddi walisema kuwa Ayah hii iliteremshwa juu ya Wayahudi na Wakristo¹. Al-'Awfi alisema kwamba Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliieleza Kauli ya Allah تعالى;

إِنَّ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيَعًا

"Hakika walioigawa Dini yao na wakawa makundi makundi".

Jambo hilo ni kwamba, Wayahudi na Wakristo, walikhitilafiana kabla Muhammad ﷺ hajaletwa, na wakafarakana. Baada ya Muhammad ﷺ kutumwa, Allah تعالى Aliteremsha;

إِنَّ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيَعًا لَسْتَ مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ

"Hakika walioigawa Dini yao na wakawa makundi makundi, huna uhusiano nao wowote."²

Ni dhahiri Ayah hii inamlenga kila anayejitenga na Dini ya Allah تعالى, na kuikhalifu. Allah تعالى Alimtuma Mtume Wake ﷺ kwa uongofu na Dini ya kweli ili izishinde dini nyingine zote, na Sharia Yake ni moja, na ambayo hakuna khitilafu wala mfarakano ndani yake. Basi wanaoleta khitilafu katika dini;

وَكَانُوا شِيَعًا

"...na wakawa makundi makundi".

Makundi, kama yale yafuatayo mila na tamaduni zao (na kudai kuwa dini hazipingani na mila za watu), basi Allah تعالى Amemuepusha Mjumbe Wake dhidi ya yale waliyo nayo.

Na Aya hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى;

¹ At-Tabari 12:269 -270.

² At-Tabari 12:269.

شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ

“Amekuamrishi Dini ile ile Aliyomuusia Nuhu na Tuli yokufunulia wewe”. (42:13)

Imepokelewa katika Hadithi kuwa;

«نَحْنُ مَعَاشِرُ الْأَنْبِيَاءِ أَوْلَادُ عُلَاتٍ دِينَنَا وَاجِدٌ»

“Sisi, Mitume, ni ndugu wa baba mmoja wa kambo, kwani Dini yetu ni moja”¹.

Basi hii ndiyo njia iliyonyooka, na ndiyo waliyokuja nayo Mitume kwa ajili ya kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, Asiyekuwa na mshirika pamoja na kushikamana na Sheria ya Mjumbe wa mwisho aliyetumwa na Allah تعالى. Ama kinyume cha hayo ni upotevu, ujahili, maoni matupu na utashi. Na Mitume wamesalimika dhidi ya hayo. Kama Kauli ya Allah تعالى inavyosema;

لَسْتُ مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ

“...huna uhusiano nao wowote”. (6:159)

Kauli ya Allah تعالى;

إِنَّمَا أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُوا يَفْعَلُونَ

“Bila ya shaka shauri yao iko kwa Mwenyezi Mungu; kisha Atawaambia yale waliyokuwa wakiyatenda”.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّابِغِينَ وَالنَّصْرَى وَالْمَجُوسَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا إِنَّ اللَّهَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Hakika walioamini, na ambao ni Mayahudi na Wasabai na Wakristo na Majusi na wale walioshiriki – hakika Mwenyezi Mungu Atawapambanua baina yao Siku ya Kiyama”. (22:17)

Kisha Allah تعالى Alibainisha kuwa Yeye ni Latifu katika Hukumu Yake na Uadilifu Wake katika Siku ya Kiyama, Alisema;

¹ Fat’hul Al-Bari 6:550.

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۗ وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٥٨﴾

"Afanyae wema atalipwa mfano wake mara kumi, na afanyae ubaya hatalipwa ila sawa nao tu. Na wao hawatadhulumiwa".
(6:160)

Tendo Jema Hulipwa Mara Kumi Mfano Wake na Ovu Hulipwa Mara Moja.

Aya hii tukufu inafafanua yaliyokusanywa na Aya nyinginezo, nayo ni Kauli ya Allah تعالى:

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۗ

"Atakayetenda wema atapata malipo bora kumi mfano wake".
(28:84)

Kuna Hadithi kadha zilizonukuliwa ambazo zinaafikiana na Aya hii. Kama Imamu Ahmad bin Hanbal رحمه الله تعالى alivyomnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ alisema katika Hadithi aliyoipokea kutoka kwa Mola Wake Mlezi;

«إِنَّ رَبَّكُمْ عَزَّ وَجَلَّ رَجِيمٌ مَنْ هَمَّ بِحَسَنَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْهَا كُتِبَتْ لَهُ حَسَنَةٌ فَإِنْ عَمِلَهَا كُتِبَتْ لَهُ عَشْرًا إِلَى سَبْعِمِائَةٍ إِلَى أضعافٍ كَثِيرَةٍ. وَمَنْ هَمَّ بِسَيِّئَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْهَا كُتِبَتْ لَهُ حَسَنَةٌ فَإِنْ عَمِلَهَا كُتِبَتْ لَهُ وَاحِدَةٌ أَوْ يَمْحُومَهَا اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ وَلَا يَهْلِكُ عَلَى اللَّهِ إِلَّا هَالِكٌ»

"Kwa hakika, Mola wenu ni Rahimu. Hivyo Mtu mwenye kudhamiria kufanya jema na akawa hakulifanya, ataandikiwa jema moja. Akilifanya, ataandikiwa mema kumi mpaka mia saba, mpaka mara nyingi zaidi. Na atakayedhamiria kufanya ovu, na akawa hakulifanya, ataandikiwa jema. Akilitenda, ataandikiwa ovu moja au Allah Atalifuta. Wala haangamii kwa Allah yeyote, isipokuwa Anayestahiki kuangamia"¹.

Ameinukuu Bukhari, Muslim na An-Nasai². Ahmad alinukuu pia, kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه kuwa alisema Mtume ﷺ alisema;

¹ Ahmad 1:279.

² Fat'hul Al-Bari 11:331, Muslim 1:118 na An-Nasai katika Al-Kubra 4:396.

«يَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: مَنْ عَمِلَ حَسَنَةً فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا وَأَزِيدُ وَمَنْ عَمِلَ سَيِّئَةً فَجَزَاؤُهَا مِثْلُهَا أَوْ أَغْفِرُ وَمَنْ عَمِلَ قُرَابَ الْأَرْضِ خَطِيئَةً نُمَّ لِقَيْبِي لَا يُشْرِكُ بِي شَيْئًا جَعَلْتُ لَهُ مِثْلَهَا مَغْفِرَةً، وَمَنْ اقْتَرَبَ إِلَيَّ شِبْرًا اقْتَرَبْتُ إِلَيْهِ ذِرَاعًا وَمَنْ اقْتَرَبَ إِلَيَّ ذِرَاعًا اقْتَرَبْتُ إِلَيْهِ بَاعًا وَمَنْ أَتَانِي بِمِثْبَ أُتَيْتُهُ هَرُونَ»

“Allah Amesema, mwenye kufanya jema Nitamlipa kumi katika wema huo na zaidi, na mwenye kufanya ovu, malipo yake ni sawa na uovu huo na Nasamehe. Mwenye kufanya makosa ujazo wa dunia kisha akakutana Nami akiwa hanishirikishi na chochote, Nitampa maghfira sawa na ujazo huo. Na atakayejisogeza Kwangu kiasi cha shubiri, Mimi Nitamsogelea kiasi cha dhira, na atakayejikurubisha Kwangu kiasi cha dhira, Mimi Nitamsogelea kiasi cha kitengele. Na atakayenijia kwa kutembea, Mimi Nitamkimbilia”¹. Ameinukuu Muslim².

Na tambueni kuwa wanaoacha kutenda dhambi walizodhamiria wamegawanyika katika namna tatu. Wenye kuacha kwa sababu ya kumuogopa Allah تعالی, huandikiwa jema moja kwa kuacha kwake dhambi kwa ajili ya Allah تعالی. Hii inatokana na nia njema, kama ilivyonyukuliwa. Katika baadhi ya nukuu za *Sahih*, Allah تعالی Anasema kuwa mja huyu, *“Ameacha dhambi kwa ajili Yangu”*. Wakati mwingine mtu huacha dhambi kwa kusahau au kuwa na shughuli nyingine (hii ni aina nyingine). Huyu hapati dhambi wala thawabu. Sababu ni kwamba, huyu hakukusudia kufanya kheri, wala kufanya shari. Na wakati mwingine mtu huiacha kwa kushindwa au kwa uvivu, baada ya kujaribu kuiendea na kujiingiza katika yanayopelekea kuitenda. Mtu huyu yuko katika daraja ya mwenye kuifanya. Sawa na ilivyokuja katika Hadithi *Sahih*, kuwa Mtume ﷺ alisema;

«إِذَا اتَّخَى الْمُسْلِمَانِ بَيْنَهُمَا قَاتِلًا وَالْمَقْتُولَ فِي النَّارِ»

“Waislamu wawili wakikabiliwa kwa panga zao basi muuaji na muuliwa wote ni wa motoni”.

Wakasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Tunajua kuhusu kosa la muuaji, vipi kuhusu muuliwa?” Akasema;

¹ Ahmad 5:153.

² Muslim 4:2068.

«إِنَّهُ كَانَ حَرِيصًا عَلَى قَتْلِ صَاحِبِهِ»

“Naye alikuwa na pupa ya kumuua mwenzake”.¹ Al-Hafidh Abul-Qasim At-Tabarani alimnukuu Abu Malik Al-Ash'ari رضى الله عنه kwamba alisema, Mtume ﷺ alisema;

«الْجُمُعَةُ كَفَّارَةٌ لِمَا بَيْنَهَا وَبَيْنَ الْجُمُعَةِ الَّتِي تَلِيهَا وَزِيَادَةُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ، وَذَلِكَ لِأَنَّ اللَّهَ تَعَالَى قَالَ: ﴿مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَثْمَالِهَا﴾»

“Ijumaa ni kafara ya madhambi ya baina yake na Ijumaa inayofuatia na nyongeza ya siku tatu. Hayo ni kwa kuwa Allah تعالى Alisema, “Afanyae wema atalipwa mfano wake mara kumi”.²

Abu Dharr رضى الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema;

«مَنْ صَامَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ مِنْ كُلِّ شَهْرٍ فَقَدْ صَامَ الدَّهْرَ كُلَّهُ»

“Mwenye kufunga siku tatu kwa kila mwezi, atakuwa amefunga mwaka mzima”.

Ameinukuu Imamu Ahmad, na hili ndilo tamko lake; An-Nasai, Ibn Majah na At-Tirmidhi walisema;

«فأنزل الله تصديق ذلك في كتابه»

“Allah Akateremsha uthibitisho wa hilo katika Kitabu Chake, kuwa;

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَثْمَالِهَا^٣

“Afanyae wema atalipwa mfano wake mara kumi”.

«اليوم بعشرة أيام»

“Kwa hivyo, siku moja inalipwa kwa siku kumi”. Halafu akasema, Hadithi hii ni Hasan.³ Kuna Hadithi na kauli nyingi zinazohusu maudhui hii, na zilizotajwa hapa zinatoshia, In shaa Allah.

قُلْ إِنِّي هَدَيْتَنِي رَبِّيَ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ دِينًا قَدِيمًا مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٥٨﴾ قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٥٩﴾ لَا شَرِيكَ لَهُ ۗ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٠﴾

¹ Al-Bukhari na. 31, 6875 na 7083.

² At-Tabarani 3:298.

³ Ahmad 5:146, Tuhfatul Al-Ahwadhi 3:470, An-Nasai 4:218 na Ibn Majah 1:545.

161. Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Mlezi Ameniongoa kwenye njia Iliyonyooka, Dini iliyo sawa kabisa, ambayo ndiyo mila ya Ibrahim aliye kuwa mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

162. Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.

163. Hana mshirika Wake. Na hayo ndiyo niliyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.

Uislamu Ndiyo Njia Iliyonyooka.

Allah تعالیٰ Anamuamuru Mtume Wake ﷺ, Bwana wa Mitume aelezee neema alizotunukiwa na Allah تعالیٰ, miongoni mwa kuongozwa katika njia iliyonyooka. Njia hiyo haiendi upogo wala haichepuki.

دِينًا قِيَمًا

“Dini iliyo sawa kabisa” Maana: Imesimamishwa katika misingi imara.

مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

“...ambayo ndiyo mila ya Ibrahim aliye kuwa mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina”.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ:

وَمَنْ يَرْغَبْ عَنْ مِلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَنْ سَفِهَ نَفْسَهُ

“Na nani atajitenga na mila ya Ibrahim isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu?” (2:130) Na;

وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ ۗ هُوَ أَجْتَبَكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ۗ مِلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ ۗ

“Na fanyeni juhudi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama inavyostahiki jihadi Yake. Yeye Amekuteueni. Wala Hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim”. (22:78) na;

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٥٨﴾ شَاكِرًا لِأَنْعُمِهِ
 أَجْتَبَنَاهُ وَهَدَيْنَاهُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٥٩﴾ وَءَاتَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ
 الصَّالِحِينَ ﴿١٦٠﴾ ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنْ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٦١﴾

“Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina. Mwenye kuzishukuru neema Zake, Mwenyezi Mungu. Kamteua yeye, na Akamuongoa kwenye njia iliyonyooka. Na Tukampa wema duniani, na hakika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema. Kisha Tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina”.
 (16:120-123)

Allah تعالیٰ Kumuamuru Mtume ﷺ kufuata mila ya Ibrahim عليه السلام, Al-Hanifiyyah¹, haimaanishi Ibrahim عليه السلام alikuwa mkamilifu zaidi ya Mtume ﷺ katika kutekeleza dini hiyo. Kwani Mtume ﷺ aliisimamisha kwa ukamilifu uliotimia, wala hakuna aliyempita katika kuikamilisha mila hiyo, na kwa hivyo, amekuwa Mtume wa mwisho na Bwana wa wana wote wa Adam عليه السلام, mwenye cheo chenye kusifiwa wanachokitamani viumbe wote, akiwemo Ibrahim عليه السلام, Khalil, mwandani wa Allah تعالیٰ.

Imamu Ahmad amenukuu kwamba Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mtume ﷺ aliulizwa, “Ni dini gani inayopendwa na Allah تعالیٰ?” Naye alisema;

«الْحَنِيفِيَّةُ السَّمْحَةُ»

“Al-Hanifiyyatus-samhah (Imani nyepesi kuwa kuna Mungu Mmoja tu)”²

Amri ya Kufanya Ikhlasu Katika Ibada.

Kauli ya Allah تعالیٰ;

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾

“Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote”.

¹ Angalia Tafsiri ya Surat Al-Baqarah na. 124.

² Ahmad 1:236.

Allah تعالی Anamuamuru Mtume ﷺ awapashe khabari washirikina wanaoabudu na kuchinja kwa jina lisilokuwa la Allah تعالی kwamba Anawapinga katika yote hayo, kwani Sala na ibada zake ni kwa ajili ya Allah تعالی Peke Yake, Ambaye Hana mshirika. Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی;

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَخَّرْ

“Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi”. (108:2)

Maana yake: Mfanyie ikhlasi Allah تعالی katika Sala yako na kuchinja kwako. Washirikina walikuwa wakiyaabudu masanamu na kuchinja kwa ajili yao. Allah تعالی Akamuamuru Mtume ﷺ awakhalifu na ayapinge wanayoyafanya. Na Akamtaka atamke kwamba nia na azma yake ni ikhlasi kwa Allah تعالی. Mujahid alisema, katika kufasiri Kauli ya Allah تعالی;

إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي

“Hakika Sala yangu, na ibada (Nusuk) zangu”. Kuwa An-Nusuk ni mnyama anayechinjwa katika Hijja na Umra. Ibn Abu Hatim alimnukuu Jabir bin 'Abdullah رضي الله عنه kuwa alisema, Mtume ﷺ alidhabihu kondoo wawili katika Sikukuu ya 'Idun-Nahr' (Idd ya kuchinja) na wakati huo wa kudhabihu alisema;

“Nimeelekeza uso wangu kwa Yule Ambaye Ameziumba mbingu na ardhi. Hali ya kuachana na Dini zote kushikamana na Uislamu. Na mimi si katika washirikina. Hakika Sala yangu na ibada zangu, na uhai wangu na kufa kwangu yote hayo yanamstahiki Mola Mlezi wa viumbe vyote. Ambaye Hana mshirika. Na kwa sababu hiyo nimeamrisha na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.”

Uislamu Ndiyo Dini ya Mitume Wote.

Kauli ya Allah تعالی;

وَأَنَا أَوْلُ الْمَسْلُومِينَ

“...na mimi ni wa kwanza wa Waislamu”.

Qatadah alisema maana yake, yeye ni Muislamu wa kwanza katika ummah huu¹. Nayo, kama alivyosema, ni kwa sababu Mitume wote wa kabla yake walikuwa wakilingania juu ya Uislamu, ambao unaamrisha imani ya kumuabudu Allah تعالی, Peke Yake, Asiye na mshirika. Sawa na Alivyosema;

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢٥﴾

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipokuwa Mimi. Basi Niabuduni Mimi tu”. (21:25)

Allah تعالى Ametupa khabari ya Nuhu عليه السلام kwamba aliwaambia kaumu yake;

فَإِنْ تَوَلَّيْتُمْ فَمَا سَأَلْتُكُمْ مِنْ أَجْرٍ ۖ إِنَّا كَجَرِيٍّ إِلَّا عَلَى اللَّهِ ۗ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٧٢﴾

“Lakini mkigeuka, basi mimi sikukuombeni ujira. Ujira wangu hauko ila kwa Mwenyezi Mungu. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu”. (10:72)

Pia Amesema;

وَمَنْ يَرْغَبْ عَنْ مِلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَنْ سَفِهَ نَفْسَهُ ۚ وَلَقَدِ اصْطَفَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٣٠﴾ إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ ۖ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٣١﴾ وَوَصَّي بِهَا إِبْرَاهِيمَ بَيْنَهُ وَيَعْقُوبَ يَنبِيُّ ۚ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ لَكُمْ الْبَيْنَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٣٢﴾

“Na nani atajitenga na mila ya Ibrahim isipo kuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu? Na kwa yakini Sisi Tulimteua yeye katika dunia, na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema. Na Mola wake Mlezi Alipomuambia: Silimu, Nyenyekea! Alinena: Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote. Na Ibrahim akawausia Wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu Amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu”. (2:130-131)

Naye Yusuf عليه السلام alisema;

* رَبِّ قَدْ آتَيْتَنِي مِنَ الْمُلْكِ وَعَلَّمْتَنِي مِنْ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ ۚ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ أَنْتَ وَلِيِّّ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۖ تَوَفَّنِي مُسْلِمًا وَأَلْحَقْنِي بِالصَّالِحِينَ ﴿١٢٤﴾

¹ At-Tabari 12:285.

“Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika Umenipa Utawala na Umenifunza tafsiri ya mambo. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe Ndiye Mlinzi wa dunia na Akhera! Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema”. (12:101)

Naye Musa عليه السلام alisema;

وَقَالَ مُوسَىٰ يَنْقُومِ إِن كُنتُمْ ءَامَنتم بِاللّهِ فَعَلَيْهِ تَوَكَّلُوا إِن كُنتُمْ مُّسْلِمِينَ ﴿١٥٨﴾ فَقَالُوا عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿١٥٩﴾ وَجِئْنَا بِرَحْمَتِكَ مِنَ الْقَوْمِ الْكٰفِرِينَ ﴿١٦٠﴾

“Na Musa alisema: Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu. Wakasema: Tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Ewe Mola wetu Mlezi! Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na hao watu madhalimu. Na Utuokoe kwa Rehema Yako na watu makafiri”. (10:84-86)

إِنَّا أَنْزَلْنَا التَّوْرَةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ تَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا لِلَّذِينَ هَادُوا وَالرَّيْبِيُّونَ وَالْأَحْبَابُ

“Hakika Sisi Tuliteremsha Taurati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii walionyenyekwa Kiislamu, na wachamungu, na wanazuoni, waliwahukumu Mayahudi”. (5:44) na:

وَإِذْ أُوحِيَتْ إِلَى الْحَوَارِيِّينَ أَنْ ءَامِنُوا بِي وَبِرَسُولِي قَالُوا ءَامَنَّا وَأَشْهَدُ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿١١١﴾

“Na Nilipowafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume Wangu, wakasema: Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu”. (5:111)

Hivyo, Allah تعالى Anaeleza kuwa Aliwatuma Mitume Wake wote ili kulingania Dini ya Uislamu, ingawa sharia zao zilitofautiana kulingana na sheria zilizowahusu watu au jamii maalumu. Sheria mpya zilifuta za zamani mpaka ilipokuja sheria ya Muhammad ﷺ iliyoziifuta sheria zote na ambayo haitafutwa milele, wala haitaacha kuwa imara, yenye kunusuriwa na Allah تعالى na bendera zake kunyanyuliwa juu mpaka kusimama kwa Kiama na kwa ajili hii, Mtume ﷺ alisema;

«نَحْنُ مَعَاشِرُ الْأَنْبِيَاءِ أَوْلَادُ عَلَاتٍ دِينًا وَاحِدًا»

“Sisi, Mitume, ni ndugu kwa baba mmoja kwani Dini yetu ni moja”¹.

“Alla-ti” katika lugha ya kiarabu ni ndugu ambao mama zao ni tofauti lakini watokanao na baba mmoja. Kwa hiyo Dini ni moja, ambayo lengo lake ni kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, Asiye na mwenzwa, ijapokuwa sharia za Mitume hazikuwa za aina moja, zilitofautiana na kuwa kama kina mama. Mama mmoja kuwa na watoto wengi, kila mmoja ana baba yake na hawa katika lugha ya kiarabu wanaitwa *Ikhwatul-Akhyaaaf*, ambao ni kinyume na wale wa kwanza. Na kuna *Ikhwatu-A'yaanul-Ashiqqaa*, ni ndugu watokanao na baba mmoja na mama mmoja.

Imamu Ahmad alimnukuu ‘Ali رضي الله عنه kuwa alisema, Mtume ﷺ alikuwa akishapiga Takbira (kusema *Allah Akbar*) wakati anapoanza Sala, alikuwa akisoma dua ya *Istiftah* ina kusema:

«وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ، إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ»

“Nimeuelekeza uso wangu kwa Yule Ambaye Ameumba mbingu na Ardhi, Hanifan, nami si miongoni mwa washirikina. Hakika, Sala yangu na ibada zangu, uhai na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allah, Mola wa ulimwengu wote”.

«اللَّهُمَّ أَنْتَ الْمَلِكُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، أَنْتَ رَبِّي وَأَنَا عَبْدُكَ ظَلَمْتُ نَفْسِي وَاعْتَرَفْتُ بِذَنْبِي فَأَغْفِرْ لِي ذُنُوبِي جَمِيعًا لَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ، وَاهْدِنِي لِأَحْسَنِ الْأَخْلَاقِ لَا يَهْدِي لِأَحْسَنِهَا إِلَّا أَنْتَ، وَاصْرِفْ عَنِّي سَيِّئَهَا لَا يَصْرِفُ عَنِّي سَيِّئَهَا إِلَّا أَنْتَ، بَارَكْتَ وَتَعَالَيْتَ، أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوبُ إِلَيْكَ»

“Ewe Allah! Wewe ni Mfalme, hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe. Wewe ni Mola wangu, nami ni mja Wako. Nimeidhulumu nafsi yangu, na nimekiri madhambi yangu. Nakuomba Unighufirie madhambi yote, kwani hapana anayeghufiria madhambi, bali Wewe. Na Uniongoze katika tabia njema, kwani hakuna aongozaye kwenye wema huo isipokuwa Wewe. Na

¹ Fat’hul Al-Bari 6:550.

Uniondolee uovu wake, kwani hakuna anayeondoa hilo isipokuwa Wewe. Umetakasika na Umetukuka. Nakuomba maghfirah na ninatubu Kwako".¹

Kisha akaitaja Hadithi yote kwa ukamilifu, pamoja na aliyokuwa akiyasema wakati wa *Rukuu, Tahiyatu, Tashahud*. Muslim aliinukuu katika *Sahih*.²

قُلْ أَغْيَرَ اللَّهُ أَبْنِي رَبًّا وَهُوَ رَبُّ كُلِّ شَيْءٍ ۗ وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ إِلَّا عَلَيْهَا ۗ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُم مَّرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿١٦٤﴾

164. Sema: Je nitafute Mola Mlezi asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na hali Yeye Ndiye Mola Mlezi wa kila kitu? Na kila nafsi haichumii ila nafsi yake. Na habebi mwenye kubeba mzigo wa mwenziwe. Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu Mlezi, Naye Atakuambieni mliyokuwa mkikhitalifiana.

Amri ya Kufanya Utegemezi wenye Ikhlasu ndani yake.

Allah تعالیٰ Anasema;

قُلْ

"Sema". Ewe Muhammad ﷺ! Uwaambie wamshirikishao Allah تعالیٰ kuwa wawe katika kumuabudu na pia katika kumtegemea Yeye.

أَغْيَرَ اللَّهُ أَبْنِي رَبًّا

"Je nitafute Mola Mlezi asiyekuwa Mwenyezi Mungu".

Maana: Nimtafute mola asiyekuwa Yeye.

وَهُوَ رَبُّ كُلِّ شَيْءٍ ۗ

"...na hali Yeye Ndiye Mola Mlezi wa kila kitu?" Yeye Ndiye Aliyenilea, Anayenilinda na Anayeniendeshea mambo yangu yote, yaani simtegemei mwingine, bali Yeye tu na sirejei kwingine, ila Kwake Yeye tu, kwa sababu Yeye ni Mola wa kila kitu na Yeye Ndiye Mwenye Kuumba na Ndiye Mwenye Mamlaka ya Kutoa amri. Katika Aya hii kuna amri juu ya ikhlasi katika kumuabudu Yeye Peke Yake, Ambaye Hana mshirika. Maana hizi mbili hutajwa

¹ Ahmad 1:102.

² Muslim 1:534.

kwa pamoja mara nyingi sana katika Qur'an. Kama vile Kauli ya Allah تعالى katika Kuwaelekeza waja Wake waseme Kumuambia Yeye;

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada”.(1:5)

فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ ؕ

“Basi muabudu Yeye na umtegemee Yeye”. (11:123) na;

قُلْ هُوَ الرَّحْمَنُ ءَامَنَّا بِهِ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا

“Sema: Yeye Ndiye Mwingi wa Rehema; tunamuamini Yeye na juu Yake tunamtegemea”. (67:29) na;

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٩﴾

“Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi, hapana mungu isipokuwa Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa wako”. (73:9) Na Aya nyingine nyingi kama hizo.

Kila Mtu Atabeba Mzigo Wake.

Hakuna mtu atakayebeba dhambi za mtu mwingine. Kauli ya Allah تعالى;

وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ إِلَّا عَلَيْهَا ؕ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَى ؕ

“Na kila nafsi haichumii ila nafsi yake. Na habebi mwenye kubeba mzigo wa mwenziwe”. (6:164)

Inajulisha Aya hii kuhusu kitakachotokea katika Siku ya Kiyama kuhusu Malipo, Hukumu na Uadilifu wa Allah تعالى. Kwamba kila nafsi italipwa kulingana na matendo yake, kheri kwa kheri, na shari kwa shari, na hakuna atakayebeba makosa ya nafsi nyingine. Huu ni katika uadilifu wa Allah تعالى. Sawa na Alivyosema Allah تعالى;

وَأِنْ تَدَّعُ مُثْقَلَةٌ إِلَىٰ جَمِيلِهَا لَا يُحْمَلْ مِنْهُ شَيْءٌ وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ

“...na mzigo wake akiomba uchukuliwe hautachukuliwa hata kidogo, na hata angemuomba jamaa yake...”. (35:18)

Kauli ya Allah تعالى;

فَلَا يَخَافُ ظُلْمًا وَلَا هَضْمًا

"...basi hatakhofu kudhulumiwa wala kupunjwa". (20:112) Wanazuoni wa Tafsiri walisema, maana yake ni: Hatadhulumiwa mtu kwa kutakiwa abebe madhambi ya mtu mwingine, wala hatapunjwa mema yake. Pia Alisema;

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ۖ إِلَّا أُولَٰئِ الَّذِينَ هُمْ

"Kila nafsi imo rahanini kwa mabaya iliyoyachuma. Isipokuwa watu wa kuliani". (74:38-39)

Maana: Kila nafsi imewekwa rahanini kwa matendo yake mabaya, isipokuwa watu wa kuliani, kwani baraka za amali zao njema zinaweza kuhamia kwa watoto na ndugu zao. Kama Allah تعالى Alivyosema katika *Surat At-Tur*.

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُم بِإِيمَانٍ أَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَمَا أَلَتْنَاهُمْ مِّنْ عَمَلِهِمْ مِّنْ شَيْءٍ

"Na walioamini na dhuriya wao wakawafuata kwa Imani Tutawakutanisha nao dhuriya wao, na wala hatutawapunja hata kidogo katika vitendo vyao." (52:21)

Maana yake: Tutawakutanisha pamoja na dhuria wao mahali pa juu katika *Jannah*, hata kama hawakuwa wameshirikiana nao kufanya mema, kitakachowasaidia ni kuwa na imani ya aina moja. Wala kwa kufanya hivyo, hatutakuwa Tumewapunguzia malipo ya amali zao waumini hawa, kwa kuwalinganisha na wale wa daraja za chini (katika dhuriya wao) bali Allah تعالى kuwanyanyua mpaka kufikia daraja za baba zao, kwa sababu ya baraka za amali zao kwa Fadhila za Allah تعالى na Neema Zake. Kisha Akasema;

كُلُّ أَمْرٍ إِلَىٰ رَبِّكُمْ ۖ فِيمَا كَسَبْتُمْ

"Kila mtu lazima atapata alichokichuma...". (52:21) Maana yake: Alichokichuma katika maovu. Kauli Yake;

ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ۖ فِيمَا كَسَبْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ

"Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu Mlezi, Naye Atakuambieni mliyokuwa mkikhitalifiana".

Maana: Fanyeni mliyo nayo, sisi tunafanya yale tuliyo nayo. Hakika, sote, sisi

na nyinyi tutakusanywa kwa Allah تعالى na Atatujulisha amali zetu na hukumu juu ya yale tuliyokuwa tukikhitilafiana kwayo duniani, Allah تعالى Anasema;

قُلْ لَا تُسْأَلُونَ عَمَّا أَجْرَمْنَا وَلَا نُسْأَلُ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٥٨﴾ قُلْ يَجْمَعُ بَيْنَنَا رَبُّنَا ثُمَّ يَفْتَحُ بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَهُوَ الْفَتَّاحُ الْعَلِيمُ ﴿١٥٩﴾

“Sema: Nyinyi hamtaulizwa kwa makosa tuliyoyafanya, wala sisi hatutaulizwa kwa mnayoyatenda nyinyi. Sema: Mola wetu Mlezi Atatukusanya, kisha Atatuhukumu kwa haki; na Yeye Ndiye Hakimu Mwenye Kujua”. (34:25-26)

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ خَلْقَ الْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِيَبْلُوكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٦٥﴾

165. Naye Ndiye Aliyekufanyeni Makhalifa wa duniani, na Amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa, ili Akujaribuni kwa hayo Aliyokupeni. Hakika Mola Mlezi wako ni Mwepesi wa Kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

Allah تعالى Amewajaalia Watu Kuwa Makhalifu na Katika Daraja Mbali Mbali Ili Awajaribu.

Allah تعالى Anasema;

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ خَلْقَ الْأَرْضِ

“Naye Ndiye Aliyekufanyeni Makhalifa wa duniani”.

Maana yake: Alikujaalieni muwe wakazi wa humo, muimarisha dunia kizazi baada ya kizazi, karne baada ya karne na dhuriya baada ya kingine. Hayo ni kwa mujibu wa Ibn Zayd na wengine. Sawa na Alivyosema Allah تعالى;

وَلَوْ دَشَاءَ لَجَعَلْنَا مِنْكُمْ مَلَائِكَةً فِي الْأَرْضِ يَخْلُفُونَ ﴿١٦٦﴾

“Na Tungelipenda Tungeliwafanyia miongoni mwenu Malaika katika ardhi wakifuatana”. (43:60)

Na Kauli Yake;

وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ^٥

"...na Akakufanyeni wenye kuendesha dunia." (27:62)

Na Kauli Yake;

إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً^ط

"Mimi nitamuweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi)." (2:30)

Na Kauli Yake;

عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ

"Huenda Mola wenu Mlezi Akamhiliki adui wenu, na Akakufanyieni nyinyi ndio wa kufuatia kushika nchi, ili Atazame mtavyokujatenda nyinyi". (7:129) Kauli ya Allah تعالى;

وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ

"...na Amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa".

Maana yake: Amekutofautisheni katika riziki, tabia, wema, uovu, mandhari, umbo, rangi ya ngozi na kadhalika. Na Yeye Ana Hikima katika hayo. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

نَحْنُ قَسَمْنَا بَيْنَهُمْ مَعِيشَتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا^٤ وَرَفَعْنَا بَعْضَهُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِّيَتَّخِذَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا سَخِرِيًّا^٥

"Sisi Tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na Tukawanyanyua baadhi yao juu ya wengine kwa daraja nyingi; kwa hivyo baadhi yao wanawafanya wengine wawatumikie". (43:32) na;

أَنْظُرَ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ^٤ وَلَلْآخِرَةُ أَكْبَرُ دَرَجَاتٍ وَأَكْبَرُ تَفْضِيلًا^٥

"Angalia vipi Tulivyowafadhili baadhi yao kuliko wengine. Na hakika Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na fadhila kubwa zaidi". (17:21)

Kauli ya Allah تعالى:

لَيَبْلُوكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ

“...ili Akujaribuni kwa hayo Aliyokupeni...”

Maana: Ili Allah تعالى Akujaribuni katika yale Aliyokuneemesheni, na ili Amfanyie mtihani tajiri juu ya utajiri wake na Apate Kumuuliza kuhusu kushukuru kwake, na fakiri naye ajaribiwe juu ya ufakiri wake na apate kuulizwa kunako subira yake. Katika *Sahih* Muslim kuna Hadithi ya Abu Sa'id Al-Khudri kuwa رضي الله عنه alisema Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ الدُّنْيَا حُلُوءٌ خَصِرَةٌ وَإِنَّ اللَّهَ مُسْتَخْلِفُكُمْ فِيهَا فَنَظِيرٌ مَّاذَا تَعْمَلُونَ، فَاتَّقُوا الدُّنْيَا وَاتَّقُوا النِّسَاءَ فَإِنَّ أَوَّلَ فِتْنَةِ بَنِي إِسْرَائِيلَ كَانَتْ فِي النِّسَاءِ»

*“Kwa hakika, dunia ni tamu na ni ya rangi ya chanikiwiti, na Allah Amekufanyieni wakazi katika hiyo dunia, kizazi baada ya kizazi, ili aone mtafanya nini. Basi tahadharini na dunia na muwaogopeni wanawake, kwani mtihani wa kwanza kwa wana wa Israili ulitokana na wanawake”.*¹

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Hakika Mola Mlezi wako ni Mwepesi wa Kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu”.

Aya hii inahofisha na inatia matumaini kuwa Hesabu na Adhabu Yake vinfanyika haraka juu ya waliomuasi na wakawakhalifu Mitume Wake;

وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ

“...na hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu”.

Huruma hiyo ni kwa wale waliomfanya ni mlinzi wao na wakawafuata Mitume Wake kwa yale waliyokuja nayo juu ya khabari na amri walizozifikisha kutoka Kwake. Mara nyingi, Allah تعالى Anazitaja pamoja sifa hizi mbili ndani ya Qur'an. Sawa na Kauli Yake nyingine;

¹ Muslim 4:2098.

وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرٍ لِّلنَّاسِ عَلٰى ظُلْمِهِمْ ۗ وَإِنَّ رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ

“Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye msamaha kwa watu juu ya udhalimu wao. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mkali wa Kuadhibu”. (13:6)

Na Kauli Yake nyingine;

• نَبِّءَ عِبَادِي أَنِّي أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٥٠﴾ وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ

“Waambie waja Wangu ya kwamba Mimi Ndiye Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu. Na kwamba Adhabu Yangu ndio Adhabu iliyo chungu”. (15:49-50)

Na ziko Aya zingine mbalimbali zinazokusanya kwa pamoja, suala la kutia moyo na kuhofisha. Utakuta mara nyingine Huwaita waja Wake Kwake kwa Kuwatia moyo na Kuwaeleza sifa za *Jannah* na Kuwahimiza kuitafuta na mara nyingine Huwahofisha kwa Kuwatajia Moto na adhabu na mateso yake, na Kiyama na vitisho vyake. Wakati mwingine yote mawili Huyataja kwa pamoja ili kila mmoja apate hayo kulingana na sifa zake. Tunamuomba Allah تعالى Atujaalie, tuwe miongoni mwa watiifu kwa yale Aliyoyaamuru, na kuyaacha Aliyoyakataza na Kuyakaripia na Atujaalie ni wenye kuyaamini Aliyoyaeleza. Kwa hakika, Yeye Yu-karibu, ni Mwenye Kujibu dua, Mwenye Kusikia maombi, Mwema, Mkarimu na Mtoaji. Imamu Ahmad alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه ambaye alisema kwamba Mtume ﷺ alisema;

«لَوْ يَعْلَمُ الْمُؤْمِنُ مَا عِنْدَ اللَّهِ مِنَ الْعُقُوبَةِ مَا طَمِعَ بِجَنَّتِهِ أَحَدٌ، وَلَوْ يَعْلَمُ الْكَافِرُ مَا عِنْدَ اللَّهِ مِنَ الرَّحْمَةِ مَا قَنَطَ أَحَدٌ مِنَ الْجَنَّةِ، خَلَقَ اللَّهُ مِائَةَ رَحْمَةٍ فَوَضَعَ وَاحِدَةً بَيْنَ خَلْقِهِ يَتَرَاخَمُونَ بِهَا وَعِنْدَ اللَّهِ تِسْعَةٌ وَتِسْعُونَ»

“Muumini angeliyajua yaliyoko kwa Allah, miongoni mwa Adhabu mbalimbali, hapana ambaye angelikuwa na matumaini na pepo Yake. Na kama kafiri Angelijua yaliyoko kwa Allah, miongoni mwa Rehema, hapana yeyote ambaye Angelikata tamaa juu ya kupata pepo yake. Allah Aliumba Rehema mia moja kati ya hizo Akaiweka moja baina ya viumbe Wake ili waitumie katika kuhurumiana. Zilizobaki kwa Allah ziko tisini na tisa”.

At-Tirmidhi aliinukuu na akasema, ni *Hasan*. Muslim naye aliinukuu¹. Huyo huyo Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema tena kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَمَّا خَلَقَ اللهُ الْخَلْقَ كَتَبَ فِي كِتَابٍ فَهُوَ عِنْدَهُ فَوْقَ الْعَرْشِ إِنَّ رَحْمَتِي تَغْلِبُ
عُصْبِي»

"Allah تعالی Alipowaumba viumbe, Aliandika katika Kitabu ambacho kiko Kwake juu ya Arshi: "Rehema Zangu zinashinda Ghadhabu Zangu".²

Mwisho wa Tafsiri ya Sura ya Al- An'am. Allah تعالی Ndiye Anastahiki Kushukuriwa na Kusifiwa.

* * *

¹ Ahmad 2:334, Tufhat Al-Ahwadhi 9:527 na Muslim 4:2109.

² Muslim 4:2107.

Tafsiri ya Suratul A'raaf

Sura ya 7

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْأَعْرَافِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْمَصَّ ۝ كَتَبْنَا أَنْزِلَ إِلَيْكَ فَلَا يَكُن فِي صَدْرِكَ حَرَجٌ مِّنْهُ لِتُنذِرَ بِهِ وَذِكْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ۝ أَنْتَبِعُوا مَا أَنْزَلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ وَلَا تَتَّبِعُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ۝ وَكَمْ مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا فَجَاءَهَا بَأْسُنَا بَيِّنًا أَوْ هُمْ قَائِلُونَ ۝ فَمَا كَانَ دَعْوَاهُمْ إِذْ جَاءَهُمْ بَأْسُنَا إِلَّا أَن قَالُوا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ۝ فَلَنَسْئَلَنَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْئَلَنَّ الْمُرْسَلِينَ ۝ فَلَنَقْصُصَنَّ عَلَيْهِمْ بِعِلْمٍ ۗ وَمَا كُنَّا غَائِبِينَ ۝ وَالْوَزْنُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ ۗ فَمَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ۝ وَمَن خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَٰئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ بِمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَظْلِمُونَ ۝ وَلَقَدْ مَكَّنَّاكُمْ فِي الْأَرْضِ وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيهَا مَعْيِشًا ۗ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ۝ وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَاكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ لَمْ يَكُن مِّنَ السَّاجِدِينَ ۝

الْمَصَّ ۝ كَتَبْنَا أَنْزِلَ إِلَيْكَ فَلَا يَكُن فِي صَدْرِكَ حَرَجٌ مِّنْهُ لِتُنذِرَ بِهِ وَذِكْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ۝ أَنْتَبِعُوا مَا أَنْزَلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ وَلَا تَتَّبِعُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ۝

“Alif Lam Mym Swaad. Kitabu kilichoteremshwa kwako – basi isiwe dhiki kifuani kwako kwa ajili yake, upate kuonya kwacho, na kiwe ni ukumbusho kwa Waumini. Fuateni mliyo-teremshiwa kutoka kwa Mola wenu, wala msifuate rafiki au walinzi wengine badala Yake. Ni machache mnyakumbuka”. (7:1-3)

Tumeshazieleza herufi (kama hizi – Alif Lam Mim) zilizo mwanzoni mwa baadhi ya Sura katika Qur'an.

كَتَبْنَا أَنْزِلَ إِلَيْكَ

“Kitabu kilichoteremshwa kwako.” Maana: Hiki ni Kitabu kilichoteremshwa kutoka kwa Mola wako.

فَلَا يَكُن فِي صَدْرِكَ حَرَجٌ مِّنْهُ

“...basi isiwe dhiki kifuani kwao kwa ajili yake”. Mujahid, Qatadah na As-Suddi walisema, maana yake, (isiwe dhiki kutokana na) kuwa na shaka nacho¹. Pia ilisemwa, usisite kuitumia Qur’an katika kufikisha ujumbe na kuonya.

فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ أُولُو الْعَزْمِ مِنَ الرُّسُلِ

“Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume wenye stahmala kubwa”.
(46:35)

Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema;

لِتُنذِرَ بِهِ

“...upate kuonya kwacho” Maana yake: Tulikuteremshia ili uwaonye kwacho makafiri.

وَذِكْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ

“...na kiwe ni ukumbusho kwa Waumini” Kisha Allah تعالى Aliuambia ulimwengu.

اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ

“Fuateni mliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wenu”. Maana yake: Fuateni nyayo za Nabii Ummiy ambaye amekujieni na Kitabu kilichoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola na Mmiliki wa kila kitu.

وَلَا تَتَّبِعُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ

“...wala msifuata rafiki au walinzi wengine badala Yake”. Maana: Msiyaache yale aliyokujieni nayo Mtume ﷺ na kuyaenda mengine, mtakuwa mmekengeuka kutoka kwenye hukumu ya Allah تعالى na kuifuata hukumu ya asiye kuwa Yeye.

قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ

“Ni machache mnayokumbuka”. Sawa na Kauli Yake nyingine;

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٧٦﴾

“Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi”. (12:103)

¹ At-Tabari 12:296.

وَأَنْ تَطْعَ أَكْثَرَ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

“Na ukiwatii wengi katika hawa waliomo duniani watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu”. (6:116) Na;

وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ ﴿١٠٦﴾

“Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasi na kuwa ni washirikina”. (12:106)

وَكَمْ مِنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا فَجَاءَهَا بَأْسُنَا بَيِّنًا أَوْ هُمْ قَائِلُونَ ﴿١٠٧﴾ فَمَا كَانَ دَعْوَاهُمْ إِذْ جَاءَهُمْ بَأْسُنَا إِلَّا أَنْ قَالُوا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿١٠٨﴾ فَلَنَسْتَلِزَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْتَلِزَّ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٠٩﴾ فَلَنَقُصَّنَّ عَلَيْهِم بِعِلْمٍ وَمَا كُنَّا غَائِبِينَ ﴿١١٠﴾

4. Na miji mingapi Tuliangamiza, ikafikia Adhabu Yetu usiku au walipokuwa wamelala adhuhuri.

5. Basi hakikuwa kilio chao ilipowafikia Adhabu Yetu, isipokuwa kusema: Hakika sisi tulikuwa wenye kudhulumu.

6. Na kwa yakini Tutawauliza wale waliopelekewa Ujumbe, na pia Tutawauliza hao Wajumbe.

7. Tena Tutawasimulia kwa ilimu, wala Sisi hatukuwa mbali.

Hali za Miji Iliyoangamizwa.

Allah تعالی Anasema;

وَكَمْ مِنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا

“Na miji mingapi Tuliangamiza”. Maana: Kwa kuwakhali Mitume Wetu na kuwakhali. Allah تعالی Akawapa Adhabu ya fedheha duniani yenye kuendelezwa na udhalili wa Akhera. Sawa na Kauli Yake nyingine;

وَلَقَدْ أَسْتَجْرَيْتَ بِرُسُلٍ مِنْ قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿١١٠﴾

“Na hakika Mitume walio kabla yako walifanyiwa kejeli, lakini waliowafanyia kejeli wakaja kuzungukwa na yale yale waliyokuwa wao wanayafanyia kejeli”. (6:10) Na;

فَكَأَيُّ مِّنْ قَرِيْبَةٍ أَهْلَكْنَهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ فَهِيَ حَآوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا وَيَبْرُ مُعْطَلَةٌ وَقَصْرٌ
مَّشِيدٌ ﴿٢٢﴾

“Miji mingapi Tuliangamiza iliyokuwa ikidhulumu, ikawa imebaki magofu, na visima vilivyoachwa, na majumba yaliyokuwa madhubuti?” (22:45) Na;

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَرِيْبَةٍ بَطَرَتْ مَعِيْشَتَهَا ۖ فَتِلْكَ مَسَكِنُهُمْ لَمْ تُسْكَنْ مِنْ بَعْدِهِمْ إِلَّا
قَلِيْلًا ۖ وَكُنَّا خُنَّ الْوَارِثِيْنَ ﴿٢٨﴾

“Na miji mingapi iliyojifakharisha Tumeiangamiza! Na hayo maskani yao hayakukaliwa tena baada yao, ila kwa uchache tu. Na Sisi ndio Tumekuwa warithi wao”. (28:58)

فَجَاءَهَا بِأُسْنَا بَيْنَنَا أَوْ هُمْ قَائِلُونَ

“...ikafikia adhabu Yetu usiku au walipo kuwa wamelala adhuhuri”.

Maana yake: Ikawa amri, adhabu na kisasi cha Allah تعالى kiliwafikia wakiwa wamelala, yaani usiku au wakiwa wamelala kidogo katika wakati wa *Qaylulah*, nako ni kujipumzisha kidogo katikati ya mchana. Nyakati hizo zote mbili ni vipindi vya kujisahau na kujiburudisha.

Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine;

أَفَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَنْ يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا بَيْنَتًا وَهُمْ نَائِمُونَ ﴿٧٧﴾ أَوْ أَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَنْ
يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا ضُحًى وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿٧٨﴾

“Je, watu wa mijini wameaminisha ya kuwa Adhabu Yetu haitawafika usiku, nao wamelala? Au watu wa mijini wameaminisha ya kuwa Adhabu Yetu haitawafika mchana, nao wanacheza?” (7:97-98) Na;

أَفَأَمِنَ الَّذِينَ مَكَرُوا السَّيِّئَاتِ أَنْ يَخْسِفَ اللَّهُ بِهِمُ الْأَرْضَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا
يَشْعُرُونَ ﴿٨٢﴾ أَوْ يَأْخُذُهُمْ فِيْ تَقْلُبِهِمْ فَمَا هُمْ بِمُعْجِزِيْنَ ﴿٨٣﴾ أَوْ يَأْخُذُهُمْ عَلَىٰ تَخَوُّفٍ
فَإِنَّ رَيْبَكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيْمٌ ﴿٨٤﴾

"Je! Wameaminisha wanaofanya vitimbi vya uovu kwamba Mwenyezi Mungu Hatawadidimiza katika ardhi, na haitawafika adhabu kutoka wasipopajua? Au katika nyendo zao, na wala hawataponyoka? Au Hawatashika kwa kitisho na kuwapunguza kidogo kidogo? Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenye Huruma, Mwenye Kurehemu". (16:45-47)

فَمَا كَانَ دَعْوَاهُمْ إِذْ جَاءَهُمْ بِأَسْنَاءِ إِلَّا أَنْ قَالُوا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٤٥﴾

"Basi hakikuwa kilio chao ilipowafikia Adhabu Yetu, isipokuwa kusema: Hakika sisi tulikuwa wenye kudhulumu".

Maana: Haikuwa kauli yao wakati wa kufika kwa adhabu, bali walikiri makosa yao na kwamba walistahili kuadhibiwa. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَكَمْ قَصَمْنَا مِنْ قَوْمٍ كَانَتْ ظَالِمَةً

"Na mingapi katika miji iliyokuwa ikidhulumu Tumeiteketeza". (21:11) Mpaka;

خَمَلَيْنَ

"...wamezimika". (21:15) Kauli ya Allah تعالى;

فَلَنَسْقَلَنَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ

"Na kwa yakini Tutawauliza wale waliopelekewa Ujumbe".

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ مَاذَا أَجَبْتُمُ الْمُرْسَلِينَ ﴿٦٥﴾

"Na siku Atapowaita na Akasema: Mliwajibu nini Mitume?"(28:65) na;

* يَوْمَ تَجْمَعُ اللَّهُ الرُّسُلَ فَيَقُولُ مَاذَا أَجَبْتُمُ قَالَوْا لَا عِلْمَ لَنَا إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّمُ الْغُيُوبِ ﴿١٠٩﴾

"Ile siku ambayo Mwenyezi Mungu Atapowakusanya Mitume Awaambie: Mlijibiwa nini? Watasema: Hatuna ujuzi; hakika Wewe Ndiye Mjuzi Mkubwa wa yote yaliyofichikana". (5:109)

Katika Siku ya Kiyama, Allah تعالى Atauliza umma mbalimbali juu ya walivyowajibu Mitume Wake kuhusu yale waliyowajia nayo kwao, na

Atawauliza Mitume kuhusu kufikisha ujumbe Wake. Kwa ajili hii, 'Ali bin Abu Twalhah alisema kwamba alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما katika kuitafsiri Aya hii;

فَلَنَسْتَعْلَنَ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْتَعْلَبَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٦٥﴾

“Na kwa yakini Tutawauliza wale waliopelekewa Ujumbe, na pia Tutawauliza hao Wajumbe”.

Kuwa alisema, ni kuhusu walichokifikisha¹. Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

فَلَنَقْصِنَّ عَنْهُمْ بَعْلَمٌ وَمَا كُنَّا غَائِبِينَ ﴿٦٦﴾

“Tena Tutawasimulia kwa ilimu, wala Sisi hatukuwa mbali”.

“Kitabu² kitawekwa katika Siku ya Kiyama na kitayasema waliyokuwa wakiyafanya³.”

وَمَا كُنَّا غَائِبِينَ

“...wala Sisi hatukuwa mbali”. Kwamba Allah تعالى Atawaambia waja Wake katika Siku ya Kiyama juu ya waliyoyasema na waliyoyatenda, ama kingi au kidogo, kitukufu au duni, kwa sababu Yeye ni Shahidi wa kila kitu, hakuna chochote kinachoghibu Kwake, wala Haghafiliki na kitu, bali Yeye Ndiye Mjuzi Mkamilifu juu ya hadaa za macho na yanayofichwa na vifua.

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي

كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦٧﴾

“Na halidondoki jani ila Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinachobainisha”.

(6:55-59)

وَالْوَزْنَ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ فَمَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٦٨﴾ وَمَنْ خَفَّتْ

مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ بِمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَظْلِمُونَ ﴿٦٩﴾

8. Na Siku hiyo kipimo kitakuwa kwa Haki. Basi watakaokuwa na uzani mzito, hao ndio watakaofanikiwa.

¹ At-Tabari 12:306.

² Kitabu. Angalia Surat Al-Kahf 18:49.

³ At-Tabari 12:308.

9. Na watakaokuwa na uzani khafifu, basi hao ndio waliozitia khasarani nafsi zao kwa sababu ya kuzipinga Ishara Zetu.

Ubainifu wa Kupimwa Amali.

Allah تعالیٰ Amesema;

وَالْوَزْنُ

“Na kipimo”. Cha kupimia haki katika Siku ya Kiyama.

الْحَقُّ

“Haki”. Maana: Allah تعالیٰ Hatamdhulumu yeyote. Sawa na Kauli Yake katika Aya nyingine.

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَإِنْ كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ
مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا وَكَفَىٰ بِنَا حَاسِبِينَ ﴿٤٧﴾

“Nasi Tukaweka Mizani za uadilifu Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali Tutaiteta. Nasi Tunatosha kuwa washika hisabu”. (21:47)

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ وَإِنْ تَكَ حَسَنَةً يُّضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَّدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٨﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Hadhulumu hata uzito wa chembe moja. Na ikiwa ni jambo jema basi Yeye Hulizidisha na Hutoa kutoka Kwake malipo makubwa”. (4:40)

فَأَمَّا مَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ ﴿١٠١﴾ فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَّاضِيَةٍ ﴿١٠٢﴾ وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ ﴿١٠٣﴾
فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ ﴿١٠٤﴾ وَمَا أَذْرَكَ مَا هِيَ ﴿١٠٥﴾ نَارٌ حَامِيَةٌ ﴿١٠٦﴾

“Basi yule ambaye Mizani yake itakuwa nzito, huyo atakuwa katika maisha ya kupendeza. Na yule ambaye Mizani yake itakuwa khafifu. Huyo maskani yake yatakuwa Moto wa Hawiya! Na nini kitakachokujulisha nini hiyo? Ni Moto mkali!” (101:6-11) Na;

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠٧﴾ فَمَنْ ثَقُلَتْ
مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٨﴾ وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ الَّذِينَ
خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ فِي جَهَنَّمَ خَالِدُونَ ﴿١٠٩﴾

“Basi litapopulizwa baragumu hapo hautakuwepo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana. Ama wale ambao Mizani zao zitakuwa nzito, hao ndio wenye kufanikiwa. Na wale ambao Mizani zao zitakuwa nyepesi, hao ndio waliozitia khasarani nafsi zao, na katika Jahannamu watadumu”. (23:101-103)

Kipambanuzi.

Kuhusu kitakachowekwa katika Mizani katika Siku ya Kiyama, ilisemwa kwamba ni amali ingawa ni katika vitu visivyoshikika, isipokuwa Allah تعالى Atazibadilisha katika Siku ya Kiyama na kuwa umbo. Al-Baghawi alisema, maneno kama haya yalinukuliwa kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما¹. Sawa na ilivyoelezwa katika *Sahih* kwamba sura ya *Al-Baqarah* na *Al’Imran* zitakuja katika Siku ya Kiyama umbile la mawingu mawili au vitu viwili au makundi makundi ya ndege waliojipanga safu (kwa ajili ya kutoa kivuli) pia katika *Sahih* kuna nukuu ya kisa cha Qur’an kuwa itamjia sahibu wake (aliyekuwa akiisoma na kuihifadhi) katika umbile la kijana mwenye muonekano wa uchovu, utauliza “Wewe ni nani?” Atamjibu, “Mimi ni Qur’an iliyokufanya uwe ukikesha usiku wako na kukusababishia kiu nyakati za mchana wako, na katika kauli nyingine, kukusababishia kiu wakati wa mchana”². Katika Hadithi ya Al-Bara juu ya kusailiwa kaburini;

«فَيَأْتِي الْمُؤْمِنَ شَابٌّ حَسَنُ اللَّوْنِ طَيِّبُ الرَّيْحِ فَيَقُولُ: مَنْ أَنْتَ؟ فَيَقُولُ: أَنَا عَمَلُكَ الصَّالِحِ»

*“Kisha Muumini atamjia kijana mwenye rangi nzuri na harufu nzuri. Atamuuliza, “Ni nani wewe?” Atamjibu, “Mimi ni amali yako njema”.*³

Mtume ﷺ alisema kinyume cha hivyo kuhusu Kafiri na Mnafiki.

Pia ilisemwa kuwa Kitabu cha kumbukumbu za Amali kitapimwa, kama ilivyoelezwa katika Hadithi ya *al-Bitwaqa* (Kadi). Kuwa mtu atakuja na Kadi na itawekewa katika upande mmoja wa mizani na upande mwingine yatawekwa madaftari tisini na tisa ya kumbukumbu. Kila Daftari moja la kumbukumbu ni masafa ya upeo wa macho. Kisha italetwa na *al-Bitwaqa* (Kadi) ambayo imeandikwa ‘*Laa ilaaha illallah*’ juu yake. Atasema, “Ewe Mola

¹ Al-Baghawi 2:149.

² Muslim 1:553.

³ Ahmad 4:287.

wangu! Uzito wa Kadi hii haulingani na madaftari haya ya kumbukumbu?" Hapo Allah تعالى Atasema: Hakika wewe hutadhulumiwa. Kadi itawekwa upande wa pili wa Mizani. Mtume ﷺ alisema;

«فَطَاسَتْ السَّجَّلَاتُ وَثَقَلَتِ الْبِطَاقَةُ»

"Angalia! Madaftari (haya tisini na tisa) ya Kumbukumbu yatakuwa hafifu, na Kadi yenye kalima ya Tawhidi itakuwa na uzito mkubwa, amali zitapanda juu kadiri ya uzito wa kadi".¹

At-Tirmidhi alinukuu maneno sawa na haya ya Hadithi hii na akasema ni *Sahih*. Ilisemwa pia, kwamba, atapimwa mwenye amali, kama ilivyoelezwa katika Hadithi;

«يُؤْتَى يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِالرَّجُلِ السَّمِينِ فَلَا يَزِنُ عِنْدَ اللَّهِ جَنَاحَ بَعُوضَةٍ»

"Siku ya Kiyama, mtu mnene ataletwa lakini uzito wake hautazidi hata ule wa ubawa wa mbu". Kisha akasoma;

فَلَا نُقِيمُ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَزْنًا

"...na wala Siku ya Kiyama hatutawathamini kitu". (18:105)²

Pia, katika matukufu ya 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه, Mtume ﷺ alisema;

«أَتَعْجَبُونَ مِنْ دَقَّةِ سَاقِيهِ وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَهُمَا فِي الْمِيزَانِ أَثْقَلُ مِنْ أَحَدٍ»

"Mnastaajabia wembamba wa miundi yake? Naapa kwa Yule Ambaye uhai wangu U-Mkononi Mwake, ni mizito zaidi katika Mizani kuliko (mlima) Uhud".³

Inawezekana kujumuisha maana za Ayah na Hadithi hizi, kwamba zote ni sahihi, kwani wakati mwingine amali ndio zitapimwa, na mara nyingine mahali zilipowekwa amali hizo hati za kumbukumbu, na muda mwingine atapimwa aliyefanya amali hizo. *Allah Aalam*.

وَلَقَدْ مَكَّنَّاكُمْ فِي الْأَرْضِ وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيهَا مَعِيشَةً قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿١٠﴾

10. Na hakika Tumekuwekeni katika ardhi, na Tumekujaalieni humo njia za kupatia maisha. Ni kuchache kushukuru kwenu.

¹ Tuhfatul Al-Ahwadhi 7:395.

² Fat'hul Al-Bari 8:279.

³ Ahmad 1:420.

Neema Zote, Mbinguni na Duniani ni kwa Ajili ya Wanadamu.

Allah تعالى Anakumbusha Neema Zake kwa waja Wake. Miongoni mwazo ni Kuifanya ardhi kuwa makazi, na Akaweka humo milima na mito, Akawajaalia makazi na majumba humo, na Kuwaruhusu kunufaika nayo. Amewadhhalishia mawingu ili wapate kutokea humo riziki zao. Na Akajaalia humo maisha, yaani njia za kujipatia kipato kama vile kibiashara na namna nyingine. Licha ya haya, wengi wao ni wachache wa kushukuru kwa neema hizo. Sawa na Kauli nyingine;

وَأَنْ تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّهِ لَا تَحْصُوهَا إِنَّ الْإِنْسَانَ لَظَلُومٌ كَفَّارٌ

“Na mkhisabu Neema za Mwenyezi Mungu hamuwezi kuzidhibiti. Hakika mwanadamu ni dhalimu mkubwa mwenye kuzikufuru neema”. (14:34)

Wanazuoni wote wa fani ya usomaji Qur'an "Qurraa", isipokuwa 'Abdur-Rahman bin Hurmuz Al-A'raj walikuwa wakilisoma neno *Ma'ayish* (maisha) bila ya *Hamzah*¹. Na *Qiraa* chenye kusibu ni ile ya walio wengi bila ya *Hamzah*.

وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَاكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ لَمْ يَكُن مِّنَ السَّاجِدِينَ ﴿١١﴾

11. Na hakika Tulikuumbeni, kisha Tukakutieni sura, kisha Tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam. Basi wakasujudu isipokuwa Ibilisi, hakuwa miongoni mwa waliosujudu.

Habari ya Malaika Kumsujudia Adam عليه السلام, na Kiburi cha Ibilisi.

Allah تعالى Anamjulisha mwanadamu heshima ya baba yao, Adam عليه السلام na Anabainisha uadui wa adui yao, Ibilisi, na kuendelea kwake na husuda dhidi yao na kwa baba yao, Adam عليه السلام, ili wawe na hadhari naye na wasifuate njia zake. Allah تعالى Alisema;

وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَاكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا

“Na hakika Tulikuumbeni, kisha Tukakutieni sura, kisha Tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam. Basi wakasujudu”.

¹ Herufi ya kiarabu inayohitaji Qarii avute katika usomaji ikiwa yenyewe haina irabu na herufi iliyotangulia ikiwa na Fat-ha.

Sawa na Kauli Yake;

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰئِكَةِ اِنِّيْ خَلَقْتُ بَشَرًا مِّنْ صَلٰصَلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُوْنٍ ﴿٢٨﴾ فَاِذَا سَوَّيْتُهُ
وَنَفَخْتُ فِيْهِ مِنْ رُّوْحِيْ فَقَعُوْا لَهٗ سٰجِدِيْنَ ﴿٢٩﴾

“Na Mola wako Mlezi Alipowaambia Malaika: Hakika Mimi Nitamuumba mtu kwa udongo unaotoa sauti, unaotokana na matope yaliyotiwa sura. Basi Nitakapomkamilisha na Nikampulizia roho Yangu, basi mumuangukie kumsujudia”. (15:28-29)

Kuutukuza Ukuu wa Allah تعالى.

Na hilo ni kuwa, Allah تعالى Alipomuumba Adam عليه السلام kwa Mkono Wake kutokana na udongo mkavu na Akampa sura ya kiumbe kamili, Alimpulizia roho Yake, Aliwaamuru Malaika wamsujudie kwa ajili ya kulitukuza jambo la Allah تعالى. Malaika wote walisikia, walitii na walisujudu, lakini Ibilisi hakuwa miongoni mwa waliosujudu. Tulikwishaeleza mada hii mwanzoni mwa Surat Al-Baqarah. Kwa hivyo, Aya (7:11) inarejea kwa Adam عليه السلام, ingawa Allah تعالى Alitumia neno la wingi hapa, kwa sababu Adam عليه السلام ni baba wa watu wote. Sawa na Anavyosema Allah تعالى kuwaambia wana wa Israil waliokuwepo katika zama za uhai wa Mtume ﷺ.

وَمَا كُنَّا عَلٰىكُمْ بِالْمُهَيَّبِيْنَ ﴿٥٧﴾

“Na Tukakutilieni kivuli kwa mawingu na Tukakuteremshieni Manna na Salwa”. (2:57)

Inakusudia wahenga wao waliokuwepo katika zama za Musa عليه السلام, lakini kwa kuwa hizo ni fadhila walizopewa wazazi wao ambao ndio asili yao, basi ikawa hizo fadhila zinaendelea kwa watoto wao. Hii haihusiani na Kauli ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْاِنْسَانَ مِّنْ سُلٰلٰةٍ مِّنْ طِيْنٍ ﴿٢٣﴾

“Na kwa yakini Tumemuumba mtu kutokana na asili ya udongo”. (23:12)

Kwani kusudio la hapa ni kuwa, Adam عليه السلام aliumbwa kutokana na udongo wa mfinyanzi. Wanawe waliumbwa kutokana na Nutfah (maji yaliyochanganyika ya mume na mke). Hili ni sahihi, kwa sababu lengo la kusema, “Tumemuumba mwanadamu” inazungumzia (asili ya) jinsi, na si kila mmoja. Allahu A’alam.

قَالَ مَا مَنَّكَ إِلَّا تَسْجُدَ إِذْ أَمَرْتُكَ ۗ قَالَ أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ
 خَلَقْتَنِي مِنْ نَارٍ وَخَلَقْتَهُ مِنْ طِينٍ ﴿١٢﴾ قَالَ فَاهْبِطْ مِنْهَا
 فَمَا يَكُونُ لَكَ أَنْ تَتَكَبَّرَ فِيهَا فَاخْرُجْ إِنَّكَ مِنَ الصَّاغِرِينَ
 ﴿١٣﴾ قَالَ أَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٤﴾ قَالَ إِنَّكَ مِنَ
 الْمُنظَرِينَ ﴿١٥﴾ قَالَ فِيمَا أُغْوَيْتَنِي لأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ
 الْمُسْتَقِيمَ ﴿١٦﴾ ثُمَّ لَا يَتَذَكَّرُ مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ
 وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ وَعَنْ شَمَائِلِهِمْ ۗ وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَاكِرِينَ
 ﴿١٧﴾ قَالَ أَخْرَجْ مِنْهَا مَذْءُومًا مَدْخُورًا ۗ لِمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ
 لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنْكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٨﴾ وَيَقَادِمُ اسْتِكْنُ أَنْتَ
 وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ فَكُلَا مِنْ حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَذِهِ
 الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٩﴾ فَوَسْوَسَ لَهُمَا الشَّيْطَانُ
 لِيُبْدِيَ لَهُمَا مَا وُورِيَ عَنْهُمَا مِنْ سَوْءَاتِهِمَا وَقَالَ مَا
 نَهَاكُمَا رَبُّكُمَا عَنْ هَذِهِ الشَّجَرَةِ إِلَّا أَنْ تَكُونَا مَلَكَتَيْنِ أَوْ
 تَكُونَا مِنَ الْخَالِدِينَ ﴿٢٠﴾ وَقَاسَمَهُمَا إِنِّي لَكُمَا لَمِنَ
 النَّاصِحِينَ ﴿٢١﴾

قَالَ مَا مَنَّكَ إِلَّا تَسْجُدَ إِذْ أَمَرْتُكَ ۗ
 قَالَ أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ خَلَقْتَنِي مِنْ نَارٍ
 وَخَلَقْتَهُ مِنْ طِينٍ ﴿١٢﴾

12. Mwenyezi Mungu Akasema: Nini kilichokuzuia kumsujudia Nilipokuamrisha? Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, naye Umemuumba kwa udongo.

Kauli ya Allah تعالیٰ:

مَا مَنَّكَ إِلَّا

“Nini kilichokuzuia kumsujudia”.

Inaweza kukadiriwa kuwa na maana kwamba, ni nini kilichokupa uzito, kilichokuzuia na kilichokupa dharura ya kutokusujudia Nilipokuamrisha, na mfano wa hivyo, kwa mujibu wa Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ.

Kauli hii ni yenye nguvu na Hasan, Allah Aalam.

Na kauli ya Ibilisi – Allah تعالیٰ Amlaani.

أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ

“Mimi ni bora kuliko yeye”. Udhuru huu ni dhambi kubwa kuliko kosa lenyewe, ni kama kwamba alijizuia kuwa mtiifu kwa sababu aliye mbora hawezi kuamrisha amsujudia wa chini yake kwa utukufu. Ibilisi, Allah تعالیٰ Amlaani, anamaanisha, “Mimi ni mbora kuliko yeye, sasa, kivipi Uniamuru kumsujudia?” Halafu Shetani akaeleza kuwa yeye ni mbora zaidi kwa sababu aliumbwa

kutokana na moto, “na moto ni bora kuliko Ulichoniambia, yaani udongo”. Maluuni huyu aliangalia katika asili ya kuumbwa, na si heshima iliyowekwa, nayo ni kwamba, Allah تعالى Alimuumba Adam عليه السلام kwa Mkono Wake na Akampulizia roho Yake. Shetani alifanya Ulinganishi mpotovu katika kukabiliana na Amri ya Allah تعالى:

فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ

“...basi muangukieni kwa kumtii”. (38:72)

Basi, Shetani alitofautiana na Malaika, kwa sababu ya kutokusujudu, akawa *Ablasa*, yaani amekata tamaa ya rehema za Allah تعالى, na akatenda kosa hili, Allah تعالى Amlaani, kwa sababu ya ulinganishi wake usio sahihi. Dai lake kwamba moto ulikuwa bora kuliko udongo, pia lilikuwa kosa, kwani udongo una sifa ya busara, upole, subira na uthibitisho. Udongo ni mahali ambapo mimea huota, inastawi, inakua na kutunzika. Kwa upande wake, moto ni kuteketeza, uharibifu na pupa. Kwa hivyo, asili yake shetani imempelekea kwenye kufeli, wakati asili ya mwanadamu imemnufaisha kwa kumuongoza katika kurejea kwa Allah تعالى kwa toba, unyenyekevu, utiifu na kujisalimisha katika Amri ya Allah تعالى, na kukiri kosa, na kuomba msamaha na toba kwa Allah تعالى. Katika *Sahih Muslim* kuna nukuu kuwa ‘Aisha رضي الله عنها alisema, Mtume ﷺ alisema;

«خُلِقَتِ الْمَلَائِكَةُ مِنْ نُورٍ وَخُلِقَ إِبْلِيسُ مِنْ مَارِجٍ مِنْ نَارٍ وَخُلِقَ آدَمُ مِنْ مِثْمَلٍ وَصِفِّ لَكُمْ»

“Malaika waliumbwa kutokana na nuru, Ibilisi aliumbwa kutokana na mwale wa moto usio na moshi na Adam aliumbwa kwa kile mlichoelezwa”.¹

Ibilisi Alikuwa wa Kwanza Kutumia Qiyas (Ulinganishi)

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu maoni ya Al-Hasan kuhusu kauli ya shetani.

خَلَقْتَنِي مِنْ نَّارٍ وَخَلَقْتَهُمْ مِنْ طِينٍ

“Umeniumba kwa moto, naye Umemuumba kwa udongo”.

Kwamba, “Ibilisi alitumia *Qiyas*, na yeye ndiye aliyekuwa wa kwanza kufanya

¹ Muslim 4:2294.

hivyo¹. Isnadi yake ni sahihi. Pia ipo nukuu ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى kwamba Ibn Sirin رحمه الله تعالى alisema; “Wa kwanza kufanya Qiyas ni Ibilisi, hata jua na mwezi havikuabudiwa isipokuwa kutokana na Qiyas.”². Hii pia ina isnadi sahihi.

قَالَ فَأَهِيْطْ مِنْهَا فَمَا يَكُوْنُ لَكَ أَنْ تَتَكَبَّرَ فِيهَا فَاخْرُجْ إِنَّكَ مِنَ الصَّاغِرِيْنَ ﴿٣٦﴾ قَالَ
 أَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُوْنَ ﴿٣٧﴾ قَالَ إِنَّكَ مِنَ الْمُنظَرِيْنَ ﴿٣٨﴾

13. Akasema: Basi teremka kutoka humo! Haikufalii kufanya kiburi humo. Basi toka! Hakika wewe ni miongoni mwa walio duni.

14. Akasema: Nipe muhula mpaka siku watakapofufuliwa.

15. Akasema: Utakuwa miongoni mwa waliopewa muhula”.

Allah تعالى Alimuamuru Ibilisi,

فَأَهِيْطْ مِنْهَا

“Basi teremka kutoka humo!” Maana yake: Kwa sababu ya kuiasi amri Yangu na kujitoa kwako katika kunitii, haustahiki kuwa na kiburi ndani yake, wanazuoni wengi wa tafsiri wamesema: makusudio yake ni *Jannah* inawezekana ikawa inarejea katika daraja ambayo aliyokuwa nayo katika hadhi za juu.

فَاخْرُجْ إِنَّكَ مِنَ الصَّاغِرِيْنَ

“Basi toka! Hakika wewe ni miongoni mwa walio duni”.

Maana yake: Katika madhalili, walio hakiri, kwa kumvunjia malengo yake na kumpatia anayoyahitaji kwa kinyume chake (kiburi). Wakati huo ndio akapata laana na akaomba kupewa muda mpaka Siku ya Hukumu.

فَأَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُوْنَ ﴿٣٧﴾ قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ الْمُنظَرِيْنَ ﴿٣٨﴾

“Akasema (Ibilisi): Mola wangu Mlezi! Nipe muhula mpaka siku watapofufuliwa. (Mwenyezi Mungu) Akasema: Hakika wewe ni katika waliopewa muhula”. (15:36-37)

Allah تعالى Alimpa Shetani aliyoyaomba, kutokana na Hekima Yake, Uamuzi na Utashi Wake ambao hakuna wa kuupinga au kuuzuia. Kwa hakika, hakuna wa kuzuia Uamuzi Wake na Yeye ni Mwepesi wa Kuhesabu.

¹ At-Tabari 12:328.

² At-Tabari 12:328.

قَالَ فِيمَا أُغْوَيْتَنِي لأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١٦﴾ ثُمَّ لَآئِيَنَّهُمْ مِن بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَنِهِمْ وَعَنْ شَمَائِلِهِمْ وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَاكِرِينَ ﴿١٧﴾

16. Akasema: Kwa kuwa umenihukumia upotofu, basi nitawavizia katika njia Yako iliyonyooka.

17. Kisha nitawazukia mbele yao na nyuma yao na kuliani kwao na kushotoni kwao. Wala hutawakuta wengi wao wenye shukrani”.

Allah تعالى Anasema kuwa baada ya kumpa muhula Ibilisi.

إِلَى يَوْمٍ يُبْعَثُونَ

“...mpaka siku watapofufuliwa.” Na ibilisi akathibitikiwa na hilo, alikipata alichokitaka, akaendelea kufanya ufidhuli zaidi, alisema;

فِيمَا أُغْوَيْتَنِي لأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ

“Kwa kuwa Umenihukumia upotofu, basi nitawavizia katika njia Yako iliyonyooka”.

Maana: Kama Umenihukumu upotofu. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, ina maana, “Umenipotosha”.¹ Wengine walisema, “Kama Ulivyoniangamiza, nitaketi kuwangojea waja Wako Unaowaumba kutokana na dhuriya ya huyu ambaye Umenibadilisha kwa sababu yake”. Akaendelea;

صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ

“Njia Yako iliyonyooka”. Maana: Njia ya haki na uokovu. Nitawapoteza na njia hiyo ili wasikuabudu wala wasikupwekeshe kutokana na kunipoteza kwako.

Mujahid alisema kuhusu, “Njia Yako iliyonyooka”. Maana yake, haki.

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alimnukuu Sabirah bin Abu Al-Fakih رضي الله عنه akisema, Nimemsikia Mtume ﷺ akisema;

«إِنَّ الشَّيْطَانَ قَعَدَ لِابْنِ آدَمَ بِطَرَفَيْهِ، فَقَعَدَ لَهُ بِطَرَفِي الْإِسْلَامِ، فَقَالَ: أُنْسِلِمُ وَتَدْرُ دِينَكَ وَدِينَ آبَائِكَ؟ قَالَ: فَعَصَاهُ وَأَسْلَمَهُ قَالَ: «قَعَدَ لَهُ بِطَرَفِي الْهِجْرَةِ فَقَالَ:

¹ At-Tabari 12:332.

أَتَهَاجِرُ وَتَدَعُ أَرْضَكَ وَسَمَاءَكَ؟ وَإِنَّمَا مَثَلُ الْمُهَاجِرِ كَالْفَرَسِ فِي الطَّوْلِ، فَعَصَاهُ وَهَاجِرَ، ثُمَّ قَعَدَ لَهُ بِطَرِيْقِ الْجِهَادِ وَهُوَ جِهَادُ النَّفْسِ وَالْمَالِ، فَقَالَ: تَقَابِلُ تَقْتُلُ فَتَنْكِحُ الْمَرْأَةَ وَيُقَسِّمُ الْمَالَ، قَالَ: فَعَصَاهُ وَجَاهِدَ، وَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «فَمَنْ قَعَلَ ذَلِكَ مِنْهُمْ فَمَاتَ، كَانَ حَقًّا عَلَى اللَّهِ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ، وَإِنْ قُتِلَ كَانَ حَقًّا عَلَى اللَّهِ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ، وَإِنْ غَرِقَ كَانَ حَقًّا عَلَى اللَّهِ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ أَوْ وَقَصَّتُهُ دَابَّةٌ كَانَ حَقًّا عَلَى اللَّهِ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ»

*“Shetani aliketi kumngojea mwanadamu katika njia zake zote. Alikaa katika njia ya Uislamu, akisema, “Unasilimu na kuiacha dini yako na ya baba zako?” Lakini mwanadamu alimuasi Shetani na akasilimu. Shetani akamngojea katika njia ya Hijrah (kuhama katika njia ya Allah), na akasema, “Unahama na kuiacha ardhi na anga yako”. Lakini mfano wa anayefanya Hijra ni wa farasi aliye katika ushupavu. Akamuasi na akahama. Kisha akamngojea katika njia ya Jihadi ya nafsi na mali. Akasema, “Ukipigana, unaweza kuuwawa, kisha mkeo kuolewa na mtu mwingine na mali yako kugawanywa”. Akamuasi na akafanya Jihadi”. Mtume ﷺ akaendelea kusema; “Mwenye kufanya haya na akafa, haki juu ya Allah Amuingize Jannah na akiuwawa, pia atakuwa na haki juu ya Allah Amuingize Janna, akizama katika maji, atakuwa na haki juu ya Allah Amuingize Janna na hata kama kifo chake ni kutokana na kuangushwa na mnyama, basi atakuwa na haki juu ya Allah Amuingize Janna”.*¹

‘Ali bin Abu Twalhah alitaarifu kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema juu ya,

ثُمَّ لَا تَيَسَّرُ لَهُمْ مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ

“Kisha nitawazukia mbele yao” Ina maana: Kuwatia shaka juu ya Akhera yao

وَمِنْ خَلْفِهِمْ

“...na nyuma yao” Kuwafanya waipende sana dunia.

وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ

“...na kuliani kwao”. Ninawashabihisha jambo la dini yao.

¹ Ahmad 3:483.

وَعَنْ سَمَائِلِهِمْ^ط

“...na kushotoni kwao”.¹ Ninawatamanisha kutenda madhambi. Kusudio ni njia zote za kheri na shari, anawazuia kufanya kheri na anawavutia kufanya shari. Al-Hakim bin Abban alisema kuwa ‘Ikrimah alisema kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu;

ثُمَّ لَا تَتَّبِعُهُمْ مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَنِهِمْ وَعَنْ شَمَائِلِهِمْ^ط

“Kisha nitawazukia mbele yao na nyuma yao na kuliani kwao na kushotoni kwao”.

Wala hakusema kutokea juu yao kwa sababu rehema huteremka kutokea juu.² ‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema;

وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَاكِرِينَ

“Wala hutawakuta wengi wao wenye shukrani”.

Maana: “Wanaompwekesha Yeye tu (katika ibada)”.³ Kauli hii ya Ibilisi, “huyu” ni dhana na makisio yake na limeafiki mahali hapa. Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

وَلَقَدْ صَدَقَ عَلَيْهِمْ إِبْلِيسُ ظَنَّهُ فَاتَّبَعُوهُ إِلَّا فَرِيقًا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٠﴾ وَمَا كَانَ لَهُ
عَلَيْهِمْ مِنْ سُلْطَانٍ إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يُؤْمِنُ بِالْآخِرَةِ مِمَّنْ هُوَ مِنْهَا فِي شَاكٍ ۗ وَرَبُّكَ عَلَىٰ كُلِّ
شَيْءٍ حَفِيظٌ ﴿٢١﴾

“Na bila ya Shaka Ibilisi alihakikisha ile dhana yake juu yao. Nao walimfuata, isipo kuwa kundi la Waumini. Na yeye hakuwa na mamlaka yoyote juu yao, ila kwa sababu ya kuwajaribu tujue nani mwenye kuamini Akhera, na nani anayetilia shaka. Na Mola wako Mlezi ni Mwenye Kuhifadhi kila kitu”. (34:20:21)

Kwa Minajili hiyo, kuna Hadithi inayohimiza kuomba kinga ya Allah تعالى dhidi ya hadaa za shetani kwa mwanadamu kutokea pande zote. Imamu Ahmad amesema kuwa ‘Abdullah bin Umar رضي الله عنهما alisema, “Mtume ﷺ hakuacha kusoma dua ifuatayo wakati wa asubuhi na jioni,

¹ At-Tabari 12:338.

² At-Tabari 12:341.

³ At-Tabari 12:342.

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَافِيَةَ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَمَرَ وَالْعَافِيَةَ فِي دِينِي وَدُنْيَايَ وَأَهْلِي وَمَالِي، اللَّهُمَّ اسْتُرْ عَوْرَاتِي وَآمِنْ رَوْعَاتِي، اللَّهُمَّ احْفَظْنِي مِنْ بَيْنِ يَدَيْ وَمِنْ خَلْفِي وَعَنْ يَمِينِي وَعَنْ شِمَالِي وَمِنْ فَوْقِي وَأَعُوذُ بِعَظَمَتِكَ أَنْ أُغْتَالَ مِنْ تَحْتِي»

“Ewe Allah! Mimi Nakuomba afya duniani na Akhera. Ewe Allah! Nakuomba msamaha na afya katika Dini, Ahli na Mali yangu. Ewe Allah! Nisitiri makosa yangu Uniondoshee yanayonitia hofu. Ewe Allah! Nilinde kwa mbele yangu, nyuma yangu, kuumeni kwangu, kushotoni kwangu na juu yangu. Na ninajikinga kwa Utukufu Wako dhidi ya kuweza kuuwawa kutokea chini yangu”.

Waki' alisema: kutoka chini, maana yake ni “tetemeko”¹. Na Abu Dawud, An-Nasai, Ibn Majah, Ibn Hibban na Al-Hakim nao waliinukuu Hadithi hii². Al-Hakim alisema: Isnadi yake ni *Sahih*.

قَالَ أَخْرَجَ مِنْهَا مَذْمُومًا مَدْحُورًا لَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ لِأَمْلَانِ جَهَنَّمَ مِنْكُمْ أَجْمَعِينَ

18. Akasema: Toka humo, nawe umekwisha fedheheshwa, umekwishafukuzwa. Hapana shaka atakayekufuata miongoni mwao, basi Nitaijaza Jahannam kwa nyinyi nyote.

Allah تعالى Alisisitiza laana Yake, Kumfukuza, Kumbaidisha na Kumtoa kutoka katika vilele vya juu zaidi, kwa Kauli Yake;

أَخْرَجَ مِنْهَا مَذْمُومًا مَدْحُورًا

“Toka humo, nawe umekwisha fedheheshwa, umekwishafukuzwa”.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema, “*Madh-um ni aliyefedheheshwa*”. Na maana ya “*Mad-huur* ni aliyetupwa mbali, aliyebaidishwa kwa kufukuzwa”³. Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema: “*Madh-um na Madhmum* ni kitu kimoja”⁴. Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisema kuwa Abu Is-haq alisema At-Tamimi alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما juu ya;

¹ Ahmad 2:25.

² Abu Dawud 5:315, An-Nasai 8:282, Ibn Majah 2:1273, Ibn Hibban 2:155 na Al-Hakim 1:517.

³ At-Tabari 12:342.

⁴ At-Tabari 12:344.

أَخْرَجَ مِنْهَا مَذءُومًا مَّدْحُورًا^ط

“Akasema: Toka humo, nawe umekwishafedheheshwa, umekwishafukuzwa”.

Kuwa ni “Aliyekasirikiwa”¹ ‘Ali bin Abu Twalhah alitaarifu kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Duni na wa kukasirikiwa”.² As-Suddi alisema, “Wa kukasirikiwa na kufukuzwa”.³ Qatadah alisema, “Mlaaniwa, wa kukasirikiwa”.⁴ Mujahid alisema, “Mwenye kufukuzwa na kufurushwa”.⁵ Ar-Rabi’ bin Anas alisema, “Madh’um ni aliyefurushwa, na madh-hur ni aliyefanywa duni”⁶. Kauli ya Allah تعالى:

لَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنْكُمْ أَجْمَعِينَ

“Hapana shaka atakayekufuata miongoni mwao, basi Nitaijaza Jahannam kwa nyinyi nyote”.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

قَالَ أَذْهَبَ فَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ فَإِنَّ جَهَنَّمَ جَزَأُؤُكُم جَزَاءً مَوْفُورًا ﴿٦٥﴾ وَأَسْتَفْزِرُ مِنْ
 أَسْطَظَعَتْ مِنْهُمْ بِصَوْتِكَ وَأَجْلَبَ عَلَيْهِمْ خَيْلِكَ وَرَجَلِكَ وَشَارِكْتَهُمْ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ
 وَعِدَّتُهُمْ^ع وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٦٦﴾ إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ
 وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ وَكِيلًا ﴿٦٧﴾

“Atasema Mwenyezi Mungu: Ondokelea mbali! Atakayekufuata katika wao, basi Jahannamu itakuwa ndiyo malipo yenu, malipo ya kutimia. Na wachochee uwawezao katika wao kwa sauti yako, na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na waendao kwa miguu. Na shirikiana nao katika mali na wana, na waahidi. Na shetani hawapi ahadi ila ya udanganyifu. Hakika wewe huna mamlaka juu ya waja Wangu. Na Mola wako Mlezi Anatosha kuwa ni wa kutegemewa”. (17:63-65)

¹ At-Tabari 12:344.

² At-Tabari 12:343.

³ At-Tabari 12:343.

⁴ At-Tabari 12:343.

⁵ At-Tabari 12:343.

⁶ At-Tabari 12:344.

وَيَقَادِمُ أَسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ فَكُلَا مِنْ حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَذِهِ
 الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٩﴾ فَوَسَّوَسَ هُمَا الشَّيْطَانُ لِيُبْدِيَ لَهُمَا مَا وُورِيَ
 عَنْهُمَا مِنْ سَوْءَاتِهِمَا وَقَالَ مَا نَهَاكُمَا رَبُّكُمَا عَنْ هَذِهِ الشَّجَرَةِ إِلَّا أَنْ تَكُونَا
 مَلَكَتَيْنِ أَوْ تَكُونَا مِنَ الْخَالِدِينَ ﴿٢٠﴾ وَقَاسَمَهُمَا إِنِّي لَكُمَا لَمِنَ النَّاصِحِينَ ﴿٢١﴾

“Na wewe, Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani hii, na kuleni humo mpendapo. Wala msiukaribie mti huu, mkawa katika wale waliodhulumu. Basi Shetani aliwatia wasiwasi ili kuwafichulia tupu zao walizofichiwa, na akasema: Mola Mlezi wenu hakukukatazeni mti huu ila msije mkawa Malaika, au msije mkawa katika wanaoishi milele. Naye akawaapia: Kwa yakini mimi ni miongoni wa wanaokunasihini”. (7:19-21)

Ulaghai wa kwa Adam عليه السلام na Hawwa na Kula kwa Matunda ya Mti

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye Aliwahalalishia Adam عليه السلام na mkewe Hawa matunda yote ya *Jannah*. Maelezo ya jambo hili yalikuwisha tangulia katika *Surat Al-Baqarah*. Kwa sababu hiyo, shetani Aliwafanyia husuda na akajiingiza katika kufanya hila, wasiwasi na hadaa, ili awanyang'anye baadhi ya neema na libasi nzuri.

وَقَالَ

“...na akasema”. Kwa uongo na uzushi.

مَا نَهَاكُمَا رَبُّكُمَا عَنْ هَذِهِ الشَّجَرَةِ إِلَّا أَنْ تَكُونَا مَلَكَتَيْنِ

“Mola Mlezi wenu hakukukatazeni mti huu ila msije mkawa Malaika”.

Maana: Ili nyote wawili msiwe malaika au msikae milele humuhumu, kama mtakula katika huo, mtayapata hayo yote mawili.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

قَالَ يَتَقَادِمُ هَلْ أَدُلُّكَ عَلَى شَجَرَةِ الْخُلْدِ وَمُلْكٍ لَّا يَبُوتُ

“...akamuambia: Ewe Adam! Nikujulishe mti wa kuishi milele na Ufalme usiokoma?” (20:120) Na;

يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ أَنْ تَضِلُّوا

“Mwenyezi Mungu Anakubainishieni ili msipotee”. (4:176)

Maana yake: Ili msipotee.

وَأَلْقَى فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ أَنْ تَمِيدَ بِكُمْ

**“Na Kaweka katika ardhi milima ili ardhi isiyumbe yumbe nanyi”.
(16:15)**

Maana: Ili isiyumbe nanyi.

وَقَاسَمَهُمَا

“Naye akawaapia”.

Maana yake: Aliwaapia kwa Jina la Allah تعالى.

إِنِّي لَكُمْ لَمِنَ النَّاصِحِينَ

“Kwa yakini mimi ni miongoni wa wanaokunasihini”.

Kwamba mimi ni wa tangu kabla yenu na ninapajua mahala hapa. Aliwaapia kwa Jina la Allah تعالى na akawahadaa. Anayemuamini Allah تعالى anaweza mara nyingine kuhadaiwa. Qatadah alieleza Aya hiyo, “Shetani aliapa kuwa, “Mimi niliumbwa kabla yenu, na nina ujuzi kuliko nyinyi, basi nifuateni ili nikuongozeni”.

* * *

فَدَلَّيْهُمَا بِغُرُورٍ ۖ فَلَمَّا ذَاقَا الشَّجَرَةَ بَدَتْ لَهُمَا سَوْءَ بَيْتِهِمَا
 وَطَفِقَا يَخْصِفَانِ عَلَيْهِمَا مِنْ وَرَقِ الْجَنَّةِ ۗ وَنَادَيْتُهُمَا رُحْمًا
 أَلَمْ أَنْهَكُمَا عَنْ تِلْكَمَا الشَّجَرَةِ وَأَقُلْ لَكُمَا إِنَّ الشَّيْطَانَ
 لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٢٢﴾ قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِن لَّمْ
 تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٢٣﴾ قَالَ
 أَهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۗ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقَرٌّ
 وَمَتَعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٢٤﴾ قَالَ فِيهَا تَحْيَوْنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنْهَا
 تُخْرَجُونَ ﴿٢٥﴾ يَبْنَئِي آدَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ لِبَاسًا يُورِي
 سَوْءَ اتِّكُمٍ وَرِدْشًا ۗ وَلِبَاسُ التَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ۗ ذَٰلِكَ مِنْ
 آيَاتِ اللَّهِ لَعَلَّكُمْ يَذَكَّرُونَ ﴿٢٦﴾ يَبْنَئِي آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمْ
 الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ مِنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا
 لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْءَ بَيْتِهِمَا ۗ إِنَّهُ يَرِيكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ
 حَيْثُ لَا تَرَوْتَهُمْ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيْطَانَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا
 يُؤْمِنُونَ ﴿٢٧﴾ وَإِذَا فَعَلُوا فَحِشَةً قَالُوا وَجَدْنَا عَلَيْهَا
 آبَاءَنَا وَاللَّهُ أَمَرَنَا بِهَا ۗ قُلْ إِنَّا لَأَنبِيَاءُ اللَّهِ لَا يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ ۗ
 أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾ قُلْ أَمَرَ رَبِّي
 بِالْقِسْطِ ۗ وَأَقِيمُوا وُجُوهَكُمْ عِندَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَادْعُوهُ
 مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ ۗ كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ ﴿٢٩﴾ فَرِيقًا
 هَدَىٰ وَفَرِيقًا حَقَّ عَلَيْهِمُ الضَّلَالَةُ ۗ إِنَّهُمْ اتَّخَذُوا الشَّيْطَانَ
 أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُم مُّهْتَدُونَ ﴿٣٠﴾

فَدَلَّيْهُمَا بِغُرُورٍ ۖ فَلَمَّا ذَاقَا الشَّجَرَةَ
 بَدَتْ لَهُمَا سَوْءَ بَيْتِهِمَا وَطَفِقَا
 يَخْصِفَانِ عَلَيْهِمَا مِنْ وَرَقِ الْجَنَّةِ ۗ
 وَنَادَيْتُهُمَا رُحْمًا أَلَمْ أَنْهَكُمَا عَنْ
 تِلْكَمَا الشَّجَرَةِ وَأَقُلْ لَكُمَا إِنَّ
 الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٢٢﴾
 قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِن لَّمْ
 تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ
 الْخَاسِرِينَ ﴿٢٣﴾

22. Basi akawateka kwa khadaa. Walipouonja ule mti, tupu zao zilifichuka na wakaingia kujibandika majani ya bustanini. Mola wao Mlezi Akawaita: Je, sikukukatazeni mti huo, na Kukuambieni ya kwamba Shetani ni adui yenu wa dhahiri?

23. Wakasema: Mola wetu Mlezi! Tumejidhulumu nafsi zetu, na kama Hutusamehe na Kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kukhasirika".

رضي الله عنه Ubayy bin Ka'b عليه السلام alisema, "Adam

alikuwa mtu mrefu kama vile mtende mrefu, Mwenye nywele nyingi kichwani. Alitumbukia katika kosa alilolifanya, uchi wake ulimdhirikia ilhali alikuwa hauoni kabla ya hapo. Akaanza kukimbia katika *Jannah*, lakini mti mmoja huko ukamzuia kichwa chake, akauambia, "Niachilie". Mti ukasema, "Mimi sikuachilii". Mola wake Akamuita, "Ewe Adam! Unanikimbia Mimi?" Akasema, "Mola wangu! Mimi nakuonea aibu"¹.

Ibn Jarir na Ibn Mardawayhi walikusanya kupitia isnadi nyingi, kutoka kwa Al-Hasan kutoka kwa Ubayy bin Ka'b رضى الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ².

Lakini kuihusisha Hadith na Ubayy رضى الله عنه ndiyo isnadi sahihi zaidi. Ibn 'Abbas رضى الله عنهما aliizungumzia Aya;

وَطَفِقًا مَخْصِفَانِ عَلَيْهِمَا مِنْ وَرَقِ الْجَنَّةِ^ط

"...na wakaingia kujibandika majani ya bustanini".

Kwa kusema, "Ni majani ya mtini"³. Hadithi ni sahihi kwa isnadi zinazopitia kwa Ibn 'Abbas رضى الله عنها. Mujahid alisema; "walianza kujisitiri kwa majani ya *Jannah*, kwa kuyafanya kama nguo"⁴. Wahb bin Munabbih alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى;

يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا

"...akawavua nguo zao". (7:27)

Alisema, Adam عليه السلام na Hawwa walikuwa na vazi la nuru katika sehemu za siri, ikawa hawaonani tupu zao, lakini walipokula katika mti huo, uchi wa kila mmoja wao ulidhikirika. Aliinukuu Ibn Jarir رحمه الله تعالى kwa isnadi *Sahih*⁵. 'Abdur-Razzaq alimnukuu Qatadah kuwa alisema, "Adam عليه السلام alisema: "Ewe Mola wangu! Je, kama nikitubu na kufanya *istighfar*?" Akasema, "Basi Nitakuingiza *Jannah*". Ibilisi hakufanya toba kwa Allah تعالى, bali alimuomba kuakhirishwa, basi Allah تعالى Akampatia kila mmoja lile aliloliomba."¹.

Adh-Dhahhak bin Muzahim alisema, juu ya Kauli ya Allah تعالى;

¹ At-Tabari 12:354.

² At-Tabari 12:352.

³ At-Tabari 12:354.

⁴ At-Tabari 12:353.

⁵ At-Tabari 12:355.

رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ

“Mola wetu Mlezi! Tumejidhulumu nafsi zetu, na kama Hutusamehe na Kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kukhasirika”.

Haya ni maneno ambayo Adam عليه السلام aliyapokea kutoka kwa Mola wake”.²

قَالَ أَهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَمَتْنَعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٢٤﴾ قَالَ
فِيهَا نَحْيُونَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنْهَا نُخْرِجُونَ ﴿٢٥﴾

24. Akasema: Teremkeni! Mtakuwa nyinyi kwa nyinyi maadui. Na kwenye ardhi itakuwa ndio makao yenu na starehe yenu mpaka ufike muda.

25. Akasema: Humo mtaishi, na humo mtakuja, na kutoka humo mtatolewa”.

Kuteremshwa Duniani Wote Watatu.

Ilisemwa: walipoambiwa;

أَهْبِطُوا

“Teremkeni!”

Ni Adam عليه السلام, Hawa, Ibilisi na nyoka. Baadhi ya wanazuoni hawamtaji nyoka, Allah Aalam. Uadui kimsingi ni baina ya Adam عليه السلام na Ibilisi. Minajili hii, Allah تعالى Alisema katika Surat Twaha,

أَهْبِطًا مِنْهَا جَمِيعًا

“Ondokeni humu nyote”. (20:123)

Na Hawa anamfuatia Adam عليه السلام, wakati nyoka, ikiwa kutajwa kwake ni sahihi anamfuatia Ibilisi. Wafasiri wameyataja maeneo waliyoteremkia kila mmoja, lakini maelezo hayo yamechukuliwa kutoka kwenye visa vya Waisrail,

¹ Abdur-Razzaq 2:226. Angalia Surat Al-Baqarah 2:37.

² At-Tabari 12:357.

Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi juu ya usahihi wake. Kama ingelikuwepo faida kwa watu kidini na dunia katika kuyajua maeneo hayo, Allah تعالى Angeliyataja katika Kitabu Chake, na Mjumbe Wake angeliyataja pia.

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَكُم فِي الْأَرْضِ مَسْتَقَرٌّ وَمَتْنَعٌ إِلَىٰ حِينٍ

“Na kwenye ardhi itakuwa ndio makao yenu”.

Maana yake: Mtakaa duniani kwa wakati uliopangwa mpaka muda maalumu utakapofikia. Kalamu imekwishaandika, Kudura Imethibiti na imeandikwa katika Kumbukumbu za Awali.

Kauli ya Allah تعالى:

قَالَ فِيهَا تَحْيَوْنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنْهَا تُخْرَجُونَ ﴿٢٥﴾

“Akasema: Humo mtaishi, na humo mtakufa, na kutoka humo mtatolewa”.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ ﴿٢٦﴾

“Kutokana nayo (ardhi) Tumekuumbeni na humo Tunakurudisheni, na kutoka humo Tutakutoeni mara nyingine”. (20:55)

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye Alijaalia ardhi kuwa ni nyumba ya mwanadamu katika muda wote wa maisha ya kidunia. Humo ndio penye uhai wao, vifo, makaburi, na kufufuliwa kwao kwa ajili ya Siku ya Kiyama, siku hiyo Allah تعالى Atawakusanya wa mwanzo na wa mwisho na Kuwalipa.

يَنبِئُ آدَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُورِي سَوَاءَ تَكْمٌ وَرِدْشًا ۗ وَلِبَاسُ التَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ
ذَٰلِكَ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿٢٧﴾

26. Enyi wanadamu! Tumekuteremshieni nguo za kuficha tupu zenu, na nguo za pambo. Na nguo za uchaMungu ndio bora. Hayo ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu mpate kukumbuka.

Kuteremshwa Libasi na Pambo kwa Wanadamu.

Allah تعالى Anawakumbusha waja Wake juu ya *Libasi* (nguo za kujisitiri) na *Rish* (nguo zinazovaliwa kama mapambo). Vazi lililotajwa hapa ni la kusitiri uchi ilhali *rish* ni vazi la mtu kujipendezesha na huvalishwa kwa nje. *Libasi* ni vazi lenye umuhimu mkubwa, na *Rish* ni la ziada. Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, "Katika lugha ya kiarabu, *Rish* ni samani na nguo za juu."¹ 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema kuwa;

وَلِبَاسُ التَّقْوَىٰ

"Na nguo za uchaMungu".

Kwa sababu ya kumchamungu, na mtu anasitiri uchi wake, basi hilo ndio *Libasut* – *Taqwa* (vazi la uchaMungu).²

يَنْبَغِي ءَادَمَ لَا يَفْتَنَنَّكُمْ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ مِنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْءَٰتِهِمَا ۗ إِنَّهُ يُرِيدُكُمُ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٧﴾

27. Enyi wanadamu! Asije shetani kukufitinini kama alivyowatoa wazazi wenu Peponi, akawavua nguo zao kuwaonesha tupu zao. Hakika yeye na kabila yake wanakuoneni, na nyinyi hamuwaoni. Hakika Sisi Tumewafanya Mashetani kuwa ni marafiki wa wasioamini.

Tahadhari Dhidi ya Fitina za Shetani.

Allah تعالى Anamtahadharisha mwanadamu dhidi ya Ibilisi na kabila lake (wafuasi wake), kwa kubainisha uadui wake wa zamani kwa baba wa wanadamu, Adam عليه السلام juu ya hila zake za kumtoa katika *Jannah* ambayo ni makazi ya neema na kumpeleka katika nyumba ya tabu na uchovu na kumsababishia uchi wake udhihirike, baada ya kusitirika kwake. Huu, kwa hakika, ni uadui wa ndani kabisa (kutoka kwa shetani dhidi ya mwanadamu).

Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 12:364.

² At-Tabari 12:368.

أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا

“Je! Mnamshika yeye na dhuriya wake kuwa marafiki badala Yangu, hali wao ni adui zenu? Ni uovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu”. (18:50)

وَإِذَا فَعَلُوا فَحِشَةً قَالُوا وَجَدْنَا عَلَيْهَا آبَاءَنَا وَاللَّهُ أَمَرَنَا بِهَا قُلْ إِنْ أَلَّهَ لَا يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ ط اتَّقُوا اللَّهَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٧﴾ قُلْ أَمَرَ رَبِّي بِالْقِسْطِ ط وَأَقِيمُوا وُجُوهَكُمْ عِندَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ ﴿٢٨﴾ فَرِيقًا هَدَىٰ وَفَرِيقًا حَقَّ عَلَيْهِمُ الضَّلَالَةُ إِنَّهُمْ اتَّخَذُوا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهم مُهْتَدُونَ ﴿٢٩﴾

28. Na wanapofanya mambo machafu husema: Tumewakuta nayo baba zetu, na Mwenyezi Mungu Ametuamrisha hayo.

29. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu Haamrishi mambo machafu. Mnamzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua? Sema: Mola Mlezi wangu Aameamrisha uadilifu, na muelekeze nyuso zenu kila mnaposujudu na mumuombeni Yeye kwa kumsafia Dini. Kama Alivyokuumbeni mwanzo ndivyo mtavyorudi.

30. Hali ya kuwa kundi moja Amelihidi, na kundi jingine limethibitikiwa na upotofu. Kwa hakika hao waliwafanya mashetani kuwa ndio marafiki walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, na wanadhani kuwa wao wameongoka”.

Makafiri Hufanya Madhambi na Kuyategemeza kwa Allah تعالى.

Mujahid alisema, “Washirikina walikuwa wanatufu Nyumba (Al-Ka’bah) huku wakiwa uchi, wakisema, “Tunatufu kama walivyotuzaa mama zetu”. Na mwanamke alikuwa akiweka kitu katika tupu yake na kusema, “Leo itadhihiri yote au baadhi yake. Na kile kitakachodhihiri sitaruhusu (hakitafanyiwa zinaa).” Allah تعالى Akateremsha;

¹ Neno kwa neno. Hasa hasa kidini. Walisema hivyo, kama alivyozoea kusema, “Sisi ni watu wa Allah, hatutaondoka mahali patakatifu.

وَإِذَا فَعَلُوا فَحِشَةً قَالُوا وَجَدْنَا عَلَيْهَا آبَاءَنَا وَاللَّهُ أَمَرْنَا بِهَا

“Na wanapofanya mambo machafu husema: Tumewakuta nayo baba zetu, na Mwenyezi Mungu Ametuamrisha hayo”. (7:28)¹

Mimi nasema, Waarabu isipokuwa Makuraishi, walikuwa hawaitufu Nyumba wakiwa wamevaa nguo zao walizovaa. Katika hilo, walikuwa wakidai kuwa hawataitufu huku wakiwa wamevaa nguo ambazo zilivaliwa katika kumuasi Allah تعالى, ama kuhusu Makuraishi waliojulikana kama *Al-Hums*, walikuwa wakitufu wakiwa wamevaa nguo zao za kawaida. Mwarabu yeyote aliyeazimwa nguo na *Al-Hums*, alikuwa akiivaa wakati wa kutufu. Mwenye kuvaa nguo mpya aliyovaa wakati wa kutufu, alilitupa wala hakumpatia mtu mwingine kuimiliki. Yule ambaye hakupata nguo mpya, wala hakuazimishwa na *Al-Hums* alitufu akiwa uchi, alikuwa akiweka kitu juu ya tupu yake ili kumsitiri kidogo. Halafu husema, “Leo itadhihiri yote au baadhi yake. Na kile kilichodhihiri sitakiruhusu (hakitafanyiwa zinaa)”.

Mara nyingi wanawake walikuwa wakitufu wakiwa uchi nyakati za usiku, hili ni jambo ambalo washirikina walilizusha wao wenyewe, na kwa kuwafuata baba zao katika hilo, na Wanachukulia kwamba matendo ya baba zao yanategemea amri na sharia ya Allah تعالى. Allah تعالى Aliwakanushia hilo, Akasema;

وَإِذَا فَعَلُوا فَحِشَةً قَالُوا وَجَدْنَا عَلَيْهَا آبَاءَنَا وَاللَّهُ أَمَرْنَا بِهَا

“Na wanapofanya mambo machafu husema: Tumewakuta nayo baba zetu, na Mwenyezi Mungu Ametuamrisha hayo”.

Allah تعالى Haamrishi Mambo Machafu, Bali Uadilifu na Ikhlas.

Allah تعالى Aliwajibu kuwa madai yao ya uongo;

قُلْ

“Sema”. Ewe Muhammad, kumuambia mwenye kudai hayo.

قُلْ إِنْ أَلَّهَ لَا يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ ط

“Hakika Mwenyezi Mungu Haamrishi mambo machafu”. Maana yake: Haya muyafanyayo ni dhambi na kwamba, Allah تعالى Haamrishi jambo hilo.

أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ

“Mnamzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua?” Maana: Mnategemeza kwa Allah تعالى, kauli ambazo hamjui usahihi wake? Kauli ya Allah تعالى;

قُلْ أَمَرَ رَبِّي بِالْقِسْطِ

“Sema: Mola Mlezi wangu Ameamrisha uadilifu”. Maana yake: Kwa uadilifu na kuwa na msimamo imara.

وَأَقِيمُوا وُجُوهَكُمْ عِندَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

“...na muelekeze nyuso zenu kila mnaposujudu na mumuombeni Yeye kwa kumsafia Dini”.

Maana yake: Amekuamrisheni msimame imara katika kumuabudu Yeye kama itakikanavyo, nako ni kuwafuata Mitume waliosaidiwa kwa miujiza juu ya yale walivyoeleza kuhusu Allah تعالى na sharia walizokuja nazo, pamoja na kumfanyia Allah تعالى ikhlasi katika kumuabudu, kwani Allah تعالى Haipokei amali yoyote, mpaka nguzo hizo mbili ziwepo pamoja: Amali hiyo iwe imewafikiana na sharia na iwe ni yenye kutakasika na ushirikina.

Maana ya Ushirikina, Kuumbwa kwa Mara ya kwanza na Kurudishiwa tena uhai.

Kauli ya Allah تعالى;

كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ

“Kama Alivyokuumbeni mwanzo ndivyo mtavyorudi.” (7:29)

mpaka;

الضَّلَالَةَ

“...upotofu”. Ibn Abu Najih alisema kutoka kwa Mujahid kuwa;

كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ

“Kama Alivyokuumbeni mwanzo ndivyo mtavyorudi.” Maana yake: “Atakuhiisheni baada ya kufa kwenu”¹. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Kama Alivyokuanzisheni humu duniani, Halikadhalika, mtarudishwa mkiwa hai katika Siku ya Kiyama”². Qatadah alisema kuwa;

¹ At-Tabari 12:385.

² At-Tabari 12:385.

كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ

“Kama Alivyo kuumbeni mwanzo ndivyo mtavyorudi.”

Ina maana, “Alianzisha kuwaumba ilhali hawakuwepo, kisha wakaondoka, na Halafu Atawarudisha”¹. ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema, “Kama Alivyokuumbeni hapo awali, Atakurejesheni Mwishowe”². Abu Jafar bin Jariri رحمه الله تعالى aliihitari kauli hii, na aliitilia nguvu kutokana na aliyoyanukuu kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما ambaye alisema, Mtume ﷺ alisimama na akatupa mawaidha kwa kusema;

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّكُمْ تُحْشَرُونَ إِلَى اللَّهِ حِفَاةَ عُرَاةٍ غُرْلًا ﴿كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ
تُعِيدُهُمْ وَعَدًّا عَلَيْنَا إِنَّا كُنَّا فَاعِلِينَ﴾

“Enyi watu! Mtakusanywa kwa Allah mkiwa bila viatu, bila nguo na bila kuwa mmetahiriwa, **“Kama Tulivyoanza umbo la mwanzo Tatalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu Yetu. Hakika Sisi ni watendao”**. (21:104)³ Hadithi hii ilikusanywa katika Sahih Mbili⁴.

‘Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما akielezea;

كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ ﴿فَرِيقًا هَدَىٰ وَفَرِيقًا حَقَّ عَلَيْهِمُ الضَّلَالَةُ﴾

“Kama Alivyo kuumbeni mwanzo ndivyo mtavyorudi. Hali ya kuwa kundi moja Amelihidi, na kundi jingine limethibitikiwa na upotofu”.

Kwamba, “Allah تعالى Alianza Kuumba wanadamu, wengine waumini na wengine makafiri. Kama alivyo sema katika Aya nyingine;

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَمِنْكُمْ مُّؤْمِنٌ

“Yeye Ndiye Aliyekuumbeni. Miongoni mwenu yupo aliyekafiri, na yupo aliyemuumini”. (64:2)

Kisha Atawarejesha katika Siku ya Kiyama huku baadhi yao Waumini na baadhi makafiri⁵. Mimi nasema kauli hii inaungwa mkono na Hadithi ya Ibn Mas’ud رضي الله عنه iliyo katika Sahih Al-Bukhari.

¹ At-Tabari 12:385.

² At-Tabari 12:385.

³ At-Tabari 12:386.

⁴ Fat’hul Al-Bari 6:445 na 8:135 na Muslim 4:2194.

⁵ At-Tabari 12:384.

﴿فَوَالَّذِي لَا إِلَهَ غَيْرُهُ إِنَّ أَحَدَكُمْ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْجَنَّةِ حَتَّىٰ مَا يَكُونُ بَيْنَهُ وَبَيْنَهَا إِلَّا بَاعٌ أَوْ ذِرَاعٌ، فَيَسْبِقُ عَلَيْهِ الْكِتَابُ فَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ النَّارِ فَيَدْخُلُهَا، وَإِنَّ أَحَدَكُمْ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ النَّارِ حَتَّىٰ مَا يَكُونُ بَيْنَهُ وَبَيْنَهَا إِلَّا بَاعٌ أَوْ ذِرَاعٌ فَيَسْبِقُ عَلَيْهِ الْكِتَابُ، فَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْجَنَّةِ فَيَدْخُلُ الْجَنَّةَ﴾

“Naapa kwa Yeye Ambaye, hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye. Mmoja wenu anaweza kufanya amali za watu wa Jannah mpaka baina yake na hiyo Jannah kunakuwa na umbali usiozidi kitengele au dhira. Lakini kilichoandikwa katika Kitabu kinamtangulia. Halafu anafanya amali za watu wa Motoni, mpaka anaingia. Na kwamba mmoja wenu anaweza akafanya amali za watu wa Motoni mpaka baina yake na Motoni kunakuwa na umbali usiozidi kitengele au dhira. Lakini kilichoandikwa katika Kitabu kinamtangulia. Halafu anafanya amali za watu wa Jannah, mpaka anaingia humo”¹.

Mimi nasema, hapana budi kauli hii, ikiwa hilo ndio lengo la Ayah, ijumuishwe na Kauli ya Allah تعالى:

﴿فَأَقْرَ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا﴾

“Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini – ndio umbile la Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu”². (30:30)

Pamoja na yalionyukuliwa katika *Sahih* Mbili kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema;

﴿كُلُّ مَوْلُودٍ يُوَلَّدُ عَلَى الْفِطْرَةِ، فَأَبَوَاهُ يُهَوِّدَانِهِ وَيُنَصِّرَانِهِ وَيَمَجْسَانِهِ﴾

“Kila mzaliwa huwa amezaliwa katika Fitrah, ni wazazi wake ndio wanaom-badili kuwa Myahudi, Mkiristo au Mmajusi”³.

Na Hadithi ya ‘Iyadh bin Hamaar iliyo katika *Sahih* Muslim aliyesema, Mtume ﷺ alisema;

¹ Fat’hul Al-Bari 11:486.

² Maana ya Ayah ni, “Jiweke katika dini ya Allah تعالى ambayo ndio asili Aliyowawekea wanadamu.”

³ Fat’hul Al-Bari 3:290 na Muslim 4:2047.

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: إِنِّي خَلَقْتُ عِبَادِي حُتَفَاءً، فَجَاءَتْهُمْ الشَّيَاطِينُ فَاجْتَالَتْهُمْ عَنْ دِينِهِمْ»

“Allah Anasema: Mimi Nimewaumba waja Wangu Hunafaa (waliompwekesha Allah katika ibada), lakini mashetani yakawajja na wakawapoteza mbali na dini yao”.¹

Maana ya kujumuisha maelezo haya ni kwamba, Allah تعالى Aliwaumba binadamu ili wawepo Waumini na Makafiri kwa hali mbili hizi. Hapo awali, Allah تعالى Alikwishawaumba viumbe wote na wakaweza kumjua Yeye, kumpwekesha na kujua kwamba hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye. Pia alichukua miadi yao ambayo Aliweka katika utambuzi wao na *Fitra*. Pamoja na haya alipitisha kudura Yake kwamba kuna muovu na mwema miongoni mwao.

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْكُمْ كَافِرٌ وَمِنْكُمْ مُؤْمِنٌ

“Yeye Ndiye Aliyekuumbeni. Miongoni mwenu yupo aliyekafiri, na yupo aliyemuumini”. (64:2)

Na Hadithi;

«كُلُّ النَّاسِ يَغْدُو فَبَائِعُ نَفْسِهِ فَمُعْتَقُهَا أَوْ مُوْبِقُهَا»

“Watu wote hutoka asubuhi na kujiuza nafsi zao, na baadhi yao huziachilia huru na wengine huziangamiza”.²

Hukumu ya Allah تعالى, kwa hakika, itawapitia viumbe wote, kwani Yeye Ndiye;

وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَىٰ

“Na Ambaye Amekadiria na Akaongoa”. (87:3) Na;

الَّذِي أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَىٰ

“Yule Aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha Akakiongoa”. (20:50)

Na katika *Sahih* Mbili, ipo Hadithi;

«فَأَمَّا مَنْ كَانَ مِنْكُمْ مِنْ أَهْلِ السَّعَادَةِ فَيَسِّرُ لِعَمَلِ أَهْلِ السَّعَادَةِ، وَأَمَّا مَنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ الشَّقَاوَةِ فَيَسِّرُ لِعَمَلِ أَهْلِ الشَّقَاوَةِ»

¹ Muslim 4:2197.

² Muslim 1:203.

“Ama yule ambaye ni miongoni mwa watu wema katika nyinyi, (Allah) Atamrahisishia kufanya amali za watu wema. Ama yule ambaye ni katika watu waovu, Atamrahisishia kufanya amali za watu waovu”¹.

Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema;

فَرِيقًا هَدَىٰ وَفَرِيقًا حَقَّ عَلَيْهِمُ الضَّلَالَةُ

“Hali ya kuwa kundi moja Amelihidi, na kundi jingine lime-thibitikiwa na upotofu”.

Kisha Allah تعالى Aliyatolea hayo sababu.

إِنَّهُمْ أَخَذُوا مِنَ الشَّيْطَانِ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ اللَّهِ

“Kwa hakika hao waliwa fanya mashetani kuwa ndio marafiki walinzi badala ya Mwenyezi Mungu”.

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, “Hii ni moja wapo ya dalili za wazi kabisa juu ya makosa ya wanaodai kwamba Allah تعالى Hatamuadhibu yeyote juu ya maasi aliyoyafanya au upotofu aliouitakidi, isipokuwa baada ya kupata ujuzi juu ya usahihi wa njia yake, kisha akayafanya hayo madhambi kwa kumfanyia ujeuri Mola wake. Kama ingelikuwa hivyo ndivyo sawa, basi kusingekuwa na tofauti ya upotovu baina ya kundi la waliopotea kwa kudhani kwamba wameongoka, na kundi lililoongoka kweli. Na katika Aya hii, Allah تعالى Alikwishagawa baina ya majina na hukumu za makundi hayo mawili”.²

* * *

¹ At-Tabari 12:388. Angalia maelezo katika Surat At-Tawbah 9:115 na maelezo ya At-Tabari kuihusu.

² Fat’hul Al-Bari 3:267 na Muslim 4:2039.

* يَبْنِيْٓ اٰدَمَ خُذُوْا زِيْنَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَكُلُوْا
 وَاَشْرَبُوْا وَلَا تُسْرِفُوْا ۗ اِنَّهٗ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِيْنَ ﴿٣١﴾ قُلْ
 مَنْ حَرَّمَ زِيْنَةَ اللّٰهِ الَّتِي اُخْرِجَ لِعِبَادِهٖ وَالطَّيِّبَاتِ مِنَ
 الرِّزْقِ ۗ قُلْ هِيَ لِلَّذِيْنَ ءَامَنُوْا فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا خَالِصَةً
 يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۗ كَذٰلِكَ نَفْصَلُ الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُوْنَ ﴿٣٢﴾
 قُلْ اِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّيَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ
 وَالْاِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَاَنْ تُشْرِكُوْا بِاللّٰهِ مَا لَمْ يُزَلْ
 بِهٖ سُلْطٰنًا وَاَنْ تَقُولُوْا عَلٰى اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٣٣﴾
 وَلِكُلِّ اُمَّةٍ اَجَلٌ ۗ فَاِذَا جَآءَ اَجَلُهُمْ لَا يَسْتَاْخِرُوْنَ سَاعَةً
 وَلَا يَسْتَقْدِمُوْنَ ﴿٣٤﴾ يَبْنِيْٓ اٰدَمَ اِمَّا يٰٓاَيُّهَا رُسُلُ
 مِنْكُمْ يَقْضُوْنَ عَلَيْكُمْ ءَايٰتِيْ ۗ فَمَنْ اَتَقٰى وَاَصْلَحَ فَلَا
 خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٣٥﴾ وَالَّذِيْنَ كَذَّبُوْا
 بِءَايٰتِنَا وَاَسْتَكْبَرُوْا عَنَّا اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيْهَا
 خٰلِدُوْنَ ﴿٣٦﴾ فَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنْ اَفْتَرٰى عَلٰى اللّٰهِ كَذِبًا اَوْ
 كَذَّبَ بِءَايٰتِهٖ ۗ اُولٰٓئِكَ يَنٰهٗمُ نَصِيْبُهُم مِّنَ الْكِتٰبِ
 حَتّٰى اِذَا جَآءَهُمْ رُسُلُنَا يَتَوَفَّوْنَهُمْ قَالُوْا اٰنَ مَا كُنْتُمْ
 تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْرٍ اللّٰهِ ۗ قَالُوْا ضَلُّوْا عَنَّا وَشَهِدُوْا عَلٰى
 اَنْفُسِهِمْ اَنَّهُمْ كَانُوْا كٰفِرِيْنَ ﴿٣٧﴾

* يَبْنِيْٓ اٰدَمَ خُذُوْا زِيْنَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ
 مَسْجِدٍ وَكُلُوْا وَاَشْرَبُوْا وَلَا تُسْرِفُوْا
 اِنَّهٗ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِيْنَ ﴿٣١﴾

**31. Enyi wanadamu! Chu-
 kueni pambo lenu kwenye
 kila pahala wakati wa ibada,
 na kuleni na kunyweni na
 wala Msifanye ubadhirifu.
 Kwa hakika Yeye Hapendi
 wanaofanya Israfu.**

**Amri ya Kujipamba Wakati
 wa Kwenda Masjid.**

Aya hii tukufu inawaka-
 nushia washirikina juu ya
 waliyokuwa wakiyate-
 gemea, katika kuitufu
 Nyumba wakiwa uchi. Kama
 walivyonyuku Muslim, An-
 Nasai na Ibn Jariri
 (na maneno
 yafuatayo ni ya Ibn Jariri
 kutokana na
 Hadithi ya Ashu'bah kutoka
 kwa Salamah bin Kuhayl
 kutoka kwa Muslim bin Al-
 Batwin kutoka kwa Sa'id bin
 Jubayr kutoka kwa Ibn
 'Abbas رضي الله عنهما, kuwa
 alisema, "Walikuwa wakii-

tufu Nyumba wanawake na wanaume wakiwa uchi. Mchana wanaume na usiku

wanawake. Mwanamke aliweza kusema, "Leo mwili wote au sehemu yake upo wazi sehemu itakayokuwa wazi sitoihalalisha"¹. Allah تعالى Akasema;

خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ

"Chukueni pambo lenu kwenye kila pahala wakati wa ibada".

Al-'Awfi alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ

"Chukueni pambo lenu kwenye kila pahala wakati wa ibada".

Kwamba, wanaume walikuwa wakiitufu Nyumba huku wakiwa uchi, basi Allah تعالى Akawaamuru wajipambe, nayo ni yale yanayowasitiri sehemu zao na zaidi ya hayo ziwe safi na zinazofaa kusitiri. Kwa hivyo waliamrisha wajipambe waendapo katika Sala². Mujahid, 'Ata, Ibrahim An-Nakhai, Sa'id bin Jubayr, Qatadah, As-Suddi na Adh-Dhahhak na Malik kwa kumnukuu Az-Zuhri, nao walisema vivyo hivyo³. Kadhalika Maimamu kadha wa *Salaf*, katika kuitafsiri, walisema kwamba iliteremshwa kuwahusu washirikina waliokuwa wakiitufu Nyumba huku wakiwa uchi. Kutokana na Aya hii. Na Sunna iliyopokelewa katika maana yake hiyo huhimiza jambo la Kujipamba minajili ya Sala, hasa hasa, katika siku ya Ijumaa na Idi. Jambo la mafuta mazuri (kwa wanaume) nalo limesisitizwa kwa kuwa ni sehemu ya kujipamba, pia kupiga mswaki, kwa kuwa kunakamilisha jambo hilo.

Nguo bora ni nyeupe, sawa na alivyonukuu Imamu Ahmad kwamba Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, Mtume ﷺ alisema;

«الْبُسُوفُ مِنْ زِينَتِكُمْ الْبَيَاضُ فَإِنَّهَا مِنْ خَيْرِ زِينَتِكُمْ، وَكَفْنَا فِيهَا مَوْتَاكُمْ وَإِنَّ خَيْرَ أَكْحَالِكُمْ الْإِثْمَدُ فَإِنَّهُ يَجْلُو الْبَصَرَ وَيُنْبِتُ الشَّعْرَةَ»

"Katika nguo zenu, vaeni nyeupe, kwani ndizo nguo zenu nzuri zaidi, pia muwakafini nazo maiti wenu. Na kohli zenu bora ni (Ithmid-antimony) kwani husafisha uonaji na huotesha nywele".³

¹ Muslim 4:2320, An-Nasai katika Al Kubra, 6:345 na At-Tabari 12:390.

² At-Tabari 12:391.

³ At-Tabari 12:392-394.

⁴ Ahmad 1:297.

Hadithi hii ina isnadi nzuri ikiwa na wasimuliaji wanaowafikiana na masharti na mwongozo wa Muslim, na imenukuliwa pia na Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibn Majah. At-Tirmidhi alisema, ni *"Sahih"*.¹

Makatazo ya Kufanya *Israfu* Katika Vyakula na Mavazi.

Kauli ya Allah تعالى:

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا

"...na kuleni na kunyweni".

Al-Bukhari alisema, Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema:

*"Kula na uvae ukitakacho ilimradi uyaepuke makosa mawili, Israfu na kiburi"*².

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, Muhammad bin 'Abdul-'Alaa alitueleza, Muhammad bin Thawri alitueleza, kutoka kwa Ma'mar, kutoka kwa Ibn Twawus, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kwamba, "Allah تعالى Amehalalisha kula na kunywa, basi kusiwe na Israfu au kiburi"³. Isnadi yake ni *Sahih*.

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alimnukuu Al-Miqaadim bin Ma'diyakarib Al-Kindy kwamba alisema, nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«مَا مَلَأَ ابْنُ آدَمَ رِغَاءَ شَرًّا مِنْ بَطْنِهِ بِحَسْبِ ابْنِ آدَمَ أَكَلَاتٍ يُعْمَنُ صَلْبُهُ فَإِنْ كَانَ فَاغِيلاً لَا مَحَالَةَ فَتَلَّتْ طَعَامٌ وَتَلَّتْ شَرَابٌ وَتَلَّتْ لِنَفْسِهِ»

*"Mwanadamu anatakiwa awe na tahadhari na tumbo lake, kwani ni kiungo kinachoweza kumletea matatizo. Inamtosha mwanadamu kula chakula kiasi cha kuupa nguvu uti wa mgongo wake. Akiamua kula zaidi, basi theluthi moja iwe ya chakula, theluthi nyingine ya kinywaji na theluthi moja kwa ajili ya kupumua kwake"*¹.

¹ Abu Dawud 4:332, Tufhat Al-Ahwadhi 7:72 na Ibn Majah 1:473.

² Fat'hul Al-Bari 1:264.

³ At-Tabari 12:394.

⁴ Ahmad 4:132

An-Nasai na At-Tirmidhi waliikusanya Hadithi hii¹, na At-Tirmidhi akasema, "Hasan na katika maandishi mengine, "Hasan". 'Ata Al-Khurasani alisema, kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kwamba Kauli ya Allah تعالى:

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ

"...na kuleni na kunywaeni na wala Msifanye ubadhirifu. Kwa hakika Yeye Hapendi wanaofanya Israfu".

"Katika chakula na vinywaji"². Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ

"Kwa hakika Yeye Hapendi wanaofanya Israfu".

Allah تعالى Anasema, Allah تعالى Hawapendi warukao mpaka Wake, katika halali au haramu. Wala wanaoruka mipaka katika Alivyovihalalisha kwa kuhalalisha haramu na kuharamisha halali. Bali Yeye Hupenda kuhalalishwa kile Alichohalalisha na kuharamishwa Alichokiharamisha Yeye, na huu ndio uadilifu Aliouamrisha³.

قُلْ مَنْ حَرَّمَ زِينَةَ اللَّهِ الَّتِي أَخْرَجَ لِعِبَادِهِمُ وَالطَّيِّبَاتِ مِنَ الرِّزْقِ قُلْ هِيَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا خَالِصَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ كَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٣٢﴾

"Sema: Ni nani aliye haramisha pambo la Mwenyezi Mungu Alilowatolea waja Wake, na vilivyo vizuri katika riziki. Sema hivyo ni kwa walioamini katika uhai wa duniani, na Siku ya Kiyama vitakuwa vyao wao tu. Namna hivi Tunazieleza Ishara kwa watu wanaojua". (7:32)

Allah تعالى Anawakanushia walioharamisha aina yoyote ya chakula, kinywaji au mavazi kwa kuifuata nafsi yake ghairi ya Sharia ya Allah تعالى:

قُلْ

"Sema". Ewe Muhammad ﷺ kuwaambia washirikina hao, ambao wanavi - haramisha walivyoviharamisha kwa rai zao potofu na uzushi wao.

¹ Tuhfatul Al-Ahwadhi 7:51 na An-Nasai 4:178.

² At-Tabari 12:394.

³ At-Tabari 12:395.

مَنْ حَرَّمَ زِينَةَ اللَّهِ الَّتِي أَخْرَجَ لِعِبَادِهِ

“Ni nani aliyeharamisha pambo la Mwenyezi Mungu Alilowatolea waja Wake”.

Inamaanisha kwamba vitu hivi viliumbwa kwa minajili ya wanaomuamini Allah تعالى na kumuabudu Yeye duniani, hata kama makafiri wanashiriki katika kunufaika na neema za humo duniani. Siku ya Kiyama itawahusu Waumini tu, wala kafiri yeyote hatashiriki, kwani *Janna* imepigwa marufuku kwa makafiri.

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّي الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ وَالْإِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَأَنْ تُشْرِكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْمُونَ ﴿٣١﴾

“Sema: Mola Mlezi wangu Ameharamisha mambo machafu ya dhahiri na ya siri, na dhambi, na uasi bila ya haki, na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na Asichokiletea uthibitisho, na Kumzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua”. (7:33)

Haramu ni Mambo Machafu, Dhambi, Dhuluma, Uasi, Ushirikina na Kumzulia Allah تعالى Uongo.

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alimnukuu ‘Abdullah رضي الله عنه kuwa, Mtume ﷺ alisema;

«لَا أَحَدٌ أَغْيُرُ مِنَ اللَّهِ فَلِذَلِكَ حَرَّمَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ، وَلَا أَحَدٌ أَحَبُّ إِلَيْهِ الْمَذْحُ مِنَ اللَّهِ»

“Hakuna mwenye wivu zaidi ya Allah تعالى, kwa sababu hiyo, Aliharamisha maovu ya dhahiri na ya ufichoni. Wala hapana apendaye kusifiwa kuliko Anavyopenda Allah تعالى”.¹

Sahih Mbili zilinukuu². Maelezo yanayoambatana na mambo machafu *“Fahishah”* ya dhahiri au siri ambayo yamekwishatangulia katika *Surat Al-An’aam*. Kauli ya Allah تعالى;

¹ Ahmad 1:381.

² Fat’hul Al-Bari 9:230 na Muslim 4:2114.

وَالْإِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ

“...na dhambi, na uasi bila ya haki”. (7:33)

As-Suddi alisema, “*Ithm* ni maasi. *Al-Baghy* ni kuwakandamiza watu pasi na haki”¹. Mujahid alisema, “*Ithm* ni maasi yote.

Allah تعالى Ameeleza kwamba, “*Al-Baghy* ni kujidhulumu nafsi yake”². Kwa hivyo, maana ya *Al-Ithm* ni madhambi anayoyafanya mtu dhidi yake mwenyewe na *Al-Baghy* ni kuwafanyia dhambi watu wengine. Allah تعالى Ameharamisha namna ya kwanza na ya pili.

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَنْ تُشْرِكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُزَلِّ بِهِ سُلْطَانًا

“...na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na Asichokiletea uthibitisho”.

Maana: Mkimfanyia washirika katika kumuabudu Yeye.

وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْمُونَ

“...na Kumzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua”.

Juu ya uzushi na uongo kama vile kudai kuwa ana mwana na kama hivyo, katika msiyokuwa na ujuzi nayo kwayo.

Sawa na Kauli Yake nyingine;

فَأَجْتَبُوا الرَّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ

“Basi Jiepusheni na uchafu wa masanamu”. (22:30)

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ ۖ فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ لَا يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً ۖ وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ ﴿٣١﴾
يَنْبِئُ آدَمَ إِمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِي ۖ فَمَنِ اتَّقَى وَأَصْلَحَ فَلَا

¹ At-Tabari 12:403.

² At-Tabari 12:403.

خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣١﴾ وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا
أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٢﴾

34. Na kila umma una muda wake. Utakapofika muda wao basi hawatakawia hata saa moja, wala hawatatangulia.

35. Enyi wanadamu! Watapokufikieni Mitume miongoni mwenu wakakuelezeni Ishara Zangu, basi watakaomchamungu na wakatengenea haitakuwa khofu kwao, wala hawatahuzunika.

36. Na wale watakaokanusha Ishara Zetu na wakazifanyia kiburi, hao ni watu wa Motoni: umo watadumu.

Allah تعالى Alisema;

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ

“Na kila umma”. Maana yake: Umma na kizazi.

أَجَلٌ مُّطَّرٌ فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ

“...una muda wake. Utakapofika muda wao”.

Maana yake: Kipindi walichopangiwa.

لَا يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ

“...basi hawatakawia hata saa moja, wala hawatatangulia”.

Kisha Allah تعالى Aliwaonya wanaadamu kuwa Yeye Atawapelekea Mitume wa kuwaeleza Aya Zake, na kutoa bishara na tahadhari. Alisema;

فَمَنْ أَتَقَىٰ وَأَصْلَحَ

“...basi watakao Mchamungu na wakatengenea”.

Maana yake: Kwa kuacha maovu na wakatenda amali za utii.

فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٣﴾ وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا

“...haitakuwa khofu kwao, wala hawatahuzunika. Na wale watakaokanusha Ishara Zetu na wakazifanyia kiburi”.

Maana yake: Nyoyo zao zilizikanusha na wakafanya kiburi kwa kutokuzijali.

أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

"...hao ni watu wa Motoni: umo watadumu".

Maana yake: Watakaa humo milele.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۗ أُولَئِكَ يَنَاهُمْ نَصِيحُهُمْ مِّنَ الْكِتَابِ ۗ حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُمْ رُسُلُنَا يَتَوَفَّوهُمْ قَالُوا أَإِنَّا مَا كُنْتُمْ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ ۗ قَالُوا ضَلُّوا عَنَّا وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَنَّهُمْ كَانُوا كَافِرِينَ ﴿٧٧﴾

37. Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, au anayezikanusha Ishara Zake? Hao Itawafikia sehemu yao waliyoandikiwa, mpaka watakapowafikia wajumbe wetu kuwafisha, wataambiwa: Wako wapi mliokuwa mkiwaomba badala ya Mwenyezi Mungu? Watasema: Wametupotea! Na watajishuhudia wenyewe kwamba walikuwa makafiri".

Washirikina Wazushi Watapata Fungu Lao Humu Duniani na Watatengana na Wasaidizi Wao Wakati wa Kufa.

Anasema;

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۗ

"Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, au anayezikanusha Ishara Zake?"

Maana yake: Hakuna dhalimu zaidi kuliko aliyemzulia Allah تعالى uongo au aliyezikadhibisha Ayah Zake zilizoteremshwa. Muhammad bin Ka'b Al-Quradhi alisema kuwa,

أُولَئِكَ يَنَاهُمْ نَصِيحُهُمْ مِّنَ الْكِتَابِ

"Hao Itawafikia sehemu yao waliyoandikiwa".

Maana yake: Amali zake, riziki na umri¹. Ndivyo walivyosema pia akina Ar-Rabi' bin Anas na 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam². Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

¹ At-Tabari 12:413

² At-Tabari 12:414.

قُلْ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾ مَتَّعٌ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ
إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الْأَشَدَّ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾

“Sema: Hao wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao”. (10:69-70)

وَمَنْ كَفَرَ فَلَا يَحْزُنكَ كُفْرُهُ ۚ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ فَنُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ
الصُّدُورِ ﴿٧١﴾ نُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا

“Na anayekufuru, isikuhuzunishe kufuru yake. Kwetu ndio marudio yao, na hapo Tutawaambia waliyoyatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani. Tunawastarehesha kwa uchache”. (31:23-24)

Kauli ya Allah تعالى:

إِذَا جَاءَهُمْ رُسُلُنَا يَتَوَفَّوهُمْ

“...mpaka watakapowafikia wajumbe wetu kuwafisha”.

Allah تعالى Anaeleza kuwa pindi washirikina wanapofikiwa na mauti, na Malaika wakazichukua roho zao kuzipeleka Jahannamu, Malaika nao huwatisha, kwa kuwaambia, “Wako wapi mliokuwa mkiwashirikisha (na Allah تعالى) duniani, mliokuwa mkiwaomba na kuwaabudu kinyume cha Allah تعالى. Basi waombeni wakuokeni ili muondokane na mnayokumbana nayo.” Watasema;

ضَلُّوا عَنَّا

“Wametupotea!” Maana yake: Wameondokana nasi, basi hatutaraji kunufaishwa wala kupata kheri yao.

وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ

“Na watajishuhudia wenyewe”. Maana: Watakiri na kutamka wao wenyewe.

أَنَّهُمْ كَانُوا كَافِرِينَ

“...kwamba walikuwa makafiri”. Kwani walikuwa makafiri.

قَالَ ادْخُلُوا فِي أُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِكُمْ مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ فِي النَّارِ كُلَّمَا دَخَلَتْ أُمَّةٌ لَعْنَتْ أُخْتَهَا حَتَّى إِذَا آذَرَكُوا فِيهَا جَمِيعًا قَالَتْ أُخْرَيْتُمْ لِأَوْلِيئِهِمْ رَبَّنَا هَؤُلَاءِ أَضَلُّونَا فَصَبِّرْهُمْ عَذَابًا ضِعْفًا مِنَ النَّارِ قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٍ وَلَكِنْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٧﴾ وَقَالَتْ أَوْلِيئُهُمْ لِأُخْرَيْتُمْ فَمَا كَانَ لَكُمْ عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٣٨﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا لَا تُفَتَّحُ لَهُمْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ وَلَا يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ حَتَّى يَلِجَ الْجَمَلُ فِي سَمِّ الْخِيَاطِ ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُجْرِمِينَ ﴿٣٩﴾ هُمْ مِنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ وَمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٤٠﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٤١﴾ وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِنْ غَلٍّ فَجَزَى مِنْ تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ ۗ وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي هَدَانَا لِهَذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَنْ هَدَانَا اللَّهُ لَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ ۗ وَنُودُوا أَنْ تِلْكَمُ الْجَنَّةُ أَوْرَثْتُمُوهَا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٢﴾

قَالَ ادْخُلُوا فِي أُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِكُمْ مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ فِي النَّارِ كُلَّمَا دَخَلَتْ أُمَّةٌ لَعْنَتْ أُخْتَهَا حَتَّى إِذَا آذَرَكُوا فِيهَا جَمِيعًا قَالَتْ أُخْرَيْتُمْ لِأَوْلِيئِهِمْ رَبَّنَا هَؤُلَاءِ أَضَلُّونَا فَصَبِّرْهُمْ عَذَابًا ضِعْفًا مِنَ النَّارِ قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٍ وَلَكِنْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٧﴾ وَقَالَتْ أَوْلِيئُهُمْ لِأُخْرَيْتُمْ فَمَا كَانَ لَكُمْ عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٣٨﴾

38. Mwenyezi Mungu atasema: Ingieni Motoni pamoja na umma uliopita kabla yenu na watu. Kila utakapoingia umma utalaani umma mwengine. Mpaka watakapokusanyika wote humo, wa mwisho wao watawasema wa mwanzo wao: Mola wetu Mlezi! Hawa ndio waliotupoteza; basi wape adhabu ya Motoni maradufu. Atasema: Itakuwa kwenu nyote maradufu, lakini nyinyi hamjui tu.

39. Na wa mwanzo wao utawaambia wa mwisho wao: Basi nyinyi pia hamkuwa na ubora kuliko sisi. Basi onjeni adhabu kwa sababu ya mliyokuwa mkiyachuma.

Kuhasimiana kwa Watu wa Motoni na Kulaaniana Baina Yao.

Allah تعالی Anajulisha juu ya Anayowaambia hao wanaomshirikisha Yeye, wenye Kumzulia uongo na kumkadhibishia Aya Zake;

أَدْخُلُوا فِي أُمَمٍ

"Ingieni pamoja na umma". Wa mfano wenu na wanaolingana nanyi kwa sifa.

قَدْ خَلَّتْ مِنْ قَبْلِكُمْ

"...uliopita kabla yenu". Maana yake: Umma za kikafiri zilizotangulia.

مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ فِي النَّارِ

"...za majini na watu Motoni". Inaweza kuchukulika kuwa ni badala ya Kauli Yake, *Fiy Umam* (katika umma). Pia inaweza kuchukulika inakusudia *Fiy Umam* kwa maana ya pamoja na umma mwengine. Kauli Yake;

كُلَّمَا دَخَلَتْ أُمَّةٌ لَعَنَتْ أُخْتَهَا

"Kila utakapoingia umma utawalaani mwenzake".

Sawa na alivyosema Al-Khalil عليه السلام;

ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُ بَعْضُكُم بِبَعْضٍ

"Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi". (29:25)

Pia Allah تعالی Alisema;

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأُوا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿٣٧﴾
 وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا لَوْ أَنَّا كُنَّا نَدْرِكُهُمْ لَسَأَلْتُمُوهُم كَمَا تَبَرَّأُوا مِنَّا كَذَلِكَ يَرِيهِمُ اللَّهُ
 أَعْمَلُهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ ﴿٣٨﴾

"Waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata, na hali ya kuwa wamekwishaiona adhabu; na yatakatika mafungamano yao. Na watasema wale waliofuata. Laiti tungeweza kurudi tukawakataa wao kama wanavyotukataa sisi! Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Atakavyowaonesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni". (2:166-167)

Kauli ya Allah تعالى:

حَتَّىٰ إِذَا آذَرَكُمَا فِيهَا جَمِيعًا

“Mpaka watakapokusanyika wote humo”. Maana yake: Watakapojumuika wote humo.

قَالَتْ أَحْرَبُهُمْ لَأُولَهُنَّ

“...wa mwisho wao watawasema wa mwanzo wao”.

Maana yake: Wa mwisho wao kuingia, nao ni wafuasi wa hao waliowatangulia wao, wa mwanzo ndio wenye kufuatwa, na kwa kuwa ndio wenye madhambi makubwa kuliko wafuasi wao na kwa hivyo wataingia kabla ya wafuasi wao ambao watawashitaki kwa Allah تعالى katika Siku ya Kiyama kwa sababu hao ndio waliowapoteza mbali na njia sahihi, watasema;

رَبَّنَا هَتُّوْنَا أَضْلُوْنَا فَفَاتِمَا عَذَابًا ضِعْفًا مِّنَ النَّارِ ط

“Mola wetu Mlezi! Hawa ndio waliotupoteza; basi wape adhabu ya Motoni maradufu.”

Maana yake: Waongezee adhabu maradufu. Sawa na Alivyosema Allah تعالى:

يَوْمَ تَقَلُّبُ وَجُوهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يَلَيْتَنَّا أَطَعْنَا اللَّهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَ ﴿٦٦﴾ وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكِبَرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلًا ﴿٦٧﴾ رَبَّنَا ءَاتِهِمْ ضِعْفَيْنِ مِنَ الْعَذَابِ

“Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa katika Moto. Watasema: Laiti tungelimtii Mwenyezi Mungu, na tungelimtii Mtume! Na watasema: Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwatii mabwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio waliotupoteza njia. Mola wetu Mlezi! Wape wao adhabu mara mbili”. (33:66-68)

Kauli ya Allah تعالى:

قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٌ

“Atasema: Itakuwa kwenu nyote maradufu”. Maana yake: Tumekwishayafanya hayo mliyoyaomba, na Tumemlipa kila mmoja kulingana na amali zake. Sawa na Kauli Yake nyingine;

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ زِدْنَهُمْ عَذَابًا

“Wale waliokufuru na kuzuilia njia ya Mwenyezi Mungu Tutawazidishia adhabu juu ya adhabu”. (16:88) na;

وَلِيَحْمِلُوا أَثْقَالَهُمْ وَأَثْقَالًا مَعَ أَثْقَالِهِمْ^ط

“Na hapana shaka wataibeba mizigo yao na mizigo mingine pamoja na mizigo yao”. (29:13) na;

وَمِنَ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ^ط

“...na sehemu ya mizigo ya wale wanaowapoteza bila ya kujua”. (16:25)

وَقَالَتْ أُولَهُنَّ لِأَخْرَجْنَهُنَّ

“Na wa mwanzo wao watawaambia wa mwisho wao”.

Maana yake: Waliofuatwa watawaambia wafuasi wao;

فَمَا كَانَتْ لَكُمْ عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ

“Basi nyinyi pia hamkuwa na ubora kuliko sisi”.

As-Suddi alisema, nyinyi mmepotea kama tulivyopotea sisi¹.

فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ

“Basi onjeni adhabu kwa sababu ya mliyokuwa mkiyachuma”.

Hali hii ni sawa na Alivyojulisha Allah تعالى juu yao katika wakati wa kufufuliwa kwao, katika Kauli Yake;

قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لِلَّذِينَ اسْتَضَعِفُوا أَنَحْنُ صَدَدْنَاكُمْ عَنِ الْهُدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ^ط بَلْ كُنْتُمْ مُجْرِمِينَ ﴿٣٧﴾ وَقَالَ الَّذِينَ اسْتَضَعِفُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرُ الْبَلِيلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ أَندَادًا^ط وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لِمَا رَأَوْا الْعَذَابَ وَجَعَلْنَا الْأَعْنَطَ فِي أَعْتَاقِ الَّذِينَ كَفَرُوا^ط هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٣٨﴾

“Waliotakabari watawaambia wanyonge: Kwani sisi ndio tuliokuzuieni na uwongofu badala ya kukujieni? Bali nyinyi wenyewe ni wakosefu. Na wanyonge watawaambia waliotakabari: Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipokuwa mkituamrisha

¹ At-Tabari 12:420.

tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie washirika. Nao wataficha majuto watakapoiona adhabu. Na Tutaweka makongwa shingoni mwao waliokufuru. Kwani wanalipwa ila kwa waliyokuwa wakiyatenda?" (34:32-33)

إِنَّ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا لَا تُفْتَحُ لَهُمْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ وَلَا يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ حَتَّى يَلِجَ الْجَمَلُ فِي سَمِّ الْخِيَاطِ ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُجْرِمِينَ ﴿٤٠﴾ هُمْ مِنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ وَمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٤١﴾

40. Hakika wale wanaozikanusha Ishara Zetu na wakazifanyia kiburi Hawatafunguliwa milango ya mbingu, wala Hawataingia Peponi mpaka apite ngamia katika tundu ya sindano. Na hivi ndivyo Tunavyowalipa wakosefu.

41. Jahannamu itakuwa kitanda chao na juu yao nguo za moto za kujifunika. Na hivi ndivyo Tunavyowalipa madhalimu". (7:40-41)

Wakadhibishaji Hawatafunguliwa Milango ya Mbinguni, Wala Hawataingia Jannah Abadani.

Kauli ya Allah تعالى: لَا تُفْتَحُ لَهُمْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ

"Hawatafunguliwa milango ya mbingu".

Ilisemwa: Makusudio ni kwamba amali zao njema wala dua hazipandishwi. Waliyasema hayo Mujahid na Sa'id bin Jubayr. Pia Al-'Awfi na 'Ali bin Abu Twalhah ndivyo walivyomnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما¹. Halikadhalika, Ath-Thawri alinukuu kutoka kwa Layth, kutoka kwa 'Ata, kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما². Pia ilisemwa maana yake ni, roho zao hazitafunguliwa milango ya mbinguni. Hayo aliyanukuu Adh-Dhahhak, kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما³. Pia As-Suddi na wengine walisema vivyo hivyo⁴. Haya yanaungwa mkono na aliyoyanukuu Ibn Jariri رحمه الله تعالى kutoka kwa Al-Baraa, kuwa Mtume

¹ At-Tabari 12:422-423.

² At-Tabari 12:422.

³ At-Tabari 12:422.

⁴ At-Tabari 12:422.

﴿﴾ alitaja utolewaji wa roho ya mtu muovu na kuwa itapandishwa kwenda mbinguni, Alisema;

فَيَضَعُونَ بِهَا، فَلَا تُمْرُ عَلَىٰ مَلَأَ مِنَ الْمَلَائِكَةِ إِلَّا قَالُوا مَا هَذِهِ الرُّوحُ الْخَبِيثَةُ؟
فَيَقُولُونَ: فَلَانٌ بِأَفْتَحَ أَسْمَائِهِ الَّتِي كَانَ يُدْعَىٰ بِهَا فِي الدُّنْيَا، حَتَّىٰ يَتَّبِعُوا بِهَا إِلَى
السَّمَاءِ فَيَسْتَفْتِحُونَ بِأَبْهَا لَهُ فَلَا يَفْتَحُ لَهُ

“Basi wanapanda nayo, na haitalipita kundi la Malaika, bali Watauliza, “Roho khabithi hii ni ya nani?” Watajibu, “Ni fulani”, wataitaja kwa jina lililo baya zaidi lililokuwa akiitwa kwalo duniani. Mpaka wanafika mbinguni na kuomba ruhusa ya kufunguliwa mlango wake, lakini hautafunguliwa”.

Kisha Mtume ﴿﴾ akasoma;

لَا تُفْتَحُ لَهُمْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ

“Hawatafunguliwa milango ya mbingu”¹.

Hivi ndivyo alivyoinukuu, nayo ni sehemu ya Hadithi ndefu. Ameinukuu Abu Dawud, An-Nasai na Ibn Majah².

Ibn Jurayj aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

لَا تُفْتَحُ لَهُمْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ

“Hawatafunguliwa milango ya mbingu”.

“Haitafunguliwa kwa ajili ya amali wala roho zao”³. Hii inajumuisha kauli mbili tulizozitaja hapo juu. Allah Aalam. Kauli ya Allah تعالى;

وَلَا يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ حَتَّىٰ يَلِجَ الْجَمَلُ فِي سَمِّ الْخِيَاطِ⁴

“...wala Hawataingia Peponi mpaka apite ngamia katika tundu ya sindano”.

Wameifasiri kwamba ni ngamia dume. Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema ni ngamia

¹ At-Tabari 12:424.

² Abu Dawud 5:114 na An-Nasai 4:87 na Ibn Majah 1:494.

³ At-Tabari 12:423.

⁴ At-Tabari 12:428.

dume⁴. Mujahid na 'Ikrimah walimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa yeye alikuwa akisoma neno *Jamal* kwa kusema *Jummal* kwa maana "Mpaka *Jummal* (kamba nene) ipite katika tundu la sindano"¹. Kauli ya Allah تعالى:

هُم مِّنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ

"Jahannamu itakuwa kitanda chao". Muhammad Al-Quradhi alisema, kwamba ni tandiko.

وَمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ

"...na juu yao nguo za moto za kujifunika". Akasema kwamba ni vya kufunikia². Kadhalika alisema hivyo Adh-Dhahhak bin Muzahim na As-Suddi³.

وَكَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ

"Na hivyo ndivyo Tunavyo walipa madhalimu". (7:42)

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٤٢﴾ وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِّنْ غَلِيٍّ تَجْرِي مِن تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي هَدَانَا لِهَذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَن هَدَانَا اللَّهُ لَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ وَنُودُوا أَن تِلْكَمُ الْجَنَّةُ أُوْرثْتُمُوهَا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾

42. Na wale wanaoamini na wakatenda mema – Hatumkalifishi mtu yeyote ila kwa kiasi cha uwezo wake - hao ndio watu wa Peponi. Wao watadumu humo.

43. Na Tutaondoa chuki vifuani mwao, na mbele yao iwe inapita mito. Na watasema: Alhamdulillah! Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, Ambaye Aliyetuhidi kufikia haya. Wala hatukuwa wenye kuhidika wenyewe ingelikuwa Mwenyezi Mungu Hakutuhidi. Hakika Mitume wa Mola wetu Mlezi walileta Haki. Na watanadiwa kwamba: Hiyo ndiyo pepo mliyorithishwa kwa sababu ya mliyokuwa mkiyafanya.

¹ At-Tabari 12:431.

² At-Tabari 12:436.

³ At-Tabari 12:436.

Maelezo Kuhusu Makazi ya Watu Wema na Hali Zao.

Baada ya kutaja hali za watu waovu, Allah تعالى Alieleza hali za watu wema.

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Na wale wanaoamini na wakatenda mema”.

Maana yake: Nyoyo zao ziliamini na wakafanya amali njema kwa maungo yao, kinyume na wale waliozikufuru Aya za Allah تعالى na kuzifanyia kiburi, Allah تعالى Anatoa angalizo kwa Kusema kuwa suala la Imani na kuifanyia kazi ni jambo jepesi. Alisema;

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١٢٧﴾ وَتَرَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِّنْ غَلٍ

“Na wale wanaoamini na wakatenda mema – hatumkalifishi mtu yeyote ila kwa kiasi cha uwezo wake - hao ndio watu wa Peponi. Wao watadumu humo. Na Tutaondoa chuki vifuani mwao”.

Maana: Husuda na kinyongo. Sawa na Hadithi iliyokusanywa na Al-Bukhari kuwa Abu Sa'id Al-Khudri رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema;

«إِذَا خَلَصَ الْمُؤْمِنُونَ مِنَ النَّارِ حُسِبُوا عَلَى قَنْطَرَةٍ بَيْنَ الْجَنَّةِ وَالنَّارِ فَاقْتَصَّ لَهُمْ مَطَالِمَ كَانَتْ بَيْنَهُمْ فِي الدُّنْيَا حَتَّى إِذَا هُدُّبُوا وَنُقُوا أُذِنَ لَهُمْ فِي دُخُولِ الْجَنَّةِ فَوَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ إِنَّ أَحَدَهُمْ بِمَثَرِ لَيْلٍ فِي الْجَنَّةِ أَدْلُ مِنْهُ بِمَسْكِيهِ كَانَ فِي الدُّنْيَا»

*“Baada ya Waumini kuokolewa dhidi ya Moto watawekwa katika daraja baina ya Jannah na Moto kwa ajili ya kusubiri. Kisha madhambi yaliyotokea baina yao duniani yatahukumiwa. Mpaka baada ya kusafishwa na kutakaswa wataruhusiwa kuingia Jannah. Naapa kwa Yule Ambaye, nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Mmoja wao anaweza kuyapata makazi yake Peponi kwa urahisi zaidi kuliko alivyokuwa duniani”.*¹

As-Suddi aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

¹ Fat'hul Al-Bari 5:115.

وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِّنْ غَلِيٍّ تَجْرِي مِن تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ

“Na Tutaondoa chuki vifuani mwao na mbele yao iwe inapita mito”.

“Watu wa *Jannah* watakapopelekwa Peponi, watakuta mti karibu na mlango wa pepo na chemchem mbili zinatokea shinani. Kisha watakunywa kutokana na kimoja wapo, basi kinyongo kinawatoka vifuani mwao. Hicho ni kinywaji cha kutwaharisha. Wataoga katika mto mwingine, basi mng’ao wa nyuso zao utadhihiri na wala hawatavurugika nywele wala hawatachafuka”¹. An-Nasai na Ibn Marduwyah walinukuu (na maneno ni ya Ibn Marduwyah) kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ alisema;

«كُلُّ أَهْلِ الْجَنَّةِ يَرَى مَقْعَدَهُ مِنَ النَّارِ، يَقُولُ: لَوْلَا أَنَّ اللَّهَ هَدَانِي، فَيَكُونُ لَهُ شُكْرًا، وَكُلُّ أَهْلِ النَّارِ يَرَى مَقْعَدَهُ مِنَ الْجَنَّةِ يَقُولُ: لَوْ أَنَّ اللَّهَ هَدَانِي، فَيَكُونُ لَهُ حَسْرَةً»

“Kila mtu wa *Jannah* atayaona makazi yake ya *Motoni*, na atasema, “Kama Allah تعالى Asingenihidi!” Huko ndiko kutakuwa kushukuru kwake, na kila mtu wa *Motoni* atayaona makazi yake ya *Jannah* na atasema, “Kama Allah تعالى Angelinihidi”. Huko kutakuwa ndiko kujuta kwake”²,

Hii ndiyo sababu Waumini watakapopewa makazi ya *Jannah* yaliyokuwa kwa ajili ya watu wa *Motoni*, wataambiwa, “Hii ni *Jannah* mliyopewa kutokana na amali zenu, mmepata rehema, kuingia *Jannah* na kukaa makazi yenu kulingana na amali zenu. Hii ndiyo maana halisi hapa, kwani *Sahih* Mbili zimenukuu kuwa Mtume ﷺ alisema;

«وَأَعْلَمُوا أَنَّ أَحَدَكُمْ لَنْ يُدْخِلَهُ عَمَلُهُ الْجَنَّةَ»

“Tambueni kwamba amali zenu hazitomuvingiza mmoja wenu *Jannah*”. Wakasema; “Hata wewe ewe Mjumbe wa Allah?” Akasema;

«وَلَا أَنَا إِلَّا أَنْ يَتَّعَمِدَنِي اللَّهُ بِرَحْمَةٍ مِنْهُ وَفَضْلٍ»

“Hata mimi, isipokuwa Allah تعالى Atakaponifunika kwa Rehema na *Fadhila* Zake”.³

¹ At-Tabari 12:439.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:447.

³ Fat’hul Al-Bari 11:300 na Muslim 4:2170.

وَنَادَىٰ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَصْحَابَ النَّارِ أَن قَدْ وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقًّا فَهَلْ وَجَدْتُمْ مَا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا قَالُوا نَعَمْ فَأَذَّنَ مُؤَذِّنٌ بَيْنَهُمْ أَن لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿٤٤﴾ الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا وَهُمْ بِالْآخِرَةِ كَافِرُونَ ﴿٤٥﴾ وَيَبْهَمَانِ سِحَابٌ وَعَلَى الْأَعْرَافِ رِجَالٌ يَعْرِفُونَ كُلًّا بِسِمَتِهِمْ وَنَادَوْا أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَن سَلِّمُوا عَلَيْنَا لَمْ يَدْخُلُوهَا وَهُمْ يَطْمَعُونَ ﴿٤٦﴾ وَإِذَا صُرِفَتْ أَبْصَارُهُمْ تِلْقَاءَ أَصْحَابِ النَّارِ قَالُوا رَبُّنَا لَا تَجْعَلْنَا مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾ وَنَادَىٰ أَصْحَابُ الْأَعْرَافِ رِجَالًا يَعْرِفُونَهُمْ بِسِمَتِهِمْ قَالُوا مَا أَغْنَىٰ عَنْكُمْ جَمْعُكُمْ وَمَا كُنْتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٤٨﴾ أَهْتُوا لَآئِ الَّذِينَ أَقْسَمْتُمْ لَا يَنَالُهُمُ اللَّهُ بِرَحْمَةٍ أَدْخُلُوا الْجَنَّةَ لَا خَوْفٌ عَلَيْكُمْ وَلَا أَنتُمْ تَحْزَنُونَ ﴿٤٩﴾ وَنَادَىٰ أَصْحَابَ النَّارِ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَن أَفِيضُوا عَلَيْنَا مِنَ الْمَاءِ أَوْ مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَهَا عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٥٠﴾ الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَهُمْ لَهْوًا وَلَعِبًا وَغَرَّتْهُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فَالْيَوْمَ نَنسَلُهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هَذَا وَمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا مَجْحَدُونَ ﴿٥١﴾

وَنَادَىٰ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَصْحَابَ النَّارِ أَن قَدْ وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقًّا فَهَلْ وَجَدْتُمْ مَا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا قَالُوا نَعَمْ فَأَذَّنَ مُؤَذِّنٌ بَيْنَهُمْ أَن لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿٤٤﴾ الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا وَهُمْ بِالْآخِرَةِ كَافِرُونَ ﴿٤٥﴾

44. Na watu wa Peponi watawanadia watu wa Motoni: Sisi Tumekuta aliyotuahidi Mola wetu Mlezi kuwa ni kweli. Je, na nyinyi pia mmekuta Aliyokuahidini Mola wenu Mlezi kuwa ni kweli? Watasema: Ndiyo! Basi mtangazaji atawatangazia: Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate waliodhulumu.

45. Wale ambao walikuwa wakizuilia njia ya Mwenyezi Mungu, na wakataka kuipotisha, nao wana ikanusha Akhera.

Watu wa Jahannam Wana Majuto Juu ya Majuto.

Allah تعالى Anaeleza namna watu wa Motoni watakavyotiwa adabu na kukaripiwa watakapokwenda katika makazi yao ya Motoni.

قَدْ وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقًّا فَهَلْ وَجَدْتُمْ مَا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا قَالُوا نَعَمْ

“Sisi tumekuta aliyotuahidi Mola wetu Mlezi kuwa ni kweli. Je,

na nyinyi pia mmekuta aliyokuahidini Mola wenu Mlezi kuwa ni kweli? Watasema: Ndiyo!

Kauli hiyo inadhahirisha uhakika wa jambo hili, pindi watu wa Motoni watakaposema hivyo. Sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Surat As-Swaffaat juu ya khabari ya mtu aliyekuwa na sahibu yake wa kikafiri;

فَاطْلَعَ فَرَّاءُهُ فِي سَوَاءِ الْجَحِيمِ ﴿٥٨﴾ قَالَ تَاللَّهِ إِنْ كِدْتَ لَتُرْدِينَ ﴿٥٩﴾ وَلَوْلَا نِعْمَةُ رَبِّي لَكُنْتُ مِنَ الْمَحْضَرِينَ ﴿٦٠﴾ أَفَمَا نَحْنُ بِمَعْتَبَرِينَ ﴿٦١﴾ إِلَّا مَوْتَتَنَا الْأُولَىٰ وَمَا نَحْنُ بِمُعَدِّينَ ﴿٦٢﴾

“Basi atachungulia amuone katikati ya Jahannamu. Atasema: Wallahi! Ulikaribia kunipoteza. Na lau kuwa si neema ya Mola wangu Mlezi bila ya shaka ningelikuwa miongoni mwa waliohudhurishwa. Je! Sisi hatutakufa, isipokuwa kifo chetu cha kwanza? Wala sisi hatutaadhibiwa”. (37:55-59)

Allah تعالى Atamuadhibu kafiri kwa sababu ya maneno aliyokuwa akiyasema duniani. Kadhalika Malaika watawakemea, watawaambia;

هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تَكْذِبُونَ ﴿١٤﴾ أَفَسِحْرٌ هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تُبْصِرُونَ ﴿١٥﴾ أَصَلَوْهَا فَاصْبِرُوا أَوْ لَا تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ إِنَّمَا تُحْزَنُونَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

“(Waambiwe): Huu ndio ule Moto mliokuwa mkiukanusha! Je! Huu ni uchawi, au hamuoni tu? Uingieni, sawa sawa mstahmili au msistahmili. Hakika mnalipwa kwa mliyokuwa mkiyatenda”. (52:14-16)

Kadhalika Mtume ﷺ aliwakaripia maadui waliouawa na kutupwa kisimani katika siku ya vita vya Badr;

يَا أَبَا جَهْلٍ بِنِ هِشَامٍ وَيَا عُثْبَةَ بِنِ رَبِيعَةَ وَيَا شَيْبَةَ بِنِ رَبِيعَةَ - وَسَمَى رُووسَهُمْ -
هَلْ وَجَدْتُمْ مَا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا فَإِنِّي وَجَدْتُ مَا وَعَدَنِي رَبِّي حَقًّا

“Ewe Abu Jahl bin Hisham! Ewe ‘Utbah bin Rabi’ah! Ewe Shaybah bin Rabi’ah – akawaita viongozi wao kwa majina – Je, Mmeyakuta Aliyokuahidini Mola wenu (Moto) kuwa ni kweli? Kwani mimi nimeyakuta Aliyoniahidi Mola wangu (ushindi) kwamba ni kweli”.

'Umar رضي الله عنه akasema. "Ewe Mjumbe wa Allah! Unawasemesha watu waliokwishakuwa mizoga?" Mtume ﷺ akasema;

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ مَا أَنْتُمْ بِأَسْمَعَ لِمَا أَقُولُ مِنْهُمْ وَلَكِنْ لَا يَسْتَعِينُونَ أَنْ يُجِيبُوا»

*"Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Nyinyi hamuyasikii vyema haya ninayoyasema zaidi yao, lakini hawawezi kujibu"*¹.

Kauli ya Allah تعالى;

فَأَذِّنْ مُؤَذِّنٌ بَيْنَهُمْ

"Basi mtangazaji atawatangazia".

Maana yake: Atajulisha mjulishaji, akapiga mbiu mpiga mbiu.

أَنْ لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ

"Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate waliodhulumu".

Maana: Laana iwafikie, kisha Allah تعالى Akaeleza alama zao kwa Kauli Yake;

الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا

"Wale ambao walikuwa wakizuilia njia ya Mwenyezi Mungu, na wakataka kuipotosha".

Maana yake: Wanawazuilia watu dhidi ya kuifuata njia ya Allah تعالى na sharia Zake na ujumbe waliokuja nao Mitume wa Allah تعالى, na wanataka njia iwe imepotoka, badala ya kuwa iliyonyooka, ili yeyote asiifuate.

وَهُمْ بِالْآخِرَةِ كَافِرُونَ

"...nao wanaikanusha Akhera".

Maana yake: Wanakataa kuwa watakutana na Allah تعالى huko Akhera, yaani wanapinga na kulikadhibisha hilo, hawalisadiki wala hawaliamini. Kwa hivyo, huwa hawajali juu ya kauli na amali zao kwa kuwa hawaikhofii hesabu ya amali zao wala adhabu na kwa kweli hao ndio watu waovu zaidi kwa kauli na kwa amali.

¹ Muslim 3:2203. Hao walikuwa makafiri wa kikuraishi waliouwawa katika vita vya Badr. Maiti zao zilitupwa kisimani.

وَيَبْتَهِمَا حِجَابٌ^٤ وَعَلَى الْأَعْرَافِ رِجَالٌ يَعْرِفُونَ كُلًّا بِسِيمَانِهِمْ^٥ وَنَادَوْا أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَنْ
 سَلِّمُوا عَلَيْنَا لَمْ يَدْخُلُوهَا وَهُمْ يَطْمَعُونَ ﴿٤٦﴾ * وَإِذَا صُرِفَتْ أَبْصَارُهُمْ تِلْقَاءَ أَصْحَابِ
 النَّارِ قَالُوا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾

46. Na baina ya makundi mawili hayo patakuwapo pazia. Na juu ya Mnyanyuko patakuwa watu watakaowajua wote kwa alama zao, na wao watawaita watu wa Peponi. Asalaam Alaykum, Amani juu yenu! Wao bado hawajaingia humo, lakini wanatumai.

47. Na yanapogeuzwa macho yao kuelekea watu wa Motoni, watasema: Mola Mlezi wetu! Usitujaalie kuwa pamoja na watu waliodhulumu.

Al-A'raaf na Watu Wake.

Baada ya Allah تعالى Kutaja mazungumzo baina ya watu wa *Jannah* na wa Motoni, alieleza kuwa baina ya *Jannah* na Motoni kuna kizuizi cha kuwazuia watu wa Motoni wasiende *Jannah*. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa huo ni ukuta ambao Allah تعالى Aliuzungumzia.

فَضْرِبَ بَيْنَهُمْ بِسُورٍ لَهُدًى بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ مِنْ قِبَلِهِ الْعَذَابُ

“Utive baina yao ukuta wenye mlango – ndani yake mna rehema, na nje upande wake wa mbele kuna adhabu”. (57:13)

Nao ni ukuta wa *Al-A'raaf* ambao Allah تعالى Aliuzungumzia kwa kusema;

وَعَلَى الْأَعْرَافِ رِجَالٌ

“Na juu ya Mnyanyuko patakuwa watu”¹. Pia alinukuu, kwa isnadi yake, kutoka kwa As-Suddi kwamba alisema juu ya Kauli ya Allah تعالى;

وَيَبْتَهِمَا حِجَابٌ

“Na baina ya makundi mawili hayo patakuwapo pazia”². Nao ni ukuta, ambao ni *Al-A'raaf*². Mujahid aliema, “*Al-A'raaf* ni kizuizi baina ya *Jannah* na Moto, ni ukuta wenye mlango”.

¹ At-Tabari 12:249.

² At-Tabari 12:249.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa neno *Al-A'raaf* ni wingi wa neno '*Urf*, na Waarabu huita sehemu ya ardhi iliyoinuka juu kuwa ni '*urfan*, kama vile '*Urfud-Diyk* (undu wa jogoo), umeitwa kwa jina '*Urf* kwa sababu ya kuwa kwake juu.

As-Suddi alisema: "Iliitwa *A'raaf* kwa sababu wakazi wake watawajua (*Ya'rifun*) watu.¹ Wakazi wa sehemu hiyo ya *Al-A'raaf* ni wale ambao mema na maovu yao yamekuwa sawa. Hayo ameyasema Hudhaifah رضي الله عنه, Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, Ibn Mas'ud رضي الله عنه na wengine katika *Salaf* na vizazi vya baada yao". Ibn Jariri رحمه الله تعالى alimnukuu Hudhaifah رضي الله عنه kwamba aliulizwa kuhusu wakaazi wa *Al-A'raaf*, akasema, "Ni watu ambao mema na maovu yao yamelingana, hivyo maovu yao yamewanyima sifa za kuingia *Jannah* na mema yao yamewapa sifa za kuepushwa na Moto. Basi watasimamishwa katika ukuta, mpaka Allah تعالى Awahukumu"². Ma'mar alimnukuu Al-Hasan kuwa alisoma Aya hii;

لَمْ يَدْخُلُوهَا وَهُمْ يَطْمَعُونَ

"Wao bado hawajaingia humo, lakini wanatumai".

Akasema, "Wallahi! Allah تعالى Hakuyaweka matumaini hayo katika nyoyo zao kwa sababu ya karama Anazotaka Kuwapatia"³.

Qatadah alisema, "Alikwishakujulisheni juu ya mahala pao hao wenye matumaini"⁴. Kauli Yake;

وَإِذَا صُرِفَتْ أَبْصَارُهُمْ تِلْقَاءَ أَصْحَابِ النَّارِ قَالُوا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ

"Na yanapogeuzwa macho yao kuelekea watu wa Motoni, watasema: Mola Mlezi wetu! Usitujaalie kuwa pamoja na watu waliodhulumu".

Adh-Dhahhak alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, "Watu wa *Al-A'raaf* wakiwatazama watu wa Motoni na wakawajua watasema, "Ewe Mola wetu! Usitujaalie kuwa pamoja na watu madhalimu"⁵.

¹ At-Tabari 12:251.

² At-Tabari 12:249.

³ At-Tabari 12:253.

⁴ Abdur-Razzaq 2:230.

⁵ At-Tabari 12:265.

وَنَادَى أَصْحَابَ الْأَعْرَابِ رِجَالًا يَعْرِفُونَهُمْ بِسِمَتِهِمْ قَالُوا مَا أَغْنَىٰ عَنْكُمْ جَمْعُكُمْ وَمَا كُنْتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٤٨﴾ أَهْتُولَاءِ الَّذِينَ أَقْسَمْتُمْ لَا يَنَالُهُمُ اللَّهُ بِرَحْمَةٍ ۖ أَدْخُلُوا الْجَنَّةَ لَا خَوْفٌ عَلَيْكُمْ وَلَا أَنْتُمْ تَحْزَنُونَ ﴿٤٩﴾

48. Na hao watu wa Mnyanyukoni watawaita watu wanaowajua kwa alama zao. Watasema: Kujumuika kwenu hakukufaeni kitu, wala hicho mlichokuwa mnafanyia kiburi.

49. Je, hawa sio wale mliokuwa mkiwaapia kuwa Mwenyezi Mungu Hatawafikishia rehema. Ingieni Peponi, hapana khofu kwenu, wala hamtahuzunika.

Allah تعالى Anaeleza kuwa watu wa Al-A'raaf watawakaripia baadhi ya wakuu wa washirikina watakaowatambua kwa alama zao Motoni.

مَا أَغْنَىٰ عَنْكُمْ جَمْعُكُمْ

"Kujumuika kwenu hakukufaeni kitu". Maana: Wingi wenu.

وَمَا كُنْتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ

"...wala hicho mlichokuwa mnafanyia kiburi". Maana yake: Wingi wenu na mali zenu hautakuokoeni dhidi ya adhabu ya Allah تعالى bali mmekuwa katika makazi ya adhabu na mateso. 'Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn 'Abbas kuhusu, رضي الله عنهما

أَهْتُولَاءِ الَّذِينَ أَقْسَمْتُمْ لَا يَنَالُهُمُ اللَّهُ بِرَحْمَةٍ ۖ

"Je, hawa sio wale mliokuwa mkiwaapia kuwa Mwenyezi Mungu Hatawafikishia rehema".

Ni watu wa Al-A'raaf, kuwa wataambiwa;

أَدْخُلُوا الْجَنَّةَ لَا خَوْفٌ عَلَيْكُمْ وَلَا أَنْتُمْ تَحْزَنُونَ

"Ingieni Peponi, hapana khofu kwenu, wala hamtahuzunika".

وَنَادَى أَصْحَابَ النَّارِ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَنْ أَيْضُوا عَلَيْنَا مِنَ الْمَاءِ أَوْ مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ

قَالُوا إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَهَا عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٥٠﴾ الَّذِينَ أَخَذُوا دِينَهُمْ لَهْوًا وَلَعِبًا

¹ At-Tabari 12:269.

وَعَزَّتْهُمْ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا ۖ فَالْيَوْمَ نَنسَنَّهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هَذَا وَمَا كَانُوا

بِعَايِنَتِنَا تَجْحَدُونَ ﴿٥٠﴾

50. Na watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi: Tumimieni maji, au chochote Alichokuruzukuni Mwenyezi Mungu. Nao watasema: Hakika Mwenyezi Mungu Ameviharamisha hivyo kwa makafiri.

51. Ambao waliifanya dini yao kuwa ni pumbao na mchezo, na maisha ya dunia yakawadanganya. Basi leo Sisi Tunawasahau kama walivyousahau mkutano wa Siku yao hii, na kwa sababu ya kule kuzikataa Ishara Zetu.

Fadhila za Jannah Zimezuiliwa kwa Watu wa Motoni.

Allah تعالی Anajulisha kuhusu fedheha ya watu wa Motoni na kuomba kwao watu wa Jannah baadhi ya vinywaji na vyakula vyao lakini hawatawapa chochote katika hayo. As-Suddi alisema;

وَتَادَى أَصْحَابِ النَّارِ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَنْ أَفِيضُوا عَلَيْنَا مِنَ الْمَاءِ أَوْ مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ

“Na watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi: Tumimieni maji, au chochote Alichokuruzukuni Mwenyezi Mungu”.

Ni chakula¹. Ath-Thawri رحمه الله تعالی alisema kwamba ‘Uthman Ath-Thaqafi alisema kuwa Sa’id bin Jubayr aliizungumzia aya hii, “Mtu mmoja wapo atamuita baba au kaka yake, na kumuambia, “Mimi nimeteketea, nakuomba unimiminie kiasi fulani cha maji”. Na waumini wataambiwa, “Wajibuni hao”. Watawaambia;

إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَهُمَا عَلَى الْكٰفِرِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Ameviharamisha hivyo kwa makafiri”.²

‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema;

إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَهُمَا عَلَى الْكٰفِرِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Ameviharamisha hivyo kwa makafiri”.

¹ At-Tabari 12:273.

² At-Tabari 12:274.

Inamaanisha vyakula na vinywaji vya *Jannah*¹.

Kisha Allah تعالى Anaeleza wasifu wa makafiri kwa yale waliyokuwa wakiyafanya duniani, kwa kuifanya Dini kuwa ni upuuzi na mchezo na kuhadaiwa kwao na maisha ya duniani na mapambo yake na wakaacha kuifanyia amali Akhera kama walivyoamrisha. Kauli ya Allah تعالى;

فَالْيَوْمَ نَنسَهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هَذَا

“Basi leo Sisi Tunawasahau kama walivyoasahau mkutano wa Siku yao hii”.

Maana: Allah تعالى Atawafanyia kana kwamba Amewasahau, kwa sababu Yeye Ana Ujuzi kamili, hakuna kinachoepuka Elimu Yake, wala Hasahau. Sawa na Kauli Yake;

فِي كِتَابٍ لَا يَضِلُّ رَبِّي وَلَا يَنسَى

“...katika Kitabu. Mola wangu Mlezi Hapotei wala hasahau”. (20:52)

Allah تعالى Atayasema haya kwa njia ya ulinganifu wa malipo. Alisema;

نَسُوا اللَّهَ فَنَسِيَهُمْ

“Wamemsahau Mwenyezi Mungu, basi na Yeye pia Amewasahau”.

(9:67) Na;

كَذَلِكَ أَتَتْكَ آيَاتُنَا فَنَسِيَتْهَا ۖ وَكَذَلِكَ الْيَوْمَ تُنْسَى

“(Mwenyezi Mungu) Atasema: Ndivyo vivyo hivyo. Zilikufikia ishara Zetu, nawe ukazisahau; na kadhalika leo unasahauliwa”.

(20:126) na;

وَقِيلَ الْيَوْمَ نَنسَنُكُمْ كَمَا نَسَيْتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَذَا

“Na itasemwa: Leo Tunakusahauni kama nyinyi mlivyosahau mkutano wa siku yenu hii”. (45:34)

Al-'Awfi alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما juu ya Kauli ya Allah تعالى;

فَالْيَوْمَ نَنسَهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هَذَا

“Basi leo Sisi Tunawasahau kama walivyoasahau mkutano wa Siku yao hii”.

¹ At-Tabari 12:274.

Akasema, "Allah تعالى Atawasahau katika kheri na Hatawasahau katika shari". 'Ali bin Abu Twalhah alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akisema, "Atawaacha kama walivyoiacha siku yao hii ya kukutana". Mujahid alisema, "Tutawaacha Motoni". As-Suddi alisema, "Tutawaacha katika rehema kama walivyoacha kujishughulisha na siku yao hii". Na katika *Sahih* kuna Hadithi inayosema kuwa Allah تعالى Atamuambia mja katika Siku ya Kiyama;

«أَلَمْ أَرْوِّجْكَ؟ أَلَمْ أُحْرِمْكَ؟ أَلَمْ أُسَخِّرْ لَكَ الْخَيْلَ وَالْإِبِلَ وَأَذْرَكَ تَرَاسُ وَتَرْبِيعُ؟
فَيَقُولُ: بَلَى، فَيَقُولُ: أَطَنَنْتَ أَنَّكَ مُلَائِي؟ فَيَقُولُ: لَا، فَيَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: فَالْيَوْمَ
أَنْسَاكَ كَمَا نَسِيتَنِي»

"Je, Sikukuozesha? Sijakukirimu? Sijakudhalilishia farasi na ngamia na kukuruhusu kuwa kiongozi na mlezi?" Atasema, "Ndiyo". Allah تعالى Atamuuliza, "Ulidhani utakutana na Mimi?" Atajibu, "Hapana". Allah تعالى Atasema, "Basi, leo Nitakusahau kama ulivyonisahau".¹

* * *

وَلَقَدْ جَعَلْنَاهُمْ بِكِتَابٍ فَصَلَّنَاهُ عَلَىٰ عِلْمٍ هُدًى وَرَحْمَةً
 لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾ هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا تَأْوِيلَهُ ۗ يَوْمَ يَأْتِي
 تَأْوِيلَهُ يَقُولُ الَّذِينَ نَسُوهُ مِنْ قَبْلُ قَدْ جَاءَتْ رُسُلُ
 رَبِّنَا بِالْحَقِّ فَهَلْ لَنَا مِنْ شُفَعَاءَ فَيَشْفَعُوا لَنَا أَوْ نُرَدُّ
 فَنَعْمَلْ غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۗ قَدْ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ وَضَلَّ
 عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٥٣﴾ إِنَّ رَبَّكُمْ اللَّهُ
 الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ
 عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ
 وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ
 تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾ أَدْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا
 وَخُفْيَةً ۗ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿٥٥﴾ وَلَا تُفْسِدُوا
 فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا وَادْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا ۗ إِنَّ
 رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِّنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٦﴾

وَلَقَدْ جَعَلْنَاهُمْ بِكِتَابٍ فَصَلَّنَاهُ عَلَىٰ
 عِلْمٍ هُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾
 هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا تَأْوِيلَهُ ۗ يَوْمَ يَأْتِي
 تَأْوِيلَهُ يَقُولُ الَّذِينَ نَسُوهُ مِنْ قَبْلُ
 قَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ فَهَلْ
 لَنَا مِنْ شُفَعَاءَ فَيَشْفَعُوا لَنَا أَوْ نُرَدُّ
 فَنَعْمَلْ غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۗ قَدْ
 خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا
 كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٥٣﴾

**52. Na hakika Tumewaletea
 Kitabu Tulichokipambanua
 kwa ilimu, uwongofu na
 rehema kwa watu wenye
 kuamini.**

**53. Je, lipo wanalolingojea
 isipokuwa matokeo yake?
 Siku yatapofika matokeo**

yake watasema wale waliokusahau: Kweli Mitume wa Mola Mlezi wetu walileta Haki! Je, tunao waombezi ili watuombe? Au turudishwe ili tufanye yasiyokuwa yale tuliyo kuwa tukiyafanya? Bila ya shaka wamejikhasiri nafsi zao, na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua.

¹ Muslim 4:2279.

Washirikina Hawatapata Nafasi ya Kutoa Udhuru wao

Allah تعالى Anasema Hajawaachia udhuru washirikina, kwani Aliwapelekea Mtume pamoja na Kitabu alichokuja nacho Mtume ﷺ na kwamba kinabainisha na kina ufafanuzi. Sawa na Kauli Yake nyingine;

كِتَابٌ أَحْكَمَتْ آيَاتُهُ ثُمَّ فُصِّلَتْ

“Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimewekwa wazi, kisha zikapambanuliwa”. (11:1)

Kauli ya Allah تعالى;

فَصَّلْنَاهُ عَلَىٰ عِلْمٍ

“Na hakika Tumewaitea Kitabu Tulichokipambanua kwa ilimu”.

Maana: Tuna ujuzi kamili juu ya Tuliyoafafanua ndani yake. Na Kauli Yake;

أَنْزَلَهُ بِعِلْمِهِ

“Ameyateremsha kwa Kujua Kwake”. (4:166)

Kusudio ni kwamba, pindi Allah تعالى Alipoeleza kuhusu khasara watakyoipata huko Akhera, Alieleza kuwa Yeye Aliwapelekea Mitume na Vitabu duniani. Na Kauli Yake nyingine;

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ تَبْعَثَ رَسُولًا

“Wala Sisi Hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume”. (17:15)

Na kwa ajili hii, Alisema;

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا تَأْوِيلَهُ

“Je, lipo wanalilingoja isipokuwa matokeo yake?”

Maana: Adhabu, mateso, *Jannah* na Moto, kwa mujibu wa Mujahid na wengine¹.

Kauli ya Allah تعالى;

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا تَأْوِيلَهُ

“Siku yatapofika matokeo yake”. Maana yake: Katika Siku ya Kiyama, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما².

¹ At-Tabari 12:479.

² At-Tabari 12:479.

يَقُولُ الَّذِينَ كَسَبُوا مِنْ قَبْلُ

"...watasema wale waliokusahau".

Maana: Waliacha kuifanya amali, na wakaisahau wakiwa duniani.

قَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ فَهَلْ لَنَا مِنْ شُفَعَاءَ فَيَشْفَعُوا لَنَا

"Kweli Mitume wa Mola Mlezi wetu walileta Haki! Je, tunao waombezi ili watuombe?"

Ili watuokoe kutoka mahali tulipo.

أَوْ نُرَدُّ

"Au turudishwe". Duniani.

فَتَعْمَلْ غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ

"...ili Tufanye yasiyokuwa yale tuliyokuwa tukiyafanya?"

Sawa na Kauli Yake nyingine;

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وَقَفُوا عَلَى النَّارِ فَقَالُوا يَلَيْتُنَا نُرَدُّ وَلَا نُكَذِّبُ بِمَا يَنْتِ رَبَّنَا وَنَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٧﴾

بَلْ بَدَأَهُمْ مَا كَانُوا يُخْفُونَ مِنْ قَبْلُ وَلَوْ رُدُّوا لَعَادُوا لِمَا بُوْهُ عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٦٨﴾

"Na ungeona watakaposimamishwa kwenye Moto wakawa wanasema: Laiti tungelirudishwa, wala hatutakukanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni mwa Waumini. Bali yamewadhahirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangelirudishwa bila ya shaka wangeparejea yale yale waliyokatazwa. Na hakika hao ni waongo". (6:27-28)

Sawa na Alivyosema hapa;

قَدْ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ وَصَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ

"Bila ya shaka wamejikasiri nafsi zao, na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua".

Maana: Wamepata khasara kwa kuingia kwao Motoni na kukaa humo milele.

وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ

“..na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua”.

Maana yake: Yamewatoka waliyokuwa wakiyaabudu ghairi ya Allah تعالى, basi hayatawanusuru wao wala kuwaombea, wala hayatawaokoa kutokana na jambo lililowakumba.

إِنَّ رَبَّكُمْ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ
يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ
الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾

54. Hakika Mola Mlezi wenu ni Mwenyezi Mungu Aliyeziumba mbingu na Ardhi katika siku sita. Kisha Akatawala juu ya Kiti cha Enzi. Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua, na mwezi, na nyota zinazotumika kwa Amri Yake. Fahamuni! Kuumba na Amri ni Zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.

Ulimwengu Uliumbwa Katika Siku Sita.

Allah تعالى Anaeleza kwamba Yeye Aliuumba ulimwengu ikiwa ni pamoja na mbingu zake na ardhi na vilivyo baina yake, katika muda wa siku sita kama Alivyoyaeleza hayo katika Ayah zaidi ya moja katika Qur'an. Siku sita ni Jumapili, Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Al-Khamis na Ijumaa. Ijumaa ndiyo siku ambayo viumbe wote waliumbwa, akiwemo Adam عليه السلام. Walikhitilafiana juu ya siku hizo ni sawa na siku zetu hizi kama inavyofahamika hilo haraka inavyokuja akilini mwetu, au ni sawa na miaka elfu moja, kama alivyotaarifu Mujahid¹, Imamu Ahmad bin Hanbal رحمه الله تعالى na katika Riwaya ya Adh-Dhahhak aliyomnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما. Ama kuhusu Jumamosi hakuna kilichoumbwa siku hiyo, kwani ni siku ya sabato na imeitwa kwa jina la *As-Sabt* kusimamisha au kukata.

¹ At-Tabari 12:482.

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema, Mtume ﷺ aliniambia;

«خَلَقَ اللهُ، [عَزَّ وَجَلَّ]، التُّرْبَةَ يَوْمَ السَّبْتِ، وَخَلَقَ فِيهَا الْجِبَالَ يَوْمَ الْأَحَدِ، وَخَلَقَ الشَّجَرَ يَوْمَ الْاِثْنَيْنِ، وَخَلَقَ الْمَكْرُوهَ يَوْمَ الثَّلَاثَاءِ، وَخَلَقَ الثُّورَ يَوْمَ الْأَرْبَعَاءِ، وَبَثَّ فِيهَا الدَّوَابَّ يَوْمَ الْخَمِيسِ، وَخَلَقَ آدَمَ، عَلَيْهِ السَّلَامُ، بَعْدَ الْعَصْرِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ، فِي آخِرِ الْخَلْقِ، فِي آخِرِ سَاعَةٍ مِنْ سَاعَاتِ الْجُمُعَةِ، فِيمَا بَيْنَ الْعَصْرِ إِلَى اللَّيْلِ».

*“Allah Aliumba udongo siku ya Jumamosi, na Akaiumba humo milima katika siku ya Jumapili, Akaiumba miti katika siku ya Jumatatu, Akaumba mambo ya karaha katika siku ya Jumanne, Akaumba nuru katika siku ya Jumatano, Akaeneza humo wanyama katika siku ya Al-Khamis, na Akamuumba Adam baada ya Al-Asr katika siku ya Ijumaa. Yeye ndiye kiumbe wa mwisho Kuumbwa katika saa ya mwisho ya siku ya Ijumaa, katika muda ulio baina ya Al-Asr na usiku”.*¹

Tafsiri ya Istawaa

Ama Kauli ya Allah تعالى;

ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ

“Kisha Akakaa juu ya Kiti cha Enzi”.

Kuhusu maana ya neno *“Istiwaa”* Watu wana maoni mengi sana yenye kupingana kuhusu maana yake lakini hapa si mahala pa kuyaeleza kwa kirefu, bali tutapita njia ya watu wema waliotangulia, kama vile Malik, Al-Awzai, Ath-Thawri, Al-Layth bin Sa'd, Ash-Shafi, Ahmad, Is-haq bin Rawayh na Maimamu wengine wa Kiislamu, wa zamani na wa sasa رضي الله عنهم. Na tunaipitisha maana yake dhahiri pasi na kujadili undani wake au kushabihisha (na sifa za viumbe) au kurekebisha au kuikana (kwa njia na kwa namna yoyote). Na tunaamini kwamba maana inayowajia wale wanaomshabihisha na viumbe ni ya kuikataa, kwani hakuna chenye kumithilishwa na Allah تعالى;

¹ Ahmad 2:327 na Muslim na. 2149.

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۚ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona”. (42:11)

Bali ni kama walivyosema Maimamu, kama vile Nu'aim Ibn Hammad Al-Khuza'iy رحمه الله تعالى, Sheikh wa Imamu Al-Bukhari: “Mwenye kumshabihisha Allah تعالى na viumbe Wake, atakuwa amekufuru, na atakayezipinga Sifa za Allah تعالى Alizojielezea Nafsi Yake, atakuwa amekufuru, wala hakuna ufananishaji katika Alivyojielezea Allah تعالى Nafsi Yake, wala aliyoeleza Mtume Wake ﷺ juu Yake. Yeyote anayezithibitisha Sifa za Allah تعالى zilizoelezwa na Ayah dhahiri na Hadithi *Sahih* katika njia inayolingana na Utukufu wa Allah تعالى na akakanusha dhidi ya kuwepo upungufu kwa Allah تعالى atakuwa amepita njia ya uongofu”.

Usiku na Mchana ni Miongoni mwa Alama za Allah تعالى.

Kauli ya Allah تعالى;

يُغْشَى اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا

“Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi”. Maana: Giza la usiku linaondoka kwa mwangaza wa mchana, na kila kimoja katika hivyo viwili hukifunika kingine haraka haraka, yaani upesi, hakichelewi bali kikiondoka hiki kinafuata hiki. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَأَيَّةٌ لَهُمُ اللَّيْلُ نَسْلَخُ مِنْهُ النَّهَارَ فَإِذَا هُمْ مُظْلِمُونَ ﴿٣٧﴾ وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا
ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٣٨﴾ وَالْقَمَرَ قَدَرْنَاهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ الْقَدِيمِ ﴿٣٩﴾
لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٤٠﴾

“Na usiku ni ishara kwao. Tunauvua humo mchana, mara wao wanakuwa gizani. Na jua linakwenda kwa kiwango chake. Hayo ni makadirio ya Mwenye Nguvu Mwenye Kujua. Na mwezi Tumeupimia vituo, mpaka unakuwa kama karara kongwe. Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao”. (36:37-40)

Kauli ya Allah تعالى;

وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ

“...wala usiku kuupita mchana”. (36:40)

Maana: Haupitwi na muda na kuchelewa, bali unaufuatia, bila ya kuwahi. Kwa ajili hii Allah تعالى Alisema;

يَطْلُبُهُ حَيْثُهَا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهٖ

“Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua, na mwezi, na nyota zinazotumika kwa Amri Yake”.

Maana yake: Vyote viko chini ya Amri, Mamlaka na Kutaka Kwake. Na kwa minajili hii Alisema;

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ

“Fahamuni! Kuumba na Amri ni Zake”. Maana: Miliki na Uamuzi.

تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

“Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote”. Na,

تَبَارَكَ الَّذِي جَعَلَ فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا

“Ametukuka Aliyezijaalia nyota mbinguni”. (25:61)

Abu Dardaa رضي الله عنه alisoma dua, ambayo pia imerufaishwa kwa Mtume ﷺ;

«اللَّهُمَّ لَكَ الْمُلْكُ كُلُّهُ وَلَكَ الْحَمْدُ كُلُّهُ وَإِلَيْكَ يُرْجَعُ الْأَمْرُ كُلُّهُ، أَسْأَلُكَ مِنَ الْخَيْرِ كُلِّهِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الشَّرِّ كُلِّهِ»

“Ewe Allah! Ufalme wote ni Wako, Sifa zote ni Zako na Kwako Wewe linarejea kila jambo. Nakuomba kila la kheri na najikinga Kwako dhidi ya kila la shari”.

ادْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿٦٠﴾ وَلَا تُفْسِدُوا فِي

الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا وَادْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا إِنَّ رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِّنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٦١﴾

55. Muombeni Mola wenu Mlezi kwa unyenyekevu na kwa siri. Hakika Yeye Hawapendi warukao mipaka.

56. Wala Msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwishatengenezwa. Na muombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanaofanya mema.”

Uhamasishaji wa Kuomba Dua kwa Allah تعالى.

Allah تعالى Aliwaelekeza waja Wake juu ya kumuomba Yeye kwani kufanya hivyo kutawahakikishia maslahi yao ya dunia na Akhera yao.

أَدْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً

“Muombeni Mola wenu Mlezi kwa unyenyekevu na kwa siri”.

Imesemwa: Maana yake ni kwa udhalili, unyenyekevu na kwa siri. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَأَذْكُرْ رَبَّكَ فِي نَفْسِكَ

“Na mkumbuke Mola Mlezi wako nafsini mwako”. (7:205)

Sahih Mbili zimenukuu Hadithi ya Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه, kuwa alisema, “Watu walipaza sauti katika dua zao, basi Mtume ﷺ alisema;

«أَيُّهَا النَّاسُ ارْبِعُوا عَلَى أَنْفُسِكُمْ فَإِنَّكُمْ لَا تَدْعُونَ أَصَمًّا وَلَا غَائِبًا إِنَّ الَّذِي تَدْعُونَ سَمِيعٌ قَرِيبٌ»

“Enyi watu! Chukulieni sahali katika nafsi zenu, kwani nyinyi hamumuombi kiziwi wala aliye mbali. Hakika mnayemuomba ni Msikivu, Aliye karibu”.¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema;

تَضَرُّعًا

“...kwa unyenyekevu”.

Maana yake: Kwa kujidhalilisha na kunyenyekea na kwa kumtii Yeye.

وَخُفْيَةً

“...na kwa siri”.

Maana: Kwa unyenyekevu wa nyoyo zenu na yakini juu ya kumpwekesha Kwake na Ungu Wake, si kuomba kwa sauti kwa nia ya ria.²

¹ Fat'hul Al-Bari 11:191 na Muslim 4:2074.

² At-Tabari 12:485.

Kukatazwa Kuchupa Mipaka Katika Dua.

Imetaarifiwa kuwa 'Ata Al-Khurasani alisema kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akiieleza juu ya Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّهُ لَا تُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ

“Hakika Yeye Hawapendi warukao mipaka”.

Katika dua na vinginevyo¹. Na Abu Mijlaz ameieleza Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّهُ لَا تُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ

“Hakika Yeye Hawapendi warukao mipaka”.

Kwamba asiombe apewe hadhi kama ya Mitume². Imamu Ahmad alimnukuu Abu Ni'amah kuwa alisema 'Abdullah bin Mughaffal alimsikia mwanaye akisema, “Ewe Allah! Mimi Nakuomba kasri jeupe kuumeni kwa *Jannah*, nitakapoingia”. Akasema, “Ewe Mwanangu! Muombe Allah تعالى Akupe *Jannah* na Akukinge na Moto, kwani mimi nilimsikia Mtume ﷺ akisema;

«يَكُونُ قَوْمٌ يَغْتَدُونَ فِي الدَّعَاءِ وَالطَّهْوَرِ»

“Watakuja watu wanaopitiliza katika dua na twahara”³.

Pia hivi ndivyo alivyonukuu Ibn Majah⁴ na Abu Dawud⁵, na isnadi yake ni *Hasan*, haina tatizo. *Allah Aalam*.

Kukatazwa Kufanya Uharibifu Ardhini.

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا

“Wala Msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwishatengenezwa”. (5:56)

¹ At-Tabari 12:486.

² At-Tabari 12:486.

³ Ahmad 5:55.

⁴ Ibn Majah 2:2171.

⁵ Abu Dawud 1:73.

Allah تعالی Anakataza uharibifu ardhini, hasa uharibifu unaotokea baada ya utengemavu. Wakati masuala yako katika hali njema, kisha uharibifu ukatokea, basi utawaletea madhara makubwa waja wa Allah تعالی, basi Allah تعالی Akayakataza hayo na Akaamuru kumuabudu Yeye, kumuomba, kumnyenyekea na kumdhalilikia Yeye. Alisema;

وَأَدْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا

“Na muombeni kwa kuogopa na kwa kutumai”.

Maana yake: Kwa kuyahofia Aliyo nayo, miongoni mwa adhabu kali, na kutumai Aliyo nayo katika malipo tele.

إِنَّ رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِّنَ الْمُحْسِنِينَ

“Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanaofanya mema”.

Maana yake: Rehema Zake ni kwa ajili watenda mema, ambao wanafuata Amri Zake na kuacha Aliyoyakataza. Sawa na Kauli ya Allah تعالی;

وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ فَسَأَكْتُمِبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ

“Na rehema Yangu imeenea kila kitu. Lakini Nitawaandikia khasa wanaomchamungu”. (7:156)

Matwar Al-Warraaq alisema, “Pateni ahadi ya Allah تعالی, kwa kumtii, kwani Yeye Alipitisha hukumu kuwa Rehema Zake ziko karibu na watenda wema”. Abu Hatim aliikusanya kauli hii¹.

* * *

¹ Ibn Majah 5:501.

وَهُوَ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ^ط
 حَتَّىٰ إِذَا أَقْلَّتْ سَحَابًا ثِقَالًا سُقْنَهُ لِبَلَدٍ مَّيِّتٍ فَأَنْزَلْنَا بِهِ
 الْمَاءَ فَأَخْرَجْنَا بِهِ مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ^ع كَذَٰلِكَ نُخْرِجُ
 الْمَوْتَىٰ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٥٧﴾ وَالْبَلَدُ الطَّيِّبُ يَخْرِجُ
 نَبَاتَهُ بِإِذْنِ رَبِّهِ^ط وَالَّذِي حَبَّتْ لَا يَخْرِجُ إِلَّا نَكْدًا^ع
 كَذَٰلِكَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَشْكُرُونَ ﴿٥٨﴾ لَقَدْ
 أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَقَالَ يَنْقُورِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ
 مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥٩﴾
 قَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِهِ إِنَّا لَنَرُكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٦٠﴾
 قَالَ يَنْقُورِ لَيْسَ بِي ضَلَالَةٌ وَلَكِنِّي رَسُولٌ مِنْ رَبِّ
 الْعَالَمِينَ ﴿٦١﴾ أُيْلِغُكُمْ رِسَالَتِ رَبِّي وَأَنْصَحُ لَكُمْ
 وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٢﴾ أَوْعَجِبْتُمْ أَنْ
 جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِنْ رَبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِنْكُمْ لِيُنذِرَكُمْ
 وَلِتُنذِرُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٦٣﴾ فَكَذَّبُوهُ فَأَنْجَيْنَاهُ وَالَّذِينَ
 مَعَهُ فِي الْفُلْكِ وَأَغْرَقْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا^ع إِنَّهُمْ
 كَانُوا قَوْمًا عَمِينَ ﴿٦٤﴾

وَهُوَ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا
 بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ^ط حَتَّىٰ إِذَا أَقْلَّتْ
 سَحَابًا ثِقَالًا سُقْنَهُ لِبَلَدٍ مَّيِّتٍ
 فَأَنْزَلْنَا بِهِ الْمَاءَ فَأَخْرَجْنَا بِهِ مِنْ
 كُلِّ الثَّمَرَاتِ^ع كَذَٰلِكَ نُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ
 لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٥٧﴾ وَالْبَلَدُ
 الطَّيِّبُ يَخْرِجُ نَبَاتَهُ بِإِذْنِ رَبِّهِ^ط
 وَالَّذِي حَبَّتْ لَا يَخْرِجُ إِلَّا نَكْدًا^ع
 كَذَٰلِكَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ
 يَشْكُرُونَ ﴿٥٨﴾

57. Na Yeye Ndiye Anaye-
 peleka pepo (za kuvuma)
 kuwa ni bishara kabla ya
 kufika Rehema Yake. Hata
 hizo pepo zinapobeba
 mawingu mazito Tunaya-
 chungu mpaka kwenye nchi
 iliyokufa. Kisha Tunate-
 remsha kwayo maji, ndio
 kama hivyo Tukatolesha
 kila aina ya matunda. Basi,

hali kadhalika ndivyo Tunavyowafufua wafu, ili mpate kukumbuka.

58. Na ardhi njema, yenye udongo wa rutuba, hutoa mimea yenye kukua
 vizuri yenye uhai kwa idhini ya Mola Mlezi wake. Na ardhi mbaya haitoi ila
 mimea michache, isiyo kuwa na faida, tena kwa shida. Na hivyo ndivyo
 Tunavyozipambanua ishara (Aya) kwa watu wanaoshukuru.

Miongoni mwa Alama za Allah تعالى ni Kuteremsha Mvua na Kuleta Matunda.

Baada ya Allah تعالى Kutaja kuwa Yeye Aliumba mbingu na ardhi, na kuwa Yeye Ndiye Mmiliki, Hakimu, Mwendeshaji Aliyevdhalilisha vitu (kwa mwanadamu), kisha Akaeleza kumuomba Yeye, kuwa Yeye ni Muweza wa kila kitu, Allah تعالى Alijulisha kuwa Yeye Ndiye Mwenye Kuruzuku na kwamba Atawafufua wafu katika Siku ya Kiyama. Hapa Allah تعالى Anasema Yeye Hupeleka upepo ambao unayaeneza mawingu ya mvua, yaani huenea upepo huo mawingu mazito yaliyobeba maji. Wengine hulisoma neno “Nushra” kwa “Bushra”.

Hiyo ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنْ آيَاتِنَا أَنْ يُرْسِلَ الرِّيَّاحَ مُبَشِّرَاتٍ

“Na katika ishara Zake ni Kuzituma pepo ziletazo bishara njema”.

(30:46)

Kauli ya Allah تعالى:

بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ

“...kabla ya kufika rehema Yake”.

Maana: Kabla ya mvua. Sawa na Alivyosema;

وَهُوَ الَّذِي يُزِيلُ أَغْصَانَهُ مِنْ بَعْدِ مَا قَنَطُوا وَيَنْشُرُ رَحْمَتَهُ ۗ وَهُوَ الْوَلِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٤٨﴾

“Naye Ndiye Anayeiteremsha mvua baada ya wao kuisha kata tamaa, na Hueneza rehema Yake. Naye Ndiye Mlinzi Mwenye Kuhimidiwa”. (42:28) na;

فَأَنْظُرْ إِلَى آثَارِ رَحْمَتِ اللَّهِ كَيْفَ نُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ لَمُعْجِزٌ لِّلْمُوتَىٰ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٥٠﴾

“Basi ziangalie athari za Rehema ya Mwenyezi Mungu, jinsi Anavyoihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Basi hakika Huyo Ndiye bila ya shaka Mwenye Kuhuisha wafu. Na Yeye ni Muweza wa kila kitu”. (30:50) Na;

حَتَّىٰ إِذَا أَقْلَّتْ سَحَابًا ثِقَالًا

“Hata hizo pepo zinapobeba mawingu mazito”.

Maana: Pepo zitakapobeba mawingu mazito kutokana na maji yaliyomo humo, yanakuwa karibu zaidi na ardhi. Kauli ya Allah تعالى;

سُقْنَهُ لِبَلَدٍ مَّيْتٍ

“...Tunayachunga mpaka kwenye nchi iliyokufa”.

Maana: Ardhi iliyokufa, kavu, isiyokuwa na mimea.

وَأَيُّهُمُ الْأَرْضُ الْمَيِّتَةُ أَحْيَيْنَاهَا

“Na Ishara hiyo kwao – ardhi iliyokufa, nasi Tukaifufua”. (36:33)

Na kwa ajili hii Allah تعالى Alisema;

فَأَخْرَجْنَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ كَذَلِكَ نُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ

“...hivyo Tukatolesha kila aina ya matunda. Basi, hali kadhalika Tunavyowafufua wafu”.

Maana yake: Kama ambavyo Tumeihisha ardhi hii baada ya kufa kwake, ndivyo pia katika Siku ya Kiyama, Tutakavyoihisha miili baada ya kugeuka na kuwa vumbi, Allah تعالى Atateremsha mvua itakayonyesha kwa muda wa siku arubaini, na miili itaota makaburini mwao, kama mbegu inavyoota ardhini. Maana hii imetajwa sehemu nyingi katika Qur'an ambapo Allah تعالى Anapiga mfano wa Siku ya Kiyama, kwa kuihisha ardhi baada ya kufa kwake, na kwa ajili hii Alisema;

لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

“...ili mpate kukumbuka”. Kauli ya Allah تعالى;

وَالْبَلَدُ الطَّيِّبُ يَخْرِجُ نَبَاتُهُ بِإِذْنِ رَبِّهِ

“Na ardhi njema, yenye udongo wa rutuba, hutoa mimea yenye kukua vizuri yenye uhai kwa idhini ya Mola Mlezi wake”.

Maana yake: Ardhi njema huotesha mimea kwa haraka na vyema. Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

وَأُنَبِّتَهَا تِبَابًا حَسَنًا

“...na Akamkuza makuzo mema”. (3:37)

وَالَّذِي حَبُتْ لَا يَخْرُجُ إِلَّا نَكِدًا

“Na ardhi mbaya haitoi ila mimea michache, isiyo kuwa na faida, tena kwa shida”.

Mujahid na wengine, kama vile As-Sibakh, pia walisema hivyo.¹

Al-Bukhari alimnukuu Abu Musa رضي الله عنه kuwa alisema, Mtume ﷺ alisema;

«مَثَلُ مَا بَعَثَنِي اللَّهُ بِهِ مِنَ الْعِلْمِ وَالْهُدَى كَمَثَلِ الْعَيْثِ الْكَثِيرِ أَصَابَ أَرْضًا فَكَانَتْ مِنْهَا نَقِيَّةٌ قِيلَتِ الْمَاءَ فَأَنْبَتَتِ الْكَلَأَ وَالْعُشْبَ الْكَثِيرَ وَكَانَتْ مِنْهَا أَجَادِبُ أَمْسَكَتِ الْمَاءَ فَتَنَعَ اللَّهُ بِهَا النَّاسَ فَشَرِبُوا وَسَقَوْا وَزَرَعُوا وَأَصَابَ مِنْهَا طَائِفَةٌ أُخْرَى إِنَّمَا هِيَ قِيَعَانٌ لَا تُمْسِكُ مَاءً وَلَا تُنْبِتُ كَلَأً، فَذَلِكَ مَثَلُ مَنْ فَقَهُ فِي دِينِ اللَّهِ وَنَفَعَهُ مَا بَعَثَنِي اللَّهُ بِهِ فَعَلِمَ وَعَلَّمَ وَمَثَلُ مَنْ لَمْ يَرْفَعْ بِذَلِكَ رَأْسًا وَلَمْ يَقْبَلْ هُدَى اللَّهِ الَّذِي أُرْسِلْتُ بِهِ»

“Mfano wa elimu na uongofu alionituma Allah تعالى kwa ajili Yake ni kama mvua nyingi iliyoifikia ardhi ambayo sehemu yake ina rutuba na ikayasharabu maji hayo na kuotesha mimea na nyasi kwa wingi. Na sehemu nyingine ya ardhi ilikuwa ngumu na ikayahifadhi maji hayo, Allah تعالى Akawanufaisha watu kwa maji hayo, kwa kuyanywa, kunywesha wanyama, kumwagilia katika kilimo. Na sehemu nyingine ya ardhi hiyo haina rutuba, na haikuweza kuhifadhi maji wala kuotesha mimea. Mfano wa kwanza ni wa mtu anayeifahamu Dini ya Allah تعالى na yakamnufaisha yale Allah تعالى Aliyonituma kwayo, akajifundisha na kuwafundisha wengine. Na mwingine ni mfano wa mtu asiyejali wala hakubali kuupokea uongofu niliotumwa nao kutoka kwa Allah تعالى.”²

¹ At-Tabari 12:497.

² Fat’hul Al-Bari 1:211.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَقَالَ يَنْقُورِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِن إِلَهٍ غَيْرُهُ ۖ إِنِّي أَخَافُ
 عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥٧﴾ قَالَ الْمَلَأُ مِن قَوْمِهِ إِنَّا لَنَرْنَكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٥٨﴾
 قَالَ يَنْقُورِ لَيْسَ بِي ضَلَالَةٌ وَلَكِنِّي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٩﴾ أُبَلِّغُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي
 وَأَنْصَحُ لَكُمْ وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٠﴾

59. Tulimpeleka Nuhu kwa kaumu yake, naye akasema: Enyi kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mola ila Yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyu kuu.

60. Wale watukufu katika kaumu yake wakasema: Hakika sisi tunakuona wewe umo katika upotofu ulio dhahiri.

61. Akasema: enyi watu wangu! Mimi simo katika upotofu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.

62. Ninakufikishieni ujumbe wa Mola Mlezi wangu, na nina kunasihini; na ninayajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua nyinyi.

Kisa cha Nuhu عليه السلام na Watu Wake.

Baada ya Allah تعالی kutaja kisa cha Adam عليه السلام mwanzoni mwa Sura hii na mambo yanayofungamana na habari hiyo na yaliyosababishwa nayo, Aliingia katika Kutaja visa vya Mitume, kwa kuanza na wa kwanza na kuendelea. Alianza Kumtaja Nuh عليه السلام, kwani huyo ni Mtume wa kwanza aliyetumwa na Allah تعالی kwa watu wa duniani, baada ya Adam عليه السلام. Jina lake ni Nuh bin Lamak bin Matushah bin Khanukh. Khanukh kama walivyodai, ni Nabii Idris عليه السلام. Nabii Idris عليه السلام alikuwa mtu wa kwanza kuandika na kutumia kalamu, na yeye alikuwa mwana wa Yardi bin Mihlil, bin Qanin, bin Yanish bin Shith, bin Adam عليه السلام. Nasaba hii ilitajwa na Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالی na Maimamu wengine wa *Salaf*.

'Abdulla bin 'Abbas رضي الله عنهما na maulamaa wengine wa *Tafsir* walisema. Mwanzo wa kuabudiwa kwa Masanamu ni pale baadhi ya watu wema walipofariki, na watu hao wakawajengea majumba ya ibada katika makaburi yao, na wakatengeza taswira zao ili ziwakumbushe juu ya hali na ibada zao na kwa ajili hiyo wawaige. Muda uliporefuka, walitengenezea maumbo yao

kupitia picha hizo. Hatimaye waliyaabudu masanamu hayo na wakayaita majina ya hao watu wema, *Wadd, Suwaa', Yaghuth, Ya'uq na Nasr*. Baada ya jambo hili kuenea, Allah تعالى Sifa na Shukrani ni Zake Alimtuma Mtume Wake, Nuh عليه السلام ambaye aliwaamuru wamuabudu Allah تعالى Peke Yake, bila kumshirikisha. Alisema;

يَنْقُورِمْ أَعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ إِنَّ أَحَافَ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ

“Enyi kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mola ila Yeye. Hakika nimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyokuu”.

Maana yake: Adhabu ya Siku ya Kiyama, mtakapokutana na Allah تعالى huku mkiwa washirikina.

قَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِيَّ

“Wale watukufu katika kaumu yake wakasema”.

Maana yake: Jamia, wakuu, makamanda na wakubwa wengine walisema;

إِنَّا لَنَرَنَّكَ فِي ضَلَلٍ مُّبِينٍ

“Hakika sisi tunakuona wewe umo katika upotofu ulio dhahiri”.

Maana: Kuhusu kutulingania kwako juu ya kuacha kuyaabudu masanamu haya ambayo tuliwakuta baba zetu wakiyaabudu. Na hii ndiyo hali ya makafiri, huwa wanawaona watu wema kuwa ni wapotevu.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

وَإِذَا رَأَوْهُمْ قَالُوا إِنَّ هَؤُلَاءِ لَضَالُونَ ﴿٨٣﴾

“Na wanapowaona husema: Hakika hawa ndio khasa waliopotea”.

(83:32) na;

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا لَوْ كَانَ خَيْرًا مَا سَبَقُونَا إِلَيْهِ ؕ وَإِذْ لَمْ يَهْتَدُوا بِهِ

فَسَيَقُولُونَ هَذَا إِفْكٌ قَدِيمٌ ﴿٤٦﴾

“Na waliokufuru waliwaambia walioamini: Lau kuwa hii ni kheri, wasingelitutangulia. Na walipokosa kuongoka wakasema: Huu ni uzushi wa zamani”. (46:11)

Pamoja na Aya nyingine;

قَالَ يَنْفَوِّرَ لَيْسَ بِي ضَلَالَةٌ وَلَكِنِّي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٣﴾

“Akasema: enyi watu wangu! Mimi simo katika upotofu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.”

Maana yake: Mimi si mpotevu, bali mimi ni Mjumbe kutoka kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote, Mola wa kila kitu na Mfalme wa vyote.

أَيُّغُكُم رَّسَلْتِ رَبِّي وَأَنْصَحُ لَكُمْ وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٤﴾

“Nikufikishieni ujumbe wa Mola Mlezi wangu, na ninakunasihini; na ninayajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua nyinyi.”

Hii ni sifa ya Mtume, kuwa anafikisha kwa ufasaha na umbuji, anatoa nasaha na ana elimu ya kutosha kuhusu Allah تعالى; hakuna wa kuwapita kwa sifa hizi. Kama ilivyo katika *Sahih Muslim* kwamba Mtume ﷺ aliwaambia masahaba wake katika siku ya Arafah, na huo ulikuwa ni mkusanyiko mkubwa zaidi wa watu. Alisema;

«أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّكُمْ مَسْئُولُونَ عَنِّي فَمَا أَنْتُمْ قَائِلُونَ؟»

“Enyi watu! Mtaulizwa juu yangu mimi, kwa hivyo mtasema nini?” Wakasema, “Tunatoa ushahidi kuwa umefikisha na umetoa nasaha”. Mtume ﷺ akawa ananyoosha kidole chake kuelekea juu mbinguni na (kukishusha) kuwaelekezea wao huku akisema;

«اللَّهُمَّ اشْهَدِ اللَّهُمَّ اشْهَدِ»

“Ewe Allah! Shuhudia, Ewe Allah! Shuhudia”.¹

أَوْعَجِبْتُمْ أَنْ جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ وَلِتَتَّقُوا وَلَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٦٥﴾ فَكَذَّبُوهُ فَأَنْجَيْنَاهُ وَالَّذِينَ مَعَهُ فِي الْفُلِّ وَأَغْرَقْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا عَمِينَ ﴿٦٦﴾

63. Je, mnastaajabu kukujieni mawaidha yanayotoka kwa Mola Mlezi wenu kwa njia ya mtu mmoja katika nyinyi, ili akuonyeni na ili mumchemungu, na ili mpate kurehemewa?

64. Basi walimkanusha. Nasi Tukamuokoa yeye na waliokuwa pamoja naye katika jahazi. Na Tukawazamisha wale waliokanusha ishara Zetu. Hakika hao walikuwa watu vipofu.

¹ Muslim 2:890.

Allah تعالى Anaeleza juu ya Nuh عليه السلام, kuwa aliwaambia kaumu yake;

أَوْعَجِبْتُمْ

“Je, mnastaajabu”.

Maana yake: “Msilistaajabie hili, kwani sio ajabu Allah تعالى Kumpa wahyi mtu mmoja miongoni mwenu kutokana na rehema, ulatifu na ihsani Yake kwenu ili akuonyeni na ili muiogope nakama kutoka kwa Allah تعالى, kwa njia ya kutomshirikisha na chochote”.

وَلَعَلَّكُمْ تَرْحَمُونَ

“...na ili mpate kurehemewa”.

Allah تعالى Alisema;

فَكَذَّبُوهُ

“Basi walimkanusha”.

Maana yake: Waling'ang'ania kumkadhibisha na kumkhalifu, wala hawakumuamini isipokuwa watu wachache.

Sawa na Allah تعالى Alivyoeleza katika Aya nyingine; Sura ya Hudi Aya ya 40.

فَأَنْجَيْنَاهُ وَالَّذِينَ مَعَهُ فِي الْفُلِّ

“Nasi Tukamuokoa yeye na waliokuwa pamoja naye katika jahazi”.

Maana yake: Safina, kama Alivyosema:

وَأَغْرَقْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا

“Na Tukawazamisha wale waliokanusha ishara Zetu”.

Sawa na Kauli Yake nyingine;

مِمَّا خَطِيئَتِهِمْ أُغْرِقُوا فَأَدْخَلُوا نَارًا فَلَمْ يَجِدُوا لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْصَارًا ﴿٧٥﴾

“Basi kwa ajili ya makosa yao waligharikishwa wakaingizwa Motoni, wala hawakuwapata wa kuwanusuru badala ya Mwenyezi Mungu”. (71:25)

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا عَمِينَ

“Hakika hao walikuwa watu vipofu”.

Maana yake: Hawaioni haki wala hawakuongoka na haki hiyo. Katika kisa hiki, Allah تعالى Amebainisha kuwa Alilipa kisasi kwa maadui Wake na kumuokoa Mtume Wake na Waumini, na Akawaangamiza maadui wao makafiri.

Sawa na Kauli Yake nyingine;

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume wetu”. (40:51)

Hii ndiyo Sunnah (njia) ya Allah تعالى kwa waja Wake duniani na Akhera kuwa mwisho mwema ni wa wachamungu, pia ushindi ni wao. Sawa na Alivyo iangamiza kaumu ya Nuh عليه السلام kwa gharika na Akamuokoa Nuhu عليه السلام na wafuasi wake Waumini. Ibn Wahb alisema, ilinifikia khabari kwamba Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema waliookolewa pamoja na Nuh عليه السلام walikuwa ni watu themanini na mmoja wao ni mtu kutoka kabila la Jurhum ambaye alikuwa akiongea nao lugha ya kiarabu. Ibn Abu Hatim aliyankuu hayo. Pia yalinukuliwa kwa isnadi nyingine inayokwenda mpaka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما.

* * *

* وَإِلَىٰ عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا ۗ قَالَ يَنْقُومِ آعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِّنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٦٥﴾ قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن قَوْمِي إِنَّا لَنرُكِبُ فِي سَفَاهَةٍ وَإِنَّا لَننظُنُّكَ مِنَ الْكٰذِبِينَ ﴿٦٦﴾ قَالَ يَنْقُومِ لَيْسَ بِي سَفَاهَةٌ وَلِيَكْتَبِي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعٰلَمِينَ ﴿٦٧﴾ أُيْلِغُكُمْ رِسٰلَتِ رَبِّي وَأَنَا لَكُمْ أَمِينٌ نَّاصِحٌ ﴿٦٨﴾ أَوْعَجِبْتُمْ أَن جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ ۗ وَأَذْكُرُوا إِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَاءَ مِن بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ وَزَادَكُمْ فِي الْخَلْقِ بَضْطَةً ۗ فَادْكُرُوا ءَالَآءَ اللَّهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾ قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَدْرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا ۗ فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِن كُنتَ مِنَ الصّٰدِقِينَ ﴿٧٠﴾ قَالَ قَدْ وَقَعَ عَلَيْكُمْ مِّن رَّبِّكُمْ رِجْسٌ وَعَظْبٌ ۗ أَنْجِدُونِي فِي أَسْمَاءِ سَمَيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ مَا نَزَّلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطٰنٍ ۗ فَانظُرُوا إِلَيَّ مَعَكُمْ مِّنَ الْمُنتَظِرِينَ ﴿٧١﴾ فَأَنجَيْنَاهُ وَالَّذِينَ مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَقَطَعْنَا دَابِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِءَايٰتِنَا ۗ وَمَا كَانُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٧٢﴾

* وَإِلَىٰ عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا ۗ قَالَ يَنْقُومِ آعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِّنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٦٥﴾ قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن قَوْمِي إِنَّا لَنرُكِبُ فِي سَفَاهَةٍ وَإِنَّا لَننظُنُّكَ مِنَ الْكٰذِبِينَ ﴿٦٦﴾ قَالَ يَنْقُومِ لَيْسَ بِي سَفَاهَةٌ وَلِيَكْتَبِي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعٰلَمِينَ ﴿٦٧﴾ أُيْلِغُكُمْ رِسٰلَتِ رَبِّي وَأَنَا لَكُمْ أَمِينٌ نَّاصِحٌ ﴿٦٨﴾ أَوْعَجِبْتُمْ أَن جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ ۗ وَأَذْكُرُوا إِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَاءَ مِن بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ وَزَادَكُمْ فِي الْخَلْقِ بَضْطَةً ۗ فَادْكُرُوا ءَالَآءَ اللَّهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾ قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَدْرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا ۗ فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِن كُنتَ مِنَ الصّٰدِقِينَ ﴿٧٠﴾ قَالَ قَدْ وَقَعَ عَلَيْكُمْ مِّن رَّبِّكُمْ رِجْسٌ وَعَظْبٌ ۗ أَنْجِدُونِي فِي أَسْمَاءِ سَمَيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ مَا نَزَّلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطٰنٍ ۗ فَانظُرُوا إِلَيَّ مَعَكُمْ مِّنَ الْمُنتَظِرِينَ ﴿٧١﴾ فَأَنجَيْنَاهُ وَالَّذِينَ مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَقَطَعْنَا دَابِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِءَايٰتِنَا ۗ وَمَا كَانُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٧٢﴾

65. Na kwa A'adi Tuli-mpeleka ndugu yao, Hud. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi

Mungu. Nyinyi hamna mungu ila Yeye. Basi, je, kwanini hamumchi yeye?

66. Wakasema watukufu wa wale waliokufuru katika kaumu yake: Sisi tunakuona umo katika upumbavu, na hakika sisi tunakufikiria kuwa wewe ni katika waongo.

67. Akasema: Enyi watu wangu! Mimi sina upumbavu. Lakini mimi ni Mtume niliyetoka kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.

68. Nakufikishieni ujumbe wa Mola wangu Mlezi. Na mimi kwenu ni mwenye kukunasihini, mwaminifu.

69. Mnaona ajabu kukufikieni mawaidha yanayotoka kwa Mola wenu Mlezi kwa mtu aliye mmoja wenu nyinyi ili akuonyeni? Na kumbukeni alivyokufanyieni mshike pahala pa kaumu ya Nuhu na Akakuzidisheni katika umbo. Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.

Kisa cha Hud عليه السلام na Ukoo wa Kaumu ya 'Aad.

Allah تعالى Anasema, kama Tulivyomtuma Nuh عليه السلام kwa kaumu yake, kadhalika, Tulimpeleka Hud عليه السلام kwa watu wa 'Aad. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema, hao ni watoto wa 'Add bin Iram, bin 'Aws bin Sam, bin Nuh عليه السلام. Mimi nasema, hao ndio watu wa 'Aad wa mwanzoni, ambao Allah تعالى Aliwataja. Na wao ndio watoto wa 'Aad bin Iram ambao walikuwa wakiishi majangwani kulikokuwa na nguzo au masanamu marefu. Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦٨﴾ إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٦٩﴾ الَّتِي لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِي الْبَلَدِ ﴿٧٠﴾

“Kwani hukuona jinsi Mola wako Mlezi Alivyowafanya kina A'di? Wa Iram, wenye majumba marefu? Ambao haukuumbwa mfano wake katika nchi”. (89:68)

Hayo ni kutokana na uwezo na nguvu zao. Ni sawa na Alivyosema Allah تعالى, katika Aya nyingine;

فَأَمَّا عَادٌ فَاسْتَكْبَرُوا فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَقَالُوا مَنْ أَشَدُّ مِنَّا قُوَّةً أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَهُمْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُمْ قُوَّةً وَكَانُوا بِآيَاتِنَا يَجْحَدُونَ ﴿٧١﴾

“Ama kina A'di walijivuna katika nchi bila ya haki, na wakasema: Nani aliyekuwa na nguvu kushinda sisi? Kwani wao hawakuona kwamba Mwenyezi Mungu Aliyewaumba ni Mwenye Nguvu Kuwashinda wao? Na wao wakawa wanazikataa ishara Zetu!” (41:15)

Makazi ya Watu wa 'Aad.

Makazi yao yalikuwa Yemen katika eneo la *Ahqaaf*, ambayo ni milima ya mchanga. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alieleza kutoka kwa abu Al-Tufail 'Amir bin Wathilah kuwa, Nilimsikia 'Ali رضي الله عنه akimuambia mtu mmoja kutoka Hadhramaut: "Umewahi kuona kilima chekundu cha mchanga ambapo kuna miti ya mswaki na mikunazi mingi, kwa upande kadha na kadha, Umeona hilo?" Akasema: "Ndiyo, ewe Amiri wa Waumini! Unapaelezea sawa sawa na mtu aliyewahi kupaona". Akasema, "Hapana (Sijawahi kupaona), bali nimeelezwa".

Mtu wa Hadhramaut akasema, "Kuna jambo gani eneo hilo, ewe Amiri wa Waumini?" Akasema. "Kuna kaburi la Hud عليه السلام".

Ibn Jariri رحمه الله تعالى aliyankuu hayo¹. Katika haya kuna faida, kwamba makazi yao yalikuwa Yemen, kwani Hud عليه السلام alizikwa huko, na ndiye alikuwa na nasaba ya kuheshimika zaidi katika kaumu yake, kwani Allah تعالى Huwapeleka kwa watu kutokana na familia na kabila lililoheshimiwa zaidi kati yao.

Hata hivyo, kaumu yake, kama ambavyo walikuwa na uwezo na nguvu nyingi, kadhalika nyoyo zao zilikuwa ngumu, na walikuwa ndiyo umma uliokadhibisha zaidi haki, kwa minajili hiyo, Hud عليه السلام aliwalingania kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, pasi na mshirika, pamoja na kumtii Yeye na kumcha.

Yaliyojiri Baina ya Hud عليه السلام na Watu Wake.

قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ

"Wakasema watukufu wa wale waliokufuru katika kaumu yake".

Maana ya *Mala-a* ni umma mzima, wakuu na viongozi wao.

إِنَّا لَنَرَنَّكَ فِي سَفَاهَةٍ وَإِنَّا لَنَظُنُّكَ مِنَ الْكٰذِبِينَ

"Sisi tunakuona umo katika upumbavu, na hakika sisi tunakufikiria kuwa wewe ni katika waongo".

¹ At-Tabari 12:507.

Maana: Katika upotevu, kwa kule kutuita kuwa tuache kuyaabudu masanamu na kugeukia katika kumuabudu Allah تعالى Peke Yake. Sawa na wanavyostaajabu wakuu wa kikuraishi juu ya wito wa kumuabudu Mola Mmoja, wakasema;

أَجْعَلِ الْآلِهَةَ إِلَهًا وَاحِدًا

“Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu mmoja tu?” (38:5)

قَالَ يَنْقَوْمٍ لَيْسَ بِي سَفَاهَةٌ وَلِنِكَتِي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٧﴾

“Akasema: Enyi watu wangu! Mimi sina upumbavu. Lakini mimi ni Mtume niliyetoka kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote”.

Maana yake: Mimi si sawa na mnavyodai, bali nimekujieni na ukweli utokao kwa Allah تعالى, Ambaye Alikiumba kila kitu. Na Yeye ni Mola na Mfalme wa kila kitu.

أُبَلِّغُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي وَأَنَا لَكُمْ أَمِينٌ نَّاصِحٌ ﴿٧٨﴾

“Nakufikishieni ujumbe wa Mola wangu Mlezi. Na mimi kwenu ni mwenye kukunasihini, mwaminifu”.

Sifa hizi ndizo ambazo Mitume hujielezea, ambazo ni suala la kuubalighisha Ujumbe, kutoa nasaha na uaminifu.

أَوْعَجِبْتُمْ أَن جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ

“Mnaona ajabu kukufikieni mawaidha yanayotoka kwa Mola wenu Mlezi kwa mtu aliye mmoja wenu nyinyi ili akuonyeni?”

Maana: Msione ajabu kuwa Allah تعالى Amekuleteeni Mtume kutokana na nyinyi, ili akuonyeni juu ya Siku za Allah تعالى (adhabu yake) na kukutana Naye. Bali mshukuruni Allah تعالى juu ya Aliyokuneemesheni.

وَأَذْكُرُوا إِذْ جَعَلْتُمْ خُلَفَاءَ مِن بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ

“Na kumbukeni Alivyokufanyieni mshike pahala pa kaumu ya Nuhu”.

Maana: Na mkumbuke neema za Allah تعالى juu yenu kwa kukujaalieni kuwa ni dhuriya wa Nuh عليه السلام, ambaye kwa dua yake, Allah تعالى Aliwaangamiza watu wa ardhini pindi walipomkhalifu na kumkadhibisha.

وَزَادَكُمْ فِي الْخَلْقِ بَسْطَةً^ط

“...na Akakuzidisheni katika umbo”. Maana yake: Alikuzidishieni urefu zaidi ya watu wengine. Amekufanyieni kuwa na vimo virefu. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى, katika kisa cha Twalut.

وَزَادَهُ بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ^ط

“...na Amemzidishia ukunjufu wa ilimu na kiwiliwili”. (2:247)

فَاذْكُرُوا ءَالَآءَ اللَّهِ

“Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu”. Maana yake: Ujazi na baraka juu yenu.

لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُونَ

“...ili mpate kufanikiwa”.

قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِنْ كُنْتَ
 مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٧٠﴾ قَالَ قَدْ وَقَعَ عَلَيْكُمْ مِّن رَّبِّكُمْ رِجْسٌ وَعَصِبٌ^ط تُجَادِلُونَنِي فِي
 أَسْمَاءِ سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ مَا نَزَّلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطٰنٍ ؕ فَانظُرُوا إِلَيَّ مَعَكُمْ مِّن
 الْمُنْتَظِرِينَ ﴿٧١﴾ فَأَجَبْنَاهُ وَالَّذِينَ مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَقَطَعْنَا دَابِرَ الَّذِينَ كَذَبُوا
 بِغَايَتِنَا وَمَا كَانُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٧٢﴾

70. Wakasema: Je! Umetujia ili tumuabudu Mwenyezi Mungu Peke Yake, na tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu? Basi Tuletee hayo unayotuahidi, ukiwa miongoni mwa wasemao kweli.

71. Akasema: Bila ya shaka adhabu na ghadhabu Zimekwisha kukuangukieni kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Mnabishana nami kwa ajili ya majina tu mliyoyaita nyinyi na baba zenu ambayo kwayo Mwenyezi Mungu Hakuteremsha uthibitisho? Basi ngojeni, mimi pia ni pamoja nanyi katika wanaongoja.

72. Basi Tukamuokoa yeye na waliokuwa pamoja naye kwa Rehema Zetu, na Tukakata mizizi ya wale waliozikanusha ishara Zetu, na hawakuwa wenye kuamini.

Allah تعالى Anaeleza uasi, ufidhuli, ukaidi na ukadhibishaji wao kwa Nabii Hud عليه السلام.

قَالُوا أَجِئْنَا لِنُعْبَدَ اللَّهَ وَحَدَهُ

“Wakasema: Je! Umetujia ili tumuabudu Mwenyezi Mungu Peke Yake”.

Sawa na kauli ya makafiri wa kikuraishi;

وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِنْ كَانَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابًا مِنَ السَّمَاءِ
أَوْ آتِنَا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٢﴾

“Na waliposema: Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo Kwako basi tunyesheshe mawe kutoka mbinguni, au Tuletee adhabu yoyote iliyochungu”. (8:32)

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى na wengine walitaja kuwa Makuraishi walikuwa wakiyaabudu masanamu, yaliyoitwa, Suda, Swamud na Al-Hibaa. Na kwa kuzingatia hilo Hud عليه السلام akasema;

قَدْ وَقَعَ عَلَيْكُمْ مِنْ رِئْسِكُمْ رِجْسٌ وَعَصَبٌ

“Bila ya shaka adhabu na ghadhabu zimekwisha kukuangukieni kutoka kwa Mola wenu Mlezi”.

Maana yake: Mmewajibikiwa juu yenu kupata Rijs, kutoka kwa Mola wenu. Ilisemwa kuwa hiyo imebadilishwa kutoka katika Rijz. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa maana yake ni fedheha na ghadhabu¹.

أَتَجِدُلُونَنِي فِي أَسْمَاءِ سَمَّيْتُمُوهَا أَنْتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ

“Mnabishana nami kwa ajili ya majina tu mliyoyaita nyinyi na baba zenu”. (7:71)

Maana yake: Je, mnabishia juu ya masanamu haya mliyoyapangia majina nyinyi na baba zenu, mkaifanya kuwa miungu, ilhali haidhuru wala hainufaishi, wala Allah تعالى Hajakujaalieni kuwa na hoja wala dalili katika kuyaabudu.

Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema;

¹ At-Tabari 12:522.

مَا نَزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطٰنٍ ۚ فَانْتَظِرُوا ۙ اِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُنْتَظِرِينَ ۙ

“Mwenyezi Mungu Hakuteremsha uthibitisho? Basi ngojeni, mimi pia ni pamoja nanyi katika wanaongoja”.

Hili ni tishio na ahadi ya Mtume kwenda kwa kaumu yake. Kwa ajili hii Alimpatia mwisho mwema (ushindi) kwa Kauli Yake.

Mwisho wa Watu wa ‘Aad Ulivyokuwa.

Kauli ya Allah تعالى:

فَاٰخِزْنٰهُ وَالَّذِيْنَ ۙ مَعَهُۥ بِرَحْمَةٍ مِّنَّا وَقَطَّعْنَا دَاۤىِٔرَ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِمَا ئٰتِيْنَا ۙ وَمَا كَانُوْا مُؤْمِنِيْنَ ۙ

“Basi Tukamuokoa yeye na waliokuwa pamoja naye kwa Rehema Zetu, na Tukakata mizizi ya wale waliozikanusha ishara Zetu, na hawakuwa wenye kuamini”.

Katika sehemu nyingine nyingi ndani ya Qur’an, Allah تعالى Anataja namna ya Kuangamizwa kwao kwa kuwa Aliwapelekea upepo mkavu ambao haukiendei kitu, bali hukifanya kama kilichomung’unyika. Sawa na Aya nyingine;

وَاَمَّا عَادٌ فَاهْلٰكُوْا بِرِيْحٍ صَّرٰصِرٍ عٰتِيَةٍ ۙ سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ سَبْعَ لَيَالٍ وَّتَمَّتْ يَوْمَۃً اَيّٰمٍ حُسُوْمًا ۙ فَتَرٰى الْقَوْمَ فِيْهَا صَرَٰى كَاٰثِمٍ ۙ اَعْجَازٌ مِّنْ خَلٍ خَاوِيَةٍ ۙ فَهَلْ تَرٰى لَهُمْ مِّنْ بَاقِيَةٍ ۙ

“Na ama A’di waliangamizwa kwa upepo mkali usiozuilika. Aliwapelekea mausiku saba, na siku nane mfululizo bila ya kusita. Utaona watu wamepinduka kama kwamba ni magogo ya mitende yaliyo wazi ndani. Basi, je! Unamuona mmoja wao aliyebaki?”
(69:6-8)

Walipoasi na kuruka mipaka, Allah تعالى Aliwaangamiza kwa upepo usiozuilika na ukawa unamnyanyua mtu mmoja mmoja na kumpaisha juu, kisha kumleta chini kwa kumpindua kichwa chini miguu juu na kukiponda na kukitenganisha na kiwiliwili. Kwa ajili hiyo Allah تعالى Alisema;

كَاٰثِمٍ ۙ اَعْجَازٌ مِّنْ خَلٍ خَاوِيَةٍ

“...kama kwamba ni magogo ya mitende yaliyo wazi ndani”. (69:7)

Muhammad bin Is-haq رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى alisema kwamba maskani yao yalikuwa Yemen, baina ya Oman na Hadhramaut. Pamoja na hapo, walikuwa wameenea ardhini na wakatumia fadhila ya nguvu zao walizopewa na Allah تَعَالَى kuwavamia watu wa maeneo hayo. Walikuwa wakiyaabudu masanamu, badala ya Allah تَعَالَى. Allah تَعَالَى Akawapelekea Nabii Hud عَلَيْهِ السَّلَام na alitokana na nasaba iliyokuwa maarufu kwao, na alikuwa na hadhi bora zaidi. Akawaamuru wampwekeshe Allah تَعَالَى wala wasimshirikishe na mungu mwingine, na wakome kuwadhulumu watu. Wakamkataa na wakamkadhibisha, na wakasema; "Ni nani walio na nguvu kuliko sisi?" Watu wachache ambao walificha imani yao ndio waliomfuata. 'Aad waliikataa Amri ya Allah تَعَالَى, wakamkadhibisha Mtume Wake, wakazidisha uharibifu duniani, wakawa jeuri na wakajenga majumba makubwa katika kila mahali pa juu bila ya manufaa kwao. Hud aliwaambia;

أَتَّبِعُونَ بِكُلِّ رِيعٍ ؕ آيَةً تَعْبَثُونَ ﴿٦٨﴾ وَتَتَّخِذُونَ مَصَانِعَ لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُونَ ﴿٦٩﴾ وَإِذَا
بَطَشْتُمْ بَطَشْتُمْ جَبَّارِينَ ﴿٧٠﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ﴿٧١﴾

"Je! Mnajenga juu ya kila mnyanyuko kumbusho la kufanyia upuuzi? Na mnajenga majengo ya fakhari kama kwamba mtaishi milele? Na mnapotumia nguvu mnatumia nguvu kwa ujabari. Basi Mcheni Mwenyezi Mungu na mtiini". (26:128-131)

قَالُوا يَهُودُ مَا جِئْتَنَا بِبَيِّنَةٍ وَمَا نَحْنُ بِتَارِكِي آلِإِهْتِنَا عَنْ قَوْلِكَ وَمَا نَحْنُ لَكَ
بِمُؤْمِنِينَ ﴿٧٢﴾ إِنْ نَقُولُ إِلَّا اعْتَرَاكَ بَعْضُ آلِهَتِنَا بِسُوءٍ ۗ

"Wakasema: Ewe Hud! Hujatuletea dalili wazi. Wala sisi hatuiachi miungu yetu kwa kufuata kauli yako. Na wala sisi hatukuamini wewe. Sisi tunasema: Baadhi katika miungu yetu imekusibu kwa baa". (11:53-54)

Maana yake: Umajinuni.

قَالَ إِنِّي أَشْهَدُ اللَّهَ وَأَشْهَدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٧٣﴾ مِنْ دُونِهِ ۗ فَكَيْدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ
لَا تُنظِرُونِ ﴿٧٤﴾ إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمْ ۗ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا
إِنَّ رَبِّي عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٧٥﴾

“Akasema: Hakika mimi namshuhudia Mwenyezi Mungu na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnaowafanya washirika. Mkamuacha Yeye. Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi, na kisha msinipe muhula!. Hakika mimi nitemtegemea Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye anamwendesha atakavyo. Hakika Mola wangu Mlezi yuko juu ya Njia Iliyo Nyooka.” (11:53-56)¹

Kisa cha Mjumbe wa A'ad

Imamu Ahmad alimnukuu Al-Harith Al-Bakr kuwa alisema, “Nilikwenda kwa Mtume ﷺ kumlalamikia juu ya Al-Alaa bin Al-Hadhrami. Nikapita sehemu iitwayo *Ar-Rabdah*, nikamkuta mwanamke kikongwe kutoka Banu Tamim, ambaye alikuwa peke yake katika eneo hilo. Akaniambia, “Ewe mja wa Allah! Mimi nina haja kwa Mjumbe wa Allah, je! Utanifikisha kwake?” Nikamchukua, na nikaja naye Madinah, na tukaukuta Msikiti ukiwa umefurika watu. Kulikuwa na bendera nyeusi iliyonyooshwa juu, na Bilal رضي الله عنه alikuwa amekamata upanga mkononi mwake mbele ya Mtume ﷺ, nikauliza: “Wana nini hawa watu?” Wakasema, “Mjumbe wa Allah anataka kumtuma ‘Amr bin ‘As sehemu (kijeshi)”. Akasema, ‘Nikaketi.’ Mtume ﷺ akaingia nyumbani kwake. Nikamuomba idhini ya kumuona. Akaniruhusu. Nikaingia na kutoa maamkizi. Akasema, “*Mna jambo (la ugomvi) baina yenu na Banu Tamim*”. Nikajibu, “Ndiyo, na sisi tuliwashinda. Na njiani nimemkuta kikongwe atokanaye na wao, anayetoka eneo analokaa peke yake. Akaniomba nimlete kwako. Yupo mlangoni”. Mtume ﷺ akamruhusu kuingia na akaingia. Nikasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Unaonaje kama utaweka kizuizi baina yetu na (kabila la) Banu Tamim, ufanye mpaka huo *Ad-Dahna* (ambayo ni ardhi yenye malisho mengi ya wanyama)”. Kikongwe akakasirika na akapinga. Akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! (shida za Mudhwar) utazielekeza wapi?” Nikasema, “Mfano wangu ni kama ilivyosemwa na wahenga zamani, ‘Mbuzi wangu amejiangamiza mwenyewe’. Nimemchukua huyu, wala sikujua kama atakuwa khasimu wangu. Najikinga kwa Allah تعالى na kwa Mtume Wake dhidi ya kuwa kama mjumbe

¹ At-Tabari 12:507.

wa 'Aad". Mtume 𐤀𐤁𐤀 akasema, "Na mjumbe wa 'Aad ni nani?" Yeye alikuwa akikijua kisa hicho zaidi lakini alitaka kupata ladha yake. Nikasema, "Watu wa 'Aad walipatwa na janga la njaa, wakamtuma mjumbe (kuhemea) aliyetitwa Qayl. Akapita kwa Muawiyyah bin Bakr. Akakaa kwake mwezi mmoja huku akipatiwa na Muawiyyah vinywaji vya ulevi na vijakazi wawili walioitwa *Al-Jaradatan* (panzi wawili) wakimuimbia. Mwezi ulipoisha, alielekea milima ya Muhrah, na akasema, "Ewe Allah! Wewe unajua kwamba mimi sikuja kwa mgonjwa kumtibu, wala kwa mateka kumkomboa. Ewe Allah! Wanyweshe 'Aad maji kama ulivyokuwa ukiwanyweshwa". Akapitiwa na mawingu meusi, na akaitwa, "Khitari (moja wapo ya mawingu haya)". Akaliashiria wingu lililokuwa jeusi. Akasikia sauti ikinadi kutokea kwenye wingu hilo, "Ichukue kama majivu ambavyo hayatasaza kitu huko kwa 'Aad. Na kuna khabari zilinifikia kwamba hewa iliyopelekwa kwao haikuzidi kiasi cha inayoweza kupita katika pete yangu hii, lakini iliwaangamiza hewa hiyo". Abu Wail alisema, "Alisema kweli. Ilikuwa kwamba mwanaume na mwanamke walipokuwa wakipeleka ujumbe waliwaambia, "Usiwe kama mjumbe wa 'Aad (kwa kuwaletea maangamizo badala ya msaada)". Imamu Ahmad alikusanya kisa hiki katika *Musnad*¹. At-Tirmidhi² alinukuu maneno sawa na hayo, pia ilinukuliwa na An-Nasai³ na Ibn Majah⁴.



¹ Ahmad 3:482.

² Tuhfatul Al-Ahwadhi 5:181.

³ Al-Kubra 5:181.

⁴ Ibn Majah 2:941.

73. Na kwa Thamud Tulimpeleka ndugu yao, Saleh. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu hamna mola mwengine ila Yeye. Hakika imekwisha kukufikieni Ishara iliyowazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Huyu ni ngamia jike wa Mwenyezi Mungu ambaye ni Ishara kwenu. Basi muachieni ale kwenye ardhi ya Mwenyezi Mungu, wala msimdhuru, isije kukushukieni adhabu chungu.

74. Na kumbukeni Alivyokufanyieni wa kushika pahala pa A'aadi na Akakuwekeni vizuri katika nchi, mnajenga majumba ya fakhari katika nyanda zake, na mnachonga majumba katika milima. Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu wala msitende uovu katika nchi kwa ufisadi.

75. Waheshimiwa wa kaumu yake wanaojivunia waliwaambia wanaoonewa wenye kuamini miongoni mwao: Je, mnaitakidi ya kwamba Saleh ametumwa na Mola Mlezi wake? Wakasema: Hakika sisi tunayaamini yale aliyotumwa.

76. Wakasema wale wanaojivuna: Sisi tunayakataa hayo mnayoyaamini.

77. Na wakamuua Ngamia yule, na wakaasi amri ya Mola wao mlezi. Na wakasema: Ewe Salehe tulettee hayo unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa Mitume.

78. Basi tetemeko la ardhi likawanyakua na kulipokucha wakawa majumbani mwao kifudifudi wamekwishakufa".

Maskani ya Kaumu ya Thamud na Nasaba Yao.

Maulamaa wa *Tafsir* na nasaba walisema, ni Thamud bin 'Aathir, bin Iram, bin Sam, bin Nuh عليه السلام. Yeye ni nduguye Jadis bin 'Aathir, Halikadhalika ni kabila la Twasm, na walitokana na Waarabu wa kale, *Al-Aaribah*,¹ kabla ya kipindi cha Ibrahim عليه السلام. Thamud walikuja baada ya 'Aad na maskani yao mashuhuri yalikuwa baina ya Hijaz (Magharibi mwa Uarabuni) na Sham (Syria)

¹ Kinyume na *Al-Musta'ribah* kama vile dhuriya ya Nabii Ismail bin Ibrahim.

mpaka katika Wadi Al-Qura na eneo linaloizunguka. Mtume ﷺ aliwahi kupita katika mabaki ya nyumba na maskani yao alipokuwa njiani kwenda Tabuk katika mwaka wa tisa.

Imamu Ahmad alimnukuu Ibn 'Umar رضي الله عنهما, "Mtume ﷺ alipoteremka katika eneo la Al-Hijr huko Tabuk pamoja na watu. Alipiga kambi jirani na masalia ya nyumba za Thamud katika sehemu ya Al-Hijr. Watu wakachota maji kutoka katika visima ambavyo Thamud walikuwa wakivitumia hapo kabla. Wakayatumia maji hayo wakakanda vinyunya, wakainjika vyungu. Mtume ﷺ akawaamuru wayamwage maji hayo, wakayamwaga maji na ngamia wakapewa hivyo vinyunya. Akasafiri nao mpaka akashuka katika kisima ambacho alikuwa akinywa ngamia (kama itakavyoelezwa). Akawakataza wasiingie katika eneo la kaumu iliyoadhibiwa. Alisema;

«إِنِّي أَخْشَى أَنْ يُصِيبَكُمْ مِثْلُ مَا أَصَابَهُمْ فَلَا تَدْخُلُوا عَلَيْهِمْ»

"Mimi nachelea kisikusibuni kilichowasibu wao. Kwa hivyo msiingie kwao".¹

Pia Ahmad alisimulia kuwa 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما alisema, Mtume ﷺ alipokuwa Al-Hijr alisema;

«لَا تَدْخُلُوا عَلَى هَؤُلَاءِ الْمُعَذِّبِينَ إِلَّا أَنْ تَكُونُوا بَاكِينَ فَإِنْ لَمْ تَكُونُوا بَاكِينَ فَلَا تَدْخُلُوا عَلَيْهِمْ أَنْ يُصِيبَكُمْ مِثْلُ مَا أَصَابَهُمْ»

"Msiingie kwa hao walioadhibiwa, isipokuwa huku mkiwa mnalia. Ikiwa hamtakuwa mkilia, basi msiingie, ili liliowasibu lisikusibuni na nyinyi".²

Asili ya Hadithi hii imetajwa katika *Sahih Mbili*.³

¹ Ahmad 2:117.

² Ahmad 2:74.

³ Fat'hul Al-Bari 5:436 na Muslim 4:2286.

Kisa cha Nabii Saleh عليه السلام na Thamud.

Kauli ya Allah تعالى; وَالْيَوْمِ نُمُودًا

“Na kwa Thamud”. Maana yake: Kabila la Thamud tulilipelekea ndugu yao, Salih عليه السلام.

قَالَ يَنْقَوْمِ أَعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ

“Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu hamna mwengine ila Yeye”.

Mitume wote wanalingania katika kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, pasi na mshirika wake. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢١﴾

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mola isipokuwa Mimi. Basi Niabuduni Mimi tu”.
(21:25) na;

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطُّغُوتَ

“Na kwa hakika kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani”. (16:36)

Thamud Walitaka Ngamia Aibuke Kutoka Katika Jiwe na Akaibuka.

Kauli ya Allah تعالى;

قَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ هَذِهِ نَاقَةُ اللَّهِ لَكُمْ آيَةٌ

“Hakika imekwishakukufikieni Ishara iliyo wazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Huyu ni Ngamia jike wa Mwenyezi Mungu ambaye ni Ishara kwenu”.

Maana yake: Muujiza kutoka kwa Allah تعالى umeshakujieni kuyasadikisha niliyokujieni nayo. Na wao ndio waliomuomba Nabii Saleh عليه السلام awalettee ishara na wakashauri kwamba ngamia huyo atoke katika jabali gumu walilolichagua wao wenyewe. Nalo ni jiwe lililokuwa limejiweka peke yake katika sehemu ya Al-Hijr na lilikuwa likiitwa Al-Kaatibah. Wakamtaka awatolee ngamia mwenye mimba kutoka katika jiwe hilo. Saleh عليه السلام akachukua ahadi

na maagano yao kwamba ikiwa Allah تعالى Angewajibu ombi lao, wangelimuamini na kumfuata yeye. Baada ya kutoa ahadi na maagano yao hayo, Saleh عليه السلام alisimama kusali na kumuomba Allah تعالى. Jiwe lile likatikisika na kupasuka kumuachilia ngamia aliyekuwa na manyoya mengi. Na kitoto chake kinajitikisa tumboni mwake kama walivyooomba. Kiongozi wa kaumu hiyo Jundu' bin 'Amr akaamini, pamoja na waliokuwa pamoja nae katika jambo lake. Wakuu wengine wa Thamud wakataka nao kuamini. Lakini Dhuab bin 'Amr bin Labid, na Al-Hubbab ambaye aliyahudumia masanamu yao na Rabbab bin Sam'ar bin Jalhas waliwazuia. Jundu bin 'Amr alikuwa na binamu yake aliyetitwa Shihab bin Khalifa bin Mikhlaat bin Labid bin Jawwas ambaye alikuwa mmoja wapo wa wakuu na wenye hadhi wa kaumu hiyo, na akataka kusilimu, lakini kikundi hicho kikamkataza. Yeye akawatii. Mtu mmoja katika waumini wa Thamud aliyetitwa, Muhush bin Anamah bin Ad-Damail akasema; Jamaa wa karibu wa 'Amr, walimuita Shihab aingie dini ya Nabii Saleh عليه السلام. Na wakuu wote wa Thamud, Wakaazimia kuitikia, lau wangekubali Saleh عليه السلام angelikuwa azizi kwetu. Na wala wasingemfuata sahibu yao Dhuab. Bali waovu katika watu wa Hijr. Waligeuka baada ya kuongoka kwao kwa kumfuata Dhubab.

Ngamia na mwanaye wakasimama baada ya kumzaa mbele ya macho yao. Akawa Ngamia huyo anakunywa katika kisima chao siku moja, na anaacha siku nyingine kwa ajili yao. Na walikuwa wakinywa maziwa yake siku anapokunywa hayo maji, walikuwa wakimkama maziwa na kuyajaza katika vyombo vyao vyote walivyovitaka. Sawa na Kauli ya Allah تعالى: nyingine;

وَنَبِّئِهِمْ أَنَّ الْمَاءَ قِسْمَةٌ بَيْنَهُمْ كُلُّ شِرْبٍ مُحْتَضَرٌ

“Na waambie kwamba maji yatagawanywa baina yao; kila sehemu ya maji itahudhuriwa na aliyekhusika”. (54:28) na;

هَذِهِ نَاقَةٌ هَآ شَرِبَتْ وَلَكُمْ شِرْبٌ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ

“Huyu ngamia jike; awe na zamu yake ya kunywa, na nyinyi muwe na zamu yenu ya kunywa katika siku maalumu”. (26:155)

Na alikuwa akienda kuchunga katika mabonde yao kwa kupita njia moja wapo na kurejea kwa njia nyingine ili aweze kwenda kwa urahisi kwani alikuwa akinywa maji mengi. Alikuwa mnyama mkubwa mno aliyekuwa na mandhari

nzuri. Alipopita karibu na mifugo yao, ilimuogopa. Jambo hili lilipoendelea kwa muda mrefu na kumkadhibisha kwao Saleh عليه السلام kukashitadi, waliazimia kumuua Ngamia huyo ili waweze kujichotea maji kila siku. Ilisemwa kwamba wote waliafikiana kumuua. Qatadah alisema: "Ilinifikia khabari kwamba, aliyemuua, aliwazungukia wote kabla ya kufanya hivyo kwa ajili ya kukubaliana nao, ikiwa ni pamoja na wanawake vyumbani mwao na watoto"¹. Jambo hili liko dhahiri kutokana na Kauli ya Allah تعالى:

فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُم بِذُنُوبِهِمْ فَسَوَّاهَا ﴿١٤﴾

"Lakini walimkadhibisha na kumchinja ngamia, kwa hivyo Mola wao Mlezi Aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na Akawafuta kabisa". (91:14) Na;

وَأَتَيْنَا ثَمُودَ النَّاقَةَ مُبْصِرَةً فَظَلَمُوا بِهَا ﴿٥٩﴾

"Na Tuliwapa Wathamudi ngamia jike ni ishara iliyo dhahiri, lakini walidhulumu kwaye". (17:59) Na;

فَعَقَرُوا النَّاقَةَ

"Na wakamuua yule ngamia".

Aya hizi zinajumuisha kabila zima kutokana na wote kuliridhia jambo hilo. Allah Aalam.

Thamud Walimuua Ngamia.

Imamu Abu Ja'far bin Jariri رحمه الله تعالى na maulamaa wengine wa *Tafsir* walisema sababu ya kumuua ngamia ni kwamba, mwanamke mmoja katika wao, aliyeitwa 'Unayzah bint Ghanm bin Mijlaz na alikuwa akiitwa kwa jina lingine Umm Ghanm, alikuwa ni kikongwe wa kikafiri, na alikuwa akimfanyia uadui mkubwa Saleh عليه السلام. Alikuwa na mwanaye wa kike mzuri na mwenye mali nyingi. Mumewe alikuwa akiitwa Dhuab bin 'Amr, mmoja wa viongozi wa Thamud. Kulikuwa na mwanamke mwingine aliyeitwa Swaduf bint Al-Muhayya bin Dahr bin Al-Muhayya. Alitoka katika familia ya heshima alikuwa na mali na pia mlimbwende. Alikuwa mke wa Muislamu mmoja katika Thamud na akamuacha mumewe. Wanawake hawa wawili waliwaahidi zawadi wale waliowaapia wao

¹ At-Tabari 12:537.

wangelimuua ngamia. Swaduf Alimuita bwana mmoja aitwaye Al-Habbab, na alijitoa nafsi yake kwake iwapo angelimuua ngamia, lakini alimkatalia. Akamuita binamu yake aliyeitwa Mis'dau bin Mahraji bin Al-Muhayya, akakubali. Ama 'Unayzah bint Ghanm alimuita Qudar bin Saalif bin Jund' ambaye alikuwa mfupi mwenye ngozi ya rangi nyekundu na bluu kidogo na alikuwa mtoto wa zinaa, Saalif hakuwa baba yake wa kumzaa. Bali yeye anatokana na mtu aliyeitwa, Sah'yaad. Hata hivyo alizaliwa katika kitanda cha Saalif. 'Unayzah alimuambia, 'Nitakupa binti yangu yeyote utakayemtaka kwa sharti kwamba umuue Ngamia.' Hivyo Qudar bin Saalif akaenda. Mis'dau' bin Mihraaji akatoka na kuwahamasisha waovu katika wathamudi, watu saba miongoni mwao wakawafuata wao. Hivyo wakawa ni watu tisa ambao Allah تعالی Amewataja kwa kusema;

وَكَانَ فِي الْمَدِينَةِ تِسْعَةٌ رَهْطٍ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿٤٨﴾

“Na walikuwamo mjini watu tisa wakifanya ufisadi katika nchi wala hawafanyi suluhu”. (27:48)

Watu hao tisa walikuwa viongozi wa kaumu yao, wakalihadaa kabila zima juu ya kuwakubalia kumuua ngamia. Wakamsubiri ngamia alipotoka kwenye maji ambapo Qudar alimngojea pembeni mwa jabali na Mis'dau' katika jabali lingine. Ngamia alipomfikia Mis'dau alimpiga mshale ukamchoma mguuni mwake. Akajitokeza Umm Ghanm, 'Unayzah akamuamuru binti yake ambaye alikuwa mzuri sana kwa uso, amfunulie Qudar uso wake. Hilo likamhimiza Qudar, akauchezesha upanga na kumchoma Ngamia katika goti lake. Ngamia alianguka chini na akalia mara moja kumtahadharisha mwanaye. Qudar alimchoma shingoni na kumchinja. Mwanaye alipanda juu ya Jabali, na akapiga makelele¹. 'Abdur-Razzaq alieleza kutoka kwa Ma'mar kutoka kwa aliyemsikia Al-Hasan Al-Basri, kwamba alisema, “Ewe Mola wangu! Mama yangu yuko wapi?” Pia ilisemwa mwanaye alipiga kelele mara tatu na akaingia katika jabali na kupotelea humo. Pia ilisemwa kwamba walimfuata na kumchinja kama mama yake.² Allah Aalam.

Walipomaliza na kufanya hivyo, yaani kumchinja, na khabari zikamfikia Saleh عليه السلام, aliwajia wakiwa wamekusanyika. Alipomuona Ngamia, alilia na kusema;

¹ At-Tabari 12:531.

² Abdur-Razzaq 2:231.

تَمَتُّعُوا فِي دَارِكُمْ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ^ط

“...Stareheni katika mji wenu muda wa siku tatu...” (11:65)

Njama za Mafisadi Kutaka Kumuuu Nabii Saleh عليه السلام na Adhabu kuwashukia wao Kwanza, Kisha, Kushuka kwa Wathamudi Wote.

Wao walimuuu ngamia huyo katika siku ya Jumatano. Ilipofika jioni ya siku hiyo, waliazimia kumuuu Saleh عليه السلام. Wakasema, “Kama ni mkweli, basi tutamuwahisha yeye kabla yetu. Na kama ni muongo tutamkutanisha na ngamia wake”.

قَالُوا تَقَاسَمُوا بِاللَّهِ لَنُبَيِّتَنَّهُ وَأَهْلَهُ ثُمَّ لَنَقُولَنَّ لِوَلِيِّهِ مَا شَهِدْنَا مَهْلِكَ أَهْلِهِ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿٥١﴾ وَمَكْرُؤًا مَكْرًا وَمَكْرًا مَكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٢﴾

“Wakasema: Apishaneni kwa Mwenyezi Mungu tutamshambulia usiku yeye na ahali wake; kisha tutamuambia mrithi wake: Sisi hatukuona maangamizo ya watu wake, na sisi bila ya shaka tunasema kweli. Basi wakapanga vitimbi (vyao); na Sisi Tukapanga Mipango (Yetu, Tukapangua vitimbi vyao) na hali ya kuwa hawana habari”. (27:49-51)

Walipomaliza hilo na kujulishana, walikuja usiku ili wamuue Nabii wa Allah تعالى. Allah تعالى Ambaye Ndiye Mwenye Ushindi pamoja na Mtume Wake, Aliwaangushia mawe yaliyowaponda wao kwanza kabla ya kaumu yao. Katika siku ya Al-Khamis, ambayo ilikuwa ndiyo siku ya kwanza kati ya tatu za kumngojea, watu waliamka huku nyuso zao zikiwa za rangi ya njano, kama Saleh عليه السلام alivyowaahidi. Siku ya pili ya kumngojea, ambayo ilikuwa Ijumaa, waliamka huku nyuso zao zikiwa nyekundu. Katika siku ya tatu ya kustarehe, ambayo ilikuwa Jumamosi, waliamka na nyuso zao zimekuwa nyeusi. Walipoamka katika siku ya Jumapili wakawa wananukia harufu ya *Hanut* (manukato kwa ajili ya kumtilia maiti kabla hajazikwa). Wakakaa kuingojea nakama ya Allah تعالى na Adhabu Yake, Tunamuomba Allah تعالى Atukinge dhidi ya hilo. Walikuwa hawajui watakachokifanya wala namna adhabu itakavyowajia. Jua likachomoza, ikawajia *Sayhah* (mlio mkali) kutoka mbinguni, na mtikisiko mkali kutokea chini yao. Roho zao zikatolewa na miili ikakosa uhai, katika saa moja tu.

فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَنِيحِينَ

"...wakawa majumbani mwao kifudifudi wamekwishakufa".

Maana yake: Wamekufa, roho zimeshatoka, wala hakuna aliyesalimika miongoni mwao, si mdogo wala mkubwa, si mwanaume wala mwanamke. Isipokuwa kijakazi mmoja mlemavu aliyelitwa Kalbah bint As-Salq. Pia alikuwa akiitwa Az-Zurayqah. Na alikuwa kafiri aliyeshitadi kwa uadui dhidi ya Saleh عليه السلام. Alipoyaona hayo, miguu yake iliweza kutembea. Akasimama na kukimbia kwa kasi kubwa sana. Akafika katika eneo mojawapo ambapo kulikuwa na watu waliokuwa hai, akawapasha khabari za yaliyowakuta kaumu yake. Akawaomba maji ya kunywa. Akafa baada ya kuyanywa¹.

Maulamaa wa *Tafsir* walisema: Hakuna aliyesalia katika dhuriya ya Thamud isipokuwa Saleh عليه السلام na wafuasi wake. Kafiri mmoja aliyelitwa Abu Righal alikuwa katika eneo takatifu wakati nakama ilipowaangukia watu wa kaumu yake. Akiwa huko mahali patakatifu, hakupatwa na jambo, siku moja alitoka kwenda kutaka radhi, akajiwa na jive kutoka mbinguni likamuua. Abdurazaq amepokea kutoka kwa Ma'mar kutoka kwa Ismail bin Umayyah alinijulisha kwamba Mtume ﷺ alipita katika kaburi la Abu Righal, akasema;

«أَتَذُرُونَ مَنْ هَذَا؟» قالوا الله ورسوله أعلم، قال «هَذَا قَبْرُ أَبِي رِغَالٍ رَجُلٍ مِنْ ثَمُودَ كَانَ فِي حَرَمِ اللَّهِ فَمَتَّعَهُ حَرَمُ اللَّهِ عَذَابَ اللَّهِ، فَلَمَّا خَرَجَ أَصَابَهُ مَا أَصَابَ قَوْمَهُ فَدُفِنَ هَاهُنَا وَدُفِنَ مَعَهُ عُضْرٌ مِنْ ذَهَبٍ، فَتَزَلَّ الْقَوْمُ فَاثْبَدَرُوهُ بِأَسْيَافِهِمْ فَبَحَثُوا عَنْهُ فَاسْتَخْرَجُوا الْعُضْرَ»

"Mnamjua ni nani huyu?" Wakasema, "Allah تعالى na Mjumbe Wake wanajua zaidi". Akasema, "Hili ni kaburi la Abu Righal, ni mtu mmoja wapo katika Thamud. Alikuwa katika sehemu tukufu ya Allah تعالى, basi hiyo sehemu ikamuokoa na adhabu ya Allah تعالى. Alipoondoka kutoka sehemu hiyo, alipatwa na yaliyoipata kaumu yake na akazikwa hapa pamoja na tawi lililotengenezwa kwa dhahabu". Watu wakafanya haraka kwa mapanga yao kuitafuta dhahabu hiyo na wakalikuta tawi hilo."²

¹ At-Tabari 12:537.

² Abdur-Razaq 2:232.

'Abdur-Razzaq alisema: Ma'mar alisema: Az-Zuhri alisema kuwa Abu Righal ni baba wa kabila la Thaqif¹.

فَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَنفَوِّرْ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَةَ رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ وَلَكِن لَّا تُحِبُّونَ
النَّصِيحِينَ ﴿٧٩﴾

79. Basi Saleh akawaacha na akasema: Enyi watu wangu! Nilikufikishieni Ujumbe wa Mola wangu Mlezi, na nikakunasihini, lakini nyinyi hamuwapendi wenye nasaha.

Haya ni maneno ya maonyo ambayo Saleh عليه السلام aliambia kaumu yake. Allah تعالى Alipowaangamiza kwa kukhalifu kwao na kumuasi Allah تعالى na kukataa kwao kuukubali ukweli na kujitenga kwao na Hidaya kwa kuukhitari upotovu. Saleh عليه السلام aliwaambia hayo ya kuonya na makaripio baada ya kuangamia kwao, na wao walikuwa wakiyasikia hayo (kama muujiza kwa Nabii Saleh عليه السلام kutoka kwa Allah تعالى). Halikadhalika, *Sahih* Mbili zilinukuu kwamba baada ya Mtume ﷺ kuwashinda makafiri katika vita vya Badr, alibakia katika eneo hilo kwa siku tatu, kisha akapanda juu ya ngamia wake ambaye aliandaliwa kwa ajili yake baada ya theluthi ya mwisho ya usiku. Alipanda, kisha akaondoka na akasimama karibu na kisima cha Badr, na akasema;

«يَا أَبَا جَهْلٍ بَنَ هِشَامٍ يَا عُبَيْةَ بَنَ رِبِيعَةَ يَا شَيْبَةَ بَنَ رِبِيعَةَ وَيَا فُلَانَ بَنَ فُلَانٍ هَلْ وَجَدْتُمْ مَا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا،؟ فَإِنِّي وَجَدْتُ مَا وَعَدَنِي رَبِّي حَقًّا»

“Ewe Abu Jahl bin Hisham! Ewe ‘Utbah bin Rabi’ah! Ewe Shaybah bin Rabi’ah! Na ewe fulani bin fulani! Je, Mmeyakuta Aliyokuahidini Allah تعالى kwamba ni kweli?” Kwani mimi nimeyakuta Aliyoniahidi Mola wangu kwamba ni kweli”.

'Umar رضي الله عنه akamuambia, “Ewe Mjumbe wa Allah! Kwa nini unaongea na watu waliokufa na kuoza?” Akasema;

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ مَا أَنْتُمْ بِأَسْمَعَ لِمَا أَقُولُ مِنْهُمْ وَلَكِنْ لَا يُجِيبُونَ»

“Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Nyinyi hamuyasikii ninayoyasema zaidi yao, lakini hawawezi kujibu”².

Halikadhalika Saleh عليه السلام aliambia kaumu yake;

¹ Abdur-Razzaq 2:232.

² Fat’hul Al-Bari 7:351 na Muslim 4:2204.

لَقَدْ أَرْسَلْنَاكُمْ رَسُولًا نَبِيًّا وَتَصَحَّتْ لَكُمْ

“Nilikufikishieni Ujumbe wa Mola wangu Mlezi, na nikakunasihini”.

Maana yake: Hamkunufaika na hilo, kwa sababu nyinyi ni watu msiopenda ukweli, wala hamuifuati nasaha. Ndiyo sababu akasema;

وَلَكِنْ لَا تُحِبُّونَ النَّصِيحِينَ

“...lakini nyinyi hamuwapendi wenye nasaha”.

وَلُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَتَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِّنَ الْعَالَمِينَ ﴿٨٠﴾

إِنَّكُمْ لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِّنْ دُونِ النِّسَاءِ ۗ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ ﴿٨١﴾

80. Na Tulimtuma Lut', alipowaambia watu wake: Je, mnafanya uchafu ambao hajakutangulieni yeyote kwa uchafu huo katika viumbe vyote!

81. Hivyo nyinyi mnawaingilia wanaume kwa matamanio mkawaacha wanawake? Kumbe nyinyi ni watu wafujaji!”

Kisa cha Lu't عليه السلام na Kaumu Yake.

Allah تعالى Anasema;

وَ

“Na”. Kwa hakika, Tulimpeleka, **“Lu't”** au, inaweza kukadiriwa hivi, **“Na”** umtaje;

لُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ

“Lut', alipowaambia watu wake”. Lut عليه السلام bin Haaran bin Azar, alikuwa mtoto wa nduguye Al-Khalil Ibrahim عليه السلام. Alikuwa ameamini pamoja na Ibrahim عليه السلام na akahama naye mpaka katika ardhi ya Sham, na Allah تعالى Akampeleka Lut عليه السلام katika ardhi ya Sadum (Sodoma) na miji iliyoizingira. Alikuwa akiwalingania kwa Allah تعالى na kuwaamuru mema na kuwakataza maovu waliyoyaanzisha na hayakuwepo kwa wanaadamu wa kabla yao wala wengineo. Nalo ni jambo la kuwaendea wanaume badala ya wanawake. Hili ni jambo ambalo mwanadamu alikuwa halijui wala halikuwahi kupita katika akili yake mpaka walipolifanya watu wa Sodoma, laana za Allah تعالى ziwashukie. 'Amr bi Dinar aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِّنَ الْعَالَمِينَ

“...ambao hajakutangulieni yeyote kwa uchafu huo katika viumbe vyote!”

Akasema, “Hakukuwepo kuingiliana baina ya mwanaume na mwanaume hapo kabla ya kaumu ya Lut عليه السلام¹. Kwa ajili hii, Lut aliwaambia’

أَتَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِّنَ الْعَالَمِينَ ﴿٧٣﴾ إِنَّكُمْ لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ
شَهْوَةً مِّنْ دُونِ النِّسَاءِ

“Je, mnafanya uchafu ambao hajakutangulieni yeyote kwa uchafu huo katika viumbe vyote! Hivyo nyinyi mnawaingilia wanaume kwa matamanio mkawaacha wanawake?”

Maana yake: Mmewaacha wanawake, ambao Allah تعالى Aliwaumba minajili yenu mkawaenda wanaume. Huu ni uchafu wenu na pia ni ujinga, kwa kukiweka kitu pasipo mahali pake. Kwa ajili hii, aliwaambia katika Aya nyingine;

هَؤُلَاءِ بَنَاتِي إِنْ كُنْتُمْ فَاعِلِينَ

“Akasema: Hawa binti zangu, ikiwa nyinyi ni watendaji”. (15:71)

Akawaelekeza kwa wanawake wao, wakajidai kutoa udhuru kwamba hawana haja na wanawake;

قَالُوا لَقَدْ عَلِمْتَمَا لَنَا فِي بَنَاتِكَ مِنْ حَقٍّ وَإِنَّكَ لَتَعْلَمُ مَا نُرِيدُ ﴿٧٩﴾

“Wakasema: Bila ya shaka umekwisha jua hatuna haki juu ya binti zako, na unayajua tunayoyataka”. (11:79)

Wakimaanisha kuwa, unajua kwamba sisi hatuna matamanio wala utashi kwa wanawake. Na wewe unayajua makusudio yetu kwa wageni wako.

وَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَخْرِجُوهُمْ مِّنْ قَرْيَتِكُمْ^ط إِنَّهُمْ أَنَاسٌ
يَتَطَهَّرُونَ ﴿٨٤﴾

¹ At-Tabari 12:534.

**82. Na haikuwa Jawabu ya kaumu yake isipokuwa kuambizana:
Wafukuzeni katika mji wenu, maana hao ni watu wanaojitakasa.**

Maana yake: Hawakumjibu Lut عليه السلام, bali walichokusudia ni kumuondoa na kumfukuza yeye na waliokuwa pamoja naye watoke mjini kwao. Allah تعالى Akamtoa akiwa salama na Akawaangamiza katika ardhi yao wakiwa wamefedheheka na kudhalilika. Kauli ya Allah تعالى;

إِنَّهُمْ أَنَاسٌ يَتَطَهَّرُونَ

“...maana hao ni watu wanaojitakasa”.

Qatadah alisema, “Walimuaibisha Lut عليه السلام (pamoja na Waumini) na wala wao hawakuwa na dosari yoyote.”¹ Akasema Mujahid, “(Kaumu yake walimsema Lut عليه السلام na Waumini) Wao ni watu wanaotaka kujitwaharisha dhidi ya vinyo (tupu za nyuma) vya wanaume na wanawake”². Pia ilinukuliwa kama hivyo kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما.

فَأَنجَيْنَاهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا أُمَّرَأَتَهُ كَانَتْ مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٧٣﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا فَانظُرْ
كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِينَ ﴿٧٤﴾

**83. Basi Tukamuokoa yeye na watu wake, isipokuwa mkewe,
alikuwa miongoni mwa waliobakia nyuma.**

**84. Na Tukawamiminia mvua. Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho
wa wakosefu.**

Allah تعالى Anasema, Tukamuokoa Lut عليه السلام na ahli wake, wala hakuna aliyeamini katika wao isipokuwa watu wa nyumbani kwake tu. Sawa na Alivyosema Allah تعالى;

فَأَخْرَجْنَا مَنْ كَانَ فِيهَا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٥﴾ فَمَا وَجَدْنَا فِيهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٧٦﴾

**“Kwa hivyo Tukawatoa katika hao wale walioamini. Lakini
Hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu”. (51:35-
36)**

¹ At-Tabari 12:550.

² At-Tabari 12:550.

Isipokuwa mkewe tu (katika familia yake) ndiye ambaye hakumuamini, bali alikuwa katika dini ya kaumu yake, akila njama pamoja nao dhidi ya Lut عليه السلام na kuwajulisha juu ya wageni wanaokuja kumtembelea, kwa njia ya kupeana ishara baina yao. Hii ndiyo sababu, Lut عليه السلام alipoamriwa aondoke usiku pamoja na familia yake, aliamriwa asimjulishe wala kumchukua mkewe kutoka katika mji. Kuna wanaosema: Aliwafuata, adhabu ilipowasili, aligeuka, hivyo ikamsibu kama ilivyowasibu. Lililo dhahiri zaidi ni kwamba hakutoka katika mji, wala Lut عليه السلام hakumjulisha, bali alibakia pamoja nao. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

إِلَّا أَمْرًا تُدْرِكُهُ كَانَتْ مِنَ الْغَيْرِينَ

“...isipokuwa mkewe, alikuwa miongoni mwa waliobakia nyuma”.

Maana yake: Waliosalia. Pia kwamba inamaanisha: Walioangamia. Hii ndiyo tafsiri iliyo wazi zaidi. Kauli ya Allah تعالى;

وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا

“Na Tukawamiminia mvua”.

Inatafsiriwa na Kauli Yake nyingine;

وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ مَّنضُودٍ ﴿٧٣﴾ مُسَوَّمَةً عِنْدَ رَبِّكَ وَمَا هِيَ مِنَ الظَّالِمِينَ بِبَعِيدٍ ﴿٧٤﴾

“Na Tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu uliokamatana wa Motoni. Zilizotiwa alama kwa Mola wako Mlezi. Na haya hayako mbali na wenye kudhulumu wengineo”. (11:82-83)

Kwa sababu hii, Allah تعالى Alisema;

فَأَنْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِينَ

“Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa wakosefu”.

Maana yake: Angalia ewe Muhammad ﷺ, namna ulivyokuwa ukomo wa waliothubutu kumuasi Allah تعالى na kuwakadhibisha Mitume Wake. Imamu Ahmad, Abu Dawud, At-Tirmidhi, Ibn Majah, waliinukuu Hadithi kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kwamba Mtume ﷺ alisema;

«مَنْ رَجَدْنُمُوهُ يَعْمَلْ عَمَلٌ قَوْمِ لُوطٍ فَأَقْتُلُوا فَاعِلًا وَالْمَفْعُولُ بِهِ»

"Mtakaowakuta wakifanya amali za kaumu ya Lut, basi muueni mtenda na mtendewa".¹

* * *

¹ Ahmad 1:300, At-Tirmidhi 1456, Abu Dawud 4462 na Ibn Majah 2561.

وَالِى مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا ۗ قَالَ يَنْقَوِرَ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنَ إِلَهِ غَيْرُهُ ۗ قَدْ جَاءَتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ ۗ فَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا ۗ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٨٥﴾ وَلَا تَقْعُدُوا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُونَ وَتَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ مَن ءَامَنَ بِهِ وَتَبْغُونَهَا عِوَجًا ۗ وَأَذْكُرُوا إِذْ كُنْتُمْ قَلِيلًا فَكَتَرْتُمْ ۗ وَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِينَ ﴿٨٦﴾ وَإِن كَانَ طَآئِفَةٌ مِّنكُمْ ءَامَنُوا بِآلِذِي أُرْسِلَتْ بِهِ وَطَآئِفَةٌ لَّمْ يُؤْمِنُوا فَاصْبِرُوا حَتَّىٰ يَحْكُمَ اللَّهُ بَيْنَنَا ۗ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ ﴿٨٧﴾

وَالِى مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا ۗ قَالَ يَنْقَوِرَ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنَ إِلَهِ غَيْرُهُ ۗ قَدْ جَاءَتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ ۗ فَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا ۗ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٨٥﴾

85. Na kwa watu wa Madyana Tulimtuma ndugu yao Shua'ib Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Hamna mola mwengine isipokuwa

Yeye. Imekwisha kufikieni hoja za wazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Basi timizeni sawasawa vipimo na Mizani, wala msiwapunje watu vitu vyao, wala Msifanye uharibifu katika nchi, baada ya kuwa imekwishatengenea. Hivi ndivyo bora kwenu ikiwa nyinyi ni Waumini.

Kisa cha Shu'ayb عليه السلام na Ardhi ya Madyan.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema, "Wao (watu wa Madyan) ni dhuriya wa Madyan bin Midyaan bin Ibrahim. Shu'ayb عليه السلام ni mwana wa Mikil bin Yashjur, na kwa lugha ya watu wa Kisariyani, jina lake lilikuwa, Yathrun (Jethro).¹ Mimi (Ibn Kathir) nasema, Madyan lilikuwa jina la kabila na la mji uliokuwa jirani na Ma'an katika njia ya kuelekea Hijaz (kutokea Ash-Sham).

¹ At-Tabari 12:554.

Allah تعالى Alisema;

وَلَمَّا وَرَدَ مَاءَ مَدْيَنَ وَجَدَ عَلَيْهِ أُمَّةً مِّنَ النَّاسِ يَسْقُونَ

“Na alipoyafikia maji ya Madyana alikuta umati wa watu wananyweshwa (wanyama wao).” (28:23)

Na wao ni masahiba wa Al-Aykah (mwitu) kama tutakavyoeleza, *In sha Allah*, na tunamuamini Yeye.

قَالَ يَنْقَوْمِ اَعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنِّ إِلٰهِ غَيْرُهُ

“Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Hamna mola mwengine isipokuwa Yeye”. (7:85)

Huu ni ulinganu wa Mitume wote.

قَدْ جَاءَتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ

“Hakika imekwisha kufikieni hoja za wazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi”.

Maana: Allah تعالى Ameleta hoja na ushahidi wa kuyasadikisha niliyokujieni nayo. Kisha akawawaidhi juu ya kuamiliana kwao na watu, kwamba wawe wanakamilisha vipimo na uzani, wala wasiwapunje watu katika vitu vyao. Yaani, wasiwakhini watu katika mali zao na kuichukua kwa njia ya upunjaji, ambayo ni upungufu katika vipimo na uzani na kufanya ghiliba. Sawa na Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine.

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ

“Ole wao hao wapunjao”. (83:1) Mpaka Aliposema;

لِرَبِّ الْعَالَمِينَ

“Mola Mlezi wa walimwengu wote?” (83:6)

Hili ni tishio kali na ahadi yenye msisitizo mkubwa, tunamuomba Allah تعالى Atuokoe dhidi ya hayo. Kisha Allah تعالى Alieleza khabari za Shu'ayb عليه السلام ambaye anaitwa, “Msemaji wa Mitume”, kwa sababu ya ufasaha wa maneno yake, na umbuji wa mawaidha yake.

وَلَا تَقْعُدُوا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُونَ وَتَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ مَن ءَامَنَ بِهِ
 وَتَبْغُونَهَا عِوَجًا ۗ وَأَذْكُرُوا إِذْ كُنْتُمْ قَلِيلًا فَكَثَرْتُمْ ۗ وَأَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
 الْمُفْسِدِينَ ﴿٨٦﴾ وَإِن كَانَ طَآئِفَةٌ مِّنْكُمْ ءَامَنُوا بِأَلَّذِي أُرْسِلْتُ بِهِ وَطَآئِفَةٌ لَّمْ يُؤْمِنُوا
 فَاصْبِرُوا حَتَّىٰ يَحْكُمَ اللَّهُ بَيْنَنَا ۗ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ ﴿٨٧﴾

86. Wala msikae katika kila njia mkitisha watu, na kuwazuilia na njia ya Mwenyezi Mungu wale wenye kumuamini, na mkataka njia ipotoke. Na kumbukeni mlipokuwa wachache, naye Akakufanyeni kuwa wengi. Na tazameni jinsi ulivyokuwa mwisho wa mafisadi.

87. Na kama liko kundi miongoni mwenu lililoamini haya niliyotumwa, na kundi jengine halikuamini, basi subirini mpaka Mwenyezi Mungu Ahukumu baina yetu. Naye Ndiye Mbora wa wenye kuhukumu.

Shu'ayb عليه السلام Anawakataza dhidi ya kuweka vizuizi njiani, kihisia na kimaana, kwa kusema;

وَلَا تَقْعُدُوا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُونَ

“Wala msikae katika kila njia mkitisha watu”.

Maana: Kuwatisha watu juu ya kuwaua ikiwa hawatakupeni mali zao. As-Suddi na wengine walisema, “Walikuwa maharamia”.¹ Ibn ‘Abbas, Mujahid na wengine رضي الله عنهم, walizungumzia Aya;

وَلَا تَقْعُدُوا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُونَ

“Wala msikae katika kila njia mkitisha watu”.

Maana: “Mnawatisha Waumini wanaokuja kwa Shu'ayb عليه السلام ili wamfuate”.² Maana ya mwanzo iko dhahiri zaidi, kwani alisema;

بِكُلِّ صِرَاطٍ

“...katika kila njia...”

¹ At-Tabari 12:557.

² At-Tabari 12:557.

وَتَصُدُّونَ عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ مَنَّ ءَامَنَ بِهِ وَتَبْغُونَهَا عِوَجًا

“...na kuwazuilia na njia ya Mwenyezi Mungu wale wenye kumuamini, na mkataka njia ipotoke”.

Na maana ya pili ni Kauli Yake;

وَأَذْكُرُوا إِذْ كُنْتُمْ قَلِيلًا فَكَفَرْتُمْ

“Na kumbukeni mlipokuwa wachache, naye Akakufanyeni kuwa wengi”.

Maana: Mlikuwa dhaifu kwa sababu ya uchache wenu, lakini baadaye mkawa na nguvu kwa sababu ya wingi wenu. Basi mkumbukeni Allah تعالى juu ya hilo.

وَأَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِينَ

“Na tazameni jinsi ulivyokuwa mwisho wa mafisadi”.

Maana yake: Katika umma na karne zilizopita na adhabu na nakama zilizowakumba kwa kuthubutu kwao kumuasi Allah تعالى na kuwakadhibisha wajumbe wake.

وَإِن كَانَ طَآئِفَةٌ مِّنْكُمْ ءَامَنُوا بِآلِدِي أُرْسِلَتْ بِهِ وَطَآئِفَةٌ لَّمْ يُؤْمِنُوا

“Na kama liko kundi miongoni mwenu lililoamini haya niliyotumwa, na kundi jengine halikuamini”.

Maana: Mmetofautiana nami.

فَاصْبِرُوا

“...basi subirini”. Maana yake: Ngojeni.

حَتَّىٰ يَخُصِمَ اللَّهُ بَيْنَنَا

“...mpaka Mwenyezi Mungu Ahukumu baina yetu”. Na nyinyi.

وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ

“Naye Ndiye Mbora wa wenye kuhukumu”. Kwani Yeye Ataujaalia mwisho mwema uwe ni kwa wachamungu, huku maangamizo yatakuwa kwa makafiri.

* قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا مِنْ قَوْمِهِ لَنُخْرِجَنَّكَ
 يَشْعِيبَ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَكَ مِنْ قَرْيَتِنَا أَوْ لَتَعُوذُنَّ فِي
 مِلَّتِنَا ۚ قَالَ أُولُو كُنُفٍ كَرِهِينَ ﴿٨٨﴾ قَدْ أَفْتَرْنَا عَلَى اللَّهِ
 كَذِبًا إِنْ عُدْنَا فِي مِلَّتِكُمْ بَعْدَ إِذْ نَجَّيْنَا اللَّهُ مِنْهَا وَمَا
 يَكُونُ لَنَا أَنْ نَعُودَ فِيهَا إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّنَا وَسِعَ رَبُّنَا
 كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا ۚ عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا ۚ رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ
 قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَأَنْتَ خَيْرُ الْفَاتِحِينَ ﴿٨٩﴾ وَقَالَ الْمَلَأُ
 الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ لَئِن آتَيْتُم شُعَيْبًا إِنْ كُنَّا إِذَا
 لَخَسِرُونَ ﴿٩٠﴾ فَأَخَذْتُمُ الرِّجْفَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ
 جِثْمِينَ ﴿٩١﴾ الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَأَن لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا
 الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَانُوا هُمُ الْخَاسِرِينَ ﴿٩٢﴾
 فَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَاقَوْمِ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي
 وَنَصَحْتُ لَكُمْ فَكَيْفَ ءَأَسَىٰ عَلَىٰ قَوْمٍ كَافِرِينَ ﴿٩٣﴾
 وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّبِيٍّ إِلَّا أَخَذْنَا أَهْلَهَا بِالْبَأْسَاءِ
 وَالضَّرَّاءِ لَعَلَّهُمْ يَضُرَّعُونَ ﴿٩٤﴾ ثُمَّ بَدَلْنَا مَكَانَ السَّيِّئَةِ
 الْحَسَنَةَ حَتَّىٰ عَفَوْا وَقَالُوا قَدْ مَسَّ ءَابَاءَنَا الضَّرَّاءُ
 وَالسَّرَّاءُ فَأَخَذْنَاهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٩٥﴾

* قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا مِنْ
 قَوْمِهِ لَنُخْرِجَنَّكَ يَشْعِيبَ وَالَّذِينَ
 ءَامَنُوا مَعَكَ مِنْ قَرْيَتِنَا أَوْ لَتَعُوذُنَّ
 فِي مِلَّتِنَا ۚ قَالَ أُولُو كُنُفٍ كَرِهِينَ ﴿٨٨﴾
 قَدْ أَفْتَرْنَا عَلَى اللَّهِ كَذِبًا إِنْ عُدْنَا
 فِي مِلَّتِكُمْ بَعْدَ إِذْ نَجَّيْنَا اللَّهُ مِنْهَا
 وَمَا يَكُونُ لَنَا أَنْ نَعُودَ فِيهَا إِلَّا أَنْ
 يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّنَا وَسِعَ رَبُّنَا كُلَّ شَيْءٍ
 عِلْمًا ۚ عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا ۚ رَبَّنَا افْتَحْ
 بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَأَنْتَ خَيْرُ
 الْفَاتِحِينَ ﴿٨٩﴾

**88. Waheshimiwa walio-
 takabari katika kaumu
 yake wakasema: Ewe
 Shu'ayb! Tutakutoa wewe
 pamoja na wale walio-
 kuamini katika mji wetu,
 au mrejee katika mila
 yetu. Akasema: Je, ingawa
 tunaichukia?**

**89. Bila ya shaka itakuwa
 tumemzuilia uwongo**

**Mwenyezi Mungu tukirudi katika mila yenu baada ya kuisha tuokoa nayo
 Mwenyezi Mungu. Wala haiwi kwetu sisi kuirejea mila hiyo, ila Akitaka
 Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wetu. Ujuzi wa Mola Mlezi wetu umeenea**

katika kila kitu. Kwa Mwenyezi Mungu tunategemea. Ewe Mola Mlezi wetu! Tuhukumie baina yetu na kaumu yetu kwa haki, Nawe Ndiye Mbora wa wanao hukumu”.

Hii ni khabari Anayowieleza Allah تعالى juu ya makafiri walivyomjibu Nabii Wake, Shu'ayb عليه السلام na Waumini waliokuwa pamoja naye, kwa kuwatishia kuwatoa katika kijiji, au kuwalazimisha kurejea katika mila zao na kuwa nao pamoja katika mila hizo walizo nazo wao. Haya ni mazungumzo yaliyofanywa kwa Mtume ﷺ, lakini walikusudiwa pia wafuasi wake waliokuwa naye pamwe katika dini yake. Kauli Yake تعالى:

أُولَٰئِكَ كَرِهِينَ

“Je, ingawa tunaichukia?”

Maana yake: Mtatufanyia hayo hata kama tunayachukia mnyotuitia, sisi tukikubali kurudi katika mila zenu, na tukaingia kuungana pamoja nanyi katika yale mliyo nayo, tutakuwa tumefanya uongo mkubwa kwa Allah تعالى kwa kumfanyia washirika kuwa washindani. Na haya ndiyo majibu ya wafuasi wake;

وَمَا يَكُونُ لَنَا أَنْ نَعُودَ فِيهَا إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّنَا

“Wala haiwi kwetu sisi kuirejea mila hiyo, ila Akitaka Mwenyezi Mungu”.

Hili limerudishwa katika Utashi wa Allah تعالى, kwa sababu Yeye Anajua kila kitu na Elimu Yake imekizingira kila kitu.

عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا

“Kwa Mwenyezi Mungu tunategemea”.

Maana yake: Juu ya mambo yetu tuyafanyayo na tunayoyaacha.

رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ

“Ewe Mola Mlezi wetu! Tuhukumie baina yetu na kaumu yetu kwa haki”.

Maana yake: Pitisha hukumu baina yetu na kaumu yetu, na Utupe ushindi dhidi yao.

وَأَنْتَ خَيْرُ الْفَاتِحِينَ

“...Nawe Ndiye Mbora wa wanaohukumu”.

Maana yake: Mbora wa Mahakimu, kwani Wewe ni Muadilifu Ambaye Humkandamizi yeyote abadani.

وَقَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ لِيَنْ آتِبَعْتُمْ شُعَيْبًا إِنْ كُنَّا إِذَا لَخَسِرُونَ ﴿٨٨﴾ فَأَخَذْتَهُمُ
الرَّجْفَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جِثْمِينَ ﴿٨٩﴾ الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَأَنْ لَمْ يَغْتَوْا فِيهَا
الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَانُوا هُمُ الْخَاسِرِينَ ﴿٩٠﴾

90. Na waheshimiwa waliokufuru katika kaumu yake wakasema: Mkimfuata Shu'aib, basi hakika hapo nyinyi mtakuwa mliokhasiri.

91. Basi tetemeko la ardhi likawanyakua, na wakaamkia majumbani mwao wamejifudikiza, wamekwishakufa.

92. Wale waliomkanusha Shu'aib wakawa kama kwamba hawakuwako. Waliomkanusha Shu'aib ndio waliokuwa wenye kukhasiri.

Allah تعالى Anaeleza ukubwa uliokithiri wa ukafiri, ulfidhuli na uasi wao na upotevu walio nao (kaumu ya Shu'aib عليه السلام) na yaliyomo nyoyoni mwao juu ya kukhalifu ukweli. Kwa sababu hiyo waliapa na wakasema;

لِيَنْ آتِبَعْتُمْ شُعَيْبًا إِنْ كُنَّا إِذَا لَخَسِرُونَ

“Mkimfuata Shu'aib, basi hakika hapo nyinyi mtakuwa mliokhasiri”.

Minajili hiyo, Aliwaadhibu kwa Kauli Yake;

فَأَخَذْتَهُمُ الرَّجْفَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جِثْمِينَ ﴿٨٩﴾

“Basi tetemeko la ardhi likawanyakua, na wakaamkia majumbani mwao wamejifudikiza, wamekwishakufa”.

Allah تعالى Ameeleza hapa kwamba, walipatwa na zilzala, kwa sababu ya kumtishia kwao Shu'aib عليه السلام na masahaba wake.

Sawa na Alivyowazungumzia Allah تعالى katika Surat Hud;

وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا شُعَيْبًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَأَخَذَتِ الَّذِينَ ظَلَمُوا
الصَّيْحَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دِيَارِهِمْ جَنِيثِينَ ﴿١١٩﴾

“Na ilipofika Amri Yetu, Tulimuokoa Shu’aib na wale walioamini pamoja naye kwa Rehema Yetu. Na ukelele uliwanyakua waliodhulumu, na wakapambazukiwa majumbani mwao wamekufa kifudifudi!” (11:94)

Aya hizi mbili zina mnasaba mmoja. Allah Aalam. Hayo ni baada ya kumdhihaki na kumuambia;

أَصَلُّوْا لِكُمْ تَأْمُرُكُمْ

“Ni Sala zako ndizo zinazokuamrisha”.

Ikaja Sayhah (ukele) na kuwanyamazisha. Katika Surat Ash-Shu’araa, Allah تعالى Anazungumzia khabari zao.

فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَهُمْ عَذَابٌ يَوْمِ الظُّلَّةِ ۗ إِنَّهُ كَانَ عَذَابٌ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٨٩﴾

“Basi walimkanusha na ikawashika adhabu ya siku kubwa”.
(26:189)

Hayo yalitokea kwa sababu wao walimuambia, kwa mujibu wa kisa kilivyoendelea,

فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ

“Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni”. (26:187)

Allah تعالى Aliwaeleza kuwa, walipatwa na adhabu hizi katika Siku ya Kivuli, Adhabu zote hizo ziliwaangukia wao. Kwanza;

فَأَخَذَهُمْ عَذَابٌ يَوْمِ الظُّلَّةِ ۗ

“...ikawashika adhabu siku ya kivuli”. (26:189)

Nayo ni mawingu yaliyowafunika, kumbe ndani yake yalikuwa na cheche za moto, miale na mwangaza mkubwa. Kisha ikaja kelele kali kutokea mbinguni na zilzala kali kwa chini yao ardhini. Roho zikatolewa, uhai ukaondoka na miili ikawa mitupu.

فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَنِيمِينَ

“...na wakaamkia majumbani mwao wamejifudikiza, wamekwisha kufa”.

Kisha Allah تعالى Akasema;

كَأَن لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا

“...kama kwamba hawakuwako”.

Kwa nakama ilivyowasibu, walikuwa kana kwamba hawakuwahi kuishi katika nyumba zao ambazo walitaka kumfukuza Mtume عليه السلام na masahaba wake. Kisha, Allah تعالى Akawakabili na Kuwakanushia madai yao.

الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَانُوا هُمُ الْخَاسِرِينَ

“Waliomkanusha Shu'aib ndio waliokuwa wenye kukhasiri”.

فَتَوَلَّى عَنْهُمْ وَقَالَ يَنْقَوْمٍ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ فَكَيْفَ ءَأَسَىٰ
عَلَىٰ قَوْمٍ كَافِرِينَ ﴿٩٣﴾

93. Basi akawaachilia mbali na akasema: Enyi kaumu yangu! Nimekufikishieni Ujumbe wa Mola Mlezi wangu, na nimekunasihini; basi vipi niwahuzunikie watu makafiri?

Nabii Shu'aib عليه السلام aliwaacha baada ya adhabu, nakama na maangamizo yaliyowasibu na akawaambia kwa kuwakaripia na kuwakosoa.

يَنْقَوْمٍ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ

“Enyi kaumu yangu! Nimekufikishieni Ujumbe wa Mola Mlezi wangu, na nimekunasihini”. (7:93)

Maana yake: Nimeyatekeleza kwenu yale niliyotumwa kwayo, basi sikujutieni kwani mliyakataa niliyokujieni nayo. Kwa ajili hiyo, alisema;

فَكَيْفَ ءَأَسَىٰ عَلَىٰ قَوْمٍ كَافِرِينَ

“...basi vipi niwahuzunikie watu makafiri?”

وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّبِيٍّ إِلَّا أَخَذْنَا أَهْلَهَا بِالْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ لَعَلَّهُمْ يَضَّرَّعُونَ ﴿٧٤﴾ ثُمَّ
 بَدَّلْنَا مَكَانَ السَّيِّئَةِ الْحَسَنَةَ حَتَّىٰ عَفَوْا وَقَالُوا قَدْ مَسَّ ءَابَاءَنَا الضَّرَّاءُ وَالسَّرَّاءُ
 فَأَخَذْنَاهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٧٥﴾

94. Na hatukumtuma Nabii yeyote katika mji ila Tuliwapatiliza wakaazi wake kwa taabu na mashaka ili wapate kunyenyekea.

95. Kisha Sisi Hubadilisha mahala pa ubaya kwa wema, hata wakazidi, na wakasema: Taabu na raha ziliwafikia baba zetu. Basi kwa ghafila Tukawashika, hali ya kuwa hawajatambua”.

Maangamizo Yaliyowakumba Kaumu Zilizotangulia.

Allah تعالی Anaeleza juu ya majaribio waliyopewa umma uliopita ambao Aliupelekea Mitume kwa Kuwapa *Ba-asaa na Dhwarraa*. *Ba-saa* ni maradhi na magonjwa yanayowapata katika miili yao. Na *Dhwarraa* ni ukafiri na haja zinazowakumba, na mfano wa hivyo;

لَعَلَّهُمْ يَضَّرَّعُونَ

“...ili wapate kunyenyekea”.

Maana yake: Wanaomba na wananyenyekea na kujitahidi katika maombi kwa Allah تعالی ili Ayaondoshe Aliyowateremshia. Maneno yanaweza kukadiriwa kwamba, Aliwapa mitihani mikali ili wanyenyekee, lakini hawakufanya hayo waliyotakiwa. Basi Allah تعالی Akawabadilishia hali na kuwa ya neema, ili apate kuwatahini, Kwa ajili hii Alisema;

ثُمَّ بَدَّلْنَا مَكَانَ السَّيِّئَةِ الْحَسَنَةَ

“Kisha Sisi Hubadilisha mahala pa ubaya kwa wema”.

Maana yake: Tunabadilisha hali kutoka shida na kuwa njema, kutoka maradhi hadi afya, kutoka ufakiri hadi utajiri, ili washukuru kwa hayo, lakini hawakufanya hivyo. Kauli Yake;

حَتَّىٰ عَفَوْا

“...hata wakazidi”. Maana yake: Wakaongezeka, na mali na watoto wao

wakakithiri. Neno 'Afaa lililiotumika katika Aya lina maana ya kukithiri.

وَقَالُوا قَدْ مَسَّ آبَاءَنَا الضَّرَّاءُ وَالسَّرَّاءُ فَأَخَذْنَاهُمْ بَعْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ

“...na wakasema: Taabu na raha ziliwafikia baba zetu. Basi kwa ghafla Tukawashika, hali ya kuwa hawajatambua”.

Allah تعالى Akasema, Tuliwapa mtihani huu na ule mwingine ili wanyenyekee na warudi kwa Allah تعالى. Hata hivyo hawakufaulu mtihani huu wala ule mwingine, wala hawakukoma kwa majaribio yote mawili, bali walisema, “Sisi tulikwishapata *Ba-saa na Dhwarraa*, lakini baadae inakuja kheri kama ilivyowapata baba zetu huko zamani. Kwa hivyo, ni mzunguko wenye kujirudia rudia, ambamo huwa tunapata tabu wakati fulani, kisha baadae inakuja kheri”.

Lakini hawakuitambua hekima ya Allah تعالى, wala hawakujua mtihani wa Allah تعالى kwao katika hali zote mbili. Hii ni tofauti na hali ya Waumini ambao huwa wanamshukuru Allah تعالى wakati wa faraji na kuwa na subra katika wakati wa *Dharraa*. Sawa na ilivyothibitishwa ndani ya *Sahih* Mbili.

«عَجَبًا لِلْمُؤْمِنِ لَا يَقْضِي اللَّهُ لَهُ قَضَاءَ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَاءٌ صَبِرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ سَرَّاءٌ شَكَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ»

*“Ni ajabu kwa Muumini, hapana kudura Aipitishayo Allah تعالى bali huwa ni kheri kwake, na akipatwa na madhara husubiri na hili ni la kheri kwake. Na anapopatwa na faraja hushukuru, na hilo ni kheri kwake”.*¹

Muumini, kwa hivyo, ndiye anayetambua mtihani wa Allah تعالى kwake kutokana na vipindi vya faraja na vya madhara. Pia katika Hadithi nyingine;

«لَا يَزَالُ الْبَلَاءُ بِالْمُؤْمِنِ حَتَّى يَخْرُجَ نَبِيًّا مِنْ دُنُوبِهِ، وَالْمُتَأَنِّقِ بِمِثْلِهِ كَمَثَلِ الْجِمَارِ لَا يَدْرِي فِيهِمْ رَبَطَهُ أَهْلُهُ وَلَا فِيهِمْ أَرْسَلُوهُ»

*“Mitihani haimuachi Muumini, mpaka atoke akiwa amesafika na dhambi zake. Na mfano wa mnafiki ni kama punda, hajui sababu ya mmiliki wake kumfunga wala ya kumtuma”.*²

¹ Muslim 4:2295.

² Ahmad 2:450.

Hivyo, Allah تعالى Aliweka mwisho mwema au mbaya kutokana na sifa hizo.

Kwa Kauli Yake;

فَأَخَذْنَا مِنْهُمُ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ

“Basi kwa ghafla Tukawashika, hali ya kuwa hawajatambua”.

Maana: Tutawachukua ghafla kwa adhabu, bila kujitambua, yaani kwa kushtukiza.

«مَوْتُ الْفَجَاءَةِ رَحْمَةً لِّلْمُؤْمِنِ وَأَخْذَةٌ لِّلْكَافِرِ»

*“Kifo cha ghafla ni cha rehema kwa Waumini, na ni cha majuto kwa kafiri”.*¹

* * *

¹ Ahmad 6:136.

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ ءَامَنُوا وَأَتَقُوا لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ
 مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ وَلَٰكِن كَذَّبُوا فَأَخَذْنَاهُم بِمَا
 كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٦﴾ أَفَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَنْ يَأْتِيَهُمْ
 بَأْسُنَا بَيِّنًا وَهُمْ نَائِمُونَ ﴿٩٧﴾ أَوَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَنْ
 يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا ضُحًى وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿٩٨﴾ أَفَأَمِنُوا مَكْرَ
 اللَّهِ ۗ فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٩٩﴾
 أَوَلَمْ يَهْدِ لِلَّذِينَ يَرِثُونَ الْأَرْضَ مِنْ بَعْدِ أَهْلِهَا أَنْ لَوْ
 نَشَاءُ أَصَبْنَاهُمْ بِذُنُوبِهِمْ ۗ وَنَطْبَعُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا
 يَسْمَعُونَ ﴿١٠٠﴾ تِلْكَ الْقُرَىٰ نَقِصُ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبِيَآئِهَا
 وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا بِمَا
 كَذَّبُوا مِنْ قَبْلُ ۗ كَذَٰلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِ
 الْكٰفِرِينَ ﴿١٠١﴾ وَمَا وَجَدْنَا لِأَكْثَرِهِمْ مِنْ عَهْدٍ ۗ وَإِن
 وَجَدْنَا أَكْثَرَهُمْ لَفٰسِقِينَ ﴿١٠٢﴾ ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ
 مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَآئِمِهِ فَظَلَمُوا بِهَا ۗ فَانظُرْ
 كَيْفَ كَانَتْ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٠٣﴾

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ ءَامَنُوا وَأَتَقُوا
 لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ مِنَ السَّمَاءِ
 وَالْأَرْضِ وَلَٰكِن كَذَّبُوا فَأَخَذْنَاهُم
 بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٦﴾ أَفَأَمِنَ
 أَهْلُ الْقُرَىٰ أَنْ يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا بَيِّنًا
 وَهُمْ نَائِمُونَ ﴿٩٧﴾ أَوَأَمِنَ أَهْلُ
 الْقُرَىٰ أَنْ يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا ضُحًى
 وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿٩٨﴾ أَفَأَمِنُوا مَكْرَ
 اللَّهِ ۗ فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ
 الْخَاسِرُونَ ﴿٩٩﴾

96. Na lau kuwa watu wa
 miji wangeliamini na
 wakamchamungu, kwa
 yakini Tungeliwafungulia
 baraka kutoka mbinguni
 na katika ardhi. Lakini wali
 kanusha basi Tukawa-
 patiliza kwa sababu ya
 yale waliyokuwa waki-
 yachuma.

97. Je, watu wa mijini wameaminisha ya kuwa Adhabu Yetu haitawafikia usiku, nao wamelala?

98. Au watu wa mijini wameaminisha ya kuwa Adhabu Yetu haitawafikia mchana, nao wanacheza?

99. Je, wamejiaminisha na Mipango ya Mwenyezi Mungu? Kwani hawajiaminishi na Mipango ya Mwenyezi Mungu ila watu wenye kukhasiri.

Neema Huja na Imani, Wakati Ukafiri Husababisha Adhabu.

Allah تعالى Anaeleza juu ya uchache wa Imani wa miji ambayo walipelekewa Mitume. Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةٌ ءَامَنَتْ فَنفَعَهَا إِيمُنُهَا إِلَّا قَوْمَ يُونُسَ لَمَّا ءَامَنُوا كَشَفْنَا عَنْهُمْ عَذَابَ
الْخِزْيِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٩٨﴾

“Kwa nini usiwepo mji mmoja ukaamini na Imani yake ikawafaa, isipokuwa kaumu Yunus? Waliamini na Sisi Tukawaondolea adhabu na hizaya katika maisha ya dunia na Tukawastarehesha kwa muda”. (10:98)

Maana yake: Hakuna mji mzima ulioamini isipokuwa kaumu ya Yunus عليه السلام, kwani wao waliamini baada ya kupatwa na adhabu. Sawa na Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine;

وَأَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ مِائَةِ أَلْفٍ أَوْ يَزِيدُونَ ﴿١٤٧﴾ فَآمَنُوا فَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿١٤٨﴾

“Na Tulimtuma kwa watu laki moja au zaidi. Basi wakaamini, na Tukawastarehesha kwa muda”. (37:147-148) Na;

وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِّنْ نَّذِيرٍ

“Na hatukumtuma Mwonyaji yeyote kwenye mji”. (34:34)

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ ءَامَنُوا وَأَتَّقَوْا

“Na lau kuwa watu wa miji wangeliamini na wakamchamungu”.

Maana: Nyoyo zao zikayaamini waliyokuja nayo Mitume kwao kwa kuwasadiki na kuwafuata, wakawa wachamungu kwa kuwa Watiifu na wakaacha mambo yaliyokatazwa.

لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

“...kwa yakini Tungeliwafungulia baraka kutoka mbinguni na katika ardhi”.

Maana: Mvua kutoka angani na mimea ya ardhini. Allah تعالى Alisema;

وَلَيْكِن كَذَّبُوا فَأَخَذْنَاهُم بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ

“Lakini walikanusha basi Tukawapatiliza kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma”.

Maana yake: Lakini waliwakadhibisha Mitume wao nasi Tukawaadhibu kwa sababu ya madhambi waliyoyachuma na kwa kufanya mambo ya haramu. Kisha Allah تعالى Akasema; kwa Kukhofisha na Kuonya dhidi ya kuzikhalifu Amri Zake na kuthubutu juu ya Makatazo Yake.

أَفَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ

“Je, watu wa mijini wameaminisha”.

Ambao walikuwa makafiri.

أَنْ يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا

“...ya kuwa Adhabu Yetu haitawafikia usiku”.

Maana yake: Adhabu na mateso ya mfano kwa wengine.

بَيِّنَاتٍ

“...Bayatan...” Wakati wa usiku.

وَهُمْ نَائِبُونَ ﴿٧٦﴾ وَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَنْ يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا ضُحًى وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿٧٧﴾

“...nao wamelala? Au watu wa mijini wameaminisha ya kuwa Adhabu Yetu haitawafikia mchana, nao wanacheza?”

Maana: Wakati wakiwa wanashughulika au wakiwa katika kughafilika kwao.

أَفَأَمِنُوا مَكْرَ اللَّهِ

“Je, wamejiaminisha na Mipango ya Mwenyezi Mungu?”

Maana yake: Adhabu, Nakama na Kudura Zake kwa Kuwaangamiza wakiwa katika kusahau na kutokuwa na khabari.

فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْخَاسِرُونَ

“Kwani hawajiaminishi na Mipango ya Mwenyezi Mungu ila watu wenye kukhasiri”.

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema; "Muumini hufanya mambo ya utii, huku akiwa na shauku na hofu, ilhali muovu hufanya maasi huku akijidhani yuko salama."

أَوَلَمْ يَهْدِ لِلَّذِينَ يَرِثُونَ الْأَرْضَ مِنْ بَعْدِ أَهْلِهَا أَنْ لَوْ نَشَاءُ أَصَبْنَاهُمْ بِذُنُوبِهِمْ
وَنَطْبَعُ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ ﴿١٠٠﴾

100. Je hawahidiki hawa wanaorithi ardhi baada ya wale wenyewe kwamba Tukitaka Tutawapatiliza kwa madhambi yao, na Tutapiga muhuri juu ya nyoyo zao, na kwa hivyo hawatasikia?

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

أَوَلَمْ يَهْدِ لِلَّذِينَ يَرِثُونَ الْأَرْضَ مِنْ بَعْدِ أَهْلِهَا

"Je hawahidiki hawa wanaorithi ardhi baada ya wale wenyewe".

Kuwa (Allah تعالى Alisema), "Je hatukuwabainishia kwamba lau Tungelitaka Tungeliwaadhibu kutokana na madhambi yao". Mujahid na wengine kadha walisema vivyo hivyo¹. Abu Ja'far bin Jariri رحمه الله تعالى alisema katika tafsiri yake, "Allah تعالى Anasema: Je, hatukuwabainishia wengine kabla yao ambao ndio waliokaa duniani, wakaenda mwenendo wao, wakafanya amali zao na wakaasi Amri ya Mola wao".

أَنْ لَوْ نَشَاءُ أَصَبْنَاهُمْ بِذُنُوبِهِمْ

"...kwamba Tukitaka Tutawapatiliza kwa madhambi yao".

Kwamba Tungelitaka Tungeliwafanyia kama Tulivyowafanyia waliokuwa kabla yao.

وَنَطْبَعُ عَلَى قُلُوبِهِمْ

"...na Tutapiga muhuri juu ya nyoyo zao".

Anasema, na kutia muhuri nyoyo zao.

فَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ

"...na kwa hivyo hawatasikia?"

¹ At-Tabari 12:580.

Mawaidha wala kukumbushwa¹. Kwa ajili hiyo Allah تعالى Alisema;

أَفَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنَ الْقُرُونِ يَمْشُونَ فِي مَسْجِدِهِمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّأُولِي
الْبَصَائِرِ

“Je! Haikuwabainikia tu; vizazi vingapi Tulviangamiza kabla yao, nao wanatembea katika maskani zao? Hakika katika hayo zimo ishara kwa wenye akili”. (20:128) Na;

أَوَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنَ الْقُرُونِ يَمْشُونَ فِي مَسْجِدِهِمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ
لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَبْصَارِ

“Je! Haijawabainikia kwamba kaumu ngapi Tulziangamiza kabla yao, nao wanapita katika maskani zao hizo? Hakika katika hayo zipo Ishara. Basi, je, Hawasikii?” (32:26) na;

أَوَلَمْ تَكُونُوا أَقْسَمْتُمْ مِنْ قَبْلِ مَا لَكُمْ مِنْ زَوَالٍ ۗ وَسَكَنتُمْ فِي مَسْجِدِ الَّذِينَ
ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ

“Kwani nyinyi si mliapa zamani kwamba hamtaondokewa? Na mkakaa katika maskani zile zile za waliozidhulumu nafsi zao”. (14:44-45) na;

وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْنٍ هَلْ نُحِيسُ مِنْهُمْ مِنْ أَحَدٍ أَوْ تَسْمَعُ لَهُمْ رِكْوًا

“Na kaumu ngapi Tumezihiliki kabla yao. Je! Unawaona hata mmoja katika wao au unasikia hata mchakato wao?” (19:98)

Maana yake: Unamuona mmoja wao au unasikia sauti toka kwao? Na Aya nyingine zinazojulisha Nakama za Allah تعالى juu ya maadui Zake na Neema kuwafikia marafiki Zake, Waumini. Kwa ajili hii, inafuata Kauli ya Allah تعالى, na Yeye Ndiye Mkweli kabisa, Mola wa viumbe wote.

¹ At-Tabari 12:579.

تِلْكَ الْقُرَى نَقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبَاءِهَا ۗ وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا كَانُوا
لِيُؤْمِنُوا بِمَا كَذَّبُوا مِنْ قَبْلُ ۗ كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِ الْكَافِرِينَ ﴿١٠١﴾ وَمَا
وَجَدْنَا لِأَكْثَرِهِمْ مِنْ عَهْدٍ ۗ وَإِنْ وَجَدْنَا أَكْثَرَهُمْ لَفَاسِقِينَ ﴿١٠٢﴾

101. Miji hiyo Tunakusimulia baadhi ya khabari zake. Na hapana shaka Mitume wao waliwafikia kwa hoja zilizo waziwazi. Lakini hawakuwa wenye kuamini waliyoyakanusha zamani. Namna hivi Mwenyezi Mungu Anazipiga muhuri nyoyo za makafiri.

102. Wala hatukuwaona wengi wao kuwa wanatimiza ahadi; bali kwa hakika Tuliwakuta wengi wao ni wapotofu.

Baada ya kumueleza Nabii Wake juu ya khabari za Nuh عليه السلام, Hud عليه السلام, Saleh عليه السلام, Lut عليه السلام na Shu'aib عليه السلام, na juu ya Kuwaangamiza makafiri na Kuwaokoa waumini, na kwamba Aliwabainishia haki na Kuwapa hoja kupitia lugha za Mitume, Allah تعالى Alisema;

تِلْكَ الْقُرَى نَقُصُّ عَلَيْكَ

"Miji hiyo Tunakusimulia". Ewe Muhammad ﷺ.

مِنْ أَنْبَاءِهَا

"...baadhi ya khabari zake". Maana: Taarifa.

وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ

"Na hapana shaka Mitume wao waliwafikia kwa hoja zilizo waziwazi".

Maana: Hoja za kuwasadikishia yale waliyoyaeleza. Sawa na katika Aya nyingine;

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ تَبْعَثَ رَسُولًا

"Wala Sisi Hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume". (17:15) Na;

ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْقُرَى نَقُصُّهُ عَلَيْكَ ۗ مِنْهَا قَائِمٌ وَحَصِيدٌ ﴿١٠٣﴾ وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِن
ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ ۗ

“Hizi ni katika khabari za miji, Tunakusimulia. Mngine ipo bado na mngine imefyekwa. Na Sisi Hatukuwadhulumu lakini wao wenyewe wamejidhulumu”. (11:100-101)

Kauli ya Allah تعالى;

فَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا بِمَا كَذَّبُوا مِنْ قَبْلُ

“Lakini hawakuwa wenye kuamini waliyoyakanusha zamani”.

Maana yake: Hawakuwa wenye kuyaamini waliyoletewa na Mitume kwa sababu ya kuukadhibisha kwao ukweli, baada ya kuwajia mwanzoni (ingawa waliyaelewa) na baada ya kuupokea. Maelezo haya yalitolewa na Ibn ‘Atwiyah, na yana nguvu, pia yanapewa nguvu na Kauli ya Allah تعالى;

وَمَا يُشْعِرُكُمْ أَنَّهَا إِذَا جَاءَتْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠٨﴾ وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَارَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا
بِهِ أَوَّلَ مَرَّةٍ

“Na nyinyi hamjui kuwa zitapokuja hawatoamini. Nasi twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza...”. (6:109-110)

Kwa ajili hii, Alisema hapa;

كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِ الْكَافِرِينَ ﴿١٠٩﴾ وَمَا وَجَدْنَا لِأَكْثَرِهِمْ

“Namna hivi Mwenyezi Mungu Anazipiga muhuri nyoyo za makafiri. Wala hatukuwaona wengi wao...”.

Maana yake: Hatukuona Umma mwingi uliopita;

مِنْ عَهْدٍ ۗ وَإِنْ وَجَدْنَا أَكْثَرَهُمْ لَفَسِيقِينَ

“...kuwa wanatimiza ahadi; bali kwa hakika Tuliwakuta wengi wao ni wapotofu”.

Maana yake: Kwa hakika Tumewakuta wengi wao ni wapotevu, wako nje ya utii na uelekevu. Ahadi Aliyoichukua ni ile Aliyowaumba nayo na Kuwawekea katika *Fitrah* na Allah تعالى Aliwaingizia wakiwa wangali katika migongo ya

baba zao na kuchukua ahadi kuwa Yeye ni Mola na Mfalme wao, na kwamba hapana wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye. Wakakiri hilo na kulishuhudisha katika nafsi zao. Lakini wakalikhaliifu na kuiacha nyuma ya migongo yao, na wakamuabudu Allah تعالى kwa kumshirikisha na ghairi yake pasi na dalili wala ushahidi, si wa kiakili wala wa kisharia. Hata hivyo, katika *Fitrah* iliyosalimika, ni kinyume cha hivyo. Na Mitume watukufu tangu mwanzo wao mpaka wa mwisho wao walikuja kulikataza hilo.

Sawa na ilivyo katika *Sahih* Muslim, kuwa Allah تعالى Anasema;

«يَقُولُ اللهُ تَعَالَى إِنِّي خَلَقْتُ عِبَادِي حُنَفَاءَ فَجَاءَتْهُمْ الشَّيَاطِينُ فَأَجْتَانَتْهُمْ عَنْ دِينِهِمْ
وَحَرَمْتُ عَلَيْهِمْ مَا أَخَلَلْتُ لَهُمْ»

“Mimi Nimewaumba waja Wangu Hunafa (wenye kumuabudu Allah tu) akawajia shetani akawakwepesha na dini yao na akawaharamishia Niliyowahalalishia”.¹

Na katika *Sahih* Mbili,

«كُلُّ مَوْلُودٍ يُوَلَدُ عَلَى الْفِطْرَةِ فَأَبَوَاهُ يُهَوِّدَانِهِ وَيُنَصِّرَانِهِ وَيُمَجْسِبَانِهِ»

“Kila mtoto huzaliwa katika Fitrah, wazazi wake ndio wanaombadili na kumfanya Myahudi, Mkristo au Majusi”.²

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ مُوسَى بِآيَاتِنَا إِلَى فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ فَظَلَمُوا بِهَا فَأَنْظَرْنَا كَيْفَ كَانَ
عَنْقَبَةُ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٠٣﴾

103. Kisha baada yao Tukamtuma Musa na Ishara Zetu kwa Firauni na waheshimiwa wake. Nao wakazikataa. Basi tazama ulikuwaje mwisho wa waharibifu.

¹ Muslim 4:2197.

² Fat'hul Al-Bari 3:290 na Muslim 4:2048.

Kisa cha Nabii Musa عليه السلام.

Allah تعالى Anasema;

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ

“Kisha baada yao Tukamtuma”.

Maana yake: Mitume Tuliokwishatangulia kuwataja, kama vile Nuh عليه السلام, Hud عليه السلام, Saleh عليه السلام, Lut عليه السلام na Shu'aib عليه السلام na Manabii wengine wa Allah تعالى;

مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا

“Musa na Ishara Zetu”.

Maana yake: Kwa hoja na dalili Zetu dhahiri kwa Firauni, ambaye alikuwa Mfalme wa Misr katika zama za Nabii Musa عليه السلام.

وَمَلَائِكَةٍ

“...na waheshimiwa wake”. Maana yake: Kaumu yake.

فَظَلَمُوا بِهَا

“Nao wakazikataa”.

Maana: Walizipinga na kuzikataa kwa dhuluma na ukaidi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٤﴾

“Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi”.
(27:14)

Maana yake: Waliozuia dhidi ya njia ya Allah تعالى, na wakawakadhibisha Mitume Wake, angalieni jinsi Tulivyo wafanya. Tuliwagarikisha wote, ilhali Musa عليه السلام na kaumu yake wakiwa wanaangalia. Na hii ni adhabu kali zaidi iliyowapata Firauni na watu wake, na ni yenye kuzifariji nyoyo za marafiki wa Allah تعالى, Musa عليه السلام na watu wake waliomuamini.

* * *

وَقَالَ مُوسَىٰ يَنْفِرْعَوْنَ إِنِّي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠٤﴾
 حَقِيقٌ عَلَىٰ أَن لَّا أَقُولَ عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ قَدْ جِئْتُكُمْ
 بَيْنَتِي مِّن رَّبِّكُمْ فَأَرْسِلْ مَعِيَ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٠٥﴾ قَالَ إِن
 كُنْتَ جِئْتَ بِآيَةٍ فَأْتِ بِهَا إِن كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٠٦﴾
 فَأَلْقَىٰ عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ ثُعْبَانٌ مُّبِينٌ ﴿١٠٧﴾ وَنَزَعَ يَدَهُ
 فَإِذَا هِيَ بَيْضَاءُ لِلنَّظِيرِينَ ﴿١٠٨﴾ قَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِ
 فِرْعَوْنَ إِنَّ هَذَا لَسَاحِرٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٩﴾ يُرِيدُ أَن يُخْرِجَكُمْ
 مِّنْ أَرْضِكُمْ ۖ فَمَاذَا تَأْمُرُونَ ﴿١١٠﴾ قَالُوا أَرْجِهْ وَأَخَاهُ
 وَأَرْسِلْ فِي الْمَدَائِنِ حَاشِرِينَ ﴿١١١﴾ يَا تُولَك بِكُلِّ سَجِرٍ
 عَلِيمٍ ﴿١١٢﴾ وَجَاءَ السَّحَرَةُ فِرْعَوْنَ قَالُوا إِنَّ لَنَا لَأَجْرًا
 إِن كُنَّا نَحْنُ الْغَالِبِينَ ﴿١١٣﴾ قَالَ نَعَمْ وَإِنَّكُمْ لَمِنَ
 الْمُفْرِقِينَ ﴿١١٤﴾ قَالُوا يَمُوسَىٰ إِمَّا أَن تُلْقَىٰ وَإِمَّا أَن نُّكُونَ
 نَحْنُ الْمُلْقِينَ ﴿١١٥﴾ قَالَ أَلْقُوا ۖ فَلَمَّا أَلْقَوْا سَحَرُوا أَعْيُنَ
 النَّاسِ وَاسْتَهْبَهُمْ وَجَاءُوا بِسِحْرِ عَظِيمٍ ﴿١١٦﴾ *
 وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَن أَلْقِ عَصَاكَ ۖ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا
 يَأْفِكُونَ ﴿١١٧﴾ فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٨﴾
 فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَبِيرِينَ ﴿١١٩﴾ وَأَلْقَى السَّحَرَةُ
 سِدْرَتَيْنِ ﴿١٢٠﴾ قَالُوا ءَأَمْنَا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٢١﴾ رَبِّ
 مُوسَىٰ وَهَارُونَ ﴿١٢٢﴾

وَقَالَ مُوسَىٰ يَنْفِرْعَوْنَ إِنِّي رَسُولٌ
 مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠٤﴾ حَقِيقٌ عَلَىٰ
 أَن لَّا أَقُولَ عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ قَدْ
 جِئْتُكُمْ بَيْنَتِي مِّن رَّبِّكُمْ فَأَرْسِلْ
 مَعِيَ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٠٥﴾ قَالَ إِن
 كُنْتَ جِئْتَ بِآيَةٍ فَأْتِ بِهَا إِن كُنْتَ
 مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٠٦﴾

104. Na Musa alisema: Ewe Firauni! Hakika mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.

105. Inafaa nisiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila lilio la Haki. Nami hakika nimekujieni na dalili waziwazi kutokana na Mola Mlezi wenu. Basi waache Wana wa Israil wende nami.

106. Akasema Firauni: Ikiwa Umekuja na Ishara basi ilete ukiwa ni katika wasemao kweli.

Allah تعالیٰ Anaeleza majadiliano kati ya Musa عليه السلام na Firauni, na Musa عليه السلام

kumkataa Firauni kwa hoja na kufanya miujiza, mbele ya Firauni na kaumu yake, Wa-Qibti wa Misri. Alisema;

وَقَالَ مُوسَىٰ 'يَنْفِرْ عَوْنُ إِنِّي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠٤﴾

“Na Musa alisema: Ewe Firauni! Hakika mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.”

Maana yake: Aliyenituma Ndiye Muumbaji wa kila kitu, Mola na Mfalme wao.

حَقِيقٌ عَلَىٰ أَن لَّا أَقُولَ عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ

“Infaa nisiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila lilio la Haki.”

Kwa maana: Ni wajibu na haki yangu juu ya hilo, kwamba nisieleze isipokuwa la haki na kweli, kwa sababu ya vile ni juavyo Utukufu na Ukuu Wake.

قَدْ جِئْتُكُمْ بِبَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ

“Nami hakika nimekujieni na dalili waziwazi kutoka kwa Mola Mlezi wenu.”

Maana yake: Kwa hoja zenye kukata alizonipa Allah تعالى kama dalili za kunisadikishia niliyokujieni nayo.

فَأَرْسِلْ مَعِيَ بَنِي إِسْرَائِيلَ

“Basi waache Wana wa Israil wende nami.”

Kwa maana: Waachilie kutoka utumwani mwako na ushurutishaji. Waache wamuabudu Mola wako na Mola wao. Nao ni katika dhuriya wa Nabii Israil عليه السلام. Naye ni Yaqub bin Is-haq bin Ibrahim عليه السلام Khalil (rafiki wa karibu sana) wa Allah تعالى.

قَالَ إِن كُنتَ جِئْتَ بِآيَةٍ فَآتِ بِهَا إِن كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٠٥﴾

“Akasema Firauni: Ikiwa Umekuja na Ishara basi ilete ukiwa ni katika wasemao kweli.”

Maana: Firauni alisema, “Sitasadiki uliyoyasema, wala sitakutii uliyoyataka. Kama una hoja ilete ili tuione, kama wewe ni mkweli katika uliyodai”.

فَأَلْفَىٰ عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ ثُعْبَانٌ مُّبِينٌ ﴿١٠٦﴾ وَنَزَعَ يَدَهُ فَإِذَا هِيَ بَيْضَاءُ لِلنَّظَرِينَ ﴿١٠٧﴾

107. Basi akaitupa fimbo yake, na mara ikawa nyoka dhahiri.

108. Na akatoa mkono wake, mara ukawa mweupe kwa watazamao.

Fimbo ya Musa عليه السلام na Kiganja Chake Cheupe.

'Ali bin Abu Twalha alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

نُعَبَّانُ مُبِينٌ

"...nyoka dhahiri".

Ina maana, "Joka dume"¹. Kadhalika As-Suddi na Adh-Dhahhak walisema hivyo². Na katika inayovutia sana, katika masimulizi ya Yazid bin Harun kutoka kwa Asbagh bin Yazid, kutoka kwa Qasim bin Abu Ayyub kutoka kwa Sa'id bin Jubayr ni kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

فَأَلْقَىٰ عَصَاهُ

"Basi akaitupa fimbo yake".

Ikageuka joka kubwa ambalo lilifunua kinywa chake na kumuendea Firauni kwa haraka. Firauni alipoliona kwamba lilikuwa likimdhamiria yeye, aliruka kutoka katika kiti chake cha enzi na akamuomba Musa عليه السلام amsaidie kwa kumuepusha nalo, na Musa عليه السلام akafanya hivyo³. As-Suddi aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

فَإِذَا هِيَ نُعَبَّانُ مُبِينٌ

"...na mara ikawa nyoka dhahiri".

Kuwa, "Ni joka dume, huku likifunua kinywa chake, na kuweka taya lake la chini katika ardhi na la juu likifika juu ya ukuta wa kasri. Kisha likaelekea alipokaa Firauni. Alipoliona, aliliogopa sana, akachupa na alivuja na jasho, ilhali kabla ya hapo alikuwa hatokwi na jasho. Akasema, "Ewe Musa! Lichukue, mimi pia nakuamini na nitawaachilia kwako wana wa Israili". Musa عليه السلام akalichukua na likarudia kuwa fimbo tena⁴.

¹ At-Tabari 13:16.

² At-Tabari 13:15-17.

³ At-Tabari 13:16.

⁴ At-Tabari 13:15.

Kauli ya Allah تعالى: وَنَزَعَ يَدَهُ فَإِذَا هِيَ بَيْضَاءُ لِلنَّظِيرِينَ ﴿١٠٤﴾

“Na akatoa mkono wake, mara ukawa mweupe kwa watazamao”.

Kwa maana: Alikitoa kiganja chake toka katika joho lake baada ya kukiingiza, mara ukawa mweupe na kung'ara, pasi na ukoma wala maradhi. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَأَدْخَلَ يَدَكَ فِي جَيْبِكَ تَخْرُجُ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ ۗ

“Na ingiza mkono wako katika mfuko wako, utatoka mweupe bila ya maradhi”. (27:12)

Na alisema Ibn 'Abbas رضي الله عنهما katika Hadithi ya kuvutia, “...bila ya maradhi” (27:12) “Bila ya Ukoma, kisha akakirudisha katika nguo yake, na kikarudia katika rangi yake ya awali”¹. Pia Mujahid na wengine walisema hivyo².

قَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِ فِرْعَوْنَ إِنَّ هَذَا لَسَاحِرٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٥﴾ يُرِيدُ أَنْ يُخْرِجَكُمْ مِنْ أَرْضِكُمْ ۖ فَمَاذَا تَأْمُرُونَ ﴿١٠٦﴾

109. Wakasema waheshimiwa wa kaumu ya Firauni: Hakika huyu ni Mchawi mjuzi.

110. Anataka kukutoeni katika nchi yenu. Basi mnatoa shauri gani?

Kauli ya Watu wa Firauni ni Kuwa Musa عليه السلام ni Mchawi, na Kuafikiana Kumpambanisha na Wachawi Wenzake.

Maana: Wakuu na umma wa watu wa Firauni uliafikiana na kauli ya Firauni juu ya Musa عليه السلام, baada ya kuondoka hofu yake na akatulizana katika mamlaka yake baada ya hayo yaliyojiri. Aliwaambia watu wake waliomzingira,

إِنَّ هَذَا لَسَاحِرٌ عَلِيمٌ

“Hakika huyu ni Mchawi mjuzi”.

Wakaafikiana na wakasema kama alivyosema, na wakashauriana juu ya namna watakavyomfanyia Musa عليه السلام na jinsi hila zao za kuizima nuru yake

¹ At-Tabari 13:17.

² At-Tabari 13:18.

zitakavyokuwa na kuonesha kwamba neno lake ni la uongo na uzushi. Walichelea kuwa angewahadaa watu kwa uchawi wake, ndivyo walivyodai na hiyo ingelikuwa ndiyo sababu ya kushinda kwake na kuwaondosha wao kutoka katika ardhi yao. Kile walichokihofia, kilitokea.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَبُرِيَ فِرْعَوْنَ وَهَمَانَ وَجُنُودَهُمَا مِنْهُمْ مَا كَانُوا يَحْتَدِرُونَ

“...na wao kuwaonesha kina Firauni na Hamana na majeshi yao mambo yale waliyokuwa wakiyaogopa”. (28:6)

Baada ya kushauriana juu ya jambo lake, waliafikiana juu ya hila, kama Allah تعالى Alivyoeleza juu yao katika Kauli Yake;

قَالُوا أَرْجِهْ وَأَخَاهُ وَأَرْسِلْ فِي الْمَدَائِنِ حَاشِرِينَ ﴿١١١﴾ يَا تَوَكَّلْ بِكُلِّ سَجِرٍ عَلِيمٍ ﴿١١٢﴾

111. Wakasema: Muache kidogo yeye na nduguye, na watume mjini wakusanyao.

112. Wakuletee kila mchawi mjuzi.

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alieleza kuwa;

أَرْجِهْ

“Muache kidogo”. Maana yake: Msubirisha.¹

وَأَرْسِلْ فِي الْمَدَائِنِ

“...na watume mjini”. Maana yake: Wapeleke, maana yake majimboni na miji iliyo katika himaya yako.

حَاشِرِينَ

“...wakusanyao”. Kwa maana: Watakaokukusanyia uchawi kutoka miji mbalimbali na kuwajumuisha. Katika zama zao, uchawi ulikuwa maarufu na umeenea. Wako miongoni mwao waliitakidi kwamba alichokileta Musa عليه السلام kilikuwa uchawi ambao wachawi wao walikuwa wakiufanya. Kwa hivyo, wakamkusanyia wachawi ili wauoneshe na kuishinda miujiza waliyoiona. Kama Allah تعالى Alivyomuelezea Firauni, Aliposema;

¹ At-Tabari 13:22

فَلَنَأْتِيَنَّكَ بِسِحْرِ مِثْلِهِ فَأَجْعَلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَكَ مَوْعِدًا لَا نُخْلِفُهُ نَحْنُ وَلَا أَنْتَ مَكَانًا
 سُوءٍ ﴿٥٨﴾ قَالَ مَوْعِدُكُمْ يَوْمَ الزَّيْنَةِ وَأَنْ تُحْشَرَ النَّاسُ ضُحًى ﴿٥٩﴾ فَتَوَلَّى فِرْعَوْنُ
 فَجَمَعَ كَيْدَهُ ثُمَّ أَتَى ﴿٦٠﴾

“Basi sisi hakika tutakuletea uchawi kama huo. Basi weka miadi baina yetu na wewe, ambayo tusiivunje sisi wala wewe, mahali patapokuwa sawa. Akasema: Miadi yetu ni siku ya Sikukuu; na watu wakusanywe kabla ya aduhuri. Basi Firauni akarudi na akitengeneza hila yake, kisha akaja”. (20:58-60)

Allah تعالی Akasema hapa;

وَجَاءَ السَّحَرَةُ فِرْعَوْنَ قَالُوا إِنَّ لَنَا لَأَجْرًا إِن كُنَّا نَحْنُ الْغَالِبِينَ ﴿٥٨﴾ قَالَ نَعَمْ
 وَإِنَّكُمْ لَمِنَ الْمُقَرَّبِينَ ﴿٥٩﴾

113. Wakaja wachawi kwa Firauni, wakasema: Hakika tutapata ujira ikiwa tutashinda.

114. Akasema: Naam! Nanyi bila ya shaka mtakuwa katika wa karibu nami.

Wachawi Wanabadili Kamba Zao na Kuwa Nyoka Mbele ya Musa عليه السلام.

Allah تعالی Anaeleza mazungumzo yaliyotokea baina ya Firauni na wachawi aliowakusanya ili wamshinde Musa عليه السلام, kwamba wangelimshinda Musa عليه السلام angeliwalipa na kuwapatia zawadi nyingi. Akawaahidi na kuwatumainisha kuwapa walichokitaka na kuwaingiza katika majilisi yake na watu wa karibu sana na yeye. Walipotumainishwa na Firauni, laana ya Allah تعالی imfikie,

قَالُوا يَمُوسَىٰ إِمَّا أَنْ تُلْقَىٰ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ نَحْنُ الْمَلْقِينَ ﴿٦١﴾ قَالَ أَلْقُوا ۗ فَلَمَّا أَلْقَوْا
 سَحَرُوا أَعْيُنَ النَّاسِ وَأَسْرَهُبُوهُمْ وَجَاءُوا بِسِحْرِ عَظِيمٍ ﴿٦٢﴾

115. Wakasema: Ewe Musa! Je, utatupa wewe, au tutakuwa sisi tutaotupa?

116. Akasema: Tupeni! Basi walipotupa waliyazuga macho ya watu na kuwatia khofu, na wakaleta uchawi mkubwa.

Hii ni changamoto ambayo wachawi wanampa Musa عليه السلام, waliposema;

إِمَّا أَنْ تُلْقَىٰ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ خُنَّ الْمُلْقِينَ

“Je, utatupa wewe, au tutakuwa sisi tutaotupa?”

Maana yake: Kabla yako. Sawa na Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine;

وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَلْقَىٰ

“...au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa?” (20:65)

Musa عليه السلام akasema, “Tupeni nyinyi kwanza”. Ilisemwa kwamba hekima ya kufanya hivyo, Allah Aalam, ni ili watu waone uchawi wa wachawi kwanza, wakishamaliza kustaajabu na kuvutia macho yao, basi haki iliyo dhahiri na safi ndio iwajie, baada ya wote kuitana na kuingojea, na kuufanya ukweli uingie vyema katika nafsi, na ndivyo ilivyokuwa. Kwa hivyo, Allah تعالى Alisema;

فَلَمَّا أَلْقَوْا سَحَرُوا أَعْيُنَ النَّاسِ وَاسْتَرَهُبُوهُمْ

“Basi walipotupa waliyazuga macho ya watu na kuwatia khofu,..”.

Kwa maana: Waliyahadaa macho kwa kudhani kwamba waliyoyafanya yalikuwa kweli, kwa nje, kumbe kilikuwa kiini macho tu. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَأَوْجَسَ فِي نَفْسِهِ خِيفَةً مُوسَىٰ ﴿٦٧﴾ قُلْنَا لَا تَخَفْ إِنَّكَ أَنْتَ الْأَعْلَىٰ ﴿٦٨﴾ وَأَلْقَىٰ مَا فِي يَمِينِكَ تَلْقَفَ مَا صَنَعُوا ﴿٦٩﴾ إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدٌ سَجِرٌ ﴿٧٠﴾ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَىٰ ﴿٧١﴾

“Basi Musa akaingia khofu nafsi yake. Tukasema: Usikhofu! Hakika wewe ndiye utakayeshinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyoviunda. Hakika walivyoviunda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo”. (20:67-69)

Sufyan bin 'Uyaynah alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, wachawi walitupa, “fimbo zilizokuwa nene na fimbo ndefu, kwa kiini macho zikaonekana zinatembea”¹.

¹ At-Tabari 13:28.

* وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ ۗ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ ﴿١٠٧﴾ فَوَقَعَ
 الْحَقُّ وَنَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٠٨﴾ فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَغِيرِينَ ﴿١٠٩﴾ وَأَلْقَى
 السَّحَرَةُ سِحْرَاجِدِينَ ﴿١١٠﴾ قَالُوا ءَأَمْنَا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١١١﴾ رَبِّ مُوسَىٰ وَهَارُونَ ﴿١١٢﴾

117. Nasi Tukamfunulia Musa kumuambia: Tupa fimbo yako. Mara ikavimeza vyote vile walivyovibuni.

118. Kweli ikathibiti na yakabatilika waliyokuwa wakiyatenda.

119. Kwa hivyo walishindwa hapo, na wakageuka kuwa wadogo.

120. Na wachawi wakaporomoka wakisujudu.

121. Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa viumbe vyote.

122. Mola Mlezi wa Musa na Haarun”.

Musa عليه السلام Anawashinda Wachawi, Kisha Wanamuamini.

Allah تعالى Anaeleza kuwa Alimteremshia wahyi mja na Mjumbe Wake, Musa عليه السلام katika wakati huo adhimu ambapo Allah تعالى Alipambanua baina ya haki na batili. Akimuamuru atupe kilichokuwa katika mkono wa kuumeni kwake, nayo ilikuwa ni fimbo.

فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ

“Mara ikavimeza”. Maana yake: Inavila.

مَا يَأْفِكُونَ

“...vyote vile walivyovibuni”.

Maana yake: Walivyofanyia mazingaombwe na kuvifanya vionekane kweli kumbe siyo. ‘Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, fimbo ya Musa عليه السلام ikawa haizipiti kamba na fimbo zao, bali ilizimeza. Wachawi Wakatambua, hili ni jambo la kutoka mbinguni, si uchawi. Wakaanguka kusujudu na wakasema;

ءَأَمْنَا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١١١﴾ رَبِّ مُوسَىٰ وَهَارُونَ ﴿١١٢﴾

“Tumemuamini Mola Mlezi wa viumbe vyote. Mola Mlezi wa Musa na Haarun”.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema, "Iianza kumeza kamba na fimbo zao moja baada ya moja, mpaka hakuna kilichotupwa na wachawi ambacho kilisalia. Kisha Musa عليه السلام aliichukua, ikageuka fimbo Mkononi mwake kama ilivyokuwa hapo kabla. Wachawi waporomoka kusujudu, na wakasema, "Tunamuamini Mola wa walimwengu wote, Mola wa Musa عليه السلام na Harun عليه السلام. Lau kama huyu angelikuwa mchawi asingelitushinda"¹.

Qasim bin Abu Bazzah alisema, "Allah تعالى Alimshushia Wahyi Musa عليه السلام kwamba, "Tupa fimbo yako". Akaitupa, tahamaki ikageuka joka kubwa la dhahiri, likifunua kinywa chake na kumeza kamba na fimbo zao. Hapo hapo wachawi wakaanguka kusujudu, na hawakuinua vichwa vyao mpaka wakaona Jannah, Moto na malipo ya wakazi wa sehemu hizo mbili"².



¹ At-Tabari 13:30.

² At-Tabari 13:30.

قَالَ فِرْعَوْنُ ءَامَنْتُمْ بِمِءِ قَبْلِ أَنْ ءَاذَنْ لَكُمْ^ط إِنَّ هَذَا لَمَكْرٌ
 مَكْرَتُمْوهُ فِي الْمَدِينَةِ لِخُرُجِوْا مِنْهَا أَهْلَهَا^ط فَسَوْفَ تَعْمَلُونَ
 ۞ لَأَقْطَعَنَّ أَيْدِيَكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ مِّنْ خِلْفِ نَمِّ
 لَأُصَلِّبَنَّكُمْ أَجْمَعِينَ ۞ قَالُوا إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا مُنْقَلِبُونَ
 ۞ وَمَا نَنقِمُ مِنَّا إِلَّا أَنْ ءَامَنَّا بِآيَاتِ رَبِّنَا لَمَّا
 جَاءَتْنَا^ط رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَتَوَقَّفْنَا مُسْلِمِينَ ۞ وَقَالَ
 الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِ فِرْعَوْنَ أَتَدْرُسُ مَوْسَىٰ وَقَوْمَهُ لِيُفْسِدُوا فِي
 الْأَرْضِ وَيَذَرَكَ وَءِآلِهَتَكَ^ط قَالَ سَنَقْبَلُ أَبْتَاءَهُمْ
 وَنَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ وَإِنَّا فَوْقَهُمْ قَاهِرُونَ ۞ قَالَ
 مَوْسَىٰ لِقَوْمِهِ اسْتَعِينُوا بِاللَّهِ وَاصْبِرُوا^ط إِنَّ الْأَرْضَ لِلَّهِ
 يُورِثُهَا مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ^ط وَءَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ۞
 قَالُوا أَوْذَيْنَا مِنْ قَبْلِ أَنْ تَأْتِيَنَا وَمِنْ بَعْدِ مَا جِئْتَنَا^ط قَالَ
 عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَنْ يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي
 الْأَرْضِ فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ۞

قَالَ فِرْعَوْنُ ءَامَنْتُمْ بِمِءِ قَبْلِ أَنْ ءَاذَنْ
 لَكُمْ^ط إِنَّ هَذَا لَمَكْرٌ مَكْرَتُمْوهُ فِي
 الْمَدِينَةِ لِخُرُجِوْا مِنْهَا أَهْلَهَا^ط
 فَسَوْفَ تَعْمَلُونَ ۞ لَأَقْطَعَنَّ
 أَيْدِيَكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ مِّنْ خِلْفِ نَمِّ
 لَأُصَلِّبَنَّكُمْ أَجْمَعِينَ ۞ قَالُوا
 إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا مُنْقَلِبُونَ ۞ وَمَا
 نَنقِمُ مِنَّا إِلَّا أَنْ ءَامَنَّا بِآيَاتِ
 رَبِّنَا لَمَّا جَاءَتْنَا^ط رَبَّنَا أَفْرِغْ
 عَلَيْنَا صَبْرًا وَتَوَقَّفْنَا مُسْلِمِينَ ۞

123. Akasema Firauni:
Mmemuamini kabla sija-
kupeni idhini? Hizi ni njama
mlizo panga mjini mpate
kuwatoa wenyewe. Lakini
karibu Mtajua!

124. Lazima nitaikata mikono yenu na miguu yenu mbali mbali. Kisha nitakutundikeni misalabani.

125. Wakasema: Sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi.

126. Nawe hukuudhika nasi ila kwa kuwa tumeziamini ishara za Mola Mlezi wetu zilipotujia. Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie uvumilivu na Utufishe hali ni Waislamu.

Firauni anawatisha Wachawi baada ya Kumuamini Musa عليه السلام.

Allah تعالى Anaeleza vitisho alivyovitoa Firauni, Laana ya Allah imfikie, kwa wachawi, baada ya wao kumuamini Musa عليه السلام na hadaa na hila zake Firauni alizozionesha kwa watu. Firauni alisema;

إِنَّ هَذَا لَمَكْرٌ مَّكْرَتُهُمْ فِي الْمَدِينَةِ لِيُخْرِجُوا مِنْهَا أَهْلَهَا ط

“Hizi ni njama mlizopanga mjini mpate kuwatoa wenyewe”.

Maana yake: Ushindi wake huu wa leo umetokana na kuwa mlishauriana na mkakubaliana hivyo.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine;

إِنَّهُ لَكَبِيرٌ كُمْ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ ط

“Hakika yeye ndiye mkubwa wenu aliyekufundisheni uchawi”.

(20:71)

Ilhali yeye mwenyewe Firauni na watu wenye akili, wakati huo walikuwa wakijua fika kuwa haya aliyoyasema ni uongo mkubwa. Kwani Musa عليه السلام mara tu baada ya kutoka Madyan alimlingania Firauni arejee kwa Allah تعالى na akaonesha miujiza mikubwa na hoja kadha zisizopingika za kuyasadikisha aliyokuja nayo. Baada ya hilo tu, Firauni aliwatuma wajumbe kwenda katika miji iliyokuwa ndani ya Himaya ya Utawala wake. Akawakusanya wachawi tofauti tofauti kutoka katika majimbo mbali mbali yaliyokuwa katika nchi ya Misri ambao waliteuliwa na yeye Firauni, pamoja na watu wake na akawakusanya na kuwaahidi kuwapa mali nyingi. Kwa hivyo wakawa na pupa ya jambo hilo la kupata ushindi na kupata nafasi ya kuwa watu wa karibu zaidi na Firauni. Wakati huo huo, Musa عليه السلام alikuwa hamjui yeyote katika wao, wala hajawahi kuwaona wala kukutana nao. Firauni alikuwa akiyajua hayo, bali aliyasema hayo kwa ajili ya kuwahadaa watu wanyonge na majahili wa umma wa dola yake.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine;

فَأَسْتَحَفَّ قَوْمَهُ فَأَطَاعُوهُ ط

“Basi aliwachezea watu wake, na wakamtii”. (43:54)

Hususan, watu waliomsadiki Firauni katika kauli yake;

أَنَا رَبُّكُمْ الْأَعْلَىٰ

“Mimi ndiye mola wenu mlezi mkuu kabisa”. (79:24)

Ni miongoni mwa majahili na wapotevu zaidi katika viumbe wa Allah تعالى. As-Suddi alisema katika tafsiri yake kwa isnadi yake mashuhuri kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه na masahaba wengine رضي الله عنهم, walizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

إِنَّ هَذَا لَمَكْرٌ مَّكْرْتُمُوهُ فِي الْمَدِينَةِ

“Hizi ni njama mlizopanga mjini”.

Alisema, “Musa عليه السلام alikutana na kiongozi wa wachawi, Musa عليه السلام alimuambia, “Ikiwa nitakushinda, utaniamini na kutoa shahada kwamba niliyokuja nayo ni ya kweli?” Akasema mchawi, “Kesho nitaleta uchawi ambao hakuna mchawi atakayeweza kushinda. Wallahi! Ukinishinda, nitakuamini, na nitatoa shahada kwamba ya kwako uliyokuja nayo ni ya kweli”. Wakati huo, Firauni alikuwa akiwatizama. Ndiyo maana aliyasema hayo aliyoyasema¹. Kauli ya Allah تعالى;

لِيُخْرِجُوا مِنهَا أَهْلَهَا

“...mpate kuwatoa wenyewe”. Maana: Ili nyinyi muungane naye, na dola na nguvu ziwe zenu, na muwatoe humo, wakuu na viongozi. Na hivyo, dola na madaraka yanakuwa yenu.

فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ

“Lakini karibu Mtajua!” Maana: Nitakachokufanyieni. Kisha akaiieleza ahadi yake hii kwa kauli yake;

لَأَقْطَعَنَّ أَيْدِيَكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ مِمِّنْ خَلْفِي

“Lazima nitaikata mikono yenu na miguu yenu mbali mbali”.

Sawa na alivyosema katika sehemu nyingine ya Qur'an.

فِي جُدُوعِ النَّخْلِ

“...katika vigogo vya mitende”. (20:71) Maana: Juu ya vigogo hivyo.

¹ At-Tabari 13:33.

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, Firauni akawa ndio wa kwanza kutekeleza zoezi la kusulubu, kukata mguu na mkono kwa upande tofauti ¹. Kauli ya Wachawi;

إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا مُنْقَلِبُونَ

“Sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi”.

Maana yake: “Sasa tumethibitisha kuwa tutarejea kwa Allah تعالى, na adhabu Yake ni kali kuliko ya kwako, na maangamizo yake ni makubwa kuliko ya yale uliyotuitia leo, na uchawi uliotushurutisha tuufanye leo ni jambo kubwa kuliko adhabu yako. Kwa hivyo, leo tutaivumilia adhabu yako, ili tunusurike na adhabu ya Allah تعالى”.

رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا

“Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie uvumilivu”.

Maana: Utuenezee subira na uimara katika Dini Yako.

وَتَوَفَّنَا مُسْلِمِينَ

“...na utufishe hali ni Waislamu”. Maana yake: Hali ya kuwa ni wafuasi wa Nabii Wako Musa عليه السلام. Na wakamuambia Firauni,

فَأَقْضِ مَا أَنْتَ قَاضٍ إِنَّمَا تَقْضِي هَذِهِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٧٦﴾ إِنَّا ءَامَنَّا بِرَبِّنَا لِيَغْفِرَ لَنَا
 خَطِيئَتَنَا وَمَا أَكْرَهْتَنَا عَلَيْهِ مِنَ السِّحْرِ وَاللَّهُ خَيْرٌ وَأَبْقَى ﴿٧٧﴾ إِنَّهُ مَنْ يَأْتِ رَبَّهُ مُجْرِمًا
 فَإِنَّ لَهُ جَهَنَّمَ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ ﴿٧٨﴾ وَمَنْ يَأْتِهِ مُؤْمِنًا قَدْ عَمِلَ الصَّالِحَاتِ
 فَأُولَٰئِكَ لَهُمُ الدَّرَجَاتُ الْعُلَىٰ ﴿٧٩﴾

“Basi hukumu utavyohukumu; kwani wewe umehukumu haya ya maisha ya dunia tu. Hakika sisi tumemuamini Mola wetu Mlezi ili Atusamehe makosa yetu na uchawi uliotulazimisha kuufanya. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora na Mwenye kudumu zaidi. Hakika atayemjia Mola wake naye ni mkhalifu, basi kwa yakini, yake huyo ni Jahannamu. Hafi humo wala haishi. Na atakayemjia naye ni Muumini aliyetenda mema, basi hao ndio wenye vyeo vya juu”.
 (20:72 -75)

¹ At-Tabari 13:34.

Basi asubuhi ya siku hiyo walikuwa wachawi, mwisho wake wakageuka kuwa mashahidi wema. Ibn 'Abbas, 'Ubayd bin 'Umayr, Qatadah na Ibn Jurayj رضي الله عنهم walisema, "Asubuhi walikuwa wachawi na mwishoni mwake mashahidi".¹

وَقَالَ أَتْلًا مِنْ قَوْمِ فِرْعَوْنَ أَتَدْرُ مُوسَى وَقَوْمَهُ لِيُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَيَذَرَكَ وَآلِهَتَكَ^ع
 قَالَ سَنُقْتِلُ آبْنَاءَهُمْ وَنَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ وَإِنَّا فَوْقَهُمْ قَاهِرُونَ ﴿١٢٧﴾ قَالَ مُوسَى
 لِقَوْمِهِ اسْتَعِينُوا بِاللَّهِ وَأَصْبِرُوا إِنَّ الْأَرْضَ لِلَّهِ يُورِثُهَا مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ وَالْعَاقِبَةُ
 لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٢٨﴾ قَالُوا أُوذِينَا مِنْ قَبْلِ أَنْ تَأْتِيَنَا وَمِنْ بَعْدِ مَا جِئْتَنَا^ط قَالَ عَسَىٰ رَبُّكُمْ
 أَنْ يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿١٢٩﴾

127. Wakasema waheshimiwa wa kaumu ya Firauni: Unamuacha Musa na watu wake walete uharibifu katika nchi na wakuache wewe na miungu yako: Akasema: Tutawauwa wavulana wao, na Tutawaacha wanawake wao. Na bila ya shaka sisi ni wenye nguvu juu yao.

128. Musa akawaambia watu wake: Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu, na subirini. Hakika ardhi ni ya Mwenyezi Mungu. Naye humrithisha Amtakaye katika waja Wake. Na mwisho ni wa wachamungu.

129. Wakasema: Tumeudhiwa kabla hatujafikia, na baada ya wewe kutujia! Musa akasema: Huenda Mola wenu Mlezi Akamhiliki adui wenu, na Akakufanyeni nyinyi ndio wa kufuatia kushika nchi, ili Atazame mtavyokuja kutenda nyinyi.

¹ At-Tabari 13:36.

Firauni anawahamasisha jamaa zake kwa Maandalizi ya Kuwaua Wana wa Israili, Mashitaka ya Wana wa Israili kwa Musa عليه السلام Kuhusu Ahadi ya Nusura ya Allah تعالى.

Allah تعالى Anaeleza juu ya njama za Firauni na watu wake, na udhia na bughudha aliyoidhamiria kwa Musa عليه السلام na watu wake.

وَقَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِ فِرْعَوْنَ

“Wakasema waheshimiwa wa kaumu ya Firauni”.

Kumuambia Firauni.

أَتَذَرُ مُوسَى وَقَوْمَهُ

“Unamuacha Musa na watu wake”.

Maana: Huwafanyii jambo.

لِيُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ

“...walete uharibifu katika nchi”.

Wawafisidi raia wako, na kuwaita katika kumuabudu Mola wao, badala ya wewe? Ala! Ajabu! Watu hawa wamegeuka na wanahofia kwamba Musa عليه السلام na watu wake watafanya ufisadi! Kwa hakika! Firauni na watu wake ndio mafisadi, lakini hawatambui. Kwa ajili hii walisema;

وَيَذَرُكَ وَءَاهَتَاكَ^٤

“...na wakuache wewe na miungu yako”.

As-Suddi aliizungumzia kauli, “Miungu yako”. Kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, “Walikuwa ni ng’ombe. Pindi walipomuona ng’ombe mzuri, Firauni alimuamuru wamuabudu. Ndiyo sababu, As-samiri aliwatengenezea ndama aliyekuwa na mlio¹”. Firauni aliyapokea waliyoyauliza, na akasema;

سَنُقَاتِلُ أِبْنَاءَهُمْ وَنَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ

“Tutawaua wavulana wao, na tutawaacha wanawake wao”.

¹ At-Tabari 13:38.

Hili ni jambo la mara ya pili, alikwishawaambia hivyo kabla ya kuzaliwa Musa عليه السلام ili auwawe mara baada ya kuzaliwa tu. Ikawa tofauti na nia na kusudio lake, Firauni. Mwisho kama ule ule ulimpata tena, alipotaka kuwadhalilisha kuwakandamiza wana wa Israil, jambo likawa kinyume na alivyotaka. Allah تعالى Aliwatukuza na Akamdhalilisha Firauni na Akamzamisha maji yeye na majeshi yake. Firauni alipokazania kuwafanyia uovu wana wa Israili.

قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ اسْتَعِينُوا بِاللَّهِ وَاصْبِرُوا^ط

“Musa akawaambia watu wake: Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu, na subirini.”

Na Akawaahidi kuwa na mwisho mwema na kwamba watapata ushindi, kwa kusema;

إِنَّ الْأَرْضَ لِلَّهِ يُورِثُهَا مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ^ط وَالْعِزَّةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٢٤﴾ قَالُوا أُوذِينَا مِنْ قَبْلِ أَنْ تَأْتِيَنَا وَمِنْ بَعْدِ مَا جِئْتَنَا

“Hakika ardhi ni ya Mwenyezi Mungu. Naye Humrithisha Amtakaye katika waja Wake. Na mwisho ni wa wachamungu. Wakasema: Tumeudhiwa kabla hatujafikia, na baada ya wewe kutujia!”

Maana: Walikwishatufanyia udhalilishaji kama ulivyoona, kabla ya uliyokuja nayo na baada yake. Akawajulisha haki yao kwa wakati huo na itakavyokuwa katika hali nyingine.

عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَنْ يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ

“Huenda Mola wenu Mlezi Akamhiliki adui wenu”

Hii inawahimiza kumshukuru Allah تعالى wakati wa kufunguliwa kwa neema na kuondoka kwa nakama.

* * *

وَلَقَدْ أَخَذْنَا آلَ فِرْعَوْنَ بِاللِّسَانِ وَنَقَصِ مِنَ الثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَذْكُرُونَ ﴿١٣٠﴾ فَإِذَا جَاءَتْهُمْ الْحَسَنَةُ قَالُوا لَنَا هَذِهِ وَإِنْ تُصِيبْ سَيِّئَةٌ يَطَّيَّرُوا بِمُوسَىٰ وَمَنْ مَعَهُ ۗ أَلَا إِنَّمَا طَّيَّرْتَهُمْ عِنْدَ اللَّهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٣١﴾ وَقَالُوا مَهْمَا تَأْتِنَا بِهِ مِنْ آيَةٍ لِنَتَّسِحَّرَنَّ بِهَا فَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٣٢﴾ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوفَانَ وَالْجَرَادَ وَالْقُمَّلَ وَالضَّفَادِعَ وَالْدَّمَ ۗ آيَاتٍ مُفَصَّلَاتٍ فَاسْتَكَرَبُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُّجْرِمِينَ ﴿١٣٣﴾ وَلَمَّا وَقَعَ عَلَيْهِمُ الرِّجْزُ قَالُوا يَا مُوسَىٰ آدَعْ لَنَا رَبَّكَ بِمَا عَهِدَ عِنْدَكَ ۗ لَئِن كَشَفْتَ عَنَّا الرِّجْزَ لَنُؤْمِنَنَّ لَكَ وَلَنُرْسِلَنَّ مَعَكَ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٣٤﴾ فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمْ الرِّجْزَ إِلَىٰ أَجَلٍ هُمْ بَلِّغُوهُ إِذَا هُمْ يَنْكُتُونَ ﴿١٣٥﴾ فَانْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ بِآيَاتِنَا كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَكَانُوا عَنْهَا غَافِلِينَ ﴿١٣٦﴾ وَأُورَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِينَ كَانُوا يُسْتَضَعُونَ مَشْرِقَ الْأَرْضِ وَمَغْرِبَهَا الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا ۗ وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ الْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ بِمَا صَبَرُوا ۗ وَدَمَرْنَا مَا كَانَ يَصْنَعُ فِرْعَوْنُ وَقَوْمُهُ وَمَا كَانُوا يَعْرُشُونَ ﴿١٣٧﴾

وَلَقَدْ أَخَذْنَا آلَ فِرْعَوْنَ بِاللِّسَانِ وَنَقَصِ مِنَ الثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَذْكُرُونَ ﴿١٣٠﴾ فَإِذَا جَاءَتْهُمْ الْحَسَنَةُ قَالُوا لَنَا هَذِهِ وَإِنْ تُصِيبْ سَيِّئَةٌ يَطَّيَّرُوا بِمُوسَىٰ وَمَنْ مَعَهُ ۗ أَلَا إِنَّمَا طَّيَّرْتَهُمْ عِنْدَ اللَّهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٣١﴾

130. Na hakika Tuliwadhivu watu wa Firauni kwa miaka (ya ukame) na kwa upungufu wa mazao, ili wapate kukumbuka.

131. Likawafika jema wakisema: Haya ni haki yetu. Na likiwafika ovu husema: Musa na walio-pamoja naye ni wakorofi. Hakika ukorofi wao huo unaowafikia unatoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui".

Firauni na Watu Wake Wakabiliwa na Ukame.

Allah تعالى Anasema;

وَلَقَدْ أَخَذْنَا آلَ فِرْعَوْنَ

"Na hakika Tuliwadhivu watu wa Firauni". Maana yake: Tuliwajaribu na Tuliwatahini.

بِالسِّينِ

“...kwa miaka (ya ukame).”

Ni miaka ya njaa kutokana na uchache wa mazao.

وَنَقَصٍ مِنَ الثَّمَرَاتِ

“...na kwa upungufu wa mazao”.

Mujahid alisema, hiyo ni chini yake (upungufu mdogo kuliko ukame)¹. Is-haqi alisema kuwa Rajaa bin Haywah alisema, “Mtende ulikuwa ukizaa tende moja tu”².

لَعَلَّهُمْ يَذْكُرُونَ ﴿٣٠﴾ فَإِذَا جَاءَتْهُمْ الْحَسَنَةُ

“...ili wapate kukumbuka. Likawafika jema”.

Maana yake: Wakati wa mavuno na riziki.

قَالُوا لَنَا هَذِهِ

“...wakisema: Haya ni haki yetu”.

Maana yake: Hii ni haki yetu.

وَإِنْ تُصِيبِهِمْ سَيِّئَةٌ

“Na likiwafika ovu”.

Maana yake: Ukame na baa la njaa.

يَطِيرُوا بِمُوسَىٰ وَمَنْ مَعَهُ

“...husema: Musa na walio pamoja naye ni wakorofi”.

Maana yake: Hii ni kwa sababu yao na waliyokuja nayo.

أَلَا إِنَّمَا طَّيَّرْتَهُمْ عِنْدَ اللَّهِ

“Hakika ukorofi wao huo unao wafikia unatoka kwa Mwenyezi Mungu”.

¹ At-Tabari 13:46.

² At-Tabari 13:46.

'Ali bin Abu Twalha alisema, kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Ayah;

أَلَا إِنَّمَا طَبَّرَهُمْ عِنْدَ اللَّهِ

“Hakika ukorofi wao huo unao wafikia unatoka kwa Mwenyezi Mungu”.

Maana yake: “Yanayowasibu yako kwa Allah تعالى na yanatoka Kwake.”

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

“Lakini wengi wao hawajui”.

وَقَالُوا مَهْمَا تَأْتِنَا بِهِ مِنْ آيَةٍ لِنَسْحَرَنَّ بِهَا فَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٣٠﴾ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوفَانَ وَالْجَرَادَ وَالْقُمَّلَ وَالضَّفَادِعَ وَالْدَّمَ ءَايَاتٍ مُفْصَلَاتٍ فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُجْرِمِينَ ﴿١٣١﴾ وَلَمَّا وَقَعَ عَلَيْهِمُ الرِّجْزُ قَالُوا يَا مُوسَى ادْعُ لَنَا رَبَّكَ بِمَا عَهِدَ عِنْدَكَ ۗ لَئِن كَشَفْتَ عَنَّا الرِّجْزَ لَنُؤْمِنَنَّ لَكَ وَلَنُرْسِلَنَّ مَعَكَ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٣٢﴾ فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمْ الرِّجْزَ إِلَىٰ أَجَلٍ هُمْ بَلِغُوهُ إِذَا هُمْ يَنْكُتُونَ ﴿١٣٣﴾

132. Na wakasema: Hata ukituletea Ishara yoyote kutuzuga hatutokuamini.

133. Basi tukawapelekea tufani, na nzige na chawa, na vyura, na damu, kuwa ni Ishara mbali mbali. Nao wakapanda kiburi, na wakawa watu wakosefu.

134. Na ilipowaangukia adhabu wakasema: Ewe Musa! Tuombe kwa Mola wako Mlezi kwa Aliyokuahidi. Ukituondolea adhabu hii hapana shaka tutakuamini, na tutawaachilia Wana wa Israili wende nawe.

135. Lakini Tukawaondolea adhabu mpaka muda fulani wao waufikie, mara wakivunja ahadi yao.

¹ At-Tabari 13:48.

Allah تعالی Anawaadhibu Watu wa Firauni kwa Sababu ya Uasi Wao.

Hapa, Allah تعالی Anaeleza juu ya uasi, uchupaji mipaka, ufidhuli na ukanushaji haki wa kaumu ya Firauni na upotovu wao, Katika kauli yao;

مَهْمَا تَأْتِنَا بِهِ مِنْ آيَةٍ لِنَسْحَرَنَّ بِهَا فَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ

“Hata ukituletea Ishara yoyote kutuzuga hatutokuamini”.

Wanasema, “Ishara, dalili na hoja yoyote unayotuletea, tutaikataa, wala hatutaikubali, wala hatutokuamini wewe wala kile ulichokuja nacho”. Kauli ya Allah تعالی:

فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوفَانَ

“Basi Tukawapelekea tufani”.

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alitoa Rai ya kuwa, “Mvua nyingi iliyogharikisha na kuhilikisha mazao na matunda”. Katika masimulizi mengine, “Ni kukithiri kwa mauti”. Mujahid alisema, “Tufani ni maji na tauni katika hali zote”¹. Ama kuhusu nzige ni mdudu mashuhuri, anayejulikana sana, na anaruhusiwa kuliwa kwa mujibu wa *Sahih* Mbili, kuwa Abu Ya’fur alisema nilimuuliza ‘ Abdullah bin Abu Awfa رضي الله عنه juu ya nzige, akasema: “Tulishiriki katika jumla ya vita saba pamoja na Mjumbe عليه السلام na tulikuwa tukila nzige.”². Ash-Shafi na Ahmad bin Hanbal na Ibn Majah walinukuu Hadithi ya ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam toka kwa baba yake toka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما kuwa Mtume عليه السلام alisema;

«أَجَلْتُ لَنَا مَيْتَانِ وَدَمَانِ: الْحُوتُ وَالْجَرَادُ وَالْكَبُذُ وَالطُّحَالُ»

“Tumehalalishiwa wafu wawili na damu mbili, samaki na nzige na ini na wengu”³.

Ibn Abu Najih alisema kuwa Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالی:

فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوفَانَ وَالْجَرَادَ

“Basi Tukawapelekea tufani na nzige”.

¹ At-Tabari 13:50.

² Fat’hul Al-Bari 9:535 na Muslim 3:1546.

³ Musnad as-Shafi 2173 na Ahmad 2:97, Ibn Majah 2:1073.

Akasema, "Walikuwa wakila misumari ya milango yao na kuziacha mbao"¹. Ama kuhusu chawa, Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, ni mdudu wa kwenye ngano² (nafaka), pia alisema kuwa ni *Ad-Daba*, ambaye ni aina ya nzige mdogo, ambaye hana mbawa³. Mujahid, 'Ikrimah na Qatadah nao walisema hivyo hivyo. Hasan na Sa'id bin Jubayr walisema, "*Qummal* ni wadudu wadogo weusi".⁴

Abu Ja'far bin Jariri رحمه الله تعالى alisema kuwa Sa'id bin Jubayr alisema, "Musa عليه السلام alipomjia Firauni, alimuambia: "Waachilie Wana wa Israili kwangu". Lakini hakuwaachilia. Allah تعالى Akawapelekea tufani juu yao, ambayo ni mvua, ikawamiminikia juu yao mfululizo kwa namna ambayo walikhofu kuwa ilikuwa adhabu. Wakamuambia Musa عليه السلام: "Muombe Mola wako Atuondolee mvua ili tukuamini na tuwaachilie Wana wa Israili kwako". Akamuomba Mola wake, Allah تعالى Akawaondolea mvua hiyo, lakini hawakumuamini, wala hawakuwaachilia Wana wa Israili.

Katika mwaka huo huo, Allah تعالى Aliotesha mimea ya mazao, matunda na majani kuliko kabla ya hapo. Wakasema, "Hivi ndivyo tulivyokuwa tukiyatamani". Allah تعالى Akawapelekea nzige ambao Aliwaachilia kwenye nyasi. Wakasema, "Ewe Musa عليه السلام! Tuombe kwa Mola wako Atuondolee nzige ili tukuamini na tuwaachilie Wana wa Israili kwako". Akamuomba Mola wake, na Allah تعالى Akawaondolea nzige. Lakini hawakumuamini, wala hawakuwaachilia Wana wa Israili.

Wakavuna mazao na kuyahifadhi majumbani, wakasema: "Tumekwisha hifadhi". Allah تعالى Akawapelekea *Qummal*, mdudu alaye nafaka anayepatikana humo. Ikafikia hatua mtu anatoa magunia matatu na kuyapeleka kusaga katika kinu basi haambullii isipokuwa takriban kilo kumi na sita tu. Wakasema, "Ewe Musa عليه السلام! Tuombe kwa Mola wako Atuondolee *Qummal* ili tukuamini na tuwaachilie Wana wa Israili kwako". Akamuomba Mola wake, na Allah تعالى Akawaondolea. Lakini hawakumuamini, wala hawakuwaachilia Wana wa Israili.

¹ At-Tabari 13:68.

² At-Tabari 13:54.

³ At-Tabari 13:58.

⁴ At-Tabari 13:55.

Wakati fulani, Musa عليه السلام akiwa amekaa mbele ya Firauni, alisikia sauti ya chura na akamuambia Firauni, “Ni kitu gani ambacho wewe na kaumu yako kitakachowapatisha tabu juu ya jambo hili?” Firauni akasema, “Kwani chura watafanya nini?” Ilipofika jioni yake, mtu aliweza kujikuta akikaa juu ya kundi la vyura ambao walirundikana mpaka kuweza kufikia kidevuni kwake, na alipoamua kuongea, basi chura aliweza kurukia kinywani mwake. Wakamuambia Musa عليه السلام, “Tuombee kwa Mola wako Atuondolee vyura hawa ili tukuamini na tuwaachilie Wana wa Israili kwako”. Akamuomba Mola wake, na Allah تعالى Akawaondolea, lakini hawakumuamini, wala hawakuwaachilia Wana wa Israili. Allah تعالى Akawapelekea damu, kiasi kwamba wakawa wanaikuta katika mito, visima, na katika maji yaliyohifadhiwa katika vyombo vyao. Wakalalamika kwa Firauni wakasema; “Kwa hakika! Tumejaribiwa kwa damu, wala hatuna kinywaji chochote”. Akasema, “Kwa hakika, Musa amekulogeni”. Wakasema, “Angewezaje kutuloga, ilhali sisi hatupati maji katika vyombo vyetu, isipokuwa damu”. Wakasema, “Ewe Musa! “Tuombee kwa Mola wako Atuondolee damu hii ili tukuamini na tuwaachilie Wana wa Israili kwako”. Akamuomba Mola wake, na Allah تعالى Akawaondolea, lakini hawakumuamini, wala hawakuwaachilia Wana wa Israili. As-Suddi, Qatadah na maulamaa wengine wa *Salaf* wanasema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alitoa masimulizi sawa na hayo.

Muhammad bin Is-haq bina Yasar alisema, “Adui wa Allah تعالى, Firauni akarejea akiwa katika hali ya kushindwa na kufedheheka baada ya wachawi kuamini. Pia akakataa kila jambo isipokuwa kubakia katika kufuru na akadumu katika shari. Allah تعالى Akampelekea ishara, Akampa mtihani wa baa la njaa, kisha akampelekea tufani kisha *Qummal*, kisha vyura, kisha damu, ni ishara zilizofuatana. Allah تعالى Alipopoleka tufani, ambayo ni maji, yalijaa juu ya uso wa ardhi, kisha yakatulia kiasi na kuwazuia kulima au kufanya amali yoyote. Wakapatwa na njaa. Walipofikwa na hayo;

قَالُوا يَا مُوسَى ادْعُ لَنَا رَبَّكَ بِمَا عَهِدَ عِنْدَكَ لَئِن كَشَفْتَ عَنَّا الرِّجْزَ لَنُؤْمِنَنَّ لَكَ
وَلَنُرْسِلَنَّ مَعَكَ بَنِي إِسْرَائِيلَ

“...wakasema: Ewe Musa! Tuombee kwa Mola wako Mlezi kwa Aliyokuahidi. Ukituondolea adhabu hii hapana shaka tutakuamini, na tutawaachilia Wana wa Israili waende nawe”.

Musa عليه السلام akamuomba Mola wake, Akawaondolea lakini hawakutekeleza chochote katika waliyoyasema. Allah تعالى Akawapelekea nzige, wakala miti na misumari iliyotengenezwa kwa vyuma ambayo ilikuwa katika milango yao mpaka ikaanguka kutoka katika maskani yao. Wakasema kama walivyosema hapo awali. Lakini hawakutekeleza chochote. Musa عليه السلام akamuomba Mola wake, Akawaondolea lakini hawakutekeleza chochote katika waliyosema. Allah تعالى Akawapelekea *Qummal* walianguka kutoka humo, wakaenea majumbani na katika vyakula na kuwazuia kulala na kupumzika. Walipoathirika na hilo, walisema kama hapo awali.

Allah تعالى Akawapelekea vyura ambavyo vilijazana majumbani, katika vyakula na katika vyombo, ikawa anayefunua nguo au chombo bali hukuta vyura wameenea. Mtihani huu ulipowashinda walisema kama walivyosema, wala hawakutekeleza chochote katika waliyoyasema. Allah تعالى Akawapelekea damu mpaka maji ya kaumu ya Firauni yakageuka kuwa damu. Hawakuweza kuchota maji ya kisima wala mto, wala katika chombo bali yalibadilika na kuwa damu.”¹

فَأَنْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ بِآيِهِمْ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَكَانُوا عَنْهَا غَافِلِينَ ﴿١٣٦﴾
 وَأَوْرَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِينَ كَانُوا يُسْتَضْعَفُونَ مَشْرِقَ الْأَرْضِ وَمغربَهَا الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا ۖ وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ الْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ بِمَا صَبَرُوا ۖ وَدَمَرْنَا مَا كَانُوا يَصْنَعُونَ ۖ فِرْعَوْنَ ۖ وَقَوْمَهُ ۖ وَمَا كَانُوا يَعْرِشُونَ ﴿١٣٧﴾

136. Basi Tuliwapatiliza, Tukawazamisha baharini kwa sababu walizikanusha ishara Zetu, na wakaghafilika nazo. Na

137. Tukawarithisha watu waliokuwa wanadharauliwa Mashariki na Magharibi ya ardhi Tuliyoibariki. Na likatimia neno jema la Mola Mlezi wako juu ya Wana wa Israili, kwa vile walivyosubiri. Na Tukayaangamiza aliyokuwa akiyafanya Firauni na kaumu yake, na waliyokuwa wakiyajenga”.

¹ At-Tabari 13:63.

Watu wa Firauni Wanagharikishwa Baharini, Wana wa Israili Wanarithishwa Ardhi Iliyobarikiwa.

Allah تعالی Anaeleza kuwa pindi walipoasi na kuruka mipaka, hata hivyo, Aliwatahini kwa ishara zenye kufuatana moja baada ya nyingine. Na kisha Aliwaadhibu kwa Kuwazamisha baharini, adhabu ambayo ilimuachia nafasi Musa عليه السلام, kuvuka pamoja na wana wa Israili. Kisha Firauni na majeshi yake wakawafuatilia, walipomalizikia ndani yake, bahari ikawazingira na kuwagharikisha wote. Hayo ni kwa kule kuzikadhibisha kwao ishara za Allah تعالی na kughafilika nazo. Pia Allah تعالی Alieleza kwamba Aliwarithisha Mashariki ya ardhi na Magharibi yake. Hasan bin Al-Basri na Qatadah walizungumzia Kauli ya Allah تعالی:

مَشْرِقِ الْأَرْضِ وَمَغْرِبِهَا الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا

“...Mashariki na Magharibi ya ardhi Tuliyoibariki”.

Maana yake: Sham (Syria). Na kuhusu Kauli ya Allah تعالی:

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ الْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ بِمَا صَبَرُوا

“Na likatimia neno jema la Mola Mlezi wako juu ya Wana wa Israili, kwa vile walivyosubiri”.

Mujahid na Ibn Jariri رحمه الله تعالی walisema kuwa inaelezewa na Kauli ya Allah تعالی:

وَتُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ
الْوَارِثِينَ ﴿٥٦﴾ وَنُمَكِّنَ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ وَنُرِيَ فِرْعَوْنَ وَهَامَانَ وَجُنُودَهُمَا مِنْهُمْ مَا
كَانُوا يُحَدِّثُونَ ﴿٥٧﴾

“Na Tukataka Kuwafadhili waliodhoofishwa katika nchi hiyo na Kuwafanya wawe viongozi na Kuwafanya ni warithi. Na Kuwapa nguvu katika nchi, na kutokana na wao kuonesha kina Firauni na Hamana na majeshi yao mambo yale waliyokuwa wakiyaogopa”.
(28:5-6)

Kauli ya Allah تعالی:

وَدَمَّرْنَا مَا كَانُوا يَصْنَعُونَ فِرْعَوْنَ وَقَوْمَهُ

“Na Tukayaangamiza aliyokuwa akiyafanya Firauni na kaumu yake”.

Maana: Tukayaharibu waliyokuwa wakiyazalisha Firauni na watu wake, mfano wa majengo na mazao.

وَمَا كَانُوا يَعْرِشُونَ

“...na waliyokuwa wakiyajenga”.

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na Mujahid walisema;

يَعْرِشُونَ

“...wakiyajenga”.

* * *

وَجَوَزْنَا بِبَنِي إِسْرَائِيلَ الْبَحْرَ فَأَتَوْا عَلَى قَوْمٍ يَعْكُفُونَ عَلَى أَصْنَامِهِمْ ۖ قَالُوا يَا مُوسَى اجْعَلْ لَنَا إِلَهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ ۚ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ ﴿١٣٨﴾ إِنَّ هَؤُلَاءِ مَثَبٌ مَّا هُمْ فِيهِ وَيَنْطَلُونَ ۚ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٩﴾ قَالَ أَغْوَى اللَّهُ أَتْبَعِيكُمْ إِلَهًا وَهُوَ فَضَّلَكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٤٠﴾ وَإِذْ أَخْبَيْنَاكُمْ مِنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ يُقْتُلُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ ۗ فِي ذَلِكُمْ بَلَاءٌ مِّنْ رَبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿١٤١﴾ * وَوَعَدْنَا مُوسَى ثَلَاثِينَ لَيْلَةً وَأَتَمَمْنَا بِعَشْرِ فِتْنَةٍ مِّمْقَتُ رَبِّمَ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً ۗ وَقَالَ مُوسَى لِأَخِيهِ هَارُونَ أَخْلِفْنِي فِي قَوْمِي وَأَصْلِحْ وَلَا تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٤٢﴾ وَلَمَّا جَاءَ مُوسَى لِمِيقَاتِنَا وَكَلَّمَهُ رَبُّهُ قَالَ رَبِّ أَرِنِي إِلَيْكَ ۗ قَالَ لَنْ تَرِنِي وَلَكِنِ أَنْظُرَ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ تَرِنِي ۗ فَلَمَّا تجلَّى رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكًّا وَخَرَّ مُوسَى صَعِقًا ۗ فَلَمَّا أَفَاقَ قَالَ سُبْحَانَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٤٣﴾

وَجَوَزْنَا بِبَنِي إِسْرَائِيلَ الْبَحْرَ فَأَتَوْا عَلَى قَوْمٍ يَعْكُفُونَ عَلَى أَصْنَامِهِمْ ۖ قَالُوا يَا مُوسَى اجْعَلْ لَنَا إِلَهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ ۚ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ ﴿١٣٨﴾ إِنَّ هَؤُلَاءِ مَثَبٌ مَّا هُمْ فِيهِ وَيَنْطَلُونَ ۚ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٩﴾

138. Na Tukawavusha bahari Wana wa Israili, wakafika kwa watu wanao-abudu masanamu yao. Wakasema: Ewe Musa! Hebu tufanyie na sisi miungu kama hawa walivyokuwa na miungu. Musa akasema: Hakika nyinyi ni watu msiojua kitu.

139. Hakika haya waliyonyo watu hawa yatakuja angamia, na hayo waliyokuwa wakiyafanya yamepotea bure.

Wana wa Israil Wanavuka Bahari, Lakini Wangali na Fikra za Ibada ya Masanamu.

Allah تعالی Anajulisha juu ya walichokisema majahili wa wana wa Israili kumuambia Musa عليه السلام, walipovuka bahari na kuziona ishara za Allah تعالی na ukubwa wa nguvu Zake.

فَأَتَوْا عَلَى قَوْمٍ يَعْكُفُونَ عَلَى أَصْنَامِهِمْ ۖ

“...wakafika kwa watu wanaoabudu masanamu yao”.

Baadhi ya maulamaa wa tafsiri walisema, watu waliotajwa hapa walitokea Kanaan, pia ilisemwa kuwa walitokea Lakhm. Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, "Walikuwa wakiyaabudu masanamu yaliyofanywa katika umbo la ng'ombe na hii iliwaathiri wana wa Israili kwa kutaka wafanane na wao kwa kutaka kumuabudu ndama, baada ya hapo". Walisema;

يَمْؤِسَىٰ أَجْعَلْ لَّنَا إِلَهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ

"Ewe Musa! Hebu tufanyie na sisi miungu kama hawa walivyokuwa na miungu. Musa akasema: Hakika nyinyi ni watu msiojua kitu".¹

Maana yake: Mmekuwa na ujahili juu ya Ukuu wa Allah تعالى na Utukufu Wake na Kusafika Kwake, dhidi ya mshirika na cha kushabihiana Naye.

إِنَّ هَتَوْلَاءِ مُتَّبِعٌ مَا هُمْ فِيهِ

"Hakika haya waliyonayo watu hawa yatakuja angamia".

Maana yake: Wamehiliki.

وَيَنْطَلِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

"...na hayo walivyokuwa wakiyafanya yamepotea bure".

Imamu Abu Ja'far bin Jariri رحمه الله تعالى katika kuitafsiri Ayah hii alisema kuwa Abu Waqid Al-Laythi alisema kwamba walitoka Makkah pamoja na Mtume ﷺ kuelekea Hunayni. Baadhi ya makafiri walikuwa na mkunazi waliokuwa wakikaa hapo na kuangika silaha zao juu yake. Mti huo ulikuwa ukiitwa *Dhat Anwaat*. Tukaupita mikunazi mkubwa wa kijani. Tukasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Tuchagulie *Dhat Anwaat* kama wao". Akasema;

«قُلْتُمْ وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ كَمَا قَالَ قَوْمُ مُوسَىٰ لِمُوسَىٰ:

"Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Mmesema kama kaumu ya Musa walivyomuambia Musa;

أَجْعَلْ لَّنَا إِلَهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ ﴿١٣٨﴾ إِنَّ هَتَوْلَاءِ مُتَّبِعٌ مَا هُمْ فِيهِ

وَيَنْطَلِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٩﴾

¹ At-Tabari 13:80.

“Hebu tufanyie na sisi miungu kama hawa walivyo kuwa na miungu. Musa akasema: Hakika nyinyi ni watu msiojua kitu. Hakika haya waliyonayo watu hawa yatakuja angamia, na hayo waliyokuwa wakiyafanya yamepotea bure”.¹

قَالَ أَغَيَّرَ اللَّهُ أَبْغِيكُمْ إِلَهًا وَهُوَ فَضَّلَكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٣٨﴾ وَإِذْ أَخْبَيْنَاكُمْ مِنْ
 ءَالِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ يُقْتُلُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ وَفِي
 ذَٰلِكُمْ بَلَاءٌ مِّنْ رَبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿١٣٩﴾

140. *“Akasema: Je nikutafutieni mola asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na Yeye Ndiye Aliyekufadhilisheni juu ya viumbe vyote?”*

141. *“Na pale Tulipokuo kweni kwa watu wa Firauni waliokupeni adhabu za mwisho wa uovu. Wakiwaua wavulana wenu, na wakawaacha hai wanawake wenu. Na katika hayo yalikuwa majaribio makubwa kutokana na Mola wenu Mlezi”.*

Kuwakumbusha Wana wa Israili Juu ya Baraka za Allah تعالی Kwao.

Musa عليه السلام Anawakumbusha Wana wa Israili juu ya neema za Allah تعالی juu yao kutokea Kuwaokoa kutoka katika utumwa chini ya Firauni na ukandamizaji wake na ufedheheshaji na udhalilishaji aliokuwa nao. Aliwakumbusha juu ya utukufu na kisasi dhidi ya adui wao na kwamba walimuona wakati akihakirika, akahiliki na kugariki na kuangamia. Tafsiri yake ilikwihatangulia katika Surat Al Baqarah kuanzia Aya (49 - 50).

* وَوَعَدْنَا مُوسَىٰ ثَلَاثِينَ لَيْلَةً وَأَتَمَمْتَهَا بِعَشْرِ فِتْمٍ مِّمَقْتُ رَبِّهِ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً وَقَالَ
 مُوسَىٰ لِأَخِيهِ هَارُونَ أَخْلِفْنِي فِي قَوْمِي وَأَصْلِحْ وَلَا تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٣٩﴾

142. *“Tulimuahidi Musa masiku thelathini na Tukayatimiza kwa kumi; ikatimia miadi ya Mola wake Mlezi masiku arubaini. Na Musa akamuambia nduguye Haarun: Shika pahala pangu kwa watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu”.*

¹ At-Tabari 13:82.

Musa عليه السلام Alifunga Swaumu kwa ajili ya Allah تعالى Siku Arubaini.

Allah تعالى Anawakumbusha Wana wa Israil juu ya Mwongozo Aliowapelekea kupitia kwa Musa عليه السلام na Kumpatia Kwake Taurati ambayo ndani yake mna hukumu zao na ufafanuzi wa Sharia zao. Allah تعالى Ametaja kuwa Alimchagulia Musa عليه السلام jumla ya masiku thelathini. Maulamaa wa Tafsiri walisema, Musa عليه السلام alifunga kwa muda huo na alipomaliza na ukatimia wakati huo ulioteuliwa, alipiga mswaki kwa kijiti cha mti. Allah تعالى Akamuamuru akamilishe siku arubaini kwa kuongeza siku kumi zaidi. Muda ulipotimia na Musa عليه السلام akaazimia kwenda katika mlima *At-Tur*.

Sawa na Alivyosema Allah تعالى;

يَبْنَئِ إِسْرَائِيلَ قَدْ أَهْجَيْنَاكُمْ مِّنْ عَدُوِّكُمْ وَوَعَدْنَاكُمْ جَانِبَ الطُّورِ الْأَيْمَنِ

“Enyi Wana wa Israili! Hakika Tulikuokoeni na adui yenu, na Tukakuahidini upande wa kulia wa mlima”. (20:80)

Wakati huo, Musa عليه السلام aliondoka na kumuacha nduguye, Haarun عليه السلام pamoja na Wana wa Israil na akamuusia kufanya wema na kutoharibu jambo. Huku ni kutanabaisha na kukumbusha, kwani Haarun عليه السلام ni Nabii Mtukufu, mwenye hadhi kubwa, ambaye alikuwa na neema na utukufu.

وَلَمَّا جَاءَ مُوسَى لِمِيقَاتِنَا وَكَلَّمَهُ رَبُّهُ قَالَ رَبِّ أَرِنِي إِلَيْكَ ۚ قَالَ لَنْ نَرَنِي
وَلَكِنِ أَنْظِرْ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ نَرِنِي ۚ فَلَمَّا تَجَلَّى رَبُّهُ لِلْجَبَلِ
جَعَلَهُ دَكًّا وَخَرَّ مُوسَى صَبَعًا ۚ فَلَمَّا أَفَاقَ قَالَ سُبْحَانَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَأَنَا أَوَّلُ

الْمُؤْمِنِينَ

143. “Na alipokuja Musa kwenye miadi Yetu, na Mola wake Mlezi Akamsemeza, alisema: Mola wangu Mlezi! Nioneshe nikutazame. Mwenyezi Mungu Akasema: Hutoniona. Lakini utazame huo mlima. Ukibaki pahala pake basi utaniona. Basi Alipojionesha Mola wake kwa mlima, Aliufanya uvurugike na Musa akaangukia chini amezimia. Alipozindikana alisema: Subhanaka, Umetakasika! Natubu Kwako, na mimi ni wa kwanza wa Waumini”.

Musa عليه السلام Alimuomba Allah تعالى Amuone.

Allah تعالى Anaeleza kuwa Musa عليه السلام alipokuja katika ahadi Yake na akazungumza moja kwa moja, alimuomba Allah تعالى aweze kumuona, alisema;

قَالَ رَبِّ أَرِنِي أَنْظُرْ إِلَيْكَ ۖ قَالَ لَنْ تَرَنِي

“Mola wangu Mlezi! Nioneshe nikutazame. Mwenyezi Mungu Akasema: Hutoniona”.

Herufi ‘Lan’ hapa ni ya kukanusha kumuona duniani. Kuna Hadithi *Mutawaatir*¹ kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba waumini watamuona Allah تعالى huko Akhera, kama tutakavyoeleza wakati wa kuelezea Kauli ya Allah تعالى;

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ ﴿٢٢﴾ إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ ﴿٢٣﴾

“Zipo nyuso siku hiyo zitato ng’ara, zinamuangalia Mola wao Mlezi”.
(75:22-23)

Katika vitabu vilivyotangulia, Allah تعالى Alimuambia Musa عليه السلام; “Ewe Musa! Hapana aliye hai wa Kuniona, bali hufa. Wala kilicho Yabisi, bali hutetemeka”.²

فَلَمَّا تَخَلَّىٰ رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكًّا وَخَرَّ مُوسَىٰ صَعِقًا

“Basi Alipojionesha Mola wake kwa mlima, Aliufanya uvurugike na Musa akaangukia chini amezimia”.

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alinukuu katika *Musnad* yake kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

فَلَمَّا تَخَلَّىٰ رَبُّهُ لِلْجَبَلِ

“Basi alipojionesha Mola wake kwa mlima”.

Alisema;

«هكذا»

“Kama hivi”. Huku akiwa ameshikilia ncha ya kidole kidogo.³ Pia hivi ndivyo alivyonukuu At-Tirmidhi katika tafsiri ya Ayah hii, kisha akasema, “Hadithi hii ni *Hasan Sahih gharib*”.⁴

¹ Ikiwa na wasimuliaji kadha katika kila hatua ya kila isnadi.

² Al-Bidayah Wan-Nihayah 3:112.

³ Ahmad 3:125. ⁴ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:401.

Na hivi ndivyo alivyosema Al-Hakim katika kitabu chake, *Al-Mustadrak* kupitia njia ya Hammad bin Salmah, na akasema, “Hadith hii ni *Sahih* kwa vigezo vya Muslim, lakini hawakuinukuu.”¹ As-Suddi alisema kuwa ‘Ikrimah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliitafsiri Kauli ya Allah تعالى:

فَلَمَّا تَخَلَّىٰ رَبُّهُ لِلْجَبَلِ

“Basi Alipojionesha Mola wake kwa mlima”.

Ni kadiri ncha ya kidole kidogo kilionekana kutoka Kwake.

جَعَلَهُ دَكًّا

“...Aliufanya uvurugike” Alisema, “Mchanga”.

وَخَرَّ مُوسَىٰ صَبَقًا

“...na Musa akaangukia chini amezimia”.

Alisema, “Alizirai”². Pia alinukuu Ibn Jarir رحمه الله تعالى kwa kuwa kuna neno linalojulisha juu ya *Al-Ghashiyy* (kupoteza fahamu).

Nalo ni Kauli ya Allah تعالى:

فَلَمَّا أَفَاقَ

“Alipozindikana”.

Na kuzindikana hakutokani isipokuwa baada ya *Al-Ghashiyy* (kupoteza fahamu).

قَالَ سُبْحَانَكَ

“...alisema: Subhanaka, Umetakasika!”

Ni njia ya Kumtakasa Allah تعالى, Kumtukuzi na Kumueka juu, kwamba duniani hakuna chenye kuweza kumuona Allah تعالى isipokuwa hufa.

Kauli ya Allah تعالى:

تُبَّتْ إِلَيْكَ

“Natubu Kwako”.

Mujahid alisema, maana yake, Mimi natubu Kwako juu ya kukuomba kukuona.

¹ At-Tabari 13:97.

² Al-Hakim 2:320.

وَأَنَا أَوَّلُ الْمُؤْمِنِينَ

“...na mimi ni wa kwanza wa Waumini”.

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na Mujahid walisema, miongoni mwa Wana wa Israil, na Ibn Jariri رحمه الله تعالى aliyakhitari maoni haya. Katika masimulizi mengine ni kwamba, Ibn 'Abbas رضي الله عنهما Kauli ya Allah تعالى;

أَوَّلُ الْمُؤْمِنِينَ

“...na mimi ni wa kwanza wa Waumini”.

Maana: Hakuna atakayekuona. Kauli ya Allah تعالى;

وَحَرَّ مُوسَىٰ صَبْعًا

“...na Musa akaangukia chini amezimia”.

Abu Sa'id na Abu Hurayrah رضي الله عنهما walisimulia Hadithi ya Mtume ﷺ. Hadithi aliyoisimulia Abu Sa'id رضي الله عنه imetajwa katika *Sahih* Al-Bukhari na inafaa tuitaje hapa. Alisema, Myahudi mmoja alikuja kwa Mtume ﷺ, baada ya uso wake kupigwa kofi, akasema, “Ewe Muhammad! Kuna sahaba wako mmoja amenipiga kofi usoni kwangu”. Mtume ﷺ akasema;

«ادْعُوهُ»

“Muiteni”

Wakamuita na Mtume ﷺ akasema;

«لِمَ لَطَمْتَ وَجْهَهُ؟»

“Kwanini umempiga kofi usoni?”

Akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Mimi nilipita karibu na Myahudi huyu nikamsikia akisema, “Naapa kwa Aliyemteua Musa عليه السلام juu ya wanaadamu”. Nikasema, “Hata juu ya Muhammad ﷺ?” Nikashikwa na hasira na nikamzaba kibao”. Mtume ﷺ akasema;

«لَا تُحَيِّرُونِي مِنْ بَيْنِ الْأَنْبِيَاءِ فَإِنَّ النَّاسَ يَضَعِفُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَأَكُونُ أَوَّلَ مَنْ يُفِيءُ،
فَإِذَا أَنَا بِمُوسَىٰ أَخَذْتُ بِقَائِمَةٍ مِنْ قَوَائِمِ الْعَرْشِ، فَلَا أَدْرِي أَفَأَقَّ قَبْلِي أَمْ جُوزِي
بِضَعْفَةِ الطُّورِ»

"Msinikhitari mimi baina ya Mitume, kwani watu watapoteza fahamu katika Siku ya Kiyama, nami nitakuwa wa kwanza kuzindukana. Na hapo nitakutana na Musa akiwa ameshikilia nguzo mojawapo ya Arshi. Sitaweza kujua kwamba alizindukana kabla yangu ama amepata malipo kutokana na kuzimia katika mlima wa At-Tur".¹

Al-Bukhari ameinukuu Hadithi hii katika sehemu nyingi ndani ya *Sahih* yake; pia Muslim chini ya sura inayozungumzia Hadithi za Manabii; na Abu Dawud chini ya Kitabu cha Sunna, katika *Sunan* yake². Ama Hadithi ya Abu Hurayrah *رضي الله عنه* ameinukuu Imamu Ahmad na Masheikh wawili (Al-Bukhari na Muslim)³.



¹ Fat'hul Al-Bari 8:152.

² Al-Bukhari 2412, 3398, 3638, 6917, 7427, 6518, Muslim 2374 na Abu Dawud 4668.

³Ahmad 2:264, Fat'h Al-Bukhari 13:455 na Muslim 4:1844.

قَالَ يَمُوسَىٰ إِنِّي اصْطَفَيْتُكَ عَلَىٰ النَّاسِ بِرِسَالَتِي
 وَبِكَلِمَىٰ فَخُذْ مَا آتَيْتُكَ وَكُن مِّنَ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾
 وَكَتَبْنَا لَهُ فِي الْأَلْوَابِ مِن كُلِّ شَيْءٍ مَّوْعِظَةً وَتَفْصِيلًا
 لِّكُلِّ شَيْءٍ فَخُذْهَا بِقُوَّةٍ وَأْمُرْ قَوْمَكَ يَأْخُذُوا بِأَحْسَنِهَا
 سَأُورِيكُمْ دَارَ الْفَاسِقِينَ ﴿١٤٥﴾ سَأَصْرَفُ عَنْ آيَاتِي الَّذِينَ
 يَتَكَبَّرُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَإِن يَرَوْا كُلاًّ آيَةٍ لَا
 يُؤْمِنُوا بِهَا وَإِن يَرَوْا سَبِيلَ الرُّشْدِ لَا يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا وَإِن
 يَرَوْا سَبِيلَ الْغَيِّ يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَذَّبُوا
 بِآيَاتِنَا وَكَانُوا عَنْهَا غَافِلِينَ ﴿١٤٦﴾ وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا
 وَلِقَاءِ الْآخِرَةِ حَبِطَتْ أُعْمَالُهُمْ هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا
 يَعْمَلُونَ ﴿١٤٧﴾ وَأَخَذَ قَوْمَ مُوسَىٰ مِن بَعْدِهِ مِن خَلْقِهِمْ
 عِجْلًا جَسَدًا لَهُ خُورٌ أَلْمَرُ يَرَوْنَ أَنَّهُ لَا يُكَلِّمُهُمْ وَلَا
 يُهْتَدِيهِمْ سَبِيلًا اتَّخَذُوهُ وَكَانُوا ظَالِمِينَ ﴿١٤٨﴾ وَكَأ
 سَفِطَ فِي أَيْدِيهِمْ وَرَأَوْا أَنَّهُمْ قَدِ ضَلُّوا قَالُوا لَئِن لَّمْ
 يَرْحَمْنَا رَبُّنَا وَيَغْفِرْ لَنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿١٤٩﴾

قَالَ يَمُوسَىٰ إِنِّي اصْطَفَيْتُكَ عَلَىٰ
 النَّاسِ بِرِسَالَتِي وَبِكَلِمَىٰ فَخُذْ مَا
 آتَيْتُكَ وَكُن مِّنَ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾
 وَكَتَبْنَا لَهُ فِي الْأَلْوَابِ مِن كُلِّ
 شَيْءٍ مَّوْعِظَةً وَتَفْصِيلًا لِّكُلِّ شَيْءٍ
 فَخُذْهَا بِقُوَّةٍ وَأْمُرْ قَوْمَكَ يَأْخُذُوا
 بِأَحْسَنِهَا سَأُورِيكُمْ دَارَ الْفَاسِقِينَ ﴿١٤٥﴾

144. "(Mwenyezi Mungu) Akasema: Ewe Musa! Mimi nimekuteua wende kwa watu na Ujumbe Wangu na Maneno Yangu. Basi chukua niliyokupa na uwe katika wanaoshukuru".

145. "Na Tukamuandikia katika mbao kila kitu, mawaidha na maelezo ya mamboyote. (Tukamuambia): Basi yashike kwa nguvu na

uwaamrishe watu wako wayashike kwa ubora wake. Nami Nitakuonesheni makazi ya wapotofu".

Allah تعالیٰ Anamteua Musa عليه السلام na Kumpa Mbao.

Allah تعالیٰ Anaeleza kwamba Yeye Alizungumza na Musa عليه السلام moja kwa moja na Akamuambia kuwa Alimteua yeye juu ya watu wa zama zake kwa ujumbe Wake na kwa Kuzungumza naye.

Hapana shaka kuwa Muhammad ﷺ ndiye mkuu wa wana wote wa Adam عليه السلام, tokea hao wa mwanzo hadi wa mwisho. Kwa ajili hiyo Allah تعالیٰ Alimteua kuwa Nabii na Mtume wa mwisho, ambaye Sharia yake inaendelea mpaka Siku ya Kiyama, na wafuasi wake ni wengi zaidi kuliko wafuasi wa

Manabii na Mitume wengine wote. Baada yake, anayefuatia kwa cheo bora ni Ibrahim *Al-Khalil* عليه السلام kisha Musa bin 'Imran عليه السلام ambaye alizungumza na Allah تعالى moja kwa moja. Kwa sababu hiyo, Allah Alisema kwa ajili yake;

فَخُذْ مَا آتَيْتُكَ

“Basi chukua Niliyokupa”. Maana yake: Maneno na Mazungumzo Yangu Mimi na wewe.

وَكُن مِّنَ الشَّاكِرِينَ

“...na uwe katika wanaoshukuru”. Maana: Juu yao, wala usiyatake yale ambayo huwezi kuyamudu. Kisha Allah تعالى Alieleza kuwa Alimuandikia katika mbao, mawaidha na upambanuzi wa kila kitu. Ilisemwa: Mbao zilikuwa zimetengenezwa kwa kito, na kwamba Allah تعالى Alimuandikia humo, mawaidha na hukumu zilizobainisha na kufafanuliwa kuhusu halali na haramu. Mbao hizi ziliikusanya Taurati, ambayo Allah تعالى Aliizungumzia.

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ مِن بَعْدِ مَا أَهْلَكْنَا الْقُرُونَ الْأُولَىٰ بَصَائِرَ لِلنَّاسِ

“Na hakika bila ya shaka Tulimpa Musa Kitabu baada ya kwisha ziangamiza kaumu za mwanzo, ili kiwafumbue macho watu”.
(28:43)

Na ilisemwa: Musa عليه السلام alipatiwa mbao kabla ya Taurati. *Allahu A'alam*. Kauli ya Allah تعالى;

فَخُذْهَا بِقُوَّةٍ

“Basi yashike kwa nguvu”. Maana yake: Kuwa imara katika Twaa.

وَأْمُرْ قَوْمَكَ يَا خُدُوعًا بِأَحْسَنِهَا

“...na uwaamrishe watu wako wayashike kwa ubora wake.”

Sufyan bin 'Uyaynah alisema: Abu Sa'id alitueleza, kutoka kwa 'Ikrimah kwamba Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Musa عليه السلام aliamrisha achukue lililo gumu kabisa katika waliyoamrisha kaumu yake”.¹ Kauli ya Allah تعالى;

سَأُورِيكُمْ دَارَ الْفَاسِقِينَ

“Nami Nitakuonesheni makazi ya wapotofu”.

¹ At-Tabari 13:110.

Maana: Mtauona mwisho wa watakaokhalifu Amri Yangu na kutoka katika Kunitii, namna atakavyohiliki, kuharibikiwa na kupata khasara kubwa kabisa.

سَأَصْرَفُ عَنْ آيَاتِي الَّذِينَ يَتَكَبَّرُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَإِنْ يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَا
يُؤْمِنُوهَا وَإِنْ يَرَوْا سَبِيلَ الرُّشْدِ لَا يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا وَإِنْ يَرَوْا سَبِيلَ الْغَيِّ يَتَّخِذُوهُ
سَبِيلًا ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَكَانُوا عَنْهَا غَافِلِينَ ﴿١٤٤﴾ وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا
وَلِقَاءِ الْآخِرَةِ حَبِطَتْ أُعْمَالُهُمْ هَلْ يُحْزَنُونَ ﴿١٤٥﴾ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٦﴾

146. "Nitawatenga na Ishara Zangu wale wanaofanya kiburi katika nchi bila ya haki. Na wao wakiona kila Ishara hawaiamini. Wakiiona njia ya uwongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia; lakini wakiiona njia ya upotofu wanaishika kuwa ndiyo njia. Hayo ni kwa sababu wamezikanusha Ishara Zetu, na wameghafilika nazo".

147. "Na waliozikanusha Ishara Zetu na mkutano wa Akhera amali zao zimeharibika. Kwani watalipwa ila kwa yale waliyokuwa wakiyatenda?"

Watu Jeuri Hawatapewa Ishara za Allah تعالى.

Allah تعالى Anasema;

سَأَصْرَفُ عَنْ آيَاتِي الَّذِينَ يَتَكَبَّرُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ

"Nitawatenga na Ishara Zangu wale wanaofanya kiburi katika nchi bila ya haki".

Kwa maana: Nyoyo za wafanyao kiburi, Nitazizuia dhidi ya ufahamu wa hoja na dalili juu ya Ukuu Wangu, Sharia Yangu na Hukumu Zangu. Ni hao wanaofanya kiburi badala ya kunitii. Na wanawafanyia kiburi watu wengine kinyume cha haki, maana yake, kama walivyofanya kiburi dhidi ya haki, Allah تعالى Amewadhaliisha kwa ujahili. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَنُقَلِّبُ أَقْصَابَهُمْ وَأَبْصُرُهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ

"Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza". (6:110) na;

فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاغَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ^١

“Walipopotoka, Mwenyezi Mungu Aliziachia nyoyo zao zipotoke”.
(61:5)

Sufyan aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

سَأَصْرِفُ عَنْ آيَاتِيَ الَّذِينَ يَتَكَبَّرُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ

“Nitawatenga na Ishara Zangu wale wanaofanya kiburi katika nchi bila ya haki”.

“Allah تعالى Anasema, Nitawaondolea ufahamu wa Qur’an na Aya Zangu”.¹ Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, “Hii inajulisha kwamba maneno haya yanahusu umma huu”.² (Mimi, Ibn Kathir) nasema, hiyo si lazima iwe kweli, kwa sababu Ibn ‘Uyaynah alimaanisha kwamba hili linajitokeza kwa kila umma, wala hakuna tofauti baina ya umma mmoja na mwingine juu ya hili. *Allah Aalam*. Kauli ya Allah تعالى:

وَأِنْ يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَا يُؤْمِنُوا بِهَا

“Na wao wakiona kila Ishara hawaiamini”. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ

يَرَوْا آعَذَابَ الْأَلِيمِ ﴿٦٧﴾

“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini, Ijapokuwa itawajia kila ishara, mpaka waione adhabu iliyochungu”. (10:96-97)

Kauli ya Allah تعالى:

وَأِنْ يَرَوْا سَبِيلَ الرُّشْدِ لَا يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا

“Wakiiona njia ya uwongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia”.

Kwa maana: Ikiwadhihirikia wao njia ya uongofu, yaani njia ya kuokoa, hawaipiti na ikiwadhihirikia njia ya hilaki na upotevu, wao hufanya ndio ya kuifuata. Kisha Allah تعالى Anaeleza sababu ya wao kuwa hivyo;

¹ At-Tabari 13:112.

² At-Tabari 13:113.

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا

“Hayo ni kwa sababu wamezikanusha Ishara Zetu”.

Kwa maana: Nyoyo zao zilikadhibisha.

وَكَانُوا عَنَّا غَافِلِينَ

“...na wameghafilika nazo”.

Maana yake: Hawaelewi mambo yaliyomo humo.

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَلِقَاءِ الْآخِرَةِ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ

“Na waliozikanusha Ishara Zetu na mkutano wa Akhera amali zao zimeharibika”.

Maana yake: Mwenye kuyafanya hayo miongoni mwao na akaendelea hivyo mpaka kifo, amali zao zitakuwa zimeharibika. Kauli ya Allah تعالى:

هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Kwani watalipwa ila kwa yale waliyokuwa wakiyatenda?”

Maana yake: Kwa hakika Tutawalipa kulingana na amali zao walizozitanguliza, kheri kwa amali njema na ubaya kwa uovu.

Ni sawa na upandacho ndicho uvunacho.

وَأَخَذَ قَوْمَ مُوسَىٰ مِنْ بَعْدِهِمْ مِنْ حُلِيِّهِمْ عِجْلًا جَسَدًا لَهُ خُورٌ أَلْمَرُّ يَرَوْنَ أَنَّهُ لَا يُكَلِّمُهُمْ
وَلَا يَهْدِيهِمْ سَبِيلًا اتَّخَذُوهُ وَكَانُوا ظَالِمِينَ ﴿١٤٨﴾ وَلَمَّا سَقَطَ فِي أَيْدِيهِمْ وَرَأَوْا أَنَّهُمْ
قَدْ ضَلُّوا قَالُوا لَئِن لَّمْ يَرْحَمْنَا رَبُّنَا وَيَغْفِرْ لَنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿١٤٩﴾

148. “Na baada yake watu wa Musa walimfanya ndama kutokana na mapambo yao (kumuabudu), kiwiliwili tu kilichokuwa na sauti. Hivyo, hawakuona kuwa hawasemezi wala hawaongoi njia? Wakamuabudu na wakawa wenye kudhulumu”.

149. “Na walipojuta na wakaona ya kwamba wamekwishapotea, walisema: Ikiwa Mola wetu Mlezi Hakuturehemu na Akatusamehe, bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa waliokhasiri”.

Kisa cha Kuabudu Ndama.

Allah تعالی Anaeleza upotevu wa Wana wa Israili walioabudu ndama ambaye Samiri aliwatengenezea kutokana na mapambo waliyoyaaazima kutoka kwa Maqibti. Aliwatengenezea katika umbo la ndama na akatupatia kiasi cha kofi la mchanga ambao aliuchukua kutoka katika vumbi la mapito ya farasi aliyekuwa amembeba Jibrili عليه السلام na ndama huyo alikuwa pia na mlio wa ng'ombe. Hili lilitokea baada ya Musa عليه السلام kwenda kwa Mola wake katika kipindi maalumu. Allah تعالی Akamjulisha hilo angali akiwa mlima wa *At-Tur*. Allah تعالی Alieleza kuhusu Nafsi Yake Tukufu.

قَالَ فَإِنَّا قَدْ فَتَنَّا قَوْمَكَ مِنْ بَعْدِكَ وَأَضَلَّهُمُ السَّمِيرُ ﴿٨٥﴾

"Mwenyezi Mungu Akasema: Sisi Tumewatia mtihani watu wako baada yako, na Ssamiriyyu amewapoteza." (20:85)

Wafasiri wana maoni tofauti kuhusu ndama huyu kama aligeuka kuwa nyama na damu na akawa na mlio, au aliendelea kuwa dhahabu, bali hewa ilikuwa ikiingia ndani mwake, na kwa hivyo akawa anatoa sauti kama ya ng'ombe. Haya ni maoni ya namna mbili. *Allahu A'alam*. Na inasemwa kwamba, baada ya kutoa sauti, wao walianza kucheza wakiwa wamemzingira na wakatahinika naye. Wakasema, huyu ndiye mola wetu na mola wa Musa عليه السلام, lakini Musa عليه السلام alisahau. Allah تعالی Alisema;

أَفَلَا يَرَوْنَ أَلَّا يَرْجِعُ إِلَيْهِمْ قَوْلًا وَلَا يَمْلِكُ لَهُمْ ضَرْبًا وَلَا نَفْعًا ﴿٨٩﴾

"Je hawakuona kuwa hakuwarudishia neno, wala hakuweza kuwadhuru wala kuwafaa?" (20:89)

Na Alisema Allah تعالی katika Aya hii tukufu;

أَلَمْ يَرَوْا أَنَّهُ لَا يُكَلِّمُهُمْ وَلَا يَهْتَدِيهِمْ سَبِيلًا

"Hivyo, hawakuona kuwa hawasemezi wala hawaongoi njia?"

Allah تعالی Anawakanusha kwa upotevu wao, kwa kumuabudu ndama na kumuacha Muumbaji wa mbingu na ardhi na Mola wa kila kitu na Mfalme wao, kwamba walimshirikisha katika ibada, sanamu la ndama lenye sauti, ambalo haliwasemeshi, wala haliwaongozi kuiendea kheri. Lakini macho yao ya kuiona haki yalifunikwa na upofu wa ujahili na upotevu. Kauli ya Allah تعالی;

وَلَمَّا سَقَطَ فِي أَيْدِيهِمْ

“Na walipojuta”.

Maana yake: Waliyajutia waliyo yafanya.

وَرَأَوْا أَنَّهُمْ قَدْ ضَلُّوا قَالُوا لَئِن لَّمْ يَرْحَمْنَا رَبُّنَا وَيَغْفِرْ لَنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ

الْخَاسِرِينَ ﴿١٤٤﴾

“...na wakaona ya kwamba wamekwishapotea, walisema: Ikiwa Mola wetu Mlezi Hakuturehemu na Akatusamehe, bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa waliokhasiri”.

Kwa maana: Miongoni mwa waliohiliki.

Huku ni kukiri madhambi yao na kurejea kwa Allah تعالیٰ.

* * *

وَلَمَّا رَجَعَ مُوسَىٰ إِلَىٰ قَوْمِهِ غَضْبَانَ أَسِفًا قَالَ بِئْسَمَا خَلَفْتُمُونِي مِنْ بَعْدِي ۗ أَعَجِلْتُمْ أَمْرَ رَبِّكُمْ ۗ وَأَلْقَى الْأَلْوَاحَ وَأَخَذَ بِرَأْسِ أَخِيهِ يَجُرُّهُ إِلَيْهِ ۗ قَالَ ابْنَ أُمَّ إِنَّ الْقَوْمَ اسْتَضَعُّوْنِي وَكَادُوا يَقْتُلُونِي ۖ فَلَا تُشْمِتْ بِيَ الْأَعْدَاءَ وَلَا تَجْعَلْنِي مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿١٥٠﴾ قَالَ رَبِّ آغْفِرْ لِي وَلَا أُخَيِّ وَأَدْخِلْنَا فِي رَحْمَتِكَ ۗ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿١٥١﴾ إِنَّ الَّذِينَ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ سَيِّئًا هُمْ غَضِبَ مِنْ رَبِّهِمْ ۖ وَذِلَّةٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُفْتِرِينَ ﴿١٥٢﴾ وَالَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ ثُمَّ تَابُوا مِنْ بَعْدِهَا وَآمَنُوا إِنَّ رَبَّكَ مِنْ بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٥٣﴾ وَلَمَّا سَكَتَ عَنْ مُوسَى الْغَضِبُ أَخَذَ الْأَلْوَاحَ ۗ وَفِي نُسْحَتِهَا هُدًى وَرَحْمَةٌ ۗ لِلَّذِينَ هُمْ لِرَبِّهِمْ يَرْهَبُونَ ﴿١٥٤﴾

وَلَمَّا رَجَعَ مُوسَىٰ إِلَىٰ قَوْمِهِ غَضْبَانَ أَسِفًا قَالَ بِئْسَمَا خَلَفْتُمُونِي مِنْ بَعْدِي ۗ أَعَجِلْتُمْ أَمْرَ رَبِّكُمْ ۗ وَأَلْقَى الْأَلْوَاحَ وَأَخَذَ بِرَأْسِ أَخِيهِ يَجُرُّهُ إِلَيْهِ ۗ قَالَ ابْنَ أُمَّ إِنَّ الْقَوْمَ اسْتَضَعُّوْنِي وَكَادُوا يَقْتُلُونِي ۖ فَلَا تُشْمِتْ بِيَ الْأَعْدَاءَ وَلَا تَجْعَلْنِي مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿١٥٠﴾ قَالَ رَبِّ آغْفِرْ لِي وَلَا أُخَيِّ وَأَدْخِلْنَا فِي رَحْمَتِكَ ۗ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿١٥١﴾

150. "Na aliporudi Musa kwa watu wake, naye

amekasirika na kuhuzunika, alisema: Ni maovu yaliyoje mlionifanyia nyuma yangu! Je, mmeitangulia Amri ya Mola wenu Mlezi? Na Akaziweka chini zile mbao, na akakikamata kichwa cha ndugu yake akimvutia kwake. (Haarun) akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Hakika hawa watu wamenidharau, na wakakaribia kuniua. Basi Usiwafurahishe maadui juu yangu, wala Usinifanye pamoja na watu madhalimu".

151. "(Musa) akasema: Mola Mlezi wangu! Nisamehe mimi na ndugu yangu, na Ututie katika Rehema Yako. Nawe ni Mwenye Kurehemu Kushinda wote wenye kurehemu".

Allah تعالیٰ Anaeleza kwamba baada ya Musa عليه السلام kurejea kwa watu wake, baada ya mazungumzo na Mola wake, alikuwa amekasirika na kujawa na majuto. Abu Darda'a رضي الله عنه alisema Al-Asaf ni hasira kali.

قَالَ بِئْسَمَا خَلَفْتُمُونِي مِنْ بَعْدِي^ط

"...alisema: Ni maovu yaliyoje mlionifanyia nyuma yangu!"

Anasema, mmefanya uovu kwa kuabudu ndama baada ya kuondoka kwangu na kukuacheni.

أَعَجَلْتُمْ أَمْرَ رَبِّكُمْ^ط

"Je, mmeitangulia Amri ya Mola wenu Mlezi?"

Anasema, mmeharakisha mno kuja kwangu kwenu, ingawa hiyo ni Kudura ya Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى;

وَأَلْفَى الْأَلْوَاخَ وَأَخَذَ بِرَأْسِ أَخِيهِ يَجُرُّهُدَّ إِلَيْهِ^ط

"Na Akaziweka chini zile mbao, na akamkamata kichwa ndugu yake akimvutia kwake".

Hii inathibitisha kuhusu maana ya Hadithi;

«لَيْسَ الْخَبْرُ كَالْمُعَابَنَةِ»

"Khabari si sawa na kuona wazi wazi".¹

Inajidhihirisha kuwa Musa عليه السلام alizitupa mbao kutokana na kughadhabikia kaumu yake. Hii ni kauli ya maulamaa wengi wa *Salaf* na wa baada yao.

Kauli ya Allah تعالى;

وَأَخَذَ بِرَأْسِ أَخِيهِ يَجُرُّهُدَّ إِلَيْهِ^ط

"...na akakikamata kichwa cha ndugu yake akimvutia kwake".

Kwa kukhofia kwamba huenda Harun عليه السلام hakufanya juhudi kubwa kuwakataza dhidi ya uovu walioufanya. Sawa na Allah تعالى Alivyosema katika Aya nyingine;

قَالَ يَبْهَرُونَ مَا مَنَعَكَ إِذْ رَأَيْتَهُمْ ضَلُّوا ﴿١٧١﴾ أَلَّا تَتَّبِعَنِ أَفَعَصَيْتَ أَمْرِي ﴿١٧٢﴾ قَالَ

يَبْتُؤُمْ لَا تَأْخُذْ بِلِخْبَتِي وَلَا بِرَأْسِي^ط إِنِّي خَشِيتُ أَنْ تَقُولَ فَرَّقْتَ بَيْنَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَلَمْ

تَرْقُبْ قَوْلِي ﴿١٧٣﴾

¹ Ahmad 1:271.

“(Musa) akasema: Ewe Harun! Ni nini kilichokuzuia ulipowaona wamepotea, hata usinifuate? Je, umeasi amri yangu? Akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Usinishike ndevu zangu, wala kichwa changu. Kwa hakika niliogopa usije sema: Umewafarikisha Wana wa Israil, na hukungojea kauli yangu”. (20:92-94)

Hapa Allah تعالى Akasema;

ابْنَ أُمَّ إِنَّ الْقَوْمَ اسْتَضَعُّوْنِي وَكَادُوا يَقْتُلُونِي فَلَا تُشْمِتْ بِيَ الْأَعْدَاءَ وَلَا تَجْعَلْنِي مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ

“(Haarun) akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Hakika hawa watu wamenidharau, na wakakaribia kuniua. Basi usiwafurahishe maadui juu yangu, wala usinifanye pamoja na watu madhalimu”.

Maana: “Usiniweke katika daraja iliyo sawa na wao, wala usinichanganye pamoja nao”. Harun عليه السلام alisema, “Ewe mtoto wa mama yangu!” ili awe na huruma na laini zaidi kwake, ingawa wao ni ndugu wa baba mmoja na mama mmoja. Baada ya Musa عليه السلام kuhakikisha kwamba ndugu yake hakuwa na kosa katika hilo;

وَلَقَدْ قَالَ لَهُمْ هَارُونُ مِنْ قَبْلُ يَا قَوْمِ إِنَّمَا فُتِنْتُمْ بِهِ وَإِنَّ رَبَّكُمُ الرَّحْمَنُ فَاتَّبِعُونِي وَأَطِيعُوا أَمْرِيَ

“Na hakika Harun alikwishawaambia kabla yake: Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmetiwa mtihanini tu kwa kitu hiki. Na kwa yakini Mola wenu Mlezi ni Arrahmani, Mwingi wa Rehema. Basi nifuateni mimi, na tiini amri yangu!” (20:90) Hapa ndipo,

قَالَ

“...akasema”. Musa عليه السلام;

قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَلِإِخِي وَأَدْخِلْنَا فِي رَحْمَتِكَ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ

“Mola Mlezi wangu! Nisamehe mimi na ndugu yangu, na Ututie katika Rehema Yako. Nawe ni Mwenye Kurehemu kushinda wote wenye kurehemu”.

Ibn Abu Hatim alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa, Mtume ﷺ alisema;

«يَرْحَمُ اللَّهُ مُوسَىٰ إِذْ أَسْرَأَ بِرَبِّهِ أَنْ يَخَرِّجَهُ رَبُّهُ عَذْرًا وَإِنَّ أَوْلَىٰ لِذَلِكَ لَأَسْرَأُ ۗ فَلَمَّا الْوَالِحُونَ لَقُوا قَالُوا إِنَّمَا أَخْرَجْتَهُ اللَّهُ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ آيَاتِهِ وَلِيُذَكِّرَ الَّذِينَ هُمْ يَخْلَعُونَ ۗ فَلَمَّا أَخْرَجْنَاهُ لِنُوحٍ إِذْ أَوْفَىٰ سُدُورِهِ أَعْزَجَ فُجُورِهِمْ أَسْرَأُ ۗ إِنَّ الْوَاقِعَ لَأَلْوَاخٌ ۗ»

“Allah Amrehemu Musa, kwani anayeona si sawa na anayeelezea. Mola Wake Alimjulisha kuwa kaumu yake walipewa jaribio baada yake, lakini yeye hakuzitupa mbao. Alipowaona kwa macho yake, basi alizitupa mbao”.¹

إِنَّ الَّذِينَ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ سَيِّئَاتِهِمْ ۗ غَضَبٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَذَلَّةٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُفْتَرِينَ ﴿١٥٢﴾ وَالَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ ثُمَّ تَابُوا مِن بَعْدِهَا وَأَمَتُوا إِنَّ رَبَّكَ مِن بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٥٣﴾

152. “Hakika wale waliomuabudu ndama, itawapata ghadhabu ya Mola wao Mlezi na madhila katika maisha ya dunia. Na hivi ndivyo Tunavyowalipa wazushi”.

153. “Na waliotenda maovu, kisha wakatubia baada yake na wakaamini, hapana shaka kuwa Mola Mlezi wako baada ya hayo ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”.

Ama kuhusu ghadhabu iliyowapata Wana wa Israili kutokana na kuabudu ndama ni kwamba, Allah تعالى Hakuwakubalia toba yao, mpaka wakauana wao kwa wao, kama ilivyotangulia katika Surat Al-Baqarah;

فَتُوبُوا إِلَىٰ بَارِيكُمْ فَاقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ عِندَ بَارِيكُمْ ۖ فَتَابَ عَلَيْكُمْ ۗ إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٢٥٤﴾

“Basi tubuni kwa Muumba wenu na ziueni nafsi zenu. Haya ni bora kwenu mbele ya Muumba wenu. Naye Akapokea toba yenu. Hakika Yeye Ndiye Apokeaye toba na Mwenye Kurehemu”. (2:54)

¹ Ibn Majah 2:380.

Akawapa adhabu ya udhalili na fedheha katika maisha ya duniani. Kauli ya Allah تعالى:

وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُفْتَرِينَ

“Na hivi ndivyo Tunavyowalipa wazushi”.

Adhabu inampata mwenye kuzusha bidaa, kwani udhalili wa bidaa na kuukhalifu ujumbe unakuwa umeunganishwa kutoka moyoni mwake mpaka juu ya mabega yake mawili. Sawa na alivyosema Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى, “Udhalili wa bidaa uko juu ya mabega yao, hata kama Watakwenda shoti juu ya baghala au kwenda matiti na farasi wao”. Hivi ndivyo pia alivyosimulia Ayyub As-Sakhtiyani kutoka kwa Abu Qilabah Al-Jarmi, kwamba alisoma Aya hii;

وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُفْتَرِينَ

“Na hivi ndivyo Tunavyowalipa wazushi”.

Akasema, “Wallahi! Hiyo inamhusu kila mzushaji, mpaka Siku ya Kiyama”.¹ Sufyan bin ‘Uyaynah alisema, “Kila sahibu wa bidaa atafedheheshwa”.² Kisha Allah تعالى Aliwafahamisha waja wake na Akawaelekeza kuwa Yeye huwa Anakubali toba za waja wake kutokana na dhambi yoyote, hata kama ni ushirikina, ukafiri, unafiki na kukosa twaa. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alikihitimisha kisa hiki kwa Kauli Yake;

وَالَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ ثُمَّ تَابُوا مِنْ بَعْدِهَا وَءَامَنُوا إِنَّ رَبَّنَا

“Na waliotenda maovu, kisha wakatubia baada yake na wakaamini, hapana shaka kuwa Mola Mlezi wako”.

Maana: Ewe Muhammad ﷺ, ewe Mtume wa Taubah na Nabii wa Rehema.

مِنْ بَعْدِهَا

“...baada ya hayo”. Maana yake: Baada ya kitendo hicho.

لَعَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”.

¹ At-Tabari 13:135.

² At-Tabari 13:136.

Ibn Hatim alisimulia kuwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه aliulizwa juu ya hilo, yaani juu ya mtu anayezini na mwanamke, kisha akamuoa, akasoma Aya hii;

وَالَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ ثُمَّ تَابُوا مِنْ بَعْدِهَا وَآمَنُوا إِنَّ رَبَّكَ مِنْ بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٥٢﴾

“Na waliotenda maovu, kisha wakatubia baada yake na wakaamini, hapana shaka kuwa Mola Mlezi wako baada ya hayo ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”.

'Abdullah رضي الله عنه akaisoma mara kumi na hakuwaamuru hivyo wala hakuwakataza.¹

وَلَمَّا سَكَتَ عَنْ مُوسَى الْغَضَبُ أَخَذَ الْأَلْوَاحَ ط وَفِي نُسْخَتِهَا هُدًى وَرَحْمَةٌ لِلَّذِينَ هُمْ لِرَبِّهِمْ يَرْهَبُونَ ﴿١٥٤﴾

154. “Na ilipomtulia Musa ghadhabu yake, aliziokota zile mbao. Na katika maandiko yake mna uwongofu na rehema kwa wanaomuogopa Mola wao Mlezi”.

Musa عليه السلام Alizichukua Mbao Baada ya Hasira Kutulia.

Allah تعالى Anasema; وَلَمَّا سَكَتَ

“...ilipomtulia”. Maana yake: Ilipopoa.

عَنْ مُوسَى الْغَضَبُ

“Musa ghadhabu yake”. Maana yake: Hasira yake kwa kaumu yake;

أَخَذَ الْأَلْوَاحَ ط

“...aliziokota zile mbao”. Alizozitupa kutokana na ukali wa ghadhabu juu ya wao kuabudu ndama na kwa sababu ya wivu wa Allah تعالى na Ghadhabu Yake kwake.

وَفِي نُسْخَتِهَا هُدًى وَرَحْمَةٌ لِلَّذِينَ هُمْ لِرَبِّهِمْ يَرْهَبُونَ

“Na katika maandiko yake mna uwongofu na rehema kwa wanaomuogopa Mola wao Mlezi”.

¹ Ad-Dur Al-Manthur 2:566.

Wanazuoni wengi wa Tafsiri wanasema: Musa عليه السلام alipozitupa mbao zilivunjika, kisha akazikusanya baada ya hapo. Kwa hivyo, baadhi ya *Salaf* walisema, alikuta katika hizo mbao kuna hidaya na rehema, lakini upambanuzi wa sharia uliondoka. Pia walidai kwamba vipande vya mbao hizo bado vipo na vimehifadhiwa katika hazina za wafalme wa Wana wa Israili, mpaka ifike dola ya Kiislamu. Allah تعالى Ndiye Anayejua zaidi usahihi wa kauli hizi. Hoja isiyopingika ni kuwa zilivunjika pindi alipozitupa, nazo zilitokana na moja wapo ya vito vya Peponi, na Allah تعالى Ameeleza kuwa Alipozichukua baada ya kuzitupa alikuta;

هُدًى وَرَحْمَةً لِّلَّذِينَ هُمْ لِرَبِّهِمْ يَرْهَبُونَ

"...mna uwongofu na rehema kwa wanaomuogopa Mola wao Mlezi".

* * *

وَأَخْتَارَ مُوسَىٰ قَوْمَهُ سَبْعِينَ رَجُلًا لِّمِيقَاتِنَا ۗ فَلَمَّا
 أَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ قَالَ رَبِّ لَوْ شِئْتَ أَهْلَكْتَهُم مِّن قَبْلُ
 وَإِنِّي أَهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ السُّفَهَاءُ مِنَّا إِن هِيَ إِلَّا فِتْنَتُكَ
 تُضِلُّ بِهَا مَن تَشَاءُ وَيَهْدِي مَن تَشَاءُ ۗ أَنْتَ وَلِيُّنَا فَاغْفِرْ
 لَنَا وَارْحَمْنَا ۗ وَأَنْتَ خَيْرُ الْغَافِرِينَ ﴿١٥٥﴾ * وَكَتُبْنَا لَنَا فِي
 هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ إِنَّا هُدُنَا إِلَيْكَ ۗ قَالَ
 عَذَابِي أُصِيبُ بِهِ مَن أَشَاءُ ۗ وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ ۗ
 فَسَأَلْتُمُنِيَ لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَالَّذِينَ هُمْ
 بِآيَاتِنَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٥٦﴾ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ
 الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ
 وَالْإِنْجِيلِ يَا أُولَئِكَ إِنَّهُمْ يُنَبِّئُونَكُم بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَهُم عَنِ الْمُنْكَرِ ۗ يُحِبُّ
 لَهُمُ الطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ الْخَبِيثَاتِ وَيَضَعُ عَنْهُمْ
 إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ ۗ فَاذْكُرُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا بِهِ
 وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَأَتَّبِعُوا النُّورَ الَّذِي أُنزِلَ مَعَهُ ۗ أُولَئِكَ
 هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٥٧﴾ قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ
 اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ
 لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ ۗ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ النَّبِيِّ
 الْأُمِّيِّ الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَكَلِمَاتِهِ وَاتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ
 تَهْتَدُونَ ﴿١٥٨﴾ وَبِئْسَ أَهْلَكُومُ قَوْمُ مُوسَىٰ ۗ إِذْ
 يَدْعُونَ بِأَلْحَقِي
 وَبِهِ يَعْذِرُونَ ﴿١٥٩﴾

وَأَخْتَارَ مُوسَىٰ قَوْمَهُ سَبْعِينَ رَجُلًا
 لِّمِيقَاتِنَا ۗ فَلَمَّا أَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ
 قَالَ رَبِّ لَوْ شِئْتَ أَهْلَكْتَهُم مِّن
 قَبْلُ وَإِنِّي أَهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ
 السُّفَهَاءُ مِنَّا إِن هِيَ إِلَّا فِتْنَتُكَ
 تُضِلُّ بِهَا مَن تَشَاءُ وَيَهْدِي مَن
 تَشَاءُ ۗ أَنْتَ وَلِيُّنَا فَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا
 ۗ وَأَنْتَ خَيْرُ الْغَافِرِينَ ﴿١٥٥﴾ *
 وَكَتُبْنَا لَنَا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا
 حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ إِنَّا هُدُنَا إِلَيْكَ ۗ
 قَالَ عَذَابِي أُصِيبُ بِهِ مَن أَشَاءُ ۗ
 وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ ۗ
 فَسَأَلْتُمُنِيَ لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤْتُونَ
 الزَّكَاةَ وَالَّذِينَ هُمْ بِآيَاتِنَا
 يُؤْمِنُونَ ﴿١٥٦﴾

**155. Na Musa akawateuwa
 watu sabiini katika kaumu
 yake kwa miadi Yetu. Na
 ulipofika mtetemeko
 mkubwa alisema: Ewe
 Mola wangu Mlezi! Ungeli
 taka Ungeli wahiliki wao na
 mimi zamani! Unatuhiliki**

kwa waliyo yafanya wajinga katika sisi? Haya si chochote ila ni mtihani Wako, Umpoteze Umtakaye na Umhidi Umtakaye. Wewe ndiye Rafiki Mlinzi wetu. Basi Tughufirie na Uturehemu. Na Wewe ndiye Mbora wa Kughufiria.

156. Na Utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera. Sisi tumerejea Kwako. (Mwenyezi Mungu) akasema: Adhabu Yangu Nitamsibu nayo Nimitakaye. Na Rehema Yangu imeenea kila kitu. Lakini Nitawaandikia khasa wanao mchamungu, na wanao toa Zaka, na wale ambao wanaziamini Ishara Zetu,

Watu Sabini Kutoka kwa Wana wa Israili Wanakwenda Mahali pa Kukutana na Allah تعالی, Kisha Allah تعالی Akawaangamiza.

'Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما katika kuitafsiri Aya hiyo, alisema, Allah تعالی Alimuamuru Musa عليه السلام achague watu sabini katika kaumu yake, akawateua nao ili wamuombe Mola wake na katika dua hiyo walisema, "Ewe Allah! Tupatie yale ambayo hukumpatia yeyote kabla yetu, wala Hutampatia yeyote baada yetu". Allah تعالی Hakuipenda dua yao, wakapelekewa zilzala. Musa عليه السلام alisema;

رَبِّ لَوْ شِئْتَ أَهْلَكْتَهُمْ مِّن قَبْلِ وَايَّتِي^ط

"Ewe Mola wangu Mlezi! Ungelitaka Ungeliwahiliki wao na mimi zamani!"¹

As-Suddi alisema: Allah تعالی Alimuamuru Musa عليه السلام amjie na Wana wa Israili ili watoe udhuru kwa kuabudu kwao ndama, na Akawapa mahali na muda ulioteuliwa.

وَأَخْتَارَ مُوسَىٰ قَوْمَهُ سَبْعِينَ رَجُلًا لِّمِيقَاتِنَا^ط

"Na Musa akawateua watu sabini katika kaumu yake". Baada ya kuwateua alikwenda nao ili wakatoe udhuru wao. Walipofika mahali hapo, walisema;

لَن نُّؤْمِنَ لَكَ

"Hatutakuamini". Ewe Musa عليه السلام.

¹ At-Tabari 13:141.

حَتَّىٰ تَرَىٰ اللَّهَ جَهْرَةً

“...mpaka tumuone Mwenyezi Mungu waziwazi”. Kwani wewe ulikwisha - zungumza Naye, basi tuoneshe Yeye.

فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ

“Wakapigwa na radi”. (4:153) Wakafa, kisha Musa عليه السلام akasimama huku akilia na kumuomba Mola wake, akisema, “Mola wangu, nitawaambia nini Wana wa Israili pindi nitakapokutana nao ilihali wateule wao wameangamia.

رَبِّ لَوْ شِئْتَ أَهْلَكْتَهُم مِّن قَبْلُ وَإِنِّي

“Ungelitaka Ungeliwahiliki wao na mimi zamani!”.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema, “Musa عليه السلام aliteua watu sabini katika Wana wa Israili walio bora zaidi miongoni mwao. Akasema, “Nendeni kwa Allah تعالى na mtubu juu ya mliyoyafanya na muwaombe toba watu wenu mliowaacha nyuma yenu. Fungeni, mjitwaharishe na mazitwaharishe nguo zenu”. Akaenda nao mpaka mlima wa Sinai kwa ajili ya mahali na wakati Alioupanga Mola Wake, na alikuwa akienda pale kwa Idhini Yake na kwa Elimu ya Allah تعالى. Katika mliyoambiwa, wale watu sabini wakamuambia Musa عليه السلام, “Omba sisi tuyasikie mazungumzo ya Allah تعالى”. Akasema, “Nitafanya hivyo”. Musa عليه السلام alipousogelea mlima, ukawa wote umefunikwa na nguzo za mawingu. Musa عليه السلام akasogea na akaingia ndani ya mawingu hayo, akawaambia watu hao, “Sogeeni”. Ilikuwa wakati Musa عليه السلام alipokuwa akizungumza na Allah تعالى, paji la uso wake lilikuwa likipatwa na nuru ing'aayo sana, kiasi mwanadamu hawezi kumtazama. Basi kukawekwa kizuizi baina yake, watu nao wakasogea, mpaka walipoingia ndani ya mawingu, waliporomoka kusujudu na wakamsikia Allah تعالى Akimuamuru Musa عليه السلام na kumuonya, fanya hiki, usifanye kile. Allah تعالى Alipomaliza jambo hilo, mawingu yaliondoka, wakamuendea na kumuambia: “Musa! Hatutakuamini mpaka tumuone Allah waziwazi.”. Wakapatwa na radi, roho zao zikachukuliwa, na wote wakafariki. Musa akasimama kumuomba Mola wake na kumsihi;

رَبِّ لَوْ شِئْتَ أَهْلَكْتَهُم مِّن قَبْلُ وَإِنِّي

“Ewe Mola wangu Mlezi! Ungelitaka Ungeliwahiliki wao na mimi zamani!”

¹ At-Tabari 13:130.

Maana yake: "Wamefanya upumbavu. Vipi unamuangamiza anayenifuata mimi miongoni mwa Wana wa Israili?"¹ Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, Qatadah na Mujahid na Ibn Jarir رحمه الله تعالى walisema, 'hawa waliadhibiwa kwa zilizala kwa sababu hawakuwakataza kaumu yao dhidi ya kuabudu ndama"². Kauli hii inapewa nguvu na kauli ya Musa عليه السلام;

أَتَيْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ السُّفَهَاءُ مِنَّا^ط

"Unatuhiliki kwa waliyoyafanya wajinga katika sisi?" Na akasema;

إِنَّ هِيَ إِلَّا فِتْنَتُكَ

"Haya si chochote ila ni mtihani wako". Maana yake: Ni mtihani na majaribio Yako. Maoni hayo yalisemwa na Ibn 'Abbas, Sa'id bin Jubayr, Abu Al-'Aliyyah, Ar-Rabi bin Anas na maulamaa wengine katika *Salaf* na waliokuja nyuma رضي الله عنهم. Wala hakuna maana nyingine zaidi ya hiyo, ambapo Musa عليه السلام anasema, "Hakuna amri isipokuwa ya Kwako, wala hakuna hukumu isipokuwa ya Kwako. Ukitakacho huwa, Unamuacha apotee Umtakaye, na Unamuongoza Umtakaye. Wala hakuna wa kumuongoza Uliyemuacha apotee, wala wa kumpoteza Uliyemuongoza. Wala hapana wa kukitoa Ulichokizuia, wala wa kukizuilia Ulichokitua. Ufalme wote na Hukumu yote ipo Kwako. Ni vyako Wewe, Kuumba na Kutoa Amri". Kauli ya Allah تعالى;

أَنْتَ وَلِيُّنَا فَآغْفِرْ لَنَا وَأَرْحَمْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الْغَافِرِينَ^ط

"Wewe Ndiye Rafiki Mlinzi wetu. Basi tughufirie na Uturehemu. Na Wewe Ndiye Mbora wa Kughufiria".

Maghfira ni kusitiriwa na kuachwa Kuadhibiwa kwa sababu ya madhambi. Rehema inapokutana na maghfira (kama ilivyo katika Dua ya Musa عليه السلام), inajumuisha matumaini kuwa mtu asitumbukie katika kitendo hicho tena katika mustakabali.

وَأَنْتَ خَيْرُ الْغَافِرِينَ

"Na Utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera".

Maana yake: Hakuna wa Kughufiria madhambi, isipokuwa Wewe.

¹ At-Tabari 13:140.

² At-Tabari 13:143-144.

وَأَكْتُمِبَ لَنَا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ

“Na Utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera”.

Sehemu ya kwanza ya dua ya Musa عليه السلام ilikuwa ni kwa ajili ya kukiondoa kinachokimbiwa, na sehemu hii ni maombi ya kinachotafutwa.

وَأَكْتُمِبَ لَنَا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ

“Na Utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera”. Kwa maana: Tuwajibishie na Utupatie mema duniani na Akhera. Tafsiri ya *Al-Hasanah* ilitangulia katika *Suurat Al-Baqarah*.¹

إِنَّا هُدْنَا إِلَيْكَ

“Sisi tumerejea Kwako”. Kwa maana: Tumetubu, tumerudi na tumerejea Kwako. Hayo aliyasema Ibn ‘Abbas , Sa’id bin Jubayr, Abu Al-‘Aliyah, Adh-Dhahhak, Ibrahim At-Taymi, As-Suddi, Qatadah na wengine رضي الله عنهم².

قَالَ عَدَالِيٌّ أُصِيبَ بِهِ مِنْ أَسَاءٍ^ط وَرَحْمَتِي وَسَعَتْ كُلَّ شَيْءٍ^ع فَسَأَكْتُمِبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ
وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَالَّذِينَ هُمْ بِقَائِمَتِنَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٦٦﴾

(Mwenyezi Mungu) Akasema: Adhabu Yangu Nitamsibu nayo Nimtakaye. Na Rehema Yangu imeenea kila kitu. Lakini Nitawaandikia khasa wanaomchamungu, na wanaotoa Zaka, na wale ambao wanaziamini ishara Zetu.” (7:156)

Rehema ya Allah تعالى ni kwa Wenye Taqwa na Wanaoamini Aya za Allah تعالى na Mitume

Allah تعالى Anajibu Nafsi Yake, kwa Kauli Yake تعالى:

إِنْ هِيَ إِلَّا فِتْنَتُكَ

“Haya si chochote ila ni mtihani wako”. (7:55) Alisema;

عَدَالِيٌّ أُصِيبَ بِهِ مِنْ أَسَاءٍ^ط وَرَحْمَتِي وَسَعَتْ كُلَّ شَيْءٍ^ع

“Adhabu Yangu Nitamsibu nayo Nimtakaye.”.

¹ Angalia Tafsir ya Surat Al-Baqarah 2:200-202.

² At-Tabari 13:154-155.

Maana: Ninafanya na Kuhukumu Nitakavyo. Nami Nina Hekima na Uadilifu katika yote hayo. Ametakasika Allah تعالى, hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye. Kauli ya Allah;

وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ

“Na Rehema Yangu imeenea kila kitu”.

Ina wasaa mkubwa na ni yenye kuenea. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى Akipasha khabari za Malaika wenye kuichukua 'Arshi na wale walioizunguka, kuwa wanasema:

رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا

“Mola wetu Mlezi! Umekienea kila kitu kwa Rehema na Ujuzi”.

(40:7)

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Jundab, ambaye ni mwana wa 'Abdullah Al-Bajali kuwa alisema, alikuja bedui mmoja na akamkalisha mnyama wake kisha akamfunga, halafu akasali nyuma ya Mtume ﷺ. Baada ya Mtume ﷺ kukamilisha Sala, yule mtu alikwenda kwa mnyama wake, akamfungua kamba yake na akampanda, kisha akanadi, “Ewe Allah! Shusha Rehema kwangu na kwa Muhammad, wala Usimshirikishe yeyote katika rehema Utakazo-tupatia”. Mtume ﷺ akasema;

«أَتَقُولُونَ هَذَا أَضَلُّ أَمْ بَعِيرُهُ أَلَمْ تَسْمَعُوا مَا قَالَ؟»

“Mnasemaje? Mtu huyu ni mpotevu zaidi ama ngamia wake? Hamkuyasikia aliyoyasema mtu huyu?”

Wakasema, “Ndiyo”.

«لَقَدْ حَظَرْتُ رَحْمَةً وَاسِعَةً إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ خَلَقَ مِائَةَ رَحْمَةٍ فَأَنْزَلَ رَحْمَةً يَتَعَاطَفُ بِهَا الْخَلْقُ جِئَهَا وَإِنْسُهَا وَبَهَائِمُهَا وَأَخْرَعَهُ عِنْدَهُ تَسْمَعًا وَتَسْمِعِينَ رَحْمَةً أَتَقُولُونَ هُوَ أَضَلُّ أَمْ بَعِيرُهُ؟»

“(Bedui) umeiwekea mpaka rehema pana, Hakika. Allah تعالى Aliumba rehema mia moja. Akashusha rehema moja ambayo wanahurumiana viumbe wote, majini, wanadamu na bahaimu wao. Na Amebakisha kwake rehema tisini na tisa. Mnasemaje?, Yeye ndiye mpotevu zaidi ama ngamia wake?”

Aliinukuu Ahmad¹ na Abu Dawud². Imamu Ahmad alinukuu tena kutoka kwa Salman رضي الله عنه، kuwa Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ لِلَّهِ عَزَّ وَجَلَّ مِائَةَ رَحْمَةٍ فَمِنْهَا رَحْمَةٌ يَتَرَاخَمُ بِهَا الْخَلْقُ وَبِهَا تُعْطَفُ الْوُحُوشُ عَلَى أَوْلَادِهَا وَأُخْرَى تَسْعَةٌ وَتَسْعِينَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Allah تعالى Ana rehema mia moja, miongoni mwazo kuna rehema moja ambayo viumbe wanahurumiana kwayo, na kwa hiyo hiyo, wanyama wanawaonea huruma watoto wao. Na Yeye Akabakia na rehema tisini na tisa kwa ajili ya Siku ya Kiyama”.³

Muslim peke yake ndiye aliyeinukuu⁴. Kauli ya Allah تعالى:

فَسَاكُنِيَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ

“Lakini Nitawaandikia khasa wanaomchamungu”.

Nitawajibisha kuwa rehema ziwafikie wao kama fadhila Zangu kwao na ihsani Yangu kwao. Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

كَتَبَ عَلَى نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ

“Yeye Amejilazimisha Nafsi Yake Kurehemu”. (6:12)

Kauli ya Allah تعالى:

لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ

“...wanaomchamungu”. Kwa maana: Nitazijaalia kwa wenye sifa hizo. Nao ni umma wa Muhammad ﷺ.

لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ

“...wanaomchamungu”. Kwa maana: Wanaojiepusha na ushirikina na madhambi makubwa. Kauli ya Allah تعالى:

وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ

“...na wanaotoa Zaka”. Ilisemwa, kuzitakasa nafsi. Na ilisemwa ni kuzitakasa mali. Pia yanaweza kukusanywa yote mawili, kwani Aya hiyo ilishushwa Makkah (kabla viwango vya Zakah havijakuwepo).

¹ Ahmad 4:312.

² Abu Dawud 5:197.

³ Ahmad 5:49.

⁴ Muslim 4:2108.

وَالَّذِينَ هُمْ بِآيَاتِنَا يُؤْمِنُونَ

"...na wale ambao wanaziamini ishara Zetu".

Maana yake: Wanazisadiki.

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ
وَالْإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُمْ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ الطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ
عَلَيْهِمُ الْخَبَائِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ ۗ فَالَّذِينَ ءَامَنُوا
بِهِ وَعَزَّوهُ وَنَصَرُوهُ وَأَتَّبَعُوا الْنُّورَ الَّذِي أُنزِلَ مَعَهُ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٥٧﴾

157. Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiyesoma wala kuandika, wanayemkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anayewaamrisha mema na anayewakanya maovu, na anawahalalishia vizuri na anawaharamishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao. Basi wale waliomuamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye – hao ndio wenye kufanikiwa.

Wasifu wa Mtume ﷺ.

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ
وَالْإِنْجِيلِ

"Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiyesoma wala kuandika, wanayemkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili".

Hizi ndio sifa za Mtume Muhammad ﷺ zilizomo ndani ya Vitabu vya Mitume waliomtangulia, ambao waliwapa bishara umma wao kuhusu kutumwa kwake na wakawaamuru wamfuata. Sifa zake ziliendelea kuwemo katika vitabu vyao na zikajulikana kwa wanazuoni wao na watawa wao. Ni sawa na alivyosimulia Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Swakhr Al-'Uqayl ambaye alisema: "Mmoja wapo katika mabedui alinieleza, "Nilimleta Al-Madinah, ngamia mwenye maziwa zama za uhai wa Mtume ﷺ. Baada ya kumuuzua nikajisemea mwenyewe kuwa nitakutana na mtu huyu ili nimsikie anachokisema. Nikakutana naye

akiwa baina ya Abubakr na 'Umar رضي الله عنهما wakitembea, nikawafuata, mpaka wakamuendea Myahudi aliyekuwa amefunua Taurati akiisoma. Alikuwa na mwanaye aliyekuwa akichungulia mauti ambaye alikuwa mmoja wapo wa vijana wazuri sana. Mtume ﷺ alisema;

«أَنْشُدُكَ بِالَّذِي أَنْزَلَ التَّوْرَةَ هَلْ تَجِدُ فِي كِتَابِكَ هَذَا صِفَتِي وَمَخْرَجِي؟»

“Nakuuliza kwa Yule Aliyeiteremsha Tawrat. Je, katika Kitabu chako hiki hukuti sifa zangu na ujio wangu?”

Akatikisa kuashiria, “Hapana”. Mwanaye akasema: “Ndiyo, naapa kwa Aliyeiteremsha Taurati, sifa huwa tunazikuta Kitabuni mwetu, sifa zako na ujio wako, nami ninatoa shahada kuwa hapana wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba wewe ni Mtume ﷺ”. Mtume ﷺ akasema;

«أَقِيمُوا الْيَهُودِيَّ عَنْ أَحْبَابِكُمْ»

“Mzuieni Myahudi (huyu) dhidi ya (kumshughulikia) ndugu yenu (huyu mtoto)”.

Baadaye Mtume ﷺ mwenyewe alimshughulikia kijana huyo na akaongoza Sala ya Jeneza¹. Hadithi hii ni *Jayyid*, pia ni yenye nguvu, tena inathibiti ndani ya *Sahih* ikisimuliwa na Anas رضي الله عنه².

Ibn Jariri رحمه الله تعالى Anasimulia kuwa 'Atwaa bin Yasaar alisema: Nilikutana na 'Abdullah bin 'Amri, nikamuambia: “Nieleze juu ya sifa za Mtume ﷺ zilizomo ndani ya Taurati”. Akasema: Ndiyo, naapa kwa Allah! Amesifiwa ndani ya Taurati sawa na ilivyomsifia Qur'an.

يَأَيُّهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَهِيدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿٣٤﴾

“Ewe Nabii! Hakika Sisi Tumekutuma uwe shahidi na mbashiri na Mwonyaji”. (33:45)

Ili awe kimbilio la walio *ummi*. Nimekuita ni mja na Mjumbe Wangu. Nimekuita *Al-Mutawakkil* (mwenye kumtawakali Allah تعالى), si mgumu wala mkali, wala Allah تعالى hatamchukua roho yake, isipokuwa mpaka azinyooshe mila zilizopinda baada ya wao kutamka kalima ya *Laa ilaaha illallah* – Hapana wa

¹ Ahmad 5:411.

² Fat'hul A-Bari 3:259.

haki kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى. Kupitia kwake, Allah تعالى Atafungua nyoyo zilizopigwa muhuri, masikio yasiyosikia na macho yaliyopofuka". Atwaa akaendelea kusema: "Halafu nikakutana na Ka'b, na nikamuuliza juu ya hilo, naye hakutofautiana naye".¹ Al-Bukhari aliandika katika *Sahih* yake, na baada ya maneno, "...si mgumu wala mkali, wala si mpigaji kelele za kipuuzi masokoni, wala halipi baya kwa ubaya, bali Husamehe na kustahamili"².

Kisha akataja Hadithi ya Ibn 'Amr. Baada ya hapo akasema: "Ilikuwa ni Desturi katika mazungumzo ya *Salaf* kueleza yaliyomo ndani ya Vitabu vya watu wa Vitabu kama ilivyo Taurati. Kuna Hadithi nyingine zilizosimuliwa yanayoshabihiana na haya. *Allah Aalam*.

Kauli ya Allah تعالى:

يَأْمُرُهُم بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ

"...anayewaamrisha mema na anayewakanya maovu".

Hizi ni sifa za Mtume ﷺ zilizopo ndani ya Vitabu Vitukufu, na hivyo ndivyo alivyokuwa Mtume ﷺ, hakuamuru isipokuwa la kheri, wala hakukataza, bali dhidi ya lililo la shari. Ni sawa na alivyosema "Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه, "Pindi utakaposikia Kauli ya Allah تعالى:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ آمَنُوا

"Basi wale waliomuamini yeye".

Basi tega sikio lako vyema, kwani hiyo huwa, ama ni kheri unayoamriwa, ama ni shari unayokatazwa. Lililo muhimu na kubwa zaidi ni amri ya kumpwekesha Yeye katika ibada, pasi na kumshirikisha na kuwakataza waja Wake dhidi ya aliye ghairi Yake. Ni sawa na alivyowatuma Mitume Wake wote. Aliwaambia:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الصُّلُوفَ

"Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani". (16:36)

Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 13:164.

² Fat'hul Al-Bari 4:402.

وَيُحِلُّ لَهُمُ الطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ الْخَبِيثَاتِ

“...na anawahalalishia vizuri na anawaharamishia viovu”.

Maana yake: Anawahalalishia yale waliyojiharamishia wao wenyewe miongoni mwa *Al-Bahair, Sawaa-ib, Waswaa-il, Al-Haam* na yasiyokuwa hayo ambayo yalizidhikisha nafsi zao. Tena Anawaharamishia vilivyo vichafu. ‘Ali bin Abu Twalhah anasimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Kama vile nyama ya nguruwe, riba na mambo mengine ya haramu waliyokuwa wakijihalalishia miongoni mwa vyakula alivyoviharamisha Allah تعالى¹.”

وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ

“...na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao”.

Inajulisha kuwa Muhammad ﷺ alikuja kusahalisha na alikuja na Dini ya wepesi.

«بُيِّنْتُ بِالْحَنِيفِيَّةِ السُّمْحَةِ»

“Nimetumwa na muongozo wa maisha ulio mwepesi - Hanifiyyah.”²

Mtume ﷺ aliwaambia maamiri wake, Mu’adh bin Jabal na Abu Musa Al-Ash-‘ari رضي الله عنهما wakati alipowatuma kwenda Yemen.

«بَشْرًا وَلَا تُنْفَرًا وَبَسْرًا وَلَا تُعْسَرًا وَتَطَاوَعًا وَلَا تَخْتِلِفَانَا»

“Toeni bishara, wala msiwafanye watu wakimbie, fanyeni wepesi wala msitie uzito, muwe watiifu baina yenu (nyinyi wawili) wala msikhitalafiane.”³

Sahaba wa Mtume ﷺ, Abu Barzah Al-Aslami رضي الله عنه alisema: “Mimi nimesuhubiana na Mtume ﷺ na nimeona namna alivyokuwa sahali. Umma uliotangulia ulikuwa ukipata dhiki kutokana na sheria zao. Allah تعالى Akaleta ukunjufu katika mambo ya Umma huu na Akausahalishia.” Kwa minajili hii, Mtume ﷺ alisema;

¹ At-Tabari 13:166.

² Ahmad 5:266 na 6:116.

³ Fat’hul Al-Bari 5:188.

«إِنَّ اللَّهَ تَجَاوَزَ لِأُمَّتِي مَا حَدَّثَتْ بِهِ أَنْفُسَهَا مَا لَمْ تَقُلْ أَوْ تَعْمَلْ»

“Allah تعالى Ameusamehe umma wangu kwa yale yanayoingia nafsini mwao maadam hawayasemi wala kuyafanya”.¹

Pia alisema;

«رُفِعَ عَنِ أُمَّتِي الْخَطَأُ وَالنَّسِيَانُ وَمَا اسْتُكْرِمُوا عَلَيْهِ»

“Umma wangu umesamehewa makosa yasiyo ya kutekeleza, ya usahaulifu na waliyolazimishwa kuyafanya”.²

Hiyo ndiyo sababu kwamba Allah تعالى Ameuelekeza Umma huu useme;

رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِنْ كُنَّا نَسِينَا أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِنَا رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ^٣ وَاعْفُ عَنَّا وَاعْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا أَنْتَ مَوْلَانَا فَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٨٦﴾

“Mola wetu Mlezi! Usituchukulie tukisahau au tukikosea, Mola wetu Mlezi! Usitubebeshe mzigo kama uliowabebesha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu Mlezi Usitutwike tusingoyaweza, na Utusamehe, na Utughufirie na Uturehemu. Wewe Ndiye Mlinzi wetu. Basi Tupe ushindi tuwashinde kaumu ya makafiri”. (2:286)

Imethibiti ndani ya *Sahih Muslim* kuwa [Mtume ﷺ alisema], baada ya kila mojawapo ya dua hizi, Allah تعالى Alisema: “Nimepokea, Nimepokea dua yenu”. Kauli ya Allah تعالى;

فَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِهِمْ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ

“Basi wale waliomuamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia”.

Maana yake: Wamemtukuza na kumheshimu Mtume Muhammad ﷺ,

وَاتَّبَعُوا النُّورَ الَّذِي أُنزِلَ مَعَهُ^٤

“...na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye”.

Inamaanisha: Qur'an na Wahyi (Sunnah) aliokuja nao na kuwafikishia watu.

¹ Fat'hul Al-Bari 9:300.

² Ibn Majah 1:659.

أُولَئِكَ هُمُ الْمَفْلُحُونَ

“...hao ndio wenye kufanikiwa”. Duniani na Akhera.

قُلْ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ النَّبِيِّ الْأُمِّيِّ الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ
وَكَالِمَاتِهِ وَأَتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥٨﴾

158. Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliyetumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana mola ila Yeye Anayehuisa na Anayefisha. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake asiyejua kusoma na kuandika, ambaye Anamuamini Mwenyezi Mungu na Maneno Yake. Na mfuateni yeye ili mpate kuongoka”.

Utume wa Muhammad ﷺ ni wa Ulimwengu Mzima.

Allah تعالیٰ Anamuambia Nabii na Mtume Wake;

قُلْ

“Sema”. Ewe Muhammad ﷺ.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ

“Enyi watu”. Hapa wanaambiwa watu wote, wekundu na weusi, Waarabu na wasio Waarabu.

إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote”.

Aya hii inataja ubora na utukufu wa Mtume ﷺ, kuwa yeye ndiye Nabii wa mwisho, na kuwa alitumwa kwa watu wote. Sawa na Kauli nyingine ya Allah

تعالى:

قُلِ اللَّهُ شَهِيدٌ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ وَأُوحِيَ إِلَيَّ هَذَا الْقُرْآنُ لِأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

“Sema: Mwenyezi Mungu. Yeye Ndiye Shahidi baina yangu na nyinyi. Na nimefunuliwa Qur’an hii ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia”. (6:19) Na;

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ قَالَ نَارُ مَوْعِدُهُ^ط

“...na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao”. (11:17) Na;

وَقُلْ لِلَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْأُمِّيِّينَ ءَأَسْلَمْتُمْ^ط فَإِنْ أَسْلَمُوا فَقَدِ اهْتَدَوْا^ط وَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ^ط

“Na waambiwe waliopewa Kitabu na wasio na kisomo: Je! Mmesilimu? Wakasilimu basi wameongoka. Na wakikengeuka basi juu yako ni kufikisha ujumbe tu”. (3:20)

Kuna Aya nyingi kuhusu mada hii. Vile vile Hadithi juu ya hilo ni nyingi zisizohesabika. Inaeleweka vyema katika Uislamu kuwa Mtume ﷺ alitumwa kwa watu wote. Al-Bukhari alinukuu katika kuitafsiri aya hii, Hadithi ya Abu Ad-Darda'a رضي الله عنه ambaye alisema, “Kulikuwa na mazungumzo baina ya Abubakr رضي الله عنه na 'Umar رضي الله عنه, basi Abubakr رضي الله عنه akamuudhi 'Umar رضي الله عنه ambaye aliondoka akiwa na hasira. Abubakr رضي الله عنه akamfuata kumuomba msamaha. 'Umar رضي الله عنه hakumkubalia Abubakr رضي الله عنه, mpaka akafika nyumbani kwake na kufunga mlango wake. Abubakr رضي الله عنه akaenda kwa Mtume ﷺ. Abu Adarda'a رضي الله عنه akasema “Na sisi tulikuwa na Mtume ﷺ wakati huo”. Mtume ﷺ akasema;

«أَمَا صَاحِبُكُمْ هَذَا فَقَدْ غَامَرَ»

“Sahibu yenu huyu amemfanya mtu akasirike”.

Maana: Aghadhibike na awe na kinyongo. 'Umar رضي الله عنه akajutia aliyoyafanya. Alikwenda kwa Mtume ﷺ, akamsalimu na kukaa mkabala naye, na Akamjulisha Mtume ﷺ khabari hiyo. Abu Ad-Darda'a رضي الله عنه anasema, “Mtume akakasirika”. Abubakr رضي الله عنه akawa anasema, “Wallahi! Ewe Mjumbe wa Allah! Mimi ndiye niliyekuwa dhalimu”. Mtume ﷺ alisema;

«هَلْ أَنْتُمْ تَارِكُو لِي صَاحِبِي؟ إِنْ قُلْتُ: يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنْ رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَوْبِعَا قُلْتُمْ: كَذَبْتَ وَقَالَ أَبُو بَكْرٍ: صَدَقْتَ»

“Muacheni rafiki yangu msimsumbue! Mimi Nilisema: “Enyi watu! Mimi ni Mjumbe wa Allah kwenu nyote”. Mkasema, “Umeongopa”,

lakini Abubakr alisema, "Umesema kweli". Al-Bukhari peke yake aliinukuu Hadithi hii.¹

Imamu Ahmad alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema;

«أُعْطِيتُ حَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ نَبِيٌّ قَبْلِي وَلَا أَقُولُهُ فَخَرًّا بُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ كَأَقْفَةِ الْأَخْمَرِ
وَالْأَسْوَدِ وَنُصِرْتُ بِالرُّغْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ وَأَجِلْتُ لِي الْغَنَائِمُ وَلَمْ تَجَلْ لِأَحَدٍ قَبْلِي
وَجُعِلَتْ لِي الْأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهْرًا وَأُعْطِيتُ الشَّفَاعَةَ فَأَخَّرْتَهَا لِأُمَّتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ
فَهِيَ لِمَنْ لَا يُشْرِكُ بِاللَّهِ شَيْئًا»

"Nimepewa mambo matano ambayo hakupewa Nabii yeyote kabla yangu. Wala siyasemi haya kwa ufakhari. Nimetumwa kwa watu wote, wekundu na weusi. Na Amenipa ushindi kwa njia ya khofu (kuwakhofisha maadui) kwa masafa ya mwendo wa mwezi mmoja. Nimehalalishiwa ghanima, wala hakuhalalishiwa yeyote kabla yangu. Ardhi yote imejaaliwa kuwa mahala pa kusali na twahara. Na Nimepewa nafasi ya shufaa, nikaiaakhirisha kwa ajili ya umma wangu mpaka Siku ya Kiyama. Hiyo ni kwa ajili ya asiyemshirikisha Allah na chochote".²

Isnadi yake ni nzuri lakini Sahih Mbili hazikuinukuu. Kauli ya Allah تعالى:

الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ

"Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana mola ila Yeye Anayehuishia na Anayefisha".

Hizi ni sifa za Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى, "Mtume" Maana: Aliyenituma mimi, Ndiye Muumbaji wa kila kitu, Mola wao na Mfalme wao Ambaye Mkononi Mwake ndipo penye Udhhibiti, Uhai na kifo, na Uamuzi ni Wake. Kauli ya Allah

تعالى:

فَقَامُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ النَّبِيِّ الْأُمِّيِّ

"Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake asiyejua kusoma na kuandika".

¹ Fat'hul Al-Bari 8:153.

² Ahmad 1:301

Aliwaeleza kuwa yeye ni Mtume kwao, kisha akawaamuru wamfuate na kumuamini yeye.

النَّبِيِّ الْأَتِيِّ

“...asiyejua kusoma na kuandika”.

Maana yake: Ambaye mliahidiwa na mkapewa bishara kumhusu katika Vitabu vilivyotangulia na yeye ana sifa zilizo katika vitabu vyao. Kwa hivyo, alisema, *“Mtume Wake asiyejua kusoma na kuandika”*. Kauli ya Allah تعالى;

الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَكَلِمَاتِهِ

“...ambaye Anamuamini Mwenyezi Mungu na Maneno Yake”. Kwa maana amali zake zinasadikisha maneno yake, na anaamini alichoteremshiwa kutoka kwa Mola wake.

وَاتَّبَعُوهُ

“Na mfuateni yeye”. Kwa maana: Piteni njia yake.

لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

“...ili mpate kuongoka”. Kwa maana: Katika njia iliyonyooka.

وَمِن قَوْمِ مُوسَىٰ أُمَّةٌ يَهْتَدُونَ بِالْحَقِّ وَيُبْغِضُونَ يَجْعَلُونَ

“Na katika kaumu ya Musa lipo kundi linaowaongoa watu kwa haki na kwa haki wanafanya uadilifu”. (7:159)

Allah تعالى Anaeleza juu ya Wana wa Israili, kuwa miongoni mwao wapo wanaoifuata haki na kuhukumu kwa kuitumia, sawa na Kauli ya Allah تعالى;

مِنَ أَهْلِ الْكِتَابِ أُمَّةٌ قَائِمَةٌ يَتْلُونَ آيَاتِ اللَّهِ آنَاءَ اللَّيْلِ وَهُمْ يَسْجُدُونَ

“Miongoni mwa Watu wa Kitabu wamo watu waliosimama barabara, wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku, na pia wanasujudu”. (3:113) Na;

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِمْ خَشِعِينَ لِلَّهِ لَا يَشْتُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۗ أُولَٰئِكَ لَئِنْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ

الْحِسَابِ ﴿١١٣﴾

“Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu wapo wanaomuamini Mwenyezi Mungu na yaliyoteremshwa kwenu na yaliyoteremshwa kwao, wakimnyenyekea Mwenyezi Mungu. Hawabadili Aya za Mwenyezi Mungu kwa thamani duni. Hao wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhesabu”. (3:199) na;

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِهِ هُمْ بِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿١٩٩﴾ وَإِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ قَالُوا ءَأَمَّا
بِهِمُ إِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلِهِ مُسْلِمِينَ ﴿٢٠٠﴾ أُولَٰئِكَ يُؤْتَوْنَ أَجْرَهُمْ مَرَّتَيْنِ
بِمَا صَبَرُوا

“Wale Tuliowapa Kitabu kabla yake wanakiamini hiki. Na wanaposomewa wanasema: Tunaiamini. Hakika hii ni Haki inayotoka kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa ni Waislamu, tulionyenyekea. Basi hao watapewa ujira wao mara mbili kwa walivyovumilia”. (28:52-54) Na;

إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِنْ قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا ﴿٢٠١﴾ وَيَقُولُونَ
سُبْحَانَ رَبِّنَا إِنْ كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿٢٠٢﴾ وَيَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ يَبْكُونَ وَيَزِيدُهُمْ
خُشُوعًا ﴿٢٠٣﴾

“Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake, wanaposomewa Qur’an hii, huanguka kifudifudi wanasujudu. Na Wanasema: Subhana Rabbina, Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika ahadi ya Mola wetu Mlezi lazima itimizwe! Na huanguka kifudifudi na huku wanalia, na inawazidishia unyenyekevu”. (17:107-109)

* * *

وَقَطَعْنَاهُمْ أَثْنَى عَشْرَةَ أَسْبَاطًا أُمَمًا ۗ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ
 إِذِ اسْتَسْقَنَهُ قَوْمُهُ رَبِّ أَنْ أَضْرِبَ بِعَصَاكَ الْحَجَرَ ۗ
 فَانْبَجَسَتْ مِنْهُ أَثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا ۗ قَدْ عَلِمَ كُلُّ أُنَاسٍ
 مَّشْرِبُهُمْ ۗ وَظَلَّلْنَا عَلَيْهِمُ الْغَمَمَ ۗ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْهِمُ الْمَنَّاءَ
 وَالسَّلْوَىٰ ۗ كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ ۗ وَمَا ظَلَمُونَا
 وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١٦٠﴾ وَإِذْ قِيلَ لَهُمْ
 اسْكُنُوا هَذِهِ الْقَرْيَةَ وَكُلُوا مِنْهَا حَيْثُ شِئْتُمْ وَقُولُوا
 حِطَّةٌ وَادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا نَفَعْنَا لَكُمْ حَطِيئَتِكُمْ ۗ
 سَنَزِيدُ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٦١﴾ فَبَدَّلَ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ
 قَوْلًا غَيْرَ الَّذِي قِيلَ لَهُمْ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِجْرًا مِنْ
 السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَظْلِمُونَ ﴿١٦٢﴾ وَسَأَلْتَهُمْ عَنِ
 الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ حَاضِرَةَ الْبَحْرِ إِذْ يَعْدُونَ فِي
 السَّبْتِ إِذْ تَأْتِيهِمْ حِيتَانُهُمْ يَوْمَ سَبْتِهِمْ شُرْعًا وَيَوْمَ لَا
 يَسْتَبِثُونَ ۗ لَا تَأْتِيهِمْ ۗ كَذَلِكَ نَبْلُوهُمْ بِمَا كَانُوا
 يَفْسُقُونَ ﴿١٦٣﴾

وَقَطَعْنَاهُمْ أَثْنَى عَشْرَةَ أَسْبَاطًا
 أُمَمًا ۗ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ إِذِ
 اسْتَسْقَنَهُ قَوْمُهُ رَبِّ أَنْ أَضْرِبَ
 بِعَصَاكَ الْحَجَرَ ۗ فَانْبَجَسَتْ مِنْهُ
 أَثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا ۗ قَدْ عَلِمَ كُلُّ
 أُنَاسٍ مَّشْرِبُهُمْ ۗ وَظَلَّلْنَا عَلَيْهِمُ
 الْغَمَمَ ۗ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْهِمُ الْمَنَّاءَ
 وَالسَّلْوَىٰ ۗ كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا
 رَزَقْنَاكُمْ ۗ وَمَا ظَلَمُونَا وَلَكِنْ
 كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١٦٠﴾
 وَإِذْ قِيلَ لَهُمْ اسْكُنُوا هَذِهِ الْقَرْيَةَ
 وَكُلُوا مِنْهَا حَيْثُ شِئْتُمْ وَقُولُوا
 حِطَّةٌ وَادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا نَفَعْنَا
 لَكُمْ حَطِيئَتِكُمْ ۗ سَنَزِيدُ
 الْمُحْسِنِينَ ﴿١٦١﴾ فَبَدَّلَ
 الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ قَوْلًا غَيْرَ
 الَّذِي قِيلَ لَهُمْ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ
 رِجْرًا مِنْ السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا
 يَظْلِمُونَ ﴿١٦٢﴾

160. Na Tuliwagawanya katika makabila kumi na mbili, mataifa mbali mbali. Na Tulimfunulia Musa walipomuomba maji watu wake, Tukamuambia: Lipige hilo jive kwa fimbo yako. Mara zikatibuka humo chemchem kumi na mbili, na kila watu wakajua mahali pao pa kunywea. Na Tukawafunika kivuli kwa

mawingu, na Tukawateremshia Manna na Salwa. Tukawaambia: Kuleni vizuri hivi Tulivyokuruzukuni. Wala hawakutudhulumu Sisi, bali wamejidhulumu wenyewe.

161. Na pale walipoambiwa: Kaeni katika mji huu, na mle humo mpendapo, na semeni: Tufutie dhambi zetu. Na injieni katika mlango wake kwa unyenyekevu, Tupate kukusameheni makosa yenu. Walio wema Tutawazidishia.

162. Lakini waliodhulumu miongoni mwao walibadilisha kauli, sio ile waliyoambiwa. Basi Tukawapelekea adhabu kutoka mbinguni kwa vile walivyokuwa wakidhulumu”.

Tafsir ya Aya hizi zote imetangulia katika *Surat Al-Baqarah*¹, ambayo ilishushwa Madina, ilhali Ayah hizi zilishushwa Makkah. Pia Tuliitaja tofauti kati ya maelezo ya sehemu zote mbili, hivyo hakuna haja ya kuyarudia hapa. Shukurani zote zinamstahikia Allah تعالى.

وَسَأَلَهُمْ عَنِ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ حَاضِرَةَ الْبَحْرِ إِذْ يَعْدُونَ فِي آلْسَبْتِ إِذْ تَأْتِيهِمْ
حِيَتَانُهُمْ يَوْمَ سَبْتِهِمْ شُرْعًا وَيَوْمَ لَا يَسْبِتُونَ^١ لَا تَأْتِيهِمْ^٢ كَذَلِكَ نَبْلُوهُمْ بِمَا كَانُوا
يَفْسُقُونَ ﴿١٧٣﴾

163. Na waulize khabari za mji uliokuwa kando ya bahari wakiivunja Sabato (Jumamosi ya mapumziko). Samaki walikuwa wakiwajia juu juu siku ya mapumziko yao, na siku zisiokuwa za kupumzika hawakuwa wakiwajia. Kwa namna hiyo Tuliwajaribu kwa sababu walikuwa wakifanya upotovu.

Uchupaji Mipaka wa Wayahudi Katika Sabato.

Ayah hii inafafanua Kauli ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ عَلَّمْتُمُ الَّذِينَ آعْتَدُوا مِنْكُمْ فِي آلْسَبْتِ

“Na hakika mlukwishayajua ya wale miongoni mwenu walioivunja Sabato, (siku ya mapumziko, Jumamosi)”. (2:65)

¹ Angalia Tafsir ya Surat Al-Baqarah (2:60).

Allah تعالیٰ Anamuambia Mtume Wake ﷺ;

وَسَأَلَهُمْ

“Na waulize”.

Kwa maana: Waulize hao Mayahudi walio pamoja na wewe juu ya khabari za wenzao ambao waliikhalifu amri ya Allah تعالیٰ, basi nakama ikawajia kwa ghafla kwa sababu ya kitendo chao, urukaji wao mipaka na hila zao katika kukhalifu, na uwaonye hao dhidi ya kuficha sifa zao ambazo wanazikuta katika Vitabu vyao ili yasiwafike yaliyowafika ndugu zao na *Salaf* wao. Kijiji hicho kilikuwa kikiitwa *Aylah*, katika pwani ya bahari ya *Qulzum* (nyekundu).

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالیٰ alisema kuwa Dawud bin Al-Haswin alipokea kutoka kwa 'Ikrimah kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما juu ya Kauli ya Allah تعالیٰ;

وَسَأَلَهُمْ عَنِ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ حَاضِرَةَ الْبَحْرِ

“Na waulize khabari za mji uliokuwa kando ya bahari”.

Alisema, “Ni kijiji kilichoitwa *Aylah*, baina ya Madyan na At-Tur (iliyoko Sinai)”¹ hivyo ndivyo walivyosema Mujahid, 'Ikrimah, Qatadah na As-Suddi².

Kauli ya Allah تعالیٰ;

إِذْ يَعْدُونَ فِي السَّبْتِ

“...wakiivunja Sabato (Jumamosi ya mapumziko)”.

Kwa maana: Wakiivunja na kukhalifu amri ya Allah تعالیٰ juu ya kuitukuza, kwani siku hiyo.

إِذْ تَأْتِيهِمْ حِيَتَانُهُمْ يَوْمَ سَبْتِهِمْ شُرَعًا

“Samaki walikuwa wakiwajia juu juu siku ya mapumziko yao”.

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Walikuwa wakionekana wazi kwenye maji”³.

¹ At-Tabari 13:180.

² At-Tabari 13:180-181.

³ At-Tabari 13:183.

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, "Kauli ya Allah تعالى:

وَيَوْمَ لَا يَسْبِتُونَ لَا تَأْتِيهِمْ كَذَلِكَ نَبْلُوهُمْ

"...na siku zisiokuwa za kupumzika hawakuwa wakiwajia. Kwa namna hiyo Tuliwajaribu".

Maana yake: Tunawajaribu kwa Kuwaonesha samaki katika usawa wa juu wa maji katika siku waliyoharamishwa kuwavua, na Kuwaficha dhidi yao katika siku ya halali kwao kuvua.

كَذَلِكَ نَبْلُوهُمْ

"Kwa namna hiyo Tuliwajaribu".

Tuliwapa mtihani.

بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ

"...kwa sababu walikuwa wakifanya upotovu".

Anasema, kwa kukiuka na kutoka katika kumtii Allah تعالى¹. Hawa walikuwa ni watu waliokuwa wakifanya hila kwa kuyakiuka Aliyoyakataza Allah تعالى, kwa kufanya matendo ambayo yana udhuru halali kwa juu juu, lakini kwa ndani ilikuwa ni kuvuka mipaka ya haramu. Imamu na mwanazuoni, Abu 'Abdullah bin Battwah alisema Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَا تَزْنِكُوا مَا ارْتَكَبَتِ الْيَهُودُ فَتَسْتَحِلُّوا مَحَارِمَ اللَّهِ بِأَذْنَى الْجِيلِ»

"Msiyarudie yale waliyoyafanya Mayahudi, ambao kwa hila kidogo walikuwa wakiyahalalisha Aliyoharamisha Allah تعالى".²

Isnadi yake ni nzuri.

* * *

¹ At-Tabari 13:183.

² Aaadab Az-Zafaaf uk. 192.

وَإِذْ قَالَتْ أُمَّةٌ مِّنْهُمْ لِمَ تَعِظُونَ قَوْمًا^{١٦٤} اللَّهُ مُهْلِكُهُمْ أَوْ
 مُعَذِّبُهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا^{١٦٥} قَالُوا مَعذِرَةٌ إِيَّايَ رَبِّنَا وَلَعَلَّهُمْ
 يَتَّقُونَ ﴿١٦٤﴾ فَلَمَّا دُسُوا مَا دُكِّرُوا بِمِآءِ أُجْحَيْنَا الَّذِينَ
 يَهْتَوُونَ عَنِ السُّوءِ وَأَخَذْنَا الَّذِينَ ظَلَمُوا بِعَذَابٍ
 بَئِيسٍ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿١٦٥﴾ فَلَمَّا عَتَوْا عَن مَّا نُهَى
 عَنْهُ قُلْنَا لَهُمْ كُونُوا قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿١٦٦﴾ وَإِذْ تَأَذَّنَ
 رَبُّكَ لِيَبْعَثَنَّ عَلَيْهِمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَن يَسُومُهُمْ سُوءَ
 الْعَذَابِ إِنَّ رَبَّكَ لَسَرِيعُ الْعِقَابِ^{١٦٧} وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ
 ﴿١٦٧﴾ وَقَطَعْنَاهُمْ فِي الْأَرْضِ أُمَمًا^{١٦٨} مِّمَّنْهُمْ الصَّالِحُونَ
 وَمِمَّنْهُمْ دُونِ ذَلِكَ^{١٦٩} وَبَلَّوْنَهُمْ بِالْحَسَنَاتِ وَالسَّيِّئَاتِ لَعَلَّهُمْ
 يَرْجِعُونَ ﴿١٦٨﴾ فَخَلَفَ مِنْ بَعدِهِمْ خَلْفٌ وَرِثُوا الْكِتَابَ
 يَأْخُذُونَ عَرَضَ هَذَا الْأَدْنَى وَيَقُولُونَ سَيُغْفَرُ لَنَا وَإِن
 يَأْتِهِمْ عَرَضٌ مِّثْلَهُ يَأْخُذُوهُ^{١٦٩} أَلَمْ يُؤْخَذْ عَلَيْهِمْ مِيثَاقُ
 الْكِتَابِ أَن لَّا يَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ وَدَرَسُوا مَا فِيهِ^{١٧٠}
 وَالْأُدَاغُ الْأَخِرَةُ خَيْرٌ لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ^{١٧١} أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٦٩﴾
 وَالَّذِينَ يُمَسِّكُونَ بِالْكِتَابِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ إِنَّا لَا نَضِيعُ
 أَجْرَ الصَّالِحِينَ ﴿١٧٠﴾ * وَإِذْ نَتَقْنَا الْجَبَلَ فَوْقَهُمْ كَأَنَّهُ ظُلَّةٌ
 وَظَنُّوا أَنَّهُ وَاقِعٌ بِهِمْ خُذُوا مَا آتَيْنَاكُمْ بِقُوَّةٍ وَاذْكُرُوا مَا
 فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٧١﴾

وَإِذْ قَالَتْ أُمَّةٌ مِّنْهُمْ لِمَ تَعِظُونَ قَوْمًا^{١٦٤}
 اللَّهُ مُهْلِكُهُمْ أَوْ مُعَذِّبُهُمْ عَذَابًا
 شَدِيدًا^{١٦٥} قَالُوا مَعذِرَةٌ إِيَّايَ رَبِّنَا
 وَلَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ﴿١٦٤﴾ فَلَمَّا دُسُوا مَا
 دُكِّرُوا بِمِآءِ أُجْحَيْنَا الَّذِينَ يَهْتَوُونَ
 عَنِ السُّوءِ وَأَخَذْنَا الَّذِينَ ظَلَمُوا
 بِعَذَابٍ بَئِيسٍ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ
 ﴿١٦٥﴾ فَلَمَّا عَتَوْا عَن مَّا نُهَى عَنْهُ
 قُلْنَا لَهُمْ كُونُوا قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿١٦٦﴾

164. Na kikundi kati yao
 walisema: kwa nini mnawa-
 waidhi watu ambao tangu
 hapo Mwenyezi Mungu
 Atawateketeza au Atawa-
 adhibu adhabu kali? Waka-
 sema: Ili uwe ni udhuru kwa
 Mola Mlezi wenu, na
 huenda nao wakamcha
 mungu.

165. Basi walipoyasahau
 waliyokumbushwa Tuli-
 waokoa waliokuwa waki-
 kataza maovu, na Tuka-
 watesa waliodhulumu kwa
 adhabu mbaya kwa vile
 walivyokuwa wakifanya
 upotovu.

166. Walipojifakharisha katika waliyokanywa Tuliwaambia: Kuweni manyani
 wa kudharauliwa.

Waliovunja Sabato Waligeuzwa Manyani na Kunusuriwa Waliokatata.

Allah تعالى Anatoa khabari juu ya watu wa kijiji hiki kwamba waligeuka kuwa makundi matatu, kundi la walioyafanya yaliyoharamishwa, na wakafanya hila kwa kuvua samaki siku ya Jumamosi, kama ilivyotangulia maelezo yake katika *Surat Al-Baqarah*. Kundi jingine liliyakatata hayo na kuyaepa. Kundi jingine lilinyamaza, na halikuyafanya hayo wala halikuyakatata, lakini liliwaambia wale walioyakatata;

لِمَ تَعْظُونَ قَوْمًا أَلَلَّهُ مُهْلِكُهُمْ أَوْ مُعَذِّبُهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا

“...kwa nini mnawawaidhi watu ambao tangu hapo Mwenyezi Mungu Atawateketeza au Atawaadhibu adhabu kali?”

Kwa maana: Kwanini mnawakatata hao, ilhali mnajua kwamba wao wameangamia na wamestahiki adhabu kutoka kwa Allah تعالى, basi hakuna faida ya kuwakatata kwenu. Wayakatatao hayo, walisema;

مَعذِرَةً إِلَىٰ رَبِّكُمْ

“Ili uwe ni udhuru kwa Mola Mlezi wenu”. Kwa maana: Katika yale tuliyoyafanya katika kuamrisha mema na kukatata maovu.

وَلَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

“...na huenda nao wakamchamungu”. Wanasema kuwa huenda kwa kuonywa huku, wakayaogopa yale waliyo nayo na kuyaacha na wakarejea kwa Allah تعالى kwa kufanya toba. Watakapotubu, Allah تعالى Atawasamehe na Atawarehemu. Allah تعالى Alisema;

فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ

“Basi walipoyasahau waliyokumbushwa”. Kwa maana: Wakiukaji hao walipokataa kupokea nasaha.

أَجْحِبْنَا الَّذِينَ يَنْهَوْنَ عَنِ السُّوْءِ وَأَخَذْنَا الَّذِينَ ظَلَمُوا

“Tuliwaokoa waliokuwa wakikatata maovu, na Tukawatesa waliodhulumu”.

Kwa maana: Waliofanya maasi.

بِعَذَابٍ بَئِيسٍ

"...**kwa adhabu mbaya**". Allah تعالى Akasema juu ya kuwaokoa watoa nasaha na kuwahiliki madhalimu na akanyamaza juu ya waliokuwa wakinyamaza, kwa sababu malipo ni kwa jinsi ya amali iliyofanyika, basi wao hawakustahili kusifiwa, wala hawakufanya madhambi makubwa ili wakaripiwe. 'Ikrimah alisema, "Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Ayah. Sijui kama waliosema;

لَمْ تَعْظُونَ قَوْمًا اللَّهُ مُهْلِكُهُمْ

"...**kwa nini mnawawaidhi watu ambao tangu hapo Mwenyezi Mungu Atawateketeza**".

Waliokolewa ama la?. Basi niliendelea kujadiliana naye mpaka nikajua kwamba waliokolewa. Akanipa zawadi ya nguo¹. Kauli ya Allah تعالى;

وَأَخَذْنَا الَّذِينَ ظَلَمُوا بِعَذَابٍ بَئِيسٍ

"...**na Tukawatesa waliodhulumu kwa adhabu mbaya**".

Inaonesha kwamba waliosalia walikuwa wameokolewa. Maana ya 'Ba-iys' kwa mujibu wa kauli ya Mujahid: 'Kali'² Na katika masimulizi mengine, 'Inaumiza'. Qatadah alisema, 'ya uchungu'³ Maana zote zinakaribiana, *Allahu A'alam*. Kauli ya Allah تعالى;

خَلْسِيئِينَ

"...**wa kudharauliwa**". Kwa maana: Hali ya kuwa wamedhalilika, wamehakirika, wamefedheheka.

وَإِذْ تَأَذَّرَ رَبُّكَ لَيَبْعَثَنَّ عَلَيْهِمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ يَسُومُهُمْ سُوءَ الْعَذَابِ إِنَّ

رَبَّكَ لَسَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ

167. Na pale Alipotangaza Mola wako Mlezi kwamba hapana shaka Atawaletea watu ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya mpaka Siku ya Kiyama. Hakika Mola wako Mlezi ni Mwepesi wa Kuadhibu, na bila ya shaka ni Mwenye Maghfira, na Mwenye Kurehemu.

¹ At-Tabari 13:202.

² At-Tabari 13:202.

³ At-Tabari 13:202

Udhalili wa Milele kwa Mayahudi.

تَأَذَّبَ

“Na pale Alipotangaza”. Maana yake: Inachukuliwa kutokana na *Al-Adhaan*. Kwa maana: ‘Aliarifu’, kwa mujibu wa Mujahid. Wengine walisema, ‘aliamuru’. Maneno haya yanaonesha kiapo. Kwa ajili hii, tamko limeanza na *lam*, *layub’athann*.

لَيَبْعَثَنَّ عَلَيْهِمْ

“...kwamba hapana shaka Atawaletea watu”. Kwa maana: Kwa Wayahudi.

إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ يَسُومُهُمْ سُوءَ الْعَذَابِ

“...ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya mpaka Siku ya Kiyama”.

Kwa sababu ya kuasi kwao na kukhalifu amri za Allah تعالى na Sharia Zake, na hila zao kwa ajili ya kujiingiza katika mambo ya haramu. Pia inasemwa kwamba Musa عليه السلام aliwataka watoe kodi ya mazao kwa miaka saba, pia ilisemwa ni miaka kumi na mitatu, na alikuwa ndiye wa kwanza kufanya hivyo. Kisha wakaangukia katika kukandamizwa na wafalme wa Kiyunani, Wakushdani na Wakaldani, kisha chini ya Wakristo ambao waliwakandamiza na kuwadhalilisha na wakawatoza kodi na ushuru (*Jizyah na Kharaj*). Kisha ukaja Uislamu na akaja Muhammad ﷺ wakawa chini yake, na pia wakawa wanalipa *Jizyah na Kharaj*. Al-‘Awfi alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliitafsiri Ayah hii, “Maana yake ni udhalili wao na kutozwa kwao *Jizyah*”¹ ‘Abdur-Razzaq alisimulia kutoka kwa Sa’id bin Al-Musayyab kuwa, “Inapendekezwa kupelekwa kwa *Al-Anbaati* katika *Al-Jizyah*.”² Mimi (Ibn Kathir) nasema, kisha mwisho wa jambo lao, wakatoka kumsaidia Ad-Dajjal na watapigwa na Waislamu pamoja na Isa bin Maryam عليه السلام. Haya yatatokea katika zama za mwisho wa maisha ya duniani. Kauli ya Allah تعالى;

إِنَّ رَبَّكَ لَسَرِيعُ الْعِقَابِ

“Hakika Mola wako Mlezi ni Mwepesi wa Kuadhibu...” Kwa wanaomuasi na wanaokataa Sheria Yake.

وَأِنَّهُمْ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ

“...na bila ya shaka ni Mwenye Maghfira, na Mwenye Kurehemu.”

¹ At-Tabari 13:205.

² Abdu Razzak 2: 240

Kwa kumtii na kurejea Kwake. Aya hii inataja rehema na adhabu ili kusiwepo kukata tamaa. Mara nyingi Allah تعالى Amehimiza na kuonya kwa pamoja, ili nyoyo kila mara ziwe na hisia ya matumaini na hofu.

وَقَطَعْنَاهُمْ فِي الْأَرْضِ أُمَّمًا مِّنْهُمْ الْأَصْلِحُونَ وَمِنْهُمْ دُونَ ذَلِكَ وَبَلَوْنَاهُمْ بِالْحَسَنَاتِ وَالسَّيِّئَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿١٦٨﴾ فَخَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ وَرِثُوا الْكِتَابَ يَأْخُذُونَ عَرَضَ هَذَا الْأَدْنَىٰ وَيَقُولُونَ سَيُغْفَرُ لَنَا وَإِنْ يَأْتِهِمْ عَرَضٌ مِّثْلَهُ يَأْخُذُوهُ ۗ أَلَمْ يُؤْخَذْ عَلَيْهِمْ مِيثَاقُ الْكِتَابِ أَنْ لَا يَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ وَدَرَسُوا مَا فِيهِ ۗ وَالَّذِينَ الْأَخِرَةَ خَيْرٌ لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٦٩﴾ وَالَّذِينَ يُمَسِّكُونَ بِالْكِتَابِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ إِنَّا لَا نَضِيعُ أَجْرَ الْمُصْلِحِينَ ﴿١٧٠﴾

168. Na Tuliwafarakisha katika ardhi makundi makundi. Wako kati yao walio wema na wengine kinyume cha hivyo. Na Tukawajaribu kwa mema na mabaya ili wapate kurejea.

169. Na wakafuatia baada yao kizazi kibaya waliorithi Kitabu. Wakashika anasa za haya maisha duni, na wakasema: Tutasamehewa! Na ikawajia tena anasa kama hiyo wataishika pia. Je, hawakufanyiwa agano la Kitabu kuwa wasiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila Haki tu? Nao wamekwisha soma yaliyomo humo. Na nyumba ya Akhera ni bora kwa wanaojikinga na maasi. Basi je, hamtii akilini?

170. Na wale wanaokishikilia Kitabu, na wakashika Sala – hakika Sisi hatupotezi ujira wa watendao mema.

Wana wa Israili Wasambaa Ardhini.

Allah تعالى Anataja kuwa Aliwagawa hao Mayahudi mataifa, madhehebu na makundi mengi duniani.

وَقُلْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ لِبَنِي إِسْرَائِيلَ اأَسْكُنُوا الْأَرْضَ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ جَعَلْنَا بِكُمْ لَفِيفًا ﴿١٧١﴾

“Na Tukawaambia baada yake Wana wa Israili: Kaeni katika nchi. Itapokuja ahadi ya Akhera Tutakuleteni nyote pamoja”. (17:104)

مِّنْهُمْ الصَّالِحُونَ وَمِنْهُمْ دُونَ ذَلِكَ

“Wako kati yao walio wema na wengine kinyume cha hivyo”.

Kwa maana: Kati yao kuna watenda mema na wengine kinyume cha hivyo, sawa na kauli ya majini;

وَأَنَا مِنَّا الصَّالِحُونَ وَمِنَّا دُونَ ذَلِكَ كُنَّا طَرَائِقَ قَدَدًا

“Na hakika katika sisi wamo walio wema, na wengine wetu ni kinyume na hivyo. Tumekuwa njia mbali mbali”. (72:11)

وَبَلَّوْنَهُمْ

“Na Tukawajaribu”.

Kwa maana yake: Tuliwapa jaribio.

بِالْحَسَنَاتِ وَالسَّيِّئَاتِ

“...kwa mema na mabaya”.

Kwa maana: Nyakati za faraja, shida, shauku, hofu, afya na balaa.

لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

“...ili wapate kurejea”.

Kisha Allah تعالى Alisema;

فَخَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ وَرِثُوا الْكِتَابَ يَأْخُذُونَ عَرَضَ هَذَا الْأَدْنَى

“Na wakafuatia baada yao kizazi kibaya waliorithi Kitabu. Wakashika anasa za haya maisha duni”.

Kwa maana: Kikafuatia kizazi hicho ambacho kilikuwa na wema na wasio wema baada ya kingine ambacho hakikuwa na kheri, na walikwisherithi usomaji wa Kitabu, ambacho ni Taurati. Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

يَأْخُذُونَ عَرَضَ هَذَا الْأَدْنَى

“Wakashika anasa za haya maisha duni”.

Alisema, “Wanaweza kutumia kila kilichopo duniani, iwe cha halali ama cha haramu na wangali wanayatamani maghfira”.

وَيَقُولُونَ سَيُغْفَرُ لَنَا وَإِنْ يَأْتِيهِمْ عَرَضٌ مِّثْلَهُ يَأْخُذُوهُ

“...na wakasema: Tutasamehewa! Na ikawajia tena anasa kama hiyo wataishika pia”.

Qatadah aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

يَأْخُذُونَ عَرَضَ هَذَا الْأَدْنَى

“Wakashika anasa za haya maisha duni”. Maana yake: “Wallah! Hiki ni kizazi kiovu”.

وَرِثُوا الْكِتَابَ

“...waliorithi Kitabu”. Baada ya Manabii na Mitume wao, Allah تعالى Aliwarithisha, kwa sababu lilikuwa ni agano lao. Allah تعالى Alisema katika Aya nyingine;

فَخَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ أَضَاعُوا الصَّلَاةَ

“Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Sala”. (19:59)

Alisema;

يَأْخُذُونَ عَرَضَ هَذَا الْأَدْنَى وَيَقُولُونَ سَيُغْفَرُ لَنَا

“Wakashika anasa za haya maisha duni, na wakasema: Tutasamehewa!”

Walikuwa na matumaini kwa Allah تعالى huku wakijidanganya wenyewe.

وَإِنْ يَأْتِيهِمْ عَرَضٌ مِّثْلَهُ يَأْخُذُوهُ

“Na ikawajia tena anasa kama hiyo wataishika pia”.

Hapana liwashughulishalo, wala liwakatazalo juu ya hayo wayafanyayo. Kila walipopata fursa humu duniani, waliitumia, hawakujali kama kilikuwa cha halali au cha haramu¹. As-Suddi alisema, Kauli ya Allah تعالى;

فَخَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ

“Na wakafuatia baada yao kizazi”. Mpaka; Kauli Yake Allah تعالى

وَدَرَسُوا مَا فِيهِ

“Nao wamekwisha soma yaliyomo humo”.

¹ At-Tabari 13:213.

Wana wa Israil walikuwa hawamchagui hakimu, bali baadaye alipokea rushwa katika kutoa hukumu. Walio bora katika wao walijumuika na wakapeana ahadi kwamba wasifanye jambo wala kupokea rushwa. Hata hivyo, mmoja wao alipopokea chirimiri, aliambiwa, 'Una nini, mbona Unachukua rushwa katika hukumu?' Na Yeye alijibu, 'Nitaghufiriwa'. Humshambulia na kumtuhumu kwa maneno kutokana na kitendo chake hicho, na pindi atakapokufa au kuuzuliwa nafasi yake. Kisha Wana wa Israili waliosalia, basi aliyechukua nafasi yake, naye alikuwa akichukua mlungula. Allah تعالى Anasema, na hao wengine (wanaomlaumu) nao, wangepewa fursa ya kupora, wangelifanya hivyo¹. Allah تعالى Alisema;

أَلَمْ يُؤْخَذْ عَلَيْهِمْ مِيثَاقُ الْكِتَابِ أَنْ لَا يَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ

“Je, hawakufanyiwa agano la Kitabu kuwa wasiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila Haki tu?”

Allah تعالى Anawakanushia kwa kitendo chao hiki, pamoja na kuchukua ahadi juu yao kwamba, wawabainishie watu haki, wala wasiifiche. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ فَنَبَذُوهُ وَرَاءَ ظُهُورِهِمْ وَأَشْرَوْا بِهِ مِمَّا قَلِيلًا فَبُئْسَ مَا يَشْتَرُونَ ﴿١٦٧﴾

“Na pale Mwenyezi Mungu Alipofungamana na waliopewa Kitabu kuwa: Lazima mtawabainishia watu, wala hamtakificha, walikitupa nyuma ya migongo yao, na wakanunua kwacho thamani duni. Basi ni kiovu hicho walichonunua”. (3:187)

Ibn Jurayj alisema, Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema;

أَلَمْ يُؤْخَذْ عَلَيْهِمْ مِيثَاقُ الْكِتَابِ أَنْ لَا يَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ

“Je, hawakufanyiwa agano la Kitabu kuwa wasiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila Haki tu?”

Alisema, “Juu ya yale waliyo na shauku nayo kutoka kwa Allah تعالى maghfira ya madhambi yao, ambayo wanaendelea kuyarejearejea, wala hawayatubii”².

¹ At-Tabari 13:213.

² At-Tabari 13:213.

Kauli ya Allah تعالى:

وَالَّذِينَ يُمَسِّكُونَ بِالْكِتَابِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ الْمُصْلِحِينَ ﴿١٦٧﴾

“Na wale wanaokishikilia Kitabu, na wakashika Sala – hakika Sisi hatupotezi ujira wa watendao mema.”

Allah تعالى Anawahimiza juu ya kupata thawabu zake nyingi, na Anawaonya dhidi ya adhabu zake kali. Maana yake: Allah تعالى Anasema, “Thawabu Zangu na yaliyo yangu ni kheri kwa mwenye kukwepa makatazo na akayaacha matamano ya nafsi yake, na akajiingiza katika kumtii Mola wake”.

أَفَلَا تَعْقِلُونَ

“Basi je, hamtii akilini?”

Allah تعالى Anasema, “Hawa watu wanaoyakhitari maisha haya badala ya yale yaliyo kwangu, hawawi na akili ya kuzuia usafihi na budhara”. Kisha Allah تعالى Akamsifia anayeshikana na Kitabu Chake ambacho kinamuongoza katika kumfuata Mjumbe Wake, Muhammad ﷺ, kama jinsi alivyoandika ndani yake. Allah تعالى Akasema:

وَالَّذِينَ يُمَسِّكُونَ بِالْكِتَابِ

“Na wale wanaokishikilia Kitabu”.

Kwa maana: Wanaoshikamana nacho, wakazifuata Amri Zake, na wakayaacha Makemeo Yake.

وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ الْمُصْلِحِينَ

“...na wakashika Sala – hakika Sisi Hatupotezi ujira wa watendao mema”.

* وَإِذْ تَعَقْنَا الْجَبَلَ فَوْقَهُمْ كَأَنَّهُ ظُلَّةٌ وَظَنُّوا أَنَّهُ وَاقِعٌ بِهِمْ خُذُوا مَا آتَيْنَاكُمْ بِقُوَّةٍ

وَأَذْكُرُوا مَا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٧١﴾

171. Na pale Tulipounyanyua mlima juu yao ukawa kama kwamba ni kiwingu kilichowafunika, na wakadhani kuwa utawaangukia, (Tukawaambia): Kamateni kwa nguvu Tuli yokupeni, na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kumcha Mungu”.

Kunyanyuliwa Mlima Turi Juu ya Vichwa vya Mayahudi kwa Sababu ya Ukaidi Wao.

'Ali bin Abu Twalhah amepokea kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, Kauli ya Allah تعالى:

وَإِذْ تَتَقْنَا الْجَبَلَ فَوْقَهُمْ

“Na pale Tulipounyanyua mlima juu yao”.

Kuwa anasema, “Tuliunyanyua, kama Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَرَفَعْنَا فَوْقَهُمُ الطُّورَ بِمِثْقَلِهِمْ

“Na Tukanyanyua mlima juu yao kwa kufanya agano nao”. (4:154)¹

Sufyan Ath-Thawri alisema kutoka kwa Al-A'mash kutoka kwa Sa'id bin Jubayr kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, “Malaika waliunyanyua juu ya vichwa vyao”. Kama inavyoelezwa na Kauli ya Allah تعالى:

وَرَفَعْنَا فَوْقَهُمُ الطُّورَ

“Na pale Tulipounyanyua mlima juu yao”.

Al-Qasim bin Abi Ayyub amepokea kuwa Sa'id bin Jubayr alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Baadaye, Musa عليه السلام akaenda pamoja nao katika Ardhi tukufu na Akazichukua mbao, baada ya ghadhabu kumtulia, na akawaamuru kazi ambayo Allah تعالى Alimuamuru aibalighishe, ikawawia uzito kwao, na walikataa kuipokea, mpaka Allah تعالى Akawanyanyulia mlima juu yao.

كَانَهُمْ ظُلَّةٌ

“...kama kwamba ni kiwingu”.

Alisema, Malaika waliunyanyua juu ya vichwa vyao. An-Nasai aliinukuu yote kwa urefu.

* * *

¹ At-Tabari 13:218.

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِنْ بَنِي آدَمَ مِنْ ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ
 وَأَشْهَدَهُمْ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ ۖ قَالُوا بَلَىٰ شَهِدْنَا
 أَن تَقُولُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّا كُنَّا عَنْ هَذَا غَافِلِينَ ﴿١٧٢﴾
 أَوْ تَقُولُوا إِنَّمَا أَشْرَكَ آبَاؤُنَا مِنْ قَبْلُ وَكُنَّا ذُرِّيَّةً مِنْ
 بَعْدِهِمْ ۖ أَفَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ الْمُبْطِلُونَ ﴿١٧٣﴾ وَكَذَلِكَ
 نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿١٧٤﴾ وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ
 الَّذِي ءَاتَيْنَاهُ ءَايَاتِنَا فَاسْلَخَ مِنْهَا فَأَتَبَعَهُ الشَّيْطَانُ فَكَانَ
 مِنَ الْغَاوِينَ ﴿١٧٥﴾ وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنَاهُ بِهَا وَلَكِنَّهُ أَخْلَدَ
 إِلَى الْأَرْضِ وَاتَّبَعَ هَوَاهُ ۖ فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ الْكَلْبِ إِنْ
 تَحَمَلَ عَلَيْهِ يَلْهَثُ أَوْ تَرَكَهٗ يَلْهَثُ ۚ ذَلِكَ مَثَلُ الْقَوْمِ
 الَّذِينَ كَذَبُوا بِآيَاتِنَا ۖ فَاقْصُصِ الْقَصَصَ لَعَلَّهُمْ
 يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٧٦﴾ سَاءَ مَثَلًا الْقَوْمُ الَّذِينَ كَذَبُوا بِآيَاتِنَا
 وَأَنفُسِهِمْ كَانُوا يَظْلِمُونَ ﴿١٧٧﴾ مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِي
 وَمَنْ يُضِلِلْ فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٧٨﴾

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِنْ بَنِي آدَمَ مِنْ
 ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَأَشْهَدَهُمْ عَلَىٰ
 أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ ۖ قَالُوا بَلَىٰ
 شَهِدْنَا أَن تَقُولُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ
 إِنَّا كُنَّا عَنْ هَذَا غَافِلِينَ ﴿١٧٢﴾
 أَوْ تَقُولُوا إِنَّمَا أَشْرَكَ آبَاؤُنَا مِنْ
 قَبْلُ وَكُنَّا ذُرِّيَّةً مِنْ بَعْدِهِمْ ۖ
 أَفَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ الْمُبْطِلُونَ ﴿١٧٣﴾
 وَكَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ
 يَرْجِعُونَ ﴿١٧٤﴾

172. Na pale Mola wako Mlezi Alipowaleta katika wanadamu kutoka miongoni mwao kizazi chao, na Akawashuhudisha juu ya nafsi zao, Akawaambia: Je, Mimi si Mola Mlezi wenu?

Wakasema: Kwani! Tumeshuhudia. Msije mkasema Siku ya Kiyama sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo.

173. Au mkasema: Hakika baba zetu ndio walioshirikisha kabla yetu, na sisi ni dhuriya zao tu baada yao. Basi Utatungamiza kwa sababu ya waliyoyafanya wapotovu?

174. Ndio kama Tunavyozipambanua Ishara, kwa kutaraji kuwa watarejea”.

Ubainifu wa Agano Lililochukuliwa kutoka kwa Dhuria wa Adam عليه السلام.

Allah تعالى Anasema kuwa Aliileta dhuria wa Adam عليه السلام kutoka katika viuno vya baba zao wakitoa ushahidi wao kuwa Allah تعالى Ndiye Mola na Mfalme wao, na kuwa hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye tu.

Allah تعالى Aliwaumba katika *Fitrah* hii. Allah تعالى Alisema;

فَأَقْرَهُ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ

“Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini – ndilo umbile la Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu”. (30:30)

Katika *Sahih* Mbili kuna Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema;

«كُلُّ مَوْلُودٍ يُوَلَّدُ عَلَى الْفِطْرَةِ، فَأَبَوَاهُ يُهَوِّدَانِهِ وَيُنَصِّرَانِهِ وَيُمَجْسَانِهِ كَمَا تُوَلَّدُ بَيْمَةً
جَمْعَاءَ هَلْ تُجَسِّرُونَ فِيهَا مِنْ جَدْعَاءَ»

“Kila mtoto huzaliwa katika Fitrah, wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi au Mmajusi. Kama azaliwavyo bahima na miili kamili, je mnamuona yeyote akiwa amekatwa pua (pindi wanapozaliwa)?”¹

Katika *Sahih* Muslim kuna Hadithi ya ‘Iyaadh bin Himar رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema;

«يَقُولُ اللَّهُ: إِنِّي خَلَقْتُ عِبَادِي حُنَفَاءَ فَجَاءَتْهُمْ الشَّيَاطِينُ فَاجْتَالَتْهُمْ عَنْ دِينِهِمْ
وَحَرَمَتْ عَلَيْهِمْ مَا أَخَلَّتْ لَهُمْ»

“Allah تعالى Anasema, “Mimi Nimewaumba waja Wangu wakiwa Hunafa (Wako katika Tauhidi), mashetani wakawajia na wakawapotosha mbali na dini yao na wakawaharamishia Nilivyowahalalishia”².

Kuna Hadithi nyingi zilizosimuliwa juu ya dhuria wa Adam عليه السلام kutokana na kiuno cha Adam عليه السلام na kugawanyika kwao baina ya watu wa kuumeni

¹ Fat’hul Al-Bari 3:290 na Muslim 4:2047.

² Muslim 4:2197.

na wa kushotoni. Imamu Ahmad alisimulia, kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema;

«يُقَالُ لِلرَّجُلِ مِنْ أَهْلِ النَّارِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَرَأَيْتَ لَوْ كَانَ لَكَ مَا عَلَى الْأَرْضِ مِنْ شَيْءٍ أَكُنْتَ مُقْتَدِرًا بِهِ قَالَ: قَيِّقُولُ: نَعَمْ قَيِّقُولُ: قَدْ أَرَدْتُ مِنْكَ أَهْوَنَ مِنْ ذَلِكَ قَدْ أَخَذْتُ عَلَيْكَ فِي ظَهْرِ آدَمَ أَنْ لَا تُشْرِكَ بِي شَيْئًا فَأَيَّتَ إِلَّا أَنْ تُشْرِكَ بِي»

"Siku ya Kiyama, mtu wa Motoni ataambiwa, "Kama ungelimiliki kila lililo ardhini, ungelijikombolea kwayo?" Atasema, "Ndiyo". Allah تعالى Atasema, "Nilikuamuru lililo jepesi mno kuliko hivyo, ulipokuwa ungali katika kiuno cha Adam, kwamba Usinishirikishe na chochote, ukakataa na ukanishirikisha"¹. Waliitoa katika Sahih Mbili².

At-Tirmidhi alisimulia katika kuitafsiri Aya hii kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema;

«لَمَّا خَلَقَ اللَّهُ آدَمَ مَسَحَ ظَهْرَهُ فَسَمَطَ مِنْ ظَهْرِهِ كُلَّ نَسَمَةٍ هُوَ خَالِقُهَا مِنْ ذُرِّيَّتِهِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَجَعَلَ بَيْنَ عَيْنِي كُلِّ إِنْسَانٍ مِنْهُمْ وَبِصَا مِنْ نُورٍ ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى آدَمَ فَقَالَ: أَيُّ رَبِّ مَنْ هَؤُلَاءِ؟ قَالَ: هَؤُلَاءِ ذُرِّيَّتُكَ فَرَأَى رَجُلًا مِنْهُمْ فَأَعْجَبَهُ وَبِصَ مَا بَيْنَ عَيْنَيْهِ قَالَ: أَيُّ رَبِّ مَنْ هَذَا؟ قَالَ: هَذَا رَجُلٌ مِنْ آخِرِ الْأُمَمِ مِنْ ذُرِّيَّتِكَ يُقَالُ لَهُ دَاوُدُ قَالَ: رَبِّ وَكَمْ جَعَلْتَ عُمْرَهُ؟ قَالَ: سِتِّينَ سَنَةً، قَالَ: أَيُّ رَبِّ وَقَدْ وَعَدْتَ لَهُ مِنْ عُمْرِي أَرْبَعِينَ سَنَةً فَلَمَّا انْقَضَى عُمْرُ آدَمَ جَاءَهُ مَلَكُ الْمَوْتِ قَالَ: أَوَلَمْ يَبْقَ مِنْ عُمْرِي أَرْبَعُونَ سَنَةً قَالَ: أَوَلَمْ تُعْطِهَا ابْنَكَ دَاوُدَ؟ قَالَ: فَجَحَدَ آدَمُ فَجَحَدَتْ ذُرِّيَّتُهُ وَنَسِيَ آدَمَ فَنَسِيَتْ ذُرِّيَّتُهُ وَحَطَى آدَمَ فَحَطَّتْ ذُرِّيَّتُهُ»

"Allah تعالى Alipomuumba Adam, Aliupangusa mgongo wa Adam akaanguka katika mgongo wake kila mtu ambaye Yeye Atamuumba katika dhuria wa Adam, mpaka Siku ya Kiyama, na Akaweka nuru hafifu baina ya macho yake mawili, kisha Akawaonesha kwa Adam, naye akauliza, "Ewe Mola wangu! Ni akina nani hawa?" Akamjibu, "Hawa ni dhuria wako". Adam akamuona mtu mmoja miongoni

¹ Ahmad 3:127.

² Fat'hul Al-Bari 6:419 na Muslim 4:2160.

mwao aliyekuwa na nuru aliyoienda. Akauliza, "Ewe Mola wangu, huyu ni nani?" Akamjibu, "Huyu ni mtu katika umma wa mwishoni, mwishoni anaitwa Dawud". Akamuuliza, "Ewe Mola wangu, Umemjaalia umri gani?" Akamjibu, "Miaka sitini". Akasema, "Nami nampa hiba ya miaka arubaini zaidi kutoka katika umri wangu". Umri wa Adam ulipomalizika, Malaika wa mauti alimjia. Adam akasema, "Kwani umri wangu haujabakia miaka arubaini?" Allah تعالی Akamuambia, "Kwani hukumpatia mwanao, Dawud umri huo toka kwako?" Adam akapinga hilo, na dhuria wake nao wakafuata namna hiyo. Adam alisahau na dhuria wake nao wakasahau. Adam alifanya makosa na dhuria wake nao wakafanya makosa".

At-Tirmidhi akasema baada ya hapo, Hadithi hii ni *Hasan Sahih*, na ilisimuliwa kupitia isnadi mbalimbali kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ¹. Na Al-Hakim aliinukuu katika Al-Mustadrak yake na akasema, "Ni *Sahih* kwa vigezo vya Muslim na hawakuinukuu"².

Hadithi hizi na nyingine kama hizi zinajulisha kuwa Allah تعالی Aliitoa dhuria wa Adam عليه السلام kutoka katika kiuno cha Adam عليه السلام na Akapambanua baina ya wakazi wa *Janna* na Motoni.

Kisha Allah تعالی Akasema;

وَأَشْهَدُهُمْ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ قَالُوا بَلَىٰ

"...na Akawashuhudisha juu ya nafsi zao, Akawaambia: Je, Mimi si Mola Mlezi wenu? Wakasema: Kwani".

Kwa maana: Aliwafanya wawe mashahidi juu ya hilo kwa mnasaba na kauli. Wakati mwingine, ushahidi hutolewa kwa kauli. Sawa na Kauli ya Allah تعالی;

قَالُوا شَهِدْنَا عَلَىٰ أَنفُسِنَا

"Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu". (6:130)

Na wakati mwingine ni kufuatana na mazingira. Sawa na Kauli ya Allah تعالی;

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:457.

² Al-Hakim 2:325.

مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَنْ يَعْمُرُوا مَسْجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ بِالْكَفْرِ

“Haiwi kuwa makafiri ndio waamirisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudishia wenyewe ukafiri”. (9:17)

Kwa maana: Hali yao inawatolea ushahidi juu ya hilo. Si kwamba wao wanasema hivi na vile. Kauli ya Allah تعالى;

وَإِنَّهُ عَلَىٰ ذَٰلِكَ لَشَهِيدٌ

“Na hakika yeye mwenyewe bila ya shaka ni shahidi wa hayo!” (100:7)

Ni kama vile kuomba, wakati mwingine huwa kwa kauli na wakati mwingine kwa hali au mazingira. Sawa na Kauli ya Allah تعالى;

وَأَتَّكُم مِّن كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ

“Na Akakupeni kila mlichomuomba”. (14:34)

Walisema, miongoni mwa viashiria vya malengo ya hayo ni kwamba Allah تعالى Alijaalia kutoa ushahidi kuwa ni hoja dhidi yao juu ya ushirikina. Kama ingelikuwa hili tayari limekwishatukia, kama wanavyodai baadhi ya watu, ingelikuwa kila mmoja anakumbuka ili iwe ni hoja juu yake. Ikiwa Patasemwa, kule Mtume ﷺ kulijulisha kunatosha juu ya kupatikana kwake. Jawabu ni kuwa, wakadhibishaji katika washirikina huyakadhibisha yote waliyoletewa na Mitume, ikiwa ni pamoja na hili na mengine. Na huku ni kuifanya hoja inayojitoshela juu yao, na ikajulisha kuwa hayo ni *Fitrah* waliyoubwa kwayo katika kuikiri Tauhidi. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema;

أَنْ تَقُولُوا

“ Msije mkasema”. Siku ya Kiyama. Maana ili msije kusema;

إِنَّا كُنَّا عَنْ هَٰذَا

“...sisi tulikuwa na jambo hili”. Kwa maana: Tawhidi.

غَافِلِينَ ﴿٧٧﴾ أَوْ تَقُولُوا إِنَّمَا أَشْرَكَ آبَاؤُنَا

“...tumeghafilika... Au mkasema: Hakika baba zetu ndio walioshirikisha”. (7:172-173)

وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ الَّذِي ءَاتَيْنَاهُ ءَايَاتِنَا فَانْسَلَخَ مِنْهَا فَاتَّبَعَهُ الشَّيْطَانُ فَكَانَ مِنَ الضَّالِّينَ
 ﴿١٧٥﴾ وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنَاهُ بِهَا وَلَكِنَّهُ أَخْلَدَ إِلَى الْأَرْضِ وَاتَّبَعَ هَوَاهُ فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ
 الْكَلْبِ إِنْ تَحْمِلَ عَلَيْهِ يَلْهَثْ أَوْ تَتْرَكْهُ يَلْهَثْ ذَٰلِكَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُوا
 بِءَايَاتِنَا ۚ فَاقْصُصِ الْقَصَصَ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٧٦﴾ سَاءَ مَثَلًا لِّلَّذِينَ كَذَّبُوا
 بِءَايَاتِنَا وَأَنْفُسُهُمْ كَانُوا يَظْلِمُونَ ﴿١٧٧﴾

175. Na wasomee khabari za yule ambaye Tulimpa ishara Zetu, naye akajivuna nazo. Na shetani akamuandama, akawa miongoni mwa waliopotea.

176. Na Tungelitaka Tungelimtukuza kwa hizo ishara, lakini yeye aliushikilia ulimwengu na akafuata pumbao lake. Basi mfano wake ni mfano wa mbwa. Ukimhujumu hupumua na kutoa ulimi na ukimuacha pia hupumua na kutoa ulimi. Huo ni mfano wa kaumu wanaozikanusha ishara Zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari.

177. Huu ni mfano muovu kabisa wa watu wanaokanusha ishara Zetu na wakajidhulumu nafsi zao.

Kisa cha Bal'am bin Ba'uraa.

'Abdur-Razzaq alisimulia kuwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema juu ya Kauli ya Allah تعالى:

وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ الَّذِي ءَاتَيْنَاهُ ءَايَاتِنَا فَانْسَلَخَ مِنْهَا

“Na wasomee khabari za yule ambaye Tulimpa ishara Zetu, naye akajivuna nazo”.

Huyo ni mtu mmoja katika Wana wa Israil, aliyetitwa Bal'am bin Ba'uraa¹. Kadhalika alisimulia hivyo Shu'bah na wengine kutoka kwa Mansuur², ambaye

¹ Abdur-Razzaq 2:443.

² At-Tabari 13:253.

aliyapata hayo kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه. Sa'id bin Abu 'Urwah alipata masimulizi kutoka kwa Qatadah, kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما: "Yeye ni Swayfi bin Ar-Rahib". Qatadah na Ka'b walisema, "Alikuwa ni mtu kutoka Al-Balqaa (jimbo moja la Jordan) na alikuwa akilijua Jina Kuu la Allah تعالى, na alikuwa akiishi Bayt Al-Muqaddas pamwe na madhalimu". Al-Awfi alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: "Yeye ni mtu aliyetokea Yemen na aliitwa Bal'am bin Ba'uraa. Allah تعالى Alimpa Aya Zake, lakini aliziacha"¹. Malik bin Dinar alisema, "Alikuwa miongoni mwa maulamaa wa Wana wa Israil, na alikuwa akitakabaliwa maombi yake. Walikuwa wakimuomba kuwaongoza katika kuomba dua juu ya shida mbalimbali. Nabii Musa عليه السلام, alimtuma kwa Mfalme wa Madyan ili amlinganie kwa Allah تعالى. Mfalme huyo alimtuliza (na kumfanya alegeze msimamo) na akampa zawadi, akafuata dini yake na akaiacha dini ya Musa". 'Imran bin 'Uyaynah alisema kutoka kwa Hisn, kutoka kwa 'Imran bin Al-Harith, kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Yeye ni Bal'am bin Ba'uraa"². Pia alisema hivyo Mujahid na 'Ikrimah³. Thaqif alisema, "Yeye ni Umayyah bin Abu As-Swalt". Ama lililo mashuhuri kuhusu sababu ya kushushwa kwa Aya hii tukufu ni kwamba, yeye ni mtu mmoja katika waliotangulia katika zama za Wana wa Israil. Sawa na alivyosema Ibn Mas'ud رضي الله عنه na wengine miongoni mwa Salaf"⁴ 'Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Yeye ni mtu kutokea katika mji wa madhalimu (mji wa Jerusalem), aliyeitwa Bal'am, alikuwa akilijua Jina Kuu la Allah تعالى.

Ali bin Abuu Twalha amesema kutoka kwa Ibn Abbasi رضي الله عنهما: Musa alipofika nao kwa watu madhalimu, na akiwemo Bal'am, walimjia wana wa ami yake na kaumu yake, na wakasema, "Musa عليه السلام ni mtu mwenye nguvu, na wanajeshi wake ni wengi. Kama atatushinda, atatuhiliki, basi muombe Allah تعالى. Atuondoshee Musa عليه السلام na walio pamoja naye". Akasema, "Kama mimi nitamuomba Allah تعالى Amzuie Musa عليه السلام na walio pamoja naye, basi nitapata hasara katika maisha yangu ya dunia na Akhera". Wakaendelea kumueleza, mpaka alipowaombea, basi Allah تعالى Akamvua alichokuwa Amemfadhili. Na hiyo ni Kauli ya Allah تعالى;

¹ At-Tabari 13:261.

² At-Tabari 13:253.

³ At-Tabari 13:254.

⁴ At-Tabari 13:253.

فَأَنسَلَخْ مِنْهَا فَاتَّبَعَهُ الشَّيْطَانُ

“...naye akajivuna nazo. Na shetani akamuandama”¹

Kauli ya Allah تعالى;

وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنَاهُ بِهَا وَلَئِنَّهُ أَخْلَدَ إِلَى الْأَرْضِ وَاتَّبَعَ هَوَاهُ

“Na Tungelitaka Tungelimtukuza kwa hizo ishara, lakini yeye aliushikilia ulimwengu na akafuata pumbao lake”.

Allah تعالى Anasema;

وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنَاهُ بِهَا

“Na Tungelitaka Tungelimtukuza kwa hizo ishara”.

Kwa maana: Tungelimtukuza dhidi ya kujinasibisha na uchafu wa dunia kwa ishara ambazo Tulimpatia yeye.

وَلَئِنَّهُ أَخْلَدَ إِلَى الْأَرْضِ

“...lakini yeye aliushikilia ulimwengu”.

Kwa maana: Aligeukia pambo la maisha ya dunia na teremo zake. Na akazielekea ladha na neema zake na yakamghuri kama yalivyowaghuri wengine, kinyume na wenye kuona na fikra nzuri.

Muhammad bin Is-haq bin Yasar رحمه الله تعالى alisema, kuwa Salim, Abu An-Nadhr alisimulia kuwa Musa عليه السلام aliposhuka katika ardhi ya Banu Kan'an katika Ardhi ya Shamu, kaumu ya Bal'am ilimjia na wakamuambia, “Huyu ni Musa bin 'Imran kutoka kwa Wana wa Israil, anataka atutoe katika miji yetu na kutuua na kuwapatia Wana wa Israil. Sisi ni kaumu yako, na hatuna sisi makazi, na wewe ni mtu ambaye huwa maombi yako yanajibiwa, basi hebu toka na umuombe Allah تعالى juu yao”. Akasema, “Ole wenu! Nabii wa Allah تعالى huwa anakuwa pamoja na Malaika na Waumini, kwa namna gani nitakwenda kuomba dhidi yao, nami nayajua kutoka kwa Allah تعالى kiasi ninachokijua?” Wakamuambia, “Sisi hatuna makazi”. Wakaendelea kumhadaa na kumsihi mpaka wakamuingiza katika mtihani. Akapanda juu ya punda huku akiuelekea

¹ At-Tabari 13:258.

mlima Husban ambao kwa nyuma yake kulikuwa na askari wa Wana wa Israil. Hakufika mbali, punda alikaa chini na akakataa kuendelea. Akateremka na kumpiga mpaka aliposimama tena, naye akapanda juu yake na kuendelea. Hakufika mbali, punda alikaa chini tena, akampiga mpaka akasimama.

Allah تعالی Akampa idhini ya kusema, "Ole wako! Ewe Bal'am! Unakwenda wapi? Unawaona Malaika wananirudisha usoni kwangu? Unakwenda kwa Nabii wa Allah تعالی na Waumini ili ukaombe dua dhidi yao?" Hakumuacha, bali alimpiga, Allah تعالی Akamuachilia aendelee baada ya hayo.

Akaenda naye mpaka walipopanda katika kilele cha mlima Husban walipokuwepo askari wa Musa عليه السلام na Wana wa Israili. Alianza kuomba dhidi yao lakini hakumudu kuwaombea shari, kwani Allah تعالی Aliyabadili maneno yake kuwaelekea kaumu yake mwenyewe, na alipoomba kheri kwa ajili ya kaumu yake, Allah تعالی Aliyabadili maneno yake na kuwaelekea Wana wa Israil. Kaumu yake wakasema, "Ewe Bal'am! Unakijua unachokifanya? Wewe unawaombea wao mema na unatuombea sisi shari!" Akasema, "Jambo hili si kama ninavyotaka mimi mwenyewe, hili ni jambo Alilopanga Allah تعالی. Ulimi wake ukaning'inia kifuani mwake, na akawaambia, "Kwa sasa nimeipoteza dunia na Akhera yangu, wala hakuna kilichosalia isipokuwa vitimbi na hila tu ambavyo nitavifanya kwa ajili yenu. Wapambeni wanawake na muwape bidhaa kisha waambieni wakaziuze bidhaa hizo kwa Jeshi la wana wa Israil, na waamrisheni wapite mbele yao, na wala wasikatae pindi watakapotakiwa kuzini nao kwani atakapozini mwanamke mmoja tu na mwanajeshi wao, hilo linatosha kwenu.

Hivyo wakafanya wanawake wao wakavamia kambi ya Jeshi, mwanamke wa Kikan'an, jina lake Kasaba bint Swur, kiongozi wao, alipita karibu na mkuu mmoja wapo katika Wana wa Israil, naye ni Zamri bin Shalum, kiongozi wa dhuria wa Shamun bin Ya'qub bin Is-haq bina Ibrahim. Alipomuona alimpenda, akasimama, akamshika mkono, na akamleta kwa Musa عليه السلام na akasema, "Mimi nadhani wewe utasema hii ni haramu kwako, usimkaribie?" Nabii Musa عليه السلام akasema, "Ndiyo, huyo mwanamke ni haramu kwako". Akasema, "Wallahi! Mimi sitakutii katika hili." Akaingia naye katika hema lake na akamuingilia.

Allah تعالی Akapeleka tauni kwa Wana wa Israili. Finhas bin lyzar bin Harun alikuwa msimamizi wa amri za Musa عليه السلام na hakuwepo wakati huo ambapo

Zamri bin Shalum alikuwa akifanya alichokifanya. Akaja na kukuta tauni inazunguka baina yao. Akapashwa khabari, akachukua mkuki wake ambao wote uliotengenezwa kwa chuma. Akaingia ndani ya hema na kuwakuta wakiwa wamelala wote wawili, akawaweka vyema kwa mkuki wake, kisha akatoka nao nje huku akiwainua juu kwa mkono wake, na akaegemeza kiwiko chake ubavuni mwake, na akaegemeza mkuki katika ndevu zake, na alikuwa ni mtoto wa kwanza wa Izar. Akawa anasema, "Allah تعالی hivi ndivyo tunavyowafanyia wanaokuasi".

Allah تعالی Akaondosha tauni. Akawahesabu wana wa Israil waliohilikishwa na tauni wakati wa baina ya Zamri kumchukua mwanamke na kuuliwa kwake na Finhas, idadi yao ilikuwa watu elfu sabini. Wapo wasimulizi waliosema kwa uchache, walifariki watu ishirini elfu katika muda mchache sana wa mchana mmoja. Kuanzia hapo, Wana wa Israili wakawa wanampatia mwana wa Finhas shingo na mikono kutokana na kila dhabihu wanayochinja.

Pia walikuwa wanamtangulizia kumpa kitu kutokana na mali zao kwa sababu alikuwa mwana wa kwanza kwa baba yake, Iyza. Allah تعالی Aliteremsha Ayah juu ya Bal'am bin Ba'uraa.

وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ الَّذِي آتَيْنَاهُ آيَاتِنَا فَانْسَلَخَ مِنْهَا

"Na wasomee khabari za yule ambaye Tulimpa ishara Zetu, naye akajivuna nazo". Mpaka;

لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ

"...huenda wakatafakari". Kauli ya Allah تعالی

فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ الْكَلْبِ إِنْ حَمَلَ عَلَيْهِ يَلْهَثُ أَوْ تَرَكَهُ يَلْهَثُ

"Basi mfano wake ni mfano wa mbwa. Ukimhujumu hupumua na kutoa ulimi na ukimuacha pia hupumua na kutoa ulimi".

Wafasiri walitoa maoni mbalimbali juu ya maana yake katika mtiririko wa ismulizi za bin s-haq رحمه الله تعالی kuwa kutoka kwa Salim, kutoka kwa Abu An-Nadhr, ni kwamba, "Ulimi wa Bal'am ulining'inia kifua ni mwake".¹

¹ At-Tabari 13:265.

Kwa hivyo akashabihishwa na mbwa anavyopumua na kutoa ulimi katika hali zote mbili, hudhihiri ikiwa atakemewa na hata akiachwa.

Pia ilisemwa kuwa maana yake ni, ukawa mfano wake katika kupotea kwake na kuendelea kupotea na kushindwa kujinufaisha kwa dua ya kumpeleka katika Imani na kule kushindwa kabisa kuomba dua, ni kama mbwa apumuavyo na kutoa ulimi katika hali zote mbili, akifanyiwa jambo au akiachwa, hupumua na kutoa ulimi.

Kadhalika, huyu hanufaiki na mawaidha na wito wa kuifuata imani wala kukusokana kwa hayo.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ

“...ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawaamini”. (2:6)

أَسْتَغْفِرُ لَهُمْ أَوْ لَا تَسْتَغْفِرُ لَهُمْ إِنْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ

“Waombee msamaha au usiwaombee. Hata ukiwaombea msamaha mara sabini, Mwenyezi Mungu Hatawasamehe”. (9:80)

Na mfano wa hivyo. Pia ulisemwa, maana yake ni kuwa: Moyo wa kafiri, mnafiki na yazingatie hayo. Yalinukuliwa maneno kama haya kutoka kwa Al-Hasan Al-Basri na wengine. Kauli ya Allah تعالى:

فَأَقْصَصَ الْقَصَصَ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ

“Basi simulia hadithi, huenda...”.

Kwa maana: Huenda Wana wa Israil wanaojua hali ya Bal'am na yaliyomkumba juu ya kupotezwa na Allah تعالى na kumuweka mbali na rehema zake, kwa sababu alitumia neema ya Allah تعالى juu yake kwa kumfundisha Jina Kuu, ambalo Allah تعالى Akiombwa kwa kutumia Jina hilo, Hutoa, na Akiombwa kwalo Hujibu. Yeye alimuomba Mola wake pasi na twaa, bali alimuomba Allah تعالى dhidi ya watu wa upande wake katika Imani, wafuasi wa Mja na Mjumbe wa zama hizo, *Kalimullah*, Musa bin 'Imran عليه السلام. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema:

لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ

“...huenda wakatafakari”.

Maana: Ili wajihadhari wasije wakawa kama yeye, kwani Elimu ya Allah تعالى imewazingira na Akawafanya kuwa bora zaidi ya mabedui waliowazunguka.

Allah تعالى Aliwapa sifa bora zaidi ya mabedui ambazo walizijua kupitia sifa hizo utume wa Muhammad ﷺ kama walivyokuwa wakiwajua watoto wao.

Wao ni miongoni mwa wanaostahiki zaidi kumfuata na kumnusuru na kumuunga mkono Muhammad ﷺ, sawa na Manabii wao walivyowapasha khabari na kuwaamuru hivyo.

Kwa hivyo, yeyote miongoni mwao ambaye atayakhalifu yaliyo katika Kitabu Chake na akaficha ili waja wasijue, Allah تعالى Atamhalalishia udhalili duniani na kuunganishwa na hilo hadi Akhera.

Kauli ya Allah تعالى;

سَاءَ مَثَلًا الْقَوْمُ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا

“Huu ni mfano muovu kabisa wa watu wanaokanusha ishara Zetu”.

Allah تعالى Anasema, mfano wa kaumu inayokadhibisha ishara Zetu ni mbaya, kiasi kuweza kushabihishwa na mbwa ambaye hana kusudio jingine lolote, isipokuwa kujipatia chakula na matamano ya nafsi yake.

Mwenye kufuata matamano yake naye, hushabihishwa na mbwa, na huo ni mfano mbaya mno.

Imethibiti Hadithi katika *Sahih* Mbili juu ya kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَيْسَ لَنَا مَثَلُ السَّوْءِ، أَلْعَائِدُ فِي هَيْبَةِ كَالْكَلْبِ يَعْرُدُ فِي قَبِيهِ»

*“Mfano mbaya si stahiki yetu, mtu anayeirudia hiba yake ni kama mbwa anayekula matapishi yake”.*¹

Kauli ya Allah تعالى;

وَأَنْفُسَهُمْ كَانُوا يَظْلِمُونَ

“...na wakajidhulumu nafsi zao”.

¹ Fat'hul Al-Bari 5:288.

Maana: Allah تعالى Hakuwadhulumu bali wao walijidhulumu wenyewe kwa kuacha kwao kufuata uongofu na kumtii Allah تعالى, na kuridhika na maisha haya ambayo hivi karibuni tu, yatafika ukomo, na wakati huo huo wakijielekeza katika kutimiza utashi na kuwafikiana na ghururi.

مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِيٌّ وَمَنْ يُضِلِّمْ فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٧٨﴾

178. Yule ambaye Mwenyezi Mungu Amemhidi basi huyo amehidika; na aliowaacha kupotea basi hao ndio waliokhasirika”.

Allah تعالى Anasema kuwa yule ambaye Allah تعالى Amemuongoza, basi hapana wa kumpotosha, na yule ambaye Allah تعالى Amempotosha, basi amefeli na amepata khasara na amepotea upotevu halisi,. Kwani kwa hakika, Akitakacho Allah تعالى huwa na Asichokitaka hakiwi.

Kwa ajili hiyo, Hadithi iliyosimuliwa na Ibn Mas'ud رضي الله عنه inaeleza;

«إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ نَحْمَدُهُ وَنُسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغِيثُهُ وَنَسْتَهْدِيهِ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ وَمَنْ يُضِلِّ اللَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ»

“Sifa zote Anazistahiki Allah تعالى, Ambaye tunamsifu, tunamuomba msaada, Hidaya, maghfira. Na tunajikinga kwa Allah تعالى dhidi ya shari za nafsi zetu na dhidi ya amali zetu mbaya. Yule Ambaye Allah تعالى Amemhidi, hatakuwa na wa kumpoteza, na yule ambaye Amempoteza hapana wa kumhidi. Na ninatoa shahada kwamba; Hapana mola wa haki wa kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى, na ninatoa shahada kwamba Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake”.

Hadithi kamili imekusanywa na Imamu Ahmad na wakusanyaji wa Sunan na wengine¹.

* * *

¹ Ahmad 1:392, Abu Dawud 2:591, Tuhfat Al-Awadhi 4:237, An-Nasai 3:105 na Ibn Majah 1:609.

Khamsini. Sawa na ilivyoandikwa katika *Sahih* Muslim, kuwa 'Abdullah bin 'Amiri رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ اللَّهَ قَدَّرَ مَقَادِيرَ الْخَلْقِ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِخَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ
وَتَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ»

*"Hakika Allah تعالى Alipitisha makadirio ya vipimo vya viumbe tangu kabla hajaziumba mbingu na ardhi kwa muda wa miaka Hamsini elfu, na Arshi Yake ilikuwa juu ya maji"*¹.

Hadithi zinazozungumzia mada hii ni nyingi, na masuala ya kudura ni makubwa, hapa si mahala pa kuyarefusha. Kauli ya Allah تعالى.

هُمْ قُلُوبٌ لَا يَفْقَهُونَ بِهَا وَهُمْ أَعْيُنٌ لَا يُبْصِرُونَ بِهَا وَهُمْ آذَانٌ لَا يَسْمَعُونَ بِهَا

"Wana nyoyo, lakini hawafahamu kwazo. Na wana macho, lakini hawaoni kwayo. Na wana masikio, lakini hawasikii kwayo".

Kwa maana: Hawanufaiki chochote kwa viungo hivyo vya mwili ambavyo Allah تعالى Alivijaalia viwe visababishi vya Hidaya. Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine;

وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَأَبْصَرَ وَأَفِيدَةً فَمَا آغَىٰ عَنْهُمْ سَمْعُهُمْ وَلَا أَبْصَرُهُمْ وَلَا أُفِيدَتُهُمْ مِنْ شَيْءٍ إِذْ كَانُوا سَاجِدُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ

"...na Tuliwapa masikio, na macho, na nyoyo. Na hayakuwafaa kitu masikio yao, wala macho yao, wala nyoyo zao kwa lolote. Kwani hao walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu". (46:26) na;

صُمُّ بِكُمْ عُمَىٰ فَهُمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿١٨﴾

"Viziwi, mabubu, vipofu kwa hivyo hawatarejea". (2:18)

Hii ni kwa upande wa wanafiki. Ama kwa upande wa makafiri, Allah تعالى Alisema;

صُمُّ بِكُمْ عُمَىٰ فَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ

"...ni viziwi, mabubu, vipofu kwa hivyo hawaelewi". (2:171)

¹ Muslim 4:2044.

Wala hawakuwa Viziwi wala mabubu wala vipofu kama wajulikanavyo, isipokuwa dhidi ya uongofu. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

﴿وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَأَسْمَعَهُمْ ۗ وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ لَتَوَلَّوْا وَهُمْ مُّعْرِضُونَ﴾

“Na Mwenyezi Mungu Angelijua wema wowote kwao Angewasikilizisha na lau Angewasikilizisha wangeligeuka wakapuza”. (8:23)

﴿فَإِنهَا لَا تَعْمَىٰ الْأَبْصَارُ وَلَكِن تَعْمَىٰ الْقُلُوبُ الَّتِي فِي الصُّدُورِ﴾

“Kwani hakika si macho yanayopofuka. Lakini zinazopofuka ni nyoyo zilizomo vifuni”. Na;

﴿وَمَنْ يَعْشُ عَنْ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقَيِّضْ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ﴾ ﴿وَأَنَّهُمْ لِيَصُدُّوهُمْ عَنِ السَّبِيلِ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ مُّهْتَدُونَ﴾

“Anayefanyia upofu maneno ya Rahmani Tunamuekea Shetani kuwa ndiye rafiki yake. Na hakika wao wanawazuilia Njia na wenyewe wanadhani kuwa wameongoka”. (43:36-37)

Kauli ya Allah تعالى:

﴿أُولَئِكَ كَالْأَنْعَامِ﴾

“Hao ni kama nyama howa.” Kwa maana: Hao hawaisikii haki, wala hawaifahamu, wala hawauoni uongofu, ni kama wanyama wanaochungwa ambao hawanufaiki na hisia hizi isipokuwa kile kinachowakimu katika maisha haya ya duniani. Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

﴿وَمَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا كَمَثَلِ الَّذِي يَنْعِقُ بِمَا لَا يَسْمَعُ إِلَّا دُعَاءً وَنِدَاءً﴾

“Na mfano wa waliokufuru ni kama mfano wa anayempigia kelele asiyesikia ila wito na sauti tu”. (2:171)

Na kwamba, mfano wao wakati wanapoitwa katika imani ni kama mifugo inapoitwa na mchungaji, Hawasikii chochote isipokuwa sauti yake, wala haifahamu, anachokisema. Kwa ajili hii Aliwazungumzia hao;

﴿بَلْ هُمْ أَضَلُّ﴾

“...bali wao ni wapotofu zaidi”. Kwa maana: Kuliko wanyama kwa sababu hao huweza kuitikia wito wa mchungaji wao, hata kama hawayafahamu maneno

yake, kinyume na hao waliokufuru. Pia wanyama hufanya yale waliyoambiwa, ima kwa malengo ya kuumbwa kwao ama kwa kutumikishwa, tofauti na kafiri, ambaye ameumbwa kwa ajili ya kumuabudu Allah تعالى na kumpwekesha, akamkanusha Allah تعالى na akamkasirisha. Minajili hii, kiumbe atakayemtii Allah تعالى atakuwa mbora zaidi kuliko aliye mfano wake katika malaika wakati wa kurejea kwake, na wanyama ni bora kuliko wanaomkufuru Allah تعالى. Kwa ajili hii Allah تعالى Alisema;

أُولَئِكَ كَالَّذِينَ نَفَعْنَا آلَهُمْ آيَاتِنَا فَكَفَرُوا بِهَا أُولَئِكَ كَانُوا فِي أَعْيُنِنَا وَأُولَئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ

“Hao ni kama nyama howa, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walioghafilika”.

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا ۖ وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِمْ سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٨٠﴾

180. Na Mwenyezi Mungu Ana Majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo. Na waacheni wale wanaoharibu Utakatifu wa Majina Yake. Hao watakuja lipa waliyokuwa wakiyatenda.

Ubainifu wa Majina Mazuri ya Allah تعالى.

Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ لِلَّهِ تِسْعًا وَتِسْعِينَ اسْمًا مِائَةً إِلَّا وَاحِدًا، مَنْ أَحْصَاهَا دَخَلَ الْجَنَّةَ وَهُوَ وَتَرٌ يُجِبُّ الْوِزْرَ»

“Kwa hakika! Allah تعالى Ana majina tisini na tisa. Mia, kasoro moja. Atakayeyahifadhi, ataingia Janna. Na Yeye ni Al-Witri na Anapenda witri (katika vitu)”. Sahihi Mbili zilinukuu Hadithi hii.¹

Halafu ijulikane kuwa Majina Mazuri ya Allah تعالى tisini na tisa tu, kwa ushahidi wa aliyoyasimulia Imamu Ahmad katika *Musnad* wake kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema Mtume ﷺ alisema;

«مَا أَصَابَ أَحَدًا قَطُّ هَمٌّ وَلَا حَزَنٌ فَقَالَ: اللَّهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ، ابْنُ أُمَّتِكَ، نَاصِيَتِي بِيَدِكَ مَاضٍ فِيَّ حُكْمُكَ، عَدْلٌ فِيَّ قَضَاؤُكَ، أَسْأَلُكَ بِكُلِّ اسْمٍ هُوَ لَكَ سَمَّيْتَ بِهِ

¹ Fat’hul Al-Bari 5:4717 na 11:218 na Muslim 4:2062.

تَنَسَّكَ أَوْ أَنْزَلْتَهُ فِي كِتَابِكَ أَوْ عَلَّمْتَهُ أَحَدًا مِنْ خَلْقِكَ أَوْ اسْتَأْذَنْتَ بِهِ فِي عِلْمِ الْغَيْبِ
عِنْدَكَ أَنْ تَجْعَلَ الْقُرْآنَ الْعَظِيمَ رِيبَ قَلْبِي، وَتُورَ صَدْرِي، وَجَلَاءَ حُزْنِي، وَذَمَّابِ
هَمِّي، إِلَّا أَذْهَبَ اللَّهُ حُزْنَتهُ وَهَمَّهُ وَأَبْدَلَ مَكَانَهُ قَرَحًا،

*"Kamwe, hapana aliyepatwa na majonzi na huzuni kisha akasema,
"Ewe Mola wangu! Mimi ni mja Wako mwana wa mjakazi Wako.
Utosi wangu uko Mkononi Mwako. Hukumu Yako juu yangu itapita.
Hukumu Yako kwangu ni ya uadilifu. Nakuomba kwa kila Jina Lako
Ulilojiita Nafsi Yako au Ulilolishusha katika Kitabu Chako au
Ulilomfundisha yeyote katika viumbe Wako au Ulilolihifadhi katika
Elimu ya ghaibu uliyo nayo. Uijaalie Qur'an Tukufu iwe chemchem
ya moyo wangu, na nuru ya kifua changu, kitu cha kuniondolea
huzuni na majonzi yangu. Isipokuwa Allah تعالی Humuondolea huzuni
na majonzi yake na Atambadilishia hali yake na kuwa ya furaha".*

Pakasemwa, "Ewe Mjumbe wa Allah! Tuelimishe maneno haya?" Akasema;

«بَلَىٰ يَنْبَغِي لِكُلِّ مَنْ سَمِعَهَا أَنْ يَتَعَلَّمَهَا»

"Ndiyo. Inatakikana kwa kila aliyoyasikia ajifundishe".¹

Al-'Awfi alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Ayah;

وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ

"Na waacheni wale wanaoharibu Utakatifu wa Majina Yake".

Alisema, "Ni ukanushaji kumuita Allah تعالی kwa majina yasiyo laiki yake, kwa kusema kuwa *Al-Lat* (sanamu) limetokana na Majina ya Allah تعالی². Ibn Jurayji alisema amepokea kutoka kwa Mujahid alisema;

وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ

"Na waacheni wale wanaoharibu Utakatifu wa majina yake".

"Wamenyambulisha jina *Al-Lat* (jina la sanamu) kutokana na Jina la Allah تعالی, na *Al-'Uzza* (sanamu jingine) kutokana na Jina *Al-'Aziz* (Mwenye Uwezo)".³

¹ Ahmad 1:391.

² At-Tabari 13:282.

³ At-Tabari 13:283.

Qatadah alisema, "Maana ya neno *Yalhidun*, wanamshirikisha Allah تعالى katika Majina Yake".¹ Neno *Ilhad*, katika lugha ya kiarabu, maana yake ni mchepuko dhidi ya kusudio, kukengeuka, ujeuri na kwenda upogo. Pia kuna neno *Al-Had*, katika kaburi, ambalo limeitwa hivyo badala ya kuitwa *Al-Hufr* (shimo) kwa sababu ni shimo ndani ya shimo, ambalo limeelekea Kibla.

وَمِمَّنْ خَلَقْنَا أُمَّةً يَهْدُونَ بِالْحَقِّ وَبِهِ يَعْدِلُونَ ﴿١٨١﴾

181. Na katika Tuliowaumba wako watu wanaoongoza kwa Haki, na kwayo wanafanya uadilifu.

Allah تعالى Alisema;

وَمِمَّنْ خَلَقْنَا

"Na katika Tuliowaumba". Allah تعالى Anasema;

أُمَّةً

"...wako watu". Walio madhubuti katika haki, kwa kauli na vitendo.

يَهْدُونَ بِالْحَقِّ

"...wanaoongoza kwa Haki". Wako imara nayo na wanalingania kwamba ifuatwe.

وَبِهِ يَعْدِلُونَ

"...na kwayo wanafanya uadilifu". Wanaenda na kuhukumu. Ilisimuliwa kuwa makusudio ya Aya hii ni Umma wa Muhammad ﷺ. Katika *Sahih* Mbili kuna nukuu kutoka kwa Mu'awiyah bin Abu Sufyan رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema;

«لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي ظَاهِرِينَ عَلَى الْحَقِّ لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَذَلَهُمْ وَلَا مَنْ خَالَفَهُمْ حَتَّى تَقُومَ السَّاعَةُ»

"Kipindi chote litaendelea kuwepo kundi katika Umma wangu ambalo litakuwa dhahiri katika ukweli lisilodhuriwa na wanaowaangusha au kuwapinga mpaka itakaposimama Saa ya (Mwisho)".

Katika masimulizi mengine;

¹ At-Tabari 13:283.

«حَتَّىٰ يَأْتِيَٰ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ عَلَىٰ ذَٰلِكَ»

“Mpaka Amri ya Allah تعالى (Saa ya Mwisho) ifike, na wao wakiwa vivo hivyo”.

Katika masimulizi mengine;

«وَهُمْ بِالشَّامِ»

“Na watakuwa wanakaa Sham (Syria)”.¹

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا سَنَسْتَدْرِجُهُم مِّنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٧٢﴾ وَأُمْلِي لَهُمْ إِنَّ كَيْدِي مَتِينٌ ﴿١٧٣﴾

182. Na wale waliokadhibisha Ishara Zetu, Tutawapururia pole pole kwa namna ambayo wenyewe hawajui.

183. Nami Nitawapa muda. Hakika Mpango Wangu ni madhubuti”.

Kauli ya Allah تعالى:

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا سَنَسْتَدْرِجُهُم مِّنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٧٢﴾

“Na wale waliokadhibisha Ishara Zetu, Tutawapururia pole pole kwa namna ambayo wenyewe hawajui”.

Maana yake: Ni kuwa, Allah تعالى Atawafungulia milango ya riziki na njia za maisha ya duniani mpaka wahadaike na watakayokuwa nayo na kujiona kwamba wako sahihi. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَلَمَّا دَسُّوا مَا دُكِّرُوا بِهِ فَتَحْنَا عَلَيْهِمَ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا أَخَذْنَاهُمْ بَغْتَةً فَإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ ﴿١٤٤﴾ فَقُطِعَ دَابِرُ الْقَوْمِ الَّذِينَ ظَلَمُوا ﴿١٤٥﴾ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٤٦﴾

“Basi waliposahau waliokumbushwa Tuliwafungulia milango ya kila kitu. Mpaka walipofurahia yale waliyopewa Tuliwashika kwa ghafila, na mara wakawa wenye kukata tamaa. Ikatwa mizizi ya watu waliodhulumu – na wa Kuhimidiwa ni Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote”. (6:44-45)

¹ Fat’hul Al-Bari 13:451 na Muslim 3:1524.

Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema;

وَأْمَلِي لَهُمْ

“Nami Nitawapa muda”. Kwa maana: Nitawarefushia yale waliyomo ndani yake.

إِن كَيْدِي مَتِينٌ

“Hakika mpango wangu ni madhubuti”. Kwa maana: Una nguvu kubwa.

أُولَٰمَ يَتَفَكَّرُونَ ۗ مَا بِصَاحِبِهِم مِّنْ جِنَّةٍ ۗ إِن هُوَ إِلَّا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿١٨٤﴾

184. Je, hawafikirii? Huyu mwenzao hana wazimu. Hakuwa yeye ila ni Mwonyaji aliye dhahiri.

Allah تعالی Anasema;

أُولَٰمَ يَتَفَكَّرُونَ ۗ

“Je, hawafikirii?” Hao wakadhibishao Ayah zetu.

مَا بِصَاحِبِهِم

“Huyu mwenzao”. Kwa maana: Muhammad ﷺ.

مِّنْ جِنَّةٍ ۗ

“...hana wazimu”. Hana mbulu, bali yeye ni kweli Mjumbe kutoka kwa Allah تعالی, mwenye kulingania katika haki.

إِن هُوَ إِلَّا نَذِيرٌ مُّبِينٌ

“Hakuwa yeye ila ni Mwonyaji aliye dhahiri”. Kwa maana: Yuko dhahiri kwa mwenye akili na moyo ambao anautumia kwa ajili ya kuelewa na kuhifadhi. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی;

وَمَا صَاحِبِكُمْ بِمَجْنُونٍ ﴿١٨٥﴾

“Na wala huyu mwenzenu hana wazimu”. (81:22) na;

* قُلْ إِنَّمَا أَعْطَيْتُكُمْ بِوَأْحِدَةٍ ۗ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مِثْلَىٰ مِثْلَىٰ وَفَرَادَىٰ ۗ ثُمَّ تَتَفَكَّرُونَ ۗ مَا بِصَاحِبِكُمْ

مِّنْ جِنَّةٍ ۗ إِن هُوَ إِلَّا نَذِيرٌ لَّكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ ﴿١٨٥﴾

“Sema: Mimi nakunasihini kwa jambo moja tu – ya kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili – wawili na mmoja – mmoja; kisha mfikiri. Mwenzenu huyu hana wazimu. Yeye si chochote ila ni Mwonyaji kabla ya kufikia adhabu kali”. (34:46)

Anasema, "Ninalolitaka kwenu ni, msimame kwa kisimamo cha ikhlasi, hakuna ugumu wala ukaidi ndani yake.

مَتَّقِيْ وَفِرَادِيْ

"...wawili – wawili na mmoja – mmoja". (34:46) Kwa maana: Kwa pamoja na kwa mmoja mmoja.

أَوْلَمْ يَتَّفَكَّرُوا

"...kisha mfikiri". (34:46) Kuhusu huyu aliyekuleteeni ujumbe kutoka kwa Allah تعالى, kwamba ana wazimu ama la. Mtakapofanya hayo, itawadhihirikieni kuwa kweli yeye ni Mtume wa Allah تعالى. Qatadah bin Di'amah alisema, "Tulitajiwa kuwa Mtume ﷺ alikuwa Swafaa, akawaita Makuraishi, kisha ikawa anaita kabila baada ya kabila, kwa kusema;

«يَا بَنِي فُلَانٍ، يَا بَنِي فُلَانٍ فَحَدَّرَهُمْ بِأَسْمَاءِ اللَّهِ وَوَقَائِعِ اللَّهِ»

"Enyi Banu fulani". Akawaonya juu ya nguvu na uwezo wa Allah تعالى.

Mmoja wao akasema, "Sahibu yenu huyu ni majununi". Aliendelea kupiga kelele mpaka asubuhi. Allah تعالى Akateremsha;

أَوْلَمْ يَتَّفَكَّرُوا مَا بِصَاحِبِهِمْ مِّنْ جَنَّةٍ إِن هُوَ إِلَّا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿١٨٤﴾

"Je, hawafikiri? Huyu mwenzao hana wazimu. Hakuwa yeye ila ni Mwonyaji aliye dhahiri". (7:184)

أَوْلَمْ يَنْظُرُوا فِي مَلَكُوتِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا خَلَقَ اللَّهُ مِنْ شَيْءٍ وَأَنْ عَسَى أَنْ يَكُونَ قَدِ اقْتَرَبَ أَجْلُهُمْ فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَهُ يُؤْمِنُونَ ﴿١٨٥﴾

185. Je hawatazami Ufalme wa mbingu na ardhi, na vitu Alivyo viumba Mwenyezi Mungu, na pengine ajali yao imekwisha karibia? Basi maneno gani baada ya haya watayaamini?"

Allah تعالى Anasema, Je hao wakadhibishao Aya zetu hawaangalii Ufalme na Nguvu za Allah تعالى mbinguni na ardhini, na katika vitu Alivyoviumba, basi wakapata mazingatio na wajue kuwa hayo ni kwa ambaye hana wa kumsimamia wala wa kushabihiana? Mwenye kuyafanya hayo Ndiye Anayestahiki kuabudiwa na Ndiye Mwenye Dini halisi, basi wamuamini na kumsadiki Mtume Wake ﷺ, na warejee katika kumtii Allah تعالى na wawakane washirika na masanamu. Pia waonywe kuwa uhai wao umekaribia kufikia

mwishoni na wataangamizwa kwa ukafiri wao na hivyo kujikuta katika adhabu ya Allah تعالى na mateso yake makali. Kauli ya Allah تعالى:

فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَهُ يُؤْمِنُونَ

“Basi maneno gani baada ya haya watayaamini?” Anasema, kuhofishwa, kuonywa, kutishiwa kupi baada ya tahadhari na vitisho alivyoeleza Muhammad ﷺ, alivyowaletea kutoka kwa Allah تعالى, katika Ayah nyingi zilizomo ndani ya Kitabu Chake, ambazo watazisadiki, iwapo hawakuyasadiki mazungumzo haya ambayo aliwajia nayo kutoka kwa Allah? Kisha Allah تعالى Akasema;

مَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَيَذُرْهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١٨٦﴾

186. Aliyemuacha Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumuongoa. Atawaacha hao wakitangatanga katika upotofu wao.

Allah تعالى Anasema: Atakavyowaandikia upotevu, hapana wa kuwaongoza, hata kama watajitahidi sana ila waupate uongofu huo, hiyo haitawatoshia kitu.

وَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ فِتْنَتَهُ فَلَنْ تَمْلِكَ لَهُ مِنْ أَلَيْسَ شَيْئًا

“Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu Anataka kumfitini hawezi kuwa na madaraka naye mbele ya Mwenyezi Mungu”. (5:41)

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

قُلْ أَنْظَرُوا مَاذَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ وَالنُّذُرُ عَنْ قَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٨٧﴾

“Sema: Angalieni yalio mbinguni na kwenye ardhi! Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasioamini”. (10:101)

يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسَلُهَا قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ رَبِّي لَا يُجِيبُهَا لَوْ قُبِحَ إِلَّا هُوَ ۗ ثَقُلَتْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا تَأْتِيكُمْ إِلَّا بَغْتَةً ۗ يَسْأَلُونَكَ كَأَنَّكَ حَفِيٌّ عَنْهَا قُلْ إِنَّمَا

عِلْمُهَا عِنْدَ اللَّهِ وَلَكِنْ أَكْثَرُ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٨٧﴾

187. “Wanakuuliza hiyo Saa (ya mwisho) itakuwa lini? Sema: Kuijua kwake kuko kwa Mola Mlezi wangu. Haidhihirishi hiyo kwa wakati wake ila Yeye. Ni nzito katika mbingu na ardhi. Haikujini ila kwa ghafla tu. Wanakuuliza kama kwamba wewe una pupa ya kujua.

Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Lakini aghalabu ya watu hawajui”.

Ubainifu wa Saa ya Mwisho na Ishara Zake.

Allah تعالی Anasema;

يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ

“Wanakuuliza hiyo Saa (ya mwisho)”.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

يَسْأَلُكَ النَّاسُ عَنِ السَّاعَةِ

“Watu wanakuuliza khabari ya Saa (ya Kiyama)” (33:63)

Ilisemwa: Ayah hii ilishushwa kuwahusu Makuraishi. Pia ilisemwa, ni juu ya kikundi cha Mayahudi. Maoni ya kwanza yana nguvu zaidi kwani Ayah hiyo ilishushwa Makkah, ambapo Makuraishi walikuwa wakiuliza juu ya muda wa kutokea Saa, kwa sababu walikuwa wakiikanusha na kukadhibisha kutokea kwake. Sawa na Kauli ya Allah تعالی:

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٨﴾

“Na wanasema: Lini ahadi hii, ikiwa mnasema kweli?” (10:48)

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا وَالَّذِينَ آمَنُوا مُشْفِقُونَ مِنْهَا وَيَعْلَمُونَ أَنَّهَا الْحَقُّ

أَلَا إِنَّ الَّذِينَ يُمَارُونَ فِي السَّاعَةِ لَفِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿٤٩﴾

“Wasioamini huimiza hiyo Saa ifike upesi; lakini wanaoamini wanaiogopa, na wanajua kwamba hakika hiyo ni kweli. Ama kwa hakika hao wanaobishana katika khabari za hizo saa wamo katika upotofu wa mbali kabisa”. (42:18)

Kauli ya Allah تعالی:

أَيَّانَ مُرْسِنَهَا

“...itakuwa lini?” ‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa ‘Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mwisho wake”¹. Maana: ni lini utakuwa mwisho wake na lini utakuwa mwisho wa dunia, ambao ndio mwanzo wa tukio la Saa.

¹ At-Tabari 13:294.

قُلْ إِنَّمَا عَلَّمَهَا عِنْدَ رَبِّي لَا يُجَلِّبُهَا لَوْ قَتَبَا إِلَّا هُوَ

“Sema: Kujua kwake kuko kwa Mola Mlezi wangu. Haidhihirishi hiyo kwa wakati wake ila Yeye”.

Allah تعالی Alimuamuru Mtume Wake ﷺ kuwa akiulizwa juu ya Saa aseme Allah تعالی Ndiye Anayejua. Yeye Ndiye Anayeidhihiri wakati wake utakapowadia, maana Anajua uwazi wa jambo hilo na lini hasa litatukia. Hapana ayajuaye hayo, isipokuwa Allah تعالی tu. Kwa ajili hiyo, Allah تعالی Alisema;

ثُقُلْتَ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ni nzito katika mbingu na ardhi”.

‘Abdur-Rahman bin Ma’mar alisema kuwa Qatadah aliizungumzia Aya;

ثُقُلْتَ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ni nzito katika mbingu na ardhi”.

Alisema, “Ujuzi Wake, umekuwa mzito kwa wakazi wa mbinguni na ardhini, kwamba wao hawajui”.¹ Ma’mar alisema Al-Hasan alisema, “Itakapofika saa, itakuwa nzito kwa wakazi wa mbinguni na wa ardhini, yaani itakuwa ni jambo kubwa kwao”.² Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالی;

ثُقُلْتَ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ni nzito katika mbingu na ardhi”.

Akasema, “Kila kiumbe atapatwa na madhara ya Siku ya Kiyama”. Ibn Jurayj alisema;

ثُقُلْتَ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ni nzito katika mbingu na ardhi”.

Kwamba, “Itakapokuja, mbingu zitapasuka, nyota zitapukutika, jua litakunjwakunjwa, milima itaendeshwa na yote Aliyoyasema Allah تعالی yatatukia. Basi huo ndio uzito wake”. As-Suddi alisema;

¹ Abdur-Razzaq 2:244.

² Abdur-Razzaq 2:245.

ثُقُلَتْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ^١

“Ni nzito katika mbingu na ardhi”. Kwa maana: “Elimu Yake imejificha mbinguni na ardhini, basi si Malaika wala Nabii Mtume ajuaye lini itatukia”¹.

لَا تَأْتِيكُمْ إِلَّا بَغْتَةً^٢

“Haikujini ila kwa ghafla tu”.

Saa itawatokezea kwa ghafla, kitawashtukizia. Qatadah aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى kuwa, “Amepitisha Uamuzi kuwa hiyo Saa;

لَا تَأْتِيكُمْ إِلَّا بَغْتَةً^٢

“Haikujini ila kwa ghafla tu”.

Kwa kusema, “Tuliambiwa kwamba Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ السَّاعَةَ تَهِيحُ بِالنَّاسِ، وَالرَّجُلُ يَضِلُّ حَوْضَهُ وَالرَّجُلُ يَسْقِي مَا شِئْتَهُ، وَالرَّجُلُ يُقِمُّ سِلْعَتَهُ فِي السُّوقِ وَيَخْفِضُ مِيزَانَهُ وَيَرْفَعُهُ»

“Saa itawashitukizia watu kwa ghafla ambapo mmoja wapo atakuwa akikarabati dimbwi lake la maji, mwingine akiwanyweshwa wanyama wake, mwingine akiweka vyema bidhaa zake sokoni na mwingine anapandisha na kushusha Mizani yake (kuuza na kununua)”².

Al-Bukhari alinukuu kupitia kwa Abu Hurayrah kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى تَطْلُعَ الشَّمْسُ مِنْ مَغْرِبِهَا، فَإِذَا طَلَعَتْ فَرَأَاهَا النَّاسُ آمَنُوا أَجْمَعُونَ، فَذَلِكَ جِئِنَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيمَانُهَا لَمْ تَكُنْ آمَنَتْ مِنْ قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيمَانِهَا خَيْرًا، وَلَتَقُومَنَّ السَّاعَةُ وَقَدْ نَشَرَ الرَّجُلَانِ ثَوْبَهُمَا بَيْنَهُمَا، فَلَا يَبْتَاعَانِهِ وَلَا يَطْوِيَانِهِ. وَلَتَقُومَنَّ السَّاعَةُ وَقَدْ انْصَرَفَ الرَّجُلُ بِلَبَنِ لِفْحِيهِ فَلَا يَطْعَمُهُ، وَلَتَقُومَنَّ السَّاعَةُ وَهُوَ يَلِيطُ حَوْضَهُ فَلَا يَسْقِي فِيهِ، وَلَتَقُومَنَّ السَّاعَةُ وَالرَّجُلُ قَدْ رَفَعَ أَكْلَتَهُ إِلَى فِيهِ فَلَا يَطْعَمُهَا»

“Saa haitasimama mpaka lichomoze jua kutokea kwenye machweo yake. Litakapochochoza hivyo, na watu wakalionga wote, basi huo

¹ At-Tabari 13:295.

² At-Tabari 13:297. Maana ya Hadithi hii inaungwa mkono na hii inayofuata.

ndio wakati ambao nafsi haitanufaika ikiwa haikuwa ilikwishaamini au kujinufaisha na kheri yoyote. Saa itatukia na kuwakuta watu wawili wakiwa wamejikunjulia nguo, wala wasiweze kuuziana (na kuwa na muda wa kuridhiana bei yake) wala kuikunja. Pia itatukia, na kumkuta mtu akiwa amekwisha mkamua mnyama wake maziwa na asiweze kuyanywa. Tena itatukia na kumkuta mtu akilikarabati dimbwi lake la maji, lakini asipate muda wa kulitumia. Na itatukia na kumkuta mtu akiwa amelinyanyua tonge lake kinywani, lakini asipate muda wa kulila".¹

Al-'Awfi alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema juu ya;

يَسْأَلُونَكَ كَأَنَّكَ حَفِيٌّ عَنْهَا

"Wanakuuliza kama kwamba wewe una pupa ya kujua".

"Kana kwamba baina yako na wao kuna mapenzi, kama vile, wewe ni rafiki yao". Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Pindi watu walipomuuliza Nabii juu ya Kiyama, walimuuliza kama vile wanamuona Muhammad ﷺ kuwa ni rafiki yao. Allah تعالى Akampa wahyi kwamba elimu ya hilo ipo kwa Allah تعالى, na wala Hakumjulisha Malaika wa karibu wala Mtume yeyote."²

يَسْأَلُونَكَ كَأَنَّكَ حَفِيٌّ عَنْهَا

"Wanakuuliza kama kwamba wewe una pupa ya kujua".

Kwa maana: Ukawa na pupa ya kuuliza mpaka ukajua wakati wake. Na kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema;

قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ اللَّهِ وَلَئِنْ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

"Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Lakini aghalabu ya watu hawajui".

Pia ni kwa ajili hiyo, alikuja Jibril katika sura ya bedui ili awafundishe watu Dini yao. Akakaa karibu ya Mtume ﷺ mkao wa muulizaji anayetaka kuelekezwa. Akamuuliza Mtume ﷺ juu ya Uislamu, kisha juu ya Imani, kisha juu ya Ihsani.

¹ Fat'hul Al-Bari 11:360.

² At-Tabari 13:298.

Kisha akauliza, “Kiyama kitawadia lini?” Mtume ﷺ alisema;

«مَا الْمَسْئُولُ عَنْهَا بِأَعْلَمَ مِنَ السَّائِلِ»

“Muulizwaji si mwenye ujuzi nayo zaidi ya muulizaji”.

Kwa maana: Mimi sina ujuzi nayo zaidi yako, wala hakuna mmoja wapo ajuaye zaidi ya mwingine. Kisha Mtume ﷺ alisoma;

إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ

“Hakika kujua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu”.

(31:34)

Katika masimulizi mengine, akamuuliza juu ya ishara za Kiyama, akambainishia ishara za Kiyama. Kisha akasema;

«فِي خَمْسٍ لَا يَعْلَمُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ»

“Mambo matano hakuna ayajuaye isipokuwa Allah”.

Na akaisoma Ayah hii. Na katika yote haya alikuwa akimuambia, “Umesema kweli”, baada ya kila jibu. Hili likawastaajabisha masahaba kwamba huyu anauliza, halafu anamkubalia. Kisha baada ya kuondoka, Mtume ﷺ akasema;

«هَذَا جِبْرِيلُ أَنَا كُمْ يُعَلِّمُكُمْ دِينَكُمْ»

“Huyu ni Jibril amekujieni kukufundisheni Dini yenu”.

Na katika masimulizi mengine;

«وَمَا أَنَا فِي صُورَةٍ إِلَّا عَرَفْتُ فِيهَا إِلَّا صُورَتَهُ هَذِهِ»

“Hajawahi kunijia kwa sura yoyote bali nilimjua isipokuwa hii”.¹

Muslim alinukuu katika *Sahih* yake kuwa ‘Aishah رضي الله عنها alisema, mabedui walipokuwa wakija kwa Mtume ﷺ, walikuwa wakimuuliza juu ya Kiyama, “Ni lini Kiyama kitatukia?” Kisha Mtume ﷺ akimtazama mdogo zaidi kuliko wao na kusema;

¹ Fat’hul Al-Bari 1:140

«إِنْ يَعْشُرْ هَذَا لَمْ يُدْرِكْهُ الْهَرَمُ حَتَّى قَامَتْ عَلَيْكُمْ سَاعَتُكُمْ»

“Akiishi kijana huyu, huenda hatapatwa na uzee kabla Kiyama chenu hakijasimama”.¹

Kwa maana: Kwa kufanya hivyo, alikuwa akikusudia mwisho wa umri wao ambao unawafanya waingie katika maisha ya *Barzakh*, ambayo ni maisha baina ya duniani na Akhera. Muslim pia aliinukuu kupitia kwa Anas رضي الله عنه, kuwa kuna mtu alimuuliza Mtume ﷺ, juu ya Saa. Mtume ﷺ akasema;

«إِنْ يَعْشُرْ هَذَا الْغُلَامُ فَعَسَى أَنْ لَا يُدْرِكْهُ الْهَرَمُ حَتَّى تَقُومَ السَّاعَةُ»

“Akiishi kijana huyu, huenda hatapatwa na uzee kabla Kiyama chenu hakijasimama”.²

Muslim peke yake aliinukuu.

Jabir bin 'Abdullah رضي الله عنه alisema, “Nilimsikia Mtume ﷺ akisema mwezi mmoja kabla hajafariki,

«تَسْأَلُونِي عَنِ السَّاعَةِ، وَإِنَّمَا عَلِمْتُهَا عِنْدَ اللَّهِ، وَأُقْسِمُ بِاللَّهِ مَا عَلَي ظَهْرِ الْأَرْضِ
الْيَوْمَ مِنْ نَفْسٍ مَنفُوسَةٍ تَأْتِي عَلَيْهَا مِائَةٌ سَنَةً»

“Mnaniuliza juu ya Saa, kwa hakika ujuzi wake uko kwa Allah تعالى. Naapa kwa Allah تعالى kuwa hakuna nafsi iliyo juu ya uso wa ardhi ambayo itaishi kwa miaka mia moja kuanzia sasa”.

Muslim aliinukuu. Na katika *Sahih* Mbili kuna Hadithi kupitia kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما na akasema, “Alichokimaanisha Mtume ﷺ ni kumalizika kwa kizazi kile kwa kuufikia muda uliopangwa, Imamu Ahmad alisimulia kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَقِيتُ لَيْلَةَ أُسْرِي بِي إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى وَعِيسَى، فَتَذَاكَرُوا أَمْرَ السَّاعَةِ - قَالَ -
فَرَدُّوا أَمْرَهُمْ إِلَى إِبْرَاهِيمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ، فَقَالَ: لَا عَلِمَ لِي بِهَا، فَرَدُّوا أَمْرَهُمْ إِلَى
مُوسَى فَقَالَ: لَا عَلِمَ لِي بِهَا، فَرَدُّوا أَمْرَهُمْ إِلَى عِيسَى فَقَالَ عِيسَى: أَمَّا وَجِبَّتُهَا
فَلَا يَعْلَمُ بِهَا أَحَدٌ إِلَّا اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ، وَبِمَا عَاهَدَ إِلَيَّ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ أَنْ الدَّجَالَ
خَارِجٌ - قَالَ - وَمَعِيَ قَضِيَّانِ، فَإِذَا رَأَيْتَ ذَابَ كَمَا يَذُوبُ الرَّصَاصُ، قَالَ: فَيُهْلِكُهُ

¹ Muslim 4:2269.

² Muslim 4:2270.

اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ إِذَا رَأَىٰ حَتَّىٰ إِنَّ الشَّجَرَ وَالْحَجَرَ يَقُولُ: يَا مُسْلِمُ إِنَّ تَخْبِي كَافِرًا
 فَتَعَالَ فَاقْتُلْهُ، قَالَ: فَيُهْلِكُهُمُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ ثُمَّ يَرْجِعُ النَّاسُ إِلَىٰ بِلَادِهِمْ وَأَوْطَانِهِمْ،
 قَالَ: فَعِنْدَ ذَلِكَ يَخْرُجُ بِأَجُوجَ وَمَاجُوجَ وَهُمْ مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ، فَيَطَّأُونَ
 بِلَادَهُمْ لَا يَأْتُونَ عَلَىٰ شَيْءٍ إِلَّا أَهْلَكَوهُ وَلَا يَمُرُّونَ عَلَىٰ مَاءٍ إِلَّا شَرِبُوهُ: قَالَ: ثُمَّ
 يَرْجِعُ النَّاسُ إِلَيَّ فَيَشْكُونَهُمْ فَأَدْعُو اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ عَلَيْهِمْ فَيُهْلِكُهُمْ وَيُمِيتُهُمْ حَتَّىٰ
 تَجُوزِيَ الْأَرْضُ مِنْ تَحْتِ رِجْلِهِمْ أَيْ تُتْرِكُ، قَالَ: فَيَتْرِكُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ الْمَطَرَ فَيَجْتَرِفُ
 أَجْسَادَهُمْ حَتَّىٰ يَقْدِفَهُمْ فِي الْبَحْرِ. قال يزيد بن هارون: ثُمَّ تُنْسَفُ الْجِبَالُ وَتُمَدُّ
 الْأَرْضُ مَدًّا الْأَدِيمِ، ثُمَّ رَجَعَ إِلَىٰ حَدِيثِ هُنَيْنِ، قَالَ: فَفِيمَا عَهْدَ إِلَيَّ رَبِّي عَزَّ
 وَجَلَّ أَنْ ذَلِكَ إِذَا كَانَ كَذَلِكَ، فَإِنَّ السَّاعَةَ كَالْحَامِلِ الْمِيَمِ لَا يَدْرِي أَهْلُهَا مَتَىٰ
 تُمْأَجُّهُمْ بِوَلَادَتِهَا قَلِيلًا أَوْ نَهَارًا»

“Katika usiku wa safari yangu ya Israa nilikutana na Ibrahim عليه السلام, Musa عليه السلام na Isa عليه السلام. Wakalitaja jambo la Saa. Wakamuuliza Ibrahim عليه السلام, akasema, “Mimi sina ujuzi nalo”. Wakamuuliza Musa عليه السلام, akasema, “Mimi sina ujuzi nalo”. Wakamuuliza Isa عليه السلام, akasema, “Kuhusu lini itatukia, basi hakuna ajuaye isipokuwa Allah, na katika Aliyoniahidi Allah ni kwamba Dajjal atatokeza, nami nitakuwa na fimbo mbili (mikuki). Atakaponiona, atayeyuka kama vile chuma kinavyoyeyuka. Basi Allah atamuangamiza mara baada ya kuniona, na miti na mawe vitasema, “Ewe Muislamu! Chini yangu kuna kafiri. Njoo umuue”. Basi Allah تعالى Atawahilikisha, kisha watu watarejea katika miji na nchi zao. Baada ya hapo watatokeza Ya’juj na Ma’juj, ambao watatembea kwa makundi makubwa kutoka katika kila kilima na kuidondosha miji yao na wala hawakiendei kitu, bali watu watanijia na kunilalamikia juu yao, nami, nitamuomba Allah تعالى, Atawaangamiza na kuwafisha mpaka ardhi itanuka kwa harufu mbaya. Kisha, Allah تعالى Atateremsha mvua ambayo itabeba miili yao na kuitupa baharini. Imamu Ahmad alisema kuwa Yazid bin Harun alisema kuwa, kisha milima italipuka, ardhi itatanuliwa mtanuko mkubwa. Kisha akarejea katika Hadithi ya Hushaim, akasema, “Miongoni mwa aliyonifahamisha Mola wangu, ni kuwa, itakapotokea hivyo, basi Kiyama kitakuwa ni kama mjamzito aliyetimiza muda wake,

familia yake hajui ni lini twashitukiza kuzaa kwake, itakuwa usiku, ama mchana".¹

Ibn Majah alisimulia sawa na hivyo². Hao ni Mitume wakubwa kabisa, hawana ujuzi juu ya wakati wa Kiyama kwa uwazi. Wao wamemuuliza Isa عليه السلام ambaye alizitaja ishara zake, kwa sababu atashuka katika kizazi cha mwisho cha ummah huu na atazitumia sheria za Mtume ﷺ, atamuua Dajjal. Allah تعالى Atawahilikisha Ya'juj na Ma'juj kwa baraka za dua yake. Kwa hivyo, Isa عليه السلام aliwajulisha juu ya khabari ambazo Allah تعالى Alimfundisha. Imamu Ahmad alisimulia kutoka kwa Hudhaifah رضي الله عنه, kwamba Mtume ﷺ aliulizwa juu ya Saa, akasema;

«عَلِمَهَا عِنْدَ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ لَا يُجَلِّيهَا لِوَقْتِهَا إِلَّا هُوَ، وَلَكِنْ سَأَخِيرُكُمْ بِمَشَارِبِهَا
وَمَا يَكُونُ بَيْنَ يَدَيْهَا، إِنَّ بَيْنَ يَدَيْهَا فِتْنَةٌ وَهَرَجًا»

"Elimu hiyo iko kwa Mola wangu, hapana wa kudhihirisha wakati wake, isipokuwa Yeye, lakini nitakupasheni juu ya ishara zake na yanayoambatana nayo, ambayo ni Fitnah (majaribio) na Harj".

Wakamuuliza, "Ewe Mjumbe wa Allah! Tunajua maana ya *Fitnah*, lakini *Haraj* ni nini?"

«بِلِسَانِ الْحَبَشَةِ الْقَتْلِ»

"Ina maana ya kuuana, katika lugha ya kihabeshi". Akaongeza kusema;

«وَرِئَقِي بَيْنَ النَّاسِ التَّنَائُرُ، فَلَا يَكَادُ أَحَدٌ يَعْرِفُ أَحَدًا»

"Litaenea baina ya watu jambo la utengano na upweke, na kwa hivyo, karibu kila mmoja hataweza kumjua mwingine".³

Hapana yeyote kati ya wakusanyaji wa vitabu sita vya *Sunan* aliyeikusanya Hadithi hii kwa kuitumia isnadi hii ya usimulizi. Twariq bin Shihab alisema, Mtume ﷺ alikuwa haachi kutaja jambo la Kiyama mpaka ikateremshwa;

يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسِنُهَا

"Wanakuuliza hiyo Saa (ya mwisho) itakuwa lini?"⁴

¹ Ahmad 1:375.

² Ibn Majah 2:1365.

³ Ahmad 5:389.

⁴ Fat'hul Al-Bari 11:355.

An-Nasai alinukuu Hadithi hiyo,¹ kwa isnadi nzuri yenye nguvu. Hivyo, Mtume huyu *Ummi*, ni mkuu wa Mitume, na mwisho wao, Muhammad ﷺ ni Nabii wa rehema, wa toba, wa *Al-Malhamah* (Angamizo kubwa kwa makafiri), *Al-'Aqib* (Aliyekuja baada ya Mitume wengi), *Al-Muafi* (Mwisho wa mfuatano), *Al-Haashir* (ambaye chini yake, watu wote watakusanywa katika Siku ya kujumuika wote). Pamoja na maneno yake Mtume ﷺ yaliyonukuliwa katika *Sahih* Mbili kupitia Hadithi ya Anas na Sahl bin Sa'd رضي الله عنهما;

«بُعِثْتُ أَنَا وَالسَّاعَةَ كَهَاتَيْنِ»

*“Nimeletwa mimi na Kiyama kama hivi viwili”.*²

Akavikutanisha vidole vyake, cha shahada na kinachofuatia. Pamoja na haya yote, Allah تعالی Alimuamuru jambo la Kiyama alirejesha Kwake pindi atakapoulizwa. Allah تعالی Alisema;

قُلْ إِنَّمَا عَلَّمُهَا عِنْدَ اللَّهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

“Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Lakini aghalabu ya watu hawajui”.

* * *

¹ At-Tabari 3:292.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:506.

قُلْ لَا أَمْلِكُ لِنَفْسِي نَفْعًا وَلَا ضَرًّا
 إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ ۗ وَلَوْ كُنْتُ
 أَعْلَمُ الْغَيْبِ لَاسْتَكْتَرْتُ مِنَ الْخَيْرِ وَمَا مَسَّنِيَ
 السُّوءُ ۗ إِنَّ أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ وَنَذِيرٌ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿١٨٨﴾ * هُوَ
 الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا
 لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا ۖ فَلَمَّا تَغَشَّيْهَا حَمَلَتْ حَمَلًا خَفِيًّا فَمَرَّتْ
 بِهِ ۖ فَلَمَّا أَثْقَلَتْ دَعَا اللَّهَ رَبَّهُمَا لَئِنْ آتَيْتَنَا صَالِحًا
 لَنُكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿١٨٩﴾ فَلَمَّا آتَتْهُمَا صَالِحًا
 جَعَلَ لَهُمْ شُرَكَاءَ فِيمَا آتَاهُمَا ۖ فَتَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ
 ﴿١٩٠﴾ أَيْشُرِكُونَ مَا لَا يَخْلُقُ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلَقُونَ ﴿١٩١﴾ وَلَا
 يَسْتَطِيعُونَ لَهُمْ نَصْرًا وَلَا أَنفُسُهُمْ يَنْصُرُونَ ﴿١٩٢﴾ وَإِنْ
 تَدْعُوهُمْ إِلَى الْهُدَىٰ لَا يَتَّبِعُوكُمْ ۖ سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ
 أَدْعَوْتُمُوهُمْ أَمْ أَن تَدْعُوهُمْ ۚ إِنَّ الَّذِينَ
 تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ عِبَادٌ أَمْثَلُكُمْ ۖ فَادْعُوهُمْ
 فَلْيَسْتَجِيبُوا لَكُمْ ۖ إِنَّ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٩٣﴾ أَلَهُمْ أَرْجُلٌ
 يَمْشُونَ بِهَا ۗ أَمْ لَهُمْ أَيْدٍ يَبْطِشُونَ بِهَا ۗ أَمْ لَهُمْ أَعْيُنٌ
 يُبْصِرُونَ بِهَا ۗ أَمْ لَهُمْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا ۗ قُلْ أَدْعُوا
 شُرَكَاءَكُمْ ثُمَّ كِيدُوا ۖ فَلَا تُنظِرُونِ ﴿١٩٤﴾

قُلْ لَا أَمْلِكُ لِنَفْسِي نَفْعًا وَلَا ضَرًّا
 إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ ۗ وَلَوْ كُنْتُ
 أَعْلَمُ الْغَيْبِ لَاسْتَكْتَرْتُ مِنَ الْخَيْرِ وَمَا
 مَسَّنِيَ السُّوءُ ۗ إِنَّ أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ وَنَذِيرٌ
 لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿١٨٨﴾

188. Sema: Siimilikii nafsi yangu manufaa wala madhara, ila Apendavyo Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ningejizidishia mema mengi, wala ovu lisengenigusa. Mimi si chochote ila ni Mwonyaji na Mbashiri kwa watu wanaoamini.

Mtume ﷺ Hajui Ghaibu Wala Hawezi Kunufaisha Wala Kudhuru, Hata kwa Nafsi Yake Mwenyewe.

Allah تعالی Alimuamuru Kuyategemeza mambo yote Kwake na yeye mwenyewe aeleze kuwa hajui ghaibu ijayo, lakini anayoyajua ni

yale tu Aliyojulishwa na Allah تعالی. Sawa na Kauli ya Allah تعالی katika Aya nyingine;

عَلَيْمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿١١﴾

“Yeye Ndiye Mwenye Kujua ya siri, wala Hamdhihirishii yeyote Siri Yake”. (72:26)

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Aya;

وَلَوْ كُنْتَ أَعْلَمُ الْغَيْبَ لَأَسْتَكْتَرْتُ مِنَ الْخَيْرِ

“Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ningejizidishia mema mengi”.

Kuwa maana yake, mali. Katika masimulizi mengine, “Ningelijua faida ambayo ningelipata baada ya kununua kitu, kwa hivyo nisingeluliza kitu chochote, bali ningepata faida kutokana nacho”.

وَمَا مَسَّنِيَ السُّوْءُ

“...wala ovu lisingenigusa”.

“Wala ufakiri usingenisibu”.¹ Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, “Na wengine walisema, maana yake, kama ningelikuwa najua ghaibu, ningejitayarisha kwa ajili ya mwaka wa baa la njaa, tangu ile ya mavuno. Na katika wakati wa bidhaa kuwa juu, ningeliutumia kujiandaa kipindi bidhaa ipo rahisi. ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema juu ya;

وَمَا مَسَّنِيَ السُّوْءُ

“...wala ovu lisingenigusa”.

“Ningelijiepusha na kujihadhari na shari kabla ya kutukia”.¹ Kisha Allah تعالى Akaeleza kuwa yeye (Mtume ﷺ) ni mwonyaji na mtoaji bishara, yaani dhidi ya Moto na mtoaji bishara kwa Waumini kuhusu *Janna*.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

فَإِنَّمَا يَسَّرْنَاهُ بِلِسَانِكَ لِتُبَشِّرَ بِهِ الْمُتَّقِينَ وَتُنذِرَ بِهِ قَوْمًا لُدًّا ﴿١٧٧﴾

“Na hakika Tumeifanya nyepesi (Qur’an) kwa ulimi wako, ili uwabashirie kwayo wachamungu, na uwaonye kwayo watu wabishi”. (19:97)

¹ Ad-Dur Al-Manthuur 3:622.

* هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا فَلَمَّا تَغَشَّهَا
 حَمَلَتْ حَمَلًا خَفِيْفًا فَمَرَّتْ بِهِ ۖ فَلَمَّا أَثْقَلَتْ دَّعَوَا اللَّهَ رَبَّهُمَا لَئِنْ ءَاتَيْنَا صَٰلِحًا
 لَّنُكُوْنَنَّ مِنَ الشَّاكِرِيْنَ ﴿١٨٨﴾ فَلَمَّا ءَاتَيْنَهُمَا صَٰلِحًا جَعَلَا لَهُ شُرَكَآءَ فِيمَا ءَاتَيْنَهُمَا ۗ
 فَتَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿١٨٩﴾

189. Yeye Ndiye Aliyekuumbeni katika nafsi moja na katika hiyo hiyo Akamfanya mwenzi wake, ili akae naye kwa utulivu. Na anapomuingilia hubeba mzigo mwepesi, akitembea nao. Anapokuwa mjamzito, wote wawili humuomba Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wao: Kama ukitupa mwana mwema tutakuwa katika wanaoshukuru.

190. Basi Anapowapa mwana mwema, wanamfanyia washirikina Mwenyezi Mungu katika kile Alichowapa. Mwenyezi Mungu Ametukuka na huko kushirikisha kwao”.

Watu Wote ni Wana wa Adam عليه السلام.

Allah تعالى Anaeleza kwamba Yeye Aliwaumba watu wote tangu Adam عليه السلام na kwamba Alimuumbia mkewe, Hawwa, halafu watu wakaenea kutokana na wawili hao.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يٰٓأَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنٰكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنٰكُمْ شُعُوْبًا وَقَبَاۗئِلَ لِتَعَارَفُوْٓا ۗ إِنَّ
 أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقٰنَكُمْ ۗ

“Enyi watu! Hakika Sisi Tumekuumbeni kutokana na mwanaume na mwanamke. Na Tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye Mchamungu zaidi katika nyinyi”. (49:13) na;

¹ At-Tabari 13:302.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ آتِفُوا رَبِّكُمْ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا

“Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi Aliyekuumbeni kutokana na nafsi moja, na Akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile”. (4:1)

Katika Aya hii tukufu, Allah تعالى Alisema;

وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا

“Akamfanya mwenzi wake, ili akae naye kwa utulivu”.

Kwa maana: Ili amzoee na atulizane naye.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَمِنْ آيَاتِنَا أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً
وَرَحْمَةً

“Na katika Ishara Zake ni kuwa Amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu”. (30:21)

Hakika, hapana mazoea baina ya roho mbili yaliyo zaidi ya baina ya wanandoa wawili. Kwa minajili hii, Allah تعالى Alitaja kwamba mlozi (Shetani) huwa wakati mwingine akifanya hila za kuwafarakanisha mtu na mkewe (dalili ya ugumu wa kuwatenganisha kwa njia za kawaida).

فَلَمَّا تَغَشَّاهَا

“Na anapomuingilia”. Kwa maana: Kufanya naye tendo la ndoa.

حَمَلَتْ حَمَلًا خَفِيًّا

“...hubeba mzigo mwepesi”.

Huo ni mwanzo wa himila, mwanamke hajisikii maumivu, kwani wakati huo huwa ni *Nutfah* (mchanganyiko wa maji ya mume na ya mke), kisha yanakuwa *'alaqah* (kipande cha damu iliyotungamana) na kisha, *Mudhghah* (pande dogo la nyama). Kauli ya Allah تعالى:

ط
فَمَرَّتْ بِهِ

"...akitembea nao".

Mujahid alisema, aliendelea na ujauzito wake.¹ Pia imesimuliwa hivyo hivyo na Al-Hasan, Ibrahim An-Nakha'i na As-Suddi.² Maymun bin Mahraan alisema kuwa baba yake alisema, "Anajikuta kwamba ujauzito wake hauhisiki". Ayyub alisema, "Nilimuuliza Al-Hasan juu ya Kauli ya Allah تعالیٰ;

ط
فَمَرَّتْ بِهِ

"...akitembea nao".

Akasema, "Ungelikuwa mwarabu, ungelijua maana yake! Ina maana kuwa, aliendelea na ujauzito (katika hatua nyingine kadha)".³ Qatadah alisema;

ط
فَمَرَّتْ بِهِ

"...akitembea nao". Maana yake: Ikambainikia kwamba alikuwa mjamzito.⁴ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema: "Maana yake, maji yaliendelea kuwepo, anaposimama na anapokaa."⁵ Al-'Awfi alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Maji yaliendelea kuwepo na akashikwa na mashaka kuwa ana mimba ama la?".

فَلَمَّا أَثْقَلَتْ

"Anapokuwa mjamzito". Kwa maana: Akiwa na ujauzito wa mimba yake⁶. As-Suddi alisema, "Kitoto kimekua tumboni mwake".⁷

دَعَا إِلَهَ رَبُّهُمَا لِيَنِّءَ آتَيْنَنَا صَالِحًا

**"...wote wawili humuomba Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wao:
Kama Ukitupa mwana mwema".**

Kwa maana: Mwanadamu kamili. Ad-Dhahhak alisema kuwa Ibn 'Abbas

¹ At-Tabari 13:305.

² At-Tabari 13:304,305.

³ At-Tabari 13:304.

⁴ At-Tabari 13:305.

⁵ At-Tabari 13:304.

⁶ At-Tabari 13:305.

⁷ At-Tabari 13:305.

رضي الله عنهما alisema, "Wote wawili walikhofia mtoto angazaliwa katika umbo la mnyama".¹ Pia Abu Bakhtari na Abu Malik walisema hivyo hivyo, "Waliogopa kwamba asingelikuwa mwanadamu".² Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, "Ikiwa, (Allah تعالى) Utatupatia mtoto".³

لَتَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿١٨٩﴾ فَلَمَّا ءَاتَتْهُمَا صَالِحًا جَعَلَا لَهُ شُرَكَاءَ فِيمَا ءَاتَتْهُمَا
فَتَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٩٠﴾

"...tutakuwa katika wanaoshukuru. Basi Anapowapa mwana mwema, wanamfanyia washirikina Mwenyezi Mungu katika kile Alichowapa. Mwenyezi Mungu Ametukuka na huko kushirikisha kwao". (7:189-190)

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Al-Hasan aliizungumzia sehemu hii ya Aya,

جَعَلَا لَهُ شُرَكَاءَ فِيمَا ءَاتَتْهُمَا

"...wanamfanyia washirikina Mwenyezi Mungu katika kile Alichowapa".

Alisema, "Hili lilitokea kwa baadhi ya wafuasi wa dini, na si kwa Adam عليه السلام (wala Hawwa)".⁴ Al-Hasan pia alisema, "Aya hii inarejea kwa miongoni mwa dhuria wa Adam ambao walitumbukia katika ushirikina baada yake". Maana;

جَعَلَا لَهُ شُرَكَاءَ فِيمَا ءَاتَتْهُمَا

"...wanamfanyia washirikina Mwenyezi Mungu katika kile Alichowapa".⁵

Qatadah alisema, "Al-Hasan alikuwa akisema, hao ni Wayahudi na Wakristo. Allah تعالى Aliwaruzuku watoto na wao wakawageuza kuwa Wayahudi na Wakristo".⁶

¹ At-Tabari 13:306.

² At-Tabari 13:306.

³ At-Tabari 13:306.

⁴ At-Tabari 13:314.

⁵ At-Tabari 13:314.

⁶ At-Tabari 13:315.

Hizi ni isnadi ambazo ni *Sahih* kutoka kwa Al-Hasan kuwa ndivyo alivyozifasiri ayah hizo, na yeye alikuwa miongoni mwa wafasiri wazuri. Makusudio ya Ayah hizi, si Adam عليه السلام na Hawwa, bali zinawarejea washirikina katika dhuria wake. Allah تعالى Ametaja mtu wa kwanza (Adam na Hawwa), na akaendelea kutaja jinsi (wanadamu) ambapo wengi wao wamefanya ushirikina, ni kama kutoka nje ya mada. Kwa kutaja dhati ya kitu lakini unamaanisha jinsia yake.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيحَ

“Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa”.

Inajulikana kuwa mataa ambayo ndio nyota zilizo pambiwa kwayo mbingu, sio vimondo ambavyo hupigwa mashetani. Na muundo huu wa maneno unakusudia kutoka nje ya dhati ya mataa na kumaanisha aina yake. Katika Qur'an kuna mifano mingi kama huo. *Allah Aalam.*

أَيُّشْرِكُونَ مَا لَا يَخْلُقُ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلِقُونَ ﴿١٨٨﴾ وَلَا يَسْتَطِيعُونَ لَهُمْ نَصْرًا وَلَا أَنْفُسَهُمْ يَنْصُرُونَ ﴿١٨٩﴾ وَإِنْ تَدْعُوهُمْ إِلَى الْهُدَىٰ لَا يَتَّبِعُوكُمْ سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَدْعَوْتُمُوهُمْ أَمْ أَنْتُمْ صَمِيمُونَ ﴿١٩٠﴾ إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ عِبَادٌ أَمْثَالِكُمْ فَادْعُوهُمْ فَلْيَسْتَجِيبُوا لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٩١﴾ أَلَهُمْ أَرْجُلٌ يَمْشُونَ بِهَا أَمْ لَهُمْ أَيْدٍ يَبْتَطِشُونَ بِهَا أَمْ لَهُمْ أَعْيُنٌ يُبْصِرُونَ بِهَا أَمْ لَهُمْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا قُلِ ادْعُوا شُرَكَاءَكُمْ ثُمَّ كِيدُوا فَلَا تُنظِرُونَ ﴿١٩٢﴾

191. “Ati wanawafanya viumbe kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu, nao hawaumbi, bali wao ndio wanaumbwa?”

192. “Wala hawana uwezo wa kuwanusuru wala wenyewe hawajinusuru”.

193. “Na mkiwaita kwenye uwongofu, hawakufuateni. Ni mamoja kwenu ikiwa mtawaita au mkinyamaza”.

194. "Hakika hao mnaowaomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni waja mfano wenu nyinyi. Hebu waombeni, nao wakuitikieni, kama mnasema kweli".

195. "Je, wao wanayo miguu ya kwendea? Au wanayo mikono ya kutetea? Au wanayo macho ya kuonea? Au wanayo masikio ya kusikizia? Sema: liteni hio miungu yenu ya ushirikina. Kisha Nifanyieni mimi vitimbi wala msinipe muhula".

Miungu ya Washirikina Hayasaidii Wala Hayana Uwezo wa Kufanya Chochote.

Allah تعالی Anawaonya washirikina ambao walimuabudu Allah تعالی pamoja na wengine wasiokuwa Yeye, miongoni mwa waungu wengine na masanamu, ilhali vitu hivyo vyote vimeumbwa na vinasimamiwa na kulelewa na Allah تعالی, havina mamlaka ya chochote, wala kudhuru wala kunufaisha. Wala havioni wala kuwasaidia wanaoviabudu. Bali ni vitu Visivyo hai, havitikisiki, wala havisikii wala havioni, ilhali wanaoviabudu ni bora kuliko hivyo kwa sababu ya kusikia kwao, kuona kwao na nguvu zao. Kwa mnasaba huu, Allah تعالی Alisema;

أَيُّشْرِكُونَ مَا لَا يَخْلُقُ شَيْئًا وَهُمْ يُخَلَّقُونَ ﴿١٨٨﴾

"Ati wanawafanya viumbe kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu, nao hawaumbi, bali wao ndio wanaumbwa?"

Kwa maana: "Mnamshirikisha Allah تعالی na ambavyo haviumbi chochote, wala haviliwezi hilo". Sawa na Kauli ya Allah تعالی;

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ ضُرْبَ مَثَلٍ فَاذْتَمِعُوا لَهُ^١ إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَنْ يَخْلُقُوا ذُبَابًا وَلَوْ اجْتَمَعُوا لَهُ^٢ وَإِنْ يَسْلُبْهُمُ الذُّبَابُ شَيْئًا لَا يَسْتَنْقِذُوهُ مِنْهُ^٣ ضَعُفَ

الطَّالِبِ وَالْمَطْلُوبِ ﴿١٨٩﴾ مَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ^٤ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿١٩٠﴾

"Enyi watu! Unapigwa mfano basi usikilizeni. Hakika wale wanaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, hawatumba hata nzi ijapokuwa watajumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Amedhoofika kweli huyo mwenye

kutaka na mwenye kutakiwa. Hawakumuadhimisha Mwenyezi Mungu Anavyostahiki kuadhimishwa. Hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mwenye Kushinda". (22:73-74)

Allah تعالى Ameeleza kuwa hata kama miungu wao wangelijumuika pamoja wasingeliweza kuumba hata nzi, bali hata ikiwa nzi atawanyakulia kisehemu kidogo cha kudharaulika kutokana na chakula chao na akaruka, wasingeliweza kukinusuru kutokana na nzi huyo. Basi, yule ambaye ni mwenye sifa na hali hizi, ataabudiwa vipi ili aweze kutoa riziki na kunusuru? Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

لَا يَخْلُقُ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلِقُونَ

"...hawaumbi, bali wao ndio wanaumbwa?"

Kwa maana: Bali wao wameumbwa na wametengenezwa.

أَتَعْبُدُونَ مَا تَنْحِتُونَ

"Hivyo mnaviabudu vitu mnavyovichonga wenyewe?" (37:95)

Kisha Allah تعالى Akasema;

وَلَا يَسْتَطِيعُونَ هُمْ نَصْرًا

"Wala hawana uwezo wa kuwanusuru wala wenyewe hawajinusuru".

Wanaowaabudu wao.

وَلَا أَنْفُسُهُمْ يَنْصُرُونَ

"...wala wenyewe hawajinusuru".

Kwa maana: Wala wao wenyewe kujinusuru dhidi ya aliyewakusudia vibaya. Kama ambavyo Nabii Ibrahim Al-Khalil alivyoyavunja masanamu ya kaumu yake, na akayafedhehesha kwa upeo wa juu. Sawa na Alivyojulisha Allah تعالى katika Kauli Yake;

فَرَاغَ عَلَيْهِمْ صَرْبًا بِالْيَمِينِ ﴿٣٧﴾

"Kisha akaigeukia kuipiga kwa mkono wa kulia". (37:93) na;

فَجَعَلَهُمْ جُودًا إِلَّا كَثِيرًا هُمْ لَعَلَّهُمْ إِلَيْهِ يَرْجِعُونَ ﴿٣٨﴾

"Basi akayavunja vipande vipande, ila kubwa lao, ili wao walirudie". (21:58)

Ni kama Mu'adh bin 'Amri bin Jamuh na Mu'adh bin Jabal رضي الله عنهما. Hawa walikuwa vijana wawili waliosilimu pindi Mtume ﷺ alipowasili Madinah. Walikuwa nyakati za usiku wakiyashambulia masanamu ya washirikina, wakiyavunja vunja na kuvichukua vipande kwa ajili ya kuni za wajane ili kaumu yao iweze kuabiri ili waelewe makosa yao. 'Amri bin Al-Jamuh ambaye alikuwa mkuu wa watu wake, alikuwa na sanamu alilokuwa akiliabudu na kulitia manukato. Vijana hao wawili wakawa wanakuja usiku na kulivunja kichwa na kulipakaza uchafu. Kisha anakuja 'Amri bin Jamuh na kuliwekea shoka na kuliambia, "Jinusuru". Kisha vijana wawili wanarudia kama hapo awali, na 'Amri anarudia kitendo chake hicho. Vijana wawili wakalichukua sanamu hilo siku moja na wakalifunga pamoja na mzoga wa mbwa, wakamning'iniza kwa kamba pamoja na sanamu kisimani. Alipokuja 'Amri bin Jamuh na kuyaona hilo, alijua kwamba dini yake ilikuwa potovu, akasema, "Wallahi! Kama ungelikuwa mungu muweza, usingeliishia kufungwa kamba pamoja na mbwa". Kisha akajirudisha chini na akasilimu, na akauwawa shahidi katika vita vya Uhud, Allah تعالى Awe radhi naye, Ampe radhi, na Ayafanye makazi yake katika Janna ya Firdaus. Kauli ya Allah تعالى:

وَإِنْ تَدْعُوهُمْ إِلَىٰ آهْدَىٰ لَا يَتَّبِعُكُمْ

"Na mkiwaita kwenye uwongofu, hawakufuateni".

Kwa maana: Masanamu haya huwa hayasikii wito wa anayeyalingania, wako sawa kwao, anayewaita na anayejitanibu nayo. Sawa na Alivyosema Ibrahim عليه السلام:

يَتَأْتَتْ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا

"Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyosikia, na visivyoona, na visivyokufaa chochote?" (19:42)

Kisha Allah تعالى Alieleza kuwa masanamu ni viumbe wake kama walivyo hao wanao yaabudu. Bali watu ni bora zaidi yao, kwani wanasikia, wanaona na wanashika, ilhali hao hawafanyi chochote katika hayo. Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ أَدْعُوا شُرَكَاءَكُمْ

"Sema: liteni hiyo miungu yenu ya ushirikina." Kwa maana: Takeni msaada kutoka kwao dhidi Yangu wala msinicheleweshe hata wasaa wa kupepesa jicho, na mfanye juhudi zenu zote.

إِنَّ وَلِيَّ اللَّهِ الَّذِي نَزَلَ الْكِتَابُ ۖ وَهُوَ يَتَوَلَّى الصَّالِحِينَ
 ۝۱۹۱ وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ لَا يَسْتَجِيبُونَ
 نَصْرَكُمْ وَلَا أَنْفُسَهُمْ يَنْصُرُونَ ۝۱۹۲ وَإِنْ تَدْعُوهُمْ
 إِلَى الْهُدَىٰ لَا يَسْمَعُوا ۖ وَتَرَاهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ وَهُمْ لَا
 يُبْصِرُونَ ۝۱۹۳ خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ
 الْجَاهِلِينَ ۝۱۹۴ وَإِنَّا يَرْعَاكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ
 فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ ۚ إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ۝۱۹۵ إِنَّ الَّذِينَ
 اتَّفَقُوا إِذَا مَسَّهُمْ طَلِيفٌ مِّنَ الشَّيْطَانِ تَذَكَّرُوا فَإِذَا هُمْ
 مُبْصِرُونَ ۝۱۹۶ وَإِخْوَانُهُمْ يَمُدُّوهُمْ فِي الْوَعْدِ ثُمَّ لَا
 يُقْصِرُونَ ۝۱۹۷ وَإِذَا لَمْ تَأْتِهِمْ بِبَيِّنَةٍ قَالُوا لَوْلَا اجْتَبَيْتَهَا
 قُلْ إِنَّمَا اتَّبَعْتُ مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ مِنْ رَبِّي ۚ هَذَا بَصَائِرٌ مِنْ
 رَبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ۝۱۹۸ وَإِذَا قُرِئَ
 الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُوا لَهُ وَأَنْصِتُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ۝۱۹۹
 وَأَذْكُرْ رَبَّكَ فِي نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَخِيفَةً وَدُونَ الْجَهْرِ مِنَ
 الْقَوْلِ بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ وَلَا تَكُن مِّنَ الْغَافِلِينَ ۝۲۰۰ إِنَّ
 الَّذِينَ عِنْدَ رَبِّكَ لَا يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِمْ وَيُسَبِّحُونَهُ
 وَلَهُ يَسْجُدُونَ ۝۲۰۱

إِنَّ وَلِيَّ اللَّهِ الَّذِي نَزَلَ الْكِتَابُ ۖ
 وَهُوَ يَتَوَلَّى الصَّالِحِينَ ۝۱۹۱ وَالَّذِينَ
 تَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ لَا يَسْتَجِيبُونَ
 نَصْرَكُمْ وَلَا أَنْفُسَهُمْ يَنْصُرُونَ
 ۝۱۹۲ وَإِنْ تَدْعُوهُمْ إِلَى الْهُدَىٰ لَا
 يَسْمَعُوا ۖ وَتَرَاهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ وَهُمْ
 لَا يُبْصِرُونَ ۝۱۹۳

196. "Hakika Mlinzi wangu ni Mwenyezi Mungu Aliye teremsha Kitabu. Naye Ndiye Awalindao walio wema".

197. "Na hao mnaowa-omba asiyekuwa Mwenyezi Mungu hawa wezi kukunusuruni, wala hawajinusu wenyewe".

198. "Na mkiwita kwenye uongofu Hawasikii. Na Unawaona wanakutazama, nao hawaoni".

إِنَّ وَلِيَّ اللَّهِ الَّذِي نَزَلَ الْكِتَابُ ۖ
 وَهُوَ يَتَوَلَّى الصَّالِحِينَ ۝۱۹۱

"Hakika Mlinzi wangu ni Mwenyezi Mungu Aliyeteremsha Kitabu. Naye Ndiye Awalindao walio wema".

Kwa maana: Allah تعالى Ananitosha kabisa na Ananikidhi. Yeye Ndiye wa Kuninusuru, nami ninatawakali Kwake na ninamtegemea Yeye. Na Yeye Ndiye Anayenilinda duniani na Akhera na Ndiye Mlinzi wa kila mja mwema baada yangu. Ni sawa na alivyosema Nabii Hud عليه السلام, pindi kaumu yake walipomuambia;

إِنْ نَقُولُ إِلَّا أَعْرَضْنَا بَعْضُ الْهَيْئَاتِ بِسُوءٍ ۗ قَالَ إِنِّي أُشْهِدُ اللَّهَ وَأَشْهَدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا
تُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾ مِنْ دُونِهِ ۗ فَكَيْدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ لَا تُنظِرُونِ ﴿٥٥﴾ إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي
وَرَبِّكُمْ ۗ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا ۗ إِنَّ رَبِّي عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٦﴾

“Sisi tunasema: Baadhi katika miungu yetu imekusibu kwa baa. Akasema: Hakika mimi namshuhudisha Mwenyezi Mungu na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnaowafanya washirika. Mkamuacha Yeye. Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi, na kisha msinipe muhula! Hakika mimi namtegemea Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye Anamuendesha Atakavyo. Hakika Mola wangu Mlezi yuko juu ya njia iliyonyooka”. (11:54-56)

Na kauli ya Nabii Ibrahim, Al-Khalil عليه السلام;

قَالَ أَفَرَأَيْتُمْ مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٧٥﴾ أَنْتُمْ وَأَبَاؤُكُمْ الْأَقْدَمُونَ ﴿٧٦﴾ فَإِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِي
إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٧﴾ الَّذِي خَلَقَنِي فَهُوَ يَهْدِينِ ﴿٧٨﴾

“Je! Mmewaona hawa mnaowaabudu, nyinyi na baba zenu wa zamani? Kwani hakika hao ni adui zangu, isipokuwa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ambaye Ndiye Aliyeniumba, na Yeye Ndiye Ananiongoa”. (26:75-78)

Pia ni sawa na kauli ya Ibrahim عليه السلام kumuambia baba yake na kaumu yake;

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٨٠﴾ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ
سَيَهْدِينِ ﴿٨١﴾ وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقْبِهِ ۗ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٨٢﴾

“Na pale Ibrahim alipomuambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi minajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu. Isipokuwa yule Aliyeniumba, kwani Yeye Ataniongoa. Na Akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee”. (43:26-28)

Kauli ya Allah تعالیٰ;

إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ

“Na hao mnaowaomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu”.

Mpaka mwisho wa Aya, inasisitiza yaliyotangulia, isipokuwa safari hii, Allah تعالیٰ Anatomia kauli ya moja kwa moja.

Kwa hivyo, alisema;

لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَكُمْ وَلَا أَنْفُسُهُمْ يَنْصُرُونَ

“...hawawezi kukunusuruni, wala hawajinusuru wenyewe”.

Kauli ya Allah تعالیٰ;

وَإِنْ تَدْعُوهُمْ إِلَىٰ آهْدَىٰ لَا يَسْمَعُوا^ط وَتَرْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ وَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ ﴿٢٦﴾

“Na mkiwaita kwenye uongofu Hawasikii. Na Unawaona wanakutazama, nao hawaoni”.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ;

إِنْ تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا دُعَاءَكُمْ

“Mkiwaomba Hawasikii maombi yenu”. (35:14)

Kauli ya Allah تعالیٰ;

وَتَرْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ وَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ

“Na Unawaona wanakutazama, nao hawaoni”.

Allah تعالیٰ Anasema, “Wanakutazama” maana, wanakabiliana nawe macho kwa macho, wakiwa katika taswira ya kukutazama, ilhali hawana uhai.

Kwa ajili hiyo wakawaamili muamala wa mwenye akili kwa kuwa wamesanifiwa kwa sura ya kibinadamu, na utawaona wanakutazama, na kwa hivyo wakawaabiri kwa dhamiri ya wenye akili.

حُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ ﴿١٩٦﴾ وَإِنَّمَا يَنزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ
فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٩٧﴾

199. *“Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majahili”.*

200. *“Na uchochezi wa Shetani ukikuchochea basi omba ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Msikizi, Mjuzi”.*

Amri ya kuwa Msamehevu

‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

حُذِ الْعَفْوَ

“Shikamana na kusamehe”.

Allah تعالى Alimuamuru (Mtume Muhammad ﷺ) kuwasamehe na kuwaacha washirikina kwa muda wa miaka kumi. Kisha Akamuamuru awe jasiri kwao¹. Wasimulizi zaidi ya mmoja walisimulia kutoka kwa Mujahid kuwa aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى, *“Shikamana na kusamehe”* akasema, “Kutokana na tabia na amali za watu bila kufanyiana ujasusi”.² Hisham bin ‘Urwah alisema kwamba baba yake alisema, “Allah تعالى Alimuamuru Mtume ﷺ kuwasamehe watu kwa tabia zao”.³ Na katika masimulizi mengine, “Samehe yale niliyokuruhusu katika tabia zao”. Na katika *Sahih* Al-Bukhari kuna Hadithi kwamba Hisham alisimulia kutoka kwa baba yake, ‘Urwah, kutoka kwa ndugu yake, ‘Abdullah bin Az-Zubayr, kwamba, Allah تعالى Alisema;

حُذِ الْعَفْوَ

“Shikamana na kusamehe”.

Kutokana na tabia za watu.⁴ Na katika masimulizi toka kwa msimuliaji mwingine, kutoka kwa Hisham, toka kwa baba yake, toka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما.⁵

¹ At-Tabari 13:328.

² At-Tabari 13:327.

³ At-Tabari 13:327.

⁴ Fat’hul Al-Bari 8:155.

⁵ Fat’hul Al-Bari 8:156.

Katika masimulizi mengine, ni kutoka kwa Hisham, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa 'Aishah رضي الله عنها. Hawa wawili walisimulia vivyo hivyo. *Allahu A'alam.*

Ibn Jariri رحمه الله تعالى na Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى kwa pamoja walisema, Yunus alisema: Ametusimulia Abu Sufyan, ambaye ni Ibn 'Uyaynah, alisimulia kwamba Umayyah alisema, "Wakati Allah تعالى Alipomteremshia Nabii Wake;

خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ ﴿١٩٦﴾

"Shikamana na kusamehe na amrisha mema, na jitenge na majahili".

Mtume ﷺ alisema;

«مَا هَذَا يَا جِبْرِيْلُ»

"Ni nini maana yake ewe Jibrili?"

Akasema, "Allah تعالى Anakuamuru uwasamehe waliokudhulumu, uwape waliokunyima na uendeleze uhusiano na walioukata udugu wako".¹ Al-Bukhari alisema, "Kauli ya Allah تعالى:

خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ ﴿٢٠٦﴾

"Shikamana na kusamehe na amrisha mema, na jitenge na majahili".

"Al-'Urf, maana yake ni mambo ya kimaadili". Pia, Al-Bukhari alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, "Uyaynah bin Hisn bin Hudhaifah alifikia kwa mtoto wa kaka yake aitwaye Hur bin Qays na alikuwa miongoni mwa watu ambao 'Umar رضي الله عنه alikuwa akiwa nao karibu, na *Qarii* wasomaji wa Qur'an, walikuwa ndio masahiba wa majilisi ya 'Umar رضي الله عنه, na ndio waliokuwa washauri wake, wazee kwa vijana. 'Uyaynah akamuambia mtoto wa kaka yake, "Ewe mwana wa kaka! Wewe u-karibu na amiri huyu, basi niombe ruhusa ya kumuona". Akasema, "Nitakuombea ruhusa kwake". Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akaendelea kusema; "Hur akamuombea 'Uyaynah ruhusa, na 'Umar رضي الله عنه akampa ruhusa. Alipoingia alisema, "Ewe Ibn Al-Khattab!

¹ At-Tabari 6:154 na Ibn Hatim 5:1638.

“Pinga uovu kwa lililo jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki, jamaa wa kukuonea uchungu. Lakini hawapewi wema huu ila wanaosubiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa”. (41:34-35)

Kwa maana: Wasia huu;

وَأَمَّا يَتَرَعَّنَكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٦﴾

“Na shetani akikuchochea kwa uchochezi wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua”. (41:36)

Pia, Alisema katika Sura hii tukufu;

وَأَمَّا يَتَرَعَّنَكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٧﴾

“Na uchochezi wa Shetani ukikuchochea basi omba ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Msikizi, Mjuzi”.(7:200)

Hizi nii Aya tatu zinazokaribiana ambazo ziko katika Surat Al-A'raaf, Al-Mu'minun na Ha Mim As-Sajdah. Hakuna ya nne. Katika Aya hizo, Allah تعالى Anaelekeza Kuwafanyia wema binadamu waovu. Hilo linaweza kuwazuia wasiendelee na maovu, kwa Idhini ya Allah تعالى. Kwa hiyo Allah تعالى Alisema;

فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ

“Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki, jamaa wa kukuonea uchungu”. (41:34)

Kisha Allah تعالى Anaelekeza kumuomba Yeye kwa ajili ya kinga dhidi ya Shetani, kwani yeye hakumtoshi kule kufanya ihsani kwako, kwani yeye anataka kuangamia kwako na kukuharibu kabisa, kwani yeye ni adui yako aliye dhahiri na kwa baba yako kabla yako. Ibn Jarir رحمه الله تعالى katika kutafsiri Kauli ya Allah تعالى:

وَأَمَّا يَتَرَعَّنَكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ

“Na uchochezi wa Shetani ukikuchochea”. Alisema, “Na kama shetani akikughadhabisha, ghadhabu inayokuzuia kuachilia na ikakupelekea katika kumtia adabu,

فَأَسْتَعِذُّ بِاللَّهِ

“...basi omba ulinzi wa Mwenyezi Mungu”.

Allah تعالى Anasema, basi jikinge kwa Allah تعالى dhidi ya uchochezi wa shetani.

إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٠١﴾

“Hakika Yeye ni Msikizi, Mjuzi”.

Ni mwenye kuusikia ujahili wa mwenye kukufanyia ujahili na maombi ya kujikinga dhidi yake, na maneno mengine yote ya viumbe. Hakifichiki Kwake Yeye chochote juu ya uchochezi wa shetani na yasiyokuwa katika mambo ya viumbe Wake.¹

Tulikwisha tangulia kutaja Hadithi za kuomba kujikinga mwanzoni mwa tafsiri hii, kiasi cha kutokuwepo haja ya kurudia hapa.

إِنَّ الَّذِينَ اتَّقَوْا إِذَا مَسَّهُمْ طَائِفٌ مِّنَ الشَّيْطَانِ تَذَكَّرُوا فَإِذَا هُم مُّبْصِرُونَ ﴿٢٠١﴾
وَأَخْوَانُهُمْ يَمُدُّوهُمْ فِي الْغَيِّ ثُمَّ لَا يُقْصِرُونَ ﴿٢٠٢﴾

201. “Hakika wale wamchao Mungu, zinapowagusa pepesi za shetani, mara huzindukana na hapo huwa wenye kuiona haki”.

202. “Na ndugu zao wanawavutia kwenye upotofu, kisha wao hawaachi”.

Njia za Wachamungu Wakati wa Wasiwasi wa Shetani.

Allah تعالى Anatoa khabari za wachamungu ambao humtii Allah تعالى juu ya Aliyoyaamuru na kuyaacha Aliyoyakaripia, kuwa wao;

إِذَا مَسَّهُمْ

“...zinapowagusa pepesi za shetani”.

Kwa maana: Zinapowapata *Twayf*, wengine wamesoma, *Twaaf*. Hivyo ni visomo (*Qiraa*) vya namna mbili vilivyo mashuhuri. Ilisemwa kwamba maana yake ni

¹ At-Tabari 13:332.

moja. Pia inasemwa maana zake ni tofauti. Miongoni mwao walilifasiri neno hilo kuwa ni ghadhabu, wengine walisema ni kupatwa na shetani kwa kupagawa na mfano wake. Wengine walitafsiri kuwa ni kudhamiria kufanya dhambi na wengine walisema ni kupata madhambi. Kauli ya Allah;

تَذَكَّرُوا

"...mara huzindukana".

Kwa maana: Juu ya Adhabu ya Allah تعالى, Malipo Yake maridhawa, Ahadi Zake na Agano Lake. Wakatubu, wakarejea, wakamuomba kinga Allah تعالى na wakarudi karibu na Allah تعالى.

فَإِذَا هُمْ مُبْصِرُونَ

"...na hapo huwa wenye kuiona haki".

Kwa maana: Wamekuwa katika mwenendo ulionyooka na wameyasahilisha yale waliyokuwa wakiyafanya.

Ndugu wa Shetani Miongoni Mwa Wanadamu Hulaghai na Kuhamasisha Kwenye Upotovu.

Kauli ya Allah تعالى;

وَإِخْوَانُهُمْ يَمُدُّوهُمْ

"Na ndugu zao wanawavutia".

Kwa maana: Ndugu wa shetani miongoni mwa wanadamu. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

إِنَّ الْمُبْدِرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيْطَانِ

"Hakika wabadhirifu ni ndugu wa mashetani". (17:27)

Na wao ni wafuasi wao na wanaowasikiliza wao, na kuwakubalia amri zao.

يَمُدُّوهُمْ فِي الْغَيِّ

"...wanawavutia kwenye upotovu". Kwa maana: Mashetani wanawasaidia katika maasi, wanawasahilishia na kuwapendezeshea. Ibn Kathir رحمه الله تعالى alisema, wanawavutia katika upotovu, yaani ujahili na usafihi.

ثُمَّ لَا يُقْصِرُونَ

"...kisha wao hawaachi".

Ilisemwa maana yake, mashetani wanawavutia wanaadamu wala hawaachi kufanya hivyo. Sawa na Alivyosema 'Ali bin Abu Twalhah kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما juu ya Kauli ya Allah تعالى:

وَإِخْوَانُهُمْ يَمُدُّوهُمْ فِي الْغَىِّ ثُمَّ لَا يُقْصِرُونَ ﴿٢٠٦﴾

"Na ndugu zao wanawavutia kwenye upotofu, kisha wao hawaachi".

Kwamba, "Hakuna wanaadamu wanaoacha maovu wanayoyaacha, wala mashetani hawaachi kuwashikilia (katika kuwahadaa)"¹

لَا يُقْصِرُونَ

"Kisha wao hawaachi".

Hawachoki wala hawaachi. Sawa na Kauli ya Allah تعالى katika ayah nyingine;

أَلَمْ تَرَ أَنَا أَرْسَلْنَا الشَّيْطَانَ عَلَى الْكَافِرِينَ تَوَّضَعُوا لِقَائِ رَبِّهِمْ أُولَئِكَ هُمُ الَّذِينَ كَانُوا يُصَوَّرُونَ ﴿١٩٨﴾

"Kwani huoni ya kwamba Tumewatuma mashetani kwa makafiri wawachochee kwa uchochezi?" (19:83)

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na wengine walisema, wanawakhadaa kufanya maasi bila kukoma.²

وَإِذَا لَمْ تَأْتِهِمْ بِعَايَةٍ قَالُوا لَوْلَا آجْتَبَيْتَهَا قُلْ إِنَّمَا أَتَّبِعُ مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ مِنْ رَبِّي هَذَا

بَصَائِرٍ مِنْ رَبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٢٠٦﴾

203. "Na usipowaletea Ishara waitakayo husema: Kwa nini hukuibuni? Sema: mimi ninafuata yanayofunuliwa kwangu kutokana na Mola Mlezi wangu. Hii (Qur'an) ni hoja zinazotoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu na rehema kwa watu wanao amini".

¹ At-Tabari 13:338.

² At-Tabari 18:252.

Washirikina Waomba Washuhudie Miujiza.

'Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;

قَالُوا لَوْلَا آجْتَبَيْتَهَا^٤

“...husema: Kwa nini hukuibuni?”

Kwa kusema, “Wanasema, “Kwa nini hukupokea muujiza?” Mara nyingine alisema, “Kwa nini hukuubuni au kuufanya?”¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa 'Abdullah bin Kathir رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Mujahid juu ya Kauli ya Allah تعالى;

وَإِذَا لَمْ تَأْتِهِمْ بِبَيِّنَةٍ قَالُوا لَوْلَا آجْتَبَيْتَهَا^٤

“Na usipowaletea Ishara waitakayo husema: Kwa nini hukuibuni?”

Wanasema: “Fanya muujiza wako mwenyewe”.² Kadhalika walisema hivyo akina Qatadah, As-Suddi, 'Abdur-Rahman bin Aslam. Na Ibn Jariri رحمه الله تعالى alikubaliana nayo³. Na maana ya Kauli ya Allah تعالى;

وَإِذَا لَمْ تَأْتِهِمْ بِبَيِّنَةٍ

“Na usipowaletea Ishara waitakayo”.

Kwa maana: Muujiza na dalili. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

إِنْ كُنَّا نُنزِلُ عَلَيْهِمْ مِنَ السَّمَاءِ آيَةً فَظَلَّتْ أَعْيُنُهُمْ هَا خَاضِعِينَ ﴿٤﴾

“Tungependa Tungeliwateremshia kutoka mbinguni Ishara zikanyenyekea shingo zao”. (26:4)

Wanamuambia Mtume ﷺ, kwa nini hufanya jitihada za kutafuta Aya (miujiza) kutoka kwa Allah تعالى ili tuishuhudie na tuiamini. Allah تعالى akamuambia;

قُلْ إِنَّمَا أُنذِرُكُمْ بِمَا يُوحَىٰ إِلَيَّ مِنْ رَبِّي^٥

“Sema: mimi ninafuata yanayo funuliwa kwangu kutokana na Mola Mlezi wangu”.

¹ At-Tabari 13:341.

² At-Tabari 13:341.

³ At-Tabari 13:341.

Mimi simuombi Mola wangu vitu kama hivyo. Nafuata kile Alichonifunulia na Kuniamuru tu. Hivyo nitaendelea kufuata kile Alichonifunulia. Akileta Aya (muujiza) nitaupokea. Lakini Akiuzuia, mimi sitamuomba kwa kuanza mimi, isipokuwa Akiniruhusu hivyo, kwani Yeye ni Mwenye Hekima nyingi, Mjuzi Zaidi. Kisha Akawaelekeza kwamba hii Qur'an ndio muujiza mkubwa zaidi, na ndio yenye dalili dhahiri zaidi, ndiyo hoja na maelezo ya ukweli mtupu. Akasema Allah تعالى:

هَذَا بَصَائِرٌ مِنْ رَبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

“Hii (Qur'an) ni hoja zinazotoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu na rehema kwa watu wanaoamini”.

وَإِذَا قُرِئَ الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُوا لَهُ وَأَنْصِتُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٢٠٤﴾

204. “Na Isomwapo Qur'an isikilizeni na mnyamaze ili mpate kurehemewa”.

Amri ya Kuisikiliza Qur'an.

Baada ya Allah تعالى Kutaja kwamba Qur'an ni ushahidi wa wazi, ni uongofu, na ni rehema, Aliamrisha unyamavu wakati wa kusomwa kwake kwa ajili ya kuitukuza na kuiheshimu. Si kama washirika wa kikuraishi wanavyofanya, kwa kauli yao;

لَا تَسْمَعُوا هَذَا الْقُرْآنَ وَالْغَوْا فِيهِ

“Na waliokufuru walisema: Msiisikilize Qur'an hii, na timueni zogo”.
(41:26)

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, Ibn Ma'ud رضي الله عنه alisema, “Tulikuwa tukisalimiana wakati wa Sala. Basi ikashushwa Aya katika Qur'an;

وَإِذَا قُرِئَ الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُوا لَهُ

“Na Isomwapo Qur'an isikilizeni”.

وَأَذْكُرَ رَبِّكَ فِي نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَخِيفَةً وَدُونَ الْجَهْرِ مِنَ الْقَوْلِ بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ وَلَا

تَكُنْ مِنَ الْغَافِلِينَ ﴿٢٠٥﴾ إِنَّ الَّذِينَ عِنْدَ رَبِّكَ لَا يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ وَذُكِّرْتَهُ

وَلَهُ يَسْجُدُونَ ﴿٢٠٦﴾

205. “Na mkumbuke Mola Mlezi wako nafsini kwako kwa unyenyekevu na khofu, na bila ya kupiga kelele kwa kauli, asubuhi na jioni. Wala usiwe miongoni wa walioghafilika”.

206. “Hakika wale walioko kwa Mola wako Mlezi hawajivuni wakaacha kumuabudu, na wanamtakasa na wanamsujudia”.

Amri ya Kumdhukuru Allah تعالی Asubuhi na Jioni.

Allah تعالی Anaamrisha kuleta *Dhkr* asubuhi na jioni kwa wingi. Kama Alivyowaamuru waja Wake katika nyakati hizi mbili, katika Kauli Yake;

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ

“...na mtakase kwa kumsifu Mola wako Mlezi kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa”. (50:39)

Hili lilikuwa kabla ya kufaradhishwa Sala tano katika usiku wa *Israa*. Aya hii ilishushwa Makkah. Hapa Allah تعالی Alisema, “...asubuhi” nao ndio mwanzo wa mchana, “...asubuhi na jioni”. Ama Kauli ya Allah تعالی;

تَضَرُّعًا وَخِيفَةً

“...kwa unyenyekevu na khofu”. Kwa maana: Mtaje Mola wako kwa matumaini na khofu na kwa kimoyo moyo, si kwa jahara. Ndiyo sababu Allah تعالی Alisema;

وَدُونَ الْجَهْرِ مِنَ الْقَوْلِ

“...na bila ya kupiga kelele kwa kauli”. Na hivi ndivyo *Dhikr* inavyopendekezwa iwe, si kwa sauti ya juu wala kwa jahara. Allah تعالی Alisema katika Aya nyingine;

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۗ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۗ

“Na waja Wangu watakapokuuliza khabari Zangu, waambie kuwa Mimi Nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba”. (2:186)¹

¹ Masimulizi haya yalinukuliwa na Ibn Hatim kwa isnadi dhaifu ya wasimulizi. Kuna vitabu vingine ambavyo vinaunga mkono tafsiri yake.

Katika *Sahih* Mbili, Abu Musa Al-Ash'ari رضى الله عنه alisema, "Watu walinyanyua sauti zao katika Dua wakati wa baadhi ya safari, Mtume ﷺ akawaambia;

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ ارْزِعُوا عَلَى أَنْفُسِكُمْ، فَإِنَّكُمْ لَا تَدْعُونَ أَصَمًّا وَلَا غَائِبًا إِنَّ الَّذِي تَدْعُونَهُ سَمِيعٌ قَرِيبٌ أَقْرَبُ إِلَيَّ أَحَدِكُمْ مِنْ عُنُقِ رَاحِلَتِهِ»

"Enyi watu! Jifanyieni wepesi katika nafsi zenu, kwani mnayemuomba si kiziwi wala hayupo mbali. Kwa hakika mnayemuomba ni Mwenye kusikia, Wa Karibu. Yu Karibu zaidi ya mmoja wenu kuliko shingo ya mnyama wake".¹

Makusudio ni Kuhimiza juu ya kukithirisha *Dhikr* asubuhi na jioni ili asiwe katika walioghafilika.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Aliwasifu Malaika ambao wanamtukuza Yeye katika nyakati za usiku na mchana, bila kuchoka.

إِنَّ الَّذِينَ عِنْدَ رَبِّكَ لَا يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ

"Hakika wale walioko kwa Mola wako Mlezi hawajivuni wakaacha kumuabudu".

Allah تعالى Alisema hivyo ili hao Malaika waigwe kwa wingi wa utii wao na ibada zao. Kwa hiyo, Allah تعالى Alituumuru tusujudu hapa, baada ya kutaja kusujudu kwao kwa ajili ya Allah تعالى. Hadithi inaeleza;

«أَلَا تَصُنُّونَ كَمَا تَصْنَعُ الْمَلَائِكَةُ عِنْدَ رَبِّهَا يُتِمُّونَ الصُّفُوفَ الْأُولَىٰ فَأَلَا تَأْتُونَ
رَبِّرَاحُونَ فِي الصَّنْفِ»

"Kwa nini hamjipangi safu, kama wajipangavyo Malaika mbele ya Mola wao, wanakamilisha safu ya kwanza kisha inayofuatia na kuendelea, na wanasimama karibu karibu katika kila safu".²

Hii ndiyo Sijda ya kwanza katika Qur'an, ambayo iliamriwa kwa msomaji na msikilizaji kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni.

* * *

¹ Fat'hul Al-Bari 6:157 na Muslim 4:2077.

² Muslim 1:322.